UKRISTO BILA BARAKOA

ELLEN G. WHITE

New Covenant Publications International Ltd. Swahili

Hakimiliki © 2020. Machapisho ya Kimataifa ya Agano Jipya

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inaweza kunakiliwa au zinaa katika aina yoyote au kwa njia yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwenye hakimiliki, isipokuwa nukuu fupi kwa kusudi la mapitio, maoni, au taaluma. Kwa maswali au habari zaidi, wasiliana na kwa mchapishaji.

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inaweza kutolewa, kutunzwa au kunakiliwa kwa muundo au kwa namna yoyote, iwe kwa elektroniki, kimakanika, kufotokopi, ku-rekodi au vinginevyo pasipo ruhusa ya maandishi ya mwandishi isipokuwa kutoa sehemu kama rejea katika kufundisho. Kwa taarifa na kibali unaweza kuwaasiliana na mchapishaji.

ISBN: 359-2-85933-609-1

ISBN: 359-2-85933-609-1

Akaorodhesha Katika - Publication Cataloging (CIP)

Kuhariri na Kubuni: Kundi la Kimataifa ya Agano Jipya

Kuchapishwa nchini Uingereza.

Kwanza Uchapishaji Mei 26 Mwaka 2020

Kuchapishwa na: Machapisho ya Kimataifa ya Agano Jipya

New Covenant Publications International Ltd.,

Kemp House, 160 City Road, London, EC1V 2NX

Tembelea tovuti: www.newcovenant.co.uk

UKRISTO KUFUNULIWA

ELLEN G. WHITE

Ulimwengu uliodhoofika ulikuwa ukitetemeka kwa misingi yake wakati Ukristo ulipotokea. Dini za kitaifa zilizowaridhisha wazazi, hazikuwatosheleza tena watoto. Vizazi vipya havikuweza kuwa na furaha na aina za kale. Miungu ya kila taifa, iliposafirishwa hadi Rumi, huko ilipoteza nguvu zao, kama vile mataifa yenyewe yalikuwa huko yalipoteza uhuru wao. Uso kwa uso katika Capitol, walikuwa wameharibu kila mmoja, na uungu wao ulikuwa umetoweka. Utupu mkubwa ulitokea ndani ya dini ya ulimwengu. Aina fulani ya deism, isiyo na roho na uhai, ilielea kwa muda juu ya shimo ambalo imani potofu zenye nguvu za zamani zilikuwa zimemezwa. Lakini, kama imani zote hasi, haikuwa na uwezo wa kujenga upya. Umiliki wa kitaifa ulitoweka na kuanguka kwa miungu ya kitaifa. Falme mbalimbali ziliyeyuka na kuunganishwa moja hadi nyingine. Katika Ulaya, Asia, na Afrika, kulikuwa na milki moja kubwa tu, na jamii ya kibinadamu ilianza kuhisi nguvu zake za ulimwengu wote na umoja wayo...

Historia ya Marekebisho ya Karne ya Kumi na Sita –

Juzuu ya 1, Kitabu cha 1, Sura ya 1

Jean-Henri Merle D'Aubigé

Ukurasa huu umeachwa tupu kwa makusudi.

New Covenant Publications

International Ltd.

Vitabu Vilivyorekebishwa, Akili Zilizobadilishwa

New Covenant Publications International Ltd.,
Kemp House, 160 City Road, London, EC1V 2NX

Email: newcovenantpublicationsintl@gmail.com

Shukrani

Kitabu hiki ni kujitolea kwa Mungu Baba.

Dibaji

New Covenant Publications International inaunganisha tena msomaji na mpango wa kimungu wa kuufunga mbingu na dunia na kuimarisha utimilifu wa sheria ya upendo. Nembo, Sanduku la Agano linawakilisha urafiki kati ya Kristo Yesu na watu Wake na umuhimu wa sheria ya Mungu. Kama ilivyoandikwa, "hii itakuwa agano nitakalofanya na nyumba ya Israeli asema Bwana, nitaweka sheria yangu ndani yao na kuiandika mioyoni mwao na watakuwa watu Wangu, nami nitakuwa Mungu wao." (Yeremia 31:31-33; Waebrania 8:8-10). Kwa kweli, agano jipya linashuhudia ukombozi, uliosababishwa na ugomvi na kuwekwa muhuri na damu.

Kwa karne nyingi, wengi wamevumilia mateso mazito na ukandamizaji usioeleweka, ulioundwa ili kufuta ukweli. Hasa katika Enzi za Giza, nuru hii ilikuwa imepingwa vikali na kufichwa na mila ya wanadamu na ujinga wa umma, kwa sababu wenyeji wa ulimwengu walikuwa wamedharau na walikiuka agano hilo. Athari ya maelewano na maovu yasiyokuwa ya mwisho yalichochea janga la udhoofishaji usiodhibitika na unyanyasaji wa kiibilisi, ambapo watu wengi walitolewa kafara kwa njia isiyo haki, wakikataa kutoa uhuru wa dhamiri. Hata hivyo, maarifa yaliyopotea yalifufuliwa, haswa wakati wa Matengenezo.

Enzi ya Matengenezo ya karne ya 16 ilizua wakati wa ukweli, mabadiliko ya kimsingi na mtikisiko, kama unavyoonyeshwa katika Upingaji wa Matengenezo. Hata hivyo, kupitia kiasi hiki, unagundua tena umuhimu usiobadilika wa mapinduzi haya ya umoja kutoka kwa mtazamo wa Wageuzi na mapainia wengine jasiri. Kutoka kwa maoni yao, unaweza kuelewa vita vinavyoibuka, sababu za kimsingi zinazosababisha upinzani huo na uingiliaji wa ajabu.

Wito wetu: "Vitabu Vilivyorekebishwa, Akili Zilizobadilishwa," hututhibisha utofauti wa tanzu ya fasihi, uliotungwa katika wakati mgumu na athari yake. Pia inaangazia dharura ya ubadilishaji wa kibinafsi, kuzaliwa upya na mabadiliko. Wakati uchapishaji wa Gutenberg, pamoja na shirika la tafsiri, ulivyosambaza kanuni za imani iliyorekebishwa, miaka 500 iliyopita, vyombo vya habari vya kidijitali na vyombo vya habari mtandaoni vingewasiliana katika kila lugha kuhusu taa ya ukweli nyakati hizi za mwisho.

Jedwali la Yaliyomo

Jedwali la Yaliyomo 2
Sura ya 1 - Unabii wa Hali ya Mwicho wa Ulimwengu 5
Sura ya 2 - Ubatizo wa Moto 20
Sura ya 3 - Zama za Giza la Kiroho 28
Sura ya 4 - Wanakinga Imani 37
Sura ya 5 - Nyota ya Asubuhi 49
Sura ya 6 - Askari wa Ukweli 62
Sura ya 7 - Utengano Mkubwa 79
Sura ya 8 - Mbele ya Mahakama Kuu 97
Sura ya 9 - Mwanamatengenezo wa Kiswisi 116
Sura ya 10 - Maendeleo ya Matengenezo Ujerumani 126
Sura ya 11 - Upinzani wa Wakuu wa Majimbo 135
Sura ya 12 - Matengenezo Ufaransa 146
Sura ya 13 - Uholanzi na Skandinavia 166
Sura ya 14 – Wanamatengenezo wa Baadaye Uingereza 172
Sura ya 15 - Biblia na Mapinduzi ya Ufaransa 187
Sura ya 16 - Makasisi Wasafiri 205
Sura ya 17 - Wajumbe wa Asubuhi 213
Sura ya 18 - Mwanamatengenezo wa Kimarekani 226
Sura ya 19 - Nuru Gizani 245
Sura ya 20 - Mwamko Mkuu wa Kidini 254
Sura ya 21 - Onyo Lililokataliwa 268
Sura ya 22 - Unabii Watimia 280
Sura ya 23 - Patakatifu ni Nini? 293
Sura ya 24 - Ndani ya Patakatifu pa Patakatifu 303
Sura ya 25 - Sheria ya Mungu Isiyobadilika 310
Sura ya 26 - Kazi ya Matengenezo 322
Sura ya 27 - Uamsho wa Kisasa 329
Sura ya 28 - Siku ya Hukumu 342

Sura ya 29 - Chimbuko la Uovu 351
Sura ya 30 - Uadui wa Kuzimu 360
Sura ya 31 - Wakala wa Pepo 365
Sura ya 32 - Mitego ya Shetani 370
Sura ya 33 - Udanganyifu Mkuu wa Kwanza 380
Sura ya 34 - Je, Wafu Wetu Wanaweza Kuongea Nasi? 395
Sura ya 35 - Uhuru wa Dhamiri Watishwa 403
Sura ya 36 - Pambano Linalotarajiwa Karibuni 424
Sura ya 37 - Maandiko ni Kinga 432
Sura ya 38 - Onyo la Mwisho 439
Sura ya 39 - Wakati wa Taabu 446
Sura ya 40 - Watu wa Mungu Wakombolewa 462
Sura ya 41 - Ukiwa wa Dunia 475
Sura ya 42 - Mwisho wa Pambano 482

Sura ya 1 - Unabii wa Hali ya Mwicho wa Ulimwengu

"Laiti ungalijua, hata wewe katika siku hii, yapasayo amani! Lakini sasa yamefichwa machoni pako. Kwa kuwa siku zitakuja, adui zako watakapokujengea boma, likuzunguke; watakuzingira na kukuhusuru pande zote; watakuangusha chini wewe na watoto wako ndani yako, wasikuachie jiwe juu ya jiwe, kwa sababu hukutambua majira ya kujiliwa kwako" (Luka 19:42-44).

Akiwa katika kilele cha Mlima wa Mizeituni, Yesu aliutazama mji wa Yerusalemu. Mji uliokuwa na mwonekano mzuri na uliojaa amani ulitanda mbele Yake. Ilikuwa majira ya Pasaka, na kutoka nchi zote wana wa Yakobo walikuwa wamekusanyika hapo kusherehekea siku kuu hiyo kubwa ya kitaifa. Katikati ya bustani na mashamba ya mizababu, na miteremko ya kijani iliyokuwa imepambwa kwa mahema ya mahujaji, viliinuka vilima, majengo ya kifalme, na kuta kubwa za mji mkuu wa Israeli. Ni kama vile binti Sayuni alionekana kwa kiburi chake akisema, nimeketi malkia na sitaona huzuni; akijiona mzuri, na akidhani kuwa yuko salama kwa sababu ya kupendelewa na Mbingu, sawa na wakati, zama nyingi zilizopita, mwimbaji wa nyumba ya mfalme alipoimba: "Kuinuka kwake ni mzuri sana, Ni furaha ya dunia yote. Mlima Sayuni,…Mji wa Mfalme mkuu" (Zaburi 48:2).

Majengo mazuri ya hekalu yalikuwa yakionekana vizuri sana. Miale ya jua lililokuwa likizama iliakisiwa na weupe uliofanana na theluji wa marumaru za kuta zake na kuifanya rangi ya dhahabu ya lango na mnara na ncha ya mnara, kung'ara. "Ukamilifu wa uzuri" ulisimama, kiburi cha taifa la Wayahudi. Ni mtoto gani wa Israeli ambaye angetazama mwonekano wa mji ule asipate msisimko wa furaha na kupigwa butwaa! Lakini fikra za Yesu zilijazwa na mawazo mengine. "Alipofika karibu aliuona mji, akaulilia" (Luka 19:41). Katikati ya shangwe na furaha kuu ya Yesu kuingia mji wa Yerusalemu, wakati matawi ya mitende yalipokuwa yakipeperushwa hewani kwa madaha, wakati hosana zenye nderemo na bashasha zilipoamsha miangwi ya milima, na maelfu ya sauti yalipomtangaza kuwa Mfalme, Mkombozi wa ulimwengu aligubikwa na huzuni iliyofichika. Yeye, Mwana wa Mungu, Ahadi ya Israeli, ambaye nguvu zake zilishinda mauti na kuwaita mateka wa mauti kutoka kaburini, alibubujikwa machozi, siyo machozi ya kawaida, bali machozi yaliyotokana na uchungu mzito, yaliyotokana na maumivu makali yasiyovumilika.

Machozi Yake hayakuwa kwa ajili Yake Mwenyewe, japokuwa alijua vema kule nyayo Zake zilikokuwa zikielekea. Mbele Yake kulikuwa na Gethsemane, mahali pa maumivu Yake yaliyokuwa yanakaribia. Mlango wa kondoo ulikuwa mbele Yake pia, mlango ambao kwa karne nyingi wanyama wa kafara walipitishiwa, ambao ulikuwa tayari umeshafunguliwa kwa ajili Yake ili "apelekwe machinjoni" (Isaya 53:7).

Kalwari, mahali aliposulubiwa, hapakuwa mbali. Kwenye njia ambayo Kristo angepita muda si mrefu ilipasa pajae hofu ya giza kuu wakati alipotoa roho Yake kuwa sadaka kwa

ajili ya dhambi. Pamoja na hayo, tafakari juu ya matukio hayo haikuwa sababu ya giza lililokuwa juu Yake wakati wa saa ya furaha. Hakuna tishio lo lote la maumivu dhidi ya mwili Wake lilifunika roho Yake isiyokuwa na ubinafsi. Alililia maelfu ya watu wa Yerusalemu waliokuwa wanaelekea kuangamia—kwa sababu ya upofu na ugumu wa mioyo ya wale aliokuja kuwabariki na kuwaokoa.

Historia ya zaidi ya miaka elfu moja ya upendeleo wa kipekee na utunzaji makini, uliooneshwa kwa watu waliochaguliwa, ilifunuliwa mbele ya Yesu. Kulikuwa na Mlima Moria, mahali ambapo mwana wa ahadi, kafara asiye na ubishi, alifungwa juu ya madhabahu—ishara ya sadaka ya Mwana wa Mungu. Pale, agano la baraka, ahadi tukufu ya Masihi, ilithibitishwa kwa baba yao watu walio waaminifu (Mwanzo 22:9, 16-18). Pale, ndimi za moto wa kafara zilizopanda juu mbinguni kutoka katika sakafu ya kupuria nafaka ya Ornani ziliweka kando upanga wa malaika anayeangamiza (1 Nyakati 21)—alama stahiki ya kafara ya Mwokozi na upatanisho kwa ajili ya wanadamu wenye hatia. Yerusalemu iliheshimiwa na Mungu kuliko miji mingine yote duniani. Bwana "aliuchagua Sayuni,""Alitaka uwe makao Yake" (Zaburi 132:13).

Pale, kwa miaka mingi, manabii watakatifu walitangaza ujumbe wao wa onyo. Pale, makuhani walipepea vyetezo vyao, na wingu la uvumba, pamoja na maombi ya watu waliokuja kuabudu, lilipaa juu hadi mbele za Mungu. Pale, kila siku damu ya wanakondoo waliochinjwa ilitolewa, ikielekeza kwa Mwanakondoo wa Mungu ajaye. Pale, Yehova alifunua uwepo Wake katika wingu la utukufu juu ya kiti cha rehema. Pale, palikaliwa na ncha ya ngazi ya kimuujiza iliyounganisha nchi na mbingu (Mwanzo 28:12; Yohana 1:51)—ngazi ile ambayo juu yake malaika wa Mungu walishuka na kupanda, na ambayo ilifungulia ulimwengu njia ya kuingia mahali patakatifu mno. Ikiwa taifa la Israeli lingedumisha utii wake kwa Mbingu, Yerusalemu ungedumu kuwa mji mteule wa Mungu milele zote (Yeremia 17:21-25). Lakini historia ya wale watu waliopata upendeleo ilikuwa kumbukumbu ya kurudi nyuma na kuasi. Walipinga neema ya Mbingu, walitumia vibaya nafasi zao za upendeleo, na walichezea fursa zao.

Ingawa Israeli "waliwadhihaki wajumbe wa Mungu, na kuyadharau maneno Yake, na kuwacheka manabii wake" (2 Nyakati 36:16), bado Mungu alijifunua kwao kuwa "Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli" (Kutoka 34:6); licha ya kukataliwa mara nyingi, rehema Yake iliendelea kuwasihi. Kwa upendo na huruma inayozidi ya baba kwa mtoto wake mpendwa, Mungu "akatuma kwao kwa mikono ya wajumbe wake, akiondoka mapema, na kutuma; kwa sababu aliwahurumia watu wake, na makao yake" (2 Nyakati 36:15). Wakati hoja, nasaha, na maonyo viliposhindwa, aliwatumia zawadi bora kabisa kuliko zote kutoka mbinguni; ndiyo, alitoa mbingu yote kupitia zawadi hiyo moja. Mwana wa Mungu mwenyewe alitumwa aubembeleze mji usiotubu. Kristo ndiye aliyewaleta Israeli kama mzabibu kutoka Misri (Zaburi 80:8). Mkono Wake Mwenyewe uliyaondoa mataifa ya kipagani mbele yao. Aliwapanda Israeli

"Kilimani penye kuzaa sana." Ulinzi na utunzaji Wake ulikuwa wigo uliolizunguka shamba pande zote. Watumishi Wake walitumwa kulitunza. "Je! Ni kazi gani iliyoweza kutendeka ndani ya shamba langu la mizabibu," alieleza, "nisiyoitenda?" (Isaya 5:1-4). Ingawa alitarajia kuwa lingezaa zabibu, lilizaa zabibu mwitu, lakini bado akiwa na tumaini la kuzaa zabibu alikuja Mwenyewe kushughulikia shamba Lake. Alililima shamba Lake; alilipogolea na kulipalilia. Alikuwa na juhudi zisizochoka za kuliokoa shamba Lake alilolipanda Mwenyewe.

Kwa miaka mitatu Bwana wa nuru na utukufu aliingia na kutoka miongoni mwa watu Wake. Naye"akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi," kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, viwete waweze kwenda, wenye ukoma watakaswe, viziwi wasikie, wafu wapate kufufuliwa, na maskini wahubiriwe habari njema (Matendo 10:38; Luka 4:18; Mathayo 11:5). Wito wa neema unatolewa kwa makundi yote ya watu: "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28).

Ingawa alizawadiwa ubaya kwa wema, na chuki kwa upendo Wake (Zaburi 109:5), aliendelea kutekeleza utume Wake wa rehema. Kamwe hakuwafukuza wale wote waliotafuta rehema Kwake. Msafiri asiyekuwa na makao rasmi, aibu na umaskini vikiwa ndiyo sehemu ya maisha Yake, aliishi kukidhi mahitaji na kupunguza maumivu ya watu, akiwasihi waipokee zawadi ya uzima. Mawimbi ya neema, yaliyorudishwa nyuma na watu wenye mioyo migumu, yalirudi katika mkondo wenye nguvu zaidi wa huruma na upendo usioelezeka. Lakini Israeli walikuwa wamemwacha Rafiki mwema na Msaidizi wao pekee. Wito Wake wa upendo ulipuuzwa, mashauri Yake yalitupiliwa mbali, na maonyo Yake yalidhihakiwa.

Saa ya tumaini na msamaha ilikuwa ikipita haraka; kikombe cha ghadhabu ya Mungu iliyokawizwa kilikuwa karibu sana kujaa. Wingu lililokuwa likijikusanya katika zama zote za uvunjaji wa sheria na uasi, sasa likiwa na weusi wa huzuni, lilikuwa linakaribia kuwapasukia watu wenye hatia; na Yeye ambaye peke Yake angeweza kuwaokoa dhidi ya hatari iliyowakabili alikuwa amepuuzwa, amekejeliwa, amekataliwa, na alikuwa karibu kusulubiwa. Wakati ambao Kristo angening'inizwa juu ya msalaba wa Kalwari, ndiyo siku ambayo Israeli kama taifa lililopendelewa na lililobarikiwa na Mungu lingekoma. Kupotea kwa roho hata moja ni janga kubwa zaidi kuliko faida na hazina za ulimwengu; lakini Kristo alipoutazama Yerusalemu, kuangamia kwa mji wote, taifa lote, kulikuwa mbele Yake—mji ule, taifa lile, ambalo awali lilikuwa taifa teule la Mungu, hazina Yake ya ajabu.

Manabii walilia machozi kwa ajili ya uasi wa Israeli na ukiwa wa kutisha ambao dhambi iliuleta kwa Waisraeli. Yeremia alitamani macho yake yawe chemchemi ya machozi, ili aweze kulia usiku na mchana kwa ajili ya mauaji ya binti wa watu wake, kwa ajili ya kundi la Bwana ambalo lilikuwa limechukuliwa mateka (Yeremia 9:1; 13:17). Kwa misingi hiyo, huzuni ya Yule ambaye mtupo Wake wa jicho la kiunabii ulihusisha siyo miaka tu, bali

ulihusisha vizazi vingi, ilikuwa kubwa kiasi gani! Alimwona malaika mwuaji akiwa na upanga ulioinuliwa dhidi ya mji ambao kwa muda mrefu ulikuwa makazi ya Yehova. Kutoka katika mlima wa Mizeituni, mahali ambapo baadaye Tito na jeshi lake walisimama, alitazama ng'ambo ya bonde na kuona ukumbi na malango ya kuingia ukumbini, na kwa macho yaliyojaa machozi aliona, kwa maono ya kutisha, kuta zilizozungukwa na majeshi ya kigeni. Alisikia vishindo vya nyayo za majeshi ikienda vitani. Alisikia sauti za akina mama na watoto wakililia mkate katika mji uliozingirwa. Aliona nyumba nzuri, majengo ya kifalme, na minara ya Yerusalemu, vikiwaka moto, na mahali viliposimama, pakiwa na rundo la mabaki yaliyokuwa yakiungua moto.

Akiangalia matukio ya zama zijazo, aliwaona watu wa agano wakiwa wametawanyika katika kila nchi, "kama mabaki ya ajali katika pwani ya jangwani." Katika kisasi cha muda mfupi kilichokuwa karibu kuwaangukia watoto wake, aliona mkupuo wa kwanza kutoka katika kikombe cha hasira ya Bwana ambacho wakati wa hukumu ya mwisho itawapasa kukinywa mpaka tone la mwisho. Huruma ya Kimungu, upendo wenye kujali, ulioneshwa katika maneno haya ya huzuni: "Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!" Ee Israeli, ambaye ulikuwa taifa lililopendelewa na Mungu zaidi ya mataifa mengine, laiti ungelijua wakati wa kujiliwa kwako, na mambo yapasayo amani yako! Nimemzuia malaika wa haki, nimekuita upate kutubu, lakini bila mafanikio. Siyo tu watumishi, wajumbe, na manabii, ambao umewagomea na kuwakataa, lakini umemkataa pia Mtakatifu wa Israeli, Mkombozi wako. Ikiwa utaangamia, utawajibika peke yako. "Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima" (Mathayo 23:37; Yohana 5:40).

Kristo aliuona mji wa Yerusalemu kama mfano wa ulimwengu uliofanywa kuwa mgumu kwa kutokuamini na uasi, na kuharakisha kukutana na hukumu za adhabu za Mungu. Maumivu ya kizazi kilichoanguka, yakimsonga rohoni Mwake, yalilazimisha kilio chenye uchungu mwingi kutoka katika midomo Yake. Aliona kumbukumbu ya dhambi ikiwa ndiyo chanzo cha mateso, machozi, na damu ya wanadamu; moyo Wake ulijaa huruma isiyokuwa na kikomo kwa ajili ya watu wanaoteseka na wanaoumia duniani; alitamani kuwasaidia wote. Lakini hata kama mkono Wake ungeweza kurudisha nyuma mkondo wa maumivu ya wanadamu; wachache wangetafuta Chanzo chao pekee cha msaada. Alikuwa tayari kumimina roho Yake hadi kifo, kuuleta wokovu mahali ambapo wangeweza kuupata; lakini wachache ambao wangemwendea ili wapate uzima.

Mfalme wa mbinguni anatokwa machozi! Mwana wa Mungu wa milele anaumia moyoni, anainama kwa uchungu! Tukio lile lilileta mshangao mbinguni. Tukio lile linadhihirisha ubaya usio wa kawaida wa dhambi; linaonesha jinsi ambavyo kazi ya kumwokoa mwenye hatia kutoka katika matokeo ya kuasi sheria ya Mungu ilivyo ngumu hata kwa Mungu Mwenyewe. Yesu, akitazama hadi kizazi cha mwisho, aliona ulimwengu

utakavyojihusisha na uongo unaofanana na huo uliosababisha uharibifu wa Yerusalemu. Dhambi kubwa ya Wayahudi ilikuwa kumkataa Kristo; dhambi kubwa ya ulimwengu wa Wakristo ni kuikataa sheria ya Mungu, msingi wa serikali Yake mbinguni na duniani. Kanuni za Yehova zitadharauliwa na kuhesabiwa kuwa si kitu. Mamilioni katika utumwa wa dhambi, watumwa wa Shetani, wakikabiliwa na mauti ya pili, wangekataa kusikiliza maneno ya ukweli katika siku ya kujiliwa kwao. Upofu wa kutisha! Kupumbazika kwa ajabu sana!

Siku mbili kabla ya Pasaka, wakati Kristo alipokuwa ameondoka hekaluni kwa mara ya mwisho, baada ya kukemea unafiki wa viongozi wa Wayahudi, alitoka tena na wanafunzi Wake hadi katika Mlima wa Mizeituni na alikaa pamoja nao kwenye mteremko wenye nyasi upande unaotazamana na mji wa Yerusalemu. Kwa mara nyingine tena alizitazama kuta zake, minara yake, na nyumba zake za kifalme. Mara nyingine tena alilitazama hekalu katika mwangaza wake wa kushangaza, taji la uzuri likiufunika mlima matakatifu.

Miaka elfu moja kabla, mwandishi wa Zaburi alieleza vizuri upendeleo wa Mungu kwa Waisraeli kwa kulifanya hekalu lao kuwa mahali Pake pa kukaa:“Kibanda chake pia kiko Salemu, Na maskani yake iko Sayuni.” Bali “aliichagua kabila ya Yuda, Mlima Sayuni alioupenda. Akajenga patakatifu pake kama vilele, Kama dunia aliyoiweka imara milele” (Zaburi 76:2; 78:68, 69). Hekalu la kwanza lilijengwa wakati wa kipindi cha mafanikio makubwa ya historia ya Israeli. Akiba kubwa ya hazina kwa ajili ya kusudi hili ilikusanywa na Mfalme Daudi, na mipango kwa ajili ya ujenzi wake ilifanywa kwa uongozi wa Mungu (1 Nyakati 28:12, 19). Suleimani, mfalme mwenye hekima kuliko wafalme wote wa Israeli, alitekeleza kazi ya ujenzi. Hekalu hili lilikuwa jengo zuri ajabu ambalo ulimwengu ulikuwa haujawahi kuliona. Pamoja na hayo, Bwana alitangaza kupitia kwa nabii Hagai, kuhusiana na hekalu la pili: “Utukufu wa mwisho wa nyumba hii utakuwa mkuu kuliko utukufu wake wa kwanza.”“Nami nitatikisa mataifa yote, na vitu vinavyotamaniwa na mataifa yote vitakuja; nami nitaijaza nyumba hii utukufu, asema Bwana wa majeshi” (Hagai 2:9, 7).

Baada ya kuharibiwa kwa hekalu na Nebukadneza lilijengwa upya takribani miaka mia tano kabla ya kuzaliwa kwa Kristo na watu ambao walitoka katika utumwa wa miaka mingi waliorudi katka nchi iliyoharibika na kukaribia kutelekezwa. Wakati huo walikuwepo miongoni mwao wazee walioona utukufu wa hekalu la Sulemani, na ambao walilia kwa kuona msingi wa jengo jipya, kuwa lilikuwa lazima liwe chini ya viwango vya lile la awali. Hisia zilizokuwepo zinaelezwa vizuri na nabii: “Miongoni mwenu amebaki nani aliyeiona nyumba hii katika utukufu wake wa kwanza? Nanyi mnaionaje sasa? Je! Mbele ya macho yenu, siyo kama si kitu?” (Hagai 2:3; Ezra 3:12). Ndipo ahadi ilipotolewa kuwa utukufu wa hekalu la baadaye utakuwa mkubwa zaidi ya lile la kwanza.

Lakini hekalu la pili halikuwa sawa na la kwanza katika uzuri; wala halikutukuzwa kwa viashiria vinavyoonekana vya uwepo wa Mungu kama vilivyoonekana katika hekalu la kwanza. Hakukuwa na udhihirisho wo wote wa wazi wa nguvu zisizokuwa za kawaida wakati

wa uwekaji wakfu wake. Hakuna wingu la utukufu lililoonekana likijaza hekalu jipya. Hakuna moto ulioshuka kutoka mbinguni kuunguza kafara juu ya madhabahu. Shekina haikuwepo tena kati ya makerubi ndani ya patakatifu pa patakatifu; sanduku la agano, kiti cha rehema, na meza za ushuhuda havikuwemo humo. Hakuna sauti iliyotoka mbinguni kumjibu kuhani aliyeuliza kuhusiana na mapenzi ya Yehova.

Kwa karne nyingi Wayahudi walijaribu bila mafanikio kuonesha ni wapi ahadi iliyotolewa na Mungu kwa njia ya Hagai ilikuwa imetimizwa; hata hivyo kiburi na kutokuamini vilipofusha akili zao zisielewe maana halisi ya maneno ya nabii. Hekalu la pili halikuheshimiwa kwa wingu la utukufu wa Yehova, bali kwa uwepo mbashara wa Yule ambaye utimilifu wa Uungu unakaa ndani Yake kwa jinsi ya kimwili— ambaye alikuwa Mungu Mwenyewe aliyejidhihirisha katika mwili. Yeye ambaye ni "Shauku ya mataifa yote" alikuja katika hekalu Lake wakati Mtu wa Nazareti alipofundisha na kuponya katika ukumbi mtakatifu. Kwa uwepo wa Kristo, na kwa njia hii tu, ndiyo utukufu wa hekalu la pili ulizidi utukufu wa lile la kwanza. Lakini Israeli walikuwa wamemkataa Yeye aliyekuwa zawadi kutoka mbinguni. Kwa Mwalimu mnyenyekevu ambaye siku ile alitoka nje kupita lango lake la dhahabu, utukufu ulikuwa umeondoka katika hekalu milele. Tayari maneno ya Mwokozi yalikuwa yametimizwa: "Nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa" (Mathayo 23:38).

Wanafunzi walipata mshtuko na mshangao kwa sababu ya utabiri wa Kristo wa kutekwa kwa hekalu, na walitamani kuelewa kikamilifu zaidi maana ya maneno Yake. Mali, kazi, na stadi za ujenzi zilikuwa zimetumika sana kuboresha uzuri wake. Herode Mkuu alikuwa amewekeza kwenye jengo hili kwa kutumia utajiri wa Kirumi na hazina ya Kiyahudi, na hata mfalme wa ulimwengu alileta zawadi kwa ajili ya uboreshaji wa hekalu. Matofali ya marumaru, yenye ukubwa wa ajabu, yaliyosafirishwa kutoka Rumi kwa kusudi hilo, yalikuwa sehemu ya jengo hilo; na haya ndiyo matofali ambayo wanafunzi walikuwa wamemwonesha Bwana wao, wakisema: "Tazama, yalivyo mawe na majengo haya!" (Marko 13:1).

Kwa maneno haya, Yesu alitoa jibu la kushangaza na kushitua: "Hamyaoni haya yote? Amin, nawaambieni, Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa" (Mathayo 24:2).

Wanafunzi walihusianisha kuharibiwa kwa Yerusalemu na matukio ya kuja kwa Kristo Mwenyewe katika utukufu wa muda na kuketi kwenye kiti cha enzi cha ufalme wa ulimwengu wote, kuwaadhibu Wayahudi wasiotubu, na kulikomboa taifa kutoka katika kongwa la utumwa wa Kirumi. Bwana aliwaambia kuwa angekuja mara ya pili. Hivyo kwa kutaja hukumu za Yerusalemu, akili zao zilirejelea kuja kule; na walipokuwa wamekusanyika pamoja wakimzunguka Mwokozi juu ya Mlima wa Mizeituni, waliuliza: "Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?" (Aya ya 3).

Wanafunzi walifichwa mambo yajayo kwa kuhurumiwa. Ikiwa wakati ule wangejua kikamilifu mambo mawili ya kutisha ya kweli— mateso na mauti ya Mkombozi, na kuharibiwa kwa mji wao na hekalu lao—wangezidiwa na hofu. Kristo aliwaeleza kwa muhtasari matukio makuu yaliyopaswa kutokea kabla ya mwisho wa wakati. Maneno Yake hayakueleweka kikamilifu wakati ule; lakini maana yake ingefunuliwa kwa kadiri watu Wake walivyohitaji maelekezo yaliyokuwa ndani yake. Unabii alioutoa ulikuwa na maana mbilia; wakati ukieleza kuharibiwa kwa Yerusalemu, uliwakilisha vitisho vya siku ya mwisho.

Yesu aliwaeleza wanafunzi waliokuwa wakimsikiliza hukumu zilizowakabili Waisraeli walioasi, na hususani hukumu ya adhabu iliyowakabili kwa kumkataa na kumsulubisha Masihi. Ishara zisizoweza kukosewa zingetangulia kilele cha kutisha. Saa ya kutisha ingekuja kwa ghafla na haraka. Na Mwokozi aliwaonya wafuasi Wake:"Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu (asomaye na afahamu), ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani"(Mathayo 24:15, 16; Luka 21:20, 21).

Wakati bendera za ibada ya sanamu za Warumi zitakaposimikwa katika uwanja mtakatifu, ambao ulipanuka na kwenda kilomita kadhaa nje ya kuta za mji, ndipo wafuasi wa Kristo iliwapasa kukimbia kwa ajili ya usalama wao. Wakati ishara ya onyo ilipoonekana, wale waliotaka kukimbia iliwapasa wasichelewe. Katika nchi yote ya Yuda, pamoja na mji wa Yerusalemu wenyewe, ishara ya kukimbia ilipaswa kutiiwa mara moja. Mtu aliyekutwa juu ya nyumba hakupaswa kuteremka na kuingia ndani ya nyumba yake, hata kuokoa hazina yake ya thamani kubwa. Watu waliokuwa wakifanya kazi mashambani au wakishughulikia mizabibu hawakupaswa kupoteza muda kwa kurudi kuchukua vazi lao la nje walilolivua wakati wakipambana na kazi kwa ajili ya joto la mchana. Hawakupaswa kusita-sita hata kwa muda mfupi sana, ili wasikumbwe na uharibifu wa jumla.

Wakati wa utawala wa Herode, siyo tu kuwa Yerusalemu ulikuwa umependezeshwa, bali pia kwa kujenga minara, kuta, na ngome, vikiongeza uimara wa asili wa mazingira yake, ulikuwa umefanyiwa uzio usioweza kupenywa kirahisi. Mtu ambaye wakati huu angebashiri hadharani juu ya uangamizaji wake, kama Nuhu katika siku zake, angeitwa mropokaji kichaa atangazaye mambo yaletayo hofu. Lakini Kriso alisema: "Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe" (Mathayo 24:35). Kwa sababu ya dhambi zake, hasira ilikuwa imetangazwa dhidi ya Yerusalemu, na usugu wake wa kutokuwa na imani ulifanya uharibifu wake uwe wa hakika. Bwana alikuwa ametangaza kupitia kwa nabii Mika: "Sikieni haya, tafadhali, enyi vichwa vya nyumba ya Yakobo, mnaoitawala nyumba ya Israeli, mnaochukia hukumu, na kuipotosha adili. Wanaijenga Sayuni kwa damu, na Yerusalemu kwa uovu. Wakuu wake huhukumu ili wapate rushwa, na makuhani wake hufundisha ili wapate ijara, na manabii wake hubashiri ili wapate fedha; ila hata hivyo watamtegemea Bwana, na kusema, Je! Hayupo Bwana katikati yetu? Hapana neno baya lo lote litakalotufikia" (Mika 3:9-11). Maneno haya yalieleza kwa uaminifu hali ya wakazi wa Yerusalemu waliojawa na

ufisadi na kujihesabia haki. Huku wakidai kutimiza matakwa ya sheria ya Mungu kikamilifu, walikuwa wakivunja kanuni zake. Walimchukia Kristo kwa sababu usafi na utakatifu Wake vilifunua uovu wao; na walimshitaki kuwa Yeye ndiye aliyekuwa chanzo cha taabu zilizowakabili kama matokeo ya dhambi zao. Ingawa walijua kuwa hakuwa na dhambi yo yote, walitangaza kuwa kifo chake kilikuwa cha lazima kwa ajili ya usalama wao kama taifa. "Tukimwacha hivi," viongozi wa Kiyahudi walisema, "watu wote watamwamini; na Warumi watakuja, watatuondolea mahali petu na taifa letu" (Yohana 11:48). Ikiwa Kristo atasulubiwa, wangeweza tena kuwa na nguvu, watu walioungana. Hivyo ndivyo walivyofikiri, na walikubaliana na uamuzi wa kuhani mkuu, kuwa ilikuwa bora kwa mtu mmoja kufa kuliko taifa zima kuangamia.

Hivyo ndivyo viongozi wa Kiyahudi walivyoijenga "Sayuni kwa damu, naYerusalemu kwa uovu"(Mika 3:10). Na bado, wakati walimwua Mwokozi wao kwa sababu ya kukemea dhambi zao, kujihesabia haki kwao kulikuwa kukubwa mno kiasi kwamba walijihesabu kuwa watu waliopendelewa na Mungu na walitarajia awaokoe dhidi ya maadui zao. "Basi," nabii aliendelea, "kwa ajili yenu, Sayuni utalimwa kama shamba lilimwavyo, na Yerusalemu utakuwa magofu; na mlima wa nyumba utakuwa kama mahali palipoinuka msituni" (Aya ya 12).

Kwa karibu miaka arobaini baada ya uharibifu wa Yerusalemu kutangazwa na Kristo Mwenyewe, Bwana alizuia hukumu Yake juu ya mji na taifa. Uvumilivu wa Mungu ulikuwa wa ajabu kwa watu waliokataa injili Yake na wauaji wa Mwana Wake. Mfano wa mtini usiozaa matunda uliwakilisha jinsi Mungu alivyoshughulika na taifa la Kiyahudi. Amri ilikuwa imetolewa, "Uukate, mbona hata nchi unaiharibu?" (Luka 13:7) lakini rehema ya Mungu iliuacha kwa muda mrefu kidogo zaidi. Kulikuwepo bado wengi miongoni mwa Wayahudi waliokuwa hawajui tabia na kazi ya Kristo. Na watoto walikuwa hawajapata fursa au nuru ambayo wazazi wao walikuwa wameitupilia mbali. Kwa njia ya mahubiri ya mitume na washirika wao, Mungu angewezesha nuru kuwaangazia; wangeweza kuruhusiwa kuona jinsi unabii ulivyokuwa umetimizwa, siyo katika kuzaliwa na maisha ya Kristo, lakini pia katika kifo na ufufuo. Watoto hawakuhukumiwa kwa dhambi za wazazi wao; bali wakati, wakiwa na ujuzi wa nuru yote iliyotolewa kwa wazazi wao, watoto walipokataa nuru ya nyongeza waliyopewa wenyewe, walikuwa washirika wa dhambi za wazazi wao, na walijaza kipimo cha uovu wao.

Uvumilivu wa Mungu kwa wakazi wa Yerusalemu ulizidi kuwafanya washupaze shingo zao zaidi katika uasi. Kwa chuki na ukatili wao dhidi ya wanafunzi wa Yesu walikataa nafasi yao ya mwisho ya rehema. Ndipo Mungu alipoondoa ulinzi Wake kwao na kuondoa nguvu Yake ya kumzuia Shetani na malaika zake, na taifa likaachwa katika utawala wa kiongozi waliyemchagua. Watoto wao waliitupilia mbali neema ya Kristo, ambayo ingewawezesha kudhibiti misukumo yao ya uovu, na sasa misukumo hii ilipata ushindi. Shetani aliamsha misisimko mikali na hatarishi ndani ya mioyo yao. Watu walipoteza uwezo wao wa kufikiri

vizuri; walikuwa kama vichaa—walitawaliwa na mihemko na hasira iliyopofushwa. Walibadilika na kuwa kama mashetani katika ukatili wao.

Katika familia na katika taifa, miongoni mwa matabaka ya juu na ya chini sawia, kulikuwa kutoaminiana, kijicho, ugomvi, uasi, na mauaji. Usalama ulitoweka kila mahali. Marafiki na ndugu wa karibu walisalitiana. Wazazi waliwachinja watoto wao, na watoto waliwachinja wazazi wao. Watawala wa watu hawakuwa na uwezo wa kujitawala wenyewe. Misisimko isiyodhibitiwa iliwafanya kuwa wakatili kupindukia. Wayahudi waliukubali ushuhuda wa uongo kumhukumu Mwana wa Mungu aliyekuwa hana hatia yo yote. Sasa mashitaka ya uongo yalifanya maisha yao kuwa ya wasiwasi. Kwa matendo yao walikuwa wakisema kwa muda mrefu: “Mkomesheni Mtakatifu wa Israeli mbele yetu” (Isaya 30:11). Sasa hitaji lao lilikidhiwa. Hofu ya Mungu haikuwasumbua tena. Shetani ndiye aliyekuwa kiongozi wa taifa, na mamlaka ya juu kabisa ya kiraia na kidini vilikuwa chini ya utawala wake.

Nyakati zingine, viongozi wa vikundi hasimu waliungana kupora na kutesa wahanga wao wasioweza kujitetea, na tena waliangukiana wao kwa wao kwa majeshi ya kikundi kimoja kuangukia kikundi hasimu na walichinjana bila huruma. Hata utakatifu wa hekalu haukuweza kudhibiti ukatili wao wa kutisha. Waabuduji walipigwa na kuuawa mbele ya madhabahu, na patakatifu palinajisiwa kwa miili ya watu waliochinjwa. Hata hivyo, katika upofu wao na kiburi chenye kufuru wachochezi wa kazi hii ya kuzimu walitangaza hadharani kuwa walikuwa hawana hofu kuwa Yerusalemu ingeangamizwa, kwa kuwa ulikuwa mji wa Mungu Mwenyewe. Kuimarisha zaidi nguvu zao, waliwahonga manabii wa uongo watangaze, hata wakati majeshi ya Kirumi walipokuwa wakilizingira hekalu, kuwa watu walipaswa kusubiri ukombozi kutoka kwa Mungu. Hatimaye, watu wengi walishikilia kwa bidii imani kuwa Mungu Aliye Juu angeingilia kati na kuwashinda maadui zao. Lakini Israeli alikuwa ameshatupilia mbali ulinzi wa Mungu, na sasa hakuwa na ulinzi. Yerusalemu wenye huzuni! Ukiwa umeraruliwa na mipasuko ya ndani, damu ya watoto wake waliochinjwa kwa mikono yao wenyewe mmoja dhidi ya mwenzake ikiweka wekundu kwenye mitaa yake, wakati majeshi ya kigeni yalipoangusha ngome zake na kuwaua watu wake wa vita!

Mambo yote yaliyoelezwa katika utabiri uliotolewa na Kristo kuhusiana na kuharibiwa kwa Yerusalemu yalitimizwa. Wayahudi walishuhudia ukweli wa maneno Yake ya onyo: “Na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa” (Mathayo 7:2). Ishara na maajabu vilitokea, majanga na matatizo ya kutisha yalitokea. Katikati ya usiku mwangaza usio wa kawaida uliangaza juu ya hekalu na madhabahu. Juu ya mawingu wakati wa jua kuzama zilichorwa picha za magari na watu wa vita wakijikusanya kwa ajili ya vita. Makuhani waliokuwa wakihudumu usiku katika patakatifu walitishwa na sauti za ajabu; dunia ilitetemeka, na sauti nyingi zilisikika zikipiga kelele: “Tuondoke haraka.”

Lango la mashariki, ambalo lilikuwa zito sana kiasi kwamba lilifungwa na watu ishirini kwa shida, na ambalo lilikuwa limefungwa kwa nondo kubwa za chuma zilizofungwa kwa uimara katika sakafu yam awe magumu, lilifunguliwa usiku bila mfunguaji ye yote anayeonekana.—Milman, The History of the Jews, book 13.

Kwa miaka saba mtu mmoja aliendelea kuzunguka akienda na kushuka katika mitaa ya Yerusalemu, akitangaza majanga yaliyokuwa yanaujia mji. Mchana na usiku aliimba wimbo wa ajabu: "Sauti kutoka mashariki! Sauti kutoka magharibi! Sauti kutoka pepo nne! Sauti dhidi ya Yerusalemu na dhidi ya hekalu! Sauti dhidi ya mabwana harusi na mabibi harusi! Sauti dhidi ya watu wote!"—Ibid. kiumbe huyu wa ajabu alifungwa na kuchpawa mijeledi, lakini hakuna neno la manung'uniko lilitoka katika midomo yake. Jibu lake kwa matusi na dharau aliyofanyiwa lilikuwa: "Ole, ole wako Yerusalemu!" "ole, ole wenu enyi wakazi wake!" Kilio chake cha onyo hakikukoma mpaka alipochinjwa katika maangamizi ambayo aliyatabiri.

Hakuna Mkristo hata mmoja aliyeangamia katika kuharibiwa kwa Yerusalemu. Kristo alitoa onyo kwa wanafunzi Wake, na wote walioamini maneno Yake na kuzingatia ishara iliyoahidiwa. "Hapo mtakapoona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi," alisema Yesu, "ndipo jueni ya kwamba uharibifu wake umekaribia. Ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani, na walio katikati yake wakimbilie nje, na walio katika mashamba wasiuingie" (Luka 21:20, 21). Baada ya Warumi chini ya Ketio kuuzunguka mji, bila kutarajiwa waliachana na kazi ya utekaji wakati kila kitu kilionekana kuwa tayari kwa ajili ya mashambulizi ya ghafla. Watekwaji, wakiwa katika hali ya kukata tamaa ya kuukabili na kuuzuia utekaji, walikuwa karibu kujisalimisha, wakati jenerali wa Kirumi aliporudisha nyuma majeshi yake bila sababu ya msingi.

Lakini uongozi wa Mungu wenye rehema ulikuwa ukielekeza matukio kwa ajili ya mazuri kwa ajili ya watu Wake. Ishara iliyoahidiwa ilikuwa imetolewa kwa Wakristo waliokuwa wakisubiri, na sasa fursa ilitolewa kwa wote ambao wangependa, watii onyo la Mwokozi. Matukio yalidhibitiwa ili kwamba Wayahudi wala Warumi wasizuie Wakristo kukimbia. Kufuatia kurudi nyuma kwa Ketio, Wayahudi, wakishambulia kuanzia Yerusalemu, walilikimbiza jeshi lakei; na wakati majeshi yote mawili yalipokuwa yameumana katika pambano, Wakristo walipata fursa ya kuondoka mjini. Wakati huu mji ulikuwa hauna maadui wo wote ambao wangejaribu kuwazuia. Wakati wa shambulio, Wayahudi walikuwa wamekusanyika kuadhimisha Siku kuu ya Vibanda, na hivyo Wakristo katika nchi nzima waliweza kukimbia bila bughudha yo yote. Bila kuchelewa walikimbilia mahali salama—mji wa Pela, katika nchi ya Perea, ng'ambo ya Yordani.

Majeshi ya Kiyahudi, yaliyokuwa yakimshambulia Ketio na jeshi lake, waliwaangukia upande wao wa nyuma kwa nguvu sana kiasi cha kutishia kuwaangamiza kabisa. Ilikuwa kwa shida kubwa sana Warumi walifaulu kukimbia na kurudi nyuma. Wayahudi walifaulu

kukimbia bila kupata hasira kubwa, na wakiwa na mali zao walizoziteka walirudi Yerusalemu kwa ushindi. Hata hivyo, ushindi huu wa juu juu uliwaletea matatizo makubwa. Uliwahamasisha kujenga roho ya upinzani na kiburi dhidi ya Warumi mambo ambayo yalisababisha madhara makubwa kwa mji uliokwisha kuhukumiwa kuharibiwa.

Majanga ya kutisha yaliukumba mji wa Yerusalemu wakati utekaji uliotekelezwa mara ya pili na Tito. Mji ulishambuliwa wakati wa Pasaka, wakati mamilioni ya Wayahudi walipokuwa wamekusanyika ndani ya kuta. Maghala yao ya vyakula, ambayo kama yangetunzwa kwa uangalifu yangeliweza kuhifadhi vyakula vya kuwatosha wakazi wa Yerusalemu kwa miaka mingi, yalikuwa yameharibiwa kwa sababu ya wivu na ulipizaji kisasi wa makundi yaliyohasimiana, na sasa tishio la kufa kwa njaa liliwakabili. Kipimo kimoja cha ngano kiliuzwa kwa talanta moja.

Maumivu ya njaa yalikuwa makali sana kiasi kwamba walitafuna ngozi za mikanda na gidamu za viatu vyao na mifuniko ya ngao zao. Idadi kubwa ya watu walitoroka usiku na kwenda kukusanya mimea ya porini iliyoota nje ya kuta za mji, japokuwa wengi wao walikamatwa na kuuliwa kwa mateso makali, na mara nyingi wale walioweza kurudi salama walinyang’anywa kile walichokuwa wamekikusanya katika mazingira mabaya na hatarishi. Mateso yasiyo na ubinadamu kabisa yalitumiwa na wale waliokuwa madarakani, kuwalazimisha walio na mahitaji wasalimishe chakula chochote kidogo ambacho walikuwa wamekificha. Na mambo haya ya ukatili hayakutendwa mara chache na watu ambao wao wenyewe walikuwa na chakula cha kutosha, na ambao lengo lao lilikuwa kujiwekea akiba kwa ajili ya wakati ujao.

Maelfu ya watu walikufa kwa njaa na magonjwa. Upendo wa asili ulionekana kuharibiwa kabisa. Waume waliibia wake zao, na wake waliwaibia waume zao. Watoto waliweza kuonekana wakinyakua chakula kutoka katika midomo ya wazazi wao wazee. Swali la nabii, “Je, mwanamke aweza kumshahu mtoto wake anyonyae?” lilipata jibu ndani ya kuta za mji uliokuwa umezingirwa pande zote: “Mikono ya wanawake wenye huruma Imewatokosa watoto wao wenyewe; Walikuwa ndio chakula chao Katika uharibifu wa binti ya watu wangu” (Isaya 49:15; Maombolezo 4:10). Tena ulitimizwa unabii wa onyo uliotolewa karne kumi na nne kabla: “Mwanamke kati yenu aliye mwororo na laini, ambaye hangehatarisha kuweka wayo wa mguu wake nchi kwa umalidadi na ulaini, jicho lake huyu litakuwa ovu juu ya mume wa kifuani mwake, na juu ya mwanawe, na juu ya binti yake,… na juu ya wanawe atakaowazaa; kwa kuwa atawala kwa siri, kwa uhitaji wa vitu vyote; katika mazingirwa na mkazo utakaokazwa na adui yako katika malango yako” (Kumbukumbu 28:56, 57).

Viongozi wa Kirumi walijaribu kuwatishia Wayahudi ili kuwafanya wajisalimishe. Wafungwa waliojaribu kupinga walipotekwa, walipigwa, waliteswa, na walisulubishwa mbele ya ukuta wa mji. Mamia waliuawa kwa njia hii, na kazi hii ya kuogofya iliendelea kufanywa mpaka, katika bonde lote la Yehoshati na Kalwari, misalaba ilisimikwa kwa wingi

kiasi kwamba kulikuwa hakuna nafsi ya kupita katikati yake. Laana ile iliyotamkwa mbele ya kiti cha hukumu cha Pilato ilileteleʐwa kwa jinsi ya kutisha: “Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu” (Mathayo 27:25).

Tito alikuwa tayari kusitisha zoezi hili la kutisha, na hivyo kutotekeleza kipimo kamili cha uharibifu wa mji wa Yerusalemu. Alitishika alipoona miili ya watu waliokufa ilivyorundikwa huko na huko katika mabonde. Kama mtu aliyeshikwa na butwaa, kutoka kilele cha mlima wa Mizeituni alitazama hekalu zuri na akatoa amri kuwa hata jiwe lake moja lisiguswe. Kabla ya kujaribu kuteka ngome hii, alitoa wito wa dhati kwa viongozi wa Kiyahudi wasimlazimishe kunajisi mahali patakatifu kwa damu. Ikiwa wangetoka na kupigania mahali pengine po pote, hakuna Mrumi ambaye angeharibu utakatifu wa hekalu. Josephus mwenyewe, kwa wito fasaha kabisa, aliwasihi wajisalimishe, ili wajiokoe wenyewe, mji wao, na mahali pao pa ibada. Lakini maneno yake yalijibiwa kwa laana kali. Mishale ilirushwa kumwelekea, mpatanishi wao wa mwisho wa kibinadamu, aliposimama kuwasihi. Wayahudi walikuwa wamekataa miito ya Mwana wa Mungu, na sasa malalamiko na nasaha viliwafanya wazidi kudhamiria kupinga mpaka mwisho. Juhudi za Tito kuliokoa hekalu hazikufua dafu; Yeye aliyekuwa mkuu kuliko yeye alikuwa ameshatangaza kuwa hakuna jiwe litakalosalia juu ya jiwe.

Ukaidi na upofu wa viongozi wa Kiyahudi, na uhalifu unaotisha uliofanyika ndani ya mji uliozungukwa, vilichochea chuki na hasira ya Warumi, na Tito hatimaye aliamua kuliteka hekalu kwa nguvu. Aliazimia, hata hivyo, kuwa ikiwezekana hekalu lisiharibiwe. Lakini amri zake zilipuuzwa. Baada ya kupumzika katika hema lake usiku, Wayahudi, wakitokea katika hekalu waliwashambulia maaskari wa Kirumi kwa nje. Katika pambano, kijinga cha moto kilirushwa na askari kupitia uwazi wa lango, na kwa ghafla, vyumba vilivyonakshiwa kwa mierezi kando kando ya nyumba takatifu viliwaka moto. Tito alifanya haraka kwenda eneo la tukio, akiwa amefuatana na majenerali na majeshi yake, na aliwaamuru maskari wauzime moto. Maneno yake hayakusikilizwa. Kwa hasira maaskari walirusha vijinga vya moto katika vyumba vilivyoshikamana na hekalu, na ndipo kwa mapanga yao waliwachinja watu wengi sana waliokuwa wamejihifadhi katika vyumba hivyo. Damu ilibubujika katika ngazi za hekalu kama maji. Maelfu kwa maelfu ya Wayahudi waliangamia. Juu ya kelele za vita, sauti zilisikika zikisema: “Ikabodi!”—utukufu umeondoka.

“Tito alishindwa kudhibiti hasira za maaskari; aliingia na maofisa wake, na kuchunguza eneo la ndani ya jengo takatifu. Uzuri wake uliwashangaza; na wakati ndimi za moto zilipokuwa bado hazijapenya na kuteketeza mahali patakatifu, alifanya juhudi zake za mwisho kupaokoa, alisogea mbele kwa haraka na kuwaagiza maaskari wasitishe zoezi la uchomaji moto hekalu. Mkuu wa kikosi husika, Liberalisi, alijaribu kuwalazimisha maofisa walio chini yake watii agizo; lakini hata heshima kwa mfalme ilishindwa na kuachia hasira na chuki dhidi ya Wayahudi, msisimko mkali wa vita, na tumaini na tamaa ya kupata nyara, vitawale. Maaskari waliona kila kitu kilichowazunguka kiking’aa kwa dhahabu iliyoakisi mwanga

mkali wa ndimi za moto; walidhania kuwa hazina ya dhahabu isiyokuwa na hesabu iliwekwa mahali fulani katika hekalu. Askari mmoja, kwa siri, alichomeka kijinga cha moto katikati za bawaba za mlango: jengo lote liliwaka moto mara moja. Moshi uliopofusha na ukali wa joto la moto viliwalazimisha maaskari kurudi nyuma, na kuliacha jengo zuri likiteketea.

"Lilikuwa tukio la kutisha kwa Mrumi—kwa Myahudi ilikuwaje? Kilele chote cha mlima uliotawala mji, kiliwaka moto kama volkano. Majengo yalianguka moja baada ya jingine, kwa mshindo mkuu, na yalimezwa katika utisho mkubwa wa moto. Mapaa ya mwerezi yalikuwa kama karatasi za ndimi za moto; vilele vya minara ya dhahabu viling'ara kama mikuki ya mwanga mwekundu; ngome za lango zilirusha juu mihimili ya ndimi za moto na moshi. Milima ya jirani ilimulikwa kwa mwanga; na makundi meusi ya watu yalionekana, watu waliangalia kwa wasiwasi na hofu maendeleo ya uharibifu: kando kando ya kuta na kwenye mitaa ya mji kulikuwa na nyuso nyingi, baadhi zikiwa nyeupe kwa uchungu wa kukata tamaa, nyingine zikiwa na mwonekano wa hasira na hitaji la kulipiza kisasi bila mafanikio.

Kelele za maaskari wa Kirumi waliokuwa wakikimbia huku na huku, na vilio vya maaskari wa Kiyahudi waliokuwa wakiungua ndani ya ndimi za moto, zilichanganyika na ngurumo za moto na sauti kubwa za mbao zilizokuwa zikidondoka chini. Myangwi ya milima ilijibu au ilirudisha sauti za uchungu za watu waliokuwa juu ya vilele vya milima; kando kando ya kuta zote zilisikika sauti za miguno ya maumivu na vilio; watu waliokuwa wakielekea kukata roho kwa kukosa chakula kwa muda mrefu walijikaza kwa nguvu kidogo zilizobaki kutoa kilio cha uchungu na kukata tamaa.

"Mauaji ya ndani yalikuwa ya kutisha zaidi kuliko mauji yaliyotokana na mashambulizi kutoka nje. Wanaume na wanawake, wazee na vijana, maaskari waasi na makuhani, waliopigana na wale waliosihi kuhurumiwa, wote walichinjwa na kuuliwa bila kuchagua. Idadi ya watu waliochinjwa ilikuwa kubwa kuliko idadi ya watu waliochinja. Majeshi ya Kirumi hayakuwa na budi kukanyaga marundo ya maiti ili waendelee na kazi yao ya kuangamiza."—Milman, The History of the Jews, book 16.

Baada ya kuharibu hekalu, mara moja mji wote uliangukia mikononi mwa Warumi. Viongozi wa Wayahudi walizikimbia ngome zao zisizopenywa kirahisi, na Tito aliwakuta wakiwa peke yao. Aliwatazama kwa mshangao, na alitangaza kuwa Mungu amewatia mikononi mwake; kwa kuwa hakuna zana yo yote, hata kama ingekuwa na nguvu kubwa kiasi gani, ingeweza kuhimili mapambano yale ya kutisha. Majengo ya mji na hekalu yaliungua hadi misingi yake, na uwanja mahali ambapo nyumba takatifu ilikuwa imesimama ulilimwa "kama shamba lilimwavyo" (Yeremia 26:18). Katika utekaji na uchinjaji uliofuata, zaidi ya watu milioni moja waliuawa; waliopona walichukuliwa mateka, waliuzwa kama watumwa, walikokotwa hadi Rumi kushuhudia ushindi wa mtekaji, walitupwa kwa wanyama wakali wa

porini katika viwanja vya michezo, au walitawanywa kama watu wasio na makazi wazururaji duniani kote.

Wayahudi walifua mikatale yao wenyewe; walikijaza kikombe cha kisasi wao wenyewe. Kwa uharibifu mkubwa uliowapata kama taifa, na kwa maumivu yaliyowafuata huko katika utawanyiko wao, walikuwa wakivuna mazao ambayo mikono yao ilikuwa imepanda. Nabii alisema: "Ee Israeli, umejiangamiza mwenyewe;" "maana umeanguka kwa sababu ya uovu wako" (Hosea 13:9; 14:1). Mateso yao mara nyingi yanawakilishwa kama adhabu iliyowasibu kwa agizo la Mungu moja kwa moja. Ndivyo mdanganyaji mkuu anavyojaribu kuficha kazi yake. Kwa kutupilia mbali upendo na neema ya Mungu kwa muda mrefu na kwa kiburi na shingo ngumu, Wayahudi walisababisha ulinzi wa Mungu uondolewe kutoka kwao, na Shetani aliruhusiwa kuwatawala kulingana na mapenzi yake. Ukatili wa kutisha katika kuiharibu Yerusalemu ni kielelezo cha nguvu ya Shetani isiyo na huruma juu ya wale wanaojiweka chini ya utawala wake.

Hatuwezi kujua ni kiasi gani tunawiwa na Kristo kwa ajili ya amani na ulinzi tulio nao. Ni nguvu inayodhibiti ya Mungu inayozuia wanadamu wasiwe chini ya utawala wa Shetani kikamilifu. Wasiokuwa watiifu na wasio na shukurani wana sababu kubwa ya kushukuru rehema na uvumilivu wa Mungu kwa kudhibiti nguvu yenye ukatili na ubaya wa mwovu. Lakini watu wanapopita mipaka ya uvumilivu wa Mungu, udhibiti unaondolewa. Mungu hasimami mbele ya mwenye dhambi kama mtekelezaji wa hukumu dhidi ya makosa yake; lakini huwaacha waliotupilia mbali rehema yake washughulikiane wenyewe kwa wenyewe, wavune walichokipanda. Kila mwale wa nuru uliotupiliwa mbali, kila onyo lililodharauliwa au kutosikilizwa, kila tamaa iliyopaliliwa, kila uvunjaji wa sheria ya Mungu, ni mbegu iliyopandwa ambayo huzaa mavuno bila kukosea. Roho wa Mungu, anapopingwa kwa wakati wote, hatimaye huondolewa kutoka kwa mwenye dhambi, na ndipo haibaki tena nguvu ya kudhibiti tamaa mbaya za moyoni, na haubaki ulinzi dhidi ya ukatili na uadui wa Shetani. Uharibifu wa Yerusalemu ni onyo la kutisha na la dhati kwa wote wanaopuuza fursa za neema na wanaopinga miito ya rehema ya Mungu. Kamwe haujawahi kutolewa ushuhuda mkubwa zaidi kuliko huo juu ya chuki ya Mungu dhidi ya dhambi na adhabu ya hakika itakayowapata wenye hatia.

Unabii wa Mwokozi kuhusu kumwagwa kwa hukumu juu ya Yerusalemu una utimizo mwingine, ambao kwao ukiwa ule wa kutisha ulikuwa kivuli hafifu tu. Katika kile kilichoupata mji mteule tunaweza kuona uharibifu wa ulimwengu ambao umekataa rehema ya Mungu na kuikanyaga sheria Yake. Kumbukumbu za taabu za wanadamu ambazo dunia imezishuhudia katika kipindi chake cha karne ndefu za uhalifu ni nyeusi. Moyo unaugua, na akili inazimia kwa kutafakari. Matokeo ya kukataa mamlaka ya Mbingu ni ya kutisha sana. Lakini tukio la kutisha zaidi limewasilishwa katika ufunuo wa wakati ujao. Kumbukumbu za matukio ya zamani,—mlolongo mrefu wa fujo, migogoro, na mapinduzi,"silaha zote za mtu mwenye silaha wakati wa mshindo, na mavazi yaliyofingirishwa katika damu" (Isaya 9:5),—

haya ni nini, ukilinganisha na vitisho vya siku ile wakati Roho wa Mungu anayedhibiti uovu atakapoondolewa kwa waovu, ili asizuie mlipuko wa misisimko na hasira za kishetani! Ndipo ulimwengu utaona, kuliko ilivyowahi kutokea, matokeo ya utawala wa Shetani.

Lakini katika siku ile, kama ilivyokuwa katika uharibifu wa Yerusalemu, watu wa Mungu watakombolewa, kila mmoja atakayeonekana ameandikwa miongoni mwa walio uzima (Isaya 4:3). Kristo alisema kuwa atakuja mara ya pili kuwakusanya waaminifu Wake awachukue Kwake: "Ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu" (Mathayo 24:30, 31). Ndipo wale ambao hawakuitii injili wataangamizwa kwa pumzi ya kinywa Chake na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo Kwake(2 Wathesalonike 2:8). Kama Israeli ya zamani waovu wanajiangamiza wenyewe; wanaanguka kwa uovu wao wenyewe. Kwa njia ya maisha yao ya dhambi, wanajiweka nje ya upatanifu na Mungu, asili zao zikiwa zimeharibiwa na uovu sana, kiasi ambacho kufunuliwa kwa utukufu Wake kunakuwa moto ulao.

Hebu watu wawe waangalifu wasije wakapuuza somo lililotolewa kwao katika maneno ya Kristo. Kama alivyowaonya wanafunzi Wake kuhusu uharibifu wa Yerusalemu, kwa kuwapa ishara ya maangamizi yaliyokuwa yanakaribia, ili waweze kukimbia na kuponya nafsi zao; kadhalika ameuonya ulimwengu kuhusu siku ya uharibifu wa mwisho na amewapa ishara ya ukaribu wake, ili wale watakaopenda kuokoa nafsi zao waweze kuikimbia hasira inayokuja. Yesu alisema: "Kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota; na katika nchi dhiki ya mataifa" (Luka 21:25; Mathayo 24:29; Marko 13:24-26; Ufunuo 6:12- 17). Wanaoziona ishara hizo za ujio Wake inawapasa watambue "kuwa yu karibu, mlangoni" (Mathayo 24:33). "Kesheni basi," ndiyo maneno Yake ya onyo (Marko 13:35). Watakaotii onyo hawatabaki gizani, hata siku ile iwakute bila maandalizi. Bali kwa wale wasiokesha, "siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku" (1 Wathesalonike 5:2-5).

Ulimwengu uko tayari zaidi kuukubali ujumbe wa wakati huu kuliko Wayahudi walivyokuwa tayari kupokea onyo kuhusu Yerusalemu. Bila kujali ni lini itafika, siku ya Mungu itakuja bila taarifa kwa watu wasiomcha Mungu. Wakati maisha yanaendelea katika hali yake ya kawaida ya siku zote; wakati watu wamemezwa katika starehe, katika biashara, katika usafiri, katika utafutaji wa pesa; wakati viongozi wa dini wanahamasisha maendeleo na elimu ya dunia, na watu wakiwa wanabembelezwa na usalama bandia— ndipo, kama mwizi anavyokuja usiku wa manane katika nyumba ambayo haina mlinzi, ndivyo uharibifu utakavyowajia wasiojali na wasiomcha Mungu, "wala hakika hawataokolewa" (Aya ya 3).

Sura ya 2 - Ubatizo wa Moto

Jesu alipowafunulia hatima ya Yerusalemu na matukio ya ujio wa pili, alitabiri pia uzoefu wa watu Wake tangu wakati ambao angechukuliwa kutoka kwao, hadi kurudi Kwake katika nguvu na utukufu kwa ajili ya ukombozi wao. Kutokea kwenye Mlima wa Mizeituni Mwokozi aliziona dhoruba ambazo zingelikabili kanisa la mitume; na akipenya zaidi katika wakati ujao, jicho Lake lilibaini pepo kali, zinazotisha ambazo zingewapiga wafuasi Wake katika zama zilizokuwa zinakuja za giza na mateso. Katika matamko machache ya maana na ya kutisha alitabiri kiwango ambacho watawala wa ulimwengu huu wangechangia katika kulitesa kanisa la Mungu (Mathayo 24:9, 21, 22). Iliwapasa wafuasi wa Kristo kupita katika njia ile ile ya unyenyekevu, aibu, na mateso aliyopitia Bwana wao. Uadui uliomkabili Mkombozi wa ulimwengu ungedhihirishwa dhidi ya wote ambao wangeliamini jina Lake.

Historia ya kanisa la awali ilishuhudia utimizo wa maneno ya Mwokozi. Nguvu za dunia na za kuzimu zilijipanga dhidi ya Kristo kwa kupinga kazi ya wafuasi Wake. Upagani ulibaini mapema kuwa ikiwa injili ingefanikiwa, mahekalu yao na madhabahu zao zingefutiliwa mbali; kwa hiyo ulikusanya majeshi yake yote kuharibu Ukristo. Mioto ya mateso iliwashwa. Wakristo walinyang'anywa mali zao na kufukuzwa kutoka katika nyumba zao. Walistahimili "mashindano makubwa ya maumivu" (Waebrania 10:32). Wengine "walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani" (Waebrania 11:36). Idadi kubwa miongoni mwao walitia muhuri ushuhuda wao kwa damu yao. Mtu huru kwa mtumwa, tajiri na maskini, wasomi na wasiokuwa wasomi, wote pamoja waliuawa bila rehema. Mateso haya, yakianzia chini ya Nero karibu na wakati wa kuuawa kwa Paulo, yaliendelea kwa kiwango kikubwa au kidogo kwa karne kadhaa.

Wakristo walishitakiwa kwa uongo wakihusishwa na uhalifu wa kutisha sana na kutangazwa kuwa chanzo cha majanga makubwa—njaa, magonjwa, na matetemeko ya ardhi. Walipofanywa kuwa walengwa wa chuki mashaka ya kila mtu, watoa taarifa walisimama tayari, kwa ajili ya mapato, kuwasaliti watu wasio na hatia. Walihukumiwa kama waasi dhidi ya dola, kama maadui wa dini, na chukizo kwa jamii. Idadi kubwa miongoni mwao walitupwa kwa wanyama wakali au waliunguzwa moto katika viwanja vya maonesho. Baadhi walisulubishwa; wengine walifunikwa kwa ngozi za wanyama pori na kusukumiwa katika viwanja vya michezo ili wararuliwe na mbwa. Adhabu yao ilifanywa kuwa burudani katika sherehe za umma. Umati mkubwa wa watu ulihudhuria kufurahia mateso yao na watazamaji waliangua vicheko na nderemo walipowaona wahanga wa mateso wakifa kwa uchungu mkubwa.

Popote walipotafuta makimbilio, hawa wafuasi wa Kristo walisakwa kama wanyama wa mawindo. Walilazimika kujificha katika maeneo ya ukiwa na upweke. "Walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa mabaya; (watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao), walikuwa wakizunguka-zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo

ya nchi" (Aya ya 37, 38). Mapango yalitumiwa na maelfu kama maficho. Chini ya milima nje ya mji wa Rumi, mahandaki marefu yalikuwa yamechorongwa katika ardhi na miamba; mtandao wenye giza na tata wa njia za mahandaki ulienea umbali wa maili kadhaa mbali na kuta za mji. Katika maficho haya ya chini ya ardhi wafuasi wa Kristo waliwazika wenzao waliokufa; na hapa pia, waliposhukiwa na kupigwa marufuku, walikuja kuishi hapa kama nyumbani kwao. Wakati Mpaji wa uzima atakapowaamsha wale waliopigana vita vizuri, wafia dini wengi kwa ajili ya Kristo watatoka katika hayo mahandaki yenye giza.

Katika mateso makali sana hawa mashahidi wa Yesu waliihifadhi imani yao bila kuichafua. Pamoja na kuwa walinyang'anywa kila aina ya utulivu, wakiwa mahali pasipokuwa na mwanga wa jua, wakiishi gizani lakini katika kifua cha ardhi, hawakutamka neno lo lote la lawama. Kwa maneno ya imani, uvumilivu, na tumaini walitiana moyo kuvumilia umaskini na maumivu. Hasara ya baraka za duniani haikuweza kuwalazimisha kuikana imani yao kwa Kristo. Majaribu na mateso yalikuwa ngazi ya kuwaleta karibu zaidi na pumziko lao na zawadi yao.

Kama watumishi wa zamani wa Mungu, wengi wao "waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufuo ulio bora" (Aya ya 35). Haya yaliwakumbusha maneno ya Bwana wao, kuwa wanapoteswa kwa ajili ya Kristo walipaswa kufurahi kwa furaha kuu, kwa kuwa thawabu yao ingekuwa kubwa mbinguni; kwa kuwa ndivyo manabii walivyoteswa kabla yao. Walifurahi kwa sababu walihesabiwa kustahimili mateso kwa ajili ya ukweli, na nyimbo za shangwe zilipanda juu kutoka katikati ya chakarika ya ndimi za moto. Wakitazama juu kwa imani, walimwona Kristo na malaika wakiwa wameinama juu ya kuta za mbinguni, wakiwaangalia kwa shauku kubwa na wakiafiki msimamo wao imara. Sauti iliwaijia kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu: "Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima" (Ufunuo 2:10).

Ilikuwa juhudi za bure kwa Shetani kujaribu kuliharibu kanisa la Kristo kwa nguvu. Pambano kuu ambamo wanafunzi wa Yesu walisalimisha maisha yao halikwisha wakati hawa wabeba bendera waaminifu walipofia kwenye lindo lao. Kwa kushindwa kwao walishinda. Watenda kazi wa Mungu walichinjwa, lakini kazi Yake ilisonga mbele daima. Injili iliendelea kusambaa na idadi ya wafuasi wake ilizidi kuongezeka. Ilipenya katika maeneo yaliyokuwa hayafikiwi na majeshi ya Kirumi. Mkristo mmoja alisema, akibishana na watawala wa kipagani waliokuwa wakihamasisha mateso ya Wakristo: Mnaweza "kutuua, kututesa, kutuhukumu Uonevu wenu ni ushahidi kuwa sisi hatuna hatia. Wala ukatili wenu hautawasaidia." Huu ulikuwa mwaliko wenye nguvu zaidi wa kuwaleta wengine katika Ukristo. "Kwa kadiri mnavyotuchinja, ndivyo idadi yetu inavyozidi kuongezeka; damu ya Wakristo ni mbegu."—Tertullian, Apology, paragraph 50.

Maelfu walifungwa na kuchinjwa, lakini wengine waliibuka na kujaza nafasi zao. Na wale waliouawa kwa ajili ya imani yao walikufa katika Kristo na kuhesabiwa kuwa washindi.

Walipiga vita vizuri, na wanatazamia kupokea taji ya utukufu wakati Kristo akija mara ya pili. Mateso waliyoyapata yaliwaleta karibu wao kwa wao na wote kwa pamoja karibu na Mwokozi wao. Mfano wao wa maisha na ushuhuda wa vifo vyao vilikuwa ushuhuda wa daima wa ukweli; na wakati ilipotarajiwa kidogo sana, wafuasi wa Shetani waliachana na utumishi wa Shetani na kuja kutumika chini ya bendera ya Kristo.

Shetani, hivyo basi, aliweka mipango kupigana vita kwa mafanikio zaidi dhidi ya serikali ya Mungu kwa kusimika bendera yake katika kanisa la Kikristo. Ikiwa wafuasi wa Kristo wangedanganywa na kuongozwa kumkosea Mungu, ndipo nguvu yao, ujasiri wao, na uimara wao vingehafifishwa, na wangekuwa mawindo rahisi ya Shetani.

Adui mkuu sasa alijielekeza kupata kwa njia ya udanganyifu alichoshindwa kukipata kwa nguvu. Mateso yalikoma, na badala yake viliingizwa vishawishi vya hatari vya mafanikio ya muda na heshima ya dunia. Waabudu sanamu waliongozwa kupokea sehemu ya imani ya Kikristo, huku wakitupilia mbali kweli zingine muhimu. Walidai kumkiri Yesu kuwa Mwana wa Mungu na kuamini mauti na ufufuo Wake, lakini hawakushawishika kuwa ni wenye dhambi wala kuhisi haja ya toba au ya badiliko la moyo. Kwa wao kupunguza mambo fulani katika imani zao walipendekeza kuwa Wakristo nao wapunguze baadhi ya mambo, ili wote waungane kwenye jukwaa la imani ya Kikristo.

Sasa kanisa lilikuwa katika hatari ya kutisha. Gereza, maumivu, moto, na upanga vilikuwa baraka ukilinganisha na mwelekeo huu. Baadhi ya Wakristo walisimama imara, wakisema kuwa wasingekubali kulegeza masharti. Baadhi yao waliunga mkono wazo la kulegeza masharti au kurekebisha baadhi ya vipengele vya imani yao na kuungana na waliokubali sehemu ya Ukristo, wakidai kuwa kufanya hivyo kungekuwa njia ya uongofu wao kamili. Huo ulikuwa wakati wa kilio kikuu kwa wafuasi wa Kristo waaminifu. Katika vazi la Ukristo bandia, Shetani alikuwa akijipenyeza katika kanisa, ili achafue imani yao na kugeuza akili zao kutoka kwenye neno la ukweli.

Hatimaye Wakristo walio wengi walikubali kushusha viwango vyao, na muungano uliundwa kati ya Ukristo na upagani. Ingawa waabudu sanamu walidai kuwa wameongoka na kujiunga na kanisa, bado waliendelea kung'ang'ania ibada zao za sanamu, wakibadilisha tu vitu vya kuabudu kuwa sanamu za Yesu, Mariamu, na watakatifu. Chachu mbaya ya sanamu, iliyoingizwa kanisani kwa njia hiyo, iliendeleza kazi yake ya uharibifu. Mafundisho potofu, kaida za kishirikina, na sherehe za ibada ya sanamu zilijumuishwa katika imani na ibada ya kanisa. Wafuasi wa Kristo walipoungana na waabudu sanamu, dini ya Kikristo ilinajisiwa, na kanisa lilipoteza usafi na nguvu yake. Walikuwepo baadhi, hata hivyo, ambao hawakupotoshwa na makosa haya. Bado walidumisha uaminifu wao kwa Mwasisi wa ukweli na walimwabudu Mungu pekee.

Kumekuwepo daima matabaka mawili miongoni mwa watu wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo. Wakati tabaka moja linajifunza maisha ya Mwokozi na kwa dhati hutafuta kusahihisha

kasoro zao na kufuata mfano wa Kristo, tabaka jingine hujiepusha na ukweli wa wazi, unaohusu maisha ya kila siku, ambao hufunua dosari zao. Hata wakati wa usafi wake wa juu kabisa, kanisa halikuundwa na watu ambao wote ni wa kweli, safi, na wa dhati. Mwokozi wetu alifundisha kuwa wale ambao kwa kuchagua waliendekeza dhambi hawakupaswa kupokelewa ndani ya kanisa; lakini alijihusisha na watu waliokuwa na kasoro katika tabia, na aliwapa msaada kwa mafundisho na mfano Wake, ili wapate fursa ya kuona kasoro zao na kuzisahihisha. Miongoni mwa wale kumi na wawili alikuwemo msaliti. Yuda alipokelewa, siyo kwa sababu ya dosari zake za tabia, bali alipokelewa pamoja na kwamba alikuwa nazo. Aliunganishwa na wanafunzi, ili, kwa njia ya mafundisho ya mfano wa Kristo, aweze kujifunza mambo yanayounda tabia ya Kikristo, na hivyo aweze kuongozwa kuona dosari zake, atubu, na, kwa msaada wa neema ya Mungu, asafishe roho yake "kwa kuitii kweli." Lakini Yuda hakutembea katika nuru ambayo kwa neema ya Mungu iliruhusiwa imwangazie. Kwa kuendekeza dhambi aliyaalika majaribu ya Shetani. Mazoea mabaya ya tabia yaliruhusiwa kutawala. Alisalimisha akili yake chini ya utawala wa nguvu za giza, alikasirika wakati makosa yake yalipokemewa, na hivyo aliongozwa

kutenda uhalifu wa kutisha wa kumsaliti Bwana wake. Kadhalika, watu wote wanaolea uovu chini ya mwavuli wa utaua huwachukia wale wanaosumbua amani yao kwa kukemea njia yao ya dhambi. Fursa inayofaa ikijitokeza, kama Yuda, wanawasaliti wale ambao kwa faida yao, wanajaribu kuwakosoa. Mitume walikutana na watu kanisani waliodai kuwa wacha Mungu wakati kwa siri walilea uovu. Anania na Safira walisema uongo, wakijifanya kuwa wametoa vyote kwa Mungu, wakati kwa uchoyo walizuia sehemu kwa ajili yao wenyewe. Roho wa ukweli aliwafunulia mitume tabia halisi ya hawa wanaojifanya, na hukumu za Mungu zilifuta doa hili la uchafu kutoka katika kanisa lililokuwa safi. Ushuhuda huu wa wazi wa utambuzi wa Roho wa Kristo katika kanisa ulikuwa ni tishio kwa wanafiki na watenda maovu.

Wasingedumu kushikamana kwa muda mrefu na wale ambao, kwa tabia na mwenendo, walikuwa wawakilishi wa kudumu wa Kristo; na majaribu na mateso yalipowajia wafuasi Wake, wale tu ambao waolikuwa tayari kuacha kila kitu kwa ajili ya ukweli ndio waliobaki kuwa wanafunzi Wake. Kwa hiyo, kwa kadiri mateso yalivyoendelea kuwepo, kanisa lilibaki kwa kiasi kikubwa likiwa safi. Lakini mateso yalipokoma, waongofu waliongezeka ambao baadhi yao hawakuwa waliojitoa kikamilifu, na njia ilifunguliwa kwa Shetani kukita mizizi ndani ya kanisa.

Lakini hakuna muungano kati ya Mfalme wa nuru na mfalme wa giza, na haiwezekani kukawepo muungano kati ya wafuasi wao. Wakristo walipokubali kuungana na wale waliokuwa wameongoka nusu kutoka katika upagani, walifuata njia ambayo iliwapeleka mbali na ukweli zaidi na zaidi. Shetani alifurahia kwa kufanikiwa kudanganya idadi kubwa ya wafuasi wa Kristo. Ndipo alipotumia nguvu zake zaidi kuwabana hawa, na kuwafanya wawatese waliobaki wakiwa waaminifu kwa Mungu. Hakuna aliyejua vizuri zaidi kupinga

imani ya kweli ya Kikristo kuliko wale ambao awali walikuwa watetezi wake; na hawa Wakristo waasi, wakiungana na wenzao ambao ni nusu wapagani, walielekeza vita yao dhidi ya vipengele muhimu sana vya mafundisho ya Kristo.

Ilihitaji jitihada kubwa sana kwa wale ambao wangekuwa waaminifu kusimama imara dhidi ya udanganyifu na machukizo yaliyofichwa katika mavazi ya kikuhani na kuingizwa katika kanisa. Biblia haikukubaliwa kama kiwango cha imani. Fundisho la uhuru wa dini liliitwa fundisho la uongo na waliolitetea walichukiwa na kutengwa.

Baada ya pambano la muda mrefu na kali, waaminifu wachache waliamua kuvunja uhusiano na kanisa lililoasi ikiwa lingeendelea kukataa kukumbatia uongo na ibada ya sanamu. Waliona kuwa kujitenga lilikuwa suala lisiloepukika ili waweze kutii neno la Mungu. Wasingeweza kuvumilia makosa ambayo yaliua roho zao, na kuonesha mfano ambao ungehatarisha imani ya watoto na wajukuu wao. Ili kupata amani na umoja walikuwa tayari

Kufanya makubaliano na jambo lo lote ambalo lilikubaliana na uaminifu kwa Mungu; lakini waliamini kuwa amani isingeweza kununuliwa kwa kuvunja kanuni. Ikiwa umoja ulimaanisha kulegeza masharti ya ukweli na utakatifu, ni afadhali kuwepo tofauti, na hata vita.

Ingekuwa vema kwa kanisa na ulimwengu ikiwa kanuni zilizowaongoza watu wale wenye msimamo zingeamshwa katika mioyo ya watu wanaodai kuwa watu wa Mungu. Kuna usingizi wa kutisha kuhusiana na mafundisho ambazo ni nguzo za imani ya Kikristo. Maoni yalikuwa yakinzidi kupata nguvu, kuwa, hata hivyo, haya siyo ya muhimu sana. Uozo huu unaoimarisha zaidi mikono ya mawakala wa Shetani, yaani nadharia potofu na uongo unaofisha ambao ulihatarisha maisha ya waaminifu walipoupinga na kuufunua katika zama zilizopita, sasa unakubaliwa na maelfu ya watu wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo.

Wakristo wa awali walikuwa kweli watu wa pekee sana. Tabia zao zisizo na doa na imani yao isiyoyumba vilikuwa ni kemeo la daima lililosumbua amani ya mwenye dhambi. Japokuwa walikuwa wachache kwa idadi, bila mali, cheo, au majina yenye heshima, walikuwa tishio kwa waovu mahali popote ambapo tabia na mafundisho yao vilijulikana. Kwa hiyo walichukiwa na watu waovu, sawa na jinsi Habili alivyochukiwa na Kaini mwovu. Kwa sababu ile ile ambayo kwayo Kaini alimwua Habili, waliotupilia mbali udhibiti wa Roho Mtakatifu, waliwaua watu wa Mungu. Ilikuwa ni kwa sababu hiyo hiyo Wayahudi walimkataa na kumsulibisha Mwokozi—kwa sababu usafi na utakatifu wa tabia Yake ulikuwa kemeo la kudumu kwa uchoyo na ufisadi wao. Tangu siku za Kristo mpaka sasa wanafunzi Wake waaminifu wameamsha chuki na upinzani wa wale wanaopenda na kufuata njia za dhambi.

Hivyo basi, ni kwa jinsi gani injili inaweza kuitwa ujumbe wa amani? Isaya alipotabiri juu ya kuzaliwa kwa Masihi, alimpa jina,“Mfalme wa Amani.”Wakati malaika

walipowatangazia wachungaji kuwa Kristo amezaliwa, waliimba juu ya mbuga za Bethlehemu: “Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia” (Luka 2:14). Kama vile kuna hali ya kukinzana kati ya matamko ya unabii na maneno ya Kristo: “Sikuja kuleta amani, bali upanga”(Mathayo 10:34).

Lakini, zikieleweka vizuri, aya hizo mbili zinapatana kabisa. Injili ni ujumbe wa amani. Ukristo ni mfumo ambao, ukipokelewa na kutiiwa, unaweza kueneza amani, mapatano, na furaha duniani. Dini ya Kristo inawaunganisha wote wanaoyapokea mafundisho yake na kuwafanya kuwa ndugu wa karibu. Ilikuwa utume wa Yesu kuwapatanisha wanadamu na Mungu, na hivyo kumpatanisha mwanadamu na mwenzake. Lakni sehemu kubwa ya ulimwengu iko chini ya utawala wa Shetani, adui mkuu wa Kristo. Injili inawasilisha kwao kanuni za maisha ambazo zinakinzana na mazoea na shauku zao, na wanainuka dhidi yake. Wanachukia usafi unaofunua na kuhukumu dhambi zao, na wanatesa na kuharibu wale wanaotetea madai yake halali na matakatifu. Ni kwa maana hii—kwa sababu ya ukweli wake ulio juu injili inasababisha chuki na migogoro—ndiyo maana injili inaitwa upanga.

Hekima ya Mungu isiyokuwa na maelezo inayoruhusu wenye haki wateswe na waovu imekuwa chanzo cha mashaka makubwa kwa wengi walio na imani dhaifu. Baadhi wanafikia hatua ya kupoteza tumaini kwa Mungu kwa sababu anaruhusu watu waovu kabisa wafanikiwe, wakati watu wazuri na walio safi kabisa wanaumia na kuteswa kwa nguvu zao za kikatili. Kwa jinsi gani, watu wanauliza, inawezekanaje Mungu ambaye ni mwenye haki na rehema, na ambaye hana ukomo katika nguvu zake, avumilie dhuluma na uonevu kama huo? Hili ni swali ambalo hatuna cho chote cha kufanya. Mungu ametupatia ushahidi wa kutosha wa upendo Wake, na hatuna mashaka kuhusu wema Wake kwa sababu hatuwezi kuelewa utaratibu wa hekma Yake. Mwokozi aliwaambia wanafunzi Wake, kwa kutarajia mashaka ambayo yangesonga roho zao nyakati za majaribu na giza: “Likumbukeni lile neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi” (Yohana 15:20). Yesu aliteseka kwa ajili yetu zaidi kuliko ye yote miongoni mwa wafuasi Wake anavyoweza kuteseka kwa sababu ya ukatili wa wanadamu waovu. Wale ambao wameitwa kuteseka na kufa kwa ajili ya Kristo wanafuta nyayo za Mwana mpendwa wa Mungu.

“Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake” (2 Petro 3:9). Hasahau au kuwatelekeza watoto Wake; bali anawaruhusu waovu waoneshe tabia yao halisi, ili ye yote aliye na shauku ya kutenda mapenzi ya Mungu asidanganyike kuhusiana nao. Kadhalika, wenye haki wanawekwa katika tanuru ya mateso ili watakaswe; ili kwamba mfano wao uwashawishi wengine kuhusiana na uhalisia wa imani na utaua; na ili kwamba mwenendo wao usioyumba uwahukumu wasiomcha Mungu na wasioamini.

Mungu anaruhusu watu waovu wafanikiwe na wadhihirishe uadui wao dhidi Yake, ili wakati watakapokuwa wamejaza kipimo cha uovu wao watu wote waweze kuona haki na

rehema Yake wakati anapowaangamiza kabisa. Siku ya kisasi chake inakuja upesi, wakati wale wote ambao wamevunja sheria Yake na kuwakandamiza watu Wake watapokea zawadi stahiki ya matendo yao; wakati kila tendo la ukatili na uonevu kwa waaminifu wa Mungu litaadhibiwa kana kwamba ni Kristo Mwenyewe aliyetendewa.

Kuna swali lingine muhimu ambalo lapaswa kujibiwa na makanisa ya leo. Mtume Paulo alisema “na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa” (2 Timotheo 3:12). Kwanini, sasa, mateso yanaonekana kwa kiasi kikubwa kusinzia? Sababu pekee ni kuwa kanisa limekubaliana na kiwango cha dunia na kwa hiyo haliamshi upinzani. Dini ambayo ipo katika siku zetu haina tabia iliyo safi na takatifu kama dini ya siku za Kristo na mitume. Ni kwa sababu tu ya roho ya mapatano na dhambi, ni kwa sababu kweli kuu za neno la Mungu hazitiliwi manani ipasavyo, ni kwa sababu kuna utawa kidogo katika kanisa, ni kana kwamba Ukristo unapendwa na ulimwengu. Hebu na kuwepo uamsho wa imani na nguvu ya kanisa la awali, na roho ya mateso itaamshwa, na mioto ya mateso makali itawashwa upya.

Sura ya 3 - Zama za Giza la Kiroho

Mtume Paulo, katika barua yake ya pili kwa Wathesalonike, alitabiri uasi mkuu ambao ungetokana na uanzishwaji wa mamlaka ya upapa. Alitangaza kuwa siku ya Kristo isingekuja, "usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu." Na zaidi hapo, mtume Paulo anatahadharisha ndugu zake kuwa "ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi; lakini yuko azuiaye sasa, hata atakapoondolewa" (2 Wathesalonike 2:3, 4, 7). Hata katika tarehe hizo za awali, aliona, yakiingia polepole kanisani, makosa ambayo yangetayarisha njia kwa ajili ya ukuaji wa upapa.

Kidogo kidogo, mwanzoni kwa siri na katika hali ya ukimya, na hatimaye kwa uwazi zaidi kwa kadiri makosa yalivyozidi kupata nguvu na kutawala akili za watu, "siri ya uasi" iliendeleza kazi yake ya udangayifu na kufuru. Karibu pasipokutambua, mila na desturi za upagani ziliingia ndani ya kanisa. Roho ya kulegeza masharti na kuiga ilidhibitiwa kwa muda kwa mateso makali ambayo kanisa liliyapata chini ya upagani. Lakini mara tu mateso yalipokoma, na Ukristo ukaingia katika mabaraza na nyumba za kifalme, kanisa liliweka pembeni usahili na unyenyekevu wa Kristo na wa mitume Wake na badala yake lilivaa kujionesha na kiburi cha makuhani wa kipagani na watawala; na badala ya matakwa ya Mungu, kanisa liliweka nadhar ia na desturi za wanadamu. Uongofu wa juu juu wa Konstantino, katika sehemu ya awali ya karne ya nne, ulileta furaha kubwa; na ulimwengu, uliojifunika joho la utakatifu bandia, uliingia kanisani.Sasa kazi ya upotovu ikaendelea kwa kasi. Upagani, wakati ukionekana kana kwamba umekwisha, ulishinda. Roho yake ilitawala kanisa. Mafundisho yake, sherehe, na ushirikina vilijumuishwa katika imani na ibada ya watu waliodai kuwa wafuasi wa Kristo.

Muungano huu wa upagani na Ukristo uliwezesha kuzaliwa kwa "mtu wa dhambi" aliyetabiriwa katika unabii kuwa atapingana na kujiinua juu ya Mungu. Mfumo huo mkubwa wa dini ya uongo ni chombo maalumu cha nguvu ya Shetani—mnara wa kumbukumbu ya juhudi zake kukaa juu ya kiti cha enzi na kuitawala dunia kulingana na mapenzi yake.

Shetani wakati fulani alijaribu kuunda umoja na Kristo. Alimjia Mwana wa Mungu katika jangwa la majaribu, na akimwonesha falme za ulimwengu na utukufu wa falme hizo, akiahidi kuziweka katika Mikono Yake ikiwa tu atakiri ukuu wa mfalme wa giza. Kristo alimkemea mjaribu mwenye kiburi na kumlazimisha aondoke. Lakini Shetani anafanikiwa sana anapomletea mwanadamu majaribu hayo hayo. Ili kupata mapato na heshima za kidunia, kanisa liliongozwa kutafuta msaada na uungwaji mkono wa watu wakubwa duniani; na baada ya kumwacha Kristo kwa njia hiyo, lilishawishika kujisalimisha chini ya wakala wa Shetani—askofu wa Rumi.

Ni moja ya mafundisho makuu ya Urumi kuwa papa ni kichwa kinachoonekana cha kanisa la ulimwengu la Kristo, aliyekabidhiwa mamlaka kuu juu ya maaskofu na wachungaji katika sehemu zote za dunia. Zaidi ya hayo, papa amepewa majina ya Mungu mwenyewe. Anatambulishwa kuwa yeye ni "Bwana Mungu Papa" (tazama Kiambatanisho), na anatangazwa kuwa yeye hakosei. Anadai aabudiwe na watu wote. Dai lile lile lililotolewa na Shetani katika jangwa la majaribu bado linatolewa naye kupitia kwa Kanisa la Rumi, na kuna idadi kubwa ya watu wanaomwabudu.

Lakini watu wanaomcha na kumheshimu Mungu wanakabiliana na madai haya ya kutisha kama Kristo alivyokabiliana na madai ya adui mkuu: "Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake" (Luka 4:8). Mungu hajadokeza mahali popote katika neno Lake kuwa amemteua mtu ye yote kuwa kichwa cha kanisa. Fundisho la ukuu wa papa linapingana kabisa na mafundisho ya Maandiko. Papa hawezi kuwa na mamlaka juu ya kanisa la Kristo isipokuwa kwa kujichukulia madaraka. Viongozi wa kanisa la Rumi wanaendelea kuleta mashitaka dhidi ya Waprotestanti kuwa wameleta mafundisho ya uongo na kwa makusudi wakajitenga na kanisa. Lakini mashtaka haya ni yao hasa. Wao ndio walioishusha bendera ya Kristo na kuikana "imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu" (Yuda 3).

Shetani alijua vizuri kuwa Maandiko Matakatifu yangewawezesha watu kutambua udanganyifu na kupinga nguvu zake. Ilikuwa ni kwa njia ya neno hata Mwokozi wa ulimwengu aliweza kuyapinga mashambulizi yake. Kwa kila shambulizi, Kristo alijikinga kwa ngao ya ukweli wa milele, akisema, "Imeandikwa." Kwa kila pendekezo la adui, aliweka pingamizi la hekima na nguvu ya neno. Ili Shetani adumishe utawala wake juu ya wanadamu, na kustawisha mamlaka ya kipapa, alilazimika kuwafanya watu wasiyajue Maandiko. Biblia inamwinua Mungu na inawaweka wanadamu katika nafasi zao stahiki; kwa hiyo kweli zake takatifu ilipaswa zifichwe na kukandamizwa. Mantiki hii iliigwa na Kanisa la Kirumi. Kwa mamia ya miaka usambazaji wa Biblia ulipigwa marufuku. Watu walikatazwa kuisoma au kuwa nayo katika nyumba zao, na mapadre na maaskofu wasiozingatia kanuni walitafsiri mafundisho yake kuunga mkono mitazamo yao. Kwa njia hiyo papa akatokea kukubaliwa duniani kote kama mwakilishi wa Mungu duniani, aliyepewa mamlaka juu ya kanisa na dola.

Baada ya mtambuzi wa makosa kuondolewa, Shetani alifanya kazi kulingana na mapenzi yake. Unabii ulikwisha tangaza kuwa upapa utafikiri "kubali nyakati na sheria" (Danieli 7:25). Hakuchelewa kuifanya kazi hii. Ili kuwapatia waongofu kutoka katika upagani mbadala wa ibada ya sanamu, na kwa njia hiyo kuhamasisha kuukubali Ukristo kwa jina tu, ibada ya sanamu na mifupa ya watakatifu polepole viliingizwa katika ibada ya Kikristo. Amri ya baraza kuu (Tazama Kiambatisho) hatimaye ilianzisha mfumo huu wa ibada ya sanamu. Kukamilisha kazi ya kufuru, Rumi iliondoa amri ya pili kutoka katika sheria ya Mungu, amri inayokataza ibada ya sanamu, na ikaigawa amri ya kumi kuwa mbili, ili kudumisha idadi ya amri kumi.

Roho ya kuungana na upagani ilifungua njia ya kuhafifisha zaidi mamlaka ya Mungu. Shetani, akifanya kazi kupitia viongozi wa kanisa wasiojiweka wakfu kikamilifu, alichezea amri ya nne pia, na kujaribu kuondoa Sabato ya kale, siku ambayo Mungu aliibariki na kuitakasa (Mwanzo 2:2, 3), na badala yake akainua siku kuu iliyoadhimishwa kama "siku ya heshima ya jua." Badiliko hili awali halikufanywa kwa uwazi. Katika karne za kwanza Sabato ya kweli ilitunzwa na Wakristo wote. Walikuwa na wivu kwa ajili ya heshima ya Mungu, na, wakiamini kuwa sheria Yake haibadiliki, walilinda kwa bidii utakatifu wa kanuni zake. Lakini kwa hila kubwa Shetani alifanya kazi kupitia mawakala wake kutimiza kusudi lake. Ili kuzifanya akili za watu ziikubali Jumapili kirahisi, Jumapili ilifanywa kuwa siku kuu ya kuheshimu ufufuo wa Kristo.

Huduma za kidini zilifanywa siku hiyo; hata hivyo ilichukuliwa kuwa siku ya maburudisho, Sabato ikiwa bado inaadhimishwa kama siku takatifu. Ili kuandaa njia kwa ajili ya kazi ambayo alikuwa amekusudia kuifanya baadaye, Shetani alikuwa amewaongoza Wayahudi, kabla ya ujio wa Kristo, kuibebesha mizigo Sabato mzigo wa masharti magumu sana, akafanya utunzaji wake kuwa mzigo. Sasa, akinufaishwa na mtazamo hasi ambao alikuwa amesababisha Sabato kutazamwa, aliifanya idharaulike kwa kuiita mila na desturi ya Kiyahudi. Wakati Wakristo walio wengi wakiendelea kuiadhimisha Jumapili kama siku kuu ya furaha, aliwaongoza, ili kuonesha chuki yao kwa dini ya Kiyahudi, kuifanya Sabato kuwa siku ya kufunga, siku ya huzuni na maumivu.

Katika sehemu ya kwanza ya karne ya nne mfalme Konstantini alitoa amri kuifanya Jumapili kuwa siku ya sherehe katika Dola lote la Rumi (Tazama Kiambatanisho). Siku ya jua iliheshimiwa na raia wake wapagani na iliheshimiwa pia na raia wake Wakristo; ilikuwa sera ya mfalme kuunganisha makundi mawili yenye maslahi yanayokinzana ya upagani na Ukristo. Alishawishiwa kufanya hivyo na maaskofu wa kanisa, ambao, kwa kusukumwa na tamaa na kiu ya madaraka, walitambua kuwa ikiwa siku ile ile ingeadhimishwa na Wakristo na wapagani, ingewahamasisha wapagani kuupokea Ukristo kwa jina na hivyo kuongeza nguvu na utukufu wa kanisa. Lakini wakati Wakristo wengi wacha Mungu waliongozwa pole pole kuikubali Jumapili kama siku iliyo na kiasi fulani cha utakatifu, bado waliendelea kuishika Sabato ya kweli kuwa ndiyo siku takatifu ya Bwana na waliiadhimisha ili kuitii amri ya nne.

Mdanganyaji mkuu alikuwa bado hajamaliza kazi yake. Alidhamiria kuukusanya ulimwengu wa Kikristo chini ya bendera yake na kupitishia madaraka yake chini ya mwakilishi wake, papa mwenye kiburi aliyedai kuwa mwakilishi wa Kristo. Kwa kupitia kwa wapagani walioongoka nusu, maaskofu wenye tamaa, na waumini wa kanisa wapenda dunia alifanikisha kusudi lake. Mabaraza makubwa yaliendeshwa mara kwa mara, ambapo viongozi wakubwa wa kansia walikusanywa pamoja kutoka duniani kote. Karibu katika kila baraza Sabato iliyowekwa na Mungu ilikandamizwa chini zaidi, wakati huo huo Jumapili iliinuliwa juu. Kwa njia hiyo sherehe ya kipagani ilikuja hatimaye iliheshimiwa kama agizo takatifu,

ilhali Sabato ya Biblia ilitangazwa kuwa mabaki ya dini ya Kiyahudi, na uadhimishaji wake ulitangazwa kuwa umelaaniwa.

Mwasi mkuu akafanikiwa kujiinua "juu ya kila kiitwacho Mungu, au kuabudiwa" (2 Wathesalonike 2:4). Alijaribu kubadili kanuni pekee ya sheria ya Mungu ambayo bila shaka inawaelekeza wanadamu kwa Mungu wa kweli na aliye hai. Katika amri ya nne, Mungu anafunuliwa kuwa ni Muumbaji wa mbingu na nchi, na hapa anatofautishwa na miungu ya uongo. Ilikuwa ni kwa ajili ya kumbukumbu ya kazi ya uumbaji ambapo siku ya saba ilitakaswa kama siku ya mapumziko kwa ajili ya mwanadamu. Sabato ilikusudiwa kumweka Mungu aliye hai mbele ya akili za wanadamu kama chanzo cha uzima na Yeye anayestahili kicho na ibada. Shetani anapambana kuondoa kicho cha wanadamu kwa Mungu, na kuondoa utii wao kwa sheria Yake; hivyo, anaelekeza juhudi zake hususani dhidi ya amri inayoelekeza watu kwa Mungu Muumbaji.

Waprotestanti sasa wanadai kuwa ufufuo wa Kristo uliifanya Jumapili kuwa Sabato ya Wakristo. Lakini hakuna ushahidi wa maandiko. Heshima kama hiyo haikutolewa kwa siku hivyo na Kristo au mitume. Uadhimishaji wa Jumapili kama siku ya ibada ya Wakristo ulitokana na "siri ya uasi" (2 Wathesalonike 2:7) ambayo, hata katika wakati wa Paulo, ilikuwa imeanza kazi yake. Ni wapi na ni lini Bwana aliidhinisha mtoto huyu wa upapa? Ni sababu gani halali inaweza kutolewa kwa ajili ya badiliko ambalo Maandiko hayaliidhinishi?

Katika karne ya sita, upapa ulikuwa umeshajijenga kikamilifu. Kiti chake cha mamlaka kilisimikwa katika mji mkuu wa dola, na askofu wa Rumi alitangazwa kuwa kiongozi wa kanisa lote. Upagani ulisalimisha nafasi yake kwa upapa. Joka alimpa mnyama "nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi" (Ufunuo 13:2). Na sasa ikaanza miaka 1260 ya ukandamizaji wa kipapa uliotabiriwa katika unabii wa Danieli na Ufunuo (Danieli 7:25; Ufunuo 13:5-7; Tazama Kiambatanisho).

Wakristo walilazimishwa kuchagua ama kusalimisha uadilifu wao na kukubali sherehe na ibada za kipapa, au kuharibu maisha yao gerezani au kuuawa kwa msumeno, moto, au shoka. Ndipo yalitimizwa maneno ya Yesu: "Nanyi mtasalitiwa na wazazi wenu, na ndugu zenu, na jamaa zenu, na rafiki zenu, nao watawafisha baadhi yenu. Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu" (Luka 21:16, 17). Mateso yalifungulia dhidi ya waaminifu kwa hasira kali zaidi kuliko ilivyowahi kutokea hapo awali, na ulimwengu uligeuka kuwa uwanja mkubwa wa vita. Kwa mamia ya miaka, kanisa la Kristo lilikimbilia mafichoni na mahali pa upweke. Nabii anasema: "Yule mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko muda wa siku elfu na mia mbili na sitini" (Ufunuo 12:6).

Kitendo cha Kanisa la Rumi kupata mamlaka kuliashiria kuanza kwa Zama za Giza. Kwa kadiri mamlaka yake yalivyoongezeka, kina cha giza kiliongezeka zaidi. Imani ilihamishwa

kutoka kwa Kristo, msingi wa kweli, kwenda kwa papa wa Rumi. Badala ya kumtumaini Mwana wa Mungu ili kupata msamaha wa dhambi na wokovu wa milele, watu walimtazama papa, na mapadri na maaskofu ambao alikasimu madaraka kwao. Walifundishwa kuwa papa alikuwa mpatanishi wao wa kidunia na kuwa hakuna ambaye angeweza kumwendea Mungu isipokuwa kwa kupitia kwake; na, zaidi ya hapo, kwamba alisimama mahali pa Mungu kwao na kwa hiyo alitakiwa kutiiwa bila maswali.

Kukiuka matakwa yake ilikuwa sababu tosha ya kustahili adhabu kali iliyotolewa kwenye miili na roho za wakosaji. Hivyo akili za watu ziliondolewa kwa Mungu na kupelekwa kwa wanadamu wanaokosea, wenye mapungufu, na wakatili, zaidi ya hao, akili zao zilielekezwa kwa mfalme wa giza mwenyewe, aliyetumia nguvu zake kupitia kwao. Dhambi ilijificha katika vazi la utakatifu. Maandiko yanapokandamizwa, na mwanadamu aanapojidhania kuwa yuko juu ya wote, tutegemee kuona ulaghai, hila udanganyifu na uovu wa kudhalilisha. Kwa kuziinua sheria na desturi za wanadamu kulijitokeza ufisadi ambao daima hujitokeza kwa sababu ya kuiweka pembeni sheria ya Mungu.

Hizo zilikuwa siku za hatari kwa kanisa la Kristo. Wainua bendera waaminifu walikuwa wachache kweli kweli. Ingawa ukweli haukuachwa bila mashahidi, lakini kwa nyakati fulani ilionekana kuwa makosa na ushirikina vingeshinda kabisa, na dini ya kweli ingefunika kabisa duniani. Injli haikusikika kabisa, badala yake kaida mbalimbali za dini ziliongezwa, na watu walibebeshwa mizigo na shughuli nzito.

Watu walifundishwa siyo tu kumwangalia papa kama mpatanishi wao, bali kutumainia kazi zao wenyewe kuwapatanisha kwa ajili ya dhambi. Safari ndefu za kwenda kuhiji, matendo ya kitubio, na ibada ya mifupa ya wataktifu, ujenzi wa makanisa, na maeneo matakatifu, na madhabahu, malipo ya pesa nyingi kwa kanisa—haya na matendo mengi kama hayo yaliingizwa ili kumfurahisha Mungu au kupata upendeleo Wake; kana kwamba Mungu alikuwa kama wanadamu. Anayekasirishwa kwa mambo madogo madogo, au anayepozwa kwa zawadi na matendo ya kitubio!

Pamoja na hayo uovu huo ulishamiri hata miongoni mwa viongozi wa Kanisa la Kirumi, mvuto wake ulionekana kuongezeka kila kukicha. Karibu na mwisho wa karne ya nane, waumini wa mfumo wa upapa walidai kuwa katika zama za kwanza za kanisa maaskofu wa Rumi walikuwa na nguvu ile ile ya kiroho ambayo wanayo kwa sasa. Kuthibitisha dai hili, mbinu za aina fulani lazima zitumike kulipatia mamlaka; na mbinu hiyo mara moja ilipendekezwa na baba wa uongo. Maandishi ya awali yalighushiwa na watawa. Matamko ya mabaraza ambayo hayakuwahi kusikika yaligunduliwa, yakithibitisha kuwa papa ndiye kiongonzi mkuu duniani tangu nyakati za awali. Na kanisa lililokuwa limetupitilia mbali ukweli kwa tamaa lilikubali mambo hayo ya uongo (Tazama Kiambatanisho).

Wajenzi wachache waaminifu juu ya msingi wa kweli (1 Wakorintho 3:10, 11) walichanganywa na kuzuiwa wakati takataka za mafundisho ya uongo zilipozuia kazi. Kama wajenzi wa kuta za Yerusalemu wakati wa Nehemia baadhi waliposema: "Nguvu zao wachukuao mizigo zimedhoofika, na kifusi tele zipo; tusiweze kuujenga ukuta" (Nehemia 4:10). Wakiwa wamechoshwa na pambano lisiloisha dhidi ya hila, uovu, na kila kikwazo ambacho Shetani aliweza kukibuni kuzuia maendeleo yao, baadhi waliokuwa wajenzi waaminifu walivunjika moyo; na kwa ajili ya amani na usalama wa mali zao na maisha yao, waligeuka na kuuacha msingi wa kweli. Wengine, pasipo kuchoshwa na upinzani wa maadui zao, walitangaza bila hofu: "Msiwaogope; mkumbukeni Bwana, aliye mkuu mwenye kuogofya" (Aya ya 14); na waliendelea na kazi, kila mmoja akiwa na upanga kiunoni mwake (Waefeso 6:17).

Roho ile ile ya chuki na upinzani kwa ukweli imewavuvia maadui wa Mungu katika kila zama, na ukeshaji na uaminifu ule ule umewavuvia watumishi wa Mungu. Maneno ya Kristo kwa mitume wa kwanza yanatumika kwa wanafunzi Wake hadi mwisho wa wakati: "Na hilo niwaambialo ninyi, nawaambia wote, Kesheni" (Marko 13:37).

Giza lilionekana kuongezeka zaidi. Ibada ya sanamu ikaonekana kuwa jambo la kawaida, na maombi yakatolewa kwa sanamu. Desturi iliyokuwa ya kishirikina kabisa ikastawi. Akili za watu zilitawaliwa kabisa na ushirikina kiasi ambacho busara ilionekana kupoteza mwelekeo wake. Wakati mapadri na maaskofu wenyewe walikuwa wapenda anasa, wenye tamaa, na mafisadi, ilitarajiwa kabisa kuwa watu waliowategemea ili kupata mwongozo kwao wangezamishwa katika ujinga na uovu.

Hatua nyingine katika utawala wa upapa ilichukuliwa, wakati, katika karne ya kumi na moja, Papa Gregori VII alipotangaza ukamilifu wa Kanisa la Kirumi. Miongoni mwa mapendekezo aliyoyaleta ni lile linalodai kuwa kanisa halijawahi kukosea, wala halitakosea, kwa mujibu wa Maandiko. Lakini uthibitisho wa Maandiko haukuambatanishwa na dai hilo. Papa mwenye kiburi alidai pia kuwa na mamlaka ya kuwaondoa wafalme, na alitangaza kuwa hakuna hukumu ambayo aliyoitangaza ingeweza kutenguliwa na mtu ye yote yule, bali kwamba alikuwa na mamlaka ya kutengua maamuzi ya wengine wote (Tazama Kiambatanisho).

Mfano wa wazi wa ukatili wa huyu anayedai kuwa hakosei ulionekana katika namna alivyomshughulikia Mfalme wa Ujerumani, Henri IV. Kwa ujasiri wake wa kutotambua mamlaka ya papa, mfalme huyu alitangazwa kuondolewa katika ushirika wa kanisa na kuondolewa madaraka ya ufalme. Kwa hofu ya kuachwa na vitisho vya wasaidizi wake ambao walishawishiwa na agizo la papa dhidi yake, Henri aliona umuhimu wa kufanya amani na Rumi. Akiandamana na mkewe na mtumishi wake mwaminifu walivuka milima ya Alps wakati wa majira ya baridi, ili ajinyenyekeshe mbele ya papa. Alipofika karibu na jengo ambalo Gregori alikuwa amekwenda kupumzika, alipelekwa bila walinzi wake, katika

ukumbi wa nje, na pale, katika baridi kali ya majira ya baridi, kichwa chake kikiwa wazi bila kufunikwa cho chote, na miguu iliyo peku, alisubiri kupata ruhusa ya papa ili aende kwake. Mpaka alipoendelea kusubiri kwa siku tatu akifunga na kuungama, ndipo papa alipokubali kumpa msamaha. Hata hivyo ilikuwa kwa sharti kuwa mfalme asubiri kibali cha papa kabla ya kurudi madarakani au kutumia mamlaka ya kifalme. Na Gregori, akifurahia ushindi wake, alitamba kuwa ilikuwa jukumu lake kushusha kiburi cha wafalme.

Tofauti iliyoje kati ya tabia kandamizi ya huyu papa mwenye kiburi na unyenyekevu na upole wa Kristo, anayejitambulisha kama anayesihi kwenye mlango wa moyo ili aingie, ili alete msamaha na amani, na ambaye aliwafundisha wanafunzi Wake: “Na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu” (Mathayo 20:27).

Karne zilizofuata zilishuhudia ongezeko la daima la makosa katika mafundisho yaliyotolewa na Roma. Hata kabla ya kuanzishwa kwa upapa mafundisho ya wanafalsafa wa kipagani yalikuwa yakitumiwa na yalikuwa na mvuto mkubwa kanisani. Wengi wa wale waliodai kuwa wameongoka bado waliendelea kushikilia kanuni za msingi za falsafa zao za kipagani, na siyo tu kuwa waliendelea kujifunza wenyewe peke yao, bali walianza kuzifundisha falsafa hizo kwa wengine kwa madai kuwa ilikuwa njia ya kueneza mvuto wao miongoni mwa wapagani. Makosa makubwa yaliingizwa katika imani ya Kikristo kwa njia hiyo. Mashuhuri miongoni mwa makosa hayo ilikuwa imani ya asili ya kutokufa ya mwanadamu na uendelevu wa ufahamu wa mtu aliyekufa. Fundisho hili liliweka msingi ambao juu yake Rumi ilijenga maombi kwa watakatifu waliokufa na kumtukuza Bikra Maria. Kutokana na fundisho hili pia kulizuka uzushi wa moto wa milele kwa watu wasiotubu, fundisho ambalo liliingizwa mapema kabisa katika imani ya kipapa.

Ndipo njia iliandaliwa kwa ajili ya uingizwaji wa ugunduzi mwingine wa upagani, ambao Rumi iliuita pagatori, uliotumika kuwaogofya watu wengi waliokwishazoezwa kupokea na kuamini kila fundisho na waliokwisha aminishwa ushirikina. Kwa njia ya fundisho hili la uongo inaonesha kuwa kuna mahali pa mateso, mahali ambapo roho za wale ambao hawastahili hukumu ya milele wanapaswa kupata adhabu kwa ajili ya dhambi zao, na ambapo, wakishasafishwa uchafu wao, wanaruhusiwa kuingia mbinguni (Tazama Kiambatanisho).

Bado kulikuwa na uongo mwingine uliohitajika kuwezesha Rumi kunufaika kutokana na hofu na uovu wa waumini. Fursa hii iliwezeshwa na fundisho la msamaha. Ondoleo kamili la dhambi, za wakati uliopita, za wakati huu, na za wakati ujao, na kuachiliwa maumivu au adhabu zo zote zinazomkabili mtu, viliahidiwa kwa wote ambao wangejiorodhesha katika vita vya papa na kupanua mipaka ya utawala wake duniani, kuwaadhibu maadui zake, au kuwaangamiza wale waliodiriki kukataa ukuu wake wa kiroho. Watu pia walifundishwa kuwa kwa kulipa pesa kwa kanisa wanaweza kujinasua kutoka katika dhambi, na pia kunasua roho za rafiki zao waliokufa ambao walikuwa wamefungiwa katika ndimi za moto zitesazo za

purgatori. Kwa njia hiyo Rumi ilijaza hazina zake ili kudumisha ukuu, raha, na uovu wa yule aliyejifanya kuwa mwakilishi wa Yule ambaye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake (Tazama Kiambatanisho)

Fundisho la Biblia la Meza ya Bwana liliondolewa na badala yake ikawekwa kafara ya ibada ya sanamu ya misa. Makasisi wa kipapa walijifanya, kwa sherehe zisizo na maana, kubadilisha mkate na divai ya kawaida kuwa "mwili na damu ya Kristo" halisi—Cardinal Wiseman, The Real Presence of the Body and Blood of Our Lord Jesus Christ in the Blessed Eucharist, Proved From Scripture, lecture 8, sec. 3, par. 26. Kwa madai ya kiburi na kufuru, walidai hadharani kuwa walikuwa na uwezo wa kumwumba Mungu, Muumbaji wa vitu vyote. Wakristo walitakiwa, kwa tishio la kifo, kuapa kuwa wanaamini fundisho hili la uongo na la kutisha, linalotukana Mbingu. Watu wengi waliokataa waliunguzwa kwa ndimi za moto (Tazama Kiambatanisho). Katika karne ya kumi na tatu ilianzishwa taasisi ya kutisha kuliko taasisi zote za upapa—Mahakama ya Kanisa Katoliki ya kukomesha uasi. Mfalme wa giza aliwahemsha viongozi wa ngazi mbalimbali za upapa. Katika mabaraza yao ya siri Shetani na malaika zake waliendesha akili za watu waovu, bila kuonekana kati kati yao alisimama malaika wa Mungu akiandika kumbukumbu za kutisha za maamuzi yao na kuandika historia ya matendo ya kutisha sana kiasi cha kutofaa kuonwa na macho ya wanadamu. "Babeli mkuu" alilewa kwa "damu za watakatifu." Kumbukumbu za mamilioni ya wafia dini zilimlilia Mungu kwa ajili ya kisasi dhidi ya mamlaka asi.

Upapa ulikuwa dikteta wa ulimwengu. Wafalme na wafalme wakuu walipiga magoti kwa papa wa Kirumi. Hatima za watu, za muda mfupi na milele, zilionekana kuwa chini ya utawala wake. Kwa mamia ya miaka mafundisho ya Rumi yalipokelewa na watu wengi na bila maswali, kaida zake zilifanywa kwa kicho, sherehe zake zilisherehekewa na wote. Viongozi wake waliheshimiwa na kutunzwa kwa ukarimu. Hakuna wakati wowote mwingine ambapo Kanisa la Kirumi lilipata heshima, ukuu au mamlaka kama hayo.

Lakini"mchanawaupapaulikuwausikuwamananewaulimwengu."—J. A. Wylie, The History of Protestantism, b. 1, ch. 4. Maandiko Matakatifu yalikuwa hayajulikani kwa kiwango kikubwa, siyo tu kwa watu wa kawaida, lakini hata kwa mapadri. Kama Mafarisayo wa zamani, viongozi wa kipapa walichukia nuru iliyofunua dhambi zao. Sheria ya Mungu, kiwango cha utakatifu, ilipoondolewa, walitumia madaraka bila mipaka, na walitenda uovu bila udhibiti. Udanganyifu, tamaa ya mali, ufujaji wa mali vilishamiri. Watu hawakujizuia kutenda uhalifu ambao kwao wangeweza kujipatia mali au cheo. Makazi ya mapapa na maaskofu yalikuwa mazingira ya uovu na ufisadi. Baadhi ya mapapa waliotawala walikuwa na hatia ya uhalifu mkubwa kiasi kwamba baadhi ya watawala wa kidunia walijaribu kuwapindua viongozi hawa wa kanisa kama watu wakatili sana wasiostahili kuvumiliwa. Kwa karne nyingi Ulaya haikupiga hatua yo yote katika elimu, sanaa, au ustaarabu. Udumavu wa kimaadili na kiakili viligubika ulimwengu wa Kikristo.

Hali ya ulimwengu chini ya mamlaka ya Kirumi iliwakilisha utimizo wa kutisha na kuogofya wa maneno ya nabii Hosea: “Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe:… kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako.” “Hapana kweli, wala fadhili, wala kumjua Mungu katika nchi. Hapana neno ila kuapa kwa uongo, na kuvunja ahadi, na kuua, na kuiba, na kuzini; huruka mpaka, na damu hugusana na damu” (Hosea 4:6, 1, 2). Hayo yalikuwa matokeo ya kutupilia mbali neno la Mungu.

Sura ya 4 - Wanakinga Imani

Katikati ya utusitusi uliotanda duniani katika kipindi kirefu cha utawala wa upapa, nuru ya ukweli haikuzimika kabisa. Katika kila zama walikuwepo mashahidi wa Mungu—watu waliodumu kumwamini Kristo kama mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu, watu, ambao waliishikilia Biblia kama kanuni pekee ya maisha, na ambao waliitakasa Sabato ya kweli. Ni kiasi gani ulimwengu unadaiwa na watu hawa, vizazi vijavyo haviwezi kujua. Waliitwa wapotoshaji, dhamiri zao zilitiliwa mashaka, sifa zao zilichafuliwa, maandishi yao yalipuuzwa, yalitafsiriwa vibaya, au yalichanwa. Hata hivyo walisimama imara, na kutoka zama moja hadi zama nyingine walishikilia imani yao katika hali yake ya usafi, kama urithi mtakatifu kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Historia ya watu wa Mungu katika zama za giza za utawala wa Rumi imeandikwa mbinguni, lakini ina sehemu ndogo sana katika kumbukumbu za wanadamu. Mabaki kidogo ya uwepo wao yanaweza kupatikana, lakini ni katika mashitaka ya watesi wao. Ilikuwa sera ya Rumi kufuta kabisa mabaki yote yaliyohusiana na watu waliopingana nao katika mafundisho au maagizo yao. Kila kitu chenye viashiria vya upinzani wa kimafundisho, kiwe kilihusiana na mtu binafsi au maandishi viliharibiwa. Maneno yaliyoonesha mashaka, au maswali yaliyohoji mamlaka ya imani kuhusu upapa, yalitosha kuondoa uhai wa mtu tajiri au maskini, wa juu au wa chini. Rumi ilijitahidi kuharibu kumbukumbu zote za ukatili waliowafanyia waliotofautiana nao. Mabaraza ya kipapa yaliamuru kuwa vitabu na maandishi yenye kumbukumbu kama hizo yachomwe moto. Kabla ya kugundua mitambo ya uchapishaji, vitabu vilikuwa vichache katika idadi, na vilikuwa katika mfumo ambao siyo mwepesi kuhifadhiwa; kwa hiyo kulikuwa na vitu vichache vya kuwazuia watawala wa Rumi kutekeleza makusudi yao.

Hakuna kanisa ndani ya mipaka ya utawala wa Rumi lililobaki kwa muda mrefu bila uhuru wao wa dhamiri kubughudhiwa. Muda mfupi baada ya kupata mamlaka upapa ulinyosha mikono yake kuwaangamiza wote waliokataa kutambua mamlaka yake, na makanisa yote, moja baada ya jingine yalijisalimisha chini ya utawala wake.

Katika nchi ya Uingereza Ukristo wa awali ulikuwa umeanza kukita mizizi mapema kabisa. Injili iliyopokelewa na Waingereza katika karne za kwanza wakati huo haikuwa imechafuliwa na uasi wa Rumi. Mateso ya wafalme wa kipagani, yaliyosambaa mpaka pwani hizi za mbali, ndiyo zawadi pekee iliyopokelewa na makanisa ya Uingereza kutoka Rumi. Wakristo walio wengi, waliokimbia mateso huko Uingereza, walipata hifadhi katika nchi ya Scotland; kutoka hapo ukweli ulipelekwa Ireland, na katika nchi zote hizi injili ilipokelewa kwa furaha.

Wakati watu wa kabila la Wasaxon walipoivamia Uingereza, upagani ulipata nguvu na kutawala. Watekaji waliona aibu kufundishwa na watumwa wao, na Wakristo walilazimika kujificha milimani na maporini. Hata hivyo nuru, iliyofichwa kwa muda, iliendelea kuwaka. Katika nchi ya Scotland, karne iliyofuata, ilimulika nuru kubwa iliyoenea hadi nchi za mbali. Kutoka Ireland aliibuka Kolumba mcha Mungu na watendakazi wenzake, ambao, wakiwakusanya karibu yao waumini waliokuwa wamesambaa katika kisiwa pweke cha Iona, walipafanya mahali pale kuwa kituo chao cha kazi za umishenari. Miongoni mwa hawa wainjilisti alikuwemo mtunzanji wa Sabato ya Biblia, na kupitia kwake, ukweli huu ulitambulishwa kwa watu wengine. Shule ilianzishwa hapo Iona, ambapo wamishenari waliandaliwa na kutumwa sehemu zingine, siyo Scotland na Uingereza, bali pia Ujerumani, Uswisi, na hata Italia.

Lakini Rumi ilikuwa imeelekeza macho yake kwa Uingereza, na iliazimia kuiweka chini ya himaya yake. Katika karne ya sita wamishenari wake walijaribu kuwaongoa Wasaxon wapagani. Walipokelewa na wapagani wenye kiburi, na waliwashawishi maelfu kuikiri imani ya Kirumi. Kadiri kazi ilivyoendelea, viongozi wa upapa na waongofu wao walikutana na Wakristo wenye msimamo wa Ukristo wa awali. Tofauti kubwa ilijitokeza. Wakristo wa kundi la awali walikuwa sahili, wanyenyekevu, wenye tabia ya Maandiko Matakatifu, wenye kuzingatia mafundisho, na waungwana, wakati Wakristo wa kundi la kwanza walionesha roho ya ushirikina, majivuno, na kiburi cha upapa. Mwakilishi wa Rumi aliyaamrisha haya makanisa ya Kikristo yakiri ukuu wa utawala wa papa. Waingereza walijibu kwa unyenyekevu kuwa walitamani kuwapenda watu wote, lakini kuwa papa hakustahili kuwa na ukuu ndani ya kanisa, na kuwa walikuwa tayari kumpa heshima ambayo anastahili kila mfuasi wa Kristo.

Majaribio yalifanywa mara kadhaa ili kupata utii kwa Rumi; lakini hawa Wakristo wanyenyekevu, wakiwa wameshangazwa kwa kiburi kilichooneshwa na mjumbe wa papa, walisimama imara na kundelea kujibu kuwa hakumjua Bwana mwingine zaidi ya Kristo. Sasa roho ya kweli ya upapa ilifunuliwa. Kiongozi wa Kirumi alisema: “Usipowapokea ndugu wanaokuletea amani, utawapokea maadui wanaokuletea vita. Msipoungana nasi ili kwa pamoja tuwaoneshe Wasaxon njia ya uzima, mtapata kutoka kwao pigo la mauti.”— J. H. Merle D’Aubigne, History of the Reformation of the Sixteenth Century, b. 17, ch. 2. Hivi havikuwa vitisho vidogo. Vita, ujanja, na udanganyifu vilitumika dhidi ya mashahidi wa imani ya Biblia, mpaka makanisa ya Uingereza yalipoharibiwa, au yalipojisalimisha kwa mamlaka ya papa.

Katika nchi zilizokuwa nje ya utawala wa Rumi walidumu kuwepo kwa karne nyingi makundi ya Wakristo waliobaki kwa kiasi kikubwa bila kuchafuliwa na ufisadi wa kipapa. Walikuwa wamezungukwa na upagani na baada ya vizazi vingi kupita waliathiriwa na makosa yaliyomo katika upagani; lakini waliendelea kuheshimu Biblia kama kanuni pekee ya imani na walizingatia nyingi ya kweli zake. Wakristo hawa waliamini kuwa sheria ilikuwa ya

kudumu na waliitunza Sabato ya amri ya nne. Makanisa yaliyoshikilia imani hii na matendo haya yalikuwepo Afrika ya Kati na miogoni mwa Waarmenia wa Asia.

Lakini kati ya wale waliopinga kuburuzwa na mamlaka ya upapa, Wawaldensia walikuwa mbele kulikowa wengine wote. Katika nchi ile ile ambapo upapa ulikuwa umesimika kiti chake, mambo hayo ya uongo na ufisadi yalipingwa kwa nguvu zote. Kwa karne nyingi makanisa ya Piedmont yalidumisha uhuru wao; lakini muda ulifika hatimaye ambapo Rumi ilisisitiza sana na wao wajisalimishe. Baada ya mgogoro ulioonekana kutozaa matunda dhidi ya adui wao katili, viongozi wa makanisa haya bila kuridhika kabisa waliitambua mamlaka ambayo ulimwengu wote uliitambua na kuiabudu. Walikuwepo baadhi, hata hivyo, waliokataa kujisalimisha kwa mamlaka ya upapa au uaskofu. Waliazimia kudumisha utii wao kwa Mungu na kutunza usafi na usahili wa imani yao. Utengano ukatokea. Walioshikilia imani ya zamani sasa walijiondoa; baadhi, wakiyakimbia makazi yao ya asili ya Alps, waliinua bendera ya ukweli katika nchi za ugenini; baadhi walijificha katika maeneo pweke ya mapangoni na kati kati ya mianya ya miamba iliyoko milimani, na huko walidumisha uhuru wao wa kumwabudu Mungu.

Imani ambayo kwa karne nyingi ilishikiliwa na kufundishwa na Wakristo Wawaldensia ilitofautiana sana na mafundisho ya uongo yaliyotolewa na Rumi. Imani yao ya dini ilijengwa juu ya neno la Mungu lililoandikwa, msingi wa kweli wa Ukristo. Lakini wakulima wale wanyenyekevu, katika maficho yao, wakiwa wamejifungia mbali na ulimwengu, na wakiwa wamegubikwa na shughuli zao za kila siku katikati ya mifugo yao na mashamba yao ya mizabibu, walikuwa wao wenyewe hawajaelewa ukweli uliopingana na uongo na upotovu wa kanisa asi. Imani yao haikuwa imani mpya waliyokuwa wameipokea. Imani yao ya dini ilikuwa ile waliyoirithi kutoka kwa baba zao. Waliridhishwa na imani ya kanisa la mitume,— "imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu" (Yuda 3). "Kanisa jangwani," na siyo mamlaka iliyoketi juu ya kiti cha enzi katika mji mkuu wa dunia, ndilo lilikuwa kanisa la Kristo, mwangalizi wa hazina za ukweli ambao Mungu amewapa watu Wake ili waueneze ulimwenguni.

Miongoni mwa sababu muhimu zilizosababisha kanisa la kweli lijitenge na Rumi ilikuwa ni chuki ya Kanisa la Rumi dhidi ya Sabato ya Biblia. Kama unabii ulivyotabiri, mamlaka ya upapa ilitupa chini ukweli. Sheria ya Mungu ilikanyagwa katika mavumbi ya ardhi, ilhali mapokeo na desturi za wanadamu vikiinuliwa juu. Makanisa yaliyokuwa chini ya utawala wa upapa yalilazimishwa kuiheshimu Jumapili kama siku takatifu mapema kabisa.

Katikati ya makosa na ushirikina ulioshamiri, wengi, hata miongoni mwa watu wa kweli wa Mungu, walichanganywa sana kiasi ambacho ingawa waliitunza Sabato, waliacha kufanya kazi siku ya Jumapili. Lakini jambo hili halikuwaridhisha viongozi wa kipapa. Walidai siyo tu kuwa Jumapili itakaswe, bali pia Sabato inajisiwe; na waliwashutumu kwa lugha kali watu waliojaribu kuiheshimu. Ilikuwa tu kwa njia ya kuikimbia mamlaka ya Rumi ndiyo mtu

yeyote angeweza kuitii sheria ya Mungu kwa amani (Tazama Kiambatanisho). Wawaldensia walikuwa miongoni mwa watu wa kwanza wa Ulaya kupata tafsiri ya Maandiko Matakatifu (Tazama Kiambatisho). Miaka mamia kabla ya Matengenezo walikuwa na Biblia katika muswada katika lugha yao ya asili. Walikuwa na ukweli usiochafuliwa, na jambo hili liliwafanya wawe walengwa wa chuki na mateso.

Walilitangaza Kanisa la Rumi kuwa Babeli iliyoasi ya Ufunuo, na kwa kuhatarisha maisha yao walisimama imara kupinga ufisadi wake. Wakati, chini ya shinikizo la mateso yaliyodumu kwa muda mrefu, baadhi walilegeza imani yao, kidogo kidogo wakiacha kanuni zake bainishi, wengine walishikilia ukweli. Katika zama zote za giza na uasi walikuwepo Wawaldensia waliokataa ukuu wa Rumi, waliokataa ibada ya sanamu, na waliotunza Sabato ya kweli. Chini ya dhoruba kali kabisa za upinzani walishikilia imani yao. Wakiwa wamechanwa na mikuki ya kisavoyadi, na kupigwa fimbo za Kirumi, walisimama bila kutetereka kwa ajili ya neno la Mungu na heshima Yake. Nyuma ya ngome ndefu za milima—katika zama zote maficho ya walioteswa na walioonewa—Wawaldensia walijificha. Hapa nuru ya ukweli ilidumu kuwaka katikati ya giza la Zama za Kati. Hapa, kwa miaka elfu moja, mashaidi wa ukweli walidumisha imani ya zamani.

Mungu aliwatunza watu Wake katika maficho mazuri ajabu—maficho yaliyofaa kuhifadhia ukweli wenye nguvu waliopewa kuutunza kama amana. Kwa watu waaminifu waliokuwa uhamishoni milima ilikuwa ishara ya haki ya Yeshova usiobadilika. Milima iliwaelekeza watoto wao kwa vilele virefu juu yao katika utukufu usiobadilika, na iliwaambia habari za Yule ambaye Kwake hakuna kubadilika wala kivuli cha kugeuka, Yeye ambaye neno Lake linadumu kama milima ya milele. Mungu aliiweka milima na kuivika nguvu; hakuna mkono isipokuwa wa Nguvu ya Milele unaoweza kuihamisha kutoka katika sehemu zao. Kwa jinsi hiyo hiyo, Mungu aliiweka sheria kuwa msingi wa serikali Yake mbinguni na duniani. Mkono wa mwanadamu ungeweza kuwafikia wanadamu wenzake na kuharibu maisha yao; lakini mkono huo huo ungeweza kirahisi pia kuing'oa milima kutoka misingi yake, na kuitupa baharini, kama ungeweza kubadili kanuni moja ya sheria ya Yehova, au kufuta moja ya ahadi Zake kwa wale wanaotenda mapenzi Yake. Katika uaminifu wao kwa sheria ya Mungu, watumishi wa Mungu wanapaswa kutobadilika kama millima isivyobadilika.

Milima iliyozungukwa na mabonde ya chini ilikuwa mashahidi wa kudumu wa nguvu za Mungu za uumbaji, na uhakikisho usiobadilika wa ulinzi na utunzaji Wake. Wasafiri wale walijifunza kupenda alama za kimya za uwepo wa Yehova. Hawakulalamika kwa sababu ya ugumu wa maisha yao; hawakuhisi upweke katika maficho yao ya milimani. Walimshukuru Mungu kwa kuwapa maficho dhidi ya chuki na ukatili wa wanadamu. Walifurahia uhuru wa kuabudu mbele Zake. Mara nyingi walipofuatiliwa na maadui zao, nguvu ya milima ilikuwa ulinzi wa hakika kwao. Katikati ya milima mingi mirefu walimwimbia Mungu nyimbo za sifa, na majeshi ya Rumi hayakuweza kunyamazisha nyimbo zao za shukurani.

Utakatifu wa hawa wafuasi wa Kristo ulikuwa safi, sahili, na wa dhati. Walithamini zaidi kanuni za ukweli zaidi kuliko nyumba na ardhi, marafiki, ndugu, hata maisha yenyewe. Walitafuta kwa bidii kuziweka kanuni hizi katika mioyo ya watoto wao. Tangu watoto wakiwa wachanga vijana walifundishwa Maandiko na walifundishwa kutambua utakatifu wa madai ya sheria ya Mungu. Nakala za Biblia zilikuwa haba; kwa hiyo maneno yake ya thamani yalikaririwa. Wengi waliweza kukariri sehemu kubwa ya Agano la Kale na Agano Jipya. Mawazo ya Mungu yaliambatana sawa sawa na mandhari nzuri ya uumbaji na baraka za kila siku katika maisha. Watoto wadogo walijifunza kumtazama Mungu kwa shukurani kama mruzuku wa fadhili na wa kila jambo jema.

Wazazi, pamoja na wema wao na kujali kwao, waliwapenda watoto wao kwa hekima sana kiasi cha kuwazoezesha maisha ya afya na kiasi. Mbele yao kulikuwa na maisha ya majaribu na ugumu, pengine kifo cha mfia dini. Walielimishwa tokea utotoni kuvumilia ugumu wa maisha, kujitawala, na walijengewa uwezo wa kufikiri na kutenda kwa ajili yao wenyewe. Mapema kabisa walifundishwa kubeba majukumu, uangalifu katika maneno yao, na kuelewa hekima ya ukimya. Neno moja lisilofaa lililoruhusiwa kutoka midomoni mwao na kusikiwa na maadui zao lingeweza kuhatarisha siyo tu maisha ya msemaji, bali pia maisha ya mamia ya ndugu zake; kwani kama vile mbwa mwitu walivyowinda mawindo yao ndivyo maadui wa ukweli walivyowawinda watu waliodai kuwa na uhuru wa imani ya dini.

Wawaldensia walitoa kafara ya mafanikio ya maisha yao ya duniani kwa ajili ya ukweli, na kwa uvumilivu endelevu walipambana kujipatia riziki. Kila sehemu iliyoweza kulimwa katikati ya milima iliweza kuboreshwa; mabonde na miteremko isiyokuwa na rutuba iliwezeshwa kutoa mazao mengi. Kubana matumizi na kujikana nafsi sana vilikuwa sehemu ya elimu waliyopewa watoto kama urithi wao pekee. Walifundishwa kuwa Mungu alipanga maisha yawe kujikana nafsi, na kuwa mahitaji yao yangeweza kukidhiwa kwa kazi binafsi, kwa kupanga, kujali, na imani. Mchakato ulikuwa mgumu na wa kuchosha, lakini ulikuwa mkamilifu, kwani ulikidhi hitaji la mwanadamu katika hali yake ya anguko, shule ambayo Mungu aliipanga kwa ajili ya mafunzo na maendeleo. Wakati vijana walifunzwa kuteseka na kufanya kazi ngumu, maendeleo ya akili hayakuachwa nyuma. Walifundishwa kuwa nguvu zao zote zilikuwa za Mungu, na kuwa zote zilipaswa kuboreshwa na kuendelezwa kwa ajili ya huduma Yake.

Makanisa ya Kivodwa, katika usafi na usahili wake, yalifanana na kanisa la nyakati za mitume. Wakikataa mamlaka ya upapa na uaskofu, walishikilia Biblia kuwa ndiyo mamlaka pekee iliyo juu, isiyokosea. Wachungaji wao, kinyume na waheshimiwa mapadre wa Roma, walifuata mfano wa Bwana wao, ambaye "hakuja kutumikiwa, bali kutumika." Walilisha kundi la Mungu, wakiliongoza kwenye majani mabichi na chemchemi hai za neno Lake takatifu. Tofauti kabisa na kumbukumbu za majivuno na kiburi, watu walikusanyika, siyo katika makanisa mazuri au katika kathedro kubwa, bali chini ya vivuli vya milima, katika

mabonde yaliyoko katika milima ya juu, au, katika nyakati za hatari, katika ngome za miamba, kusikiliza maneno ya ukweli kutoka kwa watumishi wa Kristo. Wachungaji walihubiri siyo tu injili, bali pia walitembelea wagonjwa, waliwafundisha watoto, waliwaonya wakosaji, na walifanya kazi ya kutatua migogoro na kuhamasisha mapatano na upendano wa kindugu. Katika nyakati za amani walitunzwa kwa sadaka za hiari za watu; lakini, kama Paulo mtengeneza ngozi, kila mmoja alijifunza kazi au taaluma fulani ambayo kwayo, ilibidi, aweze kujitegemeza mwenyewe.

Kutoka kwa wachungaji wao vijana walipata mafundisho. Wakati muda mwingi ulitumiwa kujifunza maarifa ya aina mbalimbali za jumla, Biblia ilifanywa kuwa somo kuu. Injili za Mathayo na Yohana zilikaririwa, pamoja na Nyaraka zilizo nyingi. Walitumika pia katika kunakili Maandiko. Baadhi ya nakala zilikuwa na Biblia nzima, zingine zilikuwa na sehemu fupi zilizochaguliwa, zikiambatana na maelezo sahili ya aya husika yaliyoongezwa na wale waliokuwa na uwezo wa kufafanua Maandiko. Kwa njia hiyo hazina za kweli zilizokuwa zimefichwa kwa muda mrefu na wale waliotafuta kujiinua juu ya Mungu ziliwekwa wazi.

Kwa kazi ya uvumilivu, iliyofanywa bila kuchoka, nyakati zingine ikifanyiwa katika mapango yenye giza chini ya ardhi, kwa kutumia mwanga wa mienge, Maandiko Matakatifu yaliandikwa, aya kwa aya, sura kwa sura. Kwa njia hiyo, kazi ilisonga mbele, mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa yaking'aa kama dhahabu safi; kwamba iling'aa zaidi, kwa uwazi zaidi, na kwa nguvu kiasi gani, kwa sababu ya majaribu waliyopitia kwa sababu ya Maandiko, wanaoweza kuelewa ni wale tu waliohusika na kazi hiyo. Malaika wa mbinguni waliwazunguka watendakazi hawa waaminifu.

Shetani aliwafanya makasisi na maaskofu wa kipapa wazike neno la ukweli chini ya takataka za makosa, upotovu, na ushirikina; lakini kwa namna ya ajabu sana neno la Mungu lilihifadhiwa bila kuchafuliwa katika zama zote za giza. Halikutiwa mhuri wa mwanadamu, bali mhuri wa Mungu. Wanadamu hawakuchoka katika juhudi zao za kuficha maana ya wazi, sahili ya Maandiko, na kuyafanya yapingane na ushuhuda wake yenyewe; lakini kama safina juu ya vilindi vya maji, neno la Mungu lilipona dhoruba iliyotishia kuliharibu. Kama vile mgodi unavyokuwa na mishipa ya dhahabu na fedha chini ya uso wa ardhi, ili watu wote walazimike kuchimba ili kugundua maghala yake ya thamani, kadhalika Maandiko Matakatifu yana hazina za ukweli ambazo hufunuliwa tu kwa mtafutaji wa dhati, mnyenyekevu, na mwenye maombi. Mungu alipanga Biblia iwe kitabu cha masomo kwa ajili ya wanadamu wote, wakati wa utoto, utu uzima, na isomwe wakati wote. Aliwapa wanadamu neno Lake kama ufunuo Wake Mwenyewe. Kila ukweli mpya unaogunduliwa ni ufunuo mpya wa tabia ya Mtunzi wake. Kujifunza Maandiko ni njia iliyowekwa na Mungu kuwaleta watu katika mshikamano wa karibu na Muumbaji wao na kuwapa uelewa wa wazi zaidi wa mapenzi Yake. Ni mfereji wa mawasiliano kati ya Mungu na mwanadamu.

Wakati Wawaldensia wakichukulia kicho cha Bwana kuwa mwanzo wa hekima, hawakuwa na upofu wa kushindwa kutambua umuhimu wa kukutana na ulimwengu, kuwaelewa watu na shughuli za maisha yao ya kila siku, ili kupanua akili na kunoa utambuzi. Baada ya shule zao za milimani baadhi ya vijana walipelekwa katika taasisi za elimu katika miji ya Ufaransa au Italia, ambapo palikuwa na uwanja mpana zaidi wa elimu, fikra, na utafiti kuliko katika shule zao za milimani. Vijana waliopelekwa huko walikutana na majaribu, walishuhudia uovu, walikutana na mawakala wa Shetani wenye hila, waliosihi wakubali mafundisho ya uongo uliojificha sana na udanyifu wa hatari sana. Lakini elimu yao ya tangu utotoni ilikuwa imewaandaa kwa ajili ya mambo haya yote.

Katika shule walizokwenda, hawakupaswa kuwa karibu sana na mtu ye yote. Mavazi yao yalikuwa yametengenezwa kwa namna ambayo yangetumiwa kuficha hazina yao yenye thamani kuu—nakala za Maandiko. Nakala hizi, ambazo zilikuwa ni matunda ya miezi na miaka ya kazi ngumu, walizibeba, na kila wakati walipoweza kufanya hivyo bila kutiliwa mashaka na mtu ye yote, kwa tahadhari waliweka baadhi ya nakala hizo katika njia za wale ambao mioyo yao ilionekana kuwa wazi kupokea ukweli. Tangu wakiwa kwenye magoti ya mama zao vijana Wawaldensia walifundishwa kusudi hili likiwa mawazoni; waliijua kazi yao na kwa uaminifu waliifanya. Waongofu wa imani ya kweli, walipatikana katika taasisi hizi za elimu, na mara nyingi kanuni zake zilionekana kupenya na kusambaa katika shule nzima; pamoja na hayo viongozi wa upapa hawakuweza, kwa uchunguzi mkali, kugundua chanzo cha kile ambacho wao walikiita mafundisho ya upotovu yanayoharibu.

Roho ya Kristo ni roho ya kimishenari. Msukumo wa kwanza kabisa wa moyo uliobadilishwa ni kuwaleta wengine pia kwa Mwokozi. Hiyo ndiyo ilikuwa roho ya Wakristo wa Kivodwaa. Waliamini kuwa Mungu alitaka jambo kubwa zaidi kutoka kwao kuliko kuhifadhi tu ukweli katika usafi wake katika makanisa yao; kuwa wajibu mkubwa ulikuwa umewekwa juu yao wa kuwaangazia nuru yao walio gizani; kwa nguvu kubwa ya neno la Mungu walitafuta kuvunja utumwa ambao Rumi ilikuwa imeuleta. Wachungaji wa Kivodwaa walikuwa wamefundishwa kuwa wamishenari, kila mtu aliyetarajia kujiunga na uchungaji akitakiwa kwanza kupata uzoefu wa kuwa mwinjilisti. Kila mmoja alitakiwa kutumika miaka mitatu katika eneo fulani la kimishenari kabla ya kupewa kanisa la kuongoza nyumbani.

Huduma hii, ikihitaji tangu mwanzo kujikana nafsi na kujinyima, ulikuwa mwanzo mzuri wa maisha ya kichungaji katika zama hizo zilizojaribu roho za watu. Vijana waliowekewa mikono ya uchungaji waliona mbele yao, siyo mustakabali wa utajiri na utukufu wa dunia, bali maisha ya kazi ngumu na hatari, na pengine hatima ya kuwa mfia dini. Wamishenari walitumwa wawili wawili, kama Yesu alivyowatuma wanafunzi Wake. Kawaida, kila kijana alipangwa kufanya kazi na mtu mwenye umri mkubwa na uzoefu, kijana akiwa chini ya uongozi wa mwenzi wake, aliyewajibika kumfundisha, na ambaye mafundisho yake ilipasa yazingatiwe na kijana. Watendakazi hawa waliofanya kazi pamoja, siyo kwamba

waliambatana kila wakati, lakini mara nyingi walikutana kwa ajili ya maombi na kushauriana, hivyo kuimarishana katika imani.

Kueleweka kwa lengo la utume wao ingekuwa ndiyo hakikisho la kushindwa kwa utume; hivyo, kwa uangalifu mkubwa walificha tabia yao halisi. Kila mchungaji alikuwa na ujuzi wa shughuli au taaluma fulani, na wamishenari walitekeleza kazi yao chini ya mwavuli wa shughuli za kawaida za utafutaji zisizokuwa za kidini. Mara nyingi walichagua kazi ya biashara ya jumla au reja reja. “Walibeba hariri, vito vya thamani, na vitu vingine, ambavyo kwa wakati huo havikupatikana maeneo ya karibu isipokuwa tu masoko ya mbali; na walikaribishwa kama wafanyabiashara wakubwa ambapo wangefukuzwa kama wamishenari” (Wylie, b. 1, ch. 7). Wakati wote huo mioyo yao iliinuliwa juu kwa Mungu kupata hekima ya kuwasilisha hazina iliyo ya thamani zaidi kuliko dhahabu au vito vya thamani. Kwa siri walibeba nakala za Biblia, zikiwa nzima au sehemu yake; na fursa ilipojitokeza waliwaeleza wateja wao kuhusu nakala hizo. Mara nyingi hamu ya kusoma neno la Mungu iliamshwa, na sehemu ya Maandiko iliachwa kwa furaha kwa wale waliotamani kuipokea.

Kazi ya wamishenari hawa ilianzia katika maeneo tambarare na mabondeni karibu na milima yao, lakini ilipanuka mbali zaidi ya mipaka ile. Wakitembea kwa miguu isiyovalishwa kitu cho chote na mavazi yaliyochakaa kwa sababu ya safari nyingi kama zilivyokuwa nguo za Bwana wao, walipita katika miji mikuu na walipenya hadi katika nchi za mbali. Kila mahali walisambaza mbegu za thamani. Makanisa yalichipuka katika njia yao, na damu ya wafia dini ilishuhudia kwa ajili ya ukweli. Siku ya Mungu itafunua mavuno makubwa ya roho zilizokusanywa kwa kazi za hawa watu waaminifu. Likiwa limejificha na likiwa kimya, neno la Mungu lilipenya katika ulimwengu wa Ukristo na lilipokelewa kwa furaha katika nyumba na mioyo ya watu.

Kwa Wawaldensia Maandiko hayakuwa tu kumbukumbu za Mungu alivyoshughulikia wanadamu hapo kale, na ufunuo wa wajibu na majukumu ya wakati huu, bali ufunuo wa hatari na utukufu wa wakati ujao. Waliamini kuwa mwisho wa mambo yote haukuwa mbali, na walivyosoma Biblia kwa maombi na machozi waliguswa zaidi na maneno yake ya thamani na wajibu wa kutangaza kwa wengine kweli zake zinazookoa. Waliuona mpango wa wokovu ukiwa umefunuliwa kwa uwazi zaidi katika kurasa zake takatifu, na walipata faraja, tumaini, na amani kwa kumwamini Yesu. Nuru ilivyoangaza ufahamu wao na kuleta furaha mioyoni mwao, walipata shauku ya kuwaangazia miale ya nuru yake kwa wale walio gizani na walio katika makosa ya upapa.

Waliona kuwa chini ya uongozi wa papa na makasisi, watu wengi walikuwa wakijaribu kupata msamaha bila mafanikio kwa kuitesa miili yao kwa ajii ya dhambi za roho zao. Wakiwa wamefundishwa kutumainia kazi zao njema kuwaokoa, walikuwa daima wakijitazama wenyewe, akili zao zikitafakari hali yao ya dhambi, wakiona walivyokabiliwa na hasira ya Mungu, wakiitesa miili na roho zao, lakini bila kupata nafuu. Hivyo roho zenye

bidii kubwa zilikuwa zimefungwa kwa mafundisho ya Rumi. Maelfu walitupilia mbali marafiki na ndugu wa karibu, walitumia maisha yao katika vyumba vya watawa. Kwa kufungwa mara kwa mara na vipigo vya kikatili, kwa kukesha mpaka usiku wa manane, kwa kuanguka kifudi-fudi kwa masaa mengi kwenye mawe yaliyolowa maji ya makazi yao yanayokera, kwa kutembea kwa miguu safari ndefu, kwa adhabu za kuaibisha na suluba za kutisha, maelfu walitafuta bila mafanikio amani ya dhamiri. Wakiteswa kwa utambuzi wa dhambi, na kuumizwa kwa hofu ya ghadhabu ya kisasi cha Mungu, wengi waliteseka, mpaka miili yao iliyoishiwa nguvu iliposalimu amri, na bila mwale mmoja wa nuru au tumaini waliingia kaburini.

Wawaldensia walitamani kuwamegea mkate wa uzima watu hawa waliokuwa wakifa kwa njaa ya kiroho, kuwafungulia ujumbe wa amani katika ahadi za Mungu, na kuwaelekeza kwa Kristo kama tumaini lao pekee la wokovu. Fundisho walililoliamini kuwa matendo mema yanaweza kupatanisha uvunjaji wa sheria ya Mungu lilijengwa juu ya uongo. Kutegemea kazi ya mwanadamu kupata wokovu kunapotosha mtazamo wa upendo wa milele wa Kristo. Yesu alikufa kuwa kafara kwa ajili ya mwanadamu kwa sababu mwanadamu aliyeanguka dhambini hawezi kufanya jambo lo lote la kumfanya akubalike mbele za Mungu. Wema wa Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka ni msingi wa imani ya Kikristo. Tegemeo la roho kwa Kristo ni jambo halisi, na uhusiano wake na Yeye lazima uwe wa karibu, kama ule wa mguu na mwili, au tawi na mzabibu.

Mafundisho ya mapapa na makasisi yalikuwa yamewafanya watu kuiona tabia ya Mungu, na hata ya Kristo, kama katili, ya huzuni, na inayotisha. Mwozi aliwakilishwa kama ambaye hana huruma kwa mwanadamu katika hali yake ya kuanguka kiasi kwamba alihitaji upatanisho wa makasisi na watakatifu. Waliokuwa wameangaziwa na neno la Mungu walitamani kuzielekeza roho hizi kwa Yesu kama Mwokozi wao mwenye huruma na upendo, akiwa amesimama na mikono iliyonyooshwa, akiwaalikwa wote wamwendee na mizigo yao ya dhambi, mashaka na uchovu wao. Walitamani kuondoa vikwazo ambavyo Shetani alikuwa amevirundika ili watu wasione ahadi, na kumwendea Mungu moja kwa moja, wakiungama dhambi zao, na kupata msamaha na amani.

Kwa shauku kubwa, mmishenari wa Kivodwaa aliwafunulia kweli za injili watu waliokuwa wanatafuta ukweli. Kwa tahadhari kubwa aliwatolea sehemu za nakala za Maandiko Matakatifu zilizonakiliwa kwa uangalifu. Ilikuwa furaha yake kubwa kuipa tumaini roho iliyokuwa na shauku kubwa, iliyopondeka kwa sababu ya dhambi, iliyomwona Mungu kuwa ni Mungu wa kisasi tu, aliyekuwa akisubiri kutekeleza haki. Kwa midomo iliyotetemeka na macho yaliyojaa machozi, alipiga magoti na kuwafunulia ndugu zake ahadi za thamani zinazofunua tumaini pekee la mwenye dhambi. Kwa njia hiyo nuru ya ukweli ilipenya akili nyingi zilizokuwa gizani, ikaondoa wingu la huzuni, mpaka Jua la Haki lilipoangaza moyoni na miale Yake inayoponya. Mara nyingi sehemu ya Maandiko ilisomwa tena na tena, msikilizaji akiwa na shauku kwamba usomaji urudiwe, kana kwamba alitaka

kujiridhisha kuwa amesikia kwa usahihi. Hususani usomaji wa kurudiwa-rudiwa ulitamaniwa sana maneno haya yaliposomwa:"Damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote" (1 Yohana 1:7). "Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye" (Yohana 3:14, 15).

Watu wengi hawakudanganyika kuhusiana na madai ya Rumi. Waliona maombi ya wanadamu au malaika kwa niaba ya mwenye dhambi hayakuwa na maana yo yote kwa mwenye dhambi: "Kristo ni kuhani wangu; damu Yake ni kafara Yangu; madhabahu Yake ni ungamo langu." Walijisalimisha kikamilifu kwa wema wa Yesu, wakikariri maneno, "Pasipo imani haiwezekani kumpendeza" (Waebrania 11:6). "Kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

Hakikisho la upendo wa Mwokozi lilionekana kubwa mno kueleweka kwa baadhi ya roho maskini zilizosukwa-sukwa na dhoruba za uongo. Maneno hayo yalileta furaha kubwa mno, mafuriko ya nuru yaliyowaangazia yaliwafanya kujiona kama wamechukuliwa mbinguni. Mikono yao ilishikiliwa kwa upendo na mkono wa Kristo; nyayo zao zimeoteshwa juu ya Mwamba wa Zama zote. Hofu zote za kifo zilitoweka. Waliweza sasa kutamani gereza na mijeledi ikiwa kwa njia hiyo wangeweza kumheshimu Mkombozi wao.

Katika mahali pa siri neno la Mungu lililetwa hivyo na kusomwa, nyakati zingine kwa roho moja, nyakati zingine kwa kikundi kidogo cha watu waliokuwa wakitamani nuru na ukweli. Mara nyingi usiku kucha ulitumiwa kwa jinsi hiyo. Kwa hiyo hali ya kushangaa na kushtuka ilikuwa kubwa kwa wasikilizaji kiasi ambacho mjumbe wa rehema alilazimishwa mara nyingi kukatisha usomaji mpaka akili ielewe habari njema ya wokovu. Mara nyingi maneno kama haya yalisemwa: "Je, kweli Mungu anaweza kukubali sadaka yangu? Je, Mungu anaweza kutabasamu akiniona? Je, Mungu anaweza kunisamehe?" Jibu lilisomwa: "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28). Imani ilishikilia ahadi, na jibu la furaha lilisikika: "Hakuna safari za kwenda mbali; hakuna safari za maumivu za kwenda mahali patakatifu. Naweza kuja kwa Yesu sasa hivi jinsi nilivyo, mwenye dhambi na mchafu, na hatatupilia mbali ombi la toba. 'Dhambi zako umesamehewa.' Zangu, hata zangu, zinaweza kusamehewa!"

Wimbi la furaha takatifu lilijaza moyo, na jina la Yesu lingekuzwa kwa sifa na shukurani. Roho zenye furaha zilirudi nyumbani kwao kueneza nuru, kuwasimulia wengine, kwa kadiri walivyoweza, uzoefu wao mpya; kuwa wamepata Njia ya kweli na uzima. Kulikuwa na nguvu ya ajabu na ya dhati katika maneno ya Maandiko yaliyosema na mioyo moja kwa moja ya wale waliokuwa wana shauku kwa ajili ya ukweli. Ilikuwa sauti ya Mungu, na ilikuwa na nguvu ya ushawishi kwa wale walioisikia.

Mjumbe wa ukweli aliendelea na safari yake; lakini mwonekano wake wa unyenyekevu, udhati wake, umakini wake na kujitoa kwake kwa moyo, viliongelewa sana mara nyingi. Katika matukio mengi wasikilizaji wake hawakupata fursa ya kumwuliza alikotoka au alikokwenda. Walikuwa wametekewa, kwanza kwa mshangao, na baadaye kwa shukurani na furaha, kiasi kwamba hawakuwa na muda wa kufikiri juu ya kumwuliza jambo lo lote. Walipomsihi afuatane nao kwenda katika nyumba zao, aliwajibu kuwa ilimpasa kuwatembelea kondoo wa kundi waliopotea. Je, pengine alikuwa malaika kutoka mbinguni? Waliuliza.

Mara nyingi mjumbe wa ukweli hakuonekana tena. Alikuwa ameenda katika nchi zingine, au alikuwa akiteseka katika gereza lisilojulikana, au pengine mifupa yake ilikuwa ikikaukia mahali alipofia kama shahidi wa ukweli. Lakini maneno aliyokuwa ameyaacha nyuma hayakuweza kuharibiwa. Yalikuwa yakifanya kazi katika mioyo ya watu; matokeo yake yaliyobarikiwa yataeleweka kikamilifu tu katika siku ya hukumu.

Wamishenari wa Wawaldensia walikuwa wanavamia ufalme wa Shetani, na nguvu za giza ziliamshwa na kuwa makini zaidi. Kila juhudi ya kueneza ukweli ilichunguzwa na mfalme wa uovu, na aliamsha hofu ya mawakala wake. Viongozi wa upapa waliona dalili za hatari kwa kazi yao kutokana na kazi za hawa waenda kwa miguu wanyenyekevu. Ikiwa nuru itaruhusiwa kuangaza bila kizuizi, ingeweza kufagilia mbali mawingu ya makosa yaliyowafunika watu. Ingeelekeza akili za watu kwa Mungu pekee na ingeweza kuamgamiza ukuu wa Rumi hatimaye.

Uwepo wa watu hawa peke yake, walioshikilia imani ya kanisa la awali, ulikuwa ni ushuhuda wa daima dhidi ya uasi wa Rumi, na hivyo uliamsha chuki na mateso makali. Kukataa kwao kusalimisha Maandiko lilikuwa pia kosa ambalo Rumi isingelivumilia. Rumi ilidhamiria kuwafuta kutoka duniani. Sasa ilianzishwa vita ya kidini ya kutisha dhidi ya watu wa Mungu katika makazi yao ya milimani. Wapelelezi walitumwa kwenda kuwafuatilia, na mandhari ya Habili akianguka mbele ya mwuaji Kaini ilirudiwa mara nyingi. Tena na tena ardhi zilizokuwa na rutuba zilibaki ukiwa, makazi na makanisa yao yakifagiliwa kabisa, kiasi kwamba mahali palipokuwa na mashamba yaliyostawi vizuri na nyumba za watu wasiokuwa na hatia, wachapa kazi, palibaki jangwa tu. Kama mnyama mkali anavyopandwa na hasira zaidi anapoonja damu, kadhalika hasira ya mapapa iliwasha zaidi mateso ya wahanga wao. Wengi wa mashahidi hawa kwa ajili ya imani safi walifuatiliwa katika milima na waliwindwa katika mabonde walipokuwa wamejificha, wakikingwa na misitu mikubwa na vilele vya miamba. Hakuna shitaka ambalo lingetolewa dhidi ya tabia na uadilifu wa kundi hili la watu waliopigwa vita. Hata maadui zao waliwatangaza kuwa wenye amani, wakimya, watu wacha Mungu. Kosa lao kubwa lilikuwa kutokumwabudu

Mungu kulingana na matakwa ya papa. Kwa uhalifu huu kila dharau, tusi, na mateso ambayo watu au mashetani wangeweza kubuni, yalirundikwa juu yao. Wakati Rumi

ilipodhamiria kukiangamiza kikundi kilichochukiwa, barua ilitolewa na papa, ikiwahukumu kuwa waasi dhidi ya mafundisho ya kanisa, na kuamuru wachinjwe (Tazama Kiambatanisho). Hawakushtakiwa kama wazururaji, au wadhulumaji, au wenye fujo; bali ilitangazwa kuwa walikuwa na mwonekano wa uchaji na utakatifu ulioshawishi "kondoo wa kundi la kweli." Hivyo papa aliamuru "kikundi kiovu na kinachochukiza cha watu waovu," ikiwa "watakataa kukana, wapondwe-pondwe kama nyoka wenye sumu kali" (Wylie, b. 16, ch. 1). Je, kiongozi huyu alitarajia kukutana na maneno haya tena? Je, alijua kuwa yalikuwa yameandikwa katika vitabu vya mbinguni, akutane nayo siku ya hukumu? "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo,"Yesu alisema, "mlinitendea mimi" (Mathayo 25:40).

Barua hii ilitaka washiriki wote wa kanisa kujiunga na vita vya msalaba dhidi ya wapinzani wa mafundisho ya kanisa. Kama motisha ya kujiunga na kazi hii ya kikatili, barua iliwapa watu wanaojiunga "kinga dhidi ya mateso na adhabu za kanisa, za jumla na mahsusi; kuliwafungua waliojiunga kutoka katika viapo ambavyo walikuwa wamefanya; iliwapa uhalali wa kumiliki mali waliyoipata kwa njia isiyo halali; na kuwapa ahadi ya ondoleo la dhambi zao zote wale ambao wangewaua wapinzani dhidi ya mafundisho yao. Ilifuta mikataba yote iliyowanufaisha Wavodwa (Wafuasi waaminifu wa Kristo), iliwaamrisha waliokuwa katika nyumba zao waende zao, iliwakataza watu wote wasiwape msaada wo wote, na iliwapa mamlaka watu wote kuchukua na kumiliki mali zao" (Wylie, b. 16, ch. 1). Waraka huu unafunua wazi roho kuu iliyo nyuma ya pazia. Ni ngurumo ya joka, na siyo sauti ya Kristo, inayosikika ndani yake.

Viongozi wa upapa hawakujenga tabia zao kulingana na kiwango kikuu cha sheria ya Mungu, bali walisimamisha kiwango kinachoendana na matakwa yao, na waliazimia kuwalazimisha wengine wote wafuate kiwango hicho kwa kuwa tu kimewekwa na Rumi. Uovu wa kutisha sana ulitendwa. Makasisi na mapapa fisadi na wenye kufuru walitenda kazi waliyopewa na Shetani. Rehema haikuwemo katika roho zao. Roho ile ile iliyomsulubisha Kristo na kuwaua mitume, roho ile ile iliyomsukuma Nero mwenye kiu ya damu dhidi ya watu waaminifu wa nyakati zake, ilikuwa kazini kuwafuta duniani watu wanaopendwa na Mungu.

Mateso waliyoyapata kwa karne nyingi watu hawa wanaomcha Mungu waliyavumilia kwa subira kubwa na bila kuyumba ili kumheshimu Mkombozi wao. Licha ya vita vya msalaba dhidi yao, na mauaji ya kinyama yaliyowapata, waliendelea kutuma wamishenari wao kusambaza ukweli wa thamani. Waliwindwa hadi wakauawa; lakini damu yao ilimwagilia mbegu zilizopandwa, na hazikukosa kuzaa matunda. Kwa hiyo Wawaldensia walishuhudia kwa ajili ya Mungu kwa karne nyingi kabla ya kuzaliwa kwa Luther. Wakiwa wametawanyika katika nchi nyingi, walipanda mbegu za Matengenezo yaliyoanza wakati wa Wycliffe, yakapanuka na kupata kina nyakati za Luther, na yanapaswa kuendelezwa mpaka wakati wa mwisho na wale walio tayari kuteseka katika mambo yote kwa ajili ya"neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu Kristo" (Ufunuo 1:9).

Sura ya 5 - Nyota ya Asubuhi

Kabla ya Matengenezo, kulikuwa na nyakati ambazo nakala za Biblia zilikuwa chache sana, lakini Mungu hakuruhusu neno Lake liharibiwe kabisa. Kweli zake hazikupaswa kufichwa milele. Aliweza kuvunja kirahisi minyororo iliyofunga maneno ya uzima kama alivyoweza kufungua milango ya chuma ya magereza ili kuwaacha watumishi wake huru. Katika nchi tofauti za Ulaya watu walisukumwa na Roho wa Mungu kuutafuta ukweli kama kutafuta hazina iliyositirika. Kwa uongozi wa Mungu wakiyapata Maandiko Matakatifu, walipekua kurasa zake kwa shauku kubwa. Walikuwa tayari kuikubali nuru kwa gharama yo yote dhidi yao. Japokuwa hawakuweza kuona mambo yote kwa uwazi, waliwezeshwa kuelewa kweli nyingi zilizozikwa kwa muda mrefu. Wakiwa wajumbe waliotumwa na mbingu walisonga mbele, wakivunja- vunja minyororo ya makosa na ushirikina, na kuwaita wale ambao kwa muda mrefu walikuwa utumwani, waamke na kupata uhuru wao.

Isipokuwa tu miongoni mwa Wawaldensia, neno la Mungu lilifungiwa kwa zama nyingi katika lugha iliyoeleweka kwa wasomi tu; lakini wakati ulikuwa umewadia kwa Maandiko kutafsiriwa na kusambazwa kwa watu wa nchi zingine katika lugha zao za asili. Ulimwengu ulikuwa umepita katika usiku wake wa manane. Saa za giza zilikuwa zinaishia, na katika nchi nyingi kulitokea ishara za kuwadia kwa mapambazuko.

Katika karne ya kumi na nne katika nchi ya Uingereza ilitokea "nyota ya asubuhi ya Matengenezo." John Wycliffe alikuwa mjumbe wa matengenezo, siyo tu kwa ajili ya Uingereza peke yake, bali pia kwa ajili ya ulimwengu wote wa Ukristo. Upinzani mkuu dhidi ya Rumi ambao aliruhusiwa kuzungumzia haukuwa rahisi kamwe kunyamazishwa. Upinzani huo ulifungua pambano ambalo liliwezesha uwekwaji huru wa watu binafsi, wa makanisa, na wa mataifa.

Wycliffe alipata elimu kubwa, na kwake kumcha Bwana kulikuwa chanzo cha hekima. Alijulikana chuoni kwa kicho chake na kwa talanta zake za ajabu na uwezo wake wa elimu. Kwa sababu ya kiu chake kwa ajili ya maarifa alijitahidi kupata ujuzi katika nyanja zote za elimu. Alipata elimu falsafa ya ualimu, sheria za kanisa, katika sheria za madai, hususani za nchi yake. Katika muda baada ya shughuli zake thamani ya mafunzo haya ya awali iliweza kuonekana. Uelewa wake wa kina wa falsafa na nadharia za wakati wake ulimwezesha kubaini dosari zake; na kwa kujifunza kwake sheria za kitaifa na kikanisa alijiandaa kwa ajili ya pambano kuu la kutafuta uhuru wa kiraia na wa kidini. Wakati ambapo aliweza kupata silaha kutoka katika neno la Mungu, alikuwa na uwezo wa kiakili upatikanao shuleni, na alizijua mbinu za wasomi. Nguvu ya uwezo wake wa kiakili na kiwango na kina cha ujuzi wake vilimpa heshima mbele ya marafiki na maadui zake. Wafuasi wake waliridhika kuwa shujaa wao alikuwa miongoni mwa watu wenye uwezo mkubwa wa kiakili kitaifa; na maadui zake walizuiwa kudharau kazi ya matengenezo kwa kubaini ujinga au udhaifu wa mtu aliyeunga mkono matengenezo.

Wakati Wycliffe alipokuwa bado chuoni, alianza kujifunza Maandiko. Katika nyakati zile za awali, wakati Biblia ilipokuwa katika lugha za awali, wasomi waliweza kuifikia chemchemi ya ukweli, ambayo ilikuwa imefungiwa isifikiwe na matabaka ya watu wasio na elimu. Hivyo njia ilikuwa imeandaliwa kwa ajili ya kazi ya baadaye ya Wycliffe kama Mwanamatengenezo. Wasomi walikuwa wamejifunza neno la Mungu na walikuwa wamepata ukweli mkuu wa neema Yake ya bure ikiwa imefunuliwa humo. Katika mafundisho yao walikuwa wametawanya ukweli huu, na walikuwa wamewaongoza wengine waugeukie ujumbe huu ulio hai.

Wakati Wycliffe alipojielekeza kuchunguza Maandiko, alianza uchunguzi wake kwa bidii ile ile iliyomwezesha kupata elimu ya shuleni. Tangu wakati huo alihisi kuwa na uhitaji mkubwa, ambao siyo masomo yake ya shuleni wala mafundisho ya kanisa yangeweza kuukidhi. Katika neno la Mungu alipata kile ambacho alikuwa akikitafuta kwa muda bila kukipata. Katika Maandiko aliweza kuona mpango wa wokovu ukiwa umefunuliwa na Kristo akiwa ameelezwa kama mtetezi wa mwanadamu. Alijitolea kuwa mtumishi wa Kristo na alidhamiria kutangaza kweli alizozigundua.

Kama wanamatengenezo wengine, Wycliffe hakuweza, mwanzoni mwa kazi yake, kuona mapema kule ambapo matengenezo yangempeleka. Hakuwa na lengo la kuipinga Rumi moja kwa moja. Bali kuupenda ukweli kwa moyo kulimfanya aingie mgogoro dhidi ya uongo. Kwa kadiri alivyogundua kwa wazi makosa ya upapa, ndivyo alivyozidi kufundisha Biblia kwa bidii zaidi. Aliona kuwa Rumi ilikuwa imeacha neno la Mungu na kukumbatia mapokeo ya wanadamu; bila hofu aliwashitaki mapadri kwa kuacha Maandiko, na alidai kuwa Biblia irudishwe kwa watu na kwamba mamlaka yake iimarishwe kanisani. Alikuwa mwalimu mahiri na mhubiri fasaha, na maisha yake ya kila siku yalionesha ukweli aliouhubiri. Ujuzi wake wa Maandiko, nguvu ya hoja zake, na ujasiri na uadilifu wake usioyumba vilimfanya aheshimiwe na kukubaliwa na watu wengi. Watu wengi walikuwa wamechoshwa na imani yao ya awali waliona uovu uliokuwemo katika Kanisa la Kirumi, na walisifia ukweli uliohubiriwa na Wycliffe kwa shangwe ya wazi; lakini viongozi wa upapa walijazwa na hasira walipotambua kuwa huyu Mwanamatengenezo alikuwa akipata ukubali wa wengi zaidi kuliko wao.

Wycliffe alikuwa mgunduzi makini wa makosa, na alikosoa bila hofu matumizi mabaya ya Maandiko yaliyoidhinishwa na mamlaka ya Rumi. Wakati akifanya kazi mchungaji wa mfalme, alisimama imara dhidi ya malipo ya kodi iliyodaiwa na papa kutoka kwa mfalme wa Uingereza na alionesha kuwa upapa kujipatia mamlaka juu ya watawala wa kiraia ilikuwa kinyume na busara ya kawaida na ufunuo wa neno la Mungu. Madai ya papa yalizusha hasira kubwa, na mafundisho ya Wycliffe yalikuwa na mvuto mkubwa katika akili za viongozi wa kitaifa. Mfalme na wasaidizi wake wa karibu waliungana kukataa madai ya mamlaka ya

kidunia ya papa kwa kukataa kulipa kodi. Hivyo pigo kubwa liligonga ukuu wa upapa katika nchi ya Uingereza.

Uovu mwingine ambao Mwanamatengenezo alipambana nao kwa muda mrefu na kwa nguvu nyingi ulikuwa uanzishwaji wa makundi ya watawa omba-omba. Watawa hawa walijaa katika nchi ya Uingereza, wakitia doa baya katika ukuu na mafanikio ya taifa. Uzalishaji, elimu, maadili, vyote viliguswa na mvuto unaodhoofisha. Maisha ya kivivu na omba-omba ya watawa siyo tu kuwa yalikuwa unyonyaji wa raslimali za watu, bali ulitia aibu kwa kazi ya uzalishaji. Vijana walikatishwa tamaa na kuharibiwa. Kwa mvuto wa hawa watawa watu wengi walivutwa kuingia nyumba za watawa na kuishi maisha ya kitawa, na walifanya jambo hili siyo tu bila ruhusa ya wazazi, bali pia bila kuwapa taarifa na kinyume na maagizo yao. Mmoja wa Mababa wa Kanisa la Kirumi akikazia madai ya utawa dhidi ya matakwa ya upendo na wajibu wa kidugu, alisema: "Hata kama baba yako angelala mbele ya mlango wako akilia na kuomboleza, na mama yako mzazi akikuonesha mwili uliokubeba na matiti yaliyokunyonyesha, inakupasa kuwakanyaga chini ya nyayo zako, na kwenda zako kwa Kristo." Kwa "unyama huu wa kutisha," kama Luther alivyouita baadaye, "ukiwa na Sura ya mbwa mwitu na ukatili zaidi kuliko Sura ya Ukristo na utu," ndivyo mioyo ya watoto ilivyofanywa kuwa migumu dhidi ya wazazi wao.—Barnas Sears, The Life of Luther, ukurasa wa 70. Hivyo ndivyo viongozi wa upapa, kama Mafarisayo wa zamani, walivyoifanya amri ya Mungu ilivyovunjwa ili kufuata mapokeo. Kwa njia hiyo, nyumba ziliachwa ukiwa na wazazi walinyang'anywa watoto wao.

Hata wanafunzi katika vyuo vikuu walidanganywa na mwonekano wa hawa watawa walishawishika kujiunga nao. Wengi wao baadaye walijutia hatua hiyo, baada ya kugundua kuwa wameharibu maisha yao na kuwaletea huzuni wazazi wao; lakini mara baada ya kunaswa katika mtego ilikuwa haiwezekani kupata uhuru wao tena. Wazazi wengi, kwa kuhofia mvuto wa watawa, walikataa kuwapeleka watoto wao katika vy vikuu. Kulikuwa na kuporomoka kwa idadi ya wanafunzi waliohudhuria masomo katika vyuo vikuu vya elimu. Shule zilikosa wanafunzi, na ujinga ulishamiri.

Papa aliwapa hawa watawa mamlaka ya kusikiliza maungamo na kutoa msamaha. Jambo hili lilikuwa chanzo cha uovu mkuu. Wakijielekeza kukuza mapato yao, watawa walikuwa tayari kutoa msamaha kwa ye yote kiasi kwamba wahalifu wa kila namna waliwaendea, na, matokeo yake, maovu makubwa kuliko kawaida yaliongezeka kwa kasi kubwa. Wagonjwa na maskini waliachwa wateseke, wakati misaada ambayo ilipaswa kupelekwa kwa wahitaji ilipelekwa kwa watawa, ambao kwa kutumia vitisho, walidai sadaka kwa watu huku wakiwashutumu watu wasiowaletea zawadi watawa kuwa ni waasi. Pamoja na madai yao ya umasikini, utajiri wa watawa uliongeza daima, na majengo yao ya gharama na meza zao za kianasa zilifanya umaskini wa taifa uliokuwa ukiongezeka uonekane wazi zaidi. Na wakati wakitumia muda wao katika anasa na raha, walituma kwa niaba yao watu wajinga, ambao waliweza kusimulia hadithi, hekaya na vichekesho kuwafurahisha watu na kuwafanya wawe

wahanga wa watawa. Hata hivyo watawa waliendelea kuwashikilia watu wengi katika ushirikina wao na waliwafanya waamini kuwa wajibu wao wa kidini ilikuwa kukiri ukuu wa papa, kuwaheshimu watakatifu, na kuwapa zawadi watawa, na kwamba kufanya hivyo kulitosha kabisa kuwapa nafasi mbinguni.

Wasomi na wacha Mungu wengi walifanya kazi ya kuleta matengenezo katika makundi haya ya watawa bila mafanikio; lakini Wycliffe, kwa ufafanuzi wa kina zaidi, aligonga kwenye mzizi wa uovu, akitangaza kuwa mfumo wenyewe ulikuwa wa uongo na kuwa ulipaswa kutupiliwa mbali. Mijadala na maswali viliamshwa. Wakati watawa walipozunguka nchi nzima, wakiuza misamaha ya papa, wengi waliongozwa kutilia mashaka juu ya uwezekano wa kununua msamaha kwa pesa, walihoji kwa nini wasitafute msamaha kwa Mungu badala ya kuutafuta kwa papa wa Rumi. (Tazama Kiambatanisho.) Watu wengi walishtushwa na tamaa ya mali ya watawa, ambao uroho wao haukuonekana kuridhishwa. "Watawa na makasisi wa Rumi," watu walisema, "wanatutafuna kama saratani. Inapasa Mungu atuokoe, vinginevyo watu wataangamia."—D'Aubigne, b. 17, ch. 7. Kuficha tamaa yao, hawa watawa omba omba walidai walikuwa wakifuata mfano wa Mwokozi, wakisema kuwa Yesu na wanafunzi Wake walitegemezwa kwa ukarimu wa watu. Dai hili liliharibu kazi yao, kwa kuwa liliwafanya watu wasome wenyewe Biblia ili kujitafutia ukweli—jambo ambalo kati ya yote halikupendwa kabisa na Rumi. Akili za watu zilielekezwa kwenye Chanzo cha ukweli, jambo ambalo Rumi ilikusudia kuuficha.

Wycliffe alianza kuandika na kuchapisha vijizuu dhidi ya watawa, siyo, hata hivyo, kwa lengo la kufanya malumbano nao, bali kuvuta akili za watu zielekee kwenye mafundisho ya Biblia na kwa Mtunzi wa Biblia. Alitangaza kuwa mamlaka ya kusamehe au kuondoa ushirika wa muumini ni ya papa na ya makasisi, na kuwa mtu hawezi kiuhalisia kuondolewa ushirika wake kanisani bila kwanza kuhukumiwa na Mungu. Hakuna njia bora zaidi kupita hii angeweza kuangusha mfumo mkubwa wa kiroho na kiutawala ambao papa alikuwa ameujenga ambamo roho na miili ilikuwa imeshikwa mateka. Tena Wycliffe alitakiwa kutetea haki za utawala wa Kiingereza dhidi ya ukandamizaji wa Rumi; na baada ya kuteuliwa kuwa mwakilishi wa mfalme, alitumia miaka miwili katika nchi ya Netherlands, kufanya mijadala na wawakalishi wa papa.

Hapa alikutanishwa na viongozi wa kanisa kutoka Ufaransa, Italia na Uhispania, na alipata fursa ya kuona nyuma ya pazia na kujipatia ufahamu wa mambo mengi ambayo yangebaki kuwa siri kwake kama angekaa tu Uingereza. Alijifunza mengi ambayo yangeongeza hoja katika hotuba zake baada ya kazi ile. Kutoka kwa hawa wawakilishi wa utawala wa papa alijifunza kikamilifu uhalisia na malengo ya upapa. Alirudi Uingereza kuyarudia mafundisho yake ya awali kwa uwazi zaidi na kwa juhudi kubwa zaidi, akitangaza kuwa tamaa, kiburi na udanganyifu vilikuwa miungu ya Rumi. Katika moja ya vijizuu vyake alisema, akiongelea juu ya papa na wakusanyaji wake wa mapato:"Wanapora riziki za watu maskini wa nchi yetu, na wanachota hazina kubwa, kila mwaka, kutoka katika pesa ya

mfalme, kwa ajili ya sakramenti na mambo ya kiroho, ambyo ni mafundisho ya uongo yaliyolaaniwa na rushwa ili kutoa vyeo kanisani, na wanawafanya Wakristo wakubaliane na wadumishe mafundisho ya uongo. Na kwa hakika ingawa nchi yetu ilikuwa na akiba kubwa ya dhahabu, na kwa kuwa hakuna mtu mwingine aliyeichukua isipokuwa huyu mkusanyaji wa kasisi wa ulimwengu, kwa mchakato wa kadiri muda unavyokwenda akiba hii lazima itaisha; kwa kuwa daima anaichukua kutoka katika nchi yetu, na hairudishi hata kidogo isipokuwa laana ya Mungu kwa sababu ya rushwa yake."—John Lewis, History of the Life and Sufferings of J. Wiclif, ukurasa wa 37.

Mara tu baada ya Wycliffe kurudi Uingereza, mfalme alimteua kuwa paroko wa Lutterworth. Huu ulikuwa uhakikisho kuwa mfalme angalau hakuwa amechukizwa na hotuba zake za uwazi na ukweli. Mvuto wa Wycliffe ulihisiwa katika uongozi na utendaji wa nyumba ya mfalme, kadhalika katika kuumba imani ya Taifa.

Radi na ngurumo za upapa zilianza kurindima dhidi yake. Barua tatu za matamko ya kipapa zilitumwa Uingereza,—kwa chuo kikuu, kwa mfalme, na maaskofu,—zote zikiamrisha uchukuliwaji wa hatua za haraka na stahiki kumnyamazisha mwalimu wa uongo. (Augustus Neander, General History of the Christian Religion and Church, period 6, sec. 2, pt. 1, par. 8. Tazama pia Kiambatanisho). Kabla ya kuwasili kwa barua hizo, hata hivyo, maaskofu, kwa juhudi zao, walikuwa wamemwita Wycliffe mbele ya hao kwa ajili ya mashtaka. Lakini wawili miongoni mwa viongozi wakuu katika ufalme waliambatana naye mahakamani; na watu waliolizunguka jengo na kuingia ndani, waliwatisha sana majaji kiasi kwamba mashtaka yaliahirishwa kwa muda, na aliachiliwa aondoke kwa amani. Muda mfupi baadaye, Edward III, ambaye katika uzee wake maaskofu walikuwa wakitafuta kumshawishi awe kinyume cha Mwanamatengezo, alifariki dunia, na mlinzi wa zamani wa Wycliffe akawa kaimu mfalme.

Lakini kuwasili kwa barua za papa kuliilazimisha Uingereza yote kumkamata na kumfunga Wycliffe. Hatua hizi zilielekeza moja kwa moja kuwa auawe kwa kuchomekwa juu ya mti wenye ncha kali. Ilionekana kana kwamba ilimpasa Wycliffe awe mawindo ya kisasi cha Rumi. Lakini Yeye alisema kwa mtu mmoja wa zamani, "Usiogope: ... Mimi ni ngao yako" (Mwanzo 15:1), alinyosha tena mkono Wake kumlinda mtumishi Wake. Mauti ilikuja, lakini siyo kwa Wycliffe, bali kwa papa aliyeamrisha kuangazwa kwa Wyclifee. Gregori XI alikufa, na viongozi wa kanisa waliokuwa wamekusanyika kuendesha mashtaka ya Wycliffe, walitawanyika.

Uwezo wa Mungu ulidhibiti matukio kutoa fursa ya ukuaji wa Matengenezo. Kifo cha Gregori kilifuatiwa na uchaguzi wa mapapa wawili walio hasimu. Mamlaka mbili zinazozozana, kila moja ikidai kutokukosea, sasa zilidai utii. (Tazama Kiambatanisho.) Kila mmoja aliwaalika waaminifu kumuunga mkono kupambana na mwingine, akishinikiza madai yake kwa laana nzito dhidi ya maadui zake, na ahadi za zawadi mbinguni kwa wanaomwunga

mkono. Tukio hili lilidhoofisha sana nguvu ya upapa. Makundi yanayopingana yalikuwa na kila kitu walichokihitaji kushambuliana wao kwa wao, na Wycliffe kwa muda fulani alipumzika. Matamko ya laana na lawama yaliruka kutoka kwa papa na kwenda kwa papa, na mito ya damu ilimwagwa kuunga mkono madai yao yanayopingana. Uhalifu na kashfa vilifurika kanisani. Wakati huo Mwanamatengenezo, katika ukimya wa mapumziko katika parokia yake ya Lutterworth, alikuwa akifanya kazi kwa bidii kuwaelekeza watu kwa Yesu Kristo, Mfalme wa Amani badala ya kuwaelekeza kwa mapapa waliokuwa wakigombana.

Utengano, pamoja na mapambano na ufisadi uliotokana na utengano huo, viliandaa njia kwa ajili ya Matengenezo kwa kuwawezesha watu kuona upapa ulivyokuwa katika uhalisia wake. Katika kijizuu alichokichapisha, Kuhusu Utengano wa Mapapa, Wycliffe aliwaalika watu waamue ikiwa wenyewe hawa makasisi wawili hawakuwa wakisema ukweli kwa kulaumiana kuwa kila mmoja wao alikuwa mpinga Kristo. “Mungu,” alisema, “hawezi kuendelea kumruhusu shetani atawale kupitia kasisi mmoja tu, bali … alileta utengano miongoni mwa hao wawili, ili kwamba watu, katika jina la Kristo, waweze kuwashinda kwa urahisi zaidi wote wawili.”—R. Vaughan, Life and Opinions of John de Wycliffe, vol. 2, uk. 6. Wycliffe, kama Bwana wake, alihubiri injili kwa maskini. Kwa kutokuridhishwa na usambazaji wa nuru katika nyumba zao za hali ya chini katika parokia yake ya Lutterworth, alidhamiria kuwa injili ipelekwe kila mahali katika nchi ya Uingereza. Kutekeleza jambo hili aliunda kikundi cha wahubiri, sahili, wacha Mungu, walioupenda ukweli na hawakupenda jambo lo lote zaidi ya kueneza injili. Watu hawa walienda kila mahali, wakifundisha katika masoko, katika mitaa ya miji mikubwa, na katika njia za vijijini. Waliwatafuta wazee, wagonjwa, na maskini, na waliwasimulia kwa furaha habari njema ya neema ya Mungu.

Kama pprofesa wa eliungu wa Oxford, Wycliffe alihubiri neno la Mungu katika kumbi za chuo kikuu. Aliwasilisha kwa uaminifu sana ukweli kwa wanafunzi wake, kiasi kwamba walimpa cheo cha“daktari wa injili.” Lakini kazi kubwa kabisa kuliko zote katika maisha yake ilikuja kuwa tafsiri ya Maandiko katika lugha ya Kiingereza. Katika kitabu, On the Truth and Meaning of Scripture, alidokeza kusudio lake la kutafsiri Biblia, ili kwamba kila mtu katika nchi ya Uingereza aweze kusoma, katika lugha aliyozaliwa nayo, matendo makuu ya Mungu.

Lakini kwa ghafla kazi zake zilikatizwa. Ingawa alikuwa bado hajafika umri wa miaka sitini, kazi nyingi bila kupumzika, kusoma, na mashambulizi ya adui zake vilidhoofisha nguvu zake na kumfanya azeeke mapema. Alishambuliwa na ugonjwa wa hatari. Habari hizi ziliwafurahisha sana watawa. Sasa walidhani atatubu kwa uchungu uovu alioufanyia kanisa, na waliharakisha kwenda katika chumba chake kusikiliza ungamo lake. Wawakilishi kutoka makundi manne ya kidini, wakiwa na viongozi wanne wa kiraia, walikusanyika kumzunguka mtu waliyedhani anaenda kufa. “Kifo kipo mdomoni mwako,” walisema; “hebu guswa na makosa yako, na kanusha mbele yetu yote uliyoyasema dhidi yetu.” Mwanamatengenezo aliwasikiliza akiwa kimya; halafu alimwambia mhudumu wake amwinue na kumkalisha kitandani, na, akiwakazia macho wakiwa wamesimama wakisubiri kanusho lake, alisema,

kwa sauti imara, yenye nguvu ambayo mara nyingi iliwafanya watetemeke: "Sifi, bali nitaishi; na nitatangaza tena matendo maovu ya watawa."—D'Aubigne, b. 17, ch. 7. Kwa mshangao, watawa walikimbia kutoka chumbani.

Maneno ya Wycliffe yalitimia. Aliishi na kuweka katika mikono ya watu wa nchi yake silaha yenye nguvu nyingi kuliko silaha nyingine yo yote dhidi ya Rumi— aliwapa Biblia, silaha ya mbinguni ya kukombolea, kuangazia, na kuhubiria habari njema kwa watu. Vilikuwepo vikwazo vingi vya kushinda ili kutekeleza kazi hii. Wycliffe alilemewa na madhaifu mengi; alijua kuwa alikuwa na miaka michache iliyobaki ya yeye kufanya kazi; aliona upinzani ambao alipaswa kukabiliana nao; lakini, kwa kutiwa moyo na ahadi za neno la Mungu, alisonga mbele bila kukatishwa tamaa na kitu cho chote. Akiwa na nguvu kamili za kiakili, uzoefu mwingi, alihifadhiwa na kuandaliwa na Mungu kwa namna ya pekee sana kwa ajili ya kazi hii, kazi iliyokuwa kubwa zaidi kuliko kazi zingnine zote. Wakati ulimwengu wote wa Kikristo ulikuwa umegubikwa na taharuki, Mwanamatengenezo katika parokia yake ya Lutterworth, bila kusikia tufani iliyokuwa ikivuma huko nje, alikuwa akiendelea na kazi aliyochaguliwa kuifanya.

Hatimaye kazi ilikamilika—tafsiri ya kwanza kabisa ya Biblia katika lugha ya Kiingereza ilipatikana. Neno la Mungu lilifunguliwa Uingereza. Mwanamatengenezo hakuogopa sasa gereza au mti wenye ncha kali. Alikuwa ameweka katika mikono ya Waingereza nuru ambayo isingeweza kuzimwa kamwe. Kwa kuwapa Biblia watu wa nchi yake, alikuwa amefanya kazi kubwa zaidi ya kukata minyororo ya ujinga na uovu, zaidi kuikomboa na kuiinua nchi yake, kuliko mafanikio mengine yo yote yaliyowahi kupatikana kwa njia ya vita.

Sanaa ya kuchapisha vitabu ikiwa bado haijajulikana, ilikuwa kwa njia ya kazi iliyofanywa polepole na kwa uchovu mwingi nakala za Biblia ziliweza kuongezeka. Hamu ya kukipata kitabu hicho ilikuwa kubwa sana kiasi ambacho wengi walijitolea kuingia katika kazi ya kuinakili, lakini ilikuwa kwa shida sana waliofanya kazi ya kunakili waliweza kukidhi mahitaji. Baadhi ya wanunuzi waliokuwa na uwezo mkubwa wa kipesa walitaka Biblia nzima. Wengine walinunua sehemu tu. Katika matukio mengi, familia kadhaa ziliungana kununua nakala moja. Ni kwa njia hiyo Biblia ya Wycliffe ilifika katika nyumba za watu.

Wito kwa watu kuwa watumie busara uliwaamsha kutoka katika utii usio na maswali kwa mafundisho yasiyohojiwa ya kipapa. Wycliffe sasa alifundisha mafundisho bainifu ya Uprotestanti—wokovu kwa njia ya imani katika Kristo, na kuwa Maandiko pekee ndiyo hayakosei. Wahubiri aliokuwa amewatuma walisambaza Biblia, pamoja na maandishi yake mwenyewe, kwa mafanikio makubwa kiasi kwamba imani hii mpya ilipokelewa na takribani nusu ya watu wa Uingereza.

Kuonekana kwa Maandiko kulileta fadhaa kwa mamlaka za kanisa. Iliwapasa sasa kukabiliana na mamlaka iliyo na nguvu nyingi zaidi kuliko ya Wycliffe—mamlaka ambayo dhidi yake silaha zao zisingefua dafu. Kwa wakati huu hakukuwa na Sheria Uingereza iliyokataza Biblia, kwa kuwa kabla ya hapo ilikuwa haijachapishwa katika lugha ya Kiingereza. Sheria kama hizo zilitungwa baadaye na kutekelezwa kwa nguvu nyingi. Kwa muda fulani, pamoja na juhudi za makasisi, kulikuwepo na kipindi chenye fursa ya kusambaza neno la Mungu.

Kwa mara nyingine tena viongozi wa upapa walipanga kunyamazisha sauti ya Mwanamatengenezo. Mbele ya mabaraza matatu aliitwa mfululizo kujibu mashitaka, lakini bila mafanikio. Kwanza kamati ya maaskofu iliyatangaza maandishi yake kuwa ya uzushi, na, wakimwongoa mfalme kijana, Richard II, upande wao, walipata amri ya mfalme ya kuwatupa gerezani wale wote ambao walishikilia mafundisho yaliyopigwa marufuku.

Wycliffe alikata rufaa kutoka kwa kamati ya maaskofu hadi kwa bunge; bila hofu alilishitaki kanisa kwa baraza la kitaifa akidai kanisa lifanye matengenezo kwa kuacha unyanyasaji na ufisadi ambao kanisa lilikuwa linaufanya. Kwa ushawishi mkubwa alionesha uporaji wa madaraka na ufisadi wa uongozi wa kipapa. Maadui zake walichanganywa. Marafiki na waungaji mkono wa Wycliffe walikuwa wamelazimishwa kujisalimisha, na ilikuwa imetarajiwa kwa ujasiri kuwa Mwanamatengenezo mwenyewe, katika uzee wake, akiwa peke yake na bila rafiki, angesujudia mamlaka ya muungano wa ufalme na upapa. Lakini badala ya matarajio hayo papa na wafuasi wake walijishuhdia wakishindwa. Bunge, likiwa limeamshwa na miito yenye nguvu ya Wycliffe, lilifuta amri ya mateso, na Mwanamatengenezo aliwekwa huru tena.

Kwa mara ya tatu alishitakiwa, na sasa alishtakiwa mbele ya mahakama ya juu kabisa ya kanisa katika ufalme. Hapa hakuna upendeleo wo wote ambao ingeoneshwa kwa uzushi. Hapa hatimaye Rumi ingeshinda, na kazi ya Mwanamatengenezo ingekomeshwa. Hivyo ndivyo walivyofikiri viongozi wa upapa. Ikiwa wangefanikiwa kutimiza kusudi lao, Wycliffe angelazimika kukana mafundisho yake, au angeondoka mahakamani kwenda kuliwa na ndimi za moto.

Lakini Wycliffe hakukana mafundisho yake; asingeweza kujifanya kukana. Bila hofu yo yote alidumu kusimamia mafundisho yake na alitupilia mbali mashtaka ya watesi wake. Akiacha kujiangalia mwenyewe, nafasi yake, na tukio lenyewe, aliwaita wasikilizaji wake mbele ya mahakama ya Mungu, na alipima nadharia zao na udanganyifu wao katika mizani ya ukweli wa milele. Nguvu ya Roho Mtakatifu ilihisiwa katika chumba cha baraza. Mguso wa Mungu ulikuwa juu ya wasikilizaji. Walionekana kana kwamba hawana nguvu ya kuondoka mahali pale. Kama mishale kutoka katika podo la Bwana, maneno ya Mwanamatengenezo yalichoma mioyo yao. Shtaka la uzushi, walilokuwa wamelileta dhidi

yake, yeye kwa ushawishi wenye nguvu aliirusha kwao wenyewe. Kwa nini, alidai, walidiriki kueneza makosa? Kwa ajili ya mapato, mkafanyia biashara neema ya Mungu?

“Mnafikiri mnapambana na nani?” aliwauliza hatimaye. Je, mnapambana na mzee aliyekuwa akichungulia kaburi? Hapana! Mnapambana na ukweli— Ukweli ulio na nguvu kubwa zaidi, na utawashinda ninyi.”—Wylie, b. 2, ch. 13. Baada ya kusema hayo, aliondoka mkutanoni, na hakuna hata mmoja wa maadui zake aliyejaribu kumzuia.

Kazi ya Wycliffe ilikuwa kama imekwisha; bendera ya ukweli aliokuwa ameubeba kwa muda mrefu ulikuwa karibu kudondoka kutoka mkononi mwake; lakini kwa mara nyingine tena alipaswa kutoa ushuhuda kwa ajili ya injili. Ukweli ulikuwa utangazwe ukitokea katika ngome ya makosa. Wycliffe aliitwa kujibu mashtaka dhidi yake mbele ya mahakama ya kipapa mjini Roma, ambapo mara nyingi palimwaga damu ya watakatifu. Hakuwa kipofu kiasi cha kutoona hatari iliyotishia maisha yake, hata hivyo alikuwa tayari kutii wito wa mahakama kama isingekuwa kwa sababu ya kiharusi kilichomfanya ashindwe kusafiri. Lakini, ingawa sauti yake isingeweza kusikilizwa mjini Roma, aliweza kusema kwa njia ya barua, na alidhamiria kulifanya hili. Kutokea katika parokia yake Mwanamatengenezo alimwambia papa barua, ambayo, wakati ikiwa na heshima na roho ya Kikristo katika uandishi wake, ilikemea majivuno na kiburi cha papa.

“Kwa hakika ninayo furaha,” alisema, “kufungua na kutangaza kwa kila mtu imani yangu, na hususani kwa askofu wa Roma: ambaye, kwa kadiri ninavyoamini kuwa sahihi na kweli, atakuwa tayari kuthibitisha imani yangu tajwa, au ikiwa itakuwa na makosa, basi ataiboresha. “Kwanza, ninachukulia kuwa injili ya Kristo ni mwili wote wa sheria ya Mungu Ninamwona na kumchukulia askofu wa Roma, yeye akiwa mwakilishi wa Kristo hapa duniani, kuwa amefungwa zaidi kuliko wengine wote, kwa sheria ya injili. Kwa kuwa ukuu miongoni mwa wanafunzi wa Kristo haukutokana na hadhi au heshima za kidunia, bali ulitokana na kuwa karibu na sahihi katika kumfuata Kristo katika maisha na tabia Yake.... Kristo, kwa muda wa uwepo Wake hapa, alikuwa maskini kuliko wote, na aliepuka na kutupilia mbali kabisa utawala na heshima za kidunia....

“Hakuna mtu mwaminifu ambaye atathubutu kumfuata papa mwenyewe au mtu mwingine ye yote mtakatifu miongoni mwa watu watakatifu, lakini katika mambo kama hayo kwa kadiri ambavyo amemfuata Bwana Yesu Kristo; kwa kuwa Petro na wana wa zebedayo, kwa kutamani heshima ya kidunia, kinyume na kufuata hatua za Kristo, alikosea, na hivyo katika makosa hayo hawapaswi kufuatwa....

“Papa anapaswa kuachana na mamlaka ya kidunia na himaya na utawala wa kilimwengu, na hivyo kwa ufanisi kuelekeza nguvu zake zote katika kazi ya kichungaji; kwa kuwa hivyo ndivyo Kristo alivyofanya, na hususani mitume Wake. Hivyo basi, ikiwa nimekosea katika vipengele hivi, kwa unyenyekevu mkubwa najisalimisha kukosolewa, hata kama kwa kifo,

ikiwa kuna haja ya kufanya hivyo; na ikiwa ningefanya kazi kulingana na mapenzi yangu au shauku ya nafsi yangu, ningetokea mbele ya askofu wa Roma; lakini Bwana ameniamuru kufanya kinyume chake, na amenifundisha kumtii Mungu kuliko mwanadamu."

Katika hitimisho alisema: "Hebu tumwombe Mungu, ili amwongoze Papa wetu Urban VI, kama alivyoanza, kwamba pamoja na viongozi wenzake wa kanisa wamfuate Bwana Yesu Kristo katika maisha na tabia; na kwamba waweze kuwafundisha watu kwa ufanisi, na kwamba wao, kadhalika, waweze kuwafuata katika hayo."—John Foxe, Acts and Monuments, vol. 3, uk. 49, 50.

Hivyo Wycliffe aliwasilisha kwa papa na makadinali wake unyenyekevu na upole wa Kristo, akionesha siyo tu kwao peke yao bali kwa Wakristo wote, tofauti kati yao na Bwana ambaye walidai kumwakilisha.

Wycliffe alitarajia kuwa maisha yake yangekuwa gharama ya uaminifu wake. Mfalme, papa, na maaskofu waliungana kufanikisha kifo chake, na ilionekana kwa hakika kuwa miezi michache ilibaki kabla ya kutundikwa kwake kwenye mti wenye ncha kali. Lakini ujasiri wake haukutetereka. "Kwa nini unatafuta mbali taji ya kifo cha mfia dini?" alisema. "Hubiri injili ya Kristo kwa maaskofu wenye kiburi, na kifo cha mfia dini hutakikosa. Nini! Je, niwe hai halafu nikae kimya? ... Kamwe! Acha pigo lianguke, ninasubiria ujio wake."—D'Aubigne, b. 17, ch. 8.

Lakini ulinzi wa Mungu ulimkinga mtumishi Wake. Mtu ambaye kwa maisha yake yote amesimama kwa ujasiri akiutetea ukweli, katika hatari za maisha yake, haikutokea kwake kuwa mhanga wa chuki ya maadui zake. Wycliffe hakutafuta kujikinga mwenyewe, lakini Bwana alikuwa mlinzi wake; na sasa, maadui zake walipohisi uhakika wa mawindo yao, mkono wa Mungu ulimweka mbali nao. Katika kanisa lake la Lutterworth, alipokuwa akiendesha huduma ya meza ya Bwana, alianguka, kwa kupigwa na kiharusi, na kwa muda mfupi alisalimisha uhai wake.

Mungu alikuwa amemchagulia Wycliffe kazi yake. Aliweka neno la kweli katika mdomo wake, na aliweka mlinzi kando yake ili neno hili liwaendee watu. Maisha yake yalilindwa, na kazi zake zilirefushwa, mpaka msingi ulipowekwa kwa ajili ya kazi kubwa ya Matengenezo.

Wycliffe alitokea katika uficho wa Zama za Giza. Hakukuwa na ye yote kabla yake aliyetokea ambaye kutokana na kazi yake angejenga mfumo wake wa matengenezo. Akiwa amelelewa na kukuzwa kama Yohana Mbatizaji kutimiza utume mahsusi, alikuwa mtangulizi wa zama mpya. Pamoja na hayo katika mfumo wa ukweli aliouwasilisha kulikuwepo umoja na ukamilifu ambao Wanamatengenezo waliofuata baadaye hawakuupita, na ambao hawakuweza kuufikia, hata miaka mia moja baadaye. Kwa hiyo, msingi mpana na wa kina

ulikuwa umekwisha kuwekwa, muundo ulikuwa imara na wa kweli, kiasi kwamba haukuhitaji kujengwa upya na wale waliokuja baadaye.

Vuguvugu kubwa ambalo Wycliffe alilizindua, ambalo lililenga kukomboa dhamiri na akili, na lililoyaweka huru mataifa yaliyokuwa yamefungwa kwa muda mrefu katika gari la ushindi wa Rumi, lilitokana na Biblia. Hapa ndipo kulikuwepo na chanzo cha mkondo wa baraka, ambazo, kama maji ya uzima, yametiririka tangu karne ya kumi na nne. Wycliffe aliyakubali Maandiko Matakatifu kwa imani thabiti kama ufunuo uliovuviwa wa mapenzi ya Mungu, kanuni toshelevu la imani na utendaji. Alielimishwa kuchukulia Kanisa la Rumi kama mamlaka ya Kimungu, isiyokosea, na kulikubali kwa uchaji usio na maswali mafundisho na desturi za miaka elfu moja; lakini aligeuka na kuyaacha hayo yote na kulisikiliza neno takatifu la Mungu. Hii ilikuwa mamlaka aliyohimiza watu waitambue. Badala ya kanisa kusema kupitia kwa papa, alitangaza mamlaka pekee ya kweli ni sauti ya Mungu akisema kupitia neno Lake. Na hakufundisha siyo tu kuwa Biblia ni ufunuo kamili wa mapenzi ya Mungu, lakini kwamba Roho Mtakatifu ni mtafsiri pekee wa Maandiko, na kwamba kila mtu ni, kwa njia ya kujifunza mafundisho yake, kujifunza wajibu wake kwa ajili yake. Hivyo aligeuza akili za watu kutoka kwa papa na kanisa la Rumi na kuzipeleka kwa neno la Mungu.

Wycliffe alikuwa mmoja wa Wanamatengenezo wakuu sana. Katika upana wa akili, na uwazi wa fikra, katika uimara wa kudumisha ukweli, na katika ujasiri wa kuulinda ukweli, alilingana na watu wachache waliotokea baada yake. Usafi wa maisha, juhudi isiyochoshwa katika kujifunza na kazi, uadilifu usiochafuliwa, na upendo kama wa Kristo na uaminifu katika huduma yake, zilikuwa sifa za Mwanamatengenezo wa kwanza. Na jambo hili lilikuwa hivyo licha ya giza la kiakili na ufisadi wa kimaadili wa zama alizozaliwa na kuishi.

Tabia ya Wycliffe ni ushuhuda wa nguvu inayoelimisha, na kubadilisha ya Maandiko Matakatifu. Biblia ndiyo ilimfanya awe vile alivyokuwa. Juhudi ya kuzishika kweli kuu za ufunuo wa neno la Mungu hutoa upya na nguvu kwa talanta zingine zote. Inapanua akili, hunoa uwezo wa ufahamu, na hukomaza maamuzi. Kujifunza Biblia kunawezesha kila wazo, hisia, na matumaini zaidi kuliko vyanzo vingine vyote vya mafunzo vinavyoweza kufanywa. Inatoa uimara wa nia, uvumilivu, ujasiri, na ustahimilivu; inalainisha tabia na kutakasa roho. Mafundisho ya dhati, yenye kicho, ya Maandiko, hukutanisha akili ya mwanafunzi na akili isiyokuwa na mipaka, inaweza kuupatia ulimwengu watu wenye nguvu zaidi za kiakili na za kiutendaji, hali kadhalika inatoa kanuni za juu zaidi, kuliko zile zinazotolewa na falsafa ya kibinadamu. “Kufafanusha maneno yako,” anasema mtunga zaburi, “kwatia nuru; Na kumfahamisha mjinga” (Zaburi 119:130).

Mafundisho makuu yaliyofundishwa na Wycliffe yaliendelea kuenea kwa muda mrefu; wafuasi wake, waliojulikana kama Wawiklifiti as “Wycliffites” na “Lollards,” siyo tu kuwa walifika kila sehemu ya nchi ya Uingereza, bali walitawanyika pia katika nchi zingine wakichukua ujumbe wa injili. Sasa kwa kuwa kiongozi wao alikuwa ameondolewa, wahubiri

walifanya kazi kwa bidii kubwa zaidi kuliko hapo mwanzo, na watu wengi walifurika kusikiliza mafundisho yao. Baadhi ya waheshimiwa, na hata mke wa mfalme, walikuwa miongoni mwa waongofu. Katika sehemu nyingi kulikuwepo na matengenezo ya dhahiri katika mienendo ya watu, na alama za ibada ya sanamu ya Urumi ziliondolewa makanisani.

Lakini dhoruba isiyokuwa na huruma ya mateso ilipasuka juu ya wale wote waliodiriki kuikubali Biblia kama mwongozo wao. Wafalme wa Kiingereza, wakitamani kuimarisha nguvu zao kwa kupata msaada wa Roma, hawakusita kuwatoa kafara Wanamatengenezo. Kwa mara ya kwanza katika historia ya Uingereza mti wenye ncha kali uliamriwa dhidi ta wanafunzi wa injili. Kufia dini kulifuata kufia dini. Watetezi wa ukweli, wakipigwa marufuku na kuteswa, waliweza tu kumwaga vilio vyao katika masikio ya Bwana wa Sabato. Wakiwindwa kama maadui wa kanisa na wasaliti wa ufalme, waliendelea kuhubiri kisiri siri, wakijificha kwa kadiri walivyoweza katika nyumba za watu maskini, na mara nyingi wakijificha katika mashimo na mapango.

Licha ya moto wa mateso, upinzani wa kimya kimya, kicho, dhati, subira, dhidi ya ufisadi wa kidini uliokuwepo wakati ule uliendelea kusemwa kwa karne nyingi. Wakristo wa siku zile za awali walikuwa na uelewa mdogo tu wa ukweli, lakini walikuwa wamejifunza kulipenda na kulitii neno la Mungu, na kwa uvumilivu mwingi waliteseka kwa ajili ya huo ukweli. Kama wanafunzi katika siku za mitume, wengi walitoa kafara mali zao za kidunia kwa ajili ya kazi ya Kristo. Wale walioruhusiwa kuishi katika nyumba zao kwa furaha waliwahifadhi ndugu zao waliofukuzwa, na wakati na wao waliokimbizwa, kwa furaha, walikubali kuishi maisha ya kukataliwa. Maelfu, ni kweli, kwa kutishwa na hasira ya watesaji, walinunua uhuru wao kwa kafara ya imani yao, na waliotoka katika magereza yao, walivaa majoho ya toba, kutangaza kuikana imani yao. Lakini idadi haikuwa ndogo—miongoni mwao walikuwemo watu wenye hadhi ya juu na watu wa hali ya chini— walioshuhudia bila hofu ukweli katika vyumba vya magereza, katika “Minara ya Lollard,” na katikati ya mateso na ndimi za moto, wakifurahia kuwa walihesabiwa kustahili kujua “ushirika wa mateso Yake.”

Wafuasi wa upapa walishindwa kutekeleza kusudi lao kwa Wycliffe wakati wa uhai wake, na chuki yao haikuridhishwa wakati mwili wake ukiwa umepumzika kimya kaburini. Kwa amri ya Baraza la Constance, zaidi ya miaka arobaini baada ya kifo chake mifupa yake ilifukuliwa na kuchomwa moto hadharani, na majivu yalitupwa katika kijito kilichokuwa jirani. “Kijito,” anasema mwandishi wa zamani, “kimesafirisha majivu yake katika mto wa Avon, Avon utayapeleka katika mto wa Severn, Severn utayapeleka katika bahari nyembamba, na bahari nyembamba zitayapeleka katika bahari kuu. Na hivyo majivu ya Wycliffe ni ishara ya mafundisho yake, ambayo sasa yamesambaa ulimwenguni kote.”—T. Fuller, Church History of Britain, b. 4, sec. 2, par. 54. Maadui zake hawakuelewa maana ya tendo lao ovu. Ilikuwa kwa njia ya maandishi ya John Huss wa Bohemia, alioongozwa kuyakataa mengi ya makosa ya Urumi na kujiunga na kazi ya matengenezo. Hivyo katika nchi hizi mbili, ambazo zimetenganishwa na umbali mkubwa, mbegu ya ukweli ilipandwa. Kutoka

Bohemia kazi iliendelea katika nchi zingine. Akili za watu zilielekezwa kwa neno la Mungu lililokuwa limesahauliwa kwa muda mrefu. Mkono wa Mungu ulikuwa ukiandaa njia kwa ajili ya Matengenezo Makuu.

Sura ya 6 - Askari wa Ukweli

Injili ilipandwa katika nchi ya Bohemia mapema katika karne ya tisa. Biblia ilitafsiriwa, na ibada ya wazi iliendeshwa, katika lugha ya watu. Lakini kadiri nguvu ya papa ilivyoongezeka, ndivyo neno la Mungu lilivyofichika. Gregori VII, aliyekuwa amedhamiria kuwanyenyekesha wafalme wenye kiburi, alikusudia pia kuwafanya watu kuwa watumwa wake, na wakati huo huo amri ilitolewa kupiga marufuku ibada ya hadhara kuendeshwa katika lugha ya Kibohemia. Papa alitangaza kuwa "inampendeza Mungu Mwenyezi kuwa ibada Yake iendeshwe katika lugha isiyoeleweka, na kwamba uovu na uzushi mwingi umeibuka kwa kutokuzingatia kanuni hii."— Wylie, b. 3, ch. 1.

Hivyo Rumi iliagiza kuwa nuru ya neno la Mungu ilipaswa izimwe na watu iliwapasa wafungiwe gizani. Lakini Mbingu ilikuwa imeweka mawakala wengine kwa ajili ya kuhifadhi kanisa. Wengi wa Wawaldensia na Waalbigensia, waliofukuzwa na mateso kutoka katika nyumba zao katika nchi ya Ufaransa na Italia, walikuja Bohemia. Japokuwa hawakuthubutu kufundisha kwa uwazi, walifanya kazi kwa siri. Kwa njia hiyo imani ya kweli ilihifadhiwa kutoka karne moja hadi nyingine.

Kabla ya siku za Huss kulikuwepo watu katika nchi ya Bohemia walioinuka na kukemea wazi ufisadi katika kanisa na ubadhirifu wa watu. Kazi zao ziliamsha shauku katika maeneo mengi. Hofu za Kanisa la Roma ziliamshwa, na mateso yalianzishwa dhidi ya wanafunzi wa injili. Wakiwa wamelazimishwa kuabudu katika misitu na milima, waliwindwa na maaskari, na wengi waliuawa. Baada ya muda iliamriwa kuwa wote walioacha ibada ya Kiroma inapasa wachomwe moto. Lakini wakati Wakristo walisalimisha maisha yao, walitazamia ushindi wa msimamo wao. Mmoja wa wale "waliofundisha kwamba wokovu ulipatikana kwa imani tu kwa Mwokozi aliyesulubiwa," alitamka wakati wa kufa: "Hasira ya maadui wa ukweli sasa inawaka dhidi yetu, lakini haitakuwa ya milele; atainuka mmoja miongoni mwa watu wa kawaida, bila upanga au mamlaka, na watapigana dhidi yake lakini hawatamshinda."—Ibid., b. 3, ch. 1. Wakati wa Luther ulikuwa bado uko mbali; lakini tayari mmoja alikuwa akiinuka, ambaye ushuhuda wake dhidi ya Roma ungetikisa mataifa.

John Huss alizaliwa katika familia maskini, na katika miaka ya awali aliachwa yatima kwa kifo cha baba yake. Mama yake mcha Mungu, kwa kuthamini elimu na kicho cha Mungu kama raslimali za thamani sana, alitafuta kumpa mwanawe urithi huu. Huss alisoma katika shule ya jimbo, na ndipo akajiunga na chuo kikuu cha Prague, ambapo alidahiliwa kwa ufadhili. Alisindikizwa kwenda Prague na mama yake; ambaye alikuwa mjane na maskini, hakuwa na zawadi za utajiri wa kidunia za kumpa mwanawe, lakini walipokaribia jiji kubwa, alipiga magoti kando ya kijana asiyekuwa na baba yake na kumwombea baraka kutoka kwa Baba yao wa mbinguni. Mama alijua kidogo sana jinsi ambavyo ombi lake lingekuja kujibiwa.

Akiwa chuoni, mara moja Huss alijitambulisha kwa juhudi zisizochoshwa na maendeleo ya kasi, wakati maisha yake yasiyolaumika na ya uungwana, na haiba inayogusa watu vilimpa heshima kwa watu wote. Alikuwa muumini mwaminifu wa Kanisa la Roma na mtafutaji wa dhati wa baraka za kiroho ambazo Kanisa linaahidi kuzitoa. Katika tukio la jubilee Huss alikwenda kuungama, alilipa sarafu za mwisho kutoka katika hazina yake ndogo, na alijiunga katika misafara, ili aweze kushiriki katika msamaha ulioahidiwa. Baada ya kumaliza kozi yake ya chuo kikuu, aliingia upadre, na akipata umaarufu upesi, mara moja alishikamanishwa na nyumba ya mfalme. Alifanywa pia kuwa profesa na baadaye paroko wa chuo kikuu alipopatia elimu yake. Katika miaka michache mwanafunzi maskini mfadhiliwa alikuwa mtu wa kujivunia katika nchi yake, na jina lake lilijulikana katika Ulaya yote. Lakini Huss alianzia kazi ya matengenezo katika uwanja mwingine.

Miaka kadhaa baada ya upadirisho alichaguliwa kuwa mhubiri wa kanisa la Bethlehemu. Jambo la muhimu kuzingatia hapa, mwasisi wa kanisa hili aligeuka kuwa mtetezi wa mahubiri ya Maandiko katika lugha ya watu. Licha ya upinzani dhidi ya mtindo huu wa mahubiri yanayotokana na Biblia, haukuwa umesimamishwa kabisa katika nchi ya Bohemia. Lakini watu hawakuwa na elimu ya Biblia, na maovu makubwa yalishamiri miongoni mwa watu wa matabaka yote. Huss alikemea bila hofu maovu hayo, akitumia neno la Mungu kuimarisha kanuni za ukweli na usafi aliouhimiza.

Mkazi wa Prague, Jerome, ambaye baadaye alikuja kuwa karibu sana na Huss, aliporudi kutoka Uingereza, alileta maandishi ya Wycliffe. Malkia wa Uingereza, ambaye alikuwa mwongofu wa mafundisho ya Wycliffe, alikuwa binti wa mfalme wa Bohemia, na kwa mvuto wake pia kazi za Mwanamatengenezo zilisambazwa katika maeneo mengi ya nchi yake alikozaliwa. Huss alisoma maandishi haya kwa shauku kubwa; aliamini mwandishi wa maandishi yale alikuwa Mkristo wa kweli na Huss alichukua mwelekeo wa kuyakubali mafundisho ya Wycliffe. Tayari, japokuwa alijua hivyo, Huss alikuwa ameshika njia ambayo ingempeleka mbali sana na Roma. Karibu na wakati huu watu wawili walifika Prague kutoka Uingereza, wasomi, waliokuwa wamepokea nuru na walikuwa wamekuja kueneza nuru hiyo katika nchi hii ya mbali.

Wakianza na shambulizi la wazi dhidi ya ukuu wa papa, mamlaka ziliwanyamazisha mara moja; lakini kwa kutokuwa tayari kukubali kuacha lengo lao, walitafuta njia zingine. Kwa kuwa walikuwa wanasanaa na wahubiri, waliendelea kwa kutumia sanaa yao. Katika eneo la wazi walichora picha mbili. Moja ilimwakilisha Kristo akiingia Yerusalemu, “mnyenyekevu, na akiwa ameketi juu ya mwanapunda” (Mathayo 21:5), na akifuatwa na wanafunzi Wake wakiwa wamevaa nguo zilizochakaa kwa sababu ya safari na wakiwa na miguu isiyokuwa na viatu. Picha nyingine ilionesha msafara wa papa—papa akiwa amevalia majoho ya kitajiri na taji tatu, akiwa amekaa juu ya farasi aliyepambwa kwa mapambo ya gharama kubwa, akiwa ametanguliwa na wapiga tarumbeta na akiwa amefuatwa na makadinali na maaskofu waliovalia mavazi yanayomeremeta.

Hapa kulikuwa na hubiri lililovuta hisia za watu wa matabaka yote. Makundi makundi makubwa ya watu yalikuja kuangalia michoro hii. Hakuna hata mtu mmoja aliyeshindwa kuelewa fundisho la michoro hiyo, na wengi waliguswa sana na tofauti kati ya upole na unyenyekevu wa Kristo Bwana na kiburi na majivuno ya papa, aliyedai kuwa mtumishi wa Kristo. Kulikuwa na taharuki kubwa mjini Prague, na wageni baada ya muda mfupi waliona umuhimu, kwa ajili ya usalama wao, wa kuondoka pale. Zile picha ziligusa sana akili za Huss na zilimsukuma kujifunza kwa makini zaidi Biblia na maandishi ya Wycliffe. Japokuwa hakuwa taari, mpaka wakati huo, kupokea matengenezo yote yaliyofundishwa na Wycliffe, aliona kwa uwazi zaidi tabia halisi ya upapa, na kwa juhudi kubwa alikemea kiburi, tamaa, na ufisadi wa mfumo wa upapa.

Kutoka katika nchi ya Bohemia nuru ilisambaa katika nchi ya Ujerumani, kwani machafuko katika Chuo Kikuu cha Prague yalisababisha mamia ya wanafunzi kutoka Ujerumani kuondoka. Wengi wao walikuwa wameshapokea mafundisho ya awali ya Biblia, na waliporudi nyumbani walieneza injili katika nchi yao.

Habari za kazi iliyofanyika kule Prague ilipelekwa Roma, na Huss aliitwa kujibu mashtaka mbele ya papa. Kutii wito huo kulimaanisha kifo moja kwa moja. Mfalme na malkia wa Bohemia, chuo kikuu, waheshimiwa wasaidizi wakuu wa mfalme, na maofisa wa serikali wote waliungana pamoja kutoa wito kwa papa kuwa Huss aruhusiwe kubaki Prague na ajibu mashtaka yake kupitia kwa mwakilishi wa Roma. Badala ya kukubali ombi hili, papa aliendelea na kusikiliza shtaka na kutoa hukumu ya Huss, na ndipo alitangaza kuwa jiji la Prague lilikuwa limefungiwa.

Katika zama zile hukumu kama hii, ilipotolewa, ilileta hofu kubwa kwa watu wengi. Hatua zilizoambatana na hukumu hii zilibuniwa kuzalisha hofu kubwa mioyoni mwa watu waliomwamini papa kuwa ni mwakilishi wa Mungu Mwenyewe, aliyeshikilia funguo za mbingu na kuzimu, na aliyekuwa na mamlaka ya kutamka hukumu za hapa duniani na za kiroho. Iliaminika kuwa milango ya mbinguni ilifungwa dhidi ya eneo lililohukumiwa kufungiwa; kuwa mpaka pale ambapo papa angependezwa kuondoa kufungiwa huko, waliokufa walikuwa wakifungiwa nje ya makao ya amani. Kama ishara ya janga hili la kutisha, huduma zote za dini zilisitishwa. Makanisa yalifungiwa. Ndoa zilifungiwa katika viwanja vya makanisa. Wafu, kwa kunyimwa mazishi katika maeneo yaliyowekwa wakfu, walizikwa, bila kaida za mazishi, katika mitaro au mashamba. Hivyo basi, kwa hatua hizi zilizogusa fikra za watu, Roma ilifanikiwa kutawala dhamiri za watu.

Jiji la Prague liliingia katika machafuko makubwa. Kundi kubwa la watu walimlaumu Huss kama chanzo cha majanga yao yote na walidai kuwa akabidhiwe kwa mamlaka za Roma ili kisasi cha kanisa kichukue mkondo wake. Kutuliza dhoruba, Mwanamatengenezo aliondoka kwa muda kwenda kukaa kijijini kwake alikozaliwa. Akiwaandikia marafiki zake

aliowaacha pale Prague, alisema: "Ikiwa nimetoweka kutoka katikati yenu, ni ili nifuate kanuni na mfano wa Yesu Kristo, nisitoe nafasi kwa watu wenye nia mbaya kujiletea hukumu ya milele juu yao, na ili nisiwe chanzo cha usumbufu na mateso kwa watakatifu. Nimepumzika pia kwa sababu ya hofu kuwa mapadre waovu wasiendelee kuzuia kazi ya kuhubiri neno la Mungu miongoni mwenu; lakini sikuondoka ili ninyi muukane ukweli wa neno la Mungu, ambao kwa ajili yake, kwa msaada wa Mungu, niko tayari kufa."— Bonnechose, The Reformers Before the Reformation, vol. 1, uk. 87. Huss hakuacha kufanya kazi zake, lakini alisafiri katika maeneo yote ya nchi jirani, akihubiri injili kwa watu waliokuwa na shauku. Hivyo hatua ambazo papa alijielekeza kuzitumia kukandamiza injili zilikuwa zikiiwezesha kusambaa zaidi. "Maana hatuwezi kutenda neno lo lote kinyume cha kweli, bali kwa ajili ya kweli" (2 Wakorintho 13:8).

"Akili ya Huss, katika hatua hii ya kazi yake, ingeonekana kuwa mandhari ya mgogoro wenye maumivu. Ingawa kanisa lilikuwa likitafuta kumshinda kwa kutumia vitisho, Huss hakuwa ameacha kutambua mamlaka yake. Kanisa la Roma lilikuwa bado mke wa Kristo, na papa alikuwa mwakilishi na msadizi wa karibu wa Mungu. Huss alikuwa akipiga vita dhidi ya matumizi mabaya ya mamlaka, na siyo kanuni yenyewe. Jambo hili lilileta mgogoro wa kutisha kati ya imani ya uelewa wake na madai ya dhamiri yake. Ikiwa mamlaka ya kanisa ilikuwa ya haki na isiyokosea, kama alivyoamini kuwa hivyo, ilikuwaje tena ajisikie kulazimika kutoitii mamlaka yenyewe? Aliona kuitii ni kutenda dhambi; lakini kwa nini utii kwa kanisa lisilokosea limfanye kujisikia kutenda dhambi?

Hili lilikuwa tatizo lililomshinda kutanzua; haya yalikuwa mashaka yaliyomtesa saa hadi saa. Suluhisho lililoelekea kumsaidia lilikuwa kwamba jambo lile lilikuwa limejirudia tena, kama ilivyowahi kutokea zamani katika siku za Mwokozi, kuwa viongozi wa kanisa walikuwa wameharibika na kuwa waovu na walikuwa wakitumia mamlaka halali kukidhi malengo yasiyokuwa halali. Wazo hili alilifanya kuwa mwongozo wake, na aliwahubiria wengine wazo hilo liwe mwongozo wao, msemo kuwa kanuni za Maandiko, zilizopatikana kwa njia ya uelewa, zinapaswa kutawala dhamiri; kwa maneno mengine, kwamba Mungu akizungumza katika Biblia, na siyo kanisa likisema kupitia upapa, ndiyo mwongozo pekee usiokosea."— Wylie, b. 3, ch. 2.

Baada ya vurugu katika jiji la Prague kutulia, Huss alirudi katika kanisa lake la Bethlehemu, kuendelea kwa juhudi na ujasiri mkubwa kuhubiri neno la Mungu. Maadui zake walikuwa kazini na walikuwa na nguvu, lakini malkia na wengi wa waheshimiwa wasaidizi wa karibu wa mfalme walikuwa marafiki zake, na watu wengi walisimama upande wake. Wakilinganisha mafundisho safi na yanayoinua na maisha matakatifu dhidi ya mafundisho yanayodhalilisha yasiyokosolewa yaliyohubiriwa na viongozi wa Roma, na tamaa ya mali na uovu walioufanya, wengi waliona kuwa heshima kuwa upande wa Huss.

Hadi wakati huo, Huss alikuwa amesimama peke yake katika kazi zake; lakini sasa Jerome, ambaye wakati akiwa Uingereza aliyakubali mafundisho ya Wycliffe, alijiunga na kazi ya matengenezo. Tangu wakati huo na siku zilizofuata watu hawa wawili waliunganisha maisha yao, na katika kifo hawakupaswa kutengana. Uwezo wa kiakili, ufasaha na elimu—karama zinazowezesha mtu kukubaliwa na wengi—zilimilikiwana kwa kiwango kikubwa na Jerome; lakini katika zile sifa zinazounda nguvu ya tabia, Huss alikuwa juu zaidi. Maamuzi yake yaliyotulia yalisaidia kudhibiti roho yenye harara ya Jerome, ambaye, kwa unyenyekevu wake wa kweli, alielewa mantiki yake, na alijisalimisha kwa ushauri wake. Kwa kazi zao zilizounganishwa pamoja, matengenezo yalienea kwa haraka.

Mungu aliruhusu nuru kubwa iangazie akili za watu hawa waliochaguliwa, ikiwafunulia makosa mengi ya Roma; lakini hawakupokea nuru yote iliyopaswa kutolewa kwa ulimwengu. Kwa njia ya hawa, watumishi Wake, Mungu alikuwa akiwaongoza watu kutoka katika giza la Uroma; lakini vilikuwepo vikwazo vingi na vikubwa ambavyo viliwakabili, na aliwaongoza kusonga mbele, hatua kwa hatua, kwa kadiri walivyoweza kubeba. Hawakuwa tayari kupokea nuru yote kwa mara moja. Kama mwanga mkali wa jua la mchana kwa watu ambao wamekaa kwa muda mrefu gizani, ingeweza, kama ingeruhusiwa kuwaangazia, ingeweza kuwafanya wageukie upande mwingine. Kwa hiyo aliifunua nuru kwa viongozi kidogo kidogo, kwa kadiri watu walivyoweza kuipokea. Kutoka karne moja hadi karne nyingine, watendakazi wengine waaminifu walipaswa kufuata, kuwaongoza watu kusonga mbele zaidi katika njia ya matengenezo.

Mpasuko katika kanisa uliendelea. Mapapa watatu walikuwa wakigombania madaraka, na mgogoro wao ulijaza uhalifu na vurugu katika ulimwengu wote wa Kikristo. Kwa kutoridhishwa na kurushiana maneno ya laana, waligeukia matumizi ya silaha za kidunia. Kila mmoja wao alijielekeza kununua silaha na kupata askari. Ili kufanikisha suala hilo ilikuwa lazima pesa ipatikane; na ili kupata pesa, zawadi, vyeo, na baraka za kanisa vilikuzwa. (Tazama Kiambatisho.) Mapadre pia, wakiwaiga wakubwa wao, waligeukia matumizi ya nguvu na vita kuwanyenyekesha wapinzani wao na kuimarisha nguvu yao. Kwa ujasiri uliokuwa ukiongezeka kila siku Huss aliunguruma dhidi ya machukizo yaliyolelewa katika jina la dini; na watu waliwalaumu viongozi wa Uroma kama chanzo cha mateso yaliyogubika Ukristo.

Kwa mara nyingine jiji la Prague lilionekana kuwa kwenye ukingo wa mgogoro na umwagaji damu. Kama ilivyokuwa katika vizazi vya zamani, mtumishi wa Mungu alishitakiwa kama “mtaabishaji wa Israeli” (1 Wafalme 18:17). Jiji lilifungiwa tena, na Huss alikwenda kujificha kijijini kwake alikozaliwa. Ushuhuda uliotolewa kwa uaminifu kutokea kanisa lake pendwa la Bethlehemu ulikomeshwa. Alikuwa anakwenda kuzungumza kutokea jukwaa pana zaidi, kwa ulimwengu wa Ukristo wote, kabla ya kusalimisha maisha yake kwa ajili ya kweli.

Kutibu maovu yaliyokuwa yameshika usikivu wa watu wa Ulaya, baraza kuu liliitwa kukutana katika jiji la Constance. Baraza liliitwa kwa utashi wa mfalme Sigismund, kupitia kwa mmoja wa mapapa watatu waliokuwa wakisigana, ambaye alikuwa Yohana XXIII. Hitaji la kuwepo kwa baraza lilikuwa mbali kabisa na utashi wa Papa Yohana, ambaye tabia na sera yake isingefaa kutathminiwa, hata na maaskofu waliokuwa dhaifu kama walivyokuwa waumini wa kanisa wa nyakati zile. Hakuthubutu, hata hivyo, kupinga matakwa ya Sigismund (Tazama Kiambatisho).

Malengo makuu yaliyokusudiwa kutimizwa na baraza yalikuwa kuponya utengano katika kanisa na kung'oa mizizi ya uzushi. Hivyo watu wawili waliokuwa wapinzani wa mapapa waliitwa kuja kujibu mashtaka mbele ya baraza hilo, akiwemo msambazaji mkuu wa hayo maoni mapya, John Huss. Mfalme Sigismund, kwa kuhofia usalama wake, hakuhudhuria yeye mwenyewe binafsi, lakini aliwakilishwa na wajumbe. Papa Yohana, wakati akionekana kuwa mwalikaji wa baraza, alikuja barazani akiwa na mashaka mengi, akishuku lengo la siri la mfalme la kumwondoa madarakani, na akihofia kuwajibishwa kwa maovu yaliyochafua cheo cha upapa, na uhalifu uliotumika kukipata. Hata hivyo aliingia katika jiji la Constance kwa mbwembwe sana, akisindikizwa na viongozi wa kanisa wa ngazi ya juu sana na msafara wa watendaji katika ofisi yake. Viongozi wote wa dini na jiji, pamoja na kundi kubwa la wakazi wa jiji, walikwenda kumlaki. Juu ya kichwa chake kulikuwepo mwavuli wa dhahabu, uliobebwa na majaji wakuu wanne. Mwenyeji alikuwa amebebwa mbele yake, na mavazi ya gharama ya makadinali na waheshimiwa vilitengeneza mandhari ya kuvutia sana.

Wakati huo huo msafiri mwingine alikuwa akikaribia jiji la Constance. Huss alijua hatari zilizotishia maisha yake. Aliachana na marafiki zake kana kwamba hataweza kukutana nao tena, na alisonga mbele akihisi safari yake ilikuwa ikimpeleka kwenye ncha kali ya mti. Pamoja na hayo alikuwa amepata hakikisho la usalama kutoka kwa mfalme wa Bohemia, na alipata tena hakikisho la usalama kutoka kwa mfalme wa Sigismund akiwa katika safari yake, alifanya mipango yake yote akitazamia uwezekano wa kifo chake. Katika barua yake kwa marafiki zake wa Prague alisema: "Ndugu zangu, ... ninaondoka nikiwa na hakikisho la usalama kutoka kwa mfalme kwenda kukutana na maadui wengi na wanaokufa. ninaweka tumaini langu lote kwa Mungu mweza wa yote, Mwokozi wangu; ninaamini atayasikia maombi yenu ya dhati, ili aweke maono na hekima katika mdomo wangu, ili kwamba niweze kuwapinga; na kwamba aniwezeshe kwa njia ya Roho Wake Mtakatifu kusimama imara katika ukweli, ili nikabiliane, kwa ujasiri, na majaribu, gereza, na, ikiwa lazima, na kifo cha kikatili.

Yesu Kristo aliteseka kwa ajili ya wapendwa Wake aliowapenda sana; na hivyo, tushangae kuwa alituachia mfano Wake, ili na sisi tukabiliane kwa uvumilivu na mambo yote kwa ajili ya wokovu wetu? Yeye ni Mungu, na sisi ni viumbe Wake; Yeye ni Bwana, na sisi ni watumishi Wake; Yeye ni Bwana wa ulimwengu, na sisi ni wanadamu wenye hali ya kufa

katika hali dhalili—na bado aliteseka! Kwa nini, hivyo basi, sisi tusiteseke pia, hususani kwa kuwa mateso kwetu ni utakaso? Kwa hiyo, wapendwa, ikiwa kifo changu kinaweza kuchangia kuleta utukufu Wake, ombeni ili kije haraka, na kwamba aniwezeshe kukabiliana na mikasa yangu yote bila kuyumba. Lakini ikiwa itakuwa bora nirudi kwenu, tuombe kwa Mungu kuwa nirudi bila doa—yaani, kwamba nisije nikaminya hata nukta moja ya ukweli wa injili, ili niwaachie ndugu zangu mfano mzuri wa kufuata. Pengine, hivyo basi, hamtauona uso wakngu tena hapa Prague; lakini ikiwa mapenzi ya Mungu yataruhusu kunirudisha, inatupasa kusonga mbele kwa moyo imara zaidi katika ujuzi na upendo wa sheria Yake."—Bonnechose, vol. 1, uk. 147, 148. Katika barua nyingine, kwa kasisi aliyekuwa ameongoka na kuwa mfuasi wa injili, Huss alizungumzia kwa unyenyekevu mkubwa juu ya makosa yake, akijishitaki mwenyewe"kuhusiana na kuhisi raha ya kuvaa mavazi ya gharama kubwa na kuwapoteza muda katika kazi zisizokuwa na maana." Ndipo aliongeza maonyo haya yanayogusa:

"Hebu utukufu wa Mungu na wokovu wa roho ujaze akili yako, na siyo mali na mashamba. Jihadhari kuipamba nyumba yako kuliko roho yako; na, juu ya yote, jali jengo lako la kiroho. Uwe mtakatifu na mnyenyekevu na watu maskini, na usile chakula kwa ulafi. Ikiwa hutatengeneza maisha yako na kuachana na mambo ya juu juu, ninaogopa utapigwa sana kama mimi. Wewe unayajua sana mafundisho yangu, kwa kuwa wewe umeyapokea maelekezo yangu tangu utoto wako; kwa hiyo sina haja ya kukuandikia tena. Lakini ninakusihi, kwa rehema ya Bwana wetu, usiniige kwa cho chote miongoni mwa mambo yasiyofaa ambamo umeona kuwa nimetumbukia." Juu ya bahasha ilimokuwa barua hiyo aliongeza maneno haya: "Ninakusihi, rafiki yangu, usiichane bahasha hii mpaka umepata cheti cha uthibitisho kuwa nimekufa."—Ibid., vol. 1, uk. 148, 149.

Katika safari yake, Huss aliona kila mahali alama za kusambaa kwa mafundisho yake na jinsi kazi yake ilivyoungwa mkono. Watu walijikusanya kumlaki, na katika baadhi ya miji, mahakimu walijitokeza kuwa naye kwenye mitaa yao.

Alipowasili katika jiji la Constance, Huss alipewa uhuru kamili. Pamoja na hakikisho la usalama kutoka kwa mfalme, kuliongezeka hakikisho la ulinzi binafsi wa papa. Lakini, kinyume na ahadi hizi za usalama zilizotolewa kwa matamko ya dhati na kwa kurudia rudia, Mwanamatengenezo alikamatwa baada ya muda mfupi, kwa amri ya papa na makadinali, na alitupwa katika gereza la kuchukiza. Baadaye alihamishiwa katika jumba moja ng'ambo ya mto Rhine na huko alishikiliwa kama mfungwa. Papa, akifaidi kidogo sana kutokana na hila yake, naye baada ya muda mfupi alitupwa katika gereza lile lile. Ibid., vol. 1, uk. 247. Alithibitika mbele ya baraza kuwa na hatia ya uhalifu wa kutisha, mbali na mauaji, utoaji wa hongo ili kupata cheo kanisani, na uzinzi, "dhambi zisizostahili kutajwa." Hivyo ndivyo baraza lenyewe lilivyotangaza, na hatimaye alivuliwa kofia ya upapa na alitupwa gerezani. Na wapinzani wa upapa pia waliondolewa madarakani, na papa mpya alichaguliwa.

Ingawa papa mwenyewe alikuwa na hatia ya kutenda uhalifu mkubwa zaidi kuliko hata Huss alivyokuwa amewatuhumu makasisi, na ambao Huss alikuwa akidai ufanyiwe matengenezo, hata hivyo baraza lile lile lililomdhalilisha papa liliendelea kumkandamiza Mwanamatengenezo. Kufungwa kwa Huss kuliamsha hasira kali katika nchi ya Bohemia. Watu waungwana wenye nguvu walipeleka malalamiko kwenye baraza dhidi ya ukatili huu mkubwa. Mfalme, ambaye alichukia kwa kuruhusu ukiukwaji wa hakikisho la usalama, alipinga hatua hiyo ya mashitaki dhidi yake. Lakini maadui wa Mwanamatengenezo walikuwa waovu na walikuwa wamedhamiria. Walijitahidi kumshawishi mfalme awaunge mkono wakijaribu kupata fadhila yake, na kumtia hofu, wakimhamasisha kuwa upande wa kanisa. Walitoa hoja nyingi kuthibitisha kuwa“imani haipaswi kuchanganywa na wazushi, wala watu wanaotuhumiwa kuwa wazushi, hata kama wamepewa hati za hakikisho la usalama kutoka kwa mkuu wa dola au wafalme wa kawaida.”—Jacques Lenfant, History of the Council of Constance, vol. 1, p. 516. Hatimaye walishinda.

Akiwa amedhoofika kwa sababu ya ugonjwa na kifungo,—kwa sababu ya hewa nzito na unyevunyevu wa gereza alipata homa ambayo karibu ikatishe uhai wake,— Huss hatimaye alifikishwa mbele ya baraza. Akiwa na mzigo mzito wa minyororo alisimama mbele ya mfalme, ambaye heshima na nia yake nzuri ilikuwa imeahidi kumlinda. Wakati wa majaribu yake alisimamia daima ukweli, na mbele ya viongozi wakuu wa kanisa na serikali waliokusanyika pamoja alitamka maneno adhimu na uaminifu ya kupinga ufisadi wa kanisa. Alipotakiwa kuchagua kati ya kukana mafundisho yake au kuuawa, alikubali kifo cha mfia dini.

Neema ya Mungu ilimshikilia. Katika majuma ya mateso yaliyopita kabla ya hukumu yake ya mwisho, amani ya mbinguni ilijaza moyo wake. “Ninaandika barua hii,” alimwambia rafiki yake, “katika gereza langu, na mkono wangu wenye pingu, nikitarajia hukumu yangu ya kifo kesho Wakati, kwa msaada wa Yesu Kristo, tutakapoonana tena katika amani tamu ya maisha yajayo, utaelewa jinsi Mungu alivyojionesha kuwa mwenye rehema kwangu, jinsi alivyonisaidia kati kati ya majaribu na mitihani.”—Bonnechose, vol. 2, uk. 67.

Katika giza la gereza lake aliona kabla ushindi wa imani ya kweli. Akirejea katika ndoto zake katika kanisa lake la Prague ambapo alikuwa amehubiri injili, aliona papa na maaskofu wake wakiziharibu picha za Kristo alizokuwa amezichora kwenye kuta zake. “Njozi hii ilimsumbua: lakini siku iliyofuata aliona wachoraji wengi wakiwa katika kazi ya kuzirudisha picha zile kwa wingi zaidi na kwa rangi zinazong’aa zaidi. Mara tu kazi yao ilipokwisha, wachoraji waliokuwa wamezungukwa na kundi kubwa la watu, walisema kwa sauti kubwa,‘Sasa acha mapapa na maaskofu waje; hawataweza kuzifuta tena!’” Alisema Mwanamatengenezo, aliposimulia ndoto yake: “Nina imani thabiti kuwa, Sura ya Kristo haitafutika kamwe. Wametamani kuiharibu, lakini itachorwa upya katika mioyo yote kwa wahubiri bora zaidi kuliko mimi.”— D’Aubigne, b. 1, ch. 6.

Kwa mara ya mwisho, Huss aliletwa mbele ya baraza. Ulikuwa mkutano mkubwa sana—mfalme, wakuu wengine wa ngazi za juu za ufalme, manaibu wakuu katika ufalme, makadinali, maaskofu, na makasisi, na kundi kubwa la watu waliokuja kama watazamaji wa matukio wa siku ile. Kutoka sehemu zote za Ukristo walikuwa wamekusanyika kushuhudia kafara kuu hii ya kwanza katika pambano refu ambalo kwalo uhuru wa dhamiri ungeweza kupatikana. Akiwa ameitwa kwa ajili ya uamuzi wake wa mwisho, Huss alitamka kukataa kwake kukana, na, akikaza macho yake yanayopenya huku akimwangalia mfalme ambaye alikuwa amekiuka ahadi yake bila aibu, alisema: "Nilidhamiria, kwa uhuru na utashi wangu mwenyewe, kuja mbele ya baraza, chini ya ulinzi na imani ya mfalme aliyeko hapa."—Bonnechose, vol. 2, uk. 84. Wekundu uliokolea sana ulipamba uso wa Sigismund huku macho ya wote waliokusanyika hapo yakigeuka kumwangalia.

Baada ya hukumu kutamkwa, sherehe ya dhihaka ilianza. Maaskofu walimvika mfungwa wao vazi la kipadre, na alipokuwa akivalishwa vazi hilo, alisema: "Bwana wetu Yesu Kristo alivikwa joho jeupe, ili kumdhihaki, wakati Herode alipompeleka mbele ya Pilato."—Ibid., vol. 2, p. 86. Alipotakiwa tena kukana, alijibu, akiwageukia watu: "Ni kwa uso gani, tena, ningeweza kutazama mbinguni? Ni kwa jinsi gani niwaangalie umati wa watu ambao nimewahubiria injili? Hapana; ninachukulia wokovu wao kuwa wa muhimu zaidi kuliko mwili huu maskini, ambao sasa umepangiwa kuuawa." Nguo ziliondolewa moja baada ya nyingine, na kila askofu alitamka laana alipokuwa akifanya sehemu yake ya sherehe. Hatimaye"waliweka kichwani mwake kofia ya karatasi yenye muundo wa piramidi, ambayo juu yake ilichorwa picha za kutisha za mashetani, pamoja na maneno 'Mzushi Mkuu' yakionekana mbele. 'Kwa furaha kuu,' Huss alisema, 'nitavaa taji hii ya aibu kwa ajili Yako, Ee Yesu, uliyevaa taji ya miiba kwa ajili yangu.'"

Baada ya kuvalishwa hivyo, "maaskofu walisema, 'Sasa tunaiweka roho yako wakfu kwa yule mwovu.' 'Na mimi,' John Huss alisema, huku akiinua macho yake juu mbinguni, 'ninaisalimisha roho yangu mikononi Mwako, Ee Bwana Yesu, kwa kuwa Wewe ulinikomboa.'"—Wylie, b. 3, ch. 7.

Sasa alikabidhiwa katika mamlaka za kidunia na kupelekwa mahali pa kuuawa. Msafara mkubwa ulifuata, mamia ya watu wakiwa na silaha, mapadre na maaskofu wakiwa katika mavazi yao ya gharama, na wakazi wa Constance. Alipokuwa amefungiwa kwenye mti wa kuulia, na kila kitu kikiwa tayari ili moto uwashwe, mfia dini aliulizwa mara nyingine tena kujiokoa kwa kukana makosa. "Makosa gani," alisema Huss, "napaswa kuyakana? Najua kuwa sina hatia yo yote. Ninamwita Mungu ashuhudie kuwa yote niliyoandika na niliyoyahubiri yalikusudiwa kuokoa roho kutoka dhambini na kuwaepusha na adhabu; na, kwa hiyo, kwa furaha kabisa nitathibitisha kwa damu yangu ukweli niliouandika na niliouhubiri."—Ibid., b. 3, ch. 7. Wakati moto ulipowashwa na kumzunguka pande zote, alianza kuimba, "Yesu, Wewe Mwana wa Daudi, unihurumie," na aliendelea kuimba mpaka sauti yake iliponyamazishwa kabisa.

Hata maadui zake waliguswa na ushujaa wake wa kipekee. Mfuasi mkereketwa wa upapa, akielezea kifo cha Huss, na cha Jerome, ambaye alikufa muda mfupi baadaye, alisema: "Wote wawili walidumisha msimamo wao wa kiakili wakati saa yao ya mwisho ilipokaribia. Walikuwa wamejiandaa kwa ajili ya moto kana kwamba walikuwa wakienda kwenye sherehe ya harusi.

Hawakutoa sauti ya kilio cha maumivu. Wakati moto ulipoinuka, walianza kuimba; na ukali wa moto haukuweza kuzuia uimbaji wao."—Ibid., b. 3, ch. 7. Wakati mwili wa Huss ulipoteketezwa kabisa, majivu yake, pamoja na udongo uliokuwa umekaliwa na majivu, vilikusanywa na kutupwa katika mto wa Rhine, na hivyo kuchukuliwa hadi baharini. Watesi wake walijidanganya kuwa wameng'oa mizizi yote ya ukweli aliouhubiri. Hawakuwa na ndoto yo yote kuwa majivu yaliyochukuliwa siku ile yalikuwa kama mbegu iliyosambazwa katika nchi zote duniani; kwamba katika nchi ambazo walikuwa hawazijui wakati ule ingezaa matunda kuwa ushuhuda kwa ajili ya ukweli. Sauti iliyokuwa imesema katika ukumbi wa baraza la Constance ilikuwa imeamsha miangwi ambayo ingesikika katika zama zote zilizofuata. Huss hakuwepo tena, lakini ukweli alioufia usingeangamia kamwe. Mfano wake wa imani na msimamo usioyumba vingewatia moyo watu wengi kusimama imara kwa ajili ya ukweli, wakikabiliwa na mateso na kifo. Kuuawa kwake kuliudhihirishia ulimwengu wote ukatili wa kutisha wa Roma. Maadui wa ukweli, ingawa hawakujua, walikuwa wakihamasisha kazi ambayo walikuwa wakijaribu kuiharibu bila mafanikio.

Hata hivyo bado mti mwingine wa kuunguzia mtu ulikuwa unaandaliwa jijini Constance. Damu ya shahidi mwingine ilipaswa kutoa ushuhuda kwa ajili ya ukweli. Jerome, baada ya kumuaga Huss alipokuwa akienda kwenye baraza, alimtia moyo awe jasiri na imara, akitangaza kuwa ikiwa angekutana na hatari yo yote, yeye mwenyewe angeruka mara moja kwenda kumsaidia. Alipopata taarifa za kufungwa kwake gerezani, mwanafunzi mwaminifu alijiandaa haraka kutimiza ahadi yake. Bila hati ya uhakikisho wa usalama aliondoka kwenda Constance akiwa na msaidizi mmoja. Alipofika pale alitambua kuwa alikuwa amejipeleka mwenyewe katika hatari, pasipokuwa na uwezekano wo wote wa kumwokoa Huss.

Alikimbia kutoka katika jiji, lakini alikamatwa akiwa njiani kuelekea nyumbani na kurudishwa akiwa amefungwa minyororo na akiwa chini ya ulinzi wa kikosi cha maaskari. Alipotokea mbele ya baraza kwa mara ya kwanza jitihada zake za kujibu mashtaka yaliyoletwa dhidi yake zilikutana na makelele, "Motoni pamoja naye! Motoni pamoja naye!"—Bonnechose, vol. 1, p. 234.

Alitupwa gerezani, akiwa amefungwa minyororo na kukalishwa katika mkao uliomletea mateso makali sana, na aliishi kwa kula mkate na kunywa maji tu. Baada ya miezi kadhaa ya ukatili wa kifungo chake ulimletea Jerome ugonjwa ambao ulitishia maisha yake, na maadui

zake, wakihofia kuwa anaweza kuwatoka, walimtendea kwa ukatili nafuu kidogo, ingawa alibaki gerezani kwa mwaka mmoja.

Kifo cha Huss hakikuleta matokeo ambayo wafuasi wa papa waliyatarajia. Ukiukwaji wa hati ya usalama iliamsha dhoruba ya hasira, na kama njia iliyo salama zaidi, baraza liliazimia, badala ya kumchoma moto Jerome, limlazimishe, ikiwezekana, akanushe. Aliletwa mbele ya mkutano wa baraza, na likampa njia mbadala ya kukanusha, au kufa kwenye mti. Kifo mwanzoni mwa kifungo chake kingekuwa jambo jema zaidi kuliko mateso makali ambayo aliyapitia; lakini sasa, akiwa amedhoofishwa na ugonjwa, kwa ukali wa gereza, na mateso ya wasiwasi na hofu ya mambo yajayo, akiwa ametengwa na marafiki, na akiwa amekatishwa tamaa kwa kifo cha Huss, ujasiri wa Jerome ulizidiwa, na alikubali kujisalimisha kwa baraza. Aliahidi kufuata imani ya kikatoliki, na alikubaliana na uamuzi wa baraza la kuhukumu mafundisho ya Wycliffe na Huss, akikubaliana, hata hivyo, na "ukweli mtakatifu" ambao waliufundisha.—Ibid, vol. 2, uk. 141.

Kwa kitendo hiki cha makusudi Jerome alijaribu kunyamazisha sauti ya dhamiri na kuepuka hukumu yake ya mwisho. Lakini katika upweke wa gereza lake alielewa vizuri kile alichokuwa amekifanya. Alifikiria juu ya ujasiri na uaminifu wa Huss, na kinyume alitafakari juu ya kuukana kwake ukweli. Alimtafakari Bwana mwenye Uungu aliyekuwa ameahidi kumtumikia, na ambaye kwa ajili yake alivumilia kifo cha msalaba. Kabla hajakana alipata faraja, katikati ya mateso yake, katika uhakikisho wa upendeleo wa Mungu; lakini sasa huzuni na mashaka vilitesa roho yake. Alijua kuwa bado atatakiwa kukana mambo mengine zaidi ili awe na imani na Roma. Njia aliyokuwa anaichukua ingeishia katika uasi kamili. Alifanya uamuzi: Kuepuka kipindi kifupi cha mateso hakupaswa kumkana Bwana wake.

Kwa mara nyingine tena alirudishwa mbele ya baraza. Kujisalimisha kwake hakukuwaridhisha mahakimu wake. Kiu yao ya damu, iliyokuwa imechochewa na kifo cha Huss, ilidai wahanga wapya. Ili kuokoa maisha yake Jerome alipaswa kuukana ukweli kabisa. Lakini aliazimia kushikilia imani yake na kumfuata ndugu yake mfia dini katika ndimi za moto.

Alibadilisha msimamo wake wa awali wa kuikana imani yake na, kama mtu anayekufa, alitamani sana apewe fursa ya kujitetea. Kwa kuogopa mvuto wa maneno yake, maaskofu walisisitiza kuwa yeye alitakiwa kukubali au kukanusha ukweli wa mashitaka yaliyoletwa dhidi yake. Jerome aliupinga ukatili na udhalimu mkubwa kama ule. "Mmenishikilia kifungoni kwa siku mia tatu na arobaini katika gereza linalotisha," alisema, "katikati ya uchafu, kelele, harufu mbaya, bila mahitaji yo yote muhimu; halafu mnanileta mbele yenu, na mnawasikiliza maadui wangu wa kimaadili, mnakataa kunisikiliza.... Ikiwa kweli ninyi ni watu wenye busara, na nuru ya ulimwengu, muwe waangalifu basi msitende dhambi dhidi ya haki. Mimi kama mimi, ni mtu dhaifu na mwenye hali ya kufa; maisha yangu yana umuhimu

mdogo sana; ninapowasihi kuwa msitoe hukumu isiyo ya haki, ninazungumza kidogo sana kwa ajili yangu bali zaidi kwa ajili yenu."—Ibid., vol. 2, uk. 146, 147.

Hatimaye ombi lake lilikubaliwa. Akiwa mbele ya majaji wake, Jerome alipiga magoti na kuomba kuwa Roho wa Mungu atawale mawazo na maneno yake, na kwamba asiseme jambo lolote linalopingana na ukweli au lolote lisilofaa kwa Bwana wake. Kwake siku ile ilitimizwa ahadi ya Mungu kwa wanafuzi wa kwanza: "Nanyi mtachukuliwa mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu…. Lakini hapo watakapowapeleka, msifikiri- fikiri jinsi mtakavyosema; maana mtapewa saa ile mtakayosema. Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu" (Mathayo 10:18-20).

Maneno ya Jerome yaliamsha mshangao na mvuto, hata kwa maadui zake. Kwa mwaka mzima alikuwa kifungoni, akiwa hawezi kusoma au kuona, katika maumivu makali ya kimwili na mashaka ya akili. Pamoja na hayo hoja zake ziliwasilishwa kwa uwazi na nguvu kana kwamba alikuwa na wakati usiobughudhiwa wa kujisomea. Aliwaelekeza wasikilizaji wake kwenye mlolongo wa watu watakatifu waliohukumiwa na majaji dhalimu. Karibu katika kila kizazi kulikuwepo na watu ambao, wakati walikuwa wakitafuta kuwainua watu wa wakati wao, walidhihakiwa na kutupwa nje, lakini ambao katika nyakati zilizofuata walikuja kuonekana kuwa walistahili heshima. Kristo mwenyewe alihukumiwa kama mkosaji katika mahakama dhalimu.

Wakati wa kukana, Jerome alikuwa amekubaliana na uhalali wa hukumu iliyomwadhibu Huss; sasa alitangaza toba yake na kushuhudia kutokuwa na hatia na utakatifu wa mfia dini yule. "Nilimjua toka utoto wake," alisema. "Alikuwa mtu mwema sana, mwenye haki na mtakatifu; alihukumiwa, licha ya kutokuwa na hatia yo yote Na mimi pia—niko tayari kufa: sitarudi nyuma kwa sababu ya mateso yaliyoandaliwa na maadui zangu na mashahidi wa uongo, ambao siku moja itawapasa kutoa hesabu ya uovu wao kwa Mungu mkuu, ambaye hawezi kudanganywa na cho chote."—Bonnechose, vol. 2, p. 151.

Kwa kujidhalilisha mwenyewe kwa kuukana kwake ukweli, Jerome aliendelea: "Miongoni mwa dhambi zote nilizowahi kuzitenda toka ujana wangu, hakuna hata moja iliyo na uzito mkubwa akilini mwangu, na kunifanya niumie sana, kama ile niliyoitenda mahali hapa pa mauaji, wakati nilipoidhinisha hukumu dhalimu iliyotoloewa dhidi ya Wycliffe, na dhidi ya mfia dini mtakatifu, John Huss, kiongozi na rafiki yangu. Ndiyo! Naiungama kwa dhati kutoka moyoni mwangu, na natangaza nikiwa na hofu na aibu kuwa niliteteteka wakati, kwa sababu tishio la kifo, niliyakana mafundisho yao. Kwa hiyo ninaomba. Mwenyezi Mungu anihurumie na kunisamehe dhambi zangu, na hususani dhambi hii, iliyo mbaya zaidi kuliko zote." Akiwaelekea majaji wake, alisema kwa mkazo: "Mliwahukumu Wycliffe na John Huss, siyo kwa kutikisa mafundisho ya kanisa, bali kwa kukemea kashifa za viongozi wa kanisa—majivuno yao, kiburi chao, na maovu yote ya maaskofu na mapadre. Mambo ambayo waliyasema, na ambayo hawezi kukanushika, mimi pia ninafikiri na kusema, kama wao."

Maneno yake yalikatishwa. Maaskofu, wakitetemeka kwa ghadhabu walipiga kelele:"Tunahitaji ushahidi mwingine wa nini? Tumeona kwa macho yetu sisi wenyewe wazushi wakorofi!"

Bila kuyumbishwa na dhoruba, Jerome alisema: "Nini! Mnadhani mimi naogopa kufa? Mmeniweka rumande kwa mwaka mzima katika gereza linalotisha, ambalo ni baya kuliko kifo chenyewe. Mmenishughulikia kwa ukatili zaidi kuliko Mturuki, Myahudi au mpagani, na nyama ya mwili wangu imeoza na kutaka kutoka kwenye mifupa nikiwa hai; na bado sijalalamika, kwa kuwa maombolezo ni jambo baya kwa mtu mwenye moyo na roho; lakini siwezi kujizuia kueleza mshangao wangu kwa unyama mkubwa mnaomtendea Mkristo."—Ibid., vol. 2, uk. 151-153.

Dhoruba ya hasira ililipuka tena, na Jerome alipelekwa haraka gerezani. Lakini walikuwepo baadhi ya watu ambao waliguswa sana na maneno yake na ambao walitamani kuokoa maisha yake. Alitembelewa na viongozi wa kanisa na walimsihi ajisalimishe kwa baraza. Marupu-rupu makubwa yaliahidiwa kwa ajili yake kama zawadi za kuachana na upinzani wake dhidi ya Roma. Lakini kama Bwana wake alipoahidiwa utukufu wa ulimwengu, Jerome alidumisha msimamo wake.

"Nithibitishieni makosa yangu katika Maandiko Matakatifu," alisema, "nami nitayakana."

"Maandiko Matakatifu!" alifoka mmoja wa wajaribu wake,"ndiyo yatumike kuhukumu kila kitu? Ni nani atayaelewa kanisa lisipoyatafsiri?"

"Je, mapokeo ya wanadamu ndiyo yastahili kuaminiwa zaidi kuliko injili ya Mwokozi wetu?" Jerome alijibu. "Paulo hakuwaagiza aliowaandikia kusikiliza mapokeo ya wanadamu, bali alisema, 'Chunguzeni Maandiko.'"

"Mzushi!" ndiyo lilikuwa jibu, "Ninajuta kwa kuwabembeleza kwa muda mrefu. Ninaona kuwa mnasukumwa na Shetani."—Wylie, b. 3, ch. 10.

Kabla hukumu ya adhabu haijapitishwa dhidi yake. Alipelekwa mahali pale pale ambapo Huss alifia. Alienda akiimba njiani, uso wake ukiwa umeng'aa kwa furaha na amani. Macho yake yalikuwa yameelekezwa kwa Kristo, na kwake kifo kilikuwa siyo tishio tena. Wakati mwuaji alipokuwa karibu kuwasha kuni moto, alisimama nyuma yake, mfia dini alisema: "Njoo kwa ujasiri; washa moto mbele ya uso wangu. Kama ningekuwa mwoga, nisingekuwa hapa."

Maneno yake ya mwisho, yaliyosemwa wakati moto ulipomzunguka, yalikuwa ya sala. "Bwana, Baba Mwenyezi," alilia, "nihurumie, na unisamehe dhambi zangu; kwa kuwa unajua

kuwa daima ninaupenda ukweli Wako."— Bonnechose, vol. 2, p. 168. Sauti yake ilikoma, lakini midomo yake iliendelea kucheza akiwa anaomba. Wakati moto ulipomaliza kazi yake, majivu ya mfia dini, pamoja na udongo uliokuwa umekaliwa na majivu, vilikusanywa, na kama ya Huss, yalitupwa katika mto wa Rhine.

Hivyo ndivyo wabeba nuru waaminifu wa Mungu walivyouawa. Lakini nuru ya ukweli walioutangaza—nuru ya mfano wao wa kishujaa— haikuzimwa. Kama vile ambavyo watu wasingeweza kugeuza mwelekeo wa jua sawa na jinsi wasingeweza kuzuia mapambazuko ya siku ile ambayo yalikuwa yakitokea ulimwenguni.

Kifo cha Huss kiliwasha moto wa hasira katika nchi ya Bohemia. Ilihisiwa na taifa lote kuwa alikufa kama mawindo ya chuki ya mapadre na hila za mfalme. Alitangazwa kuwa mwalimu mwaminifu wa ukweli, na baraza lililoamrisha kifo chake lilishitakiwa kwa kuhusika na mauaji. Mafundisho yake sasa yalikuwa na mvuto mkubwa zaidi kuliko wakati uliopita. Kwa njia ya maagizo ya papa maandishi ya Wycliffe yalitakiwa kuchomwa moto. Lakini yale yaliyokuwa yamepona kuangamizwa sasa yaliletwa kutoka mafichoni na kusomwa huku yakilinganishwa na Biblia, au sehemu zake kwa kadiri watu walivyoweza kuzipata, na wengi waliweza kuongozwa kuikubali imani iliyofanyiwa matengenezo.

Wauaji wa Huss hawakuweza kuendelea kuwa kimya na kushuhudia ushindi wa kazi yake. Papa na mfalme waliungana kuzima vuguvugu, na majeshi ya Sigismund yalitumwa Bohemia.

Lakini mkombozi aliinuliwa. Ziska, ambaye baada ya kuanza vita alipofuka kabisa, lakini ambaye alikuwa jenerali mwenye nguvu nyingi kuliko majenerali wote katika zama zake, alikuwa kiongozi wa Wabohemia. Akitumainia msaada wa Mungu na ukweli waliousimamia, watu wale waliweza kukabiliana na majeshi yenye nguvu kubwa kabisa ambayo yangeletwa dhidi yao. Tena na tena mfalme, akiandaa majeshi mapya, aliivamia Bohemia, lakini mara zote walirudishwa nyuma kwa aibu kubwa. Wafuasi wa Huss walikuwa wameinuliwa juu ya hofu ya kifo, na hakuna cho chote kingeweza kusimama dhidi yao. Miaka michache baada ya vita kuanza, Ziska jasiri alikufa; lakini nafasi yake ilijazwa na Procopius, ambaye naye alikuwa jenerali mwenye stadi nyingi za kivita, na katika mambo mengine alikuwa kiongozi mwenye uwezo mkubwa zaidi kuliko hata Ziska.

Maadui wa Wabohemia, wakijua kuwa mpiganaji kipofu alikuwa amekufa, waliona na fursa muafaka kwao kurudisha vyote walivyokuwa wamepoteza. Sasa papa alitangaza vita ya msalaba dhidi ya wafuasi wa Huss, na tena jeshi kubwa liliandaliwa dhidi ya Bohemia, lakini walishindwa vibaya sana. Vita nyingine ya msalaba ilitangazwa. Katika nchi zote zilizokuwa chini ya utawala wa papa huko Ulaya, watu, pesa, na silaha vilikusanywa. Makundi kwa makundi ya watu walifurika upande wa bendera ya papa, wakiwa na hakika kuwa hatimaye mwisho wa waumini wa uzushi wa Huss ulikuwa umefika. Wakiwa na hakika ya ushindi,

jeshi kubwa liliingia Bohemia. Watu wa Bohemia walijipanga kuwafukuza. Majeshi haya mawili yalikabiliana na mto uliokuwa katikati yao ndio uliowatenganisha. "Maaskari wa msalaba walikuwa jeshi kubwa mno, lakini badala ya kuvuka mto mara moja, na kuwavamia wafuasi wa Huss ambao ndio walikuwa wamekuja kuwakabili, walisimama kimya wakiwaangalia tu wale wapiganaji."—Wylie, b. 3, ch. 17.

Ndipo kwa ghafla tishio lisilojulikana kuwa lilitoka wapi liliwaangukia wanajeshi wa msalaba. Bila kufanya shambulio lolote, jeshi lile kubwa lilisambaratika na maaskari walitawanyika kana kwamba walifukuzwa na nguvu isiyoonekana. Idadi kubwa miongoni mwao waliuawa na jeshi la wafuasi wa Huss, lililowafuatilia wanajeshi wa msalaba waliokuwa wakijaribu kukimbia, na nyara nyingi ziliangukia katika mikono ya washindi, matokeo yake, vita, badala ya kuwaacha maskini, iliwatajirisha Wabohemia.

Miaka michache iliyofuata, chini ya papa mpya, tena vita nyingine ya msalaba ilitangazwa. Kama ilivyokuwa siku zilizotangulia, watu na mali vilikusanywa kutoka nchi zote za Ulaya zilizokuwa chini ya upapa. Vishawishi vilivyotolewa kwa watu ambao wangeweza kuingia katika shughuli hii ya hatari vilikuwa vikubwa sana. Msamaha kamili wa uhalifu mkubwa kabisa uliahidiwa kwa kila askari wa msalaba. Wote waliofia vitani waliahidiwa zawadi nono mbinguni, na waliotoka salama vitani waliahidiwa kuvuna heshima na utajiri katika uwanja wa vita. Jeshi kubwa lilikusanywa tena, na, wakifaulu kuvuka mpaka waliingia Bohemia. Majeshi ya wafausi wa Huss walirudi nyuma mbele yao, na kwa njia hiyo waliwavuta wavamizi ndani ya nchi zaidi, na kuwafanya waone kuwa tayari wameshapata ushindi.

Mwishoni jeshi la Procopius lilisimama, na likimgeukia adui, lilisonga mbele kupambana nao. Maaskari wa msalaba, sasa wakigundua kosa lao, walilala katika makambi yao wakisubiri mashambulizi yaanze. Wakati sauti ya majeshi yaliyokuwa yakisogea iliposikika, hata kabla wafuasi wa Huss hawajaonekana machoni pao, hofu iliwashika tena maaskari wa msalaba. Wakuu, majenerali, na maaskari wa kawaida, wakitupilia mbali silaha zao, walikimbia kuelekea pande zote. Bila mafanikio, mwakilishi wa papa, ambaye alikuwa kiongozi wa uvamizi, alijaribu kuyahamasisha majeshi yaliyokuwa yametishika na kusambaratika. Licha ya jitihada zake nyingi, yeye mwenyewe alijikuta amechukuliwa na mkondo wa maaskari waliokuwa wakikimbia kwa hofu. Walishindwa kabisa, na kwa mara nyingine tena nyara nyingi ziliangukia katika mikono ya washindi.

Hivyo kwa mara ya pili jeshi kubwa, lililotumwa na mataifa yenye nguvu kubwa kuliko yote huko Ulaya, jeshi la watu jasiri, wazoefu wa vita, waliofundishwa na wenye silaha zote za kivita, walikimbia bila kutumia silaha yote mbele ya walinzi wa nchi ambayo wakati huo ilikuwa dhaifu. Hapa kulikuweko udhihirisho wa nguvu ya Mungu. Wavamizi walipigwa kwa hofu inayopita nguvu za kibinadamu. Yeye aliyeyashinda majeshi ya Farao katika bahari ya Shamu, aliyeyakimbiza majeshi ya Midiani mbele ya Gideoni na watu wake mia tatu, ambaye

katika usiku moja aliwanyenyekesha majeshi ya Ashuru yenye kiburi, alikuwa amenyosha tena mkono Wake kukausha nguvu za mkandamizaji. “Hapo waliingiwa na hofu pasipokuwapo hofu, Maana Mungu ameitawanya mifupa yake aliyekuhusuru. Umewatia aibu, Kwa sababu MUNGU amewadharau” (Zaburi 53:5).

Viongozi wa upapa, baada ya kukata tamaa ya kushinda kwa kutumia nguvu, hatimaye walijielekeza katika kujenga mahusiano mema. Maafikiano yalifanywa, kuwa wakati wakidai kuwapa watu wa Bohemia uhuru wa dhamiri, kiuhalisia waliwasaliti na kuwaweka chini ya mamlaka ya Roma. Wabohemia walikuwa wameweka masharti manne ya amani na Roma: uhuru wa kuhubiri Biblia; haki ya kanisa lote kushiriki mkate na divai wakati wa ushirika mtakatifu, na matumizi ya lugha ya nyumbani katika ibada; kuwaondoa kabisa viongozi wa kanisa katika majukumu na mamlaka zisizo za kidini; na, kukitokea uhalifu, mahakama za kiraia ziwe na mamlaka juu ya viongozi wa kidini na waumini wa kawaida. Mamlaka za kipapa hatimaye “ziliafiki kuwa vipengele vinne vya wafuasi wa Huss vikubaliwe, lakini waliweka sharti kuwa haki ya kuvifafanua vipengele hivyo, yaani, haki ya kuamua maana yake hasa, ibakie kuwa ya baraza—kwa maneno mengine, ibakie kwa papa na mfalme.”—Wylie, b. 3, ch. 18.

Kwa msingi huu mkataba uliandikwa, na Roma ilipata kwa ujanja na hila kile ambacho ilishindwa kupata kwa kutumia mapambano; kwa kuwa, kuweka tafsiri yake ya masharti ya wafuasi wa Huss, kama ilivyokuwa kwa Biblia, Roma ingeweza kupotosha maana yake ili kutekeleza makusudi yake. Kundi kubwa katika Bohemia, baada ya kuona kuwa walisaliti uhuru wao, hawakuweza kukubaliana na mkataba. Mipasuko na migawanyiko iliibuka, ikasababisha migogoro na umwagaji damu miongoni mwao. Katika migogoro hii Procopio alianguka, na uhuru wa Wabohemia uliondoka.

Sigismund, msaliti wa Huss na Jerome, sasa akawa mfalme wa Bohemia, na bila kujali kiapo chake cha kuunga mkono haki za Wabohemia, alisonga mbele kuimarisha upapa. Lakini alinufaika kidogo sana kwa kujiweka kwake chini ya mamlaka ya Roma. Kwa miaka ishirini ya maisha yake ilikuwa imejaa shughuli na hatari nyingi. Majeshi yake yalidhoofika na hazina zake zilikaushwa kwa mapambano yasiyokuwa na faida na ya muda mrefu; na sasa, baada ya kutawala kwa mwaka mmoja, alikufa, akiuacha ufalme wake kwenye ukingo wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, na akirithisha kwa vizazi vilivyofuata jina linaloaibisha.

Mizozo, migogoro, na umwagaji damu viliendelea. Kwa mara nyingine tena majeshi ya kigeni yaliivamia Bohemia, na migawanyiko ya ndani iliendelea kulitafuna taifa. Wale waliobaki wakiwa waaminifu kwa injili walijikuta wakiteswa na kuuawa.

Kama ndugu zao wa awali, kuingia mkataba na Roma, walikumbatia makosa yake, wale walioshikilia imani ya zamani walijiunga pamoja na kuwa kanisa kamili linalojitegemea, wakijiita “Umoja wa Ndugu.” Tendo hili lilivuta laana kutoka kwa makundi yote ya watu.

Lakini uimara wao haukuyumbishwa. Walipolazimishwa kujificha katika misitu na mapango, bado waliendelea kukusanyika kusoma neno la Mungu na kumwabudu Mungu.

Kwa njia ya wajumbe waliotumwa kwa siri katika nchi mbalimbali, waligundua kuwa hapa na pale kulikuwa na "wafuasi wa ukweli waliotawanyika huko huko, wachache katika mji huu na wengine katika mji ule, walengwa, kama wao, wa mateso; na kwamba katikati ya milima ya Alps lilikuwepo kanisa la zamani, likiwa limejengwa juu ya misingi ya Maandiko, na wakipinga ufisadi wa ibada ya sanamu za Roma."—Wylie, b. 3, ch. 19. Kundi hili lilipokelewa kwa furaha kubwa, na mawasiliano yalianzishwa na Wakristo wa Kiwaldensia.

Wakiwa waaminifu kwa injili, Wabohemia walikesha kucha katika usiku wa mateso, katika saa ya giza wakiwa bado wanatazama hadi upeo wa macho yao kama vile watu wanavyoisubiri asubuhi. "Sehemu yao iliamriwa siku za uovu, lakini ... waliyakumbuka maneno yaliyosemwa kwanza na Huss, na kurudiwa na Jerome, kuwa karne ingepita kabla mapambazuko. Haya maneno yalikuwa kwa Watabori [wafuasi wa Huss] kama maneno ya Yusufu yalivyokuwa kwa makabila katika nyumba ya utumwa: 'Mimi ninakufa, na Mungu hakika atawajia, na kuwatoa.'"—Ibid., b. 3, ch. 19.

"Kipindi cha mwisho wa karne ya kumi na tano kilishuhudia ongezeko la pole pole lakini la hakika la makanisa ya Umoja wa Ndugu. Japokuwa siyo kweli kuwa halikushambuliwa, lakini kwa sehemu kubwa walikuwa na utulivu. Mwanzoni mwa karne ya kumi na sita makanisa yao yalikuwa mia mbili katika nchi ya Bohemia na Moravia."—Ezra Hall Gillett, Life and Times of John Huss, vol. 2, uk. 570. "Hivyo ndivyo walivyokuwa watu wema waliosalia ambao, kwa kuepuka maangamizi ya ukali wa moto na upanga, waliruhusiwa kuona mapambazuko ya siku iliyotabiriwa na Huss."—Wylie, b. 3, ch. 19.

Sura ya 7 - Utengano Mkubwa

Miongoni mwa wale walioitwa kuliongoza kanisa kutoka katika giza la upapa na kulipeleka katika nuru ya imani safi, aliyekuwa maarufu zaidi kuliko wote alikuwa Martin Luther. Akiwa mwenye, juhudi, umakini, na uaminifu, asiyeogopa kitu cho chote isipokuwa Mungu, na asiyetambua msingi mwingine wa imani ya kidini isipokuwa Maandiko Matakatifu, Luther alikuwa mtu maalumu kwa wakati wake; kupitia kwake Mungu alitimiza kazi kubwa ya matengenezo ya kanisa na kutoa mwangaza kwa ulimwengu.

Kama walivyokuwa wajumbe wa awali wa injili, Luther alizaliwa katika mazingira ya kimaskini. Miaka yake ya awali ilitumika akiishi katika nyumba ya kimaskini ya mkulima wa Kijerumani. Kwa kutoa jasho kila siku kama mfanya kazi katika mgodi wa baba yake alipata pesa kwa ajili ya elimu yake. Alidhamiria awe mwanasheria; lakini Mungu alikusudia kumfanya awe mjenzi wa hekalu kuu lililokuwa likiinuka pole pole katika karne zote. Ugumu, kujinyima, na nidhamu kali vilikuwa shule ambayo Hekima ya Milele ilimwandaa Luther kwa ajili ya utume muhimu wa maisha yake.

Baba yake Luther alikuwa mtu mwenye akili sana na utendaji na msukumo mkubwa wa tabia, mwaminifu, mwenye msimamo, na mnyoofu. Alisimamia kile alichokiamini kuwa ni wajibu wake, bila kujali kile ambacho kingetokea. Nia yake njema ilimwongoza kutilia mashaka mfumo wa kitawa. Alichukizwa sana wakati Luther alipoingia, bila ridhaa yake, nyumba ya watawa; na ilichukua miaka miwili kabla baba yake hajapatanishwa na mwanawe, na hata hivyo maoni yake yalibaki vile vile.

Wazazi wa Luther waliwekeza kwa umakini mkubwa katika elimu na mafunzo ya watoto wao. Walijitahidi sana kuwafundisha neno la Mungu na kanuni njema za maisha ya Kikristo. Ombi la baba daima lilitolewa huku mwanae akisikia kwamba mtoto akumbuke jina la Bwana na siku moja asaidie katika kuendeleza ukweli Wake. Kila fursa kwa ajili ya makuzi ya kimaadili na kiakili ambayo maisha yao ya kimaskini yalimudu kuwapatia ilitumiwa vizuri kwa furaha na wazazi hawa. Juhudi zao zilikuwa za dhati na zilizojali kuwaandaa watoto wao kwa ajili ya maisha yanayomcha Mungu na yenye manufaa maishani. Kwa uimara na nguvu ya tabia yao walitumia ukali mwingi kupita kiasi; lakini Mwanamatengenzo mwenyewe, japokuwa alifahamu kuwa walikosea, aliiona nidhamu yao kuwa ni ya kusifiwa zaidi kuliko kulaumiwa.

Shuleni, ambakoalipelekwaakiwabadonaumrimdogo, Lutheralitendewa kwa ukali na hata ukatili. Umaskini wa wazazi wake ulikuwa mkubwa kiasi kwamba alipokwenda shule iliyokuwa katika mji mwingine alilazimika kwa muda fulani kupata chakula kwa kuimba nyimbo kutoka mlango mmoja hadi mwingine, na mara kwa mara aliteseka kwa njaa. Mawazo dhaifu, ya kishirikina ya dini yaliyokuwepo wakati ule yalimjaza hofu. Mara kwa mara alilala usiku akiwa na moyo uliojazwa huzuni, akitazamia wakati ujao wenye giza huku akitetemeka

na akiwa katika hofu ya kudumu inayotokana na wazo kuwa Mungu ni mkali, jaji asiyekuwa na huruma, na jitu katili, badala ya Baba wa mbinguni aliye mwema.

Lakini chini ya mambo mengi na makubwa yanayokatisha tamaa Luther alisonga mbele kwa nguvu zaidi kuelekea kiwango cha juu cha ubora wa uadilifu na akili kilichovuta roho yake. Alikuwa na kiu kubwa ya maarifa, na tabia ya dhati na utendaji ya kitabia ya akili yake ilimwongoza kutamani kitu thabiti na chenye kina.

Akiwa na umri wa miaka kumi na minane, alijiunga na Chuo Kikuu cha Erfurt, hali yake ilikuwa nzuri zaidi na mustakabali wake ulikuwa na matumaini makubwa kuliko katika miaka yake ya mwanzoni. Wazazi wake kwa mikono yao hodari ya kazi walipata uwezo mkubwa, waliweza kumpa msaada wote aliohitaji. Na mvuto wa marafiki wenye busara kwa kiasi fulani ulipunguza madhara ya uzoefu wake wa awali. Alisoma sana vitabu vya waandishi wazuri, akihifadhi kwa bidii mawazo yao muhimu na kufanya hekima ya watu wenye busara kuwa yake. Hata chini ya nidhamu kali ya wakufunzi wa awali tangu mwanzo alionesha dalili ya uwezo mkubwa, na chini ya mivuto mizuri akili yake ilikua haraka. Akili inayoshika, yenye tafakari kubwa, nguvu kubwa ya hoja, na matumizi yasiyochoka mara moja vilimfanya kuwa katika nafasi ya mbele miongoni mwa wenzake. Nidhamu ya kiakili ilikomaza uelewa wake na iliamsha utendaji wa akili na umakini wa ufahamu uliokuwa unamwandaa kwa ajili ya migogoro ya maisha yake.

Hofu ya Mungu ilikaa ndani ya moyo wa Luther, ikimwezesha kudumisha uimara wake wa kusudi na kumwongoza kuwa na unyenyekevu mbele ya Mungu. Alikuwa na hitaji la kudumu la kutegemea msaada wa Mungu, na hakushindwa kuanza kila siku kwa maombi, wakati moyo wake ulikuwa daima ukipumua ombi kwa ajili ya mwongozo na msaada. “Kuomba vizuri,” alisema daima, “ni sehemu kubwa ya mafunzo.”—D’Aubigne, b. 2, ch. 2.

Siku moja, wakati akisoma-soma vitabu katika maktaba ya chuo kikuu, Luther aligundua Biblia ya Kilatini. Kitabu kama hicho alikuwa hajakiona kabla. Alikuwa hata hajui kuwa kuna kitabu kama hicho. Alikuwa amesikia sehemu za Injili na Nyaraka, ambazo zilikuwa zimesomwa katika mikutano ya ibada za hadhara, na alidhani kuwa hizo ndizo zilikuwa Biblia yote. Sasa, kwa mara ya kwanza, aliliona Neno lote la Mungu. Akiwa na mchanganyiko wa kicho na mshangao alifungua kurasa zake; wakati mapigo ya moyo yakiongezeka kasi na huku akiwa anatetemeka, yeye mwenyewe alijisomea maneno ya uzima, akipumzika mara kwa mara na kutamka kwa mshangao: “Yaani Mungu anaweza kunipatia kitabu hiki!”—Ibid., b. 2, Sura ya 2.

Malaika wa mbinguni walikuwa kando yake, na miale ya nuru kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu ilimfunulia hazina ya ukweli ili aweze kuelewa. Daima siku zote alikuwa mwoga wa kumkosea Mungu, lakini sasa usadikisho wa kina kuwa yeye ni mwenye dhambi ulimshika zaidi kuliko wakati wowote uliopita. Shauku ya dhati ya kuondokana na dhambi na kupata

amani mbele za Mungu vilimwongoza kujiunga na nyumba ya watawa na kujiweka wakfu kwa ajili ya maisha ya utawa. Alitakiwa kufanya kazi za chini kabisa na kuwa omba omba nyumba kwa nyumba. Alikuwa katika umri ambao kwa kawaida heshima na kutambuliwa ndipo huhitajiwa sana, na kazi hizi dhalili zilimuaibisha sana kulingana na hisia zake; lakini kwa uvumilivu mkubwa alistahimili sana kunyenyekeshwa huko, akiamini kuwa ilikuwa lazima kwa sababu ya dhambi zake.

Kila wakati alioweza kuupata baada ya kazi zake za kila siku aliutumia kusoma, akijinyima usingizi na akisikitika hata kwa muda alioutumia kula chakula chake kidogo sana. Kuliko vyote, Luther alifurahia kusoma neno la Mungu. Alikuwa ameona Biblia iliyokuwa imefungwa kwa mnyororo kwenye ukuta wa nyumba ya watawa, na alipenda kukaa hapo mara nyingi. Kwa kadiri alivyozidi kushawishika kuwa yeye ni mwenye dhambi, alizidi kutafuta kwa njia ya matendo yake mwenyewe kupata msamaha na amani. Aliishi maisha ya kujitesa sana, akijitahidi kwa kufunga, kukesha, na vipigo kudhibiti maovu katika silika yake, ambayo maisha ya utawa yalishindwa kumsaidia kuachana nayo. Hakusita kutoa kafara yo yote ambayo kwayo angeweza kupata usafi wa moyo ambao ungemwezesha kupata kibali mbele ya Mungu. "Hakika nilikuwa mtawa kamili," alikuja kusema baadaye, "na nilifuata kanuni za maisha ya kitawa kikamilifu kuliko ninavyoweza kueleza. Ikiwa mtawa angeweza kupata mbingu kwa kazi za kitawa, hakika nilipaswa kuistahili. Ikiwa ningeendelea zaidi, ningejitesa hadi kufa."— Ibid., b. 2, sura 3.

Kama matokeo ya udhibiti huu wenye maumivu makali aliishiwa nguvu na nyakati zingine alizimia, ambapo madhara yake hayakwisha kabisa katika maisha yake yote. Lakini pamoja na juhudi zake zote roho yake yenye mizigo haikupata nafuu yo yote. Hatimaye alifikia karibu kukata tamaa.

Ilipoonekana kana kwamba mambo yote yalikuwa yameharibika, Mungu alimwinua rafiki na msaidizi kwa ajili yake. Mtu mwadilifu Staupitz alimfunulia Luther na alimwagiza aache kujiangalia, aache kutafakari juu ya adhabu ya milele kwa kuvunja sheria ya Mungu, na amwangalie Yesu, Mwokozi anayesamehe dhambi zake. "Badala ya kujitesa mwenyewe kwa ajili ya dhambi zako, jitupe katika mikono ya Mkombozi. Mtegemee Yeye, tegemea haki ya maisha Yake, tegemea upatanisho wa kifo Chake Msikilize Mwana wa Mungu. Alifanyika mtu ili akupatie uhakika wa upendeleo wa Kimungu." "Mpende Yeye aliyekupenda kwanza."—Ibid., b. 2, ch. 4.

Hivyo ndivyo alivyosema huyu mjumbe wa rehema. Maneno yake yaligusa sana akili ya Luther. Baada ya mapambano mengi dhidi ya makosa yaliyojengeka kwa muda mrefu, aliwezeshwa kuushika ukweli, na amani ikaja katika roho yake iliyokuwa ikisumbuka.

Luther aliwekewa mikono ya upadiri na aliitwa atoke katika makazi ya watawa ili awe profesa katika Chuo Kikuu cha Wittenberg. Hapa alitumia muda mwingi kujifunza Maandiko

katika lugha za asili. Alianza kutoa mihadhara juu ya Biblia; na kitabu cha Zaburi, Injili, na Nyaraka zilifunguliwa na kufafanuliwa kwa makundi ya wasikilizaji wenye kiu na furaha ya kusikiliza. Staupitz, rafiki yake na mkubwa wake, alimsihi sana apande mimbarani ili ahubiri neno la Mungu. Luther alisita-sita, akijihisi kutostahili kuzungumza na watu kwa niaba ya Kristo. Ilikuwa baada ya pambano refu ndipo alipokubali ushawishi wa rafiki zake. Tayari alikuwa ameshakuwa hodari katika Maandiko, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake. Ufasaha wake uliwateka wasikilizaji wake, uwazi na uwezo ambao uliandamana na mawasilisho yake ya ukweli ulishawishi uelewa wao, na umakini wake uligusa mioyo yao.

Luther alikuwa bado mtoto halisi wa kanisa la upapa na hakuwa na wazo lolote kuwa angebadilika cho chote na kuwa mtu mwingine. Kwa uongozi wa Mungu alikwenda kutembelea Roma. Alienda safari hiyo kwa mguu, akiwa analala katika nyumba za watawa njiani. Katika nyumba moja ya watawa huko Italia alishangazwa kwa utajiri, fahari, na anasa alivyovishuhudia. Wakiwa na kipato cha juu, watawa waliishi katika nyumba za kifahari, wakivaa majoho ya kitajiri na yenye gharama kubwa, na walikula katika meza zilizojaa vyakula vya kila aina. Kwa uchungu mkubwa Luther alilinganisha mandhari hii na ile ya maisha yake ya kujikana nafsi na ugumu wa maisha yake. Akili yake ilianza kuingiwa na mashaka.

Hatimaye aliona kwa mbali mji wenye vilima saba. Kwa hisia kubwa alianguka na kulala kifudifudi juu ya ardhi, akitamka kwa nguvu: “Mji Mtakatifu wa Roma, ninakusalimia!”—Ibid., b. 2, ch. 6. Aliingia mjini, alitembelea makanisa, alisikiliza maelezo ya ajabu yaliyotolewa na makasisi na watawa kwa kurudia-rudia, na alitekeleza kaida zote zilizotakiwa. Kila mahali aliona mandhari zilizomshangaza na kumjaza hofu. Aliona kuwa uovu ulijaa miongoni mwa matabaka yote ya viongozi wa kanisa. Alisikia mizaha michafu kutoka kwa maaskofu, na alijawa hofu kwa kuona kufuru zao za ajabu, hata katika misa. Alipojichanganya na watawa na wakazi alikutana na ubadhirifu na ufisadi. Kila mahali alipokwenda, iwe katika maeneo matakatifu alikutana na kufuru.“Hakuna awezaye kufikiria,”aliandika,“dhambi na mambo machafu yanayotendwa Roma; inapaswa yaonwe na yasikiwe ili yaaminiwe. Hivyo wamejenga tabia ambayo inaendana na msemo kuwa, ‘Ikiwa kuna jehanamu, Roma imejengwa juu yake: ni shimo ambalo linatapika kila aina ya dhambi.’”—Ibid., b. 2, ch. 6.

Kutokana na amri iliyokuwa imetolewa karibuni cheti cha msamaha kilikuwa kimeahidiwa na papa kwa watu wote ambao wangeweza kupanda kwa magoti yao “Ngazi ya Pilato,” iliyosemwa kuwa Mwokozi wetu alitelemkia alipotoka katika ukumbi wa mahakama ya Kirumi na kuwa ngazi hiyo ilihamishwa kimiujiza kutoka Yerusalemu hadi Roma. Siku moja Luther kwa kicho cha dhati alikuwa akipanda ngazi hii, ambapo kwa ghafla sauti kama radi ilimwambia: “Mwenye haki ataishi kwa imani” (Warumi 1:17). Alisimama mara moja na kuondoka mahali pale kwa aibu na hofu. Kamwe, aya ile haikupoteza nguvu yake moyoni mwake. Tangu wakati ule alielewa wazi zaidi kuliko wakati wowote uliopita udanganyifu

uliomo katika kutumainia matendo ya kibinadamu kwa ajili ya wokovu, na umuhimu wa imani ya kudumu katika rehema za Kristo. Macho yake yalifunguliwa, na yasingeweza kufungwa tena, yasibaini udanganyifu wa upapa. Alipogeuza uso wake kutoka Roma alikuwa amegeuza moyo wake pia kutoka Roma, na tangu wakati huo kujitenga kwake kulizidi kuwa kukubwa, hadi alipokata kabisa mshikamano wake na kanisa la kipapa.

Baada ya kurudi kwake kutoka Roma, Luther alipokea kutoka Chuo Kikuu cha Wittenberg shahada ya uzamivu ya eliungu. Sasa alikuwa na uhuru wa kutumia muda wake mwingi, kuliko alivyoweza kufanya kabla ya hapo, kusoma Maandiko aliyoyapenda. Alikuwa ameapa kujifunza kwa uangalifu na kuhubiri kwa uaminifu neno la Mungu, siyo matamko na mafundisho ya mapapa, siku zote za maisha yake. Hakuwa tena mtawa au profesa tu, bali mjumbe wa Biblia mwenye mamlaka. Aliitwa kuwa mchungaji wa kuwalisha kondoo wa Mungu, ambao walikuwa na njaa na kiu kwa ajili ya ukweli. Alieleza kwa mkazo kuwa Wakristo hawapaswi kupokea mafundisho mengine zaidi ya yale yaliyojengwa juu ya mamlaka ya Maandiko Matakatifu. Maneno haya yaligonga kwenye msingi wa ukuu wa upapa. Yalikuwa na kanuni kuu za Matengenezo.

Luther aliona hatari ya kuinua nadharia za kibinadamu juu ya neno la Mungu. Bila hofu alishambulia mafundisho ya uongo wa wasomi na alipinga falsafa na theolojia ambayo kwa muda mrefu ilikuwa na mvuto mkubwa juu ya watu. Aliyapinga mafundisho ambayo siyo tu kuwa hayakuwa na faida yo yote bali pia yalikuwa maovu, na alitafuta kugeuza akili za wasikilizaji wake kutoka kwa mafundisho ya uongo ya wanafalsafa na wanatheolojia na kuzielekeza kwa ukweli uliofundishwa na manabii na mitume.

Ujumbe alioupeleka kwa makundi ya watu waliokuwa na shauku ya kusikiliza maneno yake ulikuwa wa thamani. Kabla ya hapo mafundisho kama hayo hayakuwahi kuingia katika masikio yao. Habari njema ya upendo wa Mwokozi, uhakika wa msamaha na amani kwa njia ya damu Yake ya upatanisho, vilifurahisha mioyo yao na vilihamasisha ndani yao tumaini la kudumu. Pale katika Chuo Kikuu cha Wittenberg nuru ilikuwa imewashwa ambayo miale yake ilikuwa inaenda kuenea mpaka sehemu za mwisho za dunia, na ambayo ilikuwa inaenda kuongezeka katika mwangaza wake hadi mwisho wa wakati.

Lakini nuru na giza haviwezi kupatana. Kati ya ukweli na makosa kuna mgogoro usiosuluhishika. Kuinua na kutetea kimojawapo ni kushambulia na kushinda kingine. Mkombozi wetu Mwenyewe alitangaza: “Sikuja kuleta amani, bali upanga” (Mathayo 10:34). Alisema Luther, miaka michache baada ya kuanzisha Matengenezo: “Mungu haniongozi, ananisukuma kwenda mbele. Ananibeba na kunipeleka mbele. Mimi siyo mtawala wa nafsi yangu. Ninatamani kuishi kwa amani; lakini nimetupwa katikati ya misukosuko na mapinduzi.”—D’Aubigne, b. 5, ch. 2. Alikuwa sasa karibu kuingizwa katika mashindano.

Kanisa la Rumi lilifanyia biashara neema ya Mungu. Meza za wabadilishao fedha (Mathayo 21:12) zilipangwa kando ya madhabahu zake, na hewa ilijazwa makelele ya wanunuzi na wauzaji. Kwa kisingizio cha kukusanya fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kanisa la Mtakatifu Petro kule Roma, vyeti vya msamaha wa dhambi viliuzwa hadharani na mamlaka ya papa. Kwa gharama ya uhalifu hekalu lilipaswa lijengwe kwa ajili ya kumwabudu Mungu—jiwe kuu la pembeni liliwekwa kwa njia ya uovu! Lakini njia zile zile zilizotumiwa kwa ajili ya utukufu wa Roma zilichochea pigo dhidi ya nguvu na ukuu wake. Ni jambo hili hili ndilo lililochochea azimio na mafanikio ya maadui wa upapa, na ndilo lililosababisha vita iliyotikisa kiti cha enzi cha upapa na kukumba taji ya ngazi tatu juu ya kichwa cha papa.

Afisa aliyeteuliwa kuuza vyeti vya msamaha katika nchi ya Ujermani— Tetzel kwa jina—alikuwa ametiwa hatiani kwa uhalifu dhalili kabisa dhidi ya jamii na kinyume na sheria ya Mungu; lakini baada ya kuponyoka kwenye adhabu kwa ajili ya uhalifu wake, alitumiwa kuendeleza zaidi miradi ya umamluki na ufisadi ya papa. Bila chembe ya aibu alisema kwa kurudia-rudia uongo mkubwa wa wazi na kusema maneno ya kuwadanganya wajinga, wasiojua kitu, na washirikina. Wangekuwa na neno la Mungu mioyoni mwao wasingedanganywa kwa njia hiyo. Ilikuwa ni kwa kusudi la kuwaweka daima chini ya utawala wa upapa, ili kulimbikiza madaraka na mali za viongozi wake wenye tamaa, ndiyo maana Biblia ilifichwa wasiweze kuiona. (Tazama John C. L. Gieseler, A Compendium of Ecclesiastical History, per. 4, sec. 1, par. 5.)

Wakati Twetzel alipoingia mji fulani, mjumbe alimtangulia, na kutangaza: "Neema ya Mungu na ya baba mtakatifu iko malangoni mwako."—D'Aubigne, b. 3, ch. 1. Na watu walimkaribisha msanii mwenye makufuru kana kwamba alikuwa Mungu Mwenyewe ambaye ameshuka kutoka mbainguni. Biashara haramu iliwekwa ndani ya kanisa, na Tetzel, akiwa madhabahuni, alisifia vyeti vya msamaha kuwa ndiyo zawadi ya thamani kutoka kwa Mungu kuliko zawadi zingine zote. Alitangaza kuwa kwa njia ya vyeti vyake vya msamaha dhambi zote ambazo mnunuzi wa vyeti angeweza baadaye kutamani kuzitenda angesamehewa, na kwamba "hata msamaha usingekuwa muhimu."—Ibid., b. 3, ch. 1.

Zaidi ya hapo, aliwahakikishia wasikilizaji wake kuwa vyeti vya msamaha vilikuwa na nguvu ya kuokoa siyo tu walio hai bali pia waliokufa; kwamba muda huo huo ambao fedha ingegusa sakafu ya sanduku lake, roho ambayo fedha ilikuwa imetolewa kwa ajili yake ingetoka mara moja katika purgatori na kuingia mbinguni. (Tazama K. R. Hagenbach, History of the Reformation, vol. 1, uk. 96.)

Wakati Simoni Magusi alipotaka kununua nguvu ya kutenda miujiza kutoka kwa mitume, Petro alimjibu: "Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali" (Matendo 8:20). Lakini biashara ya Tetzel ilikumbatiwa na maelfu ya watu kwa shauku kubwa. Dhahabu na fedha ilitiririka na kuingia katika hazina yake. Wokovu uliopatikana kwa kununuliwa kwa fedha ulipatikana kirahisi

zaidi kuliko wokovu unaohitaji toba, imani, na juhudi kubwa ya kupinga na kushinda dhambi. (Tazama maelezo katika Kiambatisho 59.)

Fundisho la msamaha wa dhambi kwa njia ya vyeti limekuwa likipingwa na wasomi na wacha Mungu katika Kanisa la Roma, na watu wengi wamekuwepo ambao hawaamini mambo ya kuigiza yaliyo kinyume kabisa na busara ya kawaida na Maandiko Matakatifu. Hakuna askofu ye yote aliyethubutu kuinua sauti yake dhidi ya biashara hii haramu; lakini akili za watu zilikuwa zikisumbuliwa na kutaabishwa, na wengi waliomba kwa dhati ili Mungu alitakase kanisa Lake kwa njia fulani.

Luther, japokuwa alikuwa bado ni muumini mwaminifu wa upapa, alijazwa na hofu kutokana na madai yenye kufuru ya wauzaji wa vyeti vya msamaha. Wengi wa waumini wa kanisa lake mwenyewe walikuwa wamenunua vyeti vya msamaha, na walianza kuja kwa mchungaji wao, wakiungama dhambi zao za aina mbalimbali, na walitarajia kutakaswa, siyo kwa sababu walikuwa wametubu na walitamani kufanya matengenezo, bali kwa msingi wa vyeti vya msamaha. Luther aliwanyima utakaso, na aliwaonya kuwa ikiwa hawatatubu na kutengeneza maisha yao, lazima wangeangamia katika dhambi zao. Kwa wasiwasi mkubwa walirudi kwa Tetzel wakiwa na malalamiko kuwa mwungamishaji wao alikataa vyeti vyake; na wengine kwa ujasiri walidai warudishiwe fedha yao. Mtawa alijazwa na ghadhabu. Alitamka maneno mazito ya laana ya kutisha, aliagiza moto uwashwe katika maeneo ya wazi, na alitangaza kuwa alikuwa "amepokea amri kutoka kwa papa kuwachoma moto wazushi wote waliojaribu kupinga vyeti vyake vya msamaha."—D'Aubigne, b. 3, ch. 4.

Luther sasa aliingia kwa ujasiri katika kazi yake kama shujaa wa ile kweli. Sauti yake ilisikika kutoka mimbarani ikitoa onyo kali na la dhati. Aliwaeleza watu uhalisia wa ubaya wa dhambi, na aliwafundisha kuwa haiwezekani mtu, kwa matendo yake mwenyewe, kupunguza hatia yake au kuepuka adhabu.

Hakuna cho chote bali toba kwa Mungu na imani katika Kristo kinachoweza kumwokoa mwenye dhambi. Neema ya Kristo haiwezi kununuliwa; ni zawadi inayotolewa bure. Aliwashauri watu wasinunue vyeti vya msamaha, bali wamtazame kwa imani Mkombozi aliyesulubiwa. Alisimulia uzoefu wake binafsi wa maumivu alivyojaribu kupata wokovu kwa kujidhili na kujitesa bila mafanikio, na aliwahakikishia wasikilizaji wake kuwa ilikuwa kwa njia ya kutokujiangalia mwenyewe na kumwamini Kristo ndivyo vilimpatia amani na furaha.

Kwa kadiri Tetzel alivyoendelea na biashara yake na maigizo yake machafu, Luther alidhamiria kuchukua hatua kubwa zaidi kupinga uonevu huu wa kutisha. Haikuchukua muda fursa ikajitokeza. Kanisa kuu la Wittenberg lilikuwa na mifupa mingi, ambayo katika siku fulani fulani takatifu ilioneshwa kwa watu, na msamaha kamili wa dhambi ulitolewa kwa wote waliotembelea kanisa lile na kuungama. Kwa hiyo katika siku hizo idadi kubwa ya watu walienda pale. Moja ya siku muhimu sana kama hizo, sikukuu ya Watakatifu Wote, ilikuwa

imekaribia. Siku moja kabla, Luther, akiungana na makundi makubwa ya watu waliokuwa wakienda kuelekea kwenye kanisa lile, alibandika kwenye mlango wake karatasi iliyoandikwa matamko tisini na tano dhidi ya fundisho la vyeti vya msamaha. Alitangaza utayari wake wa kutetea matamko haya siku iliyofuata pale katika chuo kikuu, dhidi ya watu wote ambao wangeona vema kuyashambulia.

Matamko yake yaliwavuta watu wote. Yalisomwa na kusomwa tena, na yalikaririwa na watu kila upande. Msisimko mkubwa uliibuka katika chuo kikuu na katika jiji zima. Kwa njia ya matamko hayo ilioneshwa kuwa mamlaka ya kutoa msamaha wa dhambi, na kufuta adhabu yake, haijawahi kutolewa kwa papa au kwa mwanadamu mwingine ye yote. Mpango mzima ulikuwa ni ulaghai mtupu,—ujanja wa kujipatia pesa kwa kucheza na imani za kishirikina za watu,—mbinu ya Shetani ya kuangamiza roho za wote wanaotumainia maigizo yake ya uongo. Ilioneshwa wazi pia kuwa injili ya Kristo ni hazina ya thamani ya kanisa, na kuwa neema ya Mungu, iliyofunuliwa ndani yake, imetolewa bure kwa wote wanaoitafuta kwa toba na imani.

Matamko ya Luther yaliamsha mjadala; lakini hakuna aliyethubutu kusema cho chote. Maswali aliyoyaibua siku chache yalienea katika nchi yote ya Ujerumani, na ndani ya wiki chache yalikuwa yamesikika katika ulimwengu wote wa Kikristo. Wafuasi wengi waaminifu wa Kanisa la Roma, waliokuwa wameona na kuomboleza kwa ajili ya uovu uliokuwemo kanisani, lakini hawakujua jinsi ya kuuzuia usiendelee, waliyasoma matamko kwa furaha kubwa, wakiitambua sauti ya Mungu ndani ya matamko hayo. Walihisi kuwa Bwana alikuwa amenyosha mkono Wake kuzuia wimbi lililokuwa likipanuka kwa kasi la ufisadi uliokuwa ukitokea katika ofisi ya upapa wa Roma. Wafalme na mahakimu walifurahia kwa siri kuwa udhibiti ulikuwa umekuja juu ya mamlaka yenye kiburi iliyokataa haki ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi yake. Lakini watu wengi waliopenda dhambi na ushirikina waliogopeshwa wakati imani za uongo zilizowafariji na kuwaondolea hofu zao zilipofagiliwa mbali kwa matamko ya Luther.

Makasisi wajanja, kwa kuingiliwa katika kazi yao ya kuhalalisha uhalifu, na kwa kuona kuwa mapato yao yalikuwa hatarini, walighadhibika sana, na walicharuka kutetea ulaghai wao. Mwanamatengenezo alikabiliana na washitaki wao. Baadhi walimshitaki kwa kwenda haraka na kufanya kazi kwa mihemko. Wengine walimshitaki kwa kiburi, wakidai kuwa hakuongozwa na Mungu, bali alifanya kazi kwa kiburi na majivuno. "Nani hajui," alijibu, "kuwa mtu mara chache hatoi mawazo mapya bila kuwa na mwonekano wa kiburi, na bila kushitakiwa kwa kuamsha migogoro? ... Kwa nini Kristo na wafia dini wote waliuawa? Kwa sababu walionekana kuwa wapinzani wenye kiburi dhidi ya hekima ya wakati wao, na kwa sababu walisimamia mawazo mapya bila kunyenyekea na kupata ushauri wa hekima na maoni ya wazee wa zamani." Alisema tena: "Chochote ninachokifanya kitafanyika, siyo kwa busara ya kibinadamu, bali kwa uongozi wa Mungu. Ikiwa kazi ni ya Mungu, ni nani ataisimamisha? Ikiwa siyo kazi Yake, ni nani anaweza kuiendeleza mbele?

Siyo mapenzi yangu, wala siyo mapenzi yao, wala mapenzi yetu; lakini mapenzi Yako, Ee Baba Mtakatifu, uliye mbinguni."—Ibid., b. 3, ch. 6.

Ingawa Luther aliongozwa na Roho wa Mungu kuanza kazi yake, asingeendelea nayo bila kukabiliana na migogoro mikubwa. Kejeli za maadui zake, tafsiri potofu za makusudi yake, na maelezo ya uchonganishi kuhusu tabia na nia yake, vilimwangukia kama mafuriko ya maji mengi; na mambo hayo yalikuwa na madhara. Alikuwa na ujasiri wa kuamini kuwa viongozi wa watu, katika kanisa na mashuleni, wangeungana naye kwa furaha katika juhudi za kufanya matengenezo. Maneno ya kutia moyo kutoka kwa watu waliokuwa katika nafasi za juu yalimtia moyo kwa furaha na kumpatia matumaini. Kwa matazamio tayari alikuwa ameona siku njema ikianza kupambazuka kwa ajili ya kanisa.

Lakini kutiwa moyo kulibadilika kukaja kukejeliwa na kulaumiwa. Waheshimiwa wengi, wa kanisa na dola, waliguswa na ukweli wa matamko haya; lakini wakagundua mara moja kuwa kukubali kweli hizi kungeleta mabadiliko makubwa. Kuwaeleza watu ukweli na kufanya matengenezo kungedhoofisha mamlaka ya Roma kwa kiasi kikubwa, na kungefunga maelfu ya mifereji iliyotiririshia maji yake katika hazina yake, na hivyo kukata kwa kiasi kikubwa ufujaji wa pesa na anasa za viongozi wa upapa. Zaidi ya hapo, kuwafundisha watu kufikiri na kutenda kama viumbe wanaowajibika, wakimwangalia Kristo pekee kwa ajili ya wokovu, wangepindua kiti cha enzi cha papa na hatimaye kuondoa mamlaka yao wenyewe. Kwa sababu hii walikataa ujumbe waliopewa kutoka kwa Mungu na wakajipanga dhidi ya Kristo na ukweli kwa upinzani wao dhidi ya mtu ambaye Mungu alimtuma kuwaangazia.

Luther alipojiangalia mwenyewe alitetemeka—mtu mmoja akisimama kinyume dhidi ya mamlaka kuu kabisa za ulimwengu. Nyakati zingine aliingiwa na mashaka ikiwa kweli aliongozwa na Mungu kusimama dhidi ya mamlaka ya kanisa. "Mimi nilikuwa nani," aliandika, "kupingana na mheshimiwa papa, ambaye... wafalme wa dunia na watu wote ulimwenguni kote walitetemeka mbele yake? ... Hakuna mtu hata mmoja awezaye kujua mateso ambayo moyo wangu uliyapata katika hii miaka miwili ya kwanza, na ninaweza kusema, ukataji tamaa, uvunjikaji moyo ulionipata."—Ibid., b. 3, ch. 6. Lakini hakuachwa akate tamaa kabisa. Wakati msaada wa kibinadamu ulipokosekana, alimwangalia Mungu pekee na alijifunza kuwa angeweza kutegemea kikamilifu na kuwa salama juu ya mkono wenye nguvu zote.

Kwa rafiki wa Matengenezo Luther aliandika: "Hatuwezi kuelewa Maandiko ama kwa kujifunza au kwa akili. Wajibu wako wa kwanza ni kuanza kwa maombi. Msihi Bwana akupatie, rehema zake kubwa, uelewa wa kweli wa neno Lake. Hakuna mfasiri mwingine wa neno la Mungu zaidi ya Mwasisi wa neno la Mungu, kama alivyosema Mwenyewe, 'Wote watafundishwa na Mungu.' Usitumainie kabisa kazi zako mwenyewe, kutoka kwa uelewa wako mwenyewe binafsi: mtumainie Mungu pekee, na katika mvuto wa Roho Mtakatifu.

Amini hili kwa sababu ya neno la mtu ambaye amewahi kupata uzoefu."—Ibid., b. 3, ch. 7. Hapa kuna somo muhimu sana kwa wale wanaohisi kuwa Mungu amewaita kuwapelekea wengine kweli muhimu kwa ajili ya wakati huu. Kweli hizi zitaamsha uadui wa Shetani na wa watu wanaopenda hadithi za uongo ambazo zimebuniwa na Shetani. Katika pambano dhidi ya nguvu za uovu kuna hitaji la jambo fulani muhimu kuliko nguvu za akili na hekima za kibinadamu.

Wakati adui walipotumainia desturi na mapokeo, au walipotegemea madai na mamlaka ya papa, Luther alikabiliana nao kwa kutumia Biblia na Biblia pekee. Hapa kulikuwa na maswali ambayo wasingeweza kuyajibu; kwa hiyo watumwa wa mazoea na ushirikina walitamani damu yake, kama Wayahudi walivyokuwa na kiu ya damu ya Kristo. "Ni mzushi,“ walipiga kelele wakereketwa wa Kanisa la Kiroma. "Ni uhaini dhidi ya kanisa kuruhusu mzushi wa kutisha kama huyu kuishi hata saa moja zaidi. Hebu jukwaa la kunyongea wahalifu lijengwe haraka kwa ajili yake!"—Ibid., b. 3, ch. 9. Lakini Luther hakuweza kuwa mhanga wa ghadhabu yao. Mungu alikuwa bado ana kazi ambayo alitaka Luther aifanye, na malaika wa mbinguni walitumwa kumlinda. Hata hivyo, wengi, ambao walikuwa wamepokea nuru ya thamani kutoka kwa Luther walifanywa kuwa lengo la ghadhabu ya Shetani na kwa ajili ya ukweli waliteswa na kuuawa.

Mafundisho ya Luther yalivuta usikivu wa akili zenye tafakari katika nchi yote ya Ujerumani. Kutoka katika mahubiri na machapisho yake miale ya nuru iliangazia na kuamsha maelfu ya watu. Imani hai ilikuwa inachukua nafasi ya mazoea mafu ambayo kanisa lilikuwa limeghubikwa ndani yake. Watu walikuwa wakipoteza imani katika ushirikina wa Uroma. Vizuizi vya chuki zisizokuwa na sababu vilikuwa vikiyeyuka. Neno la Mungu, ambalo kwalo Luther alipima kila fundisho na kila dai, lilikuwa kama upanga unaokata kuwili, likikata njia yake na kufikia mioyo ya watu. Kila mahali kulikuwepo maendeleo ya kiroho. Kila mahali kulikuwepo njaa na kiu ya haki kuliko ilivyowahi kutokea miaka mingi kabla ya hapo. Macho ya watu, ambayo kwa muda mrefu yalielekezwa kwa kaida za kibinadamu na wapatanishaji wa kidunia, walikuwa sasa wakigeukia toba na imani katika Kristo na Yeye aliyesulubiwa. Shauku hii kubwa iliyoenea sana iliamsha zaidi hofu za mamlaka za upapa. Luther alipokea wito wa mahakama ukimtaka aende Roma kujibu mashtaka ya uzushi. Wito huu ulijaza hofu mioyoni mwa marafiki zake. Walijua vizuri hatari iliyomkabili katika jiji lile la kifisadi, ambalo tayari lilikuwa limeshalewa damu ya mashahidi wa Yesu. Walipinga kwenda kwake Roma na kuomba ahojiwe akiwa nchini Ujerumani.

Mpango huu hatimaye ulitekelezwa, na mwakilishi wa papa aliteuliwa asikilize kesi hii. Katika maelekezo yaliyoletwa na papa kwa ofisa huyu, ilielezwa kuwa Luther alikuwa ameshatangazwa tayari kuwa mzushi. Hivyo basi, mwakilishi huyu alikuwa ameagizwa, "kumshitaki na kumzuia mara moja." Ikiwa angedumu kuwa na msimamo wake, na mwakilishi akishindwa kumkamata, alipewa mamlaka ya"kumpiga marufuku asionekane katika nchi yote ya Ujerumani; kumfukuza, kumlaani, na kuwafuta ushirika watu wote

walioshikamana naye."— Ibid., b. 4, ch. 2. Na, zaidi ya hapo, papa alimwelekeza mwakilishi wake, ili kung'oa kabisa ugonjwa wa uzushi, kuwafuta ushirika wa kanisa wote, hata kama wana hadhi kubwa kiasi gani katika kanisa au serikali, isipokuwa mfalme, watakaopuuza kumkamata Luther na wafuasi wake, na kuwapatiliza kisasi cha Roma.

Hapa pameoneshwa roho halisi ya upapa. Hakuna hata chembe ya kanuni ya Ukristo, au hata haki tu ya kawaida, haiwezi kuonekana katika waraka wote. Luther alikuwa umbali mkubwa kutoka Roma; hakuna na fursa ya kujieleza au kutetea msimamo wake; lakini kabla ya kesi yake kusikilizwa, alitangazwa kuwa mzushi moja kwa moja, na katika siku hiyo hiyo, alishauriwa, alishitakiwa, alihukumiwa, na alipewa adhabu; na haya yote yakifanywa na baba mtakatifu wa kujiweka mwenyewe, mamlaka iliyo kuu, isiyokosea katika kanisa au dola!

Wakati huu, Luther alipohitaji sana huruma na ushauri wa rafiki wa kweli, Mungu katika Majaliwa yake alimtuma Melanchthon aende Wittenberg.

Akiwa kijana kiumri, mpole na mtulivu, busara za Melanchthon, ujuzi wake mwingi, na umbuji usio na mshindani, vikichanganywa na usafi na uadilifu wa tabia yake, vilimfanya apate kibali na heshima machoni pa watu wote. Uwezo wa talanta zake haukuwa wa wazi sana zaidi ya uungwana na utu wake. Ghafla alitokea kuwa mwanafunzi mzuri wa injili, na rafiki mwaminifu na msaadizi wa Luther mwenye thamani kubwa; uungwana wake, tahadhari, na usahihi vikitumika kama nyongeza kwa ujasiri na nguvu ya Luther. Muungano wao katika kazi uliongeza nguvu katika Matengenezo na ilikuwa chanzo kikubwa cha hamasa kwa Luther.

Mji wa Augsburg ulikuwa umechaguliwa kuwa mahali pa mahakama, na Mwanamatengenezo alisafiri kwa miguu kwenda huko. Hofu kubwa ilijengeka kwa ajili yake. Vitisho vilikuwa vimetangazwa wazi wazi kuwa angekamatwa na kuuawa akiwa njiani, na marafiki zake walimwomba asiende huko. Hata walimsihi aondoke Wittenberg kwa muda na kutafuta hifadhi na wale ambao wangefurahia kumlinda. Lakini hakutaka kuondoka mahali ambapo Mungu alikuwa amemweka. Ilimpasa aendelee kudumisha kwa uaminifu ukweli, licha ya dhoruba zilizokuwa zikimpiga. Lugha yake ilikuwa: "Mimi ni kama Yeremia, mtu wa migogoro na malumbano; lakini vitisho vyao vinapoongezeka, ndivyo furaha yangu inavyoongezeka. Tayari wameshanivunjia heshima na kuniharibia sifa. Jambo moja tu limebaki; ni mwili wangu dhaifu: acheni tu wauchukue; kwa kufanya hivyo watafupisha maisha yangu kwa saa chache tu. Lakini kadiri roho yangu inavyohusika, hawawezi kuichukua kamwe. Yeyote anayetamani kutangaza neno la Mungu ulimwenguni, inampasa kutegemea kifo kila wakati."—Ibid., b. 4, ch. 4.

Habari za kufika kwa Luther jijini Augsburg kulimpa mwakilishi wa papa kuridhika kukubwa. Mzushi msumbufu aliyekuwa akiteka usikivu wa ulimwengu wote alionekana sasa kuwa katika mamlaka ya Roma, na mwakilishi wa papa aliazimia kuwa asiweze kuponyoka

kutoka katika mikono yake. Mwanamatengenezo hakuwa na cheti cha uhakika wa usalama wake. Marafiki zake walimsihi asiende mbele ya mwakilishi wa papa bila cheti cha uhakika wa usalama wake, na wao wenyewe walikusudia kuwa wamtafutie cheti hicho kutoka kwa mfalme. Mwakilishi wa papa alikusudia kumlazimisha Luther, ikiwezekana, akanushe mafundisho yake, la sivyo asipokanusha, afanye mpango wa kumpeleka Roma, akakutane na yaliyowakuta akina Huss na Jerome. Hivyo basi, kwa njia ya mawakala wake alijitahidi kumshawishi Luther aje kwake bila cheti maalumu cha uhakika wa usalama, akimwahidi kuwa hatamfanyia madhara yo yote. Mwanamatengenezo alikataa kufanya hivyo. Ni mpaka pale alipopata waraka uliomwahidi ulinzi wa mfalme, ndipo alipotokea mbele ya mwakilishi wa papa.

Kama suala la kisera, viongozi wa kanisa la Roma waliamua kujaribu kumshawishi Luther kwa mwonekano wa uungwana. Mwakilishi wa papa, katika mahojiano na Luther, alijifanya kuonesha urafiki mkubwa; lakini alidai kuwa Luther ajisalimishe kabisa kwa mamlaka ya kanisa, na asalimishe kila kipengele bila ubishi au swali. Hakuwa amejua kiwango cha tabia ya mtu aliyekuwa akishughulika naye. Luther, katika kujibu, alieleza heshima aliyokuwa nayo kwa hakika, shauku yake kwa ajili ya ukweli, utayari wake wa kujibu hoja zote zinazopingana na kile ambacho alikuwa amekifundisha, na kusalimisha mafundisho yake kwa uamuzi wa baadhi ya vyuo vikuu mashuhuri. Lakini wakati huo huo alipinga wazo la kadinali la kumtaka akanushe mafundisho yake bila kumwonesha makosa yake. Jibu pekee lilikuwa: "Kanusha, kanusha!" Mwanamatengenezo alisema kuwa msimamo wake ulikuwa umejengwa juu ya Maandiko na alieleza kwa mkazo kuwa asingeweza kukanusha ukweli. Mwakilishi wa papa, kwa kushindwa kujibu hoja za Luther, alimshambulia kwa dhoruba ya kejeli, mizaha, na sifa za uongo, na huku akiingiza dondoo kutoka katika mapokeo na misemo ya Mababa, bila kumpa Mwana matengenezo nafasi ya kusema. Baada ya kuona kuwa mkutano, kama ungeendelea vile, asingefanikiwa kusudi lake, hatimaye Luther alipata ruhusa ya kuwasilisha jibu lake kwa maandishi. "Kwa kufanya hivyo," alisema, akimwandikia rafiki yake, "wanaokandamizwa wanapata faida mbili; kwanza, kilichoandikwa kinaweza kuhukumiwa na wengine; na pili, mtu ana nafasi nzuri zaidi ya kushughulikia hofu, siyo katika dhamiri ya mtu katili mwenye kiburi na mpayukaji, anayeshinda kwa lugha yake ya kiimla."—Martyn, The Life and Times of Luther, kurasa 271, 272.

Katika mahojiano yaliyofuata, Luther aliwasilisha maelezo ya wazi, mafupi, na yenye nguvu ya maoni yake, yakiwa yamesheheni dondoo nyingi za Maandiko. Baada ya kulisoma kabrasha hilo kwa sauti, alimpatia kadinali, ambaye, hata hivyo, kwa dharau alilitupa pembeni, akisema kuwa lilijaa maneno ya upuuzi na dondoo zisizohusika. Luther, akiwa ameamshwa kikamilifu, sasa alimkabili kasisi mwenye kiburi pale pale—mapokeo na mafundisho ya kanisa—na kushinda madai yake yote.

Kadinali alipoona kuwa hoja za Luther haziwezi kujibiwa, alishindwa kujizuia kabisa, na kwa ghadhabu kubwa alipiga kelele: "Kanusha! Au nitakupeleka Roma, ili utokee mbele ya majaji waliotumwa wasikilize suala lako. Nitakuondoa katika ushirika wa kanisa na wafuasi wako wote, na wale wote ambao wakati wowote watakuona, na tutawatupa nje ya kanisa." Na mwishoni alitangaza, kwa sauti ya kiburi na hasira: "Kanusha, au usirudi tena."—D'Aubigne, London ed., b. 4, ch. 8.

Mwanamatengenezo na marafiki zake waliondoka, na kwa njia hiyo walitangaza wazi kuwa hakuna kukanusha ambako kungetegemewa kutoka kwake. Hili siyo jambo ambalo kadinali alikusudia. Alikuwa amejidanganya kuwa kwa kutumia ukatili angeweza kumfanya Luther ajisalimishe. Sasa, akiwa ameachwa peke yake na wasaidizi wake, alimwangalia mtu mmoja mmoja akiwa na hasira kali kutokana na kushindwa kwa hila zake ambako hakukutegemea.

Juhudi za Luther katika tukio hili hazikwenda bila matokeo mazuri. Umati mkubwa wa watu waliokuwepo pale walipata fursa ya kuwalinganisha watu hawa wawili, na kuamua wenyewe kuhusu roho iliyooneshwa na watu hao wawili, ikiwa ni pamoja na nguvu na ukweli wa nafasi zao. Tofauti kati yao ilikuwa kubwa sana! Mwanamatengenezo, sahili, mnyenyekevu, imara, alisimama katika nguvu ya Mungu, akiwa na ukweli kando yake; mwakilishi wa papa, mwenye majivuno, katili, mwenye kiburi, na asiyekuwa na busara, hakuwa na hoja hata moja kutoka katika Maandiko, lakini kwa hasira alipiga kelele akisema: "Kanusha, la sivyo upelekwe Roma uadhibiwe."

Pamoja na kuwa Luther alikuwa amepewa cheti cha hakikisho la usalama, viongozi wa kanisa la Roma walikuwa wakipanga kumkamata na kumweka gerezani. Marafiki zake walisisitiza kuwa ilikuwa siyo salama kuendelea kukaa kule, alipaswa kurudi Wittenberg bila kukawia, na kuwa tahadhari kubwa ingechukuliwa ili kuficha makusudi yake. Kwa kuzingatia hayo aliondoka Augsburg alfajiri, kwa punda, akiwa na mwongoza njia aliyepewa na hakimu. Kwa hofu kubwa aliondoka gizani akipita katika mitaa ya jiji iliyokuwa kimya. Maadui, wakiwa macho na katili, walikuwa wakipanga jinsi ya kumwangamiza. Je, angeweza kuepuka mitego iliyotegwa kwa ajili yake? Hizo zilikuwa nyakati za wasiwasi na maombi ya dhati.

Alifika kwenye lango dogo la ukuta wa jiji. Lilifunguliwa na mwongoza njia kwa ajili yake, na akiwa na mwongozaji wake aliweza kupita bila kikwazo. Walipofaulu kutoka salama, wakimbizi waliongeza kasi ya mwendo wao, na kabla mwakilishi wa papa hajajua kuwa Luther ameondoka, alikuwa ameshakwenda ng'ambo ya uwezekano wa kukamatwa na watesaji wake. Shetani na vibaraka wake walikuwa wameshindwa. Mtu ambaye walifikiri kuwa alikuwa katika uwezo wao alikuwa ameondoka, aliponyoka kama ndege anavyoponyoka kutoka katika mtego wa mtegaji.

Baada ya kupokea taarifa za kuondoka kwa Luther, mwakilishi wa papa alishangaa na kukasirika sana. Alitarajia kuwa angepata heshima kubwa kwa hekima yake na uimara wake katika kumshughulikia huyu msumbufu wa kanisa; lakini tumaini lake lilikuwa limepotea. Alionesha hasira yake katika barua aliyomwandikia Frederiko, aliyekuwa mtawala wa jimbo la Saxony, kwa uchungu akimshtumu Luther na akimwamuru Frederiko ampeleke Mwanamatengenezo Roma au afukuzwe Saxony.

Katika kujitetea, Luther alisihi kuwa mwakilishi wa papa amwoneshe makosa katika Maandiko, na aliapa kwa nguvu kuwa angekanusha mafundisho yake kama angeoneshwa mahali yanapopingana na neno la Mungu. Na alieleza shukurani zake kwa Mungu kuwa alistahili kuteswa kwa ajili ya kazi takatifu. Mtawala wa Saxony, mpaka wakati ule, alikuwa na ufahamu mdogo wa mafundisho ya Mwanamatengenezo, lakini aliguswa sana na uwazi, nguvu, na ufasaha wa maneno ya Luther; na mpaka Mwanamatengenezo aonekane kuwa na makosa, Frederiko aliamua kusimama kama mlinzi wa wake. Katika kujibu madai ya mwakilishi wa papa aliandika:

"Kwa kuwa Dkt. Martin amesimama mbele yake huko Augsburg, unapaswa kuridhika. Hatukutarajia ujaribu kumtaka akane mafundisho yake bila kwanza kumwonesha makosa yake. Hakuna mtu msomi katika eneo letu la utawala ambaye ameniambia kuwa mafundisho ya Martin ni maovu, yanapinga Ukristo, au yana uzushi.' Elekta wa Saxony alikataa pia kumpeleka Luther Roma, au kumfukuza kutoka katika majimbo yake."—D'Aubigne, b. 4, ch. 10.

Elekta aliona kuwa kulikuwa na uvunjifu wa jumla wa kanuni za kimaadili za jamii. Kazi kubwa ya matengenezo ilihitajika. Michakato tata na ya gharama ya kusimamia na kuadhibu uhalifu isingekuwa ya muhimu ikiwa watu wangeyatii matakwa ya Mungu na maagizo Yake kwa dhamiri iliyoangaziwa. Aliona kuwa Luther alikuwa akifanya kazi ili kutimiza lengo hili, na kwa siri alifurahia kuona kuwa mvuto bora zaidi ulikuwa ukijitokeza ndani ya kanisa. Aliona pia kuwa profesa katika chuo kikuu Luther alikuwa amefanikiwa sana. Mwaka mmoja pekee ulikuwa umepita tangu Mwanamatengenezo alipobandika matamko yake kwenye mlango wa kanisa, hata hivyo kulikuwa tayari na kupungua kukubwa kwa idadi ya mahujaji waliotembelea kanisa wakati wa siku kuu ya Watakatifu Wote. Roma ilikuwa imenyimwa waabuduji na sadaka, lakini mahali pake palijazwa na tabaka jingine, la watu waliokuja Wittenberg, siyo mahujaji waliokuja kuabudu mifupa yake, bali wanafunzi waliokuja kujaza kumbi zake za kujifunzia. Maandishi ya Luther yalikuwa yameasha shauku mpya katika Maandiko Matakatifu, na siyo tu kutoka sehemu zote za Ujerumani, bali pia kutoka katika nchi zingine, wanafunzi walifurika katika chuo kikuu. Vijana, walioliona jiji la Wittenberg kwa mara ya kwanza, "waliinua mikono yao mbinguni, na walimtukuza Mungu kwa kuwezesha nuru iangaze kutoka katika jiji lile, kama ilivyomulika kutoka Sayuni ya nyakati za kale, na kutokea hapo ilisambaa hadi nchi za mbali."— Ibid., b. 4, ch. 10.

Luther alikuwa bado ameongoka nusu kutoka katika makosa ya Uroma. Lakini alivyolinganisha Maandiko Matakatifu na amri na katiba za upapa, alijazwa na mshangao. “Ninasoma,” aliandika, “amri za mapapa, na ... sijui ikiwa papa ni mpinga Kristo mwenyewe, au mtume wake, kwa kuwa Kristo amewakilishwa vibaya na kusulubishwa sana ndani yao.”—Ibid., b. 5, ch. 1. Hata hivyo kwa wakati huo Luther alikuwa bado anaunga mkono Kanisa la Roma, na hakuwa na wazo lo lote kuwa angejitenga na ushirika wake.

Maandishi ya Mwanamatengenezo na mafundisho yake yalikuwa yakienea katika kila taifa la Kikristo. Kazi yake iliendelea katika nchi za Uswisi na Uholanzi. Nakala za maandishi yake zilifika Ufaransa na Uhispania. Katika nchi ya uingereza mafundisho yake yalipokelewa kama maneno ya uzima. Ukweli ulifika pia Ubeligiji na Italia. Maelfu ya watu waliamshwa kutoka katika usingizi wa kiroho na kuingizwa katika furaha na matumaini ya maisha ya imani.

Roma ilizidi kuudhiwa zaidi na zaidi kwa mashambulio ya Luther, na ilitangazwa na baadhi ya wapinzani wake wakereketwa, hata na baadhi ya wasomi katika vyuo vikuu vya Kikatoliki, kuwa ye yote ambaye angemwua huyo mtawa angekuwa hana dhambi. Siku moja mgeni, akiwa na bastola iliyofichwa katika joho lake, alimkaribia Mwanamatengenezo na kumwuliza kwa nini alitembea peke yake. “Niko katika mikono ya Mungu,” Luther alijibu. “Yeye ni nguvu na ngao yangu. Mwanadamu ataweza kunifanya nini?”— Ibid., b. 6, ch. 2. Alipoyasikia maneno hayo, mgeni alibadilika sura na kuwa mweupe na akakimbia kutoka mbele ya uwepo wa malaika wa mbinguni.

Roma ilikuwa imejielekeza kumwua Luther; lakini Mungu alikuwa ulinzi wake. Mafundisho yake yalisikika kila mahali—“katika nyumba za wananchi na katika nyumba za watawa, ... katika majumba ya wakuu, katika vyuo vikuu, na katika majumba ya wafalme;” na watu waungwana walikuwa wakitokea kila upande kuunga mkono juhudi zake.—Ibid., b. 6,ch. 2.

Ilikuwa karibu na wakati huu ambapo Luther, kwa kusoma maandishi ya Huss, aligundua kuwa ukweli mkuu wa kuhesabiwa haki kwa imani, ambao yeye mwenyewe alikuwa akiupigania na kuufundisha, ulikuwa ukiaminiwa na kufundishwa na Mwanamatengenezo wa Bohemia. “Sisi sote,” alisema Luther, “Paulo, Agustino, na mimi mwenyewe, tumekuwa wafuasi wa Huss bila kujua !” “Hakika Mungu atauwajibisha ulimwengu kwa ujumbe huu,” aliendelea kusema, “kwamba ukweli ulihubiriwa ulimwenguni karne moja iliyopita, na kuchomwa moto!”—Wylie, b. 6, ch. 1

Katika wito kwa mfalme na kwa wakuu wengine katika ufalme wa Ujerumani kwa niaba ya matengenezo ya Ukristo, Luther aliandika kuhusiana na upapa: “Ni jambo la kutisha kumwona mtu anayejiita mwenyewe mwakilishi wa Kristo, akionekana kuwa na utukufu ambao hakuna mfalme mwingine anayelingana naye. Je, huku ndiko sawa na Yesu maskini,

au Petro mnyenyekevu? Wanasema yeye ni bwana wa ulimwengu! Lakini Kristo, ambaye anadai kumwakilisha, alisema, 'Ufalme wangu si wa ulimwengu huu.' Je, eneo la utawala wa mwakilishi linazidi la mkubwa wake?"—D'Aubigne, b. 6, ch. 3.

Aliandika ifuatavyo kuhusu vyuo vikuu: "Ninaogopa kuwa vyuo vikuu vinaweza kuwa malango makuu ya jehanamu, visipofanya kazi kwa bidii kueleza Maandiko Matakatifu, na kuyaweka katika mioyo ya vijana. Ninashauri mtoto asipelekwe mahali ambapo Maandiko hayapewi kipaumbele. Kila taasisi ambapo watu hawajishughulishi daima kujifunza neno la Mungu lazima ufisadi utatawala."—Ibid., b. 6, ch. 3.

Wito huu ulisambazwa haraka katika nchi nzima ya Ujerumani na kuleta mvuto mkubwa kwa watu. Taifa zima lilitikiswa, na watu wengi waliamshwa na kuunga mkono bendera ya matengenezo. Wapinzani wa Luther, wakiwaka shauku ya kulipiza kisasi, walimsihi sana papa achukue hatua za haraza na kali dhidi yake. Iliamuriwa kuwa mafundisho yake yapigwe marufuku mara moja. Siku sitini zilitolewa kwa Mwanamatengenezo na wafuasi wake, ambapo baada ya siku hizo, ikiwa wasingekana mafundisho yake, wote wangeondolewa katika ushirika wa kanisa.

Hilo lilikuwa janga kwa Matengenezo. Kwa karne nyingi hukumu ya Roma ya kufutwa ushirika wa kanisa ilileta hofu kwa wafalme wenye nguvu; ilijaza uchungu na ukiwa katika himaya kuu ulimwenguni. Wale ambao walikumbwa na hukumu hiyo waliangaliwa na watu wote kwa hofu na simanzi; walikatazwa kuongea na marafiki zao na walichukuliwa kama watu waliolaaniwa, na walipaswa kuwindwa na kuuawa. Luther hakuwa kipofu wa kuona dhoruba iliyokuwa karibu kumpasukia; lakini alisimama imara, akimtegemea Kristo kama msaada na ngao yake. Akiwa na imani na ujasiri wa mfia dini aliandika:

"Kinachoenda kutokea sikijui, wala sihitaji kukijua. Acha kinachokuja kije, sina hofu kabisa. Hakuna hata jani linaloanguka chini bila mapenzi ya Baba yetu. Ni kwa kiasi gani basi Mungu anatujali! Ni jambo dogo sana kufa kwa ajili ya Neno, kwa kuwa Neno aliyefanyika mwili Mwenyewe alikufa. Tukifa Naye, tutaishi pamoja Naye; na tukipitia kile alichopitia kabla yetu, tutakuwa mahali alipo na kuishi Naye milele na milele."—Ibid., 3d London ed., Walther, 1840, b. 6, ch. 9.

Wakati barua ya papa ilipomfikia Luther, alisema: "Ninaidharau na kuishambulia, kwa kuwa ni barua ovu, ya uongo.... Ni Kristo Mwenyewe anayeshutumiwa nayo Ninafurahia kupata maumivu kama haya kwa kazi njema kuliko zote. Tayari ninahisi uhuru zaidi moyoni mwangu; kwa kuwa hatimaye nimejua kuwa papa ni mpinga Kristo, na kuwa kiti chake cha enzi ni cha Shetani mwenyewe."—D'Aubigne, b. 6, ch. 9.

Hata hivyo amri ya Roma haikupita bure—ilileta madhara. Gereza, mateso, na upanga zilikuwa silaha zilizotumiwa kushinikiza utii. Watu dhaifu na washirikina walitetemeka

mbele ya amri ya papa; na ingawa kulikuwa huruma kwa ajili ya Luther, wengi walihisi kuwa ilikuwa gharama kubwa mno kuhatarisha maisha katika vuguvugu la matengenezo. Kila kitu kilionesha kuwa kazi ya Mwanamatengenezo ilikuwa karibu kufungwa.

Lakini Luther hakuwa na hofu bado. Roma ilikuwa imemwaga laana zake dhidi yake, na ulimwengu uliangalia kinachoendelea, wakitarajia bila shaka kuwa atauawa au atalazimishwa kujisalimisha. Lakini kwa nguvu ya kutisha alirusha hukumu juu ya kanisa na kutangaza hadharani azimio lake la kuliacha kanisa milele. Akiwa mbele ya umati wa wanafunzi madaktari, na wakazi wa matabaka yote Luther aliichoma barua ya papa, iliyokuwa na sheria za kanisa, maagizo, na maandishi mengine yaliyohalalisha mamlaka ya upapa. "Maadui zangu wameweza, kwa kuchoma vitabu vyangu," alisema, "kudhuru kazi ya ukweli katika akili za watu wa kawaida, na kuangamiza roho zao; kwa sababu hiyo nimechoma vitabu vyao. Mgogoro mkubwa ulikuwa umeanza. Mpaka wakati huo nilikuwa nikishughulika na papa. Nilianza kazi hii katika jina la Mungu; itaisha bila mimi, na kwa nguvu zake."—Ibid., b. 6, ch. 10.

Luther alijibu shutuma za maadui zake ambapo walidai kuwa mwelekeo aliouchagua ulikuwa dhaifu, akisema: "Nani ajuaye ikiwa Mungu amenichagua na kuniita, na ikiwa hawapaswi kuliogopa hilo, kwa kunidhihaki, wanamdhihaki Mungu Mwenyewe? Musa alikuwa peke yake alipoondoka Misri; Eliya alikuwa peke yake katika utawala wa Mfalme Ahabu; Isaya peke yake katika mji wa Yerusalemu; Ezekieli pake yake Babeli. Mungu hakuchagua nabii aliyekuwa kuhani mkuu au mtu ye yote mwingine mwenye cheo cha juu; bali alichagua watu wa chini na waliodharauliwa, ikiwa ni pamoja na mchungaji Amosi. Katika kila zama, watakatifu wamewakosoa wakuu, wafalme, maliwali, makuhani, na watu wenye hekima, kwa kuhatarisha maisha yao Sisemi kuwa mimi ni nabii; lakini nasema kuwa inawapasa kuogopa hasa kwa sababu niko peke yangu na wao ni wengi. Ni hakika na jambo hili, kuwa neno la Mungu liko pamoja na mimi, na kwamba haliko pamoja nao."—Ibid., b. 6, ch. 10.

Hata hivyo siyo kweli kuwa Luther hakuwa na pambano kubwa ndani ya moyo wake wakatiLuther alipotoa uamuzi wake wa kujitenga na kanisa. Ilikuwa ni karibu na wakati huu ambapo aliandika: "Ninahisi zaidi na zaidi kila siku jinsi ilivyo vigumu kwa mtu kuacha uelewa ambao ameujenga tangu utotoni. Ee, ni maumivu makubwa kiasi gani niliyapata kutokana na uhalisia huo, ingawa nilikuwa na Maandiko kando yangu, kujiridhisha kuwa nilipaswa kuthubutu kusimama peke yangu kinyume na papa, na kumtangaza hadharani kuwa ni mpinga Kristo! Mateso ya moyo wangu yamekuwa makubwa kiasi gani! Mara ngapi nimejiuliza kwa uchungu maswali ambayo wafuasi wa upapa wamekuwa wakiniuliza mara nyingi: 'Wewe peke yako ndiye uliye na busara? Je, mtu mwingine ye yote anaweza kukosea? Je, itakuwaje, ikiwa, hata hivyo, ni wewe mwenyewe umekosea, na ambaye unawajumuisha wengine katika makosa yako, ambao wataangamia milele?' 'Ndivyo nilivyopigana na nafsi

yangu na Shetani, mpaka Kristo, kwa maneno Yake yasiyokosea, yalipoimarisha moyo wangu dhidi ya mashaka haya."—Martyn, kurasa 372, 373.

Papa alimtishia Luther kuwa atamfuta ushirika wa kanisa ikiwa asingekana, na tishio lilikuwa sasa limetekelezwa. Amri mpya ilitokea, ikitangaza hatua ya mwisho ya kutengwa kwa Mwanamatengenezo kutoka katika Kanisa la Roma, ikimhukumu kuwa mtu aliyelaaniwa na Mbingu, na ikiwajumuisha katika hukumu hiyo watu wote ambao wangepokea mafundisho yake. Pambano kuu lilikuwa limeingiwa kikamilifu.

Upinzani ni sehemu ya maisha ya wote ambao Mungu anawatumia kuwasilisha ukweli wa leo mahsusi unaofaa kwa ajili ya wakati wao. Kulikuwepo ukweli wa leo katika siku za Luther,—ukweli wenye umuhimu maalumu ambao kwa wakati huo; kuna ukweli wa leo kwa ajili ya kanisa leo. Ye yote anayefanya mambo kulingana na mashauri na mapenzi ya Mungu amependezwa kuwaweka watu chini ya mazingira ya aina mbalimbali na kuweka majukumu maalumu kwa nyakati walizoishi na mazingira ambayo wamewekwa. Ikiwa wangethamini nuru waliyopewa, mitazamo mipana zaidi ya ukweli ingefunguka mbele yao. Lakini siyo kweli kuwa watu wengi leo wanaupenda ukweli zaidi kuliko wafuasi wa upapa waliompinga Luther. Kuna mwelekeo ule ule wa kukubali nadharia na mapokeo ya watu badala ya neno la Mungu kama ilivyokuwa katika zama za kale. Wanaowakilisha ukweli kwa ajili ya wakati huu wasitegemee kupokelewa kwa furaha kubwa zaidi kuliko wanamatengenezo wa zama zilizopita. Pambano kuu kati ya ukweli na makosa, kati ya Kristo na Shetani, litazidi kuongezeka katika ukali wake hadi mwisho wa historia ya ulimwengu.

Yesu aliwaambia wanafunzi Wake: "Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia. Likumbukeni lile neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi; ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu" (Yohana 15:19, 20). Na kwa upande mwingine Bwana wetu alisema wazi: "Ole wenu ninyi watu wote watakapowasifu, kwa kuwa baba zao waliwatenda manabii wa uongo mambo kama hayo" (Luka 6:26). Roho ya kidunia haipatani na Roho ya Kristo leo kama ilivyokuwa nyakati za kale, na wale wanaohubiri neno la Mungu katika usafi wake hawawezi kupokelewa kirahisi zaidi sasa kuliko ilivyokwa nyakati zile. Miundo ya upinzani dhidi ya ukweli inaweza kubadilika, uadui unaweza usiwe wa wazi sana kwa sababu unaweza kuwa wa hila zaidi; lakini uhasama huo bado upo na utaendelea kuwepo mpaka mwisho wa wakati.

Sura ya 8 - Mbele ya Mahakama Kuu

Mfalme mpya, Charles V, alikuwa ndiyo tu amesimikwa rasmi katika kiti cha enzi cha Ujerumani, na wawakilishi wa Roma waliharakisha kumpelekea salamu zao za pongezi na kumshawishi mfalme atumie madaraka yake kukomesha Matengenezo. Kwa upande mwingine, elekta wa Saxony, ambaye kwa sehemu kubwa, alikuwa amechangia katika kumweka Charles madarakani, alimsihi asichukue hatua yo yote dhidi ya Luther bila kumpa nafasi ya kumsikiliza. Kwa sababu hiyo mfalme aliwekwa katika mtanziko na usumbufu mkubwa. Wawakilishi wa papa wasingeridhishwa na kitu cho chote pungufu ya amri ya kumhukumu kifo Luther. Elekta wa Saxony alikuwa ametangaza kwa nguvu kuwa "siyo ofisi ya mfalme mkuu wala mtu ye yote alikuwa ameonesha kuwa maandishi ya Luther yalikuwa yamekanushwa;" hivyo basi aliomba "kuwa Dkt. Luther apewe hakikisho la usalama, ili aweze kufika mbele ya mahakama ya majaji wasomi, wacha Mungu, na wasio na upendeleo."—D'Aubigne, b. 6, ch. 11.

Macho na masikio ya wahusika wote sasa yalielekezwa kwa mkutano wa viongozi wa majimbo ya Ujerumani ulioitishwa kukaa katika jiji la Worms mara tu baada ya Charles kutawazwa na kuwa mfalme ya dola ya Ujerumani. Kulikuwepo masuala na maslahi muhimu ya kisiasa yaliyokusudiwa kujadiliwa katika baraza lile kuu la kitaifa; kwa mara ya kwanza wakuu wa Ujerumani walikuwa wanakutana na mfalme wao kijana katika mkutano wa mashauriano. Kutoka katika nchi zote zilizoko chini ya Uroma walikuja viongozi wa kanisa na wa serikali. Viongozi wa serikali, watu wa vyeo vya juu, wenye mamlaka makubwa, wakiwa na wivu wa kutetea madaraka yao na nafasi zao za kurithishwa; viongozi wa juu wa kanisa, wakiwa na utambuzi wa ukuu wao na nguvu zao; viongozi wakuu wa mhimili wa mahakama na walinzi wao wenye silaha; na mabalozi kutoka nchi za kigeni na za mbali,- wote walikusanyika katika jiji la Worms. Pamoja na kusanyiko hilo kubwa, shauku yao kubwa ilikuwa juu ya kazi ya Mwanamatengenezo wa Saxony.

Awali, Charles alikuwa amemwagiza kiongozi wa Saxony amlete Luther mbele ya Baraza la Kitaifa, akimhakikishia ulinzi, na akiahidi mjadala huru, mbele ya watu wenye uwezo, juu ya masuala yanayobishaniwa. Luther alikuwa na shauku ya kufika mbele ya mfalme. Afya yake wakati huu ilikuwa dhaifu zaidi; hata hivyo alimwandikia kiongozi wa Saxony: "Ikiwa siwezi kwenda Worms nikiwa na afya njema, nitabebwa kwenda huko, nikiwa mgonjwa hivi hivi. Kwa kuwa ikiwa mfalme ameniita, siwezi kuwa na mashaka kuwa ni wito wa Mungu Mwenyewe. Ikiwa wana nia ya kunifanyia ukatili, na jambo hilo linawezekana kabisa (kwa kuwa siyo kwa maagizo yao wenyewe ambayo kwayo wananiamuru niende mbele yao), ninaweka jambo hilo mikononi mwa Bwana. Yeye bado Yu hai na bado anatawala, Yeye aliyehifadhi vijana watatu wasiungue katika tanuru la moto. Ikiwa hataniokoa, maisha yangu yana umuhimu mdogo sana. Hebu tusiruhusu injili kuaibishwa mbele ya watu waovu, na hebu tumwage damu yetu kwa ajili ya injili, ili tusitoe nafasi ya wao kushinda. Siyo juu yangu kuamua ikiwa maisha yangu au kifo changu

vitachangia zaidi katika wokovu wa wote Unaweza kutarajia yote kutoka kwangu… isipokuwa kukimbia na kukana. Kukimbia siwezi, na kukana haiwezekani kabisa."—Ibid., b. 7, ch. 1.

Baada ya habari kusambaa jijini Worms kuwa Luther alikuwa anakuja kusimama mbele ya Baraza Kuu la Kitaifa, msisimko mkubwa uliibuka. Aleanda, mwakilishi wa papa ambaye kesi hiyo ilikuwa imewekwa chini yake hasa, alishtuka na kukasirishwa sana. Aliona kuwa matokeo yangekuwa ya hatari kwa maslahi ya upapa. Kuanzisha uchunguzi kuhusiana na kesi ambayo papa alikuwa tayari ameshatangaza hukumu ya adhabu ingekuwa ni kuonesha dharau kwa mamlaka ya papa mkuu. Zaidi ya hapo, aliogopa kuwa hoja fasaha na zenye nguvu za mtu huyu zingeweza kugeuza viongozi wengi mbali na maslahi ya papa. Hivyo basi, kwa mkazo mkubwa alimsihi Charles asimlete Luther mbele ya Baraza Kuu la Worms. Karibu na wakati huu barua iliyotangaza kuwa Luther ameshatengwa na Kanisa ilichapishwa; na hili, likijumuishwa na maneno ya mwakilishi wa papa, vilimshawishi mfalme kukubali. Alimwandikia kiongozi wa Saxony kuwa ikiwa Luther hawezi kukana, inampasa abakie Wittenberg.

Kwa kutokuridhishwa na ushindi huu, Aleanda alifanya kazi kwa nguvu zake zote na hila zote alizoweza kuwezesha adhabu ya Luther. Kwa juhudi kubwa ambayo ingestahili kwa kazi bora zaidi kuliko hiyo, alishikiniza suala hilo lifanyiwe kazi na viongozi wa serikali, maaskofu, na wajumbe wengine wa baraza kuu la kitaifa, akimshitaki Mwanamatengenezo kwa kosa la"ushawishi, uasi, ufisadi, na kufuru." Lakini ukali na hasira vilivyooneshwa na mwakilishi wa papa vilifunua roho iliyokuwa ikimwendesha. "Anasukumwa na chuki na kisasi," yalikuwa ndiyo maoni ya jumla, "zaidi kuliko imani na kicho."—Ibid., b. 7, ch. 1. Wengi wa wajumbe wa Baraza Kuu la Kitaifa waliazimia kuwa upande wa Luther zaidi kuliko hata kabla ya wakati huo.

Kwa juhudi zilizoongezwa mara dufu Aleanda alimbana mfalme atekeleze amri za papa. Lakini kwa sheria za Ujerumani hili lisingeweza kufanyika bila ridhaa ya viongozi wengine wote wa majimbo; na, kwa kuzidiwa na juhudi za mwakilishi wa papa, Charles alimwamuru Aleanda alete madai yake mbele ya Baraza Kuu la Kitaifa. "Ilikuwa siku ya kujivunia kwa mjumbe wa papa, mama na bimkubwa wa makanisa yote." Alipaswa kuthibitisha ukuu wa Petro mbele ya wenye mamlaka na wakuu wa ulimwengu wa Kikristo. "Alikuwa na karama ya ufasaha, na alikuwa na uwezo uliokidhi hitaji la tukio la siku hiyo. Uongozi wa Mungu ulipanga kuwa Roma itangulie kwa njia ya waongeaji wake mahiri mbele ya mkutano mkuu wa majaji, kabla kanisa halijahukumiwa."—Wylie, b. 6, ch. 4.

Kwa shingo upande wale waliokuwa upande wa Mwanamatengenezo walijiandaa kusikiliza hotuba ya Aleanda. Kiongozi wa Saxony hakuhudhuria katika kikao hicho, lakini kwa maelekezo yake baadhi ya wajumbe wake walihudhuria ili kuandika maelezo ya hotuba ya mjumbe wa papa.

Kwa nguvu zote za usomi na ufasaha, Aleanda alijipanga kuushinda ukweli. Shitaka baada ya shitaka lilirushwa dhidi ya Luther kuonesha kuwa Luther ni adui wa kanisa na serikali, na adui wa watu walio hai na walio kufa, adui wa viongozi wa kanisa na walei, adui wa mabaraza na Wakristo binafsi. "Katika makosa ya Luther kuna mambo ya kutosha" alitangaza, kusababisha kuchomwa moto kwa "wazushi laki moja." Kwa kumalizia alijaribu kuonesha dharau dhidi ya wafuasi wa imani ya matengenezo: "Hawa wafuasi wa Luther ni kitu gani? Ni kikundi cha waalimu waasi, makasisi fisadi, watawa wasio waadilifu, wanasheria wasiojua kitu, na viongozi walioharibikiwa, wakijumuisha watu wa kawaida ambao wamepotoshwa na kudanganywa na hawa viongozi. Ni kwa kiasi gani jumuia ya Wakatoliki iko juu zaidi katika idadi, uwezo, na nguvu! Amri ya pamoja itakayotolewa na mkutano huu makini itaelimisha watu wa kawaida, itawaonya watu wenye busara, itawapa msimamo watu wanaotatanishwa, na itawapa nguvu watu walio dhaifu."— D'Aubigne, b. 7, ch. 3.

Kwa silaha kama hizo hizo watetezi wa ukweli katika zama zote wamekuwa wakishambuliwa. Hoja hizo hizo zimetolewa dhidi ya watu wote wanaojaribu kuwasilisha, dhidi ya makosa yaliyozoeleka, neno la wazi na la moja kwa moja la mafundisho ya neno la Mungu. "Hawa wanaohubiri mafundisho mapya ni akina nani?" Wanasema wale wanaotamani dini inayopendwa na wengi. "Ni watu wasio na elimu, idadi yao ni ndogo, na watu wa tabaka la watu walio maskini sana. Na bado wanadai kuwa wanao ukweli, na kwamba wao ni watu ambao wamechaguliwa na Mungu. Ni wajinga na wamedanganyika. Kanisa letu ni kubwa na lina idadi kubwa na mvuto mkubwa kiasi gani! Ni watu wangapi wana uwezo mkubwa na elimu ya juu miongoni mwetu! Ni nguvu kubwa kiasi gani iko upande wetu!" Hizi ndizo hoja ambazo zina mvuto mkubwa ulimwenguni; lakini peke yake hazitoshi sasa kuliko zilivyokuwa siku za Mwanamatengenezo.

Matengenezo hayakuishia kwa Luther kama wengi wanavyodhani. Yanapaswa kuendelea mpaka mwisho wa historia ya ulimwengu huu. Luther alikuwa na kazi kubwa ya kufanya katika kuwaakisia wengine nuru ambayo Mungu aliruhusu imwangazie; hata hivyo hakupokea nuru yote ambayo ilipaswa itolewe kwa ulimwengu. Tangu wakati ule mpaka wakati huu, nuru mpya imeendelea kuangazia katika Maandiko, na kweli zimekuwa daima zikifunuliwa.

Hotuba ya mjumbe wa papa ilikuwa na mguso mkubwa kwa wajumbe wa Baraza Kuu la Kitaifa. Luther hakuwepo mkutanoni, akiwa na kweli za wazi na zinazoshawishi za neno la Mungu, kumzima shujaa wa upapa. Hakuna jaribio lo lote lililofanywa la kumtetea Mwanamatengenezo. Kulikuwepo na mwelekeo wa wazi siyo tu wa kumhukumu yeye na mafundisho aliyoyafundisha, lakini ikiwezekana kung'oa mizizi ya uzushi. Roma ilikuwa na fursa kubwa ya kutetea msimamo wake. Yote ambayo Kanisa lingeweza kusema katika kuthibitisha msimamo wake yalikuwa yamesemwa. Lakini kile kilichoonekana kama ushindi

kwa Kanisa kiliashiria kushindwa kwake. Tangu wakati huo tofauti kati ya ukweli na uongo ilionekana waziwazi, kwa sababu wangepanua wigo wa mgogoro na kuuanika hadharani. Tangu siku hiyo Roma isingekuwa salama kama ilivyosimama kabla ya hapo.

Wakati wajumbe wengi wa Baraza Kuu la Kitaifa wasingesita kumtoa Luther kwa kisasi cha Roma, wengi wao waliona na walichukia uovu uliokuwemo kanisani, na walitamani kuondolewa kwa mabaya yaliyowapata watu wa Ujerumani kama matokeo ya ufisadi na tamaa ya viongozi wa kanisa. Mjumbe wa papa aliwasilisha utawala wa papa kwa kupendelea upapa kwa kiwango cha juu kabisa. Sasa Bwana alimsukuma mjumbe mmoja wa Baraza kutoa maelezo ya kweli kuhusu madhara ya ukatili wa upapa. Kwa ujasiri wa kitawala, Mtoto wa Mfalme wa Saxony alisimama katika kusanyiko lile la watawala na kutaja kwa usahihi wa kutisha uongo na machukizo ya upapa, na matokeo yake mabaya. Katika kufunga alisema:

"Haya ndiyo maudhi yanayopiga kelele dhidi ya Roma. Aibu yote imewekwa pembeni, na lengo lao pekee ni ... pesa, pesa, pesa, ... kiasi kwamba wahubiri ambao wangefundisha ukweli, hawasemi kitu zaidi ya uwongo, na siyo tu kuwa wanavumiliwa, bali pia wanapewa zawadi, kwa sababu kwa kadiri uongo wao unavyozidi kuwa mkubwa ndivyo mapato yao yanavyokuwa makubwa zaidi. Ni kutoka katika chemchemi hii chafu ndiko maji haya machafu hutiririka. Ufisadi hunyosha mkono hadi ubadhirifu....

Kwa namna ya ajabu sana, ni kashifa inayosababishwa na viongozi wa dini inayorushia watu wengi walio maskini katika hukumu ya milele. Matengenezo makubwa inapaswa yafanyike."—Ibid., b. 7, ch. 4.

Ukosoaji wenye nguvu na makini dhidi ya maovu ya upapa usingeweza kuwasilishwa na Luther binafsi; na ukweli kuwa msemaji alikuwa adui mkubwa wa Mwana matengenezo uliyapa maneno yake mvuto mkubwa.

Kama macho ya wajumbe wa mkutano yangefumbuliwa, wangeweza kuwaona malaika wa Mungu kati kati yao, wakimulika nuru dhidi ya giza la makosa na kufungua akili na mioyo ya watu ili waupokee ukweli. Ilikuwa nguvu ya Mungu wa ukweli na hekima iliyowaongoza hata maadui wa matengenezo, na hivyo iliandaa njia kwa ajili ya kazi kubwa iliyokuwa karibu kufanyika. Martin Luther hakuwepo; lakini sauti ya Yule aliyekuwa mkubwa zaidi kuliko Luther ilisikika katika mkutano ule.

Kamati iliundwa mara moja na Baraza kuandaa orodha ya manyanyaso ya upapa yaliyowalemea watu wa Ujerumani. Orodha hii, iliyokuwa na vipengele mahususi mia moja na moja, iliwakilishwa kwa mfalme, ikiwa na ombi kuwa achukue hatua za haraka kuondoa manyanyaso hayo. "Ni hasara kubwa kiasi gani kwa kupotea roho za Wakristo," waombaji walisema, "ni vitisho vingapi, unyang'anyi mkubwa kiasi gani vinawakabili watu, kwa sababu ya tamaa ya kiongozi wa kiroho wa Ukristo! Ni wajibu wetu kuzuia maumivu na

kudhalilishwa kwa watu wetu. Kwa sababu hiyo kwa unyenyekevu mkubwa lakini kwa msisitizo mkubwa tunakusihi uamuru matengenezo ya hali ya juu, na uhakikishe kuwa yanatekelezwa."—Ibid., b. 7, ch. 4.

Sasa Baraza lilidai Mwanamatengenezo atokee mbele yao. Pamoja na kusihi, mapingamizi, na vitisho vya Aleanda, mwisho wake mfalme aliafiki, na Luther aliitwa aje mbele ya Baraza. Pamoja na samasi kilitolewa pia cheti cha hakikisho la usalama wake, ili kuhakikisha kuwa atarudi nyumbani salama. Nyaraka hizi zilipelekwa Wittenberg na mjumbe, aliyeagizwa kumleta katika jiji la Worms.

Marafiki wa Luther waliingiwa na hofu na kusumbuka sana. Wakitambua chuki na uadui dhidi yake, waliogopa kuwa hata cheti cha hakikisho la usalama kisingeheshimiwa, na walimsihi asihatarishe maisha yake. Alijibu: "Wafuasi wa papa hawataki niende Worms, bali wanatamani nihukumiwe na kuuawa. Hilo siyo tatizo. Msiniombee mimi, bali ombeeni neno la Mungu Kristo atanipa Roho Wake niwashinde hawa watumishi wa uovu. Nitawadhihaki katika uhai wangu; nitawashinda kwa kifo changu. Wanajishughulisha jijini Worms ili wanilazimishe kukana; na huku ndiko kutakuwa kukana kwangu: Nilisema awali kuwa papa ni mwakilishi wa Kristo; sasa ninasema kuwa yeye ni adui mkubwa wa Bwana wetu, na mtume wa Shetani."—Ibid., b. 7,ch. 6.

Luther hakuwa peke yake katika safari hii ya kuhatarisha maisha. Kando ya mjumbe wa mfalme, watu watatu miongoni mwa marafiki zake wa karibu waliazimia kusafiri naye. Melanchthon alitamani sana kumsindikiza. Moyo wake ulikuwa umeshikamana na ule wa Luther, na alikuwa na hamu ya kuaandamana naye, ikiwa lazima, hadi gerezani au mautini. Lakini maombi yake yalikataliwa. Ikiwa Luther angeangamia, matumaini ya Matengenezo yangebaki kwa huyu mtendakzi mwenzake kijana. Mwanamatengenezo alisema alipokuwa akitengana na Melanchthon: "Ikiwa sitarudi, na maadui zangu wakaniua, endelea kufundisha, na simama imara katika ukweli. Fanya kazi badala yangu Ikiwa wewe utabaki ukiwa hai, kifo changu kitakuwa matokeo madogo sana."—Ibid., b. 7, ch. 7. Wanafunzi na raia waliokuwa wamekusanyika kushuhudia kuondoka kwa Luther waliguswa sana. Watu wengi ambao mioyo yao ilikuwa imeguswa na injili, walimuaga kwa machozi. Hivyo Mwanamatengenezo na wenzake walioondoka Wittenberg.

Wakiwa safarini waliona kuwa mawazo ya watu yalikuwa na hisia za hofu na kukata tamaa. Katika baadhi ya miji hakupewa heshima yo yote. Walipopumzika ili kulala usiku, kasisi mmoja rafiki yake Luther, alieleza hofu zake kuonesha mbele ya Luther picha ya mwanamatenegezo wa Italia ambaye alikuwa ameuawa kwa ajili ya kutetea imani yake. Siku iliyofuata waligundua kuwa maandishi ya Luther yalikuwa yamepigwa marufuku jijini Worms. Wajumbe wa mfalme walikuwa wakitangaza amri ya mfalme na kuwataka watu walete maandishi yote yaliyopigwa marufuku kwa mahakimu. Mjumbe, kwa kuhofia usalama wa Luther Barazani, na akifikiri kuwa msimamo wake unaweza kuyumbishwa, aliuliza ikiwa

bado alitamani kuendelea na safari. Alijibu: "Ingawa nimepigwa marufuku kila mji, nitaendelea na safari."—Ibid., b. 7, ch. 7.

Mjini Erfurt, Luther alipokelewa kwa heshima. Akiwa amezungukwa na kundi la watu wenye shauku, alipita katika mitaa ambayo mara nyingi aliitembelea akiwa na mkoba wa omba omba. Alitembelea chumba chake katika nyumba ya watawa, na akatafakari kuhusu mapambano ambayo kwayo nuru sasa iliyofurika Ujerumani ilimwagwa katika roho yake. Aliombwa kuhubiri. Jambo hili alikuwa amekataza kulifanya, lakini mjumbe wa mfalme alimpa ruhusa, na mtawa ambaye awali alikuwa mfagiaji wa jumba la watawa, sasa alipanda mimbarani kuhubiri.

Kwa mkutano uliohudhuriwa na watu wengi alihubiri kutoka maneno ya Kristo, "Amani iwe kwenu." "Wanafalsafa, wasomi, na waandishi," alisema, "wamejaribu kuwafundisha watu jinsi ya kupata uzima wa milele, na hawajafanikiwa. Sasa nitawaambia: ... Mungu amemfufua Mtu mmoja kutoka katika wafu, Bwana Yesu Kristo, ili kuangamiza kifo, kukomesha dhambi, na kufunga milango ya kuzimu. Hii ni kazi ya wokovu Kristo ameshinda! Hii ni habari ya furaha; na tumeokolewa kutokana na kazi Yake, na siyo kutokana na kazi yetu, na siyo kwa uwezo wetu wenyewe Bwana wetu Yesu Kristo alisema, 'Amani iwe kwenu; angalieni mikono yangu;' maana yake ni kuwa, Angalia, wee mwanadamu! Ni mimi, Mimi peke Yangu, ambaye nimeichukua dhambi yenu, na nimewakomboa; na sasa ninyi mnayo amani, asema Bwana."

Aliendelea, akionesha kuwa imani ya kweli itadhihirishwa na maisha matakatifu. "Kwa kuwa Mungu ametuokoa, hebu tupange kazi zetu ili ziweze kukubalika Kwake. Je, wewe ni tajiri? Hebu utajiri wako utumiwe kuwasaidia maskini. Je, wewe ni maskini? Hebu huduma zako zikubalike mbele ya matajiri. Ikiwa kazi zako zinakubalika mbele yako peke yake, huduma unayojifanya kumfanyia Mungu ni uongo."—Ibid., b. 7, ch. 7.

Watu walisikiliza kana kwamba waliotekewa. Mkate wa uzima ulikuwa ukigawiwa kwa roho zilizokuwa zikifa kwa njaa. Kristo alikuwa akiinuliwa juu kuliko mapapa, wakuu wa madola, na wafalme. Luther hakugusia kabisa hatari iliyokuwa ikimkabili. Hakutaka wamfikirie yeye binafsi au kuwafanya wamwonee huruma binafsi. Katika kumtafakari Kristo alisahau nafsi yake. Alijificha nyuma ya Mtu wa Kalwari, akitafuta kumwasilisha Yesu kama Mkombozi pekee wa mwenye dhambi.

Wakati Mwanamatengenezo alipokuwa akiendelea na safari yake, kila mahali aliangaliwa kwa shauku kubwa. Umati mkubwa wa watu walimzunguka, na sauti za marafiki zilimwonya juu ya kusudi la viongozi wa Kanisa la Kirumi. Baadhi wakasema, "watakuchoma moto," na kukuunguza mwili wako uwe majivu, kama walivyomfanya John Huss." Luther alijibu, "Hata kama wangewasha moto njia nzima kuanzia jiji la Worms hadi jiji la Wittenberg, ndimi za moto ziende juu hadi mbinguni, ningetembea katikati yake katika

jina la Bwana; ningetokea mbele yao, ningeingia katika mataya ya kiboko huyu, na kuvunja meno yake, nikimkiri Bwana Yesu Kristo."— Ibid., b. 7, ch. 7.

Habari za kukaribia kwake Worms zilisababisha vurumai. Marafiki zake walitetemeka kwa kuhofia usalama wake; maadui zake walikuwa na hofu ya mafanikio ya kazi yao. Juhudi kubwa zilifanywa kumshawishi asiingie jijini. Kwa uchochezi wa watetezi wa upapa aliombwa apumzike katika jengo la rafiki yake mmoja nje ya jiji, ambapo, ilitangazwa kuwa matatizo yote yangerekebishwa kwa mapatano. Marafiki zake walijitahidi kuamsha hofu zake kwa kueleza hatari zilizomkabili. Juhudi zao zote zilishindwa. Luther, akiwa bado hajatetereka, alitoa msimamo wake: "Hata kama kuna mashetani wengi katika jiji la Worms kama vigae kwenye papa la nyumba, bado nitaingia tu ndani."—Ibid., b. 7, ch. 7.

Alipofika Worms, kundi kubwa la watu lilikuja malangoni kumkaribisha. Mkusanyiko mkubwa kama huo ulikuwa haujawahi kutokea hata kumpokea mfalme mwenyewe. Msisimko ulikuwa wa kiwango cha juu, na kutoka katikati ya mkusanyiko sauti ya juu na ya huzuni iliimba wimbo wa mazishi kama onyo kwa Luther juu ya hatari iliyokuwa ikimsubiri. "Mungu atakuwa mlinzi wangu," alisema, alipokuwa akishuka kutoka katika gari lake la kukokotwa na farasi.

Watetezi wa upapa hawakuamini kuwa Luther angethubutu kutokea jijini Worms, na kufika kwake kuliwafanya waogope sana. Mfalme aliwaita wanabaraza haraka sana kutafakari juu ya hatua inayopaswa kuchukuliwa. Mmoja wa maaskofu, mtetezi wa upapa mwenye msimamo mkali, akasema: "Tumejadili sana juu ya suala hili. Tunakuomba wewe mfalme umwangamize mtu huyu mara moja. Je, Sigismund hakuwezesha John Huss achomwe moto? Hatulazimiki kutoa wala kuheshimu cheti cha usalama cha mzushi." "Hapana," mfalme alisema, "tunapaswa kutunza ahadi yetu."—Ibid., b. 7, ch. 8. Hivyo iliamuriwa kuwa Mwanamatengenezo asikilizwe.

Jiji lote lilikuwa na shauku ya kumwona mtu huyu wa ajabu, na kundi kubwa la wageni lilijaza nyumba za wageni mara moja. Luther alikuwa amepona kidogo ugonjwa wake wa siku za karibuni; alikuwa amechoshwa na safari, ambayo ilikuwa imechukua majuma mawili kamili; ilimpasa ajiandae kukutana na matukio makubwa kesho yake, hivyo alihitaji ukimya na pumziko. Lakini shauku ya kumwona ilikuwa kubwa mno kiasi kwamba alifaulu kupumzika kwa saa chache tu ambapo malodi, mashujaa, makasisi, na raia walikusanyika kwa shauku na kumzunguka. Miongoni mwao walikuwemo waheshimiwa ambao kwa ujasiri walikuwa wamemwomba mfalme asimamie matengenezo ya uovu miongoni mwa viongozi wa kanisa na wale ambao, Luther alisema, "waliokuwa wamewekwa huru na injili yangu."—Martyn, uk. 393. Maadui, na marafiki, wote kwa pamoja walikuja kumwona huyu mtawa asiye na woga; lakini aliwapokea kwa utulivu usiotetereka, akiwajibu wote kwa heshima na hekima. Mwonekano wake ulikuwa wenye uimara na ujasiri. Uso wake mweupe, mwembamba, ukiwa na viashiria vya kazi ngumu na kuugua, ulivaa mwonekano wa ukarimu

na furaha. Umakini na udhati wa kina wa maneno yake ulimpa nguvu ambayo hata maadui zake hawakuweza kuistahimili. Marafiki na maadui kwa pamoja walijazwa na mshangao. Baadhi walishawishika kuwa mvuto wa Kimungu ulikuwa ndani yake; wengine walisema, kama Mafarisayo walivyosema kuhusiana na Kristo: "Ana pepo."

Siku iliyofuata Luther aliitwa kufika mbele ya Baraza Kuu. Afisa kutoka ikulu ya mfalme aliteuliwa kwenda kumleta na kumwongoza ukumbini; hata hivyo alifika mahali pale kwa shida sana. Kila njia ilikuwa imefurika watu wenye shauku ya kumwona huyu mtawa aliyethubutu kupinga mamlaka ya papa.

Alipokuwa karibu kuingia mbele ya majaji wake, jenerali mkongwe, shujaa wa vita vingi, aliongea naye kwa upole: "Maskini mtawa, maskini mtawa, sasa unakwenda kuweka msimamo ulio bora zaidi kuliko mimi au kapteni mwingine ye yote alivyoweza kufanya katika vita iliyomwaga damu nyingi zaidi kuliko vita zote. Lakini, ikiwa kazi yako ni ya haki, na wewe una uhakika nayo, songa mbele katika jina la Mungu, na usiogope kitu chochote. Mungu hatakuacha."—D'Aubigne, b. 7, ch. 8.

Hatimaye Luther alisimama mbele ya Baraza. Mfalme alikalia kiti cha enzi. Alizungukwa na maofisa wa ngazi za juu kabisa katika ufalme. Ilikuwa haijawahi kutokea mtu ye yote kusimama mbele ya mkutano unaovutia kuliko ule ambao Martin Luther alitakiwa kutetea imani yake mbele yake. "Mwonekano huu tu peke yake ulikuwa ishara ya ushindi dhidi ya upapa. Papa alikuwa ameshamhukumu yule mtu, na sasa alikuwa amesimama mbele ya mahakama, ambayo, kwa tendo hili tu peke yake, ilikuwa imejiweka juu ya papa. Papa alikuwa ameshamweka chini ya amri ya kutengwa, na alikuwa amekata mahusiano yake na jamii yote ya watu; na bado alikuwa ameitwa kwa lugha ya heshima, na kupokelewa mbele ya mkutano mkubwa kuliko mikutano yote duniani.

Papa alikuwa ameshamhukumu kuwa kimya siku zote, na sasa alikuwa karibu kuhutubia maelfu ya wasikilizaji makini waliokusanyika pamoja kutoka kona zote za ulimwengu wa Ukristo. Mapinduzi makubwa yalikuwa yametekelezeka kupitia kwa Martin Luther. Roma ilikuwa tayari inashuka kutoka katika kiti chake cha enzi, na ilikuwa sauti ya mtawa iliyomshusha chini."—Ibid., b. 7, ch. 8.

Mbele ya mkutano wa waheshimiwa wenye vyeo vya juu, Mwanamatengenezo aliyezaliwa katika umaskini, alionekana kunyenyekeshwa na kunyanyasika. Baadhi ya wakuu, walipogundua hisia zake, walimwendea, na mmoja wao alimnong'onezea: "Usiwaogope wao wanaoua mwili, bali mwogope Yeye anayeweza kuua roho." Mwingine alisema: "Watakapowapeleka mbele ya watawala na wafalme kwa ajili Yangu, mtapewa, na Roho wa Baba, cha kusema." Hivyo maneno ya Kristo yaliletwa na watu wakuu ulimwenguni kumtia nguvu mtumishi Wake katika saa ya kujaribiwa.

Luther aliongozwa hadi sehemu iliyoangaliana moja kwa moja na kiti cha enzi cha mfalme. Ukimya mkuu uliushika umati wa watu waliokusanyika. Ndipo ofisa kutoka ikulu ya mfalme alisimama na, akinyosha kidole kuelekea mkusanyiko wa maandishi ya Luther, alimtaka Mwanamatengenezo ajibu maswali mawili—ikiwa alikiri kuwa ni maandishi yake, na ikiwa alikuwa tayari kukana maoni aliyoyaweka katika maandishi yale. Majina ya vitabu yaliposomwa, Luther alijibu kuwa kwa swali la kwanza, alikiri kuwa vitabu vile ni vyake. “Kwa swali la pili,” alisema, “kwa kuwa ni swali linalohusiana na imani na wokovu wa roho, na kwa kuwa neno la Mungu, hazina kuu na ya thamani kubwa kuliko zote iwe mbinguni au duniani, linahusika, itakuwa siyo busara kujibu haraka haraka bila kutafakari. Kuna uwezekano nikathibitisha kidogo zaidi kuliko uhalisia unavyodai, au nikathibitisha kwa nguvu zaidi kuliko ukweli unavyohitaji, na kwa sababu hiyo nikatenda dhambi dhidi ya kauli hii ya Kristo: ‘Atakayenikana mbele za watu, nitamkana mbele ya Baba Yangu wa mbinguni’ [Mathayo 10:33.] Kwa sababu hiyo ninakusihi, ee mfalme mkuu, kwa unyenyekevu wote, unipe muda, ili niweze kujibu bila kulikosea neno la Mungu.”—D’Aubigne, b. 7, ch. 8.

Kwa kutoa ombi hili, Luther alichukua hatua muafaka. Mwelekeo huu uliwashawishi wajumbe wa mkutano kuwa hakutoa majibu kwa jaziba au kukurupuka. Utulivu huo na kujitawala, ambako hakukutarajiwa kwa mtu ambaye alikuwa amejionesha kuwa jasiri na mwenye msimamo usioyumba, ulimwongezea nguvu, na kumwezesha baadaye kujibu kwa busara, uamuzi, hekima, na heshima iliyowashangaza watu wengi na kuwakatisha tamaa maadui zake, na ulikemea ufedhuli na kiburi. Siku iliyofuata alipaswa kutokea ili kutoa jibu lake la mwisho. Kwa muda fulani moyo wake ulisinyaa ndani yake alipotafakari juu ya mamlaka zilizoungana dhidi ya ukweli. Imani yake ilitetereka; hofu na kutetemeka vilimjia, na kihoro kilimgubika. Hatari ziliongezeka mbele yake; maadui zake walioonekana kushangilia, na nguvu za giza kushinda. Mawingu yalijikusanya na kumzunguka na yalionekana kama yalimtenga na Mungu. Alitamani kupata uhakikisho kuwa Bwana wa majeshi atakuwa pamoja naye. Akiwa na kilio moyoni alijitupa chini akalala kifudi-fudi na kumwaga vilio vya moyo uliopondeka na kuvunjika- vilio ambavyo hakuna mtu ye yote anayeweza kuvielewa isipokuwa Mungu peke yake.

“Ee Mungu Mwenyezi wa milele,” alisihi, “ulimwengu huu unatisha kiasi gani! Tazama, umefunua mdomo ili unimeze, na mimi nina tumaini kidogo sana Kwako Ikiwa inanipasa kutumainia nguvu ya huu ulimwengu peke yake, huu ndio mwisho wangu Saa yangu ya mwisho imefika, hukumu yangu imeshatangazwa. Ee Mungu, nisaidie dhidi ya hekima ya ulimwengu. Fanya hivyo, ... Wewe peke Yako; kwa kuwa kazi hii siyo yangu, bali ya Kwako. Sina lo lote la kufanya hapa, sina la kubishania na hawa wakuu wa ulimwengu. Lakini kazi hii ni Yako, na kazi ya haki na ya milele. Ee Bwana, nisaidie!

Mungu mwaminifu usiyebadilika, sina mtu mwingine ninayemtumainia.... Cho chote kinachotokana na mwanadamu hakina uhakika; yote yaayotokana na mwanadamu yanaangusha.... Wewe umenichagua kwa ajli ya kazi hii. Simama kando yangu, kwa ajili ya

mpendwa Wako Yesu Kristo, ambaye ni mlinzi wangu, ngao yangu, na ngome yangu imara."—Ibid., b. 7, ch. 8.

Uongozi wa Mungu wenye hekima uliruhusu Luther agundue hatari iliyokuwa mbele yake, ili asitegemee nguvu zake mwenyewe na asikimbilie kwa kiburi hatarini. Hata hivyo hofu yake haikuwa kwa ajili ya mateso binafsi, hofu ya maumivu au kifo, kilichoonekana kuwa karibu sana, ambacho kilimtisha. Alikuwa amefikia kilele cha mgogoro, na alihisi kutotosha kukabiliana na kilele hicho. Kwa sababu ya udhaifu wake kazi ya ukweli ingeshindwa. Alishindana na Mungu siyo kwa ajili ya usalama wake, bali kwa ajili ya ushindi wa injili. Kama ilivyokuwa kwa Israeli, katika pambano lile la usiku kando ya kijito cha upweke, ndivyo maumivu na mapambano ya roho yake yalivyokuwa. Kama ilivyokuwa kwa Israeli, alimshinda Mungu. Katika hali yake isiyokuwa na msaada kabisa imani yake ilimshikilia Kristo, Mkombozi mwenye nguvu. Aliimarishwa kwa uhakikisho kuwa asingekwenda mbele ya baraza akiwa peke yake. Amani ilirudi moyoni mwake, na alifurahi kuwa aliruhusiwa kuliinua neno la Mungu mbele ya watawala wa mataifa.

Akili yake ikiwa imetulizwa kwa Mungu, Luther alijiandaa kwa ajili ya mapambano yaliyokuwa mbele yake. Alifikiria juu ya mpangilio wa jibu lake, alichunguza aya katika maandishi yake, na alichota kutoka katika Maandiko uthibitisho stahiki kutetea misimamo yake. Ndipo, akiwa ameweka mkono wake wa kushoto juu Kitabu Kitakatifu, ambacho kilikuwa wazi mbele yake, aliinua mkono wake wa kulia kuelekea mbinguni na aliapa "kubaki akiwa mwaminifu kwa injili, na kukiri imani yake kwa uhuru, hata kama ingebidi kuthibitisha ushuhuda wake kwa damu yake."—Ibid., b. 7, ch. 8.

Alipopelekwa tena mbele ya Baraza, Sura ya ke haikuwa na kiashiria chochote cha hofu wala aibu. Akiwa mtulivu na mwenye amani, lakini jasiri na muungwana sana, alisimama kama shahidi wa Mungu miongoni mwa wakuu wa dunia. Yule afisa mteule wa mfalme alimwamuru atoe uamuzi wake ikiwa alikusudia kukana mafundisho yake. Luther alijibu kwa sauti tulivu na ya unyenyekevu, bila ukali wala mhemko. Mwonekano wake ulikuwa wa heshima na adabu; na bado alionesha ujasiri na furaha iliyoushangaza mkutano. "Mfalme mtulivu sana, waheshimiwa wana wa wafalme, watawala wakuu wenye neema," alisema Luther, "Nimekuja mbele yenu siku ya leo, kwa amri niliyopewa jana, na kwa rehema za Mungu ninakuomba mheshimiwa mfalme na viongozi wakuu mliopo hapa msikilize kwa neema utetezi wa kazi ambayo nina hakika ni ya haki na ya kweli. Ikiwa, kwa kutokujua, nitakosea taratibu na itifaki za baraza, ninawasihi sana mnisamehe; kwa kuwa sikulelewa katika ikulu za wafalme, bali katika upweke wa nyumba ya watawa."—Ibid., b. 7, ch. 8.

Ndipo, akijielekeza kujibu swali, alisema kuwa vitabu vyake havikuwa vya aina moja. Katika baadhi ya vitabu aliandika juu ya imani na matendo mema, na hata maadui zake walisema kuhusu hivyo vitabu kuwa licha ya kutokuwa na madhara yo yote vilikuwa na manufaa sana. Kuvikana vitabu hivi ingekuwa ni kuukataa ukweli ambao pande zote

zinaukiri. Kundi la pili la vitabu lilikuwa na maandishi yaliyofunua ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka ya upapa. Kuvikana vitabu hivi kungeimarisha ukatili wa Roma na kufungua zaidi milango kwa ajili ya uovu mkubwa zaidi. Katika kundi la tatu la vitabu vyake alishambulia watu binafsi waliotetea maovu yaliyokuwepo. Kuhusiana na vitabu alikiri wazi kuwa alitumia lugha kali kuliko ilivyostahili. Hakudai kuwa hakuwa na makosa kabisa; lakini hata hivi vitabu asingevikana kwa sababu kufanya hivyo kungewapa nguvu maadui wa ukweli, na wangetumia fursa hiyo kuwakandamiza watu wa Mungu kwa ukatili mkubwa zaidi.

"Hata hivyo mimi ni mwanadamu tu, na siyo Mungu," aliendelea; "Kwa hiyo nitajitetea kama Kristo alivyojitetea: 'Ikiwa nimesema vibaya, toeni ushahidi dhidi ya ubaya huo.' ... Kwa rehema za Mungu, ninakuomba, mfalme mtulivu sana, na ninyi, waheshimiwa sana wana wa wafalme, na watu wote wa kila ngazi, mthibitishe kutoka katika maandiko ya manabii, na mitume kuwa nimekosea. Na mara tu nikishawishika kuwa vina makosa, nitakana kila kosa, na nitakuwa wa kwanza kushika vitabu vyangu na kuvitupa motoni.

"Mambo ambayo nimeyasema wazi hivi punde yanaonesha, natumaini, kuwa nimepima na kufikria kwa uangalifu hatari zinazonikabili; lakini licha ya kutokukatishwa tamaa, ninafurahi kuona kuwa injili sasa, kama ilivyokuwa nyakati za awali, imekuwa chanzo cha taabu na mpasuko. Hii ni tabia, hii ni hatima, ya neno la Mungu. 'Sikuja kuleta amani duniani, bali upanga,' alisema Yesu Kristo. Mungu ni wa ajabu na anatisha katika mashauri Yake; angalia isije ikawa, kwa kujaribu kuepuka mipasuko, ukalitesa neno la Mungu, na kujimwagia mafuriko ya kutisha ya hatari zisizokoma, za maafa ya sasa, na ukiwa wa milele Ninaweza kunukuu mifano mingi kutoka katika Neno la

Mungu. Ninaweza kuzungumzia habari za Farao, wafalme wa Babeli, na wale wa Israeli, ambao kazi zao hazikuwahi kuchangia kwa kiwango kikubwa kwa uhabirifu wao wenyewe kuliko wakati walipofuata mashauri, ambayo kwa mtazamo wa juu juu, yalionekana kuwa ya busara katika kuimarisha utawala wao. 'Mungu anaondoa milima, na hawalijui hilo.'"—Ibid., b. 7, ch. 8. Luther alikuwa ameongea katika lugha ya Kijerumani; aliombwa arudie maneno yale yale kwa lugha ya Kilatini. Ingawa alikuwa amechoshwa na juhudi za awali, alitii, na alihutubia tena, kwa uwazi ule ule na nguvu ile ile kama alivyofanya mara ya kwanza. Uongozi wa Mungu ulielekeza jambo hilo. Akili za viongozi wengi zilikuwa zimepofushwa kwa makosa na ushirikina kiasi kwamba katika hotuba ya kwanza hawakuona nguvu ya hoja za Luther; lakini kurudia kuliwawezesha kuelewa vizuri zaidi hoja zilizotolewa.

Wale ambao walifumba macho ili wasiione nuru kwa ugumu wa moyo tu na waliazimia kutoshawishiwa na ukweli, walikasirishwa na nguvu ya maneno ya Luther. Alipomaliza kusema, msemaji wa Baraza alisema kwa hasira: "Hukujibu swali ulilouIizwa. Unatakiwa kutoa jibu la wazi na fupi. Unakana, au hukani?" Mwanamatengenezo alijibu: "Kwa kuwa mfalme mtulivu na waheshimiwa viongozi mnataka kwangu jibu la wazi, sahili, na fupi,

nitawapa jibu hilo, nalo ni hili: siwezi kusalimisha imani yangu ama kwa papa au kwa mabaraza, kwa sababu ni wazi kama ulivyo mchana kuwa wamekosea mara nyingi na wanapingana wao kwa wao. Isipokuwa, hivyom basi, nishawishiwe kwa ushuhuda wa Maandiko au kwa hoja madhubuti, isipokuwa tu pale nitakaposhawishiwa kwa njia ya aya nilizozinukuu, na isipokuwa tu pale watakapoifanya dhamiri yangu ishikamane na neno la Mungu, siwezi na sitaweza kukana, kwa kuwa siyo salama kwangu kusema jambo lolote dhidi ya dhamiri yangu. Hapa nasimama, siwezi kufanya jambo lolote jingine; ee Mungu nisaidie. Amina."—Ibid., b. 7, ch. 8.

Hivyo alisimama mtu huyu mwenye haki juu ya msingi wa hakika wa neno la Mungu. Nuru ya mbinguni iliangazia uso wake. Ukuu wake na usafi wa tabia yake, haki na furaha ya moyo wake, vilionekana kwa wote aliposhuhudia dhidi ya nguvu ya makosa na wao walivyoshuhudia nguvu ya imani ishindayo ulimwengu.

Mkutano wote kwa muda walibaki kimya wakiwa wameshikwa na mshangao. Wakati kujibu swali lake la kwanza Luther aliongea kwa sauti ya chini, katika hali ya heshima, na akiwa katika hali kama ya kujisalimisha. Watetezi wa kanisa la Roma walikuwa wametafsiri hali hii kama ushahidi kuwa ujasiri wake ulikuwa unaelekea kwisha. Walichukulia ombi lake la kupewa muda kama utangulizi wa yeye kukana mafundisho yake. Charles mwenyewe, akizingatia, nusu akionesha dharau, umbo dhaifu la mtawa, nguo zake za kimaskini, na usahili wa hotuba yake, alisema: "Mtawa huyu hatanifanya niwe mzushi." Ujasiri na uimara ambao sasa aliuonesha, pamoja na nguvu na uwazi wa hoja zake, uliwajaza wajumbe wa baraza kwa mshangao. Mfalme, baada ya kuguswa, alisema kwa hisia: "Mtawa huyu anaongea kwa moyo mkuu na ujasiri usio na mashaka." Wengi wa viongozi wa Ujerumani walimwangalia kwa kujivunia huyu mwakilishi wa taifa lao.

Wafuasi wa Roma walikuwa wameshindwa; hoja yao ilionekana kuwa dhaifu na isiyoungwa mkono na wajumbe wengi. Walitafuta kudumisha mamlaka yao, siyo kwa kutumia Maandiko, bali kwa kujielekeza kutumia hoja ya vitisho, hoja ya Roma isiyoshindwa. Alisema msemaji wa Baraza: "Usipokanusha, mfalme na majimbo ya ufalme watajadili hatua ya kuchukua dhidi ya mzushi mkorofi."

Rafiki wa Luther, aliyefurahi sana aliposikiliza utetezi wake mzuri, alitetemeshwa na maneno haya; lakini daktari mwenyewe alisema katika hali ya utulivu: "Ee Mungu uwe msaada wangu, kwa kuwa siwezi kukana cho chote."—Ibid., b. 7, ch. 8.

Aliambiwa aondoke katika ukumbi wa Baraza wakati viongozi wakijadiliana. Ilihisiwa kuwa tatizo kubwa lilikuwa limefika. Kukataa kwa daima kwa Luther kujisalimisaha kungeweza kubalidi historia ya kanisa kwa zama zijazo. Iliamuriwa kumpa nafasi nyingine tena ili akanushe. Kwa mara ya mwisho alíletwa katika mkutano. Kwa mara nyingine swali lilitolewa, ikiwa angekanusha mafundisho yake. "Sina jibu jingine la kutoa," alisema, "zaidi

ya lile nililokwisha kulitoa." Ilikuwa wazi kuwa asingeweza kushawishika, ama kwa ahadi au vitisho, kujisalimisha kwa mamlaka ya Roma.

Viongozi wawakilishi wa upapa walichukizwa kuwa mamlaka yao, ambayo iliwafanya wafalme na wakuu watetemeke, ingeweza kudhihakiwa na mtawa maskini; walitamani kumfanya ahisi hasira yao kwa kutesa maisha yake. Lakini Luther, akielewa hatari iliyomkabili, alikuwa ameongea nao wote kwa adabu na utulivu. Maneno yake hayakuwa na kiburi, hasira, na kumsingizia mtu. Alijisahau mwenyewe binafsi, na wakuu waliokuwa wamemzunguka, na alihisi kuwa alikuwa katika uwepo wa Yule aliye juu sana zaidi ya mapapa, maaskofu, wafalme, na wafalme wakuu.

Kristo alikuwa amezungumza kupitia ushuhuda wa Luther kwa nguvu na utukufu ambao kwa muda fulani uliwavutia marafiki na maadui kwa kicho na mshangao. Roho wa Mungu alikuwepo katika Baraza lile, akigusa mioyo ya viongozi wakuu wa dola. Baadhi ya wana wa wafalme walikiri kwa ujasiri uhalali wa kazi za Luther. Wengi walishawishiwa na ukweli; lakini kwa baadhi miguso iliyopokelewa haikuwa ya muda mrefu. Kulikuwepo na kundi la watu ambao hawakueleza kushawishika kwao, lakini ambao, baada ya kuchunguza Maandiko wao wenyewe, katika wakati uliofuata wakawa waungaji mkono wasio na hofu wa Matengenezo.

Elekta Frederick alikuwa ametarajia kwa hamu kubwa ujio wa Luther mbele ya Baraza, na kwa msisimko mkubwa alisikiliza hotuba yake. Kwa furaha na kujisikia vizuri alishuhudia ujasiri, uimara, na kujitawala, na aliazimia kusimama imara zaidi kumtetea. Alitofautisha wahusika katika pambano, na aliona kuwa hekima ya mapapa, wafalme, na maaskofu ilikuwa imeoneshwa kuwa siyo kitu kwa nguvu ya ukweli. Upapa ulikuwa umepata anguko ambalo lingehisiwa miongoni mwa mataifa yote na katika zama zote. Wakati mjumbe wa papa alipopokea madhara yaliyosababishwa na hotuba ya Luther, aliogopa, kuliko hapo awali, kwa ajili ya usalama wa nguvu ya Kiroma, na alidhamiria kutumia kila njia iliyokuwa katika uwezo wake kufanikisha ushindi wa Roma dhidi ya Mwanamatengenezo. Kwa kutumia ufasaha na stadi za kidiplomasia vitu ambavyo alikuwa akivimudu kwa kiwango cha juu, aliwasilisha kwa mfalme kijana upumbavu na hatari ya kuvunja urafiki na kupoteza msaada wa kiongozi wa Roma mwenye nguvu nyingi, kwa sababu ya mafundisho ya mtawa asiye na maana.

Maneno yake hayakupita bila madhara. Siku iliyofuata baada ya jibu la Luther, Charles aliagiza ujumbe upelekwe katika Baraza Kuu la Kitaifa, akitangaza azimio lake la kutekeleza sera ya watangulizi wake ya kusimamia na kulinda dini ya Kikatoliki. Kwa kuwa Luther alikuwa amekataa kukana makosa yake, hatua kali zinapaswa zichukuliwe dhidi yake na uzushi alioufundisha. "Mtawa mmoja, aliyepotoshwa na upumbavu wake mwenyewe, ameinuka dhidi ya imani ya Kikristo. Ili kudhibiti kufuru hii, nitatoa kafara falme zangu, hazina zangu, rafiki zangu, mwili wangu, damu yangu, roho yangu, na maisha yangu.

Nitamfukuza Agustino Luther, na kumpiga marufuku asisababishe vurugu hata kidogo miongoni mwa watu; halafu nitawashughulikia yeye mwenyewe na wafuasi wake kama wazushi wakaidi, kwa kuwatenga na kanisa, kwa kuwatenga na watu, na kwa kila njia inayoweza kuwaangamiza. Ninatoa wito kwa nchi wanachama kuishi kama Wakristo waaminifu."—Ibid., b. 7, ch. 9. Hata hivyo mfalme alitangaza kuwa cheti cha uhakikisho wa usalama wa Luther kilipaswa kiheshimiwe, na kuwa kabla ya hatua yo yote ile kuchukuliwa dhidi yake, alipaswa kuruhusiwa kufika nyumbani kwake salama.

Maoni mawili yanayopingana sasa yalitolewa na kusisitizwa na wajumbe wa Baraza. Wajumbe na wawakilishi wa papa walidai tena kuwa cheti cha uhakikisho wa usalama wa Mwanamatengenezo ilipaswa kipuuzwe. "Mto Rhine," walisema, "inapasa upokee majivu yake, kama ulivyopokea majivu ya John Huss karne moja iliyopita."—Ibid., b. 7, ch. 9. Lakini viongozi wakuu wa ufalme wa Ujerumani, ingawa wao wenyewe walikuwa wafuasi wa papa na maadui wakuu wa Luther, walipinga ukiukwaji wa hadharani wa uaminifu wao kwa umma, kama doa kwa heshima ya taifa. Walitolea mfano wa majanga yaliyofuata baada ya kifo cha Huss, na walisema kuwa wasingethubutu kusababisha kurudiwa kwa majanga yale ya kutisha yaangukie tena juu ya nchi ya Ujerumani, na juu ya kichwa cha mfalme wao kijana.

Charles mwenyewe, akijibu hilo pendekezo baya, alisema: "Ingawa heshima na imani vinapaswa kupigwa marufuku kutoka ulimwenguni mwote, vinapaswa kuhifadhiwa katika mioyo ya viongozi wakuu."—Ibid., b. 7, ch. 9. Aliendelea kusihiwa zaidi na maadui wakuu wafuasi wa upapa kumshughulikia Mwanamatengenezo kama Sigismund alivyomshughulikia Huss—kumwachia kanisa limshughulikie; lakini akikumbuka mandhari wakati Huss katika mkutano wa hadhara alipoonesha minyororo yake na kumkumbusha mfalme juu ya imani yake iliyopotoka, Charles V alisema: "Nisingependa kufanya kama Sigismund alivyofanya."—Lenfant, vol. 1, p. 422.

Hata hivyo Charles aliamua kwa makusudi kuukataa ukweli uliowasilishwa na Luther. "Nimedhamiria kwa nguvu zangu zote kuwaiga wazee wangu," aliandika mfalme.—D'Aubigne, b. 7, ch. 9. Aliamua kuwa asingeondoa mguu wake katika njia ya mila na desturi, ili atembee katika njia za ukweli na haki. Kwa kuwa baba zake walifanya, angeunga mkono upapa, ikiwa ni pamoja na ukatili na ufisadi wake wote. Hivyo aliweka msimamo wake, akikataa kila nuru iliyo tofauti na ile baba zake waliyoipokea, au kufanya wajibu wowote ambao hawakuufanya.

Kuna wengi leo wanaong'ang'ania mila na desturi za baba zao. Wakati Bwana anapowatumia nuru ya nyongeza, wanakataa kuipokea, kwa sababu, kwa kuwa haikutolewa kwa baba zao, isingepokelewa na wao. Hatuwekwi katika nafasi ambazo baba zetu walikuwa; matokeo yake wajibu na majukumu yetu siyo sawa na yao. Hatutakubaliwa na Mungu kwa kuangalia mfano wa baba zetu kuamua wajibu wetu badala ya kuchunguza neno la ukweli sisi wenyewe. Wajibu wetu ni mkubwa zaidi kuliko ule wa wazee wetu. Tunawajibika kwa nuru

waliyoipokea, na ambayo ililetwa kwetu kama urithi wetu, na tunawajibika pia kwa nuru ya nyongeza ambayo sasa inang'aa juu yetu kutoka katika neno la Mungu.

Alisema Kristo kuhusu Wayahudi wasioamini: "Kama nisingalikuja na kusema nao, wasingalikuwa na dhambi; lakini sasa hawana udhuru kwa dhambi yao" (Yohana 15:22). Nguvu ya Mungu ile ile ilikuwa imesema kupitia kwa Luther na kuongea na wakuu wa Ujerumani. Na kama nuru ilivyomulika kutoka katika neno la Mungu, Roho Wake aliwasihi kwa mara ya mwisho watu wengi katika mkutano ule. Kama vile Pilato, karne nyingi zilizopita, alivyoruhusu kiburi na kutaka kupendwa na watu, vifunge moyo wake dhidi ya Mkombozi wa ulimwengu; kama vile Festo alivyomuaga mjumbe wa ukweli, "Sasa enenda zako, nami nikipata nafasi nitakuita;" kama vile Agripa mwenye kiburi alivyokiri, "Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo" (Matendo 24:25; 26:28), lakini aligeuka na kuukataa ujumbe uliotumwa na Mbingu—ndivyo Charles V, akijisalimisha kwa shinikizo la kiburi na sera za ulimwengu, aliamua kuikataa nuru ya ukweli.

Minong'ono na mipango dhidi ya Luther ilienea kila mahali, ikasababisha taharuki kubwa katika jiji lote. Mwanamatengenezo alikuwa na marafiki wengi, ambao, wakijua ukatili na hila ya Roma kwa wote waliojaribu kufichua ufisadi wake, waliazimia kuwa hatatolewa kafara. Mamia ya watu wenye vyeo vya juu waliahidi kumlinda. Siyo watu wachache walioupinga ujumbe wa mfalme wa kujisalimisha kwa mamlaka ya utawala wa Roma. Kwenye malango ya nyumba na katika maeneo ya mikusanyiko ya watu, mabango yalibandikwa, baadhi yakimlaumu na mengine yakimpongeza Luther. Kwenye moja ya mabango haya yalikuwa yamendikwa tu maneno ya maana ya mtu mwenye hekima: "Ole wako, nchi, akiwa mfalme wako ni kijana" (Mhubiri 10:16). Mwamko mkubwa wa jumla uliomwunga mkono Luther katika nchi yote ya Ujerumani ulimshawishi mfalme na Baraza kuwa dhuluma yo yote ambayo ingefanywa dhidi yake ingehatarisha amani ya ufalme na hata uimara wa kiti cha enzi.

Mfalme Frederick wa Saxony alibaki kimya, na kwa uangalifu alificha hisia zake halisi dhidi ya Mwanamatengenezo, wakati huo huo akimlinda wakati wote kwa bidii bila kuchoka, akifuatilia mienendo yake yote na ile ya maadui zake. Lakini walikuwepo watu wengi ambao hawakuficha huruma zao kwa Luther. Alitembelewa na watoto wa mfalme, malodi, mabaroni, na watu wengi wenye heshima, viongozi wa kiraia na viongozi wa kikanisa.

"Chumba kidogo cha daktari," aliandika Spalatin, "hakikuwatosha wageni wote waliomtembelea."—Martyn 1:404. Watu walimwona kana kamba ni zaidi ya mwanadamu. Hata watu ambao hawakuyaamini mafundisho yake walihusudu uadilifu wake mkubwa uliomwezesha kukabiliana na kifo kwa ujasiri badala ya kukiuka dhamiri yake.

Juhudi nyingi zilifanywa kupata ukubali wa Luther wa kupatana na Roma. Malodi na wana wa wafalme walimwambia kuwa ikiwa atashikilia msimamo wake wa kujiwekea

hukumu yake dhidi ya ile ya kanisa na ya baraza siyo muda mrefu angefukuzwa atoke katika ufalme na asingekuwa na ulinzi. Kwa tishio hili Luther alijibu: "Injili ya Kristo haiwezi kuhubiriwa bila kuamsha chuki. Kwa nini sasa hofu au woga wa hatari unitenge na Bwana, na unitenge na neno la Mungu ambalo peke yake ni ukweli? Hapana; afadhali nitoe mwili wangu, damu yangu, na maisha yangu."—D'Aubigne, b. 7, ch. 10.

Kwa mara nyingine tena alisihiwa ajisalimishe kwa hukumu ya mfalme, na ndipo asingekuwa na jambo la kuogopa. "Ninakubali," alijibu, "kwa moyo wangu wote, kuwa mfalme, wana wa mfalme, na hata Mkristo wa kawaida kabisa, achunguze na ahukumu kazi zangu; lakini kwa sharti moja, watumie neno la Mungu kama kiwango chao. Wanadamu hawana cha kufanya kingine isipokuwa tu kulitii. Msiifanyie ukatili dhamiri yangu, ambayo imeshikamana na imefungwa pamoja na Maandiko Matakatifu kwa mnyororo."— Ibid., b. 7, ch. 10.

Kwa kitisho kingine alisema: "Ninakubali kuachana na cheti cha hakikisho la usalama. Ninaweka nafsi yangu katika mikono ya mfalme, lakini neno la Mungu—kamwe!"—Ibid., b. 7, ch. 10. Alieleza utayari wake kujisalimisha kwa uamuzi wa baraza kuu, lakini kwa sharti moja kuwa baraza litakiwe kuamua kulingana na Maandiko. "Katika masuala yahusuyo neno la Mungu na imani," aliongeza, "kila Mkristo ni jaji mzuri kama alivyo papa, hata kama anaungwa mkono na mabaraza milioni moja, laweza kuwa upande wake."— Martyn 1:410. Hatimaye marafiki na maadui walishawishika kuwa juhudi zaidi kwa ajili ya upatanisho zisingefua dafu.

Kama Mwanamatengenezo angesalimu amri katika pointi moja tu, Shetani na majeshi yake wangekuwa wamepata ushindi. Lakini uimara wake usioyumba ulikuwa njia ya kulikomboa kanisa, na mwanzo wa zama mpya na bora zaidi. Mvuto wa mtu huyu mmoja, aliyethubutu kufikiri na kutenda tofauti na wengine katika mambo ya dini, ulibadili kanisa na ulimwengu, siyo tu katika wakati wake, lakini pia katika vizazi vya baadaye. Uimara na uaminifu wake ungewaimarisha wote, hadi mwisho wa wakati, ambao wangepitia katika uzoefu unaofanana na huo. Nguvu na utukufu wa Mungu vilisimama juu ya mashauri ya wanadamu, juu ya nguvu nyingi za Shetani.

Luther aliamurishwa mara moja na mamlaka ya mfalme arudi nyumbani, na alijua kuwa tangazo hili lingefuatwa haraka na hukumu yake. Mawingo ya vitisho yalielea juu ya njia yake; lakini alipokuwa akiondoka Worms, moyo wake ulikuwa umejaa furaha na sifa. "Shetani mwenyewe," alisema, "alilinda ngome ya papa; lakini Kristo alikuwa ameweka ufa mpana katika ngome hiyo, na Shetani alikuwa amelazimishwa kukiri kuwa Bwana ana nguvu zaidi kuliko yeye."—D'Aubigne, b. 7, ch. 11.

Baada ya kuondoka kwake, bado akitamani kuwa uimara wake usitafsiriwe kuwa uasi, Luther alimwandikia mfalme. "Mungu, ambaye ni mchunguzi wa mioyo," alisema, "kuwa

niko tayari kwa juhudi zangu zote kumtii mfalme mtukufu, katika heshima au pasipokuwa na heshima, katika uzima au mauti, na pasipo kubagua cho chote isipokuwa tu neno la Mungu, ambalo kwalo mwanadamu anaishi. Katika mambo yote ya maisha haya ya sasa, uaminifu wangu hautatikisika, kwani hapa kupoteza au kupata siyo suala la msingi katika masuala ya wokovu. Lakini wakati masuala ya umilele yanapohusika, Mungu hapendi kuwa mwanadamu ajisalimishe kwa mwanadamu. Kwa sababu kujisalimisha kama huko katika masuala ya kiroho ni ibada halisi, na ibada inapaswa kufanywa kwa Muumbaji pekee."—Ibid., b. 7, ch. 11.

Akiwa safarini kutoka Worms, mapokezi ya Luther yalikuwa mazuri zaidi kuliko wakati alipokuwa akisafiri kuelekea huko. Viongozi wa kuu wa kanisa walimkaribisha mtawa aliyekwa ametengwa na kanisa, na watakawala wa kiraia walimheshimu mtu ambaye mfalme alikuwa amemhukumu. Alibembelezwa ahubiri, na, licha ya marufuku ya mfalme, alipanda tena kibwetani. "Sikuwahi kuahidi kulifunga minyororo neno la Mungu," alisema, "wala sitafanya hivyo."—Martyn 1:420.

Muda mfupi baada ya kuondoka Worms, wafuasi wa papa walimzidi nguvu mfalme naye alitoa amri dhidi ya Luther. Katika amri hii Luther alitangazwa kuwa "Shetani mwenyewe katika umbo la mwanadamu na aliyevaa vazi la kitawa."—D'Aubigne, b. 7, ch. 11. Iliagizwa kuwa mara tu cheti chake cha hakikisho la usalama kikiisha muda wake, hatua stahiki zichukuliwe kusitisha kazi yake. Watu wote walikatazwa kumtunza, kumpa chakula wala maji ya kunywa, au kwa njia ya neno au tendo, iwe hadharani au faraghani, kumsaidia au kumwunga mkono. Alitakiwa kukamatwa mahali popote ambapo angepatikana, na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola. Wafuasi wake pia walitakiwa kufungwa gerezani na mali zao kufilisiwa. Maandishi yake yalipaswa kuteketezwa, na, hatimaye, wote ambao wangethubutu kukaidi amri hii waliunganishwa katika hukumu ile. Elekta wa Saxony na viongozi katika ufalme waliokuwa marafiki wa Luther walikuwa wameondoka Worms mara tu baada yay eye kuondoka, na amri ya mfalme ilipata idhini ya Baraza Kuu. Sasa wafuasi wa Roma walifurahi sana. Walidhani hatima ya Matengenezo ilikuwa imetiwa muhuri.

Mungu alitengeneza mlango wa kutokea kwa ajili ya mtumishi Wake katika saa hii ya hatari. Jicho lisilosinzia lilimfuata Luther katika safari zake zote, na moyo wa kweli na safi ulikuwa umedhamiria kumwokoa. Ilionekana wazi kuwa Roama isingetulia na kuridhika bila kumwua Luther; kumficha ndiko peke yake kumwokoa na makanwa ya simba. Mungu alimpa hekima Frederick wa Saxony ya kubuni mpango wa kumhifadhi Mwanamatengenezo. Kwa ushirikiano na marafiki wa kweli kusudi la Fredrick lilitekelezwa, na Luther kweli alifichwa mahali ambapo marafiki na maadui wake hawakuweza kumfikia. Alipokuwa njiani kuelekea nyumbani alikamatwa, akatengwa na wasaidizi wake, na kwa haraka alipitishwa mstuni hadi katika jumba lililoko Wartburg, katika ngome iliyotelekezwa mlimani.

Kukamatwa kwake na kufichwa kwake kulifanywa kwa siri sana kiasi kwamba hata Frederick mwenyewe kwa muda mrefu hakujua ni wapi alikopelekwa. Kutojua huku hakukuwa kwa bahati mbaya; kwa kadiri Fredrick alivyokuwa hajui mahali Luther alipo, asingeweza kusema chochote juu yake. Alijiridhisha kuwa Mwanamatengenezo yuko salama, na kwake kujua hilo kulimfanya aridhike. Masika, kiangazi, na wakati wa joto ulipita, na wakati wa baridi ulifika, na Luther bado alibaki kuwa mfungwa. Aleanda na wafuasi wake walishangilia kwa kuwa nuru ya injili ilionekana kuzimika.

Lakini badala yake, Mwanamatengenezo alikuwa anajaza taa yake mafuta kutoka katika ghala la ukweli; na nuru yake ilikuwa inaenda kuangaza kwa mng'aro mkubwa zaidi. Katika usalama wa kirafiki wa ngome ya Wartburg, Luther kwa muda alifurahia kuwa mbali na joto na vurugu za vita. Lakini hakuridhika kuishi kwa muda mrefu katika ukimya na mapumziko. Kama mtu aliyezoea maisha ya shughuli na misuguano mikali, asingeweza kuishi maisha ya kukaa tu. Katika siku zile za kujitenga hali ya kanisa iliinuka mbele yake, na alilia katika hali ya kukata tamaa: "Hivi kweli! Hakuna mtu katika siku za hivi karibuni wa hasira Yake, wa kusimama kama ukuta mbele ya Bwana, na aokoe Israeli!"— Ibid., b. 9, ch. 2.

Kwa mara nyingine tena, mawazo yake yalirudi kwake yeye mwenyewe, na aliingiwa na hofu ya kushtakiwa kwa woga kwa kukimbia mapambano. Ndipo alijidharau yeye mwenyewe kwa uvivu wake na kupenda kwake kufurahisha nafsi yake. Lakini wakati huo huo alikuwa kila siku akifanya kazi nyingi zaidi ya zile ambazo mtu mmoja angeweza kufanya. Kalamu yake haikukaa kivivu. Wakati maadui zake wakijidanganya kuwa alikuwa amenyamazishwa, walishangaa na kuchanganyikiwa walipopata ushahidi mbashara kuwa alikuwa bado kazini. Idadi kubwa ya vijizuu, vilivyotokana na kalamu yake, vilikuwa vimesambaa katika nchi nzima ya Ujerumani. Alifanya pia huduma muhimu kuliko zote kwa watu wake wa Ujerumani kwa kutafsiri Agano Jipya katika lugha ya Kijerumani. Kutoka katika Patmo yake ya miamba aliendelea kwa karibu mwaka mzima kuhubiri injili na kukemea dhambi na makosa ya wakati wake.

Lakini ilikuwa siyo tu kumhifadhi Luther dhidi ya hasira za maadui zake, wala kumwezesha kuwa na wakati wa ukimya kwa ajili ya kazi hizi, kuwa ndiyo sababu pekee za Mungu kumwondoa mtumishi Wake kwenye jukwaa la maisha ya hadharani. Kulikuwepo na matokeo yenye thamani kubwa zaidi kuliko haya ambayo yangeweza kupatikana. Katika upweke na maficho ya mapumziko yake ya mlimani, Luther alikuwa ametengwa na misaada ya kidunia na kufungiwa mbali na sifa za kibinadamu. Kwa hiyo aliokolewa kutoka katika hatari ya kuwa na kiburi na kujitumainia, vitu ambavyo mara nyingi husababishwa na mafanikio. Kwa njia ya mateso na kunyenyekeshwa alikuwa ameandaliwa tena kutembea kwa usalama juu ya vilele smbavyo alikuwa ameinuliwa kwa ghafla.

Watu wanapofurahia uhuru ambao huletwa kwao kwa njia ya ukweli, wanakuwa na mwelekeo wa kuwasifu walee ambao Mungu anawatumia kuvunja minyororo ya makosa na

ushirikina. Shetani hutafuta kuondoa mawazo na mapenzi kutoka kwa Mungu, na kuyaelekeza kwa mawakala wa kibinadamu; huongoza watu kuheshimu chombo na kupuuza Mkono unaoelekeza matukio ya uongozi wa Mungu. Mara nyingi viongozi wa dini wanaosifiwa na kuheshimiwa hivyo hupoteza hitaji la kumtegemea Mungu na huongozwa kujitumainia wenyewe. Matokeo yake wanatafuta kutawala akili na dhamiri za watu, walio na mwelekeo wa kutafuta uongozi wao badala ya kutafuta uongozi wa neno la Mungu. Kazi ya matengenezo mara nyingi imedumaa kwa sababu ya roho hii ambayo inatawala ndani ya wale wanaounga mkono matengenezo. Mungu analinda kazi ya Matengenezo dhidi ya hatari hii. Alitamani kazi ile isipokee chapa ya mwanadamu bali chapa ya Mungu. Macho ya watu yalikuwa yameelekezwa kwa Luther kama mfafanuzi wa ukweli; aliondolewa ili macho yote yaelekezwe kwa Mwasisi wa milele wa ukweli.

Sura ya 9 - Mwanamatengenezo wa Kiswisi

Katika uchaguzi wa watu kwa ajili ya kutengeneza kanisa, mpango ule ule wa Mungu unaonekana kama ule unaoonekana katika kupanda kanisa. Mwalimu wa mbinguni aliwapita watu wakuu wa dunia, wenye vyeo, na wenye mali, waliokuwa wamezoea kupokea sifa na heshima kama viongozi wa watu. Walikuwa na kiburi na kujitumainia kwa sababu ya ukuu wao waliojivunia kiasi kwamba wasingeweza kuumbwa upya ili wawahurumie wanadamu wenzao na waweze kuwa watendakazi pamoja na Mtu mnyenyekevu wa Nazareti. Kwa wavuvi wa samaki, wasio na elimu, wanaohangaika wa Galilaya wito ulitolewa:"Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu"(Mathayo 4:19).

Wanafunzi hawa walikuwa wanyenyekevu na wanaofundishika. Kwa kadiri walivyokuwa wameathiriwa kidogo na mafundisho ya uongo ya wakati ule, ndivyo ilivyokuwa rahisi zaidi kwa Kristo kufanikiwa kuwafundisha na kuwaandaa kwa ajili ya huduma Yake. Kadhalika ndivyo ilivyokuwa katika siku za Matengenezo Makuu. Wanamatengenezo wakuu walikuwa watu waliotoka katika maisha ya chini—watu ambao hawakuwa wameathiriwa kwa wakati wowote na kiburi cha madaraka na mvuto wa itikadi kali na ujanja wa makasisi. Ni mpango wa Mungu kutumia vyombo dhaifu kufanikisha matokeo makubwa. Ndipo utukufu hautatolewa kwa wanadamu, bali kwake Yeye atendaye kupitia kwao kutaka na kutenda mapenzi Yake mema.

Majuma machache baada ya kuzaliwa kwa Luther katika kibanda cha mfanyakazi katika mgodi mjini Saxony, Ulric Zwingli alizaliwa katika nyumba ndogo ya mfugaji katika milima ya Alps. Mazingira ya Zwingli wakati wa utoto wake, na katika mafunzo yake ya awali, yalifaa kwa ajili ya maandalizi ya utume wake wa baadaye. Akiwa amelelewa katikati ya mandhari yenye kuvutia sana, uzuri, na fahari ya ajabu ya uoto wa asili, akili yake tangu awali iliguswa na hisia ya adhama, nguvu, na utukufu wa Mungu. Historia ya matendo ya kishujaa yaliyofanyika juu ya milima alipozaliwa iliwasha moto wa matarajio ya ujana wake. Na kando ya bibi yake mcha Mungu alisikiliza visa vichache vya thamani vya Biblia ambavyo Bibi yake aliviokoteza kutoka miongoni mwa hadithi za wahenga na mapokeo ya kanisa. Kwa shauku kubwa alisikia matendo makuu ya wazee na manabii, ya wachungaji waliochunga kwa zamu mifugo yao kwenye vilima vya Palestina ambapo malaika waliongea nao, kuhusu mtoto mchanga wa Bethlehemu na juu ya Mtu wa Kalwari.

Kama John Luther, baba yake Zwingli alikuwa na shauku ya elimu kwa ajili ya mwanae, na kijana alipelekwa shule mapema kutoka katika bonde lake alikozaliwa. Akili yake ilikua haraka, na haukupita muda mrefu swali likawa ni wapi pa kupata walimu wenye uwezo wa kumfundisha. Akiwa na umri wa miaka kumi na tatu alikwenda Bern, mji ambao wakati huo ulikuwa na shule bora katika nchi ya Switzerland. Hapa, hata hivyo, hatari iliibuka ambayo ilitishia kutia doa ahadi yake ya maisha. Juhudi za makusudi zilifanywa na watawa kumshawishi aingie katika nyumba ya watawa. Watawa wa Kidominika na wale wa

Kifransiskani walishindana katika kutafuta kukubalika na kupendwa. Kufikia azma hii walijitahidi kwa kuweka mapambo yanayovutia katika makanisa yao, madoido katika sherehe zao, na vivutio vya mifupa ya watu maarufu na sanamu zilizodaiwa kutenda miujiza. Wadominika wa Bern waliona kuwa ikiwa wangeweza kumpata kijana huyu mwenye karama nyingi na msomi, wangepata mapato na heshima.

Ujana wake, uwezo wake wa asili kama msemaji na mwandishi, na uwezo mkubwa katika muziki na ushairi, vingeweza kuleta mafanikio makubwa zaidi kuliko madoido na maonesho yao, katika kuwavuta watu na kuwaingiza katika huduma zao na kuongeza mapato ya shirika lao. Kwa njia ya udanganyifu na sifa za uongo walijaribu kumshawishi Zwingli aingie jumuia yao ya utawa. Luther, akiwa mwanafunzi shuleni, alijifungia katika chumba cha nyumba ya watawa, na ilikuwa apotee na asionekane ulimwenguni kama isingekuwa kwa uongozi wa Mungu kuingilia kati na kumtoa nje. Zwingli hakuruhusiwa kukutana na hatari hiyo. Kwa uongozi wa Mungu baba yake alipata habari ya mipango ya watawa. Hakuwa na nia ya kumruhusu mwanae afuate maisha ya kivivu na yasiyo na thamani ya watawa. Aliona kuwa utumishi wake wa thamani wa baadaye ulikuwa hatarini, na aliagiza arudi nyumbani haraka.

Agizo ilitiiwa; lakini kijana hakuweza kuridhika kukaa muda mrefu katika makazi yao ya bondeni, na haukupita muda mrefu alirudi masomoni kwake, akihamia, baada ya muda mfupi, katika mji wa Basel. Ni hapa ambapo kwa mara ya kwanza Zwingli alisikia injili ya neema ya Mungu ya bure. Wittembach, mwalimu wa lugha za kale, wakati akijifunza Kigiriki na Kiebrania aliongozwa kujifunza Maandiko Matakatifu, na hivyo miale ya nuru itokayo kwa Mungu iliangazia akili za wanafunzi aliokuwa akiwafundisha. Alisema kuwa kulikuwa na ukweli wa zamani zaidi, na wenye thamani kubwa zaidi, kuliko nadharia zilizofundishwa na walimu na wanafalsafa. Ukweli huu wa zamani ulikuwa kwamba kifo cha Kristo ni fidia pekee ya mwenye dhambi. Kwa Zwingli maneno haya yalikuwa ni mwale wa kwanza wa nuru inayotangulia mapambazuko.

Zwingli aliitwa baada ya muda mfupi kutoka Basel kwenda kuanza kazi yake ya maisha. Eneo lake la kwanza la kazi lilikuwa parishi ya Alpine, ambapo siyo mbali sana na bondeni alikozaliwa. Baada ya kuwekewa mikono ya wakfu wa ukasisi, "alijiweka wakfu kwa moyo wake wote kuchunguza ukweli wa Kimungu; kwani alijua kikamilifu," alisema Mwanamatengenezo mwenzake, "ni kiasi gani ilimpasa kujua yule ambaye kwake kondoo wa Kristo walikuwa wameaminiwa."—Wylie, b. 8, ch. 5. Kwa kadiri alivyochunguza Maandiko, alizidi kuona kwa uwazi zaidi tofauti kati ya ukweli wa Maandiko na uongo wa Roma. Alijisalimisha kwa Biblia kama neno la Mungu, kanuni pekee inayojitosheleza, isiyokosea. Aligundua kuwa ilipaswa kujitafsiri yenyewe. Hakuthubutu kueleza Maandiko kutetea nadharia au fundisho lililojulikana, bali alichukulia kuwa wajibu wake kujifunza kilicho cha wazi na kila fundisho lililo dhahiri. Alijitahidi kupata kila msaada alioweza kuupata wa kumwezesha kupata uelewa sahihi wa maana yake, na aliomba msaada wa Roho Mtakatifu,

ambao ungeweza, alisema, kulifunua kwa wale wote waliotafuta kwa moyo wa dhati na maombi mengi.

"Maandiko," alisema Zwingli, "yalitoka kwa Mungu, siyo kwa mtu, na hata hivyo Mungu anayeangazia atawapa ufahamu kuwa maneno hayo hutoka kwa Mungu. Neno la Mungu... haliwezi kushindwa; ni angavu, linajifundisha lenyewe, linajifunua lenyewe, linaangazia moyo juu ya wokovu wote na neema yote, linafariji moyo kwa msaada wa Mungu, linanyenyekesha moyo, kiasi kwamba moyo unajiachia na hata unajinyima wenyewe, na unamkumbatia Mungu." Ukweli wa maneno haya Zwingli mwenyewe alikuwa ameuthibitisha. Akizungumzia uzoefu wake wakati huu, aliandika baadaye: "Wakati ... nilipoanza kujitolea mwenyewe kujifunza Maandiko Matakatifu, falsafa na teolojia (kielimu) daima vilipendekeza migogoro kwangu. Hatimaye nilifikia hili, kuwa nilifikiri, 'Unapaswa kuachana na uwongo, na ujifunze maana ya Mungu kutokana na neno Lake sahili peke yake.' Ndipo nilianza kumwomba Mungu anipe nuru Yake, na Maandiko yalianza kuwa mepesi zaidi kwangu."—Ibid., b. 8, ch. 6.

Fundisho alilolihubiri Zwingli halikutoka kwa Luther. Lilikuwa fundisho la Kristo. "Ikiwa Luther anamhubiri Kristo," alisema Mwanamatengenezo wa Kiswisi, "anafanya kile ninachokifanya. Wale ambao amewaleta kwa Kristo ni wengi zaidi kuliko wale ambao mimi nimewaongoza. Lakini hili siyo muhimu. Sitashuhudia jina jingine zaidi ya lile la Kristo, ambaye mimi ni askari Wake, na ambaye Yeye ni Mkuu wangu. Sijawahi kuandika hata neno moja kwa Luther, wala Luther hajawahi kuniandikia. Na kwa nini? ... Ili ionekane jinsi ambavyo Roho wa Mungu ni Yule Yule, kwa kuwa sisi sote wawili, bila kufanya kazi pamoja, tunafundisha fundisho la Kristo linalofanana."—D'Aubigne, b. 8, ch. 9.

Mnamo mwaka 1516 Zwingli alialikwa kuwa mhubiri katika nyumba ya watawa jijini Einsiedeln. Hapa ndipo ambapo angeona kwa karibu ufisadi wa Kanisa la Roma na ndipo alikuwa anakwenda kuweka mvuto kama Mwanamatengenezo ambao ungeenda ng'ambo ya mipaka ya eneo lake la Alps. Miongoni mwa vivutio vya jiji la Einsiedeln ilikuwa sanamu ya Bikira ambayo ilisemekana kuwa ilikuwa na nguvu ya kutenda miujiza. Juu ya lango la nyumba ya watawa kulikuwa na maandishi, "Hapa ondoleo kamili la dhambi linaweza kupatikana."— Ibid., b. 8, ch. 5. Mahujaji nyakati zote walifika katika jengo la kumbukumbu la Bikira; lakini wakati wa sherehe ya kila mwaka ya kuwekwa wakfu kwake maelfu ya watu walifurika kutoka kona zote za Switzerland, na hata kutoka Ufaransa na Ujerumani. Zwingli, akiwa ameumizwa sana na kile alichokiona, alichukua fursa hiyo kutangaza uhuru upatikanao katika injili kwa hawa watumwa wa ushirikina.

"Msidhani," alisema, "kuwa Mungu yupo katika hekalu hili zaidi kuliko alivyo katika sehemu nyingine ya uumbaji. Haijalishi kuwa unaishi katika nchi gani, Mungu yuko pamoja nawe, na anakusikia. Je, inawezekana kazi zisizokuwa na manufaa, safari ndefu, sadaka, sanamu, kumwomba Bikira au kuwaomba watakatifu, kukupatia neema ya Mungu? Kuna

faida gani kuwa na maneno mengi katika maombi yetu? Kuna faida gani kuvaa kofia inayong'aa, kuwa na kichwa kilichonyolewa, kuvaa joho refu linalozagaa, au kuvaa kandambili zilizopakwa rangi ya dhahabu? Mungu anaangalia moyo, na mioyo yetu iko mbali Naye.""Kristo," alisema, "ambaye alitolewa mara moja juu ya msalaba, ni kafara na kondoo wa kafara, ambayo imetosheleza kwa ajili ya dhambi za waaminio wote milele zote."—Ibid., b. 8, ch. 5.

Kwa wasikilizaji walio wengi mafundisho haya hayakuwa ya kufurahisha. Lilikuwa jambo la kukatisha tamaa kwao kuambiwa kuwa safari yao ya kuchosha ilikuwa imefanyika bure. Msamaha uliotolewa bure kwao kwa njia ya Kristo hawakuweza kuuelewa. Walikuwa wameridhishwa na njia ya zamani ya kwenda mbinguni ambayo Roma ilikuwa imewaelekeza. Walisita kujiingiza katika mashaka ya kutafuta kitu kingine bora zaidi. Ilikuwa rahisi kwao kupata wokovu wao kupitia kwa makasisi na papa kuliko kutafuta usafi wa moyo.

Lakini tabaka lingine lilipokea kwa furaha habari za wokovu kwa njia ya Kristo. Maadhimisho yaliyofundishwa na Roma yalikuwa yameshindwa kuleta amani ya rohoni, na kwa imani waliipokea damu ya Mwokozi kama upatanisho wao. Hawa walirudi nyumbani kwao kuwafunulia wengine nuru ya thamani waliyokuwa wameipokea. Kwa njia hiyo ukweli ulipelekwa kutoka mtaa mmoja hadi mwingine, kutoka mji mmoja hadi mwingine, na idadi ya mahujaji wa hekalu la kumbukumbu ya Bikira ilipungua sana. Kulikuwepo kushuka kiasi kibaya kwa makusanyo ya sadaka, na matokeo yaliyoonekana hata kwenye mshahara wa Zwingli, ambao ulitokana na sadaka hiyo. Lakini jambo hili lilisababisha furaha tu kwake kwa kuona kuwa nguvu ya unafiki na ushirikina ilikuwa ikivunjwa.

Sio kwamba mamlaka za kanisa zilikuwa hazioni kazi ambayo Zwingli alikuwa anaifanya; lakini kwa muda huu waliacha kuingilia. Wakitumaini kuwa watamvuta mpaka awe upande wao, walijaribu kumshawishi kwa kutumia sifa za uongo; na wakati huo huo ukweli ulikuwa ukipata nguvu katika mioyo ya watu.

Kazi za Zwingli mjini Einsiedeln zilimuandaa kwa ajili ya eneo kubwa la kazi, kama alikuwa karibu kuanza kazi hiyo muda mfupi uliofuata. Baada ya miaka mitatu hapa aliitwa kufanya kazi ya mhubiri katika kanisa kuu la Zurich. Wakati ule huu ulikuwa mji muhimu kuliko miji yote katika shirikisho la Uswisi, na mvuto uliotolewa hapa uligusa kona nyingi za shirikisho. Viongozi wa dini waliokuwa wamemwita kuja Zurich walikuwa, hata hivyo, wakitamani kuzuia ubunifu wowote, na kweli walichukua hatua ya kumuelekeza majukumu yake.

"Utatumia kila juhudi," walisema, "kukusanya mapato kutoka kila chanzo, bila kupuuza hata chanzo kidogo sana. Utawahimiza waaminifu, kutoka katika kibweta na katika kizimba cha maungamo, kulipa zaka na kodi zote, na waoneshe sadaka zao na upendo wao kwa kanisa. Utakuwa na bidii katika kuongeza mapato yanayotokana na huduma kwa wagonjwa,

yanayotokana na misa, na kwa jumla yanayotokana na kila huduma ya kanisa." Waelekezaji wake walisema, "Kuhusiana na utoaji wa sakramenti, mahubiri, na utunzaji wa kundi, haya pia ni majukumu ya mlezi wa kiroho. Lakini kwa ajili ya haya unaweza kutumia mtu mbadala, na hususani katika kuhubiri. Inakupasa kugawa sakramenti kwa watu wanaoeleweka tu, na pale tu unapoalikwa; unakatazwa kufanya hivyo bila kutofautisha watu."—Ibid., b. 8, ch. 6.

Zwingli alisikiliza maelekezo haya akiwa kimya, na katika kujibu, baada ya kutoa shukurani zake kwa heshima ya kuitwa kuhudumu katika kituo hiki muhimu, aliendelea kueleza mwelekeo aliokuwa anakusudia kuuchukua. "Maisha ya Kristo," alisema, "kwa muda mrefu yamefichwa mbali na watu. Nitahubiri juu ya kitabu chote cha Injili ya Mathayo Mtakatifu, ... nikichota kutoka katika Maandiko pekee, nikizama katika vina vyake, nikilinganisha aya moja na nyingine, na nikitafuta ufahamu kwa maombi ya kudumu na ya dhati. Ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwa ajili ya sifa ya Mwana Wake pekee, kwa ajili ya wokovu halisi wa roho, na kwa ajili ya kuwajenga katika imani ya kweli, kwamba nitaiweka wakfu huduma yangu."— Ibid., b. 8, ch. 6.

Pamoja na kuwa baadhi ya viongozi wa kanisa hawakukubaliana na mpango wake, na walijaribu kumshawishi aachane nao, Zwingli alisimama imara. Alisema kuwa hakukusudia kuanzisha mbinu mpya, bali mbinu ya zamani iliyotumiwa na kanisa la awali na nyakati safi.

Tayari shauku ilikuwa imeamshwa kwa ajili ya ukweli alioufundisha; na watu walifurika katika idadi kubwa kusikiliza mahubiri yake. Wengi wa wale waliokuwa wameacha kuhudhuria ibada walikuwa miongoni mwa wasikilizaji wake. Alianza huduma yake kwa kufungua Injili na kusoma na kueleza kwa wasikilizaji wake visa vilivyovuviwa vya maisha, mafundisho, na mauti ya Kristo. Hapa, kama ilivyokuwa kule Einsiedeln, aliwasilisha neno la Mungu kama mamlaka pekee isiyokosea na mauti ya Kristo kama kafara pekee kamilifu. "Ni kwa Kristo," alisema, "ambapo ninatamani kuwaongoza— kwa Kristo, chanzo cha kweli cha wokovu."—Ibid., b. 8, ch. 6.

Watu wa matabaka mbalimbali walimzunguka mhubiri, tangu viongozi wakuu wa nchi na wasomi hadi mafundi na wakulima wadogo. Kwa shauku kubwa walisikiliza maneno yake. Siyo kuwa alitangaza toleo la wokovu wa bure, lakini pia bila hofu alikemea maovu na ufisadi wa nyakati zile. Wengi walitoka kanisani wakimtukuza Mungu. "Mtu huyu," walisema, "ni mhubiri wa ukweli. Atakuwa Musa wetu, atuongoze kutoka katika Misri hii ya giza."— Ibid., b. 8, ch. 6.

Lakini ingawa mwanzoni kazi zake zilipokelewa kwa furaha, baada ya muda upinzani uliibuka. Watawa walijipanga kuzuia kazi yake na kukosoa mafundisho yake. Wengi walimshambulia kwa kebehi na dhihaka; wengine walimshambulia kwa dharau na vitisho. Lakini Zwingli aliyabeba yote hayo kwa uvumilivu, akisema:"Ikiwa shauku yetu ni

kuwashinda waovu kwa ajili ya Yesu Kristo, ni lazima tufumbe macho yetu dhidi ya mambo mengi."— Ibid., b. 8, ch. 6.

Mnamo wakati huu, mtendakazi mpya alikuja kuendeleza kazi ya matengenezo. Mtu mmoja aitwaye Lucian alitumwa kutoka Zurich na rafiki wa mwana matengenezo aliyeishi Basel, akiwa na machapisho ya Luther, ambaye alipendekeza kuwa uuzaji wa vitabu hivi ungekuwa njia kubwa ya kutawanya nuru. "Hakikisha," aliandika Zwingli, "kuwa mtu huyu na busara na ujuzi wa kutosha; ikiwa yuko hivyo, mruhusu avichukue kutoka jiji hadi jiji, kutoka mji hadi mji, kutoka kijiji hadi kijiji, hata kutoka nyumba hadi nyumba miongoni mwa Waswisi, kazi za Luther, na hasahasa ufafanuzi wake wa Sala ya Bwana ulioandikwa kwa ajili ya walei. Kwa kadiri kazi hizi zitakavyojulikana, ndivyo watakavyopata wanunuzi wengi zaidi."—Ibid., b. 8, ch. 6. Kwa njia hiyo nuru iliweza kuingia.

Wakati Mungu anapoandaa kuvunja vifungo vya ujinga na ushirikina, ndipo Shetani hufanya kazi kwa nguvu nyingi zaidi kuwafunika watu kwa giza na kuwafunga minyororo kwa nguvu zaidi. Watu walipokuwa wakiinuka katika nchi mbalimbali kuwaletea watu ujumbe wa msamaha na kuhesabiwa haki kwa njia ya damu ya Kristo, Roma aliendelea kwa nguvu mpya kufungua masoko yake katika nchi zote za Kikristo, kuuza msamaha kwa pesa.

Kila dhambi ilikuwa na bei yake, na watu walipewa leseni ya bure kwa ajili ya uhalifu ikiwa hazina ya kanisa ilijazwa vizuri kwa pesa. Kwa hiyo, harakati mbili ziliendelea,—moja ikitoa msamaha wa dhambi kwa pesa, na nyingine msamaha kwa njia ya Kristo,—Roma ikitoa leseni ya dhambi na kufanya jambo hilo kuwa chanzo cha mapato; Wana matengenezo wakishutumu dhambi na kuwaelekeza watu kwa Kristo kama mpatanishi na mkombozi.

Katika nchi ya Ujerumani kazi ya uuzaji wa vyeti vya msamaha walikabidhiwa watawa wa Kidominika na waliongozwa na Tetzel mkorofi. Katika nchi ya Switzerland biashara hiyo iliwekwa katika mikono ya Wafransiskani, chini ya uongozi wa Samson, mtawa Muitaliano. Samson alikuwa tayari amefanya kazi kubwa kwa kanisa, akiwa amepata fedha nyingi kutoka Ujerumani na Switzerland kujaza hazina ya papa. Sasa alitembelea nchi nzima ya Uswisi, akivutia makundi makubwa ya watu, akiwanyang'anya wakulima maskini mapato yao madogo, na akidai zawadi kubwa kutoka kwa matabaka ya kitajiri. Lakini mvuto wa matengenezo tayari ulikuwa umegusa watu wengi na ulipunguza, japokuwa haukukomesha kabisa, biashara hiyo. Zwingli alikuwa bado yuko Einsiedeln wakati Samson, mara tu baada ya kuingia Switzerland, alifika na vyombo vyake katika mji jirani. Baada ya kuambiwa kusudio la ujio wa Samson, Mwana matengenezo alianza mara moja kumpinga. Hao watu wawili hawakukutana, lakini Zwingli alifanikiwa kuanika uongo wa Samson kiasi kwamba Samson alilazimika kuondoka na kwenda maeneo mengine.

Akiwa Zurich, Zwingli alihubiri kwa bidii dhidi ya wafanya biashara wa misamaha; na wakati Samson alipokaribia mji ule, alikutana na mjumbe kutoka katika baraza akiwa na

ujumbe wa Samson kuwa Samson alitarajiwa kupita na kuendelea na safari yake. Hata hivyo Samson alifanikiwa kuingia mjini kwa ujanja, lakini alifukuzwa kutoka katika mji bila kuuza hata msamaha mmoja, na mara baada ya hapo aliondoka katika nchi ya Uswisi.

Matengenezo yaliongezwa nguvu zaidi na ujio wa tauni, au Mauti Kuu, ambayo ilienea katika nchi nzima ya Uswisi katika mwaka 1519. Watu walipokutana uso kwa uso na mwuaji, wengi waliongozwa kujisikia jinsi misamaha waliyokuwa wameinunua hivi karibuni ilivyokuwa haina thamani na ilivyokosa maana; na walitamani kupata msingi wa uhakika zaidi kwa imani zao. Zwingli akiwa Zurich alipigwa na tauni kali sana; alizidiwa sana kiasi kwamba matumaini yote ya kupona kwake yaliisha kabisa, na taarifa ilienea kuwa alikuwa amekufa. Katika saa ile ya kujaribiwa, tumaini lake na ujasiri wake havikutetereka. Aliutazama msalaba wa Kalwari kwa imani, akitumainia upatanisho kamili kwa ajili ya dhambi. Aliporudi kutoka karibu na malango ya mauti, alikuwa na kazi moja tu ya kuihubiri injili kwa nguvu zaidi kuliko wakati wote uliopita; na maneno yake yalikuwa na nguvu isiyokuwa ya kawaida. Watu walimkaribisha kwa furaha mchungaji wao mpendwa, aliyerudishwa kwao kutoka ukingoni mwa kaburi. Wao wenyewe walikuwa wametoka kuhudumia wagonjwa na waliokuwa wanakufa, na walihisi, zaidi kuliko wakati mwingine wowote uliopita, thamani ya injili.

Zwingli alikuwa amefikia uelewa mkamilifu zaidi wa ukweli wa injili, na alikuwa amepata uzoefu mkamilifu zaidi ndani yake wa nguvu ya injili inayobadilisha. Kuanguka kwa mwanadamu na mpango wa wokovu yalikuwa masomo aliyochukua muda mwingi kujifunza. “Ndani ya Adamu,” alisema, “sisi sote tumekufa, tumezama katika ufisadi na tumehukumiwa.”— Wylie, b. 8, ch. 9. “Kristo ... alinunua kwa ajili yetu ukombozi usioisha. shauku Yake ni kafara ya milele, na uwezo usiokoma wa kuponya; inakidhi haki ya Kimungu ya milele kwa niaba ya wote wanaoitegemea kwa imani thabiti na isiyoyumba.” Hata hivyo alifundisha kwa uwazi kuwa siyo, kwa sababu ya neema ya Kristo, hawako huru kuendelea katika dhambi. “Mahali palipo na imani kwa Mungu, hapo yupo Mungu; na popote Mungu alipo, hapo kuna juhudi inayosihi na inayoshurutisha watu kutenda matendo mema.”— D’Aubigne, b. 8, ch. 9.

Shauku kwa ajili ya mahubiri ya Zwingli ilikuwa kubwa kiasi kwamba kanisa lilijaa hadi kufurika watu waliokuja kumsikiliza. Kidogo kidogo, kwa kadiri walivyoweza kuelewa, alifunua ukweli kwa wasikilizaji. Alikuwa mwangalifu kuanza kufundisha vipengele ambavyo vingewashtua na kuzalisha upinzani. Kazi yake ilikuwa kuongoa mioyo yao ipokee mafundisho ya Kristo, kuwalainisha kwa upendo Wake, na kuweka mbele yao mfano Wake; na baada ya kupokea kanuni za injili, imani na matendo ya ushirikina vingeshindwa hatimaye.

Hatua kwa hatua Matengenezo yalipanuka katika jiji la Zurich. Katika hali ya tahadhari maadui zake waliamka na kuanzisha upinzani. Mwaka mmoja kabla, mtawa wa Wittenberg alikuwa amesema “Hapana” kwa papa na mfalme pale Worms, na sasa kila kitu kilionekana

kuonesha kuhimili madai ya upapa pale Zurich. Mashambulizi mengi yalifanywa dhidi ya Zwingli. Katika maeneo ya upapa, mara kwa mara, wanafunzi wa injili waliuawa juu ya mti wenye ncha kali, lakini hii ilikuwa haitoshi; mwalimu wa uzushi lazima anyamazishwe. Hali kadhalika askofu wa Constance alituma wajumbe watatu wa Baraza la Zurich, akimshtaki Zwingli kwa kufundisha watu kuvunja sheria za kanisa, na hivyo kuhatarisha amani na utengemano katika jamii. Ikiwa mamlaka ya kanisa itapuuzwa, alisisitiza, uasi utatokea duniani kote. Zwingli alijibu kuwa amekuwa kwa miaka minne akifundisha injili katika jiji la Zurich, "ambayo imekuwa na ukimya na amani zaidi kuliko mji mwingine wowote katika shirikisho." "Siyo, kwamba," alisema, "Ukristo ni uhakikisho bora zaidi wa usalama kwa jumla?"—Wylie, b. 8, ch. 11.

Manaibu walikuwa wamewashauri wanabaraza waendelee kuwemo kanisani, ambamo, walisema, kulikuwa hakuna wokovu. Zwingli alijibu: "Hebu mashtaka haya yasiwatetemeshe. Msingi wa kanisa ni Mwamba ule ule, Kristo yule yule, ambao ulimpa Petro jina lake kwa sababu alimkiri kwa uaminifu. Katika kila taifa kila amwaminiye kwa moyo wake wote katika Bwana Yesu anakubaliwa na Mungu. Hapa, kwa kweli, ni kanisa, ambamo hakuna hata mmoja anayeweza kuokolewa."—D'Aubigne, London ed., b. 8, ch. 11. Kama matokeo ya mkutano huo, mmoja wa manaibu wa askofu aliipokea imani ya matengenezo.

Baraza lilikataa kuchukua hatua dhidi ya Zwingli, na Roma ilijiandaa kwa ajili ya mashambulizi mapya. Mwanamatengenezo alipojulishwa kuhusu mipango ya adui zake, alisema: "Acha waje; ninawaogopa kama vile mwamba uliotokeza juu ya bahari unavyoogopa mawimbi yanayounguruma kwenye nyayo zake."—Wylie, b. 8, ch. 11. Juhudi za viongozi wa kanisa zilisukuma mbele zaidi kazi ambayo walikuwa wakitafuta kuiangusha. Ukweli uliendelea kusambaa. Katika nchi ya Ujerumani, wafuasi wake, wakiwa wamenyong'onyea kwa sababu ya kutoweka kwa Luther, walipata ujasiri tena, walipoona maendeleo ya injili katika nchi ya Uswisi. Matengenezo yalipoimarika katika jiji la Zurich, matunda yake yalionekana kikamilifu katika kupungua kwa uhalifu na ongezeko la utulivu na utengamano."Amani imejaa tele katika mji wetu," aliandika Zwingli; "hakuna ugomvi, hakuna unafiki, hakuna wivu, hakuna migogoro. Wapi umoja kama huo unaweza kupatikana kama siyo kwa Bwana, na mafundisho yetu, yanayotujaza kwa matunda ya amani na upendo?" (Ibid., b. 8, ch. 15).

Ushindi ambao Matengenezo yaliupata uliwatetemesha viongozi wa Roma na kuwafanya waongeze juhudi za kuyashinda. Wakiona jinsi ambavyo mateso yalifaulu kidogo sana kudhibiti kazi ya Luther katika nchi ya Ujerumani, waliamua kupambana na matengenezo kwa kutumia salaha za wana matengenezo wenyewe. Walipanga kuwa na mdahalo na Zwingli, na kwa kuwa wao ndio waliosimamia mdahalo huo, wangejihakikishia ushindi kwa kuchagua, wao wenyewe, siyo tu mahali pa kufanyia mdahalo, bali pia waamuzi ambao wangeamua kati ya wao na Zwingli. Na ikiwa wangemnasa Zwingli na kumweka chini

ya mamlaka yao, wangehakikisha kuwa haponyoki. Ikiwa kiongozi angenyamazishwa, harakati ingevunjika mara moja kirahisi. Kusudi hili, hata hivyo, lilifichwa kwa uangalifu.

Mdahalo ulipangwa kufanyika katika mji wa Baden; lakini Zwingli hakuwepo. Baraza la Zurich, kwa kuhisi njama za wafuasi wa upapa, na kuonywa na marundo ya kuni ambazo zilikuwa zimekwisha washwa moto katika majimbo ya upapa kwa ajili ya wafuasi wa injili, walimkataza mchungaji wao asijipeleke katika hatari hii. Mjini Zurich alikuwa tayari kukutana na wafuasi ambao Roma ingepeleka; lakini kwenda Baden, mahali ambapo damu ya wafia dini kwa ajili ya ukweli ilikuwa imemwagwa siku za karibuni, ilikuwa kwenda katika kifo cha hakika. Okolampadio na Halla walichaguliwa kuwakilisha Wanamatengenezo, wakati Dkt. Eck, mtu mashuhuri, akisaidiwa na jopo la wasomi madaktari na maaskofu, ndiye alikuwa mwakilishi wa Roma.

Ingawa Zwingli hakuwepo katika mdahalo, nguvu yake ilihisiwa. Makatibu mhutasi wote walichaguliwa na wafuasi wa papa, na wengine walikatazwa wasiandike cho chote, kwa tishio la kifo. Pamoja na hayo, Zwingli alipokea kila siku maelezo kamili ya kile kilichosemwa kule Baden. Mwanafunzi aliyehudhuria kwenye mdahalo aliandika kila siku juu ya hoja zote zilizowasilishwa siku hiyo. Karatasi hizi zilipelekwa na wanafunzi wengine wawili, pamoja na barua za kila siku za Okolampadio, kwa Zwingli jijini Zurich. Mwanamatengenezo alijibu, akitoa ushauri na mapendekezo. Barua zake ziliandikwa usiku, na wanafunzi walirudi nazo Badeni asubuhi. Kukwepa kukamatwa na walinzi waliowekwa kulinda katika malango ya jiji, wajumbe hawa walileta makapu ya kuku vichwani mwao, na waliruhusiwa kupita bila kikwazo.

Kwa njia hiyo Zwingli aliendeleza vita na wapinzani wake. Zwingli "amefanya kazi zaidi," alisema Mikonio, "kwa kutafakari kwake, kukesha usiku, na ushauri alioupeleka Baden, kuliko ambavyo angefanya kwa kujadiliana uso kwa uso katikati ya maadui zake."—D'Aubigne, b. 11, ch. 13. Wafuasi wa Roma, wakiwa na matumaini makubwa ya kushinda, walikuja Baden wakiwa wamevaa majoho ya kifahari na wakimeremeta kwa vito vya thamani. Walikula kianasa, meza zao zilifurika vyakula vinono vya gharama kubwa na pombe kali na za bei kubwa. Mzigo wa majukumu yao ya kikanisa ulipunguzwa kwa burudani na sherehe. Mwonekano wa Wanamatengenezo ulikuwa kinyume kabisa, walionekana mbele ya watu kama kundi la omba omba, ambao chakula chao kidogo na cha kimaskini kiliwafanya wakae mezani kwa muda mfupi. Baba mwenye nyumba wa Okolampado, alipokwenda kumwangalia katika chumba chake, alimkuta mara nyingi akisoma au akiomba, na kwa mshangao mkubwa, alisema kuwa mzushi alikuwa angalau "mcha Mungu sana."

Kwenye mdahalo, "Kwa kiburi Eck alipanda kwenye mimbari iliyopambwa kifahari, wakati maskini Okolampadio, akiwa amevaa nguo za kimaskini, alilazimishwa kukaa mbele ya mpinzani wake kwenye kigoda kilichochongwa vibaya-vibaya."—Ibid., b. 11, ch. 13. Sauti kubwa ya Eck na kujiamini kusikokuwa na mipaka havijawahi. Juhudi zake zilichochewa na

tumaini la utajiri na umaarufu; kwa kuwa mtetezi wa imani alipewa malipo makubwa. Wakati hoja nzuri zaidi ziliposhindwa, alipaswa kutumia matusi, na hata laana.

Okolampadio, mtu mnyenyekevu na asiyejitumainia, alikuwa ameogopa mdahalo, na aliuingia akiwa na kiapo cha nguvu kuwa: "Sikubali kiwango kingine cha uamuzi zaidi ya neno la Mungu."—Ibid., b. 11, ch. 13. Ingawa alikuwa mpole na muungwana katika tabia, alithibitika kuwa na uwezo na asiyetetereka. Wakati wafuasi wa Uroma, kwa mujibu wa mazoea yao, walijielekeza kwenye mamlaka ya desturi za kanisa, Mwanamatengenezo alishikilia kikamilifu Maandiko matakatifu. "Desturi," alisema, "hazina nguvu katika nchi yetu ya Switzerland, labda tu kama zitaendana na katiba; sasa, katika masuala ya imani, Biblia ndiyo katiba yetu."— Ibid., b. 11, ch. 13.

Tofauti iliyojitokeza kati ya hawa washindani wawili wa mdahalo haikukosa kuwa na matokeo. Hoja ya Mwanamatengenezo iliyotolewa kwa utulivu, uwazi, upole na uungwana, ilikuwa na mvuto mkubwa zaidi kwa akili zilizokuwa zimechukizwa na maneno ya majigambo na kujikweza ya Eck.

Mdahalo uliendelea kwa siku kumi na nane. Ulipofungwa wafuasi wa upapa kwa kujiamini walidai kuwa wameshinda. Wengi wa manaibu waliungana na Roma, na Baraza Kuu lilitangaza kuwa Wanamatengenezo wamekwisha na walitangaza kuwa wao, pamoja na Zwingli, kiongozi wao, walikuwa wametengwa na kanisa. Lakini matunda ya mdahalo yalidhihirisha ni nani hasa walionufaika kutokana na mdahalo huo. Shindano lile lilizalisha ari kubwa katika kazi ya Uprotestanti, na haukupita muda mrefu baadaye majiji muhimu ya Bern na Basel yalitangaza kuunga mkono Matengenezo.

Sura ya 10 - Maendeleo ya Matengenezo Ujerumani

Kutoweka kwa siri kwa Luther kulileta wasiwasi katika nchi nzima ya Ujerumani. Maswali kumhusu yalisikika kila mahali. Uvumi mbaya ulisambazwa, na wengi waliamini kuwa alikuwa ameuawa. Kulikuwa na maombolezo makubwa, siyo tu kwa marafiki zake wa karibu, bali pia kwa maelfu ambao hawakuwa wameonesha kwa wazi msimamo wa kuwa upande wa Matengenezo. Wengi waliapa kwa kiapo kizito kuwa wangelipiza kisasi kwa ajili ya kifo chake.

Viongozi wa Roma waliona kwa hofu kiwango cha kuinuka kwa hisia za watu dhidi yao. Ingawa mwanzoni walifurahia kifo cha kudhania cha Luther, siyo muda mrefu walianza kutamani kujificha mbali na chuki ya watu. Maadui zake hawakusumbuliwa na matendo yake ya kijasiri kabisa wakati alipokuwa miongoni mwao kama wakati alipokuwa ameondolewa. Wale ambao katika hasira yao walitafuta kumwangamiza Mwanamatengenezo jasiri walijazwa na hofu wakati huu alipokuwa mateka asiyekuwa na msaada. "Njia pekee iliyobaki ya kujiokoa," mmoja alisema, "ni kuwasha mienge, na kumwinda Luther ulimwenguni kote, kumrudisha katika taifa ambalo linamwita."— D'Aubigne, b. 9, ch. 1. Amri ya mfalme ilionekana kutokuwa na nguvu. Wawakilishi wa papa walijazwa na hasira walipoona kuwa tamko hilo lilivuta usikivu mdogo sana kuliko tatizo lililompata Luther.

Habari kuwa alikuwa salama, japokuwa alikuwa mfungwa, zilituliza hofu za watu, wakati huo huo zikiamsha zaidi ari yao kwa ajili yake. Maandishi yake yalisomwa kwa shauku kubwa zaidi kuliko wakati mwingine wowote kabla. Idadi iliyokuwa ikiongezeka ya watu ilijiunga na kazi ya shujaa ambaye, wakati wa hatari kama ule, alilitetea neno la Mungu. Matengenezo yalikuwa daima yakipata nguvu. Mbegu aliyokuwa ameipanda Luther ilichipuka kila mahali. Kutokuwepo kwake kulifanya kazi ambayo kuwepo kwake kungeshindwa kuifanya. Watendakazi wengine walihisi wajibu mpya, kwa kuwa kiongozi wao mkuu alikuwa ameondolewa. Kwa imani na ari mpya walisonga mbele kufanya yote yaliyokuwa katika uwezo wao, ili kazi nzuri iliyokwisha kuanza isizuiliwe.

Lakini Shetani hakuwa amekaa kivivu. Sasa alijaribu kile ambacho amekuwa akijaribu kufanya katika kila msukumo wa matengenezo— kudanganya na kuangamiza watu kwa kuwaletea watu kitu bandia mahali pa kazi ya kweli. Kama vile kulivyokuwa na Makristo wa uongo katika karne ya kwanza ya kanisa la Kikristo, kadhalika kuliinuka manabii wa uongo katika karne ya kumi na sita.

Watu wachache, kwa kuathiriwa na msisimko katika ulimwengu wa kidini, walijidhania kuwa wamepokea ufunuo maalumu kutoka Mbinguni, na walidai kuwa walitumwa na Mungu kuendeleza mpaka mwisho Matengenezo ambayo, walisema, yalikuwa yameanzishwa na Luther kwa udhaifu. Kusema ukweli, walikuwa wanaharibu kazi ambayo alikuwa ameifanya. Walikataa kanuni kuu ambayo ilikuwa msingi halisi wa Matengenezo — kwamba neno la

Mungu ni kanuni inayojitosheleza ya imani na matendo; na badala ya mwongozo huo usiokosea waliweka kiwango kinachobadilika, kisichokuwa na uhakika cha hisia na mawazo yao. Kwa kitendo hiki cha kuweka kando mgunduzi mkuu wa makosa na uongo walimpa Shetani nafasi ya kutawala akili zao kwa kadiri alivyopenda mwenyewe.

Mmoja wa hawa manabii alidai kuwa alikuwa ameelekezwa na malaika Gabrieli. Mwanafunzi aliyekuwa ameungana naye aliacha masomo, akitangaza kuwa alipewa na Mungu Mwenyewe hekima ya kufafanua neno Lake. Wengine ambao kwa silika yao walikuwa na mwelekeo wa ushikiliaji sana wa jambo bila akili waliungana nao. Shughuli za watu hawa zilianzisha vurugu nyingi. Mahubiri ya Luther yalikuwa yameamsha watu kila mahali wahisi umuhimu wa matengenezo, na sasa baadhi ya watu ambao kwa kweli walikuwa waaminifu walipotoshwa na maagizo ya hawa manabii wapya.

Viongozi wa harakati hii walikwenda hadi Wittenberg ili kushinikiza madai yao kwa Melanchthon na watenda kazi wenzake. Walisema: “Tumetumwa na Mungu kuwafundisha watu. Tumefanya maongezi kwa karibu sana na Bwana; tunajua mambo yanayokuja; kwa kifupi, sisi ni mitume na manabii, na umwambie Dkt. Luther.”—Ibid., b. 9, ch. 7.

Wanamatengenezo walishitushwa na walichanganywa. Hili lilikuwa jambo ambalo walikuwa hawajawahi kukutana nalo, na hawakujua jambo la kufanya. Melanchthon akasema: “Hakika kuna roho zisizokuwa za kawaida ndani ya watu hawa; lakini ni roho gani? ... Upande mmoja, inatupasa tuwe makini tusimzimishe Roho wa Mungu, na upande mwingine, inatupasa tuwe makini tusipotoshwe na roho wa Shetani.”—Ibid., b. 9, ch. 7.

Haikuchukua muda tunda la fundisho jipya lilianza kuonekana. Watu waliongozwa kuipuuza Biblia au kuiacha kabisa. Shule ziliingizwa katika machafuko. Wanafunzi, wakipuuza kila kizuizi, waliacha masomo na kuondoka katika chuo kikuu. Watu waliojifikiria wenyewe kuwa na uwezo wa kuamsha na kuongoza kazi ya Matengenezo walifaulu kuyaleta karibu na ukingo wa kuyaharibu. Wafuasi wa Uroma sasa walirudisha ujasiri wao wakisema kwa furaha: “Pambano moja tu, na wote watakuwa wetu.”—Ibid., b. 9, ch. 7.

Luther akiwa jijini Wartburg, baada ya kusikia kilichokuwa kimetokea, alisema kwa huzuni kubwa: “Daima nilitegemea kuwa Shetani angetuma tauni hii.”—Ibid., b. 9, ch. 7. Alibaini tabia halisi ya watu waliojifanya manabii na sasa aliona hatari iliyohatarisha kazi ya ukweli. Upinzani wa papa na mfalme haukuwa umemletea wasiwasi na hofu kama alivyohisi sasa. Kutoka kwa watu waliojifanya kuwa marafiki wa Matengenezo kuliibuka maadui wake wakuu. Ukweli uliokuwa umemletea furaha kubwa na faraja ulitumiwa kuamsha migogoro na kuleta machafuko katika kanisa.

Katika kazi ya matengenezo, Luther alisukumwa na Roho wa Mungu kusonga mbele, na alipelekwa mbele zaidi ya vile alivyofikiria. Hakuwa amekusudia kuwa na misimamo

aliyokuja kuwa nayo hatimaye, au kuleta mabadiliko makubwa. Alikuwa tu chombo katika mkono wa Nguvu usiokuwa na Kikomo. Hata hivyo daima alitetemeka kwa sababu ya matokeo ya kazi yake. Wakati fulani alisema: "Ikiwa ningejua kuwa fundisho lilikuwa limeujeruhi mtu mmoja, mtu mmoja tu, hata kama ni mtu wa chini na asiyejulikana,—jambo ambalo haliwezekani, kwa kuwa ni injili yenyewe,— ingekuwa bora nife mara kumi zaidi kuliko kuikana."— Ibid., b. 9, ch. 7.

Na sasa Wittenberg wenyewe, ambao ulikuwa kitovu cha Matengenezo, ulikuwa unatekwa na nguvu ya msimamo mkali na uvunjaji wa sheria. Hali hii ya kutisha haikutokana na mafundisho ya Luther; lakini katika nchi ya Ujerumani maadui zake walikuwa wakimlaumu kwa machafuko haya. Katika uchungu wa roho wakati mwingine aliuliza: "Je, inawezekana, hivyo basi, kuwa suala hili litaleta mwisho wa kazi kubwa ya Matengenezo?"— Ibid., b. 9, ch. 7. Hali kadhalika, alipopambana na Mungu katika maombi, amani ilibubujika ndani ya moyo wake. "Kazi siyo yangu, bali ni Yako," alisema; "Wewe hutaruhusu kazi ya injili iharibiwe na ushirikina na misimamo ya itikadi kali." Lakini wazo la kuwa mbali na migogoro katika mazingira kama hayo, lilionekana kuwa halifai. Alidhamiria kurudi Wittenberg.

Bila kuchelewa alianza safari yake ya hatari. Alikuwa chini ya marufuku ya mfalme. Maadui walikuwa na uhuru wa kumwua; marafiki walikuwa wamekatazwa kumsaidia au kumlinda. Serikali ya kifalme ilikuwa ikichukua hatua kali sana dhidi ya wafuasi wake. Lakini aliona kuwa kazi ya injili ilikuwa hatarini, na katika jina la Bwana aliondoka bila woga kwenda kupigana vita kwa ajili ya ukweli.

Katika barua kwa elekta, baada ya kueleza kusudi lake la kuondoka Wartburg, Luther alisema: "Ninakujulisha mfalme mkuu kuwa ninaenda Wittenberg chini ya ulinzi mkubwa zaidi kuliko ulinzi wa wakuu na maelekta wa kidunia. Ninafikiri sihitaji msaada wako, na wala sihitaji ulinzi wake, badala yake nitajilinda mwenyewe. Kama ningejua kuwa ungeweza kulinda watu, nisingekwenda kabisa Wittenberg. Hakuna upanga unaoweza kupeleka mbele zaidi kazi hii. Mungu peke Yake lazima afanye kila kitu, bila msaada au ukubali wa mtu. Yeye aliye na imani kubwa kuliko wote ni yeye anayeweza zaidi kulinda."—Ibid., b. 9, ch. 8.

Katika barua ya pili, iliyoandikwa akiwa njiani kuelekea Wittenberg, Luther aliongeza: "Niko tayari kukukasirisha wewe mfalme na kuukasirisha ulimwengu wote. Kwani wakazi wa Wittenberg siyo kondoo wangu? Kwani si Mungu amewaweka katika utunzaji wangu? Na siwajibiki, ikiwa lazima, kukabiliana na kifo kwa ajili yao? Kando ya hayo, ninaogopa kuona mlipuko wa ugonjwa wa kutisha katika nchi ya Ujerumani, ambao kwao Mungu ataliadhibu taifa letu."—Ibid., b. 9, ch. 7.

Kwa tahadhari na unyenyekevu mkubwa, lakini kwa uamuzi na uimara, alianza kazi yake. "Kwa neno," alisema, "ni lazima tushinde na tuharibu kile ambacho kimewekwa kwa

ukatili. Sitatumia nguvu dhidi ya washirikina na wasioamini. Hakuna mtu atakayelazimishwa. Uhuru ni kiini hasa cha imani."—Ibid., b. 9, ch. 8.

Haukupita muda mrefu taarifa zilienea katika jiji lote la Wittenberg kuwa Luther amerudi na kuwa angehubiri. Watu walifurika kutoka pande zote, na kanisa lilijaa hadi likafurika. Alipopanda mimbarani, kwa hekima na upole mwingi alifundisha, alishauri, na alikosoa. Akigusia njia ya baadhi ambao walikuwa wameanza kutumia vurugu katika kukomesha misa, alisema:

"Misa ni kitu kibaya; Mungu anapingana nayo; inapaswa kukomeshwa; na ningefurahi kuwa katika ulimwengu wote ingebadilishwa na mahali pake iwekwe Meza ya Bwana ya injili. Lakini tafadhali asiwepo mtu ye yote atakayeachanishwa nayo kwa nguvu. Inatupasa kuliacha jambo hilo mikononi mwa Mungu. Inapasa neno lake lifanye kazi, na siyo sisi. Na kwa nini iwe hivyo? Utaniuliza. Kwa sababu sishikilii mioyo ya watu mkononi mwangu, kama vile ambavyo mfinyanzi anavyoshikilia udongo. Tunayo haki ya kusema: hatuna haki ya kutenda. Sisi tuhubiri; yaliyobaki ni ya Mungu. Nikitumia nguvu, ninapata nini? Mkunjo wa uso, urasmi, uigizaji, kanuni za kibinadamu, na unafiki. Lakini hakutakuwa na udhati wa moyo, wala imani, wala upendo. Mahali ambapo mambo haya matatu yanakosekana, vyote vinakosekana, na siwezi kuwekeza juhudi zangu katika shughuli yenye matokeo kama hayo Mungu anatenda zaidi kwa njia ya neno Lake pekee kuliko mimi na wewe na ulimwengu wote kuunganisha nguvu zetu. Mungu anashika moyo; na moyo unapochukuliwa, vyote vimepatikana....

"Nitahubiri, nitajadili, na nitaandika; lakini sitamlazimisha ye yote, kwa kuwa imani ni tendo la hiari. Angalia nilichokifanya. Nilisimama dhidi ya upapa, vyeti vya msamaha, na wafuasi wa upapa, lakini bila fujo au vurugu. Niliwasilisha neno la Mungu; Nilihubiri na niliandika—haya ndiyo niliyoyafanya. Na nilipokuwa nimesinzia, ... neno nililokuwa nimelihubiri liliushinda upapa, na hakuna mkuu au mfalme aliyeliletea madhara makubwa neno la Mungu. Na sikufanya jambo lolote; neno la Mungu lilifanya yote hayo. Ikiwa ningependa kutumia nguvu, nchi yote ya Ujerumani labda pengine ingekuwa imefurika damu. Lakini matokeo yake yangekuwa nini? Uharibifu na ukiwa kwa wa mwili na roho. Kwa hiyo mimi nilikaa kimya, na nikaacha neno litembee ulimwenguni kote peke yake."—Ibid., b. 9, ch. 8.

Siku baada ya siku, kwa juma lote, Luther aliendelea kuhubiri makundi ya watu wenye shauku kubwa. Neno la Mungu lilivunja hirizi ya msisimko wa ushikiliaji sana mambo bila akili. Nguvu ya injili iliwarudisha watu waliokuwa wamepotoka na kuwaleta katika ukweli. Luther hakuwa na shauku ya kukutana na watu walioshikilia sana mambo bila akili ambao kazi yao ilikuwa imeleta madhara makubwa. Aliwajua kuwa ni watu waliokuwa hawana uamuzi mzuri na mihemko isiyokuwa na nidhamu, ambao, wakati wakidai kuwa na ufunuo maalumu kutoka mbinguni, wasingestahimili kupingwa hata kidogo na wasingepokea onyo

au ushauri hata kama ungekuwa mzuri kiasi gani. Wakidai kuwa na mamlaka ya juu kabisa, walimtaka kila mmoja akiri madai yao bila maswali. Lakini, walipodai kuwa na mahojiano naye, alikubali kukutana nao; na alifanikiwa kuanika wazi maagizo yao kiasi kwamba walaghai wale waliondoka mara moja Wittenberg.

Ushikiliaji sana mambo bila akili ulidhibitiwa kwa muda; lakini miaka kadhaa baadaye ulilipuka tena na kuleta vurugu nyingi zaidi na matokeo ya kutisha zaidi: "Kwao Maandiko Matakatifu yalikuwa barua iliyokufa, na wote walianza kupiga kelele, 'Roho! Roho!' Lakini kwa hakika sitafuata kule roho yao inapowapeleka. Naomba Mungu kwa rehema Zake anitunze dhidi ya kanisa ambalo ndani yake kuna watakatifu pekee. Ninatamani kuishi na watu wanyenyekevu, wanyonge, wagonjwa, wanaojua na kuhisi dhambi zao, na wanaoumia na kumlilia Mungu daima kwa moyo wa dhati wapate faraja na msaada Wake."—Ibid., b. 10, ch. 10.

Thomas Munzer, mashuhuri sana kwa itikadi kali, alikuwa mtu mwenye uwezo kiasi fulani, ambao kama ungeelekezwa vizuri, ungemwezesha kutenda mema; lakini hakuwa amejifunza kanuni za kwanza za dini ya kweli. "Alikuwa na shauku ya kuutengeneza ulimwengu, na alisahau, kama watu wote wenye itikadi kali wanavyofanya, kuwa matengenezo yalipaswa yaanze na yeye mwenyewe."—Ibid., b. 9, ch. 8. Alikuwa na shauku kubwa ya kupata cheo na mvuto, na hakupenda awe wa pili, hata kwa Luther. Alitangaza kuwa Wanamatengenezo, kwa kuweka mamlaka ya Biblia badala ya papa, ilikuwa ni kuanzisha aina tofauti ya upapa. Yeye mwenyewe, alidai, alikuwa ametumwa na Mungu kuanzisha matengenezo ya kweli. "Aliye na roho hii," Munzer alisema, "ana imani ya kweli, ingawa asingeona Maandiko katika maisha yake."—Ibid., b. 10, ch. 10.

Walimu walioshikilia sana mambo bila akili walijielekeza kuongozwa na hisia, wakichukulia kila wazo na shauku kama sauti ya Mungu; matokeo yake walienda mbali sana katika imani yao. Baadhi walichoma Biblia, wakipiga kelele:"Neno linaua, lakini Roho inahuisha." Mafundisho ya Munzer yaliamsha shauku ya kupata mambo ya ajabu, huku yakifurahisha kiburi chao na kuweka mawazo na maoni ya kibanadamu juu ya neno la Mungu. Mafundisho yake yalipokelewa na maelfu ya watu. Alishutumu aina zote za utaratibu katika ibada ya hadhara, na alitangaza kuwa kutii viongozi wa serikali ilikuwa ni kujaribu kumtumikia Mungu na Beliali.

Akili za watu, tayari zikiwa zinaanza kutupilia mbali nira ya upapa, zilikuwa pia vikianza kukosa uvumilivu dhidi ya makatazo ya mamlaka za kiraia. Mafundisho ya kimapinduzi ya Munzer, akidai kuwa yalikuwa na kibali cha Mungu, yaliwaongoza kujitenga na utawala wa aina yo yote na kuruhusu kutawaliwa na chuki na tamaa. Mandhari za kutisha za uchochezi wa uasi na vurugu vilifuata, na maeneo ya Ujerumani yalitapakaa damu.

Maumivu makali ya rohoni ambayo Luther aliwahi kuyapata kabla akiwa katika mji wa Erfurt sasa yalimsonga yakiwa na nguvu iliyoongezeka mara mbili alipoona matokeo ya itikadi kali yakisababisha mashtaka dhidi ya Matengenezo. Viongozi wa upapa walisema—na wengi walikuwa tayari kuamini kauli—kuwa uasi ulikuwa tunda halisi la mafundisho ya Luther. Japokuwa shitaka hili halikuwa na msingi wowote, bado lilimsababishia dhiki kuu Mwanamatengenezo. Kwamba kazi ya ukweli iliaibishwa kwa kulinganishwa na itikadi kali, lilionekana kuwa jambo ambalo asingeweza kulistahimili. Kwa upande mwingine, viongozi wa uasi walimchukia Luther kwa sababu siyo tu kuwa alipinga mafundisho yao na kukana madai yao ya kuwa na uvuvio kutoka kwa Mungu, bali pia aliwaita waasi dhidi ya mamlaka za kiraia. Katika kulipiza kisasi walimshutumu kuwa mwigizaji mwovu. Ilionekana kana kwamba amejitengenezea mwenyewe maadui upande wa viongozi wa serikali na watu wa kawaida.

Wafuasi wa Roma walifurahia, wakitarajia kushuhudia anguko la haraka la Matengenezo; na walimlaumu Luther, hata kwa makosa ambayo yeye alijitahidi sana kuyasahihisha. Kundi la wenye itikadi kali, kwa madai ya uongo kuwa walikuwa wakidhulumiwa sana, walifanikiwa kupata huruma ya tabaka kubwa la watu, na, kama ilivyo mara nyingi kwa wale wanaokuwa upande ambao unashambuliwa, walichukuliwa kuwa kama wafia dini.

Hivyo, wale waliokuwa wakifanya kazi kwa nguvu kupinga Matengenezo walihurumiwa na walipongezwa kama wahanga wa ukatili na uonevu. Hii ilikuwa kazi ya Shetani, ikihimizwa na roho ile ile ya uasi iliyooneshwa kwanza mbinguni.

Shetani hutafuta daima kuwadanganya watu na kuwaongoza kuiita dhambi haki, na haki dhambi. Kazi yake imefanikiwa sana! Ni mara ngapi watumishi wa Mungu waaminifu hukosolewa na huaibishwa kwa sababu wanatetea ukweli bila hofu! Watu ambao kimsingi ni mawakala wa Shetani wanasifiwa na wanapongezwa, na hata wanatazamwa kama wafia dini, wakati ambao wangeheshimiwa na kutiwa moyo kwa sababu ya uaminifu wao kwa Mungu, wanaachwa kusimama peke yao, chini ya tuhuma na kutoaminiwa.

Utakatifu bandia, utakaso wa kuigiza, bado unafanya kazi yake ya uongo. Katika mifumo ya aina mbalimbali unaonesha roho ile ile kama ilivyokuwa katika siku za Luther, kuondoa akili za watu kutoka kwenye Maandiko na kuwafanya watu wafuate hisia na shauku zao kuliko kusalimisha utii wao kwa sheria ya Mungu. Hii ni moja ya mbinu za Shetani zenye mafanikio makubwa sana za kuaibisha usafi na ukweli.

Bila hofu Luther aliitetea injili dhidi ya mashambulizi yaliyotoka kila upande. Neno la Mungu lilionekana kuwa silaha yenye nguvu katika kila mgogoro. Kwa neno hilo alipigana dhidi ya mamlaka ya kujipachika ya upapa, na dhidi ya falsafa ya mantiki ya wasomi, wakati

alisimama imara kama mwamba dhidi ya ushikiliaji sana wa mambo bila akili uliotafuta kujiambatisha na Matengenezo.

Kila moja ya sekta hizi zinazopingana kila moja kwa njia yake ilikuwa ikiweka pembeni Maandiko Matakatifu na kuinua hekima ya mwanadamu kama chanzo cha ukweli na maarifa ya kidini. Falsafa mantiki huifanya mantiki kuwa sanamu ya kuabudu na huifanya kuwa kipimo cha dini. Uroma, ukidai kwa ajili ya kiongozi wao mkuu uvuvio ulioshuka katika mstari ulioshikamana tangu mitume, na usiobadilika nyakati zote, hutoa fursa maridhawa kwa kila aina ya ubadhirifu na ufisadi kufichwa chini ya utakatifu wa agizo la mitume. Uvuvio ambao Munzer na wenzake walidai kuwa nao ulitoka katika michakato ya fikra, na nguvu yake ilikuwa kinyume na mamlaka zote, za kibinadamu au za Kimungu. Ukristo wa kweli hupokea neno la Mungu kama nyumba kubwa ya hazina ya ukweli uliovuviwa.

Baada ya kurudi kutoka Wartburg, Luther alimaliza tafsiri yake ya Agano Jipya, na muda mfupi baada ya hapo injili ilitolewa kwa watu wa Ujerumani katika lugha yao wenyewe. Tafsiri hii ilipokelewa kwa furaha kubwa na wote walioupenda ukweli; lakini ilikataliwa kwa dharau na wale waliochagua mapokeo ya wanadamu na amri za wanadamu.

Makasisi walihofia wazo kuwa watu wa kawaida wangeweza sasa kubishana nao juu ya kanuni za neno la Mungu, na kuwa ujinga wa makasisi ungeanikwa kwa njia hiyo. Silaha zao za hoja za kimwili hazikuwa na nguvu dhidi ya upanga wa Roho. Roma ilitumia mamlaka zake zote kuzuia usambazaji wa Maandiko; lakini amri, laana, na maumivu vilikuwa bure. Kwa kadiri Roma ilivyozidi kushutumu na kupiga marufuku Biblia, ndivyo watu walivyojenga shauku kubwa zaidi ya kujua Biblia ilifundisha nini. Wote walioweza kusoma walitamani kujifunza neno la Mungu wao wenyewe. Waliibeba kila mahali walikokwenda, na walisoma na kusoma tena, na hakuridhika mpaka walipokariri sehemu kubwa ya Maandiko.

Alipoona jinsi watu walivyolipokea Agano Jipya kwa furaha, Luther alianza mara moja kutafsiri Agano la Kale, na alichapisha sehemu zake mara moja alipomaliza. Maandishi ya Luther yalipokelewa mahali pote, iwe mijini au vijijini. “Kilichoandikwa na Luther na marafiki zake, wengine walisambaza. Watawa, waliposhawishika kuwa matakwa ya maisha ya kitawa hayakuwa halali, kwa kutamani kubadilisha maisha yao ya kivivu ili waishi maisha ya kujishughulisha, lakini wakiwa hawajui jinsi ya kuhubiri neno la Mungu, walisafiri katika majimbo, wakitembelea mitaa na nyumba, ambapo waliuza vitabu vya Luther na marafiki zake. Kwa muda mfupi Ujerumani ilifurikan hawa wainjilisti wa vitabu jasiri.”—Ibid., b. 9, ch. 11.

Maandishi haya yalisomwa kwa shauku kubwa na matajiri na maskini, wasomi na wasio kuwa wasomi. Usiku walimu wa shule za vijijini waliwasomea kwa sauti makundi madogo

ya watu waliokusanyika kando ya moto. Kwa juhudi zote baadhi ya roho ziliuamini ukweli na, baada ya kupokea ukweli kwa furaha, ilikuwa zamu yao kuwaeleza wengine habari njema.

Maneno yaliyovuviwa yalithibitika: “Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga” (Zaburi 119:130). Kujifunza Maandiko kulileta badiliko kubwa katika akili na mioyo ya watu. Utawala wa kipapa ulikuwa umeweka juu ya wafuasi wake nira ya chuma iliyowafunga pamoja katika ujinga na umaskini. Uzingatiaji wa kishirikina wa taratibu ulisimamiwa kwa uangalifu; lakini katika huduma yao yote moyo na akili vilikuwa na sehemu ndogo sana. Mahubiri ya Luther, yaliyowasilisha ukweli wa wazi wa neno la Mungu, na halafu neno lenyewe, lililowekwa katika mikono ya watu wa kawaida, liliamsha akili zao zilizokuwa zimelala, siyo tu likisafisha na kuimarisha hali ya kiroho, bali pia likileta nguvu na uhai mpya wa akili.

Watu wa matabaka yote walionekana wakiwa na Biblia mikononi mwao, wakilinda mafundisho ya Matengenezo. Viongozi wa upapa waliokuwa wamewaachia mapadri na watawa kujifunza Maandiko waliwaita waje na kukanusha mafundisho hayo mapya. Lakini, kwa kutoyajua Maandiko na nguvu ya Mungu, viongozi wa upapa walishindwa kabisa na wale waliowashutumu kuwa wajinga na wazushi. “Kwa huzuni,” mwandishi wa Kikatoliki alisema, “Luther alikuwa amewashawishi wafuasi wake kutoamini kanuni yoyote kuliko Maandiko Matakatifu.”—D’Aubigne, b. 9, ch. 11.

Makundi ya watu walikusanyika kusikia ukweli uliowasilishwa na watu wenye elimu ndogo, na hata walipojadiliana na wasomi na wanateolojia wenye ufasaha. Ujinga wa kuaibisha wa hawa watu wakubwa ulifunuliwa wakati hoja zao zilipokutana na mafundisho sahili ya neno la Mungu. Vibarua, maaskari, wanawake, na hata watoto, waliyajua mafundisho ya Biblia zaidi ya mapadri na madaktari wasomi.

Tofauti kati ya wanafunzi wa injili na wapiga debe wa ushirikina wa kipapa ilikuwa wazi siyo tu miongoni mwa wasomi, bali pia miongoni mwa watu wa kawaida. “Tofauti na mabingwa wa zamani wa upapa, waliopuuza kujifunza lugha na stadi za fasihi, ... walikuwa vijana wenye akili za kiungwana, makini katika kujifunza, wakichunguza Maandiko, na wakijielimisha juu ya mambo ya kale yaliyomo katika vitabu vya watu mashuhuri. Wakiwa na akili ya kiutendaji, roho iliyoinuliwa, na mioyo jasiri, vijana hawa kwa muda mfupi walipata maarifa ambayo kwa muda mrefu hakuna mtu ambaye angeweza kushindana nao Kwa mantiki hiyo, wakati vijana hawa watetezi wa Matengenezo walipokutana na madaktari wasomi wa Kiroma katika kongamano lo lote, waliwashambulia kwa urahisi na kujiamini kiasi kwamba hawa watu wasiojua Maandiko walisita, waliudhika, na walidharaulika mbele ya watazamaji wote.”—Ibid., b. 9, ch. 11.

Viongozi wa Kiroma walipoona makanisa yao yalikuwa yakiishiwa watu, walitafuta msaada kwa mahakimu, na kwa kila njia iliyokuwa katika uwezo wao walijaribu kuwarudisha

wasikilizaji wao. Lakini watu walikuwa wamepata katika mafundisho mapya kile ambacho kilikidhi mahitaji ya roho zao, na waliachana kabisa na wale ambao kwa muda mrefu waliwalisha pumba zisizofaa za kaida za kishirikina na mapokeo ya wanadamu.

Mateso yalipowashwa dhidi ya walimu wa ukweli, walitii maneno ya Kristo: "Watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine" (Mathayo 10:23). Nuru ilipenya kila mahali. Wakimbizi waliweza kupata mahali fulani mlango wenye ukarimu uliofunguliwa kwa ajili yao, na wakiwepo hapo, walimhubiri Kristo, nyakati zingine kanisani, au, ikiwa walinyimwa fursa hiyo, katika nyumba binafsi au eneo la wazi. Mahali popote walipopata watu wa kuwasikiliza palikuwa hekalu takatifu. Ukweli, ulipotangazwa kwa nguvu na uhakika kama huo, ulienea kwa nguvu isiyopingika.

Bila mafanikio mamlaka za kikanisa na kiraia zilitumika kukomesha uzushi. Bila mafanikio walitumia vifungo magerezani, maumivu, moto, na upanga. Maelfu ya waumini waligonga muhuri imani yao kwa damu yao, na bado kazi iliendelea. Mateso yalikuwa kichocheo cha kuenea kwa ukweli, na unafiki ambao Shetani alijaribu kuungana nao uliishia katika kuleta tofauti kubwa zaidi kati ya kazi ya Shetani na kazi ya Mungu.

Sura ya 11 - Upinzani wa Wakuu wa Majimbo

Moja ya shuhuda za kujivunia zilizowahi kutolewa kuunga mkono Matengenezo ulikuwa upinzani uliotolewa na viongozi Wakristo wa Ujerumani katika Baraza la Spires la mwaka 1529. Ujasiri, imani, na uimara wa wale watu wa Mungu ulileta uhuru wa mawazo na dhamiri kwa vizazi vilivyofuata. Upinzani wao ndio uliololetea kanisa la matengenezo jina la Protestanti; kanuni zake ndizo "msingi halisi wa Uprotestanti."— D'Aubigne, b. 13, ch. 6.

Siku ya giza na ya kutisha ilikuwa imefika kwa Matengenezo. Licha ya Hukumu ya Worms, ikimtangaza Luther kuwa haramia na ikipiga marufuku kufundisha au kuamini mafundisho yake, uvumilivu wa kidini hadi wakati huo uliendelea kuwepo katika dola. Uongozi wa Mungu ulikuwa umedhibiti nguvu zilizopinga ukweli. Charles V alikuwa amejielekeza kukomesha Matengenezo, lakini mara nyingi alipoinua mkono wake kupiga alilazimishwa kugeuzia pigo pembeni. Tena na tena mara nyingi, mauaji yasiyoepukika ya watu waliothubutu kupinga Roma yalikuwa karibu kutekelezwa; lakini wakati mfupi kabla ya utekelezaji majeshi ya Uturuki yalitokea kwenye mpaka wa mashariki, au mfalme wa Ufaransa, au hata papa mwenyewe, kwa sababu ya wivu wa ukuu uliokuwa ukiongezeka wa mfalme, walifanya vita dhidi yake; na hivyo, katikati ya migogoro na vurugu za mataifa, Matengenezo yaliachwa kuimarika na kupanuka.

Hatimaye, hata hivyo, mamlaka za upapa zilimaliza migogoro yao, ili wawe na mwelekeo mmoja dhidi ya Wanamatengenezo. Baraza Kuu lililokaa Spires katika mwaka 1526 lilitoa kwa kila jimbo uhuru kamili katika masuala ya kidini mpaka mkutano wa Baraza Kuu; lakini mara tu baada ya hatari zilizosababisha kupewa uhuru huo kupita, mfalme aliitisha Baraza la pili katika mji wa Spires mwaka 1529 kwa kusudi la kukomesha uzushi. Wakuu wa majimbo walipaswa kushawishiwa, ikiwezekana kwa njia ya amani, waungane dhidi ya Matengenezo; lakini ikiwa mbinu hizi zingeshindwa, Charles alijiandaa kutumia upanga.

Wafuasi wa upapa walifurahi sana. Walikuja mjini Spires kwa idadi kubwa, na walionesha chuki yao wazi wazi kwa Wanamatengenezo na wote waliowaunga mkono. Alisema Melanchthon: "Sisi ni karaha na takataka za ulimwengu; lakini Kristo atawaangalia watu Wake wanyenyekevu, na atawatunza."—Ibid., b. 13, ch. 5. Wakuu wa majimbo waliokuwa wafuasi wa injili waliohudhuria katika Baraza walikatazwa kuruhusu injili kuhubiriwa hata katika makazi yao binafsi. Lakini watu wa Spires walikuwa na kiu kwa ajili ya neno la Mungu, na, licha ya kupigwa marufuku injili, maelfu walifurika kwenye huduma zilizoendeshwa katika kanisa la elekta wa Saxony.

Hili liliharakisha hali ya hatari. Ujumbe wa kifalme ulitangaza kwa Baraza kwamba kwa kuwa azimio lililotoa uhuru wa dhamiri lilikuwa limesababisha uasi mkuu, mfalme aliagiza lifutwe. Amri hii isiyokuwa na mantiki iliamsha hasira na hali ya tahadhari kwa Wakristo waaminio injili. Mmoja alisema: "Kristo ameangukia tena katika mikono ya Kayafa na

Pilato." Wafuasi wa Roma walianza tena kufanya fujo. Mfuasi wa papa mwenye msimamo mkali alisema: "Waturuki ni bora zaidi kuliko Walutheri; kwa kuwa Waturuki wanaadhimisha siku za funga, na Walutheri wanazivunja. Ikiwa inatupasa kuchagua kati ya Maandiko Matakatifu na makosa ya zamani ya kanisa, inatupasa kuacha Maandiko Matakatifu." Melanchthon alisema: "Kila siku, katika mkutano uliojaa watu, Faber alikuwa anarusha jiwe jipya kwa wafuasi wa injili."—Ibid., b. 13, ch. 5.

Uvumilivu wa kidini ulipitishwa kisheria, na majimbo yaliyoamini injili yaliazimia kupinga ukiukaji wa haki zao. Luther, akiwa bado chini ya katazo lililowekwa na Amri ya Worms, alikuwa haruhusiwi kuwepo Spires; lakini nafasi yake ilikuwa imejazwa na watendakazi wenzake na wakuu ambao Mungu alikuwa amewainua kutetea kazi Yake nyakati za \ dharura hii. Mheshimiwa Frederick wa Saxony, mtetezi wa zamani wa Luther, kifo kilikuwa kimemuondoa; lakini John, Mwana wa Mfalme, kaka na mrithi wake, aliyakaribisha Matengenezo kwa furaha, na wakati akiwa rafiki wa amani, alionesha nguvu na ujasiri mwingi katika mambo yote yaliyohusiana na maslahi ya imani.

Makasisi walidai kuwa majimbo yaliyokuwa yamekubali Matengenezo yajisalimishe kwa utawala wa Roma kimya kimya. Wanamatengenezo, kwa upande mwingine, walidai uhuru ambao ulikuwa umetolewa awali. Wasingeweza kukubali Roma iyalete chini ya utawala wake yale majimbo ambayo kwa furaha kubwa yalikuwa yamelipokea neno la Mungu.

Kama njia ya kupata mwafaka, hatimaye ilipendekezwa kuwa mahali ambapo Matengenezo hayakuwa yamepokelewa, Hukumu ya Worms itekelezwe kikamilifu; na kuwa "katika yale majimbo ambapo watu walikuwa wameikiuka, na mahali ambapo wasingeweza kuifuata bila hatari ya uasi, walitakiwa angalau wasiingize matengenezo mapya, wasiguse vipengele vinavyobishaniwa, wasipinge sherehe za misa, wasiruhusu Mromani Katoliki ajiunge na UlutheriLuther."—Ibid., b. 13, ch. 5. Uamuzi huu ulipitishwa na Baraza Kuu, na makasisi na maaskofu wa upapa waliridhika sana.

Ikiwa amri hii ingetekelezwa, "Matengenezo yasingeenea … mahali ambapo yalikuwa bado hayajulikani, wala yasingejengwa juu ya misingi imara ... mahali yalipokuwepo."—Ibid., b. 13, ch. 5. Uhuru wa kusema ungeharimishwa. Waongofu wapya wasingeruhusiwa. Na marafiki wa Matengenezo walitakiwa kujisalimisha kwa masharti na makatazo haya mara moja. Matumaini ya ulimwengu yalionekana kana kwamba yamezimwa. "Uhuishaji wa utawala wa Roma ... ungerudisha bila shaka maovu ya zamani;" na fursa ingepatikana kirahisi kwa ajili ya "kukamilisha uangamizaji wa kazi ambayo tayari ilikuwa imeshayumbishwa sana" na hali ya kuwa na itikadi kali na migawanyiko.—Ibid., b. 13, ch. 5.

Wakati kundi la wafuasi wa injili walipokutana ili kushauriana, kila mmoja alimwangalia mwenzake katika hali ya kuduwaa kabisa. Kutoka kwa mmoja hadi kwa mwingine swali hili

lilipita: “Ni jambo gani lifanyike?” Masuala mazito yanayohusu ulimwengu yalikuwa hatarini. “Je, viongozi wa Matengenezo wajisalimishe, na wakubaliane na hukumu? Ni rahisi kiasi gani Wanamatengenezo wangeweza wakati huu wa hatari, ambayo kwa kweli ilikuwa kubwa, kujenga hoja ya kuwapeleka katika njia potovu! Visingizio vilivyoeleweka vingapi na sababu zilizokubalika ngapi ambazo wangeweza kuzitoa ili wasijisalimishe! Viongozi wa Kilutheri walipewa uhakikisho wa uhuru wa kufuata dini yao.

Upendeleo huo huo walipewa pia watu wote waliokuwa chini ya utawala wao ambao, kabla ya kupitishwa uamuzi huo, walikuwa wameamini mitazamo ya kimatengenezo. Je, jambo hili isingepasa liwaridhishe? Ni hatari ngapi wangeziepuka kwa kujisalimisha! Ni hatari ngapi na migogoro mingapi ambayo upinzani wao ungewasababishia! Nani ajuaye fursa ambazo wangezipata baadaye? Hebu tuikumbatie amani; hebu tutafute tawi la mzeituni lililoinuliwa na Roma, na tufunike majeraha ya Ujerumani. Kwa hoja kama hizi, Wanamatengenezo wangeweza kufuata njia ambayo kwa hakika ingeweza, kwa muda mfupi, kuangamiza kazi yao ya matengenezo.

“Kwa furaha waliiangalia kanuni ambayo ilikuwa msingi wa mwafaka, na walitenda kwa imani. Kanuni hiyo ilikuwa ipi? Ilikuwa haki ya Roma kulazimisha na kudhibiti dhamiri na kupiga marufuku maswali huria. Lakini, Je, haikuwa haki yao wenyewe na raia zao Waprotestanti kuwa na uhuru wa kidini? Ndiyo, uhuru ulikuwepo, lakini, kama upendeleo uliowekwa katika mwafaka, na siyo kama haki yao. Lakini kwa wengine wote nje ya mwafaka, kanuni kuu ya mamlaka ilikuwa kutawala; dhamiri kutojaliwa; Roma ilikuwa jaji asiyekosea, na lazima itiiwe. Kukubaliana na mwafaka uliopendekezwa kungemaanisha kuwa uhuru wa kidini ubaki katika mji wa Saxony tu; mahali ambapo matengenezo yalikuwa yamekubaliwa na watu walio wengi; na kwa ulimwengu wa Kikristo uliosalia, kujifunza na kujiunga na imani ya matengenezo ilikuwa ni uhalifu, na ilikuwa lazima uhalifu huo adhibitiwe kwa kutupwa gerezani au kutundikwa juu ya mti wenye ncha kali.

Je, waridhie kuufanya uhuru wa dhamiri kuwa haki ya watu eneo moja tu? Yaani, itangazwe kuwa Imani ya Matengenezo imepata mwongofu wa mwisho? Kwamba imepata eka yake ya mwisho ya utawala? Na kwamba mahali popote Roma ilipokuwa imeweka mizizi yake kwa wakati ule, utawala wake ubaki hivyo milele zote? Je, Wanamatengenezo wangeweza kujitetea kuwa hawana hatia ya damu ya wale mamia kwa maelfu ambao, kwa utekelezaji wa mwafaka huo, ingewapasa kupoteza maisha yao katika nchi za upapa? Hii ingekuwa kusaliti, katika saa ile muhimu, kazi ya injili na uhuru wa ulimwengu wa Kikristo.”—Wylie, b. 9, ch. 15.

Ingekuwa heri kwao “kutoa kafara kila kitu, hata majimbo yao, miji yao, taji zao, na maisha yao.”— D’Aubigne, b. 13, ch. 5. “Tukatae amri hii,” walisema wakuu wa majimbo. “Katika masuala ya dhamiri kanuni ya wengi wape haina nguvu.” Manaibu walisema: “Ni amri ya mwaka 1526 ambayo imewezesha kuwepo kwa amani katika himaya: kuiondoa amri

hiyo kungeijaza Ujerumani kwa misuguano na migawanyiko. Mahakama haina mamlaka ya kufanya kitu cho chote zaidi ya kutunza uhuru wa dini mpaka Baraza Kuu likutane."—Ibid., b. 13, ch. 5. Kulinda uhuru wa dhamiri ni wajibu wa dola, na huu ndiyo mpaka wake katika masuala ya dini. Kila serikali yo yote ya kidunia inayojaribu kutunga au kutekeleza sheria za kidini kwa kutumia mamlaka za kiraia inavunja kanuni ambayo Wakristo wainjilisti wameipambania kwa gharama kubwa.

Wafuasi wa papa waliazimia kuangusha kile walichokiita "ukaidi usio na hofu." Walianza kwa kusababisha migawanyiko miongoni mwa watu waliounga mkono Matengenezo na kuwatisha wote ambao walikuwa bado hawajatangaza hadharani kuunga mkono Matengenezo. Wawakilishi wa miji huru hatimaye waliitwa mbele ya Baraza Kuu na walitakiwa kutangaza ikiwa walikuwa tayari kukubaliana na mapendekezo ya mwafaka. Waliomba wapewe muda, lakini hawakupewa muda. Walipojaribiwa, karibu nusu yao walichagua kuwa upande wa Wanamatengenezo. Waliokataa kukiuka uhuru wa dhamiri na haki ya uamuzi wa mtu binafsi walijua hakika kuwa msimamo wao ungewafanya wakosolewe, walaumiwe, na wateswe. Mjumbe mmoja alisema: "Inatupasa ama tulikane neno la Mungu, au—tuchomwe moto."— Ibid., b. 13, ch. 5.

Mfalme Ferdinand, mwakilishi wa mfalme mkuu kwenye Baraza Kuu, aliona kuwa amri hiyo ingesababisha migawanyiko mikubwa ikiwa wakuu wa majimbo hawatashawishiwa kuikubali na kuisimamia. Kwa hiyo alijaribu sanaa ya ushawishi, waikijua vema kuwa kutumia nguvu kwa watu wale kungewafanya wazidi kusimamia uamuzi wao. Ferdinand "aliwaomba wakuu waikubali amri, akiwathibitishia kuwa mfalme mkuu angewafurahia sana." Lakini watu hawa waaminifu walikiri mamlaka iliyokuwa juu ya watawala wa kidunia, na walijibu kwa utulivu: "Tutamtii mfalme mkuu katika kila jambo linaloweza kuchangia katika kudumisha amani na heshima ya Mungu."— Ibid., b. 13, ch. 5.

Mbele ya Baraza Kuu mfalme alitangaza hatimaye kwa elekta na marafiki zake kuwa amri "ilikuwa inakwenda kuandikwa katika muundo wa tamko la kifalme," na kwamba "njia pekee iliyobaki kwao ilikuwa kujisalimisha kwa walio wengi." Baada ya kusema hayo, aliondoka na kuuacha mkutano, bila kuwapa Wanamatengenezo fursa ya kujadili au kujibu. "Hata hivyo walituma wajumbe kwenda kumsihi mfalme arudi." Jibu lake kwa malalamiko yao lilikuwa:"Ni jambo lililokwisha kuamriwa; kujisalimisha ndiyo tu kumebaki."— Ibid., b. 13, ch. 5.

Kikosi cha mfalme kilishawishika kuwa viongozi wakuu wa Kikristo walikuwa wameshaazimia kuyaweka Maandiko Matakatifu juu ya mafundisho na matakwa ya kibinadamu; na walijua kuwa mahali popote ilipokubalika hivyo, upapa hatimaye ulishindwa. Lakini, kama ilivyokuwa kwa maelfu ya watu tangu wakati wao, walioangalia "mambo yanayoonekana," walijidanganya kuwa upande wa mfalme na papa ulikuwa na nguvu, na kuwa upande wa Wanamatengenezo ulikuwa dhaifu. Ikiwa Wanamatengenezo

wangetegemea msaada wa kibinadamu peke yake, wangekuwa dhaifu kama wafuasi wa papa walivyodhania. Lakini ingawa walikuwa wachache katika idadi, na hawakupatana na Roma, walikuwa na chanzo cha nguvu zao. Walipata nguvu "ambayo haikutokana na taarifa ya Mahakama, bali iliyotokana na neno la Mungu, siyo iliyotoka kwa mfalme mkuu Charles, bali iliyotoka kwa Yesu Kristo, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana."— Ibid., b. 13, ch. 6.

Mfalme Ferdinand alipokataa kuheshimu imani na dhamiri zao, wakuu wa majimbo ya Kikristo waliamua wasijali kutokuwepo kwake, bali walete Upinzani wao kwenye baraza la taifa bila kuchelewa. Hivyo basi, tamko rasmi, liliandaliwa na kuwasilishwa kwa Baraza:

"Tunapinga kwa hati hii, mbele ya Mungu, Muumbaji wetu pekee, Mtunzaji, Mkombozi, na Mwokozi, na ambaye siku moja atakuwa Mhukumu wetu, hali kadhalika mbele ya watu wote na viumbe wote, kwamba sisi, kwa ajili yetu na kwa ajii ya watu, hatuikubali wala kuitii kwa namna yo yote ile amri iliyopendekezwa, na jambo lolote lile ambalo ni kinyume na Mungu, na neno Lake takatifu, na haki yetu ya dhamiri, na wokovu wa roho zetu."

"Nini! Tunathibitisha amri hii! Tunasema kuwa Mwenyezi Mungu anapomwita mtu ashiriki ujuzi Wake, hata hivyo, mtu huyu hawezi kupokea ujuzi wa Mungu!" "Hakuna fundisho la hakika isipokuwa lile ambalo linapatana na neno la Mungu. Mungu anakataza. Maandiko Matakatifu yanapaswa kuelezwa kwa kutumia aya zingine na zinazoeleweka kwa uwazi zaidi; Kitabu hiki Kitakatifu, miongoni mwa mambo muhimu kwa ajili ya Mkristo, ni rahisi kueleweka, na kimekusudiwa kusambaratisha giza. Tumedhamiria, kwa neema ya Mungu, kudumisha usafi na kuhubiri neno Lake pekee, kama lilivyo katika vitabu vya kibiblia vya Agano la Kale na Agano Jipya, bila kuongeza kitu chochote humo ambacho ni kinyume chake. Neno hili ndiyo ukweli pekee; ni kanuni ya hakika ya mafundisho yote na maisha yote, na hawezi kamwe kutuangusha au kutudanganya. Anayejenga juu ya msingi huu atasimama dhidi ya nguvu zote za kuzimu, wakati majivuno yote ya kibinadamu yanapopangwa dhidi ya neno la Mungu yataanguka mbele ya uso wa Mungu."

"Kwa sababu hiyo tunakataa nira iliyowekwa juu yetu." "Wakati huo huo tunatarajia kuwa mfalme mkuu atatutendea kama kiongozi Mkristo anayempenda Mungu zaidi kuliko kitu kingine chochote; na tunawaahidi kuwapa, yeye pamoja na ninyi waheshimiwa wenye neema, upendo na utii wetu wote ambao ni haki na wajibu wetu halali."—Ibid., b. 13, ch. 6.

Mguso wa kushangaza ulihisika kwenye Baraza Kuu. Wengi wao walipatwa na mshangao na tahadhari kwa sababu ya ujasiri wa wapinzani. Mustakabali wao ulionekana kuwa wenye dhoruba na usio na uhakika. Migawanyiko, migogoro, na umwagaji damu vilionekana kutoepukika. Lakini Wanamatengenezo, baada ya kuhakikishiwa haki ya msimamo wao, na kuutegemea mkono wa Yeye Mwenye nguvu zote, walikuwa "wamejaa ujasiri na uthabiti."

"Kanuni zilizomo katika Upinzani huu unaosherehekewa ... ndiyo maudhui hasa ya Uprotestanti. Sasa Upinzani huu hupinga dhuluma mbili dhidi ya mwanadamu katika masuala ya imani: dhuluma ya kwanza ni uingiliaji wa mahakama za kiraia, na dhuluma ya pili ni mamlaka ya kiimla ya kanisa. Badala ya dhuluma hizi, Uprotestanti huweka nguvu ya dhamiri juu kuliko hakimu, na mamlaka ya neno la Mungu juu kuliko kanisa linaloonekana. Katika nafasi ya kwanza, inakataa mamlaka ya kiraia katika mambo ya Kimungu, na husema na manabii na mitume, 'Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu.' Mbele ya mfalme mkuu Charles wa Tano, unaiinua taji ya Yesu Kristo. Lakini unaenda mbele zaidi ya hapo: unaweka kanuni kuwa mafundisho yote ya kibinadamu yanapaswa kuwa chini ya udhibiti wa neno la Mungu."—Ibid., b. 13, ch. 6.

Wapinzani walikuwa wamethibitisha haki yao ya kusema kwa uhuru waliyoyaamini kuhusu ukweli. Siyo tu kuwa wangeamini na kutii, bali pia wangefundisha kile ambacho neno la Mungu linasema, na walipinga haki ya kasisi au hakimu kuingilia. Upinzani wa Spires ulikuwa ushuhuda mkubwa dhidi ya kukosa uvumilivu wa kidini, na dai la haki za binadamu wote kumwabudu Mungu kulingana na matakwa ya dhamiri zao wenyewe.

Tayari tangazo lilikuwa limetolewa. Lilikuwa limeandikwa katika kumbukumbu za maelfu ya watu na lilikuwa limeandikwa katika vitabu vya mbinguni, mahali ambapo juhudi za mwanadamu zisingeweza kulifuta. Ujerumani yote iliyokuwa imeipokea injili ilipokea tamko la Uprotestanti kama tamko lao la imani. Kila mahali watu waliona tamko hili kama ahadi ya enzi bora zaidi. Mmoja wa wakuu aliwaambia Waprotestanti wa Spires: "Mwenyezi Mungu, ambaye amewapa neema ya kukiri kwa nguvu, kwa uhuru, na bila hofu, awatunze katika uimara wa Kikristo mpaka siku ya umilele."—Ibid., b. 13, ch. 6.

Kama Matengenezo, baada ya kupata kiasi fulani cha mafanikio, ungekubali kupitisha muda ili wapendwe na ulimwengu, ungekosa uaminifu kwa Mungu na kwa matengenezo yenyewe, na ungejihakikishia kifo chake yenyewe. Uzoefu wa hawa waheshimiwa Wanamatengenezo ni somo kwa ajili ya zama zote zilizofuata. Namna ya Shetani ya kufanya kazi dhidi ya Mungu na neno Lake haijabadilika; bado yuko kinyume na Maandiko kufanywa mwongozo wa maisha kama ilivyokuwa katika karne ya kumi na sita. Katika wakati wetu kuna kuacha sana mafundisho na kanuni za Maandiko kuna hitaji la kurudi kwenye kanuni kuu za Uprotestanti—Biblia, na Biblia pekee, kama kanuni ya imani na wajibu. Shetani bado anafanya kazi kwa kila njia anayoweza kuitumia kuharibu uhuru wa dhamiri. Nguvu ya upinzani dhidi ya Ukristo ambayo waprotestanti wa Spires waliikataa, sasa kwa nguvu mpya inatafuta kurudisha utawala iliyoupoteza. Utii imara kwa neno la Mungu sawa na ule uliooneshwa wakati wa migogoro ya Matengenezo ndiyo tumaini pekee la matengenezo leo.

Kulitokea ishara za hatari kwa Waprotestanti; kulikuwepo ishara, pia, kuwa mkono wa Mungu ulikuwa umenyoshwa kuwalinda waaminifu. Ilikuwa ni wakati huu "Melanchthon

alipompitisha katika mitaa ya Spires kuelekea Rhine rafiki yake Simon Grynaeus, akimshurutisha avuke mto. Grynaeus alishangaa sana kwa tukio hilo. ‘Mtu mmoja mzee sana, lakini ambaye sikumjua,’ alisema Melanchthon, ‘alitokea mbele yangu na kusema, Ndani ya dakika mbili, maofisa watatumwa na Ferdinand kumkamata Grynaeus.’” Wakati wa mchana, Grynaeus alikuwa amesemwa vibaya katika hubiri lililotolewa na Faber, daktari msomi mfuasi wa papa; na alipofunga hubiri alimshutumu Grynaeus kwa kutetea “makosa fulani yanayochukiza.”

“Faber alituliza hasira yake, lakini mara moja alikwenda kwa mfalme, ambapo alipata amri dhidi ya profesa msumbufu wa Heidelberg. Melanchthon hakuwa na shaka kuwa Mungu alimwokoa rafiki yake kwa kumtuma mmoja wa malaika Zake watakatifu kumwonya mapema dhidi ya hatari iliyomkabili rafiki yake. “Akiwa ametulia kwenye kingo za Mto Rhine, alisubiri mpaka maji ya mto yalipokuwa yamemwokoa Grynaeus dhidi ya watesaji. ‘Hatimaye,’ alipiga kelele Melanchthon, alipomwona upande wa pili wa mto, ‘hatimaye ametenganishwa na taya katili za watu walio na kiu ya damu isiyo na hatia.’ Aliporudi nyumbani kwake, Melanchthon alipewa taarifa kuwa maofisa waliokuwa wakimtafuta Grynaeus walikuwa wamepekua kila mahali kwenye nyumba yake toka juu hadi chini.”—Ibid., b. 13, ch. 6.

Ilikuwa sasa matengenezo yaletwe mbele ya viongozi wakuu wa dunia. Viongozi wa uinjilisti walikuwa wamekataliwa fursa ya kusikilizwa na Mfalme Ferdinandi; lakini walikuwa wapewe fursa ya kuwasilisha hoja zao mbele ya mfalme mkuu na waheshimiwa waliokusanyika wa kanisa na dola. Katika mwaka uliofuata Upinzani wa Spires, ili kunyamazisha migawanyiko iliyosumbua dola, Charles V, aliitisha kikao cha Baraza Kuu katika mji wa Augsburg, ambapo alitangaza kusudi lake la kuongoza kikao hicho yeye mwenyewe binafsi. Pale viongozi wa Uprotestanti waliitwa.

Hatari kubwa zilitishia Matengenezo; lakini watetezi wake walimtumaini Mungu awasaidie katika kazi yao, na waliahidi kuwa imara katika kuunga mkono injili. Elekta wa Saxony alisihiwa na wajumbe wake wa baraza asihudhurie lile Baraza Kuu. Walisema, Mfalme alihitajika awe pamoja na wakuu kwenye lile Baraza ili awaingize katika mtego. “Je, siyo hatari kabisa kwenda na kujifungia mwenyewe ndani ya kuta za jiji pamoja na adui mwenye nguvu?” Lakini wengine walieleza kwa uungwana,“Hebu wakuu wa majimbo tujiheshimu kwa ujasiri, na kazi ya Mungu itaokolewa.”“Mungu ni mwaminifu; Hatatutupa,” alisema Luther.—Ibid., b. 14, ch. 2. Elekta aliondoka, akiwa na msafara wake, kuelekea Augsburg. Wote walielewa hatari zilizomkabili, na wengi walienda huko wakiwa na nyuso zenye huzuni na mioyo iliyojaa mashaka. Lakini Luther, ambaye aliwafuata mpaka Coburg, alifufua imani yao iliyokuwa karibu kupotea kwa kuimba wimbo, ulioandikwa katika safari ile, “Mungu ni ngome yetu imara.” Hofu nyingi zilizoleta mashaka ziliondoka, mioyo mingi mizito iliburudishwa, kwa sauti ya wimbo unaovuvia.

Wakuu waliopokea matengenezo waliazimia kuandika tamko la pamoja la maoni yao kwa mpangilio mzuri, likiwa na uthibitisho kutoka katika Maandiko, na kuliwasilisha kwa Baraza; na kazi ya uandishi wake alipewa Luther, Melanchthon, na wenzao. Ungamo hili lilikubaliwa na Waprotestanti kama ufafanuzi wa imani yao, na walikusanyika kuweka majina yao kwenye hati hii muhimu. Ulikuwa wakati muhimu lakini wa kujaribiwa sana. Wanamatengenezo walitamani kazi yao isiingiliwe na masuala ya kisiasa; walihisi kuwa Matengenezo hayakupaswa kutumia mvuto mwingine zaidi ya ule unaotoka katika neno la Mungu. Wakati wakuu wa Ukristo walipotaka kuendelea kutia sahihi Ungamo, Melanchthon aliingilia kati, na kusema: "Ni kazi ya wanateolojia na wachungaji kupendekeza mambo haya; hebu tuache mambo mengine mikononi mwa mamlaka za wakuu wa dunia."

"Haiwezekani, hata kidogo," alijibu John wa Saxony, "kunitenga. Nimeazimia kufanya kilicho sahihi, wala sijali taji yangu. Shauku yangu ni kumkiri Bwana. Kofia yangu na vazi langu la uongozi wa jimbo havina thamani sana kwangu sawa na msalaba wa Yesu Kristo." Baada ya kusema hayo, aliandika jina lake. Mwingine miongoni mwa wakuu wa majimbo alisema alipokuwa akishika kalamu: "Ikiwa heshima ya Bwana wangu Yesu Ktisto inahitaji jambo hili, niko tayari ... kuacha mali zangu na maisha yangu nyuma." "Ni heri niache raia wangu na majimbo yangu, kuiacha nchi ya baba zangu, na fimbo ya mkononi," aliendelea, "kuliko nipokee fundisho jingine tofauti na Ungamo hili."—Ibid., b. 14, ch. 6. Hiyo ndiyo iliyokuwa imani na ujasiri wa watu wa Mungu.

Wakati mwafaka ulifika wa kwenda mbele ya mfalme mkuu. Charles V, akiwa ameketi kwenye kiti cha enzi, akiwa amezungukwa na maelekta na wakuu, akiwasikiliza Wanamatengenezo wa Kiprotestanti. Ungamo la imani yao lilisomwa. Katika mkutano huo mkubwa kweli za injili ziliwekwa wazi, na makosa ya kanisa la papa yalianikwa wazi wazi. Ndiyo siku hiyo ilitangazwa "siku kuu zaidi kuliko zote za Matengenezo, na siku yenye utukufu mwingi zaidi kuliko zote katika historia ya Ukristo na wanadamu."—Ibid., b. 14, ch. 7. Lakini miaka michache ilikuwa imepita tangu mtawa wa Wittenberg aliposimama peke yake katika jiji la Worms mbele ya baraza la kitaifa. Sasa mahali pake walisimama viongozi wenye heshima kubwa na nguvu nyingi katika ufalme. Luther alikataliwa kuja Augsburg, lakini alikuwepo kwa njia ya maneno na maombi yake. "Nina furaha sana," aliandika, "kuishi hadi saa hii, ambapo Kristo ameinuliwa hadharani na waumini mashuhuri kama hao, na katika mkutano mkubwa kama huo."—Ibid., b. 14, ch. 7. Kwa njia hiyo yakatimizwa Maandiko yanayosema: "Nitazinena shuhuda zako ... mbele ya wafalme" (Zaburi 119:46).

Nyakati za Paulo injili ambayo kwayo alifungwa gerezani ilifikishwa hivyo hivyo mbele ya wakuu na waheshimiwa wa jiji la kifalme. Kwa hiyo katika tukio hili, yale ambayo mfalme alipiga marufuku yasihubiriwe mimbarani yalihubiriwa katika nyumba ya mfalme; yale ambayo yalifikiriwa kuwa yasingefaa kusikilizwa na watumishi yalisikilizwa kwa mshangao na mabwana na malodi wa himaya ya kifalme. Wafalme na watu mashuhuri walikuwa wasikilizaji, wana wa wafalme walikuwa wahubiri, na hubiri lilikuwa ukweli wa Mungu.

“Tangu enzi za mitume,” anasema mwandishi, “hakujakuwepo kazi kubwa zaidi au ungamo kubwa zaidi kuliko hilo.”— D’Aubigne, b. 14, ch. 7.

“Yote ambayo yamesemwa na Walutheri ni ya kweli; hatuwezi kuyakana,” alisema askofu wa kipapa. “Unaweza kweli kupata hoja nzuri za kukanusha ungamo lililofanywa na elekta na wenzake?” mwingine alimwuliza Dkt. Eck. “Kwa maandishi ya mitume na manabii—hapana!” lilikuwa jibu; “lakini kwa maandishi ya mababa na mabaraza—ndiyo!” “Ninaelewa,” alisema mwuliza swali. “Walutheri, kwa mujibu wa maelezo yako, wapo katika Maandiko, na sisi tuko nje.”—Ibid., b. 14, ch. 8.

Baadhi ya wakuu wa majimbo wa Ujerumani waliongoka na kujiunga na imani ya matengenezo. Mfalme mkuu mwenyewe alitangaza kuwa mafundisho ya imani ya Kiprotestanti yalikuwa ya kweli. Tamko lilitafsiriwa katika lugha nyingi na kusambazwa katika nchi zote za Ulaya, na limekubaliwa na mamilioni ya watu katika vizazi vilivyofuata kama muhtasari wa imani yao. Watumishi wa Mungu waaminifu hawakufanya kazi peke yao. Wakati mamlaka na nguvu na roho wachafu katika anga walipoungana pamoja dhidi yao, Bwana hakuwaacha watu Wake. Kama macho yao yangefumbuliwa, wangeweza kuona ushahidi wa ajabu wa uwepo na msaada wa Mungu kama ule uliotolewa kwa nabii wa zamani. Wakati mtumishi wa Elisha alipomwonesha bwana wake jeshi la adui lililokuwa limewazunguka na kukataa kabisa fursa zote za kuponyoka, nabii aliomba: “Ee Bwana, nakusihi, mfumbue macho yake, apate kuona” (2 Wafalme 6:17). Na, kumbe, mlima ulikuwa umejaa magari na farasi za moto, jeshi la mbinguni lililokuwa limepangwa kumlinda mtu wa Mungu. Hivyo ndivyo malaika walivyowalinda watendakazi katika kazi ya Matengenezo.

Moja ya kanuni zilizoshikiliwa sana na Luther ilikuwa kwamba kusiwepo na namna yo yote ya haja ya kuomba mamlaka ya kidunia iunge mkono Matengenezo, na kusiwepo na haja yo yote ya kuomba jeshi kulinda Matengenezo. Alifurahi kuwa injili ilipokelewa na wakuu wa himaya; lakini walipopendekeza kuungana ili kuunda umoja wa kujihami, alisema kuwa “fundisho la injili linapaswa kulindwa na Mungu pekee Kwa kadiri mwanadamu alivyoingilia katika kazi, ndivyo Mungu angejihusisha zaidi katika kuilinda. Tahadhari zote za kisiasa zilizopendekezwa, kwa maoni yake, zilitokana na hofu zisizo na msingi na mashaka yanayotokana na dhambi.”— D’Aubigne, London ed., b. 10, ch. 14.

Wakati adui walipoungana ili kuangamiza imani ya matengenezo, na maelfu ya mapanga yalipoonekana kuwa yanakaribiwa kuvutwa kutoka katika ala zake dhidi ya matengenezo, Luther aliandika: “Shetani anaonesha ghadhabu yake; maaskofu waovu wanakula njama; na tunatishiwa vita. Himizeni watu kupambana kwa kishujaa mbele ya kiti cha enzi cha Bwana, kwa imani na maombi, ili kwamba maadui, kwa kunyamazishwa na Roho wa Mungu, watulizwe kwa amani. Hitaji letu kuu, kazi yetu kuu, ni maombi; hebu watu wajue kuwa wanakabiliwa na ncha ya upanga na ghadhabu ya Shetani, na hebu waombe.”—D’Aubigne, b. 10, ch. 14.

Tena, tarehe nyingine ya baadaye, akizungumzia muungano uliokuwa ukifikiriwa na viongozi wa majimbo yaliyofanya matengenezo, Luther alisema kuwa silaha pekee iliyopaswa kutumiwa katika vita hii ilipaswa kuwa "upanga wa Roho." Alimwandikia elekta wa Saxony: "Hatuwezi kwa dhamiri zetu kuidhinisha muungano uliopendekezwa. Ingekuwa bora tufe mara kumi kuliko kuiona injili yetu inasababisha tone moja la damu linamwagika. Sehemu yetu ni kuwa kama mwanakondoo aendaye machinjioni. Msalaba wa Kristo lazima ubebwe. Hebu mheshimiwa kiongozi usiogope. Tutafanya mengi zaidi kwa maombi yetu kuliko maadui zetu watakavyofanya kwa majivuno yao. Jambo muhimu pekee ni kuwa mikono yenu isiwe na madoa ya damu ya ndugu zenu. Ikiwa mfalme anahitaji kutupeleka katika mahakama zake, tuko tayari kwenda. Huwezi kuilinda imani yetu: kila mmoja anapaswa kuamini kwa kuwa tayari kuhatarisha maisha yake mwenyewe."—Ibid., b. 14, ch. 1.

Kutoka katika chumba cha siri cha maombi ndiko ilipotoka nguvu iliyoutetemesha ulimwengu katika Matengenezo Makuu. Pale, kwa utulivu mtakatifu, watumishi wa Bwana walisimika miguu yao juu ya mwamba wa ahadi Zake. Wakati wa mapambano pale Augsburg, Luther "hakupitisha siku bila kutumia angalau saa tatu katika maombi, na zilikuwa saa zilizochaguliwa kutoka miongoni mwa zile zilizofaa zaidi kwa ajili ya kujifunza." Katika faragha ya chumba chake, alisikika akimimina roho yake mbele za Mungu katika maneno "yaliyojaa sifa, hofu, na tumaini, sawa na mtu aliyeongea na rafiki yake." "Ninajua kuwa Wewe ni Baba yetu na Mungu wetu," alisema, "na kwamba Wewe utawatawanya watesi wa watoto Wako; kwa kuwa Wewe Mwenyewe upo hatarini pamoja nasi. Jambo hili ni Lako, na ni kwa sababu ya msukumo Wako sisi tumeweka mikono yetu juu yake. Tutetee, basi, Ee Baba!"—Ibid., b. 14, ch. 6.

Kwa Melanchthon, ambaye alikuwa amevunjika moyo kwa sababu ya mzigo wa wasiwasi na hofu, aliandika: "Neema na amani katika Kristo— ninasema, na siyo katika ulimwengu. Amina. Ninachukia kwa chuki kali sana kwa sababu ya hiyo hali yako ya wasiwasi inayokutafuna. Ikiwa kazi hii siyo ya haki, achana nayo; ikiwa kazi hii ni ya haki, kwa nini tusiziamini ahadi Zake Yeye Ambaye ametuamuru tusinzie bila hofu? ... Kristo hatatupungukia katika kazi ya haki na ukweli. Yu hai, Anatawala; ni hofu gani, tena, tunaweza kuwa nayo?"—Ibid., b. 14, ch. 6.

Mungu alisikia vilio vya watumishi Wake. Aliwapa wakuu wa majimbo na wachungaji neema na ujasiri wa kusimama kwa ajili ya ukweli dhidi ya watawala wa giza la ulimwengu huu. Alisema Bwana: "Tazama, naweka katika Sayuni jiwe kuu la pembeni, teule, lenye heshima, Na kila amwaminiye hatatahayarika" (1 Petro 2:6). Wanamatengenezo Waprotestanti walijenga juu ya Kristo, na malango ya kuzimu yasingeweza kuwashinda.

Sura ya 12 - Matengenezo Ufaransa

Upinzani wa Spires na Ungamo la pale Augsburg—matukio ambayo yaliweka alama ya ushindi wa Matengenezo katika nchi ya Ujerumani, yalifuatiwa na miaka ya migogoro na giza. Baada ya kudhoofishwa na migawanyiko miongoni mwa wafuasi wake, na baada ya kushambuliwa na maadui zake wenye nguvu, Uprotestanti ulionekana kama unaelekea kuangamizwa. Maelfu walitia muhuri ushuhuda wao kwa damu zao. Vita ya wenyewe kwa wenyewe ililipuka; mmoja wa wafuasi wake wakuu aliisaliti kazi ya Uprotestanti; watu wema sana miongoni mwa wakuu waliokubali matengenezo waliangukia katika mikono ya mfalme mkuu na waliburuzwa kama mateka kutoka mji mmoja hadi mwingine.

Lakini katika wakati ambao mfalme mkuu alionekana kuwa anaelekea kupata ushindi, alipoteza ushindi. Alishuhudia mawindo yake yakinyakuliwa kutoka katika mikono yake, na alilazimishwa hatimaye kuvumilia mafundisho ambayo lengo kuu la maisha yake lilikuwa kuyaangamiza. Alikuwa amechezea kamari ufalme wake, hazina zake na maisha yake yote ili kuangamiza uzushi. Sasa alishuhudia majeshi yake yakipukutika katika vita, hazina zake zikikauka, falme zake nyingi zikitishiwa na uasi, wakati kila mahali imani ambayo alijaribu kuidhibiti, ilikuwa ikisambaa. Charles V alikuwa akipambana na nguvu kubwa kuliko zote. Mungu alisema,"Na iwe nuru," lakini mfalme mkuu alikuwa akipambana giza lisiondoke. Kusudi lake lilishindwa; na akiwa bado ana umri mdogo, kwa kuchoshwa sana na migogoro ya muda mrefu, alikimbia kiti cha enzi na kwenda kujificha katika nyumba ya watawa.

Katika nchi za Uswisi na Ujerumani, kulikuja siku za giza dhidi ya Matengenezo. Wakati maeneo mengi yalipokea imani ya matengenezo, mengine yalishikilia kwa nguvu ya upofu kanuni za kiimani zisizobadilika za Roma. Mateso yao dhidi ya wale waliokuwa na shauku ya kupokea ukweli hatimaye yalisababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe. Zwingli na wengi waliokuwa wameungana naye katika matengenezo walifia katika uwanja wa damu wa Cappel. Okolampadio, kwa kuzidiwa na hofu ya majanga haya ya kutisha alikufa muda mfupi baadaye. Roma ilishinda, na katika maeneo mengi ilionekana kana kwamba Roma ilirudisha mambo yote iliyokuwa imepoteza.

Lakini Yeye ambaye mashauri Yake ni ya milele hakuwa ameiacha kazi Yake wala watu Wake. Mkono Wake ulileta ukombozi kwa ajili yao. Katika nchi zingine aliinua watenda kazi wengine waendeleze kazi ya matengenezo. Katika nchi ya Ufaransa, kabla jina la Luther halijasikika kama Mwanamatengenezo, kulishaanza kupambazuka. Mmoja wa watu wa awali kupokea nuru alikuwa mzee Lefevre, mtu mwenye elimu kubwa, profesa katika Chuo Kikuu cha Paris, na mfuasi wa papa wa dhati na mwenye juhudi kubwa. Katika utafiti wake katika maandishi ya kale macho yake yalielekezwa kwenye Biblia, na alianzisha mafundisho ya Biblia kwa wanafunzi wake.

Lefevre alikuwa mtu aliyewaheshimu sana watakatifu, na alijielekeza kuandika historia ya watakatifu na wafia dini kama walivyosimuliwa katika mapokeo ya kanisa. Hii ilikuwa kazi iliyohitaji nguvu nyingi; lakini alikuwa amekwisha endelea sana katika hili, wakati, akidhania kuwa angepata msaada mkubwa kutoka katika Biblia, alianza kuisoma kwa lengo hilo. Katika Biblia, kwa hakika, aliwapata watakatifu, lakini wakiwa tofauti na jinsi walivyoelezwa katika kalenda ya Kiroma. Mafuriko ya nuru ya Mungu yalimwagika katika akili yake. Kwa mshangao na karaha aliacha kazi aliyokuwa amejipangia na kuanza kujifunza neno la Mungu kwa makini. Kweli za thamani alizozipata humo muda sio mrefu alianza kuzifundisha.

Mwaka 1512, kabla Luther na Zwingli hawajaanza kazi ya matengenezo, Levre aliandika: “Ni Mungu anayetupatia, kwa imani, uadilifu ambao kwa huo peke yake tunahesabiwa haki kwa ajili ya umilele.”—Wylie, b. 13, ch. 1. Alipotafakari sana juu ya siri za ukombozi, alisema kwa mshangao: “Ee, ukuu usioelezeka wa kubadilishana,—Yeye asiyekuwa na dhambi anahukumiwa, na yeye aliye na hatia anaachwa huru; Mbaraka unabeba laana, na aliyelaaniwa anapata mbaraka; Mzima anakufa, na mfu anaishi; Utukufu unafichwa katika giza, na yule aliyekuwa hajui cho chote isipokuwa aibu anavikwa utukufu.”—D’Aubigne, London ed., b. 12, ch. 2.

Na wakati akifundisha kuwa utukufu wa wokovu ni wa Mungu pekee, alisema pia kuwa wajibu wa utii ulikuwa wa mwanadamu. “Ikiwa wewe ni mshiriki wa kanisa la Kristo,” alisema, “wewe ni kiungo cha mwili wa Kristo; ikiwa wewe ni wa mwili Wake, basi wewe ni wa tabia ya Mungu Laiti, watu wangeweza kupata ufahamu wa fursa hii, kwa kiasi gani wangeishi maisha safi, ya haki, na matakatifu, na ni kwa kiasi gani wangepatana, wakilinganishwa na utukufu uliomo ndani yao,—utukufu ule ambao jicho la kimwili haliwezi kuuona,—ikiwa wangefikiria utukufu wote wa ulimwengu huu.”—Ibid., b. 12, ch. 2.

Walikuwemo miongoni mwa wanafunzi wa Lefevre waliosikiliza kwa makini maneno yake, na ambao, muda mrefu baada ya sauti ya mwalimu wao kunyamazishwa, wangeendelea kutangaza ukweli. Mtu kama huyo alikuwa William Farel. Alikuwa mtoto wa wazazi wacha Mungu, na aliyeelimishwa kupokea kwa imani isiyo na maswali mafundisho ya kanisa, ambaye angeweza kusema, kama mtume Paulo, aliyesema juu yake mwenyewe: “Nalikuwa Farisayo kwa kuifuata madhehebu ya dini yetu iliyo sahihi kabisa” (Matendo 26:5). Mfuasi wa Kiroma madhubuti, aliwachoma moto kwa bidii na kuwaangamiza watu wote waliothubutu kulipinga kanisa. “Nilisaga meno yangu kama mbwa mwitu mwenye hasira,” alisema baadaye, akielezea kipindi hiki cha maisha yake, “niliposikia mtu ye yote akisema neno lolote dhidi ya papa.”—Wylie, b. 13, ch. 2.

Alikuwa hachoki kuwaabudu watakatifu, akiwa na Lefevre wakizungukia makanisa ya Paris, wakiabudu kwenye madhabahu, na kuyapamba maeneo matatifu kwa zawadi. Lakini matendo haya ibada hayakuleta amani katika mioyo yao. Hatia ya dhambi ilibaki moyoni,

ambayo matendo yote ya toba aliyoyafanya hayakuweza kuiondoa. Kama sauti iliyotoka mbinguni alisikia maneno ya Mwanamatengenezo: “Wokovu ni kwa neema.”“Asiye na hatia amehukumiwa, na mhalifu ameachiliwa.”“Ni msalaba wa Kristo pekee unaofunua malango ya mbinguni, na unaofunga malango ya kuzimu.”— Ibid., b. 13, ch. 2.

Farel kwa furaha aliupokea ukweli. Kwa maongezi kama yale ya Paulo aliachana na utumwa wa mapokeo na badala yake alipokea uhuru wa wana wa Mungu. “Badala ya moyo wa mwuaji wa mbwa mwitu mkali,” aligeuka, alisema, “akawa mkimya kama mwanakondoo mpole, asiye na madhara, moyo wake ukiwa umehamishwa kabisa kutoka kwa papa na kuwekwa kwa Yesu Kristo.”—D’Aubigne, b. 12, ch. 3.

Wakati Lefevre akiendelea kueneza nuru miongoni mwa wanafunzi wake, Farel, akiwa na juhudi upande wa Kristo kama aliyokuwa nayo upande wa papa, alitoka na kutangaza ukweli hadharani. Kiongozi mkubwa wa kanisa, askofu wa Meaux, muda mfupi baadaye, aliungana nao. Walimu wengine waliokuwa mashuhuri kwa sababu ya uwezo wao na elimu yao kubwa waliungana nao katika kutangaza injili, na injili ilipata wafuasi miongoni mwa matabaka yote ya watu, kutoka katika nyumba za mafundi na wakulima hadi katika ikulu ya mfalme. Dada wa Fransis I, mfalme aliyetawala wakati huo, aliipokea imani ya matengenezo. Mfalme mwenyewe, na mama malkia, walionekana kwa muda fulani kuunga mkono kazi ya injili, na kwa matumaini makubwa Wanamatengenezo walitarajia kufika wakati ambao nchi yote ya Ufaransa ingeongolewa na kuiamini injili.

Lakini matumaini yao hayakutimia. Majaribu na mateso yaliwasubiri wanafunzi wa Kristo. Jambo hili, hata hivyo, lilifichwa lisionekana machoni pao. Wakati wa amani ulitangulia kwanza, ili wajenge uimara wa kukutana na dhoruba; na Matengenezo yalipiga hatua kubwa ya maendeleo. Askofu wa Meaux alifanya kazi kwa juhudi kubwa katika daiyosisi yake kuwafundisha mapadri na watu wa kawaida. Mapadri wasio na elimu na wasio na maadili waliondolewa kazini, na, kwa kadiri ilivyowezekana, waliwekwa watu wenye elimu na wacha Mungu. Askofu alikuwa na shauku kuwa watu wake wapate neno la Mungu wao wenyewe, na jambo hili kwa muda mfupi lilifanikiwa. Lefevre alifanya kazi ya kutafsiri Agano Jipya; na wakati uleule ambao Biblia ya Kijerumani ya Luther ilikuwa ikitoka katika mitambo ya uchapishaji ya jiji la Wittenberg, Agano Jipya la Kifaransa lilichapishwa katika jiji la Meaux. Askofu alitumia nguvu zake zote na mali zake zote kuhakikisha kuwa Agano Jipya hilo linasambazwa katika parishi zake zote, na si muda mrefu wakulima wa Meaux walimiliki Maandiko Matakatifu.

Kama wasafiri wanaoangamia kwa sababu ya kiu wanavyoshangilia kukutana na chemchemi ya maji, ndivyo roho hizi zilivyopokea ujumbe kutoka mbinguni. Wafanya kazi katika mashamba, mafundi katika karakana, walifurahia kazi zao za suluba kwa kujadili kweli za thamani za Biblia. Nyakati za jioni, badala ya kwenda kuburudika katika vilabu vya pombe, walijifunza katika nyumba zao ili wajisomee neno la Mungu na kuungana katika maombi na

kusifu. Badiliko kubwa lilionekana kwa muda mfupi katika jumuia hizi. Ingawa walikuwa watu wa tabaka la chini, wakulima wasio na elimu wachapa kazi, nguvu inayobadilisha, inayoinua ya neema ya Mungu ilionekana katika maisha yao. Wakiwa wanyenyekevu, wenye upendo, na watakatifu, walisimama kama mashahidi wa kile ambacho injili inaweza kufanya kwa wale wanaoipokea kwa moyo wa dhati.

Nuru iliyowashwa pale Meaux ilitupa miale yake mbali. Kila siku idadi ya waongofu ilikuwa ikiongezeka. Hasira ya viongozi wa kanisa ilidhibitiwa kwa muda na mfalme ambaye alidharau ufinyu wa mawazo na ubinafsi wa watawa; lakini viongozi wa upapa walishinda hatimaye. Sasa mateso yalianza. Askofu wa Meaux, alilazimishwa kuchagua kati ya moto na kukana, akachagua kukana; lakini pamoja na anguko la kiongozi, kondoo wake walibaki wakiwa na msimamo imara. Wengi walitoa ushuhuda wa ile kweli katikati ya ndimi za moto. Kwa ujasiri wao na uaminifu wao wakiwa motoni, Wakristo hawa wanyenyekevu walihubiri maelfu ya watu ambao katika siku za amani hawakuwahi kusikia ushuhuda wao.

Siyo watu wa chini na walio maskini peke yao ambao katikati ya mateso na dharau walidiriki kushuhudia kwa ajili ya Kristo. Katika vyumba vya kifahari vya majumba makubwa na ikulu walikuwepo watu wa tabaka la juu ambao kwao ukweli ulikuwa wa thamani zaidi kuliko mali au cheo au hata uhai wenyewe. Ngao ya kifalme ilificha roho ya juu na imara zaidi kuliko ya joho na kofia ya kiaskofu. Louis de Berquin alikuwa mzaliwa wa ukoo wa kifalme. Mshauri wa ikulu aliye jasiri, alikuwa msomi makini, muungwana, na mwadilifu. Mwandishi anasema, "Alikuwa mfuasi mkubwa wa taasisi za kipapa, na msikilizaji mkubwa wa misa na mahubiri; ... na alifunika sifa zake zote zingine kwa chuki maalumu dhidi ya Ulutheri." Lakini, kama watu wengi wengine, aliongozwa na Mungu kuipata na kuisoma Biblia, alishangazwa kukuta humo, "hakuna mafundisho ya Roma, badala yake aliyakuta mafundisho ya Luther."—Wylie, b. 13, ch. 9. Tangu hapo alijiweka wakfu kikamilifu kujifunza injili.

"Msomi wa juu kabisa miongoni mwa waungwana wa daraja la juu wa Ufaransa," akili zake nyingi na uwezo wake wa kuongea kwa ufasaha, ujasiri wake usiokubali kushindwa na juhudi zake za kishujaa, na mvuto wake katika nyumba ya mfalme,—kwani alikuwa na upendeleo maalumu wa mfalme,— vilimfanya achukuliwe na wengi kuwa mtu ambaye alikuwa amechaguliwa na Mungu awe Mwanamatengenezo wa nchi yake. Alisema Beza: "Berquin angeweza kuwa Luther wa pili, ikiwa Fransis I angekuwa elekta wa pili." "Yeye ni mbaya zaidi kuliko Luther," walisema watetezi wa upapa.—Ibid., b. 13, ch. 9.

Wafuasi wa Uroma wa Ufaransa walimwogopa sana. Walimtupa gerezani kama mzushi, lakini aliachiwa huru na mfalme. Kwa miaka mgogoro uliendelea. Fransis, akiyumba kati ya Uroma na Matengenezo, kwa mpokezano alistahimili na alizuia juhudi za kikatili za watawa. Berquin alifungwa gerezani mara tatu na mamlaka za kipapa, lakini aliachiliwa na mfalme, ambaye, kwa kuvutiwa na uwezo wake wa akili na tabia yake ya kiungwana, alikataa kumtoa

kafara katika uovu ule wa ukasisi. Berquin alionywa mara kwa mara juu ya hatari iliyomkabili nchini Ufaransa, na alisihiwa afuate nyayo za wale waliopata usalama kwa kukimbilia uhamishoni kwa hiari. Erasmus, mtu mwoga na mtu aliyejali maslahi ya muda mfupi, ambaye pamoja na upana wa elimu yake alishindwa katika ukuu wa kimaadili ambao unasalimisha maisha na heshima chini ya ile kweli; alimwandikia Berquin: "Omba upelekwe kama balozi katika nchi ya kigeni; nenda na ukasafari katika nchi ya Ujerumani. Unamjua Beda na jinsi alivyo—yeye ni jitu la kutisha lenye vichwa elfu moja, linalorusha sumu kali kila upande. Maadui zako wanaitwa jeshi. Hata kama kazi yako ingekuwa bora zaidi kuliko ya Yesu Kristo, hawangekuacha uondoke bali wangekuua kikatili. Usiamini sana ulinzi wa mfalme. Kwa hali yo yote ile, usinihusishe na kitivo cha teolojia."—Ibid., b. 13, ch. 9.

Lakini hatari zilivyoongezeka, juhudi za Berquin zilizidi kuimarika zaidi. Licha ya kuukataa ushauri wa kisiasa na kinafsi wa Erasmus, aliazimia kuchukua hatua za kijasiri zaidi. Siyo tu kuwa alisimama kuutetea ukweli, bali alishambulia makosa pia. Shitaka la uzushi ambalo viongozi wa Roma walilielekeza kwake, alilielekeza kwao. Wapinzani wake wakuu na wenye uchungu na juhudi kubwa walikuwa madaktari na watawa wasomi wa idara ya teolojia katika chuo kikuu mashuhuri cha Paris, moja ya mamlaka kuu ya kidini katika jiji na taifa.

Kutokana na maandishi ya hawa madaktari wasomi, Berquin alipata hoja kumi na mbili ambazo alitangaza hadharani kuwa "pinzani dhidi ya Biblia, na uzushi;" na alimwomba mfalme awe mwamuzi katika pambano hilo. Mfalme, kwa kutokuona tatizo lolote la kukutanisha pande hizi mbili zinazosigana za wasomi wazamivu na wabobezi, na kwa kufurahia kupata fursa ya kunyenyekeza kiburi cha hawa watawa wenye majivuno, aliwaagiza viongozi wa kipapa kutetea hoja zao kwa kutumia Biblia. Silaha hii, walijua kabisa, isingewafaa sana; kifungo, mateso, na mti wenye ncha kali ndizo silaha walizojua jinsi ya kuzitumia kwa mafanikio makubwa zaidi. Sasa meza zilikuwa zimepinduliwa, na walijiona wakiwa karibu kutumbukia katika shimo walilokuwa wametumaini kumtumbukiza Berquin. Kwa mshangao walitafuta karibu yao njia ya kutorokea.

"Karibu na wakati huo sanamu ya Bikra kwenye kona ya moja ya mitaa, iliharibiwa." Kulikuwa na taharuki katika jiji. Makundi ya watu walifurika mahali pale, wakiwa na mwonekano wa maombolezo na hasira. Mfalme pia alishitushwa sana. Hapa kulikuwa na fursa ambayo watawa waliweza kuigeukia ili kujenga hoja, na walidaka na kuiwekea maelezo haraka haraka. "Haya ni matunda ya mafundisho ya," walipiga kelele. "Kila kitu kinakwenda kupinduliwa—dini, sheria, kiti cha enzi chenyewe—na hila za KiLutherrani."— Ibid., b. 13, ch. 9.

Berquin alikamatwa tena. Mfalme aliondoka katika jiji la Paris, na kwa njia hiyo watawa waliachwa wafanye walivyopenda wenyewe. Mwanamatengenezo alishitakiwa na alihukumiwa kifo, na ili Fransis asije akaingilia kati kumwokoa, hukumu ilitekelezwa siku

hiyo hiyo iliposomwa. Wakati wa mchana Berquin alipelekwa mahali pa kifo. Umati wa watu ulikusanyika kushuhudia tukio lile, na kulikuwa na watu wengi waliotazama kwa mshangao na mashaka kuwa mhanga alikuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa watu wema na wajasiri katika familia za kiungwana za Kifaransa. Mshangao, hasira, dharau, na chuki kali vilitia giza katika nyuso za kundi la watu lililokuwa likiongezeka; lakini katika uso mmoja hakukuwa na kivuli cho chote. Mawazo ya mfia dini yalikuwa mbali na mandhari ile ya makelele; alihisi tu uwepo wa Bwana wake.

Mkokoteni mbovu alioupanda, nyuso zilizokunjamana za watesaji wake, kifo cha kutisha alichokuwa akikiendea, haya hakuyajali; Yeye aliye hai aliyewahi kufa, na yu hai milele na milele, na anazo funguo za mauti na kuzimu, alikuwa kando yake. Uso wa Berquin uling'aa kwa nuru na amani ya mbinguni. Alikuwa amevaa nguo nzuri, alikuwa amevaa "joho la mahameli, jaketi la kubana la mchanganyiko wa hariri na pamba, na soksi za rangi ya dhahabu."—D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 2, ch. 16. Alikuwa anakwenda kushuhudia kwa ajili ya imani yake mbele ya Mfalme wa wafalme na ulimwengu uliokuwa ukishuhudia, na hakuna kilio ambacho kificha furaha yake.

Wakati msafara ukitembea pole pole, ukipita katika mitaa iliyofurika watu, watu waligundua kwa mshangao amani isiyokuwa na mawingu, ushindi wenye furaha wa mwonekano na mwenendo wake. Walisema, "Yeye ni, kama mtu anayekaa katika hekalu, na anatafakari juu ya mambo matakatifu."— Wylie, b. 13, ch. 9.

Akiwa amefungwa kwenye mti kwa ajili ya kuchomwa moto, Berquin alijaribu kusema maneno machache kwa watu; lakini watawa, wakihofia matokeo, walianza kupiga kelele, na maaskari waligonganisha silaha zao, na kelele zao zilizima sauti ya mfia dini. Kwa njia hiyo mwaka 1529 mamlaka ya juu kabisa ya uandishi na ya kikanisa ya Paris iliyoendelea "iliuwekea umma wa 1793 mfano mbaya wa kuzima maneno matakatifu ya watu wanaokufa juu ya jukwaa la kunyongea wahalifu."—Ibid., b. 13, ch. 9.

Berquin alinyongwa, na mwili wake ulichomwa kwa ndimi za moto. Habari za kifo chake zilileta huzuni kwa marafiki wa Matengenezo katika nchi yote ya Ufaransa. Lakini mfano wake haukupotea. "Sisi, pia, tuko tayari," walisema mashahidi wa ukweli, "kukabiliana na kifo kwa furaha, tukielekeza macho yetu kwa maisha yajayo."—D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 2, ch. 16.

Wakati wa mateso ya Meaux, walimu wa imani ya matengenezo walinyang'anywa leseni za kuhubiri, na walijiunga na shughuli zingine. Baada ya muda mfupi, Lefevre aliondoka na kwenda zake nchini Ujerumani. Farel alirudi katika mji alikozaliwa upande wa mashariki ya Ufaransa, kueneza nuru katika mji wa nyumbani alikolelewa. Tayari habari zilikuwa zimepokelewa za kile kilichokuwa kikiendelea mjini Meaux, na ukweli, ambao aliufundisha bila woga na kwa juhudi kubwa, ulipata wasikilizaji. Muda si mrefu mamlaka zilishituka na

kuanza kutafuta jinsi ya kumnyamazisha, na alifukuzwa mjini. Ingawa alikuwa hawezi tena kuhubiri hadharani, alisafiri huko na huko katika nyika na vijiji, akifundisha katika nyumba za watu binafsi na maeneo yenye nyasi yaliyo pweke, na kutafuta maficho katika misitu na mapango yaliyokuwa katikati ya miamba, maeneo ambayo aliyatembelea wakati wa ujana wake. Mungu alikuwa akiwaandaa kwa ajili ya majaribu makubwa zaidi. "Misalaba, mateso, na vitendea kazi vya Shetani, ambavyo nilionywa juu yake hapo awali, havijaondoka," alisema; "vimekuwa vikali zaidi kuliko ninavyoweza kuhimili mwenyewe; lakini Mungu ni Baba yangu; Yeye amenipa na daima atanipa nguvu ninayoihitaji."—D'Aubigne, History of the Reformation of the Sixteenth Century, b. 12, ch. 9.

Kama ilivyokuwa katika siku za mitume, mateso yalikuwa "yametokea zaidi kwa kuieneza Injili" (Wafilipi 1:12). Wakiwa wamefukuzwa Paris na Meaux, "wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno" (Matendo 8:4). Na kwa njia hiyo nuru iliweza kuenea katika maeneo ya mbali ya nchi ya Ufaransa.

Mungu alikuwa bado akiandaa watenda kazi wa kueneza injili Yake. Katika moja ya shule za Paris kulikuwepo na kijana mwenye tafakari ya kina, mkimya, tayari akionesha ushahidi wa kuwa na akili yenye nguvu na inayopenya, na alijukana kwa maisha safi yasiyokuwa na lawama kama alivyojulikana kwa uwezo wa akili na bidii katika masuala ya dini. Uwezo wake wa kiakili na uchapakazi wake kwa muda mfupi vilimfanya awe mtu wa kujivunia hapo chuoni, na ilitarajiwa kuwa John Calvin angekuwa mmoja wa watetezi wa kanisa mwenye uwezo mkubwa na heshima nyingi. Lakini nuru ya Mungu ilipenya hata katika kuta za falsafa za uanazuoni na ushirikina ambamo Calvin alikuwa amefungwa ndani yake. Alisikia mafundisho mapya kwa mshtuko, na hakuwa na shaka kuwa wazushi walistahili moto ambao walichomwa nao. Lakini bila kukusudia alikutana uso kwa uso na uzushi na alilazimishwa kupima uwezo wa teolojia ya Kiroma kukabiliana na mafundisho ya Kiprotestanti.

Binamu wa Calvin, aliyekuwa amejiunga na Wanamatengenezo, alikuwa jijini Paris. Ndugu hawa wawili walikutana mara kwa mara kujadili masuala yaliyokuwa yakisumbua ulimwengu wa Kikristo. "Kuna dini mbili katika ulimwengu,"alisema Olivetan, Mprotestanti."Dini ya kwanza ni ile iliyobuniwa na wanadamu, ambayo ndani yake mwanadamu anajiokoa mwenyewe kwa njia ya sherehe na matendo mema; nyingine ni ile ambayo imefunuliwa katika Biblia, na ambayo humfundisha mwanadamu kutafuta wokovu kutoka kwa neema ya Mungu pekee." "Sipokei hata moja ya mafundisho yenu mapya," Calvin alisema kwa mkazo; "mnadhani mimi nimeishi katika makosa siku zangu zote?"—Wylie, b. 13, ch. 7.

Lakini fikra zilikuwa zimeamshwa katika akili yake ambazo asingeweza kuziondoa kwa utashi wake mwenyewe. Akiwa peke yake chumbani aliyatakafari maneno ya binamu yake. Hatia ya dhambi ilimshika; alijiona mwenyewe, bila mwombezi, mbele ya Jaji mtakatifu na

mwenye haki. Maombi ya watakatifu, matendo mema, sherehe za kanisa, vyote havikuwa na nguvu ya kuondoa hatia ya dhambi. Hakuweza kuona kitu cho chote zaidi ya giza la kukata tamaa milele. Madaktari wasomi wa kanisa walijaribu kupoza maumivu yake ya rohoni bila mafanikio. Ungamo na kitubio vilijaribishwa bila mafanikio; visingeweza kupatanisha roho na Mungu.

Akiwa bado katika mapambano haya yasiyokuwa na matunda, Calvin, bila kupanga, alitembelea moja ya viwanja vya umma vilivyotumika kutesea watu, akashuhudia kuchomwa moto kwa mzushi. Alishangazwa na amani iliyokuwa katika uso wa mfia dini. Katikati ya maumivu ya kifo kile cha kutisha, na chini ya hukumu ya kutisha zaidi ya kanisa, alionesha imani na ujasiri ambao kijana huyu mwanafunzi, Calvin, aliutofautisha kwa maumivu makali na kukata tamaa kwake mwenyewe na giza la moyoni mwake, wakati akilitii kanisa kikamilifu. Alijua kuwa wazushi walikita imani yao katika Biblia. Aliazimia kuisoma, ili agundue, ikiwezekana, siri ya furaha yao.

Katika Biblia alimpata Kristo. "Ee Baba," alilia, "Kafara Yake imepoza hasira Yako; Damu Yake imeosha uchafu wangu; Msalaba Wake umebeba laana yangu; Kifo chake kimenipatanisha na Mungu. Tumebuni kwa ajili yetu wenyewe mambo mengi ya kipumbavu ambayo hayana faida, lakini umeweka mbele yangu neno Lako kama mwenge, nawe umegusa moyo wangu, ili nichukie mambo yote mengine isipokuwa yale tu ya Yesu."— Martyn, vol. 3, ch. 13.

Calvin alisomea upadri. Wakati akiwa na umri wa miaka kumi na mbili alichaguliwa kuwa mlezi wa kanisa dogo, na kichwa chake kilinyolewa na askofu kulingana na sheria za kanisa. Hakufanyiwa huduma ya upadrisho, wala hakufanya majukumu ya upadri, lakini alihesabiwa kuwa miongoni mwa mapadri, akishikilia cheo chake, na akipokea posho kwa kazi hiyo.

Sasa, akihisi kwamba kamwe asingekuwa padri, aliamua kujifunza sheria kwa muda fulani, lakini hatimaye aliachana na lengo hilo na aliazimia kutoa maisha yake kwa kazi ya injili. Lakini alisita kuwa mwalimu wa hadhara. Kwa asili alikuwa mtu mwoga, na alikuwa na mzigo kwa ajili ya wajibu mzito wa cheo chake, na alitamani kuwekeza maisha yake katika kujifunza. Mashauri ya dhati ya marafiki, hatimaye, yalipata ukubali. "Ni jambo la kushangaza sana," alisema, "kwamba mtu mwenye asili hali ya chini hivyo anaweza kuinuliwa na kupewa heshima kubwa kiasi hicho."—Wylie, b. 13, ch. 9.

Calvin alianza kazi yake kimya kimya, na maneno yake yalikuwa kama matone ya umande yanayoburudisha ardhi. Alikuwa ameondoka Paris, na sasa alikuwa katika mji wa jimbo chini ya ulinzi wa binti wa mfalme aliyeitwa Margaret ambaye, kwa kuipenda injili, alipanua ulinzi wake kwa wanafunzi wengine wa injili. Calvin alikuwa bado kijana, mwenye haiba ya uungwana, isiyojikuza. Kazi yake ilianza na watu katika nyumba zao. Akiwa

amezungukwa na watu wa nyumbani, alisoma Biblia na alifungua ukweli wa wokovu. Waliosikia ujumbe walichukua habari njema kwa wengine, na muda si mrefu mwalimu alivuka mipaka ya jiji hadi katika miji na mitaa ya nje ya jiji. Aliingia katika majumba na vijumba, na alisonga mbele, akiweka msingi wa makanisa ambayo yangeweza kutoa ushuhuda kwa ajili ya ukweli bila hofu.

Baada ya miezi mitatu alirudi Paris. Kulikuwepo na misukosuko isiyokuwa ya kawaida miongoni mwa watu wenye elimu na wasomi. Masomo ya lugha za kale yaliwaongoza watu kuisoma Biblia, na wengi ambao mioyo yao haikuguswa na ukweli wake walijadili kwa ukweli huo kwa shauku kubwa na hata kupambana na mashujaa wa Uroma. Calvin, japokuwa alikuwa mpambanaji katika tasnia ya malumbano ya hoja za kiteolojia, alikuwa na utume wa juu zaidi wa kutekeleza kuliko ule wa kelele za wasomi. Akili za watu zilitikiswa, na sasa ulikuwa wakati wa kuwafungulia ukweli. Wakati kumbi za vyuo vikuu zilijazwa kwa makelele ya malumbano ya kiteolojia, Calvin alikuwa akitembea kutoka nyumba kwa nyumba, akiwafungulia watu Biblia, na akiwaelezea habari za Kristo na Yeye aliyesulubiwa.

Kwa uongozi wa Mungu, Paris ilipewa wito mwingine wa kuipokea injili. Wito wa Lefevre na wa Farel ilikuwa imekataliwa, lakini tena ujumbe ilipaswa usikiwe na watu wa matabaka yote katika jiji lile kubwa. Kwa sababu za kisiasa, mfalme alikuwa hajaamua kuwa upande wa Roma kikamilifu dhidi ya Matengenezo. Margaret bado aling'ang'ania tumaini kuwa Uprotestanti ulikuwa unakwenda kushinda. Margaret aliazimia kuwa imani ya matengenezo ilipaswa kuhubiriwa katika jiji la Paris. Wakati wa kutokuwepo kwa mfalme, aliamuru mchungaji wa Kiprotestanti ahubiri katika makanisa ya jiji. Baada ya jambo hili kukataliwa na viongozi wakuu wa upapa, binti wa mfalme alifungua milango ya ikulu. Chumba kiliandaliwa kitumike kama kanisa, na ilitangazwa kuwa kila siku, katika saa fulani maalumu iliyopangwa, hubiri lingehubiriwa, na watu wa kila tabaka na hadhi walialikwa kuhudhuria. Makundi ya watu walifurika kusikiliza mahubiri. Siyo tu kwenye kanisa dogo, lakini pia vyumba vya kungojea na kumbi zilijaa. Maelfu ya watu kila siku walikusanyika—wana wa mfalme, wanasiasa, wanasheria, wafanya biashara, na mafundi.

Mfalme, badala ya kupiga marufuku mikusanyiko, aliamrisha kuwa makanisa mawili ya jiji la Paris yafunguliwe. Ilikuwa haijawahi kutokea kwa jiji kutikiswa na neno la Mungu kama wakati huo. Roho ya uzima kutoka mbinguni ilionekana kama vile imepuliziwa kwa watu. Kiasi, usafi, utaratibu, na bidii vilikuwa vikichukua nafasi ya ulevi, ubadhirifu, migogoro, na uvivu. Lakini mamlaka za kanisa hazikujikalia kivivu. Mfalme bado alikataa kuingilia na kusimamisha mahubiri, na mamlaka za Kiroma ziliwageukia wananchi. Hakuna njia ambayo haikutumika kuamsha hofu, chuki, na itikadi kali kwa umati uliokuwa katika ujinga na ushirikina. Kwa kujisalimisha bila kuelewa mambo vizuri kwa walimu wao wa uongo, Paris, kama mji wa Yerusalemu wa zamani, hakujua wakati wa kujiliwa kwake wala hakujua mambo yaliyopasa kujua ili kudumisha amani yake. Kwa miaka miwili neno la Mungu lilihubiriwa katika mji mkuu; lakini, wakati wakiwepo wengi walioikubali injili, watu

walio wengi zaidi waliikataa. Fransis alijifanya kuwa na uvumilivu wa kidini kwa muda, lakini ilikuwa kwa kusudi la kulinda maslahi yake binafsi, na watetezi wa upapa walifaulu kurudi Fansikatika umaarufu na utawala. Kwa mara nyingine makanisa yalifungwa, na mateso yakaanza.

Calvin alikuwa bado Paris, akijiandaa kwa kujifunza, kutafakari, na kuomba kwa ajili ya kazi yake ya baadaye, na aliendelea kueneza nuru. Hatimaye, hata hivyo, mashaka yalijengeka juu yake. Mamlaka za kanisa ziliazimia kumleta katika ndimi za moto. Akijidhania kuwa salama katika chumba cha peke yake, hakuwa na wazo lo lote la hatari, wakati marafiki walipofika chumbani mwake wakiwa na haraka wakiwa na habari kuwa maofisa walikuwa njiani kuja kumkamata. Wakati huo huo walisikia watu wakigonga kwa nguvu kwenye lango la nje. Hakukuwa na muda wa kupoteza. Baadhi ya marafiki zake walifanya kazi ya kuwacheleweshа maofisa mlangoni, wakati marafiki zake wengine wakimsaidia kutoroka kupitia dirishani, baada ya kutoka aliondoka haraka kuelekea katika maeneo ya nje ya jiji. Baada ya kupata hifadhi katika kibanda cha kibarua aliyekuwa muumini wa matengenezo, alijigeuza kwa kuvaa nguo za mwenyeji wake, na, akiwa amebeba jembe begani, alianza safari yake. Akisafiri kuelekea upande wa kusini, alipata tena kimbilio katika utawala wa Margaret. (Tazama D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 2, ch. 30.)

Alibaki hapa kwa miezi michache, akiwa salama chini ya ulinzi wa marafiki wenye nguvu, na akiendelea kujifunza kama hapo awali. Lakini moyo wake ulikuwa umejielekeza kuihubiri Ufaransa, na hakuweza kutulia kwa muda mrefu. Muda mfupi baada ya dhoruba kutulia kwa kiasi fulani, alitafuta eneo la kufanyia kazi kule Pointiers, palipokuwa na chuo kikuu, na mahali ambapo mawazo mapya yalikuwa yamekubalika. Watu wa tabaka zote walisikiliza injili kwa furaha.

Hakukuwa na mahubiri ya hadhara, bali katika nyumba ya hakimu mkuu, katika nyumba yake ya kulala, na nyakati zingine katika bustani ya umma, Calvin alifungua maneno ya uzima kwa wale waliopenda kusikiliza. Baada ya muda mfupi, idadi ya wasikilizaji ilipoongezeka, ilifikiriwa kuwa salama zaidi kukutania nje ya jiji. Pango lililokuwa ubavuni mwa bonde lenye kina kirefu na jembamba, mahali ambapo miti na miamba iliinamia liliweka mazingira yaliyojificha kikamilifu zaidi, lilichaguliwa kuwa mahali pa kukutania. Makundi madogo madogo, yakiondoka jijini kwa njia tofauti, yalielekea kule. Katika kituo hiki kitulivu Biblia ilisomwa kwa sauti na kufafanuliwa. Hapa Meza ya Bwana ilisherehekewa kwa mara ya kwanza na Waprotestanti wa Ufaransa. Kutokana na kanisa hili wainjilisti waaminifu walitumwa kwenda maeneo mengine.

Kwa mara nyingine tena Calvin alirudi Paris. Hata wakati huo bado alikuwa na tumaini kuwa Ufaransa kama taifa itapokea Matengenezo. Lakini aligundua kuwa karibu kila mlango wa kazi ulikuwa umefungwa. Kufundisha injili ilikuwa kuingia katika barabara iliyoelekea

moja kwa moja kwenye nguzo ya kuchomea watu moto, na hatimaye aliazimia kuondoka na kwenda Ujerumani. Muda mfupi tu baada ya kuondoka Ufaransa dhoruba ya mateso iliwapasukia Waprotestanti, kiasi kwamba, ikiwa angeendelea kukaa hapo, lazima angeingizwa katika maangamizi ya jumla.

Wanamatengenezo Wafaransa, wakiwa na shauku ya kuiona nchi yao ikiwa na kasi sawa na Ujerumani na Uswisi, waliazimia kupiga bomu kwa ujasiri dhidi ya ushirikina wa Roma—bomu ambalo lingeamsha taifa lote. Katika kutekeleza jambo hilo mabango yaliyoshambulia misa katika usiku mmoja yalibandikwa katika nchi yote ya Ufaransa. Badala ya kuendeleza matengenezo, hatua hii ya kijasiri lakini isiyokuwa na busara ilileta madhara, siyo tu kwa walioitekeleza, bali pia kwa marafiki wa imani ya matengenezo katika nchi yote ya Ufaransa. Iliwapa viongozi wa Roma kile walichokuwa wakikitafuta kwa muda mrefu—kisingizio cha kudai kuwaua wazushi kama watu wenye fujo walio hatari kwa uimara wa kiti cha enzi na amani ya taifa.

Kwa njia ya mkono wa siri—iwe wa rafiki asiye na tahadhari au wa adui mwenye hila haikuweza kujulikana—moja ya mabango lilibandikwa kwenye mlango wa chumba cha kulala cha mfalme. Mfalme alipata hofu sana. Kwenye bango hilo, mambo ya kishirikina yaliyoheshimiwa kwa zama nyingi yalikuwa yameshambuliwa kwa mkono usio na hofu. Na huu ujasiri usio na mfano wa kuandika maneno haya ya wazi na kushtusha mbele ya mfalme uliamsha ghadhabu ya mfalme. Kwa mshangao alisimama kwa muda mfupi akitetemeka huku akiwa kimya. Hatimaye ghadhabu yake ilianza kuongea maneno ya kutisha: “Wakamatwe wote bila kumwacha mtu ye yote anayeshukiwa kuwa mfuasi wa uzushi wa Luther. Nitawanyonga wote.— Ibid., b. 4, ch. 10. Uamuzi ukafanyika. Mfalme aliazimia kujitupa kikamilifu upande wa Roma.

Hatua zilichukuliwa mara moja kumkamata kila mfuasi wa Luther katika jiji la Paris. Fundi mmoja maskini, mfuasi wa imani ya matengenezo, aliyekuwa na mazoea ya kuwaita waumini waende katika mikutano yao ya siri, alikamatwa na, kwa tishio la kuuawa mara moja kwenye nguzo ya kuchomea watu, aliamuriwa kuongoza wajumbe wa papa kwenda kwa nyumba ya kila Mprotestanti katika jiji. Alisita kwa hofu kubwa kukubaliana na pendekezo hilo, lakini hatimaye hofu ya ndimi za moto ilishinda, na alikubali kuwa msaliti wa ndugu zake. Akiwa ametanguliwa na mwenyeji wake, na akiwa amezungukwa na kundi la mapadri, wabeba vyetezo, watawa, na maaskari, Morin, mpelelezi wa mfalme, akiwa na msaliti, polepole na kimyakimya walipita katika mitaa ya jiji.

Gwaride lilionekana kama la kuheshimu “sakramenti takatifu,” tendo la kulipa fidia kwa ajili ya tusi la wapinzani dhidi ya misa. Lakini gwaride hilo lilificha kusudio la mauaji. Baada ya kufika karibu na nyumba ya mfuasi wa Luther, msaliti alionesha ishara, lakini bila kutamka neno lo lote. Msafara ulisimama, nyumba iliingiwa, wanafamilia waliburuzwa nje na kufungwa minyororo, na kikundi cha kutisha kiliendelea mbele kutafuta wahanga wapya.

Msafara huu “haukuacha nyumba yo yote, iwe kubwa au ndogo, hata vyuo vilivyokuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Paris.....Morin alitetemesha jiji lote Ulikuwa utawala wa hofu.”—Ibid., b. 4, ch. 10.

Wahanga waliuawa kwa maumivu ya kutisha, hususan kwa kuwa iliamuriwa kuwa moto upunguzwe ili kurefusha muda wa uchungu wao. Lakini walikuwa kama washindi. Msimamo wao haukuyumba, amani yao haikuwa na mashaka. Watesi wao, kwa kukosa nguvu ya kuyumbisha uthabiti wao usiobadilika, walijisikia kushindwa. “Vitanda vya kuchomea watu moto vilitawanywa katika mitaa yote ya Paris, na uchomaji watu ulifanywa kwa siku zilizofuata mfululizo, lengo likiwa kueneza hofu ya uzushi kwa kueneza mauaji. Faida, hata hivyo, hatimaye, ilibaki upande wa injili. Paris yote iliwezeshwa kuona aina ya watu ambao mawazo mapya yaliweza kuzalisha. Hakukuwa na mimbari bora zaidi kuzidi ile ya rundo la maiti za wafia dini. Furaha yenye amani iliyoangaza katika nyuso za hawa watu walipokuwa wakipita … wakielekea mahali pa kunyongewa, ushujaa wao waliposimama katikati ya ndimi za moto zenye uchungu, msamaha wao wa unyenyekevu kwa maumivu waliyoyapata, vilibadilisha, siyo mara chache, hasira kuwa huruma, chuki kuwa upendo, na kuunga mkono kazi ya injili kwa ufasaha usiopingika.”—Wylie, b. 13, ch. 20.

Makasisi, wakiwa wamejielekeza kudumisha hasira katika viwango vyake vya juu kama ilivyozoeleka, walisambaza mashtaka ya kutisha dhidi ya Waprotestanti. Waprotestanti walishitakiwa kwa kupanga njama za kuangamiza Wakatoliki, kupindua serikali, na kumwua mfalme. Hakuna hata kivuli cha ushahidi walichoweza kutoa ili kuthibitisha madai hayo. Hata hivyo utabiri huu wa matukio mabaya ulipaswa kufikia utimilifu; licha ya kwamba ilikuwa katika mazingira tofauti kabisa, , na kutokana na sababu zilizo kinyume kabisa katika namna yake. Mambo ya kikatili ambayo Wakatoliki waliwafanyia Waprotestanti wasiokuwa na hatia yalirundikana na kuwa mzigo wa kisasi, na baada ya karne nyingi yaliwaletea majanga yale yale ambayo walikuwa wameyatabiri kuwa yangekuja, juu ya mfalme, serikali yake, na raia wake; lakini yaliletwa na watu wasiomjua Mungu na wafuasi wa upapa wenyewe. Ilikuwa siyo ustawishaji, bali ukandamizaji wa Uprotestanti, ambao, miaka mia tatu baadaye, ulileta juu ya Ufaransa majanga haya.

Mashaka, kutoaminiana, na hofu sasa vilienea katika matabaka yote ya jamii. Katikati ya taharuki ya jumla ya watu ilionekana jinsi ambavyo mafundisho ya Luther yalivyokuwa yameshika akili za watu waliokuwa na kiwango cha juu cha elimu, mvuto, na uzuri wa tabia. Nafasi za amana na heshima kwa ghafla zikawa tupu. Mafundi, wachapishaji, wasomi, maprofesa katika vyuo vikuu, waandishi, na hata watu wa mitaani, walitoweka. Mamia ya watu walilikimbia jiji la Paris, wakiwa wakimbizi kutoka katika nchi yao walikozaliwa, katika matukio mengi jambo lililoonesha kwa mara ya kwanza kuwa waliipenda imani ya matengenezo. Viongozi wa upapa waliwatazama watu hao kwa mshangao wakipata wazo la uwepo wa wazushi walioishi nao bila kujua. Hasira yao iliwaka juu ya makundi ya watu maskini waliokuwa ndani ya uwezo wao. Magereza yalijaa wafungwa, na hewa iligeuka kuwa

na utusitusi kwa sababu ya wingi wa watu waliochomwa moto-watu waliounguzwa kwa kuikiri injili.

Fransis I alikuwa ametukuka kwa kuwa kiongozi katika vuguvugu kubwa la elimu lililoashiria ufunguzi wa karne ya kumi na sita. Alifurahia kukusanya katika ikulu yake wasomi kutoka kila nchi. Kupenda kwake elimu na dharau yake dhidi ya ujinga na ushirikina wa watawa vilikuwa, kwa kiasi fulani, sababu ya uvumilivu aliouonesha kwa matengenezo. Lakini, kwa kuchochewa na juhudi ya kukomesha uzushi, mlezi huyu wa elimu alitoa amri iliyopiga marufuku uchapishaji wa vitabu katika nchi yote ya Ufaransa! Fransis I anawasilisha mmoja miongoni mwa mifano mingi iliyopo katika kumbukumbu kuwa makuzi ya kiakili siyo tiba dhidi ya chuki za kidini na mateso.

Kwa njia ya sherehe kubwa na ya hadhara Ufaransa ilijiweka kikamilifu katika kuangamiza Uprotestanti. Makasisi walidai kuwa dharau ambayo ilikuwa imetendeka dhidi ya Mbingu za Juu kwa kupiga marufuku misa ilipaswa kupatanishwa kwa njia ya damu, na kwamba mfalme, kwa niaba ya watu wake, alitakiwa atoe tamko lake hadharani kubariki kazi hiyo ya kutisha. Tarehe 21 ya Januari, 1535, ilipangwa kwa ajili ya sherehe hiyo ya kutisha.

Hofu za kishirikina na chuki isiyokuwa na msingi ya taifa zima viliamshwa. Jiji la Paris lilifurika umati mkubwa wa watu kutoka katika nchi jirani kiasi kwamba mitaa yote ilijaa watu. Siku ilikaribishwa kwa maandamo makubwa yanayoduwaza. "Nyumba zilizokuwa kandokando ya njia maandamano yalikopita vilining'inizwa vitambaa vya maombolezo, madhabahu zilijengwa kila baada ya umbali fulani." Mbele ya kila mlango uliwashwa mwenge kuheshimu "sakramenti takatifu." Kabla ya mapambazuko waandamanaji walijipanga katika viwanja vya ikulu ya mfalme. "Mbele kulikuwepo bendera na misalaba kutoka kila parokia; halafu walifuata raia, wakitembea wawili wawili, na wakibeba mienge." Mashirika manne ya watawa yalifuata, kila shirika likiwa na mavazi yao tofauti na ya kipekee. Halafu lilikuja kundi la watu waliobeba mifupa mingi ya watakatifu. Baada ya watu hawa walifuata waheshimiwa viongozi wa kanisa katika mavazi yao ya zambarau na majoho mekundu na mapambo ya vito vya thamani, wakiwa na mwonekano wa kifahari na unaomeremeta.

"Hostia ilibebwa na askofu wa Paris chini ya mwavuli,… akisaidiwa na mapadri wanne wa damu.... Baada ya Hostia alifuata mfalme Fransis I siku hiyo hakuvaa taji, wala joho la dola." Akiwa na "kichwa wazi, macho yake yakiangalia chini, na katika mkono wake akishikilia mshumaa unaowaka moto," mfalme wa Ufaransa alionekana "katika hali ya kutubu."—Ibid., b. 13, ch. 21. Kwenye kila madhabahu aliinama chini kwa kujidhili, siyo kwa sababu maovu ya nafsi yake, wala kwa sababu isiyo na hatia iliyochafua mikono yake, bali kwa sababu ya watu wake waliothubutu kukataa misaa.

Baada ya mfalme alifuata malkia na waheshimiwa wa dola, nao wakitembea wawili wawili, kila mmoja akiwa na mwenge uliowashwa moto. Kama sehemu ya huduma za siku ile mfalme mwenyewe alihutubia maofisa wa ngazi za juu wa ufalme katika ukumbi mkubwa wa ikulu ya askofu. Kwa uso wenye huzuni alitokea mbele yao na kwa maneno yenye ufasaha na mguso aliomboleza "uhalifu, kufuru, siku ya huzuni na aibu," vimekuja juu ya taifa. Ndipo alitoa wito kwa kila raia mwema kusaidia katika kuondoa gonjwa la uzushi lililotishia kuangamiza Ufaransa. "Kwa hakika, ndugu waheshimiwa, mimi hapa mfalme wenu," alisema, "ikiwa ningejua kuwa mkono wangu mmojawapo ulikuwa na doa au umeugua uozo huu unaokera, ningeweza kuwapa muukate Na zaidi ya hapo, ikiwa ningeona mmojawapo wa watoto wangu amechafuliwa nao, nisingemwacha hai. na ningemtoa kafara kwa Mungu." Machozi yalikatiza hotuba yake, na mkutano wote ulilia na kutoa machozi, na kwa sauti moja walipiga kelele wakisema: "Tutaishi na kufa kwa ajili ya dini ya Kikatoliki!"—D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 4, ch. 12.

Giza nene la kutisha lilikuwa limekuja katika taifa lililokataa nuru ya ukweli. Neema "iletayo wokovu" ilikuwa imeonekana; lakini Ufaransa, baada ya kuangalia nguvu na utakatifu wake, baada ya maelfu kuvutwa na uzuri wake wa Kimbingu, baada ya majiji na vitongoji kuangaziwa nuru yake, ilikuwa imegeuka na kuipa nuru kisogo, na kuchagua giza kuliko nuru. Walitupilia mbali zawadi ya mbinguni ambayo ilikuwa imetolewa kwao. Waliuita uovu wema, na wema uovu, mpaka wakawa wahanga wa kujitakia wa kujidanganya wao wenyewe. Sasa, ingawa kimsingi waliamini kuwa walikuwa wakimfanyia Mungu huduma kwa kuwatesa watu Wake, bado udhati wao haukuwafanya wasiwe na hatia. Nuru ile ambayo ingewaokoa kutoka katika udanganyifu, kutoka katika kuchafua roho zao kwa hatia ya kumwaga damu, walikuwa wameikataa kwa uchaguzi wao wenyewe.

Kiapo kikuu cha kukomesha uzushi kilifanyiwa katika kanisa kubwa ambapo, takribani karne tatu baadaye, Mungu Mke wa Mantiki alitawazwa na taifa lililokuwa limemsahau Mungu aliye hai. Kwa mara nyingine tena maandamano yalipangwa, na wawakilishi wa Ufaransa walijipanga kuanza kazi ambayo walikuwa wameapa kuifanya. "Katika umbali wa karibu karibu majukwaa yalikuwa yamejengwa, ambapo Wakristo Waprotestanti fulani walipaswa kuchomwa moto wakiwa hai, na ilipangwa kuwa kuni ziwashwe wakati mfalme anapokaribia, na kwamba msafara usimame na kushuhudia mhanga akifa."—Wylie, b. 13, ch. 21. Maelezo ya kina ya maumivu waliyopitia hawa mashahidi wa Kristo yanatisha mno kiasi kwamba hayafai kusemwa; bali hakukuwa na kutetereka kwa aina yo yote kwa upande wa wahanga.

Alipolazimishwa akane, mmoja alijibu: "Ninaamini tu kile ambacho manabii na mitume walihubiri awali, na kile ambacho kundi lote la watakatifu walikiamini. Imani yangu ina uhakika kwa Mungu ambaye atazipinga nguvu zote za kuzimu."—D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 4, ch. 12.

Tena na tena msafara ulisimamishwa mahali pa mateso. Baada ya kufika mahali walipoanzia katika ikulu ya mfalme, watu walitawanyika, na mfalme na maaskofu waliondoka, wakiwa wameridhika na mwenendo wa shughuli ya siku ile huku wakijipongeza kuwa kazi ambayo ilikuwa imeanza ingeendelea hadi kukomesha kabisa uzushi.

Injili ya amani ambayo Ufaransa ilikuwa imeikataa hakika iling'olewa kabisa nchini, lakini matokeo yake yalikuwa ya kutisha. Tarehe 21 ya Mwezi Januari, 1793, miaka mia mbili hamsini na nane tangu siku ile ambayo Ufaransa ilianza rasmi kuwatesa Wanamatengenezo, maandamano mengine, yenye kusudi tofauti, yalipita katika mitaa ya Paris. "Safari hii tena mfalme ndiye alikuwa mhusika mkuu; safari hii tena kulikuwepo vurugu na makelele; safari hii tena zilikuwepo kelele kwa ajili ya wahanga wengine; safari hii tena yalikuwepo majukwaa meusi ya kuulia wahalifu; na safari hii tena mandhari ya siku hiyo ilifungwa kwa mauaji ya kikatili sana; Louis XVI, akipambana mkono kwa mkono na askari waliokuwa wakienda kumnyonga, alikokotwa kuelekea jukwaani, mahali pa kunyongea, na akiwa ameshikiliwa pale kwa nguvu shoka lilipigwa na kukata shingo na kichwa kilichotenganishwa na kiwiliwili kilibiringika jukwani."—Wylie, b. 13, ch. 21. Wala siyo mfalme peke yake aliyekuwa mhanga; jirani na hapo aliponyongewa mfalme watu elfu mbili na mia nane waliuawa kwa kunyongwa katika siku za umwagaji damu za Utawala wa Hofu.

Matengenezo yalikuwa yamewasilisha kwa ulimwengu Biblia iliyo wazi, yakifunua kanuni za sheria ya Mungu na kuhimiza madai yake katika dhamiri za watu. Upendo usio na kikomo ulikuwa umewafunulia watu amri na kanuni za mbinguni. Mungu alisema: "Zishikeni basi, mkazitende, maana hii ndiyo hekima yenu na akili zenu, machoni pa mataifa watakaozisikia amri hizi zote, nao watasema, Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili" (Kumbukumbu 4:6). Wakati Ufaransa ilipotupilia mbali zawadi ya mbinguni, Ufaransa ilipanda mbegu ya uasi na uharibifu; na utendaji kazi usioepukika wa asili na athari ulizalisha Mapinduzi na Utawala wa Hofu.

Muda mrefu kabla ya mateso yaliyochochewa na mabango, Farel jasiri na makini alilazimika kuikimbia nchi alipozaliwa. Alihamia Uswisi, na kwa kazi zake, akijenga juu ya ile ya Zwingli, alisaidia katika kuyafanya Matengenezo yapokelewe zaidi. Miaka yake ya baadaye ilitumiwa hapa, lakini bado aliendelea kuchochea matengenezo katika nchi ya Ufaransa. Katika miaka yake ya kwanza ya ukimbizi, juhudi zake zilielekezwa hasa katika kupeleka injili katika nchi yake alikozaliwa. Alitumia muda mwingi akihubiri miongoni mwa raia wa nchi yake karibu na mpakani, ambapo kwa juhudi zisizochoshwa alifuatilia mgogoro na kusaidia kwa maneno yake ya kutia shime na ushauri. Kwa msaada wa wakimbizi wengine, vitabu vya Wanamatengenezo wa Kijerumani vilitafsiriwa katika lugha ya Kifaransa na, pamoja na Biblia ya Kifaransa, vilichapishwa kwa wingi. Kwa njia ya wainjilisti wa vitabu vitabu hivi viliuzwa kwa wingi katika nchi ya Ufaransa. Viligawiwa kwa wainjilisti wa vitabu kwa bei ndogo, ili faida inayopatikana iwawezeshe kuendeleza kazi hiyo.

Farel alianza kazi yake katika nchi ya Uswisi katika vazi la unyenyekevu la ualimu. Akiwa katika Parokia isiyofikika kirahisi, alitumia muda mwingi kufundisha watoto. Kando ya kufundisha masomo ya kawaida ya mtaala husika, kwa tahadhari alianzisha kufundisha kweli za Biblia, akitumaini kuwa kwa kupitia watoto angeweza kuwafikia wazazi. Walikuwepo baadhi walioamini, lakini mapadri walikuja na kuzuia kazi hiyo, na wananchi washirikina waliamshwa na kuleta upinzani dhidi yake. “Hiyo haiwezi kuwa injili ya Kristo,” mapadri walidai, “hususan kwa kuwa kuhubiri injili hiyo hakuleti amani, bali vita.”—Wylie, b. 14, ch. 3.

Kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa kwanza, alipoteswa katika jiji moja alikimbilia jiji lingine. Kutoka kijiji hadi kijiji, kutoka jiji hadi jiji, alikwenda, akisafiri kwa mguu, akistahimili njaa, baridi, na uchovu, na kila mahali akiwa katika hatari ya kuuawa. Alihubiri katika masoko, katika makanisa, nyakati zingine katika mimbari za makanisa makubwa. Nyakati zingine alikuta makanisa hayana wasikilizaji; nyakati zingine mahubiri yake yalikatizwa kwa makelele na kuzomewa; hali kadhalika aliwahi kuburuzwa kikatili kutoka katika mimbari. Zaidi ya mara moja aliwahi kukamatwa na kundi la watu na kupigwa hadi karibu ya kufa. Lakini alisonga mbele. Ingawa mara nyingi alikataliwa, bila kukata tamaa alirudi tena katika shambulizi; na, moja baada ya mwingine, alishuhudia miji na majiji ambayo yalikuwa ngome za upapa, zikifungua malango yake na kuipokea injili. Parokia ndogo ambayo hapo awali iliwahi kutumika muda si mrefu ilipokea imani ya matengenezo. Miji ya Morat na Neuchatel nayo pia ilikataa kaida za Kiroma na kuondoa sanamu zilizoabudiwa kutoka katika makanisa yao.

Farel alitamani kwa muda mrefu kusimika bendera ya Uprotestanti katika jiji la Geneva. Ikiwa jiji hili lingeongolewa, lingekuwa kitovu cha Matengenezo katika nchi za Ufaransa, Uswisi, na Italia. Akiwa na lengo hili kichwani mwake, aliendeleza kazi zake hadi miji mingi na vitongoji vingi vya karibu vilipoongolewa. Ndipo akiwa na rafiki yake mmoja waliingia katika jiji la Geneva. Lakini aliruhusiwa kuhubiri mahubiri mawili tu. Makasisi, baada ya kushindwa kupata hukumu ya kumnyonga kutoka kwa mamlaka za kiraia, walimwita mbele ya baraza la kikanisa, ambapo walikuja wakiwa na silaha zilizofichwa ndani ya majoho yao, wakiwa wamedhamiria kumwua. Nje ya ukumbi, kundi la watu wenye hasira, wakiwa na marungu na mapanga, lilikusanyika kuhakikisha kuwa anauawa ikiwa atafanikiwa kupona katika baraza. Uwepo wa mahakimu na maaskari wenye silaha, hata hivyo, ulimwokoa. Mapema asubuhi ya siku iliyofuata alipelekwa, na rafiki yake, ng’ambo ya ziwa hadi mahali palipo salama. Hivyo ndivyo juhudi zake za kwanza za kuihubiri Geneva zilivyoishia.

Kwa ajili ya jaribio la pili mtu wa hali ya chini zaidi alichaguliwa—mtu kijana, aliye mnyenyekevu katika mwonekano kiasi kwamba alidharauliwa hata na watu waliodai kuwa marafiki wa matengenezo. Lakini mtu kama huyo angefanya nini mahali ambapo Farel alikuwa amekataliwa? Ingewezekanaje mtu ambaye ana ujasiri na uzoefu mdogo astahimili dhoruba ambayo watu wenye nguvu na ujasiri zaidi walikuwa wamelazimika kuikimbia? “Si

kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi" (Zakaria 4:6). "Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu." "Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu" (1 Wakorintho 1:27, 25).

Froment alianza kazi kama mkuu wa shule. Ukweli alioufundisha kwa watoto shuleni, watoto nao waliwafundisha watu wa nyumbani kwao. Muda si mrefu wazazi walisikiliza Biblia ikifafanuliwa; darasa lilizidi kujazwa na wasikilizaji makini. Nakala za Agano Jipya na vijizuu vilisambazwa kwa wingi, na viliwafikia watu ambao wasingethubutu kuja wazi wazi kusikiliza mafundisho mapya. Baada ya muda mfupi huyu mtendakazi naye alilazimishwa kukimbia; lakini ukweli alioufundisha ulikuwa umeota katika akili za watu. Mbegu ya matengenezo ilikuwa imepandwa, na iliendelea kukua, kupata nguvu, na kuenea. Wahubiri walirudi, na kwa njia ya kazi zao ibada ya Kiprotestanti ilianzishwa katika jiji la Geneva hatimaye.

Jiji lilikuwa tayari limeshatangaza kuunga mkono Matengenezo wakati, baada ya mizunguko na mabadiliko mbalimbali, Calvin aliingia malangoni mwake. Akirudi kutoka ziara yake ya mwisho ya mahali alipozaliwa, alikuwa njiani kuelekea Basel, ambapo, baada ya kugundua kuwa barabara ya moja kwa moja ilikuwa inatumiwa na majeshi ya Charles V, alilazimika kupita katika njia ya mzunguko ya Geneva.

Katika ziara hii Farel aliuona mkono wa Mungu. Japokuwa Geneva ilikuwa imepokea imani ya matengenezo, bado kulikuwa na kazi kubwa ya kufanya hapo. Ni mtu mmoja mmoja na wala siyo kundi la watu wanaoongoka kumfuata Mungu; kazi ya kuzaliwa upya lazima ifanyike katika moyo na dhamiri kwa nguvu ya Roho Mtaktifu, siyo kwa amri za mabaraza. Wakati watu wa Geneva walipokuwa wametupilia mbali mamlaka ya Roma, hawakuwa tayari sana kuachana na uovu ambao ulishamiri chini ya utawala wa Roma. Kujenga kanuni safi za injili na kuandaa watu hawa kujaza kikamilifu nafasi ambazo Mungu alikuwa anawaita wazijaze haikuwa kazi ndogo.

Farel alikuwa na uhakika kuwa kwa kumpata Calvin alikuwa amepata mtu ambaye angeshirikiana naye katika kazi hii. Katika jina la Mungu alimwapisha mwinjilisti kwa kiapo kikuu abaki na kufanya kazi pale. Calvin alirudi nyuma kwa tahadhari. Akiwa mtu mwoga na mpenda amani, alisita kushikamana na roho jasiri, huru, na hata iliyo na fujo ya mtu wa Geneva. Udhaifu wa afya yake, pamoja na tabia yake ya kupenda kusoma, vilimsukuma kutafuta mahali pa kupumzika. Akiamini kuwa kwa njia ya kalamu yake angeweza kuchangia zaidi katika kazi ya matengenezo, alitamani apate mahali patulivu kwa ajili ya kusoma, na akiwa pale, kwa njia ya uandishi, afundishe na ajenge makanisa. Lakini wito wenye nguvu wa Farel ulimjia kama wito kutoka Mbinguni, na hakuthubutu kuukataa. Ilionekana kwake, alisema, "kana kwamba mkono wa Mungu ulikuwa umenyoshwa kutoka mbinguni, kana

kwamba ulimshika, na kumweka daima mahali ambapo hakuwa na uvumilivu wa kupaacha."— D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 9, ch. 17.

Wakati huu hatari kubwa iliikabili kazi ya Uprotestanti. Laana za papa ziliunguruma dhidi ya Geneva, na mataifa makubwa yalitishia kuiangamiza. Ni kwa jinsi gani jiji hili dogo lingeweza kupinga mamlaka hii kubwa ambayo mara nyingi iliweza kulazimisha wafalme na wafalme wakuu kujisalimisha? Ni kwa jinsi gani Geneva ingeweza kusimama dhidi ya majeshi ya washindi wakuu wa dunia?

Katika ulimwengu wote wa Ukristo, Uprotestanti ulihatarishwa na maadui wa kutisha. Ushindi wa kwanza ulipita, Roma ilikusanya nguvu mpya, ikitumaini kuangamiza Uprotestanti. Wakati huu shirika la Majesuti liliundwa, shirika katili, fidhuli, na lenye nguvu zaidi kuliko mashirika mengine yote ya kipapa. Wakiwa wamejitenga na mshikamano wowote wa kidunia na maslahi ya wanadamu, wakiwa hawana urafiki na mtu, akili na dhamiri vikiwa vimenyamazishwa kabisa, hawakujua kanuni nyingine, hawakuwa na mahusiano na mtu, isipokuwa uhusiano na shirika lao, na hawakuwa na wajibu mwingine zaidi ya kupanua mamlaka yake. (Tazama Kiambatisho.) Injili ya Kristo iliwawezesha wafuasi wake kukutana na hatari na kustahimili mateso, bila kukatishwa tamaa na baridi, njaa, suluba, na umaskini, kushikilia bendera ya ukweli mbele ya kitanda cha kutesea, gereza, na nguzo ya kuchomea watu moto.

Kushinda nguvu hizi, Ujesuiti ulihamasisha wafuasi wake kwa ushikiliaji sana mambo bila kutumia akili uliowawezesha kustahimili hatari kama hizo, na kupinga nguvu ya ukweli kwa kutumia sila za uongo. Hakukuwa na uhalifu mkubwa wowote ambao wasingeweza kuufanya, hakuna uongo wowote mbaya ambao wasingeweza kuusema, wala uigizaji wowote ambao wasingeweza kuufanya. Wakiwa wameapa kuishi maisha ya kimaskini na ya chini daima, ilikuwa ni kusudi lao la msingi kupata utajiri na madaraka, kujitolea kuangusha Uprotestanti, na kuanzisha upya ukuu wa upapa.

Walipoonekana kama wanachama wa shirika hilo la Ujesuti, walivaa vazi la utakatifu, wakitembelea magereza na hospitali, wakiwahudumia wagonjwa na maskini, wakitangaza kwa ulimwengu kuwa wameuacha ulimwengu, na kulibeba jina la Yesu, ambaye alikwenda kila mahali akitenda wema. Lakini makusudi ya kiuhalifu na kimauaji yalikuwa yamefichwa chini ya mwonekano huu mzuri wa nje. Ilikuwa kanuni ya msingi ya shirika hilo kuwa mwisho huhalalisha njia. Kwa kanuni hii, matendo ya uongo, wizi, udanganyifu, mauaji, siyo tu kuwa yalisameheka bali pia yalisifiwa, ikiwa yalilinda maslahi ya kanisa. Kwa kofia mbalimbali Majesuiti walipenya na kufanya kazi katika ofisi za serikali, wakipanda vyeo hadi kuwa washauri wa wafalme, wakipanga sera za mataifa. Walifanya kazi ya utumishi ili wawapeleleze mabwana zao. Walianzisha vyuo kwa ajili ya watoto wa kiume wa wana wafalme na malodi, na shule kwa ajili ya watu wa kawaida; na watoto wa wazazi wa

Kiprotestanti walilazimishwa kushika kaida za kipapa. Utukufu wote wa nje na kujionesha kwa ibada za Kiroma ulitumiwa kuchanganya, kuduwaza na kushika akili, na hivyo uhuru ambao baba zao waliutaabikia ulisalitiwa na watoto wao. Majesuiti kwa muda mfupi walijieneza katika Bara zima la Ulaya, na kokote walikokwenda, uamsho wa upapa ulitokea.

Ili kuwapa nguvu kubwa zaidi, amri ilitolewa kurudisha mahakama za uchunguzi. (Tazama Kiambatisho.) Licha ya chuki ya jumla ambayo watu walikuwa nayo dhidi ya mahakama hiyo, hata katika nchi za Kikatoliki, mahakama hii ya kutisha ilianzishwa tena na watawala wa kipapa, na ukatili wa kutisha kiasi cha kutoweza kuoneshwa wakati wa mchana ulirudiwa katika magereza ya siri. Katika nchi nyingi, maelfu kwa maelfu ya maua ya taifa, watu safi na waungwana, watu wenye akili na wenye elimu ya juu sana, wachungaji wacha Mungu na waliojiweka wakfu, watu wenye bidii na wazalendo, wasomi wenye uwezo mkubwa wa akili, wanasanaa wenye talanta, mafundi wenye stadi za juu kabisa, walichinjwa au walilazimishwa kukimbilia nchi zingine.

Hizo ndizo njia ambazo Roma ilizitumia kuzima nuru ya Matengenezo, kuwatenganisha watu na Biblia, na kurudisha ujinga na ushirikina wa Zama za Giza. Lakini chini ya mbaraka wa Mungu na kazi za watu waaminifu ambao Mungu aliwainua kumfuata Luther, Uprotestanti haukuangushwa. Nguvu yake haikutokana na upendeleo au silaha za wafalme. Nchi ndogo kabisa, mataifa maskini na dhaifu kabisa, zilitokea kuwa ngome ya Uprotestanti. Ilikuwa jiji la Geneva katikati ya maadui wenye nguvu wakipanga maangamizi yake; ilikuwa nchi ndogo ya Uholanzi kwenye pwani ya mchanga ya bahari ya kaskazini, iliyopambana dhidi ya ukatili wa Uhispania, ambayo wakati ule ulikuwa ufalme tajiri sana; ilikuwa nchi ndogo ya Swideni isiyo na rutuba, isiyovutia, ambayo ilipata ushindi kwa ajili ya Matengenezo.

Kwa karibu miaka thelathini Calvin alifanya kazi katika jiji la Geneva, kwanza kuanzisha kanisa pale linalosimamia maadili ya Biblia, na halafu kwa ajili ya kueneza Matengenezo katika Bara zima la Ulaya. Siyo kweli kuwa kazi yake kama kiongozi wa umma haikuwa na dosari, na siyo kweli pia kuwa mafundisho yake hayakuwa na makosa kabisa. Lakini alikuwa chombo kilichotumika kutangazia ukweli ambao ulikuwa na umuhimu wa pekee katika wakati wake, katika kudumisha kanuni za Uprotestanti dhidi ya wimbi la upapa lililokuwa linarudi kwa kasi, na katika kuhamasisha makanisa yaliyofanya matengenezo katika usahili na usafi wa maisha, badala ya kiburi na ufisadi vilivyojengwa na mafundisho ya Kiroma.

Kutoka Geneva, machapisho na walimu walitoka na kwenda kueneza mafundisho ya matengenezo. Mahali hapa ndipo palikuwa mahali ambapo watu wote walioteswa katika nchi zote walikuja kupata mafundisho, ushauri, na kutiwa moyo. Jiji la Calvin lilitokea kuwa makimbilio ya Wanamatengenezo waliowindwa katika nchi za Ulaya Magharibi. Wakikimbia dhoruba kali zilizoendelea kwa karne nyingi, wakimbizi walikuja kwenye malango ya Geneva. Wakiwa na njaa, wakiwa na majeraha, wakiwa hawana nyumba wala ndugu, walikaribishwa kwa furaha na walitunzwa kwa upendo; na baada ya kupata makazi hapa,

walilibariki jiji kwa ujuzi wao, elimu yao, na uchaji wao. Wengi waliopata hifadhi hapa walirudi katika nchi zao kupinga ukatili wa Roma. John Knox, Mwanamatengenezo jasiri wa Kiskochi, Wapuritani wa Kiingereza ambao hawakuwa wachache, Waprotestanti wa Uholanzi na Uhispania, na Hugenoti wa Ufaransa walichukua kutoka Geneva mwenge wa ukweli kuangaza giza la nchi zao walikozaliwa.

Sura ya 13 - Uholanzi na Skandinavia

Katika nchi ya Uholanzi, ukatili wa kipapa ulipata upinzani mkali tangu mapema kabisa. Miaka mia saba kabla ya wakati wa Luther, Kiongozi wa Kanisa la Roma alipingwa bila woga na maaskofu wawili, ambao, baada ya kutumwa Roma kwa kazi maalumu, waligundua tabia halisi ya "kiongozi mkuu wa kanisa": Mungu "ameweka malkia na mwenzi Wake, kanisa, kuwa ruzuku ya kutosha na ya milele kwa ajili ya familia yake, na mahari isiyofifia wala isiyoharibika, na kumpatia taji na fimbo ya milele; ... vyote ambavyo hutenda kazi kama mtego wa mwizi. Unajiweka mwenyewe katika hekalu la Mungu; badala ya mchungaji, umekuwa mbwa mwitu kwa kondoo; ... unataka tukuamini kama askofu mkuu, lakini una tabia ya ukatili. Wakati ulipaswa kuwa mtumishi wa watumishi, kama unavyojiita, unapambana kuwa bwana wa mabwana....

Unazidharau amri za Mungu Roho Mtakatifu ni mjenzi wa makanisa ulimwenguni kote Jiji la Mungu wetu, ambalo sisi ni raia wake, linapanuka na kuhusisha maeneo yote ya mbinguni; na ni kubwa zaidi kuliko jiji, ambalo manabii watakatifu waliliita Babeli, ambalo hujifanya kuwa la Kimungu, na hujitapa kuwa hekima yake ni ya milele; na hatimaye, ingawa bila sababu, kuwa jawahi kukosea, wala hawezi kukosea kamwe."— Gerard Brandt, History of the Reformation in and About the Low Countries 1:6.

Wenginewaliinukakutokakarnehadikarnewakitoamwangwiwaupinzani huu. Na wale walimu wa awali ambao, walitembelea nchi tofauti tofauti na wakijulikana kwa majina mbalimbali, wakiwa na tabia ya wamishenari Wawaldensia, wakisambaza kila mahali ukweli wa injili, waliingia Uholanzi. Mafundisho yao yalienea haraka. Waliitafsiri Biblia ya Kiwaldensia katika lugha ya Kidachi. Walitangaza "kuwa Biblia ilikuwa na manufaa makubwa sana; haina mizaha, haina hadithi za kubuni, haina upuuzi, haina uongo, bali ina maneno ya kweli; na kwamba kweli hapa na pale kulikuwepo na mambo magumu kuyaelewa. Lakini iko hivyo ili uzuri na utamu wa yale mepesi na matakatifu ugunduliwe kirahisi."— Ibid. 1:14. Hivyo ndivyo walivyoandika marafiki wa imani ya kale, katika karne ya kumi na mbili.

Sasa ndipo yalipoanza mateso ya Kiroma; lakini katikati ya matita ya kuni na mateso waumini waliendelea kuongozeka, wakitangaza kwa ujasiri kuwa Biblia ndiyo mamlaka pekee isiyokosea katika dini, na kwamba "hakuna mtu anayepaswa kulazimishwa kuamini, bali anapaswa kuongolewa kwa kuhubiriwa."—Martyn 2:87.

Mafundisho ya Luther yalipata udongo wenye rutuba katika nchi ya Uholanzi, na watu wa kweli na waaminifu waliinuka kuihubiri injili. Kutoka moja ya majimbo ya Uholanzi alitokea Menno Simmons. Akiwa amesomeshwa na Kanisa Katoliki la Roma na kuwekwa wakfu wa upadrisho, alikuwa hajui chochote kuhusu Biblia, na hakuisoma kwa kuogopa kushawishika na kuwa mzushi. Wakati mashaka kuhusiana na fundisho kuwa mkate na

mvinyo hubadilika kuwa mwili na damu halisi ya Yesu yalipomjia, aliyachukulia kama majaribu kutoka kwa Shetani, na kwa maombi na toba alipambana kuyashinda; lakini bila mafanikio. Kwa kujichanganya katika matukio ya starehe alijaribu kunyamazisha sauti ya dhamiri; lakini bila mafanikio. Baada ya muda alivutwa kujifunza Agano Jipya, na hili, pamoja na vitabu vya Luther vilimfanya aikubali imani ya matengenezo. Muda mfupi baada ya hapo alishuhudia katika kijiji jirani kukatwa kichwa cha mtu ambaye alikuwa ameuawa kwa kubatizwa mara ya pili. Jambo lililomfanya ajifunze Biblia kuhusiana na ubatizo wa watoto. Hakupata ushahidi wake katika Maandiko, lakini aliona toba na imani kila mahali kama sharti la kupokea ubatizo.

Menno aliachana na Kanisa la Kiroma na kujitolea maisha yake kufundisha kweli alizozipokea. Katika nchi za Ujerumani na Uholanzi kikundi cha watu wenye itikadi kali kilijitokeza, wakihubiri mafundisho ya kipuuzi na uchochezi, wakivunja utaratibu na uzuri, na wakihamasisha fujo na kuchochea uasi dhidi ya serikali. Menno aliona matokeo mabaya ambayo kwa hakika hatimaye vuguvugu hili lilikuwa zlinaenda kusababisha na alichukua hatua madhubuti kupinga mafundisho potovu na mipango ya hila ya watu wenye itikadi kali. Walikuwepo watu wengi, hata hivyo, waliokuwa wamepotoshwa na wapotoshaji hawa, lakini walioacha mafundisho yao yasiyofaa; na walikuwepo bado waliosalia wengi wa Wakristo wa zamani, matunda ya mafundisho ya Wawaldensia. Menno alifanya kazi miongoni mwa makundi haya ya watu kwa bidii na mafanikio makubwa.

Kwa miaka ishirini na tano alisafiri, akiwa na mkewe na watoto wao, akistahimili shida kubwa na kujinyima kwingi, na mara nyingi kwa kuhatarisha maisha yake. Alizunguka mara nyingi katika nchi ya Uholanzi na maeneo ya magharibi ya nchi ya Ujerumani, akifanya kazi zaidi miongoni mwa makundi ya watu wa chini lakini akiwa na mvuto mkubwa miongoni mwa watu wengi zaidi. Akiwa na uwezo wa asili wa kuongea kwa ufasaha, ingawa elimu yake ilikuwa ya wastani tu, alikuwa mtu mwenye uadilifu usioyumba, mwenye roho ya unyenyekevu na tabia ya upole, na mtu mkweli na mcha Mungu wa dhati, akionesha kwa mfano maishani mwake kanuni ambazo alizifundisha, na aliaminiwa na watu. Wafuasi wake walitawanywa na kuonewa. Waliumizwa zaidi kwa kushindwa na kikundi cha wenye itikadi kali cha Wamansteri. Hata hivyo watu wengi waliongolewa kutokana na kazi zake.

Hakuna mahali ambapo mafundisho ya kimatengenezo yalipokelewa kwa furaha na watu wengi zaidi kuliko katika nchi ya Uholanzi. Ni katika nchi chache ambapo wafuasi wa matengenezo walistahimili mateso ya kutisha zaidi kuliko katika nchi ya Uholanzi. Katika nchi ya Ujerumani, Charles V alipiga marufuku Matengenezo, na alitamani kuwachoma moto wafuasi wote wa Matengenezo; lakini wakuu walikuwa kikwazo dhidi ya ukatili wake. Katika nchi ya Uholanzi, mfalme alikuwa na nguvu zaidi, na maagizo yake ya utesaji yalifuatana moja baada ya lingine kwa haraka haraka. Kusoma Biblia, kuisikiliza au kuihubiri, au hata kuizungumzia, ilikuwa ni kujitakia adhabu ya kifo cha kuchomwa moto. Kumwomba Mungu kwa siri, kukataa kuinamia sanamu, au kuimba zaburi, adhabu yake ilikuwa kifo. Hata wale

ambao walikana makosa yao walihukumiwa, ikiwa walikuwa wanaume, kuuawa kwa upanga; ikiwa walikuwa wanawake, kuzikwa wakiwa hai. Maelfu ya watu yaliangamia chini ya utawala wa Charles na wa Philip II.

Wakati mmoja familia nzima ililetwa mbele ya mahakama ya uchunguzi, wakishitakiwa kwa kutokuhudhuria misa na kuabudia nyumbani. Walipohojiwa kuhusu ibada zao za siri mtoto wao wa mwisho wa kiume alijibu: "Tunapiga magoti, na kuomba kuwa Mungu aangazie akili zetu na asamehe dhambi zetu; tunamwombea mfalme wetu, kwamba utawala wake ufanikiwe na maisha yake yawe ya furaha; tunawaombea mahakimu wetu, kwamba Mungu awalinde na awatunze."—Wylie, b. 18, ch. 6. Baadhi ya majaji waliguswa sana, hata hivyo baba na mmoja wa watoto wake wa kiume walihukumiwa kuchomwa moto.

Hasira ya watesaji ililingana na imani ya wafia dini. Siyo wanaume tu bali pia hata wanawake na mabinti dhaifu walionesha ujasiri usioyumba. "Wake walisimama pembeni mwa waume zao waliokuwa wakichomwa moto, na wakati wanaume walipokuwa wakiungua moto wake zao walinong'oneza maneno ya faraja, au kuwaimbia zaburi au kuwatia moyo." "Mabinti walilala katika makaburi yao kana kwamba walikuwa wakiingia katika vyumba vyao vya kulala usiku; au walienda kwenye jukwaa la kunyongea na moto, wakiwa wamevaa nguo nzuri kabisa, kana kwamba walikuwa wanaenda kwenye harusi zao."—Ibid., b. 18, ch. 6.

Kama ilivyokuwa katika siku ambapo upagani ulipamba moto kuangamiza injili, damu ya Wakristo ilikuwa mbegu. (Tazama Tertullian, Apology, paragraph 50.) Mateso yalichochea ongezeko la idadi ya mashahidi kwa ajili ya ukweli. Mwaka baada ya mwaka mfalme, kwa kukasirishwa sana na msimamo usioyumba wa watu, aliongeza ukatili katika kazi yake ya utesaji; lakini bila mafanikio. Chini ya uongozi wa mheshimiwa William wa Orange Mapinguzi yalileta uhuru wa kuabudu katika nchi ya Uholanzi.

Katika milima ya Piedmont, katika nyika za Ufaransa na pwani za Uholanzi, maendeleo ya kazi ya injili yalienda sambamba na umwagikaji wa damu ya wanafunzi. Lakini katika nchi za Kaskazini injili ilipenya kwa amani. Wanafunzi katika jiji la Wittenberg, waliporudi nyumbani kwao, walipeleka imani ya matengenezo katika nchi za Scandinavia. Machapisho ya maandishi ya Luther pia yalisambaza nuru. Watu sahili, wavumilivu wa Kaskazini waliacha ufisadi, majivuno, na ushirikina wa Roma, wakakaribisha usafi, usahili, na kweli za Biblia zinazobadilisha maisha.

Tausen, "Mwanamatengenezo wa Denmark," alikuwa mtoto wa kiume wa mkulima. Kijana huyu tangu awali alithibitisha kuwa na akili nyingi; alitamani sana elimu; lakini jambo hili halikuwezekana kwa sababu ya hali ya wazazi, hivyo aliingia nyumba ya watawa. Hapa, usafi wake wa maisha, pamoja na bidii na uaminifu wake, vilimfanya kupendwa na mkubwa wake. Mtihani ulionesha kuwa alikuwa na talanta ambayo kwayo siku moja angeweza

kulihudumia kanisa vizuri. Iliazimiwa kuwa asomeshwe katika moja ya vyuo vikuu vya Ujerumani au Uholanzi. Mwanafunzi huyu kijana alipewa ruhusa ya kuchagua shule aliyoipenda, kwa sharti moja tu, kuwa asiende Wittenberg. Msomi wa kanisa hakupaswa kuhatarishwa kwa sumu ya uzushi. Hivyo ndivyo watawa walivyosema.

Tausen alikwenda Cologne, mahali ambapo nyakati hizo, kama ilivyo sasa, ni moja ya ngome kubwa za Uroma. Hapa haukupita muda mrefu alianza kuchukizwa na imani zisizoeleweka za walimu. Wakati huo huo alipata maandishi ya Luther. Aliyasoma kwa mshangao na furaha, na alitamani sana kupata mafundisho binafsi kutoka kwa Mwanamatengenezo mwenyewe. Lakini ili kufanya hivyo alilazimika kumkasirisha mkubwa wake wa nyumba ya watawa na kujinyima ufadhili wa masomo yake. Muda siyo mrefu uamuzi wake ulifanywa, na haikuchukua muda alidahiliwa kama mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Wittenberg.

Aliporudi Denmark, alirudi tena katika nyumba yake ya watawa. Hakuna mtu aliyekuwa amejua juu ya Ulutheri wake; hakufichua siri yake, lakini alijitahidi, bila kuamsha chuki za wenzake, kuwaongoza kwenye imani safi na maisha matakatifu zaidi. Alifungua Biblia, na kueleza maana yake ya kweli, na mwishowe aliwahubiri juu ya Kristo kama njia ya kuhesabiwa haki kwa mwenye dhambi na tumaini pekee la wokovu. Ghadhabu ya mkuu wa nyumba ya watawa ilikuwa kubwa sana, kwani alikuwa amejenga matumaini makubwa sana kwake kama mtetezi shujaa wa Roma. Aliondolewa katika nyumba yake ya kitawa na kupelekwa katika chumba cha peke yake chini ya usimamizi mkali.

Katika hatua ambayo iliwaogofya sana wasimamizi wake baadhi ya watawa muda si mrefu walitangaza kuwa wameongoka na wamepokea Uprotestanti. Kupitia nondo za chumba chake Tausen alikuwa amewafundisha marafiki zake mafundisho ya kweli. Kama wale mapadri wangekuwa na stadi za kanisa za kushughulikia uzushi, sauti ya Tausen isingeweza kusikika tena kamwe; lakini badala ya kumtupa kaburini katika gerezani la ardhini, walimwondoa katika nyumba ya watawa peke yake. Sasa walikuwa hawana nguvu tena. Amri ya mfalme, ambayo ndiyo tu ilikuwa imetolewa, ilitoa ulinzi kwa walimu wa mafundisho mapya. Tausen akaanza kuhubiri. Makanisa yalifunguliwa kwa ajili yake, na watu walifurika kumsikiliza. Wengine pia walihubiri neno la Mungu. Agano Jipya, lililokuwa limetafsiriwa katika lugha ya Kidanishi, lilisambazwa sana. Juhudi za watetezi wa upapa za kutaka kushindana na kazi ya Uprotestanti ziliishia katika kuusambaza zaidi, na muda si mrefu nchi ya Denmark ilitangaza kupokea kwake imani ya matengenezo.

Katika nchi ya Sweden, pia, vijana waliokuwa wamekunywa maji ya kisima cha Wittenberg walibeba maji ya uzima na kuwapelekea watu wa nchi yake. Viongozi wawili wa Matengenezo ya Kiswidishi, Olafu na Laurentio Petri, watoto wa kiume wa mhunzi wa Orebro, walijifunza chini ya Luther na Melanchthon, na kweli walizojifunza walizifundisha kwa bidii. Kama Mwanamatengenezo mkuu, Luther, Olafu aliwagusa watu kwa sababu ya

bidii na ufasaha wake, wakati Laurentio, kama Melanchthon, alikuwa msomi, mwenye fikra nyingi, na mkimya. Wote wawili walikuwa wacha Mungu wa dhati, wenye uwezo mkubwa wa kiteolojia, na wenye ujasiri usiotetereka katika kueneza ukweli. Upinzani wa watetezi wa upapa ulikuwepo. Padri wa Kikatoliki aliwachochea watu wajinga na washirikina. Olafu Petri alishambuliwa na kundi la hao watu, na katika matukio kadhaa aliponea chupu chupu kuuawa. Hata hivyo, Wanamatengenezo hawa, walipendwa na kulindwa na mfalme.

Chini ya utawala wa Kanisa la Roma watu walikuwa wamezamishwa katika umaskini na kushikiliwa katika ukandamizwaji. Hawakuwa na Maandiko; na wakiwa na dini ya ishara na sherehe tu, ambayo haikupeleka nuru yoyote akilini, walikuwa wakirudi katika imani za kishirikina na matendo ya kipagani ya mababu zao waabudu mizimu. Taifa liligawanyika katika makundi makundi, ambayo migogoro yao isiyoisha iliongeza matatizo ya wote. Mfalme aliazimia kuleta matengenezo katika serikali na kanisa, na aliwakaribisha wasaidizi hawa wenye uwezo katika vita dhidi ya Roma.

Akiwa mbele ya mfalme na viongozi wa ngazi za juu wa Swideni, Olafu Petri kwa uwezo mkubwa alitetea mafundisho ya imani ya matengenezo dhidi ya mashujaa watetezi wa Uroma. Alitangaza kuwa mafundisho ya mapadri inapasa yapokelewe pale tu yanapopatana na Maandiko; kwamba mafundisho muhimu ya imani yawasilishwe katika Biblia katika namna iliyo ya wazi na sahili, ili watu wote waweze kuyaelewa. Kristo alisema, “Mafundisho Yangu siyo Yangu, bali Yake Yeye aliyenituma” (Yohana 7:16); na Paulo alitangaza kuwa kama angehubiri injili nyingine tofauti na ile aliyoipokea, angepaswa kulaaniwa (Wagalatia 1:8). “Iweje, basi,” alisema Mwanamatengenezo,“watu wengine wajipe mamlaka ya kutunga sheria zao, kwa mapenzi yao wenyewe, na kuwalazimisha wengine kuzitii kama mambo muhimu kwa ajili ya wokovu?”—Wylie, b. 10, ch. 4. Alionesha kuwa amri za kanisa hazina mamlaka ikiwa zinapingana na amri za Mungu, na alisisitiza kanuni kuu ya Kiprotestanti kuwa “Biblia na Biblia pekee” ni kanuni ya imani na matendo.

Shindano hili, ingawa lilifanyikia katika jukwaa la siri, kwa kiasi fulani, linatuonesha“ainayawatuwaliokuwamaaskariwajeshilaWanamatengenezo. Hawakuwa watu wasiojua kusoma na kuandika, wabaguzi wa kidini, wabishi na wapiga kelele tu—walikuwa tofauti kabisa na kitu kama hicho; walikuwa watu waliokuwa wamelisoma neno la Mungu, na walijua vizuri jinsi ya kutumia silaha ambazo Biblia, kama ghala la silaha, inaweza kuzitoa. Katika suala la elimu, walikuwa mbele ya zama zao. Tunapoelekeza macho yetu katika vituo makini kama Wittenberg na Zurich, na kwa majina mashuhuri kama ya akina Luther na Melanchthon, ya Zwingli na Okolampadio, tunajikuta tukiwa tayari kuambiwa, hawa walikuwa viongozi wa hili vuguvugu, na inatupasa kwa kawaida kutarajia kwao nguvu ya ziada na maarifa mengi; lakini watu waliokuwa chini yao hawakuwa kama wao. Ndiyo, tunageukia maeneo yasiyojulikana sana kama ya Swideni, na majina madogo ya Olafu na Laurentio Petri—kutoka kwa walimu hadi kwa wanafunzi—tunakuta nini? ... Wasomi na wanateolojia; watu ambao waliuelewa kikamilifu mfumo mzima wa ukweli wa injili, na

wanawaoshinda kirahisi wanafalsafa wa dhana mbalimbali na waheshimiwa wa Roma."—Ibid., b. 10, ch. 4.

Kama matokeo ya mdahalo huu, mfalme wa Swideni aliipokea imani ya Kiprotestanti, na siyo muda mrefu baadaye bunge lilitangaza kuunga mkono imani ya Kiprotestanti. Agano Jipya lilikuwa limetafsiriwa na Olafu Petri katika lugha ya Kiswidishi, na maelekezo ya mfalme wale ndugu wawili walitafsiri Biblia nzima. Kwa hiyo, kwa mara ya kwanza watu wa Swideni walipokea neno la Mungu katika lugha yao wenyewe. Baraza Kuu la Kitaifa liliamuru kuwa katika ufalme wote, wachungaji wafafanue Maandiko na kuwa watoto katika shule wafundishwe kuisoma Biblia.

Pole pole lakini kwa uhakika, baraka hii ya nuru ya injili ilifukuza giza la ujinga na ushirikina. Likiwa limekombolewa kutoka katika uonevu wa Kiroma, taifa la Swideni lilipata nguvu na utukufu ambao lilikuwa halijaupata kabla ya hapo. Swideni ikawa ngome ya Uprotestanti. Karne moja baadaye, wakati wa hatari kubwa kuliko wakati mwingine wowote, nchi hii ndogo ambayo siku za nyuma lilikuwa taifa dhaifu—taifa pekee katika Bara la Ulaya lililothubutu kutoa mkono wa msaada—liliikomboa Ujerumani katika mgogoro wa kutisha wa Vita ya Miaka Thelathini. Kaskazini yote ya Bara la Ulaya ilionekana kurejeshwa tena chini ya utawala katili wa Kiroma. Majeshi ya Swideni ndiyo yaliyoiwezesha Ujerumani kugeuza mkondo wa mafanikio ya upapa, kupata uvumilivu wa kidini kwa ajili ya Waprotestanti,--Wakalvini na Walutheri,— na kurudisha uhuru wa dhamiri kwa nchi zilizokubali Matengenezo.

Sura ya 14 – Wanamatengenezo wa Baadaye Uingereza

Wakati Luther alipokuwa akiifungua Biblia iliyokuwa imefungwa kwa watu wa Ujerumani, Roho wa Mungu alimsukuma Tyndale kufanya jambo hilo hilo kwa nchi ya Uingereza. Biblia ya Wycliffe ilikuwa imetafsiriwa kutokana na Biblia ya Kilatini, ambayo ilikuwa na makosa mengi. Haikuchapishwa, na gharama ya nakala ya muswada ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba watu wachache matajiri au wenye vyeo vya juu pekee ndio wangeweza kuinunua; na, zaidi ya hapo, kwa sababu ya kanisa kuipiga marufuku, ilikuwa na nafasi finyu sana ya kusambazwa. Mwaka 1516, mwaka mmoja kabla ya hoja za Luther, Erasmus alichapisha toleo lake la Kigiriki na Kilatini la Agano Jipya. Sasa kwa mara ya kwanza neno la Mungu lilichapishwa katika lugha ya asili. Katika toleo hili makosa mengi yaliyokuwa katika matoleo ya nyuma yalisahihishwa, na maana ilitolewa kwa uwazi zaidi. Iliwaongoza wengi miongoni mwa matabaka ya wasomi kuwa na uelewa mzuri zaidi wa ukweli, na ilitolewa msukumo mpya kwa kazi ya matengenezo. Lakini watu wa kawaida bado, kwa kiwango kikubwa, walikuwa wamenyimwa neno la Mungu. Ilimpasa Tyndale amalizie kazi ya Wycliffe ya kuwapa watu wa nchi yake Biblia.

Mwanafunzi mwenye bidii na mtafutaji wa dhati wa ukweli, alipokea injili kutokana na Agano Jipya la Kigiriki la Erasmus. Bila woga alihubiri imani yake, akikazia kuwa mafundisho yote inapaswa yapimwe kwa Maandiko. Na kwa dai la upapa kuwa kanisa ndilo lililotoa Biblia, na hivyo kanisa pekee ndilo lenye mamlaka ya kuifafanua, Tyndale alijibu: “Unamjua aliyemfundisha tai kutafuta mawindo? Ndiyo, Mungu yule yule anawafundisha watoto Wake wenye njaa kumtafuta Baba yao katika neno Lake. Mbali na kutotupatia Maandiko, ni ninyi wenyewe mlioyaficha ili tusiyaone; ni ninyi wenyewe mnaowachoma moto watu wanaoyafundisha, na kama mngeweza, mngechoma moto Maandiko yenyewe.”—D’Aubigne, History of the Reformation of the Sixteenth Century, b. 18, ch. 4.

Mahubiri yaTyndale yaliamsha shauku kubwa; na watu wengi waliukubali ukweli. Lakini mapadri walikuwa macho, na mara tu alipoondoka eneo moja, kwa njia ya vitisho na upotoshaji, walijitahidi kuharibu kazi yake. Mara nyingi walifanikiwa. “Ni jambo gani lifanyike?” alisema. “Ninapokuwa nikipanda katika eneo moja, adui anashambulia eneo ambalo nimetoka. Siwezi kuwa kila mahali. O! ikiwa Wakristo wangekuwa na Maandiko Matakatifu katika lugha yao wenyewe, wao wenyewe wangeweza kuwakabili hawa wapotoshaji. Bila Biblia haiwezekani kuwaimarisha walei katika ukweli.”—Ibid., b. 18, ch. 4.

Kusudi jipya lilikuja akilini.“Ilikuwa katika lugha ya Israeli”alisema,“zaburi ziliimbwa katika hekalu la Yehova; na je, agano jipya halipaswi kuongea nasi kwa Kiingereza miongoni mwetu? ... Je, kanisa si linapaswa kuwa na nuru kubwa zaidi wakati wa mchana kuliko wakati wa mapambazuko? ... Ni lazima Wakristo wasome Agano Jipya katika lugha yao wenyewe.” Wasomi na walimu wa kanisa hawakubaliani miongoni mwao wenyewe. Kwa njia ya Biblia

pekee ndiyo wangeweza kuujua ukweli. “Mmoja anamfuata msomi huyu, mwingine yule Sasa kila mwandishi anampinga mwenzake. Tunaweza kujua ni yupi anasema ukweli na ni anasema uongo? Kwa njia gani? ... Kwa haki ni kwa njia ya neno la Mungu.”—Ibid., b. 18, ch. 4.

Haikuchukua muda mrefu ambapo msomi mmoja wa Kikatoliki alisema: “Ni afadhali tusingekuwa na amri za Mungu kuliko kuwa na amri za papa.” Tyndale alijibu: “Ninampinga papa na sheria zake; na ikiwa Mungu atahifadhi maisha yangu, kabla ya miaka mingi kupita nitamfanya mvulana anayelima kwa jembe la kukokotwa na ng’ombe ayajue Maandiko kuliko wewe unavyoyajua.”—Anderson, Annals of the English Bible, uk. 19.

Kusudi ambalo alikuwa ameanza kulifikiria, la kuwagawia watu Maandiko ya Agano Jipya katika lugha yao wenyewe, sasa lilithibitika, na mara moja alianza kulitekeleza. Mateso yalipomfukuza nyumbani, alikimbilia mjini London, na pale, kwa muda fulani alifanya kazi zake bila usumbufu. Lakini tena fujo za watetezi wa upapa zilimlazimisha kukimbia. Uingereza yote ilionekana imefungwa dhidi yake, hivyo aliamua kutafuta hifadhi katika nchi ya Ujerumani. Hapa alianza kuchapa Agano Jipya la Kiingereza. Kazi ilisimamishwa mara mbili; lakini alipokatazwa kuchapisha katika jiji moja, alikwenda katika jiji jingine. Hatimaye alielekea katika jiji la Worms, ambapo, miaka michache kabla, Luther alitetea injili mbele ya Baraza Kuu la Kitaifa. Katika jiji lile la zamani walikuwepo marafiki wengi wa Matengenezo, na Tyndale pale alifanya kazi yake bila vikwazo zaidi. Nakala elfu tatu za Agano Jipya muda si mrefu zilikamilika, na toleo jingine lilifuata mwaka ule ule.

Kwa juhudi kubwa na uvumilivu mwingi aliendelea na kazi zake. Pamoja na kwamba mamlaka za Kiingereza zililinda bandari zake kwa ulinzi makini sana, neno la Mungu, kwa njia mbalimbali, lilisafirishwa kwa siri hadi jijini London na kutokea hapo lilisambaa katika nchi nzima. Watetezi wa upapa walijaribu kuukandamiza ukweli, lakini bila mafanikio. Askofu wa Durham wakati mmoja alinunua kwa mwuzaji wa vitabu aliyekuwa rafiki wa Tyndale Biblia zote alizokuwa nazo, kwa kusudi la kuziharibu, akidhani kuwa kwa kufanya hivyo angeweza kuizuia kazi kwa kiwango kikubwa. Lakini, kinyume chake, pesa zilizopatikana kwa njia hiyo, zilitumiwa kununua karatasi za kuchapia toleo jipya na bora zaidi, ambalo, kama isingekuwa kwa njia hiyo, lisingeweza kuchapishwa. Wakati Tyndale alipofungwa gerezani, alipewa fursa ya kuachiliwa uhuru kwa sharti la kutaja majina ya watu waliomsaidia kupata fedha za kuchapishia Biblia zake. Alijibu kuwa askofu wa Durham alikuwa amemsaidia zaidi kuliko watu wengine wote; kwa kumlipa pesa nyingi kwa ajili ya vitabu vilivyokuwa vimebaki mkononi, alimwezesha kusonga mbele kwa ujasiri mkubwa.

Tyndale alisalitiwa na kuingia katika mikono ya maadui zake, na wakati mmoja alifungwa gerezani kwa miezi mingi. Hatimaye alishuhudia kwa ajili ya imani yake kwa kifo cha mfia dini; lakini silaha alizoziandaa zimewawezesha askari wengine kupigana vita katika karne zote hadi wakati wetu huu.

Latimer alihubiri kutoka mimbarani kuwa Biblia ilipaswa kusomwa katika lugha ya watu. Mwasisi wa Maandiko Matakatifu, alisema, “ni Mungu Mwenyewe;” na Maandiko haya yanashiriki nguvu na umilele wa Mwasisi wake. “Hakuna mfalme, mkuu wa dola, hakimu, wala mtawala ... ambaye hapaswi kulitii... neno Lake.” “Hebu tusitembee katika njia zetu wenyewe, bali neno la Mungu lituongoze: tusiwafuate... mababu zetu, wala tusiangalie waliyoyafanya, bali tuyaangalie yale ambayo walipaswa kuyafanya.”—Hugh Latimer, “First Sermon Preached Before King Edward VI.”

Barnes na Frith, marafiki waaminifu wa Tyndale, waliinuka kuutetea ukweli. Ridleys na Cranmer walifuata. Viongozi hawa katika Matengenezo ya Uingereza walikuwa wasomi, na wengi wao waliheshimiwa sana kwa bidii yao au uchaji wao miongoni mwa wanajumuia wa Kirumi. Upinzani wao kwa upapa ulitokana na ugunduzi wao wa makosa “kiongozi mkuu wa kanisa.” Ugunduzi wao wa siri za Babeli uliwapa nguvu ya ushuhudiaji dhidi yake.

“Sasa niulize swali la ajabu,” alisema Latimer. “Ni askofu au kasisi yupi aliye na bidii zaidi kuliko wote katika nchi nzima ya Uingereza? ... Ninakuona ukisikiliza na ukisubiri kwa hamu kubwa nimtaje .... Ninakuambia: ni Shetani. Yeye haondoki katika jimbo lake; mwite wakati wowote unapomtaka, yuko nyumbani daima; ... yeye yuko kwenye jembe lake la kukokotwa na ng’ombe Huwezi kumkuta wakati wowote akijikalia kivivu, nakuhakikishia.... Mahali Shetani alipo, pale hakuna vitabu, badala yake kuna mishumaa; pale hakuna Biblia, badala yake kuna shanga; pale hakuna nuru ya injili, badala yake, kuna nuru ya mishumaa, ndiyo, nyakati za mchana; ... msalaba wa Kristo upo chini, uchumaji wa fedha kwa njia ya pagatori(toharani) uko juu; ... hakuna kuwavika walio uchi, maskini, wasiojiweza, badala yake kuna kuabudu sanamu na kupamba kwa uchangamfu vitu visivyokuwa na uhai; mapokeo na sheria ya mwanadamu vimeinuliwa juu, mapokeo ya Mungu na neno Lake takatifu sana vimeshushwa chini. O! kwamba makasisi wetu wangekuwa na bidii ya kupanda mbegu ya mafundisho mazuri, kama Shetani alivyo na bidii ya kupanda kila aina ya magugu!”—Ibid., “Sermon of the Plough.”

Kanuni kuu iliyoshikiliwa na hawa Wanamatengenezo—kanuni ile ile iliyoshikiliwa na Wawaldensia, na Wycliffe, na John Huss, na Luther, Zwingli, na wale walioungana nao—ilikuwa mamlaka isiyokosea ya Maandiko Matakatifu kama kanuni ya imani na matendo. Walitupilia mbali haki ya mapapa, mabaraza, Mababa, na wafalme, kutawala dhamiri katika masuala ya dini. Biblia ndiyo iliyokuwa mamlaka yao, walipima mafundisho na madai yote kwa mafundisho yake. Imani kwa Mungu na neno Lake viliwashikilia watu hawa watakatifu walipoachia maisha yao kwenye nguzo ya kuchomea moto watu. “Farijikeni,” alisema Latimer akiwaambia wenzake wakati ndimi za moto zilipokuwa karibu kunyamazisha sauti zao, “leo tunawasha mshumaa, kwa neema ya Mungu, katika nchi ya Uingereza, ambao ninaamini hautazimwa kamwe.”—Works of Hugh Latimer 1:8.

Katika nchi ya Scotland mbegu za ukweli zilizotawanywa na Columba na watendakazi wenzake hazikuharibiwa kabisa. Kwa miaka mamia baada ya makanisa ya Uingereza kujisalimisha kwa utawala wa Rumi, makanisa ya Scotland walidumisha uhuru wao. Katika karne ya kumi na mbili, hata hivyo, upapa ulianzishwa hapa, na hakuna nchi ambayo utawala wa Rumi ulikuwa na nguvu zaidi kuliko iliyokuwa nayo katika nchi ya Scotland. Hakuna mahali ambako giza lilikuwa nene zaidi kuliko lililokuwepo katika nchi ya hii. Lakini bado ilikuja miale ya nuru iliyopasua giza na kutoa ahadi ya mchana unaokuja. Waloladi, waliokuja kutoka Uingereza wakiwa na Biblia na mafundisho ya Wycliffe, walifanya kazi kubwa ya kuhifadhi ukweli wa injili, na kila karne ilikuwa na mashahidi na wafia dini wake.

Pamoja na ufunguaji wa Matengenezo Makuu yalikuja maandishi ya Luther, na halafu Agano Jipya la Kiingereza la Tyndale. Bila kuonwa na uongozi wa kanisa la Rumi, wajumbe hawa walizunguka kimya kimya katika milima na mabonde, na kuwasha upya mwenge wa ukweli ambao ulikuwa karibu kuzimika katika nchi ya Scotland, na kusahihisha makosa yaliyoingizwa na Urumi kwa karne nne za ukandamizaji wake.

Halafu damu ya wafia dini ilileta msukumo mpya kwa vuguvugu. Viongozi wa upapa, wakiamka kwa ghafla kuhusiana na hatari iliyotishia kazi yao, waliwaleta pamoja watu mashuhuri wazaliwa wa Scotland ili kuwachoma moto. Walijenga jukwaa kubwa kwa ajili ya kuwachomea moto, ambapo maneno ya mashahidi waliokuwa wakifa yalisikika katika nchi nzima, yakisisimua roho za watu kwa kusudi la kutokukata tamaa na yakawapa hamasa ya kujivua minyororo ya Roma.

Hamilton na Wishart, watu wema katika tabia na katika kuzaliwa, wakiacha nyuma yao msururu mrefu wa wanafunzi, walitoa maisha yao wachomwe moto jukwaani. Kutoka miongoni mwa wanafunzi wa Wishart alitokea mmoja ambaye ndimi za moto hazikuwa tishio kwake, ambaye chini ya uongozi wa Mungu alipiga pigo la mauti kwa upapa katika nchi ya Scotland.

John Knox alikuwa ameachana na mapokeo na imani za kishirikina za kanisa, ili kujilisha kweli za neno la Mungu; na fundisho la Wishart lilikuwa limethibitisha azimio lake la kuacha ushirika wa Rumi na kujiunga na Wanamatengenezo walioteswa.

Aliposhauriwa na marafiki zake afanye kazi ya kuhubiri, alikataa akitetemeka kwa uzito wa jukumu hilo, na ilikuwa baada ya siku nyingi za kujitenga na mgogoro wenye maumivu makali ndani ya nafsi yake mwenyewe aliweza kukubali. Lakini, mara tu alipokubali kazi hiyo, alisonga mbele akiwa na nia isiyoyumba na ujasiri usioshindwa kwa kadri alivyodumu kuwa hai. Mwanamatengenezo huyu mwenye moyo wa dhati hakuogopa uso wa mtu. Mioto ya kuunguza wafia dini, ikirusha ndimi zake kila upande wake, ilimchochea kuwa na bidii zaidi. Wakati alipotishiwa kuwa shoka la mtesaji katili litainuliwa juu ya kichwa chake,

alisimama imara, akapiga mapigo mazito upande wa kulia na upande wa kushoto na kuvunja -vunja ibada ya sanamu.

Alipoletwa mbele ya malkia wa Scotland, ambaye mbele yake juhudi za Waprotestanti wengi zilipungua, John Knox alitoa ushuhuda usioyumba kwa ajili ya ukweli. Hakushindwa kwa kubembelezwa; hakurudi nyuma kwa sababu ya vitisho. Malkia alimshitaki kwa kosa la uzushi. Alikuwa akiwafundisha watu wapokee dini iliyopigwa marufuku na serikali, malkia alisema, na kwa sababu hiyo John Knox alikuwa amevunja amri ya Mungu inayowataka raia kuwatii viongozi wa serikali. Knox alijibu kwa ujasiri:

“Kwa kuwa dini ya kweli haipokei nguvu yake ya asili wala mamlaka kutoka kwa wakuu wa dunia, bali kutoka kwa Mungu wa milele pekee, kadhalika raia hawalazimiki kujenga dini yao kulingana na matakwa ya wakuu wao. Kwa kuwa mara nyingi, wakuu wa kidunia huwa hawana ujuzi wa dini ya kweli ya Mungu kuliko watu wengine wote Ikiwa wazao wote wa Ibrahimu wangekuwa wa dini ya Farao, ambao walikuwa raia wake kwa muda mrefu, ninakuomba, mama, kungekuwa na dini gani ulimwenguni? Au ikiwa watu wote katika siku za mitume wangekuwa wa dini ya wafalme wa Rumi, ni dini gani ingekuwepo kwenye uso wa dunia? Na kwa hiyo, mama, unaweza kuelewa kuwa raia hawalazimiki kutii dini ya wakuu wao, japokuwa wameamrishwa kuwatii.” Alisema Mary: “Mnatafsiri Maandiko kwa namna moja, na wao [walimu wa Wakatoliki wa Rumi] wanatafsiri kivyao; mimi nimwamini nani, na nani awe mwamuzi?”

“MwamininiMungu,nenoLakelinasemawazi,”alijibuMwanamatengenezo; “na zaidi ya kile neno linachowafundisha, msimwamini huyu wala yule. Neno la Mungu liko wazi lenyewe; na kunapotokea kutoeleweka katika sehemu moja, Roho Mtakatifu, ambaye hawezi kujipinga Mwenyewe, hufafanua sehemu hiyo katika sehemu zingine, kwa hiyo hakuna mashaka yanayoweza kubaki isipokuwa kwa mtu ambaye anaamua kubaki mjinga kwa ugumu wa moyo wake.”—David Laing, The Collected Works of John Knox, vol. 2, pp. 281, 284.

Hizo ndizo kweli ambazo Mwanamatengenezo asiyeogopa, kwa kuhatarisha maisha yake, alimwambia malkia. Kwa ujasiri huo huo usiotetereka, alishikilia kusudi lake, akiomba na kupigana vita vya Bwana, mpaka Scotland ilipoachana kabisa na upapa.

Katika nchi ya Uingereza, ustawishaji wa Uprotestanti kama dini ya kitaifa ulipunguza, lakini haukukomesha kabisa, mateso. Wakati mengi ya mafundisho ya Kirumi yaliachwa, siyo machache yaliyobakizwa. Ukuu wa papa ulitupiliwa mbali, lakini mahali pake mfalme alitawazwa kama kiongozi mkuu wa kanisa. Huduma za kanisa bado zilitofautiana sana na usafi na usahili wa injili. Kanuni kuu ya uhuru wa dini ilikuwa bado haijaelekeweka. Ingawa mambo ya kutisha ya kikatili ambayo Rumi iliyatumia dhidi ya wazushi yalitumiwa mara chache na watawala wa Kiprotestanti, bado haki ya kila mtu kumwabudu Mungu kulingana

na uchaguzi wa dhamiri yake mwenyewe haikutambuliwa. Wote walitakiwa kukubali na kufuata mifumo ya ibada iliyoelekezwa na kanisa linalotambuliwa na serikali. Walioenda kinyume waliteswa, sana au kidogo, kwa mamia ya miaka.

Katika karne ya kumi na saba maelfu ya wachugaji walifukuzwa kazi. Watu walikatazwa, kwa tishio la faini kubwa, kifungo, na kufukuzwa nchini, kuhudhuria mikutano yoyote ya kidini isipokuwa ile tu iliyoidhinishwa na kanisa. Wale waaminifu ambao wasingeweza kuacha kukutana kumwabudu Mungu walilazimika kukutana katika vichochoro vyenye giza, katika upenu uliojificha, na nyakati zingine katika msitu wakati wa usiku wa manane. Katikati ya msitu mkubwa, hekalu lililojengwa na Mungu Mwenyewe, watoto wa Bwana waliokuwa wametawanywa na kuteswa walikusanyika kumimina roho zao kwa njia ya sala na sifa. Lakini licha ya tahadhari zao zote, wengi wao waliteswa kwa ajili ya imani yao. Magereza yalijaa watu. Familia zilivunjika. Wengi wao walifukuzwa nchini kwao wakakimbilia nchi za kigeni. Hata hivyo Mungu alikuwa pamoja na watu wake, na mateso hayakuweza kunyamazisha ushuhuda wao. Wengi walilazimika kuvuka bahari hadi Amerika na hapa wakaweka misingi ya uhuru wa kiraia na wa kidini ambao umekuwa nguzo na utukufu wa nchi ya Marekani.

Kwa mara nyingine, kama ilivyokuwa katika siku za mitume, badala ya mateso kukomesha kazi ya injili, yalikuwa yakichochea zaidi kusambaa kwake. Katika gereza chafu lililojaa mafisadi na wauaji, John Bunyan alivuta hewa ya mbinguni; na akiwa humo aliandika sitiari yake ya ajabu ya Maendeleo ya Msafiri kutoka nchi ya uharibifu hadi mji mtakatifu. Kwa zaidi ya miaka mia mbili sauti ile kutoka gereza la Bedford imezungumza kwa nguvu inayosisimua na mioyo ya watu. Vitabu vya Bunyan, Pilgrim’s Progress (Maendeleo ya Msafiri) na Grace Abounding to the Chief of Sinners (Neema Tele kwa Mkuu wa Wenye Dhambi) vimeongoza miguu ya wengi katika njia ya uzima.

Baxter, Flavel, Alleine, na watu wengine wenye talanta, elimu, na uzoefu wa kina wa Ukristo walisimama kwa ujasiri kutetea imani ambayo ilitolewa kwa watakatifu tangu zamani. Kazi iliyofanywa na watu hawa, iliyokuwa imepigwa marufuku na kuharamishwa na watawala wa dunia hii, haiwezi kamwe kufa. Vitabu vya Flavel, Fountain of Life (Chemchemi ya Uzima) na Method of Grace (Mbinu ya Neema) vimewafundisha maelfu ya watu jinsi ya kusalimisha roho zao kwa Kristo. Kitabu cha Baxter, Reformed Pastor (Mchungaji Mwanamatengenezo) kimekuwa mbaraka kwa wengi wanaotamani kuamsha kazi ya Mungu, na kitabu chake Saints’ Everlasting Rest (Pumziko la Milele la Watakatifu) limefanya kazi yake ya kuwaongoza watu kwa “pumziko) ambalo limesalia kwa watu wa Mungu.

Miaka mia moja baadaye, wakati wa giza nene la kiroho, Whitefield na wafuasi wa Wesley walionekana kama wabeba nuru kwa ajili ya Mungu. Chini yautawalawakanisalakitaifawatuwa Uingerezawalikuwawamerudinyuma katika masuala ya kidini kiasi kwamba hawakutofautiana na wapagani. Dini ya asili ilikuwa ndiyo somo lao kuu

lililopendwa na wachungaji, na lilihusu pia teolojia yao karibu yote. Matabaka ya juu ya watu yalidhihaki utakatifu wao, na walijidai kwa kuwa juu ya kile walichokiita ushikiliaji sana wao wa mambo bila akili. Matabaka ya chini walikuwa wajinga kupita kiasi na walijiingiza katika maovu bila mipaka, wakati kanisa lilikuwa halina ujasiri wala imani ya kuinua kazi ya injili iliyokuwa imeanguka chini.

Fundisho kuu la kuhesabiwa haki kwa imani, lililofundishwa kikamilifu na Luther, lilikuwa limesahauliwa kwa kiasi kikubwa; na kanuni ya Kirumi ya kutegemea matendo mema kwa ajili ya wokovu, ilikuwa imechukua nafasi yake. Whitefield na Wesley, ambao walikuwa washiriki wa kanisa la kitaifa, walikuwa watafutaji wa dhati wa mapenzi ya Mungu, na walikuwa wamefundishwa kuwa mapenzi ya Mungu yalikuwa kuishi maisha maadilifu na kushika sheria za dini.

Wakati Charles Wesley wakati mmoja alipoumwa, na kuamini kuwa kifo kilikuwa karibu, aliulizwa swali kuwa tumaini lake la uzima wa milele lilikuwa limejengwa juu ya nini. Jibu lake lilikuwa: "Nimetumia juhudi zangu zote kumtumikia Mungu." Wakati rafiki aliyekuwa amemwuliza swali alipoonekana kutoridhika na jibu lake, Wesley alifikiri: "Nini! Je, juhudi zangu siyo msingi toshelevu wa tumaini? Je, anaweza kuniibia juhudi zangu? Sina kitu kingine zaidi cha kutumainia."—John Whitehead, Life of the Rev. Charles Wesley, uk. 102. Hilo ndilo giza nene lililokuwa katika kanisa, lililoficha upatanisho, likamwibia utukufu Wake, na kugeuza akili za watu kutoka kwa tumaini lao pekee la wokovu—damu ya Mkombozi aliyesulubiwa.

Wesley na marafiki zake waliongozwa kuona kuwa dini ya kweli inakaa moyoni, na kuwa sheria ya Mungu inapanuka na kuhusisha mawazo, maneno, na matendo. Akiwa ameshawishika juu ya umuhimu wa utakatifu wa moyo, na usahihi wa mwonekano wa nje, walijielekeza kwa moyo wa dhati kutafuta maisha mapya. Kwa maombi na juhudi kubwa walijaribu kudhibiti maovu ya moyo wa asili. Waliishi maisha ya kujinyima, ukarimu, na unyenyekevu, wakitekeleza kwa uaminifu na usahihi mkubwa kila hitaji walilofikiri lingewasaidia kupata kile walichokitamani zaidi—utakatifu ule ambao ungewawezesha kukubaliwa na Mungu. Lakini hakupata kile walichokitafuta. Zilikuwa juhudi za bure kujiokoa wenyewe kutoka katika hukumu ya dhambi au kuvunja nguvu yake. Ni pambano lilelile ambalo Luther alikuwanalo akiwa katika chumba chake kule Erfurt. Ni swali lilelile lililotesa roho yake—"Lakini mtu huwaje mwenye haki mbele za Mungu?" (Ayubu 9:2).

Mioto ya ukweli wa Kiungu, iliyokuwa karibu kuzimika juu ya madhabahu ya Uprotestanti, ilipaswa kuwashwa upya kwa kutumia mwenge wa zamani uliorithishwa katika zama zote miongoni mwa Wakristo Wabohemia. Baada ya Matengenezo, Uprotestanti katika nchi ya Bohemia ulifutiliwa mbali na waumini wa Urumi. Wote waliokataa kukana ukweli walilazimishwa kukimbia. Baadhi ya hawa, walipopata hifadhi katika huko Saxony,

walidumisha imani ya zamani. Ilikuwa kutoka kwa wajukuu wa Wakristo hawa ambapo nuru ilikuja kwa Wesley na marafiki zake.

John Wesley na Charles Wesley, baada ya kuwekewa mikono ya uchungaji, walitumwa kama wamishenari huko Amerika. Katika kundi hilo walikuwemo pia Wamoravian. Wakiwa njiani walikutana na dhoruba kali, na John Wesley, alipokutana uso kwa uso na kifo, alihisi kuwa hakuwa na uhakika wa amani na Mungu. Wajerumani, kinyume chake, walionesha utulivu na tumaini ambalo alikuwa hana uzoefu nao.

"Kwa muda mrefu huko nyuma," alisema, "alichunguza umakini mkubwa wa tabia yao. Waliendelea kuonesha unyenyekevu wao kikamilifu, kwa kufanya kazi za kiutumishi kwa ajili ya wasafiri wengine ambazo hakuna Mwingereza hata mmoja angeweza kuzifanya; ambazo kwazo walistahili lakini hawakuhitaji malipo, wakisema kufanya hivyo ilikuwa furaha kwao, kwa maana Mwokozi wao alikuwa amewafanyia makubwa zaidi. Na kila siku iliwapa fursa ya kuonesha unyenyekevu ambao haukubadilishwa na maumivu ya aina yo yote. Ikiwa walisukumwa, walipigwa, au kuangushwa chini, waliinuka tena na kwenda zao; lakini hawakuwa na manung'unuko yo yote katika midomo yao.

Kulikuwa na fursa sasa ya kuwapima ikiwa walikuwa wamekombolewa kutoka katika roho ya hofu, na ya kiburi, hasira, na kulipiza kisasi. Katikati ya zaburi iliyokuwa inaanzishia ibada, bahari ilichafuka kwa ghafla, dhoruba kali ikavunja sehemu ya mbele ya meli, maji yakafunika meli, na kumwagikia katikati ya sitaha za meli kana kwamba kina kikuu cha bahari kimeshatumeza. Makelele ya kutisha yalianza miongoni mwa Waingereza. Wajerumani waliendelea kuimba kwa utulivu Zaburi. Nilimwuliza mmojawapo baadaye, 'Hukuogopa?' Alijibu, 'Namshukuru Mungu, hapana.' Niliuliza, 'Lakini wake zenu na watoto wenu hawakuogopa?' Alijibu kwa upole, 'Hapana; wake zetu na watoto wetu hawaogopi kufa.'"— Whitehead, Life of the Rev. John Wesley, uk. 10.

Baada ya kufika Savannah, Wesley alikaa na Wamoraviani kwa muda mfupi, na aliguswa sana na haiba yao ya Kikristo. Kuhusu moja ya ibada zao, kwa kutofautiana sana na ibada za kimfumo zisizo na uhai za Kanisa la Uingereza, aliandika: "Usahili mkubwa na utukufu wa ibada nzima karibu vinisahaulishe miaka elfu moja mia saba iliyokuwa imepita, nikahisi nilikuwa nashiriki katika mikutano ile ambayo mfumo na serikali ya kanisa havikuwepo; bali Paulo, mtengenezaji wa mahema, au Petro, mvuvi wa samaki, waliendesha huduma; ukiwepo udhihirisho wa Roho na nguvu."— Ibid., pages 11, 12.

Aliporudi Uingereza, Wesley, kutokana na mafundisho ya mhubiri wa Kimoraviani, alifanikiwa kuelewa vizuri zaidi imani ya Biblia. Alifikia hatua ya kushawishika kuwa ilimpasa aachane kabisa na kutegemea matendo yake mema kwa ajili ya wokovu na kwamba ilimpasa kumtumaini kabisa "Mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Wakati wa mkutano wa Chama cha Moraviani katika jiji la London kauli ilisomwa kutoka

kwa Luther, ikielezea badiliko ambalo Roho wa Mungu hulileta katika moyo wa mtu anayeamini. Wakati Wesley akisikiliza, imani iliwashwa moyoni mwake. “Nilihisi moyo wangu ukitiwa joto la ajabu,” alisema. “Nilihisi ninamtumaini Kristo, Kristo pekee, kwa ajili ya wokovu: na nilipata uhakikisho, kuwa alikuwa amezichukua dhambi zangu, zangu kabisa, na kuniokoa kutoka katika sheria ya dhambi na mauti.”—Ibid., uk. 52.

Kwa miaka mingi ya kujitahidi kwingi kunakochosha na kukosesha raha— miaka ya kujinyima sana, ya kujidhili na kujinyenyekesha—Wesley alijitahidi daima kutekeleza kusudi moja tu la kumtafuta Mungu. Sasa alimpata; na aligundua kuwa neema ambayo alitesekeka kuipata kwa njia ya maombi na kufunga, kwa matendo ya ukarimu na kujikana nafsi, ilikuwa zawadi, “bila fedha na bila bei.”

Mara tu baada ya kuimarika katika imani ya Kristo, nafsi yake yote iliwaka moto wa shauku ya kutangaza kila mahali maarifa ya injili yenye utukufu ya neema ya bure ya Mungu. “Ninautazama ulimwengu wote kama parokia yangu,” alisema; “katika sehemu yo yote ile nilipo, panastahili, tena, ni wajibu wangu kamili, kutangaza kwa wote walio tayari kusikia, habari njema za wokovu.”—Ibid., uk. 74.

Aliendeleza maisha yake yenye nidhamu na kujikana nafsi, siyo sasa kama msingi, bali matokeo ya imani; siyo mzizi, bali tunda la utakatifu. Neema ya Mungu katika Kristo ni msingi wa tumaini la Mkristo, na kwamba neema inadhihirika katika utii. Maisha ya Wesley yaliwekwa wakfu kuhubiri kweli kuu alizozipokea—kuhesabiwa haki kwa njia ya imani katika damu ya upatanisho ya Kristo, na nguvu ya Roho Mtakatifu inayoumba upya moyo, kuzaa tunda katika maisha linalopatana na mfano wa Kristo.

Whitefield na Wesley walikuwa wameandaliwa kwa ajili ya kazi yao kwa kushawishika binafsi kuhusiana na hali yao ya kupotea; na kwamba wangeweza kuvumilia mazingira magumu kama askari wa Kristo, walikuwa wamekabiliana na moto wa mateso ya kudhalilishwa, kubezwa, na kuteswa, katika chuo kikuu na wakati wa kuingia kwao katika uchungaji. Wao na wenzao wachache waliowaunga mkono waliita kwa dhihaka Wamethodisti na wanafunzi wenzao wasiomcha Mungu—jina ambalo kwa sasa linaheshimiwa na moja ya madhehebu kubwa katika nchi ya Uingereza na Bara la Amerika. Kama washiriki wa Kanisa la Uingereza walikuwa wameshikamana na mifumo yake ya ibada, lakini Bwana alikuwa ameweka mbele yao katika neno la Mungu kiwango cha juu zaidi. Roho Mtakatifu aliwaagiza kumhubiri Kristo na Yeye aliyesulibiwa. Nguvu Zake Aliye Juu sana ziliandamana na kazi zao. Maelfu waliamini na kuongolewa kikamilifu. Ilikuwa lazima kondoo hawa walindwe dhidi ya mbwa mwitu wakali. Wesley hakuwa na wazo la kuanzisha madhehebu mapya, lakini aliwaunga pamoja chini ya kilichoitwa Mshikamano wa Kimethodisti.

Wahubiri hawa walipata upinzani mkubwa wa kisirisiri toka kwa kanisa la kitaifa; lakini Mungu, katika hekima Yake, aliingilia kati kupitia matengenezo yaliyotokea ndani ya kanisa lenyewe. Ikiwa matengenezo yangetokea nje peke yake, yasingeweza kupenya na kuingia kule yalikotakiwa sana. Lakini kama wahubiri wana uamsho walikuwa watu wa kanisa, na walifanya kazi miongoni mwa washiriki wa kanisa kila mahali walipopata fursa, na ukweli uliingia mahali ambapo milango ingeweza kufungwa. Baadhi ya wachungaji waliamka kutoka katika usingizi wao na wakawa wahubiri wenye bidii katika parishi zao. Makaisa yaliyokuwa yamelala kwa sababu mifumo ya ibada ya kurudia-rudia na kukariri yaliamka na kuwa hai.

Katika wakati wa Wesley, kama ilivyo katika zama zote za historia ya kanisa, watu wa talanta mbalimbali walitenda kazi walizopangiwa kuzifanya. Hawakuafikiana katika kila kipengele cha fundisho, lakini walisukumwa na Roho wa Mungu, na waliungana katika kusudi kuu la kuleta roho kwa Kristo. Tofauti kati ya Whitefield na Wesley ilitishia wakati fulani kujenga ufa kati yao; lakini kwa kadiri walivyojifunza unyenyekevu katika shule ya Kristo, uvumilivu na ukarimu viliwasaidia kupatana.

Hawakuwa na muda wa kuzozana, wakati makosa na uovu vilikuwa vimeshamiri kila mahali, na wenye dhambi walikuwa wakiteremka kuelekea katika shimo la uharibifu. Watumishi wa Mungu walipitia katika barabara yenye mikwaruzo. Watu wenye mvuto na elimu kubwa walitumia uwezo wao dhidi yao. Baada ya muda wachungaji wengi walionesha uhasama wa wazi, na milango ya makanisa ilifungwa dhidi ya imani safi na wale walioitangaza. Hatua ya wachungaji kuwapiga marufuku kuhubiri mimbarani ilihamasisha vimelea vya giza, ujinga, na uovu. Tena na tena John Wesley alipona kifo kwa muujiza wa neema ya Mungu. Wakati hari ya watu ilipoamshwa dhidi yake, na ikaonekana hakuna njia ya kuokoka, malaika katika umbo la mwanadamu alikuja kando yake, kundi la watu lilirudi nyuma, na mtumishi wa Kristo alipita salama na kuondoka mahali palipo na hatari.

Kuhusiana na kuokolewa kwake dhidi ya kundi la watu katika moja ya matukio hayo, Wesley alisema: “Wengi walijaribu kuniangusha chini wakati tukitembea kwenye mteremko, kwenye njia inayoteleza, iliyoelekea mjini; wakifikiri ikiwa ningeanguka chini, nisingeweza kuamka tena kirahisi. Lakini sikujikwaa hata kidogo, wala sikuteleza kabisa, mpaka nikawa huru mbali kabisa na mikono yao Ingawa wengi walijaribu kunishika kwenye ukosi wa shati langu au mavazi yangu mengine, ili waniangushe chini, hawakuweza kunishika kabisa: mmoja tu ndiye aliyefanikiwa kushika pindo la kizibao changu, ambacho muda si mrefu kipande cha kizibao kilibaki mkononi mwake; kipande kingine, ambacho ndani ya mfuko wake ilikuwemo noti kilibaki. Mtu mmoja mwenye nguvu nyuma yangu, alinipiga mara kadhaa, kwa fimbo kubwa ya mwaloni; ambayo kama angenipiga mara moja kwenye kisogo, angeniua mara moja. Lakini kila wakati, pigo lilipelekwa pembeni, sijui ni kwa jinsi gani; kwa kuwa nisingeweza kukwepa kwenda kulia au kwenda kushoto Mwingine alikuja akikimbia katikati ya msongamano wa watu, na akainua mkono wake ili anipige, alichia

mkono ukadondoka, na akanishika shika tu kichwani, akisema, 'Una nywele laini sana!' Watu wa kwanza kabisa ambao mioyo yao iligeuzwa walikuwa mashujaa wa mji, viongozi wa vikundi vya wapiganaji wa mjini nyakati zote, mmoja wao akiwa alishawahi kupata tuzo ya kupambana katika bustani za duma....

"Kwa hatua za upole lakini za hakika Mungu hutuandaa kwa ajili ya mapenzi Yake! Miaka miwili iliyopita, kipande cha tofali la kuchoma kilikwangua mabega yangu. Ilikuwa mwaka mmoja baada ya hapo ambapo jiwe lilipiga katika macho yangu. Mwezi uliopita nilipokea pigo moja, na jioni ya leo mawili, moja kabla hatujafika mjini, na moja baada ya kutoka mjini; lakini yote mawili yalikuwa kana kwamba hakuna kitu kilichotokea: kwa kuwa ingawa mtu wa kwanza alinipiga kwenye kifua kwa nguvu zake zote, na mwingine alinipiga kwenye mdomo kwa nguvu nyingi kiasi kwamba damu ilitoka mara moja, sikuhisi maumivu yo yote makali zaidi kuliko yale ambayo ningeyapata kama wangenigusa kwa unyasi."—John Wesley, Works, vol. 3, pp. 297, 298.

Wamethodisti wa siku zile za awali—watu na wahubiri—walivumilia dharau na mateso, kutoka kwa washiriki wa kanisa na wasio na dini waliokasirishwa na mabaya ambayo Wamethodisti walipakaziwa. Walishtakiwa katika mahakama za haki—kwa jina, kwa kuwa haki haikuwepo, isipokuwa mara chache sana, katika mahakama za wakati huo. Mara nyingi walifanyiwa ukatili na watesaji wao. Makundi ya watu yalitembea kutoka nyumba moja hadi nyingine, wakiharibu samani na mali zingine, wakiiba chochote walichokichagua, na wakiwanajisi wanaume, wanawake, na watoto. Katika nyakati zingine, matangazo ya hadhara yalibandikwa, yakiwaita watu waliopenda kusaidia katika kuvunja madirisha na kuiba katika nyumba za Wamethodisti, wakusanyike mahali fulani na wakati fulani. Ukiukwaji huu wa wazi wa sheria ya binadamu na ya Mungu uliruhusiwa kutendeka bila kukemewa. Utesaji uliopangiliwa ulitekelezwa dhidi ya watu ambao kosa lao lilikuwa tu kutafuta kubadilisha miguu ya wenye dhambi kutoka katika njia ya uharibifu na kuielekeza katika njia ya utakatifu.

Alisema John Wesley, akizungumzia mashitaka dhidi yake na dhidi ya wenzake: "Wengi wanadai kuwa mafundisho ya watu hawa ni ya uongo, yana makosa, na ni wenye shauku; kwamba ni mafundisho mapya na hayajawahi kusikiwa mpaka siku za hivi karibuni; kwamba ni jamii ya Wakristo wasiopenda mikutano rasmi, watu wanaoshikilia sana mambo bila akili, watetezi wa upapa. Maigizo yote haya yameshakatwa katika mizizi yake, hususani baada ya kuonesha kuwa kila kipengele cha fundisho hili ni fundisho la wazi la Maandiko lililotafsiriwa na kanisa. Hivyo basi haliwezi kuwa la uongo au lenye makosa, ili mradi tu Maandiko yawe ya kweli."

"Wengine wanadai, 'Fundisho lao ni kali mno; wanaifanya njia ya kwenda mbinguni kuwa finyu mno.' Na kwa kweli hiki ndicho kipingamizi halisi, (kwa kuwa ndicho kilikuwa kipingamizi pekee kwa wakati fulani,) na kwa siri ndio msingi wa vipingamizi elfu na zaidi, ambavyo huonekana katika miundo mbalimbali. Lakini vinaifanya njia ya kwenda mbinguni

kuwa nyembamba zaidi kuliko Bwana wetu na mitume Wake walivyoifanya? Kuna fundisho kali zaidi kuliko lile la Biblia? Fikiria aya chache tu za wazi: 'Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote.' 'Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.''Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.'

"Ikiwa fundisho lao ni kali zaidi kuliko hili, wanapaswa kulaumiwa; lakini unajua katika dhamiri yako kuwa sio kweli. Na ni nani anaweza kuwa mkali kidogo chini ya hapo bila kuharibu neno la Mungu? Inawezekanaje wakili wa siri za Mungu aonekane kuwa mwaminifu ikiwa anabadilisha sehemu yo yote ya hazina takatifu? Hapana. Hawezi kupunguza cho chote, hawezi kulainisha cho chote; analazimika kutangaza kwa watu wote, 'Siwezi kushusha chini Maandiko kukidhi matakwa yako. Inakupasa kuja Biblia ilipo, au uangamie milele.' Huu ndio msingi halisi wa kile kilio kingine maarufu kuhusu 'kukosa ukarimu kwa watu hawa.' Kukosa ukarimu, ni kweli kuwa hawana ukarimu? Katika mambo gani? Hawawapi chakula wenye njaa na kuwavika walio uchi? 'Hapana; hili siyo kweli: hawana upungufu katika hili: lakini siyo wakarimu katika kuhukumu! Wanafikiri kuwa hakuna mtu anayeweza kuokolewa isipokuwa wale tu wanaofuata njia yao.'"—Ibid., vol. 3, uk. 152, 153.

Kurudi nyuma kiroho kulikokuwepo katika nchi ya Uingereza mara kabla ya wakati wa Wesley kwa sehemu kubwa kulitokana na mafundisho kuwa neema ya Mungu inawaondolea Wakristo wajibu wa kutii sheria ya maadili. Wengi walidai kuwa Kristo alifuta sheria ya maadili na kwamba Wakristo, hivyo basi, hawalaziki kuifuata; kwamba Mkristo amewekwa huru kutoka katika "utumwa wa matendo." Wengi, japokuwa walikiri uendelevu wa sheria, walifundisha kuwa ilikuwa lazima kwa wachungaji kuwahimiza watu kutii kanuni zake, kwa kuwa wale ambao Mungu aliwachagua waokolewe wangeweza, "kwa msukumo usiozuilika wa neema ya Mungu, kusukumwa kuishi maisha matakatifu na kutenda matendo mema," wakati wale waliopangiwa kupotea milele "hawakuwa na uwezo wa kutii sheria ya Mungu."

Wengine, wakishikilia pia kuwa "waliochaguliwa hawawezi kuanguka kutoka kwenye neema na wala hawawezi kunyimwa fadhila ya Mungu," walifikia majumuisho mabaya zaidi "matendo maovu wanayoyafanya kwa kweli siyo dhambi, wala hayapaswi kuchukuliwa kuwa uvunjaji wa sheria ya Mungu, na kwamba, matokeo yake, hawana haja ya kuungama dhambi au kuachana nazo kwa njia ya toba."—McClintock and Strong, Cyclo- pedia, art. "Antinomians." Kwa hiyo, walifundisha kuwa hata dhambi iliyo mbaya kabisa, "inayochukuliwa na watu wote kuwa uvunjanji mkubwa wa sheria ya Mungu, siyo dhambi mbele za Mungu," ikiwa imetendwa na mmoja wa wateule, "kwa sababu ni moja ya tabia muhimu na bainishi za wateule, kwamba hawawezi kufanya jambo lo lote lisilompendeza Mungu au jambo ambalo limekatazwa na sheria."

Mafundisho haya potovu kimsingi yanafanana na fundisho la baadaye la walimu na wanateolojia mashuhuri—kuwa hakuna sheria isiyobadilika kamakiwango cha haki, bali kwamba kiwango cha uadilifu kinaoneshwa na jamii yenyewe, na imekuwa na uwezekano wa kubadilika daima. Mawazo haya yote yanavuviwa na roho ile ile kuu—na yeye ambaye, hata miongoni mwa wakazi wa mbinguni wasio na hatia, alianza kazi yake ya kutafuta kuharibu viwango vya haki vya sheria ya Mungu.

Fundisho la maagizo ya Kiungu, yanayowapa wanadamu tabia isiyobadilika, limewafanya wengi, hatimaye, kutupilia mbali sheria ya Mungu. Kwa juhudi kubwa, Wesley aliyapinga makosa hayo ya walimu waliofundisha kuwa neema inawafanya wafuasi wa Kristo wasiwe na hitaji la sheria ya Mungu na alionesha kuwa fundisho hili lililowafanya watu waiache sheria ya Mungu lilikuwa kinyume na Maandiko. "Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa." "Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu; ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli. Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake" (Tito 2:11; 1 Timotheo 2:3-6). Roho wa Mungu anatolewa bure kumwezesha kila mwanadamu kushikilia njia ya wokovu. Hivyo Kristo, "Nuru ya kweli," "amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu" (Yohana 1:9). Wanadamu wanakosa wokovu kwa sababu ya uchaguzi wao wa hiari wa kuikataa zawadi ya uzima.

Katika kujibu dai kuwa wakati wa kufa kwa Kristo kanuni za Amri Kumi zilifutwa pamoja na sheria ya sherehe, Wesley alisema: "Sheria ya Uadilifu, iliyomo katika Amri Kumi na ambayo manabii walisimamia utekelezaji wake, Kristo hakuiondoa. Ujio Wake hakuwa na lengo la kutangua hata sehemu yake yo yote ile. Hii ni sheria ambayo kamwe haiwezi kuvunjwa, yenyewe 'husimama imara kama shahidi mwaminifu mbinguni.' ... hii ilikuwa hivyo tangu mwanzo wa ulimwengu, ikiwa 'bado haijaandikwa kwenye mbao za mawe,' lakini ikiwa imendikwa juu ya mioyo ya wanadamu, walipotoka katika mikono ya Muumbaji. Na ingawa herufi zilizoandikwa na kidole cha Mungu kwa sasa zimefutwa na dhambi kwa kiwango kikubwa, lakini bado hazijafutika kabisa, kwa kuwa bado tuna ufahamu wa mema na mabaya. Kila kipengele cha sheria ya Mungu lazima kiwe na nguvu juu ya wanadamu wote, katika zama zote; kwa kuwa sheria ya Mungu haitegemei wakati au mahali, au hali yo yote ile nyingine inayoweza kubadilika, kwani sheria ya Mungu hueleza tabia ya Mungu asiyebadilika.

"'Sikuja kutangua, bali kutimiliza.' ... Bila swali, maana Yake katika sehemu hii ni (Bila kubadilika kwa yote yaliyotangulia kabla na yanayofuata baada),—nimekuja kustawisha katika ukamilifu wake, licha ya tafsiri zote za wanadamu: nimekuja kuweka mwonekano kamili na wa wazi kila kitu kilichokuwa giza au kilichokuwa hakionekani ndani yake kionekane: nimekuja kutangaza umuhimu wa kweli na kamili wa kila sehemu; kuonesha urefu

na upana, na ukamilifu wake wote, wa kila amri iliyomo, na kimo na kina, kiini chake kiroho na usafi wake usiofikiriwa katika vipengele vyake vyote."—Wesley, sermon 25.

Wesley alifundisha upatanifu mkamilifu wa sheria na injili. "Kwa hiyo, kuna uhusiano wa karibu unaoweza kueleweka, kati ya sheria na injili. Kwa upande mmoja, sheria daima hutengeneza njia kwa ajili ya, na hutuelekeza kwa, injili; Kwa upande mwingine, injili daima hutuongoza katika utekelezaji mkamilifu zaidi wa sheria. Sheria, kwa mfano, hututaka tumpende Mungu, tumpende jirani yetu, tuwe wanyenyekevu, na tuwe watakatifu. Tunahisi kuwa tumepungua katika mambo haya; ndiyo, kwamba 'kwa mwanadamu hii haiwezekani;' lakini tunaona ahadi ya Mungu na kutupatia upendo huo, kutufanya tuwe wanyenyekevu, wapole, na watakatifu: tunashikilia hii injili, tunashikilia habari njema hizi; tunapewa kulingana na imani yetu; na 'haki ya sheria inatimizwa ndani yetu,' kwa njia ya imani iliyo katika Kristo Yesu....

"Miongoni mwa maadui wakubwa wa injili ya Kristo," alisema Wesley, "ni wale 'wanaoihukumu sheria' yenyewe, waziwazi na moja kwa moja, na 'wanao isemavibaya;'wanaowafundishawatukuvunja(kuyeyusha, kulegeza, kuondoa ulazima wa) siyo tu moja peke yake, iwe ile ndogo kabisa au ile kubwa kabisa, bali amri zote kwa mpigo Kinachoshangaza kuliko yote yanayohusiana na udanganyifu huu mkubwa, ni kuwa wale wanotawaliwa na udanganyifu huu, huamini kwa dhati kuwa wanamheshimu Kristo kwa kuangusha sheria Yake, na kwamba wanaitukuza ofisi Yake wakati wanapoharibu fundisho Lake! Ndiyo, wanamheshimu kama vile Yuda Iskariote alivyomheshimu kwa kusema, 'Salamu, Rabi, akambusu.' Na anaweza kumwambia kwa haki kabisa kila mmoja wao, 'Wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu?' Siyo jambo jingine zaidi ya kumsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu, kuzungumzia damu Yake, na kumwondolea taji Yake; kupuuza sehemu yo yote ya sheria Yake, kwa kujifanya unaeneza injili Yake. Kadhalika mtu ye yote hawezi kuepuka shitaka hili, ikiwa anahubiri imani kwa jinsi hiyo kama ama ana mwelekeo wa moja kwa moja au usiokuwa wa moja kwa moja wa kuweka pembeni kipengele cho chote cha utii: anayemhubiri Kristo huku anafuta, au anadhoofisha kwa namna yo yote ile, amri za Mungu zilizo ndogo kabisa."—Ibid.

Kwa wale waliohimiza kuwa "kuhubiri injili hujibu miisho yote ya sheria," Wesley alijibu: "Hili tunalikataa kabisa. Hakujibu hata mwisho wa kwanza wa sheria, maana yake, haiwezi kumfanya mtu ahisi hatia ya dhambi, kuwaamsha wale ambao wamelala usingizi kwenye ukingo wa kuzimu." Mtume Paulo anasema kuwa"kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria;""na ni mpaka pale tu mwanadamu anaposhawishika kuwa ni mwenye dhambi, ndipo atakapohisi hitaji lake la damu ya Kristo inayopatanisha. 'Walio wazima,' kama Bwana wetu Mwenyewe alivyosema, 'hawahitaji daktari, bali walio hawawezi.' Ni jambo lisilokuwa na maana, hivyo basi, kuwapelekea daktari walio wazima, au angalau watu wanaojidhania kuwa ni wazima. Ni lazima kwanza kuwashiwishi wakubali kuwa ni wagonjwa; vinginevyo hawatakushukuru kwa kazi yako. Kadhalika ni jambo lisilo kuwa na maana kumtoa Kristo

kwa watu ambao mioyo yao ni mizima, watu ambao bado hawajavunjika-vunjika."—Ibid., sermon 35.

Hivyo basi, alipokuwa akihubiri injili ya neema ya Mungu, Wesley, kama Bwana wake, alitafuta "kuikuza sheria, na kuifanya iheshimiwe." Kwa uaminifu alitekeleza kazi aliyopewa na Mungu, na, aliruhusiwa kuyaona matokeo yenye utukufu ya kazi yake. Mwishoni mwa maisha yake marefu yaliyopata miaka themanini—zaidi ya nusu karne iliyotumiwa katika safari za kichungaji—wafuasi wake waaminifu walikuwa zaidi ya laki tano. Lakini watu maelfu ambao kwa njia ya kazi zake waliinuliwa kutoka katika uharibifu na kudharauliwa kunakosababishwa na dhambi hadi maisha ya juu na masafi zaidi, na idadi ya watu ambao kwa njia ya mafundisho yake walipata uzoefu wa kina na mkubwa zaidi wa kiroho, hawatajulikana kamwe mpaka familia nzima itakapokusanywa katika ufalme wa Mungu. Maisha yake yanawasilisha somo la thamani isiyopimika kwa kila Mkristo. Hebu imani ile na unyenyekevu ule, juhudi zisizochoka, kujitoa mhanga, na ujisalimishaji mkamilifu wa mtumishi huyu wa Kristo uakisiwe katika makanisa ya leo!

Sura ya 15 - Biblia na Mapinduzi ya Ufaransa

Katika karne ya kumi na sita, Matengenezo yakiwasilisha Biblia iliyofunguliwa kwa watu, yalitaka kuingizwa katika nchi zote za Ulaya. Baadhi ya mataifa yaliikaribisha kwa furaha, kama mjumbe kutoka Mbinguni. Katika nchi zingine upapa ulifanikiwa kwa kiwango kikubwa kuzuia kuingia kwake; na nuru ya maarifa ya Biblia, na mivuto yake inayoinua, kwa kiwango kikubwa iliondolewa. Katika nchi moja, ingawa nuru iliingia, haikutambuliwa na giza. Kwa karne nyingi, ukweli na makosa vilishindana ili kimoja kitawale kingine. Mwishowe uovu ulishinda, na ukweli wa mbinguni ulisukumiwa nje. "Na hii ndiyo hukumu; ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru" (Yohana 3:19). Taifa liliachwa livune matokeo ya uchaguzi wao. Kizuizi cha Roho wa Mungu kiliondolewa kwa watu kudharau karama ya neema Yake. Uovu uliruhusiwa ukomae. Na ulimwengu wote uliona tunda la kuchagua kuikataa nuru.

Vita dhidi ya Biblia, iliyoendelezwa kwa karne nyingi katika nchi ya Ufaransa, iliishia katika matukio ya Mapinduzi. Mlipuko huo wa kutisha ulikuwa matokeo yasiyoepukika ya ukandamizaji wa Maandiko wa Rumi. (Tazama Kiambatanisho.) Uliwasilisha mfano wa wazi kuliko yote ambayo ulimwengu umewahi kushuhudia wa utendaji kazi wa sera ya upapa—kielelezo cha matokeo ambayo kwa zaidi ya miaka elfu moja ya mafundisho ya Kanisa la Rumi yamekuwa yakielekeza kwayo.

Ukandamizaji wa Maandiko wakati wa kipindi cha utawala wa upapa ulitabiriwa na manabii; na mwandishi wa kitabu cha Ufunuo anataja pia matokeo ya kutisha ambayo yangetokea hususani katika nchi ya Ufaransa kutokana na utawala wa "mtu wa dhambi."

Alisema malaika wa Bwana: "Nao wataukanyaga mji mtakatifu miezi arobaini na miwili. Nami nitawaruhusu mashahidi wangu wawili, nao watatoa unabii siku elfu na mia mbili na sitini, hali wamevikwa magunia…. Hata watakapoumaliza ushuhuda wao, yule mnyama atokaye katika kuzimu atafanya vita nao, naye atawashinda na kuwaua. Na mizoga yao itakuwa katika njia ya mji ule mkuu, uitwao kwa jinsi ya roho Sodoma, na Misri, tena ni hapo Bwana wao aliposulibiwa…. Nao wakaao juu ya nchi wafurahi juu yao na kushangilia. Nao watapelekeana zawadi wao kwa wao, kwa kuwa manabii hao wawili waliwatesa wao wakaao juu ya nchi. Na baada ya siku hizo tatu u nusu, roho ya uhai itokayo kwa Mungu ikawaingia, wakasimama juu ya miguu yao; na hofu kuu ikawaangukia watu waliowatazama"(Ufunuo 11:2-11).

Vipindi ambavyo vimetajwa hapa—"miezi kumi na miwili," na "siku elfu moja na mia mbili"—vinahusu kipindi kile kile, vyote vinawakilisha kipindi cha muda ambacho kanisa lingeteswa na Rumi. Miaka 1260 ya utawala wa upapa ilianza B.K. 538, na kiliisha mwaka 1798. (Tazama maelezo ya Kiambatanisho kwa ajili ya ukurasa wa 54.) Wakati huo jeshi la Ufaransa liliingia Rumi na kumfanya papa kuwa mfungwa, na alifia uhamishoni. Ingawa papa

mpya alichaguliwa muda mfupi uliofuata, utawala wa upapa haujaweza kamwe tangu wakati huo kuwa na nguvu uliokuwa nayo kabla. Mateso ya kanisa hayakuendelea kipindi chote cha miaka 1260. Kwa sababu ya rehema kwa ajili ya watu Wake, Mungu aliupunguza muda wa mateso yao makali. Alipokuwa akitabiri "taabu kuu" ambayo ingelipata kanisa, Mwokozi alisema: "Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu ye yote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo" (Mathayo 24:22). Kutokana na nguvu ya Matengenezo mateso yalikomeshwa kabla ya mwaka 1798.

Kuhusu mashahidi wawili nabii anaeleza zaidi: "Hao ndio ile mizeituni miwili na vile vinara viwili visimamavyo mbele za Bwana wa nchi.""Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu" (Ufunuo 11:4; Zaburi 119:105). Mashaidi wawili huwakilisha Maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya. Yote mawili ni ushuhuda muhimu kuhusu mwanzo na uendelevu wa sheria ya Mungu. Yote mawili ni mashahidi kwa ajili ya mpango wa wokovu. Mifano, kafara, na huelekeza kwa Mwokozi anayekuja. Injili na Nyaraka za Agano Jipya huelezea kuhusu Mwokozi aliyekuja kwa namna sahihi iliyotabiriwa na mifano na unabii.

"Watatoa unabii kwa siku elfu moja na mia mbili na sitini, wakiwa wamevaa nguo za magunia."Katika sehemu kubwa ya kipindi hiki, mashahidi wa Mungu walibaki mafichoni. Mamlaka za kipapa zilijitahidi kuwaficha watu neno la kweli, na waliweka mbele yao mashahidi wa uongo wapinge ushuhuda wao.

(Tazama Kiambatisho.) Wakati Biblia ilipopigwa marufuku na mamlaka za kidini na kiraia; wakati ushuhuda wake ulipopindishwa, na kila juhudi ikafanywa ili watu na mapepo wagundue njia ya kubadilisha akili za watu dhidi yake; wakati wale waliojaribu kutangaza ukweli wake mtakatifu walipowindwa, waliposalitiwa, walipoteswa, walipotupwa katika vyumba vya magereza, walipouawa kwa ajili ya imani yao, au walipolazimishwa kukimbilia katika maficho ya milimani, na mashimo na mapango ya ardhini— hapo ndipo mashaidi waaminifu waliposhuhudia wakiwa katika nguo za magunia. Lakini waliendeleza ushuhuda wao katika kipindi chote cha miaka 1260. Katikati ya giza kuu kabisa walikuwepo watu waaminifu waliolipenda neno la Mungu na walikuwa na wivu kwa ajili ya heshima Yake. Kwa hawa watumishi waaminifu ilitolewa hekima, nguvu, na mamlaka ya kutangaza ukweli Wake katika kipindi chote cha wakati huu.

"Na mtu akitaka kuwadhuru, moto hutoka katika vinywa vyao na kuwala adui zao. Na mtu akitaka kuwadhuru, hivyo ndivyo impasavyo kuuawa" (Ufunuo 11:5). Watu hawawezi kukanyaga neno la Mungu bila kuadhibiwa. Maana ya onyo hili la kutisha imeelezwa katika Sura ya mwisho ya kitabu cha Ufunuo: "Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki,

Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki" (Ufunuo 22:18, 19).

Hayo ndiyo maonyo ambayo Mungu ameyatoa kuwalinda watu dhidi ya kugeuza kwa namna yoyote ile kile ambacho amekifunua au amekiamuru. Maonyo haya ya kutisha ni kwa ajili ya wale wote ambao kwa sababu ya mvuto wao wanawaongoza wengine kudharau sheria ya Mungu. Walitakiwa wawasaidie wale ambao wanasema kwa kirahisi – rahisi kuwa hakuna madhara yo yote kutii au kutotiii sheria ya Mungu waogope na watetemeke. Wote wanaoinua maoni yao juu ya ufunuo wa Mungu, wote ambao hubadilisha maana ya wazi ya Maandiko ili kukidhi mahitaji yao, au kwa ajili ya kufanana na ulimwengu, wanajitwika wajibu wa kutisha.

Neno lililoandikwa, sheria ya Mungu, itapima tabia ya kila mtu na kuwahukumu wote ambao kipimo hiki kisichokosea kitawatangaza kuwa wamepungua. "Watakapokuwa wamemaliza [wanamaliza] ushuhuda wao." Kipindi ambacho mashahidi wawili walitoa unabii wakiwa katika mavazi ya magunia, kiliishia mwaka 1798. Walipokuwa wanakaribia mwisho wa kazi yao mafichoni, vita ilipigwa dhidi yao na mamlaka inayowakilishwa na "mnyama atokaye katika kuzimu." Katika mataifa mengi ya Ulaya mamlaka zilizotawala katika kanisa na serikali kwa karne nyingi ziliongozwa na Shetani kwa njia ya upapa. Lakini hapa kuna mwonekano mpya wa ufunuo wa nguvu ya kishetani. Ilikuwa sera ya Rumi, chini ya madai ya kuiheshimu Biblia, kuitunza ikiwa katika lugha isiyoeleweka na ikiwa imefichwa ili isionwe na watu. Chini ya utawala wake mashahidi walitoa unabii"wakiwa katika mavazi ya magunia."

Lakini mamlaka nyingine—mnyama atokaye kuzimu—ilipasa ainuke na kupigana vita vya wazi, vya kudhamiria dhidi ya neno la Mungu. "Mji mkuu" ambao kati kati yake mashahidi wawili wanauawa, na ambapo mizoga yao inalala, ni Misri "kiroho". Kati ya mataifa yote yaliyosimuliwa katika historia ya Biblia, Misri kwa ujasiri mkubwa ilikana uwepo wa Mungu aliye hai na ilipinga amri zake. Hakuna mfalme aliyediriki kufanya uasi wa wazi na wa kiburi cha hali ya juu dhidi ya mamlaka ya Mbingu zaidi ya alivyofanya mfalme wa Misri.

Wakati ujumbe ulipoletwa kwake na Musa, katika jina la Bwana, Faraoh alijibu kwa kiburi: "Bwana ni nani, hata niisikilize sauti yake, na kuwapa Israeli ruhusa waende zao? Mimi simjui Bwana, wala sitawapa Israeli ruhusa waende zao" (Kutoka 5:2). Huu ni ukanamungu, na taifa lililowakilishwa na Misri lingetoa sauti kama ile ile ya kukataa madai ya Mungu aliye hai na lingedhihirisha roho kama ile ile ya kutokuamini na ukaidi. "Mji mkuu" umelinganishwa pia, "kiroho," na Sodoma. Ufisadi wa Sodoma katika kuvunja amri za Mungu ulionekana hasa katika uasherati na uzinzi. Na dhambi hii ilipaswa kuwa sifa kuu ya taifa ambalo lingetimiza vipengele vya andiko hili.

Kwa mujibu wa maneno ya nabii, hivyo basi, muda mfupi kabla ya 1798 mamlaka fulani ambayo mwasisi wake ni Shetani ingeinuka na kupiga vita Biblia. Na katika nchi ambapo ushuhuda wa mashahidi wawili wa Mungu wangenyamazishwa, kungeoenekana ukanamungu wa Farao na uasherati na uzinzi wa Sodoma.

Unabii huu umepata utimizo sahihi na wa kushangaza katika historia ya Ufaransa. Wakati wa Mapinduzi, mwaka 1793, “ulimwengu kwa mara ya kwanza ulisikia mkutano wa watu, waliozaliwa na kuelimishwa katika ustaarabu, na wakidai kuwa na haki ya kuongoza moja ya mataifa mazuri sana ya Ulaya, wakiinua sauti yao pamoja kuukataa ukweli muhimu sana ambao roho ya mwanadamu hupokea, na kukana kwa umoja wao imani na ibada ya Mungu.”—Sir Walter Scott, Life of Napoleon, vol. 1, ch. 17.

“Ufaransa ni taifa pekee duniani ambalo lina rekodi iliyoandikwa na inayoendelea kuwapo, ya kwamba kama taifa iliinua mkono wake kufanya uasi wa wazi dhidi ya Mwumbaji wa Ulimwengu. Waliomkufuru Mungu ni wengi, wakanamugnu ni wengi, wamekuwepo, na wataendelea kuwepo, katika nchi ya Uingereza, Ujerumani, Uhispania, na kwingineko; lakini Ufaransa inasimama peke yake katika historia ya ulimwengu kama taifa moja pekee ambalo, kwa amri ya Bunge, lilitangaza kuwa hakuna Mungu, na ambayo raia wote wa mji mkuu, na raia walio wengi mahali pengine, wanawake kwa wanaume, walicheza na kuimba walipolipokea tangazo hilo.”—Blackwood’s Magazine, November, 1870.

Ufaransa pia ilikuza tabia zilizoifananisha na Sodoma. Wakati wa Mapinduzi kulikuwa na mwonekana wa wazi wa anguko la kimaadili na ufisadi uliofanana na ule uliosababisha kuharibiwa kwa miji ya Sodoma na Gomora. Na mwanahistoria anawasilisha kwa pamoja ukanamungu na ufisadi wa Ufaransa, kama ulivyotolewa katika unabii: “Kwa mshikamano wa karibu sana na sheria hizi zinazoathiri dini, kulikuwa na kile kilichodhoofisha muungano wa ndoa—mshikamano mtakatifu sana ambao wanadamu wanaweza kuufanya, na ambao una uendelevu unaoimarisha sana jamii— na kuifanya ndoa kuwa mkataba tu wa kiraia wenye Sura ya mpito, ambapo watu wowote wawili wanaweza kushikamana na kuachana wakati wowote kulingana na matakawa yao Ikiwa Shetani na malaika zake walikaa na kufikiria jinsi ya kuharibu kwa mafanikio kila kilicho cha kuheshimiwa, chenye neema, au cha kudumu katika maisha ya nyumbani, na wakati huo huo kupata uhakikisho kuwa tabia mbaya ambayo ilikuwa lengo lao kuanzisha na kuendeleza kutoka kizazi hadi kizazi, wasingeweza kugundua mbinu iliyo na uwezo mkubwa zaidi kuliko kushusha thamani ya ndoa.... Sophie Arnoult, mwigizaji mwanamke ambaye alijulikana sana kwa ajili ya maneno na misemo yake ya kuchekesha katika uigizaji wake, alielezea ndoa ya kiserikali kama ‘sakramenti ya uzinzi.’”—Scott, vol. 1, ch. 17.

“Mahali ambapo pia Bwana wetu alisulibiwa.” Kipengele hiki cha unabii nacho kilitimizwa pia na Ufaransa. Hakuna nchi ambapo roho ya uadui dhidi ya Kristo imeoneshwa kwa kiwango kikubwa zaidi ya kile kilichooneshwa katika nchi ya Ufaransa. Hakuna nchi

ambako ukweli ulikutana na upinzani mkali na wa kikatili zaidi ya ulivyokutana katika nchi ya Ufaransa. Katika mateso ambayo Ufaransa iliyafanya juu ya watu walioikiri injili, Ufaransa ilimsulubisha Kristo kwa kuwatesa wanafunzi Wake.

Karne baada ya karne damu ya watakatifu ilimwagwa. Wakati Wawaldensia waliposalimisha maisha yao juu ya milima ya Piedmont "kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu Kristo," ushuhuda kama huo kwa ajili ya ukweli ulitolewa na ndugu zao, Waalbegensia wa Ufaransa. Katika siku za Matengenezo wanafunzi wake waliuawa kwa maumivu ya kutisha. Wafalme na wasaidizi wake, wanawake na wajakazi wa nyumba ya mfalme, maamiri na makamanda wa jeshi la nchi, walilisha macho yao kwa kutazama maumivu ya mashahidi wa Yesu. Wahujenoti jasiri, wakipigania haki za msingi ambazo mioyo ya wanadamu huichukulia kuwa haki zao takatifu sana, walimwaga damu yao katika viwanja vingi vya mapambano. Waprotestanti walihesabiwa kama walihalifu, bei ilipangwa kwa ajili ya vichwa vyao, na waliwindwa kama wanyama wa porini.

"Kanisa jangwani," wazaliwa wachache wa Wakristo ambao walikuwa bado wapo katika nchi ya Ufaransa katika karne ya kumi na nane, wakiwa wamejificha katika milima ya kusini, bado walidumisha imani ya baba zao. Walipojaribu kukutana usiku kando kando ya mlima katika maeneo ya mbugani yaliyojificha, waliwindwa na askari wapanda farasi na kukokotwa kwenda katika utumwa wa maisha katika manchani. Watu safi, wenye tabia njema, na watu wenye akili sana wa nchi ya Ufaransa walifungwa katika minyororo, waliteswa kwa mateso ya kutisha, na walifungwa pamoja na wanyang'anyi na wauaji. (Tazama Wylie, b. 22, ch. 6.)

Wengine, ambao walitendewa kwa huruma kuliko wengine, walipigwa risasi na kufa kikatili, walianguka katika magoti yao wakiomba. Mamia ya wazee, wanawake wasioweza kujilinda, na watoto wasio na hatia waliachwa wakiwa maiti ardhini katika maeneo yao ya mikutano. Katika kuzunguka katika milima au misitu, mahali walipokuwa wamezoea kukutana, halikuwa jambo la ajabu kukuta "kila baada ya hatua nne, maiti zikiwa zimetapakaa katika nyasi, na maiti zingine zikiwa zimening'inizwa juu ya miti." Ardhi yao, ikiwa imeachwa ukiwa kwa upanga, shoka, kuni, "iligeuzwa kuwa nyika ya huzuni." "Maovu haya yalitendwa... siyo nyakati za giza, bali katika zama za mwangaza za mfalme Louis XIV. Sayansi wakati huo ilikuwa imekua, wasomi walikuwa wengi, watumishi wa ikulu na mji mkuu walikuwa wasomi tena wenye umbuji, na kwa kiwango kikubwa maendeleo hayo yalikuwa yamekuza huruma na ukarimu."—Ibid., b. 22, ch. 7.

Lakini matendo mabaya kuliko yote katika orodha ya matendo mabaya ya uhalifu, yalikuwa mauji makuu yaliyotokea eneo la Mtakatifu Bartholomayo. Ulimwengu bado unakumbuka kwa hofu inayotetemesha matukio ya kutisha sana miongoni mwa matendo ya kikatili ya karne zote za kutisha, yalikuwa mauaji ya kuogofya na ya kutisha yaliyofanyikia eneo la Mtakatifu Bartholomayo. Mfalme wa Ufaransa, baada ya kushinikizwa na mapadri na maaskofu wa Kirumi, alitoa idhini kwa ajili ya kazi ya kutisha. Kengele, ilipolia usiku wa

manane, ilikuwa ishara ya mauaji. Maelfu ya Waprotestanti, wakiwa wamesinzia katika nyumba zao, wakitumia heshima waliyoahidiwa na mfalme, walikokotwa nje bila onyo na kuuawa kikatili.

Kama vile Kristo alivyokuwa kiongozi asiyeonekena wa watu Wake kutoka katika utumwa wa Misri, hali kadhalika Shetani alikuwa kiongozi asiyeonekana katika kazi hii ya kutisha ya kuzidisha idadi ya wafia dini. Kwa siku saba mauaji ya kinyama yaliendelea katika jiji la Paris, siku tatu za kwanza kwa hasira isiyoweza kueleweka. Na mauaji hayakufanyika jijini peke yake, bali kwa amri maalumu ya mfalme yalienezwa kwa majimbo na miji mingine ambako Waprotestanti waliweza kupatikana. Kulikuwa hakuna kujali umri au jinsia. Hata watoto wachanga wasio na hatia na wazee wakongwe hawakuachwa hai. Muungwana na mkulima, mzee na kijana, mama na mtoto, walikatwa-katwa pamoja. Katika nchi yote ya Ufaransa mauaji yaliendelea kwa miezi miwili. Watu wema kabisa wapatao elfu sabini, nguvu kazi ya Ufaransa, waliuawa.

"Taarifa za mauaji makuu zilipofika Rumi, furaha miongoni mwa viongozi wa kanisa haikuwa na mipaka. Kardinali wa Lorraine alimzawadia mjumbe kwa taji elfu moja; mzinga wa Mtakatifu Angelo ulipigwa kutoa saluti ya furaha; na kengele zilipigwa katika kila mnara; mioto ya sherehe iligeuza usiku kuwa mchana; na papa Gregory XIII, akiwa na makardinali na viongozi wakuu wengine wa kanisa, walikwenda kwa maandamano marefu kuelekea katika kanisa la Mtakatifu Louis, ambapo kardinali wa Lorraine aliimba wimbo wa sifa na shukurani kwa Mungu uitwao kwa Kilatini Te Deum Medali ilipigwa kama kumbukizi ya mauaji makuu, na katika jiji la Vatikani bado kunaweza kuonekana picha tatu za kuchora za Vasari, zikielezea shambulio dhidi ya mkuu wa jeshi la wanamaji, mfalme akiwa katika kikao cha baraza wakipanga mauaji, na mauaji yenyewe. Gregory alimtumia Charles Ua la Waridi la Dhahabu; na miezi minne baada ya mauaji makuu, alisikiliza kwa kuridhika hubiri la padri wa Kifaransa, ... ambaye alizungumzia juu ya 'siku ile iliyojaa furaha na shangwe, wakati ambapo baba mtakatifu sana alipopata taarifa, na alionesha moyo wa dhati alipotoa shukurani kwa Mungu na kwa Mtakatifu Louis.'"—Henry White, The Massacre of St. Bartholomew, ch. 14, par. 34.

Roho mbaya ile ile iliyohamasisha Mauaji Makuu yaliyofanyikia katika eneo la Mtakatifu Bartholomayo ilichangia pia katika matukio ya Mapinduzi. Yesu Kristo alihukumiwa kuwa yeye ni mwongo, na sauti ya pamoja ya wakanamungu wa Ufaransa ilikuwa, "Ponda Mhuni," maana yake Kristo. Kufuru mbaya kabisa na uovu wa kuchukiza vilienda pamoja, na watu wasio na maadili kabisa, watu katili sana na waovu kupindukia, ndio walioheshimiwa na kutukuzwa sana. Katika mambo yote haya, heshima kuu alipewa Shetani; wakati Kristo, katika tabia Yake ya ukweli, usafi, na upendo usiyo na ubinafsi, alisulubiwa.

"Yulemnyamaatokayekatikakuzimuatafanyavitanao, nayeatawashinda na kuwaua." Mamlaka ya kikanisa iliyotawala katika nchi ya Ufaransa wakati wa Mapinduzi na Utawala

wa Hofu, vilipigana vita dhidi ya Mungu na neno Lake takatifu zaidi kuliko ulimwengu ulivyowahi kushuhudia. Ibada ya Mungu ilipigwa marufuku na Bunge. Biblia zilikusanywa na kuchomwa moto hadharani kwa kila aina ya dhihaka iliyowezekana. Sheria ya Mungu ilikanyagwa-kanyagwa. Taasisi zote za Biblia zilipigwa marufuku. Siku ya mapumziko ya kila juma iliondolewa na badala yake kila siku ya kumi ilitumiwa kwa kejeli na kufuru dhidi ya Mungu. Ubatizo na Meza ya Bwana vilipigwa marufuku. Na matangazo yalibandikwa katika maeneo ya makaburi yakisomeka waziwazi yaliyosema kuwa kifo ni usingizi wa milele.

Kumcha Mungu kulisemwa kuwa mbali kabisa na mwanzo wa hekima na kwamba kumcha Mungu ilikuwa mwanzo wa upumbavu. Aina zote za ibada za kidini zilipigwa marufuku, isipokuwa ibada za uhuru na za nchi. “Askofu wa kikatiba wa Paris aliletwa hadharani afanye jukumu kubwa katika upuuzi wa kijeuri na wa kashfa mbaya sana ambao haujawahi kufanyika mbele ya wawakilishi wa kitaifa.... Aliitwa mbele akiwa na wasaidizi wake katika maandamano kamili, kutangaza kwa Mkutano kuwa dini aliyoifundisha kwa miaka mingi ilikuwa, katika nyanja zake zote, uongo wa kipadri, ambao hauna msingi wowote katika historia na katika ukweli mtakatifu. Alikanusha, kwa uwazi na katika maneno yanayoeleweka kabisa, uwepo wa Mungu ambaye alitoa maisha yake kumwabudu, na aliamua kwa wakati ujao kuabudu uhuru, usawa, mambo mema, na uadilifu. Ndipo alipoweka mezani mapambo ya kiaskofu, na kupewa fursa ya kukumbatiwa na mwenyekiti wa kongamano. Baadhi ya mapadri walioasi walifuata mfano wa askofu huyu.”— Scott, vol. 1, ch. 17.

“Nao wakaao juu ya nchi wafurahi juu yao na kushangilia. Nao watapelekeana zawadi wao kwa wao, kwa kuwa manabii hao wawili waliwatesa wao wakaao juu ya nchi.” Ufaransa iliyomkana Mungu ilikuwa imenyamazisha sauti inayotoa maonyo ya mashahidi wawili wa Mungu. Neno la ukweli lililala likiwa limekufa katika mitaa yake, na wale waliochukia makatazo na masharti ya sheria ya Mungu walifurahia. Watu walimtukana hadharani Mfalme wa mbinguni. Sawa na wenye dhambi wa zamani, walipiga kelele: “Mungu ajuaje? Yako maarifa kwake aliye juu?” (Zaburi 73:11).

Kwa ujasiri wenye kufuru kuliko inavyoweza kuaminika, mmoja wa mapadri wa shirika jipya alisema: “Mungu, kama kweli upo, lipiza kisasi kwa ajili ya jina Lako lililojeruhiwa. Mimi ninakutukana Wewe! Unakaa kimya; hutumi radi Zako. Ni nani atakayeamini uwepo Wako baada ya tukio hili?”— Lacretelle, History 11:309; in Sir Archibald Alison, History of Europe, vol. 1, ch. 10. Huu ulikuwa mwangwi wa dai la Farao: “Bwana ni nani, hata niitii sauti Yake?”“Mimi simjui Bwana!”

“Mpumbavu amesema moyoni mwake, hakuna Mungu” (Zaburi 14:1). Na Bwana anasema kuhusu watu wanaopotosha ukweli: “Upumbavu wao utakuwa dhahiri kwa watu wote”(2 Timotheo 3:9). Baada ya Ufaransa kupiga marufuku ibada ya Mungu aliye hai, “Yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele,” haikuchukua muda mrefu Ufaransa iliporomoka hadi

kuanzisha ibada ya sanamu inayodhalilisha, kwa kuabudu Mungu Mke wa Mantiki, katika utu wa mwanamke fisadi. Na ibada hii ilifanywa katika kongamano lililowakilisha taifa, na mamlaka kuu kabisa za kiraia na kibunge! Anasema mwanahistoria: “Moja ya sherehe za wakati huu wa ukichaa, upuuzi uliounganishwa na uasi dhidi ya Mungu viliwekwa mbele ya watu. Milango ya uwanja ilifunguliwa kuruhusu wanamuziki, kuingia wakiwa wametanguliwa na viongozi wakuu wa jiji, waliingia kwa maandamano makubwa, wakiimba wimbo wa kusifu uhuru, wakisindikiza mtu ambaye baadaye ndiye alikuja kuwa wa kuabudiwa, mwanamke aliyefunikwa, ambaye walimwita Mungu wa Mantiki. Baada ya kuingizwa alifunuliwa, akiwa mrefu, na aliketishwa upande wa kulia wa mwenyekiti wa kongamano, ambapo alitambuliwa kuwa ni binti mchezaji wa muziki wa opera. Binti huyu, kama mwakilishi stahiki wa mungu hoja waliyemwabudu, Kongamano la Kitaifa la Ufaransa lilifanya ibada kwa ajili yake.

“Mchezo huu wa kipagani na kipuuzi ulifanywa kwa mtindo maalumu; na usimikaji huu wa Mungu Mke wa Mantiki ulifanywa na kuigizwa upya katika taifa zima, katika maeneo ambayo wakazi wake walitamani kujionesha kuwa sehemu ya Mapinduzi.”—Scott, vol. 1, ch. 17.

Alisema msemaji mahiri aliyetambulisha ibada ya Mantiki: “Watunga sheria! Ushikiliaji sana mambo bila akili umeondoka na nafasi yake imechukuliwa na mantiki. Macho yake yasiyoona vizuri yasingeweza kustahimili mwangaza mkali wa nuru. Siku ya leo mkutano mkubwa umekusanyika chini ya matao hayo ya kigothiki, ambayo, kwa mara ya kwanza, yamerudishamwangwiwaukweli. PaleWafaransawamesherehekea ibada pekee ya kweli,—ibada ya Uhuru, ibada ya Mantiki. Hapa tumefanya maombi kwa ajili ya mafanikio ya majeshi ya Jamhuri. Pale tumeachana na sanamu zisizo na uhai na badala yake tumepata mungu Mantiki, sanamu ile iliyo hai, kiumbe aliye mzuri sana katika vitu vya asili.”—M. A. Thiers, History of the French Revolution, vol. 2, uk. 370, 371.

Wakati mungu mke alipoletwa ukumbini, msemaji alimshika mkono, na akiuangalia umati alisema: “Enyi watu mnaokufa, acheni kutetemeka mbele ya radi zisizo na nguvu za Mungu ambaye amesababisha hofu zenu. Tangu sasa msimtambue mungu mwingine zaidi ya Mantiki. Ninawapa sanamu yake iliyo tukufu na safi sana, toeni kafara zenu kwa mungu huyu. Angukeni mbele ya Seneti kubwa ya Uhuru, O! Kifuniko cha Mantiki!”

“Mungu mke, baada ya kukumbatiwa na mwenyekiti wa kongamano, alipandishwa juu ya gari zuri, na aliendeshwa, katikati ya kundi kubwa la watu, hadi katika kanisa kuu la Notre Dame, kuchukua nafasi ya Mungu. Pale alipandishwa juu hadi katika madhabahu ya juu, na alipokelea hapo heshima za wote waliokuwepo.”—Alison, vol. 1, ch. 10.

Hili lilifuatwa, muda mfupi baadaye, na uchomaji wa Biblia hadharani. Wakati mmoja wanachama wa “Chama Mashuhuri cha Nyumba ya Makumbusho” waliingia katika ukumbi

wa manispaa, wakipiga kelele, “Hongera sana Mantiki!” wakiwa wameba juu ya mlingoti mabaki ya vitabu kadhaa vilivyounguzwa moto, miongoni mwake vikiwemo vitabu vya sala, vitabu vya nyimbo, na Agano la Kale na Jipya, “vilivyopatanishwa katika moto mkuu,” alisema mwenyekiti, “upumbavu wote walioubuni wamewaongoza wanadamu kuutekeleza.”—Journal of Paris, 1793, No. 318. Quoted in Buchez-Roux, Collection of Parliamentary History, vol. 30, pp. 200, 201.

Upapa ndio ulioanzisha kazi ambayo ukanamungu ulikuwa ukikamilisha. Sera za Rumi zilitengeneza yale mazingira, ya kijamii, kisiasa, na kidini, ambayo yalikuwa yakiipeleka Ufaransa katika maangamizi. Waandishi, wakizungumzia vitisho vya Mapinduzi, wanasema kuwa huku kuvuka mipaka kunapaswa kuleta lawama kwa kiti cha enzi na kanisa. (Tazama Kiambatisho.) Katika maana halisi ya kutenda haki mashitaka haya yanapaswa kurundikwa juu ya kanisa. Upapa uliweka sumu katika akili za wafalme dhidi ya Matengenezo, kama adui wa ufalme, wazo la uchonganishi ambalo lingekuwa hatarishi kwa amani na utangamano wa taifa. Ilikuwa ushawishi wa Rumi ambao kwa njia hiyo ulihamasisha ukatili wa kutisha na ukandamizaji usio kifani uliofanywa na mfalme.

Roho ya uhuru iliondoka pamoja na Biblia. Popote injili ilipopokelewa, akili za watu ziliamshwa. Walianza kutupilia mbali minyororo ambayo ilikuwa imewafunga katika utumwa wa ujinga, uovu, na ushirikina. Walianza kufikiri na kutenda kama watu. Wafalme walianza kutetemeka kwa ajili ya ukandamizaji wao.

Rumi haikuchelewa kuchochea hofu na wivu wao. Papa alimwambia balozi wa Ufaransa mwaka 1525: “Wazimu [Uprotestanti] huu siyo tu kuwa utashinda na kuharibu dini, bali utashinda na kuharibu tawala zote, utashinda na kuangamiza uungwana, sheria, utaratibu, na mamlaka zote.”—G. de Felice, History of the Protestants of France, b. 1, ch. 2, par. 8. Miaka michache baadaye balozi wa papa alimwonya mfalme: “Mheshimiwa, usidanganyike. Waprotestanti watavuruga utaratibu wote wa kiraia na wa kidini.... Kiti cha enzi na madhabahu vyote kwa pamoja viko hatarini.... Uanzishaji wa dini mpya kwa vyovyote vile utaanzisha serikali mpya.”— D’Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 2, ch. 36.

Na wanateolojia waliamsha chuki za watu kwa kutangaza kuwa mafundisho ya Kiprotestanti “yanawashawishi watu kushika mambo mapya ya kipumbavu; yanamnyang’anya mfalme heshima na utii wa raia, na yanavuruga kanisa na serikali.” Hivyo ndivyo Rumi ilivyofaulu kuipanga Ufaransa dhidi ya Matengenezo. “Ilikuwa ni kwa kusudi la kudumisha kiti cha enzi, kulinda waungwana, na kudumisha sheria, ndiyo maana upanga wa mateso kwa mara ya kwanza ulichomolewa kutoka katika ala yake katika nchi ya Ufaransa.”—Wylie, b. 13, ch. 4.

Kidogo sana watawala wa nchi walijua mapema matokeo ya sera hiyo hatarishi. Mafundisho ya Biblia yangeweza kujaza akili na mioyo ya watu kanuni za haki, kiasi, ukweli, na ukarimu ambazo ndizo jiwe kuu la pembeni la mafanikio ya taifa. “Haki huinua taifa.” Na kwa njia hiyo “kiti cha enzi huimarika” (Mithali 14:34; 16:12). “Kazi ya haki itakuwa amani;” na matokeo yake, “yatakuwa ni utulivu na matumaini daima” (Isaiah 32:17). Anayeitii sheria ya Mungu ataziheshimu na kuzitii kikamilifu sheria za nchi yake. Mtu anayemcha Mungu atamheshimu mfalme katika utekelezaji wa mamlaka yake yote ya haki na halali. Lakini Ufaransa yenye huzuni ilipiga marufuku Biblia na kuwafukuza wafuasi wake. Karne baada ya karne, watu wa kanuni na uadilifu, watu wenye akili makini na nguvu ya kimaadili, waliokuwa na ujasiri wa kusimamia kile walichokiamini na imani yao kiasi cha kuteseka kwa ajili ya ukweli—kwa karne nyingi watu hawa walifanya kazi kwa nguvu nyingi kama watumwa katika vichochoro, waliuawa kwa moto, au waliozea katika vyumba vya magereza. Maelfu kwa maelfu walipata usalama kwa kukimbia na kwenda uhamishoni; na jambo hili liliendela kwa miaka mia mbili hamsini baada ya kuanzishwa kwa Matengenezo.

“Kwa mara chache sana kulikuwepo kizazi cha watu wa Ufaransa wakati wa kipindi kirefu ambacho hakikushuhudia wanafunzi wa injili wakikimbia mbele ya hasira za kichaa za mtesaji, na wakiondoka na akili, sanaa, bidii, na utaratibu, ambapo, kama kanuni, walifanikiwa kwa viwango vya juu sana, kutajirisha nchi ambazo walipata hifadhi. Na kwa uwiano ule ule ambao walizijaza nchi nyingine kwa karama hizi, ndivyo walivyoondoa karama hizo katika nchi ya Ufaransa.

Ikiwa wale wote waliofukuzwa wangetunzwa katika nchi ya Ufaransa; ikiwa, katika miaka hii mia tatu, stadi za viwanda za wakimbizi zingekuwa zikilima udongo wake; ikiwa, katika miaka hii mia tatu, ujuzi wao wa sanaa ungekuwa ukitumiwa katika uzalishaji nchini mwao; ikiwa, katika miaka hii mia tatu, akili zao zenye ubunifu na nguvu ya uchambuzi zingetumiwa kuboresha fasihi yake na kuendeleza sayansi yake; ikiwa hekima yake ingetumiwa kuongoza mabaraza yake, mashujaa wake wakipigana vita vyao, haki yao ikitunga sheria zake, na dini ya Biblia ikiimarisha akili na ikiongoza dhamiri za watu, ni utukufu mwingi kiasi gani ungeifunika Ufaransa leo! Ufaransa leo ingekuwa nchi kubwa duniani, yenye mafanikio, na furaha—kielelezo cha kuigwa na mataifa mengine!

“Lakini chuki yenye upofu na isiyoepukika ilimfukuza kutoka katika udongo wake kila mwalimu wa tabia njema, kila shujaa wa utaratibu, kila mlinzi mwaminifu wa kiti cha enzi; iliwaambia watu ambao walikuwa na uwezo wa kuifanya nchi yao ‘ijulikane na itukuke’, chagua unachokitaka, kuchomwa moto au kukimbilia uhamishoni. Hatimaye uharibifu wa dola ulikamilika; hakukubaki dhamiri ya kupigwa marufuku; hakuna dini ya kukokotwa kwenda kwenye jukwaa la kuchomea moto watu; hakuna uzalendo wa kufukuzwa uondoke nchini.”—Wylie, b. 13, ch. 20. Na Mapinduzi, na mambo yake ya kutisha, yalikuwa ndiyo matokeo yake na machungu yake.

"Kwa kitendo cha Wahujenoti kuikimbia nchi mdororo wa jumla wa kiuchumi uliikumba nchi ya Ufaransa. Miji iliyokuwa ikistawi kwa viwanda uchumi wake uliporomoka; wilaya zenye rutuba zilirudi katika hali yake ya zamani ya nyika; udumavu wa akili na anguko la uadilifu vilifuata kipindi cha maendeleo yaliyokuwa siyo ya kawaida. Jiji la Paris liligeuka na kuwa nyumba kubwa ya ombaomba, na inakadiriwa kuwa, wakati Mapinduzi yakianza, watu ombaomba laki mbili walikuwa wakitafuta msaada kutoka katika mikono ya mfalme. Majesuti peke yao ndio waliostawi katika taifa lililokuwa likioza, na walitawala kwa ukatili wa kutisha makanisa na shule, magereza na manchani."

Injili ingekuwa imeiletea Ufaransa suluhisho la yale matatizo ya kisiasa na kijamii ambayo yalishinda stadi za viongozi wake wa kidini, mfalme wake, na wabunge wake, na mwisho wake yakaliweka taifa katika hali isiyotawalika na uharibifu mkubwa. Lakini chini ya madhehebu ya Rumi watu walipoteza masomo ya Mwokozi yenye baraka za kujikana nafsi na upendo usio na ubinafsi. Waliongozwa mbali na matendo ya kujikana nafsi kwa ajili ya wengine. Matajiri hawakukemewa kwa kuwakandamiza maskini, watu maskini hawakuwa na msaada kwa ajili ya utumwa na udhalilishwaji wao. Uchoyo wa watu maskini na wenye nguvu uliongezeka na kuongezeka katika uhalisia ukandamizaji wake. Kwa karne nyingi ulafi na ufisadi wa watu wenye fursa zao ulisababisha unyonyaji kwa wakulima wadogo. Matajiri waliwakosea watu maskini, na watu maskini waliwachukia matajiri.

Katika majimbo mengi ardhi ilimilikiwa na matajiri, na watu waliokuwa katika matabaka ya wafanya kazi walikuwa wapangaji tu; waliishi kwa rehema za wamiliki wa mashamba husika na walilazimishwa kulipa gharama za juu. Mzigo wa kutegemeza kanisa na dola uliwaangukia watu wa daraja la kati na daraja la chini, ambao walitozwa kodi kubwa na mamlaka za kiraia na mamlaka za kidini. "Raha ya matajiri ilichukuliwa kuwa sheria kuu; wakulima wakubwa na wakulima wadogo wangeweza kukosa chakula, ilhali wakandamizaji wao waliendelea kunawiri na kustawi. Watu walilazimishwa kila mahali kujali maslahi pekee ya mabwana zao. Maisha ya vibarua katika kilimo yalikuwa maisha ya kazi zisizoisha na madhila yasiyopungua; malalamiko yao, ikiwa walidiriki kulalamika, yalijibiwa kwa dharau na matusi.

Mahakama za haki ziliwasikiliza siku zote matajiri kuliko wakulima; rushwa zilipokelewa sana na majaji; na mwelekeo mdogo tu wa mtawala ulitosha kupata nguvu ya kisheria, kwa sababu ya mfumo wa rushwa iliyokithiri. Kuhusiana na kodi zilizokamuliwa kutoka kwa watu wa kawaida, kwa njia ya viongozi wa serikali kwa upande mmoja, na viongozi wa kanisa kwa upande mwingine, fedha iliyofika katika hazina ya mfalme au katika hazina ya askofu haikuzidi nusu; sehemu iliyobaki ilitapanywa katika maisha ya ufisadi na anasa. Na watu waliowafanya wenzao kuwa maskini wao wenyewe walikuwa wanasamehewa kodi, na walipewa haki na sheria au desturi kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali serikalini. Idadi ya watu waliokuwa na upendeleo maalumu walikuwa laki moja hamsini elfu, na kwa

ajili ya raha zao mamilioni ya watu walilazimishwa kuishi maisha yasiyokuwa na matumaini na ya kudhalilika sana." (Tazama Kiambatisho.)

Ofisi ya mfalme ilijaa anasa na ubadhirifu. Kulikuwa na imani ndogo sana kati ya raia na watawala. Hatua zote zilizochukuliwa na serikali zilitiliwa mashaka kwa sababu ya ubinafsi na uchoyo uliotawala. Kwa zaidi ya nusu karne kabla ya wakati wa Mapinduzi kiti cha enzi kilikaliwa na Louis XV, ambaye, hata nyakati zile za uovu, alijulikana kama mfalme mvivu, asiyekuwa makini, na mwenye tamaa. Akiwa na tabaka la watawala makabaila katili na tabaka la chini la watu maskini, dola ikiwa na matatizo makubwa ya kifedha na watu wakiwa na hasira, halikuhitajika jicho la nabii kuona mapema bomu lililokuwa karibu kulipuka. Kwa maonyo ya washauri wake mfalme alikuwa na desturi ya kujibu: "Najaribu kufanya mambo yaendelee hivyo kwa kadiri nitakavyoendelea kuishi; baada ya kifo changu mambo yatakuwa yatakavyokuwa." Mashauri ya kufanya matengenezo yalitolewa lakini aliyaona maovu, lakini hakuwa na ujasiri wala nguvu ya kukabiliana nayo. Uharibifu ulioisubiri Ufaransa ulielezwa kwa lugha ya picha katika jibu lake la kivivu na kibinafsi, "Baada yangu, gharika!"

Kwa kucheza na wivu wa wafalme na wa matabaka ya watawala, Rumi ilipata mamlaka ya kuwafanya wawafanye watu kuwa watumwa wao, Rumi ikijua vema kuwa hatimaye dola itadhoofika, na kwa njia hiyo atapata wepesi wa kuwaweka watawala na watu wao wote kwa pamoja chini kongwa lake la utumwa. Kwa sera iliyoona mbali Roma ilielewa kuwa ili kuwaweka watu katika utumwa kikamilifu, pingu zinapaswa kufungwa kwenye roho zao; na kwamba njia ya hakika kabisa ya kuwazuia watu wasitoke katika utumwa wao ilikuwa kuwafanya wasiweze kuwa huru. Jambo jingine lililoleta zaidi ya maelfu ya mateso ya kutisha kuliko mateso ya kimwili yaliyosababisha kutungwa kwa sera yake, ilikuwa kushuka kwa kiwango cha uadilifu. Wakiwa wamenyang'anywa Biblia, na wakiwa wameachiwa mafundisho ya chuki na ubinafsi, watu walifunikwa na ujinga na ushirikina, na walizama katika uovu, kiasi kwamba walijikuta hawana uwezo wa kujiongoza.

Lakini matokeo ya mambo haya yote yalikuwa tofauti sana na kile Rumi ilichokuwa imekikusudia. Badala ya kuushikilia umma katika utii usio na maswali kwa mafundisho yake yasiyohojiwa, matokeo yake yaliwafanya kuwa makafiri na wanamapinduzi. Waliudhihaki Urumi kama ni usanii wa mapadri. Waliwaona viongozi wa kidini kama kikundi cha kuwakandamiza. Mungu pekee waliyemjua alikuwa mungu wa Roma; mafundisho yake ndiyo yalikuwa dini yao pekee. Walichukulia ulafi na ukatili wako kama matunda halali ya Biblia, na hawakutamani kuwa na mojawapo ya hayo.

Rumi iliwakilisha vibaya tabia ya Mungu na ilipotosha maagizo Yake, na sasa watu walikataa Biblia na Mwasisi wake. Rumi ilitaka imani isiyohoji mafundisho yake, chini ya idhini bandia ya Maandiko. Katika mwitikio kwa hilo, Voltaire na washirika wake walitupilia mbali neno la Mungu kabisa na wakasambaza sumu ya ukanamungu kila mahali. Rumi

ilikuwa imekanyaga watu chini ya nyayo zake za chuma; na sasa umma wa watu, wakiwa wamedhalilika na kufanyiwa ukatili mkubwa, katika kujibu mapigo ya mtesaji wao katili, walitupilia mbali kila kizuizi. Wakiwa wamekasirika kwa sababu ya uongo wa wazi ambao kwa muda mrefu walikuwa wakiuabudu, walitupilia mbali ukweli na uongo kwa pamoja; na wakichukulia kuwa uvunjaji wa sheria ndiyo uhuru, watumwa wa uovu walifurahia uhuru wao wa kufikirika.

Wakati wa mwanzo wa Mapinduzi, kwa idhini ya mfalme, watu wa kawaida walipewa fursa ya uwakilishi unaozidi ule wa matajiri na viongozi wa dini wakiwekwa pamoja. Kwa njia hiyo, mzani wa mamlaka ulikwenda katika mikono yao; lakini hawakuwa wamejiandaa kuutumia mzani huo kwa hekima na kiasi. Wakiwa na shauku ya kushughulikia mabaya waliyotendewa, waliazimia kufanya kazi ya kuijenga upya jamii. Raia walioudhiwa, ambao akili zao zilikuwa zimejazwa uchungu na kumbukumbu za muda mrefu za mabaya waliyotendewa, waliazimia kuipindua hali yao ya mateso ambayo yalikuwa yamekuwa makubwa kiasi cha kutoweza kuchukulika na kulipiza kisasi kwa wale ambao waliwachukulia kuwa waasisi wa mateso yao. Waliokandamizwa walitumia somo ambalo walijifunza kutokana na ukatili na wakawa wakandamizaji wa wale waliwakandamiza.

Ufaransa yenye huzuni ilivuna umwagikaji wa damu kama mavuno ya mbegu walizopanda wao wenyewe. Matokeo ya kuutii utawala na mamlaka ya Rumi yalikuwa ya kutisha. Wakati Ufaransa, chini ya usimamizi wa Dini ya Kirumi, ilijenga nguzo ya kwanza ya kuchomea watu moto mwanzoni mwa Matengenezo, hapo ndipo Mapinduzi yalijenga bamba la kwanza la kukatia vichwa vya wahalifu. Mahali pale pale ambapo wafia dini wa kwanza wa imani ya Kiprotestanti walichomewa moto katika karne ya kumi na sita, wahanga wa kwanza wa Mapinduzi walikatwa vichwa katika karne ya kumi na nane. Kwa kitendo cha kuikataa injili, ambayo ingeleta uponyaji wa nchi yao, Ufaransa ilifungua mlango kuruhusu ukanamungu na uharibifu uingie ndani ya nchi. Mara tu baada ya vizuizi vya sheria ya Mungu kuwekwa pembeni, ilionekana wazi kuwa sheria za mwanadamu haziwezi kudhibiti mawimbi yenye nguvu ya mihemko ya kibinadamu; na taifa lilisombwa na kupelekwa katika uasi na kutotawalika. Vita dhidi ya Biblia ilizindua zama ambazo husimama kama zama za Utawala wa Hofu. Amani na furaha viliondolewa katika nyumba na mioyo ya watu. Hakuna mtu aliyekuwa salama. Aliyesherehekea ushindi leo alishukiwa, alihukumiwa, kesho. Ukatili na tamaa vilitawala bila mpinzani.

Mchungaji, viongozi wa kazi, na matajiri walilazimishwa kujisalimisha kwa mauaji ya watu walioingiwa na kichaa. Kiu yao ya kulipiza kisasi iliamshwa tu na mauaji ya mfalme; na watu walioamuru auawe muda si mrefu walimfuata kwenye jukwaa la kunyongea. Mauji ya jumla ya wote walioshukiwa kuwa kinyume na Mapinduzi yalipangwa rasmi. Magereza yalifurika wafungwa, wakati mmoja yakiwa na wafungwa zaidi ya laki mbili. Miji ya ufalme ilijaa matukio ya kutisha. Kikundi kimoja cha wanamapinduzi kilipigana na kikundi kingine, na Ufaransa iligeuka kuwa uwanja mkubwa wa makundi ya watu wanaopingana,

wakiongozwa na hasira ya mihemko yao. “Katika jiji la Paris tukio moja la ghasia lilifuata jingine, na raia waligawanyika katika mchanganyiko wa vikundi vinavyopingana, ambavyo vilionekana vilikuwa vimedhamiria kuuana na kumalizana kabisa.” Na kuongezeka kwa matatizo ya jumla ya taifa, Ufaransa iliingia katika vita ya muda mrefu na yenye madhara makubwa dhidi ya mataifa makubwa ya Ulaya. “Nchi ilikuwa karibu kufilisika, wanajeshi walikuwa wakidai malipo ya nyuma ya mishahara yao, wakazi wa jiji la Paris walikuwa wanakaribia kufa kwa njaa, majimbo yalikuwa yamebaki bila kitu kwa sababu ya wanyang’anyi, na ustaarabu ulikaribia kufutika kwa sababu ya nchi kutotawalika na uhalifu usio na mamlaka ya kuudhibiti.”

Kwa kiwango kikubwa watu walikuwa walijifunza masomo kutokana na ukatili na mateso ambayo Rumi ilikuwa imewafundisha kwa juhudi kubwa. Siku ya kupatilizwa ilikuwa imekuja hatimaye. Wakati huu siyo wanafunzi wa Yesu waliotupwa magerezani na walioburuzwa kwenda kwenye nguzo za kuchomea watu moto. Muda mrefu uliopita watu hawa waliangamizwa au walifukuzwa na kwenda kuishi uhamishoni. Roma isiyo na huruma sasa ilihisi nguvu ya mauaji ya wale ambao iliwafundisha kufurahia matendo ya umwagaji damu. “Mfano wa utesaji ambao viongozi wa kanisa la Ufaransa waliuonesha kwa zama nyingi, sasa uliwarudia wao kwa nguvu nyingi zaidi. Majukwaa ya kunyongea watu yalikuwa na wekundu wa damu ya mapadri iliyokuwa ikitiririka. Manchani na magereza, ambayo awali yalijawa na Wahujenoti, sasa yalijawa na watesaji wao. Wakiwa wamefungiwa kwa minyororo kwenye benchi na wakivuja jasho kwenye kasia, viongozi wa kanisa Katoliki la Roma walipata uzoefu wa mateso ambayo kanisa lao liliyafanya sana dhidi ya wazushi wapole” (Tazama Kiambatanisho.)

“Ndipo zilikuja siku ambazo sheria ya kikatili zaidi kuliko sheria zote ilitekelezwa na mahakama katili kuliko mahakama zote; ambapo hakuna mtu ambaye angeweza kusalimia jirani zake au kufanya maombi yake binafsi ... bila hatari ya kutenda kosa linaloadhibiwa kwa kifo; wakati wapelelezi walipotembelea kona zote; wakati bamba la kukatia vichwa vya watu lilikuwa refu na gumu likiwa kazini kila asubuhi; wakati magereza yakijazwa kama meli za watumwa zinavyojazwa; wakati mifereji ilipopitisha damu ikitiririka kuelekea mto Wakati magari ya kukokotwa na ng’ombe yaliyobeba wahanga yalipopita katika mitaa ya Paris, yakiwapeleka mahali pa kuuliwa, wawakilishi, ambao kamati ya mfalme ilikuwa imewatuma katika idara mbalimbali, walisherehekea kwa njia ya ukatili mkubwa ambao ulikuwa haujawahi kuonekana katika mji mkuu.

Kisu cha mashine ya kuulia kiliinuka na kuanguka kwa kasi ambayo ilikuwa ndogo mno kwa kazi yao ya kuchinja watu. Mistari mirefu ya mateka ilifyekwa kwa mundu wa kukatia vichara vya zabibu. Matundu yaliwekwa katika sakafu ya mtumbwi uliojaa watu. Mji wa Lyons uligeuka kuwa jangwa. Katika mji wa Arras hata rehema ya kikatili ya kifo cha haraka wafungwa walinyimwa. Maeneo yote hadi Loire, tangu Saumur hadi baharini, makundi makubwa ya kunguru na mwewe walikula maiti zilizokuwa uchi, zikiwa zimejisokota pamoja

na kukumbatiana katika namna isiyofaa kuonwa. Hakuna huruma iliyooneshwa kwa jinsia au umri. Idadi ya wavulana na wasichana wa miaka kumi na saba waliouliwa na serikali ile inayotisha, inakadiriwa kuwa mamia. Watoto wachanga walionyakuliwa kutoka katika vifua vya mama zao walitupwa kutoka mkuki hadi mkuki kwenye mtaa wa Jacobin." (Tazama Kiambatanisho.) Katika muda mfupi wa miaka kumi, maelfu ya wanadamu waliuawa.

Yote haya yalitendeka kulingana na matakwa ya Shetani. Jambo hili ndilo ambalo kwa zama nyingi amekuwa akilifanyia kazi. Sera yake ni uongo tangu mwanzo hadi mwisho, na kusudi lake ni kuleta maumivu na maafa kwa wanadamu, kuharibu na kuchafua kazi ya Mungu, kutia doa katika makusudi ya Mungu matakatifu ya ukarimu na upendo, na kwa njia hiyo alete huzuni mbinguni. Hivyo basi, kwa sanaa zake za uongo anatia upofu katika akili za watu, na anawaongoza watu kutupa lawama za kazi za Shetani kwa Mungu, kana kwamba maumivu ni matokeo ya mpango wa Muumbaji. Kwa jinsi hiyo hiyo, wakati watu ambao wamedhalilishwa na ambao wameumizwa sana kwa sababu ya nguvu yake ya kikatili wanapopata uhuru wao, anawashawishi waende mbali zaidi katika kuwatesa watesi wao. Ndipo picha ya uovu usio na mipaka unapotumiwa na watu wakatili na watesaji kama kielelezo cha matokeo ya uhuru.

Wakati kosa katika vazi moja linapogunduliwa, Shetani anavalisha kosa hilo hilo katika joho jingine, na watu wengi hulipokea kwa shauku kubwa kama walivyopokea kosa hilo katika vazi la kwanza. Watu walipogundua kuwa dini ya Kirumi ni dini ya uongo, na Shetani akatambua kuwa asingeweza tena kwa kupitia taasisi hii kuwaongoza watu kukiuka sheria ya Mungu, Shetani aliwashawishi watu kuchukulia dini zote kuwa ni udanganyifu, na kuwa Biblia ni hadithi ya uongo; na, wakitupa pembeni amri takatifu, watu walijiachia na kujiingiza katika uovu usio na mipaka.

Kosa kubwa lililoleta madhara makubwa kwa wananchi wa Ufaransa ilikuwa kupuuza ukweli huu mmoja: kuwa uhuru wa kweli unapatikana katika utii wa dhati kwa sheria ya Mungu. "Laiti ungalisikiliza amri zangu! Ndipo amani yako ingalikuwa kama mto wa maji, na haki yako kama mawimbi ya bahari." "Bali kila anisikilizaye atakaa salama, Naye atatulia bila kuogopa mabaya" (Isaya 48:18, 22; Mithali 1:33).

Wakanamungu, wasioamini, na waasi hupinga na hukataa sheria ya Mungu; lakini matokeo ya mvuto wao huthibitisha kuwa ustawi wa mwanadamu umeshikamana na utii wake kwa amri za Mungu. Wasiojifunza somo katika kitabu cha Mungu wanalazimishwa kulipata somo hilo katika historia ya mataifa.

Wakati Shetani alipolitumia Kanisa la Kirumi kuwapeleka watu mbali na utii, mbinu yake ilifichwa, na kazi yake ilikuwa imefunikwa kiasi kwamba udhalilishaji na maumivu yaliyotokana na mbinu hiyo havikuonekana kuwa ni matunda ya uasi dhidi ya sheria ya Mungu. Na nguvu yake kwa kiasi kikubwa ilidhibitiwa na utendaji kazi wa Roho wa Mungu

kwa hiyo makusudi yake yalizuiliwa kukomaa na kufika hatua ya kuzaa matunda yaliyotarajiwa. Watu hawakuweza kuunganisha madhara na chanzo chake, na hivyo, hawakuweza kugundua sababu ya taabu zao.

Lakini katika Mapinduzi sheria ya Mungu iliwekwa pembeni waziwazi na Baraza Kuu la Kutunga Sheria. Na katika Utawala wa Hofu uliofuata, utendaji kazi wa chanzo na madhara viliweza kuonekana kwa wote. Kwa sababu hukumu juu ya tendo baya haitekelezwi upesi, mioyo ya wanadamu. Wakati Ufaransa ilipomkataa Mungu na kuiweka Biblia pembeni, watu waovu na roho za mashetani walifurahia kufikia lengo ambalo walilitamani kwa muda mrefu—ufalme usiothibitiwa na sheria ya Mungu. Kwa kuwa hukumu juu ya tendo baya haitekelezwi upesi, matokeo yake mioyo ya wanadamuilithibitishwa“ndaniyaoilikutendamabaya”(Mhubiri 8:11). Lakini ukiukwaji wa sheria ya haki na takatifu lazima ulete maumivu na maangamizi kwa vyo vyote vile. Ingawa hukumu juu ya tendo baya haitekelezwi upesi, matendo maovu ya wanadamu yalikuwa yakiratibu utekelezaji wa uharibifu wao. Karne nyingi za uasi na uhalifu zilikuwa zikidunduliza ghadhabu dhidi ya siku ya kupatilizwa; na uovu wao ulipojaa, watu waliokuwa wakimdhihaki Mungu walijifunza kwa kuchelewa kuwa ni jambo linalotisha kuuchosha uvumilivu wa Mungu.

Roho wa Mungu anayedhibiti, anayeweka kizuizi dhidi ya nguvu za kikatili za Shetani, alikuwa ameondolewa kwa kiwango kikubwa, na yule ambaye furaha yake ni kuwaona wanadamu wakiwa katika mateso aliruhusiwa kutekeleza mapenzi yake. Wale ambao walikuwa wamechagua huduma ya uasi waliachwa wavune matunda ya uasi mpaka nchi ilijazwa kwa uhalifu wa kutisha kiasi ambacho kalamu haiwezi kuandika. Kutoka katika majimbo yaliyoharibiwa na miji ilivyovunjwa vunjwa kilio cha kutisha kilisikika—kilio cha uchungu mwingi sana. Ufaransa ilitikiswa kama vile tetemeko la ardhi linavyotikisa nchi.

Dini, sheria, utulivu wa kijamii, familia, dola, na kanisa— vyote viliharibiwa na mikono ya watu wasiomcha Mungu iliyokuwa imeinuliwa dhidi ya sheria ya Mungu. Mwenye hekima alisema ukweli: “Mtu mwovu ataanguka kwa uovu wake.”“Ajapokuwa mwenye dhambi amefanya maovu mara mia, akazidisha siku zake; lakini hata hivyo najua hakika ya kwamba itakuwa heri kwao wamchao Mungu, wenye kicho mbele zake; walakini haitakuwa heri kwa mwovu” (Mithali 11:5; Mhubiri 8:12, 13). “Kwa kuwa walichukia maarifa, Wala hawakuchagua kumcha Bwana;” “Kwa hiyo watakula matunda ya njia yao, Watashiba mashauri yao wenyewe” (Mithali 1:29, 31).

Mashahidi waaminifu wa Mungu, waliochinjwa na mamlaka yenye makufuru “inayopanda kutoka kuzimu,” hawakubaki kimya kwa muda mrefu. “Na baada ya siku hizo tatu u nusu, roho ya uhai itokayo kwa Mungu ikawaingia, wakasimama juu ya miguu yao; na hofu kuu ikawaangukia watu waliowatazama” (Ufunuo 11:11). Ilikuwa mwaka 1793 ambapo sheria zilizopiga marufuku dini ya Kikristo na kuweka pembeni Biblia zilipitishwa na Bunge

la Ufaransa. Miaka mitatu na nusu baadaye, azimio lililotengua sheria hizi, na hivyo kutoa uhuru wa watu kusoma Maandiko, lilipitishwa na Bunge hilo hilo. Ulimwengu ulisimama kwa mshangao na hofu kubwa baada ya kuona ukubwa wa madhara yaliyotokana na kuyakataa Maandiko Matakatifu, na watu wakatambua umuhimu wa kumwamini Mungu na kuliamini neo Lake kama msingi wa matendo mema na uadilifu. Bwana alisema:"Ni nani uliyemshutumu na kumtukana? Umeinua sauti yako juu ya nani, na kuinua macho yako juu? Juu ya Mtakatifu wa Israeli," (Isaya 37:23). "Basi, tazama, nitawajulisha, mara moja hii nitawajulisha, mkono wangu, na nguvu zangu; nao watajua ya kuwa, jina langu ni YEHOVA" (Yeremia 16:21).

Kuhusu mashahidi wawili nabii anaeleza zaidi: "Wakasikia sauti kuu kutoka mbinguni ikiwaambia, Pandeni hata huku. Wakapanda mbinguni katika wingu, adui zao wakiwatazama" (Ufunuo 11:12). Tangu Ufaransa ilipopiga vita dhidi ya mashahidi wawili wa Mungu, mashahidi hao walipewa heshima kubwa mno kuliko kabla ya hapo. Mwaka 1804 shirika la kuchapisha na kusambaza Biblia la British and Foreign Bible Society lilianzishwa. Shirika hilo lilifuatwa na mashirika mengine yanayofanana na hilo, yakiwa na matawi mengi, katika bara la Ulaya. Mwaka 1816 shirika la American Bible Society liliundwa. Wakati shirika la British Society lilipoundwa, Biblia ilikuwa imechapishwa na kusambazwa katika lugha hamsini. Tangu wakati huo Biblia imeshachapishwa katika lugha na lahaja mamia mengi. (Tazama Kiambatanisho.)

Kwa miaka hamsini kabla ya 1792, juhudi kidogo zilifanyika kwa ajili ya kazi ya umishenari katika nchi za kigeni. Hakuna vyama vipya vilivyoundwa, na ni makanisa machache sana yaliyofanya juhudi ya kueneza Ukristo katika nchi za kipagani. Lakini kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na nane badiliko kubwa lilitokea. Watu walianza kutoridhishwa na matokeo ya kutegemea falsafa ya mantiki peke yake na waligundua umuhimu wa ufunuo wa Mungu na dini halisi. Tangu wakati huu kazi ya umishenari katika nchi za kigeni ilifikia ukuaji uliokuwa haujawahi kufikiwa kabla ya hapo. (Tazama Kiambatanisho.)

Maboresho katika uchapishaji ulitoa msukumo katika kazi ya usambazaji wa Biblia. Ongezeko la miundombinu ya mawasiliano kati ya nchi mbalimbali, kuondolewa kwa vizuizi vya zamani vya chuki na ubaguzi kati ya taifa moja na jingine, na upotezaji wa nguvu za kiserikali za kiongozi mkuu wa Kanisa la Roma vilifungua njia kwa ajili ya neno la Mungu kusambaa. Kwa miaka kadhaa Biblia ilikuwa imeshaanza kuuzwa bila kizuizi katika mitaa ya Roma, na sasa ilianza kupelekwa katika kila eneo linalokaliwa watu ulimwenguni kote

Mkanamungu Voltaire aliwahi kusema kwa majivuno: "Nimechoshwa na watu wanaosema kwa kurudia-rudia kuwa watu kumi na mbili walianzisha dini ya Kikristo. Nitathibitisha kuwa mtu mmoja anatosha kuishinda dini ya Kikristo." Vizazi vingi vimepita tangu kifo chake. Mamilioni ya watu wamejiunga kupigana vita kwa ajili ya Biblia. Lakini

dini ya Kikiristo siyo tu kuwa haijaangamizwa, badala yake mahali ambapo palikuwa na Biblia mia moja wakati wa Voltaire, kuna Biblia elfu kumi sasa, ndiyo, nakala laki moja za kitabu cha Mungu. Katika maneno ya Mwanamatengenezo wa awali kuhusu kanisa la Kikristo, "Biblia ni fuawe ambayo imemaliza nyungo nyingi." Bwana alisema: "Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu" (Isaya 54:17).

"Majani yakauka, ua lanyauka; Bali neno la Mungu wetu litasimama milele." "Matendo ya mikono yake ni kweli na hukumu, Maagizo yake yote ni amini, Yamethibitika milele na milele, Yamefanywa katika kweli na adili" (Isaya 40:8; Zaburi 111:7, 8). Chochote kitakachojengwa juu ya mamlaka ya mwanadamu kitashindwa; lakini cho chote kitakachojengwa juu ya mwamba wa neno la Mungu lisilobadilika kitasimama milele.

Sura ya 16 - Makasisi Wasafiri

Wanamatengenezo wa Uingereza, wakati wakikataa mafundisho ya Kirumi, walibaki na mifumo mingi ya ibada ya Kirumi. Kwa hiyo, ingawa mamlaka na imani ya Kirumi ilikataliwa, siyo desturi na sherehe chache zilizoingizwa katika ibada ya Kanisa la Uingereza. Ilidaiwa kuwa mambo haya hayakuwa masuala ya dhamiri; kuwa ingawa hayakuwa yameagizwa katika Maandiko, wala kukataliwa katika Maandiko, hayakuwa muhimu, kwa hiyo hayakuwa na ubaya wowote. Uadhimishaji wa mambo hayo ulikuwa na mwelekeo wa kupunguza ufa uliotenganisha makanisa yaliyofanya matengenezo na kanisa la Rumi, na ilisisitizwa kuwa mambo yale yangewahamasisha wafuasi wa Rumi kuikubali imani ya Kiprotestanti. Kwa wale waliokuwa na msimamo wa kutopenda mabadiliko na wasioyumbishwa, hoja hizi zilionekana kuwa na nguvu. Lakini kulikuwepo na tabaka jingine ambalo halikuwa na mtazamo wa jinsi hiyo. Ukweli kuwa desturi hizi "zilikuwa na mwelekeo wa kupunguza tofauti kati ya Rumi na Matengenezo" (Martyn, volume 5, ukurasa wa 22), katika mtazamo wao ilikuwa hoja yenye nguvu dhidi ya kubaki nazo.

Waliziona kuwa ni alama za utumwa ambao walikuwa wameachana nao na ambao wasingependa kuurudia tena. Walifikiria kuwa Mungu ameweka katika neno Lake kanuni zinazoongoza ibada Yake, na kuwa watu hawana uhuru wa kuongeza zingine zaidi ya zile zilizopo au kuzipunguza zilizopo. Mwanzo wa uasi mkuu ulikuwa katika kutafuta kuongezea mamlaka ya kanisa kwa mamlaka ya Mungu. Rumi ilianza kwa kuongeza kile ambacho Mungu hakukikataza, na iliishia katika kukataza kile ambacho Mungu alikuwa amekiagiza waziwazi. Wengi walikuwa na shauku ya dhati ya kuurudia usafi na usahili ambao ulikuwa sifa kuu ya kanisa la awali. Walichukulia nyingi za desturi zilizozoeleka za Kanisa la Uingereza kama kumbukumbu za ibada ya sanamu, na wasingeweza kwa sababu ya kufuata dhamiri zao kuungana katika ibada yake. Lakini kanisa, likiungwa mkono na mamlaka ya serikali, lisingengeruhusu kufanya tofauti na desturi zake. Mahudhurio katika huduma zake yalitakiwa kisheria, na mikutano kwa ajili ya ibada za kidini ilipigwa marufuku, na watu waliokiuka sheria hiyo walipaswa kufungwa gerezani, kufukuzwa nchini na kulazimika kwenda kuishi uhamishoni, na kuuawa.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na saba, mfalme ambaye ndiyo tu alikuwa ametawazwa katika kiti cha enzi cha Uingereza, alitangaza azma yake ya kuwafanya wafuasi wa imani ya Wasafi (Waprotestanti waliotaka mila na desturi za Kikatoliki zisiingizwe katika Kanisa la Uingereza) "wakubaliane, au ... waharakishwe kuondoka nchini, au vinginevyo mabaya zaidi yawapate."— George Bancroft, History of the United States of America, pt. 1, ch. 12, par. 6. Wakiwindwa, wakiteswa, na wakifungwa magerezani, Wasafi waligundua kuwa siku zijazo hazikuwa na ahadi ya kuleta hali bora zaidi, na wengi wao walishawishika kuwa ikiwa wanataka kumtumikia Mungu kulingana na msukumo wa dhamiri zao, "Uingereza ilikuwa ikipungua siku kwa siku kuwa mahali salama pa kuishi."—J. G. Palfrey, History of New England, ch. 3, par. 43. Baadhi waliazimia kutafuta hifadhi katika nchi ya Uholanzi. Matatizo,

hasara, na vifungo viliwakuta. Makusudi yao yalizimwa, na walisalitiwa katika mikono ya maadui zao. Lakini msimamo imara usiokatishwa tamaa haimaye ulishinda, na walipata hifadhi katika pwani rafiki za Jamhuri ya Kidachi.

Katika kukimbia kwao Wasafi waliacha nyumba zao, mali zao, na miundombinu yao ya maisha ya kila siku. Walikuwa wageni katika nchi ya kigeni, miongoni mwa watu wa lugha na mila tofauti. Walilazimika kujifunza kazi ambazo ni mpya na ambazo hawakuzizoea ili kupata mkate wao. Watu wa umri wa kati, waliokuwa wametumia maisha yao katika kulima udongo, iliwapasa sasa kujifunza kazi za ufundi. Lakini waliikubali hali hiyo kwa furaha na hawakupoteza muda kwa kukaa kivivu au kulalamika. Pamoja na kuwa walibanwa na umasikini, walimshukuru Mungu kwa mibaraka ambayo bado waliipata na walipata furaha katika ushirika wao wa kiroho usio na usumbufu wowote. "Walijua walikuwa wasafiri, na hawakuangalia sana mambo hayo, bali waliinua macho yao mbinguni, nchi yao nzuri, na roho zao zilitulizwa."—Bancroft, pt. 1, ch. 12, par. 15.

Katikati ya ukimbizi na ugumu, upendo na imani yao viliimarika. Walizitumainia ahadi za Bwana, na Bwana hakuwapungukia wakati wa uhitaji. Malaika wa Bwana walikuwa kando yao, wakiwatia moyo na kuwategemeza. Na mkono wa Mungu ulipoonekana kuwaelekeza wavuke ng'ambo ya bahari, katika nchi ambayo wangeweza kuunda serikali yao wenyewe, na kuwaachia watoto wao urithi wa thamani wa uhuru wa dini, walisonga mbele, bila hofu, katika njia waliyoongozwa na Mungu kuipitia.

Mungu aliruhusu majaribu yawajie watu Wake kuwaandaa kwa ajili ya utekelezaji wa kusudi Lake la neema kwa ajili yao. Kanisa lilikuwa limeshushwa chini, ili liinuliwe juu. Mungu alikuwa karibu kuonesha nguvu Zake kwa ajili ya kanisa, ili kuuonesha ulimwengu ushahidi mwingine kuwa Yeye hawezi kuwatupa watu wanaomtumaini.

Mungu aliongoza matukio na kuifanya hasira ya Shetani na mipango ya watu waovu itangaze utukufu Wake na kuwaleta watu Wake hadi mahali palipo na usalama. Mateso na ukimbizi vilifungua njia ya kuelekea kwenye uhuru.

Walipolazimishwa kwa mara ya kwanza kujitenga na Kanisa la Uingereza, Wasafi waliungana pamoja kwa kiapo makini, kama watu wa Bwana walio huru, "kutembea pamoja katika njia Zake zote ambazo Mungu alikuwa amewafunulia au ambazo angewafunulia."—J. Brown, The Pilgrim Fathers, uk. 74. Hapa kulikuwa na roho ya kweli ya matengenezo, kanuni ya msingi ya Uprotestanti. Ilikuwa kwa ajili ya kusudi hili ambapo Wasafiri waliondoka Uholanzi na kwenda kutafuta makazi katika Ulimwengu Mpya. John Robinson, mchungaji wao, ambaye kwa uongozi wa Mungu alizuiwa asiambatane nao, katika hotuba yake ya kuwaaga wakimbizi alisema:

“Ndugu zangu, sasa tunakaribia kuachana, na Bwana anajua ikiwa nitaishi na kuona nyuso zenu tena au la. Lakini iwe Bwana atawezesha tuonane au ataona ni vema tusionane tena, ninawaagiza mbele za Mungu na malaika Zake waliobarikiwa mnifuate kwa kiwango kile tu ambacho nimemfuata Kristo. Ikiwa Mungu atawafunulia jambo jingine lo lote kwa njia Yake yo yote ile, muwe tayari kulipokea kama vile ambavyo mngepokea ukweli wowote unaotokana na huduma yangu; kwa kuwa nina hakika Bwana anao ukweli na nuru zaidi inayopaswa kugunduliwa katika neno Lake takatifu.”—Martyn 5:70.

“Kwa upande wangu, siwezi kuonesha masikitiko yangu kiasi cha kutosha kwa ajili ya hali ya makanisa yaliyofanya matengenezo, ambao wamefika kikomo katika dini, na hawaendi tena zaidi ya mafundisho ya matengezo yao waliyonayo sasa. Walutheri hawawezi kuvutwa kwenda mbele zaidi ya kile Luther alichokiona; ... na wafuasi wa Clavin, unaona, wanashikilia sana pale walipoachwa na yule mtu wa Mungu, ambaye hata hivyo hakuona mambo yote. Huu ni msiba unaopaswa kuombolezewa; kwa kuwa ingawa walikuwa taa zilizowaka na kuangaza katika wakati wao, lakini hawakupenya na kuingia katika mashauri yote ya neno la Mungu, lakini kama ikiwa wangekuwa hai sasa, wangekuwa tayari kupokea nuru zaidi kama walivyopokea ile ya kwanza.”—D. Neal, History of the Puritans 1:269.

“Kumbukeni agano la kanisa lenu, ambapo mmekubali kutembea katika njia zote za Bwana, ambazo mmejulishwa au ambazo mtajulishwa. Kumbukeni ahadi na agano lenu kwa Mungu na kwa kila mmoja kwa mwenzake, kupokea nuru yo yote na ukweli wowote mtakaojulishwa kutokana na neno Lake lililoandikwa; lakini hata hilo nalo lisikilizeni, ninawasihi sana, mtakachokipokea kama ukweli, mkilinganishe na kukipima na Maandiko mengine ya ukweli kabla ya kukikubali; kwa kuwa haiwezekani kwa ulimwengu wa Kikristo uliotoka hivi karibuni katika giza nene la mpingakristo, lipokee ujuzi mkamilifu wa ukweli wa neno la Mungu kwa mara moja.”—Martyn, vol. 5, pp. 70, 71.

Ilikuwa shauku kwa ajili ya uhuru wa dhamiri iliyowasukuma Wasafiri kustahimili hatari za safari ndefu ya kuvuka ng’ambo ya bahari, kustahimili ugumu na hatari za jangwa, na mbaraka wa Mungu kujenga, kwenye pwani ya Amerika, msingi wa taifa lenye nguvu nyingi sana. Pamoja na kuwa walikuwa watu waaminifu na watu wanaomcha Mungu, Wasafiri bado walikuwa hawajaelewa kanuni kuu ya uhuru wa dini. Uhuru ambao walitoa kafara kubwa sana kuupata, hawakuwa radhi kuwapa wengine. “Wachache sana, hata miongoni mwa watu wenye fikira pevu na waadilifu wa karne ya kumi na saba, waliokuwa na hata wazo dogo la hiyo kanuni kuu, fundisho la Agano Jipya, linalomkiri Mungu kama mhukumu pekee wa imani ya mwanadamu.”—Ibid. 5:297.

Fundisho kuwa Mungu amelipatia kanisa haki ya kutawala dhamiri, kufasili na kuadhibu uzushi, ni moja ya makosa yenye mizizi mirefu ya upapa. Wakati ambapo Wanamatengenezo walikataa imani za Kirumi, haimaanishi hawakuwa na roho ya kukosa uvumilivu kabisa. Giza nene ambalo, kwa zama nyingi za utawala wake, lilifunika ulimwengu wote wa Kikristo,

lilikuwa bado halijaondoka kabisa. Alisema mmoja wa wachungaji mashuhuri katika koloni la Ghuba ya Massachussetts: "Kuvumiliana ndiko kulikoufanya ulimwengu uwe kinyume na Kristo; na kanisa halijawahi kupata madhara yo yote kwa kuwaadhibu wazushi."— Ibid., vol. 5, uk. 335.

Kanuni ilitungwa na wakoloni kuwa washiriki wa kanisa peke yao ndio wawe na sauti katika serikali ya kiraia. Aina fulani ya kanisa la serikali lilianzishwa, watu wote wakitakiwa kuchanga pesa kwa ajili ya kutegemeza wachungaji, na mahakimu wakipewa mamlaka ya kudhibiti uzushi. Kwa njia hiyo nguvu ya serikali ikawa katika mikono ya kanisa. Haukupita muda mrefu kabla hatua hizi hazijaleta matokeo yasiyoepukika—mateso.

Miaka kumi na moja baada ya kuanzisha koloni la kwanza, Roger Williams alikuja katika Ulimwengu Mpya. Kama walivyokuwa Wasafiri wa awali alikuja kwa lengo la kupata uhuru wa dini; lakini, tofauti na wao, aliona—kile ambacho wachache sana wakati wake walikuwa wamekiona— kuwa uhuru huu ulikuwa haki isiyoachanika ya watu wote, bila kujali ni watu wa imani gani. Alikuwa mtafutaji wa dhati wa ukweli, na Robinson akishikilia kuwa ilikuwa jambo lisilowezekana kuwa nuru yote ilikuwa bado haijapokelewa kutoka katika neno la Mungu. Williams "alikuwa mtu wa kwanza katika Ulimwengu mpya wa Ukristo kuanzisha serikali ya kiraia kwa kuzingatia fundisho la uhuru wa dhamiri, usawa wa mawazo mbele ya sheria."—Bancroft, pt. 1, ch. 15, par. 16.

Alisema kuwa ilikuwa wajibu wa hakimu kudhibiti uhalifu, lakini siyo kutawala dhamiri. "Umma au mahakimu wanaweza kuamua," alisema, "nini wajibu wa mtu kwa mtu; lakini wanapojaribu kueleza wajibu wa mtu kwa Mungu, wanatoka nje ya mstari, na haiwezekani kukawa na usalama; kwa sababu ni wazi kuwa ikiwa hakimu anayo mamlaka, anaweza kuamrisha seti moja ya maoni au imani leo na mwingine akatangaza zingine kesho; kama ambavyo imefanyika katika nchi ya Uingereza na wafalme na malkia, na mapapa na mabaraza mbalimbali katika Kanisa la Roma; kiasi kwamba imani zingekuwa mlima wa machafuko."— Martyn, vol. 5, uk. 340.

Kushiriki ibada za kanisa rasmi la serikali ilikuwa lazima na usiposhiriki adhabu yake ilikuwa faini au kifungo. "Williams aliikataa hiyo sheria; sheria mbaya kuliko zote za Uingereza ilikuwa ile iliyowalazimisha watu kuhudhuria katika kanisa la parokia. Alichukulia tendo la kuwalazimisha watu kuungana na watu wa imani tofauti, kuwa ukiukaji wa wazi wa haki za asili; kuwakokota watu wasio na dini na wasiopenda kuabudu, ilionekana kama kuhitaji unafiki. 'Hakuna mtu yeyote anayepaswa kulazimishwa kuabudu, au,' aliongezea, 'kuendelea kuabudu, kinyume na mapenzi yao.' 'Nini!' wapinzani walisema kwa mshangao, 'si mtenda kazi anastahili ujira kwa ajili ya kazi yake?' 'Ndiyo,' alijibu, 'kutoka kwa wale waliomwajiri.'"— Bancroft, pt. 1, ch. 15, par. 2.

Roger Williams aliheshimiwa na kupendwa kama mchungaji mwaminifu, mtu mwenye vipawa ambavyo havipatikani kwa watu wengi, mwenye uadilifu usiopinda na ukarimu wa kweli; hata hivyo upinzani wake usiotetereka dhidi ya haki ya mahakimu ya kuwa na mamlaka juu ya kanisa, na madai yake kwa ajili ya uhuru wa dini, havikuweza kuvumiliwa. Matumizi ya fundisho hili jipya, ilisisitizwa sana, "yangedhoofisha dola ya msingi na serikali ya nchi."— Ibid., pt. 1, ch. 15, par. 10. Alihukumiwa kufukuzwa katika makoloni, na, hatimaye, kuepuka kukamatwa, alilazimika kukimbia, katikati ya baridi na dhoruba ya wakati wa baridi, akatokomea katika msitu ulioshikamana.

"Kwa majuma kumi na nne," alisema, "Niliteseka sana katika msimu mbaya, sikujua mkate au kitanda ni nini." Lakini "kunguru walinilisha nyikani," na mti wenye uwazi ulikuwa ndiyo makazi yangu.—Martyn, vol. 5, uk. 349, 350. Hivyo aliendelea na ukimbizi wake wenye maumivu makali katikati ya theluji na msitu usiokuwa na njia, mpaka alipopata hifadhi kwa kabila la Wahindi ambao walimwamini na kumpenda alipowafundisha ukweli wa injili.

Akifika hatimaye, baada ya miezi mingi ya mabadiliko na mizunguko, kwenye fukwe za Ghuba ya Narragansett, alijenga msingi wa dola ya kwanza ya siku hizi ambayo kwa maana halisi ilitambua haki ya uhuru wa dini. Kanuni ya msingi ya koloni la Roger Williams ilikuwa "kila mtu anatakiwa kuwa na uhuru wa kumwabudu Mungu kulingana na nuru ya dhamiri yake mwenyewe."—Ibid., vol. 5, uk. 354. Jimbo lake dogo hilo, la Rhode Island, lilikuja kuwa hifadhi ya watu walioonewa, na liliongezeka na kufanikiwa mpaka kanuni zake za msingi—za uhuru wa kiraia na wa kidini—zikawa mawe makuu ya pembeni ya Jamhuri ya Amerika.

Katika ile hati kuu ambayo waasisi wa taifa la Marekani waliitangaza kuwa muswada wao wa haki—Tamko la Uhuru—walitangaza: "Tunachukulia kuwa kweli hizi zina ushahidi ulio wazi, kuwa wanadamu wote wameumbwa wakiwa sawa; kwamba wamepewa na Muumbaji wao haki kadhaa zisizoachika; kwamba miongoni mwa hizi haki ni uhai, uhuru, na utafutaji wa furaha." Na Katiba inatoa uhakikisho, katika maana iliyo wazi, wa uhuru wa dhamiri: "Hakuna kigezo cha kidini kitakachotakiwa kama sifa ya kufanya kazi katika ofisi au dhamana ya umma yo yote katika nchi ya Marekani." "Bunge la Kongresi halitatunga sheria yo yote inayohusika na uanzishaji wa dini, au kupiga marufuku watu kujihusisha na dini."

"Waandishi wa Katiba waliitambua kanuni ya milele kuwa uhusiano wa mtu na Mungu wake uko juu ya sheria yo yote ya kibinadamu, na haki zake za dhamiri haziachiki. Mantiki haikuwa ya lazima katika kuelewa uwepo wa huu ukweli; tunatambua uwepo wake katika vifua vyetu. Ni utambuzi huu ambao, katika kushindana kwake na sheria za kibinadamu, umesababisha vifo vya mashahidi wengi kwa njia ya mateso na ndimi za moto. Walihisi kuwa wajibu wao kwa Mungu ulikuwa juu ya maagizo ya wanadamu, na kuwa mwanadamu hakupaswa kuwa na mamlaka juu ya dhamiri zao. Ni kanuni tunayozaliwa nayo ambayo

hakuna kitu cho chote kinaweza kuiondoa."—Congressional documents (U.S.A.), serial No. 200, document No. 271.

Habari zilipoenea katika nchi za Ulaya, kuhusu nchi ambayo kila mtu ana uhuru wa kufurahia matunda ya kazi yake na kutii imani ya dhamiri yake mwenyewe, maelfu walifurika kwenye fukwe na Ulimwengu Mpya. Makoloni yaliongezeka kwa kasi kubwa. "Massachusetts, kwa sheria maalumu, ilitoa ukaribisho na msaada wa bure, kwa gharama za serikali, kwa Wakristo wa taifa lolote ambao wangeruka hadi ng'ambo ya Atlantiki 'kuepuka vita au njaa, au uonevu wa watesaji wao.' Kwa njia hiyo wakimbizi na watu waliodharauliwa, kwa mujibu wa sheria, walifanywa kuwa wageni wa dola."—Martyn, vol. 5, p. 417. Kwa miaka ishirini tangu ujio wa watu wa kwanza kule Plymouth, maelfu kwa maelfu ya Wasafiri walikuja kuishi New England.

Kukidhi lengo lililowaleta, "waliridhika kupata mapato kidogo ya kukidhi kwa kiwango cha chini cha maisha ya kujinyima sana na kufanya kazi za kutoa jasho. Hawakuhitaji chochote kutoka katika ardhi zaidi ya mapato yanayolingana na kazi yao. Hakuna njozi ya dhahabu iliyoonesha utukufu wa uongo kwenye njia yao Waliridhishwa na maendeleo ya pole pole lakini yanayosonga mbele ya umoja wao wa kijamii. Walistahimili kwa uvumilivu umaskini wa nyikani, wakimwagilia mti wa uhuru kwa machozi yao, na kwa jasho la nyuso zao, mpaka ulipostawi kikamilifu katika nchi."

Biblia ilichukuliwa kuwa msingi wa imani yao, chanzo cha hekima, na mwongozo wa uhuru wao. Kanuni zake zilifundishwa kwa bidii katika nyumba, shuleni, na kanisani, na matunda yake yalionekana wazi wazi kwa njia katika kubana matumizi, uwezo mkubwa wa akili, usafi, na kiasi. Mtu angeweza kwa miaka mingi kuishi katika makazi ya Wasafi,"na asione mlevi, au asisikie kiapo, au asikutane na mtu ombaomba."—Bancroft, pt. 1, ch. 19, par. 25. Ilioneshwa kuwa kanuni za Biblia ni ulinzi wa hakika wa ukuu wa taifa. Makoloni yaliyokuwa dhaifu na yaliyotawanyika huko na huko yalikua na kuunda shirikisho la majimbo yenye nguvu, na ulimwengu ulishikwa na butwaa ulipoona amani na mafanikio ya "kanisa lisilokuwa na papa, na dola isiyokuwa na mfalme."

Lakini idadi kubwa ya watu waliendelea kufurika katika fukwe za Amerika, wakisukumwa na mamhitaji mengine tofauti kabisa na ya wale Wasafiri wa kwanza. Ingawa imani ya awali na usafi wa kwanza viliendelea kuwa na mvuto mpana na nguvu inayoumba mwenendo, lakini mvuto wake uliendelea kupungua zaidi na zaidi kwa kadiri idadi ilivyoongezeka ya watu waliokuja kutafuta manufaa ya kidunia.

Kanuni iliyofuatwa na wakoloni wa awali, ya kuruhusu washiriki wa kanisa tu kupiga kura au kushika ofisi katika serikali ya kiraia, ilileta matokeo mabaya. Hatua hii ilikuwa imechukuliwa kama njia ya kuhifadhi usafi wa dola, lakini ilisababisha ufisadi ndani ya kanisa. Kuwa na dini kulipofanywa kigezo cha kuwa na haki ya kupiga kura na kushika ofisi

katika serikali ya kiraia, watu wengi, kwa kusukumwa na hitaji la mafanikio ya kiduni, walijiunga na kanisa bila badiliko la moyo. Hivyo makanisa yalijikuta yamejaa, kwa kiwango kikubwa, watu wasioongoka; na hata miongoni mwa wachungaji walikuwemo siyo tu wale walioshikilia mafundisho yenye makosa, bali pia waliokuwa hawana uzoefu wowote wa nguvu ya Roho Mtakatifu inayoumba upya. Kwa hiyo ilidhihirisha kwa mara nyingine tena matokeo mabaya, yanayoonekana mara nyingi katika historia ya kanisa tangu tangu siku za Konstantini hadi leo, ya kujaribu kujenga kanisa kwa msaada wa dola, wa kuomba nguvu za kidunia katika kutegemeza injili Yake Yeye aliyesema: “Ufalme wangu siyo wa ulimwengu huu” (Yohana 18:36). Muungano wa kanisa la dola, hata kama ungekuwa mdogo sana, wakati unaweza kuonekana kuuleta ulimwengu karibu na kanisa, unaweza katika kiuhalisia kulileta kanisa karibu na ulimwengu.

Kanuni kuu ambayo ilihubiriwa sana na Robinson na Roger Williams, kuwa ukweli ni endelevu, kuwa inawapasa Wakrtisto kuwa tayari kuikubali nuru yote ambayo inaweza kuangaza kutoka katika neno takatifu la Mungu, haikuonwa na watoto na wajukuu wao. Kanisa la Kiprotestanti la Amerika,— na wale wa Ulaya pia,—waliopendelewa sana kwa kupokea mibaraka ya Matengenezo, walishindwa kuendelea mbele katika njia ya matengenezo. Ingawa watu waaminifu wachache waliinuka, wakati mmoja hadi mwingine, wakatangaza ukweli mpya na kufunua makosa yaliyoshikiliwa kwa muda mrefu, wengi wao, sawa na Wayahudi wa wakati wa Kristo au wafuasi wa upapa wa wakati wa Lutha, waliridhika kuamini kama baba zao walivyoamini na waliridhika kuishi kama baba zao walivyoishi.

Kwa hiyo dini kwa mara nyingine tena iliporomoka na kurudi katika hali ya mfumo tu; na makosa na ushirikina ambavyo vilipaswa kuachwa kabisa kama kanisa lingeendelea kutembea katika nuru ya neno la Mungu, vilitunzwa na kustawishwa. Hivyo roho iliyovuviwa na Matengenezo ilipotea, mpaka ikanonekana kwamba kulikuwa na hitaji kubwa la matengenezo katika Makanisa ya Kiprotestanti kama ilivyokuwa katika Kanisa la Roma wakati wa Lutha. Kulikuwa na hali ya kidunia na usingizi mkubwa wa kiroho, aina ile ile ya kuheshimu maoni ya watu, na kuweka nadharia za kibinadamu badala ya mafundisho ya neno la Mungu.

Usambazaji mkubwa wa Biblia katika sehemu ya mwanzo mwa karne ya kumi na tisa, na kwa njia hiyo, nuru kubwa iliyoangazia ulimwengu, haukufuatwa na ukuaji wa maarifa ya ukweli uliofunuliwa, au maisha yaliyobadilishwa na dini. Shetani hakuweza, kama ilivyokuwa katika zama za awali, kuficha neno la Mungu mbali na watu; ilikuwa imewekwa karibu na watu wote na kila mtu angeweza kulipata; lakini ili aweze kutekeleza lengo lake, aliwaongoza wengi kuithamini kidogo sana. Watu walipuuza kuchunguza Maandiko, na kwa njia hiyo waliendelea kukubali tafsiri potovu, na waliendelea kushikilia mafundisho ambayo hayakuwa na msingi katika Biblia.

Baada ya kuona kushindwa kwa juhudi zake za kufutlia mbali ukweli kwa njia ya mateso, Shetani kwa mara nyingine tena alichagua kutumia njia ya ulegezaji masharti ambayo ilisababisha uasi mkuu na uundwaji wa Kanisa la Roma. Aliwashawishi Wakristo waungane wenyewe kwa wenyewe, sasa siyo na upagani, bali na wale ambao, kwa kujiingiza sana katika mambo ya ulimwengu huu, walikuwa wameshakwenda mbali kiasi kwamba walishakuwa waabudu sanamu kweli kweli sawa na wale walioabudu sanamu za kuchonga. Na matokeo ya muungano huu yalikuwa mabaya kama ilivyokuwa katika zama za nyuma; kiburi na ubadhirifu vilijitokeza chini la vazi la dini, na makanisa yalianza kuwa na ufisadi ndani yake. Shetani aliendelea kupotosha mafundisho ya Biblia, na mila na desturi ambazo zingeharibu mamilioni ya watu zilikuwa zikiweka mizizi mirefu. Kanisa lilikuwa likishikilia na kutetea tamaduni hizi, badala ya kushindana kwa ajili "imani ambayo kwanza ilitolewa kwa watakatifu." Kwa njia hiyo kanuni ambazo Wanamatengenezo walizikuza na kuteseka kwazo zilidhalilishwa.

Sura ya 17 - Wajumbe wa Asubuhi

Moja ya vipengele vya ukweli uliofunuliwa katika Biblia ambavyo ni vya muhimu sana na vyenye utukufu mwingi ni kile kinachohusu ujio wa pili wa Kristo anapokuja kumalizia kazi kubwa ya ukombozi. Kwa wasafiri watu wa Mungu, waliokwisha kuondoka muda mrefu uliopita wakaenda katika "nchi na uvuli wa mauti," tumaini lenye baraka, linaloleta furaha limetolewa tena katika ahadi ya kutokea Kwake, Yeye aliye "ufufuo na uzima," "kuwarudisha nyumbani watu Wake waliofukuzwa." Fundisho la ujio wa pili wa Kristo ni ufunguo muhimu wa Maandiko Matakatifu. Tangu siku ile ambayo watu wawili wa kwanza walipogeuza hatua zao za huzuni na kuondoka kutoka katika Bustani ya Edeni, watoto wa imani wameendelea kusubiri ujio wa Yeye Aliyeahidiwa kuvunja nguvu ya mharibifu na kuwarudisha tena katika Paradiso iliyopotea. Watakatifu wa zamani walitazamia ujio wa Masihi katika utukufu, kama kilele cha tumaini lao. Heneko, mtu wa saba katika mfululizo wa ukoo wa wale walioishi katika Bustani ya Edeni, mtu ambaye kwa karne tatu duniani alitembea na Mungu, aliruhusiwa kumwona kutokea mbali Mkombozi anayekuja."Angalia," alisema,"Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote" (Yuda 14, 15).

Mzee Ayubu katika usiku wa mateso yake alisema kwa msisimko na kwa tumaini lisilo na shaka: "Najua ya kuwa Mteteaji wangu yu hai, Na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi…. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, Lakini, pasipokuwa na mwili wangu nitamwona Mungu; Nami nitamwona mimi nafsi yangu, Na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine" (Ayubu 19:25-27). Ujio wa Kristo kuleta utawala wa haki uliwahamasisha waandishi wa Maandiko Matakatifu kuandika maneno mazuri sana na yanayosisimua. Waandishi wa mashairi na manabii wa Biblia waliandika habari ya ujio wa Kristo kwa maneno yanayong'ara kwa moto wa mbinguni.

Mwandishi wa zaburi aliimba kuhusu nguvu na ukuu wa Mfalme wa Israeli: "Tokea Sayuni, ukamilifu wa uzuri, Mungu amemulika. Mungu wetu atakuja wala hatanyamaza. Ataziita mbingu zilizo juu, Na nchi pia awahukumu watu wake" (Zaburi 50:2-4). "Mbingu na zifurahi, nchi na ishangilie, Bahari na ivume na vyote viijazavyo, Mashamba na yashangilie, na vyote vilivyomo, Ndipo miti yote ya mwituni iimbe kwa furaha; Mbele za Bwana, kwa maana anakuja, Kwa maana anakuja aihukumu nchi. Atauhukumu ulimwengu kwa haki, Na mataifa kwa uaminifu wake" (Zaburi 96:11-13).

Alisema nabii Isaya: "Wafu wako wataishi, maiti zangu zitafufuka; amkeni, kaimbeni, ninyi mnaokaa mavumbini, kwa maana umande wako ni kama umande wa mimea, nayo ardhi itawatoa waliokufa.""Amemeza mauti hata milele; na Bwana MUNGU atafuta machozi katika nyuso zote; na aibu ya watu wake ataiondoa katika ulimwengu wote; maana Bwana amenena hayo. Katika siku hiyo watasema, Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, Ndiye

tuliyemngoja atusaidie; Huyu ndiye Bwana tuliyemngoja, Na tushangilie na kuufurahia wokovu wake" (Isaya 26:19; 25:8, 9).

Na Habakuki, akiwa katika njozi takatifu, aliuona ujio Wake. "Mungu alikuja kutoka Temani, Yeye aliye mtakatifu kutoka mlima Parani. Utukufu wake ukazifunika mbingu, Nayo dunia ikajaa sifa yake. Mwangaza wake ulikuwa kama nuru." "Akasimama, akaitetemesha dunia; Akatazama, akawasitusha mataifa; Na milima ya zamani ikatawanyika; Vilima vya kale vikainama; Miendo yake ilikuwa kama siku za kale." "Ukapanda farasi zako, Katika magari yako ya wokovu.""Milima ilikuona, ikaogopa; Gharika ya maji ikapita; Vilindi vikatoa sauti yake, Vikainua juu mikono yake. Jua na mwezi vikasimama makaoni mwao; Mbele ya nuru ya mishale yako ilipotapakaa, Mbele ya mwangaza wa mkuki wako umeremetao." "Ukatokea kwa ajili ya wokovu wa watu wako, Kwa ajili ya wokovu wa masihi wako; Ukakiponda kichwa cha nyumba ya waovu, Ukiuweka wazi msingi hata mwambani" (Habakuki 3:3, 4, 6, 8, 10, 11, 13).

Mwokozi alipokuwa karibu kutengana na wanafunzi Wake, aliwafariji katika huzuni zao kwa kuwahakikishia kuwa angerudi tena: "Msifadhaike mioyoni mwenu. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi. Mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo" (Yohana 14:1-3). "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye," "ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake: na mataifa yote watakusanyika mbele zake" (Mathayo 25:31, 32).

Malaika waliobaki kwenye Mlima wa Mizetuini baada ya Kristo kupaa mbinguni walirudia ahadi ya kurudi kwa Kristo kwa wanafunzi: "Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni" (Matendo 1:11). Na mtume Paulo, akizungumza kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu, alishuhudia: "Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu"(1 Wathesalonike 4:16). Anasema nabii wa Patmo: "Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma" (Ufunuo 1:7).

Ujio wake umezungukwa na habari za ule utukufu wa"kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu" (Matendo 3:21). Ndipo utawala ambao umedumu kwa muda mrefu wa uovu utavunjwa; "Falme za dunia" zimekwisha kuwa "falme za Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele" (Ufunuo 11:15). "Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja." "Ndivyo Bwana MUNGU atakavyootesha haki na sifa mbele ya mataifa yote." Atakuwa "taji ya fahari, na kilemba cha uzuri, kwa mabaki ya watu wake" (Isaya 40:5; 61:11; Isaya 28:5).

Wakati huo ndipo ufalme wa amani wa Masihi uliotamaniwa kwa muda mrefu utakaposimikwa chini ya mbingu yote. “Maana Bwana ameufariji Sayuni; amepafariji mahali pake palipokuwa ukiwa; amefanya jangwa lake kuwa kama bustani ya Edeni, na nyika yake kama bustani ya Bwana.” “Litapewa uzuri wa Lebanoni, utukufu wa Karmeli na Sharoni.” “Hutaitwa tena Aliyeachwa, wala nchi yako haitaitwa tena, Ukiwa; bali utaitwa furaha yangu; na nchi yako Beula.”“Kama vile bwana arusi amfurahiavyo bibi arusi, ndivyo Mungu wako atakavyokufurahia wewe” (Isaya 51:3; 35:2; 62:4, 5).

Ujio wa Bwana umekuwa katika zama zote tumaini la wafuasi Wake wa kweli. Ahadi ya Mwokozi wakati akiwaaga kwenye Mlima wa Mizeituni, kuwa atakuja tena, ilitoa mwangaza kwa mustakabali wa wanafunzi Wake, ukijaza mioyo yao furaha na tumani ambalo huzuni isingeweza kulizima wala majaribu yasingeweza kulihafifisha. Katikati ya mateso na majaribu, “kutokea kwa Mungu wetu mkuu na Mwokozi wetu Yesu Kristo” lilikuwa “tumaini lenye baraka.” Wakristo wa Thesalonike walipojawa na huzuni kwa kuwazika wapendwa wao, waliokuwa wametumaini kuishi na kushuhudia ujio wa Bwana, Paulo mwalimu wao, aliwaeleza juu ya ufufuo, utakaotokea wakati wa ujio wa pili wa Mwokozi. Ndipo waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza, na pamoja na walio hai tutanyakuliwa kumlaki Bwana hewani. “Na hivyo,” alisema, “tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi, farijianeni kwa maneno hayo” (1 Wathesalonike 4:16-18).

Kwenye kisiwa cha miamba cha Patmo mwanafunzi mpendwa alisikia ahadi, “Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam; naja upesi,” na sauti yake yenye shauku inatoa ombi la kanisa katika safari yake yote, “Amina; na uje, Bwana Yesu” (Ufunuo 22:20).

Kutoka katika gereza, nguzo ya kuchomea watu moto, jukwaa la kukatia vichwa vya watu, ambapo watakatifu na wafia dini walishuhudia kwa ajili ya ukweli, inakuja baada ya karne nyingi sauti ya imani na tumaini. Ikiwa “imehakikishiwa juu ya ufufuo Wake binafsi, na hatimaye ufufuo wa kwao wakati wa ujio Wake, kwa ajili ya kazi hiyo,” alisema mmoja wa Wakristo hao, “walidhihaki mauti, na walionekana kuwa juu ya mauti.”—Daniel T. Taylor, The Reign of Christ on Earth: or, The Voice of the Church in All Ages, ukurasa wa 33. Walikuwa tayari kushuka makaburini mwao, ili “wafufuke wakiwa huru.”—Ibid., ukurasa wa 54. Walitarajia kumwona “Bwana akishuka kutoka mbinguni katika mawingu akiwa na utukufu wa Baba Yake,” “kuwaletea wenye haki nyakati za ufalme.”Wawaldensia walikuwa na imani hiyo hiyo.— Ibid., ukurasa wa 129-132. Wycliffe alitazamia kutokea kwa Mkombozi kama tumaini lenye baraka la kanisa.—Ibid., ukurasa wa 132-134.

Luther alisema: “Ninashawika kwa hakika kuwa, siku ya hukumu haiwezi kukosa kuwepo ndani ya miaka mia tatu kamili. Mungu hataweza, hawezi, kuruhusu huu ulimwengu mwovu uendelee kwa muda mrefu zaidi.” “Siku kuu inakaribia ambapo ufalme wa machukizo utapinduliwa.”—Ibid., ukurasa wa 158, 134.

“Ulimwengu huu uliozeeka hauko mbali na mwisho wake,” Melanchthon alisema. Calvin aliwahimiza Wakristo “wasisite-site, wakitarajia kwa shauku kubwa siku ya ujio wa Kristo kama tukio kubwa kuliko matukio mengine yote;” na alitangaza kuwa “familia yote ya waaminifu itadumu kuitazamia siku hiyo.” “Inatupasa kuwa na njaa kwa ajili ya Kristo, inatupasa kutafuta, kutafakari,” alisema, “mpaka kupambazuka kwa siku ile kuu, ambapo Bwana wetu ataonesha kikamilifu utukufu wa ufalme Wake.”—Ibid., ukurasa wa 158, 134.

“Je, sio kuwa Bwana wetu Yesu amepeleka miili yetu mbinguni?” alisema Knox, Mwanamatengenezo wa Scotch, “na si atarudi? Tunajua kuwa atarudi, na tena haraka.” Ridley na Latimer, waliosalimisha maisha yao kwa ajili ya ukweli, walitazamia kwa imani kwa ajili ya ujio wa Bwana. Ridley aliandika: “Ulimwengu usio na mashaka—ninaamini jambo hili, na kwa hiyo ninalisema—unakaribia. Hebu sisi wote pamoja na Yohana, mtumishi wa Mungu, tumlilie katika mioyo yetu Mwokozi wetu Kristo, Njoo, Bwana Yesu, njoo.”—Ibid., ukurasa wa 151, 145.

“Mawazo ya ujio wa Bwana,” alisema Baxter, “ni matamu na yananipa furaha kubwa sana.”—Richard Baxter, Works, vol. 17, uk. 555. “Ni kazi ya imani na tabia ya watakatifu Wake kupenda kutokea Kwake na kulitazamia tumaini lile lenye baraka.” “Ikiwa mauti ni adui atakayeangamizwa wakati wa ufufuo, tunaweza kujifunza jinsi waumini wanavyopaswa kutamani na kuomba kwa ajili ya ujio wa pili wa Kristo, wakati ushindi huu mkamilifu utakapopatikana.”—Ibid., vol. 17, uk. 500. “Hii ni siku ambayo waumini wote wanapaswa kuitamani, kuingoja, kama ukamifu wa kazi yote ya ukombozi wao, na shauku na juhudi zote za roho zao.” “Harakisha, Ee Bwana, siku hii yenye baraka!”—Ibid., vol. 17, uk. 182, 183. Hili ndilo lililokuwa tumaini la kanisa la mitume, la “kanisa nyikani,” na la Wanamatengenezo.

Unabii hauelezi tu namna na kusudi la ujio wa Kristo, bali hueleza pia ishara ambazo kwazo watu watajua kukaribia kwa ujio Wake. Yesu alisema: “Kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota” (Luka 21:25). “Jua litatiwa giza, na mwezi hatautoa mwanga wake. na nyota za mbinguni zitakuwa zikianguka, na nguvu zilizo mbinguni zitatikisika. Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu nyingi na utukufu” (Marko 13:24-26). Mwandishi wa kitabu cha Ufunuo anaeleza ishara za kwanza zinazotangulia Ujio Wake wa Pili: “Palikuwa na tetemeko kuu la nchi; jua likawa jeusi kama gunia la singa, mwezi wote ukawa kama damu” (Ufunuo 6:12).

Ishara hizi zilishuhudiwa kabla ya kuanza kwa karne ya kumi na tisa. Katika utimizo wa unabii huu kulitokea, mwaka 1755, tetemeko la kutisha kuliko yote yaliyowahi kutokea na kuwekwa katika kumbukumbu ya maandishi. Ingawa linajulikana sana kama tetemeko la Lisbon, lilienea na kufika eneo kubwa la Ulaya, Afrika, na Amerika. Lilifika hadi Greenland, katika maeneo ya India ya Magharibi, katika kisiwa cha Madeira, katika nchi za Norwe na Uswidi, Uingereza Kuu na Ireland. Lilighubika kiasi cha eneo lisilopungua maili za mraba

milioni nne. Katika bara la Afrika mtikisiko ulikuwa mkubwa sana kama ulivyokuwa katika bara la Ulaya. Sehemu kubwa ya Algiers iliharibiwa; na umbali mfupi kutoka Morocco, kijiji chenye wakazi kati ya elfu nane na elfu kumi kilimezwa chote. Wimbi kubwa lilifagia pwani ya Uhispania na Afrika na kumeza miji na kusababisha uharibifu mkubwa.

Ilikuwa katika nchi za Uhispania na Ureno ambapo mtikisiko ulisababisha uharibifu mkubwa kuliko maeneo mengine yote. Katika maeneo ya Cadiz wimbi lililopitia hapo lilikuwa limeinuka kwa takribani futi sitini kwenda juu. Milima, "mirefu sana katika nchi ya Ureno, ilitikiswa sana, kama ilivyopaswa kuwa, kuanzia kwenye misingi hasa, na baadhi yake ilifunguka kwenye vilele vyake, iliyopasuka na kuachana kwa namna ya ajabu sana, mabonge makubwa ya vipande vyake yakitupwa chini katika mabonde yaliyo karibu. Ndimi za moto zilitoka katika mipasuko hiyo."— Sir Charles Lyell, Principles of Geology, ukurasa 495.

Katika jiji la Lisbon "sauti ya radi ilisikika chini ya ardhi, na muda mfupi baadaye mtikisiko mkubwa sana uliangusha chini sehemu kubwa ya jiji lile. Katika kipindi cha takribani dakika sita watu sitini elfu waliangamia. Bahari ilirudi nyuma kwanza, na kuicha sakafu ya bahari ikiwa kavu; halafu bahari ilirudi, maji yake yakiwa yameinuka kwa kiasi cha futi hamsini au zaidi juu ya usawa wake wa kawaida." "Miongoni mwa matukio mengine ambayo hayakuwa ya kawaida yaliyosimuliwa kuwa yalitokea katika jiji la Lisbon wakati wa janga hilo, ilikuwa kuzama kwa gati mpya, iliyojengwa kwa marumaru tupu, kwa gharama kubwa. Kundi kubwa la watu lilikuwa limejikusanya pale kwa ajili ya usalama, kama sehemu ambayo wangeweza kuwa mbali na majengo yaliyokuwa yakianguka chini; lakini muda mfupi gati lilianza kuzama chini na watu wate waliokuwa juu yake, na hakuna mwili hata mmoja wa waliokufa ulioelea juu ya uso wa bahari."—Ibid., ukurasa wa 495.

"Mtikisiko" uliosababishwa na tetemeko "ulifuatiwa ghafla na anguko la kila kanisa na kila nyumba ya watawa, karibu majengo makubwa yote ya serikali, na zaidi ya robo ya nyumba zote za makazi ya watu. Kama saa mbili baada ya mtikisiko, moto ulilipuka katika maeneo mbali mbali, na moto uliwaka kwa ukali mwingi kwa muda wa karibu siku tatu mfululizo, kiasi kwamba jiji lote liliteketezwa kabisa. Tetemeko lilitokea siku takatifu, wakati makanisa na nyumba za watawa zilipokuwa zimejaa watu, ni watu wachache sana waliookoka."—Encyclopedia Americana, art. "Lisbon," note (ed. 1831).

"Hofu ya watu isingeweza kuelezeka. Hakuna mtu aliyelia na kutoa machozi; tukio lile lilitisha mno kiasi kwamba hakuna aliyeweza kutoa machozi. Watu walikimbia huko na huko, wakiwa wamechanganyikiwa kwa ajili ya hofu, wakipiga-piga nyuso zao na vifua vyao, wakipiga kelele, 'Tuhurumie! Ulimwengu umekwisha!' Akina mama waliwasahau watoto wao, na kukikimbia huku na huko wakiwa wamevaa sanamu za Yesu akiwa amewambwa msalabani. Kwa bahati mbaya, wengi walikimbilia makanisani ili kupata ulinzi; lakini hawakupata msaada wowote na ibada za sakramenti ziliumbuka; viumbe hawa maskini walijaribu kukamata mimbari; sanamu, mapadri, na watu wote walizikwa pamoja katika

maangamizi ya pamoja." Imekadiriwa kuwa watu wapatao tisini elfu walipoteza maisha yao siku ile ya maangamizi.

Miaka ishirini na tano baadaye ilitokea ishara ya pili iliyotajwa katika unabii—kutiwa giza kwa jua na mwenzi. Kilichoshangaza kuhusu ishara hii ilikuwa ukweli kuwa wakati wa kutimizwa kwake ulibainishwa waziwazi. Katika maongezi ya Mwokozi na wanafunzi Wake juu ya mlima wa Mizeituni, baada ya kuelezea kipindi kirefu cha kujaribiwa kwa kanisa,— miaka 1260 ya mateso ya upapa, ambacho aliahidi kuwa mateso yatafupishwa,— alitaja matukio kadhaa ambayo yatatangulia ujio Wake, na aliweka wakati maalumu ambapo moja ya ishara hizi ingeshuhudiwa: "Lakini siku zile, baada ya dhiki hiyo, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake" (Marko 13:24). Siku 1260, au miaka 1260, iliishia mwaka 1798. Robo ya karne kabla, mateso yalikuwa yamekwisha kwa kiwango kikubwa. Baada ya mateso haya, kwa mujibu wa maneno ya Kristo, jua lilipaswa kutiwa giza. Siku ya tarehe 19 Mei 1780, unabii huu ulitimizwa.

"Karibu, kama siyo tukio la pekee kabisa, laweza kuwa tukio ambalo ni siri kubwa kuliko yote na ambalo halina maelezo,…ni siku hii ya giza ya Mei 19, 1780,—la kutiwa giza la ajabu na lisiloelezeka la mbingu na angahewa katika Uingereza Mpya." R. M. Devens, Our First Century, ukurasa wa 89.

Shuhuda wa tukio hili aliyeishi katika mji wa Massachusetts anaelezea tukio kama ifuatavyo: "Asubuhi jua lilichomoza likiwa safi, lakini ghafla lilifunikwa. Mawingu yaliteremka chini na kuwa karibu na ardhi, na kutoka katika mawingu hayo, ambayo yalikuwa meusi na ya kutisha, kama yalivyokuja kuonekana muda mfupi uliofuata, radi ilimulika, ngurumo za radi zikarindima, na mvua ya rasha-rasha ilinyesha. Kuelekea saa tatu asubuhi, mawingu yalipungua, na rangi yake iligeuka na kuwa ya shaba katika mwonekano wake, na ardhi, miamba, miti, majengo, maji, na watu walibadilishwa na mwanga huu wa ajabu, usiokuwa wa dunia hii. Dakika chache baadaye, wingu jeusi lilitanda kote angani isipokuwa tu ukingo mwembamba katika upeo wa macho, na kulikuwa na giza ambalo kwa kawaida hutokea saa tatu usiku muda wa jioni wa wakati wa joto....

"Hofu, wasiwasi, na kicho, pole pole vilianza kujaza akili za watu. Wanawake walisimama milangoni, wakiangalia nje gizani; wanaume walirudi nyumbani kutoka mashambani; seremala aliacha zana zake, mhunzi aliacha karakana yake yenye kalibu, mfanya biashara aliacha kaunta yake. Shule zilifungwa, na wanafunzi walikimbia wakitetemeka kuelekea nyumbani. Wasafiri walikatisha safari zao na kutafuta hifadhi katika nyumba zilizokuwa karibu yao. 'Ni nini kinakuja?' kila mdomo na kila moyo uliuliza. Ilionekana kana kwamba kimbunga kilikuwa karibu kupita katika nchi, au kana kwamba ilikuwa siku ya kilele cha mambo yote.

“Mishumaa ilitumika; na mioto ya nyumbani ilitoa mwanga mkali kama unavyooenekana katika usiku usiokuwa na mbalamwezi wakati wa majira ya kupukutika kwa majani. Kuku walirudi katika vibanda vyao na kusinzia, ng’ombe walirudi katika mazizi yao na kulala, vyura walitoa macho, ndege waliimba nyimbo zao za jioni, na popo waliruka-ruka huku na huko. Lakini mwanadamu alijua kuwa usiku ulikuwa bado haujawadia....

“Dkt. Nathanael Whittaker, mchungaji wa kanisa la Tabernacle katika mji wa Salem, aliendesha huduma za kidini katika nyumba ya mikutano, na alitoa hubiri ambapo alidai kuwa giza lile halikuwa la kawaida. Waumini walikusanyika makanisani katika sehemu zingine mbalimbali pia. Mafungu ya Biblia kwa ajili ya mahubiri ambayo hayakuandaliwa kwa namna tofauti tofauti yalikuwa yale yaliyoelekea kuonesha kuwa giza lile lilipatana na unabii wa Maandiko Giza liliongezeka katika uzito mara tu baada ya saa tano asubuhi.”—The Essex Antiquarian, April, 1899, vol. 3, No. 4, uk. 53, 54. “Katika maeneo mengi ya nchi giza lilikuwa nene kiasi kwamba watu wasingeweza kujua wakati kwa kutazama saa ya mkononi au ya ukutani, wala wasingeweza kula chakula, wala kufanya shughuli zao za nyumbani, bila mwanga wa mishumaa....

“Kiasi cha giza hili kilikuwa siyo cha kawaida. Giza hili lilionekana hadi mashariki sehemu za Falmouth. Upande wa magharibi lilifika sehemu ya mbali ya Connecticut, hadi Albany. Upande wa kusini, lilionekana katika fukwe za bahari; na kuelekea upande wa kaskazini giza lilifunika eneo lote la makazi ya watu wa Amerika.”—William Gordon, History of the Rise, Progress, and Establishment of the Independence of the U.S.A., vol. 3, uk. 57.

Giza nene la mchana lilifuatiwa, saa moja au mbili kabla ya jioni, na anga lisilokuwa na mawingu, na jua lilitokea na kuonekana, ingawa lilikuwa bado limefunikwa na ukungu mzito na mweusi. “Baada ya jua kuzama, mawingu yalirudi tena juu, na giza likaingia kwa muda mfupi sana.” “Wala siyo kweli kuwa giza la usiku lilikuwa la kawaida bali lilikuwa nene na lilitisha zaidi kuliko hata lile la mchana; pamoja na hayo kulikuwa na mbalamwezi iliyokuwa karibu kukomaa, na hakuna kitu chochote kilichoweza kutambuliwa bila msaada wa mwanga wa mshumaa au chanzo kingine kilichotengenezwa na mwanadamu, ambao, ulipoonekana kutokea kwa nyumba za jirani na kwingineko kote ambako ni mbali, ulionekana kupitia katika giza la Kimisri ambalo lilionekana kama lisiloweza kupenywa na miale ya nuru.”—Isaiah Thomas, Massachusetts Spy; or, American Oracle of Liberty, vol. 10, No. 472 (Mei 25, 1780).

Mtu aliyeshuhudia tukio alisema: “Nilishindwa kujizuia kuelewa wakati huo, kuwa ikiwa kila kitu chenye uwezo wa kutoa mwanga katika ulimwengu kilikuwa kimefunikwa na kivuli kisichoweza kupenywa, au kisichoweza kuondosheka, giza lisingeweza kuwa kamilifu zaidi ya pale.”— Letter by Dr. Samuel Tenney, of Exeter, New Hampshire, December, 1785 (in Massachusetts Historical Society Collections, 1792, 1st series, vol. 1, uk. 97). Ingawa ilipofika saa tatu ya usiku ule mwezi ulionekana vizuri kabisa, “haukuweza kuondoa hata

kidogo vivuli vya hofu ya kifo." Baada ya saa sita usiku giza lilitoweka, na mwezi, ulipoonekana kwa mara ya kwanza, ulikuwa na mwonekano wa damu.

Mei 19, 1780, inasimama katika historia kama "Siku ya Giza." Tangu wakati wa Musa hakuna kipindi kilichokuwa na giza lenye uzito, kiwango, na muda kama huo, lililowahi kuandikwa katika kumbukumbu. Maelezo ya tukio hili, kama yalivyotolewa na shuhuda aliyeona tukio, lilikuwa mwangwi wa maneno ya Bwana, yaliyoandikwa na nabii Yoeli, miaka elfu mbili na mia tano iliyopita kabla ya kutimizwa kwake: "Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja hiyo siku ya Bwana iliyo kuu na itishayo" (Yoeli 2:31).

Kristo aliwaeleza watu Wake waangalie ishara za ujio Wake na kufurahi kwa kuona viashiria vya ujio wa Mfalme wao. "Basi mambo hayo yaanzapo kutokea," alisema, "changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia." Aliwaonesha wafuasi Wake miti iliyokuwa ikichipuka, na kusema: "Wakati iishapo kuchipuka, mwaona na kutambua wenyewe ya kwamba majira ya mavuno yamekwisha kuwa karibu. Nanyi kadhalika, mwonapo mambo hayo yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu" (Luka 21:28, 30, 31).

Lakini kwa kuwa roho ya unyenyekevu na uaminifu ilikuwa imetoweka kanisani na badala yake kanisa likaingiwa na kiburi na ibada ya kimtindo, upendo kwa Kristo na imani Kwake ulikuwa umepoa. Kwa sababu ya kuipenda dunia na anasa, watu waliodai kuwa wa Mungu walipofushwa hata wakashindwa kukumbuka mafundisho ya Yesu kuhusu ishara za ujio Wake. Fundisho la ujio wa pili lilipuuzwa; mafundisho yanayolihusu yalifichwa na tafsiri potovu, hadi, kwa sehemu kubwa, likapuuzwa na kusahauliwa. Hususani ilikuwa hivyo katika makanisa ya Amerika. Uhuru na raha ambayo matabaka yote ya jamii waliipata, tamaa kubwa ya mali na anasa, iliyozaa matumizi ya muda mwingi katika kutafuta pesa, kukimbilia kutafuta umaarufu na madaraka, mambo ambayo yalionekana kuwa na uwezekano wa kupatikana kwa watu wote, viliwafanya watu kuelekeza nguvu zao na matumaini yao kwa vitu vya ulimwengu huu, na kusukumia mbali katika wakati ujao ile siku kuu ambayo utaratibu wa sasa wa mambo utatoweka.

Mwokozi alipowaeleza wafuasi Wake kuhusu ishara za kurudi Kwake, alitabiri hali ya kurudi nyuma itakayokuwepo muda mfupi kabla ya ujio Wake wa pili. Kungewepo, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, shughuli na pilika pilika za mambo ya kidunia na utafutaji wa anasa—kununua, kuuza, kupanda, kujenga, kuoa, na kuolewa—pamoja na kumsahau Mungu na maisha yajayo. Kwa watu wanaoishi wakati huu, maelekezo ya Kristo ni: "Basi, jiangalieni, mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi, na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafula, kama mtego unasavyo." "Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu" (Luka 21:34, 36).

Hali ya kanisa wakati huu imeelezwa katika maneno ya Mwokozi katika kitabu cha Ufunuo: "Una jina la kuwa hai, nawe umekufa. Basi kumbuka jinsi ulivyopokea, na jinsi ulivyosikia." Na wanaokataa kuamka kutoka usingizi wa usalama wa kujidanganya, onyo kali linatolewa: "Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako"(Ufunuo 3:1, 3). Ilikuwa muhimu watu waamshwe na kujulishwa hatari iliyowakabili; kuwa walipaswa wamshwe ili wajiandae kukabiliana na matukio makubwa yanayoshikamana na kufungwa kwa mlango wa rehema. Nabii wa Mungu anatangaza: "Kwa kuwa siku ya Bwana ni kuu, yenye kitisho sana; naye ni nani awezaye kuistahimili?" Ni nani awezaye kusimama wakati Yeye aliye "na macho safi hata usiweze kuangalia uovu," na hawezi "kutazama ukaidi"? (Yoeli 2:11; Habakuki 1:13).

Kwa watu wanaolia wakisema, "Mungu wangu, sisi Israeli tunakujua," lakini "wamelihalifu agano langu, wameiasi sheria yangu," na wameharakisha kumfuata mungu mwingine, huku wakiwa wameficha uovu katika mioyo yao, na wakipenda njia za uasi—kwa watu hawa siku ya Bwana ni"giza, wala si nuru? Naam, yenye giza sana, wala haina mwanga" (Hosea 8:2, 1; Zaburi 16:4; Amosi 5:20). "Kisha itakuwa wakati ule," asema Bwana, "nitauchunguza Yerusalemu kwa taa, nami nitawaadhibu watu walioganda juu ya sira zao: wasemao katika mioyo yao, Bwana hatatenda mema, wala hatatenda mabaya" (Sefania 1:12). "Nami nitaadhibu ulimwengu kwa sababu ya ubaya wake, na wenye dhambi kwa sababu ya hatia yao; nami nitaikomesha fahari yao wenye kiburi; nami nitayaangusha chini majivuno yao walio wakali" (Isaya 13:11). "Fedha yao wala dhahabu yao havitaweza kuwaokoa;" "utajiri wao utakuwa mateka, na nyumba zao zitakuwa ukiwa" (Sefania 1:18, 13).

Nabii Yeremia, akiangalia mbele hadi wakati huu wa kutisha, alisema: "Naumwa katika moyo wangu wa ndani; …. siwezi kunyamaza; kwa sababu umesikia, Ee nafsi yangu, sauti ya tarumbeta, mshindo wa vita" (Yeremia 4:19, 20).

"Siku ile ni siku ya ghadhabu, Siku ya fadhaa na dhiki, Siku ya uharibifu na ukiwa, Siku ya giza na utusitusi, Siku ya mawingu na giza kuu, Siku ya tarumbeta na ya kamsa" (Sefania 1:15, 16). "Tazama, siku ya Bwana inakuja,…. ili iifanye nchi kuwa ukiwa, na kuwaharibu watu wake, wenye dhambi, wasikae ndani yake" (Isaya 13:9).

Katika muktadha wa siku ile kuu, neno la Mungu, katika lugha makini na yenye mguso, anawaita watu Wake waamke kutoka katika usingizi wao wa kiroho na kutafuta uso Wake katika hali ya toba na unyenyekevu: "Pigeni tarumbeta katika Sayuni, Pigeni na kelele katika mlima wangu mtakatifu; Wenyeji wote wa nchi na watetemeke; Kwa maana siku ya Bwana inakuja. Kwa sababu inakaribia." "Takaseni saumu, kusanyeni kusanyiko kuu; Kusanyeni watu, litakaseni kusanyiko, Kusanyeni wazee, kusanyeni watoto,...; Bwana arusi na atoke chumbani mwake, Na bibi arusi katika hema yake. Hao makuhani, wahudumu wa Bwana, na walie Kati ya patakatifu na madhabahu." "Nirudieni mimi kwa mioyo yenu yote, na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuombolea; rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu,

mkamrudie Bwana, Mungu wenu; kwa maana yeye ndiye mwenye neema, amejaa huruma; si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa rehema, naye hughairi mabaya" (Yoeli 2:1, 15-17, 12, 13).

Kuwaandaa watu kusimama katika siku ya Mungu, kazi kubwa ya matengenezo inapaswa kufanyika. Mungu aliona kuwa wengi wa watu wanaodai kuwa ni watu Wake walikuwa hawajengi kwa ajili ya umilele, na katika rehema Yake alikuwa karibu kutuma ujumbe wa onyo wa kuwaamsha watoke katika hali yao kuzubaa na kuwaongoza katika maandalizi ya ujio wa Bwana.

Onyo hili limetolewa katika Ufunuo 14. Hapa kuna ujumbe wenye sehemu tatu unaowakilishwa na kutangazwa na malaika wa mbinguni na kufuatiwa kwa haraka na ujio wa Mwana wa Adamu kukusanya "mavuno ya nchi." Onyo la kwanza, miongoni mwa maonyo haya, linatangaza hukumu inayokaribia. Nabii alimwona malaika akiruka "katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji" (Ufunuo 14:6, 7). Ujumbe huu unaelezwa kuwa sehemu ya "injii ya milele."

Kazi ya kuihubiri injili haijawekwa katika mikono ya malaika, bali imewekwa kama dhamana katika mikono ya wanadamu. Malaika watakatifu wanatumika katika kuelekeza kazi hii, wanasimama harakati zote kubwa kwa ajili ya wokovu wa wanadamu; lakini utangazaji halisi wa injili hufanywa na watumishi wa Kristo duniani.

Watu waaminifu, ambao walitii misukumo ya Roho wa Mungu na mafundisho ya neno Lake, walipaswa kutangaza onyo hili kwa ulimwengu. Watu hawa ni wale waliosikia"neno la unabii lililo imara zaidi," ambalo ni"taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu" (2 Petro 1:19). Walikuwa wakitafuta kumjua Mungu zaidi kuliko hazina zote zilizositirika, wakiamini kuwa kumjua Mungu ni "bora kuliko biashara ya fedha, Na faida yake ni nyingi kuliko dhahabu safi" (Mithali 3:14). Na Bwana aliwafunulia mambo makuu ya ufalme. "Siri ya Bwana iko kwao wamchao, Naye atawajulisha agano lake" (Zaburi 25:14).

Siyo wanateolojia wasomi ambao walikuwa na ufahamu wa huu ukweli, naambaowalijihusishakatikautangazajiwake. Ikiwawatuhawawangekuwa walinzi waaminifu na wenye kukesha, wakiyachunguza Maandiko kwa bidii kubwa na maombi mengi, wangeweza kuujua wakati wa usiku; unabii ungeweza kuwafunulia matukio yanayokuja karibuni. Lakini hawakufanya hivyo, na ujumbe ulitolewa na watu walio wa kawaida kabisa. Yesu alisema: "Enendeni maadamu mnayo nuru hiyo, giza lisije likawaweza; maana aendaye gizani hajui aendako" (Yohana 12:35). Watu wanaoiacha nuru ambayo Mungu amewapa, au wanaopuuza kuitafuta wakati inapatikana kwa ajili yao, wataachwa gizani. Lakini Mwokozi

alisema: “Yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima” (Yohana 8:12). Yeyote aliye na kusudi moja tu la kutafuta kutenda mapenzi ya Mungu, akiifuata kwa bidii nuru aliyonayo tayari, atapokea nuru kubwa zaidi; kwa mtu kama huyo nyota ya nuru ya mbinguni itatumwa kumwongoza katika ukweli wote.

Wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo makuhani na waandishi wa Mji Mtakatifu, ambao walikuwa wamepewa dhamana ya maagizo ya Mungu, walipaswa kuzijua dalili za nyakati na kutangaza ujio wa Yule aliyekuwa ameahidiwa. Unabii wa Mika ulitangaza mahali ambapo angezaliwa; Danieli alisema wakati mahsusi wa ujio Wake (Mika 5:2; Danieli 9:25). Mungu alikabidhi unabii huu kwa viongozi wa Kiyahudi; hawakuwa na udhuru wa kutojua na kutangaza kwa watu kuwa ujio wa Masihi ulikuwa karibu. Kutokujua kwao kulikuwa matokeo ya dhambi ya kupuuzia. Wayahudi walikuwa wakijenga minara ya kumbukumbu kwa ajili ya manabii wa Mungu waliouawa, ilhali kwa kutoa heshima yao kwa watu mashuhuri walikuwa wakitoa heshima kwa watumishi wa Shetani. Wakiwa wamezama katika mapambano na tamaa zao kwa ajili ya vyeo na mamlaka miongoni mwa watu, walishindwa kutambua fadhila waliyopewa na Mungu, Mfalme wa mbinguni.

Kwa shauku na kicho kikubwa wazee wa Israeli walipaswa kujifunza na kuelewa mahali, wakati, na muktadha, wa tukio kubwa kuliko matukio yote katika historia ya ulimwengu—ujio wa Mwana wa Mungu kutekeleza ukombozi wa mwanadamu. Watu wote walipaswa kukesha na kungojea ili wawe miongoni mwa watu wa kwanza kumpokea Mkombozi wa ulimwengu. Lakini, kumbe, katika mji wa Bethlehemu wasafiri wawili waliochoka kutoka katika milima ya Nazarethi walitembea urefu wote wa mtaa mwembamba hadi mwisho wa mji upande wa mashariki, wakitafuta bila mafanikio mahali pa kupumzika na kujihifadhi wakati wa usiku. Hakuna milango iliyokuwa tayari kuwapokea. Hatimaye walipata hifadhi katika banda bovu la ng’ombe, na Mwokozi wa ulimwengu alizaliwa humo.

Malaika wa mbinguni walikuwa wameuona utukufu ambao Mwana wa Mungu alishiriki na Baba Yake kabla ulimwengu haujakuwepo, na walitarajia kwa shauku kubwa kuwa kuonekana Kwake duniani kungekuwa tukio ambalo lingeleta furaha kubwa kwa watu wote. Malaika walichaguliwa kupeleka habari ya furaha kwa wale waliokuwa tayari kuipokea na ambao kwa furaha wangeitangaza kwa wakazi wa dunia. Kristo alikuwa amejishusha ili kuchukua asili ya mwanadamu; alipaswa kubeba uzito usio na kikomo wa taabu kwa kutoa nafsi Yake kuwa sadaka kwa ajili ya dhambi; lakini malaika walitamani kuwa hata katika unyenyekevu Wake, Mwana wa Yeye Aliye Juu Sana atokee mbele ya wanadamu akiwa na angalau heshima na utukufu unaolingana na hadhi Yake. Je, wakuu wa dunia wangeweza kukusanyika katika makao makuu ya Israeli kusubiri ujio Wake? Je, majeshi ya malaika wangemtambulisha kwa mkutano mkubwa wa watu walio na shauku ya kumwona?

Malaika alitembelea dunia kuona watu ambao walikuwa wamejiandaa kumpokea Yesu. Lakini hakuona viashiria vya maandalizi ya kumpokea. Hakusikia sauti ya sifa na shangwe

kwa sababu ya kukaribia kwa ujio wa Masihi. Malaika anasimama kwa muda juu ya mji mteule na hekalu ambapo uwepo mtakatifu wa Mungu ulikuwa ukidhihirika kwa zama nyingi; lakini hata hapa kuna kutojali kule kule. Makuhani, katika majivuno na kiburi, walikuwa wakitoa kafara zilizo najisi hekaluni. Mafarisayo walikuwa wakiwahutubia watu kwa sauti kubwa au wakiomba sala za kujisifu katika kona za mitaa. Katika ikulu za wafalme, katika mikutano ya wanafalsafa, katika shule za marabi, wote hawakuwa na wazo lo lote kuhusu ukweli wa ajabu ambao ulikuwa umejaza mbingu kwa furaha na sifa—kuwa Mkombozi wa wanadamu alikuwa karibu kutokea duniani.

Hakukuwa na ushahidi wowote kuwa Kristo alitarajiwa, na hakukuwa na matayarisho kwa ajili ya Mkuu wa uzima. Kwa mshangao, mjumbe wa mbinguni alikuwa karibu kurudi mbinguni akiwa na taarifa ya kuaibisha, wakati anapogundua kundi la wachungaji ambao walikuwa wakichunga makundi yao ya kondoo usiku, na, wakiangalia katika mbingu yenye nyota, wakitafakari unabii wa Masihi aliyetarajia kuja duniani, na wakitamani ujio wa Mkombozi wa ulimwengu. Pale palikuwa na kundi la watu ambao walikuwa wakijiandaa kupokea ujumbe wa mbinguni. Na kwa ghafla malaika wa Bwana aliwatokea, akitangaza habari njema yenye furaha kubwa. Utukufu wa mbinguni ulifurika pande zote za uwanda, kundi la malaika wasio na idadi lilifunuliwa, na kana kwamba furaha ilikuwa kubwa mno kiasi kwamba isingeweza kufaa kuletwa na mjumbe mmoja kutoka mbinguni, sauti nyingi zinapasuka na kuwa wimbo ambao mataifa yote ya waliookolewa watauimba: “Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia” (Luka 2:14).

Ndiyo, kisa hiki cha Bethlehemu ni somo muhimu kiasi gani! Ni kwa uzito kiasi gani hukemea kukosa imani kwetu, kiburi chetu na kujitosheleza kwetu. Kisa hiki kinatuonya kwa umakini mkubwa kiasi gani ili tukeshe, isije ikawa, kwa kutojali kwetu ambako ni haramu tushindwe kutambua dalili za nyakati, na hivyo tushindwe kujua siku ya kujiliwa kwetu.

Ilikuwa siyo tu juu ya milima ya Yuda, siyo tu miongoni mwa wachungaji maskini peke yao, ambapo malaika waliwakuta wakeshaji kwa ajili ya ujio wa Masihi. Katika nchi za kipagani pia walikuwepo watu waliosubiri ujio Wake; walikuwa watu wenye hekima, matajiri, na waungwana, wanafalsafa wa Mashariki. Wanafunzi wa vitu vya asili, Mamajusi walimwona Mungu katika kazi za mikono Yake. Kutoka katika Maandiko ya Kiebrania walikuwa wamejifunza juu ya Nyota ambayo ingeinuka kutoka katika ukoo wa Yakobo, na wakiwa na shauku kubwa walisubiri ujio Wake, ambaye angekuwa siyo tu “Faraja ya Israeli,” lakini pia “Nuru ya kuwaangazia Mataifa,” na “kwa ajili ya wokovu wa miisho ya dunia” (Luka 2:25, 32; Matendo 13:47).

Walikuwa watu waliotafuta nuru, na nuru kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu iliangazia njia kwa ajili ya nyayo zao. Wakati makuhani na marabi wa Yerusalemu, watunzaji na wafafanuzi wa ukweli waliochaguliwa na Mungu, walikuwa wamegubikwa katika giza,

nyota iliyotumwa na Mbingu iliwaongoza hawa wageni kutoka katika Mataifa tofauti na taifa la Kiyahudi hadi mahali alipozaliwa Mfalme aliyekuwa amezaliwa punde.

Ni “kwa hao wamtazamiao” ambao Kristo “atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa wokovu” (Waebrania 9:28). Kama vile habari ya kuzaliwa kwa Mwokozi ilivyokuwa, ujumbe wa ujio wa pili haukuwekwa mikononi mwa viongozi wa kidini wa watu. Walishindwa kudumisha uhusiano wao na Mungu, na walikataa nuru kutoka mbinguni; kwa hiyo hawakuwa sehemu ya watu wanaoelezwa na mtume Paulo: “Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza” (1 Wathesalonike 5:4, 5).

Walinzi juu ya kuta za Sayuni walipaswa kuwa watu wa kwanza kudaka habari za kwanza za ujio wa Mwokozi, wa kwanza kuinua sauti zao kutangaza ukaribu Wake, wa kwanza kuwaonya watu wajiandae kwa ajili ya ujio Wake. Lakini walikuwa wamebweteka, wakiota amani na usalama, wakati walikuwa wamelala usingizi katika dhambi zao. Yesu aliliona kanisa Lake, kama mtini usiozaa matunda, ukiwa umefunikwa na majani ya kujifanya, lakini bila matunda ya thamani. Kulikuwepo uzingatiaji wa mifumo ya kidini, wakati roho ya unyenyekevu, toba, na imani ya kweli—ambayo ndiyo pekee ingekuwa ibada inayokubalika kwa Mungu—havikuwepo. Badala ya neema za Roho vilionekana kiburi, taratibu za kujirudia za kidini, kujisifu, ubinafsi, na ukandamizaji. Kanisa lililokuwa likirudi nyuma lilifumba macho yake lisione dalili za nyakati. Mungu hakuwaacha, au kuruhusu watu wake waaminifu washindwe; lakini walimwacha, na walijitenga na upendo Wake.

Kwa kukataa kutii masharti, ahadi za Mungu hazikutimizwa. Haya ndiyo matokeo ya hakika ya kutokuona umuhimu wa kuboresha nuru na fursa ambazo Mungu anazozitoa. Kanisa lisipofuatilia milango ya uongozi Wake, likipokea kila mwale wa nuru, likitekeleza kila wajibu ambao unafunuliwa kwao, dini itadidimia na kurudi katika uzingatiaji wa mambo ya kurudia-rudia, na roho ya uchaji wa kweli itaondoka. Ukweli huu umedhihirishwa kwa kurudia – rudia katika historia ya kanisa. Mungu anataka kutoka kwa watu Wake kazi za imani na utii unaolingana na mibaraka na fursa zilizotolewa. Utii unahitaji kafara na unahusisha msalaba; na hii ndiyo sababu wengi wa wafuasi wa Kristo walikataa kupokea nuru kutoka mbinguni, na, kama ilivyokuwa kwa Wayahudi wa zamani, hawakujua wakati wa kujiliwa kwao (Luka 19:44). Kwa sababu ya kiburi chao na kutokuamini kwao Bwana aliwapita na kufunua ukweli kwa wale ambao, kama wachungaji wa Bethlehemu na Mamajusi wa Mashariki, walitii nuru yote waliyoipokea.

Sura ya 18 - Mwanamatengenezo wa Kimarekani

Mkulima mwadilifu na mwaminifu, ambaye alikuwa ameshawishika kutilia mashaka mamlaka ya Kiungu ya Maandiko, lakini ambaye alitamani kwa dhati kuujua ukweli, alikuwa mtu mahsusi ambaye Mungu alimchagua kuongoza utangazaji wa ujio wa pili wa Kristo. Kama wanamatengenezo wengine wengi, William Miller katika siku zake za awali alipambana na umaskini na hivyo alijifunza masomo makuu ya nguvu na kujikana nafsi. Watu waliozaliwa katika familia aliyozaliwa walikuwa na sifa ya kupenda kujitegemea, roho ya kupenda uhuru, uwezo wa kuvumilia, na uzalendo wa hali ya juu—sifa ambazo zilijulikana kama sehemu ya maisha yake. Baba yake alikuwa kapteni katika jeshi la Mapinduzi, na mazingira ya maisha ya Miller ya awali yalimwandaa kutoa maisha yake kafara katika mapambano na mateso ya kipindi cha dhoruba.

Alikuwa na mwili wenye afya njema, na hata katika utoto wake kulikuwa na ushahidi wa uwezo wa akili usiokuwa wa kawaida. Alivyoendelea kukua na kuwa mtu mzima, jambo hili lilizidi kuwa dhahiri. Akili yake ilikuwa kazini saa zote na ilikuwa na uwezo mkubwa, na alikuwa na kiu kubwa ya kupata maarifa. Ingawa hakubahatika kupata elimu ya chuo kikuu, shauku yake ya masomo na tabia yake ya kutafakari kwa makini na kufanya uchambuzi wa mambo kwa kina vilimfanya kuwa mtu mwenye busara na mawazo mapana. Alikuwa na tabia ya uadilifu usiokuwa na dosari na alikuwa na sifa njema isiyokuwa na doa, kwa jumla akitambuliwa kwa uaminifu, matumizi mazuri ya fedha, na ukarimu. Kwa sababu ya nguvu na kufanya kazi alijenga umahiri mapema, ingawa tabia zake za kujifunza bado ziliendelea kudumishwa. Alifanya kazi mbalimbali zikiwemo za kiraia na za kijeshi kwa mafanikio makubwa, na njia za kupata mali na heshima zilionekana kuwa wazi mbele yake.

Mama yake alikuwa ni mcha Mungu kweli kweli, na katika utoto wake, William Miller alipewa mafundisho ya dini na mama yake. Katika miaka ya mwanzoni ya utu uzima, hata hivyo, alitupwa katika jamii ya wakana Mungu, ambao mvuto wao ulikuwa mkubwa zaidi kutokana na ukweli kuwa kwa sehemu kubwa walikuwa raia wema na watu wenye huruma na mwelekeo wa ukarimu. Kutokana na jinsi walivyo, wakana Mungu, wakiwa katikati ya taasisi za Kikristo, tabia zao kwa kiwango kikubwa zilijengwa na mazingira yao. Uzuri wao wa tabia uliowapa heshima na kuaminika vilivyotokana na mafundisho ya Biblia; na hata hivyo karama hizi nzuri ziliharibiwa sana kiasi ambacho zilikuwa na mvuto uliokuwa kinyume na neno la Mungu.

Kwa kujichanganya na hawa watu, Miller alianza kuiga tabia zao. Ufafanuzi wa mafundisho ya Biblia wa wakati huo ulileta matatizo yaliyoonekana kutoweza kuvukwa; hata hivyo imani yake mpya, wakati ikiweka pembeni Biblia, haikuleta jambo lolote la kuchukua nafasi ya Biblia, na hakuweza kuridhika kabisa. Aliendelea kushikilia mawazo haya, hata hivyo, kwa karibu miaka kumi na mbili. Lakini akiwa na umri wa miaka thelathini na nne Roho Mtakatifu aligusa moyo wake na akaelewa hali yake kama mtu mwenye dhambi. Imani

yake ya zamani haikumpa uhakika wa furaha ng'ambo ya kaburi. Mustakabali wake ulionekana kuwa giza na utusitusi. Akitafakari miaka ya baadaye kuhusu hisia zake za sasa alisema:

"Kupotea milele lilikuwa wazo linaloleta unyong'onyevu na hofu, na uwajibikaji ulikuwa uharibifu kwa wote. Mbingu zilikuwa kama shaba juu ya kichwa changu, na dunia ilikuwa kama chuma chini ya nyayo zangu. Umilele—ulikuwa ni nini? Na kifo—kwa nini kilikuwepo? Kwa kadiri nilivyotafakari zaidi, ndivyo nilivyozidi kwenda mbali na uhalisia. Nilivyozidi kufikiria ndivyo mahitimisho yangu yalizidi kusambaratika. Nilijaribu kuacha kufikiri, lakini mawazo yangu hayakuweza kutawalika. Nilikuwa na hali mbaya kweli kweli, lakini sikujua chanzo chake ni nini. Nilinung'unika na kulalamika, lakini sikujua ninamnung'unikia na kumlalamikia nani. Nilijua kulikuwa na jambo ambalo siyo sahihi, lakini sikujua ni kwa jinsi gani siyo sahihi au kujua mahali pa kupata jambo lililo sahihi. Niliomboleza, lakini sikuwa na tumaini."

Aliendelea katika hali hii kwa miezi kadhaa. "Kwa ghafla," anasema, "tabia ya Mwokozi ilifunuliwa na kuwa wazi katika akili zangu. Ilionekana kuwa ni lazima kutakuwa na mwenye uhai aliye mwema sana na huruma nyingi ambaye anaweza kujipatanisha yeye mwenyewe kwa ajili ya makosa yetu, na hivyo kutuokoa kutoka katika mateso na adhabu ya dhambi. Kwa ghafla nilihisi jinsi mwenye uhai huyo anavyopaswa kuwa mwema sana, na niliwaza moyoni mwangu kuwa ningejitupa mikononi mwake, na kutumainia rehema za mwenye uhai huyo. Lakini swali liliibuka, itathibitishwaje kuwa kiumbe kama huyo yupo? Kando ya Biblia, sikuweza kupata ushahidi wa uwepo wa Mwokozi kama huyo, au hata uwepo wa hali njema ya wakati ujao....

"Niliona Biblia ikichora picha ya Mwokozi niliyemhitaji; na nilitatizwa kugundua jinsi ambavyo kitabu kisichokuwa na pumzi ya Mungu kinavyoweza kujenga kanuni zinazokidhi kikamilifu mahitaji ya ulimwengu ulioanguka. Nililazimika kukiri kuwa Maandiko lazima yawe ufunuo kutoka kwa Mungu. Maandiko yakaja kuwa chanzo cha furaha yangu; na Yesu akawa rafiki yangu.

Mwokozi alikuja kuwa mkuu miongoni mwa makumi elfu, Maandiko yaliyokuwa giza na yaliyopingana kabla, sasa yalikuwa taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu. Akili yangu ilitulia na kuridhika. Niligundua kuwa Mungu ni Mwamba katikati ya bahari ya maisha. Biblia ikawa kitabu changu kikuu cha kujifunza, na ninaweza kusema kwa hakika, nilikichunguza kwa furaha kubwa. Hatimaye niligundua kuwa nusu yake ilikuwa haijasimuliwa kwangu. Nilishangaa na kujiuliza kwa nini nilikuwa sioni uzuri na utukufu wake kabla, na nilistaajabu kuwa kwa nini hata nilijaribiwa kuitupilia mbali. Niligundua kuwa mambo yote ambayo moyo wangu uliyatamani yalipatikana katika Biblia, na tiba ya kila ugonjwa wa moyo ilikuwemo humo. Nilipoteza hamu ya kusoma vitabu vingine, na

nilielekeza moyo wangu kupata hekima itokayo kwa Mungu."—S. Bliss, Memoirs of Wm. Miller, ukurasa 65-67.

Miller alitangaza hadharani imani yake katika dini ambayo alikuwa akiidhihaki. Lakini marafiki zake wakana Mungu hawakuchelewa kumletea hoja ambazo yeye mwenyewe alikuwa akizitumia dhidi ya mamlaka ya Kimungu ya Maandiko. Wakati huo hakuwa tayari kuzijibu; lakini alieleza kuwa ikiwa Biblia ni ufunuo kutoka kwa Mungu ni lazima isijipinge yenyewe; na kwamba kwa kuwa ilitolewa kwa ajili ya mafundisho ya mwanadamu, lazima iweze kueleweka kwake. Alidhamiria kujifunza Maandiko kwa ajili yake mwenyewe, na kujiridhisha ikiwa kila kupingana kunakodhaniwa kuwepo kunaafikiwa.

Akijitahidi kuondoa maoni potovu yote aliyokuwa nayo kabla, na akiweka pembeni vitabu vinavyofafanua Biblia, alilinganisha maandiko kwa maandiko kwa msaada wa rejea zilizoko pembeni mwa kurasa za Biblia na kitabu chenye orodha ya maneno yaliyo mengi ya Biblia yaliyopangiliwa kialfabeti. Alipanga kujifunza Biblia kwa muda maalumu ule ule na kwa utaratibu maalumu; akianza na Kitabu cha Mwanzo, na akisoma fungu kwa fungu, hakuendelea mbele ya aya ambazo alikuwa akijifunza mpaka maana ya aya hizo ilipoeleweka kabisa na kujiridhisha kuwa hakuna tashwishi ya aina yo yote iliyobaki. Alipogundua jambo lo lote lisiloelewekwa, ilikuwa desturi yake kulilinganisha aya husika na aya zingine zote zilizogusia jambo alilokuwa akilichunguza. Kila neno liliruhusiwa kuchangia katika kufafanua jambo lililodokezwa na aya husika, na ikiwa wazo la aya hiyo liliafikiana na aya zingine, tatizo liliisha. Kwa njia hiyo, iwe alikutana na sehemu ya Maandiko ngumu kuelekweka alipata maelezo yake katika sehemu nyingine ya Maandiko. Alivyoendelea kujifunza kwa bidii kwa maombi ya dhati ili kupata kuangaziwa na Mungu, jambo lile ambalo lilionekana kuwa giza kwake mwanzoni lilieleweka vizuri. Alipata uzoefu wa ukweli wa maneno ya mwandishi wa Zaburi: "Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga" (Zaburi 119:130).

Kwa shauku kubwa alijifunza vitabu vya Danieli na Ufunuo, akitumia kanuni ile ile ya kutafsiri aliyoitumia kwa maandiko mengine, na aligundua, kwa furaha kubwa, kuwa mifano ya kiunabii iliweza kueleweka. Aliona kuwa sehemu mbalimbali za unabii, ambazo zilikuwa zimetimizwa, zilitimizwa katika ulimwengu unaoonekana; kwamba vielelezo mbalimbali vyote, sitiari zote, mifano yote, tashbihi zote, nk., ziliweza kufafanuliwa kwa kulinganisha na muktadha ulio karibu, au maneno ambayo yametumika kuzielelezea yamefasiliwa katika sehemu zingine za Maandiko, na kwa kufafanuliwa hivyo, zilipaswa kueleweka moja kwa moja kama zilivyo.

"Kwa njia hiyo niliridhika," alisema,"kuwa Biblia ni mfumo wa ukweli uliofunuliwa, uliotolewa kwa uwazi na usahili kiasi kwamba msafiri, hata kama angekuwa mjinga kiasi gani, hawezi kushindwa kuelewa kile Maandiko yanachosema."— Bliss, ukurasa 70. Kiunganishi baada ya kiunganishi cha mnyororo wa ukweli kilibariki juhudi zake, kwa kadiri

jinsi alivyofuatilia matukio makubwa ya unabii. Malaika wa mbinguni waliongoza akili yake na kumfunulia Maandiko ili aweze kuelewa.

Akichukua jinsi ambavyo sehemu mbalimbali za unabii uliokwisha kutimizwa wakati uliopita kama kigezo cha kupima jinsi unabii wa mambo yaliyokuwa bado yanakuja katika wakati ujao, aliridhika kuwa wazo lililoenea kuwa utawala wa kiroho wa Kristo—milenia ya wakati mfupi kabla ya mwisho wa dunia—halikuungwa mkono na neno la Mungu. Fundisho hili, likielekeza kwa miaka elfu moja ya haki na amani kabla ya ujio binafsi wa Bwana, liliifanya siku ya Mungu kuonekana iko mbali sana. Lakini, haidhuru lilikuwa la lilifurahisha kiasi gani, liko kinyume na mafundisho ya Kristo na mitume Wake, waliotangaza kuwa ngano na magugu vinapaswa kukua pamoja mpaka wakati wa mavuno, mwisho wa dunia; kuwa "watu wabaya na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu;" kuwa "siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari;" na kuwa ufalme wa giza utaendelea mpaka ujio wa Bwana na utakomeshwa kwa roho ya mdomo Wake na kuangamizwa kwa mwanga wa ujio wake. (Mathayo 13:30, 38-41; 2 Timotheo 3:13, 1; 2 Wathesalonike 2:8).

Fundisho la kuongoka kwa ulimwengu na utawala wa kiroho wa Kristo halikufundishwa na kanisa la mitume. Kwa jumla halikukubaliwa na Wakristo mpaka karibu na mwanzoni mwa karne ya kumi na nane. Kama inavyokuwa kwa kosa lingine lo lote lile, matokeo yake yalikuwa mabaya. Liliwafundisha kutazama mbali katika wakati ujao kwa ajili ya ujio wa Bwana na liliwazuia wasiangalie dalili zilizoashiria ukaribu wa ujio Wake. Lilijenga hisia ya kujiamini na usalama ambao haukuwa na msingi mzuri na liliwafanya wengi kupuuzia maandalizi muhimu kwa ajili ya kumlaki Bwana wao.

Miller aligundua kuwa ujio binafsi ulio sisisi wa Kristo ulifundishwa wazi wazi katika Maandiko. Paulo anasema: "Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu" (1 Wathesalonike 4:16). Na Mwokozi alitangaza: "Nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi." "Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu" (Mathayo 24:30, 27). Ataandamana na majeshi yote ya mbinguni. "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye" (Mathayo 25:31). "Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake" (Mathayo 24:31).

Wakati wa kuja Kwake wenye haki waliokufa watafufuliwa, na wenye haki walio hai watabadilishwa. "Hatutalala sote" alisema Paulo, "lakini sote tutabadilika, "kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa" (1 Wakorintho 15:51- 53). Na katika barua kwa Wathesalonike, baada ya kueleza ujio wa Bwana, alisema: "Nao waliokufa katika Kristo

watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele" (1 Wathesalonike 4:16, 17).

Ni mpaka wakati wa ujio wa Kristo Mwenyewe ambapo watu Wake watapokea ufalme. Mwokozi alisema:"Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake; na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi; atawaweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto. Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu" (Mathayo 25:31-34).

Tumeona kwa njia ya maandiko ambayo yametolewa hapa kuwa Mwana wa Adamu atakapokuja wafu watafufuliwa na kuwa na hali ya kutokufa na walio hai wanabadilishwa. Kwa badiliko hili kubwa wanajiandaa kupokea ufalme; kwani Paulo anasema:"Nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu; wala uharibifu kurithi kutokuharibika" (1 Wakorintho 15:50). Mwanadamu katika hali yake ya sasa ana hali ya kufa, ana mwili unaoharibika; lakini ufalme wa Mungu utakuwa usioharibika, unaodumu milele. Kwa hiyo mwanadamu katika hali yake ya sasa hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu. Lakini Yesu atakapokuja, atawapa watu Wake hali ya kutokufa; na halafu atawaita kuurithi ufalme ambao tangu wakati huo utakuwa urithi wao.

Maandiko haya na maandiko mengine yalithibitisha wazi kwa akili ya Miller kuwa matukio ambayo yalitarajiwa kutokea kabla ya kuja kwa Kristo, kama vile utawala wa amani ulimwenguni kote na uanzishwaji wa ufalme wa Mungu hapa duniani, yatafuata baada ya ujio wa pili wa Kristo. Hali kadhalika, ishara zote za nyakati na hali ya ulimwengu vililandana na maelezo ya kiunabii ya siku za mwisho. Alilazimishwa kufikia majumuisho, kwa kujifunza Maandiko peke yake, kuwa kipindi kilichowekwa cha kuendelea kuwepo dunia katika hali yake ya sasa, kilikuwa karibu kuisha.

"Aina nyingine ya ushahidi ambao uliathiri kiasi kikubwa akili yangu," alisema, "ulikuwa kufuatana kwa matukio katika muda katika Maandiko. Nilikuta jambo hilo likiwa limetabiriwa katika unabii, likiwa limetimia katika wakati uliopita, mara nyingi likiwa limetokea katika kipindi husika cha wakati. Miaka mia moja na ishirini hadi wakati wa gharika (Mwanzo 6:3); siku saba ambazo zilitangulia kabla ya gharika, pamoja na siku arobaini za mvua iliyotabiriwa (Mwanzo 7:4); miaka mia nne ya safari ya uzao wa Ibahimu (Mwanzo 15:13); siku tatu za ndoto za mnyweshaji na mwokaji (Mwanzo 40:12-20); miaka saba ya Farao (Mwanzo 41:28-54); miaka arobaini jangwani (Hesabu 14:34); miaka mitatu na nusu ya njaa (1 Wafalme 17:1) [tazama Luka 4:25;] miaka sabini ya utumwani (Yeremia 25:11); Nyakati saba za Nebukadneza (Danieli 4:13-16); na majuma saba, majuma sitini na mbili, na juma moja, ambayo jumla yake ni majuma sabini, yaliyoamriwa juu ya Wayahudi

(Danieli 9:24-27),—matukio ambayo yalihusisha nyakati hizi yalikuwa mwanzoni ni unabii tu, na yalitimizwa kulingana na utabiri husika."—Bliss, pages 74, 75.

Wakati ambapo, kwa hiyo, alikuta, katika kujifunza Kwake Biblia, vipindi mbalimbali vyenye matukio yanayofuatana, kwa uelewa wake, yaliendelea mpaka wakati wa kuja mara ya pili kwa Kristo, hakuchukulia vipindi hivyo kama "nyakati zilizoteuliwa," ambazo Bwana alizifunua kwa watumishi Wake. "Mambo ya siri," alisema Musa, "ni ya Bwana Mungu wetu: lakini mambo yale yaliyofunuliwa kwetu ni yetu sisi na watoto wetu milele;" na Bwana alisema kwa njia ya nabii Amosi, kuwa Yeye "hatafanya jambo lo lote, bila kuwafunulia siri watumishi Wake" (Kumbukumbu 29:29; Amosi 3:7). Wanafunzi wa neno la Mungu wanaweza, hivyo basi, kutarajia kwa uhakika kuona tukio la kutisha sana lililotajwa kwa uwazi katika Maandiko ya ukweli likitokea katika historia ya mwanadamu.

"Kwa kuwa nilikuwa nimeamini," alisema Miller, "kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho"(2 Timotheo 3:16); kuwa halikuletwa wakati wo wote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali liliandikwa na watu watakatifu wakiongozwa na Roho Mtakatifu (2 Petro 1:21), na liliandikwa 'kwa ajili ya mafundisho yetu, kuwa sisi kwa uvumilivu na faraja ya Maandiko tuweze kuwa na tumaini' (Warumi 15:4), nililazimika kuchukulia sehemu za Biblia zinazotaja nyakati zinazofuatana kuwa sehemu ya Biblia kama sehemu zingine za neno la Mungu zilivyo, na kuwa zilistahili kutiliwa maanani, kama sehemu zingine zozote za Maandiko. Hivyo basi nilihisi kuwa katika kujaribu kuelewa kile ambacho Mungu katika rehema Yake aliona vema kutufunulia, sikuwa na haki kuruka vipindi vya kiunabii."—Bliss, uk. 75.

Unabii ulioonekana kuwa wazi zaidi katika kufunua wakati wa ujio wa pili ni ule wa Danieli 8:14: "Akamwambia, Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa." Akifuata kanuni yake ya kuyafanya Maandiko yajitafsiri yenyewe, Miller aligundua kuwa siku katika unabii wa mifano huwakilisha mwaka (Hesabu 14:34; Ezekieli 4:6); aliona kuwa kipindi cha siku 2300 za kiunabii, au miaka sisisi 2300, kingeenda mbele sana hadi kuvuka kufungwa kwa kipindi cha Wayahudi kuwa taifa takatifu, kwa hiyo kisingewakilisha hekalu la kipindi cha Wayahudi kama taifa takatifu la Mungu. Miller alikubaliana na mtazamo uliokuwepo mpaka wakati huo kuwa katika zama za Ukristo dunia ndiyo patakatifu, na hivyo alielewa kuwa kutakataswa kwa hekalu kulikotabiriwa katika Danieli 8:14 kuliwakilisha kutakaswa kwa dunia kwa moto wakati wa ujio wa pili wa Kristo.

Kwa hiyo, ikiwa mahali sahihi pa kuanzia pangepatikana kwa ajili ya siku 2300, alijumuisha kuwa wakati wa ujio wa pili wa Kristo ungeweza kuthibitishwa kirahisi. Hivyo wakati wa mwisho wa mambo yote ungeweza kufunuliwa, wakati ambao hali ya sasa, pamoja na "kiburi na nguvu zake zote, majivuno na upuuzi, uovu na uonevu, vingekoma;" wakati laana "ingeondolewa duniani, kifo kingeangamizwa, zawadi kutolewa kwa watumishi wa

Mungu, manabii na watakatifu, na wale wanaolicha jina Lake, na waangamizwe watu wanaoiharibu dunia."— Bliss, ukurasa 76.

Kwa bidii kubwa, Miller aliendelea kuchunguza unabii, wakati wote wa usiku na mchana ukitumiwa kujifunza kile ambacho kilionekana kuwa na umuhimu mkubwa na ambacho kiliamsha shauku kubwa ya kukifuatilia. Katika Sura ya nane ya Danieli hakuweza kupata kidokezo cho chote ambacho kingemwezesha kujua mwanzo wa kipindi cha siku 2300; malaika Gabrieli, ingawa alikuwa amepewa amri ya kumfanya Danieli aelewe njozi, alimpa maelezo kidogo. Wakati mateso ya kutisha yaliyotarajia kulipata kanisa yalipofunuliwa katika njozi ya nabii, nguvu za kimwili zilimtoka. Hakuweza kustahimili zaidi, na malaika alimwacha kwa muda. Danieli "alizimia, na alikuwa mgonjwa kwa siku." "Na nilishangazwa na njozi," alisema, "lakini hakuna aliyeelewa."

Walakini Mungu alimwagiza mjumbe Wake: "mfahamishe mtu huyu maono haya." Agizo hili lilitekelezwa. Katika kulitii agizo hilo, malaika, muda fulani baadaye, alimrudia Danieli, na kusema: "nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu;" "basi itafakari habari hii, na kuyafahamu maono haya" (Danieli 8:27, 16; 9:22, 23, 25-27). Kwa hiyo kulikuwa na jambo moja muhimu katika njozi ya Sura ya 8 ambayo ilikuwa imeachwa bila kutolewa maelezo, ambalo, ni lile linalohusiana na wakati—kipindi cha siku 2300; kwa hiyo malaika, kwa kurudi na kuendelea na maelezo yake, anashughulikia zaidi mada ya wakati:

"Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu, ili kukomesha makosa, na kuishiliza dhambi, na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu, na kuleta haki ya milele, na kutia muhuri maono na unabii, na kumtia mafuta yeye aliye mtakatifu. Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake masihi aliye mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu. Na baada ya yale majuma sitini na mawili, masihi atakatiliwa mbali, naye atakuwa hana kitu….. Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu."

Malaika alitumwa kwa Danieli kwa ajili ya kusudi moja tu la kumwelezea jambo ambalo alikuwa ameshindwa kulielewa katika njozi ya Sura ya nane, jambo ambalo lilihusiana na wakati—"Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa." Baada ya kumwagiza Danieli "atafakari habari hii, na kuyafahamu maono haya," maneno ya kwanza ya malaika ni haya: "Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu." Neno lililotafsiriwa hapa "umeamriwa" linamaanisha "kukata." Majuma sabini, yanayowakilisha miaka 490, yalitangazwa na malaika kuwa yamekatwa, hususani kuhusiana na Wayahudi. Lakini majuma hayo yalikatwa kutoka wapi? Kwa kuwa siku 2300 ndizo zilikuwa kipindi pekee cha wakati kilichotajwa katika Sura ya 8, ndicho kipindi ambacho kutokana nacho majuma sabini yalikatwa; majuma sabini

yanapaswa kuwa sehemu ya siku 2300, na vipindi vyote viwili vinapaswa kuanza pamoja. Majuma sabini yalitangazwa na malaika kuanza tarehe ya kutangazwa kwa amri ya kurejesha na kuujenga upya mji wa Yerusalemu. Ikiwa tarehe ya amri hii ingepatikana, tarehe ya kuanza kwa kipindi kikuu cha siku 2300 ingeweza kujulikana kwa hakika.

Katika Sura ya saba ya Ezra ndiko inakopatikana amri (Aya za 12-26). Katika ukamilifu wake wote ilitolewa na Artashasta, mfalme wa Uajemi, 457 K.K. Lakini katika Ezra 6:14 nyumba ya Bwana inasemekana kuwa ilijengwa "kulingana na amri ya Koreshi, na Dario, na Artashasta mfalme wa Uajemi." Hawa wafalme watatu, kwa kuanzisha, kukazia, na kukamilisha amri, waliifanya itekelezwe kikamilifu kama ilivyotakiwa na unabii kuonesha mwanzo wa miaka 2300. Kwa kuchukua mwaka 457 K.K., wakati amri ilipokamilishwa, kama tarehe ya kutolewa kwa amri, kila kipengele cha unabii uliohusu majuma sabini ulionekana kuwa umeshatimizwa.

"Tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake masihi aliye mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili"—yaani, majuma sitini na mbili, au miaka 483. Amri ya Artashasta ilianza kutekelezwa wakati wa vuli ya mwaka 457 K.K. Tangu tarehe hii, miaka 483 inaishia vuli ya mwaka B.K. 27. (Tazama Kiambatisho.) Wakati huu unabii huu ulitimizwa. Neno 'Masihi' linamaanisha "Mpakwa Mafuta." Katika vuli ya B.K. 27 Kristo alibatizwa na Yohana na kupokea upako wa Roho. Mtume Petro anashuhudia kuwa "Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu" (Matendo 10:38). Na Mwokozi Mwenyewe alisema: "Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema" (Luka 4:18). Baada ya ubatizo Wake alikwenda Galilaya, "akiihubiri Habari Njema ya Mungu, akisema, Wakati umetimia" (Marko 1:14, 15).

"Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja." Hili "juma" linalotajwa hapa ni juma la mwisho miongoni mwa majuma sabini; ni miaka saba ya mwisho kipindi kilichopangwa mahsusi kwa ajili ya Wayahudi. Katika kipindi hiki kinachoanzia mwaka B.K. 27 hadi mwaka B.K. 34, Kristo, mwanzoni kwa njia ya nafsi Yake Mwenyewe na baadaye kwa njia ya wanafunzi Wake, alipeleka mwaliko wa injili hususani kwa Wayahudi. Mitume walipotoka na kwenda nje wakiwa na habari njema ya ufalme, maelekezo ya Mwokozi yalikuwa: "Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie. Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Mathayo 10:5, 6).

"Na kwa nusu ya juma hilo ataikomesha sadaka na dhabihu." Mwaka B.K. 31, miaka mitatu na nusu baada ya ubatizo Wake, Bwana wetu alisulubishwa. Kwa kafara kuu iliyotolewa juu ya mlima wa Kalwari, alikomesha mfumo wa sadaka ambazo kwa miaka elfu nne zilielekeza kwa Mwanakondoo wa Mungu ajaye. Mfano ulikutana na kitu halisi, na kafara zote za mfumo wa kaida zilikomea hapo.

Majuma sabaini, au miaka 490, hususani waliyopewa Wayahudi, yaliishia, kama tulivyoona, mwaka, B.K. 34. Wakati huo, kupitia kwa tendo la Baraza Kuu la Wayahudi, Sanhedrini, taifa lilitia muhuri kukataa kwake injili kwa kumwua Stefano na kuwatesa wafuasi wa Kristo. Tangu hapo, ujumbe wa wokovu, ambao mwanzoni ulikuwa upelekwe kwanza kwa Wayahudi, ulipelekwa ulimwenguni. Wanafunzi, wakiwa wamelazimishwa na mateso kuukimbia mji wa Yerusalemu, "walienda kila mahali wakilihubiri neno." "Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo." Petro, akiongozwa na Mungu, alimfungulia injili akida wa Kaisaria, Kornelio mcha Mungu; na Paulo mwenye juhudi, akiwa ameongolewa na kuipokea imani ya Kristo, aliagizwa kupeleka habari njema "mbali kwa watu wa Mataifa" (Matendo 8:4, 5; 22:21).

Kwa kiwango hicho kila kipengele cha unabii kilitimizwa kikamilifu, na mwanzo wa majuma sabini ukathibitika wazi kuwa ni mwaka 457 K.K., na yanaishia mwaka B.K. 34. Kutokana na maelezo hayo hakuna ugumu wa kupata mwisho wa kipindi cha siku 2300. Majuma sabini— siku 490— zikiwa zimekatwa kutoka siku 2300, kulikuwa na siku 1810 zilizobaki. Baada ya mwisho wa siku 490, siku 1810 zilikuwa bado kutimizwa. Tangu mwaka B.K. 34, miaka 1810 inaishia 1844. Kwa hiyo siku 2300 za Danieli 8:14 zinaishia mwaka 1844. Mwishoni mwa hiki kipindi kikuu cha kiunabii, kwa ushuhuda wa malaika wa Mungu, "patakatifu patatakaswa." Hivyo wakati wa kutakaswa kwa patakatifu—ambako kuliaminiwa na karibu ulimwengu wote kuwa kungetokea wakati wa ujio wa pili wa Kristo—kulikuwa kumebainishwa kikakamilifu.

Miller na wenzake mwanzoni waliamini kuwa siku 2300 zingeishia msimu wa masika wa mwaka 1844, ambapo unabii huelekeza kwa msimu wa vuli wa mwaka huo. (Tazama Kiambatisho.) Kutokuelewa vizuri kipengele hiki kuliwasababishia kuvunjika moyo na kuingiwa mashaka kwa wale waliokuwa wameweka tarehe ya awali kama siku ya ujio wa Bwana. Lakini jambo hili halikuathiri hata kidogo nguvu ya hoja iliyoonesha kuwa siku 2300 ziliishia mwaka 1844, na kuwa tukio kuu lililowakilishwa na utakaso wa patakatifu lazima lingetokea.

Akianza kujifunza Maandiko kama alivyofanya, kwa lengo la kuthibitisha kuwa yalikuwa ufunuo kutoka kwa Mungu, Miller hakuwa, tangu mwanzo kabisa, na matarajio hata kidogo ya kufikia hitimisho ambalo sasa alifikia. Yeye mwenyewe hakuweza kukubali kirahisi matokeo ya utafiti wake. Lakini ushahidi wa Maandiko ulikuwa wa wazi na wenye nguvu kiasi kwamba asingeweza kuupuuza.

Alikuwa ametumia miaka miwili kwa ajili ya kujifunza Biblia, ambapo, mwaka 1818, alifikia kushawishika kwa dhati kuwa ndani ya miaka ishirini na tano Kristo angetokea kuwakomboa watu Wake. "Sihitaji kusema," Miller alisema, "kuhusu furaha iliyoujaza moyo wangu nikitafakari juu ya matazamio yenye furaha, na juu ya shauku kuu ya roho yangu ya kushiriki katika furaha za waliokombolewa. Biblia sasa kikawa kitabu kipya kwangu. Biblia

ilikuwa chakula cha fikra; kila jambo lililoonekana kuwa giza, la siri, au lisiloeleweka kwangu katika mafundisho yake, liliyeyuka kutoka katika akili yangu mbele ya nuru angavu ambayo sasa ilipambazuka kutoka katika kurasa zake takatifu; na, ndiyo, ukweli ulikuwa na mwangaza na utukufu mwingi kiasi gani! Mambo yote yaliyokuwa yakionekana kupingana na kutopatana ambayo niliyaona katika neno la Mungu yaliyotoweka; na ingawa kulikuwa na maeneo mengi ambayo nilikuwa sijaridhika kuwa nimepata uelewa kamili, hata hivyo nuru kubwa ilitoka katika Maandiko iliangazia akili yangu ambayo kabla ya hapo ilikuwa gizani, kiasi kwamba nilifurahia kujifunza Maandiko ambayo hapo awali sikudhani kuwa ningeweza kuipata katika mafundisho yake."—Bliss, ukurasa 76, 77.

"Pamoja na kushawishika sana kuwa matukio makuu hayo yalitabiriwa katika Maandiko na kuwa yalitarajiwa kutimizwa katika muda mfupi sana, suala lilikuja moyoni kwa nguvu nyingi lilihusiana na wajibu wangu kwa ulimwengu, kutokana na ushahidi ambao ulikuwa umegusa akili yangu."— Ibid., ukurasa 81. Hakuwa na njia nyingine isipokuwa kuhisi kuwa ilikuwa wajibu wake kuwaeleza wengine nuru aliyokuwa ameipokea. Alitarajia kukutana na upinzani kutoka kwa watu wasiomcha Mungu, lakini alikuwa na hakika kuwa Wakristo wote wangefurahia katika tumaini la kukutana na Mwokozi ambaye walikiri kumpenda. Hofu yake pekee ilikuwa kwamba katika furaha yao kubwa ya matarajio ya ukombozi wenye utukufu, uliokuwa tayari kukamilika, wengi wao wangepokea fundisho hilo bila kuchunguza kikamilifu Maandiko yaliyoeleza ukweli wake. Hivyo, alisita kuuwasilisha, isije ikawa pengine amekosea na yeye kuwa njia ya kuwapoteza wengine. Hivyo aliongozwa kupitia upya ushahidi uliounga mkono hitimisho alilofikia, na kufikiria kwa uangalifu kila ugumu uliojitokeza katika akili yake. Aliona kuwa kila kipingamizi kiliyeyuka mbele ya nuru ya neno la Mungu, kama ukungu unavyoyeyuka katika miale ya jua. Miaka iliyotumika kwa njia hiyo ilimwacha akiwa ameshawishika kikamilifu kuhusu usahihi wa msimamo wake.

Na sasa wajibu wa kuhakikisha kuwa wengine wanafikishiwa kile ambacho aliamini kuwa kilifundishwa kwa uwazi katika Maandiko, ulimjia kwa nguvu mpya. "Nilipokuwa nikiendelea kufanya shughuli zangu," alisema, "uliendelea daima kupiga kengele masikioni mwangu, 'Nenda ukauambie ulimwengu hatari inayowakabili.' Aya hii ilidumu kumjia akilini mwake: 'Nimwambiapo mtu mbaya, Ewe mtu mbaya, hakika utakufa, nawe husemi neno la kumwonya mtu huyo, aiache njia yake, mtu mbaya huyo atakufa katika uovu wake, lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Walakini ukimwonya mtu mbaya kwa sababu ya njia yake, kusudi aiache; wala yeye asiiache; atakufa huyo katika uovu wake, lakini wewe umejiokoa roho yako" (Ezekieli 33:8, 9). Nilihisi kuwa ikiwa watu waovu wangeonywa kikamilifu, wengi wao wangetubu; na kuwa ikiwa wasingeonywa, damu yao ingedaiwa mikononi mwangu."—Bliss, ukurasa 92.

Alianza kuwasilisha mawazo yake kwa mtu mmoja mmoja kwa kadiri fursa zilivyojitokeza, akiombea kuwa mchungaji fulani aguswe na nguvu ya mafundisho yake na ajitolee kuyatangaza. Lakini hakuweza kuondoa wazo kuwa alikuwa na wajibu binafsi wa

kufanya katika kutoa onyo hilo. Maneno yalikuwa yakirudia akilini mwake: "Nenda kauambie ulimwengu; damu yao nitaitaka mikononi mwako." Kwa muda wa miaka tisa alisubiri, mzigo ukiwa bado unalemea moyo wake, mpaka mwaka 1831 ambapo kwa mara ya kwanza aliwasilisha hadharani sababu za imani yake.

Kama Elisha alivyoitwa kuacha kufuatana na ng'ombe waliokokota jembe la kulima mashambani, na kupokea joho la wakfu kwa ajili ya kazi ya kinabii, kadhalika William Miller aliitwa na kuacha plau yake na kujiweka wakfu kuwafunulia watu siri za ufalme wa Mungu. Akiwa katika hali ya kutetemeka, alianza kazi yake, akiwaongoza wasikilizaji wake pole pole, hatua kwa hatua, na kuwapitisha katika vipindi mbalimbali vya kiunabii hadi ujio wa pili wa Kristo. Kwa kila juhudi alipata nguvu na ujasiri alipoona shauku ya watu wengi ikiongezeka kutokana na maneno yake.

Ilikuwa kwa njia ya maombi ya rafiki zake tu, ambapo katika maneno yao alisikia wito wa Mungu, akiwa mtu mzima, asiye na uzoefu wa kuongea hadharani, na akilemewa na mzigo wa hisia ya kutokufaa kwake kwa ajili ya kazi iliyokuwa mbele yake. Lakini tangu hotuba yake ya kwanza kazi zake zilibarikiwa kwa namna ya ajabu sana kwa ajili ya wokovu wa roho. Hotuba yake ya kwanza ilifuatwa na mwamko wa kidini ambapo wanafamilia wote wa familia kumi na tatu, isipokuwa watu wawili, waliongoka.

Muda mfupi baadaye aliitwa kuhubiri katika maeneo mengine, na karibu katika kila mahali kazi yake ilileta uamsho wa kazi ya Mungu. Wenye dhambi walioongolewa, Wakristo walihamasishwa kujiweka wakfu kikamilifu zaidi, na wanaoamini kuwa Mungu aliuumba ulimwengu halafu akaucha ujiendeshe wenyewe na wakana Mungu waliongozwa kukiri ukweli wa Biblia na dini ya Kikristo. Ushuhuda wa wale ambao miongoni mwao aliwafundisha ulikuwa: "Tabaka fulani la akili limefikiwa na mtu ambaye haendeshwi na mvuto wa watu wengine."—Ibid., ukurasa 138. Mahubiri yake yalikusudiwa kuamsha akili za jamii ili zitafakari mambo makubwa ya dini na kudhibiti hali ya udunia iliyokuwa ikikua na tamaa za kizazi kile.

Karibu katika kila mji kulikuwepo na makundi ya watu, wengine, wakiwa katika mamia, walioongoka kama matokeo ya mahubiri yake. Katika maeneo mengi makanisa ya Kiprotestanti ya karibu ya madhehebu zote yaliwekwa wazi kwa ajili yake, na miito kwa ajili ya kufanya kazi daima ilitoka kwa wachungaji wa makanisa kadhaa. Ilikuwa kanuni yake ya kudumu kutohubiri katika makansia ambayo hakuitwa, hata muda mfupi baadaye alijikuta hawezi kutimiza nusu ya maombi yaliyokuwa yamefurika kwake. Wengi wa wale ambao hawakukubali mawazo yake ya wakati mahsusi wa ujio wa pili walishawishika kuhusu uhakika na ukaribu wa ujio wa Kristo na hitaji lao la kujiandaa. Katika baadhi ya miji mikubwa kazi yake ilileta mguso mkubwa sana. Wauza pombe waliacha biashara yao na kugeuza vilabu vyao kuwa vyumba vya mikutano; vituo vya kuchezea kamari vilivunjwa; wasioamini, waumini uwepo wa Mungu asiyejishughulisha na viumbe wake, Waumini wa

uwepo wa ukweli usiopingika, na hata mafisadi wa kutupwa walifanya matengenezo, ambao baadhi yao walikuwa hawajakanyaga kanisani kwa miaka mingi. Mikutano ya maombi ilianzishwa na madhehebu mbalimbali, katika maeneo mbalimbali, karibu kila saa; wafanyabiashara walikutana wakati wa mchana kwa ajili ya maombi na kumsifu Mungu. Hakukuwa na misisimko bandia, badala yake kulikuwa na kicho katika mawazo ya watu karibu wote. Kazi ya William Miller, kama ilivyokuwa ya Wanamatengenezo wa awali, ilikuwa na mwelekeo wa kushawishi ufahamu na kuamsha dhamiri kuliko kusisimua hisia peke yake.

Mwaka 1833 Miller alipokea leseni ya kuhubiri, kutoka katika Kanisa la Kibaptisti, ambalo yeye alikuwa mshiriki wake. Idadi kubwa ya wachungaji wa madhehebu yake waliidhinisha kazi yake, na aliendelea na kazi zake kwa kibali chao rasmi. Alisafiri na kuhubiri kwa muda wote mfululizo bila kupumzika, ingawa kazi zake binafsi kimsingi zilikomea katika majimbo ya New England na Middle States. Kwa miaka kadhaa gharama zake zote zilitoka katika mfuko wake binafsi, na baadaye hakuweza kupata fedha ya kutosha kumwezesha kwenda kila mahali alikoalikwa. Kwa hiyo kazi zake za hadhara, zikiwa hazina ya lengo la kujipatia fedha, ziligeuka kuwa mzigo mzito kwake kwa kuwa hakuwa na kipato kikubwa, ambacho pole pole kiliendelea kupungua katika kipindi hiki cha maisha yake. Alikuwa baba wa familia kubwa, lakini kwa kuwa wote walikuwa wabanaji wazuri wa matumizi na wenye bidii kubwa ya kazi, shamba lake lilitosha kuwapa kipato cha kujikimu kama familia na cha kusaidia katika kazi zake za kuhubiri injili. Mwaka 1833, miaka miwili baada ya Miller kuanza kuwasilisha hadharani ushahidi wa ujio wa haraka wa Kristo, ishara ya mwisho miongoni mwa ishara zilizoahidiwa na Mwokozi kama dalili za ujio Wake wa pili. Yesu alisema: “Nyota zitaanguka mbinguni” (Mathayo 24:29).

Na Yohana katika kitabu cha Ufunuo, alipoona katika njozi matukio ambayo yangeashiria siku ya Mungu: “Na nyota zikaanguka juu ya nchi kama vile mtini upukutishavyo mapooza yake, utikiswapo na upepo mwingi” (Ufunuo 6:13). Unabii huu ulitimizwa kiajabu na kikamilifu kwa mvua ya vimondo ya Novemba 13, 1833. Hilo lilikuwa onesho lililoshuhudiwa eneo kubwa na la ajabu duniani la nyota kuanguka kwa namna ambayo haijapata kutokea na kuandikwa kabla ya hapo; “anga lote, juu ya nchi yote ya Marekani, ambalo, kwa saa kadhaa, lilikuwa katika misuko-suko ya kuwaka moto! Hakuna tukio kama lile lilowahi kutokea katika anga la nchi ya Marekani, tangu watu walipoanza kuishi katika nchi ile, ambalo lilitazamwa na tabaka moja la watu katika jamii kwa shauku kubwa, na kuangaliwa kwa hofu na taharuki kuwa na tabaka jingine.”

“Fahari yake na uzuri wa ajabu ungali bado katika akili za watu walio wengi Hakuna mvua yo yote iliyowahi kunyesha duniani iliyokuwa nzito zaidi kuliko ile ya vimondo; mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini, ilikuwa sawasawa, anga lote lilikuwa katika hali ya mtikisiko mkubwa. Onesho hilo, kama lilivyoelezwa na Jarida la Profesa Silliman, lilishuhudiwa katika anga lote la Amerika ya Kaskazini. Tangu saa nane alfajiri mpaka wakati

wa mchana wote, anga likiwa katika utulivu mkamilifu na bila mawingu, mchezo endelevu wa vitu vinavyong'aa sana vilidumu kuonekana katika anga lote."—R. M. Devens, American Progress; or, The Great Events of the Greatest Century, ch. 28, pars.1-5.

"Hakuna lugha, kwa hakika, inayoweza kuelezea mwonekano wa mg'aro ule wa ajabu; hakuna mtu hata mmoja ambaye hakushuhudia anaweza kuelewa kikamilifu dhana ya utukufu wa tukio lile. Ilionekana kana kwamba mbingu zenye nyota zilikuwa zimekusanyika pamoja karibu na kilele juu yao, na wakati huo huo zilikuwa zikirusha, kwa kasi ya mwanga, kila upande wa upeo; na bado hazikuchoka—maelfu ya vipande vya nyota kwa haraka vikifuatiwa na maelfu mengine ya vipande vya nyota, kana kwamba viliumbwa kwa ajili hiyo."—F. Reed, in the Christian Advocate and Journal, Dec. 13, 1833. "Mwonekano sahihi wa mtini unaopukutisha mapooza yake unapopulizwa na upepo wenye nguvu, ilikuwa haiwezekani kuangalia."— "The Old Countryman," in Portland Evening Advertiser, Novemba 26, 1833.

Katika jarida la New York Journal of Commerce la Novemba 14, 1833, ilichapishwa makala kuhusu tukio hili la ajabu, ikiwa na kauli hii: "Hakuna mwanafalsafa au msomi aliyewahi kusimulia au kuandika kumbukumbu ya tukio, ninadhani, kama lile la jana asubuhi. Nabii miaka elfu moja na mia nane iliyopita aliwahi kusimulia vizuri, ikiwa tutapata taabu ya kuelewa nyota kuanguka kumaanisha nyota zinazoanguka,. katika maana pekee ambayo inawezekana kuwa halisi."

Hivyo ndivyo ilivyoonekana ishara ya mwisho miongoni mwa dalili za ujio wa Kristo, ambazo Yesu aliwaasa wanafunzi Wake: "Nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, milangoni" (Mathayo 24:33). Baada ya dalili hizi, Yohana aliona, kama tukio kuu linalotarajiwa baada ya hili, mbingu zikiondolewa kama ukurasa uliokunjwa, wakati dunia ikitetemeka, milima na visiwa vikiondolewa mahali pake, na waovu kwa hofu wakiukimbia uso wa Mwana wa Adamu (Ufunuo 6:12-17).

Wengi wa walioshuhudia kuanguka kwa nyota, waliliona kama ujumbe wa ujio wa hukumu, "tukio la kutisha, mtangulizi wa hakika, ishara ya rehema, ya siku ile kuu ya kutisha."—"The Old Country-man," in Portland Evening Advertiser, Novemba 26, 1833. Hivyo mawazo na macho ya watu yalielekezwa kwa utimizo wa unabii, na wengi waliongozwa kuzingatia onyo la ujio wa pili wa Kristo.

Mwaka 1840 utimizo mwingine wa ajabu wa unabii uliamsha shauku kubwa ya watu. Miaka miwili kabla, Josiah Litch, mmoja wa wachungaji mashuhuri akihubiri juu ya ujio wa pili, alichapisha ufafanuzi wa Ufunuo 9, akitabiri anguko la Himaya ya Otomani. Kwa mujibu wa ukokotoaji wake, utawala huu ulipaswa kupinduliwa "mwaka B.K. 1840, wakati fulani katika mwezi wa Agosti;" na siku chache kabla ya utekelezwaji wake aliandika: "Akiruhusu kipindi cha kwanza, miaka 150, kutimizwa kikamilifu kabla ya Deacozes hajapewa ufalme kwa ruhusa ya Waturuki, na kwamba miaka 391, siku kumi na tano, kilianzia mwishoni mwa

kipindi cha kwanza, kingeishia Agosti 11, 1840, wakati mamlaka ya Otomani juu ya Konstantinopo ilitarajiwa kufikia mwisho. Na hili, niliamini, litatokea hivyo hivyo."—Josiah Litch, in Signs of the Times, and Expositor of Prophecy, August 1, 1840.

Wakati mahsusi uliotajwa, Uturuki, kupitia mabalozi wake, ilikubali ulinzi wa mamlaka ya umoja wa mataifa ya Ulaya, na kwa njia hiyo ilijiweka chini ya udhibiti wa mataifa ya Kikristo. Tukio hili lilitimiza kikamilifu utabiri. (Tazama Kiambatisho.) Ilipoeleweka vizuri, watu wengi walishawishika kuamini usahihi wa kanuni za tafsiri ya unabii zilizotumiwa na Miller na wenzake, na mwamko wa ajabu ulileta katika vuguvugu la ujio wa pili. Watu wenye elimu na cheo waliungana na Miller, katika kuhubiri na kuchapisha mafundisho yake, na tangu 1840 hadi 1844 kazi ilipanuka haraka.

William Miller alijaliwa uwezo mkubwa wa akili; na ikiwa imenidhamishwa kwa tafakari na usomaji; aliiongezea hekima ya mbinguni kwa kujiunganisha na Chanzo cha hekima. Alikuwa mtu mwenye uadilifu wa hali ya juu, ambaye katika hali zote alipewa heshima na kutambuliwa mahali popote uadilifu wa tabia na uzuri wa msimamo bora vilithaminiwa. Akichanganya ukarimu wa kweli kutoka moyoni na unyenyekevu wa Kikristo na nguvu ya kujitawala, alikuwa msikivu na mwepesi wa kufikiwa na watu wote, alikuwa tayari kusikia maoni ya wengine na kupima hoja zao. Bila uchungu wala mihemko alizipima nadharia zote na mafundisho yote kwa neno la Mungu, na mpangilio wake wa hoja na ujuzi mkubwa wa Maandiko vilimwezesha kupinga makosa na kuanika uongo.

Pamoja na hayo aliendesha kazi yake katikati ya upinzani mkali. Kama ilivyokuwa kwa Wanamatengenezo wa awali, ukweli aliouwasilisha haukupokelewa na walimu mashuhuri wa dini. Kwa kuwa watu hawa hawakuweza kutetea hoja zao kwa kutumia Maandiko, walilazimika kutumia misemo na mafundisho ya wanadamu, na mapokeo ya viongozi wa makanisa waliopita. Lakini neno la Mungu lilikuwa ushuhuda pekee uliokubaliwa na wahubiri wa ukweli wa marejeo. "Biblia, na Biblia pekee," ilikuwa ndiyo kanuni kuu. Kukosekana kwa nguvu ya Maandiko kwa upande wa wapinzani wao kulijazwa na matusi na dhihaka. Muda, pesa, na talanta vilitumiwa kuwachafua watu ambao kosa lao pekee lilikuwa kutazamia kwa furaha ujio wa Bwana wao na kujaribu kuishi maisha matakatifu na kuwasihi wengine wajiandae kwa ajili ya ujio Wake.

Juhudi kubwa zilitumiwa kuvuta akili za watu mbali na somo la ujio wa pili. Mbinu zilitumika ionekane kana kwamba ni dhambi, kana kwamba ni jambo la kuonea aibu, kujifunza unabii unaohusiana na ujio wa Kristo na mwisho wa dunia. Kwa njia hiyo huduma ya kichungaji ya wakati huo ilidhalilisha imani katika neno la Mungu. Mafundisho yao yaliwafanya watu wawe wapagani, na wengi walitiwa moyo kufuata njia zao za tamaa zinazopingana na Mungu. Waasisi wa maovu waliwasingizia Waadventista kuwa ndio waliotenda maovu waliyoyaasisi wao.

Wakati alikusanya na kujaza nyumba wasikilizaji wenye akili na walio makini, jina la Miller kwa nadra sana lilitajwa katika vyombo vya habari vya kidini isipokuwa kwa kusudi la kumdhihaki au kumpinga. Wasiojali na wasiomcha Mungu wakiwa wametiwa moyo na mafundisho ya walimu wa dini, walimwita majina ya utani ya kumdhihaki, na kumdhalilisha kwa vichekesho vyenye maneno na misemo ya kufuru, katika juhudi za kurundika matusi juu yake na juu ya kazi yake. Mzee mwenye mvi aliyekuwa ameacha nyumba yake nzuri na kusafiri kwa gharama yake kutoka jiji moja hadi jingine, kutoka mji hadi mji mwingine, akifanya kazi bila kupumzika akitoa onyo zito kwa ulimwengu juu ya hukumu iliyo karibu, alikataliwa kwa kejeli kama mtu anayeshikilia sana mambo bila kutumia akili, laghai, na tapeli.

Maneno ya dhihaka, uongo, na matusi yaliyorundikwa juu ya Miller yalialika matamko makali kutoka katika vyombo vya habari, hata visivyokuwa vya kidini, dhidi ya wapinzani wake.“Kushughulikia jambo nyeti na lenye matokeo ya kutisha kama hilo,” kwa dhihaka na kejeli kulitangazwa na kidunia kuwa “siyo tu kuumiza hisia za wahubiri na watetezi wao,” bali “kudhihaki siku ya hukumu na kumpuuza Mungu Mwenyewe, na kubeza vitisho vya hukumu Yake.”—Bliss, ukurasa wa 183.

Mwasisi wa maovu yote alitafuta siyo tu kufuta matokeo ya ujumbe wa marejeo, bali pia kumwangamiza mjumbe nwenyewe. Miller alihubiri ukweli wa Maandiko kama ulivyo na kugusa mioyo ya wasikilizaji wake, akiwaonya makosa yao na kusumbua kuridhika kwao, na maneno yake yaliyokata moja kwa moja yalimwamsha adui yao. Upinzani uliooneshwa na washiriki wa kanisa dhidi ya ujumbe wake uliwafanya wasiomcha Mungu kwenda mbali zaidi katika uovu wao; na maadui walipanga jinsi ya kuondoa uhai wake wakati akiondoka kutoka mahali pa mkutano. Lakini malaika watakatifu walikuwa katikati ya kundi la watu, na mmoja wa malaika hawa, akiwa katika umbo la mwanadamu, aliushika mkono wa mtumishi wa Bwana na kwa kumwondoa kwa usalama kutoka katikati ya kundi la watu wenye hasira.

Kazi ya Miller ilikuwa haijaisha, na Shetani na wafuasi wake walishindwa kutekeleza kusudi lao. Licha ya upinzani wote, shauku katika vuguvugu la ujio wa pili iliendelea kukua. Tangu makumi na mamia, makanisa yalikua na kufikia hadi kuwa maelfu mengi. Waumini wapya wengi walijiunga na makanisa, lakini baada ya muda mfupi roho ya upinzani ilidhihirishwa dhidi ya hata waongofu hawa wapya, na makanisa yalianza kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wale waliokumbatia mawazo ya Miller. Hatua hii ilisababisha Miller kujibu kwa njia ya kalamu yake, akawasiliana na Wakristo wa madhehebu yote, akisisitiza kuwa ikiwa mafundisho yake yalikuwa ya uongo, aoneshwe kosa lake kutoka katika Maandiko.

“Ni nini tunachokiamini,” alisema, “ambacho hatukuagizwa kuamini na neno la Mungu, ambalo ninyi wenyewe mnakubali kuwa ni kanuni, na kanuni pekee, ya imani na matendo yetu? Tumefanya nini kinachofanya tushambuliwe kwa maneno makali kutoka katika

mimbari na vyombo vya habari, na kuwapa haki ya kutuondoa sisi (Waadventista) katika makanisa na ushirika wenu?" "Ikiwa tuna makosa, tunaomba mtuoneshe ni wapi tumekosea. Tuonesheni kutoka katika neno la Mungu mahali tulipokosea; tumetukanwa vya kutosha; hilo haliwezi kutushawishi tuamini kuwa tumekosea; neno la Mungu pekee ndilo linaweza kubadilisha mitazamo yetu. Majumuisho yetu yamepatikana kwa tafakari kubwa na maombi ya dhati, kwa kadiri tulivyoona ushahidi katika Maandiko."—Ibid., ukurasa 250, 252.

Tangu zama na zama maonyo ambayo Mungu aliyatuma kwa ulimwengu kwa njia ya watumishi Wake yalikutana na mashaka na kutoamini. Wakati uovu wa watu walioishi kabla ya gharika ulipomfanya Mungu alete gharika ya maji duniani, kwanza aliwaambia kusudi Lake, ili wapate fursa ya kugeuka na kuziacha njia zao. Kwa miaka mia moja na ishirini sauti ya onyo ilisikika ili watubu, ili ghadhabu ya Mungu isidhihirishwe kwa kuangamizwa kwao. Lakini ujumbe wa onyo ulionekana kama hadithi isiyokuwa na maana, na hawakuuamini. Wakipata ujasiri katika uovu wao walimdhihaki mjumbe wa Mungu, wakapuuza miito yake ya toba, na hata wakamshitaki kuwa alikuwa na kiburi. Inawezekanaje mtu mmoja kusimama dhidi ya watu wote wenye mamlaka duniani? Ikiwa ujumbe wa Nuhu ulikuwa wa kweli, kwa nini ulimwengu wote haukuuona na kuuamini? Mtu mmoja atoe hoja dhidi ya hekima ya watu maelfu! Hawakutilia maanani onyo, wala hawakutafuta hifadhi katika safina.

Watu wenye dhihaka walionesha vitu katika maumbile ya asili,— kufuatana kusikobadilika kwa misimu, anga la bluu ambalo halijawahi kunyesha mvua, mapori ya kijani ambayo yalilowanishwa na umande laini wa usiku,—na walipiga kelele: "Si huyu anasema mifano?" Wakionesha dharau walimtangaza mhubiri wa haki kuwa mshikiliaji mkubwa wa mambo bila kutumia akili; na waliendelea, kwa shauku kubwa zaidi, kutafuta anasa, na walidhamiria kwenda katika njia za uovu zaidi, kuliko kabla ya hapo. Lakini kutokuamini kwao hakukuzuia tukio lililotabiriwa. Mungu alivumilia kwa muda mrefu uovu wao, akiwapa muda wa kutosha ili watubu; lakini kwa wakati uliopangwa hukumu Zake zilitekelezwa juu ya watu waliokataa rehema Yake.

Kristo alisema kuwa kutakuwepo kutokuamini kama huko kuhusiana na ujio Wake wa pili. Kama vile watu wa wakati wa Nuhu ambao hawakutambua "hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo," katika maneno ya Mwokozi wetu, " kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu" (Mathayo 24:39). Wakati watu wanaodai kuwa watu wa Mungu wanapoungana na ulimwengu, wakiishi kama walivyo, na wakiungana nao katika anasa zilizokatazwa; wakati anasa za dunia zinapokuwa anasa za kanisa; wakati kengele za ndoa zinapolia, na watu wote wanatarajia kuwa na miaka ya mafanikio ya kidunia—ndipo, kwa ghafla kama vile umeme wa radi unavyomulika kutoka mbinguni, ndivyo utakavyokuja mwisho wa ndoto zao nzuri na matumaini yao ya uongo.

Kama vile Mungu alivyomtuma mtumishi Wake kuuonya ulimwengu juu ya Gharika iliyokuwa inakuja, ndivyo alivyowatuma wajumbe waliochaguliwa ili wakatangaze ukaribu

wa hukumu ya mwisho. Na kama vile watu wa wakati wa Nuhu walivyocheka na kudhihaki utabiri wa mhubiri wa haki, kadhalika katika wakati wa Miller wengi, hata miongoni mwa watu waliodai kuwa watu wa Mungu, walidhihaki maneno ya onyo.

Na ni kwa nini mafundisho na mahubiri juu ya ujio wa pili wa Kristo hayakupokelewa na makanisa? Wakati kwa waovu ujio wa Bwana huleta kilio na uangamivu, kwa wenye haki umejaa shangwe na tumaini. Ukweli huu mkuu umekuwa faraja ya watu wa Mungu waaminifu katika zama zote; kwa nini ulikuja, kama Mwasisi wake, "jiwe likwazalo" na "mwamba uchukizao" kwa wanaodai kuwa watu Wake? Ni Bwana wetu aliyewaahidi wanafunzi Wake: "Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu" (Yohana 14:3). Ni Mwokozi wetu mwenye huruma, ambaye, akitarajia upweke na huzuni ya wafuasi Wake, aliwatuma malaika wawafariji kwa kuwapa uhakikisho kuwa Yesu atarudi tena akiwa vilevile walivyomwona akienda mbinguni.

Wanafunzi walipokuwa wamesimama wakitazama kwa makini juu kumwona anavyotoweka Yeye ambaye walimpenda, umakini wao ulikamatwa na maneno haya: "Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni" (Matendo 1:11). Tumaini liliamshwa upya na ujumbe wa malaika. Wanafunzi "wakarudi Yerusalemu wenye furaha kuu. Nao walikuwa daima ndani ya hekalu, wakimsifu Mungu" (Luka 24:52, 53). Walifurahia siyo kwa sababu ya Yesu kutengana nao na kuwaacha wapambane na majaribu na vishawishi vya ulimwengu, bali kwa sababu ya uhakikisho wa malaika kuwa Yesu atarudi tena.

Utangazaji wa ujio wa Kristo unapaswa kuwa sasa, kama ulivyofanywa na malaika kwa wachungaji wa Bethlehemu, habari njema ya furaha kuu. Wanaompenda Mwokozi kwa dhati hawawezi kutulia bali wahubiri kwa furaha tangazo lililojengwa juu ya neno la Mungu kuwa Yule ambaye Kwake matumaini yao ya uzima wa milele yanapatikana anakuja tena, siyo kuja kutukanwa, kudharauliwa, na kukataliwa, kama ilivyokuwa wakati wa ujio Wake wa kwanza, bali katika nguvu na utukufu, kuwakomboa watu Wake. Ni wale wasiompenda Mwokozi wanaotamani asije, na hakuwezi kuwepo ushahidi hitimishi kuwa makanisa yamemwacha Mungu kuliko mwasho na uadui unaoamshwa na ujumbe huu uliotumwa kutoka mbiguni.

Watu waliopokea fundisho la ujio wa pili wa Kristo waliamshwa na kuona umuhimu wa toba na unyenyekevu mbele ya Mungu. Watu wengi wamekuwa wakitanga-tanga kwa muda mrefu kati ya Kristo na ulimwengu; sasa walihisi kuwa ilikuwa wakati wa kuwa na msimamo. "Masuala ya umilele yalichukua Sura ya uhalisia mpya. Mbingu ilisogezwa karibu yao, na walijisikia kuwa wenye hatia mbele ya Mungu."—Bliss, ukurasa 146. Wakristo waliamshwa na kupata uzoefu mpya wa maisha ya kiroho. Waliongozwa kujisikia kuwa muda ulikuwa mfupi, kuwa kile walichopaswa kukifanya kwa ajili ya wanadamu wenzao ilipaswa kifanyike haraka. Dunia ilirudishwa nyuma, umilele ulionekana kufunguka mbele yao, na roho, pamoja

na vyote vinavyohusiana na umilele wake, vilionekana kugubika mambo ya kidunia. Roho wa Mungu alikuwa pamoja nao na aliwapa nguvu za kutoa miito kwa ndugu zao, na kwa wenye dhambi, ili wajiandae kwa ajili ya siku ya Mungu. Ushuhuda wa kimya wa maisha yao ya kila siku ulikuwa karipio la daima dhidi ya washiriki wa makanisa wa mazoea na wasiojiweka wakfu kwa Mungu kikamilifu. Watu hawa hawakupenda kusumbuliwa katika shughuli zao za kutafuta raha, kazi zao za utafutaji wa pesa, na shauku zao za kupata heshima ya ulimwengu. Hivyo basi, uadui na upinzani viliamshwa dhidi ya imani ya ujio wa Kristo na watu waliotangaza imani hiyo.

Kwa kadiri hoja zilizotokana na vipindi vya kiunabii zilivyoonekana kuwa zisizowezwa kupingwa, wapinzani walijaribu kuwakatisha tamaa watu wasijifunze somo hilo kwa kufundisha watu kuwa masuala ya unabii yalikuwa yametiwa muhuri. Hivyo basi, Waprotestanti walifuata nyayo za Waroma. Wakati kanisa la kipapa lilizuilia Biblia (tazama Kiambatisho) isionwe na watu, Makanisa ya kiprotestanti yalidai kuwa sehemu muhimu ya Neno Takatifu—na kwamba sehemu ambayo inaeleza ukweli, hususani, ukweli unaohusu wakati wetu—isingeweza kueleweka.

Wachungaji na waumini walitangaza kuwa unabii wa Danieli na Ufunuo ulikuwa siri zisizoweza kueleweka. Lakini Kristo aliwaelekeza wanafunzi Wake wasome maneno ya nabii Danieli yanayohusu matukio ambayo yangetokea katika wakati wao, na alisema: “Asomaye na afahamu” (Mathayo 24:15). Na dai kuwa kitabu cha Ufunuo ni siri, na kuwa hakiwezi kueleweka, linapingwa na kitabu cha Ufunuo chenyewe: “Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi…. Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu” (Ufunuo 1:1-3).

Nabii anasema: “Heri asomaye”—wapo ambao hawatasoma; mbaraka siyo wao. “Na wao wayasikiao”—wapo baadhi, pia, wanaokataa kusikia chochote kuhusu unabii; mbaraka siyo wa tabaka hili. “Na kuyashika yaliyoandikwa humo”—wengi wanakataa kusikia maonyo na mafundisho yaliyomo katika kitabu cha Ufunuo; hakuna hata mmoja anaweza kudai mbaraka ulioahidiwa. Wote wanaodhihaki masomo ya unabii na kufanyia mzaha mifano iliyotolewa kwa umakini mkubwa katika kitabu hiki, wote wanaokataa kufanya matengenezo ya maisha yao na kujiandaa kwa ajili ya ujio wa Mwana wa Adamu, hawatabarikiwa.

Katika kuzingatia ushuhuda wa Uvuvio, watu wanadirikije kufundisha kuwa kitabu cha Ufunuo ni siri ambayo mwanadamu hawezi kuelewa? Kitabu cha Ufunuo ni siri ambayo imefunuliwa, ni kitabu ambacho kimefunuliwa. Mafundisho ya kitabu cha Ufunuo yanaelekeza akili kuchunguza unabii wa Danieli, na vyote viwili huwasilisha mafundisho muhimu sana, ambayo Mungu amempa mwanadamu, kuhusu matukio yanayotarajiwa kutokea wakati wa kufunga kwa historia ya ulimwengu huu.

Yohana alifunuliwa mandhari za kina na zinazosisimua katika uzoefu wa kanisa. Aliona hali, hatari, migogoro, na ukombozi wa mwisho wa watu wa Mungu. Aliandika ujumbe wa mwisho utakaokomaza mavuno ya dunia, ama kama miganda ya nafaka kwa ajili ya ghala la mbinguni au mizigo ya kuni kwa ajili ya mioto ya maangamizi. Masomo ya muhimu sana yalifunuliwa kwake, hususani kwa ajili ya kanisa la siku za mwisho, kuwa wale ambao walitakiwa kuacha makosa na kuukumbatia ukweli walipaswa wafundishwe kuhusu hatari na migogoro iliyokuwa inakuja dhidi yao. Hakuna mtu hata mmoja ambaye anatakiwa kuwa gizani kuhusu kile kinachokuja duniani.

Kwa nini, basi, watu wengi hawajui chochote kuhusu sehemu hii za Maandiko Matakatifu? Kwa nini watu wengi ni wazito kuchunguza mafundisho ya kitabu cha Ufunuo? Ni matokeo ya juhudi kubwa ya mfalme wa giza kuwaficha watu kile ambacho kinafunua uongo wake. Kwa sababu hiyo, Kristo Mfunuaji, akiona kabla vita ambayo ingepigwa dhidi ya mafundisho ya kitabu cha Ufunuo, alitangaza mbaraka kwa watu wote wanaosoma, kusikia, na kuchunguza maneno ya unabii wa kitabu cha Ufunuo.

Sura ya 19 - Nuru Gizani

Kazi ya Mungu duniani inaonesha, kutoka zama moja hadi zama nyingine, kufanana sana katika kila matengenezo makubwa au vuguvugu la kidini. Kanuni za Mungu za kushughulika na watu ni zile zile daima. Matukio muhimu ya sasa yana ufanani na matukio yaliyofanyika wakati uliopita, na uzoefu wa kanisa katika zama zilizopita una masomo yenye thamani kubwa kwa ajili ya wakati wetu.

Hakuna ukweli ambao umefundishwa kwa uwazi mkubwa zaidi katika Biblia kuliko ukweli kuwa Mungu, kwa njia ya Roho Mtakatifu, ana watumishi Wake mahsusi duniani katika vuguvugu kubwa la kupeleka mbele kazi ya wokovu. Watu ni vyombo katika mkono wa Mungu, ambavyo anavitumia kutimiza makusudi Yake ya neema na rehema. Kila mtu ana sehemu ya kufanya; kila mtu anapewa kiasi fulani cha nuru, kinachokidhi mahitaji ya wakati wake, na kinachotosha kumwezesha atekeleze kazi ambayo Mungu amempa aifanye. Lakini hakuna mtu, hata kama amepewa na Mbingu heshima kubwa kiasi gani, ambaye amewahi kuwa na ufahamu kamili wa mpango mkuu wa ukombozi, au hata kuelewa kikamilifu kusudi la Mungu katika kazi kwa ajili ya wakati. Wanadamu hawafahamu kikamilifu kile ambacho Mungu anaweza kukitimiza kupitia kazi ambayo amewapa kuifanya; hawajui, katika vipengele vyake vyote, ujumbe ambao wanautangaza katika jina Lake.

“Je! Wewe waweza kuuvumbua ukuu wa Mungu? Waweza kuufikilia upeo wa huyo Mwenyezi?” “Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.” “Mimi ni Mungu, wala hapana mwingine; mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi; nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado” (Ayubu 11:7; Isaya 55:8, 9; 46:9, 10).

Hata manabii waliopata upendeleo maalumu wa mwangaza maalumu wa Roho hawakuelewa kikamilifu maana ya ufunuo waliopewa. Maana ya ujumbe wao ilipaswa kufunuliwa kizazi hata kizazi, kwa kadiri watu wa Mungu walivyohitaji mafundisho yaliyomo katika ujumbe huo. Petro, akiandika kuhusu wokovu ulioelezwa kupitia injili, anasema kuhusu wokovu huu “manabii walitafuta-tafuta na kuchunguza-chunguza, ambao walitabiri habari za neema itakayowafikia ninyi. Wakatafuta ni wakati upi, na wakati wa namna gani ulioonywa na Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao, ambaye alitangulia kuyashuhudia mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakaokuwako baada ya hayo. Wakafunuliwa ya kuwa si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yenu walihudumu” (1 Petro 1:10-12).

Hata hivyo, ingawa manabii haewakuelewa kila kitu walichofunuliwa, walifanya bidii kubwa kuhakikisha kuwa wanapata nuru yote ambayo Mungu alipenda kuwafunulia. “Walitafuta-tafuta na kuchunguza- chunguza,” “walitafuta, au walichunguza ni aina gani ya

wakati Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao aliridhia." Ni somo kubwa kiasi gani watu wa Mungu wa kizazi cha Kikristo wanapaswa kujifunza, ambao kwa ajili ya faida yao unabii ulitolewa kwa watumishi Wake! "Wakafunuliwa ya kuwa si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yenu walihudumu." Shuhudia wale watu watakatifu wa Mungu wakitafu-tafuta na "kuchuguza-chunguza kwa bidii" kuhusiana na ufunuo waliopewa kwa ajili ya vizazi ambavyo vilikuwa bado havijazaliwa. Hebu angalia tofauti kati ya bidii yao takatifu na uzembe na kutojali ambako watu waliofadhiliwa wa vizazi vya baadaye wanachukulia karama hii ya Mbinguni. Karipio kubwa kiasi gani kwa kutojali kwa watu wanaopenda starehe, wanaopenda ulimwengu ambao wanaridhika kusema kuwa unabii hauwezi kueleweka!

Ingawa akili finyu za wanadamu haziwezi kupenya mashauri ya Yule Asiye na Kikomo, au kuelewa kikamilifu utekelezaji wa makusudi Yake, pamoja na hayo ni kwa sababu ya kosa fulani au kutokujali kwao kunakofanya waelewe kidogo sana ujumbe wa Mbinguni. Siyo mara chache akili za watu, na hata za watu wa Mungu, zinapofushwa na maoni ya wanadamu, mapokeo na mafundisho ya uongo ya wanadamu, kiasi ambacho wanaweza kushika kidogo sana mambo makuu ambayo Mungu ameyafunua katika neno Lake. Hivyo ndivyo wanafunzi wa Kristo walivyokuwa, hata wakati Mwokozi alipokuwa bado yuko pamoja nao kimwili. Akili zao zilikuwa zimegubikwa na dhana iliyokuwa imeenea na kukubaliwa na wengi kuwa Masihi angekuwa mfalme wa kidunia, ambaye angeiinua Israeli juu na kuisimika kwenye kiti cha enzi cha himaya ya ulimwengu wote, na matokeo yake hawakuelewa maana ya maneno Yake yaliyotabiri mateso Yake na kifo Chake.

Kristo Mwenyewe alikuwa amewatuma wakatangaze ujumbe kuwa: "Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili"(Marko 1:15). Ujumbe ule ulikuwa umejengwa juu ya unabii wa Danieli 9. Majuma sitini na mbili yalitangazwa na malaika kuwa yangeishia wakati wa "Masihi Mfalme," na kwa matumaini makubwa na matarajio yenye furaha wanafunzi walingojea uanzishwaji wa ufalme wa Masihi katika jiji la Yerusalemu kuitawala dunia yote.

Walihubiri ujumbe waliopewa na Kristo, japokuwa hata wao wenyewe hawakuelewa maana ya ujumbe waliouhubiri. Wakati mahubiri yao yalikuwa yamejengwa juu ya Danieli 9:25, hawakuona, katika aya inayofuata katika sura hiyo hiyo, kuwa Masihi angekatiliwa mbali. Tangu kuzaliwa kwao mioyo yao ilikuwa imekitwa juu ya utukufu uliotarajiwa wa ufalme wa dunia, na matarajio haya yalipofusha ufahamu wao kuhusu vipengele mbalimbali vya unabii na maneno ya Kristo.

Walitekeleza majukumu yao ya kuwasilisha kwa taifa la Kiyahudi wito wa rehema, na ndipo, wakati waliotarajia kumwona Bwana wao akitawazwa juu ya kiti cha enzi cha Daudi, walimwona akikamatwa kama mhalifu, akipigwa, akidhihakiwa, na akihukumiwa, na akining'inizwa juu ya msalaba wa Kalvari. Ni kukata tamaa na uchungu mkubwa kiasi gani

ulinyonga mioyo ya wanafunzi wale katika kipindi cha siku tatu wakati Bwana wao alipokuwa amelala kaburini!

Kristo alikuja wakati mahsusi na kwa jinsi ilivyotabiriwa katika unabii. Ushuhuda wa Maandiko ulitimizwa katika kila kipengele cha huduma Yake. Alihubiri ujumbe wa wokovu, na"Neno Lake lilikuwa na mamlaka." Mioyo ya wasikilizaji Wake ilishuhudia kuwa ujumbe Wake ulitoka Mbinguni. Utume wa Kiungu wa Kristo ulithibitishwa na Neno na Roho wa Mungu.

Wanafunzi walidumu kumng'ang'ania Bwana wao mpendwa kwa upendo mkubwa. Lakini bado akili zao zilikuwa zimegubikwa na kutokuwa na uhakika na mashaka. Katika uchungu wao hawakuweza kukumbuka maneno ya Kristo yaliyoeleza mateso na mauti Yake. Ikiwa Yesu wa Nazareti alikuwa Masihi kweli, wanafunzi Wake wangetupwa katika huzuni na kukatishwa tamaa kwa kiwango kile? Hili lilikuwa swali lililotesa roho zao wakati Mwokozi alipokuwa amelala katika kaburi Lake wakati wa saa zisizokuwa na matumaini za Sabato iliyokuwa katikati ya kifo na kufufuka Kwake.

Ingawa usiku wa huzuni ulikusanya giza likawazunguka hawa wafuasi wa Yesu, bado hawakuwa wametelekezwa. Nabii anasema: "Nikaapo gizani, Bwana atakuwa nuru kwangu…. Atanileta nje kwenye nuru, nami nitaiona haki yake." "Giza nalo halikufichi kitu, Bali usiku huangaza kama mchana; Giza na mwanga kwako ni sawasawa." Mungu alisema: "Nuru huwazukia wenye adili gizani." "Nitawaleta vipofu kwa njia wasiyoijua; katika mapito wasiyoyajua nitawaongoza; nitafanya giza kuwa nuru mbele yao; na mahali palipopotoka kuwa pamenyoka. Haya nitayatenda, wala sitawaacha" (Mika 7:8, 9; Zaburi 139:12; 112:4; Isaya 42:16).

Tangazo lililotolewa na wanafunzi katika jina la Bwana lilikuwa sahihi katika vipengele vyote, na matukio ambayo tangazo lilihusu yalikuwa yakitendeka wakati huo huo. "Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia," ndiyo ulikuwa ujumbe wao. Mwishoni mwa "wakati"— majuma sitini na tisa ya Danieli 9, ambayo yangeishia wakati wa Masihi, "Mpakwa Mafuta"—Kristo alipokea upako wa Roho baada ya kubatizwa Kwake na Yohana katika mto wa Yordani. Na "ufalme wa Mungu" ambao waliutangaza kuwa umekaribia ulianzishwa kwa kifo cha Kristo.

Ufalme huu haukuwa, kama walivyokuwa wameaaminishwa, ufalme wa duniani. Wala haukuwa ule wa baadaye, ufalme wa milele ambao utasimikwa wakati "ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu;" ufalme ule wa milele, ambao ndani yake "wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii" (Danieli 7:27). Kama ulivyotumika katika Biblia, usemi "ufalme wa Mungu" unatumika kumaanisha ufalme wa neema na ufalme wa utukufu. Ufalme wa neema umeelezwa na Paulo katika Waraka kwa Waebrania. Baada ya kumtaja Kristo, Mwombezi mwenye huruma

ambaye anaguswa na "mambo yetu ya udhaifu," mtume anasema: "Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema" (Waebrania 4:15, 16). Kiti cha neema huwakilisha ufalme wa neema; kuwepo kwa kiti cha neema humaanisha kuwepo kwa ufalme. Katika mingi ya mifano Yake Kristo alitumia usemi "ufalme wa mbinguni" kueleza kazi ya neema ya Mungu katika mioyo ya watu.

Hivyo, kiti cha utukufu huwakilisha ufalme wa utukufu; na ufalme huu umetajwa katika maneno ya Mwokozi: "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake; na mataifa yote watakusanyika mbele zake" (Mathayo 25:31, 32). Ufalme huu ni wa wakati ujao bado. Ufalme wa utukufu hautasimikwa mpaka wakati wa ujio wa pili wa Kristo.

Ufalme wa neema ulianzishwa mara tu baada ya anguko la mwanadamu, wakati mpango ulipobuniwa wa kumkomboa mwanadamu mwenye hatia. Tangu hapo ufalme wa neema uliendelea kuwepo katika kusudi na ahadi ya Mungu; na kwa njia ya imani, wanadamu waliweza kuwa raia wa ufalme huo. Lakini kwa kweli ufalme wa neema haukuanza mpaka kifo cha Kristo kilipotokea. Hata baada ya kuanza utume Wake wa duniani, Mwokozi, ikiwa angechoshwa na ukaidi na utovu wa shukurani wa wanadamu, angeweza kubadilika na kuacha kujitoa kafara pale Kalvari. Akiwa katika Bustani ya Gethsemane kikombe cha mateso kilitetemeka mkononi Mwake. Hata wakati huo angeweza kufuta jasho la damu kutoka katika uso Wake na kuwaacha wanadamu wenye hatia waangamie katika uovu wao. Ikiwa angefanya hivyo, kusingekuwepo ukombozi wa wanadamu walioanguka dhambini. Lakini Mwokozi aliposalimisha uhai Wake na kukata roho, na wakati alipopumua pumzi Yake ya mwisho aliposema kwa sauti kuu, "Imekwisha," hapo ndipo utimilifu wa mpango wa ukombozi ulipothibitishwa kikamilifu. Ahadi ya wokovu iliyotolewa kwa jozi ya wenye dhambi katika bustani ya Edeni ilithibitishwa. Ufalme wa neema, ambao kabla ya hapo ulikuwepo kwa njia ya ahadi ya Mungu, ulisimikwa.

Hivyo basi, kifo cha Kristo—tukio ambalo wanafunzi waliliona kuwa mwisho wa tumaini lao—ndicho kilifanya tumaini lao kuwa la hakika milele. Wakati ambapo kiliwafanya waumie sana na wakate tamaa kuliko kawaida, kilikuwa kilele cha uthibitisho kuwa imani yao ilikuwa sahihi. Tukio ambalo liliwajaza huzuni na kukata tamaa kwingi ndilo lilifungua mlango wa tumaini kwa kila mtoto wa Adamu, na ambalo ni kitovu cha maisha ya baadaye na furaha ya milele ya watu wa Mungu waaminifu katika zama zote.

Makusudi ya rehema ya milele yalikuwa yamefikia utimilifu wake, licha ya wanafunzi kukatishwa tamaa. Pamoja na mioyo yao kuwa imeongolewa na neema ya Mungu na nguvu ya mafundisho Yake, ambaye "aliongea katika namna ambayo hakuna mtu aliyewahi kuongea kama Yeye," lakini dhahabu safi ya upendo wao kwa Yesu, ilichanganyika na madini hafifu ya muunganiko wa kiburi cha kidunia na tamaa za kibinafsi. Hata katika chumba cha Pasaka, wakati wa saa ile muhimu ambapo Bwana wao tayari alikuwa akiingia katika kivuli cha

Gethsemane, kulikuwepo "mashindano miongoni mwao, juu ya nani miongoni mwao alikuwa mkuu kuliko wote" (Luka 22:24). Njozi zao zilijazwa na kiti cha enzi, taji, na utukufu, ilhali mbele yao walikabiliwa na aibu na uchungu wa bustanini Gethsemane, ukumbi wa hukumu, na msalaba wa Kalvari. Ilikuwa kiburi chao cha moyoni, kiu yao ya utukufu wa ulimwenguni, ambavyo viliwafanya wang'ang'anie sana mafundisho ya uongo ya wakati wao, na kushindwa kuelewa maneno ya Yesu yaliyoonesha uhalisia wa ufalme Wake, na yaliyotabiri uchungu Wake na kifo Chake. Na makosa haya yalisababisha majaribu—makali lakini muhimu—yaliyoruhusiwa ili kuwasahihisha. Ingawa wanafunzi hawakuelewa maana ya ujumbe wao, na walishindwa kutambua matarajio yao, pamoja na hayo walihubiri onyo walilopewa na Mungu, na Bwana aliwazawadia kwa imani yao na aliheshimu utii wao. Walikabidhiwa kazi ya kutangaza kwa mataifa yote injili tukufu ya Bwana wao aliyefufuka. Ilikuwa ni kwa kusudi la kuwaandaa kwa ajili ya kazi hii ambapo uzoefu ulioonekana kuwa mchungu kwao uliruhusiwa.

Baada ya ufufuo, Yesu aliwatokea wanafunzi wakiwa njiani kuelekea Emau, na, "akianza na Musa na manabii wote, aliwaeleza kutoka katika Maandiko mambo yote yaliyomhusu Yeye Mwenyewe" (Luka 24:27). Mioyo ya wanafunzi ilisisimuliwa. Imani yao iliwashwa upya. "Walizaliwa upya katika tumaini hai" hata kabla Yesu hajajifunua kwao. Ilikuwa kusudi Lake kuwaangazia ufahamu wao na kuimarisha imani yao katika"neno la uhakika la unabii." Alitamani ukweli uoteshe mizizi yake katika akili zao, sio tu kwa sababu uliungwa mkono na ushuhuda Wake binafsi, bali kwa sababu ya ushahidi usio na maswali uliowasilishwa na mifano na vivuli vya sheria ya kaida, na unabii wa Agano la Kale. Ulihitajika kwa ajili ya wafuasi wa Kristo ili wawe na imani iliyoelimishwa, siyo tu kwa ajili yao wenyewe, bali ili waweze kupeleka elimu ya Injili ya Kristo kwa ulimwengu. Na kama hatua ya kwanza ya kutoa elimu hii, Yesu alielekeza wanafunzi kwa "Musa na manabii wote." Lakini

Badiliko kubwa kiasi gani lilitokea katika mioyo ya wanafunzi walipoona kwa mara nyingine uso mpendwa wa Bwana wao! (Luka 24:32). Katika maana timilifu na kamilifu kuliko hapo awali"walikuwa wamemwona Yeye, ambaye Musa katika torati, na manabii, waliandika." Mashaka, uchungu, kukata tamaa, vilitoweka, na badala yake, uhakika kamili, na imani isiyokuwa na mawingu, vilitawala. Hakuna cha kushangaza kuona kuwa baada ya kupaa Kwake "walidumu katika hekalu, wakimsifu na kumtukuza Mungu." Watu, wakijua tu kifo cha kutisha cha Mwokozi, walitazamia kuona katika nyuso zao mwonekano wa huzuni, kuchanganyikiwa, na kushindwa; lakini waliona furaha na ushindi.

Maandalizi makubwa kiasi gani waliyopewa wanafunzi hawa kwa ajili ya kazi iliyokuwa mbele yao! Walikuwa wamepitia katika majaribu mazito waliyoweza kuyapitia, na waliona jinsi, njozi yao ilivyokuwa imepotea, neno la Mungu lilikuwa limetekelezwa kwa ushindi mkubwa. Kuanzia wakati huo na kuendelea mbele ni kitu gani kingedhoofisha imani yao au kuhafifisha bidii ya upendo wao? Katika huzuni kubwa kabisa walipata "faraja iliyo imara,"

tumaini ambalo lilikuwa kama "nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu" (Waebrania 6:18, 19). Walikuwa mashuhuda wa hekima na mamlaka ya Mungu, na "kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote," kisingeweza kuwatenga na "upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu." "Katika mambo hayo yote," walisema, "tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda" (Warumi 8:38, 39, 37). "Bali Neno la Bwana hudumu hata milele" (1 Petro 1:25). Na "ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea" (Warumi 8:34). Maana ghadhabu zake ni za kitambo kidogo, Katika radhi yake mna uhai.

Bwana asema: "Watu wangu hawatatahayari kamwe" (Yoeli 2:26). "Huenda kilio huja kukaa usiku, Lakini asubuhi huwa furaha" (Zaburi 30:5). Siku ya ufufuo, wakati hawa wanafunzi walipokutana na Mwokozi wao, na mioyo yao ikawaka ndani yao waliposikiliza maneno Yake; wakati walipoona kichwa na mikono na nyayo zilizochubuliwa kwa ajili yao; wakati, kabla ya kupaa Kwake, Yesu alipowaongoza hadi Bethania, na kuinua mikono Yake ili kuwabariki, akawaagiza akisema, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili," akaongeza kusema, "Tazama, niko pamoja nanyi siku zote" (Marko 16:15; Mathayo 28:20); wakati Siku ya Pentekoste Mfariji aliyeahidiwa aliposhuka na nguvu itokayo juu ikatolewa na roho za waumini zikasisimka kwa uwepo halisi wa Bwana wao aliyepaa—ndipo, hata kama, kama njia Yake ilivyokuwa, njia yao iliwaongoza hadi kufikia kujitoa kafara na kufa kifo cha wafia dini, wangeacha huduma ya injili ya neema Yake, pamoja na "taji ya haki" itakayopokelewa wakati wa ujio Wake, na kupokea utukufu wa kiti cha enzi cha kidunia, ambacho kilikuwa tumaini la uanafunzi wao wa awali?

Yeye ambaye "anaweza kufanya mengi zaidi ya vyote tunavyoweza kuomba au kufikiria," aliwapa, pamoja na kushiriki mateso Yake, ushirika wa furaha Yake—furaha ya "kuleta watoto wengi katika utukufu," furaha isiyoelezeka, "uzito wa milele wa utukufu," ambayo, Paulo anaieleza akisema, "mateso yetu mepesi, ambayo ni ya kitambo,""hayawezi kulinganishwa nayo."

Uzoefu wa wanafunzi waliohubiri "injili ya ufalme" wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo, unafanana na uzoefu wa wale waliotangaza ujumbe wa ujio Wake wa pili. Kama vile wanafunzi wa Kristo walivyozunguka wakihubiri kuwa, "Wakati umewadia, ufalme wa Mungu umekaribia," kadhalika Miller na wenzake walitangaza kuwa kipindi kirefu na cha mwisho kinachoelezwa katika Biblia kilikaribia kwisha, kuwa hukumu ilikuwa imekuja, na ufalme wa milele ulikuwa umekaribia kufika. Mahubiri ya wanafunzi kuhusiana na wakati yalijengwa juu ya majuma sabini ya Danieli 9. Ujumbe uliohubiriwa na Miller na wenzake ulitangaza kukoma kwa siku 2300 za Danieli 8:14, ambazo majuma sabini ni sehemu yake. Mahubiri ya kila mmoja yalijengwa juu ya utimizwaji wa sehemu mbalimbali za kipindi

kilekile kirefu cha kiunabii. Kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa Yesu, William Miller na wenzake, nao hawakuelewa kikamilifu maana halisi ya ujumbe walioutangaza. Makosa yaliyojengeka kwa muda mrefu katika kanisa yaliwazuia kufikia tafsiri sahihi ya kipengele muhimu katika unabii. Kwa hiyo, ingawa walitangaza ujumbe ambao Mungu aliwapa waupeleke ulimwenguni, lakini kwa sababu ya kutokuelewa vizuri maana yake walipata uzoefu wa kukatisha tamaa sana.

Katika kufafanua Danieli 8:14,"Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa," Miller, kama ilivyokwisha kuelezwa, alijenga tafsiri yake juu ya fundisho lililoaminiwa na watu wote katika wakati wake kuwa dunia ilikuwa patakatifu, na aliamini kuwa kutakasa patakatifu kuliwakilisha kusafisha dunia kwa moto wakati wa ujio wa Bwana. Kwa hiyo, alipogundua kuwa mwisho wa siku 2300 ulikuwa umebainishwa katika unabii, alihitimisha kuwa unabii huu ulitaja wakati mahsusi wa ujio wa pili. Kosa hili lilitokana na kuamini mtazamo wa watu walio wengi wa wakati wake kuhusu patakatifu ni nini hasa.

Katika mfumo wa mifano, ambayo ilikuwa kivuli cha kafara na ukuhani wa Kristo, utakasaji wa patakatifu ilikuwa huduma ya mwisho iliyofanywa na kuhani mkuu katika mzunguko wa mwaka mzima wa huduma. Ilikuwa ndiyo kazi ya mwisho ya upataisho—uondoshaji wa dhambi kutoka katika Israeli. Ilikuwa mfano wa kazi ya mwisho katika huduma ya Kuhani wetu Mkuu mbinguni, katika kuondoa au kufuta dhambi za watu Wake, zilizoandikwa katika kumbukumbu za mbinguni.

Huduma hii inahusisha kazi ya uchunguzi, kazi ya hukumu; na inatangulia muda mfupi kabla ya ujio wa Kristo katika mawingu ya mbinguni akiwa na nguvu na utukufu mwingi; kwa kuwa anapokuja, kila kesi itakuwa imeamriwa. Yesu alisema: "Ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo" (Ufunuo 22:12). Ni kazi hii ya hukumu, inayotangulia muda mfupi kabla ya ujio wa pili wa Kristo, mbayo inatangazwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14:7: "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja."

Waliotangaza onyo hili walitoa ujumbe sahihi kwa wakati sahihi. Lakini kama wanafunzi wa awali walivyotangaza, "Wakati umewadia, na ufalme umekaribia," kwa kuzingatia unabii wa Danieli 9, wakati walishindwa kuelewa kuwa kifo cha Masihi kilitabiriwa katika andiko hilo hilo, kadhalika Miller na wenzake walihubiri ujumbe wa Danieli 8:14 na Ufunuo 14:7, na walishindwa kuona kuwa kulikuwepo na ujumbe mwingine uliotolewa katika Ufunuo 14, ambao pia ulipaswa kuhubiriwa kabla ya ujio wa Bwana. Kama vile wanafunzi walivyokosea kuhusu ufalme uliopaswa kusimikwa mwishoni mwa majuma sabini, kadhalika Waadventista walikosea kuhusiana na tukio ambalo lilipaswa kutokea mwishoni mwa siku 2300. Katika matukio yote mawili kulikuwepo na kukubali, au kufuata, makosa yaliyokuwepo wakati huo na makosa hayo yalipofusha akili zao wakashindwa kuuona ukweli. Makundi yote mawili

yalitimiza mapenzi ya Mungu kwa kuhubiri ujumbe ambao alitaka uhubiriwe, na makundi yote mawili, kwa kutokuelewa vizuri ujumbe wao, matarajio yao yalikwama.

Lakini Mungu alitimiza kusudi Lake jema la kuruhusu onyo la hukumu litolewe kama lilivyokuwa. Siku kuu ilikuwa karibu, na katika uongozi Wake watu walipimwa kwa mtihani wa wakati mahsusi, ili kuwafunulia kile kilichokuwa mioyoni mwao. Ujumbe ulikusudiwa kulipima na kulisafisha kanisa. Waliongozwa kuona ikiwa upendo wao ulikuwa umeelekezwa kwa ulimwengu huu au kwa Kristo aliyeko mbinguni. Walidai kumpenda Mwokozi; sasa iliwapasa kuthibitisha upendo wao. Je, walikuwa tayari kuachana na matumaini na tamaa za ulimwengu huu, na kukaribisha kwa furaha ujio wa Bwana wao? Ujumbe ulikusudiwa kuwawezesha kutambua hali yao halisi ya kiroho; ulitumwa kuwaamsha wamtafute Bwana kwa toba na kujinyenyekesha.

Kukatishwa tamaa kwao pia, japokuwa kulikuwa ni matokeo ya kutokuelewa vizuri ujumbe ambao waliuhubiri, kulikusudiwa kutumiwe na Mungu kuleta jambo jema. Kungepima mioyo ya wale waliodai kupokea onyo. Katika kukatishwa tamaa kwao wangetupilia mbali uzoefu wao haraka haraka na kuondoa imani yao kwa neno la Mungu au, kwa kuomba na kujinyenyekesha, wangetafuta ili wagundue ni wapi walishindwa kuelewa kiini cha unabii? Ni wangapi walisukumwa na hofu, au mhemko au msisimko? Wangapi walikuwa wamejitoa nusu-nusu na wasioamini? Watu wengi walidai kupenda ujio wa Bwana. Walipotakiwa kustahimili matusi na dharau za ulimwengu, na jaribu la kuchelewa na kukatishwa tamaa, wangeacha imani yao? Kwa kuwa hawakuelewa mara moja jinsi Mungu alivyokuwa akishughulika nao, wangetupilia mbali ukweli uliothibitishwa kwa ushuhuda dhahiri wa neno la Mungu?

Jaribu hili lingefunua nguvu ya wale ambao kwa imani ya kweli walitii kile walichoamini kuwa fundisho la neno na Roho wa Mungu. Lingewafundisha, kwa namna ambayo ni uzoefu kama huo peke yake ungeweza kuwafundisha, hatari ya kupokea na kukubali nadharia na tafsiri za watu, badala ya kuifanya Biblia kujitafsiri yenyewe. Kwa watoto wa imani, mashaka na huzuni iliyotokana na kosa lao ingeleta masahihisho yaliyotakiwa. Wangeongozwa kujifunza kwa maandiko ya kiunabii kwa umakini zaidi. Walijifunza kuchunguza kwa uangalifu zaidi msingi wa imani yao, na kutupilia mbali kila kitu, hata kama kinakubaliwa watu wengi kiasi gani katika ulimwengu wa Kikristo, ambacho hakikujengwa juu ya Maandiko ya ukweli.

Kwa hawa waumini, kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa awali, kile ambacho katika saa ya majaribu kilionekana kuwa giza kwa ufahamu wao baadaye kingeweza kuwa dhahiri. Wakati ambapo wangeona "lengo la Bwana"wangejua kuwa, licha ya jaribu lililotokana na makosa yao, makusudi Yake ya upendo kwao yalikuwa yakitimizwa hatua kwa hatua. Wangejifunza kwa uzoefu uliobarikiwa kuwa Yeye ni "mwenye huruma nyingi, na rehema

tele;” kuwa njia Zake zote “ni za rehema na ukweli kwa wale wanaotunza agano Lake na shuhuda Zake.”

Sura ya 20 - Mwamko Mkuu wa Kidini

Mwamko mkuu wa kidini wakati wa utangazaji wa ujio wa haraka wa Kristo umetabiriwa katika unabii wa ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14. Malaika anaonekana akiruka "katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa." "Kwa sauti kuu" anatangaza ujumbe: "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji" (Aya ya 6, 7). Ukweli kuwa malaika anatajwa kuwa ndiye anayetangaza onyo hili ni wa muhimu. Kwa njia ya usafi, utukufu, na nguvu ya mjumbe wa mbinguni, hekima ya Kiungu iliona vema kuwakilisha tabia iliyoinuliwa ya kazi iliyopaswa kutekelezwa kwa ujumbe na nguvu na utukufu ulioandamana nao. Na urukaji wa malaika "katikati ya mbingu," na "sauti kuu" ambayo kwayo onyo linatolewa, na utangazaji wake kwa wote "wakaao juu ya nchi,"—"kwa kila taifa, na kabila, na lugha na jamaa"—hutoa ushahidi wa uharaka na ueneaji wa vuguvugu hilo ulimwenguni kote.

Ujumbe wenyewe unadokeza kuhusiana na wakati mahsusi ambapo vuguvugu hilo hutokea. Unaelezwa kuwa sehemu ya "injili ya milele;" na unatangaza kuanza kwa hukumu. Ujumbe wa wokovu umehubiriwa katika zama zote; lakini ujumbe huu ni sehemu ya injili ambayo inahubiriwa wakati wa siku za mwisho peke yake, kwani wakati wa mwisho pekee ndiyo unaendana na tamko kuwa saa ya hukumu imekuja. Unabii huwasilisha mfululizo wa matukio yanayoongozana hadi wakati wa kuanza kwa hukumu. Jambo hili ni la kweli hususani katika kitabu cha Danieli. Lakini sehemu ile ya unabii wake unaohusiana na siku za mwisho, Danieli aliagizwa kuufunga na kuutia muhuri "hata wakati wa mwisho." Ni mpaka tufikie wakati huu ndipo ujumbe kuhusiana na hukumu ungehubiriwa, ukiwa umejengwa juu ya utimizwaji wa unabii huu. Lakini wakati wa mwisho, nabii anasema, "wengi watakimbia huko na huko, na maarifa yataongozeka" (Danieli 12:4).

Mtume Paulo alilionya kanisa lisitazamie ujio wa Kristo katika siku zake. "Siku ile haiji," anasema, "usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu" (2 Wathesalonike 2:3). Mpaka baada ya uasi mkuu, na kipindi kirefu cha utawala wa "mtu wa kuasi," ndipo pekee tunaweza kutazamia ujio wa pili wa Bwana. "Mtu wa kuasi," ambaye pia anajulikana kama "siri ya uasi," "mwana wa uharibifu," na "yule mwovu," huwakilisha upapa, ambao, kama ulivyotabiriwa katika unabii, ulipaswa kudumu kuwa mamlaka yenye nguvu kwa miaka 1260. Kipindi hicho kilikomea mwaka 1798. Ujio wa Kristo usingetokea kabla ya wakati huo. Paulo anaelezea kwa tahadhari kipindi chote cha Ukristo hadi mwaka 1798.

Upande huu wa wakati huo ambapo ujumbe wa ujio wa Kristo unapaswa kuhubiriwa. Hakuna ujumbe kama huo uliowahi kuhubiriwa katika zama zilizopita. Paulo, kama tulivyokwisha kuona, hakuhubiri ujumbe huo; aliwaelekeza ndugu zake kwa wakati ujao

uliokuwa bado mbali wa ujio wa Bwana. Wanamatengenezo hawakuhubiri ujumbe huo. Martin Luther aliweka siku ya hukumu kama miaka mia tatu katika wakati ujao tangu wakati wake. Lakini tangu mwaka 1798 kitabu cha Danieli kilifunguliwa, maarifa ya unabii yameongezeka, na wengi wamehubiri ujumbe mkuu wa ukaribu wa hukumu.

Kama ilivyokuwa kwa Matengenezo ya karne ya kumi na sita, vuguvugu la ujio wa pili lilitokea katika nchi tofauti za Ukristo. Katika nchi za Ulaya na Amerika watu wa imani na maombi waliongozwa kujifunza unabii, na, wakifuatilia kumbukumbu ya Maandiko yaliyovuvia, waliona ushahidi unaoshawishi kuwa mwisho wa mambo yote ulikuwa karibu. Katika nchi tofauti kulikuwepo hapa na pale makundi ya Wakristo ambao, kwa kujifunza Maandiko peke yake, walijenga imani kuwa ujio wa Mwokozi ulikuwa karibu. Mwaka 1821, miaka mitatu baada ya Miller kufikia ufafanuzi wake wa unabii ulioonesha wakati wa hukumu, Dkt. Joseph Wolff, "mmishenari kwa ulimwengu," alianza kutangaza ujio wa Bwana wa haraka. Wolff alizaliwa katika nchi ya Ujerumani, wazazi wake walikuwa Wayahudi, na baba yake alikuwa rabi wa Kiyahudi. Akiwa bado mdogo aliuamini ukweli wa dini ya Kikristo. Akiwa na akili inayojishughulisha, inayohoji, alikuwa msikilizaji makini wa maongezi yaliyofanyika katika nyumba ya baba yao kama Waebrania wacha Mungu wakisimulia matumaini na matarajio ya taifa lao, utukufu wa Masihi ajaye, na urejeshwaji wa Israeli. Siku moja aliposikia Yesu wa Nazareti akitajwa, kijana aliuliza akitaka kujua Yesu wa Nazareti alikuwa nani hasa.

"Alikuwa Myahudi mwenye talanta kubwa sana," ndilo lilikuwa jibu; "lakini alipojifanya kuwa Masihi, mahakama ya Kiyahudi ilimhukumu kifo." "Kwa nini," aliongeza swali, "Yerusalemu iliangamizwa, na kwa nini tupo utumwani?" "Ala, ala!" baba yake alijibu, "kwa sababu Wayahudi waliwaua manabii." Wazo lilijengeka mara moja kwa mtoto: "Labda Yesu pia alikuwa nabii, na Wayahudi walimwua wakati alikuwa hana hatia."— Travels and Adventures of the Rev. Joseph Wolff, vol. 1, uk. 6. Hisia zilikuwa kali sana kiasi kwamba, ingawa alikatazwa kuingia katika Kanisa la Kikristo, alikaa nje ya kanisa kusikiliza mahubiri.

Alipokuwa tu miaka saba alikuwa akitamba mbele ya jirani Mkristo mzee juu ya ushindi ujao wa Israeli wakati wa ujio wa Masihi, ambapo mzee alisema kwa utulivu: "Kijana mpendwa, nitakuambia Masihi wa kweli alikuwa nani: Alikuwa Yesu wa Nazareti, ... ambaye mababu zenu walimsulubisha, kama walivyowaua manabii wa zamani. Nenda nyumbani kasome Sura ya hamsini na tatu ya Isaya, na utashawishika kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu."—Ibid., vol. 1, uk. 7. Imani ilijengeka mara moja. Alienda nyumbani na kusoma maandiko, akiwa na shauku ya kuona jinsi maandiko yalivyotimia kikamilifu kupitia kwa Yesu wa Nazareti. Inawezekana kuwa maneno ya Mkristo yakawa ya kweli? Kijana alimwuliza baba yake ampe maelezo ya unabii, lakini alikutana na ukimya uliokuwa na hasira nyingi kiasi kwamba hakurudia tena kuzungumzia suala hilo siku zilizofuata. Lakini jambo hili, hata hivyo, liliongeza shauku yake ya kutaka kujua zaidi kuhusu dini ya Kikristo.

Maarifa aliyoyatafuta yalifichwa kwa makini katika nyumba yake ya Kiyahudi; lakini, alipofika umri wa miaka kumi na moja, aliondoka nyumbani kwa baba yake na kwenda ulimwenguni kujipatia elimu, kuchagua dini yake mwenyewe na kazi yake ya maisha. Alikaribishwa kwa muda kuishi na jamaa zake wa karibu, lakini muda si mrefu alifukuzwa kutoka kwao kama mtu mwasi, na akiwa mpweke na bila pesa alilazimika kwenda kuishi miongoni mwa watu asiowajua. Alitangatanga huku na huko, akijifunza kwa bidii na kujipatia kipato kwa kufundisha Kiebrania.

Kwa njia ya msaada wa mwalimu wa Kikatoliki aliongozwa kupokea imani ya Kirumi na alikusudia kuwa mmishenari kwa watu wake. Akiwa na kusudi hili, miaka michache baadaye, alienda kusoma katika Chuo cha Propaganda cha Rumi. Hapa, tabia yake ya mawazo huru na usemaji wa wazi vilimpa sifa mbaya ya uzushi. Alishambulia wazi wazi makosa ya kanisa na kudai umuhimu wa matengenezo. Ingawa mwanzoni alishughulikiwa kwa upendeleo na viongozi wa kipapa, baada ya muda si mrefu alifukuzwa Rumi. Chini ya ufuatiliwaji wa kanisa alihama kutoka mahali kwenda mahali kwingine, mpaka ilipothibitika kuwa asingewezekana kujisalimisha kwa utumwa wa Urumi. Alitangazwa kuwa mtu asiyewezekana aliachwa aende kokote alikopenda kwenda. Sasa alisafiri kwenda Uingereza na, akitangaza kuwa na imani ya Kiprotestanti, alijiunga na Kanisa la Kianglikana. Baada ya mafunzo ya miaka miwili aliondoka, mwaka 1821, na kwenda katika kazi yake ya umishenari.

Wakati ambapoWolff aliupokea ukweli mkuu wa ujio wa kwanza wa Kristo kama “Mtu wa huzuni, ajuaye sikitiko,” aliona kuwa unabii unafunua kwa uwazi ule ule ujio Wake wa pili katika nguvu na utukufu. Na wakati akitafuta kuwaongoza watu wake kwa Yesu wa Nazareti kama Yeye aliyeahidiwa, na kuwaonesha ujio Wake wa kwanza katika hali ya unyenyekevu kama kafara ya dhambi za wanadamu, aliwafundisha pia kuhusu ujio Wake wa pili kama mfalme na mkombozi.

“Yesu wa Nazareti, Masihi wa kweli,” alisema, “ambaye mikono na nyayo Zake zilitobolewa, aliyepelekwa kama mwakondoo apelekwavyo machinjioni, aliyekuwa Mtu mwenye huzuni ajuaye sikitiko, ambaye baada ya fimbo ya ufalme kuondolewa kwa Yuda, na nguvu ya utungaji wa sheria kuondolewa kutoka katikati ya nyayo zake, alikuja kwa mara ya kwanza; atakuja kwa mara ya pili katika mawingu ya mbinguni, pamoja na tarumbeta ya Malaika Mkuu”(Joseph Wolff, Researches and Missionary Labors, ukurasa 62) “na atasimama juu ya Mlima wa Mizeituni; na kwamba utawala, ambao wakati mmoja alipewa Adamu juu ya uumbaji, halafu akanyang’anywa (Mwanzo 1:26; 3:17), atapewa Yesu. Atakuwa mfalme juu ya dunia yote.

Maumivu na maombolezo ya viumbe yatakoma, bali nyimbo za sifa na shukurani zitasikika. Wakati Yesu anapokuja katika utukufu wa Baba Yake, pamoja na malaika watakatifu,. waaminio waliokufa watafufuka kwanza (1Wathesalonike 4:16; 1 Wakorintho 15:23). Huu ndio ambao sisi Wakristo tunauita ufufuo wa kwanza. Ndipo ufalme wa wanyama

utabadilisha silika yake (Isaya 11:6-9), na kusalimishwa kwa Yesu (Zaburi 8). Amani itatawala katika Ulimwengu wote."—Journal of the Rev. Joseph Wolff, kurasa 378, 379. "Bwana tena ataitazama dunia, na kusema, 'Tazama, ni njema sana.'"— Ibid., ukurasa 294.

Wolff aliamini ujio wa Bwana ulikuwa karibu, tafsiri yake ya vipindi vya kiunabii ikiweka hitimisho kuu hilo ndani ya miaka michache sana ya muda ulioelezwa na Miller. Kwa wale waliodai kutoka katika Maandiko, "Kuhusu siku na saa ile hakuna ajuaye," kwamba watu hawapaswi kujua chochote kuhusu ukaribu wa ujio Wake wa pili, Wolff alijibu: "Kwani Bwana wetu alisema kuwa siku na saa ile haitajulikana kamwe? Kwani hakutueleza dalili za nyakati, zitusaidie kujua angalau ukaribu wa ujio Wake, kama vile mtu anavyojua ukaribu wa msimu wa kiangazi kwa mtini kupukutisha majani yake? (Mathayo 24:32).

Je hatupaswi kamwe kujua kuwa kipindi kile, wakati Yeye Mwenyewe alituhimiza siyo tu kusoma kitabu cha nabii Danieli, bali pia kukielewa? Na katika kitabu hicho hicho cha Danieli, ambacho kinasema kuwa maneno yake yalifungwa mpaka wakati wa mwisho (ambapo ufungwaji wa maneno yake ulikuwa kwa wakati wa Danieli), na kuwa 'wengi wataenda huko na huko' (usemi wa lugha ya Kiebrania kwa ajili ya kuchunguza na kufikiri juu ya wakati), 'na maarifa' (kuhusu wakati) 'yataongezeka' (Danieli 12:4). Kando ya hili, Bwana wetu hakusudii kusema kwa kauli hii, kuwa ukaribu wa wakati hautajulikana, bali kuwa 'siku na saa mahsusi hakuna mtu ajuaye.' Inatosha, Yesu alisema, kuwa itajulikana kwa dalili za nyakati, kutuhimiza tujiandae kwa ajili ya ujio Wake, kama Nuhu alivyoandaa safina."—Wolff, Researches and Missionary Labors, ukurasa 404, 405.

Kuhusu mfumo maarufu wa kutafsiri, au kukosea kutafsiri Maandiko, Wolff aliandika: "Sehemu kubwa ya kanisa la Kikristo wameacha maana ya wazi ya Maandiko, na wamegeukia mfumo wa kufikirika wa Wabudha, wanaoamini kuwa furaha ya baadaye ya wanadamu itatokana na kutembea tembea hewani, na kudhani kuwa palipoandikwa Wayahudi ni lazima wapaelewe kumaanisha Mataifa; na wanaposoma Yerusalemu ni lazima wapafahamu kama kanisa; na ikiwa imesemwa nchi, inamaanisha anga; na kwa ajili ya ujio wa Bwana ni lazima wafahamu maendeleo ya vyama vya wamishenari; na kwenda juu ya mlima wa nyumba ya Bwana, humaanisha tabaka kubwa linalokutana na Wamethodisti."—Journal of the Rev. Joseph Wolff, ukurasa 96.

Kwa kipindi cha miaka ishirini na nne tangu 1821 hadi 1845, Wolff alisafiri sana: katika Bara la Afrika, alitembelea Misri na Ethiopia; katika Bara la Asia alizunguka katika nchi za Palestina, Siria, Uajemi, Bokhara, na India. Alitembelea pia Marekani, akiwa safarini kuelekea huko alihubiri katika kisiwa cha Mtakatifu Helena. Alifika New York mwezi wa Agosti, 1837; na, baada ya kuhubiri katika jiji lile, alihubiri katika jiji la Philadelphia na Baltimore, na mwisho alikwenda katika jiji la Washington. Hapa, alisema, "kwa njia ya hoja iliyotolewa na Rais mstaafu, John Quincy Adams, katika moja ya vikao vya Kongresi, Bunge lilipitisha kwa kauli moja azimio la kunipatia ukumbi wa Bunge la Kongresi kwa ajili yangu

mimi kutoa mhadhara, ambao niliutoa siku ya Jumamosi, nikiheshimiwa kwa uwepo wa wabunge wote wa Kongresi, na pia kwa uwepo wa askofu wa Virginia, na uwepo wa viongozi wa dini na wakazi wa jiji la Washington. Heshima hiyo hiyo nilipewa na maofisa wa serikali wa majimbo ya New Jersey na Pennsylvania, ambapo na wao wakiwepo niliwasilisha mihadhara juu ya utafiti wangu nilioufanya katika Bara la Asia, na pia juu ya utawala binafsi wa Yesu Kristo."—Ibid., ukurasa 398, 399.

Dkt. Wolff alisafiri katika nchi za watu katili sana bila ulinzi wa serikali yo yote ya Ulaya, akistahimili shida nyingi na akiwa amezungukwa na hatari zisizokuwa na idadi. Aliteswa kwa kupigwa viboko kwenye visigino na kunyimwa chakula, aliuzwa kama mtumwa, na mara tatu alihukumiwa kifo. Alishambuliwa na majambazi, na mara kadhaa alikuwa karibu kufa kwa sababu ya kiu. Mara moja alinyang'anywa kila kitu alichokuwa nacho na aliachwa kutembea kwa miguu umbali mamia ya maili katika milima, barafu ikimpiga usoni na miguu yake isiyokuwa na viatu ikipoteza hisia kwa kukanyaga ardhi iliyoganda.

Alipoonywa dhidi ya kwenda kwake bila silaha miongoni mwa makabila katili na pinzani, alisema kuwa "alikuwa na silaha"—"maombi, juhudi kwa ajili ya Kristo, na uhakika wa kupata msaada wa Mungu."“Mimi pia," alisema, "nina upendo kwa Mungu na kwa jirani yangu katika moyo wangu, na Biblia ipo mikononi mwangu."—W.H.D. Adams, In Perils Oft, ukurasa 192. Alibeba Biblia ya Kiebrania na Kiingereza kila alipokwenda. Kuhusiana na moja ya safari zake alisema: "Nilidumu kuwa na Biblia iliyo wazi mikononi mwangu. Nilihisi kuwa nguvu yangu ilikuwa katika Kitabu, na kuwa nguvu ya Kitabu ilinipatia nguvu ya kusonga mbele."—Ibid., ukurasa 201.

Alidumu kushiriki katika kazi yake mpaka ujumbe wa hukumu ulipopelekwa katika sehemu kubwa ya dunia iliyokaliwa na wakati huo. Miongoni mwa Wayahudi, Waturuki Waparsi, Wahindu, na kwa watu wengine wengi wa mataifa na makabila mengine alihubiri neno la Mungu katika lugha mbalimbali na kila mahali alitangaza ukaribu wa Masihi.

Katika safari zake katika nchi ya Bokhara alikuta fundisho la ujio wa karibu wa Bwana likishikiliwa na watu walioishi mbali na miji katika maeneo ya vijijini. Waarabu wa Yemeni, alisema, "wana kitabu kinachoitwa Seera, ambacho kinatoa tangazo la ujio wa pili wa Kristo na utawala Wake wa utukufu; na wanatarajia matukio makubwa yatokee katika mwaka 1840."— Journal of the Rev. Joseph Wolff, ukurasa 377. "Katika nchi ya Yemeni... nilitumia siku sita nikiwa na watoto wa Rekabu. Hawanywi pombe, hawalimi mizabibu, hawapandi mbegu, na wanaishi katika mahema, na wanamkumbuka mzee mwema Yonadabu, mwana wa Rekabu; na nilikuta miongoni mwao wana wa Israeli, wa kabila ya Dani, ... wanaotarajia, pamoja na wana wa Rekabu, ujio wa haraka wa Masihi katika mawingu ya mbinguni."—Ibid., ukurasa 389.

Imani kama hiyo ilikutwa na mmishenari mwingine katika eneo la Tataria. Padri wa Kitataria alimwuliza mmishenari kuhusiana na lini Kristo angerudi mara ya pili. Mmishenari alipojibu kuwa hakujua chochote kuhusiana na lini Kristo angerudi, padri alishangaa sana kuhusiana na ujinga huo kwa mtu ambaye alidai kuwa mwalimu wa Biblia, na alieleza imani yake binafsi, iliyojengwa juu ya unabii, kuwa Kristo angekuja takribani mwaka 1844.

Takribani mwanzoni mwa mwaka 1826 ujumbe wa ujio wa pili ulianza kuhubiriwa katika nchi ya Uingereza. Vuguvugu halikukua sana kama ilivyokuwa katika Bara la Amerika; wakati mahsusi wa ujio wa pili kwa jumla haukufundishwa, lakini ukweli mkuu wa ujio wa haraka wa Kristo katika nguvu na utukufu ulitangazwa maeneo mengi sana. Na ulitangazwa siyo miongoni mwa wapinzani au waungaji mkono peke yao. Mourant Brock, mwandishi wa Kiingereza, anasema kuwa takribani wachungaji mia saba wa Kanisa la Anglikana walijishughulisha na kuhubiri "injili hii ya ufalme." Ujumbe unaoeleza mwaka 1844 kama wakati wa kurudi kwa Bwana ulitolewa katika Uingereza Kuu. Machapisho ya Kiadventista kutoka Marekani yalisambazwa maeneo mengi sana. Vitabu na majarida vilichapishwa Uingereza. Na mwaka 1842 Robert Winter, Mwingereza kwa kuzaliwa, aliyekuwa amepokea imani ya marejeo katika Bara ya Amerika, alirudi katika nchi yake alikozaliwa kutangaza ujio wa Bwana. Wengi waliungana naye katika kazi, na ujumbe wa hukumu ulitangazwa katika sehemu mbalimbali na Uingereza.

Katika Amerika ya Kusini, katikati ya ukatili na udanganyifu wa kidini, Lakunza, Mhispinia na Mjesuti, alijifunza Maandiko na kwa njia hiyo alipokea ukweli wa marejeo ya haraka ya Kristo. Akisukumwa kutoa onyo, lakini akitamani kuepuka makaripio ya Rumi, alichapisha mawazo yake kwa kutumia jina tofauti na lake la "Rabbi Ben-Ezra," akijifanya kuwa Myahudi aliyeongoka. Lakunza aliishi katika karne ya kumi na nane, lakini ilikuwa takribani mwaka 1825 ambapo kitabu chake, ambacho baada ya kufika London, kilitafsiriwa katika lugha ya Kiingereza. Kuchapishwa kwake kulisaidia kukuza shauku iliyokuwa ikiamka katika nchi ya Uingereza kuhusu mada ya ujio wa pili wa Kristo.

Katika nchi ya Ujerumani fundisho hili lilifundishwa katika karne ya kumi na nane na Bengeli, mchungaji wa Kanisa la Lutherani na msomi mashuhuri na mkosoaji wa Biblia. Baada ya kuhitimu elimu yake, Bengeli"alijikita katika kujifunza teolojia, ambayo uwezo wake mkubwa wa kiakili na wa kidini uliokuzwa na mafunzo na nidhamu yake ya awali, vilimwongoza kufanya. Kama vijana wengine wenye tabia ya kutafakari mambo kwa kina, kabla na tangu hapo, alianza kupambana na mashaka na matatizo ya asili ya kidini, na anagusia, kwa hisia kubwa, 'mishale mingi ambayo ilichoma moyo wake, na kusababisha ugumu katika maisha ya ujana wake.'" Akiwa mjumbe wa Baraza la Kanisa la Wurttemberg, alitetea uhuru wa dini. "Huku akidumisha haki na fursa za kanisa, alikuwa mtetezi wa uhuru wa msingi uliotolewa kwa wale waliohisi kuwa wamefungwa, kwa misingi ya dhamiri, kujitoa katika ushirika wa kanisa."—Encyclopaedia Britannica, 9th ed., art. "Bengel." Athari chanya za sera hii bado zinahisiwa katika jimbo lake la kuzaliwa.

Ilikuwa wakati akihubiri kutoka Ufunuo 21 kwa ajili ya Jumapili ya majilio ambapo nuru ya ujio wa pili wa Kristo ilimulika katika akili ya Bengeli. Unabii wa Ufunuo ulifunuliwa katika ufahamu wake zaidi kuliko hapo awali. Akiwa amegubikwa na hisia ya umuhimu wa kushangaza na utukufu mwingi wa matukio yaliyowasilishwa na nabii, alilazimishwa kuacha kwa muda kutafakari juu ya mada hiyo. Katika mimbari lilijitokeza tena kwa uwazi wake wote na nguvu zake zote. Tangu wakati huo alielekeza nguvu zake zote katika kujifunza unabii, hususani ule uliohusu kitabu cha Ufunuo, na kwa muda mfupi alifikia hatima ya kuamini kuwa ulielezea juu ya ujio wa karibu wa Kristo. Tarehe aliyoiweka kama wakati wa ujio wa pili wa Kristo ilikuwa ndani ya miaka michache baada ya ile iliyowekwa na Miller.

Maandishi ya Bengeli yalisambazwa katika ulimwengu wote wa Kikristo. Mawazo yake ya unabii yalipokelewa kwa jumla katika jimbo lake la Wurttemberg, na kwa kiasi fulani katika maeneo mengi ya Ujerumani. Vuguvugu liliendelea baada ya kifo chake, na ujumbe wa marejeo ulisikika katika nchi ya Ujerumani kwa wakati huo huo ulipokuwa ukipata mvuto katika nchi zingine. Tarehe za mwanzoni baadhi ya waumini walienda Urusi na kule waliunda makoloni, na imani ya ujio wa haraka wa Kristo bado inashikiliwa na makanisa ya Ujerumani katika nchi ya Urusi.

Nuru iliangaza pia katika nchi ya Ufaransa na Uswisi. Katika jiji la Geneva ambapo Fareli na Kalvini walieneza ukweli wa Matengenezo, Gaussen alihubiri ujumbe wa ujio wa pili. Wakati akiwa mwanafunzi shuleni, Gaussen alikutana na roho ya mantiki iliyoenea katika nchi zote za Ulaya katika sehemu ya mwisho ya karne ya kumi na nane na sehemu ya mwanzo wa karne ya kumi na tisa; na alipojiunga na uchungaji alikuwa haelewi imani ya kweli, bali alikuwa na mwelekeo wa kutokuwa na imani. Katika ujana wake alipata shauku ya kujifunza unabii. Baada ya kusoma kitabu cha Rollin’s Ancient History, fikra zake zilielekezwa katika Sura ya pili ya Danieli, na aliguswa na usahihi wa kushangaza wa unabii uliotimizwa, kama ulivyoonekana katika kumbukumbu za kihistoria.

Hapa kulikuwa na ushuhuda wa uvuvio wa Maandiko, uliotumika kama nanga kwake katikati ya hatari za miaka ya baadaye. Hakuridhishwa na mafundisho ya mantiki, na katika kujifunza Biblia na kutafuta nuru kubwa, baada ya muda, aliongozwa kujenga imani chanya. Alipokuwa akifanya utafiti wake wa unabii alifikia hatua ya kuwa na imani kuwa ujio wa Bwana ulikuwa umekaribia. Kwa kuguswa na utukufu na umuhimu wa ukweli huu mkuu, alitamani kuuleta mbele ya watu; lakini imani iliyozoeleka kuwa unabii wa Danieli ni siri na hauwezi kueleweka kilikuwa kikwazo kikubwa katika njia yake. Hatimaye aliazimia—kama Fareli alivyofanya kabla yake katika kuihubiri Geneva—kuanza na watoto, kupitia kwao alitumaini kuwafurahisha wazazi wake.

“Natamani kueleweka,”alisema baadaye, akizungumzia lengo lake katika kazi hii, “siyo kwa sababu ya umuhimu wake mdogo, lakini kinyume chake, kwa sababu ya thamani yake kubwa, kwamba nilitamani kuuwasilisha katika muundo wake unaoeleweka, na kwamba

niliuwasilisha kwa watoto kwanza. Nilitamani kusikiwa, na niliogopa nisingesikiwa ikiwa ningeanza na watu wazima kwanza." "Niliazimia, hivyo basi, niwaendee watoto wadogo kwanza. Nilikusanya wasikilizaji ambao ni watoto wadogo; ikiwa kundi likiongozeka, ikiwa inaonekana kuwa wanasikiliza, wamefurahishwa, wanatamani, kuwa wanafahamu na kueleza mada, nina hakika ya kuwa na duara la pili, na katika zamu yao, watu wazima wataona kuwa ni muhimu kutumia muda wao kukaa chini na kujifunza. Jambo hili likitendeka, kazi itakuwa imekamilika."—L. Gaussen, Daniel the Prophet, vol. 2, Preface.

Juhudi zilifanikiwa. Alipowafundisha watoto, watu wazima walikuja kusikiliza. Korido za kanisa lake zilijaa wasikilizaji wenye usikivu mzuri. Miongoni mwao walikuwemo watu wenye vyeo na wasomi, na wageni na wasafiri kutoka nchi za nje waliotembelea jiji la Geneva; na hivyo ujumbe ulipelekwa sehemu zingine.

Kwa kutiwa moyo na mafanikio haya, Gaussen alichapisha masomo yake, kwa matumaini ya kuhamasisha ujifunzaji wa vitabu vya unabii katika makanisa ya watu wanaoongea Kifaransa. "Kuchapisha mafundisho yanayotolewa kwa watoto," Gaussen alisema, "ni kuwaambia watu wazima, ambao mara nyingi pia hupuuza vitabu kama hivyo kwa kisingizio cha uongo kuwa havieleweki, 'Vinawezaje kutoeleweka, wakati watoto wenu wanavielewa?'" "Nilikuwa na shauku kubwa," aliongeza, "ya kutoa elimu ya unabii unaopendwa na watu wetu, kama ikiwezekana." "Hakuna ujifunzaji, kwa kweli, ambao unaonekana kwangu kuwa unakidhi mahitaji zaidi." "Ni kwa sababu ya jambo hili ambalo kwalo inatupasa kujiandaa kwa ajili ya mateso yaliyo karibu, na kukesha na kumngoja Yesu Kristo."

Ingawa alikuwa mmoja wa wahubiri mashuhuri na waliokuwa wanapendwa katika lugha ya Kifaransa, Gaussen baada ya muda mfupi aliondolewa katika uchungaji, kosa lake kubwa likiwa kwamba badala ya katekisimu ya kanisa, mwongozo baridi na razini, unaokaribia kukosa kabisa imani chanya, alikuwa anatumia Biblia kuwafundisha vijana. Baadaye alifanya kazi ya kufundisha katika shule ya theolojia, wakati huo huo siku ya Jumapili aliendelea na kazi yake kama katekista, akiongea na watoto na kuwafundisha Maandiko. Kazi yake kuhusu unabii iliamsha shauku kubwa. Kutoka katika kiti cha profesa, kwa njia ya mitambo ya uchapishaji, na katika kazi yake aliyoipenda kama mwalimu wa watoto aliendelea kwa miaka mingi kuwa na mvuto mkubwa na mwezeshaji katika kujifunza unabii ulioonesha kuwa ujio wa Bwana ulikuwa karibu.

Katika nchi ya Scandinavia pia ujumbe wa marejeo ulitangazwa, na shauku ya watu mahali pengi iliamshwa. Wengi waliamshwa kutoka katika hali yao ya kutojali usalama wao wakaungama na kuziacha dhambi zao, na waliomba msamaha katika jina la Kristo. Lakini viongozi wa kanisa la dola walipinga vuguvugu, na kwa njia ya mvuto wao baadhi ya waliohubiri ujumbe walitupwa gerezani. Katika maeneo mengi ambapo wahubiri wa ujio wa haraka wa Bwana walinyamazishwa, Mungu alipendezwa kutuma ujumbe, kwa njia ya

kimuujiza, kupitia watoto wadogo. Kwa kuwa walikuwa na umri mdogo, sheria ya nchi isingewazuia, na waliruhusiwa kusema bila kubughudhiwa.

Vuguvugu lilikuwa zaidi miongoni mwa watu wa tabaka la watu wa chini, na lilipamba moto katika nyumba za kawaida za vibarua ambamo watu walikusanyika kusikiliza onyo. Wahubiri watoto wenyewe walikuwa maskini wakazi wa vibanda hivyo. Baadhi yao walikuwa na umri usiozidi miaka sita au nane; na wakati ambapo maisha yao yalishuhudia kuwa walimpenda Mwokozi, na walijaribu kuishi maisha ya utii kwa matakwa matakatifu ya Mungu, wakionesha akili na uwezo wa kawaida tu ambao huonekana kwa watoto wa umri huo. Waliposimama mbele ya watu, hata hivyo, ilishuhudiwa kuwa walisukumwa na nguvu iliyokuwa kubwa zaidi ya karama zao za asili. Mwelekeo na tabia vilibadilika, na kwa nguvu kubwa walitoa onyo la hukumu, wakitumia maneno mahsusi ya Maandiko: "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja." Walikemea dhambi za watu, siyo tu kwa kushutumu ufisadi na uovu, bali pia kwa kukemea kuipenda dunia na kurudi nyuma kiroho, na wakiwaonya wasikilizaji wao wafanye haraka kuikimbia hasira inayokuja.

Watu walisikiliza kwa kutetemeka. Roho wa Mungu anayeshawishi aliongea na mioyo yao. Wengi waliongozwa kuchunguza Maandiko kwa shauku mpya na ya kina, wasio na kiasi na wasio waadilifu walifanya matengenezo, wengine waliacha matendo yao ya dhuluma, na kazi ilifanyika kwa namna ambayo hata wachungaji wa kanisa la dola walilazimika kukiri kuwa mkono wa Mungu ulikuwa katika vuguvugu hilo.

Ilikuwa mapenzi ya Mungu kuwa habari za ujio wa Mwokozi zihubiriwe katika nchi za Skandinavia; na sauti za watumishi Wake ziliponyamazishwa, Mungu aliweka Roho Wake juu ya watoto, ili kwamba kazi itekelezwe. Yesu alipokuwa karibu na Yerusalemu akikaribishwa na makundi ya watu wenye furaha kuwa, kwa kelele za ushindi na upeperushaji wa matawi ya mitende, walimtangaza kama Mwana wa Daudi, Mafarisayo na Masadukayo walimwagiza awanyamazishe; lakini Yesu aliwajibu kuwa yote yale yalikuwa hivyo ili kutimiza unabii, na ikiwa hawa watanyamaza, mawe yatapiga kelele.

Watu, wakiwa wametishiwa kwa vitisho vya makuhani na watawala, walisitisha utangazaji wao wa furaha walipokuwa wakiingia malango ya Yerusalemu; lakini watoto katika ukumbi wa hekalu baadaye walilidaka pambio hilo, na, wakipeperusha matawi yao ya mitende, walipiga kelele: "Hosana Mwana wa Daudi!" (Mathayo 21:8-16). Mafarisayo, wakiwa wamechukizwa sana, walimwambia Yesu, "Wasikia hawa wasemavyo?" Yesu alijibu, "Naam; hamkupata kusoma, Kwa vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao umekamilisha sifa?" Mungu alitekeleza kwa njia ya watoto wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo, kadhalika aliwatumia watoto kutoa ujumbe wa ujio wa pili wa Kristo. Neno la Mungu inapasa litimizwe, kuwa utangazaji wa ujio wa Mwokozi ilipaswa utolewe kwa kila jamaa, lugha, na kabila za watu.

Kwa William Miller na washirika wake lilitolewa agizo la kuhubiri onyo kwa watu wa Amerika. Nchi ya Marekani ilikuja kuwa kitovu vuguvugu kuu la marejeo. Ilikuwa hapa ambapo unabii wa ujumbe wa malaika wa kwanza ulipata utimizwaji wake wa moja kwa moja. Maandishi ya Miller na wenzake yalisambazwa hadi nchi za mbali. Kila mahali ambapo wamishenari walipenya mahali pote ulimwenguni, ilipelekwa habari njema ya marejeo ya haraka ya Kristo. Maeneo ya mbali na mengi ulienea ujumbe wa injili ya milele: "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja."

Ushuhuda wa unabii ulioonekana kueleza kuwa ujio wa Kristo katika msimu wa masika wa mwaka 1844 ulishika akili za watu. Ujumbe ulipoenea kutoka jimbo moja hadi jimbo, kila mahali kulikuwepo mwamko mkubwa kwa watu wengi. Wengi walishawishika kuwa hoja zilizotokana na vipindi vya kiunabii zilikuwa sahihi, na, wakiacha kiburi cha maoni yao, waliupokea ukweli kwa furaha. Baadhi ya wachungaji waliweka kando mawazo yao na hisia zao za kimadhehebu, waliacha mishahara na makanisa yao, na waliungana katika kutangaza ujio wa Yesu. Walikuwepo wachungaji wachache, hata hivyo, ambao walikuwa tayari kuupokea ujumbe huu; hivyo basi uliachiwa zaidi walei wa kawaida.

Wakulima waliacha mashamba yao, mafundi waliweka chini zana zao, wafanya biashara waliacha bidhaa zao, wanataaluma waliacha vyeo vyao; na bado idadi ya wafanya kazi ilikuwa ndogo kulinganisha na kazi iliyotekelezwa. Hali ya kanisa la watu wasiomcha Mungu na ulimwengu uliolala katika uovu, ilizilemea roho za walinzi wa kweli, na walikabiliana na kazi za suluba kwa hiari yao wenyewe, kujinyima, na mateso, ili wawaite watu kutubu ili wapate wokovu. Japokuwa walimpinga Shetani, kazi ilisonga mbele hatua kwa hatua, na ukweli wa marejeo ulipokelewa na watu maelfu.

Kila mahali ushuhuda unaogusa ulisikika, ukiwaonya wenye dhambi, watu wa dunia na washiriki wa kanisa, kuikimbia hasira inayokuja. Kama alivyokuwa Yohana Mbatizaji, mtangulizi wa Kristo, wahubiri waliweka shoka katika shina la mti na waliwahimiza watu wote wazae matunda yaletayo toba. Miito yao yenye mguso ilikuwa na tofauti kubwa ukilinganisha na uhakikisho wa amani na usalama uliosikika ukitolewa katika mimbari mashuhuri; na kila mahali ambapo ujumbe ulitolewa, uliteka fikra za watu. Ushududa sahili, wa moja kwa moja wa Maandiko, ulieleweka kwa njia ya nguvu ya Roho Mtakatifu, ulileta uzito katika ushawishi ambao wachache waliweza kupinga kabisa. Maprofesa wa dini waliamshwa kutoka katika usalama wa uongo.

Waliona kurudi nyuma kwao, udunia wao na kutokuamini kwao, kiburi chao na ubinafsi wao. Wengi walimtafuta Bwana kwa toba na unyenyekevu. Mshikamano ambao kwa muda mrefu walikuwa nao na vitu vya kidunia ulielekezwa kwa mambo ya mbinguni. Roho wa Mungu alikaa juu yao, na kwa mioyo iliyolainishwa na kutiishwa waliungana na kupiga kelele kwa pamoja: "Mcheni Mungu, na kumtukuza; kwa kuwa hukumu Yake imekuja." Wenye dhambi waliuliza kwa machozi: "Nifanye nini nipate kuokoka?" Wale ambao maisha yao

yalisifika kwa kukosa uaminifu walikuwa na shauku ya kurudisha vitu walivyovipata kwa dhuluma. Wote waliopata amani katika Kristo walitamani kuwaona wengine pia wakipata mbaraka huo. Mioyo ya wazazi iliwarudia watoto wao, na mioyo ya watoto iliwarudia wazazi wao. Vizuizi vya kiburi na kujiamini vilifutiliwa mbali. Maungamo ya dhati yalifanywa, na watu wa nyumbani walifanya kazi sana kwa ajili ya wokovu wa wale walio karibu yao na wale waliowapenda. Mara nyingi ilisikika sauti ya kuombeana kwa dhati. Kila mahali kulikuwepo na roho zilizokuwa katika kumsihi Mungu kwa dhati. Wengi walipambana usiku kucha ili kupata uhakikisho wa msamaha wa dhambi zao, au kwa ajili ya kuongoka kwa ndugu zao wa karibu au majirani zao.

Tabaka zote za watu walifurika katika mikutano ya Waadventista. Matajiri kwa masikini, walio juu na walio chini, waliokuwa na kazi za aina mbalimbali, wakiwa na shauku ya kusikia wao wenyewe, fundisho la ujio wa pili. Bwana alidhibiti roho ya upinzani wakati watumishi Wake walipofafanua sababu za imani yao. Nyakati zingine chombo kilikuwa dhaifu; lakini Roho wa Mungu alitoa nguvu kwa ajili ya ukweli Wake. Uwepo wa malaika watakatifu ulihisiwa katikati ya mikutano hii, na waongofu wengi waliongezwa kila siku kwa wale waliokuwa wameamini. Kwa kadiri ushahidi wa ujio wa haraka wa Kristo ulivyorudiwa mara kwa mara, makundi makubwa ya watu walisikiliza maneno mazito kwa ukimya mkubwa. Mbingu na nchi vilionekana kukaribiana. Nguvu ya Mungu ilihisiwa na wazee na vijana na watu wa umri wa kati. Watu walirudi majumbani mwao wakiwa na sifa midomoni mwao, na sauti ya furaha ilisikika katika hewa tulivu ya usiku. Hakuna aliyehudhuria mikutano hiyo ambaye anaweza kusahau mandhari zile zinazosisimua.

Utangazaji wa wakati mahsusi wa ujio wa Kristo uliamsha upinzani mkali kutoka kwa watu wengi tabaka zote, tangu kwa mchungaji katika mimbari hadi kwa mwenye dhambi asiyejali, wa kutupwa. Maneno ya unabii yalitimizwa: "Katika siku za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wenye kudhihaki, wafuatao tamaa zao wenyewe, na kusema, Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake? Kwa maana, tangu hapo babu zetu walipolala, vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa" (2 Petro 3:3, 4). Wengi wa waliodai kumpenda Mwokozi, walitangaza kuwa hawakuwa na upinzani dhidi ya fundisho la ujio wa pili; walidai kuwa walipinga tu utangazaji wa wakati mahsusi.

Lakini jicho la Mungu linaloona kila kitu lilisoma mioyo yao. Hawakupenda kusikia habari za ujio wa Kristo kuuhukumu ulimwengu katika haki. Hawakuwa watumishi waaminifu, kazi zao zisingeweza kustahimili ukaguzi wa Mungu anayechunguza mioyo, na waliogopa kukutana na Bwana wao. Kama Wayahudi wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo hawakuwa tayari kumkaribisha Yesu. Siyo tu kuwa walikataa kusikiliza hoja za wazi za Biblia, bali pia waliwadhihaki watu waliomtarajia Bwana. Shetani na malaika zake walishangilia, na walirusha dhihaka kwa Kristo na malaika watakatifu kuwa watu Wake walimpenda kidogo sana na kuwa hawakuwa na shauku ya kuja Kwake.

"Hakuna ajuaye siku wala saa" ilikuwa hoja ambayo ilitolewa mara nyingi na watu waliokataa imani ya marejeo. Maandiko yanasema: "Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake" (Mathayo 24:36). Maelezo ya wazi na yanayopatana ya aya hii yalitolewa na wale waliomtarajia Bwana, na matumizi mabaya yaliyofanywa wapinzani wao yalioneshwa wazi wazi. Maneno yalisemwa na Kristo katika yale maongezi yanayokumbukwa na wanafunzi Wake juu ya mlima wa Mizetuini baada kutoka hekaluni kwa mara ya mwisho. Wanafunzi walikuwa wameuliza swali: "Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?" Yesu aliwapa dalili, na alisema: "Nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, milangoni" (Aya 3, 33).

Kauli moja ya Mwokozi isitumiwe kuharibu kauli yake nyingine. Ingawa hakuna mtu anayejua siku wala saa ya ujio Wake, tumeelekezwa na tumetakiwa kujua wakati unapokaribia. Tumefundishwa pia kuwa kupuuza onyo Lake, na kukataa au kupuuza kujua wakati marejeo Yake yanapokaribia, tutaangamia kama walivyoangamia watu walioishi wakati wa Nuhu kwa kukataa kujua wakati gharika ilipokuwa inakuja. Na mfano katika sura hiyo hiyo, inayoonesha matokeo tofauti kwa mtumishi mwaminifu na asiyekuwa mwaminifu, na kutoa fursa kwa mtu aliyesema moyoni mwake, "Bwana wangu anachelewa kuja," inaonesha nuru ambayo kwayo Kristo aliwachukulia na kuwazawadia wale anaowakuta wakikesha, na wakifundisha ujio Wake, na wale wanaoukataa. "Kesheni basi," alisema. "Heri mtumwa yule, ambaye Bwana wake akija atamkuta akifanya hivyo" (Aya 42, 46). "Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako" (Ufunuo 3:3).

Paulo anaongelea juu ya tabaka la watu ambao kwao kuja kwa Bwana kutakuwa jambo la kushtukiza. "Siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, Kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula, ….wala hakika hawataokolewa." Lakini anaongozea, kwa wale ambao watakuwa wamesikiliza onyo la Mwokozi: "Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza" (1 Wathesalonike 5:2-5).

Hivyo ilioneshwa kuwa Maandiko hayatoi idhini kwa watu kubaki katika ujinga kuhusiana na ukaribu wa ujio wa Kristo. Lakini wale waliokuwa na shauku ya kupata kisingizio cha kuukataa ukweli waliziba masikio yao wasisikilize maelezo haya, na maneno "Hakuna mtu ajuaye siku wala saa" yaliendelea kurudiwa na watu wenye dhihaka na hata watu waliodai kuwa wachugaji wa Kiristo. Watu walipoamshwa, na kuanza kuulizia juu ya njia ya wokovu, walimu wa dini waliingia kati yao na ukweli, wakitafuta kunyamazisha hofu zao kwa kutoa tafsiri za uongo za neno la Mungu.

Walinzi wasiokuwa waaminifu waliungana katika kazi ya mdanganyaji mkuu, wakipiga kelele, Amani, amani, wakati Mungu hakusema amani. Kama Mafarisayo katika siku za

Kristo, wengi walikataa kuingia katika ufalme wa mbinguni, na wale waliokuwa wakiingia waliwazuia. Damu ya roho hizi itatakiwa mikononi mwao.

Watu wanyenyekevu na waaminifu kabisa katika makanisa ndio ambao mara nyingi walikuwa wa kwanza kupokea ujumbe. Waliojisomea Biblia wenyewe waliona jinsi ambavyo tafsiri za unabii zilizofundishwa na kuaminiwa na watu wengi wakati huo hazikuwa na msingi wowote wa kimaandiko; na mahali popote pale ambapo watu hawakutawaliwa na mvuto wa viongozi wa makanisa, popote pale ambapo watu waliweza kuchunguza maandiko wenyewe, fundisho la marejeo lilihitaji tu kulinganishwa na Maandiko kulipatia mamlaka ya Kiungu.

Wengi waliteswa na ndugu zao wasioamini. Ili wabaki katika nafasi zao kanisani, baadhi walikubali kubaki kimya juu ya tumaini lao; lakini wengine walihisi kuwa utii wao kwa Mungu uliwakataza kuficha ukweli ambao Mungu alikuwa amewakabidhi kama dhamana. Sio wachache walioondolewa katika ushirika wa kanisa sio kwa sababu nyingine isipokuwa tu ile ya kueleza imani yao kuhusu ujio wa Kristo. Maneno ya nabii yalikuwa ya thamani kubwa sana kwa wale waliostahimili majaribu ya imani yao: “Ndugu zenu wawachukiao ninyi, waliowatupa kwa ajili ya jina langu, wamesema, Na atukuzwe Bwana, tupate kuiona furaha yenu; lakini watatahayarika” (Isaya 66:5).

Malaika wa Mungu walikuwa wakiangalia kwa shauku kubwa matokeo ya onyo. Wakati makanisa mengi yalipokataa ujumbe, malaika waligeukia upande mwingine kwa huzuni. Lakini walikuwepo watu wengi ambao walikuwa hawajajaribiwa kuhusiana na ukweli wa marejeo. Wengi walipotoshwa na waume zao, wake zao, wazazi wao, au watoto wao, walisukumwa kuaminishwa kuwa ni dhambi hata kusikiliza uzushi kama huo uliofundishwa na Waadventista. Malaika waliagizwa kuwalinda kwa uaminifu watu hawa, kwa kuwa nuru nyingi ilipaswa ing’ae tena juu yao kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu.

Kwa shauku isiyoelezeka wale waliopokea ujumbe walikesha wakingoja ujio wa Mwokozi wao. Wakati ambao walitarajia kukutana Naye ulikuwa karibu. Walikaribia saa hii kwa utulivu mkubwa. Walibaki katika tafakari nzuri kuhusu Mungu, na uhalisia wa amani ambayo wangeipata katika muda mfupi angavu baada ya wakati huo. Hakuna ye yote aliyepata uzoefu wa tumaini hili anayeweza kusahau saa zile za thamani za kungoja. Kwa majuma kadhaa kabla ya wakati huo, shughuli za ulimwengu ziliwekwa pembeni kwa muda kwa walio wengi. Waaminio waaminifu walichunguza kwa makini kila wazo na mhemko wa mioyo yao kana kwamba wapo juu ya vitanda vya kifo chao na katika saa chache wafumbe macho yao na kuachana na mandhari za kidunia. Kulikuwa hakuna ushonaji wa “majoho ya kupaalia” (tazama Kiambatisho); lakini wote walihisi hitaji la ushahidi wa ndani kuwa walikuwa tayari kukutana na Mwokozi; majoho yao meupe yalikuwa usafi wa roho zao—tabia zilizotakaswa dhambi kwa damu ya upatanisho ya Kristo. Heri kama kungekuwa bado miongoni mwa watu wanaodai kuwa wa Mungu roho ile ile ya kujichunguza mioyo, imani ile ile ya dhati, na iliyo thabiti. Ikiwa wangeendelea kujinyenyekesha mbele ya Bwana na

kupeleka maombi yao mbele ya kiti cha rehema wangeweza kuwa na uzoefu mkubwa zaidi kuliko walio nao sasa. Kuna maombi machache sana, kushawishika kudogo sana kuhusiana na dhambi, na ukosefu wa imani iliyo hai unawaacha wengi bila neema itolewayo kwa wingi na Mkombozi wetu. Mungu alipanga kuwahakiki watu Wake. Mkono Wake ulifunika kosa katika ukokotoaji wao wa vipindi vya kiunabii. Waadventista hawakugundua kosa, wala halikugunduliwa na wasomi wa hali ya juu kabisa miongoni mwa wapinzani wao. Wapinzani wao wasomi walisema: "Ukokotoaji wenu wa vipindi vya kiunabii ni sahihi. Tukio kubwa la aina fulani liko karibu kutokea; lakini siyo hilo ambalo Bwana Miller analitabiri; ni uongofu wa ulimwengu, na siyo ujio wa pili wa Kristo" (Tazama Kiambatisho.)

Wakati wa matarajio ulipita, na Kristo hakuoonekana na kuwakomboa watu Wake. Wale ambao kwa imani ya dhati na upendo wa kweli walikuwa wametarajia kumwona Mwokozi wao, walihisi maumivu makali sana. Lakini makusudi ya Mungu yalitimizwa; alikuwa akihakiki mioyo ya watu waliodai kuwa wanangojea ujio Wake. Walikuwepo miongoni mwao wengi waliokuwa wamesukumwa kungoja siyo kwa sababu ya makusudi sahihi bila hofu tu. Kutangaza imani yao kulikuwa hakujabadilisha mioyo yao wala maisha yao. Wakati tukio lililotarajiwa lilipoacha kutokea watu hawa, walitangaza kuwa hawakuumia kwa namna yo yote ile; hawakuwa na imani yo yote kuwa Kristo angekuja. Walikuwa miongoni mwa watu wa kwanza kudhihaki huzuni ya walioamini kwa dhati.

Lakini Yesu na jeshi lote la mbinguni waliwaangalia kwa upendo na huruma wale waliokuwa wamejaribiwa na waaminifu lakini waliokuwa wameumizwa. Ikiwa pazia linalogawa ulimwengu unaoonekana na usioonekana lingefunguliwa, malaika wangeweza kuonekana wakiwakaribia watu hawa waaminifu wakiwakinga dhidi ya mishale ya Shetani.

Sura ya 21 - Onyo Lililokataliwa

Katika kuhubiri fundisho la ujio wa pili wa Kristo,William Millernawenzake walifanya kazi wakiwa na lengo moja tu kuwaamsha watu wajiandae kwa ajili ya hukumu. Walijitahidi kuwaamsha waliodai kuwa wafuasi wa dini wapate tumaini la kweli na waone hitaji lao la uzoefu wa kina wa Kikristo, na walifanya kazi pia kuamsha watu wasioongoka watambue wajibu wao wa toba na uongofu wa haraka kwa Mungu. "Hawakufanya juhudi yo yote ya kujaribu kuongoa watu wajiunge na kundi au madhehebu yo yote ya dini. Hivyo basi walifanya kazi miongoni mwa vikundi vyote na madhehebu yote, pasipo kuingilia utaratibu wao au nidhamu yao."

"Katika kazi zangu zote," alisema Miller, "Sikuwahi kuwa na shauku au wazo la kuanzisha kanisa jingine tofauti na madhehebu yaliyokuwepo, au kunufaisha kanisa moja kwa kuliathiri jingine. Nilikusudia kuyanufaisha makanisa yote. Niliamini kuwa Wakristo wote wangefurahia kutarajia ujio wa Kristo, na kuwa wale ambao wasingeweza kuona kama mimi nilivyoona wasingeacha kuwapenda wale wambao wangepokea fundisho hili, sikuwahi kufikiri kuwa kungekuwa na haja ya kuwa na mikutano ya ibada tofauti. Lengo mahsusi lilikuwa shauku ya kuongoa watu wote wamtii Mungu, kuutangazia ulimwengu kuhusu hukumu inayokuja, na kuwashawishi wanadamu wenzagu wafanye matayarisho ya mioyo ambayo yatawawezesha kukutana na Mungu wao kwa amani. Idadi kubwa ya wale walioongoka kupitia kazi zangu walijiunga na makanisa mbalimbali yaliyokuwepo."—Bliss, uk. 328.

Kwa kuwa kazi yake ilikuwa na matokeo ya kuongeza waumini katika makanisa, kwa muda fulani kazi yake ilikubalika sana. Lakini kwa kuwa wachungaji na viongozi wa dini waliamua kupingana na fundisho la marejeo na shauku ya kuzima msukosuko ulioletwa na mada ya marejeo, siyo tu kuwa waliipinga mada hiyo kutokea mimbarani, bali pia waliwakatalia washiriki wasifike kwenye mikutano ambayo mahubiri ya marejeo yalitolewa, au hata wasizungumzie tumaini lao katika mikutano ya kijamii ya kanisa. Hivyo, walioamini walijikuta katika nafasi ya majaribu na mashaka makubwa. Waliyapenda sana makanisa yao na walichukia sana kutengana nayo; lakini walipoona ushuhuda wa neno la Mungu ukikandamizwa na haki yao ya kuchunguza unabii wakinyimwa walihisi kuwa utii kwa Mungu uliwakataza kujisalimisha. Waliotafuta kufungia nje ushuhuda wa neno la Mungu walishindwa kuwatambua kama sehemu ya kanisa la Kristo, "nguzo na msingi wa ukweli." Kwa hiyo, walijihisi kuwa na haki ya kujitenga na makanisa yao ya awali. Katika msimu wa kiangazi cha mwaka 1844 takribani watu hamsini elfu walijiondoa kutoka katika makanisa yao ya awali.

Karibu na wakati kama huu badiliko kubwa lilionekana katika makanisa yaliyo mengi ya Marekani yote. Kulikuwepo kwa muda mrefu ongezeko la pole pole lakini endelevu kufuata matendo na desturi za kidunia, na poromoko sawia la maisha halisi ya kiroho; lakini

katika mwaka ule kulikuwepo ushahidi mwingi wa anguko kubwa na la ghafla la kiroho katika makanisa karibu yote nchini Marekani. Wakati hakuna mtu aliyeonekana kuweza kueleza chanzo cha anguko hilo, ukweli wenyewe ulionekana wazi na ulifafanuliwa na vyombo vya habari na wahubiri mimbarani.

Katika mkutano wa wapresbiteri wa Filadelfia, Bwana Barnes, mwandishi wa kitabu cha ufafanuzi wa Biblia kilichotumiwa na watu wengi na ambaye alikuwa mchungaji wa moja ya makanisa makubwa katika jiji lile, "alisema kuwa alikuwa katika uchungaji kwa miaka ishirini, na kamwe, mpaka Meza ya Bwana ya mwisho, aliiendesha bila kupokea waumini zaidi au waliopo kupungua. Lakini sasa hakukuwa na uamsho, hakukuwa na waongofu wapya, hakuna ukuaji katika neema unaoonekana miongoni mwa wale waliodai kuwa Wakristo, na hakuna anayehudhuria mafundisho yake kuzungumzia juu ya wokovu wa roho zao. Kwa sababu ya ongezeko la shughuli, na mustakabali mzuri wa biashara na viwanda, kuna ongezeko kubwa la watu kuipenda dunia. Hivyo ndivyo ilivyo kwa madhehebu mengine yote."—Congregational Journal, Mei 23, 1844.

Katika mwezi wa Februari wa mwaka ule ule, Profesa Finney wa Chuo cha Oberlin alisema:"Tuna ukweli mbele ya akili zetu, kuwa, kwa jumla, makanisa ya Kiprotestanti ya nchi hii, kwa kweli, ama hayakujali au yalipinga karibu matengenezo yote ya kimaadili ya kizazi kile. Kuna makanisa machache ambayo yana nafuu, ambayo hata hivyo hayatoshi kubadilisha sana uhalisia wa ukweli huo kwa mtazamo wa jumla. Tunao pia ukweli mwingine wa kuunga mkono hoja hii: kutokuwepo mvuto wa uamsho karibu katika makanisa yote. Kutokujali mambo ya kiroho kunatawala karibu mahali pote, na ni kutokujali mambo ya kiroho ni kukubwa mno; hivyo ndivyo magazeti ya kidini ya nchi nzima yanavyoshuhudia.

Katika ujumla wao, washiriki wa kanisa wanazidi kuwa mateka wa mitindo,—wanashikana mikono na watu wasio wacha Mungu katika sherehe za anasa, katika densi, na matamasha ya anasa, n.k Lakini hatuna haja ya kueleza sana mada hii inayoumiza sana. Itoshe kusema kuwa ushahidi mkubwa na mpana sana juu yetu, unaoonesha kuwa makanisa kwa jumla yanazidi kuporomoka kiroho. Yameenda mbali sana na Bwana, Naye Bwana amejiondoa kutoka katika makanisa hayo." Na mwandishi katika gazeti la Religious Telescope anashuhudia: "Hatujawahi kushuhudia kurudi nyuma kukubwa katika mambo ya dini kama ilivyo sasa. Kwa kweli, kanisa linapaswa kuamka, na kutafuta chanzo cha tatizo hili; kama tatizo la kila mtu anayeipenda Sayuni anavyoliona. Tunapokumbuka matukio 'machache na ya kati' ya uongofu wa kweli, na ukosefu wa toba na ugumu wa moyo usio kifani wa wenye dhambi, tunajikuta bila kupenda tukipiga kelele, 'Je, Mungu amesahau kuwa mwenye rehema? au, Je, mlango wa rehema umefungwa?'"

Hali kama hiyo haiwezi kutokea isipokuwa chanzo chake kiwe ndani ya kanisa lenyewe. Giza la kiroho linalokalia mataifa, linalokalia makanisa na mtu mmoja mmoja, lipo, sio kwa sababu ya kuondoka kwa misaada ya neema ya Mungu bila sababu, bali kwa sababu ya

kupuuza au kukataa nuru ya Kiungu kwa upande wa wanadamu. Mfano mzuri wa ukweli huu umewasilishwa katika historia ya Wayahudi wakati wa Kristo. Kwa njia ya kujiweka wakfu kwa ulimwengu na kumsahau Mungu na neno Lake, ufahamu wao ulitiwa giza, mioyo yao ilijazwa udunia na tamaa za mwili. Hivyo hawakujua lolote kuhusu marejeo ya Masihi, na kwa sababu ya kiburi chao na kutokuamini kwao walimkataa Mkombozi. Mungu hata hivyo hakukatilia mbali taifa la Wayahudi na kuwanyima maarifa ya, au fursa ya kushiriki katika, mibaraka ya wokovu. Lakini wale waliokataa ukweli walipoteza shauku ya zawadi ya Mbinguni. "Walilifanya giza kuwa nuru, na nuru kuwa giza," mpaka nuru iliyokuwa ndani yao ikawa giza; na giza lilikuwa kubwa sana!

Inapatana na sera ya Shetani kuwa watu wabaki na mwonekano wa dini ili mradi tu roho ya uchaji halisi wa Mungu haipo. Baada ya wao kuikataa injili, Wayahudi waliendelea kutekeleza kwa bidii kaida zao za zamani, walitunza kwa uangalifu sana kujitenga kwao na mataifa, ilhali wao wenyewe hawakuweza kukiri kuwa uwepo wa Mungu haukuwa tena ukionekana miongoni mwao. Unabii wa Danieli ulionesha pasipo kukosea wakati wa ujio wa Masihi, na ulitabiri moja kwa moja kifo Chake, kiasi kwamba waliwakatisha tamaa watu wasijifunze unabii huo, na hatimaye marabi walitangaza laana kwa wale wote ambao wangejaribu kukokotoa huo wakati. Katika upofu na moyo usiokuwa na toba watu wa Israeli katika karne zilizofuata walisimama, wakipuuza fursa za neema ya wokovu, bila kujali mibaraka ya injili, na bila kujali onyo kali na la kuogofya la hatari ya kuikataa nuru kutoka mbinguni.

Mahali popote palipo na kisababishi, matokeo yale yale hufuata. Ye yote ambaye, kwa makusudi, anazima ushawishi kuhusu wajibu wake kwa sababu unaingilia matakwa yake hatimaye atapoteza uwezo wa kutofautisha kati ya ukweli na uongo. Ufahamu hujazwa giza, dhamiri huwa sugu, moyo huwa mgumu, na roho hutengwa na Mungu. Mahali ambapo ujumbe wa ukweli wa Mungu umekataliwa au umepuuzwa, pale kanisa linafunikwa na giza; imani na upendo huwa hupungua sana, na utengano na migawanyiko huingia. Washiriki wa kanisa hupeleka shauku na nguvu zao katika utafutaji wa mambo ya kidunia, na wenye dhambi hufanywa kuwa wagumu zaidi katika uasi wao.

Ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14, unaotangaza saa ya hukumu ya Mungu na kuwaita watu wamche Mungu na wamwabudu Yeye, umekusudiwa kuwatenga watu wa Mungu na mivuto ya ulimwengu na kuwaamsha ili watambue hali yao hali ya udunia na kurudi nyuma kwao. Katika ujumbe huu, Mungu ametuma kwa kanisa onyo, ambalo, kama lingekubaliwa, lingesahihisha maovu yaliyowatenga Naye. Ikiwa wangepokea ujumbe kutoka mbinguni, wakanyenyekesha mioyo yao mbele za Bwana na kufanya matayarisho ya dhati ili waweze kusimama katika uwepo Wake, Roho na nguvu ya Mungu vingedhihirika miongoni mwao. Kanisa lingeweza tena kufikia ile hali iliyobarikiwa ya umoja, imani, na upendo ambao ulikuwepo katika siku za mitume, ambapo waaminio "walikuwa na moyo mmoja na roho

moja,"na"walihubiri neno la Mungu kwa ujasiri," wakati "Bwana alipoliongeza kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa" (Matendo 4:32, 31; 2:47).

Ikiwa watu wa Mungu wangeipokea nuru kama inavyowaangazia kutoka katika neno la Mungu, wangefikia ule umoja ambao Kristo aliuombea, ule ambao mtume Paulo anauelezea, "umoja wa roho katika kifungo cha amani.""Kuna," anasema, "Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja" (Waefeso 4:3-5).

Hayo ndiyo yalikuwa matokeo yaliyobarikiwa waliyoyapata wale walioukubali ujumbe wa marejeo. Walitoka katika madhehebu mbalimbali, na vikwazo vyao vya kimadhehebu viliondolewa; imani zilizopingana zilisawazishwa; tumaini lisilokuwa na msingi wa Biblia la miaka elfu moja ya muda mfupi lilitupiliwa mbali, dhana potofu za ujio wa Yesu zilisahihishwa, kiburi na mshikamano kwa ulimwengu viliondolewa kabisa; makosa yaliungamwa; mioyo iliunganishwa katika ushirika mtamu, na upendo na furaha vilikuwa juu. Ikiwa fundisho hili lilileta mambo haya kwa wachache waliolipokea, lingeweza kufanya jambo hilo hilo kwa wote ambao wangelipokea.

Lakini makanisa kwa jumla hayakupokea onyo hilo. Wachungaji wao, ambao, kama walinzi "katika kuta za nyumba ya Israeli," walipaswa kuwa wa kwanza kutambua ishara za ujio wa Yesu, walishindwa kujifunza ukweli kutoka katika ushuhuda wa manabii au kutoka katika alama za nyakati. Kwa kadiri matumaini na tamaa ya mafanikio ya kidunia yalivyojaza mioyo yao, upendo kwa Mungu na imani katika neno Lake vilipoa; na wakati fundisho

la marejeo lilipowasilishwa, liliamsha tu chuki na kutoamini. Ukweli kuwa ujumbe ulikuwa, kwa kiwango kikubwa, ukihubiriwa na walei, ulitumiwa kama zana dhidi ya ujumbe wenyewe. Kama ilivyokuwa katika siku za kale ushuhuda wa wazi wa neno la Mungu ulikutana na swali: "Ni nani katika wakuu amwaminiye, au katika Mafarisayo?" Na baada ya kugundua jinsi ilivyokuwa kazi ngumu kukanusha hoja zilizotokana na vipindi vya kiunabii, walipiga marufuku kujifunza unabii, wakifundisha kuwa vitabu vya kiunabii vilikuwa vimetiwa muhuri na visingeweza kueleweka.

Watu wengi, kwa kuwaamini wachungaji wao bila maswali, walikataa kusikiliza onyo; na wengine, ingawa walikuwa wameshawishika na kuuamini ukweli, hawakuthubutu kuukiri, wasije "wakatupwa nje ya sinagogi." Ujumbe ambao Mungu alikuwa ameutuma kwa ajili ya kulipima na kulisafisha kanisa ulidhihirisha wazi kuwa idadi kubwa ya watu ilikuwa imeweka mioyo yao katika mambo ya kidunia kuliko kwa Kristo. Kamba zilizowafungamanisha na ulimwengu zilikuwa na nguvu zaidi ya mivuto ya mbinguni. Walichagua kusikiliza sauti ya hekima ya kidunia na kuupa kisogo ujumbe wa ukweli unaogusa moyo na kuufanya ujihoji.

Kwa kulikataa onyo la malaika wa kwanza, walikataa njia ambayo Mbingu ilikuwa imeleta kwa ajili ya wokovu wao. Walimkataa mjumbe wa neema ambaye angesahihisha maovu yao ambayo yaliwatenga na Mungu, na kwa shauku kubwa zaidi walirudi kutafuta kushikamana na ulimwengu zaidi. Hiki ndicho kilikuwa chanzo cha hali ya kutisha ya udunia, kurudi nyuma, na kifo cha kiroho iliyokuwepo katika makanisa mwaka 1844.

Katika Ufunuo 14 malaika wa kwanza anafuatwa na malaika wa pili anayetangaza: "Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake" (Ufunuo 14:8). Neno "Babeli" linatokana na neno "Babel," na linamaanisha machafuko. Linatumika katika Maandiko kuelezea namna mbalimbali za dini ya uongo au dini iliyoasi. Katika Ufunuo 17 Babeli imewasilishwa kama mwanamke—kielelezo kinachotumiwa katika Biblia kama alama ya kanisa, mwanamke safi akiwakilisha kanisa safi, mwanamke kahaba akiwakilisha kanisa lililoasi.

Katika Biblia tabia takatifu na inayostahimili ya uhusiano uliopo kati ya Kristo na kanisa Lake imewakilishwa kwa njia ya muungano wa ndoa. Bwana ameunganisha watu Wake na Yeye Mwenyewe kwa njia ya agano thabiti, Yeye akiahidi kuwa Mungu wao, na wao wakiahidi kuwa watu Wake na Wake peke yake. Anatangaza: "Nami nitakuposa uwe wangu kwa milele; naam, nitakuposa kwa haki, na kwa hukumu, na kwa ufadhili, na kwa rehema" (Hosea 2:19). Na, tena: "Maana mimi ni mume wenu" (Yeremia 3:14). Naye Paulo anatumia kielelezo hicho hicho katika Agano Jipya anaposema: "Naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi" (2 Wakorintho 11:2).

Kanisa linapokosa uaminifu kwa Kristo na kuruhusu imani na upendo kuondoka Kwake, na kukubali upendo kwa mambo ya dunia uujaze moyo, hufananishwa na uvunjaji wa kiapo cha ndoa. Dhambi ya Israeli ya kumwacha Bwana inawasilishwa kwa kielelezo hiki hiki; na upendo wa ajabu wa Mungu ambao waliupuuza umeoneshwa kwa njia inayogusa sana: "Nalikuapia, nikafanya agano nawe, asema Bwana MUNGU, ukawa wangu." "Nawe ulikuwa mzuri mno, ukafanikiwa hata kufikilia hali ya kifalme. Sifa zako zikaenea kati ya mataifa kwa sababu ya uzuri wako; kwa maana ulikuwa mkamilifu, kwa sababu ya utukufu wangu niliokutia …. Lakini uliutumainia uzuri wako, ukafanya mambo ya kikahaba kwa sababu ya sifa zako." "Hakika kama vile mke amwachavyo mumewe kwa hiana, ndivyo mlivyonitenda mimi kwa hiana, Ee nyumba ya Israeli, asema Bwana;" "Mke wa mtu, aziniye! Akaribishaye wageni badala ya mumewe!" (Ezekieli 16:8, 13-15, 32; Yeremia 3:20).

Katika Agano Jipya, lugha inayofanana na hiyo imetumiwa kuelezea Wakristo wanaotafuta urafiki na dunia zaidi kuliko kutafuta kukubaliwa na Mungu. Mtume Yakobo anasema: "Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu."

Mwanamke (Babeli) wa Ufunuo 17 anaelezewa kuwa "amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu….. Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, Babeli mkuu, mama wa makahaba." Anasema nabii: "Nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu." Babeli umeelezwa zaidi kuwa "ni mji ule mkubwa, wenye ufalme juu ya wafalme wa nchi" (Ufunuo 17:4-6, 18).

Mamlaka ambayo kwa karne nyingi iliwatawala kiimla wafalme wa nchi za Kikristo ilikuwa Rumi. Rangi ya zambarau na nyekundu, dhahabu na mawe ya thamani na lulu, huchora picha dhahiri ya utukufu na zaidi ya ukuu wa kifalme uliooneshwa na upapa wa Rumi. Na hakuna mamlaka nyingine ambayo ingeweza kutangazwa kuwa "amelewa kwa damu ya watakatifu" kama kanisa ambalo liliwatesa kikatili wafuasi wa Kristo. Babeli inashitakiwa pia kwa kuwa na uhusiano haramu na "wafalme wa dunia." Ilikuwa kwa njia ya kujitenga na Bwana, na kushikamana na upagani, ambapo kanisa la Kiyahudi lilibadilika na kuwa kahaba; na Rumi, kwa kujinajisi kwa jinsi iyo hiyo kwa kutafuta msaada wa mamlaka za kidunia, inapokea hukumu inayofanana na hiyo hiyo.

Babeli unasemwa kuwa "mama wa makahaba." Mabinti zake lazima wawakilishe makanisa ambayo yanang'ang'ania mafundisho na mapokeo yake, na yanayofuata mfano wake wa kupuuza ukweli na kukubaliwa na Mungu, ili kuunda ushirika haramu na ulimwengu. Ujumbe wa Ufunuo 14, unaotangaza kuanguka kwa Babeli unahusu mashirika ya kidini ambayo awali yalikuwa safi na sasa yamechafuka. Kwa kuwa ujumbe huu unafuata onyo la hukumu, ni lazima unatolewa katika siku za mwisho; kwa hiyo hauwezi kuhusika na Kanisa la Rumi peke yake, kwani kanisa hilo liko katika hali ya kuanguka kwa karne nyingi. Zaidi ya hapo, katika Sura ya kumi na nane ya Ufunuo watu wa Mungu wanaitwa watoke Babeli.

Kwa mujibu wa andiko hili, wengi wa watu wa Mungu ni lazima bado wako Babeli. Na ni katika mashirika gani ya kidini ambamo kuna sehemu kubwa ya wafuasi wa Kristo kwa sasa? Bila shaka, ni katika makanisa mbalimbali ya imani ya Kiprotestanti. Wakati wa kuzaliwa kwa makanisa haya yalikuwa na msimamo mzuri kwa ajili ya Mungu na ukweli, na mbaraka Wake ulikuwa pamoja nao. Hata ulimwengu usioamini ulilazimika kukiri matokeo bora yaliyofuata upokeaji wa kanuni za injili. Katika maneno ya nabii kwa Israeli: "Sifa zako zikaenea kati ya mataifa kwa sababu ya uzuri wako; kwa maana ulikuwa mkamilifu, kwa sababu ya utukufu wangu niliokutia, asema Bwana MUNGU." Lakini walianguka kwa sababu ya shauku ile ile ambayo ilikuwa laana na maangamizi ya Israeli—shauku ya kuiga na kutafuta urafiki na watu wasiomcha Mungu."Lakini uliutumainia uzuri wako, ukafanya mambo ya kikahaba kwa sababu ya sifa zako" (Ezekieli 16:14, 15).

Mengi ya makanisa ya Kiprotestanti yanafuata mfano wa Rumi wa mshikamano haramu na “wafalme wa dunia”—makanisa ya dola, kwa uhusiano wao na serikali za kiraia; na madhehebu mengine, kwa kutafuta kukubaliwa na ulimwengu. Na neno “Babeli”—machafuko—linaweza kutumiwa kwa madhehebu haya kwa usahihi kabisa, wote wakidai kupata mafundisho yao kutoka katika Biblia, lakini wakiwa wamegawanyika katika vikundi visivyokuwa na idadi, vikiwa na imani na nadharia zinazotofautiana na kupingana sana.

Pamoja na muungano haramu na ulimwengu, makanisa yaliyojitenga na Rumi yanaonesha baadhi ya tabia za Rumi. Kitabu cha Kanisa Katoliki la Rumi hutoa hoja kuwa“ikiwa Kanisa la Rumi lina hatia ya ibada ya sanamu kuhusiana na watakatifu, binti yake, Kanisa la Uingereza, lina hatia ile ile, kwa kuwa lina makanisa kumi yaliyowekwa wakfu kwa ajili ya Maria na kanisa moja tu ndilo limewekwa wakfu kwa Kristo.”—Richard Challoner, The Catholic Christian Instructed, Preface, ukurasa 21, 22.

Na Dkt. Hopkins, katika“A Treatise on the Millennium,” anasema:“Hakuna sababu ya kufikiri kuwa roho na matendo ya mpinga Kristo ipo katika kanisa linaloitwa kwa sasa Kanisa la Roma peke yake. Makanisa ya Kiprotestanti yana mambo mengi ya mpinga Kristo, na hayajafanya matengenezo kikamilifu na kuacha kabisa. ufisadi na uovu.”— Samuel Hopkins, Works, vol. 2, uk. 328. Kuhusiana na utengano kati ya kanisa la Wapresbiteri na Roma, Dkt.

Guthrie ameandika: “Miaka mia tatu iliyopita, kanisa letu, likiwa na Biblia iliyo wazi katika bendera yake, na tamko la hamasa linalosomeka,‘Chunguza Maandiko,’ kwenye waraka ulioviringishwa, lilitoka nje ya malango ya Rumi.” Halafu anauliza swali la msingi: “Walitoka Babeli wakiwa safi?”—Thomas Guthrie, The Gospel in Ezekiel, ukurasa 237.

“Kanisa la Uingereza,” anasema Spurgeon, “linaonekana kutafunwa na mfumo wa sakramenti; lakini maboresho yake nayo pia yanaonekana kuwa yamegubikwa na falsafa za kipagani. Wale tuliowatarajia kuleta mambo mema wanageuka mmoja mmoja na kuacha misingi ya imani. Tena na tena, naamini, moyo wa Uingereza umetobolewa-tobolewa na ukafiri wa kutisha unaodiriki kupanda mimbarani na kujiita Ukristo.” Chanzo cha uasi mkuu kilikuwa ni nini? Kanisa liliachaje kwa mara ya kwanza usahili wa injili? Kwa kuiga matendo ya kipagani, ili kuwawezesha wapagani waupokee Ukristo. Mtume Paulo anaeleza kuwa, hata katika siku zake, “siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi”(2 Wathelanike 2:7).

Nyakati za uhai wa mitume kanisa lilibaki safi ukilinganisha na nyakati zingine. Lakini “kuelekea sehemu ya mwisho wa karne ya pili karibu makanisa yote yalikuwa yamejenga tabia na muundo mpya; usahili wa awali ulitoweka, na bila kutambua, kwa kadiri wanafunzi wa zamani walivyopumzika katika makaburi yao, watoto wao, pamoja na waongofu wapya, ... walijitokeza na kuleta mwelekeo mpya wa kanisa.”— Robert Robinson, Ecclesiastical Researches, ch. 6, par. 17, uk. 51. Ili kupata waongofu wapya, kiwango cha juu cha imani ya Kikristo kilishushwa chini, na matokeo yake “mafuriko ya upagani, ukitiririka kuingia

kanisani, ulibeba na desturi, matendo, na sanamu zake."—Gavazzi, Lectures, ukurasa 278. Dini ya Kikristo ilipopata ukubali na msaada wa tawala za kidunia, ilipokelewa na watu wengi kwa jina; lakini wakati kwa mwonekano wa nje walikuwa Wakristo, wengi "kwa ndani walibaki wapagani, hususani wakiabudu kwa siri sanamu zao."—Ibid., ukurasa 278.

Je, mchakato huo huo si umerudiwa-rudiwa karibu katika kila kanisa linalojiita la Kiprotestanti? Kama waasisi, wale waliokuwa na roho ya dhati ya matengenezo, wanapita, watoto na wao huja na "kubuni upya mwelekeo wa kazi." Wakati katika upofu wanashikilia imani ya baba zao na kukataa kupokea nuru yo yote ya kuendeleza walichokiona, watoto wa wanamatengenezo wanaenda mbali kabisa ya unyenyekevu, kujikana nafsi, na kuukataa ulimwengu. Kwa njia hiyo "ule usahili wa kwanza unatoweka." Mafuriko ya ulimwengu, unaotiririka na kuingia ndani ya kanisa, huja "na desturi, matendo, na sanamu zake."

Ndiyo, kiwango cha ule urafiki na ulimwengu ambao ni "uadui na Mungu,"unaopaliliwa sasa miongoni mwa wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo kinatisha kiasi gani! Ni kwa idadi kubwa kiasi gani makanisa mashuhuri katika ulimwengu wote wa Kikristo yameacha kiwango cha Biblia cha unyenyekevu, kujikana nafsi, usahili, na utauwa! John Wesley alisema, akizungumzia juu ya matumizi mazuri ya pesa: "Usitumie vibaya sehemu yo yote ya talanta yako yenye thamani, kwa ajili ya kuridhisha tamaa yako ya macho, kwa nguo nzuri au bei kubwa kupita kiasi, au kwa mapambo yasiyokuwa ya lazima. Usitumie vibaya sehemu ya pesa yako kwa ajili ya kupamba nyumba zenu; kwa ajili ya samani nzuri au za gharama kupita kiasi; kwa picha za gharama kubwa, mchoro, au mapambo Usitoe chochote kwa ajili ya kuridhisha kiburi cha uzima, kuwafanya watu wakuone ni mtu mwenye uwezo mkubwa au ili watu wakusifie....

'Ili mradi unatenda wema kwa jinsi uanvyoona mwenyewe, watu watasema mema juu yako.' Ili mradi wewe 'unavaa nguo za zambarau na kitani safi,' na unakula 'vizuri kila siku,' bila shaka wengi watasifia umaridadi wako, ukarimu na upendo wako. Lakini usikubali sifa zao nzuri. Badala yake ridhika na heshima inayotoka kwa Mungu."—Wesley, Works, Sermon 50, "The Use of Money." Lakini katika makanisa mengi ya wakati huu fundisho kama hili linapuuzwa.

Tabia ya watu kukiri kufuata dini imekuwa jambo la kawaida ulimwenguni sasa. Watawala, wanasiasa, wanasheria, madaktari, wafanyabiashara, hujiunga na kanisa kama njia ya kupata heshima na kuaminiwa na jamii, na kupata maslahi yao ya kidunia. Kwa njia hiyo wanatafuta kufunika miamala yao ya udhalimu chini ya mwavuli wa Ukristo. Mashirika mbalimbali ya kidini, kwa msaada wa matajiri na mvuto wa watu dunia waliobatizwa, yanaongeza juhudi zao ili kupata umaarufu na udhamini mkubwa zaidi. Makanisa ya kifahari, yaliyopambwa kwa umaridadi mkubwa sana, yanajengwa kando kando ya barabara mashuhuri. Waabudu wanavalia nguo za gharama kubwa na za mitindo ya kisasa. Mshahara mkubwa unatolewa kwa mchungaji mwenye talanta ili kuwaburudisha na kuwavutia watu.

Mahubiri yake hayapaswi kugusa dhambi zinazopendwa na watu, lakini yanapaswa yawe laini na yanayopendeza kwa ajili ya wasikilizaji wa kisasa. Kwa njia hiyo wenye dhambi wa kisasa wanaandikwa majina yao katika kumbukumbu za kanisa, na dhambi za kisasa zinafichwa chini ya vazi la uchaji Mungu wa kuigiza.

Likitoa ufafanuzi juu ya mtazamo wa sasa wa wale wanaodai kuwa Wakristo kwa ulimwengu, jarida mashuhuri lisilokuwa la kidini lilisema: “Bila kujua kanisa linaongozwa na roho ya kizazi hiki, na limeiga mifumo ya kizazi hiki ya ibada ili kukidhi matakwa ya kisasa.”“Mambo yote, kwa kweli, yanayosaidia kuifanya dini ivutie, kanisa sasa linayatumia kama nyenzo zake.” Na mwandishi katika jarida la New York Independent anasema hayo hayo juu ya Umethodisti kama ulivyo: “Msitari unaogawa katikati ya wacha Mungu na wasio na dini unafifia na kuwa kama kivuli cha aina fulani, na watu wenye bidii pande zote wanafanya kazi kwa bidii ili kuondoa tofauti zote katika mbinu zao za kazi na burudani.” “Umashuhuri wa dini una mwelekeo wa kuongeza sana idadi ya wale wanaoweza kupata manufaa yake bila kutekeleza majukumu yake.”

Howard Crosby alisema: “Ni jambo la kusikitisha sana kuwa tunaliona kanisa la Kristo likitekeleza kidogo sana mipango ya Bwana wake. Kama vile Wayahudi wa zamani walivyoruhusu ushirikiano wao wa kawaida na mataifa walioabudu sanamu uibe mioyo yao kutoka kwa Mungu, ... kadhalika, kanisa la Yesu sasa, kwa mahusiano ya uongo na ulimwengu usioamini, linaacha mbinu za Mungu za maisha yake ya kweli, na linafuata tabia za jamii isiyokuwa na Kristo ambazo ni za uovu, japokuwa zinaonekana kuwa za busara, kwa kutumia hoja na kufikia mahitimisho ambayo hayapatani na neno la Mungu, na yakipingana na ukuaji wote katika neema.”—The Healthy Christian: An Appeal to the Church, ukurasa 141, 142.

Katika mkondo huu wa mambo ya kidunia na usakaji wa anasa, kujikana nafsi na kujitolea binafsi kwa ajili ya Kristo vimetoweka kwa kiwango kikubwa. “Baadhi ya wanaume na wanawake sasa wanaojishirikisha katika makanisa yetu walifundishwa, wakiwa watoto, kujinyima ili kuweza kutoa au kufanya kitu fulani kwa ajili ya Kristo.” Lakini “ikiwa fedha zinatakiwa sasa, ... hakuna mtu anayeitwa atoe. La, hapana! Itisha tamasha, maonesho, maigizo, mauzo ya vyakula vya zamani, au kitu fulani cha kula—kitu chochote cha kuwachekesha watu.”

Gavana Washburn wa Wisconsin, katika ujumbe wake wa kila mwaka, wa Januari 9, 1873, alieleza kuwa: “Sheria fulani inaonekana kuhitajika ili kuvunja shule ambazo zinazalisha wacheza kamari. Shule hizi zipo kila mahali. Hata kanisa (bila kujua, bila shaka) nyakati zingine linajikuta likifanya kazi ya Shetani. Maonyesho ya muziki ya zawadi, biashara na kamari za zawadi, nyakati zingine kwa kusudi la kutekeleza malengo ya kidini au msaada, lakini mara nyingi kwa makusudi yasiyofaa sana, bahati nasibu, vifurushi vya zawadi, nk., zote ni nyenzo za kupatia fedha pasipo thamani iliyopatikana. Hakuna jambo linaloharibu

maadili au linalolewesha, hususani kwa vijana, kama kupata pesa au mali bila kufanya kazi. Watu wenye hadhi wanaojihusisha katika biashara hizi, na kutuliza dhamiri zao kwa kufikiri kuwa pesa inakwenda kutekeleza kusudi jema, siyo ajabu kuwa vijana wa taifa wanajikuta mara nyingi wakiangukia katika tabia za msisimko wa michezo ya hatari ambayo kwa kiwango kikubwa huisababisha kwa hakika."

Roho ya kupatana na ulimwengu inapenya ndani ya makanisa yote ya ulimwengu wa Kikristo. Robert Atkins, katika hubiri alilohubiri jijini London, anachora picha ya anguko la kiroho lililoko katika nchi ya Uingereza: "Wacha Mungu wa kweli wanatoweka duniani, na hakuna mtu anayejali, katika kila kanisa, kuna watu wanaopenda ulimwengu, wanaopatana na ulimwengu, wanaopenda faraja ya kiumbe, na wanaotafuta kukubalika. Wameitwa kuteseka na Kristo, lakini wanaogopa kuaibika. Uasi, uasi, uasi, umechorwa mbele ya kila kanisa; na laiti wangelijua hilo, na laiti wangelihisi hilo, kungekuwa na tumaini; lakini, ala! Wanapiga kelele, 'Sisi ni matajiri, tumejitajirisha, wala hatuna haja ya kitu.'"—Second Advent Library, tract No. 39.

Dhambi kubwa ambayo Babeli unashitakiwa nayo ni kuwa Babeli uliwanywesha "mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Hiki kikombe cha mvinyo ambacho Babeli unawapa watu wa ulimwengu huwakilisha mafundisho ya uongo ambayo ameyapata kama matokeo ya mshikamano haramu na wakuu wa dunia. Urafiki wa kanisa na dunia hunajisi imani ya kanisa, na matokeo yake kanisa huwa na mvuto unaonajisi ulimwengu kwa kufundisha mafundisho yaliyo kinyume na mafundisho ya wazi ya Maandiko Matakatifu.

Rumi ilificha Biblia isisomwe na watu na liliwataka watu wote wayapokee mafundisho yake badala ya Biblia. Ilikuwa kazi ya Matengenezo kuwarudishia watu neno la Mungu; lakini siyo kweli kuwa katika makanisa ya wakati wetu watu wanafundishwa kujenga imani yao katika matamko yao ya imani na mafundisho ya kanisa kuliko Maandiko? Charles Beecher alisema, akizungumza kuhusu makanisa ya Kiprotestanti: "Wanachukia wakati neno baya linaposemwa dhidi ya imani yao kwa hisia kali kama zile za mababa watakatifu wanavyochukia wakati neno linalokosoa lilipotamkwa dhidi ya ibada ya watakatifu na wafia dini. Madhehebu ya Waprotestanti wa Kiinjiisti yameshikamana sana wao kwa wao kiasi kwamba, mtu ye yote miongoni mwao, hawezi kuwa mhubiri kabisa, mahali popote, asipokubali kitabu fulani kando ya Biblia. hakuna kitu cha kufikirika katika kauli kuwa nguvu ya mfumo wa imani inaanza kuzuia Biblia kwa hakika kama vile Rumi ilivyofanya, japo kwa njia ya hila zaidi."—Sermon on "The Bible a Sufficient Creed," delivered at Fort Wayne, Indiana, Feb. 22, 1846.

Wakati waalimu waaminifu wanapoeleza neno la Mungu, wanainuka watu wasomi, wachungaji wanaojidai kuelewa Maandiko, wanaokataa mafundisho sahihi kama uzushi, na hivyo wanarudisha nyuma juhudi za kuutafuta ukweli. Kama ulimwengu ungekuwa haujanyweshwa mvinyo wa Babeli, watu wengi wangeshawishika na kuongolewa na ukweli

ulio wazi, unaokata wa neno la Mungu. Lakini imani ya kidini inaonekana kuwa imechafuka mno na kuwa na mambo mengi yanayopingana kiasi kwamba watu hawajui ni jambo lipi la kuamini kama ukweli. Dhambi ya kutotubu kwa ulimwengu inalala katika mlango wa kanisa.

Ujumbe wa malaika wa pili wa Ufunuo 14 ulihubiriwa kwa mara ya kwanza katika msimu wa kiangazi cha mwaka 1844, na wakati ule ulihusu moja kwa moja zaidi makanisa ya Marekani, ambapo onyo la hukumu lilikuwa limehubiriwa katika maeneo mengi na kukataliwa na watu walio wengi, na mahali ambapo hali ya kurudi nyuma katika makanisa ilikuwa ya haraka zaidi kuliko maeneo mengine. Lakini ujumbe wa malaika wa pili haukufikia utimizwaji wake kikamilifu mwaka 1844. Makanisa wakati ule yalipata anguko la uadilifu, kama matokeo ya kukataa kwao nuru ya ujumbe wa marejeo; lakini anguko lile halikuwa kamili. Na kwa kadiri yalivyoendelea kukataa ukweli maalumu kwa ajili ya wakati huu yameendelea kuanguka chini na chini zaidi. Lakini, hata hivyo, haiwezi kusemwa kuwa "Umeanguka Babeli,… maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake."

Bado Babeli hajawafanya mataifa yote yafanye hivyo. Roho ya kushikamana na ulimwengu na kupuuza ukweli unaopima wa wakati wetu ipo na inaendelea kuota mizizi katika makanisa ya imani ya Kiprotestanti katika nchi zote za Ukristo; na makanisa haya yamejumuishwa katika onyo kali na kutisha la malaika wa pili. Lakini kazi ya uasi bado haijafikia kipeo chake. Biblia inatangaza kuwa kabla ya kuja kwa Bwana, Shetani atatenda "kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu;" na kwamba wale ambao "hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa," wataachwa wapokee "nguvu ya upotevu, wauamini uongo" (2 Wathesalonike 2:9-11). Ni mpaka hali hii itakapofikiwa, na muungano wa kanisa na ulimwengu utakapokamilika katika ulimwengu wote wa Ukristo, ndipo anguko la Babeli litakapokamilika. Badiliko ni la hatua kwa hatua, na utimizo wa Ufunuo 14:8 bado ni wa wakati ujao.

Licha ya giza la kiroho na utengano na Mungu ulioko katika makanisa yanayounda Babeli, kundi kubwa la wafuasi wa kweli wa Kristo bado wapo katika ushirika wao. Kuna wengi wao ambao hawajaona ukweli maalumu wa wakati huu. Siyo wachache ambao hawajaridhika na hali yao ya sasa na watamani nuru iliyo wazi zaidi. Wanaangalia Sura ya Kristo katika makanisa yaliyo na ushirika wao bila mafanikio. Na makanisa haya yanavyozidi kwenda mbali na ukweli zaidi, na kujiungamanisha kwa karibu zaidi na ulimwengu, tofauti kati ya makundi mawili itakuwa kubwa zaidi, na hatimaye watatengana. Wakati utafika ambapo wale wanaompenda Mungu kweli kweli hawataendelea kuwa na mshikamano na wale "wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; walio na mfano wa utauwa, lakini wakiikana nguvu yake." Ufunuo 18 huelezea wakati ambapo, kama matokeo ya kukataa onyo lenye sehemu tatu la Ufunuo 14:6-12, kanisa litakuwa limefikia kikamilifu hali iliyotabiriwa na malaika wa pili, na watu wa Mungu ambao watakuwa bado katika Babeli wataitwa watoke katika ushirika wake. Ujumbe huu ni wa mwisho kutolewa ulimwenguni; na utatimiza kazi

yake. Wakati wale ambao“hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu” (2 Wathesalonike 2:12), wataachwa wapokee uongo mkubwa zaidi na watauamini uongo, ndipo nuru ya ukweli itawaangazia wale ambao mioyo yao iko wazi kuupokea, na watoto wote wa Bwana ambao bado katika Babeli wataisikia sauti: “Tokeni kwake, Enyi watu wangu” (Ufunuo 18:4).

Sura ya 22 - Unabii Watimia

Muda ulipopita ambao ujio wa Bwana ulikuwa umetarajiwa kwanza,— majira ya kuchipua ya mwaka 1844,—wale waliokuwa wametazamia kwa imani ujio Wake kwa kipindi fulani walipatwa na mashaka na kutokuwa na hakika. Wakati ambapo ulimwengu uliwaona kama watu ambao wameshindwa vibaya na kuthibitika kuwa walikuwa wameamini uongo, chanzo cha faraja yao bado kilikuwa ni neno la Mungu. Wengi wao waliendelea kuchunguza Maandiko, wakipima upya ushahidi wa imani yao na kujifunza kwa makini unabii ili wapate nuru zaidi. Ushuhuda wa Biblia uliounga mkono msimamo wao ulioonekana kuwa wazi na hitimivu. Dalili ambazo zisingeweza kukosewa zilielekeza kwa ujio wa Kristo kama uliokuwa karibu. Mbaraka maalum wa Bwana, katika uongofu wa wenye dhambi na uamsho wa maisha ya kiroho miongoni mwa Wakristo, ulikuwa umethibitisha kuwa ujumbe ulikuwa wa Mbinguni. Na ingawa waaminio hawakuweza kueleza kukatishwa tamaa kwa matarajio yao, walihisi kuwa Mungu alikuwa amewaongoza katika uzoefu wao uliokuwa umepita.

Katika aya zenye unabii ambao waliamini kuwa ulihusu wakati wa ujio wa pili, yalikuwemo mafundisho mahsusi yaliyoshughulikia hali yao ya kutokuwa na hakika na ya kujawa na mashaka, na mafundisho hayo yaliwapa shime na kuwafanya wawe na uvumilivu na imani kuwa kile ambacho kilikuwa giza kwa ufahamu wao kingeweza kwa wakati mwafaka kueleweka wazi kwao.

Miongoni mwa aya hizo za unabii ni ile ya Habakuki 2:1-4: “Mimi nitasimama katika zamu yangu, nitajiweka juu ya mnara, nitaangalia ili nione atakaloniambia, na jinsi nitakavyojibu katika habari ya kulalamika kwangu. Bwana akanijibu, akasema, Iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji. Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia. Tazama, roho yake hujivuna, haina unyofu ndani yake; lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake.”

Mapema kabisa mwaka 1842 agizo lililotolewa katika unabii huu la “Iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji,”lilipendekeza kwa Charles Fitch kuandaa chati ya unabii kuonesha njozi za Danieli na Ufunuo. Uchapishaji wa chati hii ulichukuliwa kama utimizaji wa amri iliyotolewa na Habakuki. Hakuna hata mmoja, hata hivyo, aliyegundua wakati huo kuwa kuonekana kuchelewa kwa namna fulani katika utimizwaji wa njozi—muda wa kusubiri—kumewasilishwa katika unabii uo huo. Baada ya kukatishwa tamaa, andiko hili lilionekana kuwa na maana sana: “Njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia…. Mwenye haki ataishi kwa imani yake.” Sehemu ya unabii wa Ezekieli pia ilikuwa chanzo cha nguvu na faraja kwa walioamini: “Neno la Bwana likanijia, kusema, Mwanadamu, ni mithali gani hii mliyo nayo katika nchi ya Israeli, mkisema, Siku hizo zinakawia na maono yote hayatimizwi. Basi

uwaambie, Bwana MUNGU asema hivi.... Siku hizo ni karibu, na utimilizo wa maono yote.... Mimi nitanena, na neno lile nitakalolinena litatimizwa; wala halitakawilishwa tena." "Hao wa nyumba ya Israeli husema, Maono hayo ayaonayo ni ya siku nyingi zijazo, naye anatabiri habari ya nyakati zilizo mbali sana. Basi uwaambie, Bwana MUNGU asema hivi; Maneno yangu hayatakawilishwa tena hata moja, bali neno nitakalolinena litatimizwa" (Ezekieli 12:21-25, 27, 28).

Waliokuwa wakingoja walifurahia, wakiamini kuwa Yeye ajuaye mwisho tangu mwanzo aliangalia kupitia katika zama zote na, akiona zama nyingi kabla kukatishwa tamaa kwao, aliwapa maneno ya ujasiri na tumaini. Isingekuwa kwa njia ya sehemu hizo za Maandiko, zilizowahimiza kungoja kwa uvumilivu na kushikilia kwa uthabiti neno la Mungu, imani yao ingeshindwa katika saa ile ya kujaribiwa.

Mfano wa wanawali kumi wa Mathayo 25 pia huonesha kielelezo cha uzoefu wa Waadventista. Katika Mathayo 24, katika kujibu swali la wanafunzi Wake kuhusiana na dalili ya ujio Wake na ya mwisho wa dunia, Kristo alionesha baadhi ya matukio muhimu sana katika historia ya ulimwengu na ya kanisa tangu ujio Wake wa kwanza hadi ujio Wake wa pili; ambayo ni, kuharibiwa kwa Yerusalemu, dhiki kuu ya kanisa chini ya mateso ya kipagani na ya kipapa, kutiwa giza jua na mwezi, na kuanguka kwa nyota. Baada ya hayo alisema juu ya ujio Wake katika ufame Wake, na alisimulia mfano unaoeleza makundi mawili ya watumishi wanaotazamia kuja Kwake. Sura ya 25 huanza kwa maneno: "Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi." Hapa linaoneshwa kanisa linaloishi katika siku za mwisho, lile lile ambalo limetajwa katika sehemu ya mwisho ya Sura ya 24. Katika mfano huu uzoefu wao unaelezwa kwa njia ya kielelezo cha matukio ya ndoa ya Mashariki.

"Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi, waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi. Watano wao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara. Wale waliokuwa wapumbavu walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao; bali wale wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usiku wa manane, pakawa na kelele, Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki."

Ujio wa Kristo, kama unavyotangazwa na malaika wa kwanza, ulieleweka kuwakilishwa na ujio wa bwana arusi. Matengenezo yaliyoenea mahali pengi kama matokeo ya utangazwaji wa ujio Wake wa haraka, yanalinganishwa na kutoka kwa wanawali kumi. Katika mfano huu, kama ilivyo katika mfano wa Mathayo 24, makundi mawili ya watu yamewakilishwa. Wote walichukua taa zao, Biblia, na kwa njia ya nuru yake waliondoka kwenda kumlaki Bwana arusi. Lakini wakati ambapo"wale waliokuwa wapumbavu walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao," "wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao." Kundi la pili lilipokea neema ya Mungu, nguvu inayoumba upya, inayoleta ufahamu wa Roho Mtakatifu, ambaye hulifanya neno la Mungu kuwa taa ya miguu na mwanga wa njia.

Katika kicho cha Mungu walijifunza Maandiko kuujua ukweli, na walitafuta kwa dhati usafi wa moyo na wa maisha. Hawa walikuwa na uzoefu binafsi, imani kwa Mungu na kwa neno Lake, ambayo isingeweza kushindwa kwa kukatishwa tamaa au kuchelewa. Wengine "walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao." Hawa walikwenda kwa mhemko. Hofu zao zilichochewa na ujumbe wa kutisha, lakini walitegemea imani ya ndugu zao, waliridhishwa na nuru ya hisia nzuri, bila ufahamu wa kina wa ukweli au kazi halisi ya neema ndani ya moyo. Hawa walitoka kwenda kumlaki Bwana, wakiwa na tumaini la kupokea zawadi haraka; lakini hawakuwa wamejiandaa kwa ajili ya kuchelewa na kukatishwa tamaa. Majaribu yalipokuja, imani yao ilishindwa, na nuru yao ilififia.

"Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi." Kuchelewa kwa bwana arusi kunawakilishwa na kupita kwa wakati ambao Bwana alikuwa ametarajiwa, kukatishwa tamaa, na kuchelewa kulikojitokeza. Katika wakati huu wa kutokuwa na hakika, shauku ya wale walio na imani ya juu juu na waliojitokeza kumlaki Bwana wakiwa mguu mmoja ndani na mguu mwingine nje walianza kubabaika, na juhudi zao zilipungua; lakini wale ambao imani yao ilikuwa imejengwa juu ya ujuzi binafsi wa Biblia walikuwa na mwamba chini ya nyayo zao, ambao mawimbi ya kukatishwa tamaa hayakuweza kuuondosha. "Wote wakasinzia wakalala usingizi;" kundi moja likiwa katika hali ya kutojali na kutupilia mbali imani yao, kundi jingine likingoja kwa uvumilivu mpaka nuru ya wazi zaidi iweze kutolewa. Hata hivyo katika usiku wa kujaribiwa kundi la pili lilionekana kupoteza, kwa kiasi fulani, juhudi na imani yao. Wale waliojitoa nusu na wenye imani ya juu juu hawakuweza tena kutegemea imani ya ndugu zao. Kila mmoja anapaswa kusimama au kuanguka mwenyewe.

Karibu na muda huu, ushikiliaji sana wa mambo bila kutumia akili ulianza kujitokeza. Baadhi ya wale waliokuwa wamedai kuwa waumini wenye bidii wa ujumbe wa marejeo walitupilia mbali neno la Mungu kama mwongozo pekee usiokosea na, wakidai kuongozwa na Roho, walijiachia na kutawaliwa na mihemko, maono, na mawazo yao. Walikuwepo baadhi yao waliooonesha juhudi zisizo na maana na kukosa uvumilivu kwa wengine, wakiwalaumu wale wote ambao hawakukubaliana na njia zao. Mawazo na matendo yao hayakupokelewa na kundi kubwa la Waadventista; hata hivyo walileta aibu kwa njia ya ukweli.

Shetani alitaka kutumia njia hii kupinga na kuharibu kazi ya Mungu. Watu walikuwa wamepata uamsho mkubwa kutokana na vuguvugu la marejeo, maelfu ya wenye dhambi waliongoka, na watu waaminifu walijitolea kutangaza ukweli, hata wakati wa kujaribiwa. Mfalme wa uovu alikuwa anapoteza raia wake; na ili kuiaibisha kazi ya Mungu, alijaribu kuwadanganya baadhi ya watu walioikiri imani na kuwafanya wawe na misimamo mikali. Ndipo mawakala wake walijiandaa kutumia kila kosa, kila kushindwa, kila tendo la kipuuzi, na kuliweka mbele ya watu katika namna iliyokuzwa sana, kuwafanya Waadventista na imani yao wachukiwe. Hivyo kwa kadiri alivyopata idadi kubwa ya watu ambao angeweza

kuwakusanya na kuwafanya wadai kuamini injili ya ujio wa pili wakati nguvu yake ikitawala mioyo yao, ndivyo angenufaika zaidi kwa kuwafanya watu wawaone kuwa wawakilishi wa jamii yote ya waaminio.

Shetani ni "mshitaki wa ndugu" na ni roho yake ambayo huwachochea watu watafute makosa na mapungufu ya watu wa Bwana, na kuwafanya watu wengine wayaone, ilhali matendo yao mema yanapitwa bila kutajwa. Yeye yuko kazini daima wakati Mungu akiwa kazini kwa ajili ya wokovu wa roho. Wakati wana wa Mungu wanapokuja mbele za Bwana, Shetani anakuja pia miongoni mwao. Katika kila uamsho yuko tayari kuingiza wale ambao hawajatakaswa mioyoni mwao na ambao akili zao zina mashaka. Wakati hawa wanapopokea baadhi ya vipengele vya ukweli, na kupata nafasi miongoni mwa waaminio, anafanya kazi kupitia kwao kuingiza nadharia zinazowapotosha wasio na tahadhari. Hakuna mtu anayethibitika kuwa ni Mkristo wa kweli kwa sababu tu yumo miongoni mwa watu wa Mungu, hata katika nyumba ya ibada na kwenye meza ya Bwana. Shetani yupo daima katika matukio muhimu kwa njia ya wale ambao anaweza kuwatumia kama mawakala wake.

Mfalme wa uovu anapinga kila hatua ambayo watu wa Mungu wanaipiga katika safari yao ya kuelekea katika mji wa mbinguni. Katika historia yote ya kanisa hakuna matengenezo ambayo yamewahi kufanywa bila kukutana na vikwazo vya kutisha. Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Paulo. Kila mahali ambapo mtume alianzisha kanisa, wapo baadhi waliodai kupokea imani, lakini ambao waliingiza mafundisho ya uongo, ambayo, ikiwa yangepokelewa, yangeweza hatimaye kufutilia mbali roho ya kuupenda ukweli. Luther pia alipata mashaka makubwa na udhia kutokana na kazi ya watu wanaoshikilia sana mambo bila kutumia akili waliodai kuwa Mungu aliongea moja kwa moja kupitia, na ambao hatimaye waliweka mawazo na maoni yao juu ya ushuhuda wa Maandiko. Wengi ambao hawakuwa na imani na uzoefu, lakini waliokuwa na kiasi fulani cha kujitumainia na kuridhika, na waliopenda kusikiliza na kusimulia mambo mapya, walidanganywa na maigizo ya walimu wapya, na walijiunga na mawakala wa Shetani katika kazi yao ya kubomoa kile ambacho Mungu alikuwa amemwongoza Luther kukijenga. Na akina Wesley, na wengine walioubariki ulimwengu kwa mvuto wao na imani yao, walikutana katika kila hatua na hila za Shetani akiwasukuma watu wenye bidii kupita kiasi, wenye mashaka, na wasiotakaswa na kuwafanya wawe washupavu wa kidini wa kila kiwango.

William Miller alipinga sana mivuto iliyokuwa na mwelekeo wa kujenga ushupavu wa kidini. Alisema, kama alivyosema Luther, kuwa kila roho lazima ipimwe kwa neno la Mungu. "Shetani," Miller alisema, "ana nguvu nyingi juu ya akili za baadhi ya watu waliopo hapa leo. Na tutajuaje ni roho gani waliyo nayo? Biblia inajibu: 'Mtawatambua kwa matunda yao.'... Kuna roho nyingi zimeenea duniani; na tumeagizwa kuzijaribu roho. Roho ambayo haituongozi kuishi maisha ya kiasi, ya haki, na ya utauwa, katika ulimwengu huu, sio Roho ya Kristo. Nimeshawishika zaidi na zaidi kuwa Shetani anahusika na hizi vurugu Wengi miongoni mwetu wanaojifanya kuwa wametakaswa kikamilifu, wanafuata mapokeo ya

wanadamu, na kwa kiasi kikubwa hawajui ukweli kama wengine ambao hawafanyi maigizo hayo."—Bliss, ukurasa 236, 237. "Roho ya uongo itatusababisha kuuacha ukweli; na Roho wa Mungu atatuongoza katika ukweli. Lakini, mnasema, mtu anaweza kukosea, na akadhani yuko sahihi. Sasa inakuwaje? Tunajibu, Roho na neno vinakubaliana. Ikiwa mtu anaamua mwenyewe kwa njia ya neno la Mungu, na anapata mwafaka kamili katika Maandiko yote, ana haki ya kuamini kuwa ana ukweli; lakini ikiwa anakuta roho inayomwongoza haiafikiani na mwongozo wote wa sheria ya Mungu au Kitabu chote, hapo hebu aende pole, asije akanaswa katika mtego wa Shetani."—The Advent Herald and Signs of the Times Reporter, January 15, 1845.

Katika siku za Matengenezo, maadui wa matengenezo walidai maovu yanayotokana na ushikiliaji sana wa mambo bila kutumia akili yalitokana na kazi ya wanamatengenezo—ingawa wanamatengenezo ndio waliokuwa wakifanya kazi kubwa na ya dhati kuupinga. Njia kama hiyo ilifuatwa na wapinzani wa vuguvugu la marejeo. Na kwa kutoridhika na uwakilishaji potovu na kukuza makosa yanayofanana na ukweli ya watu wenye misimamo mikali na washikiliaji sana wa mambo bila kutumia akili, walisambaza taarifa mbaya ambazo hazikuwa na ukweli hata kidogo. Watu hawa walisukumwa na ubaguzi na chuki. Amani yao ilibughudhiwa na mahubiri ya ujio wa haraka wa Kristo. Waliogopa kuwa inaweza kuwa kweli, lakini walitumaini haikuwa hivyo, na hii ilikuwa siri ya vita yao dhidi ya Waadventista na imani yao.

Ukweli kuwa washupavu wa kidini wachache walikuwa miongoni mwa makundi ya Waadventista sio sababu ya kuamua kuwa vuguvugu hilo halikuwa la Mungu kuliko uwepo wa watu kama hao na wadanganyaji katika siku za Paulo au siku za Luther au kuwa kisingizio cha kuikataa kazi yao. Hebu watu wa Mungu waamke kutoka usingizini na waanze kazi ya toba na matengenezo; hebu wachunguze Maandiko ili wajifunze ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu; hebu wajisalimishe kikamilifu kwa Mungu, na ushahidi hautakosekana kuwa Shetani bado anafanya kazi na yuko macho. Kwa njia zote zinazowezekana za uongo ataonesha nguvu yake, na kuwakusanya malaika wote walioanguka walioko chini ya himaya yake kumsaidia.

Sio utangazaji wa ujio wa pili uliosababisha ushupavu wa kidini na migawanyiko. Mambo haya yalitokea katika msimu wa kiangazi mwaka 1844, wakati Waadventista walipokuwa katika hali ya mashaka na sintofahamu kuhusiana na msimamo wao hasa. Utangazaji wa ujumbe wa malaika wa kwanza na wa "kilio cha usiku wa manane" ulikuwa na mwelekeo wa kudhibiti ushikiliaji sana mambo bila kutumia akili na migawanyiko. Wale walioshiriki katika mahubiri haya makini walikuwa na upatanifu mkamilifu; mioyo yao ilijazwa na upendo wa kila mmoja kwa mwingine na wa kila mmoja kwa Yesu, ambaye walitarajia kumwona muda mfupi uliokuwa unakuja. Imani moja, tumaini moja lenye baraka, viliwainua juu ya utawala wa mvuto wowote wa kibinadamu, na vilikuwa ngao dhidi ya mashambulizi ya Shetani.

“Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usiku wa manane, pakawa na kelele, Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki. Mara wakaondoka wanawali wale wote, wakazitengeneza taa zao” (Mathayo 25:5-7). Wakati wa kiangazi cha mwaka 1844, katikati ya wakati ambao ulikuwa umefikiriwa mwanzoni kuwa siku 2300 zingekomea, na wakati wa vuli ya mwaka huo huo, ambao ilionekana baadaye kuwa siku hizo zilifika, ujumbe ulitangazwa kwa kutumia maneno yale yale ya Maandiko: “Haya, Bwana arusi anakuja!” Kilichofanya vuguvugu hili litokee ilikuwa ugunduzi wa ile amri ya Artashasta ya kuujenga upya mji wa Yerusalemu, ambayo ilichukuliwa kama tarehe ya kuanza kwa kipindi cha siku 2300, ambayo ilianza kutekelezwa wakati wa vuli ya mwaka 457 K.K., na siyo mwanzoni mwa mwaka, kama ilivyokuwa imeaminiwa mwanzoni.

Kwa kukokotoa kuanzia wakati wa vuli ya 457, miaka 2300 iliishia wakati wa vuli ya mwaka 1844. (Tazama Kiambatanisho kwa ajili ya ukurasa 329.) Hoja zilizochukuliwa kutoka katika mifano ya Agano la Kale zilielekeza pia kwa wakati wa vuli kama wakati ambao tukio lililowakilishwa na “kutakaswa kwa patakatifu” lingetokea. Hili lilielezwa vizuri pale mkazo ulipowekwa katika namna mifano iliyohusu ujio wa kwanza wa Kristo ilivyotimizwa.

Kuchinjwa kwa mwanakondoo wa Pasaka kulikuwa kivuli cha kifo cha Kristo. Paulo anasema:“Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani, Kristo” (1 Wakorintho 5:7). Mganda wa malimbuko, ambao wakati wa Pasaka ulitikiswa mbele ya Bwana, ulikuwa mfano wa ufufuko wa Kristo. Paulo anasema, akiongelea kuhusu ufufuo wa Bwana na wa watu Wake wote: “Limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja” (1 Wakorintho 15:23). Kama mganda wa kutikiswa, ambao ulikuwa nafaka za kwanza kukomaa kwanza zilizokusanywa kabla ya mavuno, Kristo ni limbuko la mavuno yale yasiyopatikana na mauti ya waliokombolewa ambao wakati wa ufufuo ujao watakusanywa katika ghala la Mungu. Atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, , kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake

Mifano hii ilitimizwa, sio tu kama tukio, bali pia kama wakati. Siku ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza wa Kiyahudi, siku ile ile na mwezi ule ule ambao kwa karne kumi na tano kondoo wa Pasaka alikuwa akichinjwa, Kristo, akiwa amekula Pasaka na wanafunzi Wake, alianzisha sherehe ambayo ilipaswa kuadhimisha kumbukumbu ya kifo Chake mwenyewe kama“Mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” Usiku ule ule alikamatwa na mikono miovu na kupelekwa kusulubiwa na kuuawa. Na kama Yule ambaye mfano wa mganda wa kutikiswa ulimlenga, Bwana wetu alifufuliwa kutoka katika wafu siku ya tatu, “limbuko lao waliolala,” mfano wa wenye haki wote watakaofufuliwa, ambapo, (mwili wetu wa unyonge” utabadilishwa, “upate kufanana na mwili wake wa utukufu” (Aya ya 20; Wafilipi 3:21).

Kwa jinsi iyo hiyo mifano inayohusu ujio wa pili wa Kristo inapaswa kutimizwa kwa wakati uliotajwa katika huduma ya mifano. Katika mfumo wa Musa, utakaso wa patakatifu,

au Siku kuu ya Upatanisho, ulitokea siku ya kumi ya mwezi wa saba wa Kiyahudi (Walawi 16:29-34), wakati kuhani mkuu, baada ya kufanya upatanisho kwa ajili ya wana wa Israeli wote, na kwa njia hiyo kuondoa dhambi zao zote kutoka katika patakatifu, alitoka nje na kuwabariki watu. Kwa hiyo iliaminika kuwa Kristo, Kuhani wetu Mkuu, angetokea kutakasa dunia kwa njia ya kuangamiza dhambi na wenye dhambi, na kuwabariki watu Wake wanaongojea kwa kuwapa hali ya kutokufa. Siku ya kumi ya mwezi wa saba, Siku kuu ya Upatanisho, wakati wa kutakasa patakatifu, ambayo mwaka 1844 ilikuwa siku ya ishirini na mbili ya mwezi Oktoba, ilichukuliwa kuwa wakati wa kuja kwa Bwana. Tarehe hii iliafikiana na uthibitisho uliokuwa umekwishatolewa kuwa siku 2300 inaishia wakati wa vuli, na hitimisho lililoonekana kutozuilika.

Katika mfano wa Mathayo 25, kipindi cha kungojea na kusinzia hufuatwa na ujio wa bwana arusi. Hili lilikuwa sawasawa na hoja zilizokuwa zimewasilishwa, kutoka sehemu zote mbili—kutoka katika unabii na kutoka katika mifano. Walikuwa wameshawishika sana kuhusiana na ukweli waliohubiri; na "kilio cha usiku wa manane" kilihubiriwa na maelfu ya walioamini.

Kama wimbi la maji kupwa na kujaa, vuguvugu la marejeo lilifagia katika nchi. Kutoka jiji hadi jiji, kutoka kijiji hadi kijiji, na sehemu za pembezoni mwa nchi vuguvugu lilifika, mpaka watu wa Mungu waliokuwa wakingoja walipoamshwa kikamilifu. Ushupavu wa kidini ulitoweka wakati wa vuguvugu hili kama umande wa asubuhi unavyoyeyuka wakati jua linapochomoza. Waaminio waliona mashaka na fadhaa zao zikitoweka, na tumaini na ujasiri vilichangamsha mioyo yao. Kazi haikuwa na misimamo mikali ambayo daima hujitokeza wakati kunapokuwepo msisimko wa kibinadamu pasipokuwepo nguvu inayodhibiti ya neno na Roho wa Mungu. Uzoefu ule ulifanana katika tabia na misimu ya unyenyekevu na kumrudia Mungu kulikotokea miongoni mwa Waisraeli wa zamani baada ya kupokea ujumbe wa onyo kutoka kwa watumishi Wake. Ulibeba tabia inayoonekana katika kazi ya Mungu katika kila zama. Furaha ilikuwepo, lakini kulikuwa na msisimko mdogo, badala yake kulikuwepo kujichunguza mioyo kwa kina, kuungama dhambi, na kuachana na ulimwengu. Kujiandaa kwa ajili ya kukutana na Bwana ulikuwa ndiyo mzigo wa roho zilizokuwa zikiumia. Kulikuwepo maombi ya dhati na kujiweka wakfu kwa Mungu kikamilifu.

Miller alisema akielezea uzoefu ule: "Hakuna onesho kubwa la furaha: yaani, ni kana kwamba, furaha ilitunzwa kwa ajili ya wakati ujao, wakati mbingu na dunia yote itakapofurahi pamoja kwa furaha isiyoneneka na ikiwa imejaa utukufu. Hakuna kupiga kelele: yaani, pia, zilihifadhiwa kwa ajili ya kupiga kelele za mbinguni. Waimbaji wako kimya: wanasubiri kujiunga na majeshi ya mbinguni, kwaya ya mbinguni. Hakuna mgongano wa hisia: wote wana moyo mmoja na akili moja."—Bliss, ukurasa 270, 271.

Mwingine aliyeshiriki katika vuguvugu lile alishuhudia: "Vuguvugu lilileta kila mahali kujichunguza moyo kwa kina sana na kujinyenyekesha kwa kila roho mbele za Mungu wa

mbinguni juu. Lilihamisha shauku ya watu kutoka kwa vitu vya ulimwengu huu, lilileta uponyaji dhidi ya mashindano na uadui, liliwafanya watu kuungama makosa yao, na kupondeka mbele za Mungu, lilileta toba, lilihamasisha maombi ya kuvunjika moyo kwa Mungu kwa ajili ya msamaha na kukubaliwa. Lilisababishwa kujishusha na kupondeka kwa roho, kwa namna ambayo haijapata kushuhudiwa kabla. Kama Mungu kupitia kwa Yoeli alivyoamuru, wakati siku kuu ya Mungu ilipokaribia, ilileta uraruaji wa mioyo na wala si mavazi, na kumrudia Bwana kwa kufunga, na kulia, na kuomboleza. Kama Mungu alivyosema kwa njia ya Zakaria, roho ya neema na dua ilimwagwa juu ya watoto Wake; walimwangalia Yeye waliyemchoma kwa mikuki, kulikuwepo maombolezo katika nchi, ... na wale waliomtazamia Bwana waalijitesa roho zao mbele Yake."—Bliss, in Advent Shield and Review, vol. I, uk. 271 (January, 1845).

Katika harakati zote za kidini tangu siku za mitume, hakuna harakati hata moja ambayo ilikuwa na kiasi kidogo cha mapungufu ya kibinadamu na hila za Shetani chache zaidi ya ile ya msimu wa vuli ya mwaka 1844. Hata sasa, baada ya kupita miaka mingi, wote walioshiriki katika vuguvugu lile na wale waliosimama imara juu ya jukwaa la ukweli bado wanahisi mvuto mtakatifu wa kazi ile iliyobarikiwa na wanatoa ushuhuda kuwa lilikuwa vuguvugu la Mungu. Baada ya kusikia wito, "Haya, bwana arusi amekuja; tokeni mwende kumlaki," waliokuwa wakingojea "wakaondoka, wakazitengeneza taa zao;" walijifunza neno la Mungu kwa shauku kubwa kabla hawajajulikana. Malaika walitumwa kutoka mbinguni kuwaamsha wale waliokuwa wamekatishwa tamaa na kuwaandaa waweze kupokea ujumbe.

Kazi haikusimama katika hekima na elimu ya watu, bali katika nguvu ya Mungu. Hawakuwa watu wenye talanta kubwa zaidi kuliko watu wengine wote, bali walikuwa watu wanyenyekevu na waliojiweka wakfu sana, ambao walikuwa wa kwanza kusikia na kutii wito. Wakulima waliacha mazao yao yakiwa yamesimama katika mashamba yao, mafundi waliweka chini zana zao, na wakiwa na machozi na furaha walitoka kwenda kutoa onyo. Wale waliokuwa wa kwanza kuongoza kazi walikuwa miongoni mwa watu wa mwisho kujiunga na vuguvugu hili. Makanisa, kwa jumla, walifunga milango yao dhidi ya ujumbe huu, na kundi kubwa la wale walioupokea waliojiondoa katika ushirika wa makanisa. Kwa uongozi wa Mungu, utangazaji huu uliungana na ujumbe wa malaika wa pili na kuleta nguvu kwa kazi ile.

Ujumbe, "Haya, bwana arusi amekuja!" halikuwa suala hasa la kubishania, ingawa ushahidi wa Maandiko ulikuwa wazi na hitimishi. Ulikwenda ukiwa na nguvu shinikizi ambayo ilitikisa roho. Hakukuwa na mashaka, na hakukuwa na maswali. Wakati Kristo alipoingia Yerusalemu kwa shangwe watu walipokuwa wamekusanyika kutoka sehemu zote za nchi kuadhimisha sikukuu walikusanyika katika Mlima wa Mizeituni, na walipojiunga na umati uliokuwa ukimsindikiza Yesu walidaka hamasa ya saa ile na kusaidia kuongeza sauti ya kelele: "Ndiye mbarikiwa, yeye ajaye kwa jina la Bwana!" (Mathayo 21:9). Hali kadhalika, wasioamini walifurika katika mikutano ya Waadventista—baadhi kwa sababu ya udadisi,

baadhi kwa kusudi la kudhihaki—kuhisi nguvu ya ushawishi iliyoandamana na ujumbe: “Haya, bwana arusi amekuja!”

Wakati huo ilikuwepo imani iliyoleta majibu kwa maombi—imani iliyoheshimiwa kwa kupewa tunu. Kama manyunyu ya mvua kwenye ardhi yenye kiu, Roho wa neema alishuka juu ya watafutaji wa dhati. Wale waliotarajia kusimama haraka uso kwa uso na Mkombozi wao walihisi furaha kuu ambayo isingeweza kuelezeka. Nguvu ya Roho Mtakatifu inayolainisha na kutiisha iliyeyusha mioyo wakati mbaraka Wake uliposhushwa kwa wingi juu ya waaminifu, waaminio.

Kwa uaminifu na uchaji wale waliokuwa wameupokea ujumbe walifikia wakati ambao walitumaini kukutana na Bwana wao. Kila asubuhi walihisi kuwa ilikuwa wajibu wao wa kwanza kupata ushahidi wa kukubaliwa kwao na Mungu. Mioyo yao iliunganishwa pamoja, na waliomba pamoja na waliombeana sana. Mara nyingi walikutana pamoja katika maeneo yaliyojitenga ili kuzungumza na Mungu, na sauti za kuombeana zilipaa kwenda mbinguni kutoka katika mashamba na vichaka. Uhakikisho wa kukubaliwa na Mwokozi ulikuwa muhimu kwao kuliko chakula chao cha kila siku; na ikiwa wingu lilitia giza akilini mwao, hawakupumzika mpaka lilipoondoka. Kwa kadiri walivyohisi ushuhuda wa neema inayosamehe, walitamani kumwona Yeye ambaye roho zao zilimpenda. Lakini pia walikuwa wakielekea kukatishwa tamaa. Wakati wa matarajio ulipita, na Mwokozi wao hakutokea. Kwa uhakika usioyumba walikuwa wametazamia ujio Wake, na sasa walihisi kama Mariamu wakati, alipokuja kwenye kaburi la Mwokozi na kulikuta likiwa tupu, alisema kwa mshangao na machozi machoni: “Wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka” (Yohana 20:13).

Hisia ya kicho, hofu kuwa ujumbe unaweza kuwa wa kweli, kwa muda fulani uliudhibiti ulimwengu usioamini. Baada ya kupita wakati hofu hii haikuondoka mara moja; mwanzoni hawakuthubutu kushangilia ushindi wao dhidi ya wale waliokatishwa tamaa; lakini kwa kuwa hakuna dalili za ghadhabu ya Mungu zilizoonekana, walipona hofu zao na wakaendelea na kejeli na dhihaka zao. Kundi kubwa la wale waliokuwa wamedai kuamini ujio wa haraka wa Bwana, walikana imani yao. Baadhi waliokuwa na uhakika sana wa tukio la ujio wa pili kiburi chao kiliumizwa sana kiasi ambacho walitamani waondoke ulimwenguni. Kama Yona alivyofanya, walimlaumu Mungu, na walichagua kifo kuliko kuishi. Wale waliokuwa wamejenga imani yao juu ya maoni ya wengine, na siyo juu ya neno la Mungu, walikuwa sasa tayari kubadili maoni yao. Wenye dhihaka waliwaongoa walio dhaifu na waoga na kuwaingiza upande wao, na hawa wote waliungana pamoja katika kutangaza kuwa kulikuwa hakuna hofu wala matarajio sasa. Wakati ulikuwa umepita, Bwana hakuja, na ulimwengu ungebaki vilevile kwa maelfu ya miaka.

Walioamini kwa dhati, kutoka moyoni, walikuwa wametoa vyote kwa ajili ya Kristo na walikuwa wameshiriki uwepo Wake kuliko wakati mwingine wote uliopita. Walikuwa, kama walivyoamini, wametoa onyo lao la mwisho kwa ulimwengu; na, wakisubiri kwa muda mfupi

kupokelewa katika jamii ya Bwana wao wa Kimungu na malaika wa mbinguni, walikuwa, kwa kiwango kikubwa, wamejitenga na jamii ya wale ambao hawakupokea ujumbe. Kwa shauku kubwa walikuwa wakiomba: "Uje, Bwana Yesu, na uje upesi." Lakini hakuja. Na sasa kuchukua majukumu mazito ya mashaka na kadhia za maisha, na kustahimili kejeli na matusi ya ulimwengu wenye dhihaka, lilikuwa jaribu la kutisha la imani na uvumilivu.

Hata hivyo, kukatishwa tamaa huku, hakukuwa kukubwa sana kama kukata tamaa kulikowapata wanafunzi wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo. Yesu alipoingia Yerusalemu kwa shangwe akiwa juu ya mwanapunda, wafuasi Wake waliamini kuwa alikuwa karibu kukalia kiti cha enzi cha Daudi na kuwakomboa Israeli kutoka katika utawala uliowakandamiza. Kwa matumaini makubwa sana na matazamio ya furaha walipigana vikumbo wao kwa wao, kila mmoja akijaribu kuonesha heshima kwa mfalme wao. Wengi walitandaza nguo zao za nje kama zulia katika njia Yake, au walisambaza matawi yenye majani ya mitende. Katika bashasha zao waliungana pamoja na kuimba wimbo wa furaha:"Hosana Mwana wa Daudi!"Wakati Mafarisayo, kwa kuudhiwa na kukasirishwa na kelele hizi za shangwe, walipomwomba Yesu awakemee wanafunzi Wake, alijibu: "Wakinyamaza hawa, mawe yatapiga kelele" (Luka 19:40). Unabii lazima utimizwe. Wanafunzi walikuwa wakitimiza kusudi la Mungu; hata hivyo, walikuwa wakielekea kukatishwa tamaa sana. Siku chache tu zilipopita walishuhudia kifo cha kutisha cha Mwokozi wao, na wakaona akilazwa kaburini. Matarajio yao hayakukidhiwa hata chembe, na matumaini yao yakafa pamoja na Yesu. Ni mpaka wakati Bwana wao alipofufuka kutoka kaburini kwa ushindi ndipo waliweza kuelewa kuwa yote yalikuwa yametabiriwa na unabii, na "kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu" (Matendo 17:3).

Miaka mia tano kabla, Bwana alikuwa ametangaza kupitia kwa nabii Zekaria: "Furahi sana, Ee binti Sayuni; Piga kelele, Ee binti Yerusalemu; Tazama, mfalme wako anakuja kwako; Ni mwenye haki, naye ana wokovu; Ni mnyenyekevu, amepanda punda, Naam, mwana-punda, mtoto wa punda" (Zekaria 9:9). Ikiwa wanafunzi wangegundua kuwa Kristo alikuwa anaenda kuhukumiwa na kufa, wasingetimiza unabii huu.

Hali kadhalika, Miller na wenzake walitimiza unabii na walitoa ujumbe ambao uvuvio ulitabiri kuwa ungetolewa kwa ulimwengu, lakini ambao wasingeutoa kama wangeelewa kikamilifu unabii ulioeleza kukatishwa tamaa kwao, na ukiwaambia ujumbe mwingine wa kuhubiri kwa mataifa yote kabla ya marejeo ya Bwana. Ujumbe wa kwanza na wa pili ulitolewa kwa wakati sahihi na ulitimiza kazi ambayo Mungu alikusudia itekelezwe nao.

Ulimwengu ulikuwa ukifuatilia, ukitarajia kuwa ikiwa wakati ungepita na Kristo asitokee, mfumo mzima wa Uadventista ungekufa. Lakini wakati wengi, kwa kujaribiwa sana, wakiikana imani yao, walikuwepo baadhi waliosimama imara. Matunda ya vuguvugu la marejeo, roho ya unyenyekevu na kujichunguza moyo, ya kuuacha ulimwengu na kufanya matengenezo ya maisha, iliyoandamana na kazi ile, vilishuhudia kuwa vuguvugu lile lilikuwa

la Mungu. Hawakuthubutu kukanusha kuwa nguvu ya Roho Mtakatifu ilishuhudia utangazaji wa ujio wa pili, na hawakuweza kugundua kosa la ukokotoaji wa vipindi vya kiunabii.

Wapinzani wao wenye uwezo mkubwa kabisa hawakuweza kuukosoa mfumo wao wa tafsiri ya unabii. Hawakuweza kuafiki, bila ushahidi wa Biblia, kuachana na misimamo yao ambayo ilifikiwa kwa njia ya kujifunza Maandiko kwa bidii kubwa na maombi mengi, kwa akili zilizoangaziwa na Roho wa Mungu na mioyo iliyokuwa ikiwaka kwa nguvu iliyo hai; misimamo iliyostahimili kukosolewa sana na upinzani mkali wa walimu mashuhuri wa dini na watu wenye hekima ya kidunia, na ambayo ilistahimili kwa uimara mkubwa dhidi ya majeshi ya pamoja ya elimu na ufasaha, na shutuma na dharau za watu wenye heshima zao na watu wa kawaida wa mitaani.

Ni kweli, kulikuwepo kukosea kuhusiana na tukio lililotarajiwa, lakini hata hivyo, hili halikuweza kuyumbisha imani yao katika neno la Mungu. Wakati Yona alipotangaza katika mitaa ya Ninawi kuwa ndani ya siku arobaini mji ungeangamizwa, Mungu alikubali unyenyekevu wa watu wa Ninawi na akawaongezea muda wao wa rehema; pamoja na hayo ujumbe wa Yona ulitoka kwa Mungu, na Ninawi ilijaribiwa kulingana na mapenzi ya Mungu. Waadventista waliamini kuwa kwa jinsi kama hiyo Mungu aliwaongoza kutoa onyo la hukumu. “Ujumbe,”walisema,“umeijaribu mioyo ya wote waliousikia, na umeamsha upendo kwa ajili ya ujio wa Bwana; au umechochea chuki, inayojulikana au isiyojulikana kwa wanadamu, lakini inayojulikana kwa Mungu, dhidi ya ujio Wake. Umechora mstari, ... ili kwamba wale watakaopima mioyo yao, waweze kujua ni upande gani wa mstari wangekutwa, ikiwa Bwana angekuwa amekuja wakati ule— iwapo wangesema kwa furaha, ‘Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja atusaidie;’ au ikiwa wangeiita miamba na milima iwaangukie ili kuwaficha wasiuone uso Wake Yeye aketie juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwanakondoo. Mungu, hivyo basi, tunavyoamini, amewajaribu watu Wake, ameijaribu imani yao, amewathibitisha, na kuona ikiwa wataogopa, katika saa ya kujaribiwa, na kuicha nafasi ambayo angeona inafaa kuwaweka; na ikiwa wangeweza kuachia ulimwengu huu na kuliamini neno la Mungu kwa uthabiti usioyumba.”—The Advent Herald and Signs of the Times Reporter, vol. 8, No. 14 (Nov 13, 1844).

Hisia za wale ambao bado waliamini kuwa Mungu aliwaongoza katika uzoefu wao uliopita zimeelezwa katika maneno ya William Miller: “Ikiwa ningekuwa na uwezo kuishi kwa mara nyingine tena, kwa ushahidi ule ule ambao nilikuwa nao wakati ule, niwe mwaminifu kwa Mungu na kwa mwanadamu, ningefanya kama nilivyofanya.” “Ni tumaini langu kuwa nimetakasa mavazi yangu kutoka kwa damu za watu. Ninahisi kuwa, kwa kadiri ya uwezo wangu, nimejinasua kutoka katika hatia zao zote na hukumu yao.” “Ingawa nimekatishwa tamaa mara mbili,” aliandika huyu mtu wa Mungu, “Sijahuzunika sana au kuvunjika moyo kabisa Tumaini langu katika ujio wa Kristo lina nguvu na litadumu kuwa na nguvu daima. Nimefanya tu kile ambacho, baada ya miaka ya tafakari ya kina, nilihisi ilikuwa wajibu wangu kulifanya. Ikiwa nimekosea, imekuwa hivyo kwa upande wa ukarimu, upendo

kwa wanadamu wenzangu, na usadikisho wa wajibu wangu kwa Mungu." "Jambo moja nalijua, sikuhubiri chochote kile isipokuwa kile tu ambacho nimekiamini; na Mungu amekuwa pamoja nami; nguvu Yake imedhihirika katika kazi, na mengi mazuri yametokea."

"Maelfu ya watu, kwa mtazamo wa kibinadamu, wamehamasishwa kujifunza Maandiko kwa kuhubiri juu ya wakati; na kwa njia hiyo, kwa njia ya imani na umwagikaji wa damu ya Kristo, wamepatanishwa na Mungu."— Bliss, ukurasa 256, 255, 277, 280, 281.

"Sikutafuta tabasamu kutoka kwa watu wenye kiburi, wala kutetemeka wakati ulimwengu ulipokunja uso. Siwezi kununua sasa upendeleo wao, wala siwezi kufanya zaidi ya wajibu wangu ili kuchokoza chuki zao. Sitafuti uhai wangu mikononi mwao, wala siogopi, natumaini, kuupoteza, ikiwa Mungu katika uongozi wake mwema ataamuru hivyo."—J. White, Life of Wm. Miller, ukurasa 315.

Mungu hakuwaacha watu Wake; Roho Wake aliendelea kuwa na wale ambao hawakuikataa mara moja nuru waliyoipokea, na kukana hadharani vuguvugu la marejeo. Katika Waraka kwa Waebrania kuna maneno ya kutia moyo na ya onyo kwa waliojaribiwa, waliongoja wakati wa janga hili: "Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi. Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia. Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu" (Waebrania 10:35-39).

Kwamba onyo hili limeelekezwa kwa kanisa la siku za mwisho huthibitishwa kwa maneno yanayoelekeza kwa ukaribu wa ujio wa Bwana: "Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia."

Na imedokezwa moja kwa moja kuwa kungekuwepo mwonenakano wa kuchelewa. Maelekezo yaliyotolewa hapa yanahusiana moja kwa moja na uzoefu wa Waadventista wakati huu. Watu wanaoonywa hapa walikuwa katika hatari ya kutokuwa na imani. Walikuwa wamefanya mapenzi ya Mungu kwa kufuata uongozi wa Roho Wake na neno Lake; lakini hata hivyo walishindwa kuelewa kusudi Lake katika uzoefu wao uliopita, wala hawakuweza kutambua njia mbele yao, na walijaribiwa kuwa na mashaka kama kweli Mungu alikuwa akiwaongoza. Wakati huu maneno haya yalikuwa na maana kwao: "Sasa mwenye haki ataishi kwa imani."

Wakati nuru kali ya "kilio cha usiku wa manane" ilipoangazia juu ya njia yao, na wakaona unabii ukifunuliwa na utimizwaji wa dalili zilizoashiria kuwa ujio wa Kristo ulikuwa karibu, walikwenda, kama hali yenyewe ilivyokuwa, kwa kuona kwa macho. Lakini sasa, wakiwa wameinamishwa chini kwa matumaini yaliyokatishwa tamaa, wangeweza kuinuka

na kusimama tu kwa kumwamini Mungu na kuliamini neno Lake. Ulimwengu wa dhihaka ulisema: "Mmedanganywa. Acheni imani yenu, na semeni kuwa vuguvugu la marejeo lilikuwa la Shetani." Lakini neno la Mungu lilitangaza: "Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye." Kuikana imani yao hadharani sasa, na kuikataa nguvu ya Roho Mtakatifu iliyoambatana na ujumbe, ingekuwa kurudi nyuma na kuelekea upotevuni. Walitiwa moyo na kupata ujasiri kutokana na maneno haya ya Paulo: "Basi msiutupe ujasiri wenu;" "mnahitaji saburi," "Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia." Usalama wao pekee ulikuwa kushikilia nuru ambayo tayari walikuwa wameipokea kutoka kwa Mungu, kushikilia sana ahadi Zake, na kuendelea kuchunguza Maandiko, na kwa uvumilivu mwingi kungoja ili kupokea nuru zaidi.

Sura ya 23 - Patakatifu ni Nini?

Andiko ambalo juu ya yote mengine limekuwa msingi na nguzo kuu ya imani ya marejeo lilikuwa tamko hili: “Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa” (Danieli 8:14). Haya ni maneno yaliyojulikana sana kwa wote walioamini ujio wa haraka wa Bwana. Katika midomo ya maelfu ya watu unabii huu ulikaririwa kama kauli mbiu ya imani yao. Wote walihisi kuwa juu ya matukio yaliyotabiriwa katika aya hii ndipo kulikuwa na matarajio na matumaini waliyojivunia. Siku hizi za kiunabii zilionekana kuishia wakati wa vuli ya mwaka 1844. Kama ulimwengu wote wa Wakristo ulivyoamini, Waadventista wa wakati ule waliaamini kuwa dunia, au sehemu yake fulani, ilikuwa patakatifu. Walielewa kuwa kutakaswa kwa patakatifu kulikuwa kusafisha dunia kwa moto wa siku kuu ya mwisho, na kuwa hili lingetokea wakati wa ujio wa pili wa Kristo. Ndiyo maana wakafikia hitimisho kuwa Kristo angerudi duniani 1844.

Lakini wakati uliopangwa ulipita, na Bwana hakutokea. Waumini walijua kuwa neno la Mungu halikosei; tafsiri yao ya unabii ndiyo inapaswa kuwa na makosa; lakini ni wapi palikuwa na makosa? Wengi walifanya haraka kukata fundo la matatizo kwa kukataa kuwa siku 2300 hazikuishia mwaka 1844. Hakuna sababu ambayo ilitolewa kwa ajili ya hili isipokuwa kwamba Kristo hakuja kwa wakati waliomtarajia. Walitoa hoja kuwa kama siku za kiunabii ziliishia mwaka 1844, Kristo angekuja kutakasa patakatifu kwa kuisafisha dunia kwa moto; na kwamba kwa kuwa hakuja, siku zilikuwa bado hazijaisha.

Kukubali hitimisho hili kulimaanisha kukanusha ukokotoaji wa awali wa vipindi vya kiunabii. Siku 2300 zilionekana kuanzia wakati amri ya Artashasta ya kuujenga upya Yerusalemu ilipotekelezwa wakati wa vuli ya mwaka 457 K.K. Kwa kuchukua wakati huu kama mahali pa kuanzia, kulikuwa na mwafaka kamili katika kutumia matukio yaliyotabiriwa katika maelezo ya kipindi kinachotajwa katika Danieli 9:25-27.

Majuma sitini na tisa, miaka 483 ya kwanza katika kipindi cha miaka 2300, yalipaswa kuishia kwa Masihi, Mpakwa Mafuta; na ubatizo wa Kristo na kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu, mwaka, 27 B.K, vilitimiza kikamilifu unabii. Katikati ya juma la saba, Masihi alipaswa kukatiliwa mbali. Miaka mitatu na nusu baada ya ubatizo Wake, Kristo alisulubishwa, wakati wa masika wa mwaka 31 B.K. Majuma sabini, au miaka 490, ilitengwa kwa ajili ya Wayahudi. Mwishoni mwa kipindi hiki taifa lilitia muhuri kumkataa kwao Kristo kwa kuwatesa wanafunzi Wake, na mitume waliwageukia Mataifa, mwaka 34 B.K. Miaka 490 ya kwanza kati ya miaka 2300 ikiwa imekwisha, miaka 1810 ilikuwa imebaki. Tangu mwaka 34 B.K. miaka 1810 inaishia mwaka 1844. “Ndipo,” alisema malaika, “patakatifu patakapotakaswa.” Vipengele vyote vinavyotangulia vya unabii vilitimizwa pasipo shaka yo yote kwa wakati uliopangwa.

Kwa ukokotoaji huu, yote yalikuwa wazi na yaliafikiana, isipokuwa halikuonekana tukio lo lote lililotimiza utakaswaji wa patakatifu likitokea mwaka 1844. Kukataa kuwa siku ziliishia wakati ule ilikuwa kuingiza unabii wote katika machafuko, na kukanusha hadharani misimamo yote iliyokuwa imewekwa kwa utimizo usio na mashaka wa matukio mbalimbali ya kiunabii. Lakini Mungu aliwaongoza watu Wake katika vuguvugu la marejeo; nguvu na utukufu Wake viliambatana na kazi, na asingeruhusu iishie gizani na kukata tamaa, idhihakiwe kama msisimko wa uongo na ushikiliaji sana mambo bila kutumia akili. Asingeruhusu neno Lake libaki katika mashaka na bila mwelekeo. Ingawa wengi waliachana na ukokotoaji wa awali wa vipindi vya kiunabii na kukataa usahihi wa vuguvugu lililojengwa juu yake, wengine hawakuwa tayari kukana vipengele vya imani na uzoefu uliokuwa na ushahidi wa Maandiko na ushuhuda wa Roho wa Mungu. Waliamini kuwa walitumia kanuni sahihi za kutafsiri Maandiko katika kujifunza kwao unabii, na kwamba ilikuwa wajibu wao kuhifadhi ukweli uliokwishapatikana, na kuendelea na jukumu la uchunguzi wa Biblia. Kwa maombi ya dhati walihakiki misimamo yao na walijifunza Maandiko ili wagundue kosa lao. Kwa kushindwa kuona kosa lao katika ukokotoaji wa vipindi vya kiunabii, walivutwa kuchunguza kwa makini somo la patakatifu.

Katika uchunguzi wao waligundua kuwa hakuna ushahidi wa kimaandiko ulioung a mkono wazo lililoaminiwa na wengi kuwa dunia ni patakatifu; lakini walipata katika Biblia maelezo kamili kuhusu somo la patakatifu, asili yake, mahali, na huduma zake; ushuhuda wa waandishi watakatifu ukiwa wazi na wa kutosha kiasi cha kuweka suala hilo katika nuru kamili isiyokuwa na swali lo lote. Mtume Paulo, katika Waraka kwa Waebrania, anasema: "Basi hata agano la kwanza lilikuwa na kawaida za ibada, na patakatifu pake, pa kidunia. Maana hema ilitengenezwa, ile ya kwanza, mlimokuwa na kinara cha taa, na meza, na mikate ya Wonyesho; ndipo palipoitwa, Patakatifu. Na nyuma ya pazia la pili, ile hema iitwayo Patakatifu pa patakatifu, yenye chetezo cha dhahabu, na sanduku la agano lililofunikwa kwa dhahabu pande zote, mlimokuwa na kopo la dhahabu lenye ile mana, na ile fimbo ya Haruni iliyochipuka, na vile vibao vya agano; na juu yake makerubi ya utukufu, yakikitia kivuli kiti cha rehema" (Waebrania 9:1-5).

Patakatifu panaporejelewa na Paulo ilikuwa hema iliyojengwa na Musa kwa amri ya Mungu kama mahali pa makazi ya duniani Yake Yeye Aliye Juu Sana. "Nao na wanifanyie patakatifu; ili nipate kukaa kati yao" (Kutoka 25:8), likuwa agizo lililotolewa kwa Musa wakati akiwa mlimani na Mungu. Waisraeli walikuwa wakisafiri kupitia jangwani, na hema lilijengwa kwa namna ambayo lingeweza kuhamishwa kutoka sehemu moja kusimikwa sehemu nyingine; lakini lilikuwa banda kubwa lenye utukufu mwingi. Kuta zake zilikuwa mbao zilizosimama wima zilizopakwa dhahabu nyingi na kuchomekwa katika soketi ya fedha, wakati paa lilitengenezwa kwa mfuatano wa mapazia, au vifuniko— vya nje vilikuwa vya ngozi, vya ndani vilikuwa vya kitani safi iliyochorwa picha nzuri za makerubi. Kando ya uwanja wa nje, ambao ulikuwa na madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, hema lenyewe ambalo liliundwa na vyumba viwili vilivyoitwa patakatifu na patakatifu pa patakatifu,

vilivyotenganishwa kwa pazia la thamani kubwa na zuri, au kifuniko; pazia kama hilo lilifunga lango la kuingilia katika chumba cha kwanza.

Ndani ya patakatifu kulikuwa na kinara cha taa, upande wa kusini, kikiwa na taa saba zilizotoa mwanga kwa ajili ya patakatifu mchana na usiku; upande wa kaskazini kulikuwepo meza ya mikate ya wonyesho; na mbele ya pazia linalogawanya patakatifu na patakatifu pa patakatifu kulikuwa na madhabahu ya dhahabu ya uvumba, ambapo wingu la harufu nzuri likiwa na maombi ya Waisraeli, lilitokea hapo na kupanda kila siku mbele ya Mungu.

Ndani ya patakatifu pa patakatifu lilisimama sanduku la agano, kasha lililotengenezwa kwa mbao za thamani kubwa na kupakwa dhahabu, hifadhi ya mbao mbili za mawe ambazo juu yake Mungu aliandika sheria ya Amri Kumi. Juu ya sanduku, na kikiwa sehemu ya sanduku takatifu, kulikuwa na kiti cha rehema, kilichotengenezwa kwa ufundi wa hali ya juu, kikiwa kimefunikwa na makerubi wawili, mmoja akiwa kila upande, na wote wawili wakiwa wametengenezwa kwa dhahabu ngumu. Katika chumba hiki uwepo wa Kimungu ulidhihirishwa kwa wingu la utukufu katikati ya makerubi.

Baada ya Waebrania kuanza maisha nchini Kanaani, hema liliachwa na badala yake hekalu la Sulemani lilitumika, ambalo, japokuwa lilikuwa jengo la kudumu na kubwa zaidi, lilijengwa kwa uwiano ule ule, na lilikuwa na samani za aina ile ile. Katika muundo huu hekalu lilidumu kuwepo— isipokuwa likiwa limebomolewa wakati wa Danieli—mpaka lilipoharibiwa na Warumi, mwaka 70 B.K.

Hapa ndipo patakatifu pekee palipowahi kuwepo duniani, ambapo Biblia inatoa habari zake. Hapa palitangazwa na Paulo kuwa patakatifu pa agano la kwanza. Lakini je, agano jipya halina patakatifu?

Tukirudi tena katika kitabu cha Waebrania, watafutaji wa ukweli waligundua kuwa uwepo wa patakatifu pa pili, au patakatifu pa agano jipya, umedokezwa katika maneno ya Paulo yaliyonukuliwa awali: “Basi hata agano la kwanza lilikuwa na kawaida za ibada, na patakatifu pake, pa kidunia.”Na matumizi ya neno“pia”kunaashiria kuwa Paulo ameshataja kabla juu ya patakatifu hapa. Tukirudi nyuma mwanzoni mwa sura inayotangulia, tunasoma: “Basi, katika hayo tunayosema, neno lililo kuu ndilo hili: Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni, mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu” (Waebrania 8:1, 2).

Hapa pamefunuliwa patakatifu pa agano jipya. Patakatifu pa agano la kwanza paliwekwa na mwanadamu; palijengwa na Musa; lakini patakatifu pa agano jipya pamewekwa na Bwana, siyo mwanadamu. Katika patakatifu pa duniani makuhani wa kibinadamu waliendesha huduma zake; katika patakatifu pa agano jipya, Kristo, Kuhani wetu Mkuu, anahudumu akiwa

mkono wa kulia wa Mungu. Patakatifu pa kwanza palikuwa duniani, patakatifu pa pili pako mbinguni.

Zaidi ya hapo, hema lililojengwa na Musa liliundwa kwa kufuata mfano. Bwana alimwelekeza Musa: "Sawasawa na haya yote nikuonyeshayo, mfano wa maskani, na mfano wa vyombo vyake vyote, ndivyo mtakavyovifanya." Na tena agizo lilitolewa, "Nawe angalia ya kwamba uvifanye kama mfano wake, ulioonyeshwa mlimani" (Kutoka 25:9, 40). Na Paulo anasema kuwa hema ya kwanza "ndiyo mfano wa wakati huu uliopo sasa; wakati huo sadaka na dhabihu zinatolewa," lakini mahali pake patakatifu palikuwa "nakala za mambo yaliyo mbinguni;" kwamba makuhani waliotoa zawadi kulingana na sheria walihudumu kama "mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni," na kuwa "Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu" (Waebrania 9:9, 23; 8:5; 9:24).

Patakatifu pa mbinguni, ambapo Yesu anahudumu kwa ajili yetu, ndipo patakatifu pakuu halisi, ambapo patakatifu palipojengwa na Musa palikuwa nakala. Mungu aliweka Roho Wake juu ya wajenzi wa hekalu la duniani. Stadi za kisanaa zilizooneshwa katika ujenzi wake zilikuwa udhihirisho wa hekima ya Kimungu. Kuta zilikuwa na mwonekano wa bonge kubwa la dhahabu, zikiakisi kila upande mwanga wa taa saba za kinara cha dhahabu cha taa. Meza ya mikate ya wonyesho na madhabahu ya uvumba vilimeremeta kama dhahabu safi. Pazia la kifahari lililofanya kazi kama dari, lililokuwa limechorwa picha za malaika kwa rangi ya bluu na zambarau na nyekundu liliongezea uzuri wa mandhari. Na ng'ambo ya pazia la pili kulikuwa na Shekina takatifu, udhihirisho unaoonekana wa utukufu wa Mungu, ambapo ni kuhani mkuu peke yake angeweza kuingia na kuendelea kuishi.

Utukufu usiokuwa na mfano wa hema ya duniani ulimwonesha mwanadamu utukufu wa hekalu la mbinguni ambapo Kristo mtangulizi wetu anahudumu kwa ajili yetu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Mahali pa kudumu pa Mfalme wa wafalme, mahali ambapo maelfu mara elfu wanamhudumia, na kumi elfu mara kumi elfu wanasimama mbele Zake (Danieli 7:10); hekalu lile, likiwa limejazwa kwa utukufu wa kiti cha enzi cha milele, mahali ambapo maserafi, walinzi wake wanaong'aa, hufunika nyuso zao katika kicho, ndipo lilipo, jengo lenye utukufu wa juu sana ambalo halijawahi kutengenezwa na mikono ya wanadamu, bali nuru yake iliyoakisiwa kwa uhafifu ya ukubwa na utukufu wake. Pamoja na hayo ukweli muhimu kuhusu patakatifu pa mbinguni na kazi inayoendeshwa pale kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu vilifundishwa kupitia patakatifu pa duniani na huduma zake.

Na malaika mwingine akaja akasimama mbele ya madhabahu, Sehemu mbili za patakatifu pa mbinguni zimewakilishwa na vyumba viwili katika patakatifu pa duniani. Wakati Yohana alipopewa fursa ya kuona hekalu la Mungu la mbinguni katika njozi, aliona pale "taa saba za moto zikiwaka mbele ya kile kiti cha enzi" (Ufunuo 4:5). Alimwona malaika "mwenye chetezo cha dhahabu, akapewa uvumba mwingi, ili autie pamoja na maombi ya

watakatifu wote juu ya madhabahu ya dhahabu, iliyo mbele ya kiti cha enzi" (Ufunuo 8:3). Hapa nabii aliruhusiwa kuona chumba cha kwanza cha patakatifu mbinguni; na aliona pale "taa saba za moto" na "madhabahu ya dhahabu," vilivyowakilishwa na kinara cha taa cha dhahabu na madhabahu ya uvumba katika patakatifu pa duniani. Tena, "hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa" (Ufunuo 11:19), na akatazama ndani ya pazia, ndani ya patakatifu pa patakatifu. Hapa aliona "sanduku la Agano Lake," lililowakilishwa na sanduku takatifu lililojengwa na Musa ili kuhifadhia sheria ya Mungu.

Hivyo, wale waliokuwa wakijifunza somo hili walipata uthibitisho usiopingika wa uwepo wa patakatifu pa mbinguni. Musa alijenga patakatifu pa duniani kwa kufuta mfano aliooneshwa. Paulo anafundisha kuwa mfano ule ulikuwa patakatifu halisi pa mbinguni. Na Yohana anashuhudia kuwa aliliona mbinguni.

Ndani ya hekalu la mbinguni, makazi ya Mungu, kiti Chake cha rehema kimeimarishwa katika haki na hukumu. Ndani ya patakatifu pa patakatifu sheria Yake, mwongozo mkuu wa haki ambao kwa huo binadamu wote wanapaswa kupimwa. Sanduku linalohifadhi mbao za sheria limefunikwa kwa kiti cha rehema, ambacho mbele yake Kristo anasihi kwa njia ya damu Yakekwaniabayamwenyedhambi. Kwanjiahiyoumewakilishwamuungano wa haki na rehema katika mpango wa ukombozi wa mwanadamu. Muungano huu, hekima isiyo na kikomo pekee ndiyo ingeweza kuubuni na nguvu isiyokuwa na kikomo pekee ndiyo ingeweza kuutekeleza; ni muungano unaojaza mbingu yote kwa mshangao na kuabudu.

Makerubi wa patakatifu pa duniani, kwa kutazama chini kwa kicho juu ya kiti cha rehema, huwakilisha shauku ambayo malaika wa mbinguni huwa wanakuwa nayo wanapotafakari kuhusu kazi ya ukombozi. Hii ndiyo siri ambayo malaika wanatamani kuielewa— kwamba Mungu anaweza kuwa mwenye haki na wakati huo huo amhesabie haki mwenye dhambi anayetubu na kurudisha uhusiano Wake na jamii ya wanadamu walioanguka; kwamba Kristo aliweza kushuka chini kuinua idadi ya watu isiyo na hesabu kutoka katika shimo la uharibifu na kuwavika mavazi yasiyokuwa na doa ya haki Yake ili awaunganishe na malaika ambao hawakuwahi kuanguka na wanaoishi daima mbele za Mungu.

Kazi ya Kristo kama mwombezi wa mwanadamu imewakilishwa katika ule unabii mzuri wa Zekaria kumhusu Kristo "ambaye jina lake ni Chipukizi." Nabii anasema: "Yeye atalijenga hekalu la Bwana; naye atauchukua huo utukufu; ataketi akimiliki katika kiti chake cha enzi; na kutakuwa na kuhani katika kiti chake cha enzi; na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili" (Zekaria 6:12, 13).

"Yeye atalijenga hekalu la Bwana." Kwa njia ya kafara Yake na upatanisho Wake, Kristo ni msingi na mjenzi wa kanisa la Mungu. Mtume Paulo anamwelezea kama "jiwe kuu la pembeni; Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu

katika Bwana: Katika yeye ninyi," anasema, "mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho" (Waefeso 2:20-22).

"Atauchukua huo utukufu." Kwa Kristo kuna utukufu wa ukombozi kwa jamii ya binadamu iliyoanguka. Katika zama zote za milele, wimbo wa walionunuliwa utakuwa:"Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, ... utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele" (Ufunuo 1:5, 6). Yeye "ataketi na kutawala juu ya kiti Chake cha enzi; na atakuwa kuhani juu ya kiti Chake cha enzi." Siyo sasa "juu ya kiti cha enzi cha utukufu Wake;" ufalme wa utukufu bado haujawadia. Ni mpaka kazi Yake kama Mpatanishi ifike mwisho ndipo Mungu "atampa kiti cha enzi cha Daudi baba Yake," ufalme ambao "hautakuwa na mwisho" (Luka 1:32, 33). Kama kuhani, Kristo ameketi na Baba Yake katika kiti Chake cha enzi (Ufunuo 3:21). Juu ya kiti cha enzi pamoja na Yule ambaye ni wa milele, aliye na uwepo Wake Mwenyewe Ndiye "aliyachukua masikitiko yetu, na kuzibeba huzuni zetu," ambaye "alijaribiwa katika mambo yote kama tujaribiwavyo, lakini hakutenda dhambi," ili aweze "kuwasaidia wanaojaribiwa."

"Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba" (Isaya 53:4; Waebrania 4:15; 2:18; 1 Yohana 2:1). Maombezi Yake ni yale ya mwili uliochomwa mikuki na uliovunjika, ya maisha yasiyokuwa na doa. Mikono iliyochubuliwa, ubavu uliochomwa mkuki, nyayo zilizoharibiwa, vinasihi kwa ajili ya mwanadamu aliyeanguka, ambaye ukombozi wake ulinunuliwa kwa gharama isiyokadirika. Na siku ile mtaomba kwa jina langu, kwa kuwa ninyi mmenipenda mimi, na kusadiki ya kwamba mimi nalitoka kwa Baba.

"Na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili." Upendo wa Baba, kadhalika na wa Mwana, ni msingi wa wokovu wa kizazi kilichopotea. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake kabla hajapaa kwenda mbinguni: "wala siwaambii ya kwamba mimi nitawaombea kwa Baba; kwa maana Baba mwenyewe awapenda" (Yohana 16:26, 27). Mungu alikuwa "akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake" (2 Wakorintho 5:19). Na katika huduma ya patakatifu pa mbinguni, "shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili." "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

Swali, Patakatifu ni nini? limejibibiwa kikamilifu katika Maandiko. Neno "patakatifu," kama linavyotumika katika Biblia, linahusu, kwanza, hema lililojengwa na Musa, kama nakala ya mambo ya mbinguni; na, pili, linahusu "hema la kweli" la mbinguni, ambalo patakatifu pa duniani palielekeza. Wakati wa kifo cha Kristo huduma ya mfano ilikoma.

"Hema la kweli" la mbinguni ni patakatifu pa agano jipya. Na unabii wa Danieli 8:14 unapotimizwa katika kipindi hiki, patakatifu panapohusishwa na unabii huu ni lazima pawe patakatifu pa agano jipya. Mwishoni mwa siku 2300, mwaka 1844, kulikuwa hakuna patakatifu pa duniani kwa karne nyingi. Kwa hiyo unabii, "Hata nyakati za jioni na asubuhi

elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa," unahusu, bila swali lo lote, patakatifu pa mbinguni.

Lakini swali muhimu ambacho linahitaji kujibiwa: Kutakaswa kwa patakatifu ni nini? Kwamba kulikuwepo na huduma kama hiyo iliyohusu patakatifu imeelezwa katika Maandiko ya Agano la Kale. Lakini kunaweza kuwepo cho chote cha kutakaswa mbinguni? Katika Waebrania 9 kutakaswa kwa patakatifu pa duniani na patakatifu pa mbinguni kumefundishwa kwa uwazi kabisa. "Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo. Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo, lakini mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo" (Waebrania 9:22, 23), ambayo ni damu ya thamani ya Kristo.

Utakaso, katika huduma ya mfano na huduma halisi, lazima ufanywe kwa njia ya damu: katika huduma ya awali, kwa damu ya wanyama; katika huduma ya pili, kwa damu ya Kristo. Paulo anasema, sababu kwa nini utakaso ni lazima utekelezwe kwa damu, ni kuwa, pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo la dhambi. Ondoleo la dhambi, au kuweka mbali dhambi, ni kazi inayopaswa kutekelezwa. Lakini ni kwa jinsi gani dhambi imeshikamana na patakatifu, ama pa mbinguni au pa duniani? Hili linaweza kueleweka kwa kuchunguza huduma ya mfano; kwa kuwa makuhani waliohudumu duniani, walihudumu kama "mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni" (Waebrania 8:5).

Huduma ya patakatifu pa mbinguni ilikuwa na sehemu mbili; makuhani walihudumu kila siku katika mahali patakatifu, wakati ambapo mara moja kwa mwaka kuhani mkuu alifanya kazi maalumu ya upatanisho katika patakatifu pa patakatifu, kwa ajili ya kutakasa patakatifu. Siku kwa siku mwenye dhambi aliyetubu alileta sadaka yake kwenye mlango wa hema na, akiweka mkono wake juu ya kichwa cha mnyama wa sadaka, aliungama dhambi zake, kwa njia hiyo, kwa mfano, alihamisha dhambi zake kutoka nafsi yake na kuziweka juu ya kafara asiyekuwa na hatia. Mnyama alichinjwa. "Pasipo kumwaga damu," anasema mtume, "hakuna ondoleo la dhambi." "Uhai wa mwili u katika hiyo damu" (Walawi 17:11).

Sheria iliyovunjwa ilidai uhai wa mkosaji. Damu, ikiwakilisha uhai alionyang'anywa mwenye dhambi, ambaye hatia yake ilibebeshwa mnyama wa kafara, ilichukuliwa na kuhani, naye kuhani alienda nayo katika chumba cha patakatifu na aliinyunyiza mbele ya pazia, ambalo nyuma yake kulikuwa na sanduku lililohifadhi sheria ambayo mwenye dhambi alikuwa ameivunja. Kwa sherehe hii dhambi ilikuwa, kwa njia ya damu, imehamishiwa kwa mfano katika patakatifu. Katika matukio mengine damu haikupelekwa ndani ya patakatifu; badala yake nyama ilipaswa kuliwa na kuhani, kama Musa alivyowaelekeza watoto wa Haruni, akisema: "naye amewapa ninyi ili kuuchukua uovu wa mkutano" (Walawi 10:17). Huduma zote mbili ziliashiria kuhamishwa kwa dhambi kutoka kwa mwenye dhambi aliyetubu na kuiingiza ndani ya patakatifu.

Hiyo ndiyo kazi iliyoendelea, siku kwa siku, katika mwaka mzima. Dhambi za Israeli zilihamishwa kutoka kwao kwa njia hiyo na kuingizwa ndani ya patakatifu, na kazi maalumu ilikuwa lazima ifanywe ili kuziondoa. Mungu aliagiza kuwa upatanisho ufanywe kwa kila chumba kitakatifu. “Naye atafanya upatanisho kwa ajili ya mahali patakatifu, kwa sababu ya mambo machafu ya wana wa Israeli, na kwa sababu ya makosa yao, naam, kwa ajili ya dhambi zao zote; naye atafanya vile vile kwa ajili ya hema ya kukutania, ikaayo pamoja nao katikati ya machafu yao.” Upatanisho ulipaswa pia kufanywa kwa ajili ya madhabahu, “kuitakasa, ili machafu yote ya wana wa Israeli yaitoke” (Walawi 16:16, 19).

Mara moja kwa mwaka, katika Siku kuu ya Upatanisho, kuhani aliingia ndani ya patakatifu pa patakatifu kwa ajili ya kupatakasa patakatifu. Kazi iliyofanywa pale ilikamilisha mzungumko wa mwaka wa huduma. Siku ya Upatanisho watoto wawili wa mbuzi waliletwa mlangoni pa hema, na kura zilipigwa juu yao, “kura moja kwa ajili ya Bwana; na kura ya pili kwa ajili ya Azazeli” (Aya ya 8). Mbuzi ambaye aliangukiwa na kura kwa ajili ya Bwana alichinjwa kama sadaka ya dhambi kwa ajili ya watu. Na kuhani alitakiwa kupeleka damu yake ndani ya pazia na kuinyunyiza juu ya kiti cha rehema na mbele ya kiti cha rehema. Damu ilitakiwa pia kunyunyizwa juu ya madhabahu ya uvumba iliyokuwa mbele ya pazia.

“Na Haruni ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai, na kuungama juu yake uovu wote wa wana wa Israeli, na makosa yao, naam, dhambi zao zote; naye ataziweka juu ya kichwa chake yule mbuzi, kisha atampeleka aende jangwani kwa mkono wa mtu aliye tayari. Na yule mbuzi atachukua juu yake uovu wao wote, mpaka nchi isiyo watu” (Aya ya 21, 22). Kamwe mbuzi wa azazeli hakurejea tena katika kambi ya Israeli, na mtu aliyempeleka jangwani alitakiwa kuoga na kufua nguo zake kwa maji kabla ya kurejea kambini.

Sherehe yote ilipangwa kuwapa picha ya utakatifu wa Mungu na chuki Yake dhidi ya dhambi; na, zaidi ya hapo, kuwaonesha kuwa wasingeweza kushiriki dhambi bila kunajisika. Kila mtu alitakiwa kutesa nafsi yake wakati kazi hii ya upatanisho ilipokuwa ikiendelea. Shughuli zote zilipaswa kuwekwa kando, na mkutano wote wa wana wa Israeli ulipaswa kutumia siku hiyo katika unyenyekevu mwingi mbele za Mungu, kwa maombi, kufunga, na kujichunguza moyoni.

Ukweli muhimu kuhusu upatanisho ulifundishwa kwa njia ya huduma ya mifano. Kafara ilikubaliwa badala ya mwenye dhambi; lakini dhambi haikufutwa kwa damu ya mnyama. Njia iliwekwa ambayo kwayo dhambi ilihamishiwa ndani ya patakatifu. Kwa njia ya sadaka ya damu mwenye dhambi alikiri mamlaka ya sheria, alikiri hatia yake ya kosa alilolifanya, na alionesha shauku yake kwa ajili ya msamaha kwa njia ya imani kwa Mkombozi ajaye; lakini hakuondolewa kabisa katika hukumu ya sheria. Siku ya Upatanisho kuhani mkuu, akiwa amechukua sadaka kutoka katika mkutano, aliingia ndani ya patakatifu pa patakatifu akiwa na damu ya sadaka hii, na alinyunyizia juu ya kiti cha rehema, juu ya sheria moja kwa moja,

kuridhisha madai yake. Halafu, kwa cheo chake kama mpatanishi, alizichukua dhambi juu yake mwenyewe na kuziondoa ndani ya patakatifu. Akiweka mikono yake juu ya kichwa cha mbuzi wa Azazeli, aliungama dhambi zote hizi, hivyo kwa njia ya kielelezo alizihamisha kutoka juu ya nafsi yake na kuziweka juu ya mbuzi. Ndipo mbuzi alizibeba na kuondoka nazo, na zilichukuliwa kuwa zimetenganishwa na watu milele.

Hiyo ndiyo huduma iliyofanywa kama "mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni." Na kile kilichofanywa kama mfano katika huduma ya patakatifu pa duniani kinafanywa katika uhalisia wake katika huduma ya patakatifu pa mbinguni. Baada ya kupaa Kwake Mwokozi wetu alianza kazi Yake kama kuhani wetu mkuu. Paulo anasema: "Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu Kristo hakuingia katika patakatifu palipotengenezwa kwa mikono ya wanadamu" (Waebrania 9:24).

Huduma ya kuhani ya mwaka mzima katika chumba cha kwanza cha patakatifu,"ndani ya pazia" ambalo lilikuwa mlango na lililotenga patakatifu na uwanja wa nje, huwakilisha kazi ya huduma ambayo Kristo alianza nayo mara tu baada ya kupaa. Ilikuwa kazi ya kuhani katika huduma ya kila siku kuwakilisha mbele ya Mungu damu ya sadaka ya dhambi, kadhalika uvumba ambao ulipanda na maombi ya watakatifu. Hivyo ndivyo Kristo alitumia damu Yake kumsihi Baba kwa niaba ya wenye dhambi, na kuwasilisha mbele Yake pia, pamoja na harufu nzuri na ya thamani ya haki Yake Mwenyewe, na maombi ya waaminio waliotubu dhambi zao. Hiyo ndiyo ilikuwa kazi ya huduma katika chumba cha kwanza cha patakatifu pa mbinguni.

Pale imani ya wanafunzi wa Kristo ilipomfuata alipopaa kutoka machoni pao. Hapa ndipo matumaini yao yalikuwa yamewekwa. "Matumaini yale yawekwayo mbele yetu," Paulo alisema,"kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia, alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu, amekuwa kuhani mkuu hata milele." "Wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele kwa ajili yetu" (Waebrania 6:18, 19, 20; 9:12).

Kwa karne kumi na nane, kazi ya huduma iliendelea katika chumba cha kwanza cha patakatifu. Damu ya Kristo, ilisihi kwa niaba ya waaminio waliotubu, ilipata msamaha na kukubaliwa na Baba, lakini bado dhambi zao zilibaki katika vitabu vya kumbukumbu. Kama ilivyokuwa katika huduma ya mfano kulikuwa na kazi ya upatanisho mwishoni mwa mwaka, hivyo kabla kazi kwa ajili ya ukombozi wa wanadamu haijakamilika kutakuwa na kazi ya upatanisho kwa ajili ya kuondoa dhambi ndani ya patakatifu. Hii ni huduma ambayo ilianza wakati siku 2300 zilipoisha. Wakati huo, kama ilivyotabiriwa na nabii Danieli, Kuhani wetu Mkuu aliingia ndani ya patakatifu pa patakatifu, kufanya sehemu ya mwisho ya kazi Yake kubwa— ya kutakasa patakatifu.

Kama ilivyokuwa zamani, ambapo dhambi za watu ziliwekwa kwa imani juu ya mnyama wa sadaka ya dhambi na kwa njia ya damu yake dhambi zilihamishiwa, kwa mfano, ndani ya patakatifu, hivyo katika agano jipya dhambi za wanaotubu zinawekwa, kwa imani, juu ya Kristo na kuhamishiwa, kiuhalisia, ndani ya patakatifu pa mbinguni. Na kama utakaso wa mfano wa patakatifu pa duniani ulivyotekelezwa kwa kuondoa dhambi ambazo zilikuwa zimepachafua, kadhalika utakaso halisi wa patakatifu pa mbinguni utatekelezwa kwa kuondoa, au kufuta, dhambi ambazo zimerekodiwa katika kitabu cha kumbukumbu. Lakini kabla hili halijafanyika, inapasa kuwepo uchunguzi wa vitabu vya kumbukumbu ili kubaini wale ambao, kwa njia ya toba ya dhambi na imani kwa Kristo, wana haki ya kupata manufaa ya upatanisho wake. Utakaso wa patakatifu, hivyo basi, unahusisha kazi ya upelelezi—kazi ya hukumu. Kazi hii inapaswa ifanyike kabla ya ujio wa Kristo kuwakomboa watu Wake; kwa kuwa atakapokuja, ujira Wake utakuwa mkononi Mwake kumlipa kila mtu sawasawa na matendo yake (Ufunuo 22:12).

Hivyo wale waliofuata katika nuru ya neno la unabii ambalo, badala ya kuja duniani mwishoni mwa siku 2300 mwaka 1844, Kristo aliingia ndani ya patakatifu pa patakatifu pa hekalu la mbinguni kufanya kazi ya mwisho ya upatanisho na kujiandaa kwa ajili ya ujio Wake wa pili duniani.

Ilionekana, pia, kuwa, wakatimnyamawasadakayadhambialimwakilisha Kristo kama kafara, na kuhani alimwakilisha Kristo kama mpatanishi, mbuzi wa Azazeli alikuwa mfano wa Shetani, mwasisi wa dhambi, ambaye juu yake dhambi za waliotubu kikamilifu zitawekwa hatimaye. Wakati kuhani mkuu, kwa njia ya damu ya mnyama wa sadaka ya dhambi, alipoondoa dhambi kutoka ndani ya hekalu, aliziweka juu ya mbuzi wa Azazeli. Wakati Kristo, kwa njia ya damu Yake Mwenyewe, ataondoa dhambi za watu Wake kutoka ndani ya hekalu la mbinguni mwishoni mwa huduma Yake, ataziweka juu ya Shetani, ambaye, wakati wa utekelezaji wa hukumu, atawajibika kwa ajili ya adhabu ya mwisho. Mbuzi wa Azazeli alipelekwa mbali katika nchi isiyokaliwa na watu, na hakutakiwa kurudi katika mkutano wa wana wa Israeli tena. Kadhalika Shetani atafukuzwa milele atoke mbele za Mungu na mbele za watu Wake, na atafutiliwa mbali asiwepo tena katika uangamizaji wa mwisho wa dhambi na wa wenye dhambi.

Sura ya 24 - Ndani ya Patakatifu pa Patakatifu

Somo la patakatifu lilikuwa ufunguo uliofungua siri ya kukatishwa tamaa kwa mwaka 1844. Ulifungua mfumo kamili wa ukweli, ulioshikamana na kuafikiana, ukionesha kuwa mkono wa Mungu uliongoza vuguvugu kuu la marejeo na ulifunua wajibu wa sasa kwa kuonesha nafasi na kazi ya watu Wake. Kama vile wanafunzi wa Yesu baada ya usiku wa huzuni na kukatishwa tamaa "walivyofurahi walipomwona Bwana," ndivyo walivyofurahi sasa wale waliokuwa wametazamia kwa imani ujio Wake wa pili. Walimtarajia aonekane katika utukufu atoe ujira kwa watumishi Wake. Matumaini yao yalipokatishwa tamaa, walishindwa kumwona Yesu, kama Mariamu kwenye kaburi walilia: "Wamemwondoa Bwana wangu, na sijui wamemweka wapi."

Sasa ndani ya patakatifu pa patakatifu walimwona tena, Kuhani wao Mkuu mwenye huruma, ambaye hivi karibuni atatokea kama mfalme na mkombozi wao. Nuru kutoka katika hekalu iliangazia wakati uliopita, wakati uliopo, na wakati ujao. Walielewa kuwa Mungu alikuwa amewaongoza kwa njia ya hekima yake isiyokosea. Ingawa, kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa kwanza, na wao wenyewe walishindwa kuelewa ujumbe waliouhubiri, ingawa ulikuwa sahihi katika kila kipengele. Katika kuuhubiri walitimiza kusudi la Mungu, na kazi yao haikuwa ya bure katika Bwana.

Wakiwa wamezaliwa "tena katika tumaini hai," walifurahi "kwa furaha isiyoneneka na iliyojaa utukufu mwingi." Unabii wa Danieli 8:14, "Akamwambia, Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa," na ujumbe wa malaika wa kwanza, "Mcheni Mungu na kumtukuza; kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja," ulielekeza kwa huduma ya Kristo ndani ya patakatifu pa patakatifu, na kwa ujio wa Kristo kwa ajili ya ukombozi wa watu Wake na uangamizaji wa waovu. Kosa halikuwa katika ukokotoaji wa vipindi vya kiunabii, lakini kosa lilikuwa katika tukio ambalo lingetokea mwishoni mwa siku 2300. Kwa njia ya kosa hili, waaminio walipata uzoefu wa kukatisha tamaa, lakini yote yaliyotabiriwa katika unabii huu, na yote waliyoyatarajia yaliyokuwa na ushahidi wa Maandiko, yalikuwa yametimia. Wakati ambao walikuwa wakiomboleza wakiwa wamepoteza matumaini yao, tukio lilikuwa limetokea ambalo lilitabiriwa na ujumbe huo, na ambalo lazima litimizwe kabla Bwana hajarudi kutoa ujira kwa watumishi Wake.

Kristo alikuwa amekuja, sio duniani, kama walivyotarajia, lakini, kama ilivyokuwa imetabiriwa katika mifano, ndani ya patakatifu pa patakatifu katika hekalu la Mungu mbinguni. Amewakilishwa na nabii Danieli kama Yeye anayekuja wakati huu kwa Mzee wa Siku:"Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja"—siyo kuja duniani, bali kuja kwa—"huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye" (Danieli 7:13). Ujio huu umetabiriwa pia na nabii Malaki: "Naye Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafula; naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema Bwana wa majeshi" (Malaki 3:1). Kuingia kwa Bwana katika hekalu lake kulikuwa kwa

ghafla, bila kutarajia, kwa watu Wake. Hawakumtarajia kwenda pale. Walimtarajia kuja duniani, "katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu" (2 Wathesalonike 1:8).

Lakini watu hawakuwa tayari bado kumpokea Bwana wao. Kulikuwa bado kuna kazi ya maandalizi kwa ajili yao. Ilipasa nuru itolewe, ikielekeza akili zao ndani ya hekalu la Mungu la mbinguni; na wakati wakimfuata kwa imani Kuhani wao Mkuu katika huduma Yake pale, majukumu mapya yangefunuliwa. Ujumbe mwingine wa onyo na maelekezo ulipaswa kutolewa tena kwa kanisa.

Nabii anasema: "Lakini ni nani atakayestahimili siku ya kuja kwake? Au ni nani atakayesimama atakapoonekana yeye? Kwa maana yeye ni mfano wa moto wa mtu asafishaye fedha, ni mfano wa sabuni ya mtu afuaye nguo; naye ataketi kama asafishaye fedha na kuitakasa, naye atawatakasa wana wa Lawi, atawasafisha kama dhahabu na fedha; nao watamtolea Bwana dhabihu katika haki" (Malaki 3:2, 3). Watakaokuwa wakiishi duniani wakati maombezi ya Kristo yakiwa yamekoma katika hekalu la mbinguni watasimama mbele ya macho ya Mungu bila mpatanishi. Majoho yao yanapaswa yasiwe na doa, tabia zinapaswa ziwe zimesafishwa dhambi kwa kunyunyiziwa damu ya Kristo. Kwa njia ya neema ya Mungu na kwa njia ya juhudi binafsi inawapasa wawe washindi katika vita dhidi ya uovu. Wakati hukumu ya upepelezi ikiendelea mbinguni, wakati dhambi za waaminio wanaotubu zikiondolewa hekaluni, kuna kazi maalumu ya utakaso ambayo inapaswa ifanywe, ya kuachana na dhambi, miongoni mwa watu wa Mungu duniani. Kazi hii imewasilishwa kwa uwazi zaidi katika ujumbe wenye sehemu tatu wa Ufunuo 14.

Wakati kazi hii itakapokuwa imekamilika, wafuasi wa Kristo watakuwa tayari kwa ajili ya ujio Wake. "Ndipo dhabihu za Yuda na Yerusalemu zitakapopendeza mbele za Bwana, kama katika siku za kale, na kama katika miaka ya zamani" (Malaki 3:4). Ndipo kanisa ambalo Bwana wetu wakati wa ujio Wake atalipokea litakuwa"Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa" (Waefeso 5:27). Ndipo litaonekana "kama alfajiri, Mzuri kama mwezi, safi kama jua, Wa kutisha kama wenye bendera" (Wimbo Ulio Bora 6:10).

Pamoja na ujio wa Bwana ndani ya hekalu Lake, Malaki pia hutabiri ujio Wake wa pili, ujio Wake kwa ajili ya kutekeleza hukumu, katika maneno haya: "Nami nitawakaribieni ili kuhukumu; nami nitakuwa shahidi mwepesi juu ya wachawi, na juu ya wazinzi, na juu yao waapao kwa uongo; na juu yao wamwoneao mwenye kuajiriwa, kwa ajili ya mshahara wake, wamwoneao mjane na yatima, na kumpotosha mgeni asipate haki yake, wala hawaniogopi mimi, asema Bwana wa majeshi" (Malaki 3:5). Yuda anarejea mandhari hiyo hiyo anaposema, "Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao zote za

upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu" (Yuda 14, 15). Ujio huu, na kuja kwa Bwana ndani ya hekalu Lake, ni matukio mawili yaliyo tofauti kabisa.

Kuja kwa Kristo kama kuhani wetu mkuu ndani ya patakatifu pa patakatifu, kwa ajili ya utakaso wa hekalu, kunakotajwa katika Danieli 8:14; kuja kwa Mwana wa Adamu kwa Mzee wa Siku, kama kulivyoelezwa katika Danieli 7:13; na kuingia kwa Bwana ndani ya Hekalu Lake, kulikotabiriwa na Malaki, ni maelezo ya tukio lile lile moja; na limewakilishwa pia na ujio wa bwana arusi kwenye harusi, ulioelezwa na Kristo katika mfano wa wanawali kumi, wa Mathayo 25.

Wakati wa kiangazi na wa vuli mwaka 1844 tangazo, "Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki," lilitolewa. Makundi mawili yanayowakilishwa na wanawali wenye busara na wapumbavu yalijitokeza—kundi moja lililotazamia ujio wa Bwana, na ambao walikuwa wakijiandaa kwa bidii kukutana Naye; na kundi jingine ambalo, wakiwa wamebanwa na hofu na wakitenda kwa msisimko, waliridhishwa na nadharia ya ukweli, lakini hawakuwa na neema ya Mungu. Katika mfano, bwana arusi alipokuja, "nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini." Kuja kwa bwana arusi kunakooneshwa hapa, kunatokea kabla ya arusi. Arusi huwakilisha upokeaji wa Kristo wa ufalme Wake. Mji Mtakatifu, Yerusalemu Mpya, ambao ni mji mkuu nao huwakilisha ufalme, na unaitwa "bibi arusi, mke wa Mwanakondoo." Malaika alimwambia Yohana: "Njoo huku, nami nitakuonyesha yule Bibi- arusi, mke wa Mwana-Kondoo." "Akanichukua katika Roho," anasema nabii, "akanionyesha ule mji mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu" (Ufunio 21:9, 10). Kwa hakika, hiyo basi, bibi arusi huwakilisha Mji Mtakatifu, na wanawali wanaokwenda kumlaki bwana arusi ni mfano wa kanisa. Katika Ufunuo watu wa Mungu wanasemekana kuwa ni wageni katika karamu ya arusi (Ufunuo 19:9). Ikiwa ni wageni, hawawezi tena kuwakilisha bibi arusi. Kristo, kama ilivyoelezwa na nabii Danieli, atapokea kutoka kwa Mzee wa Siku mbinguni, "mamlaka, na utukufu, na ufalme;" Ataupokea Yerusalemu

Mpya, mji mkuu wa ufalme Wake ambao, "umewekwa tayari, kama bibi- arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe" (Danieli 7:14; Ufunuo 21:2). Akiwa amepokea ufalme, atakuja katika utukufu Wake, kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, kwa ajili ya ukombozi wa watu Wake, ambao "wataketi pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo," kando ya meza Yake katika ufalme Wake (Mathayo 8:11; Luka 22:30), kushiriki katika karamu ya arusi ya Mwana Kondoo.

Tangazo, "Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki," katika kiangazi cha 1844, liliwasababisha maelfu ya watu kutarajia ujio wa haraka wa Bwana. Kwa wakati uliopangwa Bwana arusi alikuja, siyo duniani, kama watu walivyotarajia, bali kwa Mzee wa Siku mbinguni, arusini, karamu ya ufalme Wake. "Nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa." Wasingeweza kuwepo arusini kimwili; kwa sababu arusi inafanyikia mbinguni, wakati wao wakiwa duniani. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa

"watu wanaomngojea bwana wao, atakaporudi kutoka arusini" (Luka 12:36). Lakini inawapasa kuelewa kazi Yake, na wamfuate kwa imani anapoingia ndani mbele ya Mungu. Ni katika maana hii ambapo wanaelezwa kuwa wanakwenda arusini.

Katika mfano wa wanawali kumi ni wale waliokuwa na mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao ambao walienda arusini. Wale ambao, pamoja na kuujua ukweli kutoka katika Maandiko, walikuwa pia na Roho na neema ya Mungu, na ambao, katika giza la majaribu makali, walingoja kwa uvumilivu, wakichunguza Biblia ili kupata nuru kubwa zaidi—hawa waliuona ukweli kuhusu hekalu la mbinguni na badiliko la huduma ya Mwokozi, na kwa imani walimfuata katika kazi Yake katika hekalu mbinguni. Na wale wote ambao kwa njia ya ushuhuda wa Maandiko wanaukubali ukweli huo huo, wakimfuata Kristo kwa imani anapoingia mbele ya Mungu kufanya kazi ya mwisho ya upatanisho, na mwisho wa kazi hiyo apokeee ufalme Wake— yote haya yamewakilishwa na kwenda arusini.

Katika mfano wa Mathayo 22 kielelezo hicho hicho cha arusi kimetumiwa, na hukumu ya upelelezi imeoneshwa wazi wazi ikitokea kabla ya arusi. Kabla ya arusi mfalme anakuja kuona wageni wake, kuona kama wote wamevaa vazi la arusi, joho lisilokuwa na doa la tabia lililofuliwa na kufanywa jeupe katika damu ya Mwana Kondoo (Mathayo 22:11; Ufunuo 7:14). Anayekutwa akiwa na mapungufu anatupwa nje, lakini wote ambao baada ya kuchunguzwa wanaonekana wakiwa wamevaa vazi la arusi wanakubaliwa na Mungu na wanahesabiwa kuwa wanastahili kuwa na sehemu katika ufalme Wake na kuketi juu ya kiti Chake cha enzi. Kazi hii ya kuchunguza tabia, ya kubaini wanaojiandaa kwa ajili ya ufalme wa Mungu, ni ile ya hukumu ya upelelezi, kazi ya mwisho katika hekalu la mbinguni.

Kazi ya upelelezi ikiisha, wakati kesi za wale ambao katika zama zote walikiri kuwa wafuasi wa Kristo zitakapokuwa zimechunguzwa na kufanyiwa uamuzi, ndipo, na ni hadi hapo, ndipo kazi ya upelelezi itafikia kikomo, na mlango wa rehema utafungwa. Hivyo katika sentensi moja fupi, "Nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa," tunachukuliwa na kupitishwa katika huduma ya mwisho ya Mwokozi, hadi wakati ambapo kazi kubwa ya wokovu wa mwanadamu itakapokamilika.

Katika huduma ya hekalu la duniani, ambayo, kama tulivyokwisha kuona, ni kielelezo cha huduma ya mbinguni, wakati kuhani mkuu siku ya Upatanisho alipoingia ndani ya patakatifu pa patakatifu, huduma katika chumba cha kwanza ilisitishwa. Mungu aliamuru: "Wala hapatakuwa na mtu katika hema ya kukutania, wakati aingiapo ili kufanya upatanisho katika patakatifu, hata atakapotoka nje" (Walawi 16:17). Hivyo Kristo alipoingia patakatifu pa patakatifu kufanya kazi ya mwisho ya upatanisho, alisitisha huduma Yake katika chumba cha kwanza. Lakini huduma katika chumba cha kwanza ilipoisha, huduma katika chumba cha pili ilianza. Katika huduma ya mfano kuhani mkuu alipoondoka patakatifu katika Siku ya Upatanisho, alienda mbele za Mungu kupeleka damu ya mnyama wa sadaka ya dhambi kwa niaba ya Waisraeli wote ambao walitubu kwa dhati dhambi zao. Kwa hiyo Kristo alimaliza

sehemu moja tu ya kazi Yake kama mwombezi, ili aingie katika sehemu nyingine ya kazi, na bado aliendelea kutumia damu Yake kumwomba Baba kwa niaba ya wenye dhambi.

Somo hili halikueleweka kwa Waadventista mwaka 1844. Baada ya kupita kwa wakati ambao Mwokozi alikuwa akitarajiwa, bado waliamini ujio Wake ulikuwa karibu, walishikilia kuwa walikuwa wamefika kipeo kikuu muhimu na kuwa kazi ya Kristo kama Mwombezi wa mwanadamu ilikuwa imekoma. Ilionekana kwao kana kwamba wamefundishwa katika Biblia kuwa mlango wa rehema wa mwanadamu ungefungwa muda mfupi kabla ya ujio halisi wa Bwana katika mawingu ya mbinguni. Hili lilionekana kuwa dhahiri kutokana na yale maandiko yanayoelekeza kwa wakati ambao watu watatafuta, watagonga, na watalia kwenye mlango wa rehema, na hautafunguka.

Na ilikuwa swali kwao ikiwa tarehe waliyotarajia ujio wa Kristo ingeweza kuwa mwanzo wa kipindi hiki ambacho kingetangulia muda mfupi kabla ya ujio Wake. Wakiwa wamemaliza kutoa onyo la hukumu iliyo karibu, walihisi kuwa kazi yao kwa ajili ya ulimwengu ilikuwa imekwisha, na walipoteza mzigo kwa ajili ya wokovu wa roho za wenye dhambi. Wakati huo huo dhihaka za kijasiri na kufuru za watu wasiomcha Mungu zilionekana kwao kama ushahidi mwingine kuwa Roho wa Mungu alikuwa ameondolewa kutoka kwa waliokataa rehema Yake. Yote haya yalithibitisha kwao kuwa muda wa rehema ulikuwa umekwisha kwa ajili yao, au, kama walivyolieleza hili, “mlango wa rehema ulikuwa umefungwa.”

Lakini nuru kubwa zaidi ilipatikana kwa kuchunguza suala la patakatifu. Sasa waliona kuwa walikuwa sahihi kuamini kuwa mwisho wa siku 2300 mwaka 1844 ulikuwa alama ya kipeo kikuu muhimu. Lakini wakati ambapo ilikuwa kweli kuwa ule mlango wa tumaini na rehema ambao kwao, kwa miaka elfu moja mia nane, watu walikuwa na njia ya kumfikia Mungu, ulikuwa umefungwa, mlango mwingine ulikuwa umefunguliwa, na msamaha wa dhambi ulitolewa kwa wanadamu kwa njia ya maombezi ya Kristo ndani ya patakatifu pa patakatifu. Sehemu moja ya huduma Yake ilikuwa imefungwa, ili kutoa nafasi kwa ajili ya nyingine. Bado kulikuwa na “mlango uliofunguliwa” wa hekalu la mbinguni, ambapo Kristo alikuwa akihudumu kwa ajili ya mwenye dhambi.

Sasa yalionekana matumizi ya yale maneno ya Kristo katika kitabu cha Ufunuo, yanayolihusu kanisa wakati huu: “Haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye. Nayajua matendo yako. Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga” (Ufunuo 3:7, 8).

Ni wale ambao kwa imani wanamfuata Yesu katika kazi kubwa ya upatanisho wanapokea manufaa ya upatanisho Wake kwa ajili yao, wakati ambapo wale wanaokataa nuru inayoonesha huduma hii hawanufaishwi nayo. Wayahudi waliokataa nuru iliyotolewa wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo, na kukataa kumwamini kama Mwokozi wa ulimwengu,

hawakupokea msamaha unaopatikana kwa njia Yake. Wakati Yesu alipopaa kwenda mbinguni aliingia kwa njia ya damu Yake ndani ya patakatifu pa mbinguni kumwaga mibaraka ya maombezi Yake, Wayahudi waliachwa katika giza totoro wakiendelea na kafara na sadaka zisizo na manufaa yo yote. Huduma ya mifano na vivuli ilikuwa imekoma. Ule mlango ambao hapo awali watu waliweza kupitia na kumfikia Mungu haukuwa wazi tena. Wayahudi walikuwa wamekataa kumtafuta kwa njia ambayo kwayo peke yake angeweza kupatikana, kwa njia ya huduma ya hekalu la mbinguni. Hivyo hawakuwa na mawasiliano na Mungu. Kwao mlango ulikuwa umefungwa. Hawakumtambua Kristo kama kafara halisi na mpatanishi pekee mbele ya Mungu; kwa hiyo hawakupata manufaa ya upatanisho Wake.

Hali ya Wayahudi wasioamini ni mfano wa hali ya watu wasiojali na wasioamini miongoni mwa wanaodai kuwa Wakristo, ambao kwa kuchagua kwao wenyewe hawaijui kazi ya Kuhani wetu Mkuu mwenye rehema. Katika huduma ya mfano, kuhani mkuu alipoingia patakatifu pa patakatifu, Waisraeli wote walitakiwa kukutana pamoja karibu na hema na kunyenyekesha nafsi zao kwa kicho kikuu mbele za Mungu, ili wapate msamaha wa dhambi zao na wasikatiliwe mbali kutoka katika mkutano.

Ni kwa kiasi gani ni muhimu katika Siku hii ya Upatanisho halisi inatupasa kuelewa kazi ya Kuhani wetu Mkuu na kujua majukumu tunayotakiwa kuyafanya. Wanadamu hawawezi kupuuza onyo ambalo Mungu, kwa rehema Yake, analituma bila wapuuziaji kuadhibiwa. Ujumbe ulitumwa kutoka mbinguni kwenda kwa ulimwengu wa siku za Nuhu, na wokovu wao ulitegemea jinsi ambavyo wangeutendea kazi huo ujumbe. Kwa kuwa walilikataa onyo, Roho wa Mungu aliondolewa kutoka kizazi kile cha dhambi, na waliangamia kwa maji ya Gharika. Wakati wa Ibrahimu, rehema iliacha kusihi kwa ajili ya wakazi wa Sodoma wenye hatia, na wote waliteketezwa kwa moto uliotoka mbinguni isipokuwa Lutu na mke wake na mabinti zake wawili. Hivyo, katika siku za Kristo, Mwana wa Mumgu aliwaambia Wayahudi wasioamini: “Nyumba yenu mmeachiwa ukiwa” (Mathayo 23:38).

Akiangalia katika zama zote hadi siku za mwisho, Mungu mwenye nguvu isiyo na kikomo, anasema, kuhusu watu ambao “hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa”: “Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo; ili wahukumiwe wote ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu” (2 Wathesalonike 2:10-12). Wanapokataa mafundisho ya neno Lake, Mungu anaondoa Roho Wake na kuwaacha katika udanganyifu wanaoupenda.

Lakini Kristo bado anafanya maombi kwa ajili ya wanadamu, na nuru inatolewa kwa wale wanaoitafuta. Ingawa jambo hili halikueleweka kwa Waadventista wa awali, baadaye liliwekwa wazi wakati Maandiko yanayofasili nafasi yao halisi yalipoanza kufunguka mbele yao.

Kupita kwa wakati mwaka 1844 kulifuatwa na kipindi cha jaribu kubwa kwa wale waliobaki wakishikilia imani ya marejeo. Nafuu yao pekee, kwa kadiri uhakikisho wa nafasi yao sahihi ulivyohusika, ulikuwa nuru iliyoongoza akili zao kuelekea patakatifu pa mbinguni. Baadhi waliikana imani yao kuhusu ukokotoaji wao wa awali wa vipindi vya kiunabii na nguvu ya Roho Mtakatifu iliyoambatana na vuguvugu la marejeo waliihusisha na mawakala wa kibinadamu au wa kishetani. Kundi jingine walishikilia kwa nguvu kuwa Bwana aliwaongoza katika uzoefu wao uliopita; na walivyongoja na kukesha na kuomba kujua mapenzi ya Mungu waliona kuwa Kuhani wao Mkuu alianza kazi nyingine ya huduma, na, wakimfuata kwa imani, walioongozwa kuona pia kazi ya mwisho ya kanisa. Walikuwa na ufahamu wa wazi wa ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili, na walikuwa tayari kupokea na kutoa ulimwenguni onyo kali la malaika wa tatu wa Ufunuo 14.

Sura ya 25 - Sheria ya Mungu Isiyobadilika

"Kisha Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na sanduku la agano lake likaonekana ndani ya hekalu lake" (Ufunuo 11:19). Sanduku la agano la Mungu liko ndani ya patakatifu pa patakatifu, chumba cha pili cha hekalu. Katika huduma ya hema la duniani, ambalo lilitumika "kama mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni," chumba hiki kilifunguliwa wakati wa Siku kuu ya Upatanisho kwa ajili ya utakaso wa hema. Kwa hiyo, tangazo kuwa hekalu la Mungu lilifunguliwa mbinguni na sanduku la agano Lake lilionekana huelekeza kwa ufunguaji wa patakatifu pa patakafiu pa hekalu la mbinguni mwaka 1844 wakati Kristo alipoingia pale kutekeleza kazi ya kukamilisha upatanisho. Wale ambao kwa imani walimfuata Kuhani wao Mkuu wa mbinguni wakati akiingia katika huduma Yake ya patakatifu pa patakatifu, waliliona sanduku la Agano Lake. Walipojifunza somo la hekalu takatifu walipata uelewa wa badiliko la Mwokozi la huduma, na waliona kuwa sasa alikuwa akihudumu mbele ya sanduku la Mungu, akitumia damu yake kusihi kwa ajili ya wenye dhambi.

Sanduku katika hema la duniani lilikuwa na mbao mbili za mawe, ambazo juu yake ziliandikwa kanuni za sheria ya Mungu. Sanduku lilikuwa kasha tu la kuhifadhia mbao za sheria, na uwepo wa kanuni hizi za Kimungu ulilipatia sanduku lile thamani yake na utakatifu wake. Wakati hekalu la Mungu lilipofunguliwa mbinguni sanduku la agano Lake lilionekana. Ndani ya patakatifu pa patakatifu, katika hekalu la mbinguni, sheria ya Mungu imehifadhiwa katika hali ya utakatifu—sheria iliyotangazwa na Mungu Mwenyewe katikati ya radi za Sinai na kuandikwa kwa kidole Chake mwenyewe kwenye mbao za mawe.

Sheria ya Mungu katika hekalu la mbinguni ndiyo nakala halisi ya sheria ya Mungu, ambayo kanuni zilizoandikwa juu ya mbao za mawe na kuandikwa na Musa katika Torati ilikuwa hati isiyokosea. Wale waliofikia uelewa wa jambo hili muhimu waliongozwa hivyo kuona tabia takatifu, isiyobadilika ya sheria ya Mungu. Waliona vizuri zaidi, kuliko hata kabla ya hapo, uzito wa maneno ya Mwokozi: "Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka" (Mathayo 5:18). Sheria ya Mungu, kwa kuwa ni ufunuo wa mapenzi Yake, maelezo ya tabia Yake, ni lazima idumu milele, "kama shahidi mwaminifu wa mbinguni." Hakuna amri hata moja ambayo imefutwa; hakuna yodi wala nukta ambayo imebadilishwa. Mtunga zaburi ameandika: "Ee Bwana, neno lako lasimama Imara mbinguni hata milele." "Maagizo yake yote ni amini, Yamethibitika milele na milele" (Zaburi 119:89; 111:7, 8).

Katikati ya Amri Kumi kuna amri ya nne, kama ilivyotangazwa kwa mara ya kwanza: "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya

mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa" (Kutoka 20:8-11).

Roho wa Mungu aligusa mioyo ya wale wanafunzi wa neno Lake. Ushawishi ulijengeka katika mioyo yao kuwa waliivunja kanuni hii bila kujua kwa kupuuza siku ya mapumziko ya Mwumbaji. Walianza kuchunguza sababu za kuitunza siku ya kwanza ya juma badala ya siku ambayo Mungu aliitakasa. Hawakuweza kupata ushahidi katika Maandiko kuwa amri ya nne ilitanguliwa, au kuwa Sabato ilibadilishwa; mbaraka uliotakasa siku ya saba haujaondolewa. Walikuwa wakitafuta kwa uaminifu kuyajua na kuyafanya mapenzi ya Mungu; sasa, walipojiona wenyewe kuwa wavunjaji wa sheria Yake, huzuni ilijaza mioyo yao, na walionesha utii wao kwa Mungu kwa kuitunza Sabato na kuitakasa.

Juhudi nyingi na za dhati zilifanywa ili kupindua imani yao. Hakuna mtu ambaye angeshindwa kuona kuwa ikiwa hema ya duniani ilikuwa mfano au nakala ya hekalu la mbinguni, sheria iliyohifadhiwa katika sanduku la agano la hema ya duniani ilikuwa ni nakala ya sheria iliyoko katika sanduku la agano la mbinguni; na kuwa kukubali kwa imani ukweli kuhusu hema ya mbinguni kulijumuisha kutambua madai ya sheria ya Mungu na madai ya Sabato ya amri ya nne. Hapa ndipo kulikuwa na siri ya upinzani mkali na wa makusudi dhidi ya ufafanuzi wenye mwafaka wa Maandiko yaliyofunua huduma ya Kristo katika hekalu la mbinguni. Watu walitafuta kufunga mlango ambao Mungu alikuwa ameufungua, na kufungua mlango aliokuwa ameufunga. Lakini "Yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye," alisema: "Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga" (Ufunuo 3:7, 8). Kristo alikuwa amefungua mlango, au huduma, ya patakatifu pa patakatifu, nuru ilikuwa inang'aa kutoka katika mlango ule uliofunguliwa wa hekalu la mbinguni, na amri ya nne ilioneshwa ikiwa imejuimushwa katika sheria ambayo imehifadhiwa mle; kile ambacho Mungu alikianzisha, hakuna mwanadamu angeweza kukipindua.

Waliokuwa wameipokea nuru kuhusu upatanisho wa Kristo na uendelevu wa sheria ya Mungu waligundua kuwa haya mambo yalikuwa ukweli uliowasilishwa katika Ufunuo 14. Vipengele mbalimbali vya ujumbe wa sura hii huunda onyo lenye sehemu tatu (tazama Kiambatisho) linaloandaa wakazi wa dunia kwa ajili ya ujio wa pili wa Bwana. Tangazo,"Saa ya hukumu Yake imekuja," huelekeza macho kwa kazi ya kufunga huduma ya Kristo kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Linatoa habari njema za ukweli ambao inapasa uhubiriwe mpaka maombezi ya Mwokozi yatakapokoma na Yeye kurudi duniani awachukue watu Wake na kuwapeleka Kwake Mwenyewe. Kazi ya hukumu iliyoanza mwaka 1844 inapasa iendelee hadi kesi za watu wote ziamriwe, za makundi yote mawili ya walio hai na ya waliokufa; kwa maana hiyo hukumu hiyo itaendelea mpaka kufungwa kwa rehema ya wanadamu. Ili watu waweze kujiandaa kusimama katika hukumu, ujumbe unawaamrisha "mcheni Mungu, na kumtukuza," "na msujudieni Yeye aliyeziumba mbingu, na nchi, na bahari, na chemchemi za maji." Matokeo ya kuukubali ujumbe huu yametajwa katika neno: "Hapa ndipo penye subira

ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ili kujiandaa kwa ajili ya hukumu, ni lazima watu waishike sheria ya Mungu. Sheria ile ndiyo itakuwa kipimo cha tabia katika hukumu. Mtume Paulo anasema: "Na wote waliokosa, wenye sheria, watahukumiwa kwa sheria….katika siku ile Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu, sawasawa na injili yangu, kwa Kristo Yesu." Na anasema kuwa "waitendao sheria watakaohesabiwa haki" (Warumi 2:12-16). Imani ni ya lazima ili kuitii sheria ya Mungu; kwa kuwa "pasipo imani haiwezekani kumpendeza." Na "kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi" (Waebrania 11:6; Warumi 14:23).

Kwa njia ya malaika wa kwanza, watu wanaalikwa "kumcha Mungu na kumtukuza" na kumsujudia Yeye kama Mwumbaji wa mbingu na nchi. Ili kufanya jambo hili, inawapasa waitii sheria Yake. Alisema mwenye hekima: "Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu" (Mhubiri 12:13). Bila utii kwa amri Zake hakuna ibada inayoweza kumpendeza Mungu. "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake." "Yeye aligeuzaye sikio lake asiisikie sheria, Hata sala yake ni chukizo" (1 Yohana 5:3; Mithali 28:9).

Wajibu wa kumwabudu Mungu umejengwa juu ya ukweli kuwa Yeye ni Mwumbaji na kuwa uwepo wa wenye uhai wengine wote unamtegemea Yeye. Na mahali popote, ndani ya Biblia, dai Lake la kuheshimiwa na kuabudiwa, juu ya miungu ya wapagani, linapowasilishwa, ushahidi unaotolewa kuunga mkono dai hilo ni uwezo Wake wa kuumba. "Maana miungu yote ya watu si kitu, Lakini Bwana ndiye aliyezifanya mbingu" (Zaburi 96:5). "Mtanifananisha na nani, basi, nipate kuwa sawa naye? Asema yeye aliye Mtakatifu. Inueni macho yenu juu, mkaone; ni nani aliyeziumba hizi.""Maana Bwana, aliyeziumba mbingu, asema hivi; Yeye ni Mungu; ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya: ... Mimi ni Bwana, wala hapana mwingine" (Isaya 40:25, 26; 45:18).

Mtunga zaburi anasema: "Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake." "Njoni, tuabudu, tusujudu, Tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba" (Zaburi 100:3; 95:6). Na wenye uhai watakatifu wanaomwabudu Mungu mbinguni wanasema, kama sababu ya heshima yao kumstahili Mungu: "Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote" (Ufunuo 4:11).

Katika Ufunuo 14, watu wanaitwa kumwabudu Muumbaji; na unabii unatufunulia tabaka la watu ambalo, kama matokeo ya ujumbe wenye sehemu tatu, wanazitunza amri kumi za Mungu. Moja ya amri hizi hutaja moja kwa moja kwa Mungu kama Muumbaji. Amri ya nne inasema: "Siku ya saba ni Sabato ya Bwana Mungu wako: ... kwa siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba: kwa hiyo Bwana akaibariki siku ya Sabato, akaitakasa"(Kutoka 20:10, 11). Kuhusu Sabato, Bwana anasema, zaidi, kuwa ni "ishara, ... mpate kujua ya kuwa mimi ndimi Bwana, Mungu wenu" (Ezekieli

20:20). Na sababu inayotolewa ni kuwa: "Kwani kwa siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi, akastarehe kwa siku ya saba na kupumzika (Kutoka 31:17).

"Umuhimu wa Sabato kama kumbukumbu ya uumbaji ni kuwa inadumisha daima uwepo wa sababu ya kweli ya ibada kupaswa iwe kwa Mungu"—kwa sababu Yeye ni Muumbaji, na sisi ni viumbe Wake. "Sabato, hivyo basi, ndiyo msingi wa ibada ya Kimungu, kwani inafundisha ukweli huu mkuu kwa njia yenye mguso mkubwa sana, na hakuna agizo jingine lolote linaloweza kufanya hivyo. Msingi wa kweli wa ibada ya Kimungu sio tu wa siku ya saba peke yake, bali wa ibada zote, upo katika tofauti ya Muumbaji na viumbe Wake. Ukweli huu mkuu hauwezi kupitwa na wakati, na inapasa usisahaliuliwe kamwe."—J. N. Andrews, History of the Sabbath, Sura ya 27.

Ilikuwa kwa kusudi la kudumisha ukweli huu daima mbele ya akili za watu Mungu aliiweka Sabato katika Bustani ya Edeni; na kwa kadiri ukweli kuwa Yeye ni Muumbaji wetu utavyoendelea kuwa sababu ya sisi kumwabudu Yeye, ndivyo Sabato itakavyoendelea kuwa ishara na kumbukumbu ya ukweli huo. Ikiwa Sabato ingetunzwa na watu wote ulimwenguni na kwa wakati wote, mawazo na upendo wa watu vingeelekezwa kwa Muumbaji na Yeye peke Yake angeheshimiwa na kuabudiwa, na kusingekuwepo mwabudu sanamu, au mkanamungu, au kafiri. Utunzaji wa Sabato ni ishara ya utii kwa Mungu wa kweli, "Yeye aliyeziumba mbingu, na nchi, na bahari, na chemchemi za maji Him." Maana yake ni kuwa ujumbe unaowaagiza watu kumwabudu Mungu na kuzishika amri Zake utawaita mahsusi watu kuishika amri ya nne.

Kinyume na wale wanaozishika amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu, malaika wa tatu anataja tabaka jingine la watu, ambao dhidi ya makosa yao onyo kali na la kuogofya linatolewa: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu"(Ufunuo 14:9, 10). Tafsiri sahihi ya mifano iliyotumiwa ni ya muhimu ili kuelewa ujumbe huu. Ni nini kinawakilishwa na mnyama, sanamu, na chapa?

Mlolongo wa unabii ambamo mifano hii inapatikana unaanzia katika Ufunuo 12, ukianza kwa kumtaja joka aliyetafuta kumwangamiza Kristo wakati wa kuzaliwa Kwake. Joka anaelezwa kuwa ni Shetani (Ufunuo 12:9); yeye ndiye aliyemfanya Herode achukue hatua ya kumwua Mwokozi. Lakini wakala mkuu wa Shetani katika kupigana vita dhidi ya Kristo na watu Wake katika karne za kwanza za zama za Ukristo alikuwa Himaya ya Kirumi, ambayo upagani ulikuwa dini kuu kuliko zingine zote. Hivyo basi, ingawa, joka, kimsingi, anamwakilisha Shetani, katika maana ya pili, joka ni mfano wa Rumi ya kipagani.

Katika Sura ya 13 (aya ya 1-10) anaelezwa mnyama mwingine, "mfano wa chui," ambaye joka anampa "nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi." Mfano huu, kama Waprotestanti walio wengi wanavyoamini, huwakilisha upapa, ambao ulichukua uwezo

na nguvu na mamlaka ambayo awali yalishikiliwa na Himaya ya Rumi ya zamani. Kuhusu mnyama aliye mfano wa chui yanatolewa maelezo haya: "Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru…. Akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni. Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa." Unabii huu, ambao unafanana sana na maelezo ya pembe ndogo ya Danieli 7, bila swali lo lote unazungumzia upapa.

"Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili." Na nabii anasema, "Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti." Na tena: "Mtu akichukua mateka, atachukuliwa mateka. Mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga." Miezi arobaini na mbili ni sawa na "wakati na nyakati na nusu wakati," miaka mitatu na nusu, au siku 1260, za Danieli 7 - - muda ambao upapa ulipewa mamlaka ya kuwatesa watu wa Mungu. Kipindi hiki, kama ilivyokwisha kuelezwa katika sura zilizotangulia, kilianza na utawala wa upapa, mwaka 538 B. K. na kiliisha mwaka 1798. Wakati huo papa alifanywa mateka na jeshi la Kifaransa, utawala wa upapa ulipata jeraha la mauti, na utabiri ulitimia, "Mtu akichukua mateka, atachukuliwa mateka."

Katika hatua hii mfano mwingine unatambulishwa. Anasema nabii:"Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo" (Aya ya 11). Kwa mwonekano wake na jinsi anavyotokea hudhihirisha kuwa taifa hili linalowakilishwa hapa ni tofauti na yale yaliowakilishwa na mifano iliyotangulia. Falme kuu zilizowahi kuitawala dunia ziliwasilishwa kwa nabii Danieli kama wanyama wa mawindo, wakiinuka wakati "pepo nne za mbinguni zilivuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa" (Danieli 7:2). Katika Ufunuo 17 malaika alieleza kuwa maji mengi huwakilisha "jamaa na makutano na mataifa na lugha" (Ufunuo 17:15). Pepo ni mfano wa mashindano. Pepo nne za mbinguni zinazoshindana juu ya bahari kuu huwakilisha mandhari za kutisha za mashindano na mapinduzi ambayo kwayo falme hupata mamlaka.

Lakini mnyama mwenye pembe mbili mfano wa mwanakondoo alionekana "akipanda juu kutoka katika nchi." Badala ya kushinda falme zingine ili kujipatia mamlaka, taifa linalowakilishwa hapa huinuka katika eneo ambalo awali halikuwa na wakazi na lilikua pole pole na kwa amani. Lisingeweza, hivyo basi, kuinuka miongoni mwa mataifa yenye msongamano na yanayopambana ya Ulimwengu wa Zamani—ile bahari yenye mawimbi ya "jamaa na makutano na mataifa na lugha." Inapasa litafutwe katika Bara la Magharibi.

Ni taifa gani la Ulimwengu Mpya mwaka 1798 lilikuwa likipanda juu katika uwezo, likiwa na mwelekeo wa kuwa na nguvu na ukuu, na likivuta usikivu na macho ya ulimwengu? Matumizi ya mfano hayaruhusu uwepo wa swali lolote. Taifa moja, na moja pekee, hutimiza vipengele vya unabii huu; huelekeza bila shaka lolote kwa taifa la Marekani. Tena na tena wazo, karibu maneno yale yale, ya mwandishi mtakatifu yametumiwa na msemaji mahiri na

mwanahistoria katika kuelezea kuinuka na kukua kwa taifa hili. Mnyama alionekana "akipanda kutoka katika nchi;" na, kwa mujibu wa watafsiri, neno lililotafsiriwa "akipanda juu" kwa tafsiri sisisi humaanisha "kukua au kuchipuka kama mmea." Na, kama tulivyoona, taifa liliinuka katika eneo ambalo awali halikukaliwa na watu. Mwandishi mashuhuri, akielezea kuinuka kwa Marekani, anazungumzia juu ya"siri yake ya kupanda juu kutoka mahali pasipo na watu," na anasema: "Kama mbegu iliyo kimya tulikua na kuwa himaya."—G. A. Townsend, The New World Compared With the Old, ukurasa 462.

Jarida moja la Ulaya mwaka 1850 lilizungumzia juu ya Marekani kama taifa la ajabu, ambalo lilikuwa "likiinuka," na "katikati ya ukimya wa dunia kila siku likijiongezea nguvu na kiburi."—The Dublin Nation. Edward Everett, katika hotuba fasaha juu ya waasisi Wasafiri wa taifa hili, alisema: "Si walitafuta mahali palipojificha, palipo huru kwa sababu ya kutokujulikana kwake, na salama kwa sababu ya umbali wake, mahali ambapo kanisa dogo la Leyden lingefurahia uhuru wa dhamiri? Tazama maeneo yenye nguvu ambayo, kwa ushindi wa amani, ... wamebeba bendera za msalaba!"— Speech delivered at Plymouth, Massachusetts, Dec. 22, 1824, ukurasa 11.

"Naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo." Pembe za Mwana-Kondoo huashiria uchanga, kutokuwa na hatia, na upole, kuwakilisha kikamilifu tabia ya taifa la Marekani wakati lilipowasilishwa kwa nabii "likipanda juu" mwaka 1798. Miongoni mwa Wakristo wahamiaji wa kwanza waliokimbilia Marekani kutafuta hifadhi dhidi ya mateso ya mfalme na kukosa uvumilivu kwa makasisi walikuwemo wengi waliodhamiria kuunda serikali juu ya msingi mpana wa uhuru wa kiraia na kidini. Mawazo yao yalijumuishwa katika Azimio la Uhuru, linalobainisha ukweli mkuu kuwa "wanadamu wote wameumbwa sawa" na wamejaliwa haki isiyoachanika ya "uhai, uhuru, na utafutaji wa furaha."

Na Katiba ya Marekani inawathibitishia watu uhakika wa kujitawala, ikielekeza kuwa wawakilishi waliochguliwa kwa kura nyingi watatunga na kusimamia sheria. Uhuru wa imani ya kidini ulitolewa, kila mtu akiruhusiwa kuabudu kulingana na misukumo ya dhamiri yake. Ujamhuri na Uprotestanti ukawa kanuni za msingi za taifa. Kanuni hizi ndiyo siri ya nguvu na mafanikio yake. Walioonewa na waliokandamizwa katika Ulimwengu wote wa Kikristo wamegeukia nchi hii kwa shauku na tumaini. Mamilioni wamekimbilia katika fukwe zake, na nchi ya Marekani imeinuka na kuwa miongoni mwa mataifa yenye nguvu duniani.

Lakini mnyama mwenye pembe za mwanakondoo "akanena kama joka. Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona…..akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi" (Ufunuo 13:11-14).

Pembe za mwakondoo na sauti ya joka za mfano huelekeza kwa ukinzani mkubwa kati ya mwonekano na matendo ya taifa lililowakilishwa. "Kunena" kwa taifa ni tendo la mamlaka zake za kibunge na kimahakama. Kwa tendo hilo taifa litabadilisha zile kanuni za uhuru na amani lililojiwekea kama msingi wa sera yake. Utabiri kuwa litanena "kama joka" na kutumia "uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake" hutabiri wazi wazi ujio wa roho ya kukosa uvumilivu na mateso iliyooneshwa na mataifa yaliyowakilishwa na joka na mnyama kama chui. Na kauli kuwa mnyama mwenye pembe mbili "aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza" huashiria kuwa mamlaka ya taifa hili itatumiwa kushinikiza utekelezaji wa jambo fulani la kiibada ambalo litakuwa tendo la kuheshimu upapa.

Tendo hilo litakuwa kinyume kabisa cha kanuni za serikali hii, kinyume cha msingi wa taasisi zake huru, kinyume na viapo vikuu vya Azimio la Uhuru, na kinyume kabisa na Katiba. Waasisi wa taifa walitafuta kwa busara kutotumia mamlaka za kiserikali kuingilia mambo ya kanisa, pamoja na matokeo yake yasiyoepukika—kukosa uvumilivu na mateso. Katiba huelekeza kuwa "Bunge la Kongresi halitatunga sheria inayohusiana na uanzishaji wa dini, au kuzuia uhuru wa uanzishwaji wake," na kuwa "dini haitakuwa kigezo kwa mtu ye yote kushika ofisi au wajibu wowote wenye dhamana ya umma chini ya taifa la Marekani." Ni kwa ukiukwaji wa wazi wa tunu hizi za usalama wa uhuru wa taifa, ambapo inawezekana utekelezaji wa jambo fulani la kidini kushinikizwa na mamlaka za kiserikali. Lakini ubadilikaji wa tendo hilo hauwezi kuwa mkubwa zaidi kuliko ulivyowakilishwa katika mfano. Ni mnyama mwenye pembe mbili—kwa mwonekano yuko safi, mpole, na asiye na madhara—ambaye ananena kama joka.

"Akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama." Hapa kuna maelezo ya wazi kuhusu mfumo wa serikali ambayo mamlaka ya utungaji wa sheria uko katika mikono ya watu, ambao ni ushahidi madhubuti kabisa kuwa taifa la Marekani ndilo linalomaanishwa katika unabii huu.

Lakini "sanamu ya mnyama" ni nini? Na sanamu inafanyikaje? Sanamu inafanywa na mnyama mwenye pembe mbili, na ni sanamu kwa ajili ya mnyama. Inaitwa pia sanamu ya mnyama. Halafu kujifunza ili kuelewa sanamu hii ikoje na inafanyikaje inatupasa kujifunza sifa za mnyama mwenyewe—upapa.

Wakati kanisa la awali lilipochafuka kwa kuacha usahili wa injili na kupokea kaida na desturi za kipagani, kanisa lilipoteza Roho na nguvu ya Mungu; na ili kutawala dhamiri za watu, lilitafuta msaada wa mamlaka za kidunia. Matokeo yake yalikuwa kuzaliwa kwa mfumo wa upapa, mfumo wa kanisa uliotawala mamlaka ya kiserikali na uliotumia serikali kutekeleza maslahi ya kanisa, hususani kupambana na "uzushi." Ili Marekani ifanye sanamu ya mnyama, inapasa mamlaka ya kidini itawale serikali ya kiraia kwa namna ambayo mamlaka ya kiserikali itatumiwa pia na kanisa kutimiza mtakwa ya kanisa.

Wakati wowote kanisa lilipopata mamlaka ya kiserikali lilitumia mamlaka hayo kuwaadhibu wanaotofautiana na mafundisho yake. Makanisa ya Kiprotestanti yaliyofuata nyayo za Rumi kwa kuungana mamlaka za kidunia yamedhihirisha shauku ile ile ya kudhibiti uhuru wa dhamiri. Mfano wa jambo hili umeonekana katika mateso yaliyodumu kwa muda mrefu dhidi ya watu wanaotofautiana na Kanisa la Anglikana. Katika karne ya kumi na sita na ya kumi na saba, maelfu ya wachungaji wasiofungamana na upande wowote walilazimishwa kuyakimbia makanisa yao na wengi, wakiwa wachungaji na waumini, walilazimishwa kulipa faini, kufungwa, kuteswa, na kuuawa. Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote;,;, mwana wa uharibifu;

Ulikuwa uasi uliolifanya kanisa kutafuta msaada wa serikali ya kiraia, na jambo hili liliandaa njia ya uanzishwaji wa upapa—mnyama. Alisema Paulo: "Maana haiji usipokuja kwanza ule ukengeufu ... akafunuliwa yule mtu wa kuasi" (2 Wathesalonike 2:3). Kwa hiyo uasi ndani ya kanisa utaandaa njia kwa ajili ya sanamu ya mnyama.

Biblia inaeleza kuwa kabla ya ujio wa Bwana kutakuwepo hali ya kurudi nyuma katika mambo ya dini kama ilivyokuwa katika karne za kwanza. "Katika siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake" (2 Timotheo 3:1-5). "Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani" (1 Timotheo 4:1). Shetani atafanya kazi "kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea." Na wale wote ambao "hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa," wataachwa wapokee "nguvu ya upotevu, wauamini uongo" (2 Wathesalonike 2:9-11). Wakati hali hii ya uasi itakapofikiwa, matokeo yale yale yatafuata kama ilivyokuwa katika karne za kwanza.

Tofauti nyingi za imani katika makanisa ya Kiprotestanti huchukuliwa na wengi kuwa uthibitisho wa hakika kuwa hakuna juhudi zinazoweza kufanyika kuleta muungano wa kulazimisha miongoni mwao. Lakini kumekuwepo kwa miaka mingi, katika makanisa ya imani ya Kiprotestanti, wazo lenye nguvu na linalokua linalounga mkono muungano uliojengwa juu ya vipengele vinavyofanana vya mafundisho. Ili kufanikisha muungano huo, mjadala juu ya mada ambazo hawakubaliani wote—hata kama ni muhimu kiasi gani kutokana na mtazamo wa Biblia—ni lazima kwa vyo vyote vile uepukwe.

Charles Beecher, katika hubiri mwaka 1846, alitangaza kuwa huduma ya "madhehebu ya Waprotestanti wainjilisti siyo tu kuwa yameundwa kuanzia chini mpaka juu chini ya

shinikizo kubwa la hofu ya kibinadamu, bali pia wanaishi, na wanatembea, na wanapumua katika hali ya mambo ambayo ni ya kifisadi sana, na kila saa wakitumia kila jambo dhaifu la asili zao kunyamazisha ukweli, na kupiga magoti kwa mamlaka ya uasi. Je, si ndivyo mambo yalivyokwenda kwa upande wa Rumi? Je, haturudii kuishi maisha ya Rumi kwa mara nyingine tena? Na tunaona nini huko mbele? Baraza Kuu jingine! Mkutano Mkuu wa ulimwengu! Muungano wa wainjilisti, na imani moja ya ulimwengu wote!"—Sermon on "The Bible a Sufficient Creed," delivered at Fort Wayne, Indiana, Feb. 22, 1846. Wakati lengo hili litakapofikiwa, ndipo, katika bidii ya kupata umoja kamili, itakuwa hatua moja tu kufikia matumizi ya nguvu.

Wakati makanisa makubwa ya Marekani, yakiungana juu ya vipengele vya mafundisho vinavyoshikiliwa na wote, yatakaposhawishi serikali kulazimisha utekelezaji wa amri zao na kutegemeza taasisi zao, ndipo Marekani ya Kiprotestanti itakuwa imefanya sanamu ya Kanisa la Rumi, na utoaji adhabu za kiraia kwa wanaotofautiana nao lazima utafuata mara moja.

Mnyama mwenye pembe mbili "awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake" (Ufunuo 13:16, 17). Onyo la malaika wa tatu ni: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu." "Mnyama" anayetajwa katika ujumbe huu, ambaye ibada yake inalazimishwa na mnyama mwenye pembe mbili, ni yule wa kwanza, mnyama anayefanana na chui wa Ufunuo 13—upapa. "Sanamu ya mnyama" huwakilisha mfumo wa Uprotestanti ulioasi utakaojengeka wakati makanisa ya Kiprotestanti yatakapotafuta msaada wa mamlaka ya kiserikali ili kusimamia utekelezaji wa mafundisho yake. "Alama ya mnyama" ndiyo bado haijafasiliwa.

Baada ya onyo dhidi ya kumwabudu mnyama na sanamu yake unabii unaeleza: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Kwa kuwa wale wanaozishika amri za Mungu wamewekwa kinyume na wale wanaomwabudu mnyama na sanamu yake na kupokea alama yake, ina maana kuwa kushika amri ya Mungu, kwa upande mmoja, na kuivunja, kwa upande mwingine, kutakuwa ndiyo tofauti kati wanaomwabudu Mungu na wanaomwabudu mnyama.

Sifa mahsusi ya mnyama, na hivyo sanamu yake, ni kuzivunja amri za Mungu. Danieli anasema, kuhusu pembe ndogo, upapa: "Naye ataazimu kubadili majira na sheria" (Danieli 7:25). Na Paulo aliita mamlaka hiyo kuwa ni "mtu wa kuasi," ambaye angejiinua juu ya Mungu. Unabii mmoja unaongezea kwa unabii mwingine. Ni kwa kubadili sheria ya Mungu pekee ndiko kungeufanya upapa kujiinua juu ya Mungu; na ye yote ambaye, huku akijua, angeshika amri iliyobadilishwa, angekuwa anatoa heshimu kuu kwa mamlaka iliyofanya

badiliko hilo. Tendo hilo kwa sheria za kipapa lingekuwa alama ya utii kwa papa badala ya utii kwa Mungu.

Upapa umejaribu kubadili sheria ya Mungu. Amri ya pili inayokataza kuabudu sanamu, imeondolewa katika sheria, na amri ya nne imebadilishwa ili kuidhinisha utunzaji wa siku ya kwanza badala ya siku ya saba ya juma kama Sabato. Lakini waumini wa upapa wanadai, kama sababu ya kuiondoa amri ya pili, kuwa ni kwa sababu siyo ya muhimu, kwa kuwa imejumuishwa katika ya kwanza, na kwamba wanaitoa sheria sawasawa kabisa na jinsi Mungu alivyopanga ieleweke. Hili haliwezi kuwa badiliko lililotabiriwa na nabii. Badiliko la kimataifa, la kukusudia limewasilishwa: "Naye ataazimu kubadili majira na sheria." Badiliko katika amri ya nne linatimiza kikamilifu unabii huu. Hapa mamlaka pekee inayodaiwa ni ile ya kanisa. Hapa mamlaka ya upapa inajiweka juu ya Mungu.

Wakati ambapo watu wanaomwabudu Mungu watatambulishwa hasa hasa kwa heshima yao kwa amri ya nne,—kwa kuwa hii ni ishara ya uwezo Wake wa uumbaji na ushuhuda wa madai Yake kwa ajili ya kicho na heshima kutoka kwa mwanadamu,—watu wanaomwabudu mnyama watatambulishwa kwa juhudi zao za kuchana-chana kumbukumbu ya Muumbaji, na kuinua agizo la Roma. Ilikuwa ni kwa ajili ya Jumapili ambapo upapa kwanza ulionesha madai ya kiburi chake (tazama Kiambatisho); na hitaji la kwanza la msaada wa mamlaka ya kiserikali ilikuwa ni kwa ajili ya kulazimisha utunzaji wa Jumapili kama "siku ya Bwana." Lakini Biblia huelekeza kuwa siku ya saba, na sio siku ya kwanza, kama siku ya Bwana. Kristo alisema: "Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato pia." Amri ya nne inaeleza:"Siku ya saba ni Sabato ya Bwana." Na kwa njia ya nabii Isaya Bwana anaiita: "siku ya utakatifu wangu" (Marko 2:28; Kutoka 20:10; Isaya 58:13).

Dai linalotolewa mara nyingi kuwa Kristo alibadilisha Sabato linakanushwa na maneno Yake mwenyewe. Katika hubiri Lake juu ya Mlima alisema: "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka,yodi moja wala nukta moja ya torati haitaoondoka, hata yote yatimie. Basi mtu ye yote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni" (Mathayo 5:17-19).

Ni ukweli ambao kwa jumla unakubaliwa na Waprotestanti kuwa Maandiko hayatoi mamlaka kwa ajili ya kubadilisha Sabato. Jambo hili limeelezwa hasa hasa katika machapisho yanayotolewa na Muungano wa Shule ya Jumapili wa Amerika. Moja ya kazi hizi hukiri kuwa "kuna ukimya kamili katika Agano Jipya kuhusu amri ya moja kwa moja kuhusu Sabato (Jumapili), siku ya kwanza ya juma], au kanuni mahsusi kwa ajili ya utunzaji wake."—George Elliott, The Abiding Sabbath, ukurasa 184.

Mwingine anasema: "Mpaka wakati wa kifo cha Kristo, hakuna badiliko lo lote limewahi kufanywa katika siku;" na, "kwa kadiri kumbukumbu zinavyoonesha, wao [mitume]... hawakutoa amri mahsusi inayoagiza kutupilia mbali Sabato ya siku ya saba, na kuweka utunzaji wake siku ya kwanza ya juma."—A. E. Waffle, The Lord's Day, ukurasa 186-188.

Wakatoliki wa Rumi wanakiri kuwa badiliko la Sabato lilifanywa na kanisa lao, na wanasema kuwa Waprotestanti kwa kushika Jumapili wanakiri mamlaka ya Kanisa la Rumi. Katika Catholic Catechism of Christian Religion, katika kujibu swali kuhusu siku inayopaswa kutunzwa ili kutii amri ya nne, kauli hii inatolewa: "Katika sheria ya zamani, Jumamosi ilikuwa siku iliyotakaswa; lakini kanisa, likielekezwa na Yesu na Kristo, na likiongozwa na Roho wa Mungu, limeweka Jumapili badala ya Jumamosi; kwa hiyo sasa tunaitakasa siku ya kwanza ya juma, na sio siku ya saba ya juma. Jumapili inamaanisha, na sasa ni, siku ya Bwana."

Kama ishara ya mamlaka ya Kanisa Katoliki, waandishi ambao ni waumini wa upapa wanatumia dondoo hii: "tendo lenyewe la kubadili Sabato kuwa Jumapili, ambalo Waprotestanti wanakubaliana nalo; ... kwa sababu kwa kuishika Jumapili, wanakiri mamlaka ya kanisa kuamuru siku kuu na kuwaamrisha chini ya dhambi."— Henry Tuberville, An Abridgment of the Christian Doctrine, ukurasa 58. Badiliko hili la Sabato, hivyo basi, ni nini kama siyo ishara, au chapa, ya mamlaka ya Kanisa la Rumi—"chapa ya mnyama"?

Kanisa la Rumi halijaacha dai lake la ukuu; na wakati ulimwengu na makanisa ya Kiprotestanti unapokubali sabato iliyoanzishwa na kanisa hilo, wanapoikataa Sabato ya Biblia, kimsingi wanakubaliana na dai hilo. Wanaweza kudai mamlaka ya mapokeo na ya Mababa kwa ajili ya badiliko; lakini kwa kufanya hivyo wanapuuza kanuni ya msingi inayowatenga na Roma—kuwa "Biblia, na Biblia pekee, ndiyo dini ya Waprotestanti."Waumini wa mfumo wa upapa wanaweza kuona kuwa wanajidanganya wenyewe, wakifumba macho kwa kupenda wenyewe wasione ukweli katika suala hili. Harakati kwa ajili ya utunzaji wa lazima wa Jumapili inavyozidi kukubalika kwa kasi, wanafurahia, wakihisi kuwa hatimaye itauleta ulimwengu wote wa Waprotestanti chini ya bendera ya Roma.

Waumini wa Uroma wanasema kuwa "utunzaji wa Jumapili wa Waprotestanti ni heshima kubwa wanayoitoa, kwa kujua au kutokujua, kwa mamlaka ya Kanisa [Katoliki]."—Mgr. Segur, Plain Talk About the Protestantism of Today, ukurasa 213. Ulazimishaji wa utunzaji wa Jumapili kwa upande wa makanisa ya Kiprotestanti ni ulazimishaji wa ibada ya upapa—ya mnyama. Wale ambao, kwa kutambua madai ya amri ya nne, huchagua kushika sabato ya uongo badala ya Sabato ya kweli, na kwa njia hiyo, wanaheshimu mamlaka ambayo kwa amri yake ilianzishwa. Lakini kwa tendo hilohilo la kulazimisha wajibu wa kidini kwa kutumia mamlaka ya serikali ya kiraia, makanisa ya Kiprotestanti, kwa upande wao, yatafanya

sanamu ya mnyama; kwa hiyo, ulazimishaji wa utunzaji wa Jumapili katika nchi ya Marekani utakuwa ulazimishaji wa ibada ya mnyama na sanamu yake.

Lakini Wakristo wa vizazi vilivyopita waliishika Jumapili, wakidhani kuwa kwa kufanya hivyo walitunza Sabato ya Biblia; na hata sasa wapo Wakristo wa kweli katika kila kanisa, ikiwa ni pamoja na jumuia ya Kanisa la Roma, ambao kwa moyo wa dhati huamini kuwa Jumapili ni Sabato iliyowekwa na Mungu. Mungu anaukubali udhati wa kusudi na uadilifu wao mbele Yake. Lakini wakati ushikaji wa Jumapili utakapolazimishwa kwa sheria, na ulimwengu kuangaziwa kuhusu madai ya Sabato ya kweli, ndipo ye yote atakayevunja amri ya Mungu, ili aitii amri ambayo haina mamlaka makubwa zaidi ya yale ya Roma, atakuwa kwa njia hiyo, ameheshimu upapa zaidi kuliko Mungu. Anatoa heshima kwa Roma na kwa mamlaka inayoshinikiza agizo lililoagizwa na Roma. Anaabudu mnyama na sanamu yake. Watu wanapotupilia mbali Sabato ambayo Mungu alitangaza kuwa ishara ya mamlaka Yake, na kuheshimu badala yake ile ambayo Rumi ilichagua kuwa alama ya ukuu wake, watakuwa kwa njia hiyo, wamepokea alama ya utii kwa—“chapa ya mnyama.”

Na ni mpaka pale tu suala hili litakapokuwa limewekwa wazi, kama ilivyoelezwa, mbele ya watu, na watu kufikishwa mahali ambapo wataweza kuchagua kati ya amri za Mungu na amri za watu, ambapo wale watakaochagua kuendelea kutenda makosa watapokea “chapa ya mnyama.” Tishio la kuogofya lililowahi kutolewa kwa wanadamu walio na hali ya kufa linapatikana katika ujumbe wa malaika wa tatu. Hiyo lazima iwe dhambi ya kutisha inayosababisha ghadhabu ya Mungu isiyochanganywa na rehema. Watu hawapaswi kuachwa gizani kuhusiana na suala hili muhimu; onyo dhidi ya dhambi hii lipaswa kutolewa kwa ulimwengu kabla ya kujiliwa na hukumu za Mungu, ili kwamba wote wajue kwa nini hukumu hizi zitatolewa, na wawe na fursa ya kuziepuka. Unabii hutangaza kuwa malaika wa kwanza angetoa tangazo lake kwa “kila taifa, na kabila, na lugha, na jamaa.” Onyo la malaika wa tatu, ambalo ni sehemu ya ujumbe ule ule wenye sehemu tatu, nalo litatolewa kwa “kila taifa, na kabila, na lugha, na jamaa.”

Limewakilishwa katika unabii kuwa litatangazwa kwa sauti kuu, likitolewa na malaika anayeruka katikati ya mbingu; na litavuta usikivu wa ulimwengu. Katika shindano hili ulimwengu wote wa Wakrito utagawanyika katika matabaka mawili makubwa—wale wanaozishika amri za Mungu na imani ya Yesu kwa upande mmoja, na wale wanaomwabudu mnayama na sanamu yake na kupokea chapa ya mnyama kwa upande wa pili. Hata kama kanisa na serikali wataunganisha nguvu zao kuwalazimisha “wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa” (Ufunuo 13:16), wapokee “chapa ya mnyama,” hata hivyo watu wa Mungu hawataipokea. Nabii wa Patmo aliona “wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kando-kando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu” na wakiimba wimbo wa Musa na wa Mwana-Kondoo (Ufunuo 15:2, 3).

Sura ya 26 - Kazi ya Matengenezo

Kazi ya matengenezo ya Sabato inayofanywa katika siku za mwisho ilitabiriwa katika unabii wa Isaya: "Bwana asema hivi, Shikeni hukumu, mkatende haki; kwa maana wokovu wangu u karibu kuja, na haki yangu kufunuliwa. Heri afanyaye haya, na mwanadamu ayashikaye sana; azishikaye sabato asizivunje, auzuiaye mkono wake usifanye uovu wo wote." "Na wageni, walioandamana na Bwana ili wamhudumu, na kulipenda jina la Bwana, kuwa watumishi wake; kila aishikaye sabato asiivunje, na kulishika sana agano langu; Nitawaleta hao nao hata mlima wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala; makafara yao na dhabihu zao zitakubaliwa juu ya madhabahu zangu; kwa maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote" (Isaya 56:1, 2, 6, 7).

Maneno yanaelezea uhalisia wa zama za Ukristo, kama muktadha unavyoonesha: "Bwana MUNGU, akusanyaye waliofukuzwa katika Israeli asema, Pamoja na hayo nitamkusanyia na wengine, zaidi ya hao walio wake waliokusanywa" (Aya ya 8). Hapa pametabiriwa ukusanyaji wa watu wa Mataifa kwa njia ya injili. Na kwa wale wanaoiheshimu Sabato, mbaraka umetangazwa. Kwa hiyo madai ya amri ya nne yanadumu kuwepo hata baada ya kusulubishwa, kufufuka, na kupaa kwa Kristo, hadi wakati watumishi Wake watakapokuwa wamehubiri injili kwa mataifa yote ujumbe wa habari njema.

Bwana anaagiza kupitia kwa nabii huyo huyo: "Ufunge huo ushuhuda, ukaitie muhuri sheria kati ya wanafunzi wangu" (Isaya 8:16). Muhuri wa sheria ya Mungu unapatikana katika amri ya nne. Hii peke yake, miongoni mwa zote kumi, hudhihirisha jina na cheo cha Mtoa sheria. Inamtangaza kuwa Yeye ni Muumbaji wa mbingu na nchi, na hivyo, huonesha dai Lake la kuheshimiwa na kuabudiwa juu ya miungu yo yote mingine. Kando ya amri hii, hakuna kitu kingine katika Amri Kumi kinachoonesha ni kwa mamlaka ya nani sheria imetolewa. Wakati Sabato ilipobadilishwa na mamlaka ya upapa, muhuri uliondolewa katika sheria. Wanafunzi wa Yesu wameitwa kurudisha muhuri kwa kuinua Sabato ya amri ya nne na kuirudisha mahali pake sahihi kama kumbukumbu ya Muumbaji na ishara ya mamlaka Yake.

"Na waende kwa sheria na ushuhuda." Ingawa mafundisho na nadharia zinazopingana zipo nyingi, sheria ya Mungu ndiyo mwongozo usiokosea ambapo maoni, mafundisho, na nadharia zote vinapaswa vipimwe. Nabii anasema: "Ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi" (Aya ya 20).

Kwa mara nyingine tena, amri imetolewa: "Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao." Siyo ulimwengu wa waovu, lakini wale ambao Bwana anawaita "watu wangu," ambao inapasa waambiwe makosa yao. Anaeleza zaidi: "Walakini wanitafuta kila siku; hupenda kujua njia zangu; kama vile taifa waliotenda haki, wasioacha sheria ya Mungu wao, hutaka kwangu amri

za haki; hufurahi kumkaribia Mungu" (Isaya 58:1, 2). Hapa limedhihirishwa tabaka la watu wanaojiona wenyewe kuwa wenye haki na wanaoonekana kuwa na shauku ya kufanya kazi ya Mungu; lakini onyo kali na zito la Mchunguzaji wa mioyo anawaona kuwa wavunjaji wa amri za Mungu.

Kwa hiyo nabii anataja amri ambayo imeachwa: "Utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia. Kama ukigeuza mguu wako usihalifu sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika Bwana" (Aya ya 12-14). Unabii huu unahusu pia wakati wetu. Upotoshaji wa sheria ya Mungu ulifanywa wakati Sabato ilipobadilishwa na mamlaka ya Kiroma. Lakini wakati umefika ambapo amri hiyo ya Mungu inapaswa irudishwe. Upotoshwaji unapaswa urekebishwe na msingi wa vizazi vingi uinuliwe.

Ikiwa imetakaswa kwa pumziko na mbaraka wa Muumbaji, Sabato ilitunzwa na Adamu katika hali yake ya kutokuwa na hatia katika Edeni takatifu; ilitunzwa na Adamu, aliyeanguka lakini aliyetubu, na ilitunzwa na Adamu baada ya kufukuzwa kutoka Edeni. Sabato ilitunzwa na wazee wote, tangu Habili hadi Nuhu mwenye haki, Ibrahimu, hadi Yakobo. Wakati wateule walipokuwa utumwani Misri, wengi, katikati ya ibada ya sanamu ya wakati ule, waliisahau sheria ya Mungu; lakini Bwana alipowakomboa Israeli, aliitangaza sheria Yake katika utukufu wa kutisha kwa makutano waliokusanyika pamoja, wapate kujua mapenzi Yake na kumcha na kumtii milele.

Tangu siku hiyo hadi leo maarifa ya sheria ya Mungu yamehifadhiwa duniani, na Sabato ya amri ya nne imekuwa ikitunzwa. Ingawa "mtu wa kuasi" alifanikiwa kuikanyaga siku takatifu ya Mungu, lakini hata katika kipindi cha utawala wake walikuwepo, wakiwa wamejificha katika maeneo ya siri, watu waaminifu walioiheshimu. Tangu wakati wa Matengenezo, wamekuwepo watu katika kila kizazi waliodumu kuitunza. Ingawa mara nyingi katikati ya dhihaka na mateso, ushuhuda wa kudumu umetolewa juu ya uendelevu wa sheria ya Mungu na wajibu mtakatifu wa kuitunza Sabato ya uumbaji.

Ukweli huu, kama unavyowakilishwa katika Ufunuo 14 kuhusiana na "injili ya milele," utalitambulisha kanisa la Kristo wakati wa ujio Wake wa pili. Kwa kuwa kama matokeo ya ujumbe wenye sehemu tatu imetangazwa: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Na ujumbe huu ni wa mwisho kutolewa kabla ya ujio wa pili wa Bwana. Muda mfupi baada ya utangazaji wake Mwana wa Adamu anaonwa na nabii, akija katika utukufu kuvuna mavuno ya dunia.

Wale waliopokea nuru kuhusiana na patakatifu na kutobadilika kwa sheria ya Mungu walijaa furaha na mshangao walipoona uzuri na mwafaka wa mfumo wa ukweli uliofunuliwa

katika ufahamu wao. Walitamani kuwa nuru ambayo ilionekana kwao kuwa ya thamani sana ipelekwe kwa Wakristo wote; na waliamini kabisa kuwa ungepokelewa kwa furaha. Lakini ukweli ambao ungewafanya watofautiane na ulimwengu haukupokelewa na wengi waliodai kuwa wafuasi wa Kristo. Utii kwa amri ya nne ulihitaji kafara ambayo walio wengi walishindwa kuitoa.

Madai ya Sabato yalipowasilishwa, wengi walitoa hoja kwa mtazamo wa kidunia. Walisema: "Siku zote tumetunza Jumapili, baba zetu waliitunza, na watu wengi wema na wacha Mungu wamekufa kwa furaha huku wakiitunza. Ikiwa walikuwa sahihi, na sisi tuko sahihi. Utunzaji wa Sabato hii mpya utatutoa nje ya mwafaka na ulimwengu, na tutapoteza mvuto wetu kwa ulimwengu. Kundi dogo la wanaotunza siku ya saba linaweza kuwa na tumaini la kufanya nini dhidi ya ulimwengu wote unaotunza Jumapili?" Ilikuwa kwa hoja kama hizo ambapo Wayahudi walijaribu kujihesabia haki kwa kumkataa kwao Kristo. Baba zao walikuwa wakikubaliwa na Mungu kwa kutoa sadaka za kuteketezwa, na kwa nini watoto wasipate wokovu kwa kufuata njia ile ile waliyopita baba zao?

Kwa hiyo, wakati wa Luther, waumini wa upapa walitoa hoja kuwa Wakristo wa kweli wamefia katika imani ya Kikatoliki, na hivyo dini ile ilitosha kwa ajili ya wokovu. Hoja kama hiyo ni kikwazo kikubwa dhidi ya ukuaji katika imani au maisha ya kidini.

Wengi walidai kuwa Utunzaji wa Jumapili ulikuwa fundisho kamili na desturi ya kanisa iliyojulikana mahali pengi na iliyodumu kwa karne nyingi.

Dhidi ya hoja hii ilioneshwa kuwa Sabato na utunzaji wake vilikuwa vya zamani na ulioenea sehemu nyingi zaidi, hata ilikuwa na umri sawa na umri wa dunia yenyewe, na ilikuwa na idhini ya malaika na Mungu. Wakati misingi ya dunia ilipowekwa, wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu wote walipopiga kelele za shangwe, ndipo msingi wa Sabato uliwekwa (Ayubu 38:6, 7; Mwanzo 2:1-3). Ni halali kabisa amri hii inastahili heshima yetu; haikuanzishwa na mamlaka ya kibinadamu na wala haikujengwa juu ya mapokeo ya kibinadamu; ilianzishwa na Mzee wa Siku na iliamriwa kwa neno Lake la milele.

Wakati akili za watu zilipovutwa kutafakari juu ya mada ya matengenezo ya Sabato, wachungaji mashuhuri walipotosha neno la Mungu, wakitoa tafsiri kuhusu ushuhuda wa Sabato kwa namna ambayo ilinyamazisha akili zilizokuwa zikitafuta kuujua ukweli. Na wale ambao hawakuchunguza Maandiko wao wenyewe binafsi waliridhika kupokea mahitimisho ambayo yalipatana na matakwa yao. Kwa njia ya hoja, hila, mapokeo ya mababa, na mamlaka ya kanisa, wengi walijitahidi kuupindua ukweli. Mawakala wa ukweli walisukumwa kusoma zaidi Biblia ili waweze kutetea uhalali wa amri ya nne. Watu wanyenyekevu, wakiwa na neno la ukweli peke yake, walistahimili mashambulizi ya wasomi, ambao, kwa mshangao na hasira,

maneno yao fasaha ya uongo yakiwa hayana nguvu dhidi ya hoja sahili, za moja kwa moja za watu waliokuwa na ujuzi wa kina wa Maandiko badala ya mafundisho ya uongo ya vyuoni.

Kwa kukosa ushahidi wa Biblia unaounga mkono hoja zao, wengi kwa juhudi zisizochoka walisisitiza—wakisahau jinsi ambavyo hoja kama hiyo ilitumiwa dhidi ya Kristo na mitume Wake: "Kwa nini watu wetu mashuhuri hawajui lolote kuhusu suala la Sabato? Lakini wachache ndio huamini kama mnavyoamini. Haiwezekani ninyi muwe sahihi na wasomi wengine wote ulimwenguni wasiwe sahihi."

Kukanusha hoja kama hizo ilikuwa muhimu kutumia Maandiko na historia ya jinsi Bwana alivyoshughulika na watu Wake katika zama zote. Mungu hufanya kazi kupitia wale wanaosikia na kutii sauti Yake, wale ambao, ikiwa lazima, watasema ukweli usiokuwa mtamu, wale ambao hawaogopi kukemea dhambi zinazopendwa. Sababu za Bwana mara nyingi kutotumia watu walio na elimu ya juu na wenye vyeo vikubwa kuongoza katika harakati za matengenezo ni kwamba wanatumainia imani zao, nadharia, na mifumo yao ya kiteolojia, na hawaoni haja ya kufundishwa na Mungu. Wale tu walio na uhusiano binafsi na Chanzo cha hekima ndio wanaweza kuelewa au kueleza Maandiko. Watu walio na elimu ndogo ya shuleni nyakati zingine wanaitwa kutangaza ukweli, sio kwa sababu hawajasoma, bali kwa sababu ni watu wanaohisi kuwa na hitaji la kufundishwa na Mungu. Wanajifunza katika shule ya Kristo, na unyenyekevu na utii wao unawafanya kuwa wakuu.

Kwa kuwapatia maarifa ya ukweli Wake, Mungu anawapa heshima kubwa ukilinganisha na heshima ya kidunia na ukuu wa kibinadamu ambao baada ya muda mfupi hupoteza uzito na umuhimu wake.

Waadventista walio wengi waliukataa ukweli kuhusu hekalu na sheria ya Mungu, na wengi pia waliikana imani yao kuhusiana na vuguvugu la kiadventista na badala yake waliamini mawazo yasiyo ya kweli na yaliyopingana kuhusiana na unabii uliozungumzia vuguvugu lile. Baadhi walioongozwa kufanya kosa la kurudia-rudia kupanga wakati maalumu wa ujio wa Kristo. Nuru ambayo sasa ilikuwa iking'aa juu ya somo la patakatifu ingeweza kuwaonesha kuwa hakuna kipindi cha kiunabii ambacho kilifika hadi wakati wa ujio wa pili; ambacho wakati mahsusi wa ujio huo haukutabiriwa. Lakini, wakiwa wameiacha nuru, waliendelea kupanga wakati baada ya wakati kwa ajili ya kuja kwa Bwana mara ya pili, kwa kadiri walivyoendelea kukatishwa tamaa.; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu

Wakati kanisa la Wathesalonike lilipopokea mawazo potofu kuhusu ujio wa Kristo, mtume Paulo aliwashauri wapime matumaini na matarajio yao kwa uangalifu kwa njia ya neno la Mungu. Alichukua dondoo kutoka katika unabii ulioonesha matukio ambayo yangetokea kabla Kristo hajaja mara ya pili, na alionesha kuwa hawakuwa na sababu ya kutegemea ujio Wake katika siku zake. "Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote"

(2 Wathesalonike 2:3), ni maneno yake ya onyo. Ikiwa wangeendelea kuwa na matarajio ambayo hayana msingi katika Maandiko, wangeongozwa kupita katika njia isiyokuwa sahihi; kutokupata kile walichotarajia kungewapa nafasi wasioamini kuwadhihaki na kuwacheka, na wangekuwa katika hatari ya kusalimu amri kwa ukatishwaji tamaa huo na wangejaribiwa kutilia mashaka ukweli ulio muhimu kwa ajili ya wokovu wao.

Onyo la mtume kwa Wathesalonike limebeba somo kwa watu wanaoishi katika siku za mwisho. Waadventista wengi walihisi kuwa ikiwa wasingeweka imani yao kwenye siku mahsusi ya ujio wa Bwana, wasingeweza kuwa na bidii na juhudi katika maandalizi. Lakini matumaini yao yanaposisimuliwa tena na tena, na wakati wote wakiishia kukatishwa tamaa, imani yao inapata mshtuko mkubwa kiasi kwamba wanakaribia sana kupoteza uwezo wa kuamini ukweli mkuu wa unabii.

Kuhubiri wakati mahsusi kwa ajili ya hukumu, katika utangazaji wa ujumbe wa malaika wa kwanza, kuliagizwa na Mungu. Ukokotoaji wa vipindi vya kiunabii vilivyokuwa msingi wa ujumbe ule, ukiweka mwisho wa siku 2300 katika msimu wa vuli ya mwaka 1844, hauna dosari. Juhudi za mara kwa mara za kutafuta tarehe mpya kwa ajili ya mwanzo na mwisho wa vipindi vya kiunabii, na hoja zisizo na msingi zinazotumiwa kuunga mkono misimamo hiyo, siyo tu kuwa zinapeleka akili mbali na ukweli wa leo, bali pia zinasababisha dharau kwa juhudi zote za kuelezea unabii. Kwa kadiri upangaji wa siku mahsusi wa ujio wa pili wa Bwana unavyofanywa mara kwa mara, na kwa kadiri unavyofundishwa katika maeneo mengi, ndivyo unavyotimiza makusudi ya Shetani kwa ufanisi zaidi. Baada ya muda kupita, Shetani huchochea dhihaka na dharau dhidi ya mawakala wa siku hizo mahsusi za ujio wa Kristo, na kwa njia hiyo analeta aibu juu ya vuguvugu kuu la ujio wa pili wa Kristo la mwaka 1843 na mwaka1844.

Wale wanaodumu katika kufanya kosa hili mwishowe wataweka tarehe ya baadaye sana kwa ajili ya ujo wa Kristo. Kwa njia hiyo wataongozwa kupumzika katika usalama bandia, na wengi hawataachana na uongo huo mpaka wajikute wamechelewa. Historia ya Israeli ya zamani ni mfano mzuri wa uzoefu uliopita wa Waadventista. Mungu aliwaongoza watu Wake katika vuguvugu la ujio wa pili, wakati alipowaongoza wana wa Israeli kutoka Misri. Katika kukatishwa tamaa huku kwao, imani yao ilijaribiwa kama vile imani ya Waebrania ilipojaribiwa kwenye Bahari ya Shamu. Ikiwa wangeendelea kuutumaini mkono unaoongoza uliokuwa nao katika uzoefu wao wa nyuma, wangeuona wokuvu wa Mungu. Ikiwa watu wote waliohusika kwa umoja wao katika vuguvugu la marejeo la mwaka 1844, wangepokea ujumbe wa malaika wa tatu na kuutangaza kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, Bwana angetenda matendo makuu pamoja na juhudi zao. Mafuriko ya nuru yangeangazia ulimwengu wote. Miaka mingi iliyopita wakazi wa dunia wangekuwa wameonywa, kazi ya kufungia historia ya ulimwengu ingekuwa imekamilika, na Kristo angekuwa amerudi kwa ajili ya ukombozi wa watu Wake.

Haikuwa mapenzi ya Mungu kuwa Israeli watange-tange jangwani kwa miaka arobaini; Alitamani waende moja kwa moja hadi katika nchi ya Kanaani na kuwastawisha pale, na kuwafanya kuwa watu watakatifu, wenye furaha. Lakini "hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao" (Waebrania 3:19). Kwa sababu ya kurudi nyuma kwao na uasi wao waliangamia jangwani, wengine waliinuliwa ili waingie katika Nchi ya Ahadi. Kwa misingi hiyo hiyo, haikuwa mapenzi ya Mungu kuwa Kristo akawie sana kwa kiasi hicho na watu Wake wabaki kwa miaka mingi katika ulimwengu huu wa dhambi na huzuni. Lakini kutokuamini kuliwatenga na Mungu. Walipokataa kufanya kazi aliyokuwa amewapangia, wengine waliinuliwa kuutangaza ujumbe. Kwa sababu ya rehema Yake kwa ulimwengu, Yesu amecheleweshа ujio Wake, ili wenye dhambi wapate fursa ya kusikiliza onyo na kupata hifadhi ndani Yake kabla ghadhabu ya Mungu haijamwagwa.

Sasa kama ilivyokuwa katika zama zilizopita, wasilisho la ukweli linalokemea dhambi na makosa ya wakati huu litaamsha upinzani. "Maana kila mtu atendaye mabaya huichukia nuru, wala haji kwenye nuru, matendo yake yasije yakakemewa" (Yohana 3:20). Watu wanapoona kuwa hawawezi kuthibitisha hoja zao kwa Maandiko, wengi wanadhamiria kushikilia kwa gharama zote, na kwa roho mbaya wanashambulia tabia na nia za wale wanaotetea ukweli usiopendwa sana. Ni sera hiyo hiyo ambayo imetumiwa katika zama zote. Eliya alitangazwa kuwa mtaabishaji wa Israeli, Yeremia aliitwa msaliti, Paulo aliitwa mchafuzi wa hekalu. Tangu siku ile mpaka siku hii ya leo, wote wanaochagua kuwa watiifu kwa ukweli wanahukumiwa kuwa wachochezi, wazushi, au wanaogawa watu. Watu wengi wasioamini kiasi cha kulipokea neno la hakika la unabii watapokea kwa wepesi usio na swali shitaka dhidi ya wale wanaothubutu kukemea dhambi zinazopendwa na watu. Roho hii itaongezeka zaidi na zaidi. Na Biblia inafundisha wazi wazi kuwa wakati unakaribia ambapo sheria ya nchi itapingana na sheria ya Mungu kiasi ambacho yeyote ambaye atazitii amri zote za Mungu itampasa kukabiliana na adhabu kama mkosaji.

Katika mazingira kama haya, wajibu wa mjumbe wa ukweli ni nini? Ahitimishe kuwa ukweli usihubiriwe, kwa kuwa mara nyingi matokeo yake ni kuwafanya watu wakwepe au wapinge madai yake? Hapa; hana sababu zaidi ya kutokutoa ushuhuda wa neno la Mungu, kwa sababu unaamsha upinzani, kuliko ilivyokuwa kwa Wanamatengenezo wa awali. Kuikiri imani kulikofanywa na watakatifu na wafia dini wa zamani kuliandikwa na kuwekwa katika kumbukumbu kwa manufaa ya vizazi vilivyofuata. Mifano ile hai ya utakatifu na uaminifu usioyumba imehifadhiwa ili kuchochea ujasiri kwa wale ambao sasa wanaitwa kusimama kama mashahidi kwa ajili ya Mungu. Walipokea neema na ukweli, siyo kwa ajili yao peke yao, bali ili, kupitia kwao, maarifa ya Mungu yaangazie dunia. Je, Mungu ametoa nuru kwa ajili ya watumishi Wake katika kizazi hiki? Ikiwa hivyo, inapasa waiache iangaze ulimwenguni.

Zamani Bwana alimwambia mtu mmoja aliyesema katika jina Lake: "Bali nyumba ya Israeli hawatakusikiliza wewe; kwa kuwa hawanisikilizi mimi." Hata hivyo alisema: "Nawe

utawaambia maneno yangu, kwamba watasikia, au kwamba hawataki kusikia” (Ezekieli 3:7; 2:7). Kwa mtumishi wa Mungu wakati huu amri inatolewa: “Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao” (Isaya 58:1).

Kwa kadiri fursa zake zinavyopanuka, kila mmoja ambaye amepokea nuru ya ukweli yuko chini ya wajibu ule ule mzito na kutisha kama aliokuwa nabii Ezekieli, ambaye kwake neno la Bwana lilimjia, likisema: “Basi wewe, mwanadamu, nimekuweka kuwa mlinzi kwa nyumba ya Israeli; basi ulisikie neno hili kinywani mwangu, ukawape maonyo yangu. Nimwambiapo mtu mbaya, Ewe mtu mbaya, hakika utakufa, nawe husemi neno la kumwonya mtu huyo, aiache njia yake, mtu mbaya huyo atakufa katika uovu wake, lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Walakini ukimwonya mtu mbaya kwa sababu ya njia yake, kusudi aiache; wala yeye asiiache; atakufa huyo katika uovu wake, lakini wewe umejiokoa roho yako” (Ezekieli 33:7-9). Kikwazo

kikuu katika kuukubali na kuutangaza ukweli ni ukweli kuwa unajumuisha usumbufu na aibu. Hii ndiyo hoja pekee dhidi ya ukweli ambao mawakala wake hawajawahi kukanusha. Lakini hili haliwazuii wafuasi wa kweli wa Kristo. Hawa hawasubiri mpaka ukweli upendwe na watu wengi. Wakishawishika kuhusu wajibu wao, wanakubali kwa hiari yao wenyewe kubeba msalaba, wakihesabu pamoja na Paulo kuwa “dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana;” pamoja na yule wa zamani, “akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri” (2 Wakorintho 4:17; Waebrania 11:26).

Bila kujali taaluma zao ni zipi, ni wale tu wanaoutumikia ulimwengu kwa moyo wa dhati wanaotenda kazi kwa sera zaidi kuliko kwa maoni binafsi katika masuala ya dini. Inatupasa kuchagua ukweli kwa sababu ni ukweli, na kuacha matokeo kwa Mungu. Ulimwengu unapaswa kuwashukuru watu wa kanuni, imani, na uthubutu kwa ajili ya mabadiliko yake.

Hivyo ndivyo asemavyo Bwana: “Nisikilizeni, ninyi mjuao haki, watu ambao mioyoni mwenu mna sheria yangu; msiogope matukano ya watu, wala msifadhaike kwa sababu ya dhihaka zao. Maana nondo itawala kama vazi, na funza atawala kama sufu; bali haki yangu itakuwa ya milele, na wokovu wangu hata vizazi vyote” (Isaiah 51:7, 8).

Sura ya 27 - Uamsho wa Kisasa

Mahali popote pale ambapo neno la Mungu lilihubiriwa kwa uaminifu, matokeo yalifuata yaliyothibitisha kuwa neno lilitoka kwa Mungu. Roho wa Mungu alifuatana na ujumbe wa watumishi Wake, na neno lilikuwa na nguvu. Wenye dhambi walihisi dhamiri zao zikihuishwa. "Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu" aliangazia katika vyumba vya siri vya mioyo yao, na mambo yaliyofichika ya giza yaliwekwa dhahiri. Walishawishika sana katika akili zao na mioyo yao. Walisadikishwa kuhusu dhambi na haki na hukumu inayokuja. Walipata ufahamu wa haki ya Yehova na walihisi hofu ya kutokea, katika hatia yao na uchafu wao, mbele ya Mchunguzi wa mioyo. Kwa uchungu walilia: "Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?" Msalaba wa Kalwari, pamoja na kafara yake isiyo na kikomo kwa ajili ya dhambi za wanadamu, ulipofunuliwa, waliona kuwa hakuna kitu kingine isipokuwa haki ya Kristo pekee ndiyo ingetosha kufanya upatanisho wa dhambi zao; haki ya Kristo pekee ndiyo ingeweza kumpatanisha mwanadamu na Mungu. Kwa imani na uvumilivu walimpokea Mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Kwa njia ya damu ya Yesu walipata "ondoleo la dhambi zilizopita."

Roho hizi zilileta matunda yapasayo toba. Waliamini na kubatizwa, na waliinuka na kutembea katika upya wa uzima—viumbe wapya katika Kristo Yesu; wakiachana na maisha yao ya zamani waliyoishi kwa kufuata tamaa za mwili, bali waishi kwa imani ya Mwana wa Mungu na kufuata nyayo Zake, wakiakisi tabia Yake, na kujitakasa kama Yeye alivyo mtakatifu. Mambo ambayo awali waliyachukia sasa wanayapenda, na mambo ambayo awali waliyapenda sasa wanayachukia. Wenye kiburi na waliojikweza waligeuka na kuwa wapole na wanyenyekevu wa moyo. Watu wa ovyo na wenye majivuno walibadilika na kuwa watu makini na wasiojitanguliza mbele. Watu waliokuwa wakimkufuru Munngu walibadilika wakawa wacha Mungu, walevi wa pombe waliacha pombe, na mafisadi waliacha ufisadi wao. Mitindo ya maisha isiyofaa ya ulimwengu iliwekwa pembeni. Wakristo hawakutafuta"kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali … utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu" (1 Petro 3:3, 4).

Mikutano ya uamsho ilichochea ari ya kujichunguza mioyo na unyenyekevu. Mikutano hiyo ilihusisha miito mizito na ya dhati kwa mwenye dhambi, kwa kutamani huruma ya upatanisho wa damu ya Kristo. Wanaume na wanawake waliomba na kupigana mieleka na Mungu kwa ajili ya wokovu wa roho. Matunda ya mikutano hiyo ya uamsho ilionekana kwa idadi ya watu ambao hawakusita kujikana nafsi na kujitoa kafara, bali walifurahia kuwa walistahili kupata aibu na majaribu kwa ajili ya Kristo. Watu waliona badiliko katika maisha ya wale walioliamini jina la Yesu. Jamii ilinufaika kwa njia ya mvuto wao. Walikusanya pamoja na Kristo, na kupanda kwa Roho, ili kuvuna uzima wa milele.

Maneno haya yaliweza kusemwa juu yao: "Mlihuzunishwa, hata mkatubu." "Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti. Maana, angalieni, kuhuzunishwa kuko huko kwa jinsi ya Mungu kulitenda bidii kama nini ndani yenu; naam, na kujitetea, naam, na kukasirika, naam, na hofu, naam, na shauku, naam, na kujitahidi, naam, na kisasi! Kwa kila njia mmejionyesha wenyewe kuwa safi katika jambo hilo"(2 Wakorintho 7:9-11).

Haya ni matokeo ya kazi ya Roho wa Mungu. Hakuna ushahidi wa toba ya kweli ikiwa toba hiyo haileti matengenezo. Hebu aliyetubu atimize ahadi aliyoitoa, arudishe kile alichokiiba, aungame dhambi zake, ampende Mungu na wanadamu wenzake, hapo ndipo mwenye dhambi anaweza kuwa na hakika ya kuwa na amani na Mungu. Wakipimwa kwa matunda yao, walijulikana kuwa wamebarikiwa na Mungu katika wokovu wa wanadamu na kuwainua wanadamu kwa jumla.

Lakini matukio mengi ya uamsho wa siku hizi yameonesha tofauti kubwa na ule udhihirisho wa neema ya Mungu ambao katika siku za awali uliandamana na kazi za watumishi wa Mungu. Ni kweli kuwa shauku ya watu wengi inaamshwa, na wengi wanakiri kuwa wameongoka, na watu wengi wanajiunga na makanisa; hata hivyo matokeo hayathibitishi kwa hakika kabisa kuwa kuna ukuaji wa dhati wa maisha ya kiroho unaowiana na ongezeko la waumini wapya. Nuru inayomulika kwa muda mfupi huzimika, ikiacha giza nene zaidi kuliko lililokuwepo kabla.

Matukio ya uamsho yanayopendwa sana na watu ni yale ambayo huchochea fikra juu ya mambo ya kufikirika lakini yasiyo na uhalisia, ambayo husisimua hisia za watu, na ambayo huchochea tamaa ya kupenda mambo mapya yanayoshtua. Waongofu wanaopatikana kwa njia hizi huwa na hamu ndogo sana ya kusikiliza ukweli wa Biblia, na huwa na shauku kidogo sana ya ushuhuda wa manabii na mitume. Huduma ya kidini isipokuwa na misisimko haina mvuto kwao kabisa. Ujumbe ambao hugusa akili iliyotulia hauamshi mwitikio wo wote kwao. Maonyo ya wazi ya neno la Mungu, yanayohusiana moja kwa moja na maslahi yao ya milele, hayapokelewi.

Kwa kila roho iliyoongoka kikamilifu, uhusiano wake na Mungu na mambo ya milele utakuwa mada kuu ya maisha. Lakini ni wapi, katika makanisa makuu ya leo, kuna roho ya kujiweka wakfu kwa Mungu? Waongofu hawaachi kiburi chao na upendo wao kwa ulimwengu. Hawako tayari kujikana nafsi, wala kubeba msalaba, na kumfuata Yesu aliye mpole na mnyenyekevu, kuliko kabla ya kuongoka kwao. Dini imekuwa kichekesho kwa wasioamini na wenye mashaka kwa sababu wengi wa wale wanaobeba jina la dini hawazijui kanuni zake. Nguvu ya utaua imekaribia kutoweka kabisa katika makanisa yaliyo mengi. Pikiniki, michezo ya kuigiza makanisani, maonesho ya kanisa, nyumba nzuri, maonesho binafsi, vimeondoa mawazo ya watu juu ya Mungu. Ardhi na mali na shughuli za kidunia

hujaa akilini mwa watu, na mambo yenye maslahi ya umilele mara chache sana hutupiwa macho.

Pamoja na kushuka kwa imani na utakatifu kulikoenea kila mahali, wapo wafuasi wa kweli wa Kristo katika makanisa haya. Kabla hukumu ya mwisho ya Mungu haijamwagwa juu ya dunia kutakuwepo miongoni mwa watu wa Bwana uamsho wa utauwa wa kweli ambao haujawahi kushuhudiwa tangu nyakati za mitume. Roho na nguvu ya Mungu vitamwagwa juu ya watoto Wake. Wakati ule wengi watajitenga na makanisa ambayo ndani yake kuupenda ulimwengu kumechukua nafasi ya kumpenda Mungu na neno Lake.

Wengi, miongoni mwa wachungaji na watu wengine, wataupokea ukweli mkuu ambao Mungu ameagiza utangazwe kwa wakati huu kuwaandaa watu kwa ajili ya ujio wa pili wa Bwana. Adui wa roho anatamani kuzuia kazi hii; na kabla ya wakati wa vuguvugu hilo kufika, atajaribu kuzuia vuguvugu hilo kwa kuleta vuguvugu lake bandia. Katika makanisa yale ambayo ataweza kuyaweka chini ya nguvu yake ya udanganyifu atafanya ionekane kana kwamba mbaraka maalumu wa Mungu umemwagwa; kutakuwepo udhihirisho wa kile kitakachodhaniwa kuwa ni shauku kubwa ya kidini. Watu wengi watafurahia kuwa Mungu anatenda miujiza kwa ajili yao, wakati kazi ile ni ya roho nyingine. Chini ya mwavuli wa dini, Shetani atatafuta kueneza mvuto wake juu ya ulimwengu wa Kikristo.

Katika matukio mengi ya uamsho ambayo yametokea katika nusu karne iliyopita, nguvu ya aina hiyo imekuwa kazini, kwa kiwango kikubwa au kidogo zaidi, nguvu hiyo itatenda kazi kwa upana zaidi katika wakati ujao. Kunakuwepo misisimko na mihemko, mchanganyiko ya mambo ya kweli na ya uongo, vyote hivi vikiwa na kusudi la kupoteza watu. Lakini hakuna hata mtu mmoja anayelazimika kudanganywa. Katika nuru ya neno la Mungu siyo vigumu kugundua asili ya harakati hizi. Mahali popote watu wanapopuuza ushuhuda wa neno la Mungu, wakiuacha ukweli wa wazi, unaopima mioyo, unaotaka kujikana nafsi na kuachana na dunia, hapo tunaweza kujua kuwa mbaraka wa Mungu hauwezi kutolewa. Na kwa mwongozo ambao Kristo Mwenyewe aliutoa, “Mtawatambua kwa matunda yao” (Mathayo 7:16), ni dhahiri kuwa harakati hizi siyo kazi ya Roho wa Mungu.

Katika ukweli wa neno Lake, Mungu amejifunua kwa watu; na watu wote wanaoupokea huo ukweli wanakingwa dhidi ya uongo wa Shetani. Ni kupuuza ukweli huu ambako kumefungua mlango kwa ajili ya maovu ambayo sasa yanazidi kuenea katika ulimwengu wa kidini. Msingi na umuhimu wa sheria ya Mungu, kwa kiasi kikubwa, havipo akilini mwa watu. Uelewa potovu kuhusu sifa, uendelevu, na ulazima wa sheria ya Mungu umesababisha makosa kuhusiana na uongofu na utakaso, na umesababisha kushuka kwa kiwango cha utakatifu katika kanisa. Na hii ndiyo siri ya kutokuwepo kwa Roho na nguvu ya Mungu katika matukio ya uamsho ya nyakati zetu hizi.

Wapo, katika madhehebu mbalimbali, watu mashuhuri kwa uadilifu wao, wanaoukiri na wanaoukataa ukweli huu. Profesa Edwards A. Park, akielezea hatari za sasa za kidini alisema kwa ufasaha: "Chanzo kimoja cha hatari ni uzembe wa mimbari katika kusimamia utekelezaji wa sheria ya Mungu. Katika siku za awali mimbari ilikuwa mwangwi wa sauti ya dhamiri. Wahubiri wakuu walio wengi waliyapa mahubiri yao utukufu wa ajabu kwa kufuata mfano wa Bwana wao, wakiweka uzito kwa sheria ya Mungu, kanuni zake, na utisho wake. Walirudia misemo miwili ya hekima, kuwa sheria ni nakala ya tabia ya utakatifu wa Mungu, na kuwa mtu asiyeipenda sheria ya Mungu haipendi injili; kwa kuwa sheria na injili ni kioo kinachoakisi tabia ya kweli ya Mungu. Hatari hii inaongozana na hatari nyingine, hatari ya kushindwa kubaini ubaya wa dhambi, ukubwa wake, na madhara yake. Kuna uwiano kati ya kiwango cha uzuri wa kuitii sheria ya Mungu na kiwango cha ubaya wa kutoitii....

"Pamoja na hatari zilizokwisha kutajwa, kuna hatari nyingine ya kushindwa kubaini haki ya Mungu. Mwelekeo wa mimbari za leo ni kutenganisha haki ya Mungu na wema wa Mungu; mimbari za leo kushusha hadhi ya wema wa Mungu na kuuona kama hisia tu badala ya kuupa hadhi ya kanuni. Ufafanuzi wa kiteolojia unatenganisha alivyoviunganisha Mungu. Je, sheria ya Mungu ni njema au ni mbaya? Ni njema. Haki ni njema; kwa kuwa kazi yake ni kutekeleza sheria. Kutokana na tabia ya kushindwa kubaini wema wa sheria na haki ya Mungu, na kushindwa kubaini kiwango na hasara ya uasi wa mwanadamu, wanadamu ni wepesi kuteleza na kujikuta wakipuuza neema ambayo inawezesha upatanisho kwa ajili ya dhambi." Hivyo injili inapoteza thamani yake na umuhimu wake katika akili za watu, na haichukui muda mrefu wanakuwa tayari kutupilia mbali Biblia yenyewe.

Walimu wa dini wengi wanadai kuwa, Kristo, kwa njia ya kifo Chake, aliitangua sheria, na watu sasa hawabanwi na matakwa yake. Wapo baadhi wanaoiwasilisha sheria ya Mungu kama mzigo mzito, na kinyume na utumwa wa sheria, wanawasilisha uhuru unaopatikana chini ya injili.

Lakini sivyo manabii na mitume walivyoichukulia sheria takatifu ya Mungu. Daudi alisema: "Nami nitakwenda panapo nafasi, Kwa kuwa nimejifunza mausia yako" (Zaburi 119:45). Mtume Yakobo, aliyeandika baada ya kifo cha Kristo, anaeleza Amri Kumi kuwa "sheria ya kifalme" na "sheria kamilifu iliyo ya uhuru" (Yakobo 2:8; 1:25). Na nabii wa ufunuo, nusu ya karne baada ya kusulubishwa kwa Kristo, alitangaza baraka juu yao "wazishikao amri Zake, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake" (Ufunuo 22:14).

Daikuwa Kristo, kwanjiayakifo Chake, alitanguasheriaya BabaYakehalina msingi. Kama kungekuwa na uwezekano wa kubadilisha sheria au kuiweka pembeni, Kristo asingelazimika kufa kumwokoa mwanadamu kutoka katika adhabu ya dhambi. Kifo cha Kristo, mbali na kuwa hakikutangua sheria, kinathibitisha kuwa sheria haibadiliki. Mwana wa Mungu alikuja "kuitukuza sheria, na kuiadhimisha" (Isaya 42:21). Alisema: "Msidhani ya kuwa nalikuja

kuitangua torati;""Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka" (Mathayo 5:17, 18). Na Kristo Mwenyewe anaeleza msimamo Wake: "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu" (Zaburi 40:8).

Sheria ya Mungu, kutokana na ilivyo, haiwezi kubadilika. Ni ufunuo wa mapenzi na tabia ya Mwasisi wake. Mungu ni pendo, na sheria Yake ni pendo. Kanuni zake kuu mbili ni kumpenda Mungu na kumpenda mwanadamu. "Pendo ndilo utimilifu wa sheria" (Warumi 13:10). Tabia ya Mungu ni haki na ukweli; na hiyo ndiyo asili ya sheria Yake. Mwandishi wa zaburi anasema: "Sheria yako ni kweli:""Sheria yako ni haki ya milele" (Zaburi 119:142, 172). Na mtume Paulo anasema: "Torati ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema" (Warumi 7:12). Sheria hiyo, kwa kuwa inaeleza kilichomo katika akili na mapenzi ya Mungu, lazima iwe ya milele kama Mwasisi wake alivyo wa milele.

Ni kazi ya uongofu na utakaso kuwapatanisha watu na Mungu kwa kuwapatanisha na kanuni za sheria Yake. Hapo mwanzo, mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Alikuwa akiafikiana na asili na sheria ya Mungu; kanuni za haki zilikuwa zimeandikwa ndani ya moyo wake. Lakini dhambi ilimtenga na Muumbaji wake. Hakuweza tena kuakisi Sura ya Mungu. Moyo wake ulipigana vita dhidi ya kanuni za sheria ya Mungu. "Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii" (Warumi 8:7).

Lakini "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee," ili mwanadamu apatanishwe na Mungu. Kwa njia ya haki ya Kristo anaweza kurudishwa katika mwafaka na Mwumbaji wake. Moyo wake unapaswa uumbwe upya kwa neema ya Mungu; ni lazima apokee maisha mapya yatokayo mbinguni. Badiliko hili ni uzoefu wa kuzaliwa upya, ambao, mtu asipokuwa nao, Yesu anasema, "hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Hatua ya kwanza katika upatanisho na Mungu ni mtu kushawishika na kukiri kuwa ni mwenye dhambi. "Dhambi ni uasi wa sheria." "Kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria" (1 Yohana 3:4; Warumi 3:20). Ili aone hatia yake, mwenye dhambi lazima apime tabia yake kwa njia ya kiwango cha Mungu cha haki. Ni kioo kinachoonesha ukamilifu wa tabia ya haki na humwezesha mwenye dhambi kutambua mapungufu yake.

Sheria inamfunulia mtu dhambi zake, lakini sheria haitoi tiba. Wakati ambapo inaahidi uzima kwa mtu mtiifu, inatangaza kuwa kifo ndiyo mshahara wa mkosaji. Injili ya Kristo pekee ndiyo inaweza kumwokoa mwenye dhambi kutoka katika hukumu au uchafu wa dhambi. Inampasa mwenye dhambi kutubu kwa Mungu, ambaye sheria Yake imevunjwa; na imani katika Kristo, kafara yake pekee ya upatanisho. Hivyo anapokea "ondoleo la dhambi zilizopita" na anakuwa mshirika wa asili ya uungu. Yeye ni mwana wa Mungu, akiwa amepokea roho ya kupangwa, ambapo analia: "Aba, Baba!"

Je, sasa yuko huru kuvunja sheria ya Mungu? Paulo anasema: "Basi, je! Twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! Kinyume cha hayo twaithibitisha sheria." "Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?" Na Yohana anatangaza: "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito" (Warumi 3:31; 6:2; 1 Yohana 5:3). Katika kuzaliwa mara ya pili moyo unaafikishwa na Mungu, kwa kuwa unapatanishwa na sheria Yake. Wakati badiliko hili kubwa linapokuwa limetokea ndani ya mwenye dhambi, ametoka katika mauti na kuingia katika uzima, kutoka dhambini na kuingia katika utakatifu, kutoka katika makosa na uasi na kuingia katika utii na uaminifu. Maisha ya zamani ya kujitenga na Mungu yamekoma; maisha mapya ya upatanisho, ya imani na upendo, yameanza. Ndipo "maagizo ya torati" yatatimizwa "ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho" (Warumi 8:4). Na lugha ya roho itakuwa: "Sheria yako naipenda mno ajabu, Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa" (Zaburi 119:97).

"Sheria ya Bwana ni kamilifu, Huiburudisha nafsi" (Zaburi 19:7). Bila sheria, wanadamu hawana ufahamu wa haki wa usafi na utakatifu wa Mungu au wa hatia yao na uchafu wao. Hawana hisia ya kweli ya hatia ya dhambi na hawahisi hitaji la toba. Kwa kutokuona hali yao ya kupotea kama wavunjaji wa sheria ya Mungu, hawatambui hitaji lao la damu inayopatanisha ya Kristo. Tumaini la wokovu hupokelewa bila badiliko la moyo au matengenezo ya maisha. Kwa njia hiyo waongofu wa juu juu ni wengi, na watu wengi wanaunganishwa na kanisa ambao hawajawahi kamwe kuunganishwa na Kristo.

Nadharia potovu za utakaso, pia, zinazotokana na kupuuza au kukataa sheria ya Mungu, zinashika nafasi ya juu katika harakati za kidini za siku hizi. Nadharia hizi ni za uongo na ni za hatari katika matokeo ya kila siku; na ukweli kuwa zinakubaliwa na wengi kwa jumla, zinafanya iwe muhimu mara mbili kwamba watu wote wawe na uelewa sahihi wa kile kinachofundishwa na Maandiko kuhusu suala hili.

Utakaso wa kweli ni fundisho la Biblia. Mtume Paulo, katika barua yake kwa kanisa la Thesalonike, anasema: "Haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu." Na anaomba kuwa: "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa" (1 Wathesalonike 4:3; 5:23). Biblia inafundisha wazi juu ya utakaso na jinsi unavyopatikana. Mwokozi aliomba kwa ajili ya wanafunzi Wake: "Uwatakase kwa ile kweli, neno Lako ndiyo kweli" (Yohana 17:17). Na Paulo anafundisha kuwa waaminio wanapaswa "kutakaswa na Roho Mtakatifu" (Warumi 15:16). Kazi ya Roho Mtakatifu ni nini? Yesu aliwaambia wanafunzi Wake: "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote" (Yohana 16:13).

Na mwandishi wa Zaburi anasema: "Sheria Yako ni kweli." Kwa njia ya neno na Roho wa Mungu kanuni kuu za haki zilizowekwa katika sheria Yake zinafunuliwa. Na kwa kuwa sheria ya Mungu ni"takatifu, na ya haki, na njema," nakala ya ukamilifu wa Kimungu, ina maana kuwa tabia inayojengwa kwa njia ya kuitii sheria ile itakuwa takatifu. Kristo ni mfano mkamilifu wa tabia hiyo. Anasema: mimi nimezishika "amri za Baba yangu." "Kwa sababu

nafanya sikuzote yale yampendezayo." (Yohana 15:10; 8:29). Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa kama Yeye alivyo—kwa neema ya Mungu inawapasa wajenge tabia zinazopatana na kanuni za sheria takatifu. Huu ni utakaso wa Biblia.

Kazi hii inaweza kutekelezwa tu kwa njia ya imani katika Kristo, kwa nguvu ya Roho wa Mungu anayekaa ndani yao. Paulo anawahimiza waaminio: "Utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema" (Wafilipi 2:12, 13). Mkristo atahisi misukumo ya dhambi, lakini atadumu kuipiga vita dhambi. Hapa ndipo msaada wa Kristo unapohitajika. Udhaifu wa mwanadamu unaungana na nguvu ya Mungu, na imani inasema: "Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo" (1 Wakorintho 15:57).

Maandiko yanaoneshwa wazi kuwa kazi ya utakaso ni endelevu. Wakati wa uzoefu wa uongofu, mwenye dhambi anapopata amani na Mungu kwa njia ya damu ya upatanisho, maisha ya Ukristo ndiyo yameanza tu. Sasa inampasa "akaze mwendo ili aufikilie utimilifu;" akue "hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo." Mtume Paulo anasema: "Natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu" (Wafilipi 3:13, 14). Na Petro anaweka mbele yetu hatua ambazo inampasa mtu kuzifuata ili kupata utakaso wa Biblia: "Mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. … mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe" (2 Petro 1:5-10).

Watu wanaopata uzoefu wa utakaso wa Biblia watadhihirisha roho ya unyenyekevu. Kama Musa, wamepata udhihirisho wa utukufu wa kutisha wa utakatifu, na wanaona kutokustahili kwao wakijilinganisha na usafi na ukamilifu ulioinuliwa juu wa Yeye asiyekuwa na Kikomo.

Nabii Danieli alikuwa mfano wa utakaso wa kweli. Maisha yake marefu yalijazwa na huduma njema kwa ajili ya Bwana wake. Alikuwa mtu "apendwaye sana" (Danieli 10:11) na Mbingu. Hata hivyo, badala ya kudai kuwa msafi na mtakatifu, nabii huyu aliyeheshimiwa alijitambulisha kuwa mmoja wa wana wa Israeli ambao kwa kweli walikuwa watenda dhambi hasa alipokuwa akimlilia Mungu kwa niaba ya watu: "Hatukutolei maombi yetu kwa sababu ya haki yetu, lakini kwa sababu ya rehema zako nyingi." "Tumefanya dhambi, tumetenda maovu." Anasema: "Nilipokuwa nikisema, na kuomba, na kuiungama dhambi yangu, na dhambi ya watu wangu." Na wakati wa baadaye Mwana wa Mungu alitokea, kumpa maelekezo, Danieli anasema: "Uzuri wangu uligeuzwa ndani yangu kuwa uharibifu, wala sikusaziwa nguvu" (Danieli 9:18, 15, 20; 10:8).

Ayubu aliposikia sauti ya Bwana ikitoka katika upepo wa kisulisuli, alisema kwa huzuni: “Kwa sababu hiyo najichukia nafsi yangu, na kutubu katika mavumbi na majivu” (Ayubu 42:6). Ilikuwa wakati Isaya alipouona utukufu wa Bwana, na alipomsikia kerubi akipiga kelele, “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana wa majeshi,” ambapo alipiga kelele ya hofu, “Ole wangu! Kwa maana nimepotea” (Isaya 6:3, 5). Paulo, baada ya kuchukuliwa mpaka mbingu ya tatu na kusikia mambo ambayo yalikuwa hayawezekani kwa mwanadamu kuyatamka, anaeleza uzoefu wake kuwa alijona kuwa “mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote” (2 Wakorintho 12:2- 4; Waefeso 3:8). Ilikuwa Yohana mpendwa, ambaye aliegemea kwenye kifua cha Yesu na kuuona utukufu Wake, ambaye alianguka chini kama mtu aliyekufa mbele ya miguu ya malaika (Ufunuo 1:17).

Haiwezekani kuwepo kujiinua, madai ya majivuno ya kutokuwa na dhambi, kwa wanaotembea katika kivuli cha msalaba wa Kalwari. Wanatambua kuwa dhambi zao ndizo zilizosababisha uchungu uliovunja moyo wa Mwana wa Mungu, na wazo hili linawafanya wajishushe. Wanaoishi karibu kabisa na Yesu wanatambua kwa uwazi zaidi udhaifu na udhambi wa mwanadamu, na tumaini lao pekee linapatikana katika haki ya Mwokozi aliyesulubiwa na aliyefufuka.

Utakaso ambao sasa unashika kasi sana katika ulimwengu wa kidini unabeba pamoja nao roho ya kujiinua na kupuuza sheria ya Mungu ambayo inaupinga kama jambo geni katika dini ya Biblia. Watetezi wa utakaso huo wanafundisha kuwa utakaso ni kazi ya kufumba na kufumbua, ambao kwa njia yake, kwa njia ya imani peke yake, wanafikia utakatifu kamili. “Amini peke yake,” wanasema, “na mbaraka ni wako.” Hakuna juhudi zaidi kwa upande wa mpokeaji inayohitajika. Kwa wakati huo huo wanakataa mamlaka ya sheria ya Mungu, wakidai kuwa wameachiliwa kutoka katika ulazima wa kutunza amri. Lakini inawezekanaje kwa wanadamu kuwa watakatifu, kulingana na mapenzi na tabia ya Mungu, pasipokuwa na mwafaka kati yao na kanuni ambazo zinaeleza asili na mapenzi Yake, na ambazo zinaonesha kile kinachompendeza Yeye?

Tamaa ya kuwa na dini rahisi isiyohitaji kujitahidi, isiyohitaji kujikana nafsi, isiyohitaji kuachana na upuuzi wa kiulimwengu, imelifanya fundisho la imani, na imani pekee, kuwa fundisho pendwa; lakini neno la Mungu linasemaje? Mtume Yakobo anasema: “Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yaweza kumwokoa?... Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai? Je! Baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipomtoa Isaka mwanawe juu ya madhabahu? Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale? ... Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake” (Yakobo 2:14-24).

Ushuhuda wa neno la Mungu uko kinyume cha fundisho hili lenye mtego la imani pasipo matendo. Siyo imani inayodai upendeleo wa Mbingu pasipo utii kwa masharti ambayo ni ya lazima ili rehema itolewe, ni kujidanganya; kwa kuwa imani ya kweli msingi wake ni ahadi na maagizo ya Maandiko.

Mtu yeyote asijidanganye kuwa kuna imani ambayo kwayo mtu anaweza kuwa mtakatifu huku, kwa uchaguzi wake mwenyewe, anavunja moja ya matakwa ya Mungu. Utendaji wa dhambi inayojulikana unanyamazisha sauti inayoshuhudia ya Roho na unaitenga roho na Mungu. "Dhambi ni uasi wa sheria." Na "kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua" (1 Yohana 3:6). Ingawa Yohana katika nyaraka zake anazungumzia kikamilifu juu ya upendo, lakini hasiti kufunua tabia halisi ya tabaka la watu wanaodai kuwa wametakaswa huku wakiishi katika uasi wa sheria ya Mungu.

"Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli" (1 Yohana 2:4, 5). Hapa kuna kipimo cha kila imani ya mtu. Hatuwezi kumhesabu mtu kuwa mtakatifu bila kumpima kwa kipimo cha kiwango pekee cha Mungu cha utakatifu mbinguni na duniani. Watu wasipohisi uzito wa sheria ya uadilifu, ikiwa wanapuuza na kudharau kanuni za Mungu, ikiwa wanavunja amri iliyo ndogo kabisa miongoni mwa amri Zake, na kuwafundisha watu hivyo, wanajidhalilisha wenyewe mbele za Mbingu, na tunaweza kutambua kuwa madai yao hayana msingi.

Na dai la kutokuwa na dhambi, kwa lenyewe, ni ushahidi kuwa yeye anayetoa dai hilo yuko mbali kabisa na utakatifu. Ni kwa sababu hana uelewa sahihi wa usafi na utakatifu usio na kikomo wa Mungu au hana uelewa sahihi wa jinsi anavyopaswa kuwa yule ambaye atapatana na tabia Yake; kwa sababu hana uelewa sahihi wa usafi na uzuri ulioinuliwa juu wa Yesu, na hana uelewa sahihi wa madhara na madhila ya dhambi, ambapo mwanadamu anaweza kujidhania kuwa yeye ni mtakatifu. Kwa kadiri umbali kati yake na Kristo unavyokuwa mkubwa zaidi, na kwa kadiri uelewa wake wa tabia ya Mungu na matakwa Yake unavyokuwa mdogo zaidi, ndivyo anavyojiona kuwa yeye ni mwenye haki mbele ya macho yake mwenyewe. Utakaso ulioelezwa katika Maandiko hujumuisha uhai wote—roho, akili, na mwili. Paulo aliwaombea Wathesalonike kuwa nafsi zao na roho zao na miili yao wahifadhiwe wawe "kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo" (1 Wathesalonike 5:23).

Tena aliwaandikia waaminio: "Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu" (Warumi 12:1). Nyakati za Israeli ya zamani kila sadaka iliyoletwa kama kafara kwa Mungu ilipimwa kwa auangalifu. Ikiwa kasoro yo yote iligundulika katika mnyama aliyeletwa, mnyama yule alikataliwa; kwa sababu Mungu alikuwa ameagiza sadaka "asiyekuwa na mawaa." Kwa hiyo Wakristo wameagizwa kutoa miili yao, "dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu."

Ili kufanya hivyo, nguvu zao zote inapasa zitunzwe katika hali nzuri kabisa kwa kadiri inavyowezekana. Kila tendo linalodhoofisha nguvu za mwili au za akili linamfanya mtu asifae kwa ajili ya huduma ya Muumbaji wake.

Na je, Mungu atapendezwa na kitu chochote kilicho chini ya kiwango tunachoweza kutoa? Kristo alisema: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote." Wale wanaompenda Mungu kwa moyo wao wote watakuwa na shauku ya kumpa huduma bora kabisa ya maisha yao, na watatafuta daima kuleta kila nguvu ya maisha yao katika mwafaka na sheria zitakazokuza uwezo wao wa kutenda mapenzi Yake. Hawatadhoofisha au kuchafua, kwa kuendekeza uchu au tamaa, sadaka ambayo wanaitoa kwa Baba yao wa mbinguni.

Petro anasema: "Ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho" (1 Petro 2:11). Kila dhambi inayotendwa inatia ganzi fahamu na kuua utambuzi wa kiakili na kiroho, na neno au Roho huwa na mguso hafifu katika moyo wa mhusika. Paulo aliwaandikia Wakorintho: "Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu" (2 Wakorintho 7:1). Na pamoja matunda ya Roho—"upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole"—anajumuisha "kiasi" (Wagalatia 5:22, 23).

Licha ya matamko haya yaliyovuviwa, ni Wakristo wangapi hudhoofisha nguvu zao katika kutafuta faida ibada ya mitindo; ni wangapi hudhalilisha utu wao wenye Sura ya Mungu kwa ulafi, unywaji wa pombe, na anasa zilizokatazwa. Na kanisa, badala ya kukemea, mara nyingi huhamasisha uovu kwa kuchochea uchu, tamaa ya mapato au kupenda anasa, ili kujaza hazina ya kanisa, ambayo upendo wa Kristo umeshindwa kuijaza kwa sababu ni dhaifu mno. Ikiwa Yesu angeingia makanisa ya leo na kuona sherehe na biashara najisi zinazoendeshwa humo kwa jina la dini, je, si angewatoa nje hao watu wanaonajisi makanisa, kama alivyotoa nje wabadilishao fedha kutoka hekaluni?

Mtume Yakobo anasema kuwa hekima itokayo juu "kwanza ni safi." Ikiwa angekutana na watu wanaolikiri jina la Yesu kwa midomo iliyochafuliwa na sigara, wale ambao pumzi na miili yao imechafuliwa kwa harufu yake mbaya, na huchafua hewa ya angani na kuwalazimisha wote wanaomzunguka kuvuta sumu—ikiwa mtume angekutana na tabia hii ambayo ni kinyume na usafi wa injili, si angeikemea na kuiita "ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani"? Watumwa wa tumbaku, wakidai kuwa wamepata mbaraka wa utakaso kamili, wanazungumzia tumaini lao la mbinguni; lakini neno la Mungu linasema waziwazi kuwa "ndani yake hakitaingia kamwe cho chote kilicho kinyonge" (Ufunuo 21:27).

"Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu, na katika roho zenu, ambayo ni ya Mungu" (1 Wakorintho 6:19, 20). Yeye ambaye mwili wake ni hekalu la Roho Mtakatifu hatakuwa

mtumwa wa tabia inayomdhuru. Nguvu zake ni mali ya Kristo, ambaye amemnunua kwa ghrama ya damu. Mali yake ni mali ya Bwana. Atakosaje kuwa na hatia kwa kufuja mtaji aliopewa dhamana kuusimamia? Wanaojiita Wakristo hutumia kiasi kikubwa cha pesa kununulia vitu visivyo na manufaa na vyenye madhara, wakati roho zinaangamia kwa kukosa neno la uzima. Mungu anaibiwa zaka na sadaka, huku wakiteketeza juu ya madhabahu ya tamaa zinazoangamiza kiasi kikubwa zaidi kuliko kile wanachotoa kusaidia maskini au kwa ajili ya kutegemeza injili.

Ikiwa wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wangekuwa wametakaswa kikamilifu, mali zao, badala ya kutumika kwa ajili ya matumizi yasiyo ya lazima na hata yenye madhara, zingepaswa kuletwa katika hazina ya Bwana, na Wakristo inawapasa kuonesha mfano kiasi, kujikana nafsi, na kutoa kafara. Ndipo watakuwa nuru ya ulimwengu. Ulimwengu umejitumbukiza katika anasa. “Tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima” vinatawala idadi kubwa ya watu. “Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu.” Katika nuru ya neno la Mungu tuna haki ya kusema kuwa utakaso hauwezi kuwa wa kweli ikiwa hauwezi kufanya kazi hii ya kuukataa kabisa utafutaji wa dhambi na anasa za dunia.

Kwa wale wanaotimiza masharti, “Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, … Msiguse kitu kilicho kichafu,” ahadi ya Mungu ni, “Nami nitawakaribisha, na nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi”(2 Wakorintho 6:17, 18). Ni fursa na wajibu wa kila Mkristo kuwa na uzoefu mkubwa na mwingi katika mambo ya Mungu. “Mimi ndimi nuru ya ulimwengu,”Yesu alisema.“Yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima” (Yohana 8:12). “Bali njia ya wenye haki ni kama nuru ing’aayo, Ikizidi kung’aa hata mchana mkamilifu” (Mithali 4:18). Kila hatua ya imani na utii huileta roho katika mshikamano wa karibu zaidi na Nuru ya ulimwengu, ambamo ndani Yake “giza lo lote hamna.” Miale inayong’ara ya Jua la Haki inawamulika watumishi wa Mungu, na wao wanaakisi miale ya nuru Yake. Kama vile nyota zinavyotuambia kuwa kuna nuru kubwa mbinguni ambayo inazifanya zinang’are, kadhalika Wakristo wanapaswa kudhihirisha kuwa kuna Mungu juu ya kiti cha enzi cha Ulimwengu ambaye anastahili sifa na kuigwa. Neema za Roho, usafi na utakatifu wa tabia Yake, vitaonekana miongoni mwa mashahidi Wake.

Paulo katika barua yake kwa Wakolosai anataja mibaraka mikubwa inayotolewa kwa watoto wa Mungu. Anasema: “Hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mjazwe maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni; mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu; mkiwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake, mpate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha” (Wakolosai 1:9-11).

Kadhalika anaandika kuhusu shauku yake kuwa ndugu walioko Efeso wajue kimo cha upendeleo wa Mkristo. Anawaeleza, kwa lugha fasaha kabisa, nguvu na maarifa ya ajabu ambayo wanaweza kuwa nayo kama wana na binti za Yeye Aliye Juu sana. Ilikuwa stahiki yao "kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani," kuwa "na shina na msingi katika upendo ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu." Lakini ombi la mtume linafikia kilele cha upendeleo anapoomba kuwa "mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu" (Waefeso 3:16-19).

Hapa kuna kimo cha mafanikio ambacho tunaweza kukifikia kwa njia ya imani katika ahadi za Baba yetu wa mbinguni, tunapotimiza matakwa Yake. Kwa njia ya haki ya Kristo tunayo fursa ya kukiendea kiti cha enzi cha Nguvu Isiyokuwa na Mipaka. "Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?" (Warumi 8:32). Baba alimtoa Roho Wake kwa Mwana Wake bila kipimo, na sisi pia tunaweza kushiriki ukamilifu Wake. Yesu anasema, "Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" (Luka 11:13). "Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya." "Ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu" (Yohana 14:14: 16:24).

Ingawa maisha ya Mkristo yatadhihirisha unyenyekevu, hayapaswi kugubikwa na huzuni na kutojithamini. Ni fursa iliyo wazi kila mmoja kuishi kwa jinsi ambayo Mungu atamkubali na kumbariki. Siyo mapenzi ya Baba yetu wa mbinguni kuwa tuwe chini ya hukumu na giza daima. Hakuna ushahidi wa unyenyekevu wa kweli katika kutembea huku kichwa kimeinamishwa chini na moyo ukiwa umejaa mawazo ya ubinafsi. Tunaweza kumwendea Yesu ili tutakaswe, na kusimama mbele ya sheria bila aibu wala hatia. "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu" (Warumi 8:1).

Kwa njia ya Yesu wana wa Adamu walioanguka wanakuwa "wana wa Mungu." "Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake" (Waebrania 2:11). Maisha ya Mkristo yanapaswa kuwa ya imani, ushindi, na furaha ndani ya Mungu. "Kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu" (1 Yohana 5:4). Mtumishi wa Mungu Nehemia alisema ukweli: "Furaha ya Bwana ni nguvu zenu" (Nehemia 8:10). Na Paulo anasema: "Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, Furahini.""Furahini siku zote; ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu" (Wafilipi 4:4; 1 Wathesalonike 5:16-18).

Haya ndiyo matunda ya uongofu na utakaso wa Biblia; na ni kwa sababu kanuni kuu za haki zilizotajwa katika sheria ya Mungu hazipendwi sana na ulimwengu wa Wakristo ndio maana matunda haya hayaonekani sana. Hii ndiyo sababu kuna udhihirisho mdogo sana wa

kazi endelevu na ya kina ya Roho wa Mungu iliyokuwepo katika harakati za uamsho za miaka ya awali. Ni kwa kutazama tunabadilishwa. Na zile kanuni takatifu ambazo ndani yake Mungu amewafunulia watu ukamilifu na utakatifu wa tabia Yake zinapopuuzwa, na akili za watu zikavutwa kutafakari mafundisho na nadharia za kibinadamu, hatupaswi kushangaa kuwa kuna poromoko la utakatifu kanisani. Bwana alisema: "Wameniacha mimi, niliye chemchemi ya maji ya uzima, wamejichimbia mabirika, mabirika yavujayo, yasiyoweza kuweka maji" (Yeremia 2:13).

"Heri mtu yule asiyekwenda Katika shauri la wasio haki…. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa" (Zaburi 1:1-3). Ni pale tu sheria ya Mungu inaporudishwa mahali pake stahiki kunaweza kuwepo uamsho wa imani na utauwa wa awali miongoni mwa watu wa Mungu. "Bwana asema hivi, Simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu." (Yeremia 6:16).

Sura ya 28 - Siku ya Hukumu

"Nikatazama", anasema nabii Danieli, "hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa" (Daniel 7:9, 10).

Hivyo ndivyo nabii Danieli alivyooneshwa katika njozi siku kuu na ya kutisha wakati tabia na maisha ya watu vitakapochunguzwa na Jaji Mkuu wa dunia yote, na kila mtu kulipwa "sawasawa na matendo yake." Mzee wa Siku ni Mungu Baba. Anasema mwandishi wa Zaburi: "Kabla haijazaliwa milima, wala hujaiumba dunia, Na tangu milele hata milele ndiwe Mungu" (Zaburi 90:2). Ni Yeye, aliye chanzo cha uhai, na chemchemi ya sheria, atakayekalia kiti cha hukumu. Na malaika kama wahudumu na mashahidi ambao idadi yao ni "maelfu elfu … na elfu kumi mara elfu kumi," wanahudhuria mahakama kuu hii.

"Na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe" (Danieli 7:13, 14). Ujio wa Kristo unaoelezwa hapa siyo ujio Wake wa pili duniani. Anakuja kwa Mzee wa Siku mbinguni apewe mamlaka na utukufu na ufalme, ambao atapewa mwisho wa kazi Yake kama mpatanishi. Ni ujio huu, ule uliotabiriwa katika unabii kuwa utatimizwa mwishoni mwa siku 2300 mwaka 1844, na siyo ujio Wake wa pili duniani. Akisindikizwa na malaika wa mbinguni, Kuhani wetu Mkuu anaingia patakatifu pa patakatifu na pale anakwenda mbele ya Mungu afanye kazi ya huduma Yake kwa ajili ya mwanadamu—kufanya kazi ya hukumu ya upelelezi na kufanya upatanisho kwa ajili ya wote wanaoonekana kuwa wanastahili kupata manufaa ya upatanisho.

Katika huduma ya mfano wale tu waliokuja mbele ya Mungu wakiungama na kutubu, na ambao dhambi zao, kwa njia ya sadaka ya dhambi, zilihamishiwa katika chumba cha patakatifu, walikuwa na sehemu katika huduma ya Siku ya Upatanisho. Kwa hiyo, katika siku kuu ya upatanisho wa mwisho na hukumu ya upepelezi kesi zitakazoshughulikiwa zitakuwa zile tu za wanaodai kuwa watu wa Mungu. Hukumu ya waovu ni kazi ya pekee na inayojitegemea, na hutokea kipindi cha baadaye. "Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje?" (1 Petro 4:17).

Vitabu vya kumbukumbu mbinguni, ambamo majina na matendo ya wanadamu yameandikwa, vitatumiwa kufanyia maamuzi ya hukumu. Nabii Danieli anasema: "Hukumu

ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa.” Nabii wa Ufunuo, akieleza mandhari hiyo hiyo, anaongezea: “na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao” (Ufunuo 20:12).

Kitabu cha uzima kina majina ya wote waliowahi kuingia katika huduma ya Mungu. Yesu aliwaagiza wanafunzi Wake: “Furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni” (Luka 10:20). Paulo anazungumzia juu ya watenda kazi wenzake waaminifu, “ambao majina yao yamo katika kitabu cha uzima” (Wafilipi 4:3). Danieli, akitazama kwa mbali hata “wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo,” anaeleza kuwa watu wa Mungu wataokolewa, “kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile.” Na nabii wa Ufunuo anasema kuwa wataingia katika jiji la Mungu wale tu ambao majina yao yameandikwa “katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo” (Danieli 12:1; Ufunuo 21:27).

“Kitabu cha ukumbusho” kimeandikwa mbele ya Mungu, ambamo yameandikwa matendo mema “ya hao waliomcha Bwana, na kulitafakari jina lake” (Malaki 3:16). Maneno yao ya imani, matendo yao ya upendo, yameandikwa mbinguni. Nehemia anaeleza jambo hili anaposema: “Unikumbukie hayo, Ee Mungu wangu, wala usifute fadhili zangu nilizozitenda kwa ajili ya nyumba ya Mungu wangu”(Nehemia 13:14). Katika kitabu cha Mungu cha kumbukumbu kila tendo la haki limeandikwa. Pale, kila jaribu lililopingwa, kila uovu ulioshindwa, kila neno la huruma na upendo lililotamkwa, linaandikwa kwa uaminifu. Na kila tendo la kujitoa kafara, kila teso na huzuni iliyopitiwa kwa ajili ya Kristo, linaandikwa. Mwandishi wa zaburi anasema: “Umehesabu kutanga-tanga kwangu; Uyatie machozi yangu katika chupa yako; (Je! Hayamo katika kitabu chako?)” (Zaburi 56:8).

Kuna kumbukumbu pia ya dhambi za watu. “Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya.” “Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.” Mwokozi anasema: “Kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa” (Mhubiri 12:14; Mathayo 12:36, 37). Makusudi na nia ya siri vinaonekana katika kitabu cha kumbukumbu kisichokosea; kwa kuwa Mungu “atayamulikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo” (1 Wakorintho 4:5). “Tazama, neno hili limeandikwa mbele zangu…. maovu yenu na maovu ya baba zenu pamoja, asema Bwana” (Isaya 65:6, 7).

Kila kazi ya mtu inachunguzwa na Mungu na inaandikwa ama kama ni ya uaminifu au sio ya uaminifu. Mbele ya kila jina katika vitabu vya mbinguni pameandikwa kwa usahihi wa kutisha kila neno lisilo sahihi, kila tendo la ubinafsi, kila wajibu ambao haukutimizwa, na kila dhambi ya siri, na kila aina ya udanganyifu uliofichika. Maonyo yaliyotumwa kutoka mbinguni yakapuuzwa, muda uliopotezwa, fursa ambazo hazikufanyiwa kazi, mvuto

uliohamasisha wema au uliochochea uovu, pamoja na matokeo yake mapana, yote yameandikwa na malaika anayetunza kumbukumbu.

Sheria ya Mungu ndicho kiwango kitakachotumika kupima tabia na maisha ya watu katika hukumu. Alisema mtu mwenye hekima: "Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu; Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi" (Mhubiri 12:13, 14). Mtume Yakobo anawaonya ndugu zake: "Semeni ninyi, na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru" (Yakobo 2:12).

Wale ambao katika hukumu wanahesabiwa "kuwa wamestahili" watakuwa na sehemu katika ufufuo wa wenye haki. Yesu alisema: "Wale wahesabiwao kuwa wamestahili kuupata ulimwengu ule, na kule kufufuka katika wafu, … huwa sawasawa na malaika, nao ni wana wa Mungu, kwa vile walivyo wana wa ufufuo" (Luka 20:35, 36). Na tena anasema kuwa "wale waliofanya mema" watatoka "kwa ufufuo wa uzima" (Yohana 5:29). Wenye haki waliokufa hawatafufuliwa mpaka baada ya hukumu ambayo kwayo wamehesabiwa kuwa wamestahili "ufufuo wa uzima." Kwa hiyo hawatakuwepo mahakamani kimwili wakati kumbukumbu zao zikichunguzwa na kesi zao zikiamriwa.

Yesu atakuwepo kama wakili wao, akiomba na kusihi kwa ajili yao mbele za Mungu. "Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki" (1 Yohana 2:1). "Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu.""Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee" (Waebrania 9:24; 7:25).

Vitabu vya kumbukumbu vilifunguliwa katika hukumu, maisha ya wote waliomwamini Yesu vilichunguzwa mbele za Mungu. Uchunguzi ukianza na watu wa kwanza kuishi duniani, Wakili wetu anawasilisha kesi za kizazi baada ya kizazi, na anamalizia na walio hai. Kila jina linatajwa, kila kesi inachunguzwa kwa makini. Majina mengine yanakubaliwa, na majina mengine yanakataliwa. Ikiwa jina lo lote lina dhambi ambazo bado zimebaki katika vitabu vya kumbukumbu, ambazo mhusika hajazitubu na kusamehewa, majina yao yanafutwa kutoka katika kitabu cha uzima, na kumbukumbu ya matendo mema yanafutwa kutoka katika kitabu cha ukumbusho. Bwana alimwambia Musa: "Mtu ye yote aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta katika kitabu changu" (Kutoka 32:33).

Na anasema nabii Ezekieli: "Mwenye haki atakapoghairi, na kuiacha haki yake, na kutenda uovu, matendo yake yote ya haki aliyoyatenda halitakumbukwa hata mojawapo" (Ezekieli 18:24). Wote ambao wametubu dhambi kweli kweli, na kwa imani wakadai damu ya Kristo kuwa kafara yao ya upatanisho, msamaha huingizwa mbele ya majina yao katika vitabu vya mbinguni; kwa kuwa wamekuwa washirika wa haki ya Kristo, na tabia zao zinaonekana kupatana na sheria ya Mungu, dhambi zao zitafutwa kutoka katika vitabu, na

wao watahesabiwa kuwa wanastahili uzima wa milele. Bwana anasema, kupitia kwa nabii Isaya: "Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako" (Isaya 43:25). Yesu alisema: "Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake." "Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni" (Ufunuo 3:5; Mathayo 10:32, 33).

Shauku kubwa inayooneshwa miongoni mwa wanadamu katika maamuzi ya mahakama za kidunia inawakilisha japo kwa uhafifu shauku inayodhihirishwa katika mahakama ya mbinguni wakati majina yaliyoingizwa katika kitabu cha uzima yanapoletwa kuchunguzwa na Jaji Mkuu wa dunia yote. Mwombezi wa Kimungu anawasilisha ombi kuwa wote walioshinda kwa njia ya imani katika damu Yake wasamehewe dhambi zao, kuwa warudishwe katika nyumba yao ya Edeni, na wavikwe taji kama warithi pamoja Naye wa "mamlaka ya kwanza" (Mika 4:8). Shetani katika juhudi zake za kudanganya na kujaribu wanadamu alikusudia kuharibu mpango wa Kimungu wa kumuumba mwanadamu; lakini Kristo sasa anaomba kuwa mpango huu utekelezwe kana kwamba mwanadamu hajawahi kuanguka. Anaomba kwa ajili ya watu Wake siyo tu msamaha na kuhesabiwa haki, kuliko kamili na kamilifu, bali pia wapewe sehemu ya utukufu Wake na waketishwe katika kiti Chake cha enzi.

Wakati Yesu akiwaombea wanufaikaji wa neema yake, Shetani anawashitaki mbele za Mungu kama wakosaji. Mdanganyaji mkuu alitafuta kuwaingiza katika mashaka, kuwafanya wamshuku Mungu, ili wajitenge na upendo Wake, na wavunje sheria Yake. Sasa anaonesha kumbukumbu za maisha yao, anawaonesha dosari katika tabia zao, jinsi wasivyofanana na Kristo, ambako kumemwaibisha Mkombozi wao, anawaonesha dhambi zote alizowashawishi kuzitenda, na kwa sababu ya hizo dhambi anadai kuwa ni watu wake.

Yesu hatoi udhuru kwa ajili ya dhambi zao, bali anaonesha toba na imani yao, na, anadai msamaha kwa ajili yao, ananyosha juu mikono Yake iliyojeruhiwa mbele ya Baba na malaika, akisema: nawajua kwa majina yao. Nimewachora juu ya viganja vya mikono Yangu. "Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau" (Zaburi 51:17). Na kwa mshitaki wa watu Wake anasema: "Bwana akamwambia Shetani, Bwana na akukemee Ewe Shetani; naam, Bwana, aliyechagua Yerusalemu, na akukemee; je! Hiki si kinga kilichotolewa motoni?" (Zekaria 3:2). Kristo aliwavika watu Wake waaminifu kwa haki Yake, ili awawasilishe kwa Baba Yake kama "Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa" (Waefeso 5:27). Majina yao yamebaki yakiwa yameandikwa katika kitabu cha uzima, na kuhusiana nao imeandikwa: "Nao watakwenda pamoja nami hali wamevaa mavazi meupe, kwa kuwa wamestahili" (Ufunuo 3:4).

Kwa njia hiyo itatimia kikamilifu ahadi ya agano: “Nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena.”“Katika siku hizo na wakati huo, asema Bwana, uovu wa Israeli utatafutwa, wala uovu hapana; na dhambi za Yuda zitatafutwa, wala hazitaonekana” (Yeremia 31:34; 50:20). “Siku hiyo chipukizi la Bwana litakuwa zuri, lenye utukufu, na matunda ya nchi yatakuwa mema sana, na kupendeza, kwa ajili ya Waisraeli wale waliookoka. Tena itakuwa ya kwamba yeye aliyebaki katika Sayuni, na yeye aliyeachwa ndani ya Yerusalemu, ataitwa mtakatifu; yaani, kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa hao walio hai ndani ya Yerusalemu” (Isaya 4:2, 3).

Kazi ya hukumu ya upelelezi na utakasaji wa dhambi inapaswa kutekelezwa kabla ya ujio wa pili wa Bwana. Kwa kuwa watu waliokufa wanahukumiwa kutokana na mambo yaliyoandikwa katika vitabu, haiwezekani kuwa dhambi zao zifutwe mpaka baada ya hukumu ambapo kesi zao zinachunguzwa. Lakini mtume Petro anasema wazi kuwa dhambi za waaminio zitafutwa “nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo” (Matendo 3:19, 20). Wakati hukumu ya upelelezi itakapofungwa, Kristo atakuja, na ujira Wake utakuwa pamoja Naye kumlipa kila mmoja sawasawa na matendo yake.

Katika huduma ya mfano kuhani mkuu, baada ya kufanya upatanisho kwa ajili ya Israeli, alitoka nje kuwabariki watu. Kadhalika Kristo, mwishoni mwa kazi Yake kama mwombezi, atatokea, “pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu” (Waebrania 9:28), kuwabariki watu Wake kwa uzima wa milele. Kama kuhani, kwa kuondoa dhambi kutoka katika hema, aliziungama juu ya kichwa cha mbuzi wa Azazeli, kadhalika Kristo ataweka dhambi zote juu ya Shetani, mwanzilishi na mchochezi wa dhambi. Mbuzi wa Azazeli, akiwa amebeba dhambi za Israeli, alipelekwa mbali “mpaka nchi isiyo watu” (Walawi 16:22); kadhalika Shetani, akiwa amebeba hatia ya dhambi zote alizosababisha watu kuzitenda, atafungwa kwa miaka elfu moja duniani, ambayo wakati huo itakuwa ukiwa, bila watu, na mwishowe atapewa adhabu ya mwisho ya dhambi katika moto ambao utawaangamiza waovu wote. Hivyo, mpango mkuu wa ukombozi utafikia ukamilifu wake kwa kuondoa kabisa dhambi na kwa wokovu wa wote waliochagua kuachana na uovu.

Wakati uliopangwa wa hukumu—mwishoni mwa siku 2300, mwaka 1844—ilianza kazi ya upepelezi na utakaso wa dhambi. Wote waliowahi kubeba jina la Kristo itawapasa kupita katika uchunguzi wa kina wa hukumu ya upelelezi. Walio hai na waliokufa watapaswa kuhukumiwa “katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.” Dhambi ambazo hazikuungamwa na kuachwa hazitasamehewa wala kufutwa katika vitabu vya kumbukumbu, lakini zitasimama na kutoa ushuhuda dhidi ya mwenye dhambi katika siku ya Mungu. Anaweza kuwa alizitenda wakati wa nuru ya mchana au katika giza la usiku; lakini zilikuwa wazi na dhahiri mbele Yake Yeye tunayewajibika Kwake. Malaika wa Mungu walishuhudia kila dhambi na waliiandika katika kumbukumbu zisizokosea. Dhambi inaweza kufichwa, kukanwa, kufunikwa isionwe na baba, mama, mke, watoto, na marafiki;

hakuna mtu mmoja isipokuwa mwenye hatia anayeweza kuwa na mashaka kuhusu dhambi hiyo; lakini iko wazi mbele za wenye akili wa mbinguni. Giza la usiku wenye giza totoro, usiri wa sanaa zote za udanganyifu, halitoshi kuficha wazo hata moja lisijulikane kwa Yule aliyepo milele zote. Mungu anayo kumbukumbu sahihi ya kila taarifa isiyo ya haki na kila tendo la uonevu. Hadanganywi na mwonekano wa utakatifu.

Hafanyi makosa katika tathmini Yake ya tabia. Watu wanaweza kudanganywa na wale walio mioyo miovu, lakini Mungu anapenya mionekano yote na kusoma maisha ya ndani. Wazo hilo linatisha kiasi gani! Siku baada ya siku, hadi katika umilele, linabeba mzigo wake wa kumbukumbu za mbinguni. Maneno yanapotamkwa mara moja, matendo yakitendwa mara moja, hayawezi kukumbukwa. Malaika wameandika mema na mabaya. Mshindi mwenye nguvu kuliko wote duniani hawezi kurudisha kumbukumbu hata za siku moja. Matendo yetu, maneno yetu, hata nia zetu za sirini kabisa, yote yana uzito katika kuamua hatima yetu kwa wema kwa ubaya. Hata kama tutakuwa tumeyasahau, yatatoa ushahidi wao kututhibitisha au kutuhukumu.

Kama vile alama za usoni zinavyonakiliwa kwa usahihi usiokosea kwenye bamba lililong'arishwa la mchoraji, kadhalika tabia imenakiliwa kwa uaminifu katika vitabu vya mbinguni. Ni kujali kidogo kiasi gani kunahisiwa kuhusiana na kumbukumbu ambazo inapasa zichunguzwe na wenye uhai wa mbinguni. Ikiwa pazia linalotenganisha ulimwengu unaoonekana na usioonekana lingeondolewa, na wanadamu wamwone malaika akiandika kila neno na tendo, ambalo itawapasa kukutana nalo katika hukumu, ni maneno mangapi ambayo yanasemwa kila siku yangebaki bila kusemwa, na ni matendo mangapi yangebaki bila kutendwa.

Katika hukumu, uchunguzi utafanywa kuhusiana na jinsi kila talanta ilivyotumika. Tumetumiaje mtaji tuliokopeshwa na Mbingu? Bwana atakaporudi atapata iliyo yake pamoja na faida? Tumeboresha uwezo tuliodhaminiwa, katika mkono na moyo na akili, kwa ajili ya utukufu wa Mungu na kwa ajili ya kuubariki ulimwengu? Tumetumiaje muda wetu, kalamu zetu, sauti zetu, pesa zetu, na mvuto wetu? Tumemfanyia nini Kristo, katika kuwahudumia maskini, yatima na wajane? Mungu ametufanya kuwa wahifadhi wa neno Lake takatifu; tumefanya nini na nuru na ukweli tuliopewa kuwafanya watu wawe na hekima kwa ajili ya wokovu? Hakuna thamani yo yote imeambatanishwa na madai ya mdomo ya kuwa na imani katika Kristo peke yake; upendo ambao unadhihirishwa kwa vitendo ndio pekee unahesabiwa kuwa wa dhati. Lakini ni upendo pekee mbele za Mbingu ambao unafanya tendo lolote liwe na thamani. Lo lote ambalo linatendwa kutokana na upendo, hata kama lingekuwa dogo kiasi gani katika tathmini ya kibinadamu, linakubaliwa na kuzawadiwa na Mungu.

Uchoyo uliofichika wa wanadamu umefunuliwa katika vitabu vya mbinguni. Pale kuna kumbukumbu ya wajibu ambao haukutimizwa kwa wanadamu wenzao, ya usahaulifu wa madai ya Mwokozi. Pale wataona ni mara ngapi wakati, fikra, na nguvu ambazo ni mali ya

Kristo vilitolewa kwa Shetani. Kumbukumbu ambazo malaika wanapeleka mbinguni ni za kuhuzunisha kiasi gani. Wenye uhai wenye akili, wanaotangaza kuwa wafuasi wa Kristo, wanajishughulisha zaidi na kukusanya mali za kidunia au kufurahia anasa za dunia. Pesa, wakati, na nguvu vinatolewa kafara kwa ajili ya kujionesha na kukidhi tamaa binafsi; lakini ni nyakati chache sana zinatumiwa kwa ajili ya maombi, kwa ajili ya kuchunguza Maandiko, kujinyenyekesha na kuungama dhambi.

Shetani anagundua mipango isiyokuwa na idadi ya kushikilia akili zetu, ili zisijishughulishe na kazi ambayo tulipaswa kuifahamu vizuri kuliko kitu kingine cho chote. Mdanganyaji mkuu anachukia vipengele muhimu vya ukweli vinavyodhihirisha kafara ya upatanisho na mwombezi mwenye nguvu zote. Anajua kuwa kwake yeye kila kitu hutegemea kuelekeza akili za watu mbali na Yesu na ukweli Wake.

Wale ambao wanapaswa kuwaeleza wengine manufaa ya upatanisho wa Mwokozi hawapaswi kuruhusu kitu chochote kuingilia wajibu wao wa kuwa na utakatifu kamili katika kicho cha Mungu. Saa za thamani, badala ya kutumiwa katika anasa, kujionesha, kutafuta mapato, zinapaswa kutumiwa usomaji wa neno la kweli kwa moyo wa dhati na kwa maombi mengi. Somo la patakatifu na hukumu ya upelelezi inapasa lieleweke kikamilifu kwa watu wa Mungu. Wote wanahitaji kujua wenyewe nafasi na kazi ya kuhani wao Mkuu. Vinginevyo haitawezekana kwao kufanyia mazoezi imani ambayo ni ya muhimu kwa wakati huu au kujaza nafasi ambayo Mungu amepanga waijaze. Kila mtu ana nafsi ya kuokoa au kupoteza. Kila mtu ana kesi inayomngoja katika mahakama ya Mungu. Kila mmoja inampasa kukutana na Jaji Mkuu uso kwa uso. Ni muhimu kiasi gani, hivyo basi, kuwa kila akili itafakari mara kwa mara mandhari ya kutisha wakati hukumu itakapokaa na vitabu vitakapofunguliwa, wakati, pamoja na Danieli, kila mtu atapaswa asimame katika kizimba chake, mwishoni mwa siku.

Wote ambao wamepokea nuru juu ya masomo haya inawapasa kutoa ushuhuda wa ukweli mkuu ambao Mungu amewakabidhi. Patakatifu pa mbinguni ndiyo kituo mahsusi cha kazi ya Kristo kwa ajili ya wanadamu. Panaihusu kila nafsi inayoishi duniani. Panafunua mpango wa ukombozi, pakituleta karibu kabisa na mwisho wa wakati na pakifunua suala la ushindi wa pambano kati ya haki na dhambi. Ni suala muhimu sana kuwa wote wajifunze masomo haya na waweze kumjibu kila mtu awaulizaye sababu ya tumaini lililoko ndani yao.

Maombezi ya Kristo kwa ajili ya mwanadamu ndani ya patakatifu pa mbinguni ni muhimu sana kwa ajili ya mpango wa wokovu kama kifo Chake msalabani kilivyo muhimu. Kwa kifo Chake alianza kazi ambayo baada ya ufufuo Wake alipaa kumalizia mbinguni. Inatupasa kwa imani kuingia ndani ya pazia, "alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu" (Waebrania 6:20). Mle nuru kutoka kwenye msalaba wa Kalwari inaakisiwa. Mle tunaweza kupata uelewa wa wazi zaidi kuhusu siri za ukombozi. Wokovu wa mwanadamu unatekelezwa kwa gharama isiyokuwa na kikomo ya mbinguni; kafara iliyotolewa ni

sawasawa na madai mapana ya sheria ya Mungu iliyovunjwa. Yesu amefungua njia ya kwenda kwenye kiti cha enzi cha Baba, na kwa njia ya upatanisho Wake, shauku ya dhati ya wote wanaokwenda Kwake kwa imani wanaweza kuwasilishwa kwa Mungu.

"Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; Bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema" (Mithali 28:13). Ikiwa wale wanaoficha na kutoa udhuru kwa ajili ya makosa yao wangeona jinsi Shetani anavyofurahia kwa ajili yao, jinsi anavyomsuta Kristo na malaika watakatifu kwa sababu ya ufichaji na udhuru wao huo, wangeharakisha kuungama dhambi zao na kuziacha. Kwa njia ya dosari katika tabia zao, Shetani anatenda kazi kutawala akili yote, na anajua kuwa ikiwa dosari hizi zitapaliliwa, atafaulu. Kwa hiyo anatafuta daima kuwadanganya wafuasi wa Kristo kwa hila zake zinazofisha kiasi ambacho haiwezekani wao wenyewe kushinda. Lakini Yesu anasihi kwa ajili yao kwa njia ya mikono Yake iliyojeruhiwa, mwili Wake uliochubuliwa; na anawaambia wafusi Wake: "Neema yangu yakutosha" (2 Wakorintho 12:9). "Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi" (Mathayo 11:29, 30). Hivyo basi, asiwepo mtu anayechukulia kuwa dosari zake hazitibiki. Mungu atatoa imani na neema ili kuzishinda.

Tunaishi sasa katika siku kuu ya upatanisho. Katika huduma ya mfano, wakati kuhani mkuu alipokuwa akifanya upatanisho kwa ajili ya Israeli, wote walitakiwa kutesa nafsi zao kwa toba na kujinyenyekesha mbele za Bwana, ili wasije wakaondolewa kutoka miongoni mwa watu. Hali kadhalika, wale wote ambao wanapenda kudumisha majina yao katika kitabu cha uzima inawapasa sasa, katika siku chache zilizosalia za rehema, kutesa nafsi zao mbele za Mungu kwa kuhuzunikia dhambi zao na kufanya toba ya kweli. Inapasa kujichunguza moyoni kwa kina na kwa uaminifu.

Roho ya kurahisisha mambo ya kejeli inayoendekezwa na wengi wanaodai kuwa Wakristo inapaswa kuachwa. Kuna vita kali kabisa inayowakabili wote wanaojitahidi kudhibiti mielekeo ya uovu inayotaka kutawala nafsi. Kazi ya matayarisho ni kazi ya mtu mmoja mmoja binafsi. Hatuokolewi katika makundi. Usafi na uaminifu wa mtu mmoja hautafidia upungufu wa sifa hizi kwa mtu mwingine. Ingawa inapasa mataifa yote kupita katika hukumu ya Mungu, pamoja na hayo, atachunguza kesi ya mtu mmoja mmoja kwa karibu na kwa kina kana kwamba hakuna mtu mwingine duniani. Kila mmoja inapasa ajaribiwe na aonekane kuwa hana doa au kunyanzi au chochote cha aina hiyo.

Mandhari zinazoambatana na kazi ya mwisho ya upatanisho zinatisha sana. Maslahi makubwa yanahusishwa na kazi hiyo. Hukumu inapita sasa katika patakatifu pa mbinguni. Kwa miaka mingi kazi hii imekuwa ikiendelea. Muda mfupi—hakuna anayejua ni muda mfupi kiasi gani— itahamia kwa kesi za walio hai. Mbele ya uwepo wa kutisha wa Mungu maisha yetu yanapaswa kupelekwa kwa ajili ya uchunguzi. Wakati huu juu ya nyakati zingine zote inapasa kila nafsi kuzingatia onyo la Yesu:"Angalieni, kesheni, ombeni, kwa kuwa

hamjui wakati ule utakapokuwapo" (Marko 13:33). "Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako" (Ufunuo 3:3).

Wakati kazi ya hukumu ya upelelezi itakapofungwa, hatima ya wote itakuwa imeamriwa kwa ajili ya uzima au mauti. Rehema inafungwa muda mfupi kabla ya kuonekana kwa Bwana katika mawingu ya mbinguni. Kristo katika Ufunuo, akitazama mbele na kuuona wakati huu, alisema: "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa.

Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo" (Ufunuo 22:11, 12). Wenye haki na waovu watakuwa bado wakiishi duniani katika hali ya kufa—watu watakuwa wakipanda na kujenga, wakila na kunywa, wote bila kujua kuwa uamuzi wa mwisho, usiotenguliwa umekwisha kutangazwa katika patakatifu pa mbinguni. Kabla ya Gharika, baada ya Nuhu kuingia katika safina, Mungu alimfungia ndani na kuwafungia nje wasiomcha Mungu; lakini kwa siku saba watu, bila kujua kuwa maangamizi yao yamekwisha kupangwa, waliendelea na maisha yao ya kutokujali, ya kupenda anasa na waliendelea kudhihaki hukumu iliyokuwa mbele yao. "Ndivyo," anasema Mwokozi, "kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu" (Mathayo 24:39). Kimya kimya, bila taarifa, kama mwizi wa usiku wa manane, itafika saa ile ya uamuzi ambayo itapanga hatima ya kila mtu, saa ya kuondolewa kabisa kwa fursa ya rehema kwa mwanadamu mwenye hatia.

"Kesheni basi, … asije akawasili ghafula akawakuta mmelala" (Marko 13:35, 36). Hali ya hatari inawakabili wale wote ambao, kwa kuchoka kukesha, wanageukia vivutio vilivyopo ulimwenguni. Wakati mfanya biashara amemezwa na utafutaji wa mapato, wakati mtafutaji wa anasa amezama katika tamaa zake, na wakati binti wa mitindo anapangilia mapambo yake—inawezekana katika saa ile Jaji Mkuu wa dunia yote akatangaza hukumu: "Umepimwa katika mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka" (Daniel 5:27).

Sura ya 29 - Chimbuko la Uovu

Kwa akili za watu wengi, chimbuko la dhambi pamoja na sababu ya kuwepo kwake ni jambo linalotatanisha sana. Wanaona kazi ya uovu, na matokeo yake ya kutisha ya huzuni na taabu, na wanahoji ni kwa jinsi gani haya yote yanaweza kuwepo chini ya utawala wa Mungu ambaye hana kikomo katika hekima, nguvu, na upendo. Hapa kuna siri ambayo hawana maelezo yake. Na katika kutokuwa na hakika kwao na kwa sababu ya mashaka yao wanapofushwa wasione ukweli uliofunuliwa kwa uwazi katika neno la Mungu na ulio muhimu kwa ajili ya wokovu. Kuna wale ambao, katika maswali yao kuhusu uwepo wa dhambi, wanajaribu kutafuta mambo ambayo Mungu hakuyafunua; matokeo yake hawapati suluhisho la matatizo yao; na kwa kuwa wanasukumwa na mashaka wanachukulia kukosa suluhisho huko kama udhuru wa kutupilia mbali maneno ya Maandiko Matakatifu. Wengine, hata hivyo, hawana uelewa wa kutosha wa tatizo kubwa na uovu, kutokana na ukweli kuwa mapokeo na tafsiri potovu vimefunika fundisho la Biblia kuhusu tabia ya Mungu, msingi wa serikali Yake, na kanuni Zake za kushughulikia dhambi.

Haiwezekani kueleza chimbuko la dhambi kwa namna ambayo inawezesha kutoa sababu za kuwepo kwake. Hata hivyo inawezekana kuelewa chimbuko na mwisho wa dhambi kwa namna ambayo inawezesha kudhihirisha kikamilifu haki na ukarimu wa Mungu katika kushughulikia uovu.

Hakuna wazo ambalo limefundishwa kwa uwazi zaidi katika Maandiko kuliko wazo kuwa Mungu kwa namna yo yote ile hawajibiki kwa ajili ya uingiaji wa dhambi; kwamba hakukuwa na uondoaji wa kiimla wa neema ya Mungu, kwamba hakukuwa na dosari katika serikali ya Mungu, iliyosababisha kuinuka kwa uasi. Dhambi ni mvamizi, ambaye hakuna sababu inaweza kutolewa kwa ajili ya uwepo wake. Dhambi ni fumbo, haielezeki; kuitolea udhuru ni kuitetea. Ikiwa udhuru kwa ajili ya dhambi ungepatikana, au sababu ioneshwe kwa ajili ya uwepo wake, ingekoma kuwa dhambi. Fasili pekee ya dhambi ni ile iliyotolewa katika neno la Mungu; dhambi ni "uasi wa sheria;" ni matokeo ya utekelezaji wa kanuni inayopingana na sheria kuu ya upendo ambao ni msingi wa serikali ya Mungu.

Kabla ya kuingia kwa uovu kulikuwa na amani na furaha katika Ulimwengu wote. Mambo yote yalikuwa katika mwafaka na mapenzi ya Mungu. Upendo kwa Mungu ulikuwa juu, upendo wa mtu mmoja kwa mwingine ulikuwa hauna upendeleo. Kristo aliye Neno, Mwana Pekee wa Mungu, alikuwa mmoja na Baba wa milele,—mmoja katika asili, katika tabia, na katika kusudi,—mwenye uhai pekee katika Ulimwengu wote aliyekuwa na fursa ya kushiriki mashauri na makusudi ya Mungu. Kwa njia ya Kristo Baba alitekeleza uumbaji wa wote wenye uhai walioko mbinguni. "Katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni…ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka" (Wakolosai 1:16); na kwa Kristo, sawasawa na Baba, mbingu yote ilitoa utii.

Sheria ya upendo ikiwa ndiyo msingi wa serikali ya Mungu, furaha ya viumbe wote ilitegemea utii wao kamili kwa kanuni kuu zake za haki. Mungu hutamani kupata kwa viumbe Wake wote huduma ya upendo—heshima inayotokana na utambuzi wa kina wa tabia Yake. Hafurahishwi na utii wa shuruti, na kwa wote anatoa uhuru wa uchaguzi, kwamba wamtumikie kwa hiari.

Lakini kuna kiumbe mmoja aliyechagua kutumia vibaya uhuru huu. Dhambi ilitokana na yeye ambaye, akiwa wa pili baada ya Kristo, aliheshimiwa sana na Mungu na alikuwa juu sana katika nguvu na utukufu miongoni mwa wakazi wa mbinguni. Kabla ya kuanguka kwake, Lusifa alikuwa wa kwanza miongoni mwa makerubi wafunikao, akiwa mtakatifu na safi. "Bwana MUNGU asema hivi; Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri. Ulikuwa ndani ya Adeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako….Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto. Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako" (Ezekieli 28:12-15).

Kulikuwa na uwezekano wa Lusifa kudumisha fadhila aliyopewa na Mungu, akipendwa na kuheshimiwa na jeshi la malaika, akitumia uwezo wake mkubwa kuwabariki wengine na kumtukuza Muumbaji wake. Lakini, nabii anasema,"Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako" (Aya ya 17). Kidogo kidogo, Lusifa aliendekeza shauku ya kujiinua. "Kwa kuwa umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu." "Nawe ulisema, … Nitapanda mpaka mbinguni,

Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano….Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu" (Aya ya 6; Isaya 14:13, 14). Badala ya kutafuta kumfanya Mungu awe juu katika kupendwa na kuheshimiwa na viumbe Wake, Lusifa alielekeza nguvu zake kuwashawishi viumbe wa Mungu wamtumikie na kumheshimu yeye binafsi. Na akitamani heshima ambayo Baba wa milele alimpa Mwana Wake, huyu mkuu wa malaika alipigania kuchukua mamlaka ambayo yalikuwa ya Kristo peke Yake.

Mbingu yote ilifurahia kuakisi utukufu wa Muumbaji na kuimba sifa Zake. Na wakati Mungu alipoheshimiwa hivyo, hali ilikuwa ya amani na furaha. Lakini tabia hii ya kujiinua ya Lusifa iliharibu utangamano wa mbinguni. Huduma ya uinuaji wa nafsi, kinyume na mpango wa Mungu, iliamsha hisia za uovu katika akili za yule ambaye utukufu wa Mungu ulikuwa mwingi sana. Mabaraza ya mbinguni yalimbeleleza sana Lusifa. Mwana wa Mungu aliwasilisha mbele yake ukuu, wema, na haki ya Muumbaji, na asili takatifu, isiyobadilika ya sheria Yake. Mungu Mwenyewe aliweka utaratibu mbinguni; na kwa kuuvunja, Lusifa alimvunjia heshima Muumbaji wake, na alileta maangamizi juu yake mwenyewe. Lakini onyo, lililotolewa katika upendo na rehema zisizo na kikomo, liliamsha roho ya upinzani.

Lusifa aliruhusu wivu wake dhidi ya Kristo ushinde, na alidhamiria kuendeleza mapambano. Kiburi kilichotokana na utukufu wake kilipalilia hamu yake ya ukubwa.

Heshima kubwa aliyopewa hakuichukulia kama karama kutoka kwa Mungu na haikumpa shauku ya kumshukuru Muumbaji wake. Alijitukuza kwa sababu ya mwangaza wake na cheo chake cha juu, na alipigania kuwa sawa na Mungu. Alipendwa na aliheshimiwa na jeshi la mbinguni. Malaika walifurahia kutekeleza amri zake, na alivikwa hekima na utukufu mwingi zaidi kuliko wengine wote. Lakini Mwana wa Mungu alitambuliwa kuwa Mtawala wa mbingu, akiwa mmoja na Baba katika nguvu na mamlaka. Katika mabaraza yote ya Mungu, Kristo alikuwa mshiriki, lakini Lusifa hakuruhusiwa kushiriki katika makusudi ya Kimungu kama Kristo alivyoruhusiwa. “Kwa nini,” malaika huyu mwenye nguvu nyingi alihoji, “Kristo awe mkubwa kiasi hicho? Kwa nini apewe heshima kubwa zaidi kuliko Lusifa?”

Akiondoka mahali pake ambapo palikuwa karibu sana na uwepo wa Mungu, Lusifa alikwenda kueneza roho ya kutoridhika miongoni mwa malaika. Akifanya kazi kwa siri iliyofichika sana, na kwa muda fulani akificha kusudi lake halisi chini ya mwonekano wa kicho kwa Mungu, alichochea roho ya kutoridhika kuhusiana na sheria zilizotawala wenye uhai wa mbinguni, akieleza kuwa ziliweka mipaka isiyokuwa ya lazima. Kwa kuwa asili zao zilikuwa takatifu, alidai kuwa malaika walipaswa kutii maagizo ya nia zao wenyewe. Alitafuta kujenga mazingira ya kuhurumiwa kwa kuwasilisha hoja kuwa Mungu hakumtendea haki kwa kumpa Kristo heshima kubwa kiasi kile. Alidai kuwa kwa kupigania madaraka makubwa zaidi hakuwa na kusudi la kujiinua, bali alitafuta uhuru kwa ajili ya wakazi wote wa mbinguni, na kwamba kwa njia hiyo wakazi wa mbinguni wangepata maisha yaliyo juu na bora zaidi.

Mungu katika rehema yake kuu alimvumilia Lusifa kwa muda mrefu. Lusifa hakushushwa kutoka nafasi yake ya juu alipoonesha kwa mara ya kwanza roho ya kutoridhika, wala hata alipoanza kuwasilisha madai yake ya uongo mbele ya malaika watiifu. Kwa muda mrefu alibakizwa mbinguni. Tena na tena alipewa fursa ya msamaha kwa sharti la kutubu na kujisalimisha. Juhudi ambazo upendo usio na mwisho na hekima isiyo na kikomo pekee ndiyo ingeweza kubuni zilifanywa kumsaidia aone kosa lake. Roho ya kutoridhika ilikuwa haijawahi kujulikana mbinguni kabla ya hapo. Lusifa mwenyewe mwanzoni hakuelewa kule alikokuwa akielekea; hakuelewa asili hasa ya hisia zake.

Lakini alipoona kuwa kutoridhika kwake hakuna msingi, Lusifa alishawishika kuwa alikuwa amekosea, kuwa madai ya Mungu yalikuwa ya haki, na kuwa ilimpasa ayakubali kama yalivyokubaliwa mbinguni kote. Ikiwa angefanya hivyo, angeweza kuokoa nafsi yake na kuwaokoa malaika wengi. Wakati huo alikuwa bado hajaondoa utii wake wote kwa Mungu. Ingawa alikuwa ameicha nafasi yake kama kerubi afunikaye, lakini ikiwa angekuwa tayari kurudi kwa Mungu, akiikubali hekima ya Mungu, na kuridhika kujaza nafasi aliyopangiwa katika mpango mkuu wa Mungu, angeweza kurudishwa katika ofisi yake.

Lakini kiburi kilimzuia kujisalimisha. Alishikilia msimamo wake na kutetea njia yake, alisimama kidete kuwa hakuwa na haja ya kutubu, na alijisalimisha kwa nafsi yake mwenyewe kikamilifu, na kujipanga kuingia katika pambano kuu, dhidi ya Mwumbaji wake.

Nguvu zote za akili yake yenye uwezo mkubwa zilielekezwa katika kazi ya udanganyifu, ili aungwe mkono na malaika waliokuwa chini ya usimamizi wake. Hata ukweli kuwa Kristo alimwonya na kumshauri ulipotoshwa ili kujenga hoja ya kuunga mkono mipango yake ya usaliti. Kwa wale ambao upendo wao wenye dhamana kwake ulishikamana naye kwa karibu, Shetani alieleza kuwa alihukumiwa kwa makosa, kuwa cheo chake hakikuheshimiwa, na kuwa uhuru wake uliminywa. Kutoka kuwakilisha vibaya maneno ya Kristo alianza kukwepa kusema ukweli na hatimaye alisema uongo moja kwa moja, akimtuhumu Mwana wa Mungu kuwa alikuwa na mpango wa kumdhalilisha mbele ya wakazi wa mbinguni. Alitafuta pia kuleta fitina kati yake na malaika watiifu.

Wote wale ambao hakufaulu kuwapotosha na kuwavuta upande wake aliwatuhumu kuwa walikuwa hawajali maslahi ya wenye uhai wa mbinguni. Kazi ambayo alikuwa akiifanya mwenyewe ndiyo aliyowatuhumu kufanywa na wale waliobaki wakiwa waaminifu kwa Mungu. Na ili kuthibitisha mashitaka yake dhidi ya dhuluma za Mungu dhidi yake, aliwakilisha vibaya maneno na matendo ya Muumbaji. Ilikuwa sera yake kuwatatanisha malaika kwa hoja zake zenye hila kuhusu makusudi ya Mungu. Kila kitu ambacho kilikuwa rahisi alikivika joho la usiri, na upotoshaji uliorembwa vizuri alitia mashaka juu ya maneno ya wazi ya Yehova. Nafasi yake ya juu, akiwa karibu kabisa na utawala wa Kimungu, ilichangia nguvu nyingi zaidi katika upotoshaji wake, na wengi waliungana naye katika uasi dhidi ya mamlaka ya Mbinguni.

Mungu katika hekima Yake alimruhusu Shetani aendelee na kazi yake, mpaka roho ya kutoridhika ilipokomaa na kuwa uasi kamili. Ilikuwa muhimu mipango yake iendelezwe hadi ikomae kikamilifu, ili asili yake na mwelekeo wake halisi vidhihirike mbele ya wote. Lusifa, kama kerubi aliyepakwa mafuta, alikuwa na hadhi ya juu sana; alipendwa sana na wenye uhai wa mbinguni, na mvuto wake kwao ulikuwa mkubwa. Serikali ya Mungu ilijumuisha siyo tu wakazi wa mbinguni, bali pia wakazi wa sayari zingine zilizoumbwa na Mungu; na Shetani alifikiri kuwa ikiwa angefanikiwa kuwabeba malaika wote wa mbinguni katika uasi wake, angefaulu kubeba hata sayari zingine. Alikuwa amewasilisha upande wake wa mgogoro kwa ujanja sana, akitumia hila na ulaghai kutimiza makusudi yake. Nguvu yake ya kudanganya ilikuwa kubwa, na kwa kujifunika katika koti la uongo alifanikiwa. Hata malaika watiifu hawakutambua tabia yake wala kuona kile ambacho kingekuwa matokeo ya kazi yake.

Shetani alikuwa akiheshimiwa sana, na matendo yake yote yalifunikwa na usiri mkubwa, kiasi ambacho ilikuwa vigumu kuwafunulia malaika asili halisi ya kazi yake. Bila kukomaa kikamilifu, dhambi isingeonekana kuwa ni jambo baya. Mpaka wakati huo dhambi haikuwepo katika ulimwengu wa Mungu, na wenye uhai watakatifu hawakujua asili yake na

ubaya wake. Hawakujua matokeo ya kutisha ambayo yangefuata baada ya kuiweka kando sheria ya Mungu. Shetani, kwa mara ya kwanza, aliificha kazi yake chini ya madai maalumu ya utii kwa Mungu. Alidai alikuwa akitafuta kuhamasisha heshima kwa Mungu, uimara wa serikali Yake, na ustawi wa wakazi wa mbinguni. Wakati akipenyeza kutoridhika katika mawazo ya malaika walioko chini yake, kwa hila alifanya ionekane kana kwamba alikuwa akitaka kuondoa kutoridhika. Wakati akidai kuwa mabadiliko yafanywe katika utaratibu na sheria za serikali ya Mungu, alidai kuwa mabadiliko haya yalikuwa muhimu ili kudumisha utangamano mbinguni.

Katika kushughulika na dhambi, Mungu alitumia haki na kweli tu. Shetani alitumia kile ambacho Mungu hawezi kutumia—udanganyifu na uongo. Alitafuta kubadilisha ukweli wa neno la Mungu uonekane uongo na aliwasilisha vibaya mpango wa serikali Yake mbele ya malaika, akidai kuwa Mungu hakuwa na haki ya kuweka sheria na kanuni za kuwaongoza wakazi wa mbinguni; kwamba katika kuwataka viumbe Wake wajisalimishe Kwake na kumtii Yeye, Mungu alikuwa akitafuta kujiinua tu. Kwa hiyo ilipasa idhihirike mbele ya wakazi wote wa mbinguni, na mbele ya sayari zote, kuwa serikali ya Mungu ilikuwa ya haki, sheria Yake ilikuwa kamili. Shetani alitengeneza mazingira yaliyoonesha kana kwamba yeye mwenyewe alikuwa akipambania usitawi wa Ulimwengu wote. Tabia halisi ya Ibilisi, na lengo lake halisi, ilikuwa lazima vieleweke kwa wote. Ilipasa apewe muda ili ajifunue mwenyewe kwa kazi zake ovu.

Uhasama uliokuwa umesababishwa na matendo yake mwenyewe huko mbinguni, Shetani alidai kuwa ulisababishwa na sheria na serikali ya Mungu. Alitangaza kuwa maovu yote yalikuwa matokeo ya utawala wa Mungu. Alidai kuwa ilikuwa kusudi lake kuboresha sheria za Yehova. Kwa hiyo ilikuwa muhimu apewe nafasi aoneshe asili ya madai yake, na aoneshe utendaji wa mabadiliko aliyoyapendekeza katika sheria takatifu. Ilipasa kazi yake yenyewe imhukumu. Shetani alidai tangu mwanzo kuwa hakuwa anafanya uasi. Ilipasa ulimwengu wote umwone mwongo akiwa amefunuliwa wazi.

Hata baada ya kuamriwa kuwa asingeweza kuendelea kubaki mbinguni, Hekima Isiyo na Kikomo haikumwangamiza Shetani. Kwa kuwa huduma ya upendo ndiyo pekee inayokubalika kwa Mungu, utii wa viumbe Wake inapasa ujengwe juu ya kushawishika kwao kuwa Mungu ni mwenye haki na mwenye ukarimu. Wakazi wa mbinguni na wa sayari zingine, kwa kutokujiandaa kuelewa asili na athari za dhambi, wasingeona haki na rehema za Mungu katika kumwangamiza Shetani. Ikiwa angeangamizwa asiwepo kabisa mara moja, wangemtumikia Mungu kwa hofu kuliko kwa upendo. Mvuto wa mdanganyaji usingeangamizwa kabisa, wala roho ya uasi isingeondolewa kabisa. Ilipasa uovu uruhusiwe ukomae kabisa. Kwa manufaa ya ulimwengu wote katika vizazi vyote, Shetani alipaswa kuendeleza kanuni zake kikamilifu, ili shutuma zake dhidi ya serikali ya Mungu zionekane katika nuru yake halisi kwa wenye uhai wote walioumbwa, ili haki na rehema za Mungu na kutobadilika kwa sheria Yake visihojiwe milele zote.

Uasi wa Shetani ulipaswa uwe fundisho kwa ulimwengu wote katika zama zote zijazo, ushuhuda wa kudumu wa asili na athari za kutisha za dhambi. Utendaji kazi wa utawala wa Shetani, madhara yake kwa wanadamu na malaika, vingeonesha kile ambacho lazima kiwe tunda la kukiuka mamlaka ya Mungu. Utendaji kazi wa Shetani ungeshuhudia kuwa uwepo wa serikali ya Mungu na sheria Yake umeambatana na ustawi wa viumbe wote aliowaumba. Kwa hiyo, historia ya jaribio hili la uasi, litakuwa ulinzi wa daima kwa wote wenye akili, kuwazuia wasidanganywe kuhusiana na asili ya uasi, na kuwaepusha na dhambi na mateso ya adhabu zake.

Karibu kabisa na mwisho wa pambano mbinguni, mdanganyaji mkuu aliendelea kujihesabia haki. Ilipotangazwa kuwa yeye pamoja wafuasi wake ilipasa wafukuzwe na watoke katika makao ya mbinguni, ndipo kiongozi wa uasi aliapa kwa ujasiri kuidharau sheria ya Muumbaji. Alirudia dai lake kuwa malaika hawakuhitaji kutawaliwa, bali ilipasa waachiwe wafuate mapenzi yao wenyewe, ambayo yangeweza kuwaongoza kwa usahihi. Alizishutumu amri za Mungu kuwa ni kizuizi dhidi ya uhuru wao na alitangaza kuwa ilikuwa kusudi lake kuhakikisha kuwa anafutilia mbali sheria; kuwa, wakiondolewa kizuizi hiki, majeshi ya mbinguni yataweza kuingia katika hali ya juu, ya utukufu zaidi ya maisha.

Kwa nia moja, Shetani na jeshi lake walirusha lawama za uasi wao wote kwa Kristo, wakidai kuwa ikiwa wasingekemewa, wasingeasi hata kidogo. Pamoja na ugumu wa mioyo na ujeuri katika uasi wao, wakitafuta bila mafanikio kupindua serikali ya Mungu, lakini wakidai kwa kufuru kuwa wao ni wahanga wasiokuwa na hatia wa mamlaka kandamizi, mwasi mkuu na wafuasi wake wote hatimaye walifukuzwa mbinguni.

Roho ile ile iliyoanzisha uasi mbinguni bado inachochea uasi duniani. Shetani akiwa na wanadamu anaendeleza sera ileile aliyotumia akiwa na malaika. Roho yake sasa inatawala ndani ya watoto wa uasi. Kama yeye, wanatafuta kuvunja vizuizi vya sheria ya Mungu na wanawaahidi watu uhuru kwa njia ya kukiuka kanuni zake. Kukemea dhambi kunaamsha roho ya chuki na upinzani. Wakati ujumbe wa Mungu wa onyo unapoletwa nyumbani katika dhamiri, Shetani anawaongoza kujihesabia haki na kutafuta huruma za watu katika njia yao ya dhambi. Badala ya kusahihisha makosa yao, wanaamsha hasira dhidi ya yule anayewakemea, kana kwamba yeye pekee ndiye chanzo cha tatizo. Tangu siku za Habili mwenye haki hadi wakati wetu roho hiyo imeoneshwa kwa wale wanaothubutu kukemea dhambi.

Kwa kuwakilisha vibaya kama huko kwa tabia ya Mungu kama alivyofanya mbinguni, akisababisha Mungu aonekane kuwa ni mkali na katili, Shetani alishawishi wanadamu kutenda dhambi. Na baada ya kufaulu katika hilo, alitangaza kuwa vizuizi vya Mungu visivyokuwa vya haki vimesababisha wanadamu kuanguka, kama vilivyosababisha uasi wake mwenyewe mbinguni.

Lakini Yule Ambaye Anaishi Milele anatangaza tabia Yake: “Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe” (Kutoka 34:6, 7).

Katika kufukuzwa kwa Shetani kutoka mbinguni, Mungu alitangaza haki Yake na alidumisha heshima ya kiti Chake cha enzi. Lakini wakati mwanadamu alipotenda dhambi kwa kusikiliza uongo wa hii roho iliyoasi, Mungu alitoa ushahidi wa upendo Wake kwa kumtoa Mwana Wake wa pekee afe kwa ajili ya wanadamu walioanguka dhambini. Katika upatanisho tabia ya Mungu ilifunuliwa. Hoja ya nguvu ya msalaba huonesha kwa sayari zote kuwa ile njia ya dhambi ambayo Lusifa aliichagua kwa namna yoyote ile haikutokana na serikali ya Mungu.

Katika shindano kati ya Kristo na Shetani, wakati wa huduma ya Mwokozi duniani, tabia ya mdanganyaji mkuu iliwekwa wazi. Hakuna jambo lo lote lile lingeweza kumng’oa Shetani na kumtoa katika mioyo ya malaika wa mbinguni na ya wakazi watiifu wa sayari zote kwa ufanisi kama pambano lake la kikatili dhidi ya Mkombozi wa ulimwengu. Kufuru yake ya kijasiri ya kumtaka Kristo amsujudie, ujasiri wake wa kiburi wa kumchukua hadi juu ya kilele cha mlima na mnara wa hekalu, kusudi lake lenye nia mbaya lililonekana wakati akimwagiza ajitupe chini kutoka katika kilele chenye kutia kizunguzungu, ubaya usiosinzia uliomwinda Kristo kila mahali alipokwenda, ukivuvia mioyo ya makuhani na watu kuukataa upendo Wake, na hatimaye wakapiga kelele, “Asulubiwe! Asulubiwe!”—yote haya yaliamsha mshangao na hasira ya Kimungu ya sayari zote.

Shetani ndiye aliyeuchochea ulimwengu umkatae Kristo. Mkuu wa uovu alitumia nguvu na hila zake zote kumwangamiza Yesu; kwani aliona kuwa rehema na upendo wa Mwokozi, huruma Yake na uvumilivu Wake usiochoka, viliwakilisha kwa ulimwengu tabia ya Mungu. Shetani alipinga kila dai lililotolewa na Mwana wa Mungu na alitumia watu kama mawakala wake kujaza maisha ya Mwokozi kwa mateso na huzuni. Ulaghai na uongo aliotumia kuzuia kazi ya Yesu, chuki aliyoionesha kwa njia ya wana wa uasi, ukatili wake dhidi Yake Yeye ambaye maisha Yake yalijaa wema usiokuwa na mfano, yote yalitokana na ulipizaji kisasi wenye mizizi mirefu. Mioyo iliyominywa ya kijicho na ubaya, chuki na kulipiza kisasi, vilipasukia Kalwari dhidi ya Mwana wa Mungu, wakati mbingu yote ikitazama kwa ukimya wenye hofu kuu na mshangao.

Wakati kafara kuu ilipokamilishwa, Kristo alipaa juu, akikataa kutukuzwa na malaika mpaka awasilishe ombi hili: “Hao ulionipa nataka wawe pamoja nami po pote nilipo” (Yohana 17:24). Ndipo kwa upendo na nguvu zisizoelezeka jibu lilitoka katika kiti cha enzi cha Baba: “Na wamsujudu malaika wote wa Mungu” (Waebrania 1:6). Hakuna doa lililokuwa juu ya Yesu. Kudhalilishwa kuliisha, kafara Yake ilikamilika, na alipewa jina lipitalo majina yote.

Sasa hatia ya Shetani ilionekana wazi bila udhuru. Alidhihirisha tabia yake ya kweli kuwa yeye ni mwongo na muuaji. Ilionekana kuwa roho ile ile ambayo kwayo aliwatawala wanadamu, ambao walikuwa chini ya mamlaka yake, ndiyo ambayo angeitumia ikiwa angeruhusiwa kuwatawala wakazi wa mbinguni. Alidai kuwa kukiuka sheria ya Mungu kungeleta uhuru na kuinuliwa juu; lakini ilionekana kuwa kulileta utumwa na kushushwa chini. Mashitaka ya uongo ya Shetani dhidi ya tabia na serikali ya Mungu yalionekana katika nuru yake ya kweli.

Alikuwa amemshitaki Mungu kuwa alikuwa akitafuta kujiinua Mwenyewe tu kwa kuwataka viumbe Wake wajisalimishe Kwake na kumtii Yeye, na alikuwa ametangaza kuwa, wakati Muumbaji alidai wengine wote wajikane nafsi, Yeye Mwenyewe hakujikana nafsi na hakutoa kafara yoyote. Sasa ilikuwa imedhihirika kuwa kwa ajili ya wokovu wa jamii iliyoanguka na kutenda dhambi, Mtawala wa sayari zote alitoa kafara kubwa kuliko zote ambazo upendo ungeweza kutoa; kwa kuwa "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake" (2 Wakorintho 5:19). Ilionekana, pia, kuwa wakati Lusifa alifungua mlango na dhambi kwa sababu ya tamaa yake ya heshima na ukuu, Kristo, ili kuangamiza dhambi, alijinyenyekesha na akawa mtii hadi mauti.

Mungu alionesha chuki Yake dhidi ya kanuni za uasi. Mbingu yote iliona haki Yake ikiwa imefunuliwa, katika hukumu ya Shetani na katika ukombozi wa mwanadamu. Lusifa alikuwa ametangaza kuwa ikiwa sheria ya Mungu haibadiliki, na adhabu yake isingeondolewa, na mkosaji lazima asingekubaliwa na Mwumbaji tena. Alikuwa amedai kuwa jamii ya wanadamu waliotenda dhambi walikuwa nje ya wigo wa ukombozi na hivyo basi walikuwa mawindo yake halali. Lakini kifo cha Kristo kilikuwa hoja kwa ajili ya mwanadamu ambayo isingeshindwa. Adhabu ya sheria ilianguka juu Yake Yeye aliyekuwa sawa na Mungu, na mwanadamu walipewa uhuru wa kupokea haki ya Kristo na kwa maisha ya toba na unyenyekevu aweze kushinda, kama Mwana wa Mungu alivyoshinda, juu ya nguvu ya Shetani. Hivyo Mungu ni Mwenye haki na Mhesabiaji wa haki wa wale wote wanaomwamini.

Lakini haikuwa kwa ajili ya utekelezaji wa ukombozi wa mwanadamu tu Kristo alikuja duniani kuteseka na kufa. Alikuja "kuitukuza sheria" na "kuiadhimisha" (Isaya 42:21). Siyo wakazi wa sayari hii pekee ambao walipaswa kuichukulia sheria kama ilivyopaswa kuchukuliwa; bali ilikuwa kwa ajili ya kuonesha kwa wakazi wa sayari zote kuwa sheria ya Mungu haibadiliki. Ikiwa madai yake yangeweza kuwekwa pembeni, basi Mwana wa Mungu asingelazimika kupoteza uhai Wake kwa ajili ya upatanisho wa dhambi. Kifo cha Kristo huthibitisha kuwa haibadiliki. Na kafara ambayo upendo usio na kikomo ulilazimisha Baba na Mwana kuitoa, ili wenye dhambi waweze kukombolewa, huonesha kwa sayari zote—hakuna kitu chochote chini ya mpango huu wa upatanisho kingeweza kukidhi upatanisho—kwamba haki na rehema ni msingi wa sheria ya serikali ya Mungu.

Katika utekelezaji wa mwisho wa hukumu itakuja kuonekana kuwa hakuna sababu yo yote ya kuwepo kwa dhambi. Wakati Jaji Mkuu wa dunia yote atakapomwuliza Shetani, “Kwa nini uliniasi, na kuninyang’anya raia wa ufalme Wangu?” Mwasisi wa uovu hawezi kutoa udhuru wo wote. Kila mdomo utafumbwa, na majeshi yote walioasi watakaa kimya.

Msalaba wa Kalvari, wakati ukitangaza kuwa sheria haibadiliki, unahubiri ulimwenguni kuwa mshahara wa dhambi ni mauti. Katika kilio cha kukata roho cha Mwokozi, “Imekwisha,” kengele ya kifo cha Shetani ilipigwa.

Pambano kuu ambalo limedumu kuwepo kwa muda mrefu liliamriwa hapo, na uondoshwaji wa mwisho wa dhambi ulithibitishwa. Mwana wa Mungu alipita katika milango ya kaburi, ili “kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi” (Waebrania 2:14). Shauku ya Lusifa ya kujiinua ilimfikisha mahali ambapo aliweza kusema: “Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; … Nitafanana na yeye Aliye juu.” Mungu anatangaza: “Nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, … wala hutakuwapo tena” (Isaya 14:13, 14; Ezekieli 28:18, 19). Wakati siku ile itapofika, ikiwaka kama tanuru, “wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi” (Malaki 4:1).

Ulimwengu wote utakuwa mashahidi wa asili na athari za dhambi. Na uondoshwaji wake kamili, ambao mwanzoni ungeleta hofu na dharau kwa Mungu, sasa utathibitisha upendo Wake na utaimarisha heshima Yake mbele ya ulimwengu wa wenye uhai wanaofurahia kutenda mapenzi Yake, na ambao mioyoni mwao wanayo sheria Yake. Kamwe uovu hautaonekana tena. Neno la Mungu linasema: “Mateso hayatainuka mara ya pili” (Nahumu 1:9). Sheria ya Mungu, ambayo Shetani aliikashifu kama kongwa la utumwa, itaheshimiwa kama sheria ya uhuru. Uumbaji uliojaribiwa na kuthibitishwa hautayumbishwa tena katika utii wake Kwake Yeye ambaye tabia Yake imedhihirishwa kwa uwazi mbele yao kama upendo usio kifani na hekima isiyo na kikomo.

Sura ya 30 - Uadui wa Kuzimu

"Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino" (Mwanzo 3:15). Hukumu ya Mungu dhidi ya Shetani baada ya anguko la mwanadamu ilikuwa pia unabii, ukijumuisha zama zote hadi wakati wa mwisho na ukiashiria kuwa pambano kuu litahusisha kabila zote za watu watakaoishi duniani.

Mungu anatangaza: "Nami nitaweka uadui." Uadui huu hautokei kwa asili moja kwa moja. Mwanadamu alipovunja sheria ya Mungu, asili yake ilibadilika na kuwa ya uovu, na alikuwa na upatanifu, na siyo tofauti, na Shetani. Hakuna uadui wa asili kati ya mwanadamu mwenye dhambi na mwasisi wa dhambi. Wote ni waovu kwa sababu ya uasi. Mwasi hatulii, mpaka apate huruma na kuungwa mkono kwa kuwashawishi wengine wafuate mfano wake. Kwa sababu hiyo malaika walioanguka na watu waovu huungana katika urafiki wa kutapatapa. Ikiwa Mungu asingeingilia, Shetani na mwanadamu wangeungana na kuunda umoja dhidi ya Mbingu; na badala ya kujenga uadui dhidi ya Shetani, familia nzima ya mwanadamu ingejiunga dhidi ya Mungu.

Shetani alimjaribu mwanadamu kutenda dhambi, kama alivyosababisha malaika kuasi, ili aweze kupata ushirikiano wao katika vita yake dhidi ya Mbingu. Kulikuwa hakuna mgawanyiko kati yake na malaika walioanguka katika suala la chuki dhidi ya Krito; wakati katika mambo mengine yote kulikuwa na uhasama miongoni mwao, waliungana kikamilifu katika kupinga mamlaka ya Mtawala wa Ulimwengu. Lakini Shetani aliposikia tangazo kuwa uadui unapaswa kuwepo kati yake na mwanamke, na kati ya uzao wake na uzao wa mwanamke, alitambua kuwa juhudi zake za kuharibu asili ya mwanadamu zingeingiliwa; kuwa kwa namna fulani mwanadamu angewezeshwa kupinga nguvu zake.

Uadui wa Shetani dhidi ya uzao wa mwanadamu unawashwa moto kwa sababu, kwa njia ya Kristo, wanapata fursa ya kupokea upendo na rehema za Mungu. Shetani anatamani kukwamisha mpango wa Mungu wa ukombozi wa mwanadamu, kumkosesha Mungu heshima, kwa kufuta na kuharibu kazi ya mikono Yake; anatamani kuleta huzuni mbinguni na kuijaza dunia kwa huzuni na ukiwa. Na anaonesha mabaya yote haya kama matokeo ya kazi ya Mungu katika kumuumba mwanadamu.

Ni neema anayoweka Kristo katika roho ambayo huleta uadui ndani ya mtu dhidi ya Shetani. Bila neema hii inayobadilisha na nguvu inayoumba upya, mwanadamu angeendelea kuwa mateka wa Shetani, mtumishi aliye tayari daima kutii maagizo ya Shetani. Lakini kanuni mpya katika roho inaumba mgogoro mahali palipokuwa na amani. Nguvu ambayo Kristo anaitoa inamwezesha mwanadamu kumpinga dhalimu na mnyang'anyi. Ye yote anayeonekana kuichukia dhambi badala ya kuipenda, ye yote anayezipinga na kuzishinda

tamaa ambazo zimekuwa zikitawala ndani yake, anaonesha utendaji kazi wa kanuni inayotoka mbinguni.

Upinzani uliopo kati ya roho ya Kristo na roho ya Shetani ulionekana kwa uwazi zaidi katika namna ulimwengu ulivyompokea Yesu. Sababu kubwa ya Wayahudi kumkataa Yesu haikuwa mwonekano Wake wa kutokuwa na mali za dunia, kutokuwa na ufahari, au kutokuwa na utukufu. Waliona kuwa alikuwa na nguvu ambayo ilikuwa muhimu zaidi kuliko hata hayo mambo ya kidunia. Lakini usafi na utakatifu wa Kristo ulisababisha chuki dhidi yake kutoka kwa watu wasiomcha Mungu. Maisha yake ya kujikana nafsi na uaminifu usiokuwa na dhambi ulikuwa kemeo la daima dhidi ya watu wenye kiburi na tamaa. Jambo hili ndilo liliwasha moto wa uadui dhidi ya Mwana wa Mungu. Shetani na malaika waovu waliungana na watu waovu. Nguvu zote za uasi ziliungana dhidi ya Jemadari wa ukweli.

Uadui huo huo unaoneshwa dhidi ya wafuasi wa Kristo kama ulivyooneshwa dhidi ya Bwana wao. Ye yote anayeona ukakasi wa dhambi, kwa nguvu itokayo mbinguni anapinga majaribu, kwa hakika atawasha moto wa ghadhabu wa Shetani na wa wafuasi wake. Chuki dhidi ya kanuni safi za ukweli, na shutuma na mateso dhidi ya watetezi wa ukweli, vitaendelea kuwepo kwa kadiri dhambi na wenye dhambi wanavyodumu kuwepo. Wafuasi wa Kristo na watumwa wa Shetani hawawezi kuafikiana. Kwazo la msalaba halijabatilika. “Wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa” (2 Timotheo 3:12).

Mawakala wa Shetani wanafanya kazi daima chini ya maelekezo yake kustawisha mamlaka yake na kujenga ufalme wake katika kupingana na serikali ya Mungu. Kwa ajili hii wanatafuta kuwadanganya wafuasi wa Kristo na kuwafanya waachane na utiifu wao kwa Kristo. Kama kiongozi wao alivyo, wanatafsiri vibaya na kupotosha Maandiko ili kutimiza lengo lao. Kama vile Shetani alivyomtupia lawama Mungu, kadhalika mawakala wa Shetani huwasingizia watu wa Mungu. Roho ile iliyomwua Yesu inawachochea waovu kuwaangamiza wafuasi Wake. Yote haya yalitabiriwa katika unabii ule wa kwanza: “Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake.” Na uadui huu utaendelea mpaka mwisho wa wakati.

Shetani hukusanya majeshi yake yote na kuingiza nguvu zake zote vitani. Kwa nini hakutani na upinzani mkubwa zaidi? Kwa nini askari wa Kristo wanasinzia na hawajali? Ni kwa sababu wana mshikamano mdogo sana na Kristo; ni kwa sababu hawana Roho Wake. Kwa hiyo dhambi haipingwi na haichukiwi, kama Bwana wao ilivyoipinga na alivyoichukia. Hawaikabili, kama Kristo alivyoikabili, kwa upinzani mkubwa na wa makusudi. Hawatambui uovu na ubaya wa dhambi, na ni vipofu wasioweza kuona tabia na nguvu ya mfalme wa giza. Kuna uadui mdogo sana dhidi ya Shetani na kazi zake, kwa sababu kuna ujinga mkubwa kuhusu nguvu yake na ubaya wake, na ukubwa wa vita yake dhidi ya Kristo na Kanisa Lake. Watu wengi wanadanganyika hapa. Hawajui kuwa adui yao ni generali mwenye nguvu nyingi anayetawala akili za malaika waovu, na kwamba kwa mipango kabambe na mikakati makini

anapigana vita dhidi ya Kristo ili kuzuia wokovu wa roho. Miongoni mwa wanaojiita Wakristo, na hata miongoni mwa wahudumu wa injili, mara chache utasikia Shetani akigusiwa, isipokuwa pengine kumtaja kwa dharura mimbarani. Wanashindwa kuona ushahidi wa utendaji wake na mafanikio yake endelevu; wanapuuza maonyo mengi dhidi ya hila zake; wanaonekana kutojali hata uwepo wake mwenyewe.

Wakati ambapo watu hawana ufahamu wa mbinu zake, adui huyu asiyelala usingizi anafuatilia nyendo zao kila wakati. Anapenyeza uwepo wake katika kila idara ya nyumbani, katika kila mtaa wa miji, katika makanisa, katika mabaraza ya kitaifa, katika mahakama, akileta mashaka, akidanganya, akishawishi, kila mahali akiharibu roho na miili ya wanaume, wanawake, na watoto, akivunja familia, akipanda mbegu za chuki, ushindani, ugomvi, uasi, na mauaji. Na ulimwengu wa Kikristo unaelekea kuchukulia mambo haya kana kwamba yamepangwa na Mungu na kuwa ni lazima yawepo.

Shetani anatafuta daima kuwashinda watu wa Mungu kwa kuvunja vizuizi ambavyo vinawatenga na ulimwengu. Waisraeli wa zamani walishawishiwa kutenda dhambi walipojiingiza katika mahusiano haramu na wapagani. Kwa jinsi ile ile wana Israeli wa leo wanapotoshwa. "Mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye Sura ya ke Mungu" (2 Wakorintho 4:4). Wote ambao siyo wafuasi wa Kristo wenye msimamo thabiti ni watumishi wa Shetani. Ndani ya moyo usioumbwa upya kuna kuipenda dhambi na tabia ya kuipalilia na kuitolea udhuru. Ndani ya moyo ulioumbwa upya kuna kuichukia dhambi na upinzani wa makusudi dhidi ya dhambi. Wakristo wanapochagua kushirikiana na watu wasiomcha na wasiomwamini Mungu, wanakaribisha majaribu wenyewe. Shetani anajificha ili asionekane na anawafunika macho yao wasione mitego ya hila zake. Hawawezi kuona kuwa urafiki kama huo umepangwa kuwaumiza; na huku kwa wakati wote huo wakiwa wanajenga tabia ya ulimwengu, katika maneno na matendo, wanazidi kuwa vipofu.

Kufuata desturi za ulimwengu kunaongoa kanisa na kulifanya liwe la ulimwengu; hakuwezi kuuongoa ulimwengu na kuuleta kwa Kristo. Kuzoeana na dhambi kwa muda mrefu hatimaye kunaifanya dhambi ionekane kana kwamba haina madhara. Yeyote anayechagua kujichanganya na watumwa wa Shetani si muda mrefu ataacha kumwogopa bwana wao. Ikiwa katika utekelezaji wa majukumu yetu tunakutana na majaribu, kama Danieli alivyokutana nayo katika nyumba ya mfalme, tunaweza kuwa na hakika kuwa Mungu atatulinda; lakini ikiwa tunajiweka wenyewe chini ya majaribu tutaanguka chini punde.

Mjaribu anafanya kazi kwa mafanikio zaidi kupitia kwa wale ambao siyo rahisi kufikiria kuwa wako chini ya utawala wake. Watu wenye talanta na elimu wanavutia na kuheshimiwa, kana kwamba sifa hizi zinaweza kuchukua nafasi ya kicho cha Mungu au kuwastahilisha kupata fadhila ya Mungu. Talanta na ustaraabu, vikichukuliwa vyenyewe kama vilivyo, ni zawadi za Mungu; lakini zawadi hizi zikitumiwa kuziba nafasi ya utakatifu, wakati, badala ya

kuzileta roho karibu na Mungu, zinazipeleka roho mbali Naye, ndipo zinakuwa laana na mtego. Kuna wazo ambalo watu wengi wanalo kuwa cho chote kinachoonekana kuwa na Sura ya ukarimu au ustaarabu lazima, kwa namna fulani, kiwe upande wa Kristo. Hakuna kosa kubwa kama hilo. Sifa hizi zinapasa kuwa sehemu ya maisha ya kila Mkriso, kwa kuwa zinaleta mvuto mkubwa kwa ajili ya dini ya kweli; lakini inapasa zisalimishwe kikamilifu kwa Mungu, kinyume chake zinakuwa pia nguvu ya uovu. Watu wengi ambao wana akili iliyokuzwa na tabia inayovutia, ambao hawawezi kushiriki katika tendo lo lote lile linalojulikana kuwa ni tendo la kukosa uadilifu, ni vyombo vilivyonolewa katika mikono ya Shetani. Mvuto na mfano wake wa tabia iliyofichika, ya udanganyifu, unamfanya kuwa adui wa hatari zaidi kwa kazi ya Kristo kuliko wale ambao hawana elimu na hawana uzoefu mwingi.

Kwa maombi mengi na kumtegemea Mungu, Sulemani alipata hekima iliyoleta mshangao na mvuto mkubwa ulimwenguni. Lakini alipogeuka na kuacha Chimbuko la nguvu zake, akasonga mbele akijitegemea mwenyewe, aliangushwa na majaribu. Ndipo nguvu za ajabu zilizowekwa juu ya mwenye hekima huyu zilimfanya wakala mwenye ufanisi mkubwa wa adui wa roho. Shetani anapotafuta daima kuwapofusha akili zao wasiuone ukweli huu, inawapasa Wakristo wasisahau kamwe kuwa “kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho” (Waefeso 6:12). Onyo lililovuviwa linatoa sauti katika karne zote hadi wakati wetu: “Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze” (1 Peter 5:8). “Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani” (Waefeso 6:11).

Tangu nyakati za Adamu hadi wakati wetu, adui yetu mkubwa amekuwa akitumia nguvu yake kuonea kuangamiza. Kwa sasa anajiandaa kwa ajili ya kampeni ya mwisho dhidi ya kanisa. Wote wanaotafuta kumfuata Yesu wataingia katika migogoro dhidi ya adui huyu asiyechoka. Kwa kadiri Mkristo anavyokaribia zaidi kufanana na sura wa Mungu, ndivyo atakavyokuwa mlengwa mkubwa zaidi wa mashambulizi ya Shetani. Wote wanaojishughulisha na kazi ya Mungu, wakitafuta kufunua udanganyifu wa Ibilisi na kumwasilisha Kristo mbele ya watu, ataweza kujiunga katika ushuhuda wa Paulo, ambapo anaeleza juu ya kumtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote wa akili, kwa machozi na majaribu mengi.

Shetani alimshambulia Kristo kwa majaribu makali na yaliyojaa hila, lakini alishindwa katika kila pambano. Vita vile vilipiganwa kwa kwa ajili yetu; ushindi ule unatuwezesha tushinde. Kristo atatoa nguvu kwa wote wanaoitafuta. Hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kushindwa na Shetani bila ridhaa yake. Mjaribu hana mamlaka ya kutawala nia au kumlazimisha mtu atende dhambi. Anaweza kuudhi, lakini hawezi kuchafua. Anaweza kusababisha uchungu, lakini hawezi kusababisha uchafu. Ukweli kuwa Kristo ameshinda

unapaswa kuwahamasisha wafuasi Wake kuwa na ujasiri wa kupigana kiume vita dhidi ya dhambi na Shetani.

Sura ya 31 - Wakala wa Pepo

Mshikamano wa ulimwengu unaoonekana na usioonekana, huduma za malaika wa Mungu, na ya wakala wa pepo, umefunuliwa katika Maandiko, na umeshikamana na historia ya mwanadamu. Kuna mwelekeo unaokua wa kutokuamini katika uwepo wa pepo wachafu, wakati malaika watakatifu "watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu" (Waebrania 1:14) wanachukuliwa kama roho za watu waliokufa. Lakini Maandiko yanafundisha siyo tu juu ya uwepo wa malaika, wema na wabaya, bali pia huwasilisha uthibitisho usio na mashaka kuwa malaika hawa sio roho za watu waliokufa.

Kabla ya uumbaji wa mwanadamu, malaika walikuwepo; kwa kuwa wakati misingi ya dunia ilipowekwa, "nyota za asubuhi ziliimba pamoja, Na wana wote wa Mungu walipiga kelele kwa furaha" (Ayubu 38:7). Baada ya anguko la mwanadamu, malaika walitumwa kuulinda mti wa uzima, na hili lilitokea kabla mwanadamu hajafa. Malaika katika asili yao wako juu zaidi kuliko wanadamu, kwani mtunga zaburi anasema mwanadamu aliumbwa "akiwa mdogo punde kuliko malaika" (Zaburi 8:5).

Tumefahamishwa katika Maandiko kuhusu idadi, na nguvu, na utukufu, wa malaika, na mshikamano wao na serikali ya Mungu, na pia kuhusu uhusiano wao na kazi ya ukombozi. "Bwana ameweka kiti chake cha enzi mbinguni, Na ufalme wake unavitawala vitu vyote." Na nabii anasema, "Nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi." Mbele ya uwepo wa Mfalme wa wafalme wanahudumu—"malaika zake … hodari," "watumishi wake wafanyao mapenzi yake," "Wakiisikiliza sauti ya neno lake" (Zaburi 103:19- 21; Ufunuo 5:11). Kumi elfu mara kumi elfu na maelfu kwa maelfu, walikuwa wajumbe walioonwa na nabii Danieli. Mtume Paulo alitangaza kuwa wao ni "majeshi ya malaika elfu nyingi" (Danieli 7:10; Waebrania 12:22).

Kama wajumbe wa Mungu wanasafiri kama "kuonekana kwa kumulika kwa umeme," (Ezekieli 1:14), ndivyo ulivyo mng'ao wa utukufu wao, na ndivyo ilivyo kasi ya urukaji wao. Malaika aliyetokea kwenye kaburi la Mwokozi, Sura ya ke iliyokuwa "kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji," iliwafanya walinzi kutetemeka kwa hofu, na "wakawa kama wafu" (Mathayo 28:3, 4). Senakeribu, Mwashuri mwenye kiburi, alipomtukana na kumkufuru Mungu, na kutishia kuwaangamiza Israeli, "Ikawa usiku uo huo malaika wa Bwana alitoka, akakiingia kituo cha Waashuri, akawapiga watu mia na themanini na tano elfu." "Naye Bwana akatuma malaika aliyewakatilia mbali mashujaa wote, na majemadari, na maakida," wa jeshi la Senakeribu. "Basi akarudia nchi yake mwenye haya ya uso" (2 Wafalme 19:35; 2 Nyakati 32:21).

Malaika wanatumwa kwa ajili ya utume wa rehema kwa watoto wa Mungu. Kwa Ibrahimu, walikwenda wakiwa na ahadi ya baraka; kwenye malango ya Sodoma, walikwenda kumwokoa Lutu mwenye haki kutoka katika maangamizi ya moto; kwa Eliya, alipokuwa

karibu kufa kwa sababu ya uchovu na njaa katika jangwa, alimpelekea chakula; kwa Elisha, walikwenda wakiwa na magari na farasi wa moto wakauzunguka mji mdogo uliokuwa umezingirwa na adui zake; kwa Danieli, wakati akitafuta hekima ya Kimungu katika ikulu ya mfalme mpagani, au akiwa ameachwa aliwe na simba walikwenda kumwokoa; alikwenda kwa Petro, akikabiliwa na kifo katika gereza la Herode, na kumtoa gerezani; alikwenda kwa wafungwa pale Filipi; alikwenda kwa Paulo na wenzake katikati ya usiku wa dhoruba baharini; alitumwa kufungua akili ya Kornelio ili apokee injili; alimtuma Petro na ujumbe wa wokovu kwa mgeni Mmataifa—hivyo malaika watakatifu, katika zama zote, wamewahudumia watu wa Mungu.

Malaika mlinzi amepangwa kwa ajili ya kila mfuasi wa Kristo. Walinzi hawa wa mbinguni wanakinga wenye haki dhidi ya nguvu za yule mwovu. Shetani alilitambua hili aliposema: “Je! Huyo Ayubu yuamcha Bwana bure? Wewe hukumzingira kwa ukingo pande zote?” (Ayubu 1:9, 10). Wakala anayetumiwa na Mungu kuwalinda watu Wake ameelezwa katika maneno ya mtunga zaburi: “Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa” (Zaburi 34:7). Mwokozi alisema, akiongea juu ya wale wanaomwamini: “Angalieni msidharau mmojawapo wa wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu” (Mathayo 18:10). Malaika waliopangwa kuwahudumia watoto wa Mungu wakati wote wanakwenda mbele za Mungu.

Hivyo watu wa Mungu, kwa sababu ya kukabiliwa na nguvu ya udanganyifu na uovu usiokoma wa mfalme wa giza, na kwa sababu ya kukabiliwa na mapambano dhidi ya nguvu za uovu wakati wote, wamehakikishiwa ulinzi usiokoma wa malaika wa mbinguni. Wala uhakika hautolewi bila hitaji. Mungu amewapa watoto Wake ahadi ya neema na ulinzi, kwa sababu kuna mawakala wenye nguvu wa uovu wa kukabiliana nao—mawakala wengi, waliodhamiria, na wasiochoka, ambao ubaya na nguvu yake hakuna hata mtu mmoja anaweza kuwa salama kutokujua na kutokujali.

Pepo wabaya, mwanzoni waliumbwa wakiwa hawana na dhambi, wakiwa sawa na malaika watakatifu, ambao kwa sasa ni wajumbe wa Mungu, katika asili, nguvu, na utukufu. Lakini wakiwa wameanguka dhambini, wameungana pamoja ili kumvunjia heshima Mungu na kuwaangamiza wanadamu. Wakiwa wameungana na Shetani katika uasi wake, wakifukuzwa mbinguni pamoja naye, katika zama zote mfululizo, wameshirikiana naye katika vita yake dhidi ya mamlaka ya Mungu. Tumeambiwa katika Maandiko kuhusu shirikisho lao na serikali yao, kuhusu makundi yao mbalimbali, kuhusu akili na hila zao, na kuhusu mipango yao mibaya dhidi ya amani na furaha ya wanadamu.

Historia ya Agano la Kale hutaja mara chache uwepo wao na mawakala wao; lakini wakati Kristo alipokuwa duniani pepo wabaya walidhihirisha nguvu zao kwa namna iliyokuwa wazi zaidi. Kristo alikuwa ameingia katika mpango uliobuniwa kwa ajili ya

ukombozi wa mwanadamu, na Shetani alidhamiria kuonesha haki yake ya kuutawala ulimwengu. Alikuwa amefanikiwa kuanzisha ibada ya sanamu kila sehemu ya dunia isipokuwa katika nchi ya Palestina. Katika nchi pekee ambayo ilikuwa haijajisalimisha kikamilifu chini ya himaya ya mjaribu, Kristo alikuja kuwaangazia watu nuru ya mbinguni. Hapa, nguvu mbili hasimu zilidai ukuu. Yesu alikuwa akinyosha mikono Yake ya upendo, akiwaalika wote wanaotafuta msamaha na amani ndani Yake. Majeshi ya giza yaliona kuwa hayakuwa na utawala usio na ukomo, na yalielewa kuwa ikiwa utume wa Kristo ungefaulu, utawala wao ungekoma ndani ya muda mfupi. Shetani alikasirika kama simba aliyefungwa mnyororo na alionesha nguvu zake kwa ukali katika miili na roho za watu.

Ukweli kuwa watu walipagawa na pepo wachafu, umeelezwa wazi wazi katika Agano Jipya. Watu walioteswa hivyo hawakuwa wanaumwa ugonjwa uliotokana na sababu za kawaida. Kristo alikuwa na uelewa kamili wa kile alichokuwa akishughulika nacho, na alitambua uwepo wa moja kwa moja na wakala wa pepo.

Mfano wa wazi wa idadi, nguvu, na ubaya wao, na pia nguvu na rehema ya Kristo, umetolewa katika maelezo ya Maandiko juu ya watu waliopagawa na pepo katika nchi ya Wagerasi. Wale wendawazimu maskini, wakivunja kila kizuizi, wakigaragara na kujitupa huku na huku, wakitokwa povu mdomoni, wakionesha hasira, waliijaza hewa kwa kelele zao, wakiifanyia ukatili miili yao, na kuhatarisha wote waliowakaribia. Miili yao iliyokuwa ikivuja damu na iliyokuwa imeharibika; na akili zao zilizopotezwa mwelekeo, viliwasilisha kituko ambacho kilimfurahisha sana mfalme wa giza. Mmoja wa pepo waliopagaa wagonjwa wale alisema: “Jina langu ni Legioni, kwa kuwa tu wengi” (Marko 5:9). Katika jeshi la Kirumi, legioni inaundwa na watu kuanzia elfu tatu hadi elfu tano. Majeshi ya Shetani nayo pia yamepangwa katika makundi, na kundi moja ambalo hawa pepo walikuwa sehemu yake walikuwa siyo chini ya legioni moja.

Kwa amri ya Yesu pepo waliwaacha wahanga wao, wakiwaacha wamekaa kwa utulivu karibu na miguu ya Mwokozi, wakiwa katika hali ya kujitawala, wakiwa na akili timamu, na wapole. Lakini pepo waliruhusiwa kufagia kundi la nguruwe na kuwatosa baharini; na kwa wakazi wa Wagerasi hasara ya hawa nguruwe ilikuwa kubwa zaidi kuliko mibaraka ambayo Kristo alikuwa ameileta, na Mponyaji wa Kiungu alisihiwa aondoke. Hili lilikuwa matokeo ya mipango ya Shetani. Kwa kurushia lawama ya hasara yao kwa Yesu, alichochea hofu za kibinafsi za watu na aliwazuia wasisikilize maneno Yake. Daima Shetani huwashitaki Wakristo kama chimbuko la hasara, balaa, na mateso, badala ya kuruhusu shutuma ziende mahali pake—juu yake mwenyewe na mawakala wake.

Lakini makusudi ya Yesu hayakukwamishwa. Aliruhusu pepo waangamize nguruwe kama kemeo kwa wale Wayahudi waliofuga wanyama hawa najisi kwa ajili ya mapato. Ikiwa Kristo asingewazuia hawa pepo, wangewatosa baharini, siyo tu nguruwe, bali pia wafugaji na wamiliki wa nguruwe. Utunzaji wa wafugaji na wa wamiliki wa nguruwe ulitokana na

mamlaka Yake, ambayo ilitumiwa kwa ajili ya wokovu wao. Zaidi ya hapo, tukio hili liliruhusiwa ili wanafunzi washuhudie nguvu ya kikatili ya Shetani kwa wanadamu na wanyama. Mwokozi alitamani wafuasi Wake wamwelewe adui ambaye wangekabiliana naye, ili wasidanganywe na kushindwa na hila zake. Ilikuwa pia mapenzi Yake pia kuwa watu wa eneo lile wauone uwezo Wake wa kuvunja utumwa wa Shetani na kuwaachilia mateka wake. Na ingawa Yesu Mwenyewe aliondoka, watu ambao kwa njia ya miujiza walikuwa wameachiliwa, walibaki kutangaza rehema ya Mfadhili wao.

Matukio mengine yenye sura hiyo yamerekodiwa katika Maandiko. Binti wa mwanamke Myunani, Msirofoenike aliteswa sana na pepo, ambaye Yesu alimtoa kwa neno Lake (Marko 7:26-30). "Mtu mwenye pepo, kipofu, naye ni bubu" (Mathayo 12:22); kijana aliyekuwa na pepo bubu, ambaye mara nyingi "amemtupa katika moto, na katika maji, amwangamize" (Marko 9:17- 27); mtu ambaye, kwa kuteswa na "roho wa pepo mchafu" (Luka 4:33-36), alivuruga utulivu wa Sabato wa sinagogi Kapernaumu—wote waliponywa na Mwokozi mwenye huruma. Katika kila tukio, Kristo alizungumza na pepo kama nafsi yenye akili, akimwamru amtoke mhanga wake na asimtese tena. Waabudu wa Kapernaumu, baada ya kuona uwezo Wake mkuu, "Mshangao ukawashika wote, wakasemezana wakisema, Ni neno gani hili, maana awaamuru pepo wachafu kwa uwezo na nguvu, nao hutoka" (Luka 4:36).

Waliopagawa na pepo wanaoneshwa kuwa katika hali ya mateso makubwa; lakini kulikuwepo na tofauti katika matukio mengine ya kupagawa. Kwa ajili ya kupata nguvu zisizokuwa za kawaida baadhi ya watu walikaribisha nguvu ya pepo. Lakini hawa hawakuwa na mgogoro na pepo. Katika kundi hili walikuwemo wale waliokuwa na pepo la uaguzi,—Simoni Magus, Elima mchawi, na binti aliyemfuata Paulo na Sila kule Filipi.

Hakuna mtu aliye katika hatari zaidi ya mvuto wa pepo kuliko wale ambao, licha ya ushahidi maridhawa wa Maandiko, wanakana uwepo na wakala wa Shetani na malaika zake. Kwa kadiri tunavyokosa ufahamu wa hila zao, ndivyo wanavyopata faida kubwa ajabu; wengi wanafuata mapendekezo yao wakidhani kuwa wanafuata maagizo ya hekima zao. Hii ndiyo sababu, kwa kadiri tunavyokaribia mwisho wa wakati, wakati Shetani anapofanya kazi kwa nguvu kubwa zaidi ya kudanganya na kuangamiza, anaeneza kila mahali imani kuwa hayupo. Ni sera yake kujificha na kuficha mbinu anazotumia kufanya kazi yake. Hakuna kitu mdanganyaji mkuu anachoogopa zaidi kuliko sisi kujua mbinu zake. Ili kuficha tabia na makusudi yake halisi, amejifanya mwenyewe awasilishwe kwa namna ambayo inawafanya watu wamdhihaki na kumdharau. Anafurahi sana anapochorwa akiwa na umbo la kuchekesha au kuchukiza, lisilo la kawaida, nusu mnyama nusu mwanadamu. Anafurahi sana anaposikia jina lake lilikitumiwa katika michezo na dhihaka na wale wanaofikiri kuwa wao ni wenye akili nyingi na wasomi.

Ni kwa sababu amejifunika kwa barakoa ya udanganyifu wa stadi za juu sana swali linaulizwa kila mahali: "Kiumbe wa aina hii yupo kweli?" Ushahidi wa mafanikio yake ni

nadharia za uongo zilizo kinyume na ushahidi wa wazi wa Maandiko zinavyopokelewa na watu wengi katika ulimwengu wa kidini. Na ni kwa sababu Shetani anaweza kutawala kwa urahisi zaidi akili za wale ambao hawana habari za nguvu zake, neno la Mungu linatupatia mifano mingi ya kazi yake mbaya, likitufunulia nguvu zake za siri, na hivyo kutupatia tahadhari dhidi ya mashambulizi yake.

Nguvu na ubaya wa Shetani na jeshi lake hutuweka katika hali ya tahadhari kwa haki kabisa ili tutafute hifadhi na wokovu katika nguvu kubwa zaidi ya Mwokozi wetu. Sisi tunafunga nyumba zetu kwa komeo na kufuli kulinda mali zetu na maisha yetu dhidi ya watu wabaya; lakini ni mara chache sana tunafikiria juu ya malaika waovu wanatutafuta daima, na ambao mashambulizi yao, katika nguvu zetu sisi wenyewe, hatuna mbinu ya kujilinda dhidi yake. Wakiruhusiwa, wanaweza kupotosha akili zetu, kuharibu na kutesa miili yetu, wanaweza kuharibu mali zetu na kuangamiza maisha yetu. Furaha yao pekee ni taabu na maangamizi. Hali ya kuogofya inawakabili wanaopinga madai ya Mungu na kujisalimisha kwa majaribu ya Shetani, mpaka Mungu anawaachia kwa utawala wa pepo. Lakini wale wanaomfuta Kristo daima wako salama chini ya ulinzi Wake. Malaika wenye nguvu nyingi wanatumwa kutoka mbinguni kuwalinda. Shetani hawezi kupenya ulinzi ambao Mungu amewazungushia watu Wake.

Sura ya 32 - Mitego ya Shetani

Pambano kuu kati ya Kristo na Shetani, ambalo limekuwa likipiganwa kwa takribani miaka elfu sita, linakaribia kufungwa; na Shetani anaongeza juhudi mara mbili kuishinda kazi ya Kristo kwa niaba ya mwanadamu na kushikilia roho katika mitego yake. Kuwashikilia watu gizani na katika hali ya kutotubu hadi upatanisho wa Mwokozi uishe, na kusiwepo tena kafara kwa ajili ya dhambi, ndiyo lengo analotafuta kulifikia.

Kunapokuwa hakuna juhudi maalumu zinazofanywa kupinga mamlaka yake, kutojali kunaposhamiri katika makanisa na katika ulimwengu, Shetani hana wasiwasi; kwa kuwa hayuko katika hatari ya kupoteza wale ambao anawashikilia mateka kama apendavyo. Tahadhari inapotolewa ili kujali mambo ya umilele, na roho zinapouliza, “Nifanye nini nipate kuokoka?” anakaa chonjo, akitafuta kupambana dhidi ya nguvu ya Kristo na kupinga mvuto wa Roho Mtakatifu.

Maandiko yanaeleza kuwa wakati mmoja, malaika wa Mungu walipokuja kujihudhurisha mbele za Bwana, Shetani naye alikuja miongoni mwao (Ayubu 1:6), siyo kusujudu mbele ya Mfalme wa Milele, bali kutafuta fursa ya kutimiza mipango yake mibaya dhidi ya wenye haki. Kwa lengo hilo hilo, anakuwepo katikati ya watu wanapokusanyika kumwabudu Mungu. Ingawa anajificha asionekane kwa macho, anafanya kazi kwa bidii zake zote kutawala akili za watu wanaokuja kuabudu. Kama jenerali mwenye ujuzi anapanga mipango yake mapema. Anapoona mjumbe wa Mungu akichunguza Maandiko, analiona somo litakalohubiriwa kwa watu. Ndipo anatumia hila zake zote na akili zake zote kwa kutawala mazingira ili ujumbe usiwafikie wale ambao anawadanganya kuhusiana na kipengele hicho kinachoandaliwa. Yule ambaye anahitaji sana onyo hilo anaingizwa katika miamala ya shughuli zingine zinazohitaji uwepo wake, au kwa njia nyingine atazuiwa asisikie maneno ambayo yangekuwa chumvi ya uzima kwa ajili ya uzima.

Kwa mara nyingine tena, Shetani anawaona watumishi wa Bwana wakiwa na mzigo kwa sababu ya giza la kiroho linalowafunika watu. Anasikia maombi ya dhati kwa ajili ya neema na nguvu ya Kiungu ivunje laana ya kutojali, uzembe, na uvivu. Ndipo kwa juhudi mpya anatumia werevu wake. Anawajaribu watu waendekeze uchu wa chakula au aina nyingine ya anasa, na kwa njia hiyo anatia ganzi fahamu zao washindwe kusikiliza mambo ambayo walihitaji sana kuyasikia.

Pamoja na hayo, Shetani anajua sana kuwa wale ambao anaweza kuwaongoza wapuuze maombi na wasijali kuchunguza Maandiko, wataangushwa na mashambulizi yake. Hivyo anatengeneza kila nyenzo inayowezekana kufunga kila akili. Kumekuwepo daima kundi la watu wanaodai kuwa wataua, ambao, badala ya kufuatilia ili kuujua ukweli, hufanya dini yao kuwa utafutaji makosa katika tabia au dosari katika imani ya wale wasiokubaliana nao. Watu hao ni wasaidizi wa mkono wa kulia wa Shetani. Washitaki wa ndugu sio wachache, na daima

wanajishughulisha Mungu anapokuwa kazini na watumishi Wake wanapomwabudu Mungu kwa kicho cha kweli. Wataweka rangi ya uongo katika maneno na matendo ya wale wanaoipenda na kuitii kweli. Watawakilisha watumishi wa Kristo wenye moyo wa dhati wenye bidii, wanaojikana nafsi kama watu waliodanganywa au wadanganyaji. Ni kazi yao kuwakilisha vibaya nia ya kila tendo la kweli na zuri, kueneza maneno yasiyothibitishwa, na kuchochea mashaka katika akili za watu wasiokuwa na uzoefu. Katika kila njia inayoweza kufikiriwa watatafuta kusababisha kile ambacho ni safi na cha haki kichukuliwe kama kibaya na cha uongo.

Lakini hakuna anayepaswa kudanganywa kuhusiana na watu hao. Inaweza kujulikana kuwa wao ni watoto wa nani, ni mfano wa nani wanafuata, na wanafanya kazi ya nani. “Mtawatambua kwa matunda yao” (Mathayo 7:16). Kazi yao inafanana na ile ya Shetani, mzushi mwenye sumu, “mshitaki wa ndugu zetu” (Ufunuo 12:10).

Mdanganyaji mkuu ana mawakala wengi walio tayari kuwasilisha kila aina ya kosa ili kunasa roho—uongo ulioandaliwa kufaa kwa kila mazingira na uwezo wa wale ambao anataka kuwaangamiza. Ni mpango wake kuleta kanisani watu wasio na moyo wa dhati, wasioumbwa upya, watakaochochea mashaka na kutokuamini, na kuwa kikwazo kwa wale wote wanaotamani kuiona kazi ya Mungu ikisonga mbele na wao kusonga mbele pamoja nayo. Wengi wasiokuwa na imani ya kweli kwa Mungu au kwa neno Lake wanakubaliana na baadhi ya kanuni za ukweli na wanapitishwa kama Wakristo, na hivyo wanawezeshwa kuingiza makosa yao kama mafundisho ya Maandiko.

Msimamo kuwa haidhuru watu wanaamini kitu gani ni moja ya imani za uongo za Shetani ambazo zinampa mafanikio makubwa sana. Anajua kuwa ukweli, ukipokelewa kwa kuupenda, unaitakasa roho ya mpokeaji; hivyo, anatafuta daima kuweka nadharia potovu, hadithi za uongo, injili nyingine badala ya ukweli wa neno la Mungu. Tangu mwanzo, watumishi wa Mungu wameshindana na walimu wa uongo, siyo tu kama watu wakatili, bali kama wapandikizaji wa mafundisho ya uongo yaliyokuwa hatari kwa uhai wa roho. Eliya, Yeremia, Paulo, kwa uthabiti na bila woga waliwapinga wale waliokuwa wakiwageuza watu waliache neno la Mungu. Ule uhuru unaochukulia imani sahihi ya kidini kuwa sio muhimu haukupata kibali cha hawa watetezi watakatifu wa ukweli.

Tafsiri za Maandiko zisizo dhahiri na za kufikirika, na nadharia nyingi zinazopingana kuhusu imani za dini, zinazopatikana katika ulimwengu wa Kikristo ni kazi za adui yetu mkuu kuchanganya akili ili watu wasitambue ukweli. Na misuguano na migawanyiko iliyomo miongoni mwa makanisa ya Kikristo inasababishwa kwa kiwango kikubwa na desturi zilizopo za kutumia vibaya Maandiko kuunga mkono nadharia zinazopendwa. Badala ya kujifunza kwa uangalifu neno la Mungu kwa unyenyekevu wa moyo ili kujua mapenzi Yake, wengi wanatafuta kugundua kitu kisichokuwa cha kawaida au kipya.

Ili kuhalalisha mafundisho yao yenye makosa na mtendo yao yasiyokuwa ya kikristo, baadhi wanachukua aya za Maandiko zikiwa zimetengwa na muktadha, pengine wakinukuu nusu ya aya moja kuthibitisha hoja yao, wakati sehemu iliyobaki ingeonesha maana iliyo kinyume kabisa. Kwa werevu wa nyoka, wanajibanza nyuma ya kauli zisizokuwa na uhusiano, zilizobuniwa kukidhi tamaa zao za kimwili. Kwa njia hiyo, watu wengi kwa uchaguzi wao wanapotosha neno la Mungu. Wengine, wanaofikiria sana juu ya mambo ya kuwazika tu, yasiyo halisi, wanachukua misemo na mifano ya Maandiko Matakatifu, wanaitafsiri kuhalalisha ubunifu wao, huku wakijali kidogo sana kanuni kuwa ushuhuda wa Maandiko hujitafsiri wenyewe, na ndipo huwasilisha mawazo yao yasiyo na msingi kama mafundisho ya Biblia.

Wakati wowote, kujifunza Maandiko kunapofanyika bila roho ya maombi, unyenyekevu, na kufundishika, aya za wazi na rahisi kabisa pamoja na zile ngumu kabisa zitaeleweka tofauti na maana yake ya kweli. Viongozi wa upapa wanachagua sehemu za Maandiko zinazokidhi vizuri zaidi kusudi lao, wanazitafsiri wanavyopenda wenyewe, na ndipo huwasilisha tafsiri hizi kwa watu, huku wakiwanyima fursa ya kujifunza Biblia na kuelewa ukweli mtakatifu wao wenyewe. Biblia nzima inapaswa kutolewa kwa watu kama inavyosomeka. Ingekuwa bora zaidi kwao wasipate kabisa mafundisho ya Biblia kuliko kupata mafundisho ya Maandiko yaliyowakilishwa vibaya kwa kiwango hicho.

Biblia ilikusudiwa iwe mwongozo kwa wale wote wanaopenda kuyajua mapenzi ya Muumbaji wao. Mungu aliwapa wanadamu neno la kweli la unabii; malaika na hata Kristo Mwenyewe walikuja kumfahamisha Danieli na Yohana mambo ambayo hayana budi kuja upesi. Yale mambo muhimu yanayohusu wokovu wetu hayakuachwa sirini. Hayakufunuliwa katika namna ambayo inamtatanisha na kumpoteza mtafutaji wa dhati wa ukweli. Bwana alisema kupitia kwa nabii Habakuki: “Bwana akanijibu, akasema, Iandike njozi ukaifanye iwe wazi …, ili aisomaye apate kuisoma kama maji” (Habakuki 2:2). Neno la Mungu liko wazi kwa wote wanaolisoma kwa moyo wa maombi. Kila mtu aliye mwaminifu na wa kweli atapokea nuru ya ukweli. “Nuru imemzukia mwenye haki” (Zaburi 97:11). Na hakuna kanisa linaweza kukua katika utakatifu isipokuwa washiriki wake wanautafuta ukweli kwa dhati kama kutafuta hazina iliyositirika.

Kwa makelele ya “Uhuru”, watu wanapofushwa wasione mbinu za adui yao, wakati yeye anafanya kazi wakati wote bila kuchoka afanikishe lengo lake. Baada ya kufanikiwa kuondoa Biblia na badala yake akaingiza fikra za kibinadamu, sheria ya Mungu imewekwa pembeni, na makanisa yako chini ya utumwa wa dhambi wakati wanadai kuwa wako huru.

Kwa wengi, utafiti wa kisayansi umekuwa laana. Mungu ameruhusu mafuriko ya nuru yamwagwe ulimwenguni kwa njia ya ugunduzi wa sayansi na sanaa; lakini hata watu wenye uwezo mkubwa wa akili, wasipoongozwa na neno la Mungu katika utafiti wao, wanachanganyikiwa katika jitihada zao za kuchunguza mahusiano ya sayansi na ufunuo.

Ujuzi wa mwanadamu wa mambo ya kimwili na ya kiroho ni mdogo na siyo kamili; matokeo yake wengi hawawezi kupatanisha mawazo yao ya sayansi na kauli za Maandiko. Wengi wanapokea nadharia na mambo ya kufikirika yasiyo halisi kama ukweli wa kisayansi, na wanafikiri kuwa neno la Mungu linapaswa kupimwa kwa mafundisho ya "elimu iitwayo elimu kwa uongo"(1 Timotheo 6:20). Muumbaji na kazi Zake vipo nje ya ufahamu wao; na kwa kuwa hawawezi kueleza mambo haya kwa sheria za asili, historia ya Biblia inachukuliwa kama taarifa isiyoweza kutumainiwa. Wanaotilia mashaka ukweli wa kumbukumbu za Agano la Kale na Agano Jipya mara nyingi wanaenda hatua nyingine mbele na wanatilia mashaka uwepo wa Mungu na wanadai kuwa vitu vya asili vina nguvu isiyo na mipaka. Wakiwa wameachia nanga yao, wanaachwa wagonge miamba ya ukafiri.

Kwa njia hiyo wengi wanajikwaa katika imani na wanadanganywa na Ibilisi. Wanadamu wanajaribu kuwa na hekima zaidi kuliko Muumba wao; falsafa ya kibinadamu imejaribu kuchunguza na kueleza siri ambazo hazitafunuliwa kamwe milele zote. Ikiwa wanadamu wangeridhika kuchunguza na kuelewa yale ambayo Mungu ameyafunua juu Yake Mwenyewe na makusudi Yake, wangeona mandhari ya utukufu, nguvu, na mamlaka ya Yehova kiasi kwamba wangegundua udogo wao na wangeridhishwa na yale ambayo yamefunuliwa kwa ajili yao na kwa ajili ya watoto wao.

Ni udanganyifu wa Shetani unaofanywa kwa ustadi wa hali ya juu kuwafanya watu watumie sana akili zao kuchunguza na kujaribu kueleza yale ambayo Mungu hajayafunua na ambayo Mungu hakusudii yaeleweke. Ilikuwa kwa sababu hiyo Lusifa alipoteza nafasi yake mbinguni. Alitokea kutoridhika kwa sababu siri zote za makusudi ya Mungu hazikufunuliwa kwake, na alijikuta akipuuza yale ambayo yalikuwa yemefunuliwa kuhusiana na kazi yake katika cheo chake cha juu alichokuwa amepewa. Kwa kuchochea hali ya kutoridhika huko katika mioyo ya malaika waliokuwa chini ya uongozi wake, alisababisha anguko lao. Sasa anatafuta kujaza roho ile ile katika akili za watu ili na wao wapuuze amri za Mungu zinazoeleweka moja kwa moja.

Watu ambao hawapendi kupokea ukweli wa Biblia ulio wazi, unaochoma daima wanatafuta hadithi zinazofurahisha ili kunyamazisha dhamiri zao. Kwa kadiri mafundisho yanayotolewa yasivyokuwa ya kiroho sana, yasivyodai kujikana nafsi, na yasivyodai kujinyenyekesha, ndivyo yanavyopendwa na watu zaidi na yanavyopokelewa kwa wepesi zaidi. Watu hawa wanashusha uwezo wao wa kiakili ili kutimiza tamaa zao za mwili. Wakiwa na hekima nyingi katika kiburi chao kiasi cha kufikia hatua ya kuacha kuchunguza Maandiko kwa unyenyekevu wa moyo na maombi ya dhati ili wapate uongozi wa Kimungu, hawana ngao ya kuwakinga dhidi ya udanganyifu. Shetani yuko tayari kukidhi shauku ya moyo, na anagawa uongo wake badala ya ukweli. Hivyo ndivyo upapa ulivyopata mamlaka yake juu ya akili za watu; na kwa kuukataa ukweli kwa sababu unahusisha msalaba, Waprotestanti wanafuata njia ile ile. Wote wanaopuuza neno la Mungu ili wajifunze njia nyepesi na sera, ili

wasiwe tofauti na watu wa ulimwengu, wataachwa wapokee uongo wa kutisha badala ya ukweli wa kidini. Kila aina ya uongo itapokelewa na watu ambao kwa kuchagua wao wenyewe wanaukataa ukweli wa neno la Mungu. Mtu anayetazama kwa hofu uongo wa aina moja atapokea uongo wa aina nyingine kwa urahisi. Mtume Paulo, akizungumzia juu ya tabaka la watu ambao "hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa," anasema: "Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo; ili wahukumiwe wote ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu" (2 Wathesalonike 2:10- 12). Kwa onyo hili lililoko mbele yetu, inatupasa tuwe makini kuhusiana na fundisho tunalolipokea.

Miongoni mwa mawakala wanaofanikiwa sana wa mdanganyaji mkuu ni mafundisho na maajabu yanayodanganya ya imani ya kuwasiliana na watu waliokufa. Akijigeuza na kuwa kama malaika wa nuru, Shetani anatandaza wavu wake mahali asipotarajiwa sana. Ikiwa watu wangejifunza Kitabu cha Mungu kwa maombi ya dhati wangeweza kulijua hili, wasingeachwa gizani na wasingepokea mafundisho ya uongo. Lakini kwa kuwa wameukataa ukweli wanajikuta wakiwa mawindo ya udanganyifu.

Uongo mwingine wa hatari ni fundisho linalokana na uungu wa Kristo, likidai kuwa hajawahi kuwepo hata kidogo kabla ya ujio Wake duniani. Nadharia hii inapokelewa kwa furaha na tabaka kubwa la watu wanaodai kuiamini Biblia; lakini inapingana na kauli za wazi kabisa za Mwokozi wetu juu ya uhusiano Wake na Baba, tabia Yake ya Kiungu, na uwepo Wake kabla ya ujio Wake duniani. Fundisho hili haliwezi kutetewa bila kupotosha Maandiko. Siyo tu kuwa linashusha uelewa wa mwanadamu wa kazi ya ukombozi, lakini pia linafanya watu wasiiamini Biblia ipasavyo kama ufunuo kutoka kwa Mungu.

Wakati kutokuiamini Biblia kunalifanya fundisho la kuukana uungu wa Yesu liwe la hatari zaidi, kunalifanya pia lisiweze kupingwa kwa urahisi. Watu wakikataa ushuhuda wa Maandiko yaliyovuviwa kuhusu uungu wa Kristo, ni kazi bure kubishana nao juu ya mada hii; kwa sababu hakuna hoja, hata kama ina nguvu kiasi gani, inayoweza kuwashawishi."Mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni" (1 Wakorintho 2:14). Hakuna mtu ye yote yule ambaye anashikilia kosa hili anayeweza kuwa na uelewa wa kweli wa tabia au utume wa Kristo, au wa mpango mkuu wa ukombozi wa mwanadamu.

Na bado kuna kosa jingine lenye hila na ubaya mwingi linaloenea haraka, imani kuwa Shetani hayupo na siyo kiumbe mwenye nafsi; kuwa jina la Shetani linatumika tu kumaanisha mawazo na tamaa mbaya za watu. Fundisho linalohubiriwa mahali pengi kutoka katika mimbari maarufu, kuwa ujio wa pili wa Kristo ni ujio Wake kwa kila mtu wakati wa kifo chake, ni zana ya kuhamisha akili za watu zisifikirie ujio Wake binafsi katika mawingu ya

mbinguni. Kwa miaka mingi, Shetani amekuwa akisema, “Tazama, yumo katika vyumba vya siri” (Mathayo 24:23-26); na roho nyingi zimepotea kwa kuukubali uongo huu.

Tena, kuna hekima ya kidunia inayofundisha kuwa maombi sio muhimu. Wanasayasi wanadai kuwa hakuna jibu halisi kwa maombi; kwamba hili lingekuwa kukiuka sheria, muujiza, na kuwa miujiza haipo. Sayari zote, wanasema, zinatawaliwa na sheria zisizobadilika, na Mungu Mwenyewe hafanyi cho chote kinyume na sheria hizi. Hivyo wanamwakilisha Mungu kuwa anabanwa na sheria Zake Mwenyewe—kana kwamba utendaji wa sheria za Kimungu ungeweza kuondoa uhuru wa Kiungu. Fundisho hilo linapingana na ushuhuda wa Maandiko. Je, miujiza haikufanywa na Kristo na mitume Wake? Mwokozi Yule yule mwenye huruma yuko hai leo, na yuko tayari kusikia maombi ya imani kama alivyofanya alipoonekana kwa macho akitembea miongoni mwa watu. Vitu vya asili vinashirikiana na vitu vilivyo juu ya vitu vya asili. Ni sehemu ya mpango wa Mungu kutupatia, kama jibu kwa ombi la imani, kile ambacho asingetupatia ikiwa tusingemwomba.

Kuna idadi kubwa ya mafundisho yenye makosa na mawazo ya kufikirika yanayozidi kushamiri miongoni mwa makanisa ya ulimwengu wa Kikristo. Ni vigumu kukadiria matokeo mabaya ya kuondoa moja ya viwango vilivyowekwa na neno la Mungu. Ni watu wachache wanaodiriki kufanya hivyo wanaoachia kukataa fundisho moja tu la ukweli. Walio wengi huendelea kuweka pembeni kanuni moja ya ukweli baada ya nyingine, hadi wanafikia kuwa makafiri kamili.

Makosa katika teolojia inayokubaliwa na wengi yamesababisha watu wengi kuwa na mashaka ambapo kama isingekuwa kwa sababu hiyo wangeyaamini Maandiko. Ni vigumu kwa mtu kukubali mafundisho ambayo hukiuka maadili ya haki, rehema, na ukarimu; na kwa kuwa mambo haya huwakilishwa kama mafundisho ya Biblia, mtu anakataa kuyapokea kama neno la Mungu.

Na hili ndilo lengo ambalo Shetani anatafuta kulitimiza. Hakuna jambo jingine analolitamani zaidi kuliko kuua imani kwa Mungu na kwa neno Lake. Shetani ni kiongozi mkuu wa jeshi kubwa la watu wenye mashaka, na anafanya kazi kwa nguvu zake zote kuwadanganya watu na kuwaleta upande wake. Kuwa na mashaka kumekuwa mtindo wa maisha. Kuna tabaka kubwa la watu ambao kwao neno la Mungu linatazamwa kwa mashaka kwa sababu ile ile kama ilivyokuwa kwa Mwasisi wake—kwa sababu linakemea na kuhukumu dhambi. Wale ambao hawako tayari kutii matakwa yake wanajaribu kushinda mamlaka yake. Wanasoma Biblia, au wanasikiliza mafundisho yake yanapowasilishwa kutoka katika dawati takatifu, kwa kusudi tu la kutafuta makosa katika Maandiko au katika hubiri.

Siyo watu wachache wakuwa makafiri ili kuhalalisha au kupata udhuru wa kukimbia wajibu wao. Wengine wanashika kanuni za kutoamini kwa sababu ya kiburi na uvivu.

Wanapenda raha, ili wajitambulishe kwa kufanya jambo lolote la kuwaletea heshima, ambalo linahitaji juhudi na kujikana nafsi, wanadhamiria kujipatia umaarufu kwa kukosoa Biblia wakififikiri kuwa kwa kufanya hivyo wataonekana ni wenye hekima. Kuna mengi ambayo akili yenye mipaka, ambayo haijaangaziwa kwa hekima ya Kiungu, haina uwezo wa kuyaelewa; na hivyo wanapata kisingizio cha kukosoa. Kuna wengi ambao huonekana kufikiri kuwa ni sifa njema kusimama upande wa kutokuamini, mashaka, na ukafiri. Lakini chini ya mwonekano wa uwazi wao itagundulika kuwa watu kama hao wanachochewa na kujiamini na kiburi. Wengi wanafurahia kupata jambo fulani katika Maandiko la kutatanisha akili za wengine. Baadhi mwanzoni wanakosoa na kutoa hoja upande usio sahihi, kwa sababu tu wanapenda ubishi. Hawatambui kuwa kwa njia hiyo wanajinasisha wenyewe katika mtego wa mwindaji. Lakini baada ya kueleza wazi kutokuamini kwao, wanahisi wanapaswa kutetea msimamo wao. Hivyo wanaungana na wasiomcha Mungu na kujifungia wenyewe malango ya Paradiso.

Mungu ametoa katika neno Lake ushahidi wa kutosha wa tabia yake ya Kiungu. Ukweli mkuu ambao unahusu ukombozi wetu umewasilishwa kwa uwazi. Kwa msaada wa Roho Mtakatifu, ambao umeahidiwa kwa wale wote wanaoutafuta kwa dhati, kila mtu anaweza kuelewa ukweli huu yeye mwenyewe. Mungu amewapa watu msingi imara ambao juu yake wanaweza kusimika imani yao.

Lakini akili za watu zenye kikomo haziwezi kuelewa kikamilifu mipango na makusudi ya Yeye Asiye na Kikomo. Hatuwezi kamwe kumwona Mungu kwa kuchunguza. Hatupaswi kujaribu kutumia mikono yetu yenye kiburi kufungua pazia ambalo nyuma yakeameficha ukuu Wake. Mtume anapiga kelele kwa mshangao: “Hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani!” (Warumi 11:33).

Tunaweza tu kuelewa jinsi anavyoshughulika na sisi, na nia inayomsukuma kufanya hivyo, ili tuweze kutambua upendo usio na mipaka na rehema zilizoshikamana na nguvu isiyokuwa na mipaka. Baba yetu aliyeko mbinguni anapanga kila jambo kwa hekima na haki, na hatupaswi kutoridhishwa na kutokuwa na imani Naye, bali tumsujudie na tujisalimishe Kwake kwa kicho. Atatufunulia makusudi Yake mengi ambayo ni kwa ajili ya ustawi wetu tukiyajua, na zaidi ya hayo inatupasa kuutumainia Mkono ambao una nguvu zisizo na mpaka, Moyo uliojaa upendo.

Wakati Mungu ametoa ushahidi wa kutosha kwa ajili ya imani yetu, kamwe hataondoa visingizio vyote ya kutokuamini. Watu wote wanaotafuta ndoana za kuning’iniza mashaka yao watazipata. Na wale wanaokataa kukubali na kutii neno la Mungu mpaka kila kikwazo kimeondolewa, na kusiwe kabisa na fursa ya kuwa na mashaka, hawatakuja nuruni.

Kutokumwamini Mungu ni tunda la asili ya moyo usioumbwa upya, moyo ulio na uadui na Mungu. Lakini imani inavuviwa na Roho Mtakatifu, na itastawi ikipaliliwa. Hakuna mtu

anayeweza kuwa na imani bila juhudi za makusudi. Kukosa imani kunakuzwa kwa kuchochewa na kuhimizwa; na ikiwa watu, badala ya kutafakari juu ya ushahidi uliotolewa na Mungu kujenga imani yao, wanajielekeza katika kuhoji na kulaumu, wataona mashaka yao yakiendelea kuwa makubwa zaidi.

Lakini wale wanaotilia mashaka ahadi za Mungu na wanakosa imani katika hakika ya neema Yake wanamkosea Mungu heshima; na mvuto wao, badala ya kuwavuta wengine kwa Kristo, unakuwa na mwelekeo wa kuwasukumia mbali Naye. Wao ni miti isiyozaa matunda, inayoeneza matawi yake meusi mbali na katika maeneo mengi, ikizuia mwanga wa jua usiifikie mimea mingine, na kuifanya isinyae na kufa chini ya kivuli chenye baridi. Kazi ya maisha ya watu hawa huonekana kama ushuhuda wa kudumu dhidi yao. Wanapanda mbegu za mashaka na kutoamini ambazo zitatoa mavuno hatimaye.

Kuna njia moja tu ya kufuata kwa wale wanaotamani kwa dhati kuondokana na mashaka. Badala ya kuhoji na kulalamikia yale wasiyoyaelewa, hebu wao wapokee nuru ambayo tayari inawaangazia, na watapokea nuru kubwa zaidi. Hebu wao watimize wajibu wao uliowekwa wazi kwa ufahamu wao, nao watawezeshwa kuelewa na kutekeleza yale ambayo kwa sasa wanayatilia mashaka.

Shetani anaweza kuwasilisha kitu bandia kinachofanana sana na ukweli kiasi cha kuwadanganya watu walio tayari kudanganywa, wanaotamani kukwepa kujikana na kujitoa kafara kunakotakiwa na ukweli wa neno la Mungu; lakini haiwezekani kwake kumshikilia chini ya mamlaka yake mtu ambaye anatamani kwa uaminifu, na kwa gharama yo yote, kuujua ukweli. Kristo ni kweli na ni “Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu” (Yohana 1:9). Roho wa kweli ametumwa kuwaongoza watu katika ukweli wote. Na kwa mamlaka ya Mwana wa Mungu imetangazwa: “Tafuteni, nanyi mtaona.” “Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo” (Mathayo 7:7; Yohana 7:17).

Wafuasi wa Kristo wanajua kidogo sana kuhusu njama ambazo Shetani na majeshi yake wanazipanga dhidi yao. Lakini Yeye aketiye mbinguni juu atazigeuza njama hizi kutekeleza mipango Yake ya kina. Bwana huruhusu watu Wake wapitishwe katika tanuru la moto wa majaribu, siyo kwa sababu anafurahia maudhi na mateso yao, lakini kwa sababu mchakato huu ni muhimu kwa ajili ya ushindi wao. Mungu asingeweza, daima kwa utukufu Wake Mwenyewe, kuwakinga dhidi ya majaribu; kwa kuwa kusudi la msingi la majaribu ni kuwaandaa kupinga vishawishi vyote vya uovu.

Sio watu wabaya wala mashetani wanaoweza kuzuia kazi ya Mungu, au kufungia uwepo Wake dhidi ya watu Wake, ikiwa watakuwa watiifu, wenye mioyo iliyopondeka, waliotubu na kuachana na dhambi zao, na kwa imani wanadai ahadi Zake. Kila jaribu, kila nguvu ya

upinzani, ikiwa ya wazi au ya siri, inaweza kupingwa kwa mafanikio, "Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi" (Zekaria 4:6).

"Macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio yake husikiliza maombi yao;.... Naye ni nani atakayewadhuru, mkiwa wenye juhudi katika mema?" (1 Petro 3:12, 13). Balaamu aliposhawishiwa kwa ahadi ya zawadi, alifanya uchawi dhidi ya Israeli, na kwa kumtolea Bwana kafara alitaka kutamka laana juu ya watu Wake, Roho wa Mungu alikataa uovu aliotamani kuutamka, na Balaamu alilazimishwa kusema: "Nimlaanije, yeye ambaye Mungu hakumlaani? Nimshutumuje, yeye ambaye Bwana hakumshutumu?"

"Na nife kifo chake mwenye haki, Na mwisho wangu uwe mfano wa mwisho wake!" Baada ya kafara kutolewa tena, nabii asiyemcha Mungu alitangaza: "Tazama, nimepewa amri kubariki, Yeye amebariki, nami siwezi kulitangua. Hakutazama uovu katika Yakobo, Wala hakuona ukaidi katika Israeli. Bwana, Mungu wake, yu pamoja naye, Na sauti kuu ya mfalme i katikati yao." "Hakika hapana uchawi juu ya Yakobo, Wala hapana uganga juu ya Israeli. Sasa habari za Yakobo na Israeli zitasemwa, Ni mambo gani aliyoyatenda Mungu!" Pamoja na hizo madhabahu zilizojengwa kwa mara ya tatu, na kwa mara nyingine tena Balaamu alijaribu kutamka laana. Lakini kutoka katika midomo isiyopenda, Roho wa Mungu alitangaza mafanikio ya wateule Wake, na alikemea upumbavu na ubaya wa maadui zao: "Na abarikiwe kila akubarikiye, Na alaaniwe kila akulaaniye" (Hesabu 23:8, 10, 20, 21, 23; 24:9).

Watu wa Israeli walikuwa watiifu kwa Mungu kwa wakati huu; na kwa kadiri walivyodumu kuitii sheria Yake, hakuna nguvu duniani au kuzimuni ambayo ingeweza kuwashinda. Lakini laana ya Balaamu aliyokatazwa kuitamka dhidi ya watu wa Mungu, hatimaye alifaulu kuileta juu yao kwa kuwashawishi na kuwafanya watende dhambi. Walipokiuka amri za Mungu, walijitenga Naye, nao waliachwa wakutane na nguvu ya mwangamizaji.

Shetani anajua vizuri kuwa roho dhaifu kabisa kuliko zote inayokaa ndani ya Kristo ina nguvu nyingi zaidi kuliko majeshi yote ya giza, na kuwa, kama angejifunua wazi wazi, angekabiliwa na kushindwa. Hivyo anajitahidi kuwavuta askari wa msalaba watoke katika ngome yao imara, wakati yeye pamoja na majeshi yake wakiwavizia, wakiwa tayari kuwaangamiza wale wote wanaokwenda katika eneo lake. Kumtegemea Mungu kwa moyo mnyenyekevu, na kumtii Mungu kikamilifu ndiyo njia pekee ya usalama wetu. Hakuna mtu ambaye yuko salama kwa siku moja au saa moja bila maombi.

Muhimu kuliko yote, inatupasa kumlilia Bwana kwa ajili ya hekima ya kulielewa neno Lake. Humo zimefunuliwa hila za mjaribu na njia ambazo kwazo anaweza kupingwa kwa ufanisi. Shetani ni mjuzi wa kudondoa Maandiko, akiweka tafsiri yake ya mafungu, ambayo kwayo anatumaini kuwa anaweza kutukwaza. Inatupasa kujifunza Biblia kwa unyenyekevu

wa moyo, bila kusahau hitaji letu la kumtegemea Mungu. Wakati ambapo inatupasa daima kuwa macho dhidi ya mbinu za Shetani, inatupasa kuomba daima: “Usitutie majaribuni.”

Sura ya 33 - Udanganyifu Mkuu wa Kwanza

Tangu mwanzoni kabisa mwa historia ya mwanadamu, Shetani alianza juhudi zake za kudanganya jamii yetu. Yule aliyechochea uasi mbinguni alitamani kuwaleta wakazi wa dunia waungane naye katika vita yake dhidi ya serikali ya Mungu, na ukweli huu ulikuwa ushuhuda wa daima dhidi ya dai alilolitoa Shetani mbinguni, kuwa sheria ya Mungu ni kandamizi na iko kinyume na maslahi ya viumbe Wake. Na zaidi ya hapo, kijicho cha Shetani kiliamshwa alipoona makazi mazuri yaliyoandaliwa kwa ajili ya wawili hao wasiokuwa na dhambi. Alidhamiria kusababisha anguko lao, halafu, baada ya kuwatenganisha na Mungu na kuwaleta chini ya mamlaka yake, angeimiliki dunia na hapa ndipo angesimika ufalme wake akipingana na Yeye Aliye Juu.

Ikiwa Shetani angejifunua katika tabia yake halisi, angepingwa mara moja, kwa kuwa Adamu na Hawa walikuwa wameshaonywa dhidi ya adui huyo wa hatari; lakini alifanya kazi gizani, akificha kusudi lake, ili atekeleze lengo lake kwa ufanisi zaidi. Akitumia nyoka kama mwili wake, kiumbe ambaye wakati ule alikuwa wa kuvutia katika mwonekano wake, alizungumza na Hawa: "Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?" (Mwanzo 3:1). Ikiwa Hawa angejizuia asiingie katika mahojiano na mjaribu, angekuwa salama; lakini alijiingiza katika mazungumzo na Ibilisi na akawa mhanga wa hila zake. Hivi ndivyo ambavyo bado wengi wanashindwa. Wanatilia mashaka na kuhoji matakwa ya Mungu; na badala ya kutii amri za Mungu, wanapokea nadharia za kibinadamu, ambazo kimsingi zinaficha mitego ya Shetani.

"Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya" (Aya ya 2-5). Shetani alitangaza kuwa wangekuwa kama Mungu, wakiwa na hekima kubwa zaidi kuliko kabla na wakiwa na uwezo wa kuishi maisha ya hali ya juu zaidi. Hawa alishindwa na jaribu; na kwa ushawishi wa Hawa, Adamu aliongozwa kutenda dhambi. Walikubali maneno ya nyoka, kuwa Mungu hakumaanisha kile alichosema; walimtilia shaka Muumba wao na walidhani kuwa Mungu aliminya uhuru wao na kuwa wangeweza kupata hekima kubwa zaidi na kuinuliwa juu kwa kukiuka sheria Yake.

Lakini Adamu, baada ya dhambi yake, aligundua kitu gani kuhusu maana ya maneno, "Siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika"? Je, aligundua kuwa maneno haya yalimaanisha, kama Shetani alivyomwongoza kuamini, kuwa angeingizwa katika maisha ya hali ya juu? Kama kweli ilikuwa hivyo basi maana yake kulikuwa na faida kubwa iliyopatikana kwa kutenda dhambi, na Shetani alithibitika kuwa mfadhili wa jamii ya wanadamu. Lakini Adamu hakugundua kuwa hii ndiyo ilikuwa maana ya hukumu ya Mungu. Mungu alitangaza kuwa kama adhabu ya dhambi yake, mwanadamu angerudi mavumbini

alikotolewa:"Kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi" (Aya ya 19). Maneno ya Shetani, "mtafumbuliwa macho," yalithibitika kuwa ya kweli katika maana hii pekee: Baada ya Adamu na Hawa kumwasi Mungu, macho yao yalifumbuliwa waone upumbavu wao; hawakujua uovu, na walionja matunda machungu ya kutenda dhambi.

Katikati ya Edeni ulikuwepo mti wa uzima, ambao matunda yake yalikuwa na uwezo wa kuendeleza uhai. Ikiwa Adamu angedumu kuwa mtii kwa Mungu, angeendelea kuwa huru kuuendea mti huu na angeishi milele zote. Lakini alipotenda dhambi, alikatazwa asiuendee mti wa uzima, na alikabiliwa na kifo. Hukumu ya Mungu, "Maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi," huzungumzia kutoweka kabisa kwa uzima.

Hali ya kutokufa, ambayo mwanadamu aliahidiwa kwa sharti la utii, iliondolewa kwa sababu ya kutenda dhambi. Adamu asingeweza kurithisha kwa watoto wake kile ambacho yeye mwenyewe hakuwa nacho; na kulikuwa hakuna tumaini kwa jamii iliyoanguka dhambini ikiwa Mungu, kwa njia ya kafara ya Mwana Wake, asingerudisha hali ya kutokufa katika uwezekano wa kuipata. Wakati ambapo "mauti iliwafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi," Kristo alimebatilisha mauti, na "kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili" (Warumi 5:12; 2 Timotheo 1:10). Ni kwa njia ya Kristo pekee hali ya kutokufa inaweza kupatikana. Yesu alisema: "Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima" (Yohana 3:36). Kila mtu anaweza kupata mbaraka huu wa thamani kubwa ikiwa atatimiza masharti. Wote "ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika," watapokea "uzima wa milele" (Warumi 2:7).

Mdanganyaji mkuu pekee ndiye aliyemwahidi Adamu uzima katika uasi. Na tangazo la nyoka kwa Hawa katika Bustani ya Edeni— "Hakika hamtakufa"—lilikuwa hubiri la kwanza lililowahi kuhubiriwa juu ya hali ya kutokufa kwa roho. Hata hivyo, tangazo hili, likiwa limejengwa juu ya mamlaka ya Shetani pekee, linahubiriwa katika mimbari za ulimwengu wa Ukristo na kupokelewa na watu wengi kwa utayari ule ule wa wazazi wetu wa kwanza. Hukumu ya Mungu,"Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa" (Ezekieli 18:20), inatafsiriwa kumaanisha: Roho itendayo dhambi, siyo itakayokufa, bali ndiyo itakayoishi milele. Ni jambo linaloshangaza kuona jinsi wanadamu wanavyoweza kupumbazwa kiasi cha kuamini maneno ya Shetani na kukataa kuamini maneno ya Mungu.

Ikiwa mwanadamu baada ya anguko angeruhusiwa kuuendea mti wa uzima, angeishi milele, na hivyo mwenye dhambi angekuwa na hali ya kutokufa. Lakini makerubi na upanga wa moto vililinda "njia ya mti wa uzima" (Mwanzo 3:24), na hakuna hata mtu mmoja wa familia ya Adamu amewahi kuruhusiwa kupita kizuizi kile na kula matunda yanayotoa uzima. Kwa hiyo hakuna mwenye dhambi ambaye hafi.

Lakini baada ya Anguko, Shetani aliwaagiza malaika zake kufanya juhudi maalumu za kupandikiza imani ya hali ya kutokufa kwa mwanadamu; na baada ya kuwashawishi watu kupokea kosa hili, iliwapasa kuwaongoza kuhitimisha kuwa mwenye dhambi angeweza kuishi katika mateso ya milele. Sasa mfalme wa giza, akifanya kazi kwa njia ya mawakala wake, anamwakilisha Mungu kama jitu katili linalolipiza kisasi, akitangaza kuwa Mungu anawatupa jehanamu wale wote wasiompendeza, na kuwafanya wahisi ghadhabu Yake; na kuwa wakati wakiteseka kwa uchungu usioelezeka na wakihangaika katika ndimi za moto za milele, Muumbaji wao anawatazama na kuridhika.

Kwa hiyo adui mkuu anamvika kwa sifa zake mwenyewe Muumbaji na Mruzuku wa wanadamu. Ukatili ni wa kishetani. Mungu ni pendo; na vyote alivyoviumba vilikuwa vyema, vitakatifu, na vya kupendeza, mpaka dhambi ilipoingizwa kwa njia ya mwasi mkuu wa kwanza. Shetani mwenyewe ni adui anayemjaribu mwanadamu atende dhambi, na ndipo anamwangamiza akiweza; na akifaulu kumwangusha mhanga wake, anafurahia uharibifu anaokuwa amefaulu kuufanya. Akiruhusiwa, anaweza kufutilia mbali jamii yote ya wanadamu katika wavu wake. Isingekuwa kwa ajili ya kuingilia kwa nguvu za Mungu, hakuna mwanadamu ye yote hata mmoja angepona.

Shetani anatafuta kuwashinda watu leo, kama alivyowashinda wazazi wetu wa kwanza, kwa kutikisa imani yao kwa Muumba wao na kuwaongoza kutilia shaka hekima ya serikali Yake na haki ya sheria Yake. Shetani na vibaraka wake wanamwakilisha Mungu kana kwamba Mungu ni mbaya zaidi kuliko wao, ili kuhalalisha uovu na uasi wao. Mdanganyaji mkuu anajitahidi kuhamisha ukatili wa kutisha wa tabia yake na kuuweka juu ya Baba yetu wa mbinguni, ili atengeneze mazingira ya yeye kuonekana kuwa ndiye aliyekosewa alipofukuzwa mbinguni kwa sababu asingekubali kujisalimisha chini ya mtawala dhalimu kama huyo. Anawasilisha mbele ya ulimwengu uhuru ambao wangeweza kuufurahia chini ya utawala wake mwepesi, kinyume na utumwa wa kulazimishwa wa amri kali za Yehova.

Kwa njia hiyo anafanikiwa kudanganya watu na kuwafanya wasimtii Mungu. Ni kero kubwa kiasi gani kwa mhemko wa upendo na rehema, na hata kwa uelewa wetu wa haki, kuna fundisho kuwa waovu waliokufa wanateswa kwa moto wa kiberiti katika jehanamu inayowaka moto milele zote; kuwa kwa ajili ya dhambi za maisha mafupi ya duniani inawapasa kupata mateso wakati wote ambao Mungu atadumu kuwepo. Lakini fundisho hilo limekuwa likifundishwa mahali pengi na bado ni moja ya mafundisho ya imani za msingi za ulimwengu wa Kikristo. Alisema daktari msomi wa theolojia: “Mwonekano wa mateso ya jehanamu utaongeza furaha ya watakatifu milele zote. Wakati wengine walio na asili kama ya kwao na waliozaliwa chini ya mazingira yaliyo sawa na ya kwao, wakitupwa katika taabu ile, na wao wakiwa wameheshimiwa sana, italeta maana ya kwa nini wao wawe na furaha.” Mwingine alitumia maneno haya: “Wakati amri ya kukataliwa ikitekelezwa milele na milele kwa walengwa wa ghadhabu, moshi wa maumivu yao utakuwa ukipanda mbele ya macho ya

walengwa wa rehema, ambao, badala ya kushiriki mateso ya hawa waliokataliwa, wao watakuwa wakisema, Amina, Aleluya! Msifuni Bwana!"

Ni wapi, katika kurasa za neno la Mungu, unaweza kupata fundisho hili? Je, waliokombolewa wakiwa mbinguni watapoteza kabisa mhemko wa huruma na kujali, na hata hisia za umoja wa ubinadamu? Je, hisia zitaondolewa na badala yake waliokombolewa watakuwa na hali ya kutojali kwa ukakamavu au ukatili wa mshenzi? Hapana, hapana; hili sio fundisho la Kitabu cha Mungu. Watu wanaowasilisha mawazo yaliyoelezwa katika dondoo zilizotolewa hapo juu wanaweza kuwa watu wenye elimu na hata watu waaminifu, lakini wamepotoshwa na uongo wa Shetani. Anawaongoza kutafsiri vibaya kauli nzito za Maandiko, akiipa lugha rangi ya uchungu na ubaya ambao ni wake yeye mwenyewe, lakini siyo wa Muumbaji wetu. "Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi. Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa, Enyi nyumba ya Israeli?" (Ezekieli 33:11).

Je, Mungu angepata nini, ikiwa tungekubali kuwa Anafurahia kuona mateso yasiyokoma; kuwa anaburudishwa na vilio na kelele na maneno ya laana ya viumbe wake aliowashikilia katika moto wa jehanamu? Je, inawezekana kuwa sauti hizi mbaya zikawa muziki mzuri katika sikio la Upendo wa Milele? Kuna hoja inatolewa kuwa adhabu ya maumivu yasiyokoma kwa waovu itaonesha chuki ya Mungu kwa dhambi kama uovu unaoharibu amani na utaratibu wa ulimwengu. Aha! kufuru ya kutisha! Kana kwamba chuki ya Mungu dhidi ya dhambi ndiyo sababu mateso yanaendelezwa. Kwani, kulingana na mafundisho ya wanatheolojia hawa, kuendelezwa kwa mateso bila tumaini la rehema kunawafanya wahanga maskini wawe na hasira zaidi, na kwa kadiri wanavyomwaga nje hasira zao kwa laana na kufuru, wanaongeza mzigo wao wa hatia milele na milele.

Utukufu wa Mungu hauongezwi kwa njia hiyo ya kuongeza mzigo wa dhambi daima milele na milele. Ni nje ya uwezo wa akili ya mwanadamu kukadiria uovu ambao umefanywa kwa njia ya fundisho la uongo la mateso ya adhabu ya milele. Dini ya Biblia, ikiwa imejaa upendo na wema, na ikiwa imesheheni huruma tele, inatiwa giza kwa ushirikina na kuvikwa hofu kuu. Tunapotafakari kiasi cha rangi za uongo ambazo Shetani ameipaka tabia ya Mungu, tunaweza kushangaa kama kweli Muumbaji wetu mwenye rehema anaheshimiwa, anahofiwa, na hata anachukiwa? Mawazo ya kutisha kuhusu Mungu ambayo yamesambazwa ulimwenguni kote kutokana na mafundisho yanayotolewa katika mimbari yamewafanya maelfu, ndiyo, mamilioni, wawe na mashaka na Mungu, na wengine wawe makafiri kabisa.

Nadharia ya mateso ya adhabu ya milele ni moja ya mafundisho ya uongo yanayotengeneza mvinyo ya machukizo ya Babeli, ambayo anawanywesha watu wa mataifa yote (Ufunuo 14:8; 17:2). Ukweli kuwa watumishi wa Kristo walilipokea fundisho hili la uongo na kulihubiri kutoka katika meza takatifu ni siri ya ajabu. Walilipokea kutoka Roma,

kama walivyopokea sabato ya uongo. Ni kweli, limefundishwa na watu wanaoheshimiwa sana na watu walio wema kabisa; lakini nuru kuhusu somo hili ilikuwa haijawafikia kama ilivyotufikia sisi. Waliwajibika tu kwa ile nuru iliyomulika katika wakati wao; sisi tunawajibika kwa ajili ya nuru inayomulika katika wakati wetu. Ikiwa tutaacha ushuhuda wa neno la Mungu, na kupokea mafundisho ya uongo kwa sababu baba zetu waliyafundisha, tunanaswa katika hukumu iliyotangazwa juu ya Babeli; tunakunywa mvinyo ya machukizo ya Babeli.

Tabaka kubwa la wale ambao fundisho la mateso ya adhabu ya milele halileti maana kwao wanasukumwa upande mwingine wa kosa hilo lililo kinyume cha lile la kwanza. Wanaona kuwa Maandiko yanamwakilisha Mungu kama mwenye uhai mwenye upendo na huruma, na hawawezi kuamini kuwa atawatupa viumbe Wake katika jehanamu inayowaka moto milele. Lakini kushikilia kuwa roho kwa asili haifi, hawaoni njia nyingine isipokuwa kuhitimisha kuwa wanadamu wote hatimaye wataokoka. Wengi wanachukulia vitisho vya Biblia kama vile vimepangwa kuwatisha tu watu wawe watiifu, na siyo kweli kuwa vitatimizwa. Hivyo basi, mwenye dhambi anaweza kuishi katika anasa za kibinafsi, huku akipuuza matakwa ya Mungu, na bado atarajie hatimaye kupokelewa na kukubaliwa Naye. Fundisho hilo, ambalo hudaiwa kujengwa juu ya rehema za Mungu, lakini likipuuza uwepo wa haki ya Mungu, huufurahisha moyo wa mwanadamu asiye na Mungu na unawaimarisha watu waovu katika uovu wao.

Kuonesha jinsi wanaoamini katika wokovu wa watu wote wanavyopotosha Maandiko ili kuhalalisha imani zao potofu zinazoangamiza roho, inatupasa kutaja tu kauli zao wenyewe. Wakati wa mazishi ya kijana mwanaume asiyekuwa na dini, aliyekuwa amekufa kwa ghafla kwa sababu ya ajali, mchungaji anayeamini katika wokovu wa watu wote alichagua kama aya yake kuu kauli ya Maandiko inayomhusu Daudi: “Kwa kuwa ametulizwa kwa habari ya Amnoni, kwa maana amekufa” (2 Samweli 13:39).

“Ninaulizwa mara kwa mara,” mhubiri alisema, “kuhusu hatima ya wale wanaoondoka duniani wakiwa wenye dhambi, wanaokufa, pengine, wakiwa wamelewa, wanaokufa wakiwa na madoa mekundu ya uhalifu wa kijinai bila kuoshwa na kuondolewa kwenye majoho yao, au wanaokufa kama alivyokufa kijana huyu, bila kukiri wakati wowote au kupata uzoefu wo wote ule wa kidini. Tunaridhishwa na Maandiko; jibu lao linatatua tatizo kubwa sana. Amnoni alikuwa mwenye dhambi kuliko kawaida; hakuwa na muda wa kutubu; alikuwa amelewa pombe, na akiwa amelewa aliuawa. Daudi alikuwa nabii; na hivyo basi, ni lazima alikuwa na uwezo wa kujua ikiwa hatima ya Amnoni ingekuwa nzuri au mbaya katika ulimwengu ujao. Maelezo kutoka katika moyo wa Daudi yalikuwa na ujumbe gani? ‘Mfalme Daudi akatamani kutoka kumwendea Absalomu kwa kuwa ametulizwa kwa habari ya Amnoni, kwa maana amekufa’ (Aya ya 39).”

“Na ni fundisho gani tunalipata kutokana na lugha hii? Sio kuwa mateso yasiyokoma hayakuwa sehemu ya imani yake ya kidini? Kwa hiyo tunaelewa; na hapa tunagundua hoja ya ushindi inayounga mkono nadharia yenye ukarimu, inayofurahisha zaidi, yenye nuru kubwa zaidi ya hatima ya usafi na amani kwa watu wote. Daudi alifarijika alipoona mwanawe amekufa. Kwa nini afarijike? Kwa sababu ya jicho la kiunabii aliweza kuona mbele katika wakati ujao wenye utukufu na akaona kuwa mwanawe akiwa ameepushwa na majaribu yote, akiwa ameachiwa kutoka katika utumwa na akiwa ameoshwa uchafu wote wa dhambi, na baada ya kutakaswa kiasi cha kutosha na kupewa nuru ya kutosha, aliruhusiwa kuingia katika mkutano wa roho zilizokwisha kupaa na zinazofurahia. Faraja pekee ilikuwa, kwa kuondolewa katika hali ya sasa ya dhambi na mateso, mwanawe mpendwa alikuwa amekwenda mahali ambapo pumzi za juu za Roho Mtakatifu zingemulika nuru juu ya roho yake yenye giza, ambapo akili yake ingefunguliwa ili kupokea hekima ya mbinguni na furaha tamu ya upendo usio na kikomo, na hivyo kupata asili iliyotakaswa na kufurahia pumziko pamoja na jamii yote ya warithi wa mbinguni.

“Katika mawazo haya ingekuwa vema tueleweke kuwa, tunaamini kuwa wokovu wa mbinguni hautegemei kitu cho chote ambacho tunaweza kukifanya katika maisha haya; wala juu ya badiliko la sasa la moyo, wala imani ya sasa, au kukiri kwa sasa kuwa una dini.”

Hivyo, mtu anayedai kuwa ni mtumishi wa Kristo, anakariri uongo uliosemwa na nyoka katika bustani ya Edeni: “Hakika hamtakufa.” “Siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu.” Anadai kuwa, watu wenye dhambi kupindukia—mwuaji, mwizi, na mzinzi—baada ya kifo, wataandaliwa kuingia katika furaha ya milele.

Na ni kutokana na nini huyu mpotoshaji wa Maandiko anapata hitimisho lake? Kutoka sentensi moja inayoeleza kujisalimisha kwa Daudi kwa uongozi wa Mungu. Roho yake ilitamani “kutoka kumwendea Absalomu kwa kuwa ametulizwa kwa habari ya Amnoni, kwa maana amekufa.” Baada ya makali ya uchungu wake kupozwa kwa kadiri muda ulivyozidi kusonga mbele, mawazo yake yalihama kutoka kwa mtoto aliyekwisha kufa yakaelekea kwa mwanawe aliye hai, akiwa amejiachia na kujisalimisha kwa Mungu kwa sababu ya hofu ya adhabu ya haki ya Amnoni kwa sababu ya uhalifu wake mwenyewe. Na huu ndiyo ushahidi kuwa Amnoni, mbakaji wa dada yake na mlevi wa pombe, mara baada ya kifo chake alichukuliwa hadi katika makao ya amani, pale akatakaswa na kuandaliwa kwenda kuishi na malaika wasiokuwa na dhambi! Hadithi ya kufurahisha kweli, inayopendeza moyo usio na Roho wa Mungu! Hili ni fundisho la Shetani mwenyewe, na linamsaidia katika kazi yake kwa ufanisi mkubwa. Je, tushangae, kwa fundisho kama hilo, uovu ukizidi kuongezeka?

Njia iliyofuatwa na huyu mwalimu mmoja wa uongo ni mfano wa njia zinazofuatwa na wengine wengi. Maneno machache ya Maandiko yanatenganishwa na muktadha, ambao mara nyingi ungeonesha maana yake kuwa kinyume kabisa na tafsiri inayotolewa kwa maneno

hayo; na aya hizo zilizokatwa katwa zinapotoshwa na kutumiwa kama uthibitisho wa mafundisho ambayo hayana msingi katika neno la Mungu. Ushuhuda uliotolewa kuwa Amnoni mlevi yuko mbinguni ni tafsiri inayopingana moja kwa moja na kauli za wazi na chanya za Maandiko kuwa hakuna mlevi atakayeurithi ufalme wa Mungu (1 Wakorintho 6:10). Ndivyo hivyo wenye mashaka, wasioamini, na wenye kushuku hugeuza ukweli kuwa uongo. Na watu wengi wamedanganywa kwa uongo wao na kubembelezwa hadi wanasinzia katika kitanda cha usalama wa kimwili.

Kama ingekuwa ni kweli kuwa roho za wanadamu wote hupita moja kwa moja na kuingia mbinguni wakati wa saa ya kufa, basi wote tungetamani kufa kuliko kuishi. Wengi wameongozwa na imani hii kukatisha maisha yao. Wanapozidiwa na matatizo, mashaka, na kukatishwa tamaa, inaonekana kuwa jambo rahisi kukata uzi mwepesi wa maisha na kupaa kwenda katika amani ya ulimwengu wa milele.

Mungu ametoa katika neno Lake ushahidi wa kutosha kuwa atawaadhibu wavunjaji wa sheria. Wale wanaojifariji kwa kujidanganya kuwa Yeye ni mwenye rehema nyingi sana kiasi kwamba hawezi kutekeleza haki kwa mwenye dhambi, hebu na watazame msalaba wa Kalwari. Kifo cha Mwana wa Mungu asiyekuwa na doa kinathibitisha kuwa “mshahara wa dhambi ni mauti,” kuwa kila uvunjaji wa sheria ya Mungu lazima upokee adhabu yake ya haki.

Kristo alifanyika dhambi kwa ajili ya mwanadamu. Alibeba hatia ya dhambi, na alivumilia kufichwa kwa uso wa Baba Yake, mpaka moyo Wake ukavunjika na uhai Wake kutoka. Kafara yote hii ilifanywa ili mwenye dhambi akombolewe. Kulikuwa hakuna njia nyingine ambayo ingewezesha mwanadamu aokolewe kutoka katika adhabu ya dhambi. Na kila mtu anayekataa kuwa mshirika wa upatanisho uliopatikana kwa gharama kubwa kama hiyo atalazimika kubeba katika nafsi yake mwenyewe hatia na adhabu ya uasi wake.

Hebu tuangalie kile ambacho Biblia inafundisha kuhusu watu wasiomcha Mungu na wasiotubu, ambao, mtetezi wa wokovu kwa wote bila kujali hali yao ya kiroho, anasema watakwenda mbinguni kukaa pamoja na malaika watakatifu, wenye furaha.

“Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima, bure” (Ufunuo 21:6). Ahadi hii ni kwa wale tu wenye kiu. Ni wale tu walio na hitaji la maji ya uzima, na wanayatafuta kwa gharama ya vitu vyote vingine, ndio watakaopewa. “Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu”(Aya ya 7). Hapa, pia, masharti yameelezwa wazi. Ili kurithi vitu vyote, inatupasa kuipinga na kuishinda dhambi.

Bwana anatangaza kupitia kwa nabii Isaya: “Waambieni wenye haki ya kuwa watakuwa heri, kwa maana watakula matunda ya matendo yao.”“Ole wake mtu mbaya; shari itakuwa

kwake, kwa maana atapewa ijara ya mikono yake" (Isaya 3:10, 11). "Ajapokuwa mwenye dhambi amefanya maovu mara mia," anasema mwenye hekima, "akazidisha siku zake; lakini hata hivyo najua hakika ya kwamba itakuwa heri kwao wamchao Mungu, wenye kicho mbele zake; walakini haitakuwa heri kwa mwovu" (Mhubiri 8:12, 13). Na Paulo anashuhudia kuwa mwenye dhambi anajiwekea "akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu, atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake;" "dhiki na shida juu ya kila nafsi ya mwanadamu atendaye uovu" (Warumi 2:5, 6, 9).

"Hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu" (Waefeso 5:5). "Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao" (Waebrania 12:14). "Heri wazifuao nguo zao, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake. Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi, na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya" (Ufunuo 22:14, 15).

Mungu ametoa tamko kwa wanadamu kuhusu tabia Yake na mbinu Yake ya kushughulikia dhambi. "Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe." "Wakosaji wataangamizwa pamoja, Wasio haki mwisho wao wataharibiwa" (Zaburi 145:20; 37:38). Uwezo na mamlaka ya serikali ya Mungu vitatumika kukomesha uasi; lakini udhihirisho wote wa adhabu ya haki utapatana kikamilifu na tabia ya Mungu ambaye ni mwenye rehema, mvumilivu, na mkarimu.

Mungu halazimishi nia au uamuzi wa mtu ye yote. Yeye hafurahii utii usiotumia akili. Anatamani kuwa viumbe wa mikono Yake wampende kwa sababu anastahili kupendwa. Angependa kuwaona wakimtii kwa sababu wametambua kwa kutumia akili zao wenyewe kuwa Mungu ni mwenye hekima, haki, na ukarimu. Na wote walio na utambuzi sahihi wa sifa hizi watampenda kwa sababu wanavutwa Kwake kwa kuvutiwa na sifa Zake.

Kanunizaukarimu, rehema, naupendo, zilizofundishwana Mwokoziwetu akazionesha kwa vitendo na, ni nakala ya mapenzi na tabia ya Mungu. Kristo alisema kuwa hakufundisha chochote kile isipokuwa kile tu alichokipokea kutoka kwa Baba Yake. Kanuni za serikali ya Mungu zinapatana kikamilifu na kanuni ya Mwokozi, "Wapendeni adui zenu." Mungu anatekeleza hukumu juu ya waovu kwa manufaa ya ulimwengu wote, na hata kwa wale ambao hukumu inatekelezwa juu yao. Angeweza kuwafanya wawe na furaha ikiwa angeweza kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria za serikali Yake na haki ya tabia Yake. Anawazungushia viashiria vya upendo Wake, anawapa fursa ya kuijua sheria Yake, na anawafuatilia kwa kuwapa fursa ya rehema Yake; lakini wanadhihaki upendo Wake, wanahesabu sheria Yake

kuwa si kitu, na wanatupilia mbali rehema Yake. Wakati daima wakipokea zawadi Zake, wanamkosea heshima Mtoaji; wanamchukia Mungu kwa sababu wanajua anachukia dhambi zao. Bwana anavumilia sana ukengeufu wao; lakini saa ya uamzi itafika hatimaye, wakati mustakabali wao utakapoamriwa. Je, atawakamata hawa waasi na kuwafunga kwa mnyororo upande Wake? Je, atawalazimisha kufanya mapenzi Yake?

Wale ambao wamemchagua Shetani kuwa kiongozi wao na wanatawaliwa na nguvu yake hawako tayari kuingia katika uwepo wa Mungu. Kiburi, uongo, anasa, ukatili, vimejengeka katika tabia zao. Je, wanaweza kuingia mbinguni na kuishi milele na wale ambao waliwadhihaki na waliwachukia duniani? Ukweli kamwe hautakubalika kwa mtu muongo; unyenyekevu hautamridhisha mtu mwenye kujiinua na mwenye kiburi; utakatifu haukubaliki kwa mtu aliye fisadi; upendo usio na upendeleo haumvutii mtu mchoyo. Mbingu itakuwa na chanzo gani cha furaha kwa watu ambao mawazo yao yote yanatafuta mambo ya kidunia na maslahi ya kichoyo?

Ikiwa wale ambao maisha yao yametumiwa katika uasi dhidi ya Mungu wangepelekwa kwa ghafla mbinguni na kushuhudia hali ya juu na takatifu ya ukamilifu ambao daima uko pale,—kila roho ikiwa imejazwa kwa upendo, na kila uso uking'ara kwa furaha, muziki wa kufurahisha wenye sauti tamu ukiinuka juu kwa heshima ya Mungu na Mwanakondoo, na miale ya nuru ikimwagwa juu ya waliokombolewa kutoka katika uso Wake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi,—je, wale ambao mioyo yao imejaa chuki dhidi ya Mungu, na dhidi ya ukweli na utakatifu wangeweza kuchanganyika na mkutano huo wa mbinguni na kujiunga nao kuimba nyimbo za sifa?

Je, wangeweza kustahimili utukufu wa Mungu na wa Mwanakondoo? Hapana, hapana; miaka ya rehema ilitolewa kwao, ili waweze kujenga tabia za mbinguni; lakini hawakufundisha akili kupenda utakatifu; hawakujifunza lugha ya mbinguni, na sasa muda wao wa kujifunza umeshapita. Maisha ya uasi dhidi ya Mungu hayawapi sifa ya kuishi mbinguni. Usafi wake, utakatifu wake, na amani yake vingekuwa mateso kwao; utukufu wa Mungu ungekuwa moto ulao kwao. Wangetamani kukimbia kutoka mahali pale patakatifu. Wangekuwa tayari kukaribisha kifo, ili wafichwe wasiuone uso Wake Yeye aliyekufa ili awakomboe. Hatima ya waovu inaamriwa na uchaguzi wao wenyewe. Kutokwenda mbinguni kwa waovu ni hiari yao wenyewe, na ni haki na rehema ya Mungu.

Kama maji ya Gharika ya Nuhu, moto wa siku kuu ya mwisho hutangaza hukumu kuwa waovu hawaponyeki. Hawana mwelekeo wa kujisalimisha kwa mamlaka ya Mungu. Nia yao ilitumika kuasi; na maisha yao yanapokoma, tayari wameshachelewa kugeuza mwelekeo wa mawazo yao katika upande wa kinyume chake, wamechelewa kuacha makosa na kuwa watiifu, kuacha chuki na kuwa na upendo.

Katika kuhifadhi maisha ya Kaini mwuaji, Mungu alitoa mfano kwa ulimwengu kile ambacho kingekuwa matokeo ya kumruhusu mwenye dhambi aendelee kuishi maisha ya uovu usiodhibitiwa. Kwa njia ya mvuto wa mafundisho ya Kaini na ya mfano wake, umati mkubwa wa uzao wake uliongozwa kuishi maisha ya dhambi, hadi "maovu ya mwanadamu yakawa makubwa duniani" na "kila kusudi analowaza moyoni mwake likawa baya tu sikuzote." "dunia ikaharibika mbele za Mungu, dunia ikajaa dhuluma" (Mwanzo 6:5, 11).

Kwa kuuhurumia ulimwengu, Mungu alifutilia mbali wakazi wa dunia waovu wa wakati wa Nuhu. Kwa rehema Zake, Mungu aliwaangamiza wakazi wa Sodoma. Kwa njia ya nguvu ya uongo wa Shetani, watendaji wa uovu huungwa mkono na kuvutia watu, na kwa njia hiyo daima wanawaongoza wengine kufanya uasi. Ilikuwa hivyo katika siku za Kaini na ilikuwa hivyo katika siku za Nuhu, na ilikuwa hivyo katika siku za Ibrahimu na Lutu; na iko hivyo wakati wetu. Ni kwa sababu ya rehema kwa ajili ya ulimwengu Mungu atawaangamiza, hatimaye, wote wanaotupilia mbali neema Yake.

"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu"(Warumi 6:23). Wakati uzima ni urithi wa wenye haki, mauti ni mshahara wa waovu. Musa aliwatangazia Waisraeli: "nimekuwekea leo mbele yako uzima na mema, na mauti na mabaya" (Kumbukumbu 30:15). Mauti inayozungumziwa katika maandiko haya siyo ile aliyotangaziwa Adamu, kwa kuwa wanadamu wote wanapata adhabu ya kosa lake. Hii ni "mauti ya pili" ambayo ni kinyume na uzima wa milele.

Kufuatia dhambi ya Adamu, mauti ilirithishwa hadi kwa jamii yote ya wanadamu. Wote kwa pamoja wanaenda kaburini. Na kupitia fursa ya mpango wa wokovu, wote wataletwa kutoka katika makaburi yao. "Kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia;" "kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa" (Matendo 24:15; 1 Wakorintho 15:22). Lakini tofauti imewekwa kati ya matabaka haya mawili ya watu wanaofufuliwa. "Watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu" (Yohana 5:28, 29). Wale ambao watakuwa "wamehesabiwa kustahili" kufufuliwa kwa ajili ya uzima wanaitwa "heri na watakatifu.""Juu ya hao mauti ya pili haina nguvu"(Ufunuo 20:6).

Lakini wale ambao, kwa njia ya msamaha na imani, hawakupata msamaha, itawapasa kupata adhabu ya dhambi yao—"mshahara wa dhambi." Wanapata adhabu inayotofautiana katika urefu wa muda na uzito wake, "kwa kadiri ya matendo yao," lakini hatimaye wakiishia katika mauti ya pili. Kwa kuwa haiwezekani kwa Mungu, kulingana na matakwa ya haki na rehema Yake, kumwokoa mwenye dhambi na dhambi zake, Mungu hampi maisha ambayo dhambi zake zimempokonya na ambayo amethibitika kutostahili kuwa nayo. Mwandishi aliyevuviwa anasema: "Maana bado kitambo kidogo asiye haki hatakuwapo, Utapaangalia mahali pake wala hatakuwapo." Na mwingine anatangaza: "Nao watakuwa kana kwamba

hawakuwa kamwe" (Zaburi 37:10; Obadia 16). Wakiwa na aibu, wanazama katika upotevu usio na matumaini, wa milele.

Huo ndio utakuwa mwisho wa dhambi, pamoja na tabu na uharibifu uliotokana nayo. Anasema mtunga zaburi: "Umewakemea mataifa; Na kumwangamiza mdhalimu; Umelifuta jina lao milele na milele; Adui wamekoma na kuachwa ukiwa milele" (Zaburi 9:5, 6). Yohana, katika Ufunuo, akitazama mbele hadi katika maisha ya umilele, anasikia wimbo wa ulimwengu wote wa sifa bila kuharibiwa na noti moja iliyo nje ya mwafaka. Kila kiumbe mbinguni na duniani alisikika akimtukuza Mungu (Ufunuo 5:13). Hakutakuwa na roho hata moja iliyopotea itakayomkufuru Mungu ikihangaika katika maumivu ya moto usiokoma; hakuna wenye uhai masikini katika jehanamu watakaochanganya vilio vyao na nyimbo za waliokombolewa.

Juu ya kosa la msingi la hali ya asili ya kutokufa, limejengwa fundisho la ufahamu katika hali ya kifo—fundisho ambalo, sawa na mateso katika moto wa milele, liko kinyume na mafundisho ya Maandiko, kinyume na uelewa wenye mantiki, na kinyume na hisia zetu za ubinadamu. Kwa mujibu wa imani iliyoenea mahali pengi, waliokombolewa mbinguni wanajua yote yanayotokea duniani na hususani maisha ya marafiki zao ambao wamewaacha nyuma. Lakini ni kwa jinsi gani hili linaweza kuwa chanzo cha furaha kwa watu waliokufa kujua taabu za walio hai, kushuhudia dhambi zilizotendwa na wapendwa wao, na kuwaona wakikabiliana na huzuni, kukatishwa tamaa, na maumivu ya maisha? Ni kwa kiasi gani amani ya mbinguni ingefurahiwa na wale ambao walikuwa wakiwazunguka marafiki zao waliowaacha duniani? Na ni kwa kiasi gani inakera imani kuwa mara tu pumzi inapoondoka mwilini roho ya mtu asiyetubu inapelekwa moja kwa moja jehanamu! Na ni kiasi gani cha maumivu kinawapata wanaowaona marafiki zao wakienda makaburini bila maandalizi, kuingia katika mateso na dhambi ya milele! Wengi wamepata hali kuchanganyikiwa kwa sababu ya wazo hili linalosumbua akili.

Maandiko yanasema nini kuhusu mambo haya? Daudi anatangaza kuwa mwanadamu hana fahamu mautini. "Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, Siku hiyo mawazo yake yapotea" (Zaburi 146:4). Sulemani anatoa ushuhuda huo huo: "Walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lo lote.""Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja; wala hawana sehemu tena katika jambo lo lote lililofanyika chini ya jua.""kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe" (Muhubiri 9:5, 6, 10).

Wakati, kama jibu kwa sala yake, maisha ya Hezekia yalirefushwa kwa miaka kumi na tano, mfalme mwenye shukrani alimwimbia Mungu wimbo wa sifa kwa ajili ya rehema Yake kuu. Katika wimbo huu anaeleza sababu kwa nini anafurahia hivyo: "Kuzimu hakuwezi kukusifu; mauti haiwezi kukuadhimisha; Wale washukao shimoni hawawezi kuitarajia kweli yako. Aliye hai, naam, aliye hai, ndiye atakayekusifu, kama mimi leo" (Isaya 38:18, 19).

Theolojia inayofundishwa na watu mengi hueleza kuwa wenye haki waliokufa wako mbinguni, wakiwa wameingia katika raha na wakimsifu Mungu kwa ulimi ulio na hali ya kutokufa; lakini Hezekia hakuona mustakabali wenye utukufu kama huo mautini. Maneno yake yanapatana na ushuhuda wa mtunga zaburi: "Mautini hapana kumbukumbu lako; Katika kuzimu ni nani atakayekushukuru?""Sio wafu wamsifuo Bwana, Wala wo wote washukao kwenye kimya" (Zaburi 6:5; 115:17).

Petro katika Siku ya Pentekoste alieleza kuwa mzee Daudi "alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo." "Maana Daudi hakupanda mbinguni" (Matendo 2:29, 34). Ukweli kuwa Daudi yuko kaburini mpaka wakati wa ufufuo huthibitisha kuwa wenye haki hawaendi mbinguni wakati wanapokufa. Ni kwa njia ya ufufuo pekee, na kwa njia ya ukweli kuwa Kristo alifufuka, ambapo Daudi anaweza hatimaye kuketi mkono wa kuume wa Mungu.

Na Paulo alisema: "Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka. Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu. Na hapo wao nao waliolala katika Kristo wamepotea" (1 Wakorintho 15:16-18). Ikiwa kwa miaka elfu nne wenye haki walikuwa wanakwenda moja kwa moja mbinguni wakati wa kufa, Paulo angesemaje kuwa ikiwa hakuna ufufuo, "wao nao waliolala katika Kristo wamepotea"? Ufufuo usingekuwa wa muhimu.

Mfia dini Tyndale, akizungumzia hali ya wafu, alisema: "Ninakiri wazi wazi, siamini kuwa tayari wako katika utukufu kamili ambao Kristo anao, au walionao malaika wateule wa Mungu. Wala sio fundisho mojawapo la imani yangu; kwani ikiwa ingekuwa hivyo, bila shaka kuhubiri ufufuo wa mwili kungekuwa jambo lisilo na maana yoyote ile."—William Tyndale, Preface to New Testament (ed. 1534). Reprinted in British Reformers—Tindal, Frith, Barnes, page 349.

Ni ukweli usiokanushika kuwa tumaini la mbaraka wa kutokufa wakati wa kufa limesababisha watu wengi kupuuzia fundisho la Biblia kuhusu ufufuo. Mwelekeo huu ulitolewa maelezo na Dkt Adam Clarke, akisema: "Fundisho la ufufuo linaonekana kuwa lilikuwa muhimu zaidi kwa Wakristo wa awali kuliko ilivyo hivi sasa! Hili limetokeaje? Mitume walikuwa wakilisisitizia, na wakiwahamasisha wafuasi wa Mungu kuwa na bidii, utii, na furaha kupitia fundisho hilo. Lakini warithi wao wa siku hizi kwa nadra sana hulitaja! Mitume walihubiri hivyo, na Wakristo wa awali waliamini hivyo; kadhalika sisi tukihubiri hivyo, wasikilizaji wetu wataamini hivyo. Hakuna fundisho katika injili ambalo limepewa mkazo mkubwa zaidi kama hili; na hakuna fundisho katika mfumo wa sasa wa mahubiri ambalo limepuuzwa zaidi kuliko hili!"—Commentary, remarks on 1 Corinthians 15, paragraph 3.

Jambo hili limeendelea kuwepo mpaka ukweli wenye utukufu wa ufufuo umefunikwa na umepotea machoni pa ulimwengu wa Kikristo. Kwa hiyo mwandishi mashuhuri wa kidini,

akifafanua maneno ya Paulo katika 1 Wathesalonike 4:13-18, anasema: “Kwa makusudi ya matumizi ya kila siku, fundisho la hali iliyobarikiwa ya kutokufa ya wenye haki inachukua, kwa ajili yetu, nafasi ya fundisho lo lote lenye mashaka la ujio wa pili wa Bwana. Wakati wa kufa kwetu Bwana anakuja kutuchukua. Hilo ndilo tunalopaswa kulingojea na kukesha kwa ajili yake. Waliokufa tayari wameshaingia katika utukufu. Hawasubiri tarumbeta kwa ajili ya hukumu na kubarikiwa.”

Lakini muda mfupi kabla ya kuwaacha wanafunzi Wake, Yesu hakuwaambia kuwa wangekwenda Kwake mara moja.“Naenda kuwaandalia mahali,” Yesu alisema. “Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu” (Yohana 14:2, 3). Na Paulo anatueleza, kwa kina zaidi, kuwa “Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.” Na anaongeza: “Farijianeni kwa maneno hayo” (1 Wathesalonike 4:16-18).

Tofauti kubwa iliyoje kati ya maneno haya ya faraja na maneno ya mchungaji anayeamini kuwa wokovu ni kwa wote bila kujali hali zao za kiroho ambaye maneno yake yalinukuliwa katika kurasa zilizotangulia! Huyu wa pili aliwafariji marafiki zake waliofiwa kwa kuwapa uhakika kuwa, hata kama aliyekufa angekuwa mwenye dhambi nyingi kiasi gani, alipotoa pumzi yake ya mwisho ya maisha angepokelewa na kuishi miongoni mwa malaika. Paulo anawaelekeza ndugu zake mbele kwa wakati ujao wa ujio wa Bwana wakati vifungo vya kaburi vitakapovunjwa, na “waliokufa katika Kristo” watakapofufuliwa ili waishi milele.

Kabla mtu ye yote hajaingia katika majumba ya waliobarikiwa, kesi zao lazima zipelelezwe, na tabia zao na matendo yao lazima yapitishwe mbele ya Mungu kwa ajili ya uchunguzi. Wote ni lazima wahukumiwe kulingana na mambo yaliyoandikwa katika vitabu na wapewe malipo sawasawa na kazi zao zilivyokuwa. Hukumu hii haifanyiki wakati wa kufa. Zingatia maneno ya Paulo: “Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu” (Matendo 17:31). Hapa mtume alisema wazi wazi kuwa muda mahsusi, wakati ule ukiwa ni wa baadaye, ulikuwa umepangwa kwa ajili ya hukumu ya ulimwengu.

Yuda anazungumzia wakati huo huo: “Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu.” Na, tena, Yuda ananukuu maneno ya Henoko: “Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote”(Yuda 6, 14, 15). Yohana anatangaza kuwa aliwaona “wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; … na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu” (Ufunuo 20:12).

Lakini waliokufa tayari wanafurahia raha ya mbinguni au wanahangaika katika ndimi za moto wa jehanamu, hukumu ya wakati ujao ni ya nini tena? Mafundisho ya neno la Mungu kuhusu vipengele hivi muhimu ni ya wazi na wala hayapingani; yanaweza kueleweka kwa akili za kawaida. Lakini ni akili gani iliyo makini inaweza kuona ama hekima au haki katika nadharia iliyopo sasa? Je, wenye haki, baada ya upelelezi wa kesi zao wakati wa hukumu yao, watapokea maneno ya pongezi, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu: ... ingia katika furaha ya Bwana wako," wakati watakuwa wameishi mbele Yake, pengine kwa zama nyingi? Je, waovu wanaitwa kutoka mahali pa maumivu yao motoni wapokee hukumu kutoka kwa Jaji Mkuu wa dunia yote: "Ondokeni kwangu, ninyi mliolaaniwa, nendeni katika moto wa milele"? (Mathayo 25:21, 41). Aha, dhihaka kubwa! Ukosoaji wa aibu wa hekima na haki ya Mungu!

Nadharia ya hali ya kutokufa kwa roho ilikuwa moja ya mafundisho ya uongo ya Roma, yaliyotoka katika upagani. Martin Lutha aliweka fundisho hili miongoni mwa "hekaya za kutisha zilizokuwa sehemu ya rundo la barua zenye mamlaka ya kipapa."—E. Petavel, The Problem of Immortality, ukurasa 255. Akitoa ufafanuzi wa maneno ya Sulemani katika Mhubiri, wafu hawajui neno lolote, Mwanamatengenezo anasema: "Mahali pengine panapothibitisha kuwa wafu hawana... hisia. Anasema, kule hakuna wajibu, hakuna sayansi, hakuna maarifa, hakuna hekima. Sulemani anatoa hitimisho kuwa waliokufa wamelala usingizi, na hawana hisia zozote. Kwa kuwa wafu wamelala pale, bila kuhesabu siku wala miaka, lakini watakapoamshwa, wataonekana kama wamelala muda usiozidi hata dakika moja."—Martin Luther, Exposition of Solomon's Booke Called Ecclesiastes, ukurasa 152. Kabla haijakatika kamba ya fedha; Au kuvunjwa bakuli la dhahabu; Au mtungi kuvunjika kisimani; Au gurudumu kuvunjika birikani;

Hakuna mahali popote katika Maandiko ambapo tunapata kauli kuwa wenye haki wanakwenda mahali pa zawadi yao au kuwa waovu wanakwenda mahali pa adhabu yao wakati wa kufa. Wazee na manabii hawakuacha uhakika wa aina hiyo. Kristo na mitume Wake hawakutoa dokezo lolote kuhusiana na hilo. Biblia inafundisha wazi kuwa wafu hawaendi mara moja mbinguni. Wanaoneshwa kuwa wamelala usingizi mpaka wakati wa ufufuo (1 (Wathesalonike 4:14; Ayubu 14:10-12). Siku ile kamba ya fedha inapokatika na bakuli la dhahabu kuvunjwa (Mhubiri 12:6), mawazo ya mtu hupotea. Wanaokwenda chini kaburini wapo katika ukimya. Hawajui jambo lolote linalotendeka chini ya jua (Ayubu 14:21).

Pumziko lenye baraka kwa wenye haki waliochoka! Wakati, uwe mrefu au mfupi, ni kufumba na kufumbua tu kwao. Wanalala usingizi; wataamshwa na tarumbeta ya Mungu ili wapokee hali ya kutokufa yenye utukufu. "Maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa. Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, Mauti imemezwa kwa kushinda" (1 Wakorintho 15:52- 54). Wanapoamshwa kutoka katika usingizi wao mzito

wanaanza kufikiri kuanzia pale walipoishia. Hisia ya mwisho ilikuwa ya maumivu ya kifo; wazo la mwisho, kuwa walikuwa wakianguka chini ya nguvu ya kaburi. Wanapoamka kutoka kaburini, wazo la furaha la kwanza litasikika kama mwangi wa kelele za ushindi: “Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?” (Aya ya 55).

Sura ya 34 - Je, Wafu Wetu Wanaweza Kuongea Nasi?

Huduma ya malaika watakatifu, kama ilivyoelezwa katika Maandiko, ni ukweli unaofariji na wa thamani sana kwa kila mfuasi wa Kristo. Lakini fundisho la Biblia juu ya mada hii limefunikwa na kupotoshwa na makosa ya theolojia inayokubaliwa na watu wengi. Fundisho la hali ya asili ya kutokufa, lililoazimwa kwanza kutoka katika falsafa ya kipagani, na katika giza nene la uasi likaingizwa katika imani ya Kikristo, limechukua nafasi ya ukweli, ambao umefundishwa wazi katika Maandiko, kuwa "wafu hawajui neno lo lote." Watu wengi wamefikia kuamini kuwa ni roho za watu waliokufa ambazo ni "roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu." Imefikia kueleweka hivyo licha ya ushuhuda wa Maandiko kuhusiana na uwepo wa malaika wa mbinguni, na mshikamano wao na historia ya mwanadamu, kabla ya kifo cha mwanadamu.

Fundisho la ufahamu wa mwanadamu katika hali ya kifo, hususani imani kuwa roho za watu waliokufa hurudi kuwatumikia watu walio hai, limeandaa njia kwa ajili ya imani ya kisasa ya kuwasiliana na mizimu. Ikiwa watu waliokufa wamekwenda kwa Mungu na kwa malaika watakatifu, na wakiwa na fursa ya maarifa makubwa zaidi waliyokuwa nayo kabla, kwa nini wasirudi duniani kuwaangazia na kuwafundisha walio hai? Ikiwa, kama inavyofundishwa na wanatheolojia walio wengi, roho za waliokufa zinaruka ruka juu ya rafiki zao walio duniani, kwa nini wasiruhusiwe kuwasiliana nao, kuwaonya dhidi ya uovu, au kuwafariji wakati wa huzuni? Inawezekanaje watu wanaoamini katika ufahamu wa mwanadamu aliyekufa wakatae kile kinachowajia kama nuru ya Kiungu iliyowasilishwa na roho zenye utukufu? Hapa kuna mfereji unaochukuliwa kama mfereji mtakatifu, ambao Shetani anautumia kutimiza makusudi yake. Malaika walioanguka wanaotekeleza maagizo yake hutokea kama wajumbe kutoka ulimwengu wa roho. Wakati wakidai kuleta walio hai katika mawasiliano na waliokufa, mfalme wa uovu anatumia nguvu zake za kichawi kuteka akili zao.

Ana uwezo wa kuleta mbele ya watu mfano wa marafiki zao waliokufa. Igizo linakuwa kamili; mwonekano uliozoeleka, maeneo, sauti, vinatokea kwa usahihi wa kushangaza. Wengi wanafarijika kuwa wapendwa wao wanafurahia uzuri wa mbinguni, na bila tahadhari ya hatari, wanasikiliza "roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani."

Wanapoongozwa kuamini kuwa waliokufa wanarudi kweli kuongea nao, Shetani anawezesha kutokea kwa wale waliozikwa makaburini bila kujiandaa kiroho. Wakitokea, wanadai kuwa wana furaha mbinguni na hata wanashika nyadhifa za juu huko, na kwa njia hiyo uongo unazidi kuenezwa ukifundishwa kuwa hakuna tofauti iliyopo kati ya wenye haki na waovu. Wageni hao wa kuigiza kutoka ulimwengu wa pepo, wakati mwingine hutoa tahadhari na maonyo ambayo huweza kuwa sahihi kabisa. Ndipo, wakati kuaminiwa kunapojengeka, wageni hao huwasilisha mafundisho huwafanya watu wapoteze imani katika Maandiko. Kwa mwonekano wa kuwa na nia ya kuwaletea mambo mema marafiki zao wa

duniani, wanawafanya wauamini uongo wa hali ya juu sana. Ukweli kuwa wanasema baadhi ya mambo yaliyo ya kweli, wakati mwingine wanaweza kutabiri matukio ya wakati ujao, hufanya kauli zao ziwe na mwonekano wa kuaminiwa; na mafundisho yao ya uongo yanakubaliwa na watu wengi kwa urahisi, na huaminiwa bila maswali, kana kwamba ni ukweli mtakatifu sana wa Biblia. Sheria ya Mungu inawekwa pembeni, Roho wa neema anadhihakiwa, damu ya agano huhesabiwa kuwa kitu kisicho kitakatifu. Pepo wanakataa uungu wa Kristo na wanamweka Muumbaji katika daraja lao. Hivyo, katika joho jipya mwasi mkuu anaendesha vita yake dhidi ya Mungu, iliyoanzia mbinguni na kwa miaka elfu sita ameendelea kuifanya duniani.

Wengi hujaribu hueleza kuwa vitendo hivi vya maonesho ya pepo ni maigizo na viini macho tu vinavyofanywa na wahusika. Lakini, ingawa ni kweli kuwa viini macho vinaweza kuwazuga watu wakafikiri ni matukio ya kweli, huwa kunakuwepo, pia, matukio halisi yanayotokana na nguvu kubwa zaidi kuliko za mwanadamu wa kawaida. Milio ya kugonga-gonga inayosikika bila kujua inatokea wapi ambayo imani ya kuwasiliana na mizimu ilianza nayo haikuwa matokeo ya ujanja au viini macho, bali ilikuwa kazi ya moja kwa moja ya malaika waovu, ambao walianzisha moja ya mambo ya uongo unaoharibu roho kwa ufanisi mkubwa sana. Wengi watanaswa kwa kuamini kuwa imani ya kuongea na mizimu ni udanganyifu wa kibinadamu pekee; wanapokutana uso kwa uso na matukio ambayo hawawezi kuyachukulia vinginevyo zaidi ya kuamini kuwa ni zaidi ya nguvu za kibinadamu, watadanganywa, na watajikuta wakiongozwa kuyapokea kama nguvu kuu ya Mungu.

Watu hawa wanapuuza ushahidi wa Maandiko kuhusu maajabu yanayofanywa na Shetani na mawakala wake. Ilikuwa kwa msaada wa kishetani ambapo wachawi wa Farao waliwezeshwa kuigiza kazi ya Mungu. Paulo anathibitisha kuwa kabla ya kuja kwa Kristo mara ya pili, kutakuwepo matukio ya nguvu za kishetani zinazofanana na hizo. Kuja kwa Kristo mara ya pili kutatanguliwa na "kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu" (2 Wathesalonike 2:9, 10). Na mtume Yohana, akieleza utendaji kazi wa miujiza katika siku za mwisho, anasema: "Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya " (Ufunuo 13:13, 14). Hapa siyo wadanganyaji wanaotabiriwa kuwa watafanya ishara. Watu watadanganywa kwa miujiza itakayofanywa na mawakala wa Shetani wenye nguvu ya kuifanya, siyo wanaoigiza kuifanya.

Mfalme wa giza, ambaye kwa muda mrefu anaelekeza nguvu za akili yake kufanya mambo ya uongo, kwa ufundi mkubwa akipanga majaribu yake kulingana na tabaka na hali mbali mbali za watu. Kwa wasomi na watu wenye uelewa mpana anawasilisha imani ya kuongea na mizimu katika namna ambayo imeboreshwa na kuwa ya kisasa, na hivyo anafanikiwa sana kuwavuta watu katika mtego wake. Hekima ambayo hutolewa na imani ya kuongea na mizimu ni ile ambayo imeelezwa na Yakobo, ambayo "siyo ile ishukayo kutoka

juu, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani" (Yakobo 3:15). Hii, hata hivyo, mdanganyaji mkuu anaficha pale ufichaji unapomsaidia kufanikisha malengo yake.

Yeye aliyeweza kutokea akiwa na nuru ya maserafi wa mbinguni mbele ya Kristo katika jangwa la majaribu, anakuja kwa watu katika namna inayovutia sana kama malaika wa nuru. Anashawishi akili kwa kuwasilisha mwonekano mzuri; anapenda ubunifu wa mandhari zinazosisimua; na anavutia watu wampende kwa njia ya maonesho fasaha ya upendo na ukarimu. Anaamsha fikra juu ya mambo ya makubwa, akiwaongoza kuwa na kiburi katika hekima yao ambapo katika mioyo yao wanamdhihaki Yeye aliye wa Milele. Yule kiumbe mwenye nguvu ambaye aliweza kumchukua Mwokozi wa ulimwengu hadi katika kilele cha mlima mrefu sana na kuleta mbele Yake falme zote za dunia na utukufu wa falme hizo, ataleta majaribu yake kwa watu katika namna ambayo ataharibu hisia za wote ambao hawana ulinzi wa nguvu ya Mungu.

Shetani anawadanganya watu kama alivyomdanganya Hawa kwa ghiliba, kwa kuamsha shauku ya kupata ujuzi uliokatazwa, kwa kuamsha tamaa ya kujiinua. Ilikuwa kupalilia maovu haya kulikosababisha anguko lake, na kwa njia ya maovu hayo analenga kuangamiza watu. "Nanyi mtakuwa kama Mungu," alisema, "mkijua mema na mabaya" (Mwanzo 3:5). Imani ya kuongea na mizimu inafundisha "kuwa mwanadamu ni kiumbe wa maendeleo; kwamba ni lengo lake tangu anapozaliwa kuendelea, hata hatimaye afikie, hadi umilele, hadi Uungu." Na tena: "Kila mtu ataamua mwenyewe na siyo mwingine." "Hukumu itakuwa sahihi, kwa sababu ni hukumu ya nafsi yake mwenyewe.... Kiti cha enzi kimo ndani yako mwenyewe." Mwalimu wa imani ya kuongea na mizimu alisema, "ufahamu wa kiroho" ulipoamka ndani yake: "Ndugu zangu, wote walikuwa nusu miungu ambayo haijaanguka." Mwalimu mwingine anatangaza kuwa: "Kila kiumbe mwenye haki na aliye mkamilifu ni Kristo."

Hivyo, badala ya haki na ukamilifu wa Mungu asiyekuwa na kikomo, ambaye ndiye anapaswa kutukuzwa; badala ya haki kamilifu ya sheria Yake, kiwango cha kweli cha upeo wa kibidamu, Shetani ameweka asili ya mwanadamu mwenyewe mwenye dhambi na anayekosea kuwa kitu pekee cha kutukuzwa, kanuni pekee ya hukumu, au kiwango cha tabia. Haya ni maendeleo, lakini siyo ya kwenda juu, bali ya kwenda chini.

Ni sheria ya kiakili na ya asili ya kiroho kuwa kwa kutazama tunabadilika. Akili, pole pole inabadilika na kupatana na mambo ambayo imeruhusiwa kuyatafakari. Inajiunga na kile ambacho imezoea kukipenda na kukiheshimu. Mwanadamu hawezi kuinuka juu kuliko kiwango cha usafi au wema au ukweli. Ikiwa nafsi ndiyo kitu cha juu sana kwake, hatainuka juu zaidi ya kitu ambacho kiko juu ya nafsi yake. Badala yake, atakuwa kila wakati akififikiria kuzama chini na chini zaidi. Ni neema ya Mungu pekee iliyo na nguvu ya kumwinua mwanadamu. Mwanadamu akiachwa peke yake, njia yake lazima ielekee chini tu.

Kwa mtu mwenye kujipenda, mpenda anasa, mwenye tamaa za mwili, imani ya kuongea na mizimu hujitokeza kwa uwazi zaidi kuliko kwa mtu mstaarabu na msomi zaidi; katika muundo usio wa kistaarabu zaidi wanapata mambo ambayo wana mwelekeo wa kuwa na mwafaka nayo zaidi. Shetani anasoma kila kiashiria cha udhaifu katika asili ya mwanadamu, anaona viashiria vya dhambi ambazo kila mtu ana mwelekeo wa kuzitenda, na ndipo huhakikisha kuwa fursa zinakuwepo za kutosha kukidhi huo mwelekeo wa uovu. Anawajaribu watu kuzidisha kile ambacho chenyewe ni halali, na kuwafanya, kwa kutokuwa na kiasi, kudhoofisha nguvu yao wa kimwili, kiakili, na kimaadili. Ameharibu na anaharibu maelfu ya watu kwa njia ya uchu na tamaa za mwili, na kwa njia hiyo kuharibu utu wa mtu. Na kuhitimisha kazi yake, anasema, kupitia pepo kuwa "ujuzi wa kweli humweka mwanadamu juu ya sheria zote;" kuwa "chochote kile, ni sahihi;" kuwa "Mungu hakikatazi;" na kuwa "dhambi zote zilizotendwa hazina hatia."

Watu wanapoongozwa kwa njia hiyo kuamini kuwa hamu ndiyo sheria ya juu kabisa, kuwa uhuru ni kuipuuza sheria, na kuwa mwanadamu anawajibika kwa nafsi yake mwenyewe, ni nani anayeweza kushangaa kuwa ufisadi na uhalifu vimeenea kila mahali? Watu wengi hupokea mafundisho yanayowaacha huru kutii misukumo ya myoyo isiyozaliwa upya. Uwezo wa kujitawala unaachwa kupelekeshwa na tamaa za mwili, nguvu za akili na roho zinawekwa chini ya mamlaka ya mielekeo ya kinyama, na Shetani kwa furaha anafagilia katika wavu wake maelfu ya wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo.

Lakini hakuna mtu anayelazimika kudanganywa na madai ya uongo ya imani ya kuongea na wafu. Mungu ameupatia ulimwengu nuru ya kutosha kuwawezesha kugundua mtego. Kama ilivyokwisha kuoneshwa, nadharia ambayo ni msingi hasa wa imani ya kuongea na wafu inashindana na kauli za wazi za Maandiko. Biblia inatangaza kuwa wafu hawajui neno lo lote, kuwa mawazo yao yamepotea; hawana sehemu yo yote katika mambo yanayotokea chini ya jua; hawajui lo lote la furaha au huzuni la wale waliokuwa wapendwa sana duniani.

Zaidi ya hapo, Mungu amekataza moja kwa moja mawasiliano bandia na watu waliokufa. Katika siku za Waebrania kulikuwepo na tabaka la watu waliodai, kama wanavyodai leo kuamini katika mawasiliano na wafu, kuwa huwa wanaongea na wafu. Lakini "roho za utambuzi," kama wageni hawa kutoka ulimwengu mwingine walivyoitwa, zinaelezwa na Biblia kuwa ni "roho za mashetani." (Linganisha na Hesabu 25:1-3; Zaburi 106:28; 1 Wakorintho 10:20; Ufunuo 16:14.) Kazi ya kushughulika na roho za utambuzi ilitangazwa kuwa chukizo kwa Bwana, na ilipigwa marufuku kabisa na adhabu ya mkosaji katika suala hili ilikuwa kifo. Walawi 19:31; 20:27. Jina la uchawi kwa sasa linadharauliwa. Dai kuwa watu wanaweza kuongea na roho wachafu huchukuliwa kama hekaya za Zama za Giza. Lakini imani katika kuongea na wafu, ambayo wafuasi wake wanafikia mamia ya maelfu, ndiyo, hata mamilioni, ambayo imeshaingia katika ulimwengu wa sayansi, ambayo imevamia makanisa, na imekubaliwa na vyombo vya kutunga sheria, na hata katika ikulu za wafalme—uongo huu

mkubwa ni uamsho wa uchawi, katika joho jipya uliokatazwa na kupigwa marufuku wakati ule wa zamani.

Ikiwa kusingekuwa na ushahidi mwingine wowote wa tabia halisi ya imani ya kuwasiliana na wafu, ingetosha kwa Mkristo kuwa roho za mashetani hazitofautishi kati ya haki na dhambi, kati ya mitume waungwana na safi wa Kristo na watumishi wa Shetani walio waovu sana. Kwa kusema kuwa watu waovu kabisa wako mbinguni, na wameinuliwa pale, Shetani anauambia ulimwengu: "Haidhuru jinsi mtu alivyo mwovu; haidhuru ikiwa unamwamini Mungu na unaiamini Biblia. Ishi upendavyo; mbinguni ni nyumbani mwako." Walimu wa imani ya kuongea na mizimu wanatangaza moja kwa moja: "Kila atendaye mabaya ni mwema machoni pa Bwana, naye huwafurahia watu hao, au, Mungu mwenye kuhukumu yuko wapi?" (Malaki 2:17). Neno la Mungu linasema: "Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu; watiao giza badala ya nuru, na nuru badala ya giza" (Isaya 5:20).

Mitume, wanapoigizwa na roho hizi zidanganyazo, wanaongozwa kupinga kile walichokiandika kwa uongozi wa Roho Mtakatifu walipokuwa duniani. Wanakanusha chimbuko la Kiungu la Biblia, na kwa njia hiyo wanavunja vunja msingi wa tumaini la Mkristo na kuzima nuru inayofunua njia ya kwenda mbinguni. Shetani anaufanya ulimwengu uamini kuwa Biblia ni riwaya tu, au angalau ni kitabu kilichofaa jamii changa, lakini sasa kitiliwe maanani kidogo tu, au kiwekwe pembeni kama kitabu kilichopitwa na wakati. Na kuchukua nafasi ya neno la Mungu huonesha utendaji wa imani ya kuongea na wafu. Hapa pana njia mawasiliano yaliyoko chini ya utawala wake kamili; kwa njia hii anaweza kuufanya ulimwengu uamini cho chote anachokitaka. Kitabu ambacho kitamhukumu na wafuasi wake anakiweka kivulini, mahali anapotaka kiwe; Mwokozi wa ulimwengu anamfanya aonekana kuwa kama mwanadamu wa kawaida. Na kama vile mlinzi wa Kirumi aliyelilinda kaburi la Yesu alivyosambaza taarifa za uongo ambazo makuhani na wazee waliwawekea midomoni ili kuthibitisha kutokufufuka Kwake, ndivyo waumini wa imani ya kuongea na wafu wanavyojaribu kufanya ionekane kuwa hakuna cho chote cha kimuujiza katika asili ya maisha ya Mwokozi. Baada ya kutafuta kumweka Yesu nyuma ya pazia, wanawaonesha miujiza yao, wakitangaza kuwa miujiza yao ni mikubwa zaidi kuliko kazi za Kristo.

Ni kweli kuwa imani ya kuongea na mizimu sasa inabadilisha muundo wake na, huku ikificha baadhi ya mambo yake mabaya, inajivika joho la Ukristo. Lakini matamko yake kutoka mimbarani na kupitia vyombo vya habari yamekuwa mbele ya umma kwa miaka mingi, na katika mambo haya tabia yake halisi inadhihirika. Mafundisho haya hayawezi kupingwa au kufichwa.

Hata katika muundo wake wa sasa, mbali na kustahili kuvumilika zaidi kuliko ilivyokuwa siku za nyuma, wakati huu imani ya kuongea na wafu ni ya hatari zaidi, kwa sababu ni uongo ambapo umepangwa kijanja zaidi. Wakati pale mwanzoni imani hii ilimkataa

Kristo na Biblia, kwa sasa inadai kumkiri Kristo na Biblia. Lakini Biblia inatafsiriwa katika namna ambayo inaufurahisha moyo usiozaliwa mara ya pili, wakati ukweli wake muhimu ukivurugwa ili usiwe na mguso. Upendo unachukuliwa kuwa sifa kuu ya Mungu, lakini unadhoofishwa hadi kuwa hisia dhaifu, na kuweka tofauti ndogo kati ya wema na uovu. Haki ya Mungu, makemeo Yake dhidi ya dhambi, matakwa ya sheria Yake takatifu, vinafichwa visionekane machoni pa watu. Watu wanafundishwa Amri Kumi kama kanuni zilizopitwa na wakati. Hadithi zinazopendeza, zinazochangamsha zinatia ganzi fahamu na kuwaongoza watu kuikataa Biblia kama msingi wa imani yao. Kristo anakataliwa kweli kweli kama alivyokataliwa kabla; lakini Shetani amepofusha macho ya watu kiasi kwamba uongo haugunduliwi.

Kuna watu wachache walio na utambuzi kamili wa nguvu ya imani ya kuongea na wafu na hatari ya kuwa chini ya mvuto wake. Wengi wanaichezea kukidhi udadisi wao. Hawaiamini na wangejazwa hofu dhidi ya kujazwa na wazo la kujiweka chini ya utawala wa roho za mashetani. Lakini wanathubutu kwenda uwanja uliokatazwa, na mharibifu mkuu anatumia nguvu yake juu yao dhidi ya nia yao. Wakijaribiwa tu kusalimisha akili zao chini ya uongozi wake, mara moja atawafanya kuwa mateka wake. Haiwezekani, kwa nguvu zao wenyewe, kupona kunaswa na mtego wake unaoteka, unaovutia. Ni nguvu ya Mungu pekee, inayotolewa kama jibu kwa ombi la imani, inayoweza kuziokoa roho hizi zilizonaswa.

Wote wanaojenga tabia ya dhambi, au wanaopalilia kwa makusudi dhambi inayojulikana, wanaalika majaribu ya Shetani. Wanajitenga na Mungu na ulinzi wa malaika Wake; wakati Shetani anapoleta uongo wake, hawana ulinzi na wanakuwa mawindo rahisi. Wale wanaojiweka hivyo katika nguvu yake wanatambua kidogo mahali ambapo njia yao itaishia. Baada ya kufanikisha anguko lao, mjaribu atawatumia kama mawakala wake kuwajaribu wengine na kuwaharibu.

Nabii Isaya anasema: "Na wakati watakapokuambia, Tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunong'ona; je! Haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? Je! Waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi" (Isaya 8:19, 20). Ikiwa watu wangekuwa tayari kupokea ukweli ambao umeelezwa wazi wazi katika Maandiko kuhusu asili ya mwanadamu na hali ya wafu, wangeweza kuona katika madai na vituko vya imani ya kuongea na wafu utendaji kazi wa Shetani kwa nguvu na ishara na miujiza ya uongo. Lakini badala ya kusalimisha uhuru unaopatana na moyo usioongoka, na kuachana na dhambi wanazozipenda, watu wengi hufumba macho yao wasiione nuru na kutembea katika hiyo nuru na wanasonga mbele, licha ya maonyo, wakati Shetani akisuka mitego yake kuwazunga pande zote, na wanakuwa mawindo yake. "Kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa," kwa hiyo "Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo" (2 Wathesalonike 2:10, 11).

Watu wanaopinga mafundisho ya imani za kuongea na wafu wanashambulia, siyo wanadamu peke yao, bali Shetani na malaika zake. Wameingia katika pambano dhidi ya mamlaka na nguvu na roho wachafu katika anga za juu. Shetani hatarudi nyuma hata inchi moja katika pambano isipokuwa tu asukumwe nyuma kwa nguvu ya wajumbe wa mbinguni. Watu wa Mungu wanapaswa kukabiliana naye, kama Mwokozi alivyokabiliana Naye, kwa maneno: "Imeandikwa." Shetani anaweza kunukuu Maandiko sasa kama alivyofanya katika siku za Kristo, na anapotosha mafundisho yake ili kuunga mkono uongo wake. Watu wanaoweza kusimama katika wakati huu wa hatari lazima waelewe wao wenyewe ushuhuda wa Maandiko.

Wengi watakutana na roho za mashetani wakiwa wamejigeuza na kujifanya ndugu au rafiki zao wapendwa waliokufa na wakifundisha mafundisho ya uongo wa hatari sana. Wageni hawa watagusa hisia zetu upendo na huruma na watatenda miujiza kuunga mkono maigizo yao. Inatupasa kujiandaa kusimama imara dhidi yao kwa ukweli wa Biblia kuwa wafu hawajui neno lo lote na kuwa hao wanaotokea ni roho za mashetani. Karibuni mbele yetu kuna "saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi" (Ufunuo 3:10). Wote wale ambao imani yao haina mizizi katika neno la Mungu watadanganywa na watashindwa na adui. Shetani "hufanya kazi kwa madanganyo yote ya udhalimu" kuwatawala wanadamu, na madanganyo yake daima yataongezeka. Lakini anaweza kufikia lengo lake pale tu wanadamu wanapojisalimisha wenyewe chini ya majaribu yake. Wale ambao wanatafuta kwa dhati ujuzi wa ukweli na wajitahidi kutakasa roho zao kwa njia ya uvumilivu, huku wakifanya kila wanachoweza kukifanya kujiandaa kwa ajili ya shindano, watagundua, kwa Mungu wa ukweli, ulinzi wa hakika. "Kwa kuwa umelishika neno la subira yangu, mimi nami nitakulinda" (aya ya 10), ni ahadi ya Mwokozi. Angeweza kumtuma kila malaika kutoka mbinguni kuwalinda watu Wake kuliko kuacha roho moja inayomtumaini Mungu ishindwe na Shetani.

Nabii Isaya anafunua uongo wa kutisha utakaokuja juu ya waovu, utakaowafanya wajihesabu kuwa salama dhidi ya hukumu za Mungu: "Tumefanya agano na mauti, tumepatana na kuzimu; pigo lifurikalo litakapopita, halitatufikia sisi; kwa maana tumefanya maneno ya uongo kuwa kimbilio letu, tumejificha chini ya maneno yasiyo kweli" (Isaya 28:15). Katika tabaka lililoelezewa hapa wamejumuishwa wale ambao katika ugumu wao wa kutokutubu wanajifariji kwa imani kuwa hakutakuwa na adhabu kwa mwenye dhambi; kwamba wanadamu wote, haidhuru jinsi walivyo mafisadi, wanatarajia kuinuliwa mbinguni, kuwa kama malaika wa Mungu.

Lakini bado, kwa mkazo zaidi, kuna wale ambao wanafanya agano na kifo na makubaliano na kuzimu, wanaokataa ukweli ambao Mbingu imeutoa kama ulinzi kwa ajili wenye haki katika siku ya taabu, na wanakubali hifadhi ya uongo inayotolewa na Shetani mahali pake—maigizo ya uongo wa imani ya kuongea na wafu.

Jambo la kushangaza kuliko maelezo ni upofu wa watu wa kizazi hiki. Maelfu ya watu hulikataa neno la Mungu kama lisilofaa kuaminiwa na kwa imani na shauku kubwa hupokea madanganyo ya Shetani. Wenye mashaka na wenye dhihaka hukemea ubaguzi wenye chuki wa wale wanaotetea imani ya manabii na mitume, na wanapotoka kwa kudharau matamshi makuu ya Maandiko kuhusu Kristo na mpango wa wokovu, na adhabu inavyokaribia kuja juu ya wale wanaoukataa ukweli. Yana athari kubwa sana kwa akili ambazo ni finyu, dhaifu, na zinazoamini ushirikina kiasi kwamba wahusika hawawezi kutambua madai ya Mungu na kutii maagizo ya sheria Yake. Wanakuwa na uhakika mkubwa, kwa kweli, kana kwamba wamefanya agano na kifo na wamekubaliana na kuzimu—kana kwamba wamejenga ukuta usiopenywa kati yao na adhabu ya Mungu. Hakuna jambo lo lote linaloweza kuamsha hofu zao. Wamejisalimisha kikamilifu katika mikono ya mjaribu, wameshikamana naye kwa karibu sana, na kujazwa na roho wake kikamilifu, kiasi kwamba hawana nguvu wala wazo la kutoka katika mtego wake.

Shetani kwa muda mrefu amekuwa akijiandaa kwa ajili ya juhudi yake ya mwisho ya kuudanganya ulimwengu. Msingi wa kazi yake ulijengwa kwa uhakikisho aliompa Hawa katika Bustani ya Edeni kuwa: "Hakika hamtakufa.""Siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya" (Mwanzo 3:4, 5). Kidogo kidogo amekuwa akiandaa kwa ajili ya udanganyifu mkubwa kwa kuanzisha imani ya kuongea na wafu. Hajafikia kilele cha mafanikio yake katika mipango yake; lakini itafikiwa katika sehemu ya mwisho ya wakati. Nabii anasema: "Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi" (Ufunuo 16:13, 14). Isipokuwa wale tu ambao wanatunzwa na nguvu za Mungu, kwa njia ya imani katika neno Lake, ulimwengu wote utatekwa na kuwa wahanga wa uongo wake. Watu wanabembelezwa ili wasinzie huku wakihatarisha usalama wao, ili hatimaye waamshwe tu na mvua ya hasira ya Mungu.

Bwana Mungu anasema: "Nami nitafanya hukumu kuwa ndiyo kanuni, na haki kuwa ndiyo timazi; na mvua ya mawe itachukulia mbali hilo kimbilio la maneno ya uongo, na maji yatapagharikisha mahali pa kujisitiri. Na agano lenu mliloagana na mauti litabatilika, tena mapatano yenu mliyopatana na kuzimu hayatasimama; pigo lifurikalo litakapopita, ndipo ninyi mtakapokanyagwa nalo" (Isaya 28:17, 18).

Sura ya 35 - Uhuru wa Dhamiri Watishwa

Ukatoliki sasa unaangaliwa na Waprotestanti kwa kukubalika zaidi kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma. Katika nchi ambazo Ukatoliki hauendelei kukua, na viongozi wa kipapa wanafanya kazi ya upatanisho ili kuwa na mvuto, kuna ongezeko la kutojali mafundisho yanayotenganisha makanisa yaliyofanya matengenezo na kanisa la kipapa; maoni yanaendelea kushika kasi kubwa, hata hivyo, hatutofautiani sana katika mambo ya msingi kama ambavyo imekuwa ikidhaniwa, na kuwa kupunguza kidogo upande wetu kutatuwezesha kuelewana vizuri zaidi na Rumi. Wakati ulikuwepo ambapo Waprotestanti walithamini sana uhuru wa dhamiri ambao ulikuwa umenunuliwa kwa gharama kubwa mno. Waliwafundisha watoto wao kuuchukia upapa na walishikilia kuwa kutafuta mapatano na Rumi ni kukosa utii kwa Mungu. Lakini ni mawazo tofauti sana yanayotolewa sasa!

Watetezi wa upapa wanatangaza kuwa kanisa limeharibika, na ulimwengu wa Uprotestanti una mwelekeo wa kukubali kauli hiyo. Wengi wanasisitiza kuwa siyo haki kulihukumu kanisa leo kwa machukizo na upuuzi uliofanywa na kanisa katika karne za kutokujua na giza. Wanatoa udhuru kwa ukatili wake kama matokeo ya ujinga wa nyakati zile na wanadai kuwa ustaarabu wa kisasa umebadilisha mawazo yake.

Je, watu hawa wamesahau madai ya kutokukosea yaliyotolewa kwa miaka mia nane na mamlaka hii yenye kiburi? Mbali kabisa na kuachwa, si dai hili lilithibitishwa katika karne ya kumi na tisa kwa mkazo mkubwa zaidi kuliko kabla ya hapo? Kama Rumi inavyodai kuwa "kanisa halijawahi kukosea; wala, kwa mujibu wa Maandiko, halitakosea kamwe" (John L. von Mosheim, Institutes of Ecclesiastical History, book 3, century II, part 2, chapter 2, section 9, note 17), linawezaje kuacha kanuni zilizoliongoza zama zilizopita?

Kanisa la kipapa halitaacha kamwe dai lake la kutokukosea. Yote ambayo limewahi kufanya katika mateso yake kwa watu wanaokataa mafundisho yake ya imani yasiyobadilika linayachukulia kuwa sahihi kabisa; na je, halitarudia matendo yake yale yale, ikiwa fursa itajitokeza? Hebu ngoja vizuizi vinavyowekwa sasa na serikali zisizokuwa za kidini viondolewe na Rumi irudi katika mamlaka yake ya awali, ndipo kutakuwa na uamsho wa haraka wa ukatili na mateso yake.

Mwandishi mashuhuri anasema hivyo kuhusiana na mtazamo wa kanisa la kipapa kuhusu uhuru wa dhamiri, na hatari zinazotishia hasa Marekani kutokana na mafanikio ya sera yake:"Kuna watu wengi wenye mwelekeo wa kutokuwa na hofu dhidi ya Ukatoliki wa Rumi ndani ya Marekani kuhusiana na ubaguzi wenye chuki na utoto. Watu kama hao hawaoni chochote katika tabia na mtazamo wa Urumi ambacho ni cha chuki dhidi ya taasisi zetu huru, au wala hawaoni cho chote kinachotisha katika ukuaji wake. Hebu, basi, kwanza tulinganishe baadhi ya kanuni za msingi za serikali ya Marekani na zile za Kanisa Katoliki.

“Katiba ya Marekani inatoa uhakika wa uhuru wa dhamiri. Hakuna jambo jingine linapendwa au la msingi zaidi kuliko hili. Papa Pius IX, katika Barua yake aliyoituma kwa Maaskofu wote wa Kanisa la Rumi ya Agosti 15, 1854, alisema: ‘Mafundisho au matamko ya kipuuzi na yenye makosa yanayotetea uhuru wa dhamiri ni moja ya makosa makubwa sana—ni mdudu mharibifu, miongoni mwa wengine, anayepaswa kuogopwa kuliko wengine wote katika dola.’ Papa huyo huyo, katika Barua yake kwa Maaskofu wote ya Desemba 8, 1864, aliwakemea ‘wale wanaodai uhuru wa dhamiri na uhuru wa ibada ya kidini,’ pia ‘wote wanaodai kuwa kanisa halipaswi kutumia nguvu.’

“Mwelekeo wa amani wa Roma katika nchi ya Marekani haumaanishi kuwa moyo wa Urumi umebadilika. Kanisa la Rumi limekuwa stahimilivu kwa kutokuwa na uwezo wa kufanya vinginevyo. Askofu O’Connor anasema: ‘Uhuru wa dini unavumiliwa tu mpaka pale ambapo kinyume chake kinaweza kutekelezwa bila kuhatarisha ulimwengu wa Kikatoliki.’... Askofu Mkuu wa St. Louis alisema wakati mmoja: ‘Uzushi na kukosa imani ni uhalifu; na katika nchi za Kikristo, kama ilivyo katika nchi za Italia na Hispania, kwa mfano, ambapo watu wote ni Wakatoliki, na mahali ambapo dini ya Kikatoliki ni sehemu muhimu ya sheria ya nchi, uzushi na kutoamini vinaadhibiwa kama uhalifu mwingine.’...

“Kila kadinali, askofu mkuu, na askofu katika Kanisa Katoliki anakula kiapo cha utii kwa papa, ambapo maneno haya hutokea: ‘Uzushi, watenganishaji, na waasi kwa bwana wetu aliyetajwa (papa), au wafuasi wake waliokwisha kutajwa, nitawatesa na kuwapinga kwa nguvu zangu zote.’”—Josiah Strong, Our Country, ch. 5, pars. 2-4. [Tazama Kiambatanisho kwa ajili ya Rejea zilizosahihishwa.]

Ni kweli kuwa kuna Wakristo halisi katika jumuia ya Kanisa Katoliki la Rumi. Maelfu katika kanisa wanamtukia Mungu kulingana na nuru yote waliyonayo. Hawaruhusiwi kusoma neno la Mungu, na kwa hiyo hawautambui ukweli. [Published in 1888 and 1911. Tazama Kiambatisho.] Hawajawahi kuona tofauti kati ya huduma hai inayotoka moyoni na mzunguko wa taratibu na kaida pekee. Mungu anawatazama watu hawa kwa huruma kama ya mama mzazi, watu walioelimishwa kama walivyo katika imani inayodanganya na isiyoridhisha. Atawezesha miale ya nuru kupenya giza nene linalowazunguka. Atawafunulia ukweli kama unavyopatikana ndani ya Yesu, na wengi watasimama pamoja na watu wa Mungu.

Lakini Urumi kama mfumo haupatani zaidi na injili ya Kristo sasa kuliko wakati mwingine wo wote katika kipindi cha zamani cha historia ya Urumi. Makanisa ya Kiprotestanti yapo katika giza kubwa, isipokuwa kama wangeweza kutambua dalili za nyakati. Kanisa la Kirumi linaona mbali katika mipango yake na mbinu zake za kiutendaji. Linatumia kila njia kupanua mvuto wake na kuongeza nguvu yake katika maandalizi ya mgogoro mkali na wa makusudi wa kurudisha utawala wake juu ya dunia, kuanzisha upya mateso, na kutengua mambo yote ambayo Uprotestanti umeyafanya. Ukatoliki unaendelea kupata nguvu kila upande. Angalia ongezeko la idadi ya makanisa yake na nyumba zake za

ibada katika nchi za Kiprotestanti. Angalia umaarufu wa vyuo na seminari zake katika Bara la Amerika, ambavyo hutumiwa sana na Waprotestanti. Angalia ukuaji wa kaida katika nchi ya Uingereza na jinsi watu wanavyorudi nyuma na kujiunga na Wakatoliki. Mambo haya yanapaswa kuamsha wasiwasi wa wote wanaothamini kanuni safi za injili.

Waprotestanti wamechezea na kuulea upapa; wamelegeza misimamo yao na kuacha baadhi ya mafundisho yao kiasi ambacho hata wafuasi wa upapa wenyewe wanashangaa kuona na wanashindwa kuelewa. Watu wanafumba macho yao kiasi kwamba hawaoni tabia halisi ya Urumi na hatari zinazotokana na ukuu wake. Watu wanahitaji kuamshwa ili kupinga madai ya adui huyu adui wa hatari dhidi ya uhuru wa kiraia na kidini.

Waprotestanti wengi wanadhani dini ya Kikatoki haivutii na ibada zake zimepoa, zikiwa na mizunguko isiyo na maana ya kaida. Hapa wanakosea. Wakati ambapo Urumi umejengwa juu ya udanganyifu, Urumi sio uigizaji usio na adabu na usio na weledi. Huduma ya kidini ya Kanisa la Kirumi ni kaida inayovutia sana. Maonesho yake ya kifahari na kaida zake za dhati hugusa sana hisia za watu na kunyamazisha sauti ya mantiki na dhamiri. Macho hufurahishwa. Makanisa makubwa ya kifahari, maandamano yanayovutia, mimbari za dhahabu, madhabahu za vito vya thamani, picha zenye ubora wa hali ya juu, na sanamu maridadi huvutia watu wote wanaopenda uzuri. Sikio nalo hutekwa. Muziki hauna mshindani. Noti tamu za ogani yenye sauti nzito, zikichanganywa na utamu wa sauti nyingi zinazopaa na kujaza kuba za juu na njia kati ya nguzo za makanisa yake makubwa, haziwezi kuacha kuifanya akili iwe na kicho na heshima.

Huu utukufu, ufahari, na usherehekeaji wa nje ambao hudhihaki tu shauku ya roho iliyoumizwa na dhambi, ni ushahidi wa ufisadi wa ndani. Dini ya Kristo haihitaji vivutio vyote hivyo ili ikubalike. Katika nuru inayong'aa kutoka katika msalaba, Ukristo wa kweli huonekana kuwa safi na unaopendeza kiasi kwamba hakuna mapambo ya nje yanayoweza kuongezea thamani yake ya kweli. Ni uzuri wa utakatifu, roho ya upole na ukimya, ambavyo ni vya thamani mbele za Mungu.

Uzuri wa mtindo sio lazima uwe kipimo cha fikra safi na za juu. Uelewa wa juu wa sanaa, uchaguzi bora wa mambo mazuri, mara nyingi huwa katika akili ambazo zimezama katika mambo ya kidunia na ya kimwili. Hutumiwa mara nyingi na Shetani kuwaongoza watu wasahau mambo muhimu ya kiroho, washindwe kuona mambo yajayo, maisha yanayokufa, kumwacha Msadizi asiyekuwa na kikomo, na kuishi kwa ajili ya dunia peke yake.

Dini ya nje inavutia kwa moyo usioumbwa upya. Ufahari na usherehekeaji wa ibada ya Kikatoliki una nguvu ya kurubuni, kuteka, ambayo kwa njia yake watu wengi wanadanganyika; na wanakuja kuliona Kanisa la Rumi kama lango la mbinguni. Ni wale tu ambao wamesimika miguu yao kikamilifu juu ya msingi wa ukweli, na ambao mioyo yao imeumbwa upya kwa Roho wa Mungu, wana kinga dhidi ya mvuto wake. Maelfu ya watu

ambao hawana ujuzi halisi wa Kristo wataongozwa kupokea maigizo ya utauwa ambayo hayana nguvu. Dini kama hiyo ndiyo watu walio wengi wanataka.

Dai la Kanisa la kuwa na haki ya kusamehe humwongoza Mrumi kuhisi kuwa ana uhuru wa kutenda dhambi; na huduma ya maungamo, ambayo isipokuwepo msamaha hautolewi, huwa na mwelekeo wa kupalilia uovu. Yeyote anayepiga magoti mbele ya mwanadamu aliyeanguka dhambini, na kufunua katika maungamo mawazo yake ya siri na fikra zake za moyoni, anashusha hadhi ya utu wake na kudhalilisha kila silika bora ya nafsi yake. Kwa kufunua dhambi za maisha yake kwa padri,—mwanadamu mkosaji, mwenye dhambi na anayekufa, na mara nyingi ambaye amenajisiwa kwa pombe na tamaa,—kiwango chake cha tabia hushuka chini, na matokeo yake anachafuka. Mawazo yake kuhusu Mungu hushushwa chini hadi kumfananisha Mungu na mwanadamu aliyeanguka, kwa kuwa padri husimama kama mwakilishi wa Mungu.

Ungamo hili linalodhalilisha la mwanadamu kwa mwanadamu ndiyo chemchemi ya siri ambapo mengi ya maovu hububujika ambayo yanachafua ulimwengu na kuundaa kwa ajili ya maangamizi yake ya mwisho. Hata hivyo, kwa mtu anayependa ubinafsi, inafurahisha zaidi, kuungama kwa mwanadamu mwenzake kuliko kufunua roho mbele ya Mungu. Ni jambo tamu kwa silika ya mwanadamu kufanya kitubio kuliko kuacha dhambi; ni rahisi zaidi kutesa mwili kwa magunia na upupu na minyororo inayoudhi kuliko kusulibisha tamaa za kimwili. Mzigo ni mzito ambao moyo usioongoka uko tayari kuubeba kuliko kuinama chini ya nira ya Kristo.

Kuna mfanano wa wazi kati ya Kanisa la Rumi na Kanisa la Kiyahudi wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo. Wakati Wayahudi walipokanyaga kisiri-siri kanuni ya sheria ya Mungu, walikuwa na juhudi kubwa katika kutunza miongozo yake, wakiibebesha matakwa na mapokeo yaliyofanya utii kuwa wa maumivu na mzigo. Kama Wayahudi alivyodai kuiheshimu sheria, ndivyo na Warumi nao wanavyodai kuuheshimu msalaba. Wanainua alama ya mateso ya Kristo, wakati katika maisha yao wanamkana Yeye ambaye msalaba unamwakilisha.

Waumini wa upapa huweka misalaba kwenye makanisa yao, kwenye madhabahu zao, na kwenye mavazi yao. Kila mahali panaonekana alama ya msalaba. Kila mahali unaheshimiwa kwa nje na kuinuliwa. Lakini mafundisho ya Kristo yanazikwa chini ya wingi wa mapokeo yasiyokuwa na maana, tafsiri potofu, na matakwa magumu. Maneno ya Mwokozi kwa Wayahudi waliong'ang'ania imani yao kupita kiasi, yanawafaa kwa uzito mkubwa zaidi viongozi wa Kanisa Katoliki la Rumi: "Wao hufunga mizigo mizito na kuwatwika watu mabegani mwao; wasitake wenyewe kuigusa kwa kidole chao" (Mathayo 23:4). Roho adilifu huwekwa katika hofu ya kudumu zikiogopa ghadhabu ya Mungu aliyekosewa, wakati viongozi wa kanisa wakiishi maisha ya anasa na ya uridhishaji wa tamaa za kimwili.

Ibada ya sanamu na mifupa, maombi kwa watakatifu waliokufa, na uinuaji wa papa ni mbinu za Shetani kuvuta akili za watu kutoka kwa Mungu na kutoka kwa Mwana Wake. Kutekeleza maangamizi yao, anajaribu kuvuta akili zao kutoka kwa Yule ambaye peke Yake wanaweza kupata wokovu. Atawaelekeza kwa kitu kingine cho chote kinachoweza kuwa badala ya Yeye aliyesema: "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28).

Ni juhudi ya kudumu ya Shetani kuwakilisha vibaya tabia ya Mungu, asili ya dhambi, na mambo halisi yaliyoko hatarini katika pambano kuu. Uongo wake hupunguza uwajibikaji kwa sheria ya Mungu na huwapatia watu leseni ya kutenda dhambi. Wakati huo huo anawafanya wawe na uelewa potofu wa Mungu ili wamtazame kwa hofu na chuki badala ya kumtazama kwa upendo. Ukatili ambao ni sehemu ya tabia yake mwenyewe anampakazia Mwumbaji; ukatili umewekwa katika mifumo ya dini na huoneshwa katika namna za ibada. Hivyo akili za watu zimepofushwa, na Shetani anawapata na kuwafanya mawakala wake dhidi ya Mungu. Kwa uwelewa potovu wa sifa za Mungu, mataifa ya kipagani waliongozwa kuamini kuwa kafara za wanadamu zilikuwa muhimu ili kupata fadhila ya Mungu; na ukatili wa kutisha ulitendeka chini ya mifumo mbalimbali ya ibada za sanamu.

Kanisa Katoliki la Rumi, likiunganisha mifumo mbalimbali ya upagani na Ukristo, na, kama ulivyo upagani, likiwakilisha vibaya tabia ya Mungu, limekumbatia siyo ukatili na uasi kidogo. Katika siku za utawala wa Rumi kulikuwepo na zana za kutesea watu kuwalazimisha wayakubali mafundisho yake. Kulikuwepo nguzo ya kutesea kwa ajili ya wale ambao walikataa kuyakubali madai yake. Kulikuweko mauaji ya halaiki kwa kiwango ambacho hakitajulikana mpaka yatakapofunuliwa katika hukumu. Viongozi wakuu wa kanisa walijifunza, chini ya Shetani bwana wao, kugundua njia ambazo zingewezesha kuleta mateso makali sana kwa kadiri ambavyo ingewezekana na kumaliza kabisa maisha ya mhanga. Katika matukio mengi ya mchakato huo kuunguza mtu kwa moto kulirudiwa-rudiwa kwa kiwango ambacho mwanadamu asingeweza kustahimili, mpaka mtu alipoacha kupigania uhai wake, na mteswaji alishangilia kukaribisha kifo kama suluhisho tamu.

Hayo ndiyo yalikuwa masahibu ya wapinzani wa Rumi. Kwa wafuasi wake, Kanisa lilikuwa na nidhamu ya viboko, njaa kali, maumivu makali ya mwili ya kila aina, yanayoumiza moyo. Ili kupata ukubali wa Mbingu, waliofanya toba walikiuka sheria ya Mungu kwa kukiuka sheria ya asili. Walifundishwa kutenganisha kile ambacho Mungu alikiumba kubariki ili kufurahisha maisha ya mwanadamu hapa duniani. Viwanja vya makanisa vina mamilioni ya wahanga waliotumia maisha yao bure wakijaribu kutiisha hisia zao za kimwili za asili, kudhibiti, kama jambo linalomchukiza Mungu, kila wazo na hisia ya huruma kwa viumbe wenzao.

Ikiwa tunatamani kuelewa ukatili wa makusudi wa Shetani, uliodhihirishwa kwa mamia ya miaka, siyo miongoni mwa wale ambao hawajawahi kusikia habari za Mungu, bali katikati

na katika ulimwengu wote wa Kikristo, tunapaswa kuangalia historia ya Urumi. Kwa njia ya mfumo huu mkubwa wa uongo mfalme wa uovu anafanikisha kusudi lake la kumkosea heshima Mungu na kuharibu maisha ya mwanadamu. Na kama tunavyoona jinsi anavyofanikiwa katika kujigeuza na kutekeleza kazi yake kupitia viongozi wa kanisa, tunaweza kuelewa vizuri zaidi kwa nini anaichukia sana Biblia. Ikiwa Kitabu hiki kitasomwa, rehema na upendo wa Mungu vitafunuliwa; itaonekana kuwa Mungu haweki hii mizigo mizito. Anachohitaji pekee ni moyo uliopondeka, roho ya unyenyekevu, ya utii.

Kristo hatoi mfano wowote katika maisha Yake kwa wanaume na wanawake kujifungia katika nyumba za watawa ili kufaa kuishi mbinguni. Hakuwahi kufundisha kuwa upendo na huruma lazima vidhibitiwe. Moyo wa Mwokozi ulibubujika upendo. Kwa kadiri mwanadamu anapokaribia ukamilifu wa uadilifu, hisia zake zinazidi kuwa makini zaidi, uwezo wake wa kutambua dhambi unakuwa na makali zaidi, na huruma yake kwa wanaotesaka inakuwa ya kina zaidi. Papa anadai kuwa anasimama mahali pa Kristo; lakini kwa jinsi gani tabia yake inafanana na Mwokozi? Je, Mwokozi alijulikana wakati wowote kuwasweka watu gerezani au kwenye kichanja cha kukatia watu shingo kwa sababu walikataa kumpa heshima kama Mfalme wa mbinguni? Je, sauti yake ilisikika ikiwahukumu watu kifo wale ambao hawakumpokea? Alipopuuzwa na watu wa kijiji cha Samaria, mtume alijazwa na hasira, na aliuliza : "Bwana, wataka tuagize moto ushuke kutoka mbinguni, uwaangamize; kama Eliya naye alivyofanya?" Yesu alimtazama mtume Wake na kumkemea kwa roho yake ya ukali, akisema: "Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa" (Luka 9:54, 56). Ni tofauti kubwa kiasi gani kati ya roho iliyodhihirishwa na Kristo na ile ya yule anayedai kuchukua mahali pa Kristo.

Kanisa la Roma sasa linawakilisha mwonekano wa haki kwa ulimwengu, likifunika kwa kuomba radhi kwa ajili ya kumbumbu zake za ukatili wa kutisha. Kanisa limejivika mwonekano unaofanana na wa Kristo; lakini bado halijabadilika. Kila kanuni ya upapa uliokuwepo katika zama zilizopita ipo pale pale leo. Mafundisho yaliyobuniwa katika zama za giza bado yanashikiliwa. Mtu yeyote asijidanganye. Upapa ambao Waprotestanti sasa wako tayari kuuheshimu ni ule ule uliotawala ulimwengu katika siku za Matengenezo, wakati watu wa Mungu waliposimama imara, wakihatarisha maisha yao, kuanika uovu wake. Kanisa bado lina kiburi kile kile na majivuno yale yale kama nyakati zile Kanisa lilipokuwa juu zaidi ya wafalme na wakuu wa nchi mbalimbali duniani, na lilipodai kuwa na mamlaka sawa na ya Mungu. Roho ya Kanisa haijaacha ukatili na ukandamizaji sasa kuliko wakati lilipovunja vunja uhuru wa binadamu na kuwaua watakatifu Wake Yeye Aliye Juu sana.

Upapa ni ule ule ambao unabii ulitangaza kuwa ungekuwa, uasi wa siku za mwisho (2 Wathesalonike 2:3, 4). Ni sehemu ya sera yake kuwa na tabia inayoweza kulisaidia kutekeleza kusudi lake; lakini chini ya mwonekano unaobadilika wa kinyonga Kanisa linaficha sumu isiyobadilika ya nyoka. "Imani haipaswi kuchanganywa na wazushi, wala watu wanaohisiwa kuwa na uzushi" (Lenfant, volume 1, page 516), Kanisa linasema. Je, mamlaka hii, ambayo

kumbukumbu yake ya miaka elfu moja imeandikwa katika damu ya watakatifu, ikubaliwe sasa kama sehemu ya kanisa la Kristo?

Sio kweli kuwa hakuna sababu ya msingi inayowafanya watu wa nchi za Kiprotestanti kutoa madai kuwa Ukatoliki hauna tofauti kubwa sana na Uprotestanti kuliko ilivyokuwa katika nyakati za zamani. Kumekuwepo na badiliko; lakini badiliko haliko katika upapa. Ni kweli kuwa Ukatoliki unafanana na Uprotestanti uliopo sasa, kwa sababu Uprotestanti umeporomoka sana tangu siku za Wanamatengenezo.

Makanisa ya Kiprotestanti yalipoanza kutafuta kukubaliwa na ulimwengu, ukarimu wa uongo ulifumba macho yao. Hawaoni isipokuwa kwamba ni vyema kuangalia wema katika uovu wote, na kama matokeo yasiyoepukika watafikia kuamini hatimaye kuwa uovu wote ni wema. Badala ya kusimama imara kutetea imani waliyoiamani iliyotolewa mara moja kwa watakatifu, kama walivyofanya zamani, sasa wanaomba msamaha kwa Rumi kwa maoni yao yasiyo na ukarimu kwa Kanisa la Kikatoliki, wakiomba msamaha kwa ubaguzi wao wenye chuki dhidi ya Kanisa Katoliki.

Tabaka kubwa, hata la wale wanasiounga mkono Urumi, wanajua kidogo sana kuhusiana na hatari inayotokana na mamlaka yake na mvuto wake. Wengi wanasisitiza kuwa giza la kiakili na kimaadili lililokuwepo katika Zama za Giza liliruhusu usambazaji wa mafundisho yake, ushirikina wake, na ukandamizaji wake, na kwamba akili nyingi zaidi za nyakati hizi za sasa, ueneaji wa jumla wa maarifa, na ongezeko la uhuru katika masuala ya dini huweka mazingira magumu kwa ajili ya uamsho wa kukosa uvumilivu na ukatili. Wazo lenyewe kuwa hali kama hiyo inaweza kutokea katika zama hizi za maendeleo ya elimu, sayansi, na teknolojia linadhihakiwa. Ni kweli kuwa nuru kubwa ya kiakili, kimaadili, na kidini, inaangazia kizazi hiki. Katika kurasa zilizo wazi za Neno Takatifu la Mungu, nuru kutoka mbinguni imeangaza ulimwenguni. Lakini inapaswa ikumbukwe kuwa kwa kadiri nuru kubwa inavyotolewa, ndivyo giza linavyozidi kuwa kubwa zaidi kwa wale wanaoipotosha na kuikataa nuru.

Usomaji wenye maombi wa Biblia ungewaonesha Waprotestanti tabia halisi ya upapa na ungewafanya wauchukie na kuukataa upapa; lakini wengi ni wenye hekima katika kiburi chao wenyewe kiasi kwamba hawahisi hitaji la kumtafuta Mungu kwa unyenyekevu ili waongozwe katika ukweli. Ingawa wanajivunia maarifa yao, hawajui cho chote kuhusu Maandiko wala uwezo wa Mungu. Wao wanacholilia ni kupata njia fulani ya kunyamazisha dhamiri zao, na kukidhi hitaji hilo wanatafuta mambo ambayo ni ya kiroho kidogo sana na ambayo yananyenyekesha kwa kiwango kidogo sana. Wanachotamani ni kupata mbinu ya kumsahau Mungu ambayo itaonekana kama mbinu ya kumkumbuka Mungu. Upapa umejipanga kukidhi mahitaji haya yote. Upapa umejiandaa kwa ajili ya matabaka yote mawili ya wanadamu, ukikumbatia karibu ulimwengu wote—wale ambao wanataka kuokolewa kwa matendo yao

mema, na wale ambao wanapenda kuokolewa wakiwa na dhambi zao. Hapa ndipo palipo siri ya nguvu yake.

Siku ya giza kubwa la kiakili imeonesha kuwa na msaada kwa mafanikio ya upapa. Itakuja kudhihirika pia kuwa siku ya nuru kubwa ya kiakili ni msaada mkubwa kwa mafanikio ya upapa. Katika zama zilizopita, watu walipokuwa hawana neno la Mungu na walipokuwa hawana maarifa ya ukweli, macho yao yalikuwa yamefumbwa, na maelfu walinaswa, kwa kutokuona wavu uliotandazwa kutega miguu yao. Katika kizazi hiki kuna wengi ambao macho yao yamepofushwa kwa mng'ao wa makisio ya kibinadamu, "sayansi kama inavyoitwa kwa uongo;" hawatambui wavu, na wanaingia katika wavu kirahisi kama vile hawana macho. Mungu alipanga kuwa uwezo wa kiakili wa mwandamu uchukuliwe kuwa zawadi kutoka Muumbaji wake na utumiwe katika huduma ya ukweli na haki; lakini kiburi na tamaa vinapopaliliwa, na wanadamu wanapoinua nadharia zao juu ya neno la Mungu, akili inaweza kufanya madhara makubwa zaidi kuliko ujinga. Hivyo basi, sayansi ya uongo ya siku hizi, ambayo inadhoofisha imani katika Biblia, italeta mafanikio makubwa katika maandalizi ya nje ya kuupokea upapa, na sherehe zake zinazofurahisha, kama kuzuia maarifa kulivyoleta mafanikio makubwa katika kufungua njia kwa ajili ya kujijengea umaarufu wake katika Zama za Giza.

Katika harakati zinazoendelea sasa katika nchi ya Marekani za kupata kwa ajili ya taasisi na matumizi ya kanisa msaada wa serikali, Waprotestanti wanafuata nyayo za upapa. Hapana, zaidi, wanafungua mlango kwa ajili ya upapa kupata tena katika Amerika ya Kiprotestanti ukuu ambao upapa uliupoteza katika Ulimwengu wa Kale. Na kinachozipa harakati hizi uzito ni ukweli kuwa lengo kuu linalofikiriwa ni ulazimishaji wa utunzaji wa Jumapili— desturi iliyoanzishwa na Rumi, na ambayo Rumi inadai kuwa alama ya mamlaka yake. Ni roho ya upapa—roho ya kufuata desturi za kidunia, kuheshimu mapokeo ya kibinadamu juu zaidi kuliko amri za Mungu—ambayo inapenya na kuenea katika makanisa ya Kiprotestanti na kuwaongoza kufanya kazi ile ile ya kuiinua Jumapili kazi ambayo upapa ulikwisha kuifanya kabla yao.

Ikiwa msomaji anataka kuwaelewa mawakala watakaotumiwa katika pambano ambalo linakuja karibuni, anachopaswa kufanya ni kufuatilia kumbukumbu za njia ambazo Rumi ilizitumia kwa makusudi hayo hayo katika zama zilizopita. Ikiwa anataka kujua jinsi wadau wa upapa na Waprotestanti kwa pamoja watakavyoshughulika na wale waliokataa mafundisho yao, hebu na aangalie roho ambayo Rumi ilionesha kwa Sabato na watetezi wa Sabato. Maagizo ya kifalme, mabaraza makuu, na sheria za kanisa zilizotekelezwa kwa mamlaka za kiserikali zilikuwa ngazi ambazo ziliwezesha siku kuu za kipagani kupata nafasi ya heshima katika ulimwengu wa Kikristo. Amri ya kwanza iliyolazimisha utunzaji wa Jumapili ilitungwa na Konstantino. (B.K. 321; tazama Kiambatisho maelezo kwa ajili ya ukurasa wa 53.) Amri hii iliwataka wakazi wa mijini kupumzika "siku ya heshima ya jua,"

lakini amri iliwaruhusu watu wa vijijini kuendelea na shughuli zao za kilimo. Japokuwa ni sheria ya kipagani kabisa, ililazimishwa na mfalme baada ya kupokea Ukristo kwa jina.

Wakati ambapo mamlaka ya kifalme haikuwa na uwezo wa kusimama badala ya mamlaka ya Mungu, Eusebius, askofu ambaye alitafuta kukubaliwa na wakuu wa kidunia, na ambaye alikuwa rafiki na kibaraka maalumu wa Konstantini, alitoa dai kuwa Kristo alikuwa amehamisha Sabato kutoka Jumamosi kwenda Jumapili. Hakuna aya ya Maandiko hata moja iliyotolewa kuthibitisha fundisho hilo jipya. Eusebius mwenyewe bila kujua anakiri uongo wake na anaelekeza kidole kwa waasisi halisi wa badiliko. "Mambo yote," anasema, "kila jambo ambalo lilikuwa wajibu kulifanya siku ya Sabato, yote haya tumeyahamishia katika Siku ya Bwana."—Robert Cox, Sabbath Laws and Sabbath Duties, ukurasa 538. Lakini hoja ya Jumapili, pamoja na kutokuwa na msingi wo wote, ilitumika kuwapa watu ujasiri katika kuikanyaga Sabato ya Bwana. Wote waliotamani kuheshimiwa na ulimwengu waliipokea siku kuu hiyo mpya ambayo ilitokea kuwa maarufu. Upapa ulipoimarika kikamilifu, kazi ya kuiinua Jumapili iliendelea.

Kwa muda fulani watu walijihusisha na kazi ya kilimo ikiwa hawakwenda kanisani, na siku ya saba ilikuwa bado ikichukuliwa kama Sabato. Lakini pole pole badiliko lilitekelezwa. Watu waliokuwa katika ofisi takatifu walikatazwa kupitisha hukumu katika shauri lolote la madai siku ya Jumapili. Muda mfupi baadaye, watu wote, wa daraja lo lote, waliamriwa kuacha kazi za kawaida kwa tishio kuumizwa kwa faini kwa watu walio huru na kwa viboko kwa watumwa. Baadaye, iliamuriwa kuwa watu matajiri walipaswa kuadhibiwa kwa kupoteza nusu ya utajiri wao; na mwisho, kuwa ikiwa wangekuwa wakaidi baada ya hatua hizo kuchukuliwa, wangefanywa watumwa. Watu wa madaraja ya chini wangeadhibiwa kwa kufukuzwa kabisa kutoka nchini na wasionekane tena humo maisha yao yote.

Miujiza pia ilihusishwa. Miongoni mwa maajabu mengine ilielezwa kuwa wakati mkulima ambaye alikuwa anataka kwenda kulima shamba lake siku ya Jumapili aliposafisha jembe lake la kukokotwa na ng'ombe kwa kipande cha chuma, kipande cha chuma kilinata kwenye kiganja cha mkono, na kwa miaka miwili kiling'ang'ania kiganjani mwake na alipaswa kukibeba kila mahali alikokwenda, "akiwa na maumivu makali na aibu."— Francis West, Historical and Practical Discourse on the Lord's Day, ukurasa wa 174.

Baadaye papa alitoa maagizo kuwa kila paroko katika kila parokia alipaswa kuwaonya wavunjaji wa Jumapili na kuwataka waende kanisani na kutoa maombi yao, vinginevyo wangejiletea majanga wao wenyewe na majirani zao. Baraza la Kanisa Katoliki lilitoa hoja, tangu wakati huo ambayo imetumiwa mahali pengi, hata na Waprotestanti, kuwa kwa sababu watu walipigwa na radi wakifanya kazi Jumapili, ni lazima Jumapili iwe Sabato. "Inaonesha," walisema maaskofu, "jinsi chuki ya Mungu ilivyokuwa kubwa kwa sababu ya kupuuza siku hii." Wito ulitolewa baada ya hapo kuwa mapadri na wachungaji, wafalme na wakuu, na watu wote waaminifu "wajitahidi sana na wawe makini kuhakikisha kuwa siku hii inarudishiwa

heshima yake, na, kwa ajili ya heshima ya Ukristo, ituzwe kwa kicho zaidi katika siku zinazokuja."—Thomas Morer, Discourse in Six Dialogues on the Name, Notion, and Observation of the Lord's Day, ukurasa 271.

Amri za mabaraza zikionekana na zikithibitika kutotosha, mamlaka za serikali za kidunia ziliombwa zitoe amri ambazo zingechochea hofu katika mioyo ya watu na kuwalazimisha kuacha kufanya kazi siku ya Jumapili. Katika kikao cha sinodi kilichokaa Rumi, maamuzi yote yaliyopita yalithibitishwa kwa nguvu nyingi na uzito mkubwa zaidi. Ziliingizwa katika sheria za kanisa na utekelezaji na mamlaka za kiraia karibu katika ulimwengu wote wa Kikristo. (Tazama Heylyn, History of the Sabbath, pt. 2, ch. 5, sec. 7.)

Bado kutokuwepo kwa mamlaka ya Maandiko kwa ajili ya utunzaji wa Jumapili kulileta sio usumbufu kidogo. Watu walihoji haki ya walimu wao kuweka pembeni tamko chanya la Yehova,"Siku ya saba ni Sabato ya Bwana Mungu wako," ili kuheshimu siku ya jua. Kufidia upungufu wa ushahidi wa Biblia, mbinu zingine zilikuwa za lazima. Mtetezi mwenye bidii wa Jumapili, ambaye karibu na mwisho wa karne ya kumi na mbili alitembelea makanisa ya Uingereza, alipingwa na mashahidi waaminifu kwa ajili ya ukweli; na kwa hiyo juhudi zake hazikuzaa matunda, hivyo, aliondoka nchini kwa muda na akatafutafuta njia ya kulazimisha mafundisho yake.

Aliporudi, mapengo yalizibwa, na katika juhudi zake baada ya hapo alipata mafanikio makubwa. Alileta gombo alilodai kuwa lilitoka kwa Mungu Mwenyewe, ambalo lilikuwa na amri iliyokuwa ikihitajika kwa ajili ya utunzaji wa Jumapili, kwa ajili ya kuwatishia na kuwatia hofu wasiokuwa watiifu. Waraka huu wa thamani— ambao ulikuwa wa kughushi kama amri yenyewe iliyoungwa mkono nao — ulidaiwa kuwa ulianguka kutoka mbinguni na ulikutwa Yerusalemu, kwenye madhabahu ya Mtakatifu Simeoni, kwenye mlima wa Golgotha. Lakini, kwa kweli, waraka ule ulitoka katika ikulu ya papa, Roma. Udanganyifu na kughushi ili kuendeleza mamlaka na mafanikio ya kanisa katika zama zote vimeonekana kuwa halali mbele ya mamlaka za kipapa.

Gombo lilikataza kufanya kazi kuanzia saa ya tisa, yaani saa tisa, Jumamosi mchana, mpaka mapambazuko siku ya Jumatatu; na mamlaka yake yalitangazwa kuwa yalithibitishwa kwa miujiza mingi. Ilitolewa taarifa kuwa watu waliofanya kazi zaidi ya saa zilizopangwa walipata ugonjwa wa kiharusi. Msagishaji wa mashine alipojaribu kusaga mahindi yake, aliona, badala ya unga, damu ikitiririka, na mashine ilitulia, licha ya bubujiko kubwa la maji. Mwanamke mmoja aliyeoka mikate katika oveni aliitoa ikiwa mibichi, ingawa oveni ilikuwa na joto kali. Mwingine aliyekuwa ameandaa madonge ya mikate, ilipofika saa tisa kabla ya kuioka, alidhamiria kuitunza mpaka Jumatatu alfajiri, ambapo aliikuta, siku iliyofuata, kuwa ilikuwa imeiva na ilikuwa imeokwa na nguvu ya Mungu. Mtu aliyeoka mikate baada ya saa tisa Jumamosi alikuta, alipoivunja asubuhi iliyofuata, kuwa damu ilivuja kutoka ndani ya mikate. Kwa maagizo hayo ya kipuuzi na kishirikina watetezi wa Jumapili walijaribu

kuonesha utakatifu wa Jumapili. (Tazama Roger de Hoveden, Annals, vol. 2, ukurasa 526-530.)

Katika nchi ya Scotland, kama ilivyokuwa katika nchi ya Uingereza, heshima kubwa zaidi kwa ajili ya Jumapili ilipatikana kwa kuiunganisha na sehemu ndogo ya Sabato ya zamani. Lakini wakati uliotakiwa kuheshimiwa kama wakati mtakatifu ulikuwa tofauti. Amri kutoka kwa mfalme wa Scotland ilitangaza kuwa "Jumamosi kuanzia saa sita mchana inatakiwa kuhesabiwa kuwa takatifu," na kuwa hakuna mtu tangu wakati huo mpaka Jumatatu asubuhi, anapaswa kujihusisha na shughuli za kidunia.—Morer, ukurasa 290, 291.

Lakini licha ya juhudi zote za kujenga utakatifu wa Jumapili, wadau wa upapa wenyewe walikiri hadharani mamlaka ya Kiungu ya Sabato na chimbuko la kibinadamu la Jumapili ambayo ilikuwa iwekwa badala ya Sabato ya Jumamosi. Katika karne ya kumi na sita baraza la papa lilitangaza wazi wazi: "Inawapasa Wakristo wote wakumbuke kuwa siku ya saba ilitakaswa na Mungu, na ilipokelewa na kutunzwa, sio tu na Wayahudi peke yao, bali pia na wengine wote wanaojifanya kumwabudu Mungu; japokuwa sisi Wakristo tulibadilisha Sabato yao na kuwa Siku ya Bwana."— Ibid., ukurasa 281, 282. Waliochezea sheria ya Mungu hawakuwa wajinga kuhusiana na kazi waliyofanya. Kwa makusudi walijiweka juu ya Mungu.

Kielelezo kizuri cha sera ya Rumi dhidi ya wale wanaopingana na Kanisa lao ni mateso ya muda mrefu na ya umwagaji damu ya Wawaldensia, ambao baadhi yao walikuwa watunza Sabato. Wengine waliteswa kwa jinsi hiyo hiyo kwa ajili ya uaminifu wao kwa amri ya nne. Historia ya makanisa ya Ethiopia na Abyssinia ni ya muhimu sana. Katikati ya utusitusi wa Zama za Giza, Wakristo wa Afrika ya Kati hawakuonwa na walisahauliwa na ulimwengu, na kwa karne nyingi walikuwa huru kutekeleza imani yao. Lakini hatimaye Rumi iligundua uwepo wao, na mfalme wa Abyssinia alihadaiwa kwa muda mfupi na kukiri kuwa papa alikuwa mwakilishi wa Kristo. Matukio mengine yalifuata. Amri ilitolewa iliyokataza utunzaji wa Sabato kwa tishio la adhabu kali. (Tazama Michael Geddes, Church History of Ethiopia, ukurasa 311, 312.)

Lakini ukatili wa papa muda si mrefu ulikuja kuwa mzigo unaoudhi sana kiasi kwamba watu wa Abyssiania waliazimia kuuondoa mabegani mwao. Baada ya pambano la kutisha Warumi walifukuzwa kutoka katika maeneo yao, na imani yao ya zamani ilirudishwa upya. Makanisa yalifurahia uhuru wao, na hawakusahau somo walilojifunza kuhusu udanganyifu, ushikiliaji sana mambo bila kutumia akili, na mamlaka ya kiimla ya Rumi. Ndani ya ufalme wao uliojitenga waliridhika kubaki bila kujulikana kwa ulimwengu uliobaki wa Kikristo.

Makanisa ya Afrika yalishika Sabato kama ilivyoshikwa na kanisa la papa kabla ya uasi kamili. Wakati ambapo walishika siku ya saba kutii amri ya nne ya Mungu, waliacha kazi siku ya Jumapili ili kwenda sawa na desturi ya kanisa. Baada ya kupata mamlaka ya juu

kabisa, Rumi ilikanyaga Sabato ya Mungu na kuinua Jumapili yake; lakini makanisa ya Afrika, yakiwa yamefichwa kwa karibu miaka elfu moja, hayakushiriki katika uasi huu.

Yalipoletwa chini ya utawala wa Rumi, yalilazimishwa kuacha Sabato ya kweli na kuinua sabato ya uongo; lakini haukupita muda mrefu baada ya kupata uhuru wao walirudia kuitii amri ya nne. (Tazama Kiambatisho.)

Kumbukumbu hizi za nyuma hufunua waziwazi uadui wa Rumi na Sabato ya kweli na watetezi wa Sabato ya kweli, na mbinu ambazo Roma inazitumia kuheshimu siku waliyoiweka wenyewe. Neno la Mungu linafundisha kuwa mandhari hizi zitarudiwa wakati Wakatoliki wa Rumi na Waprotestanti watakapoungana katika kuiinua Jumapili.

Unabii wa Ufunuo 13 hueleza kuwa mamlaka inayowakilishwa na mnyama mwenye pembe mbili mfano wa mwanakondoo ataifanya "dunia na wote wakaao ndani yake" wausujudie upapa—ambao katika unabii unawakilishwa na mnyama "mfano wa chui." Mnyama mwenye pembe mbili pia atawaambia "wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama;" na, zaidi ya hapo, atawaamrisha wote, "wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa," wapokee alama ya mnyama (Ufunuo 13:11-16).

Imeoneshwa kuwa nchi ya Marekani ndiyo mamlaka inayowakilishwa na mnyama mwenye pembe mbili mfano wa mwanakondoo, na kwamba unabii huu utatimizwa wakati nchi ya Marekani itakapolazimisha utunzaji wa Jumapili, jambo ambalo Rumi inadai kuwa utambuzi wa ukuu wake. Lakini katika heshima hii kwa upapa nchi ya Marekani haitakuwa peke yake. Nguvu ya Roma katika nchi ambazo wakati fulani zilikiri utawala wake bado haijaisha. Na unabii unatabiri urejeshwaji wa nguvu yake. "Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule" (Aya 3). Pigo la jeraha la mauti huwakilisha kuanguka kwa upapa mwaka 1798. Baada ya hili, nabii anasema, "pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule." Paulo anataja wazi wazi kuwa"mtu wa kuasi"ataendelea hadi wakati wa ujio wa pili (2 Wathesalonike 2:3-8).

Hadi mwisho wa wakati ataendelea na kazi yake ya kudanganya. Na nabii wa Ufunuo anaeleza, pia akizungumzia upapa: "Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima" (Ufunuo 13:8). Katika Ulimwengu wa Kale na Ulimwengu Mpya, upapa utasujudiwa kwa heshima itakayotolewa kwa agizo la Jumapili, ambayo imejengwa juu ya mamlaka ya Kanisa la Rumi. Tangu katikati ya karne ya kumi na tisa, wanafunzi wa unabii katika nchi ya Marekani wamekuwa wakitoa ushuhuda huu kwa ulimwengu. Katika matukio yanayotokea sasa kunaonekana maendeleo ya haraka kuelekea kutimizwa kwa utabiri. Kwa upande wa walimu wa Kiprotestanti kuna dai lile lile la mamlaka ya Kiungu ya utunzaji wa Jumapili, na kutokuwepo kule kule kwa ushahidi wa Kimaandiko, kama ilivyo kwa viongozi wa kipapa walioghushi miujiza ili kujaza pengo la kutokuwepo kwa amri ya Mungu. Dai kuwa hukumu za Mungu zinamwagwa juu ya watu

kwa kuvunja kwao sabato ya Jumapili, litarudiwa; tayari linaanza kusisitizwa. Na harakati za kulazimisha utunzaji wa Jumapili zinazidi kushika kasi.

Kanisa la Rumi ni la ajabu katika werevu na ujanja. Linaweza kusoma kile kitakachokuwa. Linasubiri wakati mzuri, likizingatia kuwa makanisa ya Kiprotestanti yanalisujudia Kanisa la Rumi kwa kukubali sabato yake ya uongo na kuwa wanajiandaa kuilazimisha kwa njia zile zile lilizotumia katika siku zilizopita. Wanaokataa nuru ya ukweli watatafuta msaada wa mamlaka hii iliyojiweka yenyewe ili kuinua Jumapili ambayo ilianzishwa na mamlaka yenyewe. Ni kwa haraka kiasi gani Kanisa la Rumi litakuja kutoa msaada kwa Waprotestanti katika kazi hii ambayo siyo ngumu kujua cha kufanya. Ni nani anayejua vizuri zaidi ya viongozi wa upapa jinsi ya kushughulika na wale ambao siyo watiifu kwa kanisa?

Kanisa Katoliki la Rumi, pamoja na taasisi zake zote ulimwenguni kote, huunda shirika moja kubwa chini ya udhibiti, na limebuniwa kukidhi maslahi ya, uongozi wa papa. Mamilioni ya waumini wake, katika kila nchi duniani kote, wanafundishwa kushikamana kwa pamoja katika utii kwa papa. Hata kama wana utaifa gani au wako chini serikali ipi, inawapasa kuchukulia kuwa mamlaka ya kanisa iko juu ya mamlaka zingine zote. Ingawa wanaweza kula kiapo cha utii kwa serikali zao, lakini nyuma yake kipo kiapo cha utii kwa Rumi, kikiwaondoa katika kila kiapo kilicho kinyume na maslahi ya Rumi.

Historia inathibitisha juhudi za Rumi zenye ustadi wa hali ya juu na uvumilivu mkubwa za kujipenyeza katika mambo ya serikali; na ikipata nafasi, kuendeleza makusudi yake, hata kwa kuwaua wakuu na watu. Mwaka 1204, Papa Innocent III alipata kutoka kwa Petro II, mfalme wa Aragoni, kiapo kifuatacho, ambacho si cha kawaida: “Mimi, Petro, mfalme wa Waaragoni, nakiri na kuahidi kuwa mwaminifu na mtiifu daima kwa bwana wangu, Papa Innocent, kwa warithi wake wa Kikatoli, na Kanisa la Rumi, na kwa uaminifu kuhifadhi ufalme wangu katika utii wake, kuilinda imani ya Kikatoliki, na kuwatesa wazushi.”—John Dowling, The History of Romanism, b. 5, ch. 6, sec. 55. Jambo hili linaafikiana na madai yanayohusu mamlaka ya kiongozi wa Kanisa la Rumi “kuwa ni halali kwake kuwapindua wafalme” na “kwamba anaweza kuondoa utii wa raia kutoka kwa watawala dhalimu.”—Mosheim, b. 3, cent. 11, pt. 2, ch. 2, sec. 9, note 17. (Tazama pia maelezo ya Kiambatisho kwa ajili ya ukurasa wa 447.)

Na ikumbukwe, ni majivuno ya Kanisa la Rumi kuwa halibadiliki. Kanuni za Gregori VII na Innocent III bado ndizo kanuni za Kanisa Katoliki la Rumi. Na kama lingekuwa na uwezo, lingeweza kutekeleza yote hayo kwa nguvu kama ilivyokuwa karne zilizopita. Waprotestanti wanajua kidogo kile wanachokifanya wanapopendekeza kukubali misaada ya Rumi katika kazi ya kuiinua Jumapili. Wakati wanajielekeza kutimiza kusudi lao, Rumi analenga kurudisha mamlaka yake, kufufua ukuu wake uliopotea. Acha kanuni ianzishwe katika nchi ya Marekani kuwa kanisa liweze kutumia au litawale nguvu ya dola; kuwa siku

kuu za kidini zilazimishwe kuwa sheria za kiserikali; kwa kifupi, kuwa mamlaka ya kanisa na dola itawale dhamiri, na ushindi wa Rumi katika nchi ya Marekani utakuwa umethibitishwa.

Neno la Mungu limetoa onyo la hatari inayokuja; acha onyo hili lisisikilizwe, na ulimwengu wa Waprotestanti utajifunza kile ambacho ni makusudi halisi ya Rumi, wakati ambao watakuwa wamechelewa kuepuka mtego. Kanisa la Rumi linaendelea kukua katika mamlaka yake kimya kimya. Mafundisho yanaendelea kueneza mvuto wake katika majengo ya kutunga sheria, katika makanisa, na katika mioyo ya watu. Linaendelea kurundika makanisa marefu na makali katika maeneo yaliyojificha ambayo ndani yake mateso yake ya zamani yatarudiwa. Kimya kimya na bila kushukiwa linaimarisha majeshi yake kuendeleza malengo yake ili wakati ukiwadia liweze kupiga. Linachohitaji ni kupata mazingira mazuri, na mazingira haya tayari linaendelea kutengenezewa. Siyo muda mrefu tutaona na tutahisi kusudi la Uroma ni nini. Ye yote atakayeliamini na kulitii neno la Mungu atapata aibu na mateso.

Sura ya 36—Pambano Linalotarajiwa Karibuni Tangu mwanzo kabisa wa pambano kuu mbinguni, kusudi la Shetani ni kupindua sheria ya Mungu. Ilikuwa kwa kusudi la kufanikisha jambo hili aliingia katika uasi dhidi ya Muumbaji wake, na ingawa alitupwa nje ya mbingu, anaendelea na vita ile ile duniani. Kudanganya wanadamu, na hatimaye kuwaongoza kuvunja sheria ya Mungu, ni lengo lake ambalo analitafuta kwa bidii sana. Iwe anafanikisha lengo hili kwa kutupilia mbali sheria yote kabisa, au kukataa sheria moja, matokeo ni yale yale hatimaye. Anayejikwaa "katika neno moja," anaonesha dharau kwa sheria yote; mvuto na mfano wake vipo upande wa uvunjaji wa sheria; na huwa "amekosa juu ya yote" (Yakobo 2:10).

Katika kutafuta kuonesha dharau kwa sheria ya Mungu, Shetani amepotosha mafundisho ya Biblia, na makosa hayo yameingizwa katika imani ya maelfu wanaodai kuamini Maandiko. Pambano kuu la mwisho kati ya ukweli na uongo ni shindano la mwisho la pambano la muda mrefu juu ya sheria ya Mungu. Tunaingia sasa katika vita hii—vita kati ya kanuni za Yehova na sheria za wanadamu, kati ya dini ya Biblia na dini ya hadithi za kubuni na mapokeo ya wanadamu.

Mawakala ambao wataungana dhidi ya ukweli na haki katika shindano hili sasa wako kazini. Neno takatifu la Mungu, ambalo limerithishwa kwetu kwa gharama kubwa ya mateso na damu, linathaminiwa kidogo sana. Biblia inaweza kupatikana kwa watu wote, lakini kuna watu wachache sana wanaoikubali kama mwongozo wa maisha. Ukafiri unatawala kwa kiwango kikubwa na cha kutisha, siyo katika ulimwengu pekee, bali pia kanisani. Wengi wameyakana mafundisho ambayo ni nguzo hasa za Imani ya Kikristo. Ukweli mkuu wa uumbaji kama ulivyowasilishwa na waandishi waliovuviwa, anguko la mwanadamu, upatanisho, na uendelevu wa sheria ya Mungu, vinakataliwa wazi wazi, ama sheria yote au sehemu yake, na ulimwengu unaodai kuwa wa Kikristo. Maelfu ya watu wanaojivuna kuwa

wenye hekima na walio huru huchukulia kuwa ni udhaifu kuiamini kabisa Biblia; wanafikiri kuwa ni ushahidi wa talanta ya juu na usomi wa hali ya juu kuyakataa Maandiko na kuupinga ukweli wake muhimu. Wachungaji wanawafundisha watu wao, na maprofesa na walimu wanawafundisha wanafunzi wao, kuwa sheria ya Mungu imebadilishwa au imefutwa; na wale wanaochukulia matakwa yake kuwa bado ni ya halali, yanayopaswa kutiiwa kama yalivyo, wanafikiriwa kuwa watu wa kudharauliwa au kudhihakiwa.

Kwa kuukataa ukweli, wanadamu wanamkataa Mwasisi wa ukweli. Kwa kuikataa sheria ya Mungu, watu wanaikana mamlaka ya Mtoa sheria. Ni rahisi kuchonga sanamu ya mafundisho ya uongo na nadharia za uongo sawa na kuchonga sanamu ya mti au jiwe. Kwa kuwasilisha vibaya sifa za Mungu, Shetani anawaongoza watu kumwelewa Mungu kwa tabia isiyokuwa sahihi. Kwa watu wengi, sanamu ya kifalsafa imewekwa juu ya kiti cha enzi badala ya Yehova; wakati Mungu aliye hai, kama alivyofunuliwa katika neno Lake, ndani ya Kristo, na katika kazi za uumbaji, anaabudiwa na watu wachache. Maelfu ya watu wanafanya vitu vya asili kuwa miungu yao huku wakimkataa Mungu wa vitu vya asili. Japokuwa ni katika miundo mbalimbali, ibada ya sanamu ipo katika ulimwengu wa Kikristo leo katika uhalisia wake kama ilivyokuwa miongoni mwa Waisraeli katika siku za Eliya. Mungu wa wengi wanaodai kuwa wenye hekima, wanafalsafa, watunzi wa mashairi, wanasiasa, waandishi wa habari—mungu wa wanamitindo, mungu wa vyuo na vyuo vikuu, hata mungu wa baadhi ya taasisi za kitheolojia—ni miungu isiyomzidi sana Baali, mungu jua wa Wafoinike.

Hakuna kosa ambalo likikubaliwa na ulimwengu wa Kikristo linapiga kwa ujasiri zaidi dhidi ya mamlaka ya Mbingu, hakuna kosa ambalo linapingana zaidi na busara tu ya kawaida, hakuna kosa lililo na matokeo mabaya zaidi, kuliko fundisho la kisasa, ambalo linaendelea kukubaliwa na watu wengi kwa kasi, kuwa sheria ya Mungu haiwafungi watu tena. Kila taifa lina sheria zake, ambazo zinaheshimiwa na kutiiwa; hakuna serikali inayoweza kudumu kuwepo ikiwa haina sheria; na inawezaje kuingia akilini kuwa Muumbaji wa mbingu na nchi hana sheria za kutawala viumbe aliowaumba? Hebu chukulia kuwa wachungaji mashuhuri waanze kufundisha hadharani kuwa sheria zinazotawala nchi na zinazotawala haki za wananchi si za lazima— kuwa zinabana uhuru wa watu, na hivyo hazipaswi kutiiwa; watu hao wangeweza kuvumiliwa kwa muda gani wakifundisha hivyo mimbarani? Lakini, je, ni kosa kubwa zaidi kupuuza sheria za nchi na za mataifa kuliko kukanyaga kanuni za Mungu ambazo ndiyo msingi wa serikali zote?

Ingekuwa afadhali kwa mataifa kuondoa sheria zao, na kuwaruhusu watu wafanye wanavyopenda, kuliko Mtawala wa sayari zote kubatilisha sheria Yake, na kuuacha ulimwengu bila kiwango cha kuhukumu mwenye hatia au kumpa haki mtiifu. Je, tungependa kujua matokeo ya kubatilisha sheria ya Mungu? Jaribio limeshawahi kufanywa. Matokeo yake yalikuwa ya kutisha kama nini katika nchi ya Ufaransa wakati ukanamungu ulipofanywa kuwa mamlaka ya utawala. Wakati huo ilidhihirika kwa ulimwengu kuwa kutupilia mbali vizuizi ambavyo Mungu ameviweka ni kuruhusu utawala wa ukatili wa watu katili. Kiwango

cha haki kinapoondolewa, njia inafunguliwa kwa ajili ya mfalme wa uovu kuimarisha mamlaka yake duniani.

Mahali popote sheria za Mungu zinapokataliwa, dhambi inaacha kuwa na ubaya na haki inakosa umuhimu na haitamaniwi. Wanaokataa kujisalimisha chini ya serikali ya Mungu hawafai kabisa kujiongoza wenyewe. Kwa njia ya mafundisho yao mabaya roho ya uasi inapandikizwa katika mioyo ya watoto na vijana, ambao kwa asili hawana uvumilivu wa kutawaliwa; na matokeo yake ni hali ya uasi na uvunjaji wa sheria katika jamii. Wakati wakidhihaki wepesi wa kuamini wale wanaotii matakwa ya Mungu, watu walio wengi wanapokea kwa furaha udanganyifu wa Shetani. Wanasalimisha hatamu zao kwa tamaa na wanatenda dhambi ambazo zinaleta hukumu juu ya wapagani. Wale ambao wanafundisha watu kuchukulia kwa wepesi amri za Mungu wanapanda mbengu ya uasi wavune matunda ya uasi. Acha kizuizi kilichowekwa na sheria ya Mungu kiondolewe kabisa, na sheria za wanadamu zitapuuzwa muda si mrefu.

Kwa kuwa Mungu anakataza matendo yasiyokuwa ya uaminifu, kutamani, kusema uongo, na kudanganya, wanadamu wako tayari kukanyaga amri za Mungu kama kikwazo cha kupata mafanikio ya kidunia; lakini matokeo ya kuondoa kabisa kanuni hizi yangekuwa tofauti kabisa na jinsi walivyotegemea. Ikiwa sheria haimbani mtu, kwa nini mtu ye yote aogope kuivunja? Mali isingeweza salama tena. Watu wangejipatia mali za jirani zao kwa mabavu, na walio na nguvu zaidi kuliko wengine ndiyo wangekuwa matajiri kuliko watu wote. Uhai wenyewe usingeheshimiwa. Kiapo cha ndoa kisingekuwa tena ngome takatifu ya kuilinda familia. Yule ambaye angekuwa na nguvu nyingi, angeweza, akipenda, kumchukua mke wa jirani yake kwa nguvu. Amri ya tano ingeondolewa na amri ya nne. Watoto wasingesita kuwaua wazazi wao ikiwa kwa kufanya hivyo wangeweza kupata mahitaji ya mioyo yao iliyoharibika. Ulimwengu uliostaarabika ungekuwa genge la majambazi na wauaji; na amani, utulivu, na furaha vingetoweka duniani.

Tayari fundisho kuwa watu wameachiliwa kutoka katika utii wa matakwa ya Mungu limedhoofisha nguvu ya uwajibikaji wa kiuadilifu na limefungulia mafuriko ya uovu ulimwenguni. Uasi, ubadhirifu, na ufisadi vinatufunika kama wimbi la maji. Katika familia, Shetani yuko kazini. Bendera yake inapepea hata katika nyumba zinazodai kuwa za Kikristo. Kuna kijicho, kuwazia mabaya wengine, unafiki, utengano, uadui, ugomvi, usaliti wa mambo matakatifu, uendekezaji wa tamaa mbaya. Mfumo mzima wa kanuni na mafundisho ya kidini, ambao ungeunda msingi na mwelekeo wa maisha ya kijamii, unaonekana kama bonge linaloyeyuka, linaloekea kutoweka. Wahalifu wakuu, wanapotupwa gerezani kwa makosa yao, mara nyingi wanapewa zawadi na kushabikiwa sana kana kwamba wamepata ushindi fulani mkubwa wa kuonewa wivu. Tabia yao na uhalifu wao unatanganzwa sasa. Vyombo vya habari vinatangaza uovu wao kwa kina, na kwa njia hiyo vinawafundisha wengine kufanya matendo ya wizi, unyang'anyi, na mauaji; na Shetani anashangilia mafanikio ya mipango yake ya kijehanamu. Kufurahia uovu, mauaji ya kikatili, ongezeko la kutisha la

kutokuwa na kiasi na uovu wa kila aina na wa kila kiwango, vyapaswa kuwaamsha wote wanaomcha Mungu, kujiuliza nini kifanyike kuzuia wimbi la uovu.

Mahakama zinapokea rushwa. Watawala wanasukumwa na tamaa ya mapato na kupenda anasa za mwili. Kukosa kiasi kumetia mawingu akili za wengi kiasi kwamba Shetani anawatawala karibu katika kila hali. Ulevi na sherehe, tamaa, kijicho, kukosa uaminifu kwa njia mbalimbali, vinawakilishwa miongoni mwa wale wanaosimamia sheria."Haki inasimama mbali sana; maana kweli imeanguka katika njia kuu, na unyofu hauwezi kuingia" (Isaya 59:14).

Uovu na giza la kiroho vilivyotawala chini ya himaya ya Rumi vilikuwa matokeo ya moja kwa moja ya kukandamiza Maandiko; lakini ni wapi tunapata chimbuko la ukafiri ulioenea kote, kuikataa sheria ya Mungu, na ufisadi unaofuata baada ya kuikataa sheria ya Mungu, chini ya nuru kamilifu ya injili katika zama za uhuru wa kidini? Sasa kwa kuwa Shetani hawezi kuendelea zaidi kuutawala ulimwengu kwa kuzuia Maandiko, anatumia njia zingine kutimiza lengo lile lile. Kuharibu imani kwa Biblia kunamsaidia Shetani kutimiza kusudi lake na kuharibu Biblia yenyewe. Kwa kuingiza imani kuwa sheria ya Mungu haimbani mtu, Shetani anawaongoza watu kirahisi kuivunja kana kwamba hawajui kanuni zake. Na sasa, kama ilivyokuwa katika zama za kale, amefanya kazi kupitia kanisa kuendeleza mipango yake.

Mashirika ya kidini ya leo yamekataa kusikiliza ukweli usiopendwa ulioelezwa wazi wazi katika Maandiko, na ili kuushinda huo ukweli wameupatia tafsiri na wameweka misimamo ambayo imepanda kila mahali mbegu za mashaka. Wakishikilia makosa ya kipapa ya asili ya kutokufa na ufahamu katika umauti, wamekataa ulinzi pekee dhidi ya madanganyifu ya imani ya kuongea na wafu. Fundisho la maumivu ya milele motoni limewafanya wengi kutoiamini Biblia. Na madai ya amri ya nne yanapoelezwa kwa watu, inaonekana kuwa utunzaji wa Sabato ya siku ya saba umeamriwa; na kama njia pekee ya kujinasua kutoka katika wajibu ambao hawako tayari kuufanya, walimu mashuhuri walio wengi hutangaza kuwa sheria ya Mungu haimbani mtu tena. Hivyo wanatupilia mbali sheria pamoja na Sabato. Kwa kadiri kazi ya matengenezo ya Sabato inavyopanuka, ukataaji huu wa sheria ya Mungu ili kuepuka madai ya amri ya nne utakuwa karibu na watu wote duniani. Mafundisho ya viongozi wa dini wamefungulia mlango ukafiri, imani ya kuongea na wafu, na dharau kwa sheria takatifu ya Mungu; na juu ya viongozi hawa kuna uwajibikaji wa kutisha kwa ajili ya uovu uliomo katika ulimwengu wa Kikristo.

Hata hivyo, tabaka hili hili wanadai kuwa ufisadi unaoenea kwa kasi unatokana na kunajisi kile kinachoitwa "sabato ya Kikristo," na kuwa ulazimishaji wa utunzaji wa Jumapili utaweza kuboresha zaidi maadili ya jamii. Dai hili linasisitizwa hasa hasa Amerika, mahali ambapo fundisho la Sabato ya kweli limehubiriwa sana. Hapa, kazi ya kiasi, moja ya matengenezo ya kimaadili na muhimu sana, mara nyingi inaunganishwa na vuguvugu la

Jumapili, na watetezi wa Jumapili wenyewe wanajinasibu kuwa wanafanya kazi ya kutetea maslahi ya jamii; na watu wanaokataa kuungana nao wanalaumiwa kama maadui wa kiasi na matengenezo. Lakini ukweli kuwa vuguvugu la kuendeleza uongo limeunganishwa na kazi ambayo kama ilivyo yenyewe ni nzuri, siyo hoja ya kuunga mkono uongo. Tunaweza kuificha sumu kwa kuichanganya na chakula kizuri, lakini hatubadilishi asili yake. Kinyume chake, imefanywa kuwa ya hatari zaidi, kwa kuwa ina uwezekano wa kumezwa na mtu bila habari. Ni moja ya mbinu za Shetani kuchanganya uongo na ukweli ili kuupa uongo uwezo wa kukubalika. Viongozi wa vuguvugu la Jumapili wanaweza kutetea matengenezo ambayo watu wanayahitaji, kanuni ambazo zinapatana na Biblia; lakini, kwa kuwa matengenezo haya yamechanganywa na takwa ambalo ni kinyume na sheria ya Mungu, watumishi Wake hawawezi kuungana nao. Hakuna jambo lolote linaloweza kuwahalalisha kwa kuacha amri za Mungu na badala yake kutii kanuni za wanadamu.

Kwa njia ya mafundisho mawili ya uongo, kutokufa kwa roho na utakatifu wa Jumapili, Shetani atawaweka watu chini ya madanganyifu yake. Wakati fundisho la kwanza linajenga msingi wa imani ya kuongea na wafu, fundisho la pili linajenga mshikamano wa kuikubali Rumi. Waprotestanti wa Marekani watakuwa mstari wa mbele katika kunyosha mikono yao kutoka upande mmoja hadi mwingine wa korongo refu kushikana mikono na imani ya kuongea na wafu; watavuka shimo kubwa kushikana mikono na mamlaka ya Kirumi; na chini ya mvuto wa muungano wa mamlaka tatu, nchi hii itafuata katika nyayo za Rumi katika kukanyaga haki za dhamiri.

Kwa kuwa imani ya kuongea na wafu inaigiza kwa karibu sana Ukristo wa jina wa wakati wetu, ina nguvu zaidi ya kudanganya na kunasa. Shetani mwenyewe ameongoka, kulingana na hali ya sasa ya mambo. Atatokea katika tabia na mwonekano wa malaika wa nuru. Njia ya wakala wa imani ya kuongea na wafu, miujiza itatendwa, wagonjwa wataponywa, na maajabu mengi yasiyokanushika yatafanywa. Na kwa kuwa pepo watadai kuwa wanaiamini Biblia, na kuonesha heshima kwa taasisi za kanisa, kazi zao zitakubaliwa kama udhihirisho wa nguvu ya Mungu.

Mstari unaogawa watu kati ya wanaojiita Wakristo na watu wasiomwamini Mungu kwa sasa hauonekani vizuri. Washiriki wa Kanisa wanapenda vitu ambavyo watu wa kidunia wanavipenda na wako tayari kujiunga nao, na Shetani ameazimia kuwaunganisha wote katika jumuiya moja na kwa njia hiyo aweze kuimarisha kazi yake kwa kuwaingiza watu wote katika imani ya kuongea na wafu. Waumini wa mfumo wa upapa, wanaojivunia miujiza kama ishara ya kanisa la kweli, watadanganywa kirahisi na nguvu hii inayotenda miujiza; na Waprotestanti, wakiwa wametupilia mbali ngao ya ukweli, nao pia watadanganywa. Waumini wa upapa, Waprotestanti, na watu wa kidunia wote kwa pamoja wataupokea mfano huo wa utauwa usiokuwa na nguvu ya Mungu, na wataona katika muungano huo vuguvugu kubwa la kuuongoa ulimwengu na uingizaji wa kipindi cha miaka elfu moja kilichosubiriwa kwa muda mrefu.

Kwa njia ya imani ya kuongea na wafu, Shetani ataonekana kama mfadhili wa jamii ya wanadamu, akiponya magonjwa ya watu, na akidai kuwasilisha mfumo mpya na wa juu zaidi wa imani ya kidini; lakini wakati huo huo anafanya kazi kama muuaji. Majaribu yake yanawaongoza wengi kwenda kuuawa. Kutokuwa na kiasi kunaondoa uwezo wa kufikiri vizuri; kupenda anasa, migogoro, na umwagaji damu hufuata. Shetani anapenda sana vita, kwa sababu vita vinaamsha mihemko mibaya zaidi kuliko yote kutoka rohoni na vinawafagilia wahanga wote katika umilele wakiwa na mwelekeo wa uovu na umwagaji damu. Ni kusudi lake kuchochea mataifa yapigane vita taifa moja dhidi ya taifa jingine, kwa sababu kwa njia hiyo anaweza kuhamisha akili ya watu isijishughulishe na kazi ya maandalizi ya kusimama katika siku ya Mungu.

Shetani hufanya kazi kupitia nguvu za asili kukusanya mavuno yake ya roho zisizojiandaa. Amejifunza siri za maabara ya ulimwengu, na anatumia nguvu zake zote kutawala nguvu za asili kwa kiwango kile ambacho Mungu anaruhusu. Aliporuhusiwa kumtesa Ayubu, ni kwa kasi kubwa kiasi gani kondoo, ngamia, ng’ombe, watumishi, nyumba, watoto, walifagiliwa mbali, janga moja likifuata jingine kama kwa dakika moja. Ni Mungu anayewakinga viumbe Wake na kuwazungushia wigo dhidi ya nguvu ya mwuaji. Lakini ulimwengu wa Kikristo umeonesha dharau kwa sheria ya Yehova; na Bwana atafanya vile ambavyo ameahidi kuwa atafanya—ataondoa mibaraka Yake duniani na ataondoa ulinzi Wake kwa wale wanaoasi dhidi ya sheria Yake na kuwafundisha na kuwalazimisha wengine kuasi kama wao. Shetani anawatawala wale wote ambao hawako chini ya ulinzi wa Mungu. Shetani anawapendelea na kuwafanikisha baadhi ili kuendeleza mipango yake, na atawaletea matatizo wengine na kuwaongoza watu kuamini kuwa ni Mungu anayewatesa.

Wakati akionekana kwa wanadamu kama mganga mkuu anayeweza kuponya magonjwa yao, ataleta magonjwa na majanga, hadi miji yenye wakazi wengi itabaki magofu na ukiwa. Hata sasa yuko kazini. Katika ajali na majanga katika bahari na katika nchi kavu, ajali za mioto mikubwa, katika vimbunga vikali na tufani ya mvua ya mawe ya kutisha, katika dhoruba, mafuriko, tufani, mawimbi ya kujaa na kupwa kwa bahari, na matetemeko ya ardhi, kila mahali na katika miundo maelfu, Shetani anatumia nguvu yako. Anafagia mazao yanayoelekea kukomaa, na njaa na hofu hufuata. Anaweka hewani harufu mbaya inayofisha, na maelfu huangamia kwa magonjwa. Matukio haya yatazidi kuwa ya mara kwa mara na ya kutisha zaidi. Mauti itakuwa juu ya mwanadamu na mnyama. “Dunia inaomboleza, inazimia,” “watu wakuu … wanadhoofika. Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele” (Isaya 24:4, 5).

Na ndipo mdanganyaji mkuu atawashawishi watu kuwa wanaomtumikia Mungu ndiyo chimbuko la majanga hayo. Tabaka ambalo limechokoza hasira ya Mbingu litatupia lawama kwa wale ambao utii wao kwa amri za Mungu ni kemeo la kudumu kwa wakosaji. Itatangazwa kuwa watu wanamkosea Mungu kwa kuvunja sabato ya Jumapili; kuwa dhambi imeleta majanga ambayo hayatakoma mpaka utunzaji wa Jumapili utakapotekelezwa kikamilifu; na

kuwa wale wanaowasilisha madai ya amri ya nne, na kwa njia hiyo kuharibu heshima kwa ajili ya Jumapili, ni wataabishaji wa watu, wakizuia urejeshwaji wao kwa upendeleo wa Mungu na mafanikio ya duniani. Kwa hiyo shitaka lililotolewa zamani na mtumishi wa Mungu litarudiwa na kwa sababu ambazo ni za msingi: "Ikawa, Ahabu alipomwona Eliya, Ahabu akamwambia, Je! Ni wewe, Ewe mtaabishaji wa Israeli? Naye akajibu, Si mimi niliyewataabisha Israeli; bali ni wewe, na nyumba ya baba yako, kwa kuwa mmeziacha amri za Bwana; nawe umewafuata mabaali" (1 Wafalme 18:17, 18). Wakati hasira ya watu itakapochochewa kwa mashitaka ya uongo, watafuata njia ya kutafuta kuwaua mabalozi wa Mungu sawa sawa na jinsi Waisraeli walioasi walivyotafuta kumuua Eliya.

Nguvu itendayo miujiza inayodhihirishwa kwa njia ya imani ya kuongea na wafu itaeneza mvuto wake dhidi ya wale wanaochagua kumtii Mungu kuliko wanadamu. Mawasiliano kutoka kwa roho za pepo yatatangaza kuwa Mungu amewatuma kuwashawishi wapinzani wa Jumapili kuhusu kosa lao, yakithibitisha kuwa sheria za nchi zinapaswa kutiiwa kama sheria ya Mungu. Watasikitika kwa sababu ya uovu mkubwa ulioko ulimwenguni na wataunga mkono ushuhuda wa viongozi wa dini kuwa hali ya maadili yaliyoporomoka imesababishwa na kunajisi Jumapili. Hasira kubwa itachochewa dhidi ya wote watakaokataa kukubali ushuhuda wao.

Sera ya Shetani katika mgogoro huu wa mwisho na watu wa Mungu ni ile ile aliyoitumia wakati wa uanzishaji wa pambano kuu mbinguni. Alieleza kwamba alikuwa akitafuta kuongeza uimara wa serikali ya Mungu, wakati kisirisiri alikuwa akielekeza juhudi zake zote kutafuta njia za kuipindua. Na kazi ile ile aliyokuwa akitafuta kuifanya aliwasingizia malaika watiifu kuwa ndio walikuwa wakiifanya. Sera ile ile ya udanganyifu imekuwa sifa ya historia ya Kanisa la Rumi. Linaeleza kuwa linafanya kazi kama mwakilishi wa Mbingu, wakati likitafuta kujiinua juu ya Mungu na kubadilisha sheria Yake. Chini ya utawala wa Rumi, wale waliouawa kwa ajili ya uaminifu wao kwa injili walilaumiwa kama watenda maovu; walitangazwa kuwa na mshikamano na Shetani; na kila njia inayowezekana ilitumika kuwafanya wadharauliwe, kuwafanya waonekane katika macho ya watu na hata kwao wenyewe kuwa ni wabaya kuliko wahalifu wote. Ndivyo itakavyokuwa hata sasa. Wakati akitafuta kuwaangamiza wale wanaoheshimu sheria ya Mungu, atasababisha washitakiwe kama wavunja sheria, kama watu wanaomkosea heshima Mungu na kuleta hukumu juu ya dunia.

Mungu halazimishi nia au dhamiri; lakini juhudi ya Shetani daima— kutawala wale ambao hawezi kuwashawishi— ni kulazimisha kwa ukatili. Kwa njia ya hofu au nguvu hutafuta kutawala dhamiri na kupata fursa ya yeye mwenyewe kuabudiwa. Kufanikisha hili kusudi, hufanya kazi kupitia mamlaka za kidini na kiserikali, akiwaongoza kulazimisha sheria za wanadamu zinazopingana na sheria ya Mungu.

Wanaoheshimu Sabato ya Biblia watashutumiwa kama maadui wa sheria na utaratibu, kama watu wanaovunja vizuizi vya maadili vya jamii, wakisababisha uasi na ufisadi, na kuita hukumu za Mungu juu ya ardhi. Uaminifu wao usioyumba utatangazwa kuwa ukaidi, ukorofi, na dharau kwa mamlaka. Watashitakiwa kwa kukosa uzalendo kwa serikali. Wachungaji wanaokataa uwajibishaji wa sheria ya Mungu watahubiri kutoka madhabahuni wajibu wa utii kwa mamlaka za kidunia umeamuriwa na Mungu. Katika majengo ya kutunga sheria na mahakama za kutoa haki, watunza amri watawakilishwa vibaya na kuhukumiwa. Tafsiri ya uongo itatolewa kwa maneno yao; na nia zao zitatafsiriwa vibaya.

Makanisa ya Kiprotestanti yanapokataa hoja za wazi, za Kimaandiko zinazotetea sheria ya Mungu, watatamani kuwanyamazisha wale ambao imani yao hawawezi kuishinda kwa Biblia. Ingawa wanafumba macho yao wasiuone ukweli, sasa wanapita katika njia ambayo itawaongoza kuwatesa wale ambao, kwa kutii dhamiri zao, watakataa kufanya kile ambacho ulimwengu wote wa Kikristo unakifanya, na kukiri madai ya sabato ya kipapa. Viongozi wa kanisa na wa dola wataungana kuhonga, kushawishi, au kulazimisha matabaka yote kuiheshimu Jumapili.

Kukosekana kwa mamlaka ya Kiungu kutajazwa kwa sheria kandamizi. Ufisadi wa kisiasa unaua kupenda haki na kuheshimu ukweli; na hata katika nchi huru ya Marekani, watawala na watunga sheria, ili wapate ukubali wa umma, watajisalimisha kwa madai ya walio wengi kwa ajili ya sheria ya kulazimisha utunzaji wa Jumapili. Uhuru wa dhamiri, ambao umegharimu kafara kubwa, hautaheshimiwa tena. Katika pambano linalokuja tutaona mfano wa maneno ya nabii: “Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu” (Ufunuo 12:17).

Sura ya 36 - Pambano Linalotarajiwa Karibuni

Tangu mwanzo kabisa wa pambano kuu mbinguni, kusudi la Shetani ni kupindua sheria ya Mungu. Ilikuwa kwa kusudi la kufanikisha jambo hili aliingia katika uasi dhidi ya Muumbaji wake, na ingawa alitupwa nje ya mbingu, anaendelea na vita ile ile duniani. Kudanganya wanadamu, na hatimaye kuwaongoza kuvunja sheria ya Mungu, ni lengo lake ambalo analitafuta kwa bidii sana. Iwe anafanikisha lengo hili kwa kutupilia mbali sheria yote kabisa, au kukataa sheria moja, matokeo ni yale yale hatimaye. Anayejikwaa "katika neno moja," anaonesha dharau kwa sheria yote; mvuto na mfano wake vipo upande wa uvunjaji wa sheria; na huwa "amekosa juu ya yote" (Yakobo 2:10).

Katika kutafuta kuonesha dharau kwa sheria ya Mungu, Shetani amepotosha mafundisho ya Biblia, na makosa hayo yameingizwa katika imani ya maelfu wanaodai kuamini Maandiko. Pambano kuu la mwisho kati ya ukweli na uongo ni shindano la mwisho la pambano la muda mrefu juu ya sheria ya Mungu. Tunaingia sasa katika vita hii—vita kati ya kanuni za Yehova na sheria za wanadamu, kati ya dini ya Biblia na dini ya hadithi za kubuni na mapokeo ya wanadamu.

Mawakala ambao wataungana dhidi ya ukweli na haki katika shindano hili sasa wako kazini. Neno takatifu la Mungu, ambalo limerithishwa kwetu kwa gharama kubwa ya mateso na damu, linathaminiwa kidogo sana. Biblia inaweza kupatikana kwa watu wote, lakini kuna watu wachache sana wanaoikubali kama mwongozo wa maisha. Ukafiri unatawala kwa kiwango kikubwa na cha kutisha, siyo katika ulimwengu pekee, bali pia kanisani. Wengi wameyakana mafundisho ambayo ni nguzo hasa za imani ya Kikristo. Ukweli mkuu wa uumbaji kama ulivyowasilishwa na waandishi waliovuviwa, anguko la mwanadamu, upatanisho, na uendelevu wa sharia ya Mungu, vinakataliwa wazi wazi, ama sheria yote au sehemu yake, na ulimwengu unaodai kuwa wa Kikristo. Maelfu ya watu wanaojivuna kuwa wenye hekima na walio huru huchukulia kuwa ni udhaifu kuiamini kabisa Biblia; wanafikiri kuwa ni ushahidi wa talanta ya juu na usomi wa hali ya juu kuyakataa Maandiko na kuupinga ukweli wake muhimu. Wachungaji wanawafundisha watu wao, na maprofesa na walimu wanawafundisha wanafunzi wao, kuwa sheria ya Mungu imebadilishwa au imefutwa; na wale wanaochukulia matakwa yake kuwa bado ni ya halali, yanayopaswa kutiiwa kama yalivyo, wanafikiriwa kuwa watu wa kudharauliwa au kudhihakiwa.

Kwa kuukataa ukweli, wanadamu wanamkataa Mwasisi wa ukweli. Kwa kuikataa sheria ya Mungu, watu wanaikana mamlaka ya Mtoa sheria. Ni rahisi kuchonga sanamu ya mafundisho ya uongo na nadharia za uongo sawa na kuchonga sanamu ya mti au jiwe. Kwa kuwasilisha vibaya sifa za Mungu, Shetani anawaongoza watu kumwelewa Mungu kwa tabia isiyokuwa sahihi. Kwa watu wengi, sanamu ya kifalsafa imewekwa juu ya kiti cha enzi badala ya Yehova; wakati Mungu aliye hai, kama alivyofunuliwa katika neno Lake, ndani ya Kristo, na katika kazi za uumbaji, anaabudiwa na watu wachache. Maelfu ya watu wanafanya vitu

vya asili kuwa miungu yao huku wakimkataa Mungu wa vitu vya asili. Japokuwa ni katika miundo mbalimbali, ibada ya sanamu ipo katika ulimwengu wa Kikristo leo katika uhalisia wake kama ilivyokuwa miongoni mwa Waisraeli katika siku za Eliya. Mungu wa wengi wanaodai kuwa wenye hekima, wanafalsafa, watunzi wa mashairi, wanasiasa, waandishi wa habari—mungu wa wanamitindo, mungu wa vyuo na vyuo vikuu, hata mungu wa baadhi ya taasisi za kitheolojia—ni miungu isiyomzidi sana Baali, mungu jua wa Wafoinike.

Hakuna kosa ambalo likikubaliwa na ulimwengu wa Kikristo linapiga kwa ujasiri zaidi dhidi ya mamlaka ya Mbingu, hakuna kosa ambalo linapingana zaidi na busara tu ya kawaida, hakuna kosa lililo na matokeo mabaya zaidi, kuliko fundisho la kisasa, ambalo linaendelea kukubaliwa na watu wengi kwa kasi, kuwa sheria ya Mungu haiwafungi watu tena. Kila taifa lina sheria zake, ambazo zinaheshimiwa na kutiiwa; hakuna serikali inayoweza kudumu kuwepo ikiwa haina sheria; na inawezaje kuingia akilini kuwa Muumbaji wa mbingu na nchi hana sheria za kutawala viumbe aliowaumba? Hebu chukulia kuwa wachungaji mashuhuri waanze kufundisha hadharani kuwa sheria zinazotawala nchi na zinazotawala haki za wananchi si za lazima— kuwa zinabana uhuru wa watu, na hivyo hazipaswi kutiiwa; watu hao wangeweza kuvumiliwa kwa muda gani wakifundisha hivyo mimbarani? Lakini, je, ni kosa kubwa zaidi kupuuza sheria za nchi na za mataifa kuliko kukanyaga kanuni za Mungu ambazo ndiyo msingi wa serikali zote?

Ingekuwa afadhali kwa mataifa kuondoa sheria zao, na kuwaruhusu watu wafanye wanavyopenda, kuliko Mtawala wa sayari zote kubatilisha sharia Yake, na kuuacha ulimwengu bila kiwango cha kuhukumu mwenye hatia au kumpa haki mtiifu. Je, tungependa kujua matokeo ya kubatilisha sheria ya Mungu? Jaribio limeshawahi kufanywa. Matokeo yake yalikuwa ya kutisha kama nini katika nchi ya Ufaransa wakati ukanamungu ulipofanywa kuwa mamlaka ya utawala. Wakati huo ilidhihirika kwa ulimwengu kuwa kutupilia mbali vizuizi ambavyo Mungu ameviweka ni kuruhusu utawala wa ukatili wa watu katili. Kiwango cha haki kinapoondolewa, njia inafunguliwa kwa ajili ya mfalme wa uovu kuimarisha mamlaka yake duniani.

Mahali popote sheria za Mungu zinapokataliwa, dhambi inaacha kuwa na ubaya na haki inakosa umuhimu na haitamaniwi. Wanaokataa kujisalimisha chini ya serikali ya Mungu hawafai kabisa kujiongoza wenyewe. Kwa njia ya mafundisho yao mabaya roho ya uasi inapandikizwa katika mioyo ya watoto na vijana, ambao kwa asili hawana uvumilivu wa kutawaliwa; na matokeo yake ni hali ya uasi na uvunjaji wa sheria katika jamii. Wakati wakidhihaki wepesi wa kuamini wale wanaotii matakwa ya Mungu, watu walio wengi wanapokea kwa furaha udanganyifu wa Shetani. Wanasalimisha hatamu zao kwa tamaa na wanatenda dhambi ambazo zinaleta hukumu juu ya wapagani.

Wale ambao wanafundisha watu kuchukulia kwa wepesi amri za Mungu wanapanda mbengu ya uasi wavune matunda ya uasi. Acha kizuizi kilichowekwa na sheria ya Mungu

kiondolewe kabisa, na sheria za wanadamu zitapuuzwa muda si mrefu. Kwa kuwa Mungu anakataza matendo yasiyokuwa ya uaminifu, kutamani, kusema uongo, na kudanganya, wanadamu wako tayari kukanyaga amri za Mungu kama kikwazo cha kupata mafanikio ya kidunia; lakini matokeo ya kuondoa kabisa kanuni hizi yangekuwa tofauti kabisa na jinsi walivyotegemea. Ikiwa sheria haimbani mtu, kwa nini mtu ye yote aogope kuivunja? Mali isingeweza salama tena. Watu wangejipatia mali za jirani zao kwa mabavu, na walio na nguvu zaidi kuliko wengine ndiyo wangekuwa matajiri kuliko watu wote. Uhai wenyewe usingeheshimiwa.

Kiapo cha ndoa kisingekuwa tena ngome takatifu ya kuilinda familia. Yule ambaye angekuwa na nguvu nyingi, angeweza, akipenda, kumchukua mke wa jirani yake kwa nguvu. Amri ya tano ingeondolewa na amri ya nne. Watoto wasingesita kuwaua wazazi wao ikiwa kwa kufanya hivyo wangeweza kupata mahitaji ya mioyo yao iliyoharibika. Ulimwengu uliostaarabika ungekuwa genge la majambazi na wauaji; na amani, utulivu, na furaha vingetoweka duniani.

Tayari fundisho kuwa watu wameachiliwa kutoka katika utii wa matakwa ya Mungu limedhoofisha nguvu ya uwajibikaji wa kiuadilifu na limefungulia mafuriko ya uovu ulimwenguni. Uasi, ubadhirifu, na ufisadi vinatufunika kama wimbi la maji. Katika familia, Shetani yuko kazini. Bendera yake inapepea hata katika nyumba zinazodai kuwa za Kikristo. Kuna kijicho, kuwazia mabaya wengine, unafiki, utengano, uadui, ugomvi, usaliti wa mambo matakatifu, uendekezaji wa tamaa mbaya. Mfumo mzima wa kanuni na mafundisho ya kidini, ambao ungeunda msingi na mwelekeo wa maisha ya kijamii, unaonekana kama bonge linaloyeyuka, linaloekea kutoweka. Wahalifu wakuu, wanapotupwa gerezani kwa makosa yao, mara nyingi wanapewa zawadi na kushabikiwa sana kana kwamba wamepata ushindi fulani mkubwa wa kuonewa wivu. Tabia yao na uhalifu wao unatanganzwa sasa. Vyombo vya habari vinatangaza uovu wao kwa kina, na kwa njia hiyo vinawafundisha wengine kufanya matendo ya wizi, unyang'anyi, na mauaji; na Shetani anashangilia mafanikio ya mipango yake ya kijehanamu. Kufurahia uovu, mauaji ya kikatili, ongezeko la kutisha la kutokuwa na kiasi na uovu wa kila aina na wa kila kiwango, vyapaswa kuwaamsha wote wanaomcha Mungu, kujiuliza nini kifanyike kuzuia wimbi la uovu.

Mahakama zinapokea rushwa. Watawala wanasukumwa na tamaa ya mapato na kupenda anasa za mwili. Kukosa kiasi kumetia mawingu akili za wengi kiasi kwamba Shetani anawatawala karibu katika kila hali. Ulevi na sherehe, tamaa, kijicho, kukosa uaminifu kwa njia mbalimbali, vinawakilishwa miongoni mwa wale wanaosimamia sheria."Haki inasimama mbali sana; maana kweli imeanguka katika njia kuu, na unyofu hauwezi kuingia" (Isaya 59:14).

Uovu na giza la kiroho vilivyotawala chini ya himaya ya Rumi vilikuwa matokeo ya moja kwa moja ya kukandamiza Maandiko; lakini ni wapi tunapata chimbuko la ukafiri

ulioenea kote, kuikataa sheria ya Mungu, na ufisadi unaofuata baada ya kuikataa sheria ya Mungu, chini ya nuru kamilifu ya injili katika zama za uhuru wa kidini? Sasa kwa kuwa Shetani hawezi kuendelea zaidi kuutawala ulimwengu kwa kuzuia Maandiko, anatumia njia zingine kutimiza lengo lile lile. Kuharibu imani kwa Biblia kunamsaidia Shetani kutimiza kusudi lake na kuharibu Biblia yenyewe. Kwa kuingiza imani kuwa sheria ya Mungu haimbani mtu, Shetani anawaongoza watu kirahisi kuivunja kana kwamba hawajui kanuni zake. Na sasa, kama ilivyokuwa katika zama za kale, amefanya kazi kupitia kanisa kuendeleza mipango yake.

Mashirika ya kidini ya leo yamekataa kusikiliza ukweli usiopendwa ulioelezwa wazi wazi katika Maandiko, na ili kuushinda huo ukweli wameupatia tafsiri na wameweka misimamo ambayo imepanda kila mahali mbegu za mashaka. Wakishikilia makosa ya kipapa ya asili ya kutokufa na ufahamu katika umauti, wamekataa ulinzi pekee dhidi ya madanganyifu ya imani ya kuongea na wafu. Fundisho la maumivu ya milele motoni limewafanya wengi kutoiamini Biblia. Na madai ya amri ya nne yanapoelezwa kwa watu, inaonekana kuwa utunzaji wa Sabato ya siku ya saba umeamriwa; na kama njia pekee ya kujinasua kutoka katika wajibu ambao hawako tayari kuufanya, walimu mashuhuri walio wengi hutangaza kuwa sheria ya Mungu haimbani mtu tena. Hivyo wanatupilia mbali sharia pamoja na Sabato. Kwa kadiri kazi ya matengenezo ya Sabato inavyopanuka, ukataaji huu wa sheria ya Mungu ili kuepuka madai ya amri ya nne utakuwa karibu na watu wote duniani. Mafundisho ya viongozi wa dini wamefungulia mlango ukafiri, imani ya kuongea na wafu, na dharau kwa sheria takatifu ya Mungu; na juu ya viongozi hawa kuna uwajibikaji wa kutisha kwa ajili ya uovu uliomo katika ulimwengu wa Kikristo.

Hata hivyo, tabaka hili hili wanadai kuwa ufisadi unaoenea kwa kasi unatokana na kunajisi kile kinachoitwa "sabato ya Kikristo," na kuwa ulazimishaji wa utunzaji wa Jumapili utaweza kuboresha zaidi maadili ya jamii. Dai hili linasisitizwa hasa hasa Amerika, mahali ambapo fundisho la Sabato ya kweli limehubiriwa sana. Hapa, kazi ya kiasi, moja ya matengenezo ya kimaadili na muhimu sana, mara nyingi inaunganishwa na vuguvugu la Jumapili, na watetezi wa Jumapili wenyewe wanajinasibu kuwa wanafanya kazi ya kutetea maslahi ya jamii; na watu wanaokataa kuungana nao wanalaumiwa kama maadui wa kiasi na matengenezo. Lakini ukweli kuwa vuguvugu la kuendeleza uongo limeunganishwa na kazi ambayo kama ilivyo yenyewe ni nzuri, siyo hoja ya kuunga mkono uongo.

Tunaweza kuificha sumu kwa kuichanganya na chakula kizuri, lakini hatubadilishi asili yake. Kinyume chake, imefanywa kuwa ya hatari zaidi, kwa kuwa ina uwezekano wa kumezwa na mtu bila habari. Ni moja ya mbinu za Shetani kuchanganya uongo na ukweli ili kuupa uongo uwezo wa kukubalika. Viongozi wa vuguvugu la Jumapili wanaweza kutetea matengenezo ambayo watu wanayahitaji, kanuni ambazo zinapatana na Biblia; lakini, kwa kuwa matengenezo haya yamechanganywa na takwa ambalo ni kinyume na sheria ya Mungu,

watumishi Wake hawawezi kuungana nao. Hakuna jambo lolote linaloweza kuwahalalisha kwa kuacha amri za Mungu na badala yake kutii kanuni za wanadamu.

Kwa njia ya mafundisho mawili ya uongo, kutokufa kwa roho na utakatifu wa Jumapili, Shetani atawaweka watu chini ya madanganyifu yake. Wakati fundisho la kwanza linajenga msingi wa imani ya kuongea na wafu, fundisho la pili linajenga mshikamano wa kuikubali Rumi. Waprotestanti wa Marekani watakuwa mstari wa mbele katika kunyosha mikono yao kutoka upande mmoja hadi mwingine wa korongo refu kushikana mikono na imani ya kuongea na wafu; watavuka shimo kubwa kushikana mikono na mamlaka ya Kirumi; na chini ya mvuto wa muungano wa mamlaka tatu, nchi hii itafuata katika nyayo za Rumi katika kukanyaga haki za dhamiri.

Kwa kuwa imani ya kuongea na wafu inaigiza kwa karibu sana Ukristo wa jina wa wakati wetu, ina nguvu zaidi ya kudanganya na kunasa. Shetani mwenyewe ameongoka, kulingana na hali ya sasa ya mambo. Atatokea katika tabia na mwonekano wa malaika wa nuru. Njia ya wakala wa imani ya kuongea na wafu, miujiza itatendwa, wagonjwa wataponywa, na maajabu mengi yasiyokanushika yatafanywa. Na kwa kuwa pepo watadai kuwa wanaiamini Biblia, na kuonesha heshima kwa taasisi za kanisa, kazi zao zitakubaliwa kama udhihirisho wa nguvu ya Mungu.

Mstari unaogawa watu kati ya wanaojiita Wakristo na watu wasiomwamini Mungu kwa sasa hauonekani vizuri. Washiriki wa Kanisa wanapenda vitu ambavyo watu wa kidunia wanavipenda na wako tayari kujiunga nao, na Shetani ameazimia kuwaunganisha wote katika jumuiya moja na kwa njia hiyo aweze kuimarisha kazi yake kwa kuwaingiza watu wote katika imani ya kuongea na wafu. Waumini wa mfumo wa upapa, wanaojivunia miujiza kama ishara ya kanisa la kweli, watadanganywa kirahisi na nguvu hii inayotenda miujiza; na Waprotestanti, wakiwa wametupilia mbali ngao ya ukweli, nao pia watadanganywa. Waumini wa upapa, Waprotestanti, na watu wa kidunia wote kwa pamoja wataupokea mfano huo wa utauwa usiokuwa na nguvu ya Mungu, na wataona katika muungano huo vuguvugu kubwa la kuuongoa ulimwengu na uingizaji wa kipindi cha miaka elfu moja kilichosubiriwa kwa muda mrefu.

Kwa njia ya imani ya kuongea na wafu, Shetani ataonekana kama mfadhili wa jamii ya wanadamu, akiponya magonjwa ya watu, na akidai kuwasilisha mfumo mpya na wa juu zaidi wa imani ya kidini; lakini wakati huo huo anafanya kazi kama muuaji. Majaribu yake yanawaongoza wengi kwenda kuuawa. Kutokuwa na kiasi kunaondoa uwezo wa kufikiri vizuri; kupenda anasa, migogoro, na umwagaji damu hufuata. Shetani anapenda sana vita, kwa sababu vita vinaamsha mihemko mibaya zaidi kuliko yote kutoka rohoni na vinawafagilia wahanga wote katika umilele wakiwa na mwelekeo wa uovu na umwagaji damu. Ni kusudi lake kuchochea mataifa yapigane vita taifa moja dhidi ya taifa jingine, kwa

sababu kwa njia hiyo anaweza kuhamisha akili ya watu isijishughulishe na kazi ya maandalizi ya kusimama katika siku ya Mungu.

Shetani hufanya kazi kupitia nguvu za asili kukusanya mavuno yake ya roho zisizojiandaa. Amejifunza siri za maabara ya ulimwengu, na anatumia nguvu zake zote kutawala nguvu za asili kwa kiwango kile ambacho Mungu anaruhusu. Aliporuhusiwa kumtesa Ayubu, ni kwa kasi kubwa kiasi gani kondoo, ngamia, ng'ombe, watumishi, nyumba, watoto, walifagiliwa mbali, janga moja likifuata jingine kama kwa dakika moja. Ni Mungu anayewakinga viumbe Wake na kuwazungushia wigo dhidi ya nguvu ya mwuaji. Lakini ulimwengu wa Kikristo umeonesha dharau kwa sheria ya Yehova; na Bwana atafanya vile ambavyo ameahidi kuwa atafanya—ataondoa mibaraka Yake duniani na ataondoa ulinzi Wake kwa wale wanaoasi dhidi ya sheria Yake na kuwafundisha na kuwalazimisha wengine kuasi kama wao. Shetani anawatawala wale wote ambao hawako chini ya ulinzi wa Mungu. Shetani anawapendelea na kuwafanikisha baadhi ili kuendeleza mipango yake, na atawaletea matatizo wengine na kuwaongoza watu kuamini kuwa ni Mungu anayewatesa.

Wakati akionekana kwa wanadamu kama mganga mkuu anayeweza kuponya magonjwa yao, ataleta magonjwa na majanga, hadi miji yenye wakazi wengi itabaki magofu na ukiwa. Hata sasa yuko kazini. Katika ajali na majanga katika bahari na katika nchi kavu, ajali za mioto mikubwa, katika vimbunga vikali na tufani ya mvua ya mawe ya kutisha, katika dhoruba, mafuriko, tufani, mawimbi ya kujaa na kupya kwa bahari, na matetemeko ya ardhi, kila mahali na katika miundo maelfu, Shetani anatumia nguvu yako. Anafagia mazao yanayoelekea kukomaa, na njaa na hofu hufuata. Anaweka hewani harufu mbaya inayofisha, na maelfu huangamia kwa magonjwa. Matukio haya yatazidi kuwa ya mara kwa mara na ya kutisha zaidi. Mauti itakuwa juu ya mwanadamu na mnyama. "Dunia inaomboleza, inazimia," "watu wakuu … wanadhoofika. Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele" (Isaya 24:4, 5).

Na ndipo mdanganyaji mkuu atawashawishi watu kuwa wanaomtumikia Mungu ndiyo chimbuko la majanga hayo. Tabaka ambalo limechokoza hasira ya Mbingu litatupia lawama kwa wale ambao utii wao kwa amri za Mungu ni kemeo la kudumu kwa wakosaji. Itatangazwa kuwa watu wanamkosea Mungu kwa kuvunja sabato ya Jumapili; kuwa dhambi imeleta majanga ambayo hayatakoma mpaka utunzaji wa Jumapili utakapotekelezwa kikamilifu; na kuwa wale wanaowasilisha madai ya amri ya nne, na kwa njia hiyo kuharibu heshima kwa ajili ya Jumapili, ni wataabishaji wa watu, wakizuia urejeshwaji wao kwa upendeleo wa Mungu na mafanikio ya duniani. Kwa hiyo shitaka lililotolewa zamani na mtumishi wa Mungu litarudiwa na kwa sababu ambazo ni za msingi: "Ikawa, Ahabu alipomwona Eliya, Ahabu akamwambia, Je! Ni wewe, Ewe mtaabishaji wa Israeli? Naye akajibu, Si mimi niliyewataabisha Israeli; bali ni wewe, na nyumba ya baba yako, kwa kuwa mmeziacha amri za Bwana; nawe umewafuata mabaali" (1 Wafalme 18:17, 18). Wakati hasira ya watu

itakapochochewa kwa mashitaka ya uongo, watafuata njia ya kutafuta kuwaua mabalozi wa Mungu sawa sawa na jinsi Waisraeli walioasi walivyotafuta kumuua Eliya.

Nguvu itendayo miujiza inayodhihirishwa kwa njia ya imani ya kuongea na wafu itaeneza mvuto wake dhidi ya wale wanaochagua kumtii Mungu kuliko wanadamu. Mawasiliano kutoka kwa roho za pepo yatatangaza kuwa Mungu amewatuma kuwashawishi wapinzani wa Jumapili kuhusu kosa lao, yakithibitisha kuwa sheria za nchi zinapaswa kutiiwa kama sheria ya Mungu. Watasikitika kwa sababu ya uovu mkubwa ulioko ulimwenguni na wataunga mkono ushuhuda wa viongozi wa dini kuwa hali ya maadili yaliyoporomoka imesababishwa na kunajisi Jumapili. Hasira kubwa itachochewa dhidi ya wote watakaokataa kukubali ushuhuda wao.

Sera ya Shetani katika mgogoro huu wa mwisho na watu wa Mungu ni ile ile aliyoitumia wakati wa uanzishaji wa pambano kuu mbinguni. Alieleza kwamba alikuwa akitafuta kuongeza uimara wa serikali ya Mungu, wakati kisirisiri alikuwa akielekeza juhudi zake zote kutafuta njia za kuipindua. Na kazi ile ile aliyokuwa akitafuta kuifanya aliwasingizia malaika watiifu kuwa ndio walikuwa wakiifanya. Sera ile ile ya udanganyifu imekuwa sifa ya historia ya Kanisa la Rumi. Linaeleza kuwa linafanya kazi kama mwakilishi wa Mbingu, wakati likitafuta kujiinua juu ya Mungu na kubadilisha sheria Yake. Chini ya utawala wa Rumi, wale waliouawa kwa ajili ya uaminifu wao kwa injili walilaumiwa kama watenda maovu; walitangazwa kuwa na mshikamano na Shetani; na kila njia inayowezekana ilitumika kuwafanya wadharauliwe, kuwafanya waonekane katika macho ya watu na hata kwao wenyewe kuwa ni wabaya kuliko wahalifu wote. Ndivyo itakavyokuwa hata sasa. Wakati akitafuta kuwaangamiza wale wanaoheshimu sheria ya Mungu, atasababisha washitakiwe kama wavunja sheria, kama watu wanaomkosea heshima Mungu na kuleta hukumu juu ya dunia.

Mungu halazimishi nia au dhamiri; lakini juhudi ya Shetani daima— kutawala wale ambao hawezi kuwashawishi— ni kulazimisha kwa ukatili. Kwa njia ya hofu au nguvu hutafuta kutawala dhamiri na kupata fursa ya yeye mwenyewe kuabudiwa. Kufanikisha hili kusudi, hufanya kazi kupitia mamlaka za kidini na kiserikali, akiwaongoza kulazimisha sheria za wanadamu zinazopingana na sheria ya Mungu.

Wanaoheshimu Sabato ya Biblia watashutumiwa kama maadui wa sheria na utaratibu, kama watu wanaovunja vizuizi vya maadili vya jamii, wakisababisha uasi na ufisadi, na kuita hukumu za Mungu juu ya ardhi. Uaminifu wao usioyumba utatangazwa kuwa ukaidi, ukorofi, na dharau kwa mamlaka. Watashitakiwa kwa kukosa uzalendo kwa serikali. Wachungaji wanaokataa uwajibishaji wa sheria ya Mungu watahubiri kutoka madhabahuni wajibu wa utii kwa mamlaka za kidunia umeamuriwa na Mungu. Katika majengo ya kutunga sheria na mahakama za kutoa haki, watunza amri watawakilishwa vibaya na kuhukumiwa. Tafsiri ya uongo itatolewa kwa maneno yao; na nia zao zitatafsiriwa vibaya.

Makanisa ya Kiprotestanti yanapokataa hoja za wazi, za Kimaandiko zinazotetea sheria ya Mungu, watatamani kuwanyamazisha wale ambao imani yao hawawezi kuishinda kwa Biblia. Ingawa wanafumba macho yao wasiuone ukweli, sasa wanapita katika njia ambayo itawaongoza kuwatesa wale ambao, kwa kutii dhamiri zao, watakataa kufanya kile ambacho ulimwengu wote wa Kikristo unakifanya, na kukiri madai ya sabato ya kipapa. Viongozi wa kanisa na wa dola wataungana kuhonga, kushawishi, au kulazimisha matabaka yote kuiheshimu Jumapili. Kukosekana kwa mamlaka ya Kiungu kutajazwa kwa sheria kandamizi. Ufisadi wa kisiasa unaua kupenda haki na kuheshimu ukweli; na hata katika nchi huru ya Marekani, watawala na watunga sheria, ili wapate ukubali wa umma, watajisalimisha kwa madai ya walio wengi kwa ajili ya sheria ya kulazimisha utunzaji wa Jumapili. Uhuru wa dhamiri, ambao umegharimu kafara kubwa, hautaheshimiwa tena. Katika pambano linalokuja tutaona mfano wa maneno ya nabii: "Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu" (Ufunuo 12:17).

Sura ya 37 - Maandiko ni Kinga

"Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi" (Isaya 8:20). Watu wa Mungu wameelekezwa kuyachukulia Maandiko kuwa kinga dhidi ya mvuto wa walimu wa uongo na nguvu ya udanganyifu ya roho wa giza. Shetani anatumia kila njia inayowezekana kuzuia watu wasipate ujuzi wa Biblia; kwa kuwa maneno yake ya wazi hufunua uongo wake. Katika kila uamsho wa kazi ya Mungu mfalme wa uovu anaamshwa na kujishughulisha zaidi; sasa anafanya kazi kwa juhudi zake zote kwa ajili ya pambano dhidi ya wafuasi Wake. Uongo mkuu wa mwisho karibu utafunuliwa mbele yetu. Mpinga Kristo atafanya kazi zake za maajabu mbele yetu. Vitu bandia vitafanana sana na vitu halisi kiasi kwamba haitawezekana kutofautisha kati ya kitu bandia na kitu halisi isipokuwa kwa njia ya Maandiko Matakatifu. Kwa njia ya ushuhuda wa Maandiko kila kauli na kila muujiza lazima vipimwe.

Wale watakaojitahidi kutii amri zote za Mungu watapingwa na kudhihakiwa. Wataweza kusimama kwa uwezo wa Mungu tu. Ili kustahimili jaribu lililoko mbele yao, inawapasa waelewe mapenzi ya Mungu kama yalivyofunuliwa katika neno Lake; wanaweza kumheshimu tu ikiwa wana uelewa sahihi wa tabia Yake, serikali, na makusudi Yake, na kutenda kulingana nayo. Ni wale tu ambao wameimarisha akili zao kwa ukweli wa Biblia watasimama na kushinda katika pambano kuu la mwisho. Kwa kila roho kutakuja mtihani wa kujihoji: Je, nimtii Mungu kuliko wanadamu? Saa ya uamuzi imewadia hata sasa. Je, miguu yetu imesimikwa juu ya mwamba wa neno la Mungu lisilobadilika? Je, tuko tayari kusimama imara kutetea amri kumi za Mungu na imani ya Yesu?

Kabla ya kusulubiwa Kwake Mwokozi aliwaelezea wanafunzi Wake kuwa alikuwa anaelekea kuuawa na kufufuka tena kutoka kaburini, na malaika walikuwepo kunatisha maneno Yake katika akili na mioyo. Lakini wanafunzi walikuwa wakitarajia kupata ukombozi wa kidunia kutoka katika nira ya ukoloni wa Warumi, na wasingeweza kuvumilia wazo kuwa Yule ambaye matumaini yao yote yalikuwa yamekitwa kwake angekufa kifo cha aibu. Maneno waliyotakiwa kuyakumbuka yaliyeyuka na kuondoka katika akili zao; na wakati wa jaribu ulipofika, hawakuwa tayari. Kifo cha Yesu kiliharibu matumaini yao yote kiasi kwamba ni kana kwamba hakuwa amewapa tahadhari yo yote. Kwa hiyo, katika unabii, wakati ujao umefunuliwa mbele yetu kwa uwazi kama vile ulivyokuwa umefunuliwa kwa wanafunzi kwa njia ya maneno ya Kristo. Matukio ambayo yameshikamana na kufungwa kwa mlango wa rehema na kazi ya matayarisho kwa ajili ya wakati wa taabu, vyote vimeelezwa kwa uwazi kabisa. Lakini watu wengi hawana ufahamu wa ukweli huu muhimu kuliko kama ungekuwa haujafunuliwa. Shetani yuko macho akihakikisha kuwa anadaka na kufuta kila wazo ambalo lingeweza kuwafanya wawe na hekima ya kupata wokovu, na wakati wa taabu utawakuta wakiwa hawako.

Mungu anapowatumia watu maonyo yaliyo muhimu kiasi kwamba yanawakilishwa kana kwamba yanahubiriwa na malaika watakatifu wanaoruka katikati ya mbingu, anataka kila mtu mwenye ufahamu asikie ujumbe. Hukumu za kutisha zinazotangazwa dhidi ya ibada ya mnyama na sanamu yake (Ufunuo 14:9-11), zinapaswa kuwaongoza wote katika kujifunza kwa bidii unabii na kuelewa ni nini alama ya mnyama, na jinsi wanavyoweza kuepuka kuipokea. Lakini watu walio wengi wanageuza masikio yao wasisikie ukweli na wanageukia hadithi za kubuni. Mtume Paulo alitangaza, akizitazama siku za mwisho: "Utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima" (2 Timotheo 4:3). Wakati umeshafika tayari. Watu walio wengi hawataki ukweli wa Biblia, kwa sababu unaingilia tamaa za moyo wenye dhambi, unaopenda ulimwengu; na Shetani anawapa uongo wanaoupenda.

Lakini Mungu atakuwa na watu duniani watakaodumisha Biblia, na Biblia pekee, kama kiwango cha mafundisho yote na msingi wa matengenezo yote. Maoni ya wasomi, mahitimisho ya sayansi, imani na maamuzi ya mabaraza ya makanisa, yakiwa mengi na yanayohitilafiana kama makanisa yenyewe yanayoyawakilisha yalivyo, sauti ya walio wengi—hakuna moja wala yote yanapaswa kuchukuliwa kama ushahidi unaounga mkono au unaopinga wazo lo lote la imani ya kidini. Kabla ya kukubali fundisho lo lote au kanuni yo yote, inatupasa kudai tamko la wazi la "Hivi ndivyo Bwana asemavyo" kuunga mkono fundisho hilo au kanuni hiyo.

Shetani anajitahidi daima kuvuta usikivu uelekezwe kwa watu badala ya kuelekezwa kwa Mungu. Anawaongoza watu wawatazame maaskofu, wachungaji, maprofesa wa theolojia, kama viongozi wao, badala ya kuchunguza Maandiko ili wajifunze wajibu wao wenyewe moja kwa moja.

Ndipo, kwa kutawala na kuongoza akili za hawa viongozi, anaweza kutawala watu wengi kulingana na matakwa yake mwenyewe. Kristo alipokuja kutangaza maneno ya uzima, watu wa kawaida walimsikiliza kwa furaha; na wengi, hata miongoni mwa makuhani na watawala, walimwamini. Lakini wakuu wa makuhani na viongozi wa ngazi ya juu wa kitaifa walidhamiria kupinga na kukosoa mafundisho Yake. Ingawa walishindwa katika juhudi zao zote kupata mashitaka dhidi Yake, ingawa hata wao walihisi mvuto wa nguvu na hekima ya Mungu katika maneno Yake, bado walijifungia katika chuki isiyo na sababu; walikataa ushahidi wa wazi kabisa wa Umasihi Wake, ili wasije wakajikuta wamelazimika kuwa wanafunzi Wake.

Hawa wapinzani wa Yesu walikuwa watu ambao watu wote walikuwa wamefundishwa tangu utotoni kuwaheshimu sana, watu ambao mamlaka yao watu wote walikuwa wamezoea kuyatii bila maswali. "Inawezekanaje," waliuliza, "viongozi wetu na waandishi wasomi wasimwamini Yesu? Hawa watu watakatifu si wangempokea kama kweli angekuwa Kristo?" Ilikuwa kwa sababu ya mvuto wa hawa viongozi taifa la Kiyahudi lilimkataa Mkombozi wao. Roho iliyowaendesha makuhani na viongozi wale ingali ikidhihirishwa na watu wote

wanaodai kuwa watakatifu sana. Wanakataa kuchunguza ushuhuda wa Maandiko kuhusu ukweli maalumu kwa ajili ya wakati huu. Wanaonesha idadi yao, utajiri wao, na umaarufu wao, na wanawatazama kwa dharau watetezi wa ukweli kama watu wachache, maskini, na wasiopendwa na watu, walio na imani inayowatenga na ulimwengu.

Kristo aliona tangu mwanzo kuwa kujichukulia mamlaka kusikostahili kwa waandishi na Mafarisayo kusingekomeshwa na kusambaa kwa Wayahudi katika mataifa mbalimbali. Aliona kwa macho ya kinabii kazi ya kuinua mamlaka ya wanadamu na kutawala dhamiri, ambako kumekuwa laana ya kutisha kwa kanisa katika zama zote. Na maonyo ya kutisha kwa waandishi na Mafarisayo, na maonyo Yake kwa watu ili wasifuate viongozi hawa vipofu, yaliwekwa katika kumbukumbu kama maonyo kwa vizazi vya baadaye.

Kanisa la Rumi, ni viongozi wa dini tu ambao wana haki ya kutafsiri Maandiko. Kwa misingi kuwa viongozi wa dini peke yao ndio wenye uwezo wa kufafanua neno la Mungu, Biblia imeondolewa kwa watu wa kawaida. [Tazama Kiambatanisho kwa ajili ya maelezo ukurasa wa 340.] Ingawa Matengenezo yalitoa Maandiko kwa wote, lakini kanuni ile ile iliyoshikiliwa na Rumi inawazuia watu wengi katika makanisa ya Kiprotestanti wengi kusoma Biblia wenyewe. Wanafundishwa kupokea mafundisho ya Biblia kama yanavyotafsiriwa na kanisa; na kuna maelfu ya watu wasiopokea cho chote, hata kama kimefunuliwa kwa uwazi katika Maandiko, kilicho tofauti na imani au fundisho lililokwishawekwa na kanisa lao.

Licha ya Biblia kujaa maonyo dhidi ya walimu wa uongo, watu wengi wako tayari kusalimisha amana ya roho zao kwa viongozi wa kanisa. Wapo watu maelfu leo wanaodai kuwa wafuasi wa dini wasioweza kutoa sababu ya imani yao zaidi ya kusema tu kuwa wao wamefundishwa hivyo na viongozi wa dini. Wanapita bila kuyaona mafundisho ya Mwokozi, na wanaweka imani yao isiyo na swali kwa maneno ya wachungaji wao. Lakini, je, wachungaji hawakosei? Tunawezaje kuweka amana roho zetu kwa uongozi wao tusipojua kwa njia ya neno la Mungu kuwa ni wabeba nuru? Ukosefu wa ujasiri wa kimaadili wa kwenda kando ya njia iliyozoeleka ya ulimwengu huwafanya wengi wafuate nyayo za wasomi; na kwa sababu ya uzembe wa kuchunguza wenyewe, wanajikuta wamenaswa katika minyororo ya makosa bila matumaini. Wanaona kuwa ukweli kwa ajili ya wakati huu umefunuliwa katika Biblia; na wanahisi nguvu ya Roho Mtakatifu katika utangazaji wake; lakini bado wanaruhusu upinzani wa viongozi wa dini kuwageuza na kuwapeleka mbali na nuru. Ingawa busara na dhamiri vimeshawishika, roho hizi zilizodanganyika haziwezi kuthubutu kufikiri tofauti na mchungaji wao; na uamuzi wao binafsi, maslahi yao ya umilele, vinatolewa kafara kweye madhabahu ya mashaka, kiburi, na chuki, ya mtu mwingine.

Kuna njia nyingi ambazo Shetani anazitumia kufanya kazi kupitia mvuto wa kibinadamu kuwafunga mateka wake. Anajipatia wafuasi kwa kuwashikamanisha, kwa njia ya kamba za hariri ya upendo, na wale ambao ni adui za msalaba wa Kristo. Mshikamano huu waweza

kuwa wa wazazi, ndugu, ndoa, au kijamii, madhara ni yale yale; wapinzani wa ukweli wanatumia nguvu kutawala dhamiri, na roho zilizo chini ya utawala wao hazina ujasiri au uhuru wa kutosha kufuata kile wanachokiamini kuwa ndiyo wajibu wao.

Ukweli na utukufu wa Mungu havitenganishwi; haiwezekani kwetu sisi, ambao tuna uwezo wa kupata Biblia kirahisi, tumheshimu Mungu kwa maoni yenye makosa. Wengi hudai kuwa siyo jambo muhimu kuwa mtu anaamini nini, ikiwa maisha yake ni mazuri. Lakini maisha huendeshwa na imani. Ikiwa nuru ya ukweli iko ndani ya uwezo wetu wa kuipata, na tunazembea kutumia fursa tulizonazo za kuusikia ukweli na kuiona nuru, ina maana kuwa tumeukataa ukweli kwa makusudi; tumechagua giza kuliko nuru.

"Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu; Lakini mwisho wake ni njia za mauti"(Mithali 16:25). Kutokujua siyo udhuru wa makosa au dhambi, kunapokuwepo kila fursa ya kuyajua mapenzi ya Mungu. Mtu anatembea barabarani na anafika mahali ambapo kuna barabara kadhaa na kuna ubao unaoeleza kila barabara inakokwenda. Ikiwa mtu huyu atapuuza huo ubao wenye maelezo, na anaamua kupita katika barabara yo yote anayoiona sawa machoni pake, anaweza kuwa na nia nzuri kabisa, lakini kwa namna yo yote ile atajikuta akiwa katika barabara isiyokuwa sahihi.

Mungu ametupatia neno Lake ili tuyajue mafundisho yake na tujue kile ambacho Mungu anakitaka kwetu. Wakati mwanasheria alipokuja kwa

Yesu akiwa na swali, "Nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" Mwokozi alimpeleka katika Maandiko, akisema: "Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje?" Kutokujua hakutakuwa udhuru kwa vijana au wazee, wala kuwaokoa wasipate adhabu kwa kuvunja sheria ya Mungu; kwa sababu katika mikono yao wanalo wasilisho kamili la sheria ya Mungu na la kanuni zake na madai yake. Haitoshi kuwa na nia nzuri peke yake; haitoshi mtu kufanya kile anachodhani kuwa ni sahihi au kile ambacho mchungaji wake anamwambia kuwa ni sahihi. Wokovu wa roho yake uko hatarini, na anapaswa kuchunguza Maandiko kwa ajili yake mwenyewe. Haidhuru ameshawishika kiasi gani, haidhuru anamwamini mchungaji wake kuwa anaujua ukweli kiasi gani, huu sio msingi wake. Anao mwongozo unaomwonesha kila alama ya njia katika safari ya kwenda mbinguni, na hapaswi kubahatisha katika jambo lo lote.

Ni wajibu wetu wa kwanza na wa juu kabisa wa kila mtu mwenye akili kujifunza kutoka katika Maandiko kile ambacho ni ukweli, na halafu kutembea katika nuru na kuwatia moyo wengine wafuate mfano wake. Inatupasa siku kwa siku kujifunza Biblia kwa bidii, tukipima kila wazo kwa kulinganisha andiko kwa andiko. Kwa msaada wa Mungu inatupasa kujenga maoni yetu kwa ajili yetu sisi wenyewe kwa kuwa itatupasa kujibu wenyewe mbele ya Mungu.

Ukweli ambao umefunuliwa kwa uwazi katika Biblia umetiliwa mashaka na kuwekwa giza na wasomi, ambao, kwa kujifanya kuwa wana hekima kubwa, hufundisha kuwa Maandiko yana maana yenye fumbo, ya siri, na ya kiroho isiyoonekana katika lugha iliyotumiwa. Watu hawa ni walimu wa uongo. Ilikuwa tabaka kama hili ambalo Yesu aliliambia: "Hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu" (Marko 12:24). Lugha ya Biblia inapaswa kueleweka kulingana na maana yake ya wazi, isipokuwa pale ambapo ishara imetumiwa au kielelezo kimetumiwa. Kristo ametoa ahadi: "Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo" (Yohana 7:17). Ikiwa watu wangeielewa kama inavyosomeka, ikiwa wasingekuwepo walimu wa uongo wanaopotosha na wanaochanganya akili za watu, kazi ingefanyika ambayo ingewafurahisha malaika na ambayo ingeleta maelfu kwa maelfu kundini ambao kwa sasa wanatangatanga katika makosa.

Inatupasa kuelekeza nguvu zetu zote za akili katika kusoma Maandiko na inatupasa tujipe kazi ya kufahamu na kuelewa, kwa kadiri inavyowezekana kwa watu wenye hali ya kufa, mambo ya kina ya Mungu; lakini hatupaswi kusahau kuwa utiifu na ujisalimishaji wa mtoto ndiyo roho ya kweli ya mwanafunzi wa Biblia kwa sababu matatizo ya kuielewa Biblia hayawezi kutanzuliwa kwa mbinu zinazotumiwa katika kuchambua matatizo ya kifalsafa. Hatupaswi kuingia katika kujifunza Biblia na ile hali ya kujitegemea ambayo wengi wanaingia nayo katika uwanja wa sayansi, bali kwa maombi na kumtegemea Mungu na shauku ya dhati ya kujifunza mapenzi Yake.

Inatupasa kuja kwa unyenyekevu na roho ya kufundishika ili kupata maarifa kutoka kwa Yeye ambaye ni MIMI NIKO. Vinginevyo, malaika waovu watapofusha akili zetu na kuifanya mioyo yetu kuwa migumu ili tusiweze kuupokea ukweli.

Sehemu nyingi za Maandiko ambazo wasomi wanazitangaza kuwa zina mafumbo, au wanaziruka kwa kigezo kuwa siyo za muhimu, zimejaa faraja na mafundisho kwa mtu ambaye amepata mafunzo katika shule ya Kristo. Sababu moja ambayo inawafanya wanatheolojia wasiwe na uelewa sahihi wa neno la Mungu ni, wanafumba macho yao wasiuone ukweli ambao hawako tayari kuuishi. Ufahamu wa ukweli wa Biblia hautegemei sana nguvu ya akili iliyoingizwa katika utafiti; bali hutegemea zaidi udhati wa kusudi, shauku ya dhati ya kuwa mtakatifu.

Kamwe Biblia isijifunzwe bila maombi. Roho Mtakatifu pekee Ndiye anaweza kutufanya tuhisi umuhimu wa mambo yale ambayo ni rahisi kueleweka, au kutuzuia tusianze kupotosha ukweli ambao ni mgumu kwetu kuuelewa. Ni kazi ya malaika wa mbinguni kuuandaa moyo kuelewa neno la Mungu kiasi cha kuweza kufurahia uzuri wake, kubadilishwa na maonyo yake, au kuchangamshwa na kuimarishwa na ahadi zake. Inatupasa kulifanya ombi la mtunga Zaburi kuwa ombi letu: "Unifumbue macho yangu niyatazame Maajabu yatokayo katika sheria yako" (Zaburi 119:18). Majaribu yanaonekana kuwa yasiyozuilika kwa sababu, kwa kuzembea maombi na kujifunza Biblia, mtu anayejaribiwa

hawezi kukumbuka kirahisi ahadi za Mungu na kumkabili Shetani kwa silaha za Maandiko. Lakini malaika wanawazunguka wale walio tayari kufundishwa mambo ya Mungu; na katika wakati wa mahitaji makubwa watakumbuka ukweli ambao unahitajika kwa wakati huo. Kwa hiyo "wakati adui atakapokuja kama mkondo wa mto wa mafuriko; Roho wa Bwana atainua bendera dhidi yake" (Isaya 59:19).

Yesu aliwaahidi wanafunzi Wake: "Huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yohana 14:26). Lakini mafundisho ya Kristo yanatakiwa kuhifadhiwa mapema akilini ili Roho wa Mungu aweze kutukumbusha wakati wa hatari. "Moyoni mwangu nimeliweka neno lako" Daudi alisema, "Nisije nikakutenda dhambi" (Zaburi 119:11).

Wote wanaothamini maslahi yao ya milele inawapasa kuwa macho dhidi ya kuvamiwa na kutokuamini. Nguzo muhimu za ukweli zitashambuliwa. Haiwezekani kutokufikiwa na dhihaka na falsafa za uongo, mafundisho nyemelezi na hatarishi, ya ukafiri wa kisasa. Shetani anabuni majaribu yanayolingana na hali ya matabaka yote ya watu. Anawashambulia wasio na elimu kwa kejeli na dharau, wakati anawakabili wenye elimu kwa vipingamizi vya kisayansi na hoja za kifalsafa, njia zote zikilenga kuchochea mashaka au kudharau kwa Maandiko. Hata vijana wenye uzoefu mdogo wanapenyeza mashaka kuhusiana na kanuni za msingi za Ukristo. Na huu ukafiri wa vijana, ingawa ni wa juu juu, bado una mvuto mbaya. Wengi wanaongozwa kukejeli imani ya baba zao na kumdhihaki Roho wa neema (Waebrania 10:29). Maisha ya watu wengi yaliyokuwa na mwelekeo wa kumheshimu Mungu na kuwa baraka kwa ulimwengu yamechafuliwa na pumzi chafu ya ukafiri. Wote wanaotumainia maamuzi yenye majivuno ya hoja za kibinadamu na kudhani kuwa wanaweza kueleza siri za Kimungu na kufikia ukweli bila msaada wa hekima ya Mungu wananaswa katika mtego wa Shetani.

Tunaishi katika kipindi muhimu sana cha historia ya ulimwengu. Hatima ya umati mkubwa wa wakazi wa dunia inakaribia kuamriwa. Hali yetu njema ya baadaye na pia wokovu wa roho zingine hutegemea njia ambayo tunaifuata sasa. Tunahitaji kuongozwa na Roho wa ukweli. Kila mfuasi wa Kristo inampasa kuuliza kwa: "Bwana, inanipasa nifanye nini?" Inatupasa kujinyenyekesha mbele ya Bwana, kwa kufunga na kuomba, na kutafakari zaidi juu ya neno la Mungu, hususani juu ya matukio ya hukumu. Inatupasa sasa kutafuta uzoefu wa kina na hai katika mambo ya Mungu. Hatuna wakati wa kupoteza. Matukio muhimu yanatokea mbele yetu; tupo katika eneo ambalo limerogwa na Shetani. Msisinzie, askari wa Mungu; adui anavizia karibu, akiwa tayari wakati wowote, ikiwa mtazembea na kulala, kuwarukia na kuwafanya mawindo yake.

Wengi wamedanganyika kuhusiana na hali yao ya kweli mbele za Mungu. Wanajipongeza kwa matendo mabaya ambayo hawayafanyi, na wanasahau kuorodhesha matendo mema na yanayofaa ambayo Mungu anataka wayafanye, lakini ambayo

wamezembea kuyafanya. Haitoshi kuwa wao ni miti katika bustani ya Mungu. Inawapasa kukidhi matarajio Yake kwa kuzaa matunda. Anawawajibisha kwa kushindwa kutekeleza mambo yote mema ambayo walipaswa kuyafanya, akiwaimarisha kwa njia ya neema Yake. Katika vitabu vya mbinguni wameandikwa kama wataabishaji wa ardhi. Lakini hata tabaka hili sio kuwa halina tumaini kabisa. Hawa ambao wamedhihaki rehema ya Mungu na kudharau neema Yake, moyo wenye upendo na uvumilivu ungali unasihi. "Hivyo husema, Amka, wewe usinziaye, Ufufuke katika wafu, Na Kristo atakuangaza. Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; … mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu" (Waefeso 5:14-16).

Wakati wa kujaribiwa utakapofika, wale ambao wamelifanya neno la Mungu kuwa kanuni ya maisha yao watafunuliwa. Wakati wa kiangazi hakuna tofauti kati ya miti ya kijani na miti mingine; lakini wakati pepo za wakati wa baridi zinapokuja, miti ya kijani hubaki bila kubadilika, wakati miti mingine ikivuliwa majani yote. Kwa hiyo mtu anayejifanya kuwa Mkristo hawezi kutofautishwa na Mkristo wa kweli, lakini wakati umekaribia ambapo tofauti itaonekana. Acha upinzani utokee, acha ubaguzi wenye chuki na kukosa uvumilivu vishike hatamu, acha mateso yawashwe, ndipo wenye mioyo isiyojitoa kikamilifu na wanafiki watakapoyumba na kuiacha imani; lakini Mkristo wa kweli atasimama kama mwamba, imani yake itakuwa na nguvu zaidi, tumaini lake litang'ara zaidi, kuliko katika siku za mafanikio.

Anasema mtunga Zaburi: "Shuhuda zako ndizo nizifikirizo. Kwa mausia yako najipatia ufahamu, Ndiyo maana naichukia kila njia ya uongo" (Zaburi 119:99, 104). "Heri mtu yule aonaye hekima." "Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, Uenezao mizizi yake karibu na mto; Hautaona hofu wakati wa hari ujapo, Bali jani lake litakuwa bichi; Wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, Wala hautaacha kuzaa matunda" (Mithali 3:13; Yeremia 17:8).

Sura ya 38 - Onyo la Mwisho

"Naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza." "Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake" (Ufunuo 18:1, 2, 4).

Andiko hili huonesha mbele kwa wakati ambapo tangazo la anguko la Babeli, kama lilivyotolewa na malaika wa pili wa Ufunuo 14 (aya 8), litarudiwa, likiwa na nyongeza ya orodha ya matendo ya kifisadi ambayo yamekuwa yakiingia katika mashirika mbalimbali yanayounda Babeli, kwa kuwa ujumbe huo ulitolewa kwanza, wakati wa kiangazi cha mwaka 1844. Hali ya kutisha ya ulimwengu wa kidini imeelezwa hapa. Kwa kila tukio la kuukataa ukweli, akili za watu zinaingiwa na giza zaidi, mioyo yao inazidi kuwa migumu zaidi, mpaka wananaswa katika ugumu wa ukafiri. Kwa kupuuza maonyo ambayo Mungu ameyatoa, wataendelea kukanyaga moja ya kanuni za Amri Kumi, mpaka wanawatesa wale wanaoitakasa. Kristo anaonekana kuwa si kitu kwa sababu ya dharau ambayo imewekwa juu ya neno Lake na watu Wake. Mafundisho ya imani ya kuongea na wafu yanapokelewa na makanisa, kizuizi kilichowekwa kudhibiti moyo usiozaliwa upya kimeondolewa, na kukiri kuwa mtu wa dini kutakuwa joho la kuficha uovu uliokithiri. Imani katika maonesho ya kiroho inafungua mlango kwa roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani, na kwa njia hiyo mvuto wa malaika waovu utahisiwa katika makanisa.

Kuhusu Babeli, wakati ikioneshwa katika unabii huu, imeelezwa: "Dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake" (Ufunuo 18:5). Babeli imejaza kikombe cha hatia yake, na maangamizi yanakaribia kuiangukia. Lakini Mungu bado ana watu ndani ya Babeli; na kabla ya kutekelezwa kwa hukumu Zake, hawa watu waaminifu inapasa waitwe na watoke nje, ili wasishiriki dhambi zake na "wasipokee mapigo yake." Ndiyo maana kuna vuguvugu linawakilishwa na malaika anayeshuka kutoka mbinguni, akiangazia dunia yote kwa utukufu wake, akilia kwa sauti kuu, kutangaza dhambi za Babeli. Pamoja na ujumbe wake sauti inasikika: "Tokeni kwake, enyi watu wangu." Matangazo haya, yakiungana na ujumbe wa malaika wa tatu, huunda onyo la mwisho litakalotolewa kwa wakazi wa dunia.

Tukio linaloukabili ulimwengu ni la kutisha. Mamlaka za dunia, zikiungana pamoja kupigana vita dhidi ya amri za Mungu, zitatoa agizo kuwa "wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa" (Ufunuo 13:16), wafuate desturi za kanisa kwa utunzaji wa sabato ya uongo. Wote wanaokataa kutii agizo hilo watapata adhabu za kiserikali, na hatimaye watatangazwa kuwa wanastahili kifo. Kwa upande mwingine,

sheria ya Mungu inayoagiza pumziko la siku ya Muumbaji inadai utii na inatishia ghadhabu dhidi ya wale wote wanaovunja kanuni zake.

Baada ya agizo kuletwa kwa uwazi mbele ya mtu, yeyote atakayekanyaga sheria ya Mungu ili kutii agizo la mwanadamu anapokea alama ya mnyama; anapokea ishara ya utii kwa mamlaka anayochagua kuitii badala ya Mungu. Onyo kutoka mbinguni ni: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake" (Ufunuo 14:9, 10).

Lakini hakuna mtu hata mmoja ambaye atakutana na hasira ya Mungu mpaka ukweli umeingia katika akili yake na dhamiri yake, na umekataliwa. Kuna watu wengi ambao hawajapata fursa ya kusikia ukweli maalumu wa wakati huu. Ulazima wa amri ya nne haujawasilishwa mbele yao katika nuru yake halisi. Yeye anayesoma kila moyo na kupima kila nia hatamwacha mtu hata mmoja aliye na shauku ya kuujua ukweli, adanganywe kuhusu masuala ya msingi katika pambano. Amri haitashinikizwa juu ya watu katika hali ya upofu. Kila mtu atapewa nuru ya kutosha ili afanye uamuzi kwa akili.

Sabato itakuwa kipimo kikuu cha utiifu, kwa sababu ni kipengele cha ukweli ambacho kinabishaniwa sana kwa namna ya pekee. Wakati jaribio la mwisho litakapofika, mstari unaoonesha tofauti utachorwa kati ya wale wanaomtumikia Mungu na wale wasiomtumikia. Wakati ambapo utunzaji wa sabato ya uongo katika kutii sheria ya nchi, kinyume na amri ya nne, utakuwa uthibitisho wa kuitii mamlaka inayompinga Mungu, utunzaji wa Sabato ya kweli, katika kuitii sheria ya Mungu, ni ushahidi wa utii kwa Muumbaji. Wakati tabaka moja, kwa kukubali alama ya kujisalimisha kwa mamlaka za kidunia, wanapokea alama ya mnyama, tabaka jingine likichagua ishara ya utii kwa mamlaka ya Kimungu, wanapokea muhuri wa Mungu.

Tangu wakati huo na kurudi nyuma watu waliohubiri ukweli wa ujumbe wa malaika wa tatu, mara nyingi walionekana kama wavumishaji wa mambo ya kutisha. Utabiri wao kuwa kukosa uvumilivu wa kidini utatawala nchini Marekani, kuwa kanisa na serikali vitaungana na kuwatesa wale wanaotunza amri za Mungu, umetangazwa kuwa usio na msingi na imetangazwa kwa uhakika kuwa nchi hii haiwezi kuwa tofauti na jinsi ambavyo imekuwa siku zote—mtetezi wa uhuru wa kidini. Lakini suala la ulazimishaji wa utunzaji wa Jumapili linahamasishwa kila mahali, tukio ambalo limetiliwa mashaka na kutoaminiwa kwa muda mrefu linaonekana kama linakaribia, na ujumbe wa tatu utaleta matokeo ambayo hayajawahi kuletwa kabla ya hapo.

Katika kila kizazi Mungu ametuma watumishi wakemee dhambi, ulimwenguni na kanisani. Lakini watu wanatamani kuambiwa mambo laini, na ukweli ulio safi usiopakwa

vanishi haukubaliki. Wanamatengenezo wengi, walipoanza kazi yao, waliazimia kutumia busara kubwa katika kushambulia dhambi za kanisa na za taifa. Walitumaini, kwa njia ya mfano wa maisha safi ya Kikristo, wangewaongoza watu kwenye mafundisho ya Biblia. Lakini Roho wa Mungu alikuja juu yao kama alivyokuja kwa Eliya, akamsukuma kukemea dhambi za mfalme mwovu na watu walioasi; hawakuweza kujizuia kuhubiri matamko ya wazi ya Biblia—mafundisho ambayo walikuwa wazito kuyahubiri. Walisukumwa kutangaza kwa bidii ukweli na hatari iliyotishia roho. Maneno waliyopewa na Bwana waliyasema, bila kuogopa matokeo, na watu walilazimishwa kusikia onyo.

Hivyo ndivyo ujumbe wa malaika wa tatu utakavyohubiriwa. Wakati ukifika wa kuutangaza kwa nguvu nyingi zaidi kuliko wakati mwingine wo wote, Bwana atatenda kazi kwa njia ya vyombo vinyenyekevu, akiongoza akili za wale ambao wamejiweka wakfu kwa ajili ya huduma ya Bwana. Watendakazi watawezeshwa hususani kwa upako wa Roho Mtakatifu kuliko kwa njia ya mafunzo katika vyuo vya elimu. Watu wenye imani na maombi watabidishwa kutoka kwa juhudi takatifu, wakitangaza maneno ambayo Mungu atawapa. Dhambi za Babeli zitawekwa wazi. Matokeo ya kutisha ya kushinikiza uadhimishaji wa siku kuu za kikanisa kwa njia ya mamlaka za kiserikali, madhara ya imani ya kuongea na wafu, maendeleo ya kimya lakini ya kasi ya mamlaka ya upapa—vyote vitawekwa wazi. Kwa njia ya maonyo haya watu wataamshwa. Maelfu kwa maelfu watasikia ambao hawajawahi kusikia maneno kama haya. Kwa mshangao watasikia ushuhuda kuwa Babeli ni kanisa, lililoanguka kwa sababu ya makosa yake na dhambi zake, kwa sababu liliukataa ukweli liliotumiwa na Mbingu. Watu watakapowaendea walimu wao wa zamani wakiwa na swali la dhati, Je, mambo haya yako hivyo? Wachungaji watawasimulia hadithi za kutunga, watatoa unabii wa mambo laini, ili kupoza hofu zao na kunyamazisha dhamiri zao zilizoamshwa. Lakini, kwa kuwa wengi watakataa kuridhishwa na mamlaka za watu na kudai tamko la wazi la "Hivi ndivyo Bwana asemavyo," viongozi wa kanisa, sawa na Mafarisayo wa zamani, wakiwa wamekasirika kwa kuwa mamlaka yao imehojiwa, watakemea ujumbe huo wakisema kuwa ni ujumbe wa Shetani na watawachochea wapenda dhambi wawatukane na kuwatesa wale wanaoutangaza.

Pambano litakapopanuka na kuingia katika maeneo mapya na akili za watu kuvutwa na kugundua sheria ya Mungu iliyokanyagwa, Shetani ataamka. Nguvu iliyomo katika ujumbe itawakasirisha zaidi wale wanaoupinga ujumbe. Viongozi wa kidini watatumia nguvu nyingi sana kuizima nuru isije ikawamulikia waumini wao. Kwa kila njia iliyoko katika uwezo wao watajitahidi kukomesha mjadala wa masuala haya muhimu.

Kanisa litaomba msaada wa mkono wenye nguvu wa serikali, na, katika kazi hii wafuasi wa upapa na Waprotestanti wataungana. Vuguvugu la ulazimishaji wa Jumapili litakuwa na ujasiri mkubwa zaidi na litawekewa mikakati ya makusudi, sheria itatungwa dhidi ya watunzaji wa amri kumi. Watatishiwa kutozwa faini na kupelekwa kifungoni, na baadhi watapewa vyeo vikubwa, na zawadi na fursa zingine, kama vishawishi vya kuwafanya

wakane imani zao. Lakini jibu lao lisilobadilika ni: "Mtuoneshe kosa letu katika neno la Mungu"—ombi ambalo liliwahi kutolewa na Luther katika mazingira yanayofanana na hayo. Wanaofikishwa mahakamani wanatoa ushuhuda thabiti wenye nguvu kwa ajili ya ukweli, na baadhi ya wale wanaousikia wanachukua uamuzi wa kusimama pamoja na wale wanaotunza amri za Mungu. Kwa njia hiyo, nuru itapelekwa kwa maelfu ambao, kama isingekuwa kwa njia hiyo, wasingepata fursa ya kuujua ukweli huu.

Utii uliojengwa juu ya uelewa wa neno la Mungu utachukuliwa kuwa uasi. Kwa kufumbwa macho na Shetani, mzazi atatumia ukali na ukatili dhidi ya mtoto wake atakayeuamini ukweli. Upendo utatoweka; watoto watanyang'anywa urithi wao na watafukuzwa nyumbani. Maneno ya Paulo yatatimizwa kama yanavyosomeka: "Wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa" (2 Timotheo 3:12). Watetezi wa ukweli watakapokataa kuiheshimu sabato ya Jumapili, baadhi watatupwa gerezani, baadhi yao watakimbia nchi zao, badhi watafanywa kuwa watuma. Kwa hekima ya kibinadamu yote haya kwa sasa yanaonekana kama mambo yasiyowezekana; lakini Roho wa Mungu anayezuia atakapoondolewa kwa watu, wabaki wakiwa chini ya utawala wa Shetani, ambaye anachukia kanuni za Kiungu, kutakuwepo matukio ya ajabu.

Moyo unaweza kuwa mkatili wakati hofu ya Mungu na upendo Wake vinapokuwa vimeondolewa. Dhoruba inapokaribia, tabaka kubwa la wale ambao wameuamini ujumbe wa malaika wa tatu, lakini hawakutakaswa kwa njia ya kuutii ukweli, watatupilia mbali msimamo wao na watajiunga na kundi la wapinzani. Kwa kuungana na ulimwengu na kushiriki roho yake, watakuwa na mtazamo wa mambo unaofanana sana na wa ulimwengu; na wakati jaribu litakapokuja, watakuwa tayari kuchagua upande ulio rahisi, upande unaopendwa na wengi. Watu wenye talanta na wenye nafasi katika jamii, ambao awali walifurahia ukweli, watatumia mivuto yao kudanganya na kupoteza. Wanatokea kuwa maadui wakuu wa ndugu zao wa zamani. Wakati watunza Sabato watakapoletwa mbele ya mahakama kujibu maswali kuhusu imani yao, hawa waasi watakuwa mawakala makini wa Shetani katika kuwawakilisha vibaya na kuwashitaki, na kwa njia ya taarifa za uongo na kauli zisizokuwa za kweli watawachochea watawala dhidi yao.

Katika kipindi hiki cha mateso imani ya watumishi wa Bwana itajaribiwa. Watakuwa wametoa onyo kwa uaminifu, wakimwangalia Mungu na neno Lake pekee. Roho wa Mungu, akigusa mioyo yao, amewabidisha kusema. Wakisukumwa na bidii takatifu, na nguvu ya Mungu ikiwa juu yao, wataingia katika utekelezaji wa majukumu yao bila ya kuhofia matokeo ya kuwahubiria watu neno ambalo Bwana atawapa. Hawatajali maslahi yao ya muda, wala hawatajali heshima yao, au maisha yao. Hata hivyo, wakati dhoruba ya upinzani na dhihaka itakapopasukia juu yao, baadhi yao, kwa hofu na mshangao, watafikia hatua ya kusema: "Ikiwa tungejua mapema matokeo ya maneno yetu, tungenyamaza kabisa." Watazingirwa na matatizo makubwa. Shetani atawashambulia kwa majaribu makali. Kazi ambayo walikuwa wamejaribu kuifanya inaonekana kana kwamba iko nje ya uwezo wao kuikamilisha.

Watatishiwa kuuawa. Hamasa watakayoanza nayo itatoweka; lakini hawatakuwa na uwezo wa kurudi nyuma. Ndipo, kwa kuhisi kutokuwa na msaada kabisa, watamkimbilia Yeye aliye na nguvu zote awape nguvu. Watakumbuka kuwa maneno waliyoyasema hayakuwa maneno yao, bali Yake Yeye aliyekuwa amewaagiza kutoa onyo. Mungu aliweka ukweli katika mioyo yao, na wasingeweza kujizuia kuutangaza.

Majaribu kama hayo yalishawapata watu wa Mungu zama zilizopita. Wycliffe, Huss, Luther, Tyndale, Baxter, Wesley, walisisitiza kuwa mafundisho yote lazima yapimwe kwa kuyalinganisha na Biblia na walitangaza kuwa wangekataa kila kitu ambacho Biblia ilikitaa. Dhidi ya hawa mateso yalirindima kwa hasira kali; hata hivyo hawakuacha kutangaza ukweli. Vipindi mbalimbali na tofauti katika historia ya kanisa vina alama na kila kipindi kikiwa na alama yake ya ukweli fulani maalumu ulioibuliwa na kufundishwa kukidhi mahitaji maalumu ya watu wa Mungu kwa wakati huo. Kila ukweli mpya ulisonga mbele dhidi ya chuki na upinzani; wale waliobarikiwa na nuru ya ukweli huo walijaribiwa na kuteswa. Bwana hutoa ukweli maalumu kwa watu wakati wa dharura. Ni nani wanaothubutu kukataa kuutangaza? Anawaagiza watumishi wake kutangaza wito wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu. Hawawezi kukaa kimya, isipokuwa kwa kuhatarisha roho zao. Mabalozi wa Kristo hawapaswi kufikiria juu ya matokeo ya kutekeleza agizo la Mungu. Inawapasa kutekeleza wajibu wao na kumwachia Mungu matokeo.

Upinzani unapoinuka juu katika kilele cha ukali wake, watumishi wa Mungu wanatatizika; hii ni kwa sababu inaonekana kana kwamba wao ndio wamesababisha mgogoro huo. Lakini dhamiri na neno la Mungu vinawathibitishia kuwa wapo katika njia sahihi; na japokuwa majaribu yanaendelea, wanapewa nguvu ya kukabiliana nayo. Shindano hukua na kuwa karibu yao zaidi na kuwa kali zaidi, lakini imani na ujasiri huongezeka na kupanda kukabiliana na dharura iliyopo. Ushuhuda wao ni: “Hatuwezi kuthubutu kuchezea neno la Mungu, kuigawa sheria Yake takatifu; tukisema sehemu hii ni muhimu na sehemu hii siyo muhimu, ili tupendwe na ulimwengu.

Bwana tunayemtumikia aweza kutuokoa. Kristo amezishinda mamlaka za dunia; sisi tuogope ulimwengu ambao tayari umeshashindwa?” Mateso katika miundo yake mbalimbali ni mwendelezo wa kanuni ambayo itadumu kuwepo kwa kadiri Shetani atakavyodumu kuwepo na kwa kadiri Ukristo utakavyodumu kuwa na nguvu. Hakuna mtu anayeweza kumtumikia Mungu bila kujiletea upinzani wa majeshi ya giza dhidi yake mwenyewe. Malaika waovu watamshambulia, wakiogopa kuwa mvuto wake utawapokonya mateka wao kutoka katika mikono yao. Watu waovu, kwa kukemewa na mfano wake, wataungana pamoja wakitafuta kumtenga na Mungu kwa majaribu yanayovutia. Haya yasipofaulu kumwangusha, ndipo mamlaka yenye nguvu inatumika kumlazisha aende kinyume na dhamiri yake.

Lakini kwa kadiri Yesu anaendelea kuwa mwombezi wa mwanadamu katika patakatifu pa mbinguni, nguvu inayozuia ya Roho Mtakatifu inahisiwa na Watawala na watu. Kwa kiasi

fulani bado nguvu hii inatawala sheria za nchi. Isingekuwa kwa njia ya sheria hizi, hali ya ulimwengu ingekuwa mbaya zaidi ya ilivyo sasa. Wakati wengi wa watawala wetu ni mawakala hai wa Shetani, Mungu pia anao mawakala Wake miongoni mwa watu wakuu wa nchi. Adui anawasukuma watumishi wake wapendekeze hatua ambazo zingeweza kuzuia kazi ya Mungu; lakini viongozi wa serikali wanaomcha Bwana wanashawishiwa na malaika watakatifu wapinge mapendekezo kama hayo kwa hoja zisizoweza kujibiwa. Kwa njia hiyo watu wachace wanadhibiti mkondo wenye nguvu wa uovu. Upinzani wa maadui wa ukweli utadhibitiwa ili ujumbe wa malaika wa tatu uweze kufanya kazi yake. Wakati onyo la mwisho litakapotolewa, litavuta usikivu wa hawa viongozi wa umma ambao kwa njia yao Bwana anatenda kazi, na baadhi yao watakubali kuonya, na watasimama na watu wa Mungu katika kipindi cha taabu.

Malaika anayejiunga katika utangazaji wa ujumbe wa malaika ataangazia dunia yote kwa utukufu wake. Kazi inayoenea duniani kote na ambayo ina nguvu isiyokuwa ya kawaida imetabiriwa hapa. Vuguvugu la ujio wa pili la miaka ya 1840-44 lilikuwa udhihirisho wenye utukufu wa mamlaka ya Mungu; ujumbe wa malaika wa kwanza ulipelekwa kwa kituo cha umishenari ulimwenguni kote, na katika baadhi ya nchi kulikuwepo shauku ya kidini kubwa kuliko ilivyowahi kushuhudiwa katika nchi yoyote tangu wakati wa Matengenezo ya karne ya kumi na sita; lakini haya yote yatazidiwa na vuguvugu kuu litakalotokea chini ya onyo la mwisho la malaika wa tatu.

Kazi itakuwa kama ile ya Siku ya Pentekoste. Kama “mvua ya vuli” ilivyotolewa, kwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu wakati wa ufunguzi wa injili, kuwezesha kuchipuka kwa mbegu za thamani, kadhalika “mvua ya masika” itatolewa wakati wa kufunga injili kwa ajili ya kukomaza mavuno. “Nasi na tujue, naam, tukaendelee kumjua Bwana; kutokea kwake ni yakini kama asubuhi; naye atatujilia kama mvua, kama mvua ya vuli iinyweshayo nchi” (Hosea 6:3). “Furahini, basi, enyi wana wa Sayuni, mkamfurahie Bwana, Mungu wenu; kwa kuwa yeye huwapa ninyi mvua ya masika, kwa kipimo cha haki, naye huwanyeshea mvua, mvua ya masika, na mvua ya vuli, kama kwanza” (Yoeli 2:23). “Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu.”“Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa” (Matendo 2:17, 21).

Kazi kubwa ya injili itafungwa kwa udhihirisho wa nguvu ya Mungu ambayo siyo chini zaidi ya ile iliyoonekana wakati wa kuifungua. Unabii uliotimizwa katika umwagwaji wa mvua ya vuli wakati wa kufungua injili utatimizwa tena katika umwagwaji wa mvua vya masika wakati wa kufunga injili. Hapa kuna“nyakati za kuburudishwa” ambazo Petro alikuwa akizifikiria aliposema:“Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu” (Matendo 3:19, 20).

Watumishi wa Mungu, nyuso zao zote zikiwa zimeangazwa na kung’arishwa kwa mbaraka wa utakatifu, wataharakisha kutoka sehemu moja kwenda nyingine wakiwa na

ujumbe kutoka mbinguni. Kwa maelfu ya sauti duniani kote, onyo litatolewa. Miujiza itafanywa, wagonjwa wataponywa, na ishara na maajabu vitaandamana na waaminio. Shetani pia atatenda, kwa maajabu ya uwongo, hata akishusha moto kutoka mbinguni mbele ya watu (Ufunuo 13:13). Hivyo wakazi wa duniani watatakiwa kutoa msimamo wao.

Ujumbe utahubiriwa siyo kwa njia ya kutumia hoja sana bali kwa njia ya ushawishi wa kina wa Roho wa Mungu. Hoja zimekwishawasilishwa. Mbegu zimeshapandwa, na sasa zitachipuka na kuzaa matunda. Machapisho yaliyotawanywa na watenda kazi wa kimishenari yametoa mvuto wake, lakini wengi ambao akili zao ziliguswa walizuiwa kuelewa vizuri ukweli au walizuiwa kuutii ukweli. Sasa miale ya nuru inapenya kila mahali, ukweli unaonekana katika uwazi wake na watoto waaminifu wa Mungu wanakata kamba zilizokuwa zimewashika. Mishikamano ya kifamilia, mahusiano ya kikanisa, havina nguvu ya kuwazuia sasa. Ukweli una thamani kubwa zaidi kuliko mambo yote mengine. Licha ya mawakala ambao wataungana kusimama dhidi ya ukweli, watu wengi watakata shauri kusimama upande wa Bwana.

Sura ya 39 - Wakati wa Taabu

Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile" (Danieli 12:1).

Ujumbe wa malaika wa tatu utakapofungwa, rehema haitasihi tena kwa ajili ya wakazi wa dunia wenye hatia. Watu wa Mungu watakuwa wamekamilisha kazi yao. Tayari watakuwa wamekwishapokea "mvua ya masika," "kuburudishwa kwa kuwepo kwa Bwana," na watakuwa wamekwishajiandaa kwa ajili ya saa ya kujaribiwa iliyoko mbele yao. Malaika wanaharakisha kutoka na kuingia mbinguni. Malaika anayerudi kutoka duniani atatangaza kuwa kazi yake imekamilika; jaribio la mwisho limefanyika duniani, na wote ambao wamethibitika kuwa watiifu kwa amri za Mungu wamepokea "muhuri wa Mungu." Ndipo Yesu anasitisha maombezi Yake katika patakatifu pa mbinguni. Ananyanyua juu mikono Yake na kwa sauti kubwa anasema, "Imekwisha;" na jeshi lote la malaika wanavua taji zao anapotoa tangazo hili zito: "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa" (Ufunuo 22:11).

Kila kesi itakuwa imeamriwa kwa ajili ya uzima au mauti. Kristo atakuwa ameshafanya upatanisho kwa ajili ya watu Wake na atakuwa ameshafuta dhambi zao. Idadi ya raia Wake itakuwa imeshajulikana; "ufalme na mamlaka, na ukuu wa ufalme chini ya mbingu yote," karibu utatolewa kwa warithi wa wokovu, na Yesu karibu atatawazwa kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Anapotoka katika patakatifu, giza linawafunika wakazi wa dunia. Katika wakati ule wa kutisha wenye haki watapaswa kuishi mbele za Mungu mtakatifu bila mwombezi. Kizuizi kilichokuwa kimewekwa kuwadhibiti waovu kinaondolewa, na Shetani anapata utawala kamili juu ya watu wasiotubu. Uvumilivu wa Mungu umefikia kikomo chake. Ulimwengu umekataa rehema Yake na umedhihaki upendo Wake, na umeikanyaga sheria Yake. Waovu wamevuka mpaka wa rehema yao; Roho wa Mungu, amepingwa kabisa kwa muda mrefu, hatimaye ameondolewa. Bila wigo wa neema ya Mungu, hawana ulinzi dhidi ya yule mwovu. Shetani atawaingiza wakazi wa dunia katika taabu moja, kubwa. Malaika wa Mungu wanapoacha kuzuia pepo kali za tamaa za kibinadamu, nguvu zote za asili za mapambano zitaachiliwa. Ulimwengu mzima utatumbukizwa katika maangamizi ya kutisha zaidi ya yale yaliyoupata mji wa Yerusalemu ya zamani.

Malaika mmoja aliwaangamiza wazaliwa wote wa kwanza wa Wamisri na kuijaza nchi yote kwa kilio. Wakati Daudi alipomkosea Mungu kwa kuhesabu watu, malaika mmoja alisababisha maangamizi ambayo kwa njia ya hayo dhambi ya Daudi iliadhibiwa. Nguvu hiyo

ya maangamizi inayotumiwa na malaika watakatifu Mungu anapowaamrisha kufanya hivyo, inatumiwa na malaika waovu Mungu anaporuhusu. Kuna majeshi sasa kila mahali yaliyo tayari, na ambayo yanasubiri tu ruhusa ya Mungu, kusambaza ukiwa kila mahali. Wale wanaoheshimu sheria ya Mungu wamekuwa wakishitakiwa kwa kuleta hukumu juu ya ulimwengu, na watachukuliwa kuwa chanzo cha matetemeko ya nguvu za asili na migogoro na umwagaji damu miongoni mwa watu vitu ambavyo vinajaza misiba duniani kote. Nguvu iliyomo katika onyo la mwisho itaamsha ghadhabu ya waovu; hasira inawashwa dhidi ya wote waliopokea ujumbe, na Shetani atachochea tena kwa nguvu zaidi roho ya chuki na mateso.

Wakati uwepo wa Mungu ulipoondolewa hatimaye kutoka kwa taifa la Kiyahudi, makuhani na watu wa kawaida hawakujua. Ingawa walikuwa chini ya utawala wa Shetani, na wakiendeshwa na tamaa za kutisha sana na mbaya kuliko kawaida, bado walijihesabu kuwa wao ni wateule wa Mungu. Huduma katika hekalu ziliendelea; kafara ziliendelea kutolewa juu ya madhahabu zake zilizonajisiwa, na kila siku mbaraka wa Mungu ulikuwa ukiombwa kwa ajili ya watu ambao walikuwa na hatia ya kumwaga damu ya Mwana mpendwa wa Mungu na waliokuwa wakitafuta kuwaua waumishi na mitume Wake. Kadhalika wakati uamuzi usioweza kubadilishwa wa patakatifu utakapotangazwa na hatima ya ulimwengu kuamriwa milele, wakazi wa dunia hawatajua kinachoendelea. Ibada za aina mbalimbali za dini zitakuwa zikiendelezwa na watu ambao Roho wa Mungu atakuwa ameondolewa kwao hatimaye; na bidii ya kishetani ambayo mwovu ataivuvia ndani yao ili watekeleze mipango yake mibaya, itafanana na bidii kwa ajili ya Mungu.

Kwa kuwa Sabato itakuwa imekuwa suala maalumu linalobishaniwa katika ulimwengu wote wa Ukristo, na mamlaka za kidini na kiserikali zitakuwa zimeungana pamoja kulazimisha uadhimishaji wa Jumapili, kukataa bila kubadilika kwa kundi la watu wachache kujisalimisha kwa matakwa ya watu wengi kutawafanya kuwa walengwa wa laana ya ulimwengu wote. Itadaiwa kuwa watu wachache wanaopingana na taasisi ya kanisa na sheria ya nchi hawapaswi kuvumiliwa; kuwa ni bora kwao wateswe kuliko mataifa yote kuingizwa katika machafuko na uasi. Hoja hiyo hiyo karne nyingi zilizopita ilitolewa dhidi ya Kristo na "wakubwa wa watu." "Wala hamfikiri ya kwamba," alisema Kayafa mwerevu, "yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala lisiangamie taifa zima" (Yohana 11:50). Hoja hii itaonekana kuwa hitimisho; na amri itatolewa hatimaye dhidi ya wale wote wanaotukuza Sabato ya amri ya nne, ikiwahukumu kuwa wanaostahili adhabu kali sana na ikiwapa watu uhuru, baada ya muda fulani, kuwaua. Urumi katika Ulimwengu wa Kale na Uprotestanti ulioasi katika Ulimwengu Mpya watapitia njia hiyo hiyo dhidi ya wale wanaoheshimu amri zote za Mungu.

Watu wa Mungu watatumbukizwa katika zile mandhari za mateso na maudhi yaliyoelezwa na nabii kama wakati wa taabu ya Yakobo. "Maana Bwana asema hivi, Tumesikia sauti ya tetemeko, na ya hofu, wala si ya amani. … nyuso zote zimegeuka rangi.

Ole! Maana siku ile ni kuu, hata hapana inayofanana nayo, maana ni wakati wa taabu yake Yakobo; lakini ataokolewa nayo" (Yeremia 30:5-7).

Usiku wa maumivu ya moyoni ya Yakobo, alipopambana katika maombi kwa ajili ya ukombozi kutoka katika mkono wa Esau (Mwanzo 32:24-30), huwakilisha uzoefu wa watu wa Mungu katika wakati wa taabu. Kwa sababu ya udanganyifu uliotumiwa na Yakobo kupata mbaraka wa baba yake, mbaraka uliokuwa umekusudiwa kwa ajili ya Esau kaka yake, Yakobo alikimbia kuokoa maisha yake, akijihami dhidi ya vitisho vya kifo vya kaka yake. Baada ya kukaa kwa miaka mingi uhamishoni, aliamua kurudi nyumbani, kwa amri ya Mungu, kurudi pamoja na wake zake na watoto wake, kondoo na ng'ombe, katika nchi alikozaliwa. Alipokaribia katika mpaka wa nchi, alijazwa na hofu alipopata habari kuwa Esau alikuwa anakaribia akiongoza kundi la watu wa vita, bila shaka akiwa amejielekeza kulipiza kisasi.

Kundi la Yakobo, likiwa halina silaha na bila ulinzi, lilionekana kukaribia kuwa wahanga wa ukatili na kifo bila msaada wowote. Na juu ya mzigo wa wasiwasi na hofu uliongezeka uzito uliomwumiza zaidi wa aibu binafsi, kwa sababu ilikuwa dhambi yake iliyoleta hatari hii. Tumaini lake pekee lilikuwa katika rehema ya Mungu; ulinzi wake pekee lazima uwe maombi. Lakini haachi kufanya kila jambo lililo katika uwezo wake kufanya upatanisho kwa kosa alilomfanyia kaka yake ili kuepusha hatari iliyotishia kutokea. Kadhalika inawapasa wafuasi wa Kristo, wanapokaribia wakati wa taabu, wafanye kila linalowezakana kujiweka katika nuru sahihi mbele ya watu, kupunguza chuki isiyokuwa na sababu, na kuepusha hatari inayotishia uhuru wa dhamiri.

Baada ya kuondoa familia, ili wasione taabu yake, Yakobo anabaki peke yake kumwomba Mungu. Anaungama dhambi yake na anakiri, kwa shukurani kubwa, rehema ya Mungu kwake wakati huo huo, kwa unyenyekevu mkubwa, anajenga hoja ya maombi yake kwa kurejea agano ambalo Mungu alifanya na baba zake na ahadi ambazo Mungu alizitoa kwake yeye mwenyewe katika njozi ya usiku kule Betheli na wakati akiwa katika nchi ya uhamishoni. Kilele cha taabu katika maisha yake kilikuwa kimefika; kila kitu kipo hatarini. Akiwa gizani na akiwa mpweke anaendelea kuomba na kujinyenyekesha mbele ya Mungu. Kwa ghafla mkono unalazwa juu ya bega lake. Anafikiri kuwa adui anatafuta uhai wake, na kwa nguvu zake zote za kukata tamaa anashikana mweleka na mpinzani wake.

Kunapoanza kupambazuka, mgeni anaongeza nguvu zake zisizo za kibinadamu; kwa mguso wa huyo mgeni Yakobo aliyekuwa na nguvu nyingi anaonekana kama aliyepigwa na kiharusi, na Yakobo, mwombaji asiye na msaada, anayelia, anaangukia kwenye shingo ya mpinzani wake wa maajabu. Yakobo anagundua sasa kuwa ni Malaika wa agano ambaye alikuwa akipigana naye mieleka. Japokuwa alipata ulemavu na kubaki na maumivu makali, hakuacha kusudi lake. Kwa muda mrefu amehimili mashaka, huzuni, na taabu kwa ajili ya dhambi yake; sasa ni lazima apate uhakika kuwa dhambi yake imesamehewa. Mgeni wa

Kimungu anaonekana kama anataka kuondoka; lakini Yakobo anamng'ang'ania, akimwomba ambariki. Malaika anasisitiza, "Niache, niende, maana kunapambazuka;" lakini mzee akapiga kelele, "Sikuachi, usiponibariki." Ni ujasiri, uimara, na uthabiti mkubwa kiasi gani unaooneshwa hapa! Kama lingekuwa dai la kujivuna, lenye kiburi, Yakobo angeuawa mara moja; lakini dai lake lilikuwa la uhakikisho wa mtu anayeungama udhaifu wake na kutokufaa kwake, lakini linalotumaini rehema ya Mungu atunzaye agano.

"Alikuwa na uwezo juu ya malaika akashinda" (Hosea 12:4). Kwa njia ya kujishusha, toba, na kujisalimisha, mtu huyu mwenye dhambi, mkosaji, na anayekufa, alishinda pamoja na Mungu Mkuu wa mbinguni. Ingawa alikuwa akitetemeka alidumu kushikilia ahadi za Mungu, na moyo wenye Upendo usio na Kikomo haukuweza kutupilia mbali ombi la mwenye dhambi. Kama ushahidi wa ushindi wake na neno la kuwatia moyo wengine wajifunze mfano wake, jina lake lilibadilishwa kutoka lile lililokumbushia dhambi yake, hadi lile lililosherehekea ushindi wake. Na ukweli kuwa Yakobo alishinda pamoja na Mungu ulikuwa uhakikisho kuwa angeweza kushinda pamoja na wanadamu. Hakuwa na hofu tena ya kukutana na hasira ya kaka yake, kwa kuwa Bwana alikuwa ulinzi wake.

Shetani alikuwa amemshitaki Yakobo mbele ya malaika wa Mungu, akidai haki ya kumwua kwa sababu ya dhambi yake; alikuwa amemsukuma Esau dhidi yake; na katika usiku mrefu wa mzee kupigana mieleka na Malaika, Shetani alijaribu kumshinikiza Yakobo ajisikie kuwa mwenye hatia ili amkatishe tamaa hatimaye ajiondoe kwa Mungu. Karibu Yakobo afikie hatua ya kukata tamaa; lakini alijua kuwa bila msaada wa Mungu alikuwa amekwisha kabisa. Alikuwa ametubu kwa dhati dhambi yake kubwa, na alimwomba Mungu amrehemu. Asingeweza kugeuzwa aliache kusudi lake, badala yake alimshikilia Malaika na akasisitiza ombi lake kwa kilio cha dhati na uchungu mwingi hadi akapata ushindi.

Kama Shetani alivyomshawishi Esau aende dhidi ya Yakobo, kadhalika Shetani atawachochea waovu wawaangamize watu wa Mungu katika wakati wa taabu. Na kama alivyomshitaki Yakobo, atashinikiza mashitaka yake dhidi ya watu wa Mungu. Anahesabu watu wote ulimwenguni kama raia wake; lakini kundi dogo la watu wanaotunza amri za Mungu wanapinga utawala wake. Ikiwa angeweza kuwafutilia mbali wote watoke duniani, ushindi wake ungekuwa kamili. Anaona kuwa malaika wanawalinda, na anagundua kuwa dhambi zao zimesamehewa; lakini hajui kuwa kesi zao zimekwisha kuamriwa katika patakatifu mbinguni. Anayo taarifa kamili ya dhambi ambazo aliwajaribu wakazitenda, na anaziwasilisha mbele ya Mungu katika mwonekano ulioongezwa chumvi, akiwakilisha watu hawa kuwa wanaostahili kama yeye kuwekwa nje ya ukubali wa Mungu. Anatangaza kuwa Bwana hawezi kwa haki kusamehe dhambi zao na bado amwangamize yeye na malaika zake. Anadai kuwa wao ni mawindo yake na anasisitiza kuwa wawekwe mikononi mwake awaangamize.

Shetani anapowashitaki watu wa Mungu kuhusiana na dhambi zao, Bwana anamruhusu awajaribu kwa nguvu zake zote. Matumaini yao kwa Mungu, imani yao na uimara wao, vitajaribiwa sana. Wanapotafakari maisha yao ya nyuma, matumaini yao yanazama; kwa kuwa katika maisha yao hawaoni jambo lo lote jema walilolitenda. Wanatambua zaidi udhaifu wao na kutokufaa kwao. Shetani anajitahidi kuwatishia akiwa na wazo kuwa kesi zao hazina matumaini, kuwa doa la uchafu wao halitasafishika kamwe. Anatumaini kuwaharibu imani yao kiasi cha kufanya wajisalimishe kwa majaribu yake na waache kumtii Mungu.

Ingawa watu wa Mungu watazungukwa na adui wanaojielekeza kuwaangamiza, taabu waliyonayo siyo hofu ya mateso kwa ajili ya ukweli; wanaogopa kuwa kila dhambi haijatubiwa, na kwamba kwa njia ya kosa lao wao wenyewe watashindwa kutimiziwa ahadi ya Mwokozi: "mimi nami nitakulinda, utoke katika saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi" Ufunuo 3:10). Ikiwa wangekuwa na hakika ya msamaha wasingekuwa na hofu ya mateso au kifo; lakini ikiwa wataonekana hawastahili, na watapoteza maisha yao kwa sababu ya dosari zao za tabia, maana yake jina takatifu la Mungu lingedharauliwa.

Kila upande wanasikia mipango ikifanywa ya uhaini na wanaona utendaji wa harakati za uasi; na shauku kubwa inaamka ndani yao, tamanio la dhati la moyoni, kwamba uasi huu mkubwa ukomeshwe na uovu wa waovu ufike mwisho. Lakini wakati wakimlilia Mungu asitishe kazi ya uasi, ni katika hali ya utambuzi makini wa kujidhili kuwa wao wenyewe hawana nguvu zaidi ya kupinga na kurudisha nyuma mkondo wenye unguvu wa uovu. Wanahisi kuwa ikiwa wangetumia siku zote uwezo wao wote katika huduma ya Kristo, wakienda mbele kutoka nguvu hadi nguvu, majeshi ya Shetani yangekuwa na nguvu ndogo ya kushindana nao.

Wanatesa roho zao mbele ya Mungu, wakielekeza akili zao kwa toba za zamani za dhambi zao nyingi, na kudai ahadi ya Mwokozi:"Au azishike nguvu zangu, Afanye amani nami; Naam, afanye amani nami" (Isaya 27:5). Imani yao haitindiki kwa sababu maombi yao hayajibiwi upesi. Ingawa wanapata wasiwasi, hofu, na udhia, hawaachi kufanya maombi. Wanang'ang'ania nguvu ya Mungu kama Yakobo alivyomng'ang'ania Malaika; na lugha ya roho zao ni: "Sikuachi, usiponibariki."

Kama Yakobo angekuwa hajatubu dhambi yake ya kupata haki ya uzaliwa wa kwanza kwa udanganyifu, Mungu asingesikia ombi lake na asingehifadhi maisha yake. Kadhalika, wakati wa taabu, ikiwa watu wa Mungu wangekuwa na dhambi zisizoungamwa zikatokea mbele yao wakati wakiteswa kwa hofu na maumivu, wangezidiwa; kukata tamaa kungekata imani yao, na wasingekuwa na ujasiri wa kuendelea kumwomba Mungu awaokoe. Lakini wakati wakiwa na ufahamu wa kina wa kutokustahili kwao, hawana makosa yaliyofichwa ya kufunua. Dhambi zao zimetangulia hukumuni na zimekwisha kufuta, na hawawezi kuzikumbuka.

Shetani huwaongoza wengi kuamini kuwa Mungu hajali ukosefu wa uaminifu katika mambo madogo ya maisha; lakini Bwana anaonesha katika jinsi alivyoshughulika na Yakobo kuwa kwa vyo vyote vile hawezi kuidhinisha au kuvumilia uovu. Wote wanaojaribu kutolea udhuru au kuficha dhambi zao, na wanaruhusu zibaki katika vitabu vya mbinguni, bila kuungamwa na kusamehewa, watashindwa na Shetani. Kwa kadiri kazi zao zinavyokuwa za juu na vyeo vyao vinavyokuwa vya heshima zaidi, ndivyo mwonekano wao mbele za Mungu unavyokuwa mbaya zaidi na ndivyo ushindi wa adui mkuu unavyokuwa wa hakika zaidi. Wale wanaochelewa kufanya matayarisho kwa ajili ya siku ya Mungu hawatakuwa tayari wakati wa taabu au wakati mwingine wo wote utakaofuata. Kesi za wote kama hao hazina matumaini.

Wakristo wanaokuja katika pambano la mwisho la kutisha bila kujiandaa, katika hali ya kukata tamaa, wataungama dhambi zao kwa maneno yenye maumivu makubwa, wakati waovu wakifurahia dhiki zao. Maungamo haya yana sifa zinazofanana na zile za maovu ya Esau na Yuda. Wanaofanya maungamo ya jinsi hiyo, huhuzunikia matokeo ya makosa yao, siyo hatia yao. Hawahisi toba ya kweli, hakuna chuki dhidi ya dhambi. Wanakiri dhambi yao, kwa sababu ya kuogopa adhabu; lakini, kama alivyokuwa Farao wa zamani, wanarudia kumkufuru Mungu baada ya hukumu kuondolewa.

Historia ya Yakobo pia ni uhakikisho kuwa Mungu hawatupi watu wan aodanganywanakujaribiwakutendadhambi, lakiniambaowanamrudia kwa toba ya kweli. Wakati ambapo Shetani hutafuta kuliangamiza tabaka hili la watu, Mungu hutuma malaika kuwafariji na kuwalinda wakati wa hatari. Mashambulizi ya Shetani ni makali na ya kudhamiria, madanganyifu yake ni ya kutisha; lakini jicho la Bwana liko juu ya watu Wake, na jina Lake husikia vilio vyao. Mateso yao ni makali, ndimi za mioto za tanuru zinaonekana kuwaangamiza; lakini Mtakasaji atawatoa wakiwa safi kama dhahabu iliyojaribiwa katika moto. Upendo wa Mungu kwa ajili ya watoto Wake wakati wa kipindi cha majaribu yao makali una nguvu na huruma kama ulivyo nyakati za mafanikio makubwa; lakini ni muhimu kwao kuwekwa katika tanuru la moto; kutofaa kwao lazima kuunguzwe, ili Sura ya Kristo iakisiwe kikamilifu.

Kipindi cha taabu na maumivu kilichopo mbele yetu kitahitaji imani inayoweza kustahimili uchovu, kuchelewa, na njaa—imani ambayo haitazimia hata kama ikijaribiwa vikali. Wakati wa rehema umetolewa kwa wote kujiandaa kwa ajili ya wakati huo. Yakobo alishinda kwa sababu alivumilia bila kukata tamaa na alidhamiria. Ushindi wake ni ushahidi wa nguvu ya maombi ya kutokukata tamaa. Wote wanaoshikilia ahadi za Mungu, kama alivyofanya, na wakawa wenye moyo wa dhati na wasiokata tamaa kama alivyokuwa, watafanikiwa kama alivyofanikiwa. Wale ambao hawako tayari kujikana nafsi, kuomboleza mbele za Mungu, kuomba kwa muda mrefu na kwa dhati kwa ajili ya mbaraka Wake hawataupata. Kupigana mieleka na Mungu—ni wachache kiasi gani! Ni wachache kiasi gani wameruhusu roho zao zivutwe kumtafuta Mungu kwa shauku kubwa mpaka kila msuli wa

nguvu zao umefika kikomo chake. Mawimbi ya kukata tamaa ambayo hakuna lugha inayoweza kueleza juu ya mwombaji, ni wachache kiasi gani hung'ang'ania kwa imani isiyokata tamaa ahadi za Mungu.

Wale ambao wana imani kidogo sasa, wapo katika hatari ya kuangukia chini ya nguvu ya udanganyifu wa kishetani na amri ya kulazimisha dhamiri. Na hata kama wakistahimili jaribu watatumbukizwa katika udhia na huzuni zaidi wakati wa taabu, kwa sababu hawana mazoea ya kumtumaini Mungu. Masomo ya imani ambayo watalazimishwa kujifunza chini ya shinikizo kubwa la kukata tamaa.

Inatupasa kujielimisha wenyewe kuhusu Mungu kwa kuthibitisha ahadi zake. Malaika wanaandika kumbukumbu ya kila ombi la dhati na kung'ang'ania. Inatupasa zaidi kuachana na tamaa za kujipendeza nafsi kuliko kuacha mawasiliano na Mungu. Umaskini wa kutupwa, kujikana nafsi sana, kwa idhini Yake, ni muhimu zaidi kuliko utajiri, heshima, urahisi, na urafiki bila idhini yake. Ikiwa tutaruhusu akili zetu zitawaliwe na mambo ya kidunia, Bwana anaweza kutupatia muda kwa kutunyang'anya miungu yetu ya dhahabu, ya nyuma, au ya ardhi yenye rutuba.

Vijana wasingedanganywa kutenda dhambi ikiwa wangekataa kuingia katika njia yo yote ile isipokuwa ile ambayo wakiipita wangeweza kuomba mbaraka wa Mungu. Ikiwa wajumbe wanaochukua onyo kuu la mwisho ulimwenguni wangeomba kwa ajili ya mbaraka wa Mungu, siyo kwa ubaridi, ulegevu, na uvivu, bali kwa hamasa na imani, kama Yakobo alivyofanya, wangepata mahali pengi ambapo wangeweza kusema: "Nimeonana na Mungu uso kwa uso, na nafsi yangu imeokoka" (Mwanzo 32:30). Wangehesabiwa na mbingu kuwa wakuu, wakiwa na nguvu ya kushinda pamoja na Mungu na wanadamu.

"Wakati wa taabu, ambao mfano wake haujawahi kuwapo," umekaribia; na tutahitaji uzoefu ambao hatuna kwa sasa na ambao tunaweza kuwa wavivu kuupata. Mara nyingi taabu ni kubwa katika kuitarajia kuliko uhalisia; lakini haiko hivyo katika uzoefu wa zahama iliyoko mbele yetu. Wasilisho la wazi zaidi kuliko yote haliwezi kuelezea vizuri kiwango cha mateso hayo. Katika wakati huo wa majaribu, kila roho itapaswa kusimama yenyewe peke yake mbele za Mungu. "Wajapokuwamo ndani yake Nuhu, na Danieli, na Ayubu, kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, hawataokoa wana wala binti; watajiokoa nafsi zao tu kwa haki yao" (Ezekieli 14:20).

Sasa, wakati Kuhani wetu Mkuu anafanya upatanisho kwa ajili yetu, inatupasa kutafuta kuwa wakamilifu katika Kristo. Siyo hata kwa wazo angeweza Mwokozi wetu kushindwa na jaribu. Shetani hupata katika mioyo ya wanadamu jambo analoweza kushikilia; shauku ya dhambi inayolelewa, ambayo kwa njia yake majaribu yake huelekeza nguvu zake. Lakini Kristo Mwenyewe alisema: "Yuaja mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu kwangu" (Yohana 14:30). Shetani hakuweza kupata chochote ndani ya Mwana wa Mungu ambacho

kingemwezesha kupata ushindi. Alitunza amri za Baba Yake, na hakukuwa na dhambi ndani Yake ambayo Shetani angeweza kuitumia kwa maslahi yake. Hii ndiyo hali ambayo wanapaswa kuwa nayo wale watakaosimama wakati wa taabu.

Ni katika maisha haya ambapo inatupasa kujitenga na dhambi, kwa njia ya imani katika damu ya upatanisho ya Kristo. Mwokozi wetu wa thamani anatualika tushikamane Naye, tuunganishe udhaifu wetu na nguvu Yake, ujinga wetu na hekima Yake, kutostahili na kustahili Kwake. Uongozi wa Mungu ni shule ambayo inatuwezesha kujifunza unyenyekevu na upole wa Yesu. Bwana anaweka daima mbele yetu, siyo kama tunavyochagua, kinachoonekana kuwa rahisi kwetu na kinachotupendeza zaidi, lakini kilicho na makusudi ya kweli katika maisha. Inabaki wajibu wetu kushirikiana na mawakala ambao Mbingu huwatumia katika kazi ya kujenga tabia zetu kulingana na mfano wa Mungu. Hakuna anayeweza kupuuzia au kuahirisha kazi hii bila kuhatarisha roho yake.

Mtume Yohana katika njozi alisikia sauti kuu mbinguni ikitangaza: “Ole wa nchi na bahari! Kwa maana yule Ibilisi ameshuka kwenu mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu” (Ufunuo 12:12). Mandhari zinazosababisha kutolewa kwa sauti hii ya mbinguni ni za kutisha. Hasira ya Shetani inaongezeka kwa kadiri wakati wake unavyozidi kuwa mfupi, na kazi ya uongo na uuaji itafikia kilele chake wakati wa taabu. Matukio yanayopita akili za kibinadamu siyo muda mrefu yataanza kuonekana mbinguni, kama ishara ya nguvu ya utendaji kazi wa kimiujiza wa mashetani. Roho za mashetani zitawaendea wafalme wa dunia na ulimwengu wote, kuwafungia katika uongo, na kuwasihi wajiunge na Shetani katika pambano lake la mwisho dhidi ya serikali ya mbinguni. Kwa njia ya mawakala hawa, watawala na watawaliwa kwa pamoja watadanganywa. Watu watainuka wakijifanya kuwa Kristo Mwenyewe, na wakidai kuwa na cheo na hadhi ya kuabudiwa ambavyo vinamstahili Mkombozi wa ulimwengu. Watatenda miujiza ya ajabu ya uponyaji na watadai kuwa na mafunuo kutoka mbinguni yanayopingana na ushuhuda wa Maandiko.

Kama tendo la juu kabisa katika sakata kuu la uongo, Shetani mwenyewe atajifanya kuwa Kristo. Kwa muda mrefu kanisa limetangaza kuwa ujio wa pili wa Kristo ndiyo kilele cha matumaini yake. Sasa mdanganyaji mkuu atafanya ionekane kana kwamba Kristo amekuja. Katika sehemu mbalimbali za dunia, Shetani atajidhihirisha miongoni mwa wanadamu kama mfalme mkuu mwenye nuru kuu, akifanana na mwonekano wa Mwana wa Mungu aliyeelezewa na Yohana katika kitabu cha Ufunuo (Ufunuo 1:13-15).

Utukufu unaomzunguka haupitwi na kitu chochote ambacho macho ya mwanadamu anayekufa yamewahi kukiona. Kelele za ushindi zinasikika hewani: “Kristo amekuja! Kristo amekuja!” Watu wanaanguka kifudifudi chini kwa heshima mbele yake, wakati ameinua mikono yake juu na anatamka baraka juu yao, kama vile Kristo alivyowabariki wanafunzi Wake alipokuwa duniani. Sauti yake ni laini na tulivu, lakini ikiwa tamu. Kwa sauti ya upole na huruma anasema baadhi ya mambo ya neema ile ile, kweli za mbinguni ambazo Kristo

alizisema; anaponya magonjwa ya watu, na ndipo, katika kujifanya kwake Kristo, anadai aliibadili Sabato na kuifanya Jumapili, na anawaamrisha watu wote kuiadhimisha siku ambayo ameibariki. Anatangaza kuwa wale watakaoendelea kutunza siku ya saba wanakufuru jina lake kwa kukataa kuwasikiliza malaika zake aliowatuma kwao wakiwa na nuru na ukweli. Huu ni uongo wenye nguvu, unaowanasa karibu watu wote. Kama vile Wasamaria walivyodanganywa na Simoni Magusi, umati wa watu, kutoka mdogo hadi mkubwa kabisa, wanasikiliza uchawi huu, wakisema: Huu ni "uweza wa Mungu, ule Mkuu" (Matendo 8:10).

Lakini watu wa Mungu hawatapotoshwa. Mafundisho ya Kristo bandia yanapingana na Maandiko. Mbaraka unatamkwa juu ya watu wanaomwabudu mnyama na sanamu yake, tabaka lile lile ambalo Biblia inasema kuwa ghadhabu ya Mungu isiyochanganywa itamwagwa juu yao. Na, zaidi ya hapo, Shetani hapewi ruhusa ya kuigiza jinsi Kristo atakavyokuja mara ya pili. Mwokozi aliwaonya watu Wake dhidi ya uongo kuhusiana na kipengele hiki, na alieleza kwa uwazi jinsi ujio Wake wa pili utakavyokuwa. "Watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki. Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu" (Mathayo 24:24-27, 31; 25:31; Ufunuo 1:7; 1 Wathesalonike 4:16, 17). Ujio huu hakuna uwezekano wa kuuigiza. Utajulikana mahali pote—utashuhudiwa na ulimwengu wote.

Ni wale tu ambao watakuwa wanafunzi wa Maandiko wenye bidii na ambao wanaupenda ukweli watakingwa dhidi ya madanganyifu yenye nguvu ambayo yatauteka ulimwengu. Kwa njia ya ushuhuda wa Biblia hawa watamgundua mdanganyaji katika joho lake bandia. Wakati wa kujaribiwa utakuja kwa watu wote. Kwa njia ya chekeche la jaribu Mkristo wa kweli atafunuliwa. Je, watu wa Mungu sasa wameimarishwa juu ya neno Lake kiasi kwamba hawataangushwa na ushahidi wa hisia zao? Je, katika zahama hiyo, wataweza kung'ang'ania Biblia na Biblia pekee? Shetani, ikiwezekana, atawazuia wasifanye maandalizi ya kuwawezesha kusimama katika siku ile. Anapanga mambo kwa namna ambayo anazuia njia yao, anawanasa kwa hazina za dunia, kuwafanya wabebe mzigo mzito, unaochosha, kwamba kazi yao iweze kuzidiwa na shughuli za maisha haya na siku ya kujaribiwa iwajie kama mwizi.

Wakati amri itakayotolewa na watawala mbalimbali wa ulimwengu wa Kikristo dhidi ya watunzao amri kumi watakapoondoa ulinzi wa serikali na kuwaachia mikononi mwa wale wanaotamani kuwaua, watu wa Mungu watakimbia kutoka mijini na vijijini na watajiunga pamoja katika vikundi, wakiishi katika maeneo ya mbali na yaliyojificha. Wengi watajificha katika miamba na milima. Kama Wakristo wa mabonde ya Piedmonti, watatumia vilele vya milima kuwa maficho na watamshukuru Mungu kwa ajili ya"ngome ya majabali" (Isaya 33:16). Lakini mengi ya mataifa yote na ya matabaka ya wote, ya juu na ya chini, tajiri na maskini, weusi na weupe, watatupwa katika utumwa wa kidhalimu na katili kuliko utumwa wa mwingine wo wote ule. Wapendwa wa Mungu wanapitia katika siku za uchovu, wakiwa

wamefungwa kwa minyororo, wakiwa wamefungwa magerezani, baadhi wakiwa wameachwa wafe kwa njaa gizani na magereza machafu.

Hakuna sikio la kibinadamu liko wazi kusikia vilio vyao; hakuna mkono wa kibinadamu ulioko tayari kutoa msaada. Je, Bwana atawasahau watu wake katika saa hii ya majaribu? Je, Mungu alimsahau Nuhu mwaminifu wakati hukumu zilipomwagwa juu ya ulimwengu wakati wa Gharika? Je, Mungu alimsahau Lutu wakati moto uliposhuka kutoka mbinguni kuiteketeza miji ya uwandani? Je, Mungu alimsahau Yusufu alipokuwa amezungukwa na waabudu sanamu wa Misri? Je, Mungu alimsahau Eliya wakati kiapo cha Yezebeli kilipomtisha baada ya kuwaua manabii wa Baali? Je, alimsahau Yeremia katika shimo lenye giza na kina kirefu la nyumba ya gereza lake? Je, Mungu aliwasahau vijana watatu wa Kiebrania katika tanuru liwakalo moto? Je, Mungu alimsahau Danieli katika tundu la sima?

"Sayuni alisema, YEHOVA ameniacha, Bwana amenisahau. Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye, hata asimhurumie mwana wa tumbo lake? Naam, hawa waweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe. Tazama, nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu" (Isaya 49:14-16). Bwana wa majeshi anasema: "Yeye awagusaye ninyi aigusa mboni ya jicho lake" (Zekaria 2:8).

Ingawa adui waweza kuwatupa gerezani, bado kuta za gereza haziwezi kukata mawasiliano kati ya roho zao na Kristo. Yeye aonaye kila udhaifu wao, Yeye ajuaye kila jaribu lao, yuko juu ya mamlaka zote za kidunia; na malaika watawatembelea katika vyumba vyao vya upweke, kuwaletea nuru na amani kutoka mbinguni. Gereza litakuwa kama ikulu; kwa kuwa wenye imani kubwa wanaishi pale, na kuta zenye huzuni zitaangaziwa kwa nuru ya mbinguni kama wakati ule Paulo na Sila walipoimba nyimbo za sifa katika usiku wa manane katika gereza la Filipi.

Hukumu za Mungu zitamwagwa juu ya watu wanaotafuta kuwatesa na kuwaua watu wa Mungu. Huruma Yake kwa waovu inawapa watu ujasiri katika uovu, lakini adhabu yao, ni ya hakika na ya kutisha kwa sababu imecheleweshwa kwa muda mrefu. "Bwana ataondoka kama vile katika mlima Perasimu, ataghadhibika kama vile katika bonde la Gibeoni; apate kufanya kazi yake, kazi yake ya ajabu; na kulitimiza tendo lake, tendo lake la ajabu" (Isaya 28:21). Kwa Mungu wetu mwenye rehema tendo la kuadhibu ni tendo la ajabu. "Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu" (Ezekieli 33:11).

Bwana ni "mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli,... mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi." Hata hivyo siyo "mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe." "Bwana si mwepesi wa hasira, ana uweza mwingi, wala hatamhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe" (Kutoka 34:6, 7; Nahumu 1:3). Kwa njia ya mambo ya kutisha ya haki atathibitisha mamlaka ya sheria Yake iliyokanyagwa. Ukali wa adhabu inayomsubiri mkosaji inaweza kupimwa kwa subira ya

Mungu katika kutekeleza hukumu. Taifa ambalo Mungu analivumilia sana, taifa ambalo hatalipiga mpaka lijaze kipimo cha uovu wake katika akaunti ya Mungu, hatimaye litakunywa kutoka katika kikombe cha hasira isiyochanganywa na rehema.

Wakati Kristo anapomaliza maombezi Yake katika patakatifu, hasira isiyochanganywa na kitu inayotishia wale wanaomwabudu mnyama na sanamu yake na kuipokea chapa yake (Ufunuo 14:9, 10), itamwagwa. Mapigo juu ya Misri wakati Mungu alipokuwa karibu kuwaokoa Waisraeli yalifanana katika sifa na zile hukumu za kutisha na kubwa zaidi zitakazoanguka juu ya ulimwengu mara tu kabla ya ukombozi wa mwisho wa watu wa Mungu. Anasema nabii wa Ufunuo, akielezea mapigo yale ya kutisha: "Pakawa na jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wenye kuisujudia sanamu yake." Bahari "ikawa damu kama damu ya mfu, na vitu vyote vyenye roho ya uhai katika bahari vikafa." Na "mito na chemchemi za maji … zikawa damu."

Mapigo haya, ya kutisha kama yalivyo, yanathibitisha haki ya Mungu kikamilifu. Malaika wa Mungu anatangaza: "Wewe u mwenye haki, uliyeko na uliyekuwako, Mtakatifu, kwa kuwa umehukumu hivi; kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu na ya manabii, nawe umewapa damu wainywe; nao wamestahili" (Ufunuo 16:2-6). Kwa kuwahukumu watu wa Mungu wafe, wamejipatia hatia ya damu kana kwamba ilimwagwa na mikono yao. Kwa jinsi iyo hiyo Kristo aliwatangaza Wayahudi wa wakati Wake kuwa wenye hatia ya damu ya watakatifu iliyomwagwa tangu siku za Habili; kwani walikuwa na roho ile ile na walikuwa wakitafuta kufanya kazi ile ile ya wauaji wa manabii.

Katika pigo linalofuata, nguvu inatolewa kwa jua "kuwaunguza wanadamu kwa moto. Wanadamu wakaunguzwa maunguzo makubwa" (Aya ya 8, 9). Manabii wanaeleza hali ya dunia wakati huu wa kutisha kama ifuatavyo: "Nchi inaomboleza; ... Maana mavuno ya mashamba yamepotea. Miti yote ya mashamba imekauka; Maana furaha imekauka katika wanadamu." "Mbegu zinaoza chini ya udongo wake; ghala zimeachwa ukiwa. Jinsi wanyama wanavyougua! Makundi ya ng'ombe yamefadhaika, kwa sababu hawana malisho Vijito vya maji vimekauka,

Na moto umeyateketeza malisho ya nyikani." "Tena nyimbo za hekaluni zitakuwa vilio siku ile, asema Bwana MUNGU; mizoga itakuwa mingi; kila mahali wataitupa, wakinyamaza kimya" (Yoeli 1:10-12, 17-20; Amosi 8:3). Mapigo haya hayatokei duniani kote, vinginevyo wakazi wote wa dunia wangefyekwa. Hata hivyo, yatakuwa mapigo ya kutisha zaidi kuliko mapigo yo yote yanayojulikana kwa wanadamu. Hukumu zote juu ya wanadamu, kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema, yamekuwa yakichanganywa na rehema. Damu ya Kristo inayosihi imekuwa ikimkinga mwenye dhambi asipokee kipimo kamili cha hatia yake; lakini katika hukumu ya mwisho, hasira inamwagwa pasipo kuchanganywa na rehema.

Katika siku hiyo, watu watatamani hifadhi ya rehema ya Mungu ambayo wamekuwa wakiidhihaki kwa muda mrefu. “Angalia, siku zinakuja, asema Bwana MUNGU, ambazo nitaleta njaa katika nchi; si njaa ya kukosa chakula, wala kiu ya kukosa maji, bali ya kukosa kuyasikia maneno ya Bwana. Nao watatanga-tanga toka bahari hata bahari; na toka upande wa kaskazi hata upande wa mashariki; watapiga mbio, wakienda huko na huko, kulitafuta neno la Bwana, wasilione” (Amosi 8:11, 12).

Watu wa Mungu hawataepuka kabisa mateso; lakini hata katika mateso na fadhaa, pamoja na umaskini na ukosefu wa chakula, hawataachwa waangamie. Kwamba Mungu aliyemtunza Eliya hatamwacha hata mmojawapo wa watoto Wake waliojitoa kafara kwa ajili Yake. Yeye ajuaye idadi ya nywele za vichwa vyao atawatunza, na wakati wa njaa watashibishwa. Wakati waovu wakifa kwa njaa na magonjwa, malaika watawalinda wenye haki na kuwapa mahitaji yao. Kwake “yeye aendaye kwa haki” kuna ahadi: “Atapewa chakula chake; maji yake hayatakoma.” “Maskini na wahitaji wanatafuta maji, wala hapana; ndimi zao zimekauka kwa kiu; mimi, Bwana, nitawasikia, mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha” (Isaya 33:15, 16; 41:17).

“Maana mtini hautachanua maua, Wala mizabibuni hamtakuwa na matunda; Taabu ya mzeituni itakuwa bure, Na mashamba hayatatoa chakula; Zizini hamtakuwa na kundi, Wala vibandani hamtakuwa na kundi la ng’ombe;” lakini wanaomcha Bwana “watamfurahia Bwana” na kumshangilia Mungu wa wokovu wao (Habakuki 3:17, 18).

“Bwana ndiye mlinzi wako; Bwana ni uvuli mkono wako wa kuume. Jua halitakupiga mchana, Wala mwezi wakati wa usiku. Bwana atakulinda na mabaya yote, Atakulinda nafsi yako.” “Maana Yeye atakuokoa na mtego wa mwindaji, Na katika tauni iharibuyo. Kwa manyoya yake atakufunika, Chini ya mbawa zake utapata kimbilio; Uaminifu wake ni ngao na kigao. Hutaogopa hofu ya usiku, Wala mshale urukao mchana, Wala tauni ipitayo gizani, Wala uele uharibuo adhuhuri, Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako. Naam, kumi elfu mkono wako wa kuume! Hata hivyo hautakukaribia wewe. Ila kwa macho yako utatazama, Na kuyaona malipo ya wasio haki. Kwa kuwa Wewe Bwana ndiwe kimbilio langu; Umemfanya Aliye juu kuwa makao yako. Mabaya hayatakupata wewe, Wala tauni haitaikaribia hema yako” (Zaburi 121:5-7; 91:3-10).

Walakini kwa macho ya kibinadamu itaonekana kana kwamba watu wa Mungu muda si mrefu watalazimika kuweka muhuri ushuhuda wao kwa damu yao kama walivyofanya wafia dini kabla yao. Wao wenyewe wanaanza kuogopa kuwa Bwana amewaacha wafie katika mikono ya maadui zao. Ni kipindi cha uchungu wa kutisha. Mchana na usiku wanamlilia Mungu awakomboe. Waovu wanafurahia, na vicheko vyao vya kejeli vinasikika: “Imani yenu sasa iko wapi? Kwa nini Mungu asiwaokoe kutoka katika mikono yetu ikiwa kweli ninyi ni watu Wake?” Lakini wenye subira wanamkumbuka Yesu akifa juu ya msalaba wa Kalwari na makuhani wakuu na watawala wakipiga kelele kwa dhihaka: “Aliokoa wengine, hawezi

kujiokoa mwenyewe Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini" (Mathayo 27:41, 42). Kama Yakobo, wote wanapigana mieleka na Mungu. Nyuso zao zinaeleza pambano lililoko ndani yao. Kusinyaa kunaonekana katika kila uso. Lakini hawaachi maombi yao.

Ikiwa watu wangeona kwa macho ya kimbingu, wangeona makundi ya malaika wenye nguvu nyingi na za ajabu wakiwa wamewazunguka wale ambao wamelitunza neno la subira ya Kristo. Kwa huruma na upole, malaika wameshuhudia fadhaa zao na wamesikia maombi yao. Wanasubiri neno la Kamanda wao wawachomoe na kuwatoa katika hatari inayowakabili. Lakini inawapasa wasubiri kidogo zaidi. Inawapasa watu wa Mungu kukinywea kikombe na kubatizwa kwa ubatizo. Kuchelewa, pamoja na maumivu yake, ndiyo jibu zuri zaidi kuliko yote kwa maombi yao. Wanapojitahidi kusubiri, huku wakimtumainia Bwana atende kazi wanajikuta wakitumia imani, tumaini, na uvumilivu, ambao ulitumiwa kidogo sana wakati wa uzoefu wao wa kidini. Lakini kwa ajili ya wateule muda wa taabu utafupishwa. "Na Mungu, je! Hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku? …. Nawaambia, atawapatia haki upesi" (Luka 18:7, 8). Mwisho utafika kwa haraka zaidi kuliko watu wanavyotegemea. Ngano itakusanywa na kufungwa matita matita kwa ajili ya kuwekwa katika ghala la Mungu; magugu yatafungwa pamoja kama miganda kwa ajili ya kuteketezwa.

Walinzi wa mbinguni, wakiwa waaminifu kwa dhamana yao, wanaendelea na ulinzi wao. Japokuwa amri ya jumla imeweka tarehe maalumu ya kuwaua watunza amri za Mungu, maadui zao katika baadhi ya mazingira watatarajia amri hiyo, na kabla ya wakati ulioamriwa, watajaribu kuwaua watunza amri za Mungu. Lakini hakuna hata mmoja atakayeweza kupenya jeshi la malaika wenye nguvu kubwa waliomzunguka kila mtu wa Mungu mwaminifu. Baadhi wanashambuliwa katika kukimbia kwao wakitoka katika miji na vijiji; lakini panga zilizoinuliwa dhidi yao zinavunjika na zinakosa nguvu na kuwa kama mabua. Wengine wanalindwa na malaika katika mfano wa watu wa vita.

Katika zama zote, Mungu ametenda kazi kwa njia ya malaika kuwasaidia na kuwaokoa watu Wake. Wenye uhai wa mbinguni wameshiriki katika masuala ya wanadamu. Wametokea katika mavazi yao yanayong'aa kama umeme wa radi; wamekuja kama watu waliovaa mavazi ya watu maskini. Malaika wametokea katika umbo la watu wa Mungu. Wamepumzika, kama watu waliochoka, mwaloni. Wamepokea ukarimu wa nyumba za wanadamu. Wamefanya kazi ya waongozaji kwa wasafiri waliochelewa kufika nyumbani. Kwa mikono yao, wamewasha mioto kwenye madhabahu.

Wamefungua milango ya magereza na kuwaachilia watumishi wa Bwana. Wakiwa wamevikwa mavazi ya mbinguni, walikuja kuliondoa jiwe kwenye mlango wa kaburi la Yesu. Katika umbo la wanadamu, malaika daima wako katika mikutano ya wenye haki; na wanatembelea mikutano ya waovu, kama walivyokwenda Sodoma, kuandika kumbukumbu za matendo yao, kuamua ikiwa wamevuka mpaka wa uvumilivu wa Mungu. Bwana hupenda

rehema; na kwa sababu ya watu wachache wanaomtumikia kwa moyo wa dhati, anazuia majanga na anaendeleza utangamano miongoni mwa makundi ya watu. Kidogo sana wenye dhambi dhidi ya Mungu hutambua kuwa wanawiwa kwa ajili ya maisha yao na waaminifu wachache ambao wanapenda kuwadhihaki na kuwatesa.

Ingawa watawala wa ulimwengu huu hawalitambui hili, lakini katika mabaraza yao malaika wamekuwa wasemaji. Macho ya wanadamu yamewaangalia; masikio ya wanadamu yamesikiliza hoja zao; midomo ya wanadamu imepinga mapendekezo yao na kudhihaki mashauri yao; mikono ya wanadamu imekutana nao kwa matusi na dharau. Katika ukumbi wa baraza na mahakama hawa wajumbe wa mbinguni wameonesha uelewa wa kina wa historia ya wanadamu; wamekuwa watetezi wazuri wa watu wanaokandimizwa kuliko watetezi wao wenye uwezo mkubwa na wenye ufasaha mkubwa. Wameshinda makusudi na kusitisha uovu ambao ungerudisha sana nyuma kazi ya Mungu na kusababisha mateso ya watu wa Mungu. Katika saa ya hatari na udhia "Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa" (Zaburi 34:7).

Kwa shauku ya dhati, watu wa Mungu wanasubiri kuona ishara za Mfalme wao ajaye. Kama walinzi walivyolikabili, "Habari gani za usiku?" jibu linatolewa bila kusita sita, "'Mchana unakuja na usiku pia' (Isaya 21:11, 12). Nuru inaangaza juu ya mawingu yaliyoko juu ya vilele vya milima. Siyo muda mrefu kutakuwepo na udhihirishaji wa utukufu Wake. Jua la haki litaangaza. Asubuhi na usiku vimekaribia—kufunguliwa kwa siku isiyo na mwisho kwa wenye haki, kuingia kwa usiku wa milele kwa waovu."

Wakati wapiga mieleka wanapeleka maombi yao ya dhati kwa Mungu, pazia linalowatenga na wenye uhai wasioonekana linaondolewa kwa sehemu kubwa. Mbingu zinang'aa kwa pambazuko la siku ya umilele, na kama sauti nzuri ya nyimbo za malaika maneno yanasikika: "Simama imara katika utii wako. Msaada unakuja." Kristo, Mshindi Mwenyezi, anawavalisha askari Wake waliochoka taji ya utukufu usioharibika; na sauti inatoka nje ya malango yaliyofunguliwa wazi: "Tazama, niko pamoja nawe. Usiogope. Ninazijua huzuni zako; nimeyachukua masikitiko yako. Vita yako siyo dhidi ya maadui ambao hawajajaribiwa. Nimepigana vita kwa ajili yenu, na katika jina Langu ninyi ni zaidi ya washindi."

Mwokozi wa thamani atatuma msaada wakati tunaouhitaji. Njia ya kwenda mbinguni imewekwa wakfu kwa njia ya alama ya nyayo. Kila mwiba unaoumiza nyayo zetu ulijeruhi nyayo Zake. Kila msalaba ambao tunaitwa kuubeba ameubeba kabla yetu. Bwana huruhusu mashindano, kuindaa roho kwa ajili ya amani. Wakati wa taabu ni wa mateso makubwa kwa watu wa Mungu; lakini ni wakati wa kila muumini wa kweli kutazama juu, na kwa imani waweze kuuona upinde wa ahadi ukiwazunguka pande zote.

“Nao waliokombolewa na Bwana watarejea, Watafika Sayuni, wakiimba; Furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao; Watapata shangwe na furaha; Huzuni na kuugua zitakimbia. Mimi, naam, mimi, ndimi niwafarijiye; wewe u nani hata ukamwogopa mtu atakayekufa, na mwanadamu atakayefanywa kuwa kama majani? Ukamsahau Bwana, Muumba wako, … nawe unaogopa daima mchana kutwa kwa sababu ya ghadhabu yake yeye aoneaye, hapo afanyapo tayari kuharibu; nayo i wapi ghadhabu yake aoneaye? Yeye aliyehamishwa na kufungwa atafunguliwa kwa haraka; wala hatakufa na kushuka shimoni, wala chakula chake hakitapunguka. Maana mimi ni Bwana, Mungu wako, niichafuaye bahari, mawimbi yake yakavuma. Bwana wa majeshi ndilo jina lake. Nami nimetia maneno yangu kinywani mwako, nami nimekusitiri katika kivuli cha mkono wangu, ili nizipande mbingu, na kuiweka misingi ya dunia, na kuuambia Sayuni, Ninyi ni watu wangu” (Isaya 51:11-16).

“Basi, kwa sababu ya hayo, ulisikilize neno hili, ewe uliyeteswa, na kulewa, lakini si kwa mvinyo; Bwana, Bwana wako na Mungu wako, awateteaye watu wake, asema hivi, Tazama, nimeondoa mkononi mwako kikombe cha kulevya-levya, hilo bakuli la kikombe cha hasira yangu; hutakinywea tena; nami nitakitia mikononi mwao wakutesao; waliokuambia nafsi yako, Inama, tupate kupita; nawe uliufanya mgongo wako kuwa kama nchi, na kama njia, kwa hao wapitao juu yake” (Aya 21-23).

Jicho la Mungu, likitazama katika zama zote, liliona zahama ambayo itawakabili watu Wake, wakati mamlaka za kidunia zitakapojipanga dhidi yao. Kama mateka wanavyokuwa uhamishoni, wataogopa kifo kwa kukosa chakula au kwa kufanyiwa ukatili. Lakini Yule Aliye Mtakatifu aliyegawanya Bahari ya Shamu, ataonesha nguvu Yake na kubadili umateka wao. “Nao watakuwa wangu, asema Bwana wa majeshi, katika siku ile niifanyayo; naam, watakuwa hazina yangu hasa; nami nitawaachilia, kama vile mtu amwachiliavyo mwanawe mwenyewe amtumikiaye” (Malaki 3:17).

Ikiwa damu ya mashahidi waaminifu ingemwagwa wakati huu, isingekuwa, kama ilivyokuwa damu ya wafia dini, kama mbegu iliyopandwa kutoa mavuno kwa ajili ya Mungu. Uaminifu wao usingekuwa ushuhuda wa kuwashawishi wengine waukubali ukweli; kwa kuwa moyo mgumu umerudisha nyuma mawimbi ya rehema mpaka hayawezi kuja tena. Ikiwa wenye haki wangeachwa wawe mawindo ya maadui zao, ingekuwa ushindi kwa upande wa mfalme wa giza. Mwandishi wa zaburi anasema: “Mradi atanisitiri bandani mwake siku ya mabaya, Atanisitiri katika sitara ya hema yake, Na kuniinua juu ya mwamba” (Zaburi 27:5).

Kristo alisema: “Njoni, watu wangu, ingia wewe ndani ya vyumba vyako, ukafunge mlango nyuma yako ujifiche kitambo kidogo, mpaka ghadhabu hii itakapopita. Kwa maana, tazama, Bwana anakuja kutoka mahali pake, ili kuwaadhibu wakaao duniani, kwa sababu ya uovu wao” (Isaya 26:20, 21). Ukombozi wa wale ambao wamesubiri kwa uvumilivu kwa ajili

ya ujio Wake na wale ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima utakuwa wa utukufu.

Sura ya 40 - Watu wa Mungu Wakombolewa

Wakati ulinzi wa sheria za kibinadamu utakapoondolewa kwa wale wanaoheshimu sheria ya Mungu, zitakuwepo, katika nchi mbalimbali, harakati za wakati uleule za kuwaua. Wakati uliopangwa utakapokaribia, watu watapatana kuangamiza kikundi cha watu wanaochukiwa. Itaazimiwa kuwapiga pigo moja la uhakika, ambalo litanyamazisha kabisa sauti ya mfarakano wa mawazo na onyo.

Watu wa Mungu—baadhi yao wakiwa katika vyumba vya gereza, baadhi wakiwa wamejificha katika maeneo ya siri misituni na milimani—wakingali katika kuomba kwa ajili ya ulinzi wa Mungu, wakati kila mahali makundi ya watu wenye silaha, wakishawishiwa na majeshi ya malaika waovu, wanajiandaa kwa ajili ya kazi ya mauji. Ni sasa, katika saa ya uhitaji, ambapo Mungu wa Israeli ataingilia kati kuwaokoa wateule Wake. Bwana anasema; “Mtakuwa na wimbo kama vile wakati wa usiku, ishikwapo sikukuu takatifu, mtakuwa na furaha ya moyo kama vile mtu aendapo ... katika mlima wa Bwana, aliye Mwamba wa Israeli. Naye Bwana atawasikizisha watu sauti yake ya utukufu, naye atawaonyesha jinsi mkono wake ushukavyo, na ghadhabu ya hasira yake, na mwako wa moto ulao, pamoja na dhoruba, na tufani, na mvua ya mawe ya barafu” (Isaya 30:29, 30).

Katikati ya kelele za ushindi, dhihaka, na laana, makundi ya watu waovu wanavamia mawindo yao, ambapo, tazama, giza nene, giza totoro kuliko usiku, linaifunika dunia. Ndipo upinde wa mvua, uking'aa kwa utukufu utokao katika kiti cha enzi cha Mungu, unaonekana mbinguni na unaonekana kuwazunguka kila kundi la watu wanaoomba. Makundi ya watu wenye hasira yanashtuka. Kelele zao za dhihaka zinakoma. Walengwa wa hasira zao za uuaji wanasahauliwa. Kwa hisia zenye hofu wanaona ishara ya agano la Mungu na wanatamani wakingwe dhidi ya mwangaza mkali unaowazidi nguvu.

Kwa upande wa watu wa Mungu sauti, ya wazi na tamu, inasikika, ikisema, “Tazameni juu,” na wanapoinua macho yao kutazama mbinguni, wanaona upinde wa ahadi. Mawingu meusi, yenye hasira yaliyokuwa yamefunika anga yanatawanyika, na, kama Stefano, wanatazama juu mbinguni kwa bidii, na wanauona utukufu wa Mungu na wa Mwana wa Adamu wakiwa wamekaa juu ya kiti Chake cha enzi. Katika umbo Lake la Kimungu wanatambua unyenyekevu Wake; na kutoka katika midomo Yake wanasikia ombi likiwasilishwa mbele ya Baba Yake na malaika watakatifu: “Hao ulionipa nataka wawe pamoja nami po pote nilipo” (Yohana 17:24). Tena sauti, nzuri na ya ushindi, inasikika, ikisema: “Waje! waje! watakatifu, hawana madhara, na ni safi. Wamelitunza neno la subira Yangu; watembee miongoni mwa malaika;” na midomo mikavu, inayotetemeka ya wale walioishika sana imani yao inapiga kelele ya ushindi.

Ni wakati wa usiku wa manane ambapo Mungu anadhihirisha nguvu Yake kwa ajili ya ukombozi wa watu Wake. Jua linatokea, liking'aa katika nguvu yake. Ishara na maajabu

vinatokea mfululizo na haraka haraka. Waovu wanayaona matukio hayo kwa hofu na mshangao, wakati wenye haki wanatazama kwa furaha kuu viashiria vya ukombozi wao. Kila kitu miongoni mwa vitu vya asili kinaonekana kuondoka katika utaratibu wake. Vijito vinaacha kutiririka. Mawingu meusi, mazito yanaibuka na yanagongana. Katikati ya mbingu zenye giza totoro kunaonekana mwanya mmoja wenye utukufu usioelezeka, ambamo kunatokea sauti ya Mungu kama sauti ya maji mengi, Ikisema: "Imekwisha kuwa" (Ufunuo 16:17).

Sauti ile inatetemesha mbingu na dunia. Kunatokea tetemeko kubwa sana, "ambalo tangu wanadamu kuwako juu ya nchi hapakuwa namna ile, jinsi lilivyokuwa kubwa tetemeko hilo" (Aya 17, 18). Anga linaonekana kufunguliwa na kufungwa. Utukufu kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu unakaribia kupenya anga. Milima inayumbayumba kama tete katika upepo, na mawe yenye sura mbaya yanasambazwa kila upande. Inasikika ngurumo kama ya tufani inayokuja. Bahari inachafuka. Inasikika sauti ya tufani kama sauti ya pepo waliotumwa kwenda kuangamiza. Dunia nzima inanyumbuka ikipanda na kushuka kama mawimbi ya bahari. Uso wa dunia unataka kuchanika. Misingi yake yenyewe inaonekana kama imeng'oka. Vilele vya milima vinazama. Visiwa vyenye wakazi vinatoweka. Bandari ambazo zimekuwa kama Sodoma kwa uovu zinamezwa na maji yenye dhoruba kali. Babeli mkuu unakumbukwa mbele za Mungu, "kupewa kikombe cha mvinyo ya ghadhabu ya hasira yake." Mvua ya mawe kubwa sana, kila moja "kama uzito wa talanta," inafanya kazi yake ya kuangamiza (Aya 19, 21). Miji yenye kiburi ya dunia inashushwa chini. Maeneo ya kifahari, ambayo wakuu wa dunia hii wameteketezea mali zao ili kujitukuza, yanaanguka na kuwa magofu mbele ya macho yao. Magereza yanapasuliwa, na watu wa Mungu, walioko mahabusu kwa sababu ya imani yao, wanaachiwa huru.

Makaburi yanafunguka, na "wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele" (Danieli 12:2). Wote ambao wamekufa katika imani ya ujumbe wa malaika wa tatu wanatoka makaburini wakiwa na utukufu, kusikia agano la Mungu la amani na wale ambao wameishika sheria Yake. "Na hao waliomchoma" (Ufunuo 1:7), wale waliodhihaki na kukejeli maumivu ya kifo cha Kristo, na wapinzani wakuu wa ukweli Wake na watu Wake, wanafufuliwa washuhudie heshima ikitolewa kwa wale waaminifu na watiifu.

Mawingu mazito bado yamelifunika anga; lakini jua linapenya mawingu na kuonekana kila baada ya muda fulani kupita, likionekana kama jicho la Yehova linalolipiza kisasi. Radi kali zinapiga kutoka mbinguni, zikiifunika dunia kwa shuka la ndimi za moto. Juu ya ngurumo za kutisha za radi, sauti, zisizojulikana na za kutisha, zinatangaza kifo kwa ajili ya waovu. Maneno yaliyosemwa hayaeleweki kwa wote; lakini yanaeleweka kikamilifu kwa walimu wa uongo. Wale waliokuwa kabla wakiwa wakorofi, waliokuwa wakijivuna na wasiojali, waliokuwa wakifurahia ukatili wao kwa watu watunzao amri za Mungu, sasa wanazidi kuwa na wasiwasi na wanatetemeka kwa hofu. Vilio vyao vinasikika juu ya sauti ya vitu vya asili.

Mashetani yanakiri uungu wa Kristo na yanatetemeka mbele ya nguvu Yake, wakati watu wakiomba kwa ajili ya rehema na kubembeleza katika hofu iliyokithiri.

Manabii wa zamani walisema, walipoiona siku ya Mungu katika njozi takatifu: "Pigeni kelele za hofu; maana siku ya Bwana i karibu; itanyesha kama maangamizi yatokayo kwa Mwenyezi Mungu" (Isaya 13:6). "Ingia ndani ya jabali; ukajifiche mavumbini mbele za utisho wa Bwana, mbele za utukufu wa enzi yake. Macho ya mwanadamu yaliyoinuka yatashushwa chini, na kiburi cha mwanadamu kitainamishwa, naye Bwana, yeye peke yake, atatukuzwa siku hiyo. Kwa maana kutakuwa siku ya Bwana wa majeshi juu ya watu wote wenye kiburi na majivuno, na juu ya yote yaliyoinuka; nayo yatashushwa chini." "Siku hiyo kila mtu atazitupilia mbali sanamu zake za fedha, na sanamu zake za dhahabu, walizojifanyia ili kuziabudu, kwa fuko na popo; ili aingie ndani ya pango za majabali, na ndani ya tundu za miamba iliyopasuka, mbele za utisho wa Bwana na utukufu wa enzi yake, atakapoondoka ili aitetemeshe mno dunia" (Isaya 2:10-12, 20, 21).

Kupitia ufa uliopo katikati ya mawingu nyota inamulika ambayo ukali wa mwanga wake umeongezwa mara nne kinyume na giza lililokuwepo. Inatangaza tumaini na furaha kwa waaminifu, lakini ukali na hasira kwa wavunjaji wa sheria ya Mungu. Wale ambao wameteseka kwa ajili ya Kristo sasa wako salama, wamefichwa katika hema la siri la Bwana. Wamejaribiwa, na mbele ya ulimwengu na mbele ya wenye dhihaka dhidi ya ukweli wameonesha uaminifu wao Kwake Yeye aliyekufa kwa ajili yao. Badiliko la ajabu limetokea kwa wale ambao wamedumisha uaminifu wao mbele ya kifo. Wamekombolewa kutoka katika ukatili wa giza na wa kutisha wa watu waliogeuzwa kuwa kama mashetani. Nyuso zao, ambazo mpaka wakati mfupi uliopita zilikuwa zimekauka, zikiwa na wasiwasi, na zikisumbuka, sasa zinang'aa kwa mshangao, imani, na upendo. Sauti zao zinapaa juu kwa wimbo wa ushindi: "Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari. Maji yake yajapovuma na kuumuka, Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake" (Zaburi 46:1-3).

Wakati maneno haya ya dhamana takatifu yanapanda kwa Mungu, mawingu yanarudi nyuma, na mbingu zenye nyota zinaonekana, zikiwa na utukufu usioelezeka kinyume na anga jeusi totoro upande huu na upande huu. Utukufu wa jiji la mbinguni unatiririka kutoka katika malango yaliyo wazi. Ndipo kunatokea angani mkono ulioshikilia mbao mbili za mawe pamoja. Nabii anasema: "Na mbingu zitatangaza haki yake, Kwa maana Mungu ndiye aliye hakimu" (Zaburi 50:6). Sheria takatifu, haki ya Mungu, ambayo katikati ya radi na ndimi za moto ilitangazwa kutoka Mlima Sinai kama mwongozo wa maisha, sasa inafunuliwa kwa watu kama kanuni ya hukumu. Mkono unafungua mbao zile, na zinaonekana Amri Kumi kama vile zimeandikwa kwa kalamu ya moto. Maneno ni ya wazi sana kiasi ambacho wote wanaweza kuyasoma. Kumbukumbu inaamshwa, giza la ushirikina na uzushi vinafutwa

kutoka akilini, na kauli kumi za Mungu, fupi, za kina, zenye mamlaka, zinawasilishwa machoni pa wakazi wa dunia.

Haiwezekani kueleza hofu na kukata tamaa kwa wale ambao wamekanyaga matakwa matakatifu ya Mungu. Mungu aliwapa sheria Yake; wangeweza kulinganisha na tabia zao na sheria hiyo na kurekebisha dosari zao wakati bado fursa ya kutubu na kufanya matengenezo ilipokuwepo; lakini ili kupata ukubali wa ulimwengu, waliweka pembeni kanuni zake na kuwafundisha wengine kuzivunja. Walijaribu kuwalazimisha watu wa Mungu kuinajisi Sabato Yake. Sasa wanaadhibiwa kwa sheria waliyoidharau. Kwa uwazi wa kutisha wanaona kuwa hawana udhuru. Walichagua yule ambaye walimtumikia na kumwabudu. “Ndipo mtakaporudi, nanyi mtapambanua kati ya wenye haki na waovu, na kati ya yeye amtumikiaye Mungu na yeye asiyemtumikia” (Malaki 3:18).

Maadui wa sheria ya Mungu, kutoka kwa wachungaji hadi kwa yule mdogo wao kabisa miongoni mwao, wanapata uelewa mpya wa ukweli na wajibu. Kwa kuchelewa sana wanaona kuwa Sabato ya amri ya nne ni muhuri wa Mungu aliye hai. Kwa kuchelewa sana wanaona asili ya kweli ya sabato yao bandia na msingi wa mchanga ambao wamekuwa wakijenga juu yake. Wanagundua kuwa wamekuwa wakipambana dhidi ya Mungu. Walimu wa dini wameongoza roho upotevuni huku wakifikiri kuwa waliwaongoza kwenda katika malango ya Paradiso. Ni mpaka siku ya hukumu ya mwisho ndipo utakapojulikana ukubwa wa wajibu wa watu walioko katika kazi takatifu na jinsi yalivyo ya kutisha matokeo ya kukosa uaminifu. Ni katika umilele peke yake ndipo tunaweza kukisia kwa usahihi hasara ya roho moja. Maangamizi yatakuwa ya kutisha ya mtu ambaye Mungu atamwambia: Ondoka, wewe mtumwa mwovu.

Sauti ya Mungu inasikika mbinguni, ikitangaza siku na saa ya kuja kwa Yesu, na inatoa agano la milele kwa watu Wake. Kama milio ya radi yenye sauti kubwa sana maneno Yake yanabiringika na kuenea duniani kote. Israeli wa Mungu wanasimama wakisikiliza, macho yao yakiwa yametazama juu. Nyuso zao zinang'aa kwa utukufu Wake, na wanang'aa kama uso wa Musa ulivyong'aa aliposhuka kutoka Mlima wa Sinai. Waovu hawawezi kuwaangalia. Na mbaraka unapotangazwa kwa wale waliomheshimu Mungu kwa kutunza Sabato Yake takatifu na kuitakasa, kuna sauti kubwa ya ushindi.

Muda si mrefu kunatokea upande wa mashariki wingu dogo jeusi, takribani ukubwa wa kiganja cha mtu. Ni wingu linalomzunguka Mwokozi na ambalo linaonekana kwa mbali kuzungukwa na giza. Watu wa Mungu wanatambua kuwa hii ni ishara ya Mwana wa Adamu. Kwa ukimya mkubwa wanalitazama linapokaribia duniani, likiwa jepesi na lenye utukufu zaidi, mpaka linakuwa wingu kubwa jeupe, chini kuna utukufu kama wa moto unaoteketeza, na juu yake kuna upinde wa mvua wa agano. Yesu anatokea kama mshindi mkuu.

Sasa siyo “Mtu wa huzuni,” ili kunywa kikombe kichungu cha aibu na mateso, anakuja, akiwa mshindi wa mbingu na nchi, awahukumu walio hai na waliokufa. “Mwaminifu na Wa-

kweli," "kwa haki ahukumu na kufanya vita." Na "majeshi yaliyo mbinguni" (Ufunuo 19:11, 14) wakamfuata. Pamoja na nyimbo za sauti ya mbinguni malaika, wengi, wasiokuwa na idadi, wanamsindikiza katika safari Yake. Anga lilionekana kujazwa na maumbo yanayong'aa—"elfu kumi mara elfu kumi, na elfu mara elfu." Hakuna kalamu inayoweza kueleza mandhari hiyo; hakuna akili yenye uwezo wa kuelewa utukufu wake. "Utukufu wake ukazifunika mbingu, Nayo dunia ikajaa sifa yake. Mwangaza wake ulikuwa kama nuru" (Habakuki 3:3, 4) . Wakati wingu lililo hai liliposogea zaidi, kila jicho lilimwona Mfalme wa uzima. Hakuna taji ya miiba inayoharibu kile kichwa kitakatifu; lakini utepe wa utukufu unatulia juu ya uso Wake mtakatifu. Uso Wake unang'aa zaidi kuliko mwangaza mkali wa jua la mchana." Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA" (Ufunuo 19:16).

Mbele Yake "nyuso zote zimegeuka rangi;" hofu ya kukata tamaa milele inaanguka juu ya wakataaji wa rehema ya Mungu. "Moyo unayeyuka, na magoti yanagongana-gongana; ... na nyuso za wote zimekuwa nyeupe kwa hofu" (Yeremia 30:6; Nahumu 2:10). Kilio cha haki na kutetemeka: "Ni nani awezaye kusimama?" Wimbo wa malaika ulisitishwa, na kinatokea kipindi cha ukimya mkubwa. Ndipo sauti ya Yesu inasikika, ikisema: "Neema Yangu inakutosha." Nyuso za wenye haki zinang'aa, na furaha inajaa ndani ya kila moyo. Na malaika wanapiga noti iliyo juu zaidi na kuimba tena wanavyosogea karibu na dunia.

Mfalme na wafalme anashuka juu ya wingu, akiwa amezingirwa na ndimi za moto. Mbingu zinakunjwa kama karatasi, dunia inatetemeka mbele Yake, na kila mlima na kisiwa kinaondoka mahali pake. "Mungu wetu atakuja wala hatanyamaza, Moto utakula mbele zake, na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote. Ataziita mbingu zilizo juu, Na nchi pia awahukumu watu wake" (Zaburi 50:3, 4).

"Na miguu yake kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba imesafishwa katika tanuru; na sauti yake kama sauti ya maji mengi. Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume; na upanga mkali, wenye makali kuwili, ukitoka katika kinywa chake; na uso wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake. Nami nilipomwona, nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akisema, Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho" (Ufunuo 6:15-17).

Kejeli na dharau vinakoma. Midomo ya waongo inanyamazishwa. Mgongano wa silaha, ghasia za vita, "wakati wa mshindo na mavazi yaliyofingirishwa katika damu" (Isaya 9:5), vinasitishwa. Hakuna sasa kinachosikika zaidi ya sauti ya maombi na sauti ya kilio na maombolezo. Kilio kinalipuka kutoka katika midomo ambayo muda mfupi uliopita ilikuwa ikidhihaki: "Siku kuu ya hasira Yake imekuja; ni nani awezaye kusimama?" Waovu wanaomba wafunikwe chini ya miamba na milima kuliko kukutana na uso wa Yeye ambaye wamekuwa wakimdhihaki na kumkataa.

Sauti ile ipenyayo sikio la wafu, wanaijua. Mara ngapi sauti inayosihi, ya upole imekuwa ikiwaita watubu. Mara ngapi sauti hiyo imesikika katika miito inayogusa ya rafiki, kaka, na Mkombozi. Kwa wanaokataa neema Yake hakuna sauti nyingine ambayo ilikabiliwa na lawama, kulemewa na shutuma sana, kama sauti ile ambayo kwa muda mrefu ilitoa wito: "Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa?" (Ezekieli 33:11). O, laiti ingekuwa sauti ya mgeni kwao! Yesu anasema: "Nimeita, nanyi mkakataa; Nimeunyosha mkono wangu, asiangalie mtu; Bali mmebatilisha shauri langu, Wala hamkutaka maonyo yangu" (Mithali 1:24, 25). Sauti inaamsha kumbukumbu ambazo walitamani zingekuwa zimefutwa— maonyo yaliyodhihakiwa, miito iliyokataliwa, fursa zilizopuuzwa.

Wapo wale waliomdhihaki Kristo wakati wa kudhalilishwa Kwake. Kwa nguvu na msisimko mkubwa wanayakumbuka maneno ya Yesu, alipoagizwa kwa kiapo na kuhani mkuu, alisema kwa mkazo: "Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni" (Mathayo 26:64). Sasa wanautazama utukufu Wake, na bado hawajamwona akiwa ameketi mkono wa kuume wa nguvu.

Waliodharau dai Lake la kuwa Mwana wa Mungu hawana cha kusema sasa. Yupo Herode mwenye kiburi aliyekejeli cheo Chake cha kifalme na kuwaagiza askari wenye dhihaka kumvika taji kama Mfalme. Kuna watu ambao kwa mikono yao najisi waliweka juu ya mwili Wake joho la zambarau, juu ya paji la uso Wake mtakatifu taji ya miiba, na katika mkono Wake usiokuwa na ubishi fimbo ya kifalme ya kuigiza, na kuinama mbele Yake kwa dhihaka yenye kufuru. Watu waliompiga na kumtemea mate Mfalme wa uzima sasa wanageuka pembeni wasiyatazame macho Yake na kutafuta kukimbia waende mbali na utukufu wa uwepo Wake. Waliopigilia misumari katika mikono Yake na nyayo Zake, askari aliyechoma mkuki ubavuni Mwake, wanaziona alama hizi kwa aibu.

Kwa uwazi wa kutisha makuhani na wandishi wanayakumbuka matukio ya Kalwari. Kwa hofu kubwa wanakumbuka sasa jinsi, wakitikisa vichwa vyao kwa furaha ya kishetani, walivyodai:"Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe. Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini. Amemtegemea Mungu; na amwokoe sasa, kama anamtaka; kwa maana alisema, Mimi ni Mwana wa Mungu" (Mathayo 27:42, 43).

Wanakumbuka wazi wazi mfano wa Mwokozi wa mpanzi aliyekataa kumpa bwana wao matunda ya shamba la mizabibu, aliyewadhihaki watumwa wake na kumwua mwanae. Wanakumbuka, pia, sentensi ambayo wao wenyewe waliitamka: Bwana wa shamba la mizabibu "atawaua wale watu waovu." Katika dhambi na adhabu ya wale wasiokuwa waaminifu makuhani na wazee wanaona njia yao na hatima yao. Na sasa kinainuka kilio cha uchungu wa kufa. Kikiwa cha sauti ya juu zaidi kuliko kelele za "Msulubishe, Msulubishe" zilizosikika katika mitaa yote ya Yerusalemu, kinageuka kuwa maombolezo ya kutisha, na kukata tamaa, "Ni Mwana wa Mungu! Ni Masihi wa kweli!" Wanatafuta kukimbia na

kuondoka katika uwepo wa Mfalme wa wafalme. Katika mashimo yenye kina kirefu ardhini, yaliyochimbwa na migongano ya vitu vya asili, wanajaribu kujificha bila mafanikio.

Katika maisha ya wote wanaoukataa ukweli kuna nyakati ambapo dhamiri inaamshwa, wakati kumbukumbu zinapoleta mambo ya zamani yanayotesa ya maisha ya unafiki na roho inaumia na kuwa na masikitiko yasiyosaidia cho chote. Lakini masikitiko haya ni nini ukilinganisha na huzuni ya siku ile wakati "hofu ... ifikapo kama tufani," wakati "msiba ... ufikapo kama kisulisuli"! (Mithali 1:27). Wale ambao walimwua Kristo na watu Wake waaminifu sasa wanashuhudia utukufu ukiwa juu yao. Katikati ya hofu yao wanasikia sauti za watakatifu wakiimba nyimbo za furaha wakishangilia: "Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja atusaidie" (Isaya 25:9).

Katikati ya kuwayawaya kwa dunia, mwangaza wa radi, na ngurumo za radi, sauti ya Mwana wa Mungu inawaita watakatifu waliolala usingizi wa mauti. Anayatazama makaburi ya wenye haki, ndipo, akiinua mikono yake juu mbinguni, anapiga kelele: "Amkeni, amkeni, amkeni, ninyi mnaolala katika mavumbi, na msimame!" Katika marefu na mapana ya dunia yote waliokufa wataisikia sauti ile, na watakaoisikia wataishi. Na dunia nzima itarindima kwa vishindo vya jeshi kubwa sana la watu wa kila taifa, jamaa, lugha, na kabila. Kutoka katika gereza la makaburi wanatoka, wakiwa wamevikwa utukufu usiokufa, wakisema: "Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?" (1 Wakorintho 15:55). Na wenye haki walio hai na watakatifu waliofufuliwa wanaunganisha sauti zao pamoja katika kelele za furaha na ushindi kwa muda mrefu.

Wote wanatoka katika makaburi yao wakiwa na kimo kilekile walichoingia nacho kaburini. Adamu, ambaye anasimama miongoni mwa watu waliofufuliwa, ana kimo kikubwa na umbo adhimu. Anaonekana kuwa na tofauti kubwa sana na watu wa vizazi vya baadaye; katika kipengere hiki kimoja kunaonekana poromoko katika ubora wa maisha ya mwanadamu. Lakini wote wanaamka wakiwa na upya na uhai wa ujana wa milele. Hapo mwanzo, mtu aliumbwa katika mfano wa Mungu, siyo tu katika tabia, bali pia katika umbo na mwonekano. Dhambi iliharibu na kufuta karibu kila mfano wa Kimungu; lakini Kristo alikuja kurudisha kile kilichopotea.

Atabadilisha miili yetu michafu na kuiumba upya ifanane na mwili Wake wa utukufu. Mwili unaokufa, ulioharibika, usiokuwa na uzuri, uliochafuliwa na dhambi, unakuwa kamili, mzuri, na usiokufa. Kasoro zote na ulemavu wa aina yo yote vinaachwa kaburini. Wakiwa wamerudishwa mahali palipo na mti wa uzima katika Edeni iliyopotea kwa miaka mingi, waliokombolewa "watakua" (Malaki 4:2) hadi wafikie kimo cha kizazi cha mwanadamu katika utukufu wake wa awali. Viashiria vya mwisho-mwisho vya laana ya dhambi vitaondolewa, na watu waaminifu wa Kristo watatokea katika "uzuri wa Bwana Mungu wetu," katika akili na roho na mwili, wakiakisi sura takatifu ya Bwana wao. Ndiyo, ukombozi

wa ajabu! Ulioongelewa kwa muda mrefu, uliotumainiwa kwa muda mrefu, uliofikiriwa kwa matarajio na shauku kubwa, lakini bila kueleweka kikamilifu.

Wenye haki walio hai wanabadilishwa "dakika moja, kufumba na kufumbua" Kwa sauti ya Mungu walitukuzwa; sasa wanafanywa kuwa wasiokufa na watakatifu waliofufuliwa wanachukuliwa kumlaki Bwana wao hewani. Malaika "wanawakusanya pamoja wateule Wake kutoka pepo nne, kutoka mwisho mmoja wa mbingu hadi mwisho mwingine." Watoto wadogo wanabebwa na malaika watakatifu na kuwapeleka kwa mama zao na kuwakabidhi katika mikono yao. Marafiki waliotenganishwa kwa kifo wanaunganishwa, wasitenganishwe tena, na wakiimba nyimbo za furaha wanapaa kwenda pamoja kuelekea katika mji wa Mungu.

Kila upande wa gari la wingu kuna mabawa, na chini yake kuna magurudumu hai; na magari yanapopaa kwenda juu, magurudumu yanapiga kelele, "Mtakatifu," na mabawa, yanaporuka, yanapiga kelele, "Mtakatifu," na msafara wa malaika wanapiga kelele, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mwenyezi." Na waliokombolewa wanapiga kelele, "Haleluya!" wakati gari linapoondoka kuelekea Yerusalemu.

Kabla ya kuingia Mji wa Mungu, Mwokozi anawapa wafuasi Wake nishani za ushindi na anawavalisha tepe za hadhi zao za kifalme. Waliokombolewa wakiwa wanang'aa wanapangwa katika umbo la mraba wenye nafasi katikati kumzunguka Mfalme wao, ambaye umbo Lake limepanda juu ya kila malaika na kila mtakatifu, ambaye uso Wake unaonekana kujaa upendo na wema. Kutoka kwa jeshi la watu wasiokuwa na idadi kila jicho limekazwa Kwake, kila jicho linauona utukufu Wake Yeye ambaye "Uso Wake uliharibiwa zaidi kuliko mtu mwingine ye yote, na umbo Lake liliharibiwa zaidi kuliko wanadamu wengine wote." Juu ya vichwa vya washindi, Yesu kwa mkono Wake wa kulia anaweka taji ya utukufu. Kwa kila mmoja kuna taji, iliyoandikwa "jina jipya" lake mwenyewe (Ufunuo 2:17), na maandishi, "Utakatifu kwa Bwana."

Katika kila mkono kunawekwa tawi la mtende la ushindi na kinubi kinachong'aa. Ndipo, wakati malaika waongozaji wanapopiga noti, kila mkono unafagia nyuzi za kinubi kwa mguso wenye stadi, ukiamsha muziki mtamu wenye sauti zenye melodi nzuri. Furaha isiyoelezeka inachemka ndani ya kila moyo, na kila sauti inainuliwa katika sifa na shukurani: "Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele" (Ufunuo 1:5, 6).

Mbele ya mkutano wa watu waliokombolewa kuna Mji Mtakatifu. Yesu anafungua malango ya lulu, na mataifa walioutunza ukweli wanaingia ndani. Pale wanaiona Paradiso ya Mungu, nyumba ya Adamu katika utakatifu wake. Ndipo sauti, iliyo nzuri kuliko muziki wo wote uliowahi kuingia sikio la mtu anayekufa, inasikika ikisema: "Pambano lenu

limekwisha.” “Njooni, nyinyi mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mlioandaliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

Sasa ombi la Mwokozi kwa wanafunzi Wake: “Hao ulionipa nataka wawe pamoja nami po pote nilipo.” “Mbele ya utukufu Wake bila mawaa katika furaha kuu” (Yuda 24), Kristo anawasilisha kwa Baba watu walionuliliwa kwa damu Yake, akitangaza:“Nipo hapa, na watoto ulionipa.” “Wote ulionipa nimewatunza.” Ndiyo, maajabu ya upendo unaokomboa! Furaha ya saa ile wakati Baba wa milele, akiwaangalia waliokombolewa, ataiona Sura ya ke, misuguano ya dhambi ikiwa imeondolewa, uozo wake ukiwa umefutiliwa mbali, na wanadamu wakiwa wamerudishwa tena katika mwafaka na Mungu!

Kwa upendo usioelezeka, Yesu anawakaribisha watu Wake waaminifu katika furaha ya Bwana wao. Furaha ya Mwokozi ni katika kuona, katika ufalme wa utukufu, roho zilizookolewa kwa mateso Yake na kudharauliwa Kwake. Na waliokombolewa watakuwa washiriki katika furaha Yake, wanapowaona, miongoni mwa waliokombolewa, wale waliowaleta kwa Kristo kupitia maombi yao, kazi zao, na upendo wao wa kujitoa kafara. Wanapokusanyika kando kando ya kiti cha enzi cheupe, furaha isiyoelezeka inajaza mioyo yao, wanapoona wale waliowaleta kwa Kristo, na kugundua kuwa mmoja aliwapata wengine, na bado hawa waliwapata wengine, wote wakiwa wameletwa katika bandari ya pumziko, pale kuweka taji zao kwenye miguu ya Yesu na kumsifu Yeye katika mizunguko isiyokoma ya umilele.

Wakati waliokombolewa walipokaribishwa katika Mji wa Mungu, kunatokea mlipuko wa furaha hewani kelele za furaha. Akina Adamu wawili wanakaribia kukutana. Mwana wa Mungu anasimama mikono Yake ikiwa imenyooshwa kumpokea baba wa kizazi chetu—mwenye uhai aliyemuumba Mwenyewe, aliyetenda dhambi dhidi ya Muumbaji wake, na ambaye kwa ajili ya dhambi yake alama za kuslubishwa zinaonekana katika mwili wa Mwokozi. Wakati Adamu anapotambua alama za misumari ya kikatili, haanguki katika kifua cha Bwana wake, lakini kwa unyenyekevu anajitupa chini kwenye nyayo Zake na kupiga kelele: “Anastahili, anastahili Mwanakondoo aliyechinjwa!” Kwa huruma Mwokozi anamwinua na kumwambia aitazame tena nyumba ya Edeni ambayo aliondolewa muda mrefu uliopita.

Baada ya kufukuzwa Edeni, maisha ya Adamu duniani yalijaa huzuni. Kila jani lililokauka, kila mnyama wa kafara, kila dosari katika uso mzuri wa uumbaji wa asili, kila doa katika usafi wa mwanadamu, ilikuwa ukumbusho wa dhambi yake. Ulikuwa wa kutisha uchungu wake alipoona ongezeko la uovu kila mahali, na, kama jibu kwa maonyo yake, alikutana na aibu iliyorushwa kwake kama msababishaji wa dhambi. Kwa uvumilivu na unyenyekevu alibeba, kwa takribani miaka elfu moja, adhabu ya makosa yake. Kwa uaminifu alitubu dhambi yake na kutumainia huruma za Mwokozi aliyeahidiwa, na alikufa katika

tumaini la ufufuo. Mwana wa Mungu alikomboa kushindwa na kuanguka kwa mwanadamu; na sasa, kwa njia ya kazi ya upatanisho, Adamu anarudishwa katika utawala wake wa kwanza.

Akiwa amebebwa na furaha, anatazama miti ambayo ilikuwa furaha yake kuiona mwanzoni—miti ile ile ambayo yeye mwenyewe alikuwa akikusanya matunda yake siku za maisha yake yasiyokuwa na hatia na nyakati ambazo alikuwa na furaha daima. Anaiona mizabibu ambayo mikono yake mwenyewe iliifundisha, na miti ile ile ya maua aliyofurahia kuitunza. Akili yake inaelewa uhalisia wa mandhari; anaelewa kuwa Edeni hii iliyorejeshwa upya, ni nzuri zaidi sasa kuliko ilivyokuwa wakati alipofukuzwa kutoka ndani yake. Mwokozi anamwongoza kwenda mahali ulipo mti wa uzima na anachuma tunda lenye utukufu na anamwagiza alile. Anawatazama waliomzunguka na anaona umati wa familia yake waliokombolewa, wakisimama katika Paradiso ya Mungu. Ndipo anatupa taji yake inayong'aa kwenye nyayo za Yesu na, akiangukia katika kifua cha Yesu, anamkumbatia Mwokozi. Anagusa kinubi cha dhahabu, na makuba ya mbinguni yanarudisha mwangwi wa wimbo wa ushindi: “Astahiliye, astahiliye, astahiliye ni Mwakondoo aliyechinjwa, na yuko hai tena!” Familia ya Adamu wanadaka wimbo na kutupa taji zao kwenye nyayo za Mwokozi na wanainama mbele yake kwa heshima na kicho.

Muungano huu wa watu waliokuwa pamoja wakati fulani unashuhudiwa na malaika waliolia machozi wakati wa anguko la Adamu na kufurahia wakati Yesu, baada ya ufufuko, alipopaa mbinguni, baada ya kufungua kaburi kwa ajili ya wote ambao wangeliliamini jina Lake. Sasa wanatazama kazi ya ukombozi ikiwa imekamilika, na wanaunganisha sauti zao kuimba wimbo wa sifa.

Panapo bahari ya fuwele mbele ya kiti cha enzi, bahari ile ya kioo iliyonekana kana kwamba ilikuwa imechanganywa na moto,—kwa kung'arishwa na utukufu wa Mungu,— umesimama mkutano wa wale walioshinda “watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake.” Pamoja na Mwanakondoo juu ya Mlima Sayuni, “wenye vinubi vya Mungu,” wanasimama, watu mia moja arobaini na nne elfu waliokombolewa kutoka miongoni mwa watu; na inasikika sauti kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi kuu, “sauti ya wapiga vinubi, wakivipiga vinubi vyao.”

Na wanaimba “wimbo mpya” mbele ya kiti cha enzi, wimbo ambao hakuna anayeweza kuujifunza isipokuwa wale mia arobaini na nne elfu. Ni wimbo wa Musa na Mwanakondoo— wimbo wa ukombozi. Hakuna mtu hata mmoja anayeweza kujifunza wimbo ule isipokuwa wale mia arobaini na nne peke yao; kwa kuwa ni wimbo wa uzoefu wao— uzoefu ambao hakuna kundi jingine lolote liliwahi kuwa nao. “Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako.” Hawa, wakiwa wamehamishwa kutoka duniani, kutoka miongoni mwa walio hai, wanachukuliwa kuwa “malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo” (Ufunuo 15:2, 3; 14:1 5) .

"Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu;" wamepita katika wakati wa taabu ambayo haijawahi kuwepo tangu kuwepo kwa taifa lo lote; wamevumilia maumivu ya wakati wa taabu ya Yakobo; wamesimama bila mwombezi wakati wote mpaka umwagaji wa mwisho wa hukumu za Mungu. Lakini wamekombolewa, kwa kuwa "wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo." "Katika vinywa vyao haukuonekana uongo. Maana hawana mawaa" mbele za Mungu. "Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao." Wameiona dunia ikiharibiwa kwa njaa na magonjwa, jua likipewa nguvu ya kuwaunguza watu kwa joto kubwa, na wao wenyewe wamekabiliana na mateso, njaa, na kiu. Lakini "hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao" (Ufunuo 7:14-17).

Katika zama zote wateule wa Mwokozi wamelelewa katika shule ya majaribu. Wametembea katika njia nyembamba duniani; wamesafishwa katika tanuru la mateso. Kwa ajili ya Kristo wamevumilia upinzani, chuki, na kusingiziwa. Walimfuata katikati ya mapambano makali; walivumilia kujikana nafsi na walipata uchungu wa kukatishwa tamaa. Kwa njia ya uzoefu wa maumivu waligundua ubaya wa dhambi, nguvu yake, na madhara yake; na wanaichukia. Utambuzi wa kafara kubwa iliyotolewa ili kuitibu unawanyenyekesha machoni pao wao wenyewe na unajaza mioyo yao kwa shukrani na sifa ambazo wale ambao hawakuanguka hawawezi kuelewa. Wanapenda zaidi kwa kuwa wamesamehewa mno. Wakiwa washiriki wa mateso ya Kristo, wanafaa kuwa washirika wa utukufu Wake.

Warithi wa Mungu wametoka katika upenu, kutoka katika vibanda vibovu, kutoka katika magereza ya chini ya ardhi, kutoka katika majukwaa ya kunyongea watu, kutoka milimani, kutoka majangwani, kutoka katika mapango ya ardhini, kutoka katika mapango ya baharini. Duniani walikuwa "maskini, watu wa kuteseka, watu wa kuudhiwa." Mamilioni walikwenda makaburini wakiwa hawana sifa njema kwa sababu walikataa daima kukubali madai ya uongo ya Shetani. Kwa njia ya mahakama za kibinadamu walihukumiwa kama wahalifu wakubwa zaidi kuliko wahalifu wengine wote. Lakini sasa "Mungu ndiye aliye hakimu" (Zaburi 50:6). Sasa maamuzi ya dunia yanageuzwa. "Aibu ya watu wake ataiondoa katika ulimwengu wote" (Isaya 25:8). "Nao watawaita, Watu watakatifu, Waliokombolewa na Bwana." Mungu amepanga "wapewe taji ya maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito" (Isaya 62:12; 61:3). Wao sio watu dhaifu tena, wanaoteswa, waliosambaa, na wanaoudhiwa. Tangu hapo wanakuwa na Bwana milele zote. Wanasimama mbele ya kiti cha enzi wakiwa katika majoho mazuri zaidi kuliko majoho yote yaliyowahi kuvaliwa na waheshimiwa na wakuu wa duniani.

Wamevalishwa vilemba vyenye utukufu mwingi zaidi kuliko vilemba vyote vilivyowahi kuvaliwa na wafalme wa kidunia. Siku za maumivu na kutoa machozi zimekoma milele.

Mfalme wa utukufu amefuta kutoka katika nyuso zao kila kitu kinacholeta huzuni. Katikati ya matawi ya mitende inayopepea wanaimba wimbo wa sifa, unaosikika vizuri, mtamu, na wenye upatanifu; kila sauti inajiunga katika uimbaji mpaka wimbo unapanda na kujaa katika makuba ya mbinguni: "Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo." Na wakazi wote wa mbinguni wanaitikia kwa kuimba kibwagizo cha kukiri: "Amina; Baraka na utukufu na hekima na shukrani na heshima na uweza na nguvu zina Mungu wetu hata milele na milele" (Ufunuo 7:10, 12).

Katika maisha haya tunaweza tu kuanza kuelewa mada ya ajabu ya ukombozi. Kwa uelewe wetu wenye kikomo tunaweza kufikiria kwa bidii sana juu ya aibu na utukufu, uzima na mauti, haki na rehema, ambavyo hukutana msalabani; pamoja na hayo, hata kwa kupanua sana uwezo wetu wa kiakili bado tunashindwa kuelewa uzito wake kikamilifu. Urefu na mapana, kina na kimo, cha upendo unakomboa vinaeleweka kidogo sana. Mpango wa ukombozi hautaeleweka kikamilifu, hata wakati waliokombolewa watakapoona kama wanavyoonwa na kujua kama wanavyojulikana; bali katika zama zote ukweli mpya utafunuliwa daima kwa akili zinazoshangaa na kufurahia. Ingawa huzuni na maumivu na majaribu ya duniani yamekoma na chimbuko lake kuondolewa, watu wa Mungu watadumu kuwa na uelewa wa wazi, akilini mwao wa gharama ya wokovu wao.

Msalaba wa Kristo utakuwa sayansi na wimbo wa waliokombolewa milele zote. Ndani ya Kristo aliyetukuzwa watamwona Kristo aliyesulibiwa. Kamwe haitasahaulika kuwa Yeye ambaye uwezo Wake uliumba na kushikilia sayari zisizo na idadi katika anga lisilokuwa na kikomo, Mpendwa wa Mungu, Mfalme wa mbinguni, Yeye ambaye makerubi na maserafi wanaong'aa wanafurahia kumwabudu—alijinyenyekesha Mwenyewe ili amwinue mwanadamu aliyeanguka; kuwa alibeba hatia na aibu ya dhamgi, na akificha uso wa Baba Yake, mpaka misiba ya ulimwengu uliopotea ilipopasua moyo Wake na kuondoa uhai Wake juu ya msalaba wa Kalwari. Kwamba Mwumbaji wa sayari zote, Mwamuzi wa miisho ya watu wote, aliweka kando utukufu Wake na kujinyenyekesha kwa sababu ya upendo Wake kwa mwanadamu— daima yote haya yataamsha mshangao na kuhamasisha ibada katika sayari zote. Wakati mataifa ya waliookolewa yatakapomtazama Mkombozi wao na kuona utukufu wa milele wa Baba uking'aa katika uso Wake; wanapoangalia kiti Chake cha enzi, ambacho ni cha milele na milele, na kujua kuwa ufalme Wake hautakuwa na mwisho, wanaimba wimbo wa furaha: "Anastahili, anastahili Mwanakondoo aliyechinjwa, na ametukomboa na kutuleta kwa Mungu kwa njia ya damu Yake Mwenyewe yenye thamani kubwa!"

Siri ya msalaba inaeleza mambo mengine yote yasiyoeleweka. Katika nuru inayotiririka kutoka Kalwari sifa za Mungu ambazo zilitujaza hofu na kicho zinaonekana kuvutia na kuwa nzuri. Rehema, upole, na upendo wa mzazi vinaonekana kuungana na utakatifu, haki na nguvu. Wakati tunaona utukufu wa kiti Chake cha enzi, kilichoinuliwa juu, tunaona tabia

Yake katika udhihirisho wa neema, na kuelewa, kuliko kabla ya hapo, umuhimu wa cheo kile kinachoashiria upendo, "Baba yetu."

Itakuja kuonekana kuwa Yeye aliye na hekima isiyokuwa na kikomo hakuweza kubuni mpango mwingine kwa ajili ya wokovu wetu isipokuwa kwa njia ya kafara ya Mwana Wake. Malipo kwa ajili ya kafara hii ni furaha ya kuijaza dunia kwa watu waliokombolewa, watakatifu, wenye furaha, na wasiokufa. Matokeo ya pambano kati ya Mwokozi na nguvu za giza na furaha ya waliokombolewa, vitamletea Mungu utukufu milele zote. Na hii ndiyo thamani ya roho kwamba Baba anaridhishwa na gharama iliyolipwa; na Kristo Mwenyewe, akitazama matunda ya kafara Yake kubwa, anaridhika.

Sura ya 41 - Ukiwa wa Dunia

"Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake. Mlipeni kama yeye alivyolipa, mkamlipe mara mbili kwa kadiri ya matendo yake. Katika kikombe kile alichokichanganyisha, mchanganyishieni maradufu. Kwa kadiri alivyojitukuza na kufanya anasa, mpeni maumivu na huzuni kadiri iyo hiyo. Kwa kuwa husema moyoni mwake, Nimeketi malkia, wala si mjane, wala sitaona huzuni kamwe. Kwa sababu hiyo mapigo yake yatakuja katika siku moja, mauti, na huzuni, na njaa, naye atateketezwa kabisa kwa moto. Kwa maana Bwana Mungu aliyemhukumu ni mwenye nguvu. Na hao wafalme wa nchi, waliozini naye na kufanya anasa pamoja naye, watalia na kumwombolezea; ...wakisema, Ole, ole, mji ule ulio mkuu, Babeli, mji ule ulio na nguvu! Kwa kuwa katika saa moja hukumu yako imekuja" (Ufunuo 18:5-10).

"Na wafanya biashara ya vitu hivyo, waliopata mali kwake, watasimama mbali, kwa hofu ya maumivu yake; wakilia na kuomboleza, wakisema, Ole, ole, mji ule mkuu! Uliovikwa kitani nzuri, na nguo ya rangi ya zambarau, na nguo nyekundu, na kupambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu! kwa kuwa katika saa moja utajiri mwingi namna hii umekuwa ukiwa" (Ufunuo 18:11, 3, 15-17).

Hizo ndizo hukumu ambazo zinaanguka juu ya Babeli katika siku ya ujio wa hasira ya Mungu. Babeli umejaza kipimo cha uovu wake; wakati wake umefika; umekomaa kwa ajili ya kuangamizwa.

Wakati sauti ya Mungu inapogeuza kifungo cha watu Wake, kuna mwamko wa kutisha wa wale ambao wamepoteza vyote katika pambano kuu la maisha. Wakati pambano lilipokuwa likiendelea walipofushwa na madanganyifu ya Shetani, na walihalalisha njia yao ya dhambi. Matajiri walijivunia ukuu wao kwa kujilinganisha na wale waliokuwa na kipato cha chini kuliko wao; lakini walipata utajiri wao kwa kuvunja sheria ya Mungu. Walipuuza kuwalisha wenye njaa, kuwavika walio uchi, kutenda kwa haki, na kupenda rehema. Walitafuta kujiinua na kuabudiwa na viumbe wenzao.

Sasa wamenyang'anywa vyote vilivyowafanya kujiona wakubwa na wameachwa bila kitu na bila ulinzi. Wanaangalia kwa hofu uangamizaji wa sanamu walizozipatia umuhimu zaidi kuliko Muumbaji wao. Waliuza roho zao kwa ajili ya utajiri na furaha za kidunia, na hawakutafuta kuwa matajiri mbele za Mungu. Matokeo yake, maisha yao yameishia kushindwa kabisa; raha zao zimegeuzwa kuwa uchungu, hazina zao zimegeuka kuwa uozo. Mapato ya maisha yao yote yanafutiliwa mbali kwa muda mfupi, kufumba na kufumbua. Matajiri wanaombolezea uharibiwaji wa majumba yao makubwa, kutawanywa kwa dhahabu na fedha zao. Lakini maombolezo yao yananyamazishwa na hofu kuwa wao wenyewe wanakwenda kuangamizwa pamoja na sanamu zao.

Waovu wanajazwa na masikitiko, siyo kwa sababu ya dhambi yao kumpuuza Mungu na wanadamu wenzao, bali kwa sababu Mungu ameshinda. Wanaomboleza kwa sababu ya jinsi matokeo yalivyo; lakini hawatubii uovu wao. Wasingeweza kuacha kujaribu kutumia njia yo yote ili waweze kushinda ikiwezekana.

Ulimwengu unawaona wale ambao waliwadhihaki na kuwakejeli, na kutamani kuwaangamiza, wakipita bila kudhurika katikati ya magonjwa, tufani, na tetemeko. Yeye ambaye kwa wavunjaji wa sheria Yake ni moto ulao, kwa watu Wake ni hema salama.

Mchungaji ambaye alitoa kafara ya ukweli kupata ukubali wa watu sasa anagundua asili na mvuto wa mafundisho yake. Inaonekana wazi kuwa jicho linalojua mambo yote lilikuwa likimfuatilia aliposimama kibwetani, alipotembea mitaani, alipojichanganya na watu katika mazingira mbali mbali ya maisha. Kila mhemko wa roho, kila mstari ulioandikwa, kila neno lililotamkwa, kila tendo lililowafanya kutulia katika maficho ya uongo, alikuwa akitawanya mbegu; na sasa katika roho maskini, zilizopotea zinazomzunguka, anaona mavuno.

Bwana anasema: "Kwa maana wameiponya jeraha ya binti ya watu wangu kwa juu-juu tu, wakisema, Amani, Amani, wala hapana amani." "Kwa kuwa ninyi mmemhuzunisha moyo mwenye haki kwa uongo, ambaye mimi sikumhuzunisha; na kuitia nguvu mikono ya mtu mbaya, hata asigeuke, na kuiacha njia yake mbaya, na kuhifadhika" (Yeremia 8:11; Ezekieli 13:22).

"Ole wao wachungaji, wanaoharibu kondoo za malisho yangu na kuwatawanya! ... Angalieni, nitawapatiliza uovu wa matendo." "Pigeni yowe, enyi wachungaji, na kulia; na kugaagaa katika majivu, enyi mlio hodari katika kundi; maana siku za kuuawa kwenu zimetimia kabisa; ... Nao wachungaji watakuwa hawana njia ya kukimbia, wala walio hodari katika kundi hawataokoka" (Yeremia 23:1, 2; 25:34, 35).

Wachungaji na watu wanaona kuwa hawakudumisha uhusiano mzuri na Mungu. Wanaona kuwa wamemwasi Mwasisi wa sheria yote ya haki na takatifu. Kuziacha kanuni takatifu za Mungu kulifungulia chemchemi maelfu za uovu, mashindano, chuki, ubaya, mpaka dunia ikawa uwanja mkubwa wa mapambano, eneo la ufisadi. Huu ndio uhalisia ambao sasa unaonekana kwa wale wanaokataa ukweli na kuchagua kukumbatia uongo. Hakuna lugha inaweza kuelezea shauku ambayo wasiokuwa watiifu na wasiokuwa wanyenyekevu wanayo kwa ajili ya kile ambacho wamekipoteza milele—uzima wa milele. Watu ambao ulimwengu uliwaabudu kwa sababu ya talanta zao na ufasaha wao sasa wanaona mambo haya katika nuru yake ya kweli. Wanagundua kile ambacho wamejinyima kwa uasi wao, na wanaanguka chini kwenye nyayo za wale ambao uaminifu wao waliudhihaki na kuukejeli, na wanakiri kuwa Mungu alikuwa anawapenda.

Watu wanaona kuwa walidanganywa. Wanalaumiana kwa kupelekana katika maangamizi; lakini wote wanaungana pamoja katika kurundika lawama zao chungu juu ya wachungaji. Wachungaji wasiokuwa waaminifu waliwatabiria mambo laini; waliwaongoza wasikilizaji wao kuibatilisha sheria ya Mungu na kuwatesa walioitakasa. Sasa, katika kukata tamaa kwao, walimu hawa wanakiri mbele ya ulimwengu kuwa kazi yao ilikuwa ya uongo. Umati wa watu unajazwa hasira kali. "Tumepotea!" wanapiga kelele, "na ninyi ndio sababu ya kuangamia kwetu;" na wanawashambulia wachungaji wa uongo. Watu wale wale ambao huko nyuma waliwastahi sana watatamka maneno ya kutisha ya laana juu yao. Mikono ile ile ambayo huko nyuma iliwavalisha taji za heshima itainuliwa juu kwa ajili ya kuwaangamiza. Panga ambazo zilikuwa zimenolewa kuwaua watu wa Mungu sasa zinatumika kuwaua adui zao. Kila mahali kuna migogoro na umwagaji damu.

"Mshindo utafika hata mwisho wa dunia; Maana Bwana ana mashindano na mataifa, Atateta na watu wote wenye mwili; Na waovu atawatoa wauawe kwa upanga" (Yeremia 25:31). Kwa miaka elfu sita, pambano kuu limekuwa likiendelea; Mwana wa Mungu na wajumbe Wake wa mbinguni wamekuwa wakipambana na nguvu ya mwovu, kuonya, kuangazia, na kuwaokoa wanadamu. Sasa wote wamefanya maamuzi yao; waovu wameungana kikamilifu na Shetani katika vita yake dhidi ya Mungu. Wakati umefika wa Mungu kuthibitisha mamlaka ya sheria Yake iliyokanyagwa. Sasa pambano siyo la Shetani peke yake, bali ni la Shetani pamoja na watu. "Bwana ana mashindano na mataifa;" "Na waovu atawatoa wauawe kwa upanga."

Alama ya ukombozi imewekwa kwa wale "wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yote yanayofanyika kati yake." Sasa malaika wa kifo anatoka, akiwakilishwa katika njozi ya Ezekieli na watu walio na silaha za kuulia, ambao wanapewa amri: "Waueni kabisa, mzee, na kijana, na msichana, na watoto wachanga, na wanawake; lakini msimkaribie mtu ye yote mwenye hiyo alama; tena anzeni katika patakatifu pangu." Nabii anasema: "Wakaanza kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba" (Ezekieli 9:1-6). Kazi ya uangamizaji inaanzia kwa wale waliokuwa walinzi wa kiroho wa watu. Walinzi waongo wanakuwa wa kwanza kuanguka. Hakuna wa kuhurumiwa au kubakiza. Wanaume, wanawake, wasichana, na watoto wachanga wanaangamia pamoja.

"Bwana anakuja kutoka mahali pake, ili kuwaadhibu wakaao duniani, kwa sababu ya uovu wao; ardhi nayo itafunua damu yake, wala haitawafunika tena watu wake waliouawa" (Isaya 26:21). "Na hii ndiyo tauni, ambayo Bwana atawapiga watu wote waliofanya vita juu ya Yerusalemu; nyama ya mwili wao itaharibika, wasimamapo juu ya miguu yao, na macho yao yataharibika ndani ya vichwa vyao, na ndimi zao zitaharibika vinywani mwao. Tena itakuwa siku hiyo, ya kwamba mashaka makubwa yatokayo kwa Bwana yatakuwa kati yao; na kila mmoja wao atakamata mkono wa jirani yake, na mkono wake utainuliwa ili kushindana na mkono wa jirani yake" (Zekaria 14:12, 13). Katika migogoro yenye hasira ya mihemko yao mikali, na umwagaji mkubwa wa hasira ya Mungu isiyochanganywa na rehema,

wanaanguka wakazi waovu wa dunia—makuhani, watawala, na watu wengine, matajiri na maskini, walio juu na walio chini. "Na waliouawa na Bwana siku ile watakuwapo, toka upande mmoja wa dunia hata upande wa pili; hawataliliwa, wala kukusanywa, wala kuzikwa; watakuwa samadi juu ya uso wa nchi." (Yeremia 25:33).

Wakati wa kuja kwa Kristo waovu wanafutiliwa mbali kutoka katika uso wa dunia nzima—wakiteketezwa kwa roho ya kinywa Chake na kuangamizwa kwa ukali wa nuru ya utukufu Wake. Kristo anawachukua watu Wake hadi katika Jiji la Mungu, na dunia inabaki tupu bila wakazi. "Tazama, Bwana ameifanya dunia kuwa tupu, aifanya ukiwa, aipindua, na kuwatawanya wakaao ndani yake." "Dunia hii itafanywa tupu kabisa, na kuharibiwa kabisa; maana Bwana amenena neno hilo" "Kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele. Ndiyo sababu laana imeila dunia hii, na hao wanaoikaa wameonekana kuwa na hatia, ndiyo sababu watu wanaoikaa dunia wameteketea" (Isaya 24:1, 3, 5, 6).

Dunia yote itaonekana kama jangwa tupu. Mabaki ya miji na vijiji vilivyoharibiwa na tetemeko, miti iliyong'olewa, mawe makubwa yanayokwaruza yaliyotupwa kutoka baharini au yaliyokatwa na kurushwa kutoka ardhini, vitakuwa vimesambaa juu ya uso wote wa dunia, wakati mashimo makubwa yatakuwa alama ya mahali ambapo milima iling'olewa kutoka katika misingi yake. Na Haruni ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai, na kuungama juu yake, kisha atampeleka aende jangwani kwa mkono wa mtu aliye tayari.

Sasa tukio linatokea lililoashiriwa katika huduma nzito ya Siku ya Upatanisho. Wakati huduma katika patakatifu pa patakatifu ilipokuwa imekamilika, na dhambi za Israeli kuondolewa kutoka katika hema kwa njia ya damu ya sadaka ya dhambi, ndipo mbuzi wa Azazeli aliwasilishwa akiwa hai mbele za Bwana; na mbele ya mkutano kuhani mkuu aliungama "uovu wote wa wana wa Israeli, na makosa yao, naam, dhambi zao zote; naye akaziweka juu ya kichwa chake yule mbuzi" (Walawi 16:21). Hali kadhalika, wakati kazi ya upatanisho itakapokamilika katika hekalu la mbinguni, ndipo mbele za Mungu na malaika wa mbinguni na majeshi ya waliokomboleewa dhambi za watu wa Mungu zitawekwa juu ya Shetani; atatangazwa kuwa na hatia ya uovu aliosababisha waufanye. Na kama mbuzi wa Azazeli alivyopelekwa katika nchi isiyokaliwa na watu, kadhalika Shetani atalazimishwa kukaa katika dunia iliyo tupu, jangwa lisilokaliwa na watu na linalochosha.

Nabii wa Ufunuo anatabiri kifungo cha Shetani na hali ya machafuko na ukiwa utakaoipata dunia, na anaeleza hali hii itadumu kuwepo kwa miaka elfu moja. Baada ya kuwasilisha mandhari za ujio wa pili wa Bwana na uangamizwaji wa waovu, unabii unaendelea kueleza: "Nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu, na mnyororo mkubwa mkononi mwake. Akamshika yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga miaka elfu; akamtupa katika kuzimu,

akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache" (Ufunuo 20:1-3).

Kwamba neno "kuzimu" huwakilisha dunia katika hali ya vitu vyake vilivyosambaratika huko na huko na ikiwa imefunikwa na giza huthibitishwa na maandiko mengine. Kuhusiana na hali ya dunia "hapo mwanzo," kumbukumbu za Biblia zinasema kuwa ilikuwa "ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji." [Neno la Kiebrania lililotafsiriwa hapa "vilindi" limetafsiriwa katika Biblia ya Kigiriki cha Septuaginta cha Agano la Kale kwa neno lile lile lililotafsiriwa "kuzimu" katika Ufunuo 20:13.] (Mwanzo 1:2). Unabii hufundisha kuwa dunia itarudishwa, angalau kwa sehemu, katika hali hii. Akiangalia mbele na kuiona siku kuu ya Mungu, nabii Yeremia alisema: "Naliiangalia nchi, na tazama, ilikuwa ukiwa, haina watu; naliziangalia mbingu, nazo zilikuwa hazina nuru. Naliiangalia milima, na tazama, ilitetemeka, na milima yote ilisogea huko na huko. Nikaangalia, na tazama, hapakuwa na mtu hata mmoja, na ndege wote wa angani wamekwenda zao. Nikaangalia, na tazama, shamba lililozaa sana limekuwa ukiwa, na miji yake yote ilikuwa imebomoka" (Yeremia 4:23-26).

Hapa patakuwa nyumbani kwa Shetani na malaika zake waovu kwa miaka elfu moja. Akiwa kizuizini duniani, hatakuwa na uwezo wa kwenda katika sayari zingine kuwajaribu na kuwaudhi wale ambao hawajawahi kuanguka. Ni katika maana hii anakuwa kifungoni: hakuna mtu ye yote aliyebaki, ambaye Shetani anaweza kutumia uwezo wake juu yake. Ameachanishwa kabisa na kazi ya udanganyifu na uharibifu ambao kwa karne nyingi ilikuwa chanzo pekee cha furaha yake.

Nabii Isaya, akitazama mbele hadi wakati wa kushindwa kwa Shetani, anasema: "Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! ... Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; ... Nitafanana na yeye Aliye juu. Lakini utashushwa mpaka kuzimu; Mpaka pande za mwisho za shimo. Wao wakuonao watakukazia macho, Watakuangalia sana, wakisema, Je! Huyu ndiye aliyeitetemesha dunia, Huyu ndiye aliyetikisa falme; Aliyeufanya ulimwengu ukiwa, akaipindua miji yake; Asiyewafungua wafungwa wake waende kwao?" (Isaya 14:12-17).

Kwa miaka elfu sita, kazi ya Shetani ya uasi imeitetemesha dunia. Ameufanya ulimwengu wote ukiwa, na ameipindua "miji yake yote." Na "hakuwafungulia wafungwa wake waende kwao." Kwa miaka elfu sita nyumba yake ya gereza imepokea watu wa Mungu, na angeendelea kuwaweka kifungoni milele; lakini Kristo alizikata kamba zake na kuwaweka huru.

Hata waovu sasa wamewekwa nje ya uwezo wa Shetani, na yeye peke yake na malaika zake wanabaki wakiangalia madhara ya laana iliyoletwa na dhambi. "Wafalme wote wa mataifa wamezikwa wote kwa heshima, Kila mmoja ndani ya nyumba [kaburi] yake

mwenyewe. Bali wewe umetupwa mbali na kaburi lako, Kama chipukizi lililochukiza kabisa. Hutaungamanishwa pamoja nao katika mazishi, Kwa maana umeiharibu nchi yako, Umewaua watu wako" (Isaya 14:18-20).

Kwa miaka elfu moja, Shetani atakuwa akizunguka huku na huko katika dunia iliyo na ukiwa akiangalia matokeo ya uasi wake dhidi ya sheria ya Mungu. Katika kipindi hiki mateso yake ni makubwa mno. Tangu kuanguka kwake maisha yake ya shughuli zisizokoma yaliondoa muda wa kutafakari; lakini sasa amenyang'anywa uwezo na ameachwa kutafakari sehemu aliyoifanya tangu alipoasi kwa mara ya kwanza dhidi ya serikali ya mbinguni, na kutazama mbele kwa kutetemeka na hofu hadi wakati ujao unaotisha wakati ambao atalazimika kuteseka kwa ajili ya uovu alioutenda na adhabu atakayoipata kwa ajili ya dhambi alizosababisha watu wa Mungu kuzitenda.

Kwa watu wa Mungu, kifungo cha Shetani kitaleta shangwe na furaha. Nabii alisema: "Itakuwa katika siku ile, ambayo Bwana atakupa raha baada ya huzuni yako, na baada ya taabu yako, na baada ya utumishi ule mgumu uliotumikishwa; utatunga mithali hii juu ya mfalme wa Babeli [hapa akimwakilisha Shetani], na kusema, Jinsi alivyokoma mwenye kuonea; Jinsi ulivyokoma mji ule wenye jeuri! Bwana amelivunja gongo la wabaya, Fimbo ya enzi yao wenye kutawala. Yeye aliyewapiga mataifa kwa ghadhabu, Kwa mapigo yasiyokoma; Aliyewatawala mataifa kwa hasira, Ameadhibiwa asizuie mtu" (Aya 3-6).

Katika kipindi cha miaka elfu moja, katikati ya ufufuo wa kwanza na wa pili hukumu ya waovu itafanyika. Mtume Paulo anaongelea hukumu hii kama tukio litakalofuata baada ya ujio wa pili. "Msihukumu neno kabla ya wakati wake, hata ajapo Bwana; ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo" (1 Wakorintho 4:5). Danieli anaeleza kuwa wakati Mzee wa Siku alipokuja, "watakatifu wake Aliye juu wakapewa hukumu" (Danieli 7:22). Wakati huu wenye haki wanatawala kama wafalme na makuhani kwa Mungu. Yohana katika Ufunuo anasema: "Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu." "Watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu" (Ufunuo 20:4, 6). Ni wakati huu ambapo, kama ilivyotabiriwa na Paulo, "watakatifu watauhukumu ulimwengu" (1 Warintho 6:2). Wakiungana na Kristo wanawahukumu waovu, wakilinganisha matendo yao na kitabu cha sheria, Biblia, na kuamua kila kesi kulingana na matendo yaliyotendwa katika mwili. Na kipimo cha adhabu watakayopata waovu kinapangwa, kulingana na matendo yao; na kinaandikwa dhidi ya majina yao katika kitabu cha mauti.

Shetani na malaika waovu pia wanahukumiwa na Kristo na watu Wake. Paulo anasema: "Hamjui ya kuwa mtawahukumu malaika?" (Aya 3). Na Yuda anatangaza kuwa "malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu" (Yuda 6).

Mwishoni mwa miaka elfu moja ufufuo wa pili utatokea. Ndipo waovu watafufuliwa kutoka katika wafu na kutokea mbele ya Mungu kwa jili ya utekelezaji wa "hukumu iliyoandikwa." Nabii wa Ufunuo, baada ya kuelezea ufufuo wa wenye haki, anasema: "Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu" (Ufunuo 20:5). Na Isaya anatangaza, kuhusiana na waovu: "Nao watakusanywa pamoja kama vile wakusanywavyo wafungwa katika shimo nao watafungwa katika gereza; na baada ya muda wa siku nyingi watajiliwa" (Isaya 24:22).

Sura ya 42 - Mwisho wa Pambano

Mwishoni mwa miaka elfu moja, Kristo anarudi tena duniani. Anaandamana na jeshi la waliokombolewa na kusindikizwa na msafara wa malaika. Anaposhuka katika utukufu wa kutisha anawaamuru waovu waliokufa waamke ili wapokee adhabu yao. Wanaamka, jeshi kubwa, wasioweza kuhesabika kama mchanga wa bahari. Tofauti iliyoje ukiwalinganisha na wale waliofufuliwa katika ufufuo wa kwanza! Wenye haki walikuwa wamevikwa ujana wenye uzuri na hali ya kutokufa. Waovu wana viashiria vya magonjwa na hali ya kufa.

Kila mmoja katika umati mkubwa wa watu unageuka kuangalia utukufu wa Mwana wa Mungu. Kwa sauti moja waovu wanatamka kwa mshangao: "Amebarikiwa Yeye ajaye katika jina la Bwana!" Siyo upendo kwa ajili ya Yesu unaohamasisha tamko hili. Nguvu ya ukweli ilazimishayo maneno hayo kutoka katika midomo isiyopenda. Wakati waovu walipokwenda katika makaburi yao, wanatoka wakiwa vile vile wakiwa na uadui ule ule dhidi ya Kristo na roho ile ile ya uasi. Hawapewi rehema mpya ili warekebishe kasoro za maisha yao yaliyopita. Hakuna lo lote la maana lingeweza kupatikana kwa njia hii. Maisha yao ya uasi hayakulainisha mioyo yao. Muda wa pili wa rehema, hata kama wangepewa, ungetumiwa kama ulivyotumika ule wa kwanza kwa kukwepa matakwa ya Mungu na kuchochea uasi dhidi Yake.

Kristo anashuka juu ya mlima wa Mizeituni, mahali ambapo, baada ya kufufuka Kwake, kutokea hapo alipaa, na mahali ambapo malaika walirudia kutangaza ahadi ya kurudi Kwake. Nabii anasema: "Bwana, Mungu wangu, atakuja, na watakatifu wote pamoja naye." "Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki, nao mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake, ... na litakuwako huko bonde kubwa sana." "Naye Bwana atakuwa Mfalme juu ya nchi yote; siku hiyo Bwana atakuwa mmoja, na jina lake moja" (Zekaria 14:5, 4, 9). Wakati Yerusalemu Mpya, katika utukufu wake mwingi, unaposhuka chini kutoka mbinguni, unatua mahali ambapo pamesafishwa na kuandaliwa kuupokea, na Kristo, pamoja na watu Wake na malaika, wanauingia Mji Mtakatifu.

Sasa Shetani anajiandaa kwa ajili ya pambano lake la mwisho kwa ajili ya ukuu. Wakati ameshanyang'anywa nguvu zake na kuachishwa kazi yake ya udanganyifu, mfalme wa uovu akiwa na hali mbaya na akiwa amechoka sana; lakini waovu wanapofufuliwa na yeye akiuona mkutano mkubwa ukiwa upande wake, matumaini yake yanafufuka, na anaazimia kutokuacha pambano kuu. Atawakusanya majeshi ya waliopotea chini ya bendera yake kwa kupitia kwao atajaribu kutekeleza mipango yake. Waovu ni mateka wa Shetani. Katika kumkataa Kristo wameukubali utawala wa kiongozi aliyeasi. Wako tayari kupokea mapendekezo yake na kutii amri zake. Hata hivyo, akishikilia msimamo wake wa tangu awali, hataki kukiri kuwa yeye ni Shetani. Anadai kuwa yeye ni mfalme ambaye ni mmiliki halali wa ulimwengu na ambaye urithi wake umeporwa kutoka kwake kinyume na sheria. Anajinasibu mwenyewe kwa watu

wake waliodanganyika kuwa yeye ni mkombozi, akiwahakikishia kuwa uwezo wake umewatoa katika makaburi yao na kuwa anakwenda kuwaokoa kutoka katika utawala wa kikatili. Uwepo wa Kristo ukiwa umeondolewa, Shetani anatenda maajabu kuunga mkono madai yake. Anawafanya walio dhaifu kuwa na nguvu na anavuvia wote kwa roho yake na nguvu yake. Anapendekeza kuwaongoza dhidi ya kambi ya watakatifu na kuuteka Mji wa Mungu. Kwa furaha ya kishetani anaonesha mamilioni yasiyo na idadi ya watu ambao wamefufuliwa kutoka makaburini na anatangaza kuwa kama kiongozi wao anaweza kabisa kuushinda mji na kurudisha kiti chake cha enzi na ufalme wake.

Katika mkutano ule mkubwa wapo watu wengi wa kizazi cha watu waliokuwa na maisha marefu walioishi kabla ya Gharika; watu wenye maumbo marefu na akili nyingi, ambao, kwa kujisalimisha chini ya utawala wa malaika walioanguka, walitumia stadi zao na ujuzi wao kujiinua wenyewe; watu ambao kazi zao za ajabu za sanaa ziliufanya ulimwengu kuabudu uwezo wao wa kiakili, lakini ambao ukatili wao na ugunduzi wao wa uovu, vikiichafua dunia na kuondoa Sura ya Mungu duniani, vilimfanya Mungu kuwafutilia mbali kutoka katika uso wa uumbaji Wake. Wapo wafalme na majenerali walioshinda mataifa, watu mashujaa ambao hawakuwahi kushindwa vitani, wenye kiburi, wapiganaji wenye tamaa ya kufanya makubwa ambao ujio wao ulizifanya falme kutetemeka. Mautini hawakupoteza uzoefu wao. Wanapotoka makaburini, wanarudia mkondo wa mawazo yao pale yalipokomea. Wanachochewa na shauku ile ile ya kushinda iliyowatawala walipofariki.

Shetani anashauriana na malaika zake, na ndipo anashauriana na hawa wafalme na washindaji na watu wenye nguvu. Wanatathmini nguvu na idadi ya wapiganaji walio upande wao, na wanatangaza kuwa jeshi lililoko ndani ya mji ni dogo ukilinganisha na jeshi lao, na kuwa wanaweza kulishinda lile jeshi dogo. Wanaweka mipango yao ya kuteka mali na utajiri na utukufu wa Yerusalemu Mpya. Wote mara moja wanaanza kujiandaa kwa ajili ya vita. Mafundi wenye stadi wanaunda zana za vita. Viongozi wa kijeshi, waliotukuka kwa mafanikio yao, wanawapanga watu wa vita katika vikosi na migawanyo mbalimbali.

Hatimaye amri ya kusonga mbele inatolewa, na wapiganaji wasiokuwa na idadi wanatembea kwenda mbele—jeshi ambalo halijawahi kukusanywa na washindi wa kidunia, jeshi ambalo litaunganisha wapiganaji wa zama zote tangu vita ya kwanza kutokea duniani. Shetani, mpiganaji mwenye nguvu nyingi kuliko wapiganaji wengine wote, anaongoza msafara wa kivita, na malaika zake wanaunganisha nguvu zao pamoja kwa ajili ya pambano hili la mwisho. Wafalme na wapiganaji wamo katika msafara wake, na watu wasiokuwa na idadi wanafuata katika vikosi vikubwa, kila kikosi kikiwa chini ya kiongozi aliyeteuliwa. Kwa umahiri mkubwa wa kijeshi askari waliosongamana wanasonga mbele wakitembea juu ya ardhi iliyoharibika wakiuelekea Mji wa Mungu. Kwa amri ya Yesu, malango ya Yerusalemu Mpya yanafungwa, na majeshi ya Shetani yanauzingira mji na wanajiandaa kwa ajili ya mashambulizi.

Sasa Kristo anatokea tena na kusimama mahali ambapo anaonwa na maadui Zake. Juu sana ya mji, juu ya msingi wa dhahabu iliyosafishwa sana, kuna kiti cha enzi, kilicho juu na kilichoinuliwa sana. Juu ya kiti hiki cha enzi anakaa Mwana wa Mungu, na kando kando Yake kuna raia wa ufalme Wake. Nguvu na utukufu wa Kristo hakuna lugha inayoweza kueleza, hakuna kalamu inayoweza kuandika. Utukufu wa Baba wa Milele unamfunika Mwanaye. Utukufu wa uwepo Wake unaujaza Mji wa Mungu, na unatiririka na kutoka nje ya malango ya mji, na kufurika duniani kote kwa mwangaza wake.

Karibu kabisa na kiti cha enzi kuna wale ambao awali walikuwa na bidii sana upande wa Shetani, lakini, ambao baada ya kuopolewa kama kijinga kutoka motoni, walimfuata Mwokozi wao kwa kujitoa kikamilifu. Safu inayofuata ni yale wale waliokamilisha tabia ya Kikristo katikati ya madanganyifu na ufisadi, wale walioiheshimu sheria ya Mungu wakati ulimwengu wa Kikristo ukitangaza kuwa sheria hiyo imebatilishwa, na mamilioni ya watu, wa zama zote, waliouawa kwa ajili ya imani yao. Na baada ya hao kuna "mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, ... mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao" (Ufunuo 7:9). Vita yao imekwisha, ushindi wao umepatikana. Wameshiriki katika shindano na wamepokea tuzo. Tawi la mtende katika mikono yao ni ishara ya ushindi wao, vazi jeupe ni nembo ya haki ya Kristo isiyokuwa na doa ambayo ni yao sasa.

Waliokombolewa wanaimba wimbo wa sifa ambao mwangwi wake unaakisiwa na kuakisiwa katika makuba ya mbinguni: "Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo" (Aya 10). Na malaika na maserafi wanaunganisha sauti zao katika kusifu. Baada ya waliokombolewa kuona nguvu na ubaya wa Shetani, wamethibitisha, kwa uhakika zaidi kuliko kabla ya hapo, kuwa ni nguvu ya Kristo peke yake ingeweza kuwasaidia wapate ushindi. Miongoni mwa wale wote wanaong'aa hakuna mtu hata mmoja ambaye anaweza kujitapa kuwa alipata wokovu kwa uwezo wake mwenyewe, kuwa alishinda kwa nguvu zake na wema wake mwenyewe. Hakuna jambo lo lote linatajwa kuhusiana na kile walichokifanya au mateso waliyoyapata; lakini maudhui ya kila wimbo, wazo kuu la kila wimbo, ni: Wokovu una Mungu wetu na Mwanakondoo.

Mbele ya wakazi wa duniani na mbinguni waliokusanyika pamoja uvalishwaji taji wa Mwana wa Mungu unafanyika. Na sasa, akiwa amekabidhiwa ukuu na mamlaka ya juu kabisa, Mfalme wa wafalme anatangaza hukumu juu ya waasi dhidi ya serikali Yake na anatekeleza haki juu ya wote walioivunja sheria Yake na kuwatesa watu Wake. Nabii wa Mungu anasema: "Nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao" (Ufunuo 20:11, 12).

Mara tu vitabu vya kumbukumbu vinapofunguliwa, na jicho la Yesu kuwatazama waovu, wanatambua kila dhambi waliyowahi kuitenda katika maisha yao. Wanatambua mahali nyayo zao zilipoteleza na kuondoka katika njia ya usafi na utakatifu, kiasi ambacho kiburi na uasi vilipowafikisha katika kuvunja sheria ya Mungu. Majaribu ya udanganyifu waliyopalilia kwa kulea dhambi, mibaraka iliyotumiwa vibaya, wajumbe wa Mungu waliodharauliwa na kupuuzwa, maonyo yaliyotupiliwa mbali, mawimbi ya rehema yaliyorudishwa nyuma na moyo mgumu, usiotubu—vyote vinaonekana kama vilivyoandikwa kwa herufi za moto.

Juu ya kiti cha enzi kunafunuliwa msalaba; na kama onesho la filamu zinatokea mandhari za majaribu na anguko la Adamu, na mfululizo wa hatua katika mpango mkuu wa ukombozi. Kuzaliwa kwa Mwokozi katika mazingira ya kimaskini; maisha Yake ya awali ya usahili na utii; ubatizo Wake katika mto waYordani; mfungo na majaribu katika jangwa; huduma Yake ya hadhara, kuwafunulia wanadamu mibaraka ya mbinguni yenye thamani kubwa; siku zilizojaa matendo ya upendo na rehema, nyakati za usiku zilizotumiwa katika maombi na kukesha katika maeneo ya faragha milimani; mipango ya wivu, chuki, na ubaya iliyopangwa dhidi Yake kama malipo kwa wema Wake; uchungu wa kutisha, wa siri katika Bustani ya Gethsemane chini ya mzigo mzito wa dhambi za ulimwengu wote; kusalitiwa Kwake katika mikono ya kundi la wauaji; matukio ya kutisha ya usiku ule wa hofu—mfungwa asiye na ubishi, aliyekimbiwa na wanafunzi Wake wapendwa, akiburuzwa kikatili katika mitaa ya Yerusalemu; Mwana wa Mungu akioneshwa mbele ya Anasi kwa furaha, akishitakiwa katika nyumba ya kuhani mkuu, katika ukumbi wa hukumu wa Pilato, mbele ya Herode mwoga na katili, akidhihakiwa, akitukanwa, akiteswa, na akihukumiwa kufa—vyote vinaoneshwa wazi wazi.

Na sasa mbele ya umati mkubwa wa watu zinafunuliwa mandhari za mwisho—Mtesekaji mvumilivu akitembea katika njia inayoelekea Kalwari; Mfalme wa mbinguni akining'inia juu ya msalaba; makuhani wenye kiburi na umati wa watu wenye zogo wakikejeli uchungu Wake unaoishia; giza lisilo la kawaida; dunia iliyoumka na kusinyaa, miamba iliyopasuka, makaburi yaliyofunguka, vikiashiria wakati Mkombozi wa ulimwengu alipotoa uhai Wake.

Tukio la kutisha linatokea kama lilivyokuwa. Shetani, malaika zake, na wafuasi wake hawana uwezo wa kugeuka wasiitazame picha ya kazi yao. Kila mhusika anakumbuka sehemu aliyofanya. Herode, aliyewaua watoto wasio na hatia wa Bethlehemu ili amuue Mfalme wa Israeli; Herodia mwovu, ambaye moyoni mwake kuna hatia ya damu ya Yohana Mbatizaji; Pilato dhaifu na kigeukigeu; askari wanaodhihaki; makuhani na wakuu na umati uliofyatuka akili wakipiga kelele, "Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu!"—wote wanaona ukubwa wa hatia yao. Wanatafuta bila mafanikio kujificha wasionekane mbele ya utukufu wa Kimungu wa uso Wake, ambao unang'aa zaidi kuliko utukufu wa jua, wakati waliokombolewa wakizitupa taji zao kwenye nyayo za Mwokozi, wakisema: "Alikufa kwa ajili yangu!"

Miongoni mwa waliokombolewa wamo mitume wa Kristo, Paulo shujaa, Petro mwenye juhudi, Yohana anayependwa na mwenye upendo, na ndugu zao wa kweli, na pamoja nao jeshi kubwa la wafia dini; wakati nje ya kuta, palipo na kila kitu kichafu na kila kitu kinachochukiza, kuna wale ambao kwa mikono yao watumishi wa Mungu wa kweli waliteswa, walifungwa, na kuuawa. Yupo Nero, jitu lile katili na ovu, likiona furaha ya kuinuliwa kwa wale ambao huko nyuma aliwatesa, na ambao kwa sababu ya uchungu wao mwingi alipata furaha ya kishetani. Mama yake yupo pale akishuhudia matokeo ya kazi yake; aone jinsi mfano wake mbaya wa tabia aliorithisha kwa mwanaye, mihemko iliyochochewa na kukuzwa kwa mvuto na mfano wake, vimezaa matunda ya uhalifu ulioufanya ulimwengu kutetemeka.

Kuna mapadri na makasisi wa kipapa, waliodai kuwa mabalozi wa Kristo, lakini walitumia kitanda cha kutesea, gerezani la ardhini, na nguzo ya kuchomea watu moto kudhibiti dhamiri za watu Wake. Kuna mapapa wenye kiburi waliojiinua juu ya Mungu na kujaribu kubadili sheria ya Yeye Aliye Juu sana. Wale waliojifanya kuwa mababa wa kanisa wanatakiwa kutoa maelezo ambayo wanatamani wasamehewe. Kwa kuchelewa sana wanagundua kuwa Yeye anayejua mambo yote ana wivu juu ya sheria Yake na kuwa hawezi kumhesabia anayeivunja kuwa hana hatia. Wanagundua kuwa Kristo alijali maslahi ya watu Wake wanaoteseka; na wanahisi uzito wa maneno Yake: "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi" (Mathayo 25:40).

Ulimwengu wote mwovu unasimama ukiwa katika kizimba cha Mungu wakishtakiwa kwa kosa la uhaini mkuu dhidi ya serikali ya mbinguni. Hawana wa kuwatetea; hawana udhuru; na hukumu ya mauti ya milele inatangazwa dhidi yao.

Inakuwa dhahiri kwa wote kuwa mshahara wa dhambi siyo uhuru kamili na uzima wa milele, bali utumwa, uharibifu, na kifo. Waovu wanaona kile ambacho wamekipoteza kwa maisha yao ya uasi. Uzito wa milele wa utukufu ulio muhimu zaidi kuliko kitu kingine cho chote ulidhihakiwa ulipotolewa kwao; lakini sasa unaonekana kuhitajika sana. "Yote haya," roho iliyopotea inalia, "ningekuwa nayo; lakini nilichagua kujitenga nayo. Aa! kupumbazwa kwa ajabu! Nimepoteza amani, furaha, na heshima, na badala yake nimepata umaskini, kudharaulika, na kukata tamaa." Wote wanaona kuwa kutengwa na mbingu ni haki kabisa. Kwa maisha yao walitangaza kuwa: "Hatumtaki huyu Mtu [Yesu] atutawale."

Kama watu walio katika maono, waovu wanamwona Mwana wa Mungu akivikwa taji. Wanaona katika mikono Yake mbao za sheria ya Mungu, amri ambazo walizidhihaki na kuzivunja. Wanashuhudia mlipuko wa mshangao, furaha, na sifa kwa waliookolewa; na wakati wimbi la sauti tamu linapopaa juu ya umati watu walioko nje ya mji, wote kwa sauti moja wanashangilia, "Ni makuu, na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; Ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa mataifa" (Ufunuo 15:3); na, wakianguka kifudifudi, wanamwabudu Mfalme wa uzima.

Shetani anaonekana kana kwamba amepigwa kiharusi anapouona utukufu na ukuu wa Kristo. Yeye aliyekuwa kerubi afunikaye anakumbuka ni wapi alipoangukia. Serafi ang'aaye, "mwana wa asubuhi;" amebadilika kiasi gani, ameshuka chini kiasi gani! Kutoka katika baraza alipokuwa akiheshimiwa, ameondolewa milele zote. Anamwona mwingine akisimama karibu na Baba, akifunika utukufu Wake. Ameona taji ikiwekwa juu ya kichwa cha Kristo na malaika mmoja mrefu na mwonekano wenye utukufu mwingi, na anatambua kuwa cheo cha juu cha malaika huyu kilikuwa kiwe chake.

Kumbukumbu zinamrudisha hadi wakati alipokuwa hana hatia na wakati alipokuwa msafi, amani na kuridhika vilikuwa vyake mpaka alipojiingiza katika manung'uniko dhidi ya Mungu, na kumwonea wivu Kristo. Mashtaka yake, uasi wake, madanganyifu yake ili apate huruma na kuungwa mkono na malaika, ukaidi wake na kutofanya juhudi yo yote ya kuungama makosa yake wakati Mungu alipokuwa tayari kumsamehe— yote yanakuja mbele yake kwa uwazi. Anatathmini kazi yake kati ya watu na matokeo yake—uadui wa mwanadamu kwa mwanadamu mwenzake, maangamizi ya kutisha ya wanadamu, kuinuka na kuanguka kwa falme, kupinduliwa kwa viti vya enzi, mfululizo mrefu wa fujo, migogoro, na mapinduzi. Anakumbuka juhudi zake zisizochoka za kupinga kazi ya Kristo na kumdidimiza mwanadamu chini zaidi na zaidi. Anaona kuwa mipango yake ya kuzimu imeshindwa kuwaangamiza wale walioweka tumaini lao kwa Yesu. Shetani anapoangalia ufalme wake, matunda ya kazi zake, anaona tu kushindwa na kuangamizwa. Anawaongoza watu wengi kuamini kuwa Mji wa Mungu ni windo rahisi; lakini anajua kuwa huu ni uongo. Tena na tena, katika mwenendo wa pambano kuu, ameshindwa na kulazimishwa kujisalimisha. Anajua vizuri pia mamlaka na nguvu za Yule Aishie Milele.

Kusudi la mwasi mkuu limekuwa daima kujihesabia haki na kuonesha kuwa serikali ya Mungu ndiyo inawajibika kwa uasi. Ili kufikia azma hii ameelekeza nguvu zote za akili yake kubwa. Amefanya kazi kwa kudhamiria na kwa kupangilia, na kwa mafanikio ya kushangaza, kuwaongoza watu wengi kukubali tafsiri yake hii ya pambano kuu ambalo limedumu kuwepo kwa muda mrefu. Kwa miaka mingi, huyu mkuu wa njama ametawanya uongo badala ya ukweli. Lakini wakati umefika sasa ambapo uasi unapaswa kushindwa na historia na tabia ya Shetani ifunuliwe. Katika juhudi yake kubwa ya mwisho ya kumpindua Kristo na kumwondoa kwenye kiti Chake cha enzi, kuwaangamiza watu Wake, na kuutwaa Mji wa Mungu, mdanganyaji mkuu anajifunua kikamilifu. Wale waliounganana naye wanaona kushindwa kwa mipango yake. Wafuasi wa Kristo na malaika waaminifu wanatazama upana wa mikakati yake dhidi ya serikali ya Mungu. Anachukiwa na wenye uhai wote.

Shetani anaona kuwa uasi wake wa kujitolea umemfanya asifae kuishi mbinguni. Amezoeza nguvu zake kufanya vita dhidi ya Mungu; usafi, amani na mwafaka wa mbinguni vingekuwa mateso makubwa kwake. Mashtaka yake dhidi ya rehema na haki ya Mungu sasa yamenyamazishwa. Aibu ambayo amejitahidi kuirundika juu ya Yehova inamrudia yeye kikamilifu. Na sasa Shetani anainama chini na anakiri haki ya hukumu yake.

"Ni nani asiyekucha, Ee Bwana, na kulitukuza jina lako? Kwa kuwa wewe peke yako u Mtakatifu; kwa maana mataifa yote watakuja na kusujudu mbele zako; kwa kuwa matendo yako ya haki yamekwisha kufunuliwa" (Aya 4). Kila suala kuhusu ukweli na uongo katika pambano kuu la muda mrefu litakuwa limewekwa wazi. Matokeo ya uasi, matunda ya kuweka pembeni amri za Mungu, yatakuwa yamewekwa wazi na kuonwa na viumbe wote wenye akili. Tofauti ya utendaji kazi wa utawala wa Shetani na serikali ya Mungu umewekwa wazi kwa ulimwengu wote. Kazi za Shetani zimekwisha kumhukumu. Hekima ya Mungu, haki Yake, na wema Wake vimethibitishwa kikamilifu.

Imedhihirika kuwa utendaji kazi Wake wote katika pambano kuu umefanyika kwa kuzingatia manufaa ya milele kwa ajili ya watu Wake na kwa maslahi ya sayari zote alizoziumba. "Kazi zako zote zitakushukuru, Na wacha Mungu wako watakuhimidi" (Zaburi 145:10). Historia ya dhambi itabaki milele zote kama ushuhuda kuwa uwepo wa sheria umeshikamana na furaha ya wenye uhai wote walioumbwa na Mungu. Kwa kuzingatia ukweli wote kuhusu pambano kuu, ulimwengu, wa waaminifu na waasi, kwa sauti moja wanatangaza: "Ni za haki na kweli njia Zako, Ee Mfalme wa watakatifu."

Mbele ya ulimwengu wote imewasilishwa kwa uwazi kafara kuu iliyotolewa na Baba na Mwana kwa ajili ya mwanadamu. Saa imekuja ambapo Kristo anakalia nafasi Yake ya haki anaadhimishwa juu ya mamlaka na nguvu na kila jina linalotajwa. Ilikuwa kwa ajili ya furaha iliyoko mbele Yake—kwamba awaingize watu wengi katika utukufu—kuwa aliustahimili msalaba na kuidharau aibu. Na kwa kadiri huzuni na aibu ilivyokuwa kubwa, ndivyo furaha ilivyokuwa kubwa na utukufu ulivyokuwa mwingi zaidi. Anawaangalia waliokombolewa, wakiwa wameumbwa upya katika Sura ya ke, kila moyo ukiwa na chapa kamilifu ya Sura ya Mungu, kila uso ukiaksi mfano wa Mfalme wao. Anaona ndani yao matokeo ya kazi ya nafsi Yake, na anaridhika. Ndipo, kwa sauti inayosikika kwa wote waliokusanyika, wenye haki na waovu, anatangaza: "Tazama thamani ya damu Yangu! Kwa ajili ya hawa niliteseka, kwa ajili ya hawa nilikufa, ili waweze kuishi mbele Yangu katika zama zote milele na milele." Na wimbo wa sifa unapanda juu kutoka kwa wale waliova mavazi meupe waliokizunguka kiti cha enzi: "Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka" (Ufunuo 5:12).

Licha ya kuwa Shetani amelazimishwa kukiri haki ya Mungu na kuinama kwa ukuu wa Kristo, tabia yake inabaki bila kubadilika. Roho ya uasi, kama mkondo wa maji wenye nguvu, inainuka tena. Akiwa amejazwa na wazimu, anaazimia kutokujisalimisha katika pambano kuu. Wakati umefika kwa ajili ya pambano la mwisho la kufa na kupona dhidi ya Mfalme wa mbinguni. Anaharakisha kwenda katikati ya wafuasi wake anajaribu kuwachochea kwa hasira zake na kuwahamasisha waingie vitani mara moja. Lakini miongoni mwa mamilioni yote ambao amewadanganya kufanya uasi, hakuna hata mmoja wao anayetambua ukuu wake. Mamlaka yake imefikia mwisho. Waovu wamejazwa na chuki ileile dhidi ya Mungu iliyoko ndani ya Shetani; lakini wanaona kuwa hali yao haina tumaini, kuwa hawawezi kumshinda

Yehova. Hasira yao inawaka dhidi ya Shetani na wale ambao walikuwa mawakala wake katika udanganyifu, na kwa ghadhabu ya mashetani wanamshambulia.

Bwana anasema: "Kwa kuwa umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu; basi, tazama, nitaleta wageni juu yako, watu wa mataifa wenye kutisha; nao watafuta panga zao juu ya uzuri wa hekima yako, nao watautia uchafu mwangaza wako. Watakushusha hata shimoni." "Nami nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto.... Nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme, wapate kukutazama. Nami nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao. Umekuwa kitu cha kutisha, wala hutakuwapo tena hata milele" (Ezekieli 28:6-8, 16-19).

"Maana silaha zote za mtu mwenye silaha wakati wa mshindo, na mavazi yaliyofingirishwa katika damu, yatakuwa tayari kuteketezwa, yatakuwa kuni za kutiwa motoni" "Maana Bwana ana ghadhabu juu ya mataifa yote, na hasira kali juu ya jeshi lao lote; amewaangamiza kabisa, amewatoa waende kuchinjwa" "Awanyeshee wasio haki mitego, Moto na kiberiti na upepo wa hari, Na viwe fungu la kikombe chao" (Isaya 9:5; 34:2; Zaburi 11:6). Moto unashuka kutoka kwa Mungu mbinguni. Dunia inapasuka. Silaha zilizofichwa katika vina vyake zinatoka nje. Mioto inayoteketeza inalipuka kutoka katika uwazi wa kila shimo ardhini. Miamba yenyewe inawaka moto. Siku imekuja ambayo inaunguza kama tanuru. Vitu vya asili vinayeyuka kwa joto kali, dunia pia, na kazi zote zilizomo zinaunguzwa (Malaki 4:1; 2 Petro 3:10). Uso wa dunia unaonekana kama donge moja kubwa lililoyeyuka—ziwa kubwa la moto. Ni wakati wa hukumu na kuangamizwa kwa watu wasiomcha Mungu—"siku ya kisasi cha Bwana, mwaka wa malipo, ili kushindania Sayuni" (Isaya 34:8).

Waovu wanapokea mshahara wao duniani (Mithali 11:31). Waovu "watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi" (Malaki 4:1). Baadhi wanaangamizwa kwa muda mfupi, wakati wengine wanateseka kwa siku nyingi. Wote wanaadhibiwa "kulingana na matendo yao" Kwa dhambi za wenye haki kuhamishiwa kwa Shetani, anawajibika kuteseka siyo tu kwa ajili ya uasi wake peke yake, bali pia kwa ajili ya dhambi alizosababisha watu wa Mungu kuzitenda. Adhabu yake inapaswa kuwa kubwa zaidi kuliko adhabu ya wale aliowadanganya. Baada ya wote walioanguka kwa kudanganywa kuteketea, Shetani ataendelea kuishi na kuteseka zaidi. Katika moto unaosafisha, waovu hatimaye wanaangamizwa, shina na tawi—Shetani ndiye shina, wafuasi wake ni matawi. Adhabu kamili ya sheria imetekelezwa; madai ya haki yametimizwa; na mbingu na dunia, zikiangalia, zinatangaza haki ya Yehova.

Kazi ya Shetani ya uharibifu imefikia kikomo milele. Kwa miaka elfu sita ametekeleza mapenzi yake, akiijaza dunia kwa misiba na kuleta huzuni katika ulimwengu wote. Uumbaji wote umekuwa ukiugua na kutaabika kwa pamoja kwa sababu ya maumivu. Sasa viumbe wa Mungu wamekombolewa milele na kuwa mbali kabisa na uwepo wake na majaribu yake. "Dunia yote inastarehe na kutulia; Hata [wenye haki] huanzilisha kuimba" (Isaya 14:7). Na

kelele za sifa na ushindi zinapanda juu kutoka kwa ulimwengu wote mtiifu. “Nikasikia sauti kama sauti ya makutano mengi, na kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi yenye nguvu, ikisema, Haleluya; kwa kuwa Bwana Mungu wetu, Mwenyezi, amemiliki” (Ufunuo 19:6).

Wakati dunia itakapokuwa imefunikwa kwa moto wa maangamizi, wenye haki wanaishi katika Mji Mtakatifu. Mauti ya pili haina nguvu juu ya wale walio na sehemu katika ufufuo wa kwanza. Wakati Mungu ni moto ulao kwa waovu, Yeye ni jua na ngao kwa watu Wake (Ufunuo 20:6; Zaburi 84:11).

“Nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita” (Ufunuo 21:1). Moto utateketeza waovu na kusafisha dunia. Kila kiashiria cha laana kinafutiliwa mbali. Hakuna kuzimu inayowaka moto itakayodumu kuwepo milele mbele ya waliokombolewa kama kumbukumbu ya matokeo ya kutisha ya dhambi.

Kumbukumbu moja tu itabaki: Mkombozi wetu atadumu kuwa na alama Zake za kusulubiwa. Katika kichwa Chake kilichojeruhiwa, ubavuni Mwake, mikono na miguu Yake, ndizo alama pekee za kazi ya kikatili iliyofanywa na dhambi. Nabii anasema, akimtazama Kristo katika utukufu Wake: “Mwangaza wake ulikuwa kama nuru; Alikuwa na mishale ya nuru ubavuni pake; Ndipo ulipofichwa uweza wake” (Habakuki 3:4). Ubavu ule uliochomwa mkuki ambapo ilitoka damu iliyompatanisha mwanadamu na Mungu—pale ndipo palipo na utukufu wa Mwokozi, pale“Ndipo ulipofichwa uweza wake.” “Uweza wa kuokoa,” kwa njia ya kafara ya ukombozi, alikuwa na nguvu za kutekeleza hukumu juu ya wale waliodhihaki neema ya Mungu. Na ishara za mateso Yake ndiyo heshima Yake ya juu kuliko vitu vyote; katika zama zote, milele na milele, majeraha ya Kalwari yataonesha sifa Yake na kutangaza uweza Wake. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta, kuwa sifa ya utukufu wake.

“Ee mnara wa kundi, kilima cha binti Sayuni, utajiliwa; naam, mamlaka ya kwanza yatakuja” (Mika 4:8). Wakati umefika ambao watu watakatifu wamekuwa wakiutazamia kwa shauku kubwa tangu upanga wa moto ulipowazuia Adamu na Hawa kuingia katika Bustani ya Edeni, wakati kwa ajili ya “ukombozi wa milki yake” (Waefeso 1:14). Dunia ambayo awali ilikabidhiwa kwa mwanadamu kama ufalme wake, ikasalitiwa na mwanadamu na kuwekwa katika mikono ya Shetani, na kwa muda mrefu ikashikiliwa na adui mwenye nguvu, imerudishwa kwa njia ya mpango mkuu wa ukombozi. Kila kitu kilichokuwa kimepotea kwa ajili ya dhambi sasa kinarudishwa. “Maana Bwana, ... asema hivi; ... ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya; ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu” (Isaya 45:18). Kusudi la Mungu la awali katika uumbaji wa dunia linatimizwa wakati dunia inapofanywa kuwa makao ya milele ya waliokombolewa. “Wenye haki watairithi nchi, Nao watakaa humo milele” (Zaburi 37:29).

Hofu ya kuufanya urithi wa milele kuwa ni wa vitu zaidi imewafanya watu wengi kuona kila kitu ni cha kiroho katika kutafsiri ukweli unaoeleza mahali tutakapoishi mbinguni. Kristo aliwahakikishia wanafunzi Wake kuwa alikwenda kuandaa makao kwa ajili yao katika nyumba ya Baba. Watu wanaoyakubali mafundisho ya neno la Mungu hawatashindwa kuelewa kabisa kuhusiana na makao ya mbinguni. Na bado, "jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao" (1 Wakorintho 2:9). Lugha ya kibinadamu haitoshi kueleza zawadi ya wenye haki. Itaeleweka tu kwa wale watakaoiona. Hakuna akili yenye kikomo inaweza kuelewa utukufu wa Paradiso ya Mungu.

Katika Biblia, urithi wa waliookolewa unaitwa "nchi" (Waebrania 11:14-16). Pale Mchungaji wa mbinguni anawaongoza kondoo Wake hadi kwenye chemchemi ya maji ya uzima. Mti wa uzima unazaa matunda yake kila mwezi, na majani ya mti ni kwa ajili ya kuwahudumia mataifa. Pale kuna mito inayotiririka daima maji, meupe kama bilauri, na kando ya mito kuna miti inayopepea na kuweka kivuli chake juu ya njia zilizoandaliwa kwa ajili ya waliokomobolewa na Bwana. Pale nyika pana na kubwa zinaenea na kupanda katika vilima vizuri, na milima ya Mungu nyuma ya vilele vyake virefu. Kwenye nyanda hizo za amani, kando ya mito hiyo iliyo hai, watu wa Mungu, watu waliosafiri na kutanga-tanga kwa muda mrefu, wataishi humo.

"Watu wangu watakaa katika kao la amani; na katika maskani zilizo salama, na katika mahali pa kupumzikia penye utulivu." "Jeuri haitasikiwa tena katika nchi yako, Ukiwa na uharibifu hazitakuwa mipakani mwako; Bali utaziita kuta zako, Wokovu, Na malango yako, Sifa." "Nao watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu, na kula matunda yake. Hawatajenga, akakaa mtu mwingine ndani yake; hawatapanda, akala mtu mwingine; ... wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi" (Isaya 32:18; 60:18; Isaya 65:21, 22).

Pale, "nyika na mahali palipo ukiwa patafurahi; jangwa litashangilia na kuchanua maua kama waridi." "Badala ya michongoma utamea msonobari, Na badala ya mibigili, mhadesi." "Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwanakondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi; ... na mtoto mdogo atawaongoza." "Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu," asema Bwana (Isaya 35:1; 55:13; Isaya 11:6, 9).

Maumivu hayawezi kuwepo katika angahewa la mbinguni. Hakutakuwa na machozi tena, hakuna misafara ya mazishi, hakuna alama za maombolezo. "Mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, ... kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita." "Wala hapana mwenyeji atakayesema, Mimi mgonjwa; watu wakaao humo watasamehewa uovu wao" (Ufunuo 21:4; Isaya 33:24).

Pale kuna Yerusalemu Mpya, mji mkuu wa dunia mpya iliyotukuzwa, “taji ya uzuri katika mkono wa Bwana, na kilemba cha kifalme mkononi mwa Mungu wako.” “mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi, safi kama bilauri.” “Mataifa watatembea katika nuru yake. Na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake.” Bwana anasema: “Nami nitaufurahia Yerusalemu, nitawaonea shangwe watu wangu.” “Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao” (Isaya 62:3; Ufunuo 21:11, 24; Isaya 65:19; Ufunuo 21:3).

Katika Mji wa Mungu “Usiku hautakuwepo.” Hakuna atakayehitaji au kuwa na shauku ya pumziko. Hakutakuwa na kuchoka kufanya mapenzi ya Mungu na kutoa sifa kwa jina Lake. Daima tutahisi upya wa asubuhi na daima hatutakaribia mwisho wake. “Wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru.” (Ufunuo 22:5). Nafasi ya nuru ya jua itachukuliwa na mwangaza ambao mng'ao wake hauumizi, lakini ambao unaupita mbali mno mwangaza wa adhuhuri. Utukufu wa Mungu na Mwanakondoo unajaza jiji hili takatifu kwa nuru isiyofifia. Watakatifu wanatembea katika utukufu usio na jua wa siku isiyo na ukomo.

“Nami sikuona hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo, ndio hekalu lake” (Ufunuo 21:22). Watu wa Mungu wanapata fadhila ya kuwa na maongezi ya wazi na Baba na Mwana.

“Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo” (1 Wakorintho 13:12). Tunaiona Sura ya Mungu ikiwa imeakisiwa, kama katika kioo, katika kazi za vitu vya asili na katika ushughulikiaji Wake wa watu; lakini wakati huo tunamwona uso kwa uso, bila kiambaza kinachotukinga katikati na kupunguza mwanga. Tutasimama mbele Yake na kuuona utukufu wa uso Wake.

Pale waliokombolewa watajua, kama wanavyojuliwa. Upendo na huruma ambao Mungu ameweka rohoni pale vitapata matumizi ya kweli na mazuri sana. Ushirika safi na wenye uhai mtakatifu, maisha ya kijamii yenye mwafaka na malaika waliobarikiwa na watu waaminifu wa zama zote walioosha mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwanakondoo “ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa” (Waefeso 3:15), vifungo vitakatifu vinavyowafunga pamoja—hivi vinasaidia kuleta furaha ya waliokombolewa.

Pale, akili zisizokuwa na hali ya kufa zitatafakari kwa furaha isiyo na kikomo maajabu ya uwezo wa uumbaji, siri za upendo na ukombozi. Hakutakuwa na adui katili wa kumjaribu mtu kumsahau Mungu. Kila karama itakuzwa, kila talanta itaongezwa. Matakwa ya kupata maarifa hayatachosha akili wala kudhoofisha uwezo. Pale shughuli muhimu zitaendelezwa, vilele vya juu vya matarajio vitafikiwa, matamanio ya juu kabisa yatapatikana; na bado

kutatokea vilele vipya vya kupanda na kupita, maajabu mapya ya kufurahia, na ukweli mpya wa kujifunza, malengo mapya ya kuhitaji nguvu za akili na roho na mwili.

Hazina zote za uumbaji zitakuwa wazi kwa ajili ya mafunzo ya watu wa Mungu waliokombolewa. Bila kukatishwa na hali ya kufa, wanaruka kwa mabawa yao na kwenda katika sayari za mbali—sayari zilizozizima kwa huzuni kwa sababu ya tabu za mwanadamu na kurindima nyimbo za furaha kwa ajili ya roho moja iliyokombolewa. Kwa furaha isiyoelezeka watoto wa duniani wanaingia katika furaha na hekima ya viumbe ambao hawakuanguka. Wanashiriki hazina za ujuzi na ufahamu uliopatikana kwa zama nyingi kwa kutafakari juu ya kazi za mikono ya Mungu. Kwa macho yasiyokuwa na hali ya kufifia wanauona utukufu wa uumbaji—mifumo ya jua na nyota, vyote katika mpangilio wake wa awali vikizunguka kiti cha enzi cha Mungu. Juu ya vitu vyote, kuanzia vitu vidogo kabisa hadi vitu vikubwa kabisa, jina la Muumbaji limeandikwa, na vyote vinadhihirisha utajiri wa nguvu Zake.

Na miaka katika umilele, itakavyoendelea, italeta ufunuo mkubwa na wenye utukufu mwingi zaidi kumhusu Mungu na kumhusu Kristo. Uelewa ni endelevu, kadhalika upendo, kicho, na furaha vinaongezeka siku kwa siku. Kwa kadiri watu wanavyomwelewa Mungu zaidi, ndivyo wanavyoipenda zaidi tabia Yake. Yesu alipofungua mbele yao upana wa ukombozi na mafanikio ya kushangaza katika pambano kuu dhidi ya Shetani, mioyo ya waliokombolewa ilizizima kwa kujiweka wakfu na kumpenda Yesu zaidi, na kwa furaha kubwa wanapiga vinubi vyao vya dhahabu; na sauti kumi elfu mara kumi elfu na maelfu kwa maelfu ya sauti yanafumka na kuimba kibwagizo cha sifa.

"Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele" (Ufunuo 5:13).

Pambano kuu limekwisha. Dhambi na wenye dhambi havipo tena. Ulimwengu wote uko safi. Mdundo wa mwafaka na furaha unapiga katika uumbaji wake wote. Kutoka Kwake Yeye aliyewaumba wote, vinatiririka uzima na nuru na furaha, katika maeneo yote na nafasi isiyokuwa na ukomo. Kutoka kwa atomu ndogo sana hadi ulimwengu mkubwa sana, mambo yote, vyenye uhai na visivyo na uhai, katika uzuri wao usiokuwa na kivuli na furaha kamili, vinakiri kuwa Mungu ni pendo.

Kungojea Mwisho

Kungojea Mwisho